

تَفْسِيرُ الْقُرْآنِ الْعَظِيمِ

للإمام ابن كثير

# TAFSIR IBN KATHIR

**Juzuu ya Sita**

**Al-Isra mpaka Al-Muminun**

Kimetafsiriwa na:  
**Kamati ya Wataalamu**

**IBN HAZM MEDIA CENTER**  
Dar es Salaam, Tanzania

تفسير القرآن العظيم  
للإمام ابن كثير

# TAFSIR IBN KATHIR

© Ibn Hazm Media Centre.


Chapa ya Kwanza 2021.

**Msimamizi Mkuu wa Mradi:**  
Yassir Salim Awadh Masoud

**Kimetafsiriwa na:**  
Kamati ya Wataalamu

**Kimehaririwa na:**  
Wanazuoni wa Kiislamu

**Usanifu Kurasa:**  
Ally Said Abdallah  
Ibn Hazm Media Center  
P.O. Box 22197,  
Dar es Salaam  
Tanzania.

**Kimechapwa:**  
 Alhuda Publications, New Delhi, India.

**Haki Zote Zimehifadhiwa.**

## Yaliyomo:

|  |          |
|--|----------|
| <b>Tafsiri ya <i>Suratu Al-Isra'</i></b> .....                       | <b>1</b> |
| Fadhila za <i>Suratul- Israa</i> .....                               | 1        |
| <i>Israa'</i> (Usiku wa Safari).....                                 | 2        |
| Kutaja Hadithi zilizopokelewa Kuhusu <i>Israa</i> .....              | 4        |
| Safari ya <i>Israa'</i> na Hakika Ilikuwa Mwili na Roho.....         | 25       |
| Kutajwa kwa Musa عليه السلام na Kupewa Kwake Kitabu cha Taurati..... | 30       |
| Imetajwa katika Taurati kuwa Mayahudi Watafanya Uharibifu.....       | 33       |
| Ufisadi wa Kwanza wa Wana wa Israeli na Jaza ya Adhabu yao.....      | 33       |
| Uharibifu wa Pili.....   | 35       |
| Kuisifu Qur'ani.....   | 37       |
| Haraka ya Mwanadamu na Kujiombea Mabaya Mwenyewe.....                | 38       |
| Usiku na Mchana ni Ishara za Uweza Mkubwa wa Allah تعالى.....        | 40       |
| Kila Mtu Atakuwa na Kitabu cha Amali Yake.....                       | 43       |
| Hakuna Atakayebeba Mzigo wa Mwingine.....                            | 46       |
| Hakuna Adhabu ila baada ya Kumtuma Mtume.....                        | 47       |
| Mas-ala ya Watoto Wadogo Wanaokufa .....                             | 49       |
| Ukaraha wa Kuzungumzia Masiala Haya.....                             | 52       |
| Maana ya " <i>Amarnaa</i> ".....                                     | 53       |
| Vitisho kwa Maquraysh.....   | 54       |
| Malipo na Jaza kwa Anayetaka Dunia hii na Akhera.....                | 55       |
| Usimshirikishe Allah تعالى na Chochote.....                          | 59       |
| Amri ya Kumuabudu Allah تعالى Pekee na Kuwatendea Wema Wazazi.....   | 61       |
| Makosa Dhidi ya Wazazi Yanasamehewa kwa Kurudisha Mahusiano.....     | 65       |
| Amri ya Kudumisha Uhusiano wa Kindugu.....                           | 67       |
| Kuwa Mtu wa Wastani Katika Matumizi.....                             | 70       |
| Makatazo ya Kuwauwa Watoto.....                                      | 73       |
| Amri ya Kujiepusha na Zinaa na Kila Kitu.....                        | 74       |
| Katazo la Kuu Nafsi pasi na Haki.....                                | 77       |
| Amri ya Kuitumia Vizuri Mali ya Yatima .....                         | 79       |
| Usizungumze Bila Elimu.....  | 82       |
| Karipio la Kutembea kwa Maringo.....                                 | 83       |
| Yote Yaliyopita ni Wahyi na Hekima .....                             | 85       |
| Kukanushwa kwa Wanaodai Kuwa Malaika ni Mabinti wa Allah تعالى.....  | 86       |

|   |     |
|---|-----|
| Kila Kitu Kinamsabihi na Kumtakasa Allah تعالی .....                    | 89  |
| Pazia Kwenye Nyoyo za Washirikina .....                                 | 92  |
| Shura ya Siri ya Makuraishi .....                                       | 96  |
| Kuwarudi Wasioamini Maisha baada ya Mauti.....                          | 98  |
| Waja Wazungumze Maneno Mazuri na kwa Adabu.....                         | 103 |
| Kufadhilishwa Baadhi ya Manabii juu ya Wengine.....                     | 105 |
| Miungu ya Washirikina Haiwezi Kunufaisha wala Kudhuru.....              | 108 |
| Maangamizi ya Adhabu kwa Wasioamini.....                                | 110 |
| Sababu za Allah تعالی Kutotuma Ishara na Miujiza .....                  | 111 |
| Allah تعالی Kuwazunguka Watu na Kuifanya Ndoto ya Mtume ni Mtihani..... | 114 |
| Kisa cha Adam عليه السلام na Iblisi.....                                | 116 |
| Marikebu ni katika Ishara za Rehema ya Allah تعالی.....                 | 122 |
| Wanapofikiwa na Taabu, Wasioamini Hawamkumbuki Yeyote ila Allah.....    | 123 |
| Je, Hakuna Adhabu ya Allah تعالی Itakayokuja Duniani?.....              | 124 |
| Allah تعالی Ana Uwezo wa Kuwarudisha Baharini.....                      | 125 |
| Utukufu wa Kimaumbile wa Mwanadamu.....                                 | 126 |
| Kila Mmoja Ataitwa na Imaam wake Siku ya Kiyama.....                    | 128 |
| Jinsi ya Adhabu kwa Mtume ﷺ Lau Angewakubalia Makafiri.....             | 132 |
| Amri ya Kusimamisha Sala katika Nyakati Zake Maalumu.....               | 134 |
| Kujumuika Malaika katika Sala ya Alfajiri na Alasiri.....               | 136 |
| Amri ya Kuswali Tahajjud.....   | 137 |
| Amri ya Kuhama.....   | 146 |
| Onyo kwa Wasioamini Katika Maquraysh.....                               | 148 |
| Qur'ani ni Shifaa (Tiba) na Rehema.....                                 | 149 |
| Kugeuka na Kuwa Mbali na Allah تعالی Wakati wa Ukunjufu.....            | 150 |
| Kutajwa kwa Roho (Ruuh).....  | 152 |
| Roho na Nafsi.....  | 155 |
| Angetaka Allah تعالی Angeichukua Qur'ani.....                           | 157 |
| Changamoto ya Qur'ani.....  | 157 |
| Matakwa ya Maquraysh ya Kuoneshwa Ishara Maalumu.....                   | 158 |
| Sababu ya Kukataliwa Matakwa ya Washirikina.....                        | 162 |
| Kukataa Washirikina Kuamini kwa kuwa Mtume ni Mwanadamu.....            | 166 |
| Uongofu na Upotevu Uko Mikononi mwa Allah تعالی.....                    | 170 |
| Adabu kwa Watu Walioongoza Kinyume na Maagizo ya Allah تعالی.....       | 171 |
| Kuzuia ni katika Silka ya Mwanadamu.....                                | 175 |

|   |            |
|---|------------|
| Ishara Tisa za Nabii Musa عليه السلام.....                          | 177        |
| Kuangamizwa kwa Firauni na Watu Wake .....                          | 179        |
| Kuteremshwa Qur’ani Kidogo Kidogo.....                              | 181        |
| Wale Waliopewa Elimu Kabla kwa Ukweli na Dhati.....                 | 183        |
| Allah تعالی. Ndiye Mwenye Majina Mazuri Kabisa.....                 | 186        |
| Amri ya Kusoma kwa Sauti ya Kati na Kati .....                      | 187        |
| Tamko la Dhati la Kumpwekesha Allah تعالی (Tauhid).....             | 189        |
| <b>Tafsiri ya Suratul Kahf.....</b>                                 | <b>191</b> |
| Yaliyotajwa Kuhusu Fadhila za Sura .....                            | 191        |
| <b>Wahyi wa Qur’ani unaleta Bishara Njema na Onyo.....</b>          | <b>194</b> |
| Usisikitike na Kuona Vibaya kwa kuwa Washirikina Hawaamini.....     | 198        |
| Dunia ni Mahali pa Majaribio.....                                   | 199        |
| Kisa cha Watu wa Pangoni.....                                       | 201        |
| Kumuamini Kwao Allah تعالی na Kujitenga Mbali na Jamaa Zao.....     | 205        |
| Mahali pa Pango.....  | 211        |
| Kulala kwao Pangoni.....  | 214        |
| Kuamka Kwao na Kumtuma Mmoja wao kwenda Kununua Chakula.....        | 217        |
| Vipi watu wa Mji Walipowajua na Kujenga Ukumbusho juu ya Pango..... | 219        |
| Idadi Yao.....  | 222        |
| Sema Insha’Allah Unapoazimia Kufanya Jambo katika Mustakbali.....   | 225        |
| Muda Waliokaa Pangoni.....  | 228        |
| Amri ya Kusoma Qur’ani na Subra pamoja na Waumini.....              | 231        |
| Ukweli Watoka kwa Allah تعالی na Adhabu kwa Wale Wasioamini.....    | 235        |
| Malipo ya Jaza ya Walioamini kwa kutenda Matendo Mema.....          | 238        |
| Mfano wa Washirikina Matajiri na Muislamu Fakiri.....               | 242        |
| Majibu ya Muumini Fakiri.....                                       | 245        |
| Matokeo Mabaya ya Ukafiri.....                                      | 249        |
| Hadithi inayotufundisha Maadili Mema Katika Maisha ya Dunia.....    | 253        |
| Baina ya Mali, Watoto na Amali Njema .....                          | 255        |
| Vitisho Vikubwa vya Siku ya Kiyama.....                             | 257        |
| Kisa cha Adam عليه السلام na Ibilisi.....                           | 264        |
| Miungu ya Washirikina Hawakushuhudia Uumbaji wa Chochote.....       | 267        |
| Washirika Wao Wameshindwa Kujibu na Kuhudhurishwa Wahalifu.....     | 268        |
| Mifano Iliyopewa Kipaumbele Katika Qur’an .....                     | 271        |
| Uasi wa Wasioamini.....   | 272        |

|   |            |
|---|------------|
| Watu Wabaya Zaidi na Waliiodhulumu.....                               | 275        |
| Kisa cha Musa عليه السلام na Al-Khidhwr.....                          | 279        |
| Musa عليه السلام Kukutana na Al-Khidhwr na Kuongozana Naye.....       | 288        |
| Kisa cha Kuiharibu Safina.....  | 290        |
| Kisa cha Kuuliwa Kijana.....  | 293        |
| Kisa cha Kukarabati Ukuta.....  | 295        |
| Tafsiri Kwanini Safina Iliharibiwa.....                               | 296        |
| Tafisi ya Kwanini Ukuta Ulijengwa Bila Ujira .....                    | 299        |
| Je, Al-Khidhwr Alikuwa Nabii?.....                                    | 300        |
| Kwa Nini Akaitwa Al-Khidhwr?.....                                     | 301        |
| Kisa cha Dhul Qarnayn.....  | 303        |
| Dhul Qarnayn Alikuwa Mwenye Nguvu Kubwa.....                          | 304        |
| Kusafiri na Kufika Kwake Machweo ya Jua (Magharibi).....              | 306        |
| Safari Yake Upande wa Mashariki.....                                  | 309        |
| Safari Yake katika Ardhi ya Juju (Ya'ajuuj) na Majuju (Ma'ajuuj)..... | 310        |
| Kizuizi Kinawazuia lakini Kitavunjwa Karibu na Kiyama.....            | 315        |
| Jahanamu Itaoneshwa kwa Makafiri Siku ya Kiyama.....                  | 319        |
| Waliokhasirika Mno kwa Matendo Yao na Malipo Wanayostahili.....       | 320        |
| Jaza ya Waumini Wema.....   | 324        |
| Maneno ya Mola Mlezi Hayamaliziki.....                                | 325        |
| Muhammad ﷺ ni Mwanadamu na Mtume.....                                 | 326        |
| <b>Tafsiri ya Suratu Maryam.....</b>                                  | <b>329</b> |
| Kiasi cha Zakaria عليه السلام na Kuomba Kwake Mtoto.....              | 331        |
| Kuitikiwa kwa Dua Yake.....   | 335        |
| Kustaajabu Kwake baada ya Kujibiwa Dua Yake.....                      | 336        |
| Jibu la Malaika.....  | 336        |
| Alama ya Ujauzito.....  | 337        |
| Kuzaliwa kwa Kijana na Sifa Zake.....                                 | 340        |
| Kisa cha Maryam na Al-Masih (Isa) عليه السلام.....                    | 345        |
| Kubeba Mimba na Kujifungua.....                                       | 350        |
| Alichambiwa baada ya Kujifungua.....                                  | 353        |
| Maryam Akiwa Mbele ya Watu Wake na Kumkataa Kwao.....                 | 358        |
| Isa عليه السلام ni mja wa Allah تعالى, sio mtoto Wake.....            | 364        |
| Issa عليه السلام Aliamuru Kumpwekesha Allah .....                     | 365        |
| Kuwaonya Makafiri Siku ya Majuto.....                                 | 368        |

|   |            |
|---|------------|
| Mawaidha ya Ibrahimu عليه السلام kwa Baba Yake.....                         | 373        |
| Jawabu la Babake Ibraahim عليه السلام.....                                  | 375        |
| Jawabu la Ibraahim عليه السلام.....   | 376        |
| Allah تعالى Kumtunukia Ibraahim عليه السلام, Is-haaq عليه السلام.....       | 379        |
| Kutajwa kwa Musa عليه السلام na Haarun عليه السلام.....                     | 382        |
| Kumtaja Ismaail عليه السلام.....  | 384        |
| Kumtaja Idrisa عليه السلام.....   | 388        |
| Manabii Hao ni Wateule.....   | 389        |
| Wakarithiwa baada Yao na Watu Wabaya na Wazuri.....                         | 392        |
| Maelezo ya Ufafanuzi wa Bustani (Pepo).....                                 | 395        |
| Malaika Hawateremki ila kwa Amri ya Allah تعالى.....                        | 399        |
| Kustaajabu kwa mwanadamu Kufufuliwa baada ya Umuti.....                     | 402        |
| Kila mmoja Ataletwa motoni, kisha Wataokolewa Waadilifu.....                | 406        |
| Makafiri Wanajivuna kwa Hadhi yao Nzuri hapa Duniani.....                   | 409        |
| Muovu Anapatiwa Muda lakini Hajasahuliwa.....                               | 412        |
| Kuongozeka Uongofu kwa Walioongoka.....                                     | 414        |
| Kuwarudi Wasioamini Wale Wanaodai Watapewa Huko Akhera.....                 | 415        |
| Miungu ya Washirikina Itakataa Ibadah zao.....                              | 417        |
| Uchochezi wa Mashetani kwa Makafiri.....                                    | 418        |
| Hali ya Wachamungu na Hali ya Wahalifu Siku ya Kiyama.....                  | 421        |
| Kukataliwa Kabisa Kumnasibishia Allah تعالى kuwa ana mtoto.....             | 424        |
| Allah تعالى Anajaalia Mapenzi ya Watu Wema Nyoyoni.....                     | 429        |
| Qur'ani Imeteremka Kutoa Bishara Njema na Kuonya.....                       | 430        |
| <b>Tafsiri ya Suratu Twaha.....</b>   | <b>433</b> |
| Qur'ani ni Ukumbusho na Uteremsho kutoka kwa Allah تعالى.....               | 434        |
| Majadiliano Kuhusu Ujumbe wa Musa عليه السلام.....                          | 438        |
| Wahyi wa Kwanza kwa Musa عليه السلام.....                                   | 440        |
| Fimbo ya Musa عليه السلام Kugeuka na kuwa Nyoka.....                        | 446        |
| Mkono wa Musa عليه السلام Kubadilika kuwa mweupe bila Maradhi.....          | 448        |
| Allah تعالى Anamuamuru Musa عليه السلام Kwenda kwa Firauni.....             | 449        |
| Dua ya Musa عليه السلام.....  | 450        |
| Kukubaliwa Dua ya Musa عليه السلام na Kukumbushwa Neema za Awali.....       | 453        |
| Kuchaguliwa Musa عليه السلام Kwenda kwa Firauni na Kuamrisha.....           | 456        |
| Khofu ya Musa عليه السلام kwa Firauni na Kutiliwa Nguvu na Allah تعالى..... | 460        |
| Waadhi wa Musa عليه السلام mbele ya Firauni.....                            | 461        |

|   |            |
|---|------------|
| Mjadala Baina ya Musa عليه السلام na Firauni.....                         | 463        |
| Kukamilika Jawabu la Musa عليه السلام kwa Firauni.....                    | 465        |
| Firauni Alioneshwa Kila Miujiza lakini Hakuamini.....                     | 467        |
| Firauni Anaelezea Miujiza ya Musa عليه السلام kuwa ni Uchawi.....         | 468        |
| Pande Mbili Zakutana na Wito wa Musa عليه السلام kwa Wachawi.....         | 471        |
| Mpambano, Ushindi wa Musa عليه السلام na Imani ya Wachawi.....            | 475        |
| Idadi ya Wachawi.....   | 477        |
| Firauni Kuwageukia Wachawi, Kuwatisha na Jawabu lao kwake.....            | 478        |
| Wachawi Wanampa Nasaha Firauni.....                                       | 482        |
| Wana wa Israeli Wanaondoka Misri.....                                     | 486        |
| Kuwakumbusha Wana wa Israeli Neema ya Allah تعالى Juu Yao.....            | 489        |
| Musa عليه السلام Kwenda katika Miadi ya Allah تعالى.....                  | 493        |
| Harun عليه السلام Anawakataza Wana wa Israeli Kuabudu Ndama.....          | 499        |
| Yaliyotokea baina ya Musa عليه السلام na Haarun عليه السلام.....          | 500        |
| Jinsi Samiri Alivyomtengeneza Ndama.....                                  | 503        |
| Kuadhibiwa Samiri na Kuchomwa kwa Ndama.....                              | 504        |
| Qur'ani Yote ni Utajo wa Allah تعالى na Ubainifu wa Adhabu.....           | 507        |
| Kupulizwa Parapanda na Siku ya Ufufuo (Kiyama).....                       | 510        |
| Kuvurugwa kwa Milima na Kuachwa Ardhi Uwanda Tambarare.....               | 513        |
| Watu Watafanya Haraka Kuielekea Sauti ya Muitaji.....                     | 514        |
| Uombezi na malipo.....  | 517        |
| Qur'ani Imeteremshwa ili Watu Wawe na Uchamungu na Kutafakari.....        | 521        |
| Amri kwa Mtume Kuisikiliza Qur'an Iliyoteremshwa.....                     | 522        |
| Kisa cha Adamu عليه السلام na Ibilisi.....                                | 524        |
| Adamu عليه السلام Kuteremshwa Ardhini.....                                | 530        |
| Adhabu Kali kwa mwenye Kuvuka mipaka.....                                 | 532        |
| Kuangamizwa Ummah Zilizopita Pana Mafunzo kwa Wenye Kuzingatia.....       | 533        |
| Amri ya Kusubiri na Kutekeleza Sala Tano.....                             | 535        |
| Usitizame Starehe za Watu na Subiri katika Ibada ya Allah تعالى.....      | 538        |
| Ombi la Washirikina Kutaka Muujiza Ilihali Qur'an Yenyewe ni Miujiza..... | 544        |
| <b>Tafsiri ya Surat Al-Anbiyaa.....</b>                                   | <b>549</b> |
| Fadhila za Suratul-Anbiyaa.....   | 549        |
| Saa ipo Karibu na Watu Wameghafilika.....                                 | 551        |
| Mawazo na Dhana za Makafiri kwa Qur'an.....                               | 553        |
| Mitume ni Binadamu.....   | 555        |



|   |     |
|---|-----|
| Fadhila za Qur'ani.....   | 559 |
| Uumbaji Ulifanywa kwa Uadilifu na Hekima.....   | 562 |
| Kila kitu ni Miliki ya Allah <b>تعالى</b> .....   | 564 |
| Kukanusha miungu ya Uongo.....  | 565 |
| Kuwarudi Wenye Kudai kuwa Malaika ni Mabinti wa Allah <b>تعالى</b> .....                    | 570 |
| Ishara za Allah <b>تعالى</b> mbinguni na katika Ardhi na Usiku na mchana.....               | 572 |
| Katika Kila Kitu Kuna Alama za Allah <b>تعالى</b> .....                                     | 573 |
| Hakuna Atakayepewa Uhai wa Kuishi Milele Hapa Duniani.....                                  | 577 |
| Washirikina Kumfanyia Istihzai Mtume <b>ﷺ</b> .....   | 579 |
| Washirikina Kutaka Waharakishiwe Adhabu.....  | 581 |
| Mafunzo Tunayopata kwa wale Waliowafanyia Mzaha Mitume.....                                 | 584 |
| Kudanganyika Washirikina kwa muda wao mrefu wa Kustarehe.....                               | 587 |
| Kuteremshwa Taurati na Qur'ani.....   | 591 |
| Kisa cha Ibrahimu <b>عليه السلام</b> na Watu Wake.....                                      | 593 |
| Ibrahim <b>عليه السلام</b> Ayavunja masanamu.....   | 597 |
| Watu wa Ibrahimu <b>عليه السلام</b> Kukubali Udhaifu wa miungu Yao.....                     | 601 |
| Ibrahimu <b>عليه السلام</b> Kutupwa Motoni na Allah <b>تعالى</b> Kuudhibiti (Moto huo)..... | 603 |
| Kuhamia Shamu kwa Ibrahimu <b>عليه السلام</b> na Lutwi <b>عليه السلام</b> .....             | 606 |
| Kutajwa kwa Lutwi <b>عليه السلام</b> .....  | 607 |
| Kutajwa Nuhu <b>عليه السلام</b> na Watu Wake.....   | 608 |
| Dawud <b>عليه السلام</b> na Sulaymaan <b>عليه السلام</b> na Ishara Walizopewa pamoja.....   | 611 |
| Nabii Ayyuub <b>عليه السلام</b> .....   | 617 |
| Ismaail <b>عليه السلام</b> , Idris <b>عليه السلام</b> na Dhul-Kifl <b>عليه السلام</b> ..... | 620 |
| Yunus <b>عليه السلام</b> .....  | 621 |
| Zakariyya <b>عليه السلام</b> na Yahya <b>عليه السلام</b> .....                              | 626 |
| Kutajwa kwa Isa <b>عليه السلام</b> na Maryam Aliye mkweli.....                              | 628 |
| Wanadamu ni Umma mmoja.....   | 630 |
| Wale Walioangamizwa Hawatarudi Duniani.....   | 633 |
| Yaa'Juuju na Maa'Juuju.....   | 634 |
| 'Washirikina na miungu yao ni Kuni za Jahanamu.....   | 643 |
| Hali ya Watu Wema.....  | 644 |
| Kukunjwa Mbingu Siku ya Kiyama.....   | 650 |
| Ardhi Itarithiwa na Watu Wema.....  | 653 |
| Muhammad <b>ﷺ</b> ni Rehema kwa Walimwengu Wote.....  | 655 |
| Hoja katika Madhumuni ya Wahyi ni Kumuabudu Allah <b>تعالى</b> .....                        | 657 |

|   |            |
|---|------------|
| Hakuna Ajuaye Wakati wa Kiyama.....                               | 658        |
| <b>Tafsiri ya <i>Suratu Al-Hajj</i>.....</b>                      | <b>661</b> |
| Vitisho vya Saa (Kiyama).....                                     | 661        |
| Kushutumiwa kwa Wafuasi wa Shetani.....                           | 669        |
| Ushahidi wa Kufufuliwa katika Kuumbwa Binadamu na Mimea.....      | 672        |
| Hatua za Ukuaji wa Tone la Manii Katika Mfuko wa Uzazi.....       | 673        |
| Hatua za Ukuaji wa Mwanadamu Kutoka Utoto Hadi Utuuzima.....      | 674        |
| Mfano Mwingine wa Ufufuo Kutoka katika Mimea.....                 | 675        |
| Kubainishwa Hali ya Viongozi na Uzushi na Wale Waliowaongoza..... | 678        |
| Maana ya Kumuabudu Allah تعالی Kama Vile Upo Ukingoni.....        | 681        |
| Malipo ya Watu Wema.....  | 684        |
| Bila Shaka Allah تعالی Atamnusuru Mtume Wake ﷺ.....               | 685        |
| Hakika Allah تعالی Atahukumu Makundi Siku ya Kiyama.....          | 687        |
| Kila Kitu Kinamsujudia Allah تعالی.....                           | 687        |
| Sababu ya Kuteremshwa aya ya 19.....                              | 691        |
| Malipo ya Makafiri.....   | 692        |
| Malipo ya Waumini.....  | 695        |
| Onyo kwa Wanaozuia Njia ya Allah تعالی na Msikiti Mtakatifu.....  | 699        |
| Masuala ya Kukodisha Nyumba Makka.....                            | 700        |
| Onyo Kali kwa Wanaotaka Kufanya Upotofu katika Haram.....         | 703        |
| Kujengwa kwa Ka'bah na Kulinganiwa Hijjah.....                    | 705        |
| Hija ina manufaa katika maisha ya Duniani na Akhera.....          | 709        |
| Ujira kwa Kuepuka Maasi.....                                      | 715        |
| Uhalali wa Nyama Hoa.....   | 716        |
| Amri ya Kujiepusha Ushirikina na Uongo.....                       | 716        |
| Ubainifu wa Kuchinja na Kutukuza Ibada za Allah تعالی.....        | 720        |
| Manufaa ya Ngamia wa Kuchinjwa.....                               | 721        |
| Ibada ya Kuchinja ni Sharia Iliyowekwa kwa Kila Umma Duniani..... | 723        |
| Amri ya Kuchinja Ngamia wa Sadaka.....                            | 726        |
| Makusudio ya Kuchinja Mbele ya Allah تعالی ni Ikhlasu ya Mja..... | 734        |
| Kuchinja ni Sunnah Inayopendeza.....                              | 736        |
| Bishara Njema ya Kukingwa Walioamini.....                         | 737        |
| Idhini ya Kupigana, nayo ni Aya ya Kwanza ya Jihadi.....          | 738        |
| Wajibu wa Waislamu Wanapopata Madaraka.....                       | 744        |
| Matokeo ya Wasioamini.....  | 746        |

|   |            |
|---|------------|
| Makafiri Wanataka Adhabu.....   | 750        |
| Malipo ya Watu Wema na Watu Waovu.....  | 753        |
| Shetani Hutumbukiza Uongo katika maneno ya Mitume.....                        | 755        |
| Makafiri Wataendelea kuwa katika Shaka na Kuchanganyikiwa.....                | 759        |
| Ujira mkubwa kwa Wale Waliohama kwa Ajili ya Allah تعالی.....                 | 763        |
| Muumba wa Dunia na Mwenye Kuiongoza ni Allah تعالی.....                       | 766        |
| Ishara na Uweza wa Allah تعالی.....   | 769        |
| Kila Watu Wana Matukufu Yao ya Dini.....                                      | 774        |
| Washirikina Kuabudu Asiyekuwa Allah تعالی na Kuchukia Kwao Ishara Zake.....   | 779        |
| Kutokuwa na Thamani kwa Masanamu na Ujinga wa wenye kuyaabudu.....            | 781        |
| Allah تعالی Huteuwa Mitume Miongoni mwa Malaika na Binadamu.....              | 784        |
| Amri ya Kumuabudu Allah تعالی na Kupigana Jihadi.....                         | 786        |
| <b>Tafsiri ya Surat Al-Mu'minun.....</b>                                      | <b>793</b> |
| Kufaulu kwa Waumini na Kutaja Sifa zao.....                                   | 794        |
| Ishara za Allah تعالی katika Hatua za Uumbaji wa Mwanadamu.....               | 800        |
| Ishara za Allah تعالی katika Kuumba Mbingu.....                               | 805        |
| Ishara za Allah تعالی na Baraka Zake katika mvua, mimea, miti na Ng'ombe..... | 809        |
| Kisa cha Nuhu عليه السلام na Watu Wake.....                                   | 813        |
| Kisa cha 'Adi au Thamuud.....   | 819        |
| Kutajwa Mataifa Mengine.....  | 622        |
| Kisa cha Musa عليه السلام na Firauni.....                                     | 824        |
| Kutajwa kwa 'Isa عليه السلام na Maryam.....                                   | 826        |
| Amri ya Kula Halali na Kufanya Matendo Mema.....                              | 830        |
| Dini ya Mitume Wote ni Uislamu na Ukaripiaji kwa Walioasi.....                | 832        |
| Sifa za Watu Wema.....  | 836        |
| Hukumu na Uadilifu wa Allah تعالی na Upumbavu wa Washirikina.....             | 838        |
| Majibu kwa Washirikina na Kukaripiwa Kwao.....                                | 844        |
| Nabii Haombi Ujira Anahubiri Katika Njia Iliyonyooka.....                     | 847        |
| Hali za Makafiri.....   | 849        |
| Kukumbushwa Neema za Allah تعالی na Uweza Wake Mkubwa.....                    | 853        |
| Washirikina Kukanusha Kwao Kufufuliwa Baada ya Kufa.....                      | 854        |
| Washirikina Hukubali Kuwepo Muumba Lakini Wanamshirikisha Allah.....          | 857        |
| Allah تعالی Hana mshirika.....  | 862        |
| Amri ya Kuomba Dua wakati wa Majanga, na Kuondosha Maovu.....                 | 864        |
| Matamanio ya Kafiri wakati wa Kuaga.....                                      | 867        |

---

|   |     |
|---|-----|
| Maisha ya <i>Barzakh</i> na Adhabu Yake.....                  | 870 |
| Kupulizwa kwa Baragumu na Kupimwa Amali.....                  | 873 |
| Kuwakemea Watu wa Motoni, Kukiri uovu Wao na Kutaka Kwao..... | 876 |
| Jibu la Allah تعالی katika Kuwarudi Kwake Makafiri.....       | 878 |
| Allah تعالی Hakuwaumba Waja Bure Bure.....                    | 882 |
| Shirki ni Dhuluma Kubwa na Wala Hafaulu Mshirikina.....       | 884 |

## Tafsiri ya Suratul Isra'

### Sura ya 17

### Iliteremshwa Makkah

#### Fadhila za Suratul Israa'

Imaam Al-Haafidh Abu 'Abdallah Muhammad bin Isma'il Al-Bukhaariy رحمه الله تعالى anatarifu kuwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه amesema yafuatayo kuhusu Sura hii ya Bani Israa'il (au Suratul Israa'), Al-Kahf na Maryam: "Zilikuwa miongoni mwa Surah za mwanzo na nzuri sana, nazo ni hazina yangu."<sup>1</sup>

Imaam Ahmad amepokea kutoka kwa Mama Aishah رضي الله عنها amesema: "Mtume ﷺ alikuwa akifunga mpaka tukawa tunasema, hataki kufunja saumu yake, baadaye alikuwa anaacha kufungua mpaka tukawa tunasema, hataki tena kufunga. Na alikuwa anasoma Suratul Israa' na az-Zumar kila usiku."<sup>2</sup>



---

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Baari 8:655.

<sup>2</sup> Ahmad 6:189.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

## سُورَةُ الْاِسْرَاءِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

سُبْحَانَ الَّذِي أَسْرَى بِعَبْدِهِ لَيْلًا مِنَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ إِلَى الْمَسْجِدِ الْأَقْصَا الَّذِي بَرَكْنَا حَوْلَهُ لِنُرِيَهُ مِنَ آيَاتِنَا إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ ﴿١﴾  
 وَاللَّيْلَةَ إِذْ نَبَّأْنَا مُوسَى الْكُتُبَ وَجَعَلْنَاهُ هُدًى لِبَنِي إِسْرَائِيلَ آلَا تَتَّخِذُوا مِنْ دُونِي وَكَيْلًا ﴿٢﴾ ذُرِّيَّةً مِمَّنْ حَمَلْنَا مَعَ نُوحٍ إِنَّهُ كَانَ عَبْدًا شَكُورًا ﴿٣﴾ وَقَضَيْنَا إِلَى بَنِي إِسْرَائِيلَ فِي الْكِتَابِ لَتُفْسِدُنَّ فِي الْأَرْضِ مَرَّتَيْنِ وَلَتَعْلُنَّ عُلُوًّا كَبِيرًا ﴿٤﴾ فَإِذَا جَاءَ وَعْدُ أُولُنَّهُمَا بِعَثْنَا عَلَيْكُمْ عِبَادًا لَنَا أُولَى بَأْسٍ شَدِيدٍ فَجَاسُوا خِلَالَ الدِّيَارِ وَكَانَ وَعْدًا مَفْعُولًا ﴿٥﴾ ثُمَّ رَدَدْنَا لَكُمُ الْكَرَّةَ عَلَيْهِمْ وَأَمْدَدْنَاكُمْ بِأَمْوَالٍ وَبَنِينَ وَجَعَلْنَاكُمْ أَكْثَرَ نَفِيرًا ﴿٦﴾ إِنَّ أَحْسَنَكُمْ أَحْسَنْتُمْ وَأَخْسَنَكُمْ لَأَخْسَرُكُمْ وَإِنْ سَأَلْتُمْ فَلَهَا فَإِذَا جَاءَ وَعْدُ الْآخِرَةِ لِيَسْتَوْفُوا وَجُوهَكُمْ وَلِيَدْخُلُوا الْمَسْجِدَ كَمَا دَخَلُوهُ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَلِيُتَبِّرُوا مَا عَلَوْا تَتْبِيرًا ﴿٧﴾ عَسَىٰ رَبُّكُمْ أَنْ يَرْحَمَكُمُ وَإِنْ عُدتُمْ عُدتْنَا وَجَعَلْنَا جَهَنَّمَ لِلْكَافِرِينَ حَصِيرًا ﴿٨﴾

سُبْحَانَ الَّذِي أَسْرَى بِعَبْدِهِ لَيْلًا مِنَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ إِلَى الْمَسْجِدِ الْأَقْصَا الَّذِي بَرَكْنَا حَوْلَهُ لِنُرِيَهُ مِنَ آيَاتِنَا إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ ﴿١﴾

**1. Subhana, Ametakasika Aliyemchukua mja Wake usiku mmoja kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali, ambao Tumevibariki vilivyouzunguka, ili Tumuoneshe baadhi ya Ishara Zetu. Hakika Yeye ni Mwenye Kusikia na Mwenye Kuona.**

**Israa' (Usiku wa Safari)**

Allah تعالى Anaitukuza Nafsi Yake na Kulikuza Jambo Lake kwa Uwezo Wake ambao hakuna auwezaye yeyote awaye. Hakuna Muabudiwa ila Yeye wala Mola Mlezi asiyekuwa Yeye.

الَّذِي أَسْرَى بِعَبْدِهِ

**"Aliyempeleka mja Wake."**

Maana yake: Muhammad ﷺ. Safari hiyo ilikuwa,

لَيْلًا

**"Usiku."**

Maana yake: Katika sehemu ya usiku.

مِنَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ

**"Kutoka Msikiti Mtukufu."**

Nao ni Msikiti wa Makkah. Safari hii ilimfikisha Mtume Muhammad ﷺ:

إِلَى الْمَسْجِدِ الْأَقْصَا

**"Mpaka Msikiti wa mbali."**

Nao ni Msikiti wa *Baytil Maqdis* ambao upo *Ilyaa', al-Quds* au Jerusalem, mji wa Manabii kutoka katika kizazi kuanzia cha Ibraahim *al-Khaliil* عليه السلام. Kwa hiyo, hapo alikusanyiwa mitume wote, naye akawa Imaam katika mahali pao na nyumba zao. Hii ni dalili ya kuwa yeye ndiye Imaam Mtukufu na raisi wa kutangulizwa na amani iwe juu ya wote. Na Kauli Yake تعالى:

الَّذِي بَرَكْنَا حَوْلَهُ

**"Ambao Tumevibariki vilivyo uzunguka."**

Kwa Ukulima, Mimea na Matunda.

لِنُرِيَهُ

**"Ili Tumuoneshe."**

Maana: yeye Muhammad ﷺ.

مِنَ آيَاتِنَا

**"Baadhi ya Ishara Zetu."** Maana: Kubwa. Kama Alivyosema Aliyetukuka:

لَقَدْ رَأَى مِنْ آيَاتِ رَبِّهِ الْكُبْرَى ﴿١٧﴾

**"Hakika aliona (Nabii Muhammad) mambo makubwa kabisa katika alama za Mola wake Mlezi." (53:18).**

Tutataja hayo yaliyopokewa katika Sunna mingoni mwa Hadithi za Mtume ﷺ. Na Kauli Yake تعالى:

إِنَّهُ هُوَ السَّمِيعُ الْبَصِيرُ ﴿١٧﴾

**"Hakika Yeye ni Mwenye Kusikia na Mwenye Kuona."**

Maana: Mwenye Kusikia kwa kauli za waja Wake walio Waumini na makafiri, wenye kusadiki na kukadhibisha miongoni mwao, Mwenye kuwaona wao na Kuwapatia kila mmoja miongoni mwao kwa wanayostahiki duniani na Akhera.

### Kutaja Hadithi Zilizopokewa kuhusu Israa'

**Riwaya ya Anas bin Maalik رضي الله عنه**

Imaam Ahmad amepokea kutoka kwa Anas bin Maalik رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

هَاتَيْتُ بِالرِّاقِ وَهُوَ دَابَّةٌ أَيْضُ فَوْقَ الْجَمَارِ وَدُونَ الْبِغْلِ، يَضَعُ حَافِرُهُ عِنْدَ مُتَهَيِّ طَرَفِهِ، فَرَكِبْتُهُ فَسَارَ بِي حَتَّى آتَيْتُ بَيْتَ الْمَقْدِسِ، فَرَبَطْتُ الدَّابَّةَ بِالْحَلَقَةِ الَّتِي يَرْبُطُ فِيهَا الْأَنْبِيَاءَ، ثُمَّ دَخَلْتُ فَصَلَّيْتُ فِيهِ وَرَكَعَتَيْنِ ثُمَّ خَرَجْتُ فَأَتَانِي جِبْرِيلُ بِإِنَاءٍ مِنْ خَمْرٍ وَإِنَاءٍ مِنْ لَبَنٍ، فَاخْتَرْتُ اللَّبَنَ فَقَالَ جِبْرِيلُ: أَصَبْتَ الْفِطْرَةَ. قَالَ: ثُمَّ عُرِجَ بِي إِلَى السَّمَاءِ الدُّنْيَا فَاسْتَفْتَحَ جِبْرِيلُ فَقِيلَ لَهُ: مَنْ أَنْتَ؟ قَالَ: جِبْرِيلُ. قِيلَ: وَمَنْ مَعَكَ؟ قَالَ: مُحَمَّدٌ. قِيلَ: وَقَدْ أُزِيلَ إِلَيْهِ؟ قَالَ: قَدْ أُزِيلَ إِلَيْهِ. فَفُتِحَ لَنَا فَإِذَا أَنَا بِآدَمَ فَرَحَّبَ بِي وَدَعَا لِي بِخَيْرٍ، ثُمَّ عُرِجَ بِنَا إِلَى السَّمَاءِ الثَّانِيَةِ فَاسْتَفْتَحَ جِبْرِيلُ فَقِيلَ لَهُ: مَنْ أَنْتَ؟ قَالَ: جِبْرِيلُ. قِيلَ: وَمَنْ مَعَكَ؟ قَالَ: مُحَمَّدٌ. قِيلَ: وَقَدْ أُزِيلَ إِلَيْهِ؟ قَالَ: قَدْ أُزِيلَ إِلَيْهِ، فَفُتِحَ لَنَا فَإِذَا أَنَا بِابْنَتِي الْخَالَةَ بِحَمِي وَعِيسَى فَرَحَّبَا بِي وَدَعَوَا لِي بِخَيْرٍ ثُمَّ عُرِجَ بِنَا إِلَى السَّمَاءِ الثَّالِثَةِ فَاسْتَفْتَحَ جِبْرِيلُ فَقِيلَ لَهُ: مَنْ أَنْتَ؟ قَالَ: جِبْرِيلُ، قِيلَ: وَمَنْ مَعَكَ؟ قَالَ: مُحَمَّدٌ قِيلَ: وَقَدْ أُزِيلَ إِلَيْهِ؟ قَالَ: قَدْ أُزِيلَ إِلَيْهِ. فَفُتِحَ لَنَا، فَإِذَا أَنَا بِيُوسُفَ عَلَيْهِ السَّلَامُ، وَإِذَا هُوَ قَدْ أُعْطِيَ شَطْرَ الْحُسَيْنِ



فَرَحَّبَ بِي وَدَعَا لِي بِخَيْرٍ. ثُمَّ عُرِّجَ بِنَا إِلَى السَّمَاءِ الرَّابِعَةِ فَاسْتَفْتَحَ جِبْرِيلُ قَبِيلَ:  
 مَنْ أَنْتَ؟ قَالَ: جِبْرِيلُ قَبِيلَ: وَمَنْ مَعَكَ؟ قَالَ: مُحَمَّدٌ قَبِيلَ: وَقَدْ أُرْسِلَ إِلَيْهِ؟  
 قَالَ: قَدْ بُعِثَ إِلَيْهِ. فَفُتِحَ لَنَا فَإِذَا أَنَا بِإِدْرِيسَ فَرَحَّبَ بِي وَدَعَا لِي بِخَيْرٍ، ثُمَّ قَالَ:  
 يَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى:

"Nililetewa Buraaq, naye ni mnyama mweupe mkubwa kuliko punda na mdogo kuliko nyumbu. Anaweka kwato zake pale anapoon. Nilimpanda, akanipeleka mpaka Bayt Al-Maqdis (Al-Quds), nami nikamfunga katika kikuku walichokuwa wakitumia Manabii kufunga mnyama. Kisha niliingia na kusali ndani yake raka mbili, na baadae nikatoka. Jibril alinjia na chombo cha pombe na kingine cha maziwa, nami nikachagua maziwa. Akasema Jibril: 'Umeshapewa na kupatia fitrah (maumbile)'. Akasema: 'Kisha nikapandishwa mbingu ya dunia (ya kwanza) na Jibril akataka ruhusa ya kufunguliwa.' Akaulizwa: 'Wewe nani?' Akasema: 'Jibril'. Akaulizwa: 'Uko na nani?' Akajibu: 'Muhammad'. Akaulizwa: 'Je, Ameshapewa Utume?' Akajibu: 'Ndio, tayari ameshapewa'. Tulifunguliwa, na hapo nikakutana na Adam, ambaye alinikongowea (alinikaribisha) na kuniombea kheri. Kisha nikapandishwa hadi mbingu ya pili, Jibril akaomba afunguliwe. Akaulizwa: 'Wewe nani?' Akasema: 'Jibril'. Akaulizwa: 'Uko na nani?' Akajibu: 'Muhammad'. Akaulizwa: 'Je, ameshapewa Utume?' Akajibu: 'Ndio, tayari ameshapewa Utume'. Tulifunguliwa, na hapo nikakutana na watoto wawili wa mama mkubwa na mama mdogo (halati), Yahya na 'Isaa, waliniamkia na kuniombea kheri. Kisha nikapandishwa hadi mbingu ya tatu, Jibril akaomba afunguliwe. Akaulizwa: 'Wewe nani?' Akasema: 'Jibril'. Akaulizwa: 'Uko na nani?' Akajibu: 'Muhammad'. Akaulizwa: 'Je, ameshapewa utume?' Akajibu: 'Ndio, tayari ameshapewa'. Tulifunguliwa, na hapo nikakutana na Yusuf, ambaye amepatiwa nusu ya uzuri, naye aliniamkia na kuniombea kheri. Kisha nikapandishwa hadi mbingu ya nne, Jibril akaomba afunguliwe. Akaulizwa: 'Wewe nani?' Akasema: 'Jibril'. Akaulizwa: 'Uko na nani?' Akajibu: 'Muhammad'. Akaulizwa: 'Je, ameshapewa Utume?' Akajibu: 'Ndio, tayari ameshapewa'. Tulifunguliwa, na hapo nikakutana na Idris, naye akaniamkia na kuniombea kheri. Kisha Mtume ﷺ akasema, Allah تعالى Amesema:

وَرَفَعْنَاهُ مَكَانًا عَلِيًّا ﴿٥٧﴾

“Na Tulimuinua daraja ya juu kabisa” (19:57).

ثُمَّ عَرَجَ بِنَا إِلَى السَّمَاءِ الْخَامِسَةِ فَاسْتَفْتَحَ جِبْرِيلُ قَبِيلَ: مَنْ أَنْتَ؟ قَالَ جِبْرِيلُ قَبِيلَ: وَمَنْ مَعَكَ؟ قَالَ: مُحَمَّدٌ قَبِيلَ: وَقَدْ أُرْسِلَ إِلَيْهِ؟ قَالَ: قَدْ بُعِثَ إِلَيْهِ. فَفُتِحَ لَنَا فَإِذَا أَنَا بِهَارُونَ فَرَحَّبَ بِي وَدَعَا لِي بِخَيْرٍ ثُمَّ عَرَجَ بِنَا إِلَى السَّمَاءِ السَّادِسَةِ فَاسْتَفْتَحَ جِبْرِيلُ قَبِيلَ مَنْ أَنْتَ؟ قَالَ: جِبْرِيلُ قَبِيلَ: وَمَنْ مَعَكَ؟ قَالَ: مُحَمَّدٌ قَبِيلَ: وَقَدْ بُعِثَ إِلَيْهِ؟ قَالَ: قَدْ بُعِثَ إِلَيْهِ. فَفُتِحَ لَنَا فَإِذَا أَنَا بِمُوسَى عَلَيْهِ السَّلَامُ فَرَحَّبَ بِي وَدَعَا لِي بِخَيْرٍ ثُمَّ عَرَجَ بِنَا إِلَى السَّمَاءِ السَّابِعَةِ فَاسْتَفْتَحَ جِبْرِيلُ قَبِيلَ مَنْ أَنْتَ؟ قَالَ: جِبْرِيلُ قَبِيلَ: وَمَنْ مَعَكَ؟ قَالَ: مُحَمَّدٌ قَبِيلَ: وَقَدْ بُعِثَ إِلَيْهِ؟ قَالَ: قَدْ بُعِثَ إِلَيْهِ. فَفُتِحَ لَنَا فَإِذَا أَنَا بِإِبْرَاهِيمَ عَلَيْهِ السَّلَامُ، وَإِذَا هُوَ مُسْتَبِدٌّ إِلَى النَّبِيِّ الْمَعْمُورِ، وَإِذَا هُوَ بِدُخْلِهِ كُلَّ يَوْمٍ سَبْعُونَ أَلْفَ مَلَكٍ ثُمَّ لَا يَتَعَوَّدُونَ إِلَيْهِ، ثُمَّ ذَهَبَ بِي إِلَى سِدْرَةِ الْمُتَهَيِّئَةِ فَإِذَا وَرَثَتُهَا كَأَذَانِ الْفَيْلَةِ، وَإِذَا تَمَرُّهَا كَأَلْفِ لَيْلٍ، فَلَمَّا غَشِيَهَا مِنْ أَمْرِ اللَّهِ مَا غَشِيَهَا تَغَيَّرَتْ فَمَا أَحَدٌ مِنْ خَلْقِ اللَّهِ تَعَالَى يَسْتَطِيعُ أَنْ يَصِفَهَا مِنْ حُسْنِهَا.

Kisha nikapandishwa hadi mbingu ya tano, Jibril akaomba afunguliwe. Akaulizwa: ‘Wewe nani?’ Akasema: ‘Jibril’. Akaulizwa: ‘Uko na nani?’ Akajibu: ‘Na Muhammad’. Akaulizwa: ‘Je, ameshapewa utume (ametumilizwa)?’ Akajibu: ‘Ndio, tayari ameshapewa (ametumilizwa)’. Tulifunguliwa, na hapo nikakutana na Haaran, naye akaniamkia na kuniombea kheri. Kisha nikapandishwa hadi mbingu ya sita, Jibril akaomba afunguliwe. Akaulizwa: ‘Wewe nani?’ Akasema: ‘Jibril’. Akaulizwa: ‘Uko na nani?’ Akajibu: ‘Na Muhammad’. Akaulizwa: ‘Je, ameshapewa Utume (ametumilizwa)?’ Akajibu: ‘Ndio, tayari ameshapewa (ametumilizwa)’. Tulifunguliwa, na hapo nikakutana na Musa, naye akanikongowea na kuniombea kheri. Kisha nikapandishwa hadi mbingu ya saba, Jibril akaomba afunguliwe. Akaulizwa: ‘Wewe nani?’ Akasema: ‘Jibril’. Akaulizwa: ‘Uko na nani?’ Akajibu: ‘Na Muhammad’. Akaulizwa: ‘Je, ameshapewa Utume (ametumilizwa)?’ Akajibu: ‘Ndio, tayari ameshapewa (ametumilizwa)’. Tulifunguliwa, na hapo nikakutana na Ibrahim (Alayhis Salaam), akiwa

ameegemea kwenye Bayt Al-Ma'muur (Nyumba inayozuriwa). Kila siku wanaingia Malaika sabiini elfu, kisha hawarudi tena. Kisha nilichukuliwa mpaka Sidrat Al-Muntahaa (Mkunazi wa kumalizikia mambo, ambako mbele ya hapo hakuna anayeruhusiwa kupita), majani yake yakiwa makubwa kama masikio ya ndovu na matunda yake kama Mtungi wa kabila la Hajara, na pindi ilipofunikwa kwa kilichoifunika kwa amri ya Allah, ilibadilika, na hakuna kiumbe chochote cha Allah Aliyetukuka kinachoweza kusifia uzuri wake.

قَالَ: فَأَوْحَى اللَّهُ إِلَيَّ مَا أَوْحَى، وَقَدْ قَرَضَ عَلَيَّ فِي كُلِّ يَوْمٍ وَرَبْلَةَ خَمْسِينَ صَلَاةً فَتَزَلْتُ حَتَّى انْتَهَيْتُ إِلَى مُوسَى، قَالَ: مَا قَرَضَ رَبُّكَ عَلَيَّ أُمَّتِكَ؟ قُلْتُ: خَمْسِينَ صَلَاةً فِي كُلِّ يَوْمٍ وَرَبْلَةَ، قَالَ: ارْجِعْ إِلَى رَبِّكَ فَاسْأَلْهُ التَّخْفِيفَ لِأُمَّتِكَ، فَإِنَّ أُمَّتَكَ لَا تُطِيقُ ذَلِكَ وَإِنِّي قَدْ بَلَوْتُ بَنِي إِسْرَائِيلَ وَخَبَّرْتُهُمْ، قَالَ: فَرَجَعْتُ إِلَى رَبِّي فَقُلْتُ أَيُّ رَبِّ خَفَّفَ عَنِّ أُمَّتِي فَحَطَّ عَنِّي خَمْسًا، فَتَزَلْتُ حَتَّى انْتَهَيْتُ إِلَى مُوسَى فَقَالَ: مَا فَعَلْتَ؟ قُلْتُ: قَدْ حَطَّ عَنِّي خَمْسًا فَقَالَ: إِنَّ أُمَّتَكَ لَا تُطِيقُ ذَلِكَ فَارْجِعْ إِلَى رَبِّكَ فَاسْأَلْهُ التَّخْفِيفَ لِأُمَّتِكَ، قَالَ: فَلَمْ أَزَلْ أَرْجِعُ بَيْنَ رَبِّي وَبَيْنَ مُوسَى وَيَحْطُّ عَنِّي خَمْسًا خَمْسًا حَتَّى قَالَ: يَا مُحَمَّدُ هُنَّ خَمْسُ صَلَوَاتٍ فِي كُلِّ يَوْمٍ وَرَبْلَةَ بِكُلِّ صَلَاةٍ عَشْرًا، فَبَلَغَ خَمْسُونَ صَلَاةً وَمَنْ هَمَّ بِحَسَنَةٍ فَلَمْ يَعْمَلْهَا كُتِبَتْ لَهُ حَسَنَةٌ، فَإِنْ عَمِلَهَا كُتِبَتْ عَشْرًا، وَمَنْ هَمَّ بِسَيِّئَةٍ فَلَمْ يَعْمَلْهَا لَمْ تُكْتَبْ شَيْئًا، فَإِنْ عَمِلَهَا كُتِبَتْ سَبْعَةٌ وَاحِدَةً، فَتَزَلْتُ حَتَّى انْتَهَيْتُ إِلَى مُوسَى فَأَخْبَرْتُهُ، فَقَالَ: ارْجِعْ إِلَى رَبِّكَ فَاسْأَلْهُ التَّخْفِيفَ لِأُمَّتِكَ فَإِنَّ أُمَّتَكَ لَا تُطِيقُ ذَلِكَ، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ: «لَقَدْ رَجَعْتُ إِلَى رَبِّي حَتَّى اسْتَحْيَيْتُ»

Akasema: Allah Akaniteremshia wahyi kwa Aliyoniteremshia. Na Alinifaradhia kwa kila mchana na usiku Sala hamsini. Nilishuka chini mpaka nikafika kwa Musa, naye aliniambia: 'Je, Mola wako Mlezi Ameufaradhia Ummah wako nini?' Nilisema: 'Sala hamsini kwa kila mchana na usiku'. Akaniambia: 'Rudi kwa Mola wako Mlezi na umuombe tahfifu kwa Ummah wako kwani Ummah wako hautaweza hilo. Na hakika niliwajaribu Bani Israili na kuwajua walivyo'. Akasema (Mtume): 'Nilirudi kwa Mola wangu Mlezi na kumuambia: 'Ewe Mola wangu Mlezi! Upatie tahfifu Ummah wangu

*mzigo huo kwani hawataweza kufanya hilo'. Akanipunguzia tano katika hiyo idadi. Niliteremka mpaka nikakutana na Musa, naye akaniuliza: 'Umefanya nini?' Nikamuambia: 'Nimepunguziwa tano'. Akasema: 'Hakika Ummah wako hautaweza hilo, rudi kwa Mola wako Mlezi umuombe tahfifu kwa Ummah wako'. Akasema (Mtume): Nikaendelea kurudi baina ya Mola wangu Mlezi na Musa na kupunguziwa tano tano mpaka Akasema: 'Ewe Muhammad! Hizo ni Sala tano kwa kila siku na kila Sala moja ni sawa na Sala kumi (yaani Sala moja ina thawabu ya Sala kumi), kwa hivyo hizo ni hamsini. Na mwenye kukusudia jambo jema na asilifanye huandikiwa jema moja (kamili), na akilifanya huandikiwa kumi. Na mwenye kukusudia kufanya jambo baya na asilifanye hataandikiwa chochote, na akilifanya ataandikiwa baya moja.' Niliteremka mpaka nikafika kwa Musa, nami nikamjulisha habari hiyo. Akaniambia: 'Rudi kwa Mola wako Mlezi umuombe tahfifu kwa Umami wako kwani Umami wako hawataweza hilo. Akasema Mtume ﷺ: 'Hakika nilikuwa nikirudi kwa Mola wangu Mlezi mpaka nikaona haya"<sup>1</sup>. Riwaya hii imenukuliwa pia na Muslim<sup>2</sup>.*

Imaam Ahmad amepokea kutoka kwa Anas رضي الله عنه ambaye amesema kuwa *al-Buraaq* aliletewa Mtume ﷺ usiku wa *Israa'* akiwa na sogi na hatamu yake tayari kupandwa. Mnyama huyo akakukuruka, Jibril عليه السلام akamuambia: "Kwa nini unafanya hivi? Kwa Allah, hakuna hata mmoja aliyekupanda aliye mtukufu mbele ya Allah kuliko yeye". Kwa kuambiwa hayo, *Buraaq* akaanza kutokwa na jasho. Hii imepokewa na At-Tirmidhiy<sup>3</sup>, aliyesema ni *Gharib*<sup>4</sup>.

Amenukuu Ahmad tena kuwa Anas رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema:

«لَمَّا عَرَجَ بِي رَبِّي عَزَّ وَجَلَّ مَرَزْتُ بِقَوْمٍ لَهُمْ أَظْفَارٌ مِنْ نَحَاسٍ يَخْمِشُونَ بِهَا  
رُجُوهَهُمْ وَصُدُورَهُمْ، فَقُلْتُ: مَنْ هَؤُلَاءِ يَا جِبْرِيْلُ؟ قَالَ: هَؤُلَاءِ الَّذِينَ يَأْكُلُونَ  
لُحُومَ النَّاسِ وَيَقْعُونَ فِي أَعْرَاضِهِمْ»

<sup>1</sup> Ahmad 3:148.

<sup>2</sup> Muslim 1:145.

<sup>3</sup> At-Tirmidhiy, na. 3131.

<sup>4</sup> Hadithi *Gharib* ni ile isiyokuwa ya kawaida, nayo huwa imeletwa kupitia kwa mapokezi ya mtu mmoja au imeletwa na mtu ambaye haaminiki riwaya zake hivyo hii hutwiwa nguvu na Hadithi nyingine ili ifanye kazi kama Hadithi nyingine.

*“Nilipochukuliwa kwa Mola wangu Mlezi (wakati wa Mi'raaj), nilipita kwa kaumu waliokuwa na makucha ya shaba nyekundu waliokuwa kwayo wakikwaruza nyuso na vifua vyao. Nikasema: ‘Ewe Jibriil! Hawa ni kina nani?’ Alisema: ‘Hawa ni wale waliokuwa wakila nyama za watu (kwa kuwasengenywa) na kuwakashifu”<sup>1</sup>.*

Haya pia yalinukuliwa na Abu Daawuud<sup>2</sup>. Pia alisema Anas رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«مَرَزْتُ لَيْلَةَ أُسْرِي بِي عَلَى مُوسَى عَلَيْهِ السَّلَامُ قَائِمًا بُصَلِّي نِي قَبْرِهِ»

*“Nilipopelekwa kwa safari ya usiku (Al-Israa') nilipita kwa Nabii Musa, aliyekuwa amesimama akiswali kwenye kaburi lake”<sup>3</sup>.*

Pia imepokewa na Muslim<sup>4</sup>.

**Riwaya ya Anas bin Maalik رضي الله عنه kutoka kwa Maalik bin Swa'swa'ah**

رضي الله عنه

Imenukuliwa na Imaam Ahmad kutoka kwa Anas bin Maalik رضي الله عنه amesema kuwa Maalik bin Swa'swa'ah رضي الله عنه amemuambia kuwa Mtume ﷺ alimuambia kuhusu usiku aliochukuliwa kwa safari ya Israa'. Alisema:

«بَيْنَمَا أَنَا فِي الْحَطِيمِ - وَرَبَّمَا قَالَ قَتَادَةُ: فِي الْحَجْرِ - مُضْطَجِعًا إِذْ أَتَانِي آتٌ، فَجَمَلَ يَقُولُ لِصَاحِبِهِ الْأَوْسَطِ بَيْنَ الثَّلَاثَةِ - قَالَ - فَأَتَانِي فَقَدَّ - سَمِعْتُ قَتَادَةَ يَقُولُ: فَشَقَّ - مَا بَيْنَ هَذِهِ إِلَى هَذِهِ»

*“Nilipokuwa nimejinyoosha Al-Hatwim – na huenda ikawa kama alivyosema Qatadah: Al-Hijr, alipokuja mtu aliyemuambia sahibu wake aliyekuwa wa kati, kati ya watatu. Akasema: Akanijia na kunifunua.” Nimemsikia Qatadah akisema: ‘Wakanipasua baina ya hapa na hapa.”*

<sup>1</sup> Ahmad 3: 224.

<sup>2</sup> Abu Daawuud 4878.

<sup>3</sup> Ahmad 3: 120.

<sup>4</sup> Muslim 2375.

Qatadah akasema: 'Nikamuuliza Al-Jaarud aliyekuwa karibu nami, 'Hiyo inamaanisha nini?' Akasema: 'Kuanzia juu ya kifua chake hadi chini ya kitovu chake', na pia nimemsikia akisema: 'Kuanzia kooni mwake hadi chini ya kitovu'. Mtume ﷺ akasema:

فَأَسْخِرَجَ قَلْبِي - قَالَ - فَأَنْتِ بِطَسْتٍ مِنْ ذَهَبٍ مَمْلُوءَةٍ إِيمَانًا وَحِكْمَةً فَفَعِيلَ قَلْبِي  
ثُمَّ حُسْبِي ثُمَّ أُعِيدَ ثُمَّ أَنْتِ بَدَائِيهِ دُونَ الْبُعْلِ وَفَوْقَ الْحِمَارِ أَيْضًا

*'Aliutoa moyo wangu, kikaletwa chombo cha dhahabu kilichojazwa Imani na hekima. Aliuosa moyo wangu kisha akaujaza (kwa hayo) na kuurudisha (mahali pake). Baadaye nikaletewa mnyama aliyekuwa mdogo kuliko nyumbu na mkubwa kuliko punda'.*

Al-Jaarud akasema: 'Ewe Abu Hamza, huyo alikuwa ni Al-Buraaq?' Akajibu: 'Ndio, na hatua yake ni upeo wa kuona kwake'. Mtume ﷺ akasema:

فَحَبِلْتُ عَلَيْهِ فَاذْطَلَقَ بِي جِبْرِيلُ عَلَيْهِ السَّلَامُ حَتَّى أَتَى بِي إِلَى السَّمَاءِ الدُّنْيَا  
فَأَسْتَفْتَحُ، فَقِيلَ: مَنْ هَذَا؟ قَالَ: جِبْرِيلُ، قِيلَ: وَمَنْ مَعَكَ؟ قَالَ: مُحَمَّدٌ، قِيلَ: أَوْ  
قَدْ أُرْسِلَ إِلَيْهِ؟ قَالَ: نَعَمْ، قِيلَ: مَرَحَبًا بِهِ وَلِنِعْمَ الْمَجِيءُ جَاءَ - قَالَ - فَفَتِّحْ لَنَا  
فَلَمَّا خَلَصْتُ فَإِذَا فِيهَا آدَمُ عَلَيْهِ السَّلَامُ، قَالَ: هَذَا أَبُوكَ آدَمُ فَسَلِّمْ عَلَيْهِ، فَسَلَّمْتُ  
عَلَيْهِ فَرَدَّ السَّلَامَ ثُمَّ قَالَ: مَرَحَبًا بِالابْنِ الصَّالِحِ وَالنَّبِيِّ الصَّالِحِ، قَالَ - فَلَمَّا  
تَجَاوَزْتُهُ بَكَى قِيلَ لَهُ: مَا يُبْكِيكَ؟ قَالَ: أَبْيَكِي لِأَنَّ غُلَامًا بَعِثَ بَعْدِي يَدْخُلُ الْجَنَّةَ  
مِنْ أُمَّتِهِ أَكْثَرَ مِنَّا يَدْخُلُهَا مِنْ أُمَّتِي. قَالَ: ثُمَّ صَعِدَ حَتَّى أَتَى السَّمَاءَ السَّابِعَةَ  
فَأَسْتَفْتَحُ قِيلَ: مَنْ هَذَا؟ قَالَ: جِبْرِيلُ، قِيلَ: وَمَنْ مَعَكَ؟ قَالَ: مُحَمَّدٌ، قِيلَ: أَوْ  
قَدْ بُعِثَ إِلَيْهِ؟ قَالَ: نَعَمْ، قِيلَ: مَرَحَبًا بِهِ وَلِنِعْمَ الْمَجِيءُ جَاءَ، قَالَ: فَفَتِّحْ لَنَا فَلَمَّا  
خَلَصْتُ فَإِذَا إِبْرَاهِيمُ عَلَيْهِ السَّلَامُ فَقَالَ: هَذَا إِبْرَاهِيمُ فَسَلِّمْ عَلَيْهِ قَالَ: فَسَلَّمْتُ عَلَيْهِ  
فَرَدَّ السَّلَامَ، ثُمَّ قَالَ: مَرَحَبًا بِالابْنِ الصَّالِحِ وَالنَّبِيِّ الصَّالِحِ - قَالَ - ثُمَّ رُفِعَتْ إِلَيَّ  
سِدْرَةُ الْمُتَهَيَّئِ فَإِذَا تَبَقُّهَا مِثْلُ قِلَالِ حَجَرٍ، وَإِذَا وَرَفُّهَا مِثْلُ آذَانِ الْفَيْلَةِ، فَقَالَ: هَذِهِ  
سِدْرَةُ الْمُتَهَيَّئِ، قَالَ: وَإِذَا أَرَبَعَةٌ أَنْهَارٍ: نَهْرَانِ بَاطِنَانِ وَنَهْرَانِ ظَاهِرَانِ، فَقُلْتُ: مَا  
هَذَا يَا جِبْرِيلُ؟ قَالَ: أَمَّا الْبَاطِنَانِ فَنَهْرَانِ فِي الْجَنَّةِ، وَأَمَّا الظَّاهِرَانِ فَالنَّيْلُ وَالْفَرَاتُ  
- قَالَ - ثُمَّ رُفِعَ إِلَيَّ النَّبِيُّ الْمُعْمُورُ

'Nilipandishwa juu yake na akaondoka nami Jibril mpaka akanifikisha uwingu wa dunia (wa kwanza). Jibril akataka ruhusa ya kufunguliwa. Akaulizwa: 'Wewe nani?' Akasema: 'Jibril'. Akaulizwa: 'Uko na nani?' Akajibu: 'Na Muhammad'. Akaulizwa: 'Je, ameshapewa Utume (ametumilizwa)?' Akajibu: 'Ndio, tayari ameshapewa (ametumilizwa)'. Pakasemwa: 'Anakaribishwa na ni neema kwa ujio wake.' Tukafunguliwa, nami nikaingia, hapo nikakutana na Adam. Jibril akasema: 'Huyu ni baba yako Adam, msalimie'. Nilimsalimia, naye akarudisha salamu. Kisha akasema Adam: 'Karibu mtoto na Nabii mwema'. akasema – pindi nilipompita (Adam) alianza kulia. Akaulizwa: 'Kwa nini unalia?' Akajibu: 'Ninalia kwa kuwa kijana amepewa Utume baada yangu, wataingia Peponi Umati wake zaidi kuliko watakavyoingia Umati wangu'. Akasema: 'Kisha nikapanda mpaka nikafika uwingu wa saba, Jibril akaomba afunguliwe. Akaulizwa: 'Wewe nani?' Akasema: 'Jibril'. Akaulizwa: 'Uko na nani?' Akajibu: 'Na Muhammad'. Akaulizwa: 'Je, ameshapewa Utume (ametumilizwa)?' Akajibu: 'Ndio, tayari ameshapewa (ametumilizwa)'. Pakasemwa: 'Anakaribishwa na ni neema kwa ujio wake.' Tukafunguliwa, nami nikaingia, hapo nikakutana na Ibraahim. Akasema Jibril: 'Huyu hapa Ibraahim, msalimie'. Nami nilimsalimia, naye akarudisha salamu. Kisha akasema: 'Karibu mtoto na Nabii mwema'. Baada ya hapo nikapelekwa hadi Sidratul Muntahaa, matunda yake yakiwa kama majagi ya Hajar (eneo lilioko Arabuni) na majani yake kama sikio la ndovu. Akasema Jibril: 'Hapa ni Sidratul Muntahaa'. Kulikuwa na mito minne: miwili iliyofichika na miwili iliyokuwa ikionekana. Nikauliza: 'Ewe Jibril, ni nini hiki?' Akasema: 'Ama kuhusu mito iliyoyofichwa, ni mito iliyopo Peponi na ile miwili iliyo dhahiri ni mto Nile (ambao upo Misri) na Furaat (Euphrates uliopo Iraq). Kisha nikapelekwa mpaka Bayt Al-Ma'muur.

Amesema Qatadah: Al-Hasan ametuambia akipokea kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ aliona Bayt Al-Ma'muur. Kila siku Malaika elfu sabiini huingia ndani yake, kisha hawarudi tena. Baadaye aliendelea kuihadithia Hadithi ya Anas رضي الله عنه:

«ثُمَّ آتَيْتُ بِإِنَاءٍ مِنْ خَمْرٍ وَإِنَاءٍ مِنْ لَبَنٍ وَإِنَاءٍ مِنْ عَسَلٍ. - قَالَ - فَأَخَذْتُ اللَّبَنَ  
قَالَ: هَذِهِ الْفِطْرَةُ أَنْتَ عَلَيْهَا وَأَمْتُكَ - قَالَ - ثُمَّ فَرَضْتُ عَلَيَّ الصَّلَاةَ خَمْسِينَ  
صَلَاةً كُلَّ يَوْمٍ - قَالَ - فَتَزَلْتُ حَتَّى آتَيْتُ مُوسَى، فَقَالَ: مَا فَرَضَ رَبُّكَ عَلَيَّ  
أَمْتِكَ؟ قَالَ: قُلْتُ: خَمْسِينَ صَلَاةً كُلَّ يَوْمٍ، قَالَ: إِنَّ أَمْتَكَ لَا تَسْتَطِيعُ خَمْسِينَ  
صَلَاةً وَإِنِّي قَدْ خَيْرْتُ النَّاسَ قَبْلَكَ، وَعَالَجْتُ بَنِي إِسْرَائِيلَ أَشَدَّ الْمَعَالَجَةِ، فَارْجِعْ  
إِلَى رَبِّكَ فَاسْأَلْهُ التَّخْفِيفَ لِأَمْتِكَ - قَالَ - فَرَجَعْتُ فَوَضَعَ عَنِّي عَشْرًا - قَالَ -  
فَرَجَعْتُ إِلَى مُوسَى فَقَالَ: بِمِ أَمْرْتُ؟ قُلْتُ: بِأَرْبَعِينَ صَلَاةً كُلَّ يَوْمٍ، قَالَ: إِنَّ  
أَمْتَكَ لَا تَسْتَطِيعُ أَرْبَعِينَ صَلَاةً كُلَّ يَوْمٍ، وَإِنِّي قَدْ خَيْرْتُ النَّاسَ قَبْلَكَ وَعَالَجْتُ بَنِي  
إِسْرَائِيلَ أَشَدَّ الْمَعَالَجَةِ، فَارْجِعْ إِلَى رَبِّكَ فَاسْأَلْهُ التَّخْفِيفَ لِأَمْتِكَ - قَالَ - فَرَجَعْتُ  
فَوَضَعَ عَنِّي عَشْرًا أُخَرَ، فَرَجَعْتُ إِلَى مُوسَى فَقَالَ: بِمِ أَمْرْتُ؟ قُلْتُ: بِثَلَاثِينَ  
صَلَاةً، قَالَ: إِنَّ أَمْتَكَ لَا تَسْتَطِيعُ ثَلَاثِينَ صَلَاةً كُلَّ يَوْمٍ، وَإِنِّي قَدْ خَيْرْتُ النَّاسَ  
قَبْلَكَ وَعَالَجْتُ بَنِي إِسْرَائِيلَ أَشَدَّ الْمَعَالَجَةِ، فَارْجِعْ إِلَى رَبِّكَ فَاسْأَلْهُ التَّخْفِيفَ  
لِأَمْتِكَ - قَالَ - فَرَجَعْتُ فَوَضَعَ عَنِّي عَشْرًا أُخَرَ، فَرَجَعْتُ إِلَى مُوسَى فَقَالَ: بِمِ  
أَمْرْتُ؟ قُلْتُ: أَمْرْتُ بِعِشْرِينَ صَلَاةً كُلَّ يَوْمٍ، قَالَ: إِنَّ أَمْتَكَ لَا تَسْتَطِيعُ عِشْرِينَ  
صَلَاةً كُلَّ يَوْمٍ، وَإِنِّي قَدْ خَيْرْتُ النَّاسَ قَبْلَكَ وَعَالَجْتُ بَنِي إِسْرَائِيلَ أَشَدَّ الْمَعَالَجَةِ،  
فَارْجِعْ إِلَى رَبِّكَ فَاسْأَلْهُ التَّخْفِيفَ لِأَمْتِكَ - قَالَ - فَرَجَعْتُ فَوَضَعَ عَنِّي عَشْرًا أُخَرَ،  
فَرَجَعْتُ إِلَى مُوسَى فَقَالَ: بِمِ أَمْرْتُ؟ قُلْتُ: أَمْرْتُ بِعَشْرِ صَلَوَاتٍ كُلَّ يَوْمٍ، فَقَالَ:  
إِنَّ أَمْتَكَ لَا تَسْتَطِيعُ لِعَشْرِ صَلَوَاتٍ كُلَّ يَوْمٍ، وَإِنِّي قَدْ خَيْرْتُ النَّاسَ قَبْلَكَ وَعَالَجْتُ  
بَنِي إِسْرَائِيلَ أَشَدَّ الْمَعَالَجَةِ، فَارْجِعْ إِلَى رَبِّكَ فَاسْأَلْهُ التَّخْفِيفَ لِأَمْتِكَ - قَالَ -  
فَرَجَعْتُ فَأَمْرْتُ بِخَمْسِ صَلَوَاتٍ كُلَّ يَوْمٍ، فَرَجَعْتُ إِلَى مُوسَى فَقَالَ: بِمِ أَمْرْتُ؟  
قُلْتُ: أَمْرْتُ بِخَمْسِ صَلَوَاتٍ كُلَّ يَوْمٍ، فَقَالَ: إِنَّ أَمْتَكَ لَا تَسْتَطِيعُ لِحَمْسِ  
صَلَوَاتٍ كُلَّ يَوْمٍ، وَإِنِّي قَدْ خَيْرْتُ النَّاسَ قَبْلَكَ وَعَالَجْتُ بَنِي إِسْرَائِيلَ أَشَدَّ  
الْمَعَالَجَةِ، فَارْجِعْ إِلَى رَبِّكَ فَاسْأَلْهُ التَّخْفِيفَ لِأَمْتِكَ - قَالَ - قُلْتُ: قَدْ سَأَلْتُ  
رَبِّي حَتَّى اسْتَحْيَيْتُ، وَلَكِنْ أَرْضَى وَأَسْلَمُ، فَتَمَدَّدْتُ فَنَادَى مُنَادٍ: قَدْ أَمْضَيْتُ  
فَرِيضَتِي وَحَقَّقْتُ عَنْ عِبَادِي»

"Baadaye nikaletewa chombo cha pombe, chombo cha maziwa na chombo cha asali. Nilichagua maziwa, naye Jibril akaniambia: 'Hii ni Fitrah uliokuwa nayo na Ummah wako'. Akasema: 'Kisha



*nikafaradhiwa Sala hamsini kwa kila siku'. Akasema: Nikateremka mpaka nikaja kwa Musa. Akaniuliza: 'Je, Mola wako Mlezi Ameufaradhisia nini Ummah wako?' Nikamuambia: 'Sala hamsini kila siku'. Akasema: 'Hakika Umma wako hautaweza hizo Sala hamsini, nimewajaribu watu kabla yako. Nimekabiliana na Wana wa Israili na ilikuwa ni shida kubwa kwangu. Rudi kwa Mola wako umuombe tahfifu kwa ajili ya Ummah wako'. Akasema: 'Nikarudi kwa Mola wangu, Naye Akanipunguzia kumi.' Baada ya hapo, nikarudi kwa Musa. Akaniuliza: 'Umeamriwa nini?' Nikamuambia: 'Sala arobaini kwa kila siku'. Akasema: 'Hakika Umma wako hautaweza hizo Sala arobaini, nimewajaribu watu kabla yako. Nimekabiliana na Wana wa Israili na ilikuwa ni shida kubwa kwangu. Rudi kwa Mola wako umuombe tahfifu kwa ajili ya Umma wako'. Akasema: 'Nikarudi kwa Mola wangu, Naye Akanipunguzia kumi nyingine.' Baada ya hapo, nikarudi kwa Musa. Akaniuliza: 'Umeamriwa nini?' Nikamuambia: 'Kwa Sala thelathini kwa kila siku'. Akasema: 'Hakika Umma wako hautaweza hizo Sala thelathini, nimewajaribu watu kabla yako. Nimekabiliana na Wana wa Israili na ilikuwa ni shida kubwa kwangu. Rudi kwa Mola wako umuombe tahfifu kwa ajili ya Umma wako'. Akasema: Nikarudi kwa Mola wangu, Naye Akanipunguzia kumi nyingine. Baada ya hapo, nikarudi kwa Musa. Akaniuliza: 'Umeamriwa nini?' Nikamuambia: 'Sala ishirini kwa kila siku'. Akasema: 'Hakika Umma wako hautaweza hizo Sala ishirini, nimewajaribu watu kabla yako. Nimekabiliana na Wana wa Israili na ilikuwa ni shida kubwa kwangu. Rudi kwa Mola wako umuombe tahfifu kwa ajili ya Umma wako'. Akasema: Nikarudi kwa Mola wangu, Naye Akanipunguzia kumi nyingine. Baada ya hapo, nikarudi kwa Musa. Akaniuliza: 'Umeamriwa nini?' Nikamuambia: 'Sala kumi kwa kila siku'. Akasema: 'Hakika Umma wako hautaweza hizo Sala kumi, nimewajaribu watu kabla yako. Nimekabiliana na Wana wa Israili na ilikuwa ni shida kubwa kwangu. Rudi kwa Mola wako umuombe tahfifu kwa ajili ya Umma wako'. Akasema: Nikarudi kwa Mola wangu, Naye Akaniamuru Sala tano kwa kila siku. Baada ya hapo, nikarudi kwa Musa. Akaniuliza: 'Umeamriwa nini?' Nikamuambia: 'Sala tano kwa kila siku'.*

Akasema: 'Hakika Umma wako hautaweza hizo Sala tano kwa kila siku, nimewajaribu watu kabla yako. Nimekabili na Wana wa Israili na ilikuwa ni shida kubwa kwangu. Rudi kwa Mola wako umuombe tahfifu kwa ajili ya Umma wako'. Akasema – Nikamuambia: Hakika nimemuomba Mola wangu mpaka nikaona haya lakini nimeridhia na kujisalimisha kwa kutekeleza hilo. Akanadi mwenye kunadi: 'Hakika Amri Yangu imepitishwa ya Kuwapunguzia mzigo waja Wangu'.

Masimulizi kama haya yamepokewa katika Sahihi mbili<sup>2</sup>.

**Alivyopokea Anas bin Maalik رضي الله عنه kutoka kwa Abu Dharr رضي الله عنه**

Al-Bukhaariy anatupatia ripoti Kutoka kwa Anas bin Maalik رضي الله عنه kuwa amesema: Abu Dharr رضي الله عنه alikuwa akituambia kuwa Mtume wa Allah تعالى amesema:

«فَرَجَ عَنْ سَفْفِ بَيْتِي وَأَنَا بِمَكَّةَ، فَتَزَلَّ جِبْرِيْلُ فَفَرَجَ صَدْرِي ثُمَّ غَسَلَهُ بِمَاءٍ زَمْزَمَ، ثُمَّ جَاءَ بِطُسْتٍ مِنْ ذَهَبٍ مُنْتَلِيَةٍ حِكْمَةً وَإِيمَانًا، فَأَفْرَعَهُ فِي صَدْرِي، ثُمَّ أَطْبَقَهُ ثُمَّ أَخَذَ بِيَدِي فَفَرَجَ بِي إِلَى السَّمَاءِ الدُّنْيَا، فَلَمَّا جِئْتُ إِلَى السَّمَاءِ قَالَ جِبْرِيْلُ لِحَازِنِ السَّمَاءِ: افْتَحْ قَالَ: مَنْ هَذَا؟ قَالَ: جِبْرِيْلُ، قَالَ: هَلْ مَعَكَ أَحَدٌ؟ قَالَ: نَعَمْ مَعِيَ مُحَمَّدٌ ﷺ، فَقَالَ: أُرْسِلْ إِلَيْهِ؟ قَالَ: نَعَمْ فَلَمَّا فَتَحَ عَلَوْنَا السَّمَاءَ الدُّنْيَا فَإِذَا رَجُلٌ قَاعِدٌ عَلَى يَمِينِهِ أَسْوَدَةٌ وَعَلَى يَسَارِهِ أَسْوَدَةٌ، إِذَا نَظَرَ قِبَلَ يَمِينِهِ ضَحِكَ وَإِذَا نَظَرَ قِبَلَ شِمَالِهِ بَكَى، فَقَالَ: مَرَّحِبًا بِالنَّبِيِّ الصَّالِحِ وَالْأَبْنِ الصَّالِحِ - قَالَ - قُلْتُ لِجِبْرِيْلَ: مَنْ هَذَا؟ قَالَ: هَذَا آدَمُ وَهَذِهِ الْأَسْوَدَةُ عَنْ يَمِينِهِ وَعَنْ شِمَالِهِ نَسَمُ بَيْتِهِ، فَأَهْلُ الْيَمِينِ مِنْهُمْ أَهْلُ الْجَنَّةِ، وَالْأَسْوَدَةُ الَّتِي عَنْ شِمَالِهِ أَهْلُ النَّارِ، فَإِذَا نَظَرَ عَنْ يَمِينِهِ ضَحِكَ، وَإِذَا نَظَرَ عَنْ شِمَالِهِ بَكَى، ثُمَّ عَرَجَ بِي إِلَى السَّمَاءِ الثَّانِيَةِ فذكر الحديث قال: «ثُمَّ مَرَرْتُ بِإِبْرَاهِيمَ فَقَالَ: مَرَّحِبًا بِالنَّبِيِّ الصَّالِحِ وَالْأَبْنِ الصَّالِحِ، قُلْتُ: مَنْ هَذَا؟ قَالَ: هَذَا إِبْرَاهِيمُ»

“Sakafu ya nyumba yangu ilifunuliwa nikiwa Makka, Jibril aliteremka

<sup>1</sup> Ahmad 4:208.

<sup>2</sup> Fat'hul Baariy 6:348 na Muslim 1:151.

na kukifunua kifua changu, kisha akakiosha kwa maji ya Zamzam. Kisha akaleta chombo cha dhahabu kilichojaa hekima na Imani, na kuvimimina katika kifua changu na kukifunga tena. Baadae akanishika mkono na kupanda nami hadi uwingu wa dunia (wa kwanza). Tulipofika katika uwingu huo (wa kwanza) alisema Jibril kumuambia mlinzi wa mbingu: 'Fungua'. Akasema: 'Wewe ni nani?' Akasema: 'Jibril'. Akauliza tena: 'Je, upo na yeyote pamoja nawe?' Akajibu: 'Ndio, nipo pamoja na Muhammad'. Akauliza: 'Je, ameshapata Utume (ametumilizwa)?' Akajibu: 'Ndio'. Alipofungua, tulikwenda juu katika uwingu wa kwanza, ambapo nilimuona mtu akiwa ameketi na kundi kubwa la watu kuumeni kwake na wengine kushotoni mwake. Alipoangalia kuumeni kwake alicheka na anapoangalia kushotoni kwake alikuwa analia. Akasema: 'Karibu Nabii mwema na mtoto mwema'. Akasema – Nikamuuliza Jibril: 'Huyu ni nani?' Akasema: 'Huyu ni Adam, na ule umati upande wake wa kulia na kushoto ni roho za kizazi chake. Watu wa kuumeni ni wa Peponi, na wa kushotoni ni wa Motoni. Hivyo, anapoangalia kuliani mwake hucheka (hufurahi) na anapotizama kushotoni mwake hulia'. Kisha akanichukua hadi uwingu wa pili. Akaitaja Hadithi. Baadaye tukampitia Ibraahim, naye akasema: 'Karibu Nabii mwema na mtoto mwema'. Nikauliza: 'Huyu ni nani?' Akasema: 'Huyu ni Ibraahim'.

Az-Zuhriy رحمه الله تعالى akasema: Ibn Hazm رحمه الله تعالى aliniambia kuwa Ibn 'Abbaas na Abu Habbaah al-Answaariy رضي الله عنهما walikuwa wakisema: Mtume ﷺ alisimulia hapa:

«ثُمَّ عَرَّجَ بِي حَتَّى ظَهَرْتُ لِمُسْتَوَى أَسْمَعُ فِيهِ صَرِيْفَ الْأَقْلَامِ»

'Kisha nilipelekwa mpaka nikafika sehemu ambayo nilikuwa nasikia sauti za kalamu'.

Ibn Hazm رحمه الله تعالى na Anas bin Maalik رضي الله عنه walisema: Mtume wa Allah تعالى alisema:

«فَقَرَضَ اللَّهُ عَلَى أُمَّتِي خَمْسِينَ صَلَاةً، فَرَجَعْتُ بِذَلِكَ حَتَّى مَرَرْتُ عَلَى مُوسَى عَلَيْهِ السَّلَامُ، فَقَالَ: مَا قَرَضَ اللَّهُ عَلَى أُمَّتِكَ؟ قُلْتُ: قَرَضَ خَمْسِينَ صَلَاةً، قَالَ مُوسَى: فَارْجِعْ إِلَى رَبِّكَ فَإِنَّ أُمَّتَكَ لَا تُطِيقُ ذَلِكَ، فَرَجَعْتُ فَوَضَعْتُ شَطْرَهَا،

فَرَجَعْتُ إِلَى مُوسَى، قُلْتُ: وَضَعَ شَطْرَهَا، فَقَالَ: ارْجِعْ إِلَى رَبِّكَ، فَإِنَّ أُمَّتَكَ لَا تُطِيقُ ذَلِكَ، فَرَجَعْتُ فَوَضَعَ شَطْرَهَا، فَرَجَعْتُ إِلَيْهِ فَقَالَ: ارْجِعْ إِلَى رَبِّكَ فَإِنَّ أُمَّتَكَ لَا تُطِيقُ ذَلِكَ، فَرَاغَتْهُ فَقَالَ: هِيَ خَمْسٌ وَهِيَ خَمْسُونَ لَا يُبَدِّلُ الْقَوْلُ لَدَيْ، فَرَجَعْتُ إِلَى مُوسَى فَقَالَ: ارْجِعْ إِلَى رَبِّكَ، قُلْتُ: قَدْ اسْتَحْيَيْتُ مِنْ رَبِّي، ثُمَّ انْطَلَقَ بِي حَتَّى انْتَهَى إِلَى سِدْرَةِ الْمُنْتَهَى فَغَشِيَهَا أَلْوَانٌ لَا أُدْرِي مَا هِيَ، ثُمَّ أُدْخِلْتُ الْجَنَّةَ، فَإِذَا فِيهَا حَبَائِلُ اللَّوْلُؤِ، وَإِذَا تُرَابُهَا الْمِسْكَ،

*'Allah Aliufaradhia Umma wangu Sala hamsini, nikarudi nazo mpaka nikafika kwa Nabii Musa. Akaniuliza: 'Allah Ameufaradhisia nini Umma wako?' Nikamuambia: 'Sala hamsini'. Akasema Musa: 'Rudi kwa Mola wako kwani Umma wako hautaweza hilo'. Nikarudi, Naye (Allah) Akanipunguzia nusu yake. Nikarudi tena kwa Musa, nikamuambia: 'Zimepunguzwa nusu'. Akasema: 'Rudi kwa Mola wako kwani Ummah wako hautaweza hilo'. Nikarudi, zikapunguzwa nusu yake. Nikarudi kwake akaniambia: 'Rudi kwa Mola wako kwani Umma wako hautaweza hilo'. Nikarudi, Akaniambia: 'Hizo ni Swala tano nazo ni hamsini, kwani Neno Langu halibadiliki'. Nikarudi kwa Musa, akaniambia: 'Rudi kwa Mola wako'. Nikamuambia: 'Hakika ninaona haya sana kurudi kwa Mola wangu.' Kisha nikachukuliwa mpaka nikafika Sidratul Muntahaa iliyofunikwa na rangi nyingi zisizoeleweka. Baada ya hapo nikaingizwa Peponi, ambamo niliona kamba za lulu na mchanga wake ni manukato ya miski'.*

Riwaya hii imesimuliwa na Al-Bukhaariy katika Kitabu cha Sala, pia katika Kitabu cha Tafsiri, chini ya mazungumzo kuhusu Bani Israili (yaani *Suratul Israa*), Kitabu cha Hijja na Visa vya Manabii kupitia kwa Isnadi tofauti kwa mapokezi ya Yunus رضي الله عنه. Muslim amepokea Hadithi kama hizi katika Sahihi yake Kitabu cha Imani<sup>1</sup>.

Imaam Ahmad amenukuu kuwa 'Abdallah bin Shaqiq amesema: Nilimuuliza Abu Dharr رضي الله عنه: "Lau ningemuona Mtume ﷺ, basi ningemuuliza". Akasema: "Ungemuuliza nini?" Akasema ('Abdallah): "Ningemuuliza kama

<sup>1</sup> Fat'hul Baariy 1: 547, 3: 576, 6: 431 na Muslim 1: 148.

alimuona Mola wake?" Abu Dharr رضي الله عنه akasema: "Nilimuuliza hilo, naye akasema:

«قَدْ رَأَيْتَهُ نُورًا، أَنَّى أَرَاهُ»

*'Nilimuona kama nuru, ningemuona namna gani?'*

Hivi ndivyo ilivyonukuliwa katika mapokezi ya Ahmad<sup>1</sup>. Muslim amehadithia kuwa 'Abdallah bin Shaqiq amesema kuwa Abu Dharr رضي الله عنه amesema: "Nilimuuliza Mtume ﷺ: 'Je, ulimuona Mola wako?' Akasema:

«نُورٌ أَنَّى أَرَاهُ»

*'Ni nuru, vipi nitamuona?'*<sup>2</sup>

'Abdallah bin Shaqiq amesema: Nilimuuliza Abu Dharr رضي الله عنه: 'Lau ningemuona Mtume ﷺ ningemuuliza'. Akasema: 'Ungemuuliza nini?' Nikasema: 'Ningemuuliza: Je, ulimuona Mola wako?' Abu Dharr رضي الله عنه akasema: 'Nilimuuliza kuhusu hilo, naye akaniambia:

«رَأَيْتُ نُورًا»

*'Niliona nuru'*<sup>3</sup>.

**Alivyopokea Jaabir bin 'Abdallah رضي الله عنه**

Ahmad amehadithia kuwa Jaabir bin 'Abdallah رضي الله عنه amesema kuwa alimsikia Mtume ﷺ,

«لَمَّا كَدَّبْتَنِي فَرَنْسَ جِبْنَ أُسْرِي بِي إِلَى بَيْتِ الْمَقْدِسِ، قُمْتُ فِي الْحَجْرِ فَجَلَى اللَّهُ لِي بَيْتِ الْمَقْدِسِ، فَطَفِقْتُ أُخْبِرُهُمْ عَنْ آيَاتِهِ وَأَنَا أَنْظُرُ إِلَيْهِ»

*"Pale Makuraysh waliponikadhibisha nilipokuwa nimepelekwa safari ya usiku mpaka Baytil Maqdis, nilisimama kwenye Al-Hijr. Hapo Allah Alinionesha mbele yangu Baytil Maqdis, hivyo nikawaambia kuhusu ishara zote nilipokuwa naziangalia"*<sup>4</sup>.

Riwaya hii pia imenukuliwa katika Sahihi mbili kwa Isnadi tofauti ya mapokezi<sup>5</sup>.

<sup>1</sup> Ahmad 5:147.

<sup>2</sup> Muslim 1:161.

<sup>3</sup> Muslim 1:161.

<sup>4</sup> Ahmad 3:377.

<sup>5</sup> Al-Bukhaariy 4710 na Muslim 170.

Kulingana na Al-Bayhaqiy na Ibn Shihaab wamesema: Abu Salamah bin 'Abdur-Rahmaan amesema: "Baadhi ya Makuraysh walikwenda kwa Abubakr رضي الله عنه na kumuambia: 'Je, umesikia alivyosema sahibu wako? Anadai kuwa amekwenda *Baytil Maqdis* na kurudi Makkah kwa usiku mmoja!" Abubakr رضي الله عنه akasema: "Je, amesema hivyo?" Wakasema: "Ndio". Abubakr رضي الله عنه akasema: "Ikiwa ni hivyo basi nashuhudia kuwa anasema ukweli". Wakasema: "Unaamini kuwa alikwenda Shaam (Syria Kubwa) kwa usiku mmoja na kurudi Makka kabla ya Alfajiri?" Akasema: "Ndio, ninamuamini kwa mambo yaliyo makubwa kuliko hayo. Ninamuamini kuhusiana na wahyi unaokuja kwake kutoka mbinguni". Abu Salama رضي الله عنه amesema, kuanzia wakati huo Abubakr رضي الله عنه akajulikana kwa jina la *Asw-Swiddiq* (mwenye kusadiki)<sup>1</sup>.

### Alivyopokea 'Abdallah bin 'Abbaas رضي الله عنهما

Imaam Ahmad amehadithia kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: "Usiku aliopolekwa Mtume wa Allah تعالى alipochukuliwa kwa safari ya usiku (*Israa'*), aliingia Peponi, ambamo katika sehemu moja alisikia sauti. Akauliza 'Ewe Jibril, hiyo ni nini?' Akamjibu (Jibril):

*'Huyo ni Bilaal, muadhini'.*

Mtume ﷺ aliporudi kwa watu, alisema:

**«قَدْ أَفْلَحَ بِلَالٌ، رَأَيْتُ لَهُ كَذَا وَكَذَا»**

*'Hakika Bilaal amefaulu, nimeona atakuwa na kadha na kadha'.*

Yeye (Mtume ﷺ) alikutana na Musa عليه السلام, aliyemkaribisha na kumuambia: 'Karibu Mtume *ummiy* (asiyejua kusoma wala kuandika)'. Alikuwa mtu mrefu, mweusi akiwa na nywele zilizonyooka, ndefu zikifika hadi kwenye masikio yake au juu ya masikio yake. Akasema: 'Ee Jibril, huyu ni nani?' Akasema: 'Huyu ni Musa عليه السلام'. Kisha alikwenda mbele na kukutana na mzee wa kustahiwa, kutukuzwa na kuheshimiwa, aliyemkaribisha na kumsalimia kwa salamu, na wote wakawa wanamsalimia. Akasema: 'Ee Jibril, huyu ni nani?' Akajibu (Jibril): 'Huyu ni babako Ibraahim عليه السلام'. Kisha akatizama kwenye Jahannam na kuwaona baadhi ya watu wakila nyama iliyooza. Akauliza: 'Ni

<sup>1</sup> Dalaa'il An-Nubuwwah 2:359.

kina nani hawa, ewe Jibril?' Akasema: 'Hawa ni wale watu waliokuwa wakila nyama za watu (yaani kwa kusengenyu). Baadae akamuona mtu aliyekuwa mwekundu sana na bluu iliyoiva, akauliza: 'Huyu ni nani, ewe Jibril?' Akajibu: 'Huyu ni yule aliyemuua ngamia wa kike wa Swaalih عليه السلام'. Mtume ﷺ alipofika katika Msikiti wa Aqswa, alisimama kwa ajili ya kuswali, na Manabii wote walikusanyika na kuswali naye. Alipomaliza, aliletewa vikombe viwili, kimoja kuliani mwake na kingine kushotoni, kimoja kikiwa na maziwa na kingine asali. Alichukua maziwa na kunywa. Yule aliyechukua kikombe alisema: 'Umechagua *Fitrah* (maumbile)<sup>1</sup>'. Isnadi yake ni Sahihi, japokuwa wao (al-Bukhaariy na Muslim) hawakuipokea.

Imaam Ahmad amehadithia kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: "Mtume ﷺ alichukuliwa kwa safari ya usiku hadi *Baytil Maqdis*, na kisha akarudi na kuwaambia (Makuraysh) kuhusu safari yake na sifa za *Baytil Maqdis* na msafara wa Makuraysh. Baadhi ya watu walisema: 'Hatuamini aliyosema Muhammad', na wakauacha Uislamu na kurudi katika ukafiri. Allah تعالى Aliwaangamiza pale Alipomuangamiza Abu Jahl ('Amr bin Hishaam). Abu Jahl alisema: 'Muhammad anajaribu kutuhofisha na mti wa Zaqqum; lete tende na siagi na tuache tupate zaqqum kidogo'. Mtume ﷺ pia alimuona *Dajjaal* katika sura yake kwa macho yake, sio kumuona katika ndoto. Pia alimuona 'Isaa عليه السلام, Musa عليه السلام na Ibraahim عليه السلام. Mtume ﷺ aliulizwa kuhusu *Dajjaal*, naye akasema:

«رَأَيْتَهُ فَيَلْمَانَا أَفَمَرَّ هَجَانَا، إِحْدَى عَيْنَيْهِ قَائِمَةٌ كَأَنَّهَا كَزَكَبَ دُرِّي، كَأَنَّ شَعْرَ رَأْسِهِ  
أَغْصَانُ شَجَرَةٍ، وَرَأَيْتُ عَيْسَى عَلَيْهِ السَّلَامُ [شَابًا] أَبْيَضَ، جَعَدَ الرَّأْسِ حَدِيدَ  
الْبَصْرِ، وَمُبْطَنَ الْخَلْقِ، وَرَأَيْتُ مُوسَى عَلَيْهِ السَّلَامُ أَسْحَمَ آدَمَ، كَثِيرَ الشَّعْرِ، شَدِيدَ  
الْخَلْقِ، وَنَظَرْتُ إِلَى إِبْرَاهِيمَ عَلَيْهِ السَّلَامُ فَلَمْ أَنْظُرْ إِلَى إِرْبٍ مِنْهُ إِلَّا نَظَرْتُ إِلَيْهِ مِنِّي  
حَتَّى كَأَنَّهُ صَاحِبُكُمْ، قَالَ جِبْرِيلُ: سَلَّمْ عَلَى أَبِيكَ، فَسَلَّمْتُ عَلَيْهِ»

'Nilimuona kama mtu mrefu na mkubwa, akiwa na rangi nyeupe. Moja ya jicho lake lilisimama nje kama nyota ing'ayo. Nywele zake za kichwa zilikuwa kama matawi ya mti. Na nilimuona 'Isaa عليه السلام, kijana mweupe akiwa na nywele zilizopinda, uoni mkali na umbile

<sup>1</sup> Ahmad 1:257.

la mwili wa wastani. Nilimuona Musa عليه السلام, aliyekuwa mweusi, nywele nyingi na mwili wenye nguvu. Nilimtizama Ibraahim عليه السلام, wala sikuona kitu chochote kwake ambacho sikioni kwangu; hata ni kama kwamba yeye ni sahibu wenu'. Akasema Jibrili: 'Msalimie babako'. Nami nikamsalimia".

Na ameipokea An-Nasaa'iy kutoka kwa Hadithi ya Abu Zayd Thaabit bin Yazid kutoka kwa Hilaal رضي الله عنهم, ambaye ni Ibn Khabbaab<sup>1</sup>, na Isnadi yake ni Sahihi.

Na imepokewa kwa Al-Bayhaqiy kutoka kwa Abu Al-'Aaliyah aliyesema: Ametuhadithia mtoto wa Nabii wenu ﷺ, Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما aliyetusimulia kutoka kwa Mtume ﷺ, alisema:

رَأَيْتُ لَيْلَةَ أُسْرِي بِي مُوسَى بْنِ عِمْرَانَ رَجُلًا طَوَّالًا جَعْدًا، كَأَنَّهُ مِنْ رِجَالِ شَوْءَةَ،  
رَأَيْتُ عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ عَلَيْهِ السَّلَامُ مَرْبُوعَ الْخَلْقِ إِلَى الْحُمْرَةِ وَالْبَيَاضِ سَبْطَ  
الرَّأْسِ،

"Usiku wa Israa' nilimuona Musa bin 'Imraan عليه السلام, mrefu mwenye nywele zilizopinda, kama kwamba alikuwa katika kabila la Shanu'ah. Na nilimuona 'Isaa bin Maryam عليه السلام, mwenye umbile la wastani, baina ya weupe na wekundu na nywele zilizonyooka".

Na nikamuona Maalik عليه السلام, mlinzi wa Moto (Jahannam) na Dajjaal, akiwa na alama ambazo Allah تعالى Amenifunulia. Akasema:

فَلَا تَكُنْ فِي مَرْيَةٍ مِّنْ لِّقَائِهِ<sup>ع</sup>

**"Basi usiwe na shaka na kukutana na Allah." (32:23).**

Qataadah alikuwa akifasiri hii kumaanisha kuwa Mtume ﷺ alikutana na Musa عليه السلام:

وَجَعَلْنَاهُ هُدًى لِّبَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿٣٢﴾

**"Na Tukakifanya (au Tukamfanya) uwongofu kwa Wana wa Israili" (32:23).**

Akasema: 'Hii inamaanisha kuwa Allah تعالى Alimjaalia Musa عليه السلام kuwa ni uwongofu kwa Wana wa Israili<sup>2</sup>.

<sup>1</sup> Ahmad 1:374 na an-Nasaa'iy katika al-Kubraa 11484.

<sup>2</sup> Dalaa'il An-Nubuwwah 2:386.



Imepokewa na Muslim katika Sahihi yake na imenukuliwa na Al-Bukhaariy na Muslim kwa muhtasari kutoka kwa Qataadah<sup>1</sup>.

Pia imepokewa na Imaam Ahmad kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: Mtume ﷺ amesema:

«لَمَّا كَانَ لَيْلَةَ أُسْرِي بِي، فَأَضْبَحْتُ بِمَكَّةَ فَطِغْتُ وَعَرَفْتُ أَنَّ النَّاسَ مُكَذِّبِي»

*"Ulipokuwa usiku wa Israa' yangu, nilipambazukiwa Makkah asubuhi ya pili nikiwa na wasiwasi nikijua kuwa watu hawataniamini".*

Akajitenga na watu, akiwa na wasiwasi na huzuni, akapita adui wa Allah, Abu Jahl na akaja kuketi naye akisema kwa stihzai: 'Je, lipo lolote jipya?' Mtume ﷺ akasema:

«نَعَمْ»

'Ndio'. Akauliza: 'Ni lipi hilo?' Akasema ﷺ:

«إِنِّي أُسْرِي بِي اللَّيْلَةَ»

'Nilichukuliwa kwa safari usiku wa jana'. Akaulizwa: 'Mpaka wapi?' Akasema:

«إِلَى بَيْتِ الْمَقْدِسِ»

'Mpaka Baytil Maqdis'. Akaulizwa: 'Kisha asubuhi hii umepambazukiwa pamoja nasi?' Akasema:

«نَعَمْ»

'Ndio'. Abu Jahl hakutaka kumuambia usoni mwake kuwa ameongopa, ili asiwe ni mwenye kubadilika anapowaita watu wengine kuja kumsikiliza. Hivyo alivyomwambia: 'Unaonaje nikiwaita watu wako, utawahadithia kama ulivyo nihadithia?' Mtume ﷺ akasema:

«نَعَمْ»

'Ndio'. Abu Jahl akasema: 'Enyi kongamano la Bani Ka'b bin Lu'ay!' Watu waliinuka pale walipokuwa wameketi na kuja kuketi pamoja nao. Abu Jahl akasema: 'Waambie watu wako uliyoniambia'. Mtume ﷺ akasema:

<sup>1</sup> Al-Bukhaariy 3239 na Muslim 165.

«إِنِّي أُسْرِي بِي اللَّيْلَةَ»

'Hakika nilipelekwa kwa safari ya usiku jana'. Wakauliza: 'Mpaka wapi?' Akasema:

«إِلَى بَيْتِ الْمُقَدِّسِ»

'Mpaka Bayti Maqdis'. Wakasema: 'Kisha asubuhi hii umekuwa nasi?' Akasema:

«نَعَمْ»

'Ndio'. Walianza kupiga makofi na wengine wakaweka mikono yao juu ya vichwa vyao kwa kustaajabu kwa 'uongo' – kama walivyodai. Wakasema: 'Waweza kutuelezea kuhusu Msikiti?' Wapo miongoni mwao waliosafiri kwenye ardhi hiyo na kuuona Msikiti, hivyo Mtume wa Allah تعالى akasema:

*'Nilianza kuwaelezea mpaka nikawa sina yakini kuhusu baadhi ya mambo. Akasema – hapo Msikiti uliletwa karibu na kuwekwa karibu na nyumba ya 'Uqayl – au – 'Iqaal, kwa hiyo nikaweza kuutizama na kuwaelezea.*

Akasema: Sikuweza kukumbuka na kuyahifadhi maelezo hayo. Akasema: watu wakasema: "Ama kuhusu maelezo, naapa kwa Allah تعالى amepatia"<sup>1</sup>. Hii imepokewa na An-Nasaa'iy na Al-Bayhaqiy<sup>2</sup>.

### Riwaya ya 'Abdallah bin Mas'ud رضي الله عنه

Amepokea al-Haafidh Abu Bakr Al-Bayhaqiy رحمه الله تعالى: 'Abdallah bin Mas'ud رضي الله عنه amesema: "Alipopelekwa Mtume ﷺ safari ya usiku, alifika hadi *Sidratul Muntahaa*, nayo iko katika uwingu wa sita. Kila kitu kinachopanda kinamalizikia hapo, mpaka kitakapochukuliwa kutoka hapo, na kila kinachoshuka hukomea hapo, mpaka kitakapochukuliwa kutoka hapo.

إِذْ يَغْشَى السِّدْرَةَ مَا يَغْشَى ﴿١٦﴾

**"Kilipoufinika mkunazi huo kilichoufinika." (53:16)**

<sup>1</sup> Ahmad 1:309.

<sup>2</sup> An-Nasaa'iy katika Al-Kubraa 11285 na Dalaa'il An-Nubuwwah 2:363.

Akasema Ibn Mas'ud رضي الله عنه: 'Umefunikwa na vipepeo wa dhahabu. Na Mtume ﷺ alipatiwa Sala tano na mwisho wa Suratul Baqarah na msamaha ulitolewa kwa madhambi makubwa kwa wasiomshirikisha Allah تعالى kabisa". Muslim ameipokea katika Sahihi yake.

### Riwaya ya 'Umar bin al-Khattwaab رضي الله عنه

Amepokea Imaam Ahmad kuwa Umar bin Al-Khattwaab رضي الله عنه alikuwa katika mji wa Jaabiyah. Akataja kufunguliwa kwa *Baytil Maqdis* akasema: Akasema Abu Salamah, akanihadithia Abu Sinaan kutoka kwa 'Ubayd bin Adam aliyesema: Nilimsikia 'Umar bin Al-Khattwaab رضي الله عنه akimuambia Ka'b: "Waona niswali wapi?" Akajibu: "Ukichukua rai yangu nakushauri uswali nyuma ya jiwe, itakuwa *al-Quds* yote mbele yako". Akasema Umar bin Al-Khattwaab رضي الله عنه: "Umewaiga Mayahudi, lakini nitaswali aliposwali Mtume ﷺ." Hivyo, alikwenda mbele kwenye Qiblah akaswali" Kisha alikuja na kuitandaza nguo yake na kusafisha uchafu kwa nguo yake na watu nao wakamfuata kufanya hilo<sup>1</sup>. Hakulitukuza jiwe kwa kuswali nyuma yake nalo likiwa mbele yake kama alivyoashiria Ka'b, mwanachuoni wa kiyahudi, naye ni katika kaumu waliokuwa wakilitukuza mpaka wakalijaalia kuwa Qiblah chao. Lakini Allah تعالى baadae Alimtunukia Uislamu Ka'b na kumuongoza katika haki, hivyo alipoashiria hilo, Amiri wa Waumini 'Umar رضي الله عنه alimuambia: "Kuwaiga Mayahudi sitaweza na wala siwezi kufanya udhalilishaji kama Wakristo ambao wameifanya kuwa ni jaa la taka - kwa kuwa ni Qiblah cha Mayahudi, lakini aliuondosha uchafu kwa nguo yake".

### Riwaya ya Abu Hurayrah رضي الله عنه

Imenukuliwa katika Sahihi mbili, al-Bukhaariy na Muslim kutoka Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema:

«جِئْنَا أَسْرِيَّ بِي، لَقَيْتُ مُوسَى عَلَيْهِ السَّلَامُ - فَتَعَتَهُ، فَإِذَا رَجُلٌ حَسْبُهُ قَالَ -  
مُضْطَرِبٌ رَجُلٌ الرَّأْسِ كَأَنَّهُ مِنْ رِجَالِ شَتْوَةَ، قَالَ: وَلَقَيْتُ عَيْسَى - فَتَعَتَهُ  
النَّبِيُّ ﷺ قَالَ - رَبِغَةٌ أَحْمَرٌ كَأَنَّمَا خَرَجَ مِنْ دِيمَاسٍ - يَغْنِي حَمَامًا، قَالَ - وَلَقَيْتُ  
إِبْرَاهِيمَ وَأَنَا أَشْبَهُ وَلَدِهِ بِهِ، قَالَ: وَأَتَيْتُ بِإِنَاءَيْنِ فِي أَحَدِهِمَا لَبَنٌ وَفِي الْآخَرِ خَمْرٌ،

<sup>1</sup> Ahmad 1:38.

قِيلَ لِي: خُذْ أَيُّهُمَا شِئْتَ، فَأَخَذْتُ اللَّبْنَ فَشَرِبْتُ، فَقِيلَ لِي: هُدَيْتَ الْفِطْرَةَ - أَوْ  
أَصَبْتَ الْفِطْرَةَ - أَمَا إِنَّكَ لَوْ أَخَذْتَ الْخَمْرَ عَوْتُ أُمَّتِكَ

*"Nilipochukuliwa katika safari ya usiku, nilikutana na Musa عليه السلام. Alimuelezea kama mtu – nadhania alisema – mwenye nywele zilizo kunjana, kama kwamba ni mtu wa kabila la Shanu'ah. Akasema: Nilikutana na 'Isa عليه السلام, Mtume ﷺ akamuelezea kuwa ni mtu mwenye kimo cha wastani, wa rangi nyekundu, kama aliyetoka bafuni. Akasema: Nikakutana na Ibraahim عليه السلام, nami nashabihiana naye sana miongoni mwa watoto wake. Akasema: Nikaletewa vyombo viwili, ndani ya kimoja wapo kilikuwa na maziwa na cha pili pombe. Nikaambiwa: 'Chukua chochote unachotaka'. Nilichukua maziwa na kuyanywa. Nikaambiwa: 'Umeongozwa katika asili yenyewe "Fitrah" au umechagua Fitrah. Hakika lau ungechukua pombe Ummah wako ungekengeuka (ungepotea)"<sup>1</sup>.*

Pia wameipokea kwa njia nyingine. Na katika Sahihi Muslim kutoka kwa Abu Hurayrah عنه رضي الله امهsema: Mtume ﷺ amesema:

لَقَدْ رَأَيْتِي فِي الْحَجْرِ وَقُرَيْشٌ تَسْأَلُنِي عَنْ مَسْرَائِي، فَسَأَلُونِي عَنْ أَشْيَاءٍ مِنْ بَيْتِ  
الْمَقْدِسِ لَمْ أَنْبِئْهَا، فَكُرْبْتُ [كُرْبَةً] مَا كُرْبْتُ مِنْهُ قَطُّ، فَرَفَعَهُ اللَّهُ إِلَيَّ أَنْظُرُ إِلَيْهِ مَا  
سَأَلُونِي عَنْ شَيْءٍ إِلَّا أَنْبَأْتُهُمْ بِهِ، وَقَدْ رَأَيْتِي فِي جَمَاعَةٍ مِنَ الْأَنْبِيَاءِ، وَإِذَا مُوسَى  
قَائِمٌ يُصَلِّي، وَإِذَا هُوَ رَجُلٌ جَعَدَ كَأَنَّهُ مِنْ رِجَالِ سُوءَةٍ، وَإِذَا عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ قَائِمٌ  
يُصَلِّي أَقْرَبَ النَّاسِ شَبَهَا بِهِ عَزْرَةَ بَنِي مَسْعُودٍ التَّقْفِيِّ، وَإِذَا إِبْرَاهِيمَ قَائِمٌ يُصَلِّي  
أَقْرَبَ النَّاسِ شَبَهَا بِهِ صَاحِبِكُمْ - يَعْنِي نَفْسَهُ - فَحَانَتِ الصَّلَاةُ فَأَمَمْتُهُمْ، فَلَمَّا  
فَرَعْتُ قَالَ قَائِلٌ: يَا مُحَمَّدُ هَذَا مَالِكُ حَازِرُنْ جَهَنَّمَ، [فَسَلَّمْ عَلَيْهِ] فَانْتَقَتْ إِلَيْهِ  
قَبْدَانِي بِالسَّلَامِ

*"Nakumbuka nilikuwa kwenye Al-Hijr, na Quraysh wananiuliza kuhusu safari yangu ya usiku. Waliniuliza vitu kuhusu Baytil Maqdis ambavyo sikuwa na hakika navyo, nilipatwa na wasiwasi na mfadhaiko ambao sijawahi kabisa kupatwa. Allah Aliinyanyua Baytil Maqdis kwangu ili nipate kuiona, hawakuniuliza chochote ila*

<sup>1</sup> Fat'h al-Baariy 6:493 na Muslim 1:154.

*niliwaambia. Hakika nilikuwa pamoja na kundi la Manabii. Musa عليه السلام alikuwa amesimama akiwa anasali, naye alikuwa na nywele zilizopinda kama kwamba ni mtu wa Shanu'ah. Nilimuona 'Isa bin Maryam عليه السلام akiwa amesimama anasali, na anafanana sana na 'Urwah bin Mas'ud. Na nilimuona Ibraahim عليه السلام akiwa amesimama anasali, na anayefanana naye sana miongoni mwa watu ni sahibu wenu (akimaanisha yeye mwenyewe). Wakati wa Sala ulifika, nami niliwaongoza (Imaam wao) katika Sala. Nilipomaliza, alisema msemaji: 'Ewe Muhammad! Huyu ni Maalik, mlinzi wa Moto (msalimie)'. Niligeuka kumtizama, akaanza yeye kunisalimia"<sup>1</sup>.*

### **Riwaya ya Aishah رضي الله عنها**

Al-Bayhaqiy رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa mama Aishah رضي الله عنها aliyesema: "Alipopeleka safari ya usiku Mtume ﷺ hadi *Baytil Maqdis*, alipambazuka akiwahadithia watu kuhusu hilo. Waliritadi watu waliokuwa wameamini na kumsadiki, wakaenda haraka kwa Abubakr رضي الله عنه na habari hizo. Wakamuambia: 'Je, umesikia anavyosema sahibu wako? Anadai kuwa amekwenda safari ya usiku mpaka *Baytil Maqdis*'. Akawauliza: 'Je, amesema hayo?' Wakasema: 'Ndio'. Akasema: 'Lau amesema hilo basi itakuwa ni kweli'. Wakasema: 'Unamsadikisha kuwa amekwenda usiku mpaka *Baytil Maqdis* na kurudi kabla hakuja pambazuka?' Akasema: 'Ndio, hakika mimi namsadiki yeye kwa yaliyo zaidi ya hayo. Mimi namsadiki kwa habari za mbinguni katika asubuhi na mapema au jioni'. Kwa ajili hiyo akaitwa Abubakr Asw-iddiq (mwenye kusadiki) رضي الله عنه"<sup>2</sup>.

### **Safari ya Israa': Hakika Ilikuwa Mwili na Roho, Mtume ﷺ akiwa Macho Si Usingizini wala Si katika Ndoto.**

Musa bin Uqbah amesema kutoka kwa Az-Zuhri رحمه الله تعالى: "*Israa'* ilikuwa kabla ya Hijrah kwa mwaka"<sup>3</sup>. Hivyo ndivyo alivyosema Urwah<sup>4</sup>. Na As-Suddiy amesema: "Ilitokea miezi kumi na sita (16) kabla ya Hijrah"<sup>5</sup>.

<sup>1</sup> Muslim 1:156 kutoka kwa Zuhayr bin Harb.

<sup>2</sup> Dalaa'il An-Nubuwwah 2:360.

<sup>3</sup> Dalaa'il An-Nubuwwah 2:355.

<sup>4</sup> Dalaa'il An-Nubuwwah 2:354.

<sup>5</sup> Al-Qurtwubiy 10:210.

Uhakika wa mambo ni kuwa Mtume ﷺ alichukuliwa kwa safari ya usiku akiwa macho, sio katika ndoto kutoka Makkah mpaka *Baytil Maqdis* akiwa amempanda *Buraaq*. Alipowasili katika mlango wa Msikiti alimfunga mnyama mlangoni na kuingia ndani, ambamo aliswali raka mbili ya kuusalimia Msikiti (*Tahiyatul Masjid*). Kisha akaletewa *Mi'raaj*, nayo ni kama ngazi ambayo ina vidaraja vya kupandia juu. Akapanda kwayo mpaka uwingu wa dunia (wa kwanza), kisha kwa mbingu saba zilizobakia. Katika kila uwingu alikaribishwa na walio wema miongoni mwa wakazi wake, na kuwasalimia Manabii waliokuwa katika kila wingu kulingana na daraja na hadhi zao. Alipita kwa Musa عليه السلام, Nabii aliyezungumza na Allah تعالى, katika uwingu wa sita na Ibraahim عليه السلام, rafiki wa karibu wa Allah تعالى (*Khalil*) katika uwingu wa saba. Kisha aliwapita wote na Manabii wote kwa hadhi na kufikia daraja ambayo aliweza kusikia sauti za kalamu, yaani kalamu za Kudura ambazo zinaandika yaliyokadariwa kufanyika. Aliona *Sidratul Muntahaa*, ukiwa umefunikwa na Maagizo ya Allah تعالى, na Ukubwa Wake, vipepeo vyake vya dhahabu na rangi tofauti, ukiwa umezungukwa na Malaika. Hapo alimuona Jibril katika hali yake ya asili, akiwa na mabawa mia sita (600). Zikiwa na mapambo ya kijani zimeziba mbinguni. Aliona *Bayt al-Ma'muur*, na Ibraahim al-Khalil عليه السلام, mjenzi wa Ka'bah ya duniani akiwa ameegemea kwayo, Ka'bah ya mbinguni; kila siku, Malaika elfu sabiini huingia kuabudu ndani yake, baadae hawarudi tena mpaka Siku ya Kiyama. Aliona Pepo na Moto, na Allah تعالى Akamfaradhisia Sala hamsini, kisha Akazipunguza mpaka zikafika tano, kwa Rehema, Upole na Huruma kutoka Kwake kwa waja Wake. Katika hili kuna ishara ya Ukubwa, Uzito na Fadhila za Sala.

Baada ya hapo alirudi mpaka *Baytil Maqdis*, na Manabii walishuka naye, naye akawaongoza katika Swala, wakati wa Swala ulipofika. Inawezekana kuwa ilikuwa ni Swala ya Alfajiri ya siku hiyo. Baadhi ya watu wanadai kuwa aliwaswalisha Swala huko mbinguni, lakini riwaya zinaashiria kueleza kuwa ilikuwa *Baytil Maqdis*. Katika riwaya nyingine zinatueleza kuwa hilo lilifanyika pale alipoingia mara ya kwanza (kabla ya kuelekea mbinguni), lakini uwezekano ni mkubwa zaidi kuwa hilo lilifanyika aliporudi, kwa sababu alipopita alipokuwa anapanda katika kila uwingu mmoja alikuwa anamuuliza Jibril عليه السلام kuhusu wao, mmoja baada ya mwingine, naye Jibril عليه السلام alikuwa akimuelezea kuhusu wao. Na hili ndilo lawezekana zaidi kwani awali ya yote alihitajika kufika mbele ya Allah تعالى, ili yale Aliyotaka Allah تعالى yaamuriwe kwake na

Umma wake. Pindi lile jambo ambalo alihitajika kulipata lishashughulikiwa, yeye na ndugu zake – Manabii walikusanywa, hapo fadhila na daraja yake kuu kulingana nao ilijitokeza wazi alipoashiriwa na Jibril عليه السلام kuswalisha.

Kisha alitoka *Baytil Maqdis* na kumpanda *Buraaq* hadi Makka katika giza la usiku. Na Allah تعالى Anajua zaidi. Ama kule kupatiwa vyombo vya vinywaji vilivyokuwa na maziwa na asali, au maziwa na pombe, au maziwa na maji, au vyote hivyo, baadhi ya riwaya zinatueleza kuwa hilo lilifanyika *Baytil Maqdis*, na wengine wanasema kuwa zoezi hilo lilifanyika mbinguni. Upo uwezekano kuwa hilo lilifanyika katika sehemu hizo zote, kwa sababu ni kama kumpatia mgeni chakula au kinywaji anapofika. Allah تعالى Anajua zaidi.

Mtume ﷺ alichukuliwa kwa safari ya usiku kimwili na kiroho, alikuwa macho, wala sio usingizini. Dalili ya hili ni Aya ifuatayo:

سُبْحَانَ الَّذِي أَسْرَى بِعَبْدِهِ لَيْلًا مِّنَ الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ إِلَى الْمَسْجِدِ الْأَقْصَا الَّذِي  
بَرَكْنَا حَوْلَهُ

***“Ametakasika Aliyemchukua mja Wake usiku mmoja kutoka Msikiti Mtukufu mpaka Msikiti wa Mbali, ambao Tumevibariki vilivyouzunguka”.*** (17:1)

Neno la *Tasbih* (*Subhaanallaah* – Utakaso na Utukufu ni wa Allah تعالى) linazungumzwa kuhusiana na jambo kuu. Ingekuwa ni katika ndoto basi halingekuwa ni jambo kubwa, wala makafiri wa Kikuraish wasingelistaajabu na wala wasingeliharakisha kumuambia yeye kuwa muongo, na kikundi cha Waislamu hawangeritadi. Kadhalika neno ‘*Abd* (mja)’ ni ibara inayojumlisha roho na mwili. Na hakika Amesema Aliyetukuka:

أَسْرَى بِعَبْدِهِ لَيْلًا

***“Aliyemchukua mja Wake usiku mmoja.”*** Na Allah تعالى Amesema

وَمَا جَعَلْنَا الرُّءْيَا الَّتِي أَرَيْنَاكَ إِلَّا فِتْنَةً لِلنَّاسِ

***“Na Hatukufanya muono (Ru’ya) Tuliokuonesha ila ni kuwajaribu watu.”*** (17:60).

Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Huu ni uonaji wa macho aliooneshwa

Mtume ﷺ katika safari aliyopelekwa usiku. Na mti uliolaaniwa, ni mti wa *Zaqquum*<sup>1</sup>. Hii imenukuliwa na Al-Bukhaariy. Allah تعالى Anasema:

مَا زَاغَ الْبَصَرُ وَمَا طَغَىٰ

**“Jicho halikuhangaika wala halikuruka mpaka uliowekewa.” (53:17).**

Na *Al-Baswar* (jicho) ni miongoni mwa ala na kiungo cha dhati sio roho, na pia kuwa alichukuliwa na *Buraaq*, naye ni mnyama mweupe anaye ng’aa. Hakika hili linakuwa kwa kiwiliwili, sio roho, kwa sababu roho haihitajii harakati na usafiri wa aina hii unahitajia kipando. Na Allah تعالى Anajua zaidi.

### Hadithi ya Kupendeza

Al-Haafidh Abu Nu’aym Al-Iswbahaaniy رحمه الله تعالى Amepokea katika kitabu chake *Dalaa’il An-Nubuwwah* kutoka kwa Muhammad bin Umar Al-Waaqidiy aliyesema: Amenihadithia Malik bin Abir Rijaal kutoka kwa ‘Amr bin ‘Abdallah kutoka kwa Muhammad bin Ka’b al-Quradhiy, ambaye amesema: Mtume ﷺ alimtuma Dihyah bin Khalifah kwa Kaisari (Kaisari – cheo cha mfalme wa Warumi). Alitaja alivyokuja kwake, na katika maelezo kuna uthibitisho mkubwa kwa umahiri na hekima ya Kaisari. Kisha aliwaita wafanya biashara (wa Kiarabu) waliokuwa Shaam (Syria kubwa). Akaja Abu Sufyaan Swakhr bin Harb na sahibu zake. Aliwauliza maswali mashuhuri yaliyonukuliwa na al-Bukhaariy na Muslim, kama tutakavyojadili hapa chini, naye Abu Sufyaan alijaribu sana kulitweza jambo hilo na kulifanya dogo sana mbele yake. Akasema (Abu Sufyaan) katika maelezo yake (baadaye): “Wallahi (Naapa kwa Allah تعالى), hakuna kilichonizuilia kusema kitu kwa Heraql (Heraclius) kumfanya amchukie (Muhammad) lakini ule ukweli kuwa sikutaka kusema uongo ambao baadaye utakuja gunduliwa, naye hataniamini tena baada ya hapo. Kisha nilimuambia kuhusu ule usiku ambao (Mtume Muhammad) alichukuliwa kwa safari. Nikamuambia: ‘Ewe mfalme! Sikuambii jambo ambalo kwayo utajua kuwa yeye ni mwongo?’ Akasema: “Ni jambo gani hilo?” Nikasema: “Anadai kuwa alikwenda nje ya ardhi yetu, ardhi Tukufu, kwa usiku mmoja, akaja mpaka Msikiti wenu, Msikiti wa *Ilyyaa’* (al-Quds au Jerusalem) na akarudi kwetu usiku huo huo kabla kupambazuka (asubuhi)”. Askofu mkuu wa Al-Quds alikuwepo hapo, akiwa amesimama ubavuni mwa Kaisari. Askofu mkuu wa

<sup>1</sup> Fat’h al-Baariy 8: 250.



Al-Quds alisema: “Naujua usiku huo”. Kaisari alimtizama, akasema: “Na ni nani aliyekujulisha hilo?” Akasema: “Sikuwa nikilala usiku mpaka nifunge milango yote ya Msikiti. Usiku huo nilifunga milango yote ila mmoja, ambao sikuweza kuufunga. Niliwaambia wafanya kazi wangu na wengineo waliokuwa pamoja nami wanisaidie kuushughulikia, lakini hatukuweza kuusukuma. Ilikuwa ni kama kusukuma mlima. Hivyo, niliwaita mafundi seremala, nao wakautizama na kusema: ‘Linta na sehemu ya mlango imeachana. Hatuwezi kuusukuma mpaka asubuhi, ambamo tutaweza kutizama tatizo lake’. Kwa hiyo, nilikwenda zangu nikaiacha milango hiyo ikiwa wazi. Kulipopambazuka nilirudi tena, nikaona kuwa jiwe lililokuwa pembeni mwa Msikiti lilikuwa na tundu, na kulikuwa na alama za mnyama aliyekuwa amefungwa hapo. Niliwaambia sahibu zangu (tuliokuwa nao): ‘Mlango huu haukufungwa usiku uliopita kwa sababu ya Mtume ﷺ, aliyesali usiku uliopita katika Msikiti wetu”. Akataja Hadithi kwa ukamilifu wake.

(Faida) Al-Haafidh Abul Khattwaab ‘Umar bin Dihyah رحمه الله تعالى katika Kitabu chake *“At-Tanwiir fi Mawlid As-Siraaj Al-Munir”* ameitaja Hadithi ya Israa’ iliyopokewa na Anas رضي الله عنه, na kuizungumzia vyema. Kisha akasema: “Riwaya za Hadithi za *Israa’* zimefikia daraja ya *Mutawaatir* (upokezi wa watu wengi katika kila kipindi cha mapokezi yake). Zimepokewa kutoka kwa Umar bin Al-Khattwaab, ‘Aliy, Ibn Mas’ud, Abu Dharr, Malik bin Swa’swa’ah, Abu Hurayrah, Abu Sa’id, Ibn ‘Abbaas, Shaddaad bin Aws, Ubayy bin Ka’b, ‘Abdur-Rahman bin Qarat, Abu Habbah Al-Answaariy, Abu Laylaa Al-Answaariy, Abdallah bin ‘Amr, Jaabir bin Hudhayfah, Buraydah, Abu Ayyub, Abu Umaamah, Samurah bin Jundub, Abu Al-Hamraa’, Suhayb Ar-Rumiy, Umm Haaniy, Aishah na Asmaa bint Abubakar *Asw-Swiddiq* رضي الله عنهم. Baadhi yao wamekisimulia kisa hiki kwa kina na wengine kwa kifupi kama kilivyonukuliwa kutoka katika Musnad. Japokuwa, baadhi ya riwaya hazijatimiza masharti ya Hadithi Sahihi, hata hivyo, Waislamu wamekubaliana kwa kauli moja (*Ijmaa’*) uhakika na ukweli wa kuwa *Israa’* ilitokea. Tukio hilo lilikataliwa tu na waasi pamoja na wakanaji Dini”. Allaah تعالى Anasema:

يُرِيدُونَ لِيُطْفِئُوا نُورَ اللَّهِ بِأَفْوَاهِهِمْ وَاللَّهُ مُتِمُّ نُورِهِ وَلَوْ كَرِهَ الْكَافِرُونَ ﴿٦٨﴾

**“Wanataka kuzima nuru ya Allah (ya Uislamu) kwa vinywa vyao; na Allah Atakamilisha nuru Yake ijapokuwa makafiri watachukia” (61:8).**

وَأَتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ وَجَعَلْنَاهُ هُدًى لِّبَنِي إِسْرَائِيلَ إِلَّا تَتَّخِذُوا مِن دُونِي وَكَيْلًا ﴿١٧﴾  
 ذُرِّيَّةً مِّن حَمَلْنَا مَعَ نُوحٍ إِنَّهُ كَانَ عَبْدًا شَكُورًا ﴿١٨﴾

**2. Na Tukampa Musa Kitabu, na Tukakifanya uongofu kwa Wana wa Israili. (Tukawambia): Msiwe na mtegemewa ila Mimi!**

**3. Enyi kizazi Tuliowachukua pamoja na Nuuh! Hakika yeye alikuwa mja mwenye shukrani.**

**Kutajwa kwa Musa عليه السلام na Vipi Kapewa Kwake Kitabu cha Taurati**

Allah Aliyetukuka Alipotaja kuwa Alimchukua mja Wake Muhammad ﷺ kwa safari ya usiku, Alifuatia kwa kumtaja Musa عليه السلام, mja na Mtume Wake ﷺ, ambaye ni mzungumzi Wake. Allah تعالى mara nyingi sana Anawataja Musa na Muhammad (Rehema na Amani ya Allah تعالى iwashukie wao) pamoja, pia Anaitaja Taurati na Qur'ani pamoja. Hivyo, baada ya kuitaja *Israa'* Anasema Aliyetukuka:

وَأَتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ

**"Na Tukampa Musa Kitabu."** Maana: Taurati.

وَجَعَلْنَاهُ

**"Na Tukakifanya (Tukakijaalia)."** Kumaanisha Kitabu,

هُدًى

**"Uongofu."** Kumaanisha kuwaongoza,

لِّبَنِي إِسْرَائِيلَ إِلَّا تَتَّخِذُوا

**"Wana wa Israili. Tukawaambia: Msimchukue."**

Maana yake: Msinfanye.

مِن دُونِي وَكَيْلًا ﴿١٧﴾

**"Asiyekuwa Mimi mtegemewa."**

Maana yake: Mlinzi, msaidizi au muabudiwa mbali na Mimi (asiyekuwa Mimi), kwani Allah تعالى Alimteremshia kila Mtume aliyempa muongozo awe ni mwenye kumuabudu Yeye Peke Yake bila kumshirikisha kabisa. Kisha Akasema:

ذُرِّيَّةَ مَنْ حَمَلْنَا مَعَ نُوحٍ

**“Enyi kizazi Tuliowachukua pamoja na Nuuh!”** Kwa kukadiria Kwake kuwahutubia kizazi cha wale waliochukuliwa katika safina pamoja na Nuuh عليه السلام, upo ukumbusho kwa ile baraka, ni kama kwamba Allah تعالى Anasema: ‘Enyi kizazi, cha wale Tuliowaokoa na Kuwachukua katika safina pamoja na Nuuh عليه السلام, fuateni nyayo (muigeni na jifananisheni) za baba yenu.’ Sababu ya hilo ni kuwa:

إِنَّهُ كَانَ عَبْدًا شَكُورًا ﴿٢٠﴾

**“Hakika yeye alikuwa mja mwenye shukrani”.** Kwa hiyo, kumbukeni neema Yangu kwenu kwa Kuwatumia Muhammad ﷺ.

Ampokea Imaam Ahmad kutoka kwa Anas bin Maalik عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ اللَّهَ لَيَرْضَى عَنِ الْعَبْدِ أَنْ يَأْكُلَ الْأَكْلَةَ أَوْ يَشْرَبَ الشَّرْبَةَ فَيَحْمَدَ اللَّهَ عَلَيْهَا»

*“Hakika Allah Anamridhia mja Wake pindi anapokula chakula au kunywa kinywaji, akamshukuru Allah kwayo.”<sup>1</sup>*

Hadithi hii imenukuliwa pia na Muslim, at-Tirmidhiy na an-Nasaa’iy<sup>2</sup>.

Maalik amesema kuhusu Zayd bin Aslam: “Alikuwa akimshukuru na kumsifu Allah تعالى katika hali zote”. Katika muktadha huu, Al-Bukhaariy ameitaja Hadithi ya Abu Zur’ah akisimulia kutoka kwa Abu Hurayrah عنه رضي الله aliyesema kuwa Mtume ﷺ amesema:

«أَنَا سَيِّدُ وَلَدِ آدَمَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

*“Mimi nitakuwa bwana (kiongozi) wa watoto wa Adam Siku ya Kiyama...”*

Kwa urefu wake, na ndani yake – watamjia Nuuh عليه السلام na kumuambia:

«فَيَأْتُونَ نُوحًا فَيَقُولُونَ: يَا نُوحُ إِنَّكَ أَنْتَ أَوَّلُ الرُّسُلِ إِلَى أَهْلِ الْأَرْضِ، وَقَدْ سَمَّاكَ  
اللهُ عَبْدًا شَكُورًا، فَاشْفَعْ لَنَا إِلَى رَبِّكَ»

*‘Ewe Nuuh! Wewe ni Mtume wa kwanza uliyetumwa kwa watu wa*

<sup>1</sup> Ahmad 3:117.

<sup>2</sup> Muslim 4:2095, Tuhfatul Al-Ahwadhiy 5:536 na An-Nasaa’iy katika Al-Kubraa 4:202.

ardhi na Allah Amekuita mja mwenye shukrani, hivyo tuombe kwa Mola wako Mlezi<sup>1</sup>. Akaitaja Hadithi kwa ukamilifu wake.

وَقَضَيْنَا إِلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ فِي الْكِتَابِ لَتُفْسِدُنَّ فِي الْأَرْضِ مَرَّتَيْنِ وَلَتَعْلُنَّ عُلُوًّا كَبِيرًا ﴿١﴾  
 فَإِذَا جَاءَ وَعْدُ أُولُنهُمَا بَعَثْنَا عَلَيْكُمْ عِبَادًا لَنَا أُولَىٰ بَأْسٍ شَدِيدٍ فَجَاسُوا خِلَلِ الدِّيَارِ  
 وَكَانَ وَعْدًا مَّفْعُولًا ﴿٢﴾ ثُمَّ رَدَدْنَا لَكُمُ الْكَرَّةَ عَلَيْهِمْ وَأَمْدَدْنَاكُم بِأَمْوَالٍ وَبَنِينَ  
 وَجَعَلْنَاكُمْ أَكْثَرَ نَفِيرًا ﴿٣﴾ إِنَّ أَحْسَنَكُمْ أَحْسَنْتُمْ لِأَنْفُسِكُمْ ۗ وَإِنْ أَسَأْتُمْ فَلَهَا ۗ فَإِذَا جَاءَ  
 وَعْدُ الْآخِرَةِ لِيَسُئَرُوا وُجُوهَكُمْ وَلِيَدْخُلُوا الْمَسْجِدَ كَمَا دَخَلُوهُ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَلِيُتَبَرُوا مَا  
 عَلَوُا تَتْبِيرًا ﴿٤﴾ عَسَىٰ رَبُّكُمْ أَنْ يَرْحَمَكُمْ ۗ وَإِنْ عُدتُمْ عُدتْنَا ۗ وَجَعَلْنَا جَهَنَّمَ لِلْكَافِرِينَ  
 حَصِيرًا ﴿٥﴾

**4. Na Tukawahukumia Wana wa Israili katika Kitabu kwamba: Hakika nyinyi mtafanya ufisadi katika nchi mara mbili, na kwa yakini mtapanda kiburi, kiburi kikubwa.**

**5. Basi itapofika ahadi ya kwanza yake Tulikupelekeeni waja Wetu wa kali kwa vita. Watakuingilieni ndani ya majumba. Na hii ilikuwa ahadi iliyotimizwa.**

**6. Kisha Tukakurudishieni nguvu zenu dhidi yao, na Tukakuongezeeni mali na wana, na Tukakujaalieni mkawa wengi zaidi.**

**7. Basi mkifanya wema, mnajifanyia wema nafsi zenu. Na mkifanya ubaya, mnajifanyia wenyewe. Na ikifika ahadi ya mwisho ili wazidhalilisha nyuso zenu, na waingie Msikitini kama walivyoingia mara ya kwanza, na waharibu kila walichokiteka kwa uharibifu mkubwa.**

**8. Huenda Mola wenu Mlezi Akakurehemuni. Na mkirudia na Sisi Tutarudia. Na Tumeifanya Jahannamu kuwa ni gereza kwa ajili ya makafiri.**

<sup>1</sup> Fat'hul al-Baari 6:428.

### Imetajwa katika Taurati kuwa Mayahudi Watafanya Uharibifu mara Mbili

Allah تعالی Anatupasha habari kuwa Yeye Amehukumu kwa Wana wa Israili katika Kitabu, kumaanisha kuwa Amewaambia katika Kitabu walicho - teremshiwa kuwa watafanya uharibifu (ufisadi) katika ardhi mara mbili, na kuwa watapanda kiburi, kiburi kikubwa. Hii inamaanisha kuwa watafanya ujabari na udikteta, watakengeuka, watajawa na kiburi na kunyanyasa watu. Kama isemavyo Kauli Yake Allah تعالی,

﴿وَقَضَيْنَا إِلَيْهِ ذَلِكَ الْأَمْرَ أَنَّ دَابِرَ هَتُولَاءِ مَقْطُوعٌ مُّصْبِحِينَ﴾

**“Na Tukamkatia jambo hilo; ya kwamba mizizi yao itakatwa asubuhi (wataangamizwa).” (15:66),**

Maana: Tulimjulisha na kumfahamisha tayari kuhusu hilo.

### Ufisadi wa Kwanza wa Wana wa Israili na Jaza ya Adhabu Juu Yao

Na Kauli Yake تعالی:

﴿فَإِذَا جَاءَ وَعْدُ أُولَئِهِمَا﴾

**“Basi itapofika ahadi ya kwanza yake.”** Maana yake: Uharibu wa mwanzo kati ya miwili iliyotajwa.

﴿بَعَثْنَا عَلَيْكُمْ عِبَادًا لَّنَا أُولِي بَأْسٍ شَدِيدٍ﴾

**“Tulikupelekeeni waja Wetu wa kali kwa vita.”** Maana yake: Tuliwasaliti dhidi yenu jeshi miongoni mwa viumbe Vyetu waliokuwa wakali katika vita. Hii ina maana kuwa hao viumbe walikuwa na nguvu, maandalizi, silaha na uongozi. Waliingia mpaka ndani kabisa ya nyumba zenu, kumaanisha walichukua umiliki wa ardhi yenu na kuvamia vyumba vya ndani kabisa katika nyumba zenu, wakitembea baina ya nyumba zenu huku wakienda na kurudi kwa uhuru wao wakiwa hawana hofu na yeyote. Hii ilikuwa ni ahadi iliyotimia kikamilifu.

Wafasiri wa mwanzo na wa baadae wametofautiana kuhusu wavamizi hawa. Je, wao ni kina nani? Hakika zimepokewa riwaya nyingi za *Israiliat* (masimulizi kutoka katika machimbuko ya Kiyahudi), lakini sikutaka kukifanya kitabu hiki kuwa kikubwa kwa kuzitaja kwani baadhi ya hizo zimebuniwa (kuzuliwa) na baadhi ya wazandiki wao na nyingine huenda zikawa ni Sahihi. Hata hivyo,

hatuna haja nazo hapa. Allah تعالی Ndiye Mwenye Kuhimidiwa. Yale Aliyotusimulia Allah تعالی katika Kitabu Chake (Qur'ani) inatosha nasi hatuna haja kwa yaliyokuwa katika Vitabu vingine vilivyokuja kabla yake. Hakututaka Allaah تعالی wala Mtume Wake ﷺ kuvipekua na kuvirudia. Allah تعالی Alimpasha habari Mtume Wake ﷺ kuhusu wao walipokengeuka, wakavunja sheria na wakafanya ujeuri, Allah تعالی Aliwasaliti wao na maadui zao walioiharibu nchi yao na kuingia vyumba vyao vya ndani vya majumba yao. Walidhalilishwa na kutenzwa nguvu, jaza na adhabu ya uasi wao, wala Mola wako Mlezi si dhalimu kwa waja Wake. Hakika wao waliasi na kukaidi na kuwaua Manabii na wanazuoni wengi. Ibn Jariir رحمه الله تعالی amepokea kutoka kwa Yahyaa bin Sa'iid aliyesema: Nimemsikia Said bin Al-Musayyab akisema: "Bukhtanasswar (Nebukadneza) aliiteka Shaam (Syria Kubwa<sup>1</sup>), akaiharibu *Baytil Maqdis* na kuwaua wao (Mayahudi), kisha alikuja Damascus na kuikuta damu ikichemka juu ya chetezo. Akawauliza: 'Hii damu ni ya nini?' Wakajibu, 'Tuliwakuta mababa zetu wakifanya haya (wakiwa na tamaduni hii), kila alipodhihiri kwenye chetezo ilidhihiri damu'. Akasema: 'Kwa ajili ya damu hiyo akawaua sabiini elfu na zaidi'. Baada ya hapo damu ikatulia kuchemka."<sup>2</sup> Na hii ni sahihi kutoka kwa Said bin Al-Musayyab, na tukio hili linajulikana sana, kwani yeye Bukhtanasswar (Nebukadneza) aliwaua watukufu na wanazuoni wao, wala hakumuacha yeyote aliyekuwa ameihifadhi Taurat. Alichukua mateka wengi sana miongoni mwa watoto wa Manabii na wengineo, na alifanya mengine mengi ambayo yatarefusha utajo wake. Na lau tungepata yaliyokuwa sahihi au yaliyokaribiana nayo, tungeyaandika na kuyanukuu hapa. Na Allah تعالی Anajua zaidi. Kisha Akasema Allah تعالی :

إِنْ أَحْسَنْتُمْ أَحْسَنْتُمْ لِأَنْفُسِكُمْ وَإِنْ أَسَأْتُمْ فَلَهَا<sup>ط</sup>

***"Basi mkifanya wema, mnajifanyia wema nafsi zenu. Na mkifanya ubaya, mnajifanyia wenyewe."***

Maana: Juu yao kama Allah تعالی Alivyosema:

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا فَلِنَفْسِهِ<sup>ط</sup> وَمَنْ أَسَاءَ فَعَلَيْهَا<sup>ط</sup> ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ تُرْجَعُونَ ﴿١٥﴾

***"Mwenye kutenda wema basi ni kwa ajili ya nafsi yake (mwenyewe) na mwenye kufanya uovu ni juu yake (mwenyewe)." (45:15)***

<sup>1</sup> Hili ni eneo linalojumlisha nchi ya Syria, Jordan, Lebanon, Palestina na sehemu ya Iraq.

<sup>2</sup> Tabari 17: 369.

**Uharibifu wa Pili**

Na Kauli Yake:

فَإِذَا جَاءَ وَعْدُ الْآخِرَةِ

**“Na ikifika ahadi ya mwisho.”**

Maana yake: Tukio la pili la uharibifu wenu na maadui zenu watakapokuja tena,

لِيُسْتَفُوا وَجُوهَكُمْ

**“Ili wazidhalilishe nyuso zenu.”**

Maana yake: Kuwateza nguvu na kuwashinda. Wakati huo,

وَلِيَدْخُلُوا الْمَسْجِدَ

**“Na waingie Msikitini.”**

Kwa maana ya Msikiti wa Bayt Al-Maqdis na haya yatakuwa ni marudia:

كَمَا دَخَلُوهُ أَوَّلَ مَرَّةٍ

**“Kama walivyoingia mara ya kwanza.”**

Maana yake: Walipowaingilieni ndani ya majumba. Hapo basi,

وَلِيَتَّيَبُوا

**“Na waharibu.”**

Maana yake: Wavunje na kuharibu,

مَا عَلَوْا

**“Kwa kila walichokiteka.”**

Ikiwa na maana kila watakachokitia mkononi bila kuchagua. Uharibifu huo hautakuwa mdogo:

تَتَّبِعُوا ۝ عَسَىٰ رَبُّكُمْ أَن يَرْحَمَكُمْ

**“Uharibifu mkubwa. Huenda Mola wenu Mlezi Akakurehemuni.”**

Maana yake: Huenda hata hivyo, Akakuepusheni nao.

وَإِنْ عُدْتُمْ عُدْنَا

**“Na mkirudia na Sisi Tutarudia.”**

Maana yake: Mnaporudia tu kufanya uharibifu basi nasi,

عُدْنَا

**“Tutarudia.”**

Ibara hii ina maana kuwa Tutawaadhibu tena hapa duniani, pamoja na adhabu na mateso Tutakayowaekea Kesho Akhera. Kwa ajili hii Akasema:

وَجَعَلْنَا جَهَنَّمَ لِلْكَافِرِينَ حَصِيرًا ﴿١٧﴾

**“Na Tumeifanya Jahannamu kuwa ni gereza kwa ajili ya makafiri.”**

Maana yake: Mahali pa kufungiwa daima, jela ambayo huwezi kuiepuka wala kutoroka. Ibn 'Abbas رضي الله عنهما amesema: “*Haswiiraa*, hapa ina maana jela”<sup>1</sup>.

Na amesema Mujaahid, “Watafungiwa humo.”<sup>2</sup> Na hivyo ndivyo walivyosema wengineo. Akasema Al-Hasan kuhusu maana ya neno hilo: “Kitanda na godoro la Moto”<sup>3</sup>.

Na amesema Qataadah: “Walirudi tena wana wa Israili kukiuka mipaka na ujeuri, Allah تعالى Akawasaliti dhidi yao, kikundi hiki cha Muhammad ﷺ na Maswahaba wake, wakachukua kutoka kwao *jizyah*<sup>4</sup> (kodi) kwa hiari yao, hali wametii na kuhisi kuwa wameshindwa.”<sup>5</sup>

\* \* \*

<sup>1</sup> Tabari 17:390.

<sup>2</sup> Tabari 17:390.

<sup>3</sup> Tabari 17:390.

<sup>4</sup> Hii ni kodi inayotozwa *Ahlul - Kitab* (Mayahudi na Manasara) walio chini ya himaya na ulinzi wa Dola ya Kiislamu.

<sup>5</sup> Tabari 17:389.



إِنَّ هَذَا الْقُرْآنَ يَهْدِي لِلَّتِي هِيَ أَقْوَمُ وَيُبَشِّرُ الْمُؤْمِنِينَ الَّذِينَ يَعْمَلُونَ الصَّالِحَاتِ أَنَّ لَهُمْ أَجْرًا كَبِيرًا ﴿٩﴾ وَأَنَّ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ أَعْتَدْنَا لَهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٠﴾ وَيَدْعُ الْإِنْسَانَ بِالْشَّرِّ دُعَاءَهُ بِالْخَيْرِ ۖ وَكَانَ الْإِنْسَانُ عَجُولًا ﴿١١﴾ وَجَعَلْنَا اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ آيَاتٍ ۖ فَمَحْوًى آيَةَ اللَّيْلِ وَجَعَلْنَا آيَةَ النَّهَارِ مُبْصِرَةً لِّتَبْتَغُوا فَضْلًا مِّن رَّبِّكُمْ وَلِتَعْلَمُوا عَدَدَ السِّنِينَ وَالْحِسَابَ ۗ وَكُلُّ شَيْءٍ فَصْلَانَةٌ تَفْصِيلًا ﴿١٢﴾ وَكُلُّ إِنْسَانٍ لِّزَمَانِهِ طَيْرُهُ ۖ فِي عُنُقِهِ ۖ وَخُرُجُ لَهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ كِتَابًا يَلْقَاهُ مَنشُورًا ﴿١٣﴾ أَقْرَأَ كِتَابَكَ كَفَىٰ بِنَفْسِكَ عَلَيْكَ حَسِيبًا ﴿١٤﴾ مِّنْ أُمَّتَدَىٰ فَإِنَّمَا يَهْتَدِي لِنَفْسِهِ ۖ وَمَنْ ضَلَّ فَإِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا ۖ وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ۗ وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ نَبْعَثَ رَسُولًا ﴿١٥﴾ وَإِذَا أَرَدْنَا أَن نُّهْلِكَ قَوْمًا فَمَرَّنا بِمُتْرِفِهَا فَفَسَقُوا فِيهَا فَحَقَّ عَلَيْهَا الْقَوْلُ فَدَمَّرْنَاهَا تَدْمِيرًا ﴿١٦﴾ وَكَمْ أَهْلَكْنَا مِن الْقُرُونِ مِن بَعْدِ نُوحٍ ۗ وَكَفَىٰ بِرَبِّكَ بِذُنُوبِ عِبَادِهِ خَبِيرًا بَصِيرًا ﴿١٧﴾ مَّن كَانَ يُرِيدُ الْعَاجِلَةَ عَجَلْنَا لَهُ فِيهَا مَا نَشَاءُ لِمَن نُّرِيدُ ثُمَّ جَعَلْنَا لَهُ جَهَنَّمَ يَصْلَاهَا مَدْمُومًا مَّدْحُورًا ﴿١٨﴾ وَمَن أَرَادَ الْآخِرَةَ وَسَعَىٰ لَهَا سَعْيَهَا وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَأُولَٰئِكَ كَانَ سَعْيُهُم مَّشْكُورًا ﴿١٩﴾

إِنَّ هَذَا الْقُرْآنَ يَهْدِي لِلَّتِي هِيَ أَقْوَمُ وَيُبَشِّرُ الْمُؤْمِنِينَ الَّذِينَ يَعْمَلُونَ الصَّالِحَاتِ أَنَّ لَهُمْ أَجْرًا كَبِيرًا ﴿٩﴾ وَأَنَّ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ أَعْتَدْنَا لَهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٠﴾

**9. Hakika hii Qur'ani inaongoa kwenye ya yaliyonyooka kabisa, na inawapa habari njema Waumini ambao wanatenda mema ya kwamba wata-pata malipo makubwa.**

**10. Na ya kwamba wale wasio iamini Akhera Tume-waandalia adhabu chungu.**

### Kuisifu Qur'ani

Allah تعالى Anakisifu Kitabu Chake Kitukufu ambacho Alimteremshia Mtume Wake Muhammad ﷺ. Nayo ni Qur'ani inayowaongoza na kuwaelekeza kaumu njia bora na iliyo wazi. Kwayo,

وَيُبَشِّرُ الْمُؤْمِنِينَ

**"Inawapa habari njema Waumini."**

Miongoni mwa,

الَّذِينَ يَعْمَلُونَ الصَّالِحَاتِ

**“Ambao wanatenda mema.”**

Kulingana nayo. Kwa kuwaambia,

أَنَّ لَهُمْ أَجْرًا كَبِيرًا ﴿٩﴾

**“Watapata malipo makubwa.”**

Maana yake: Siku ya Kiyama. Anasema Aliyetukuka:

وَأَنَّ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ

**“Na ya kwamba wale wasioamini Akhera.”** Maana yake: inwabashiria wale wasioamini Akhera kwamba,

هُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٠﴾

**“Watapata adhabu chungu sana.”** Siku hiyo ya Kiyama kama Anavyosema Aliyetukuka:

فَبَشِّرْهُمْ بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿١١﴾

**“Wabashirie adhabu iumizayo.” (84:24).**

وَيَدْعُ الْإِنْسَانَ بِالشَّرِّ دُعَاءَهُ بِالْخَيْرِ وَكَانَ الْإِنْسَانُ عَجُولًا ﴿١٢﴾

**11. Na mwanadamu huomba shari kama vile aombavyo kheri, kwani mwanadamu ni mwenye pupa.**

### Haraka ya Mwanadamu na Kujiombea Mabaya Mwenyewe

Allah تعالیٰ Anatuambia kuhusu haraka ya mwanadamu ni kujiombea mabaya mwenyewe baadhi ya wakati juu ya nafsi yake, watoto wake au mali yake. Lau Mola wake Mlezi Angemjibu dua yake angeangamia kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَيَدْعُ الْإِنْسَانَ بِالشَّرِّ دُعَاءَهُ بِالْخَيْرِ

**“Na mwanadamu huomba shari kama vile aombavyo kheri.”**

Maana yake: Kuomba mauti, hilaki, maangamivu, laana na kadhalika.

﴿ وَلَوْ يُعَجِّلُ اللَّهُ لِلنَّاسِ الشَّرَّ ﴾

**“Na kama Allah Angaliwapa watu upesi upesi shari...” (10:11).**

Na hivyo ndivyo alivyofasiri Ibn ‘Abbaas, Mujaahid na Qataadah رضي الله عنهم<sup>1</sup>.  
Na tayari tumetangulia kuielezea katika Hadithi:

﴿ لَا تَدْعُوا عَلَىٰ أَنْفُسِكُمْ، وَلَا عَلَىٰ أَمْوَالِكُمْ أَنْ تُوَافِقُوا مِنْ اللَّهِ سَاعَةً إِجَابَةً  
يَسْتَجِيبُ فِيهَا ۝﴾

*“Musiombe dua dhidi ya nafsi zenu au mali zenu, isije ikaafikiwa ndani yake saa ya kujibiwa na Allaah”<sup>2</sup>.*

Linalosababisha mwanadamu kufanya hilo ni wasiwasi, hamu na haraka yake. Kwa ajili hilo Amesema Allah تعالى:

﴿ وَكَانَ الْإِنْسَانُ عَجُولًا ۝﴾

**“Kwani mwanadamu ni mwenye pupa”.**

Salmaan Al-Faarisiy na Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما wametaja kisa cha Adam عليه السلام pale alipotaka kuinuka kwa miguu yake kabla ya nafsi haijafika kwenye miguu yake. Pale roho ilipopuliziwa, iliingia mwilini mwake kutoka kichwani mwake kuelekea chini. Ilipofika ubongoni mwake, alichemua (alikwenda chafya), hapo akasema: *“Alhamdulillah - Sifa zote njema Anastahiki Allah”*.

Na Allah تعالى Akasema: *“Ewe Adam! Mola wako Mlezi Akurehemu”*. Roho ilipofika kwenye macho yake, aliyafunua, na ilipofika katika viungo vyake na mwilini mwake alianza kuvitizama na kustaaajabia. Alitaka kunyanyuka kabla haijafika miguuni mwake, lakini hakuweza. Alisema: *“Ewe Mola wangu Mlezi! Iharakishe kabla ya kufika usiku”<sup>3</sup>.*

<sup>1</sup> Tabari 17:393 – 394.

<sup>2</sup> Muslim 4:2304.

<sup>3</sup> Tabari 17:394 – 395.

وَجَعَلْنَا اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ آيَاتَيْنِ ۗ فَمَحْوَنًا آيَةَ اللَّيْلِ وَجَعَلْنَا آيَةَ النَّهَارِ مُبْصِرَةً لِّتَبْتَغُوا فَضْلًا  
مِّن رَّبِّكُمْ وَلِتَعْلَمُوا عَدَدَ السِّنِينَ وَالْحِسَابَ ۗ وَكُلُّ شَيْءٍ فَضْلَنَاهُ تَفْصِيلًا ﴿١٧﴾

**12. Na Tumefanya usiku na mchana kuwa ishara mbili. Tena Tukaifuta ishara ya usiku, na Tukaifanya ishara ya mchana ni yenye mwangaza ili mtafute Fadhila itokayo kwa Mola wenu Mlezi, na mpate kujua idadi ya miaka na hesabu. Na kila kitu Tumekifafanua waziwazi.**

### Usiku na Mchana ni Ishara za Uwezo Mkubwa wa Allah تعالى

Allah تعالى Anatumkumbusha zile ishara kubwa Alizoziumba, ikiwemo kubadilika kwa usiku na mchana, ili watu wapate kupumzika usiku na mchana kwenda kushughulika na maisha, wanafanya kazi na kusafiri mchana, na ili wapate kujua idadi ya siku, wiki, miezi na miaka. Hilo litawajulisha wao nyakati za kulipa madeni, kufanya Ibada, mahusiano na mauzo ya kibiashara, kulipa ijara ya nyumba na kadhalika. Kwa kuzingatia hilo Allah تعالى Anasema:

لِتَبْتَغُوا فَضْلًا مِّن رَّبِّكُمْ

**“Ili mpate Fadhila itokayo kwa Mola wenu Mlezi.”** Maana: Katika maisha na safari zenu, na kadhalika.

وَلِتَعْلَمُوا عَدَدَ السِّنِينَ وَالْحِسَابَ ۗ

**“Na mpate kujua idadi ya miaka na hesabu”.**

Lau kama wakati ungesimama wima na kutobadilika, hatungejua chochote katika haya. Kama Alivyosema Allah تعالى:

قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِن جَعَلَ اللَّهُ عَلَيْكُمُ اللَّيْلَ سَرْمَدًا إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ مَنْ إِلَهُ غَيْرُ اللَّهِ  
يَأْتِيكُمْ بِضِيَاءٍ ۗ أَفَلَا تَسْمَعُونَ ﴿١٨﴾ قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِن جَعَلَ اللَّهُ عَلَيْكُمُ النَّهَارَ  
سَرْمَدًا إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ مَنْ إِلَهُ غَيْرُ اللَّهِ يَأْتِيكُمْ بِاللَّيْلِ تَسْكُونُونَ فِيهِ ۗ أَفَلَا  
تُبْصِرُونَ ﴿١٩﴾ وَمِن رَّحْمَتِي جَعَلَ لَكُمُ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ لِتَسْكُنُوا فِيهِ وَلِتَبْتَغُوا مِن  
فَضْلِهِ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٢٠﴾

**“Sema: ‘Niambieni, kama Allah Akiufanya usiku ukukalieni moja kwa moja mpaka siku ya Kiyama, ni mungu gani asiyekuwa Allah Atakayekuleteeni mwanga? Basi je, hamsikii?’ Sema: ‘Niambieni, kama Allah Akiufanya mchana kukukalieni moja kwa moja mpaka siku ya Kiyama, ni mungu gani asiyekuwa Allah Atakayekuleteeni usiku, mnaopumua humo? Basi je, hamuoni (ihsani za Allah)?’ Na kwa Rehema Zake Amekufanyieni usiku na mchana ili mpumue hapo usiku na mtafute Fadhila Zake (hapo mchana) na ili mpate kushukuru.” (28:71-73).** Aidha Allah تعالى Amesema,

تَبَارَكَ الَّذِي جَعَلَ فِي السَّمَاءِ بُرُوجًا وَجَعَلَ فِيهَا سِرَاجًا وَقَمَرًا مُنِيرًا ﴿٧١﴾ وَهُوَ الَّذِي جَعَلَ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ خِلْفَةً لِمَنْ أَرَادَ أَنْ يَذَّكَّرَ أَوْ أَرَادَ شُكُورًا ﴿٧٢﴾

**“Ni Mwenye kuleta baraka (kweli kweli) Yule Aliyezijaalia nyota mbinguni, na Akajaalia humo jua na mwezi unaong’ara. Naye Ndiye Aliyefanya usiku na mchana ufuatane; kwa anayetaka kukumbuka au anayetaka kushukuru.” (25:61-62)**

Na Allah تعالى Amesema,

يُكَوِّرُ اللَّيْلَ عَلَى النَّهَارِ وَيُكَوِّرُ النَّهَارَ عَلَى اللَّيْلِ وَسَخَّرَ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ كُلٌّ يَجْرِي لِأَجَلٍ مُّسَيَّءٍ أَلَا هُوَ الْعَزِيزُ الْغَفُورُ ﴿٥﴾

**“Hufunika usiku juu ya mchana, na hufunika mchana juu ya usiku. Na Ametiisha jua na mwezi; vyote vinakwenda tu (bila kusita) mpaka muda wake uliowekwa, jueni kwamba Yeye (Allaah) ni Mwenye Nguvu, Mwingi wa Kusamehe.” (39:5).**

Allah تعالى Amesema,

فَالِقُ الْإِصْبَاحِ وَجَعَلَ اللَّيْلَ سَكَنًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ حُسْبَانًا ذَٰلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ ﴿٩٦﴾

**“Ndiye Anayepambazua mwangaza asubuhi; na Ameufanya usiku kuwa mapumziko, na jua na mwezi kwenda kwa hesabu. Hicho ndicho kipimo cha Mwenye Nguvu na Ajuaye.” (6:96)**

Allah تعالى Amesema tena,

وَأَيُّهُ لَّهُمْ أَلْيَلٌ نَسَلَخُ مِنْهُ النَّهَارَ فَإِذَا هُمْ مُظْلِمُونَ ﴿١٧﴾ وَالشَّمْسُ تَجْرِي لِمُسْتَقَرٍّ لَهَا  
ذَلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ الْعَلِيمِ ﴿١٨﴾

**“Na usiku ni alama kwao; Tunauvua humo mchana; mara wao wanakuwa kizani. Na jua (pia ni alama kwao); linakwenda maisha mpaka kituoni pake. Hayo ni matengenezo ya Allaah Mwenye Nguvu na Mwenye Kujua.” (36:37-38)**

Kisha Allah تعالى Ameufanya usiku kuwa ni ishara, alama inayojulikana kwayo, nayo kuingia giza na kujitokeza kwa mwezi ndani yake. Pia mchana una alama, nayo ni muangaza na kutoka kwa jua linalong’aa. Sifa hizo zinatofautisha baina nuru ya mwezi na muangaza wa jua, ili ijulikane hili kwa hili. Kama Allah تعالى Alivyosema:

هُوَ الَّذِي جَعَلَ الشَّمْسَ ضِيَاءً وَالْقَمَرَ نُورًا وَقَدَرَهُ مَنَازِلَ لِتَعْلَمُوا عَدَدَ السِّنِينَ  
وَالْحِسَابَ ۗ مَا خَلَقَ اللَّهُ ذَلِكَ إِلَّا بِالْحَقِّ ۗ يُفَصِّلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿١٩﴾ إِنَّ فِي  
أَخْتِلَافِ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ وَمَا خَلَقَ اللَّهُ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يَتَّقُونَ ﴿٢٠﴾

**“Yeye (Allah) Ndiye Aliyelifanya jua kuwa mwanga, na mwezi kuwa nuru, na Akaupimia vituo (huo mwezi) ili mjue idadi ya miaka na hesabu (nyinginezo). Allah Hakuviumba hivyo ila kwa haki. Anapambanua aya Zake kwa watu wanaotaka kujua. Hakika katika mfuatano wa usiku na mchana; na katika Alivyoviumba Allaah katika mbingu na ardhi; ziko dalili kwa watu wanaoogopa...” (10:5-6)** Aidha Allah تعالى Amesema,

﴿ يَسْأَلُونَكَ عَنِ الْأَهْلِ قُلْ هِيَ مَوَاقِيتُ لِلنَّاسِ وَالْحَجَّ

**“Wanakuuliza juu ya miezi. Sema: ‘Hiyo ni vipimo vya nyakati kwa ajili ya mambo ya watu mengine na ya Hija zao.’ (2:189).**

Amepokea Ibn Jurayj kutoka kwa ‘ Abdallah bin Kathir Amefasiri aya ifuatayo: “Tena Tukaifuta ishara ya usiku, na Tukaifanya ishara ya mchana ni yenye muangaza’. Amesema: ‘Kiza cha usiku na muangaza wa mchana.”<sup>1</sup>

<sup>1</sup> Tabari 17:396.

Ibn Jurayj amepokea kutoka kwa Mujaahid aliyesema: "Jua ni ishara ya mchana na mwezi ni ishara ya usiku."

فَمَحَوْنَا آيَةَ اللَّيْلِ

**"Tena Tukaifuta ishara ya usiku".**

Akasema: 'Weusi uliopo katika mwezi, na hivyo ndivyo Alivyouumba Allah Aliyetukuka"<sup>1</sup>. Na ameipokea Ibn Abi Najih kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kwamba Aya ifuatayo,

وَجَعَلْنَا اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ آيَتَيْنِ

**"Na Tumefanya usiku na mchana kuwa ishara mbili".**

Akasema: 'Usiku na mchana, pia hivi ndivyo Alivyoviumba Allah تعالى"<sup>2</sup>.

وَكُلَّ إِنْسَانٍ أَلْزَمْنَاهُ طَبْعَهُ فِي عُنُقِهِ ۗ وَنُخْرِجُ لَهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ كِتَابًا يَلْقَاهُ مَنشُورًا ﴿١٧﴾

أَقْرَأُ كِتَابِكَ كَفَىٰ بِنَفْسِكَ الْيَوْمَ عَلَيْكَ حَسِيبًا ﴿١٨﴾

**13. Na kila mtu Tumemfungia amali yake shingoni mwake. Na Siku ya Kiyama Tutamtotea kitabu atakachokikuta kiwazi kimekunjuliwa.**

**14. Ataambiwa: Soma kitabu chako! Nafsi yako inakutosha leo kukuhisabu.**

### Kila Mtu Atakuwa na Kitabu cha Amali Yake

Baada kutaja wakati na yanayotokea ndani yake katika amali za mwanadamu. Anasema Aliyetukuka:

وَكُلَّ إِنْسَانٍ أَلْزَمْنَاهُ طَبْعَهُ فِي عُنُقِهِ ۗ

**"Na kila mtu Tumemfungia amali yake shingoni mwake".**

Na maana ya *Twa'irahu* (kilugha ni kinachoruka) inahusisha matendo ya mwanadamu yanayoruka kutoka kwake kama walivyosema Ibn 'Abbaas, Mujaahid na wengineo رضي الله عنهم. Hii inajumlisha amali njema zote na mbaya, atalazimishwa kuzikubali na hivyo kulipwa kulingana na amali hizo<sup>3</sup>.

<sup>1</sup> Tabari 17: 396.

<sup>2</sup> Tabari 17: 397.

<sup>3</sup> Tabari 17: 398, 400.

Allah تعالى Amesema:

﴿٨﴾ وَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ﴿٩﴾

**“Basi anayefanya wema hata wa kiasi cha uzito wa atomu (kitu kidogo chenye wizani mdogo) ataona jaza yake. Na anayefanya uovu hata wa kiasi cha uzito wa atomu ataona jaza yake.” (99:7-8)**

Na Allah تعالى Amesema:

﴿١٧﴾ إِذْ يَتَلَقَى الْمُتَلَقِيَانِ عَنِ الْيَمِينِ وَعَنِ الشِّمَالِ قَعِيدٌ ﴿١٨﴾ مَا يَلْفِظُ مِنْ قَوْلٍ إِلَّا لَدَيْهِ رَقِيبٌ عَتِيدٌ ﴿١٩﴾

**“Wanapopokea wapokeaji wawili, anayekaa kuliani na anayekaa kushotoni (Malaika). Hatoi kauli yoyote isipokuwa karibu naye yuko mngojeaji tayari kuandika.” (50:17-18) Aidha Amesema,**

﴿١٢﴾ وَإِنَّ عَلَيْكُمْ لَحَافِظِينَ ﴿١٣﴾ كِرَامًا كَاتِبِينَ ﴿١٤﴾ يَعْمَلُونَ مَا تَفْعَلُونَ ﴿١٥﴾

**“Na hakika juu yenu kuna wenye kuwatunza. Watukufu wenye kuandika. Wanayajua yote mnayoyatenda.” (82:10-12). Amesema tena,**

﴿١٦﴾ إِنَّمَا تُحْزَنُونَ مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٧﴾

**“Mnalipwa mliyokuwa mkiyatenda.” (52:16).**

Na Amesema,

﴿١٢٣﴾ مَنْ يَعْمَلْ سُوءًا يُجْزَ بِهِ

**“Atakayefanya ubaya atalipwa kwa ubaya huo.” (4:123)**

Makusudio ya Aya zote hizi ni kuwa amali za mwanadamu zinahifadhiwa kwa ajili yake, chache au nyingi, na anaandikiwa usiku na mchana, asubuhi na jioni. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

﴿١٠٤﴾ وَنُخْرِجُ لَهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ كِتَابًا يَلْقَاهُ مَنْشُورًا ﴿١٠٥﴾

**“Na Siku ya Kiyama Tutamtotea kitabu atakachokikuta kiwazi kimekunjuliwa.”**

Maana: Tutamjumlishia amali zake zote katika kitabu atakachopewa Siku ya



Kiyama, kwa mkono wake wa kulia akiwa ni mwema, na wa kushoto akiwa ni muovu. “*Manshuuraa*” ina maana ya kukunjuliwa, yaani kipo wazi hivyo kusomwa na yeye mwenyewe na wengineo. Ndani yake zipo amali zake zote kuanzia mwanzo wa umri wake mpaka mwisho wake. Amesema Aliyetukuka:

يُنذِرُوا الْإِنْسَانَ يَوْمَئِذٍ بِمَا قَدَّمَ وَأَخَّرَ ﴿١٣﴾ بَلِ الْإِنْسَانُ عَلَىٰ نَفْسِهِ بَصِيرَةٌ ﴿١٤﴾ وَلَوْ أَلْقَىٰ مَعَاذِيرَهُ ﴿١٥﴾

**“Siku hiyo ataambiwa mwanadamu aliyoyatanguliza na aliyoyaakhirisha. Bali mtu ni shahidi juu ya nafsi yake. Ingawa anatoa nyudhuru zake za uongo.” (75:13-15)**

Kwa ajili hiyo Akasema Aliyetukuka:

اقْرَأْ كِتَابَكَ كَفَىٰ بِنَفْسِكَ الْيَوْمَ عَلَيْكَ حَسِيبًا ﴿١٧﴾

**“*(Ataambiwa): Soma kitabu chako! Nafsi yako inakutosha leo kukuhisabu.*” (17:14)**

Maana: Hakika wewe unajua kwamba hujadhulumiwa na hakuna kilichoandikwa dhidi yako isipokuwa ulichokifanya. Kwani unakumbuka kila kitu ulichofanya, na hakuna atakayesahau chochote alichofanya. Kila mmoja ataweza kusoma kitabu chake, ikiwa ni msomi au *ummiy* (asiyejua kusoma wala kuandika). Allah تعالى Anatuambia:

الزَّيْمَةَ طَبَّرَهُ فِي عُنُقِهِ ۗ

**“Na kila mtu Tumemfungia amali yake shingoni mwake.”** Shingo imetajwa hapa kwa sababu ndiyo sehemu ya mwili ambayo haina mfano wake, na mmoja akizuiliwa nayo, hana pa kukimbilia. Ma'mar amempokea Qataadah akisema: “Na kila mtu Tumemfungia amali yake shingoni mwake.” Maana: Matendo yake.

وَنُخْرِجُ لَهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

**“Na Siku ya Kiyama Tutamtolea.”** Akasema: Tutaitoa amali hiyo kutoka kwa,

كِتَابًا يَلْقَاهُ مَنشُورًا ﴿١٨﴾

**“Kitabu atakacho kikuta kiwazi kimekunjuliwa.”** Amesema Ma'mar, amesoma al-Hasan Al-Baswriy:

عَنِ الْيَمِينِ وَعَنِ الشِّمَالِ قَعِيدٌ ﴿١٧﴾

***“Anayekaa kuliani na anayekaa kushotoni (Malaika).” (50:17)***

Akaielezea: “Ewe mwanadamu! Kitabu chako kimefunuliwa kwa ajili yako, na Malaika wawili watukufu wamepatiwa jukumu la kukufuata. Mmoja wao yuko kuliani na mwingine kushotoni mwako. Wa kuliani mwako anaandika mazuri yako ilhali wa kushotoni kwako anaandika maovu unayoyatenda. Hivyo, fanya utakayo, machache au mengi, mpaka utakapokufa, kisha nitakikunja kitabu chako na kukifunga shingoni kaburini mwako. Kisha utakapokuja Siku ya Kiyama, utakikuta kitabu kimekunjuliwa kikiwa wazi kabisa, hivyo soma kitabu chako. Naapa kwa Allah تعالى, Yule Anayewaita kwa hesabu ya amali zenu ni Muadilifu kabisa.<sup>1</sup> Haya ni baadhi ya maneno yaliyo mazuri sana ya Al-Hasan aliyoyazungumza, Allah تعالى Amrehemu.

مَنْ أَهْتَدَىٰ فَإِنَّمَا يَهْتَدِي لِنَفْسِهِ ۗ وَمَنْ ضَلَّٰ فَإِنَّمَا يَضِلُّ عَلَيْهَا ۗ وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ۗ وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ نَبْعَثَ رَسُولًا ﴿١٧﴾

***15. Anayeongoka basi anaongoka kwa ajili ya nafsi yake. Na anayepotea basi anapotea kwa khasara yake mwenyewe. Wala habebi mbebaji mzigo wa mwengine. Wala Sisi hatuadhibu mpaka Tumpeleke Mtume.***

### **Hakuna Atakayebeba Mzigo wa Mwengine**

Allah تعالى Anatueleza kuwa yeyote aliyeongoka na kufuata ukweli, akifuata nyayo za Mtume muhammad ﷺ, atapata malipo mema kwa ajili ya nafsi yake. Ama kwa yule,

وَمَنْ ضَلَّٰ

***“Anayepotea.”*** Maana yake: Kutoka katika ukweli, akakengeuka kutokana na njia au uongofu, anaidhulumu nafsi yake, kwa hiyo hayo maovu yatamrudia nafsi yake. Kisha Anasema Aliyetukuka:

وَلَا تَزِرُ وَازِرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ۗ

***“Wala habebi mbebaji mzigo wa mwengine.”***

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 17:400.

Maana yake: Hatabeba mtu madhambi ya mwengine, na hamfanyii ubaya mwengine ila nafsi yake mwenyewe. Kwani Allah تعالى Anasema:

وَإِنْ تَدْعُ مُثْقَلَةٌ إِلَىٰ جَمَلِهَا لَا تُحْمَلْ مِنْهُ شَيْءٌ

**“Na kama aliyetopewa na mzigo wake akimuita mwengine kwa ajili ya mzigo wake hautachukuliwa hata kidogo na mtu huyo.” (35:18)**

Wala hapana ukinzani baina Aya hii na Kauli Yake:

وَلِيَحْمِلُوا أُنْفُسَهُمْ وَأَثْقَالَ مَعَهُمْ

**“Na watabeba mizigo yao, na mizigo mingine pamoja na mizigo yao.” (29:13)** Na Kauli Yake Allah تعالى,

وَمِنَ أَوْزَارِ الَّذِينَ يُضِلُّونَهُمْ بِغَيْرِ عِلْمٍ

**“Na pia sehemu ya mizigo ya wale wanaopoteza bila ya kuwa na ilimu.” (16:25)**

Kwa wale wenye kuwaita wengine kufanya madhambi watabeba madhambi ya makosa yao wenyewe na vile vile madhambi ya wale waliowapoteza, bila kupunguza hata kidogo sehemu kutoka kwa mizigo ya watu hao, na hakuna mzigo wowote kati ya hiyo itakayoondolewa kutoka kwao. Huu ndio Uadilifu na Rehema ya Allah تعالى kwa waja Wake. Kama Anavyosema:

وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ نَبْعَثَ رَسُولًا

**“Wala Sisi Hatuadhibu mpaka Tumpeleke Mtume.”**

**Hakuna Adhabu ila baada ya Kumtuma Mtume**

Allah تعالى Anatupasha habari kutokana na Uadilifu Wake kuwa Hamuadhibu mtu yeyote yule mpaka kumsimamishia dalili na hoja juu yake kwa Kumtuma Mtume kwao. Hii ni kama Kauli ya Aliyetukuka:

كُلَّمَا أُلْقِيَ فِيهَا فَوْجٌ سَأَلْتَهُمْ خَزَنَتُهَا أَلَمْ يَأْتِكُمْ نَذِيرٌ ﴿١٧﴾ قَالُوا بَلَىٰ قَدْ جَاءَنَا نَذِيرٌ فَكَذَّبْنَا

وَقُلْنَا مَا نَزَّلَ اللَّهُ مِن شَيْءٍ إِنْ أَنْتُمْ إِلَّا فِي ضَلَالٍ كَبِيرٍ ﴿١٨﴾

***“Kila mara litakapotupwa humo kundi la wabaya walinzi wake watauliza: ‘Je! Hakukufikieni mwonyaji?’ Watasema: ‘Kwa nini? Alitujia muonyaji lakini tulikadhibisha na tulisema: ‘Allah Hakuteremsha chochote, nyinyi hamumo ila katika upotofu mkubwa.” (67:8-9)***

Na pia Kauli Yake Allah تعالى:

وَسِيقَ الَّذِينَ كَفَرُوا إِلَىٰ جَهَنَّمَ زُرَّامًا ۗ حَتَّىٰ إِذَا جَاءُوهَا فَتَحَتْ أَبْوَابُهَا وَقَالَ لَهُمْ خَزَنَتُهَا أَلَمْ يَأْتِكُمْ رُسُلٌ مِّنكُمْ يَتْلُونَ عَلَيْكُمْ آيَاتِ رَبِّكُمْ وَيُنذِرُونَكُمْ لِقَاءَ يَوْمِكُمْ هَٰذَا قَالُوا بَلَىٰ وَلَٰكِن حَقَّتْ كَلِمَةُ الْعَذَابِ عَلَىٰ الْكَافِرِينَ ﴿١٧﴾

***“Na waliokufuru watapelekwa katika Jahanamu makundi-makundi mpaka watakapoifikia itafunguliwa milango yake na walinzi wake watawaambia: ‘Je, hawakukujieni Mitume miongoni mwenu wakikusomeeni aya za Mola wenu Mlezi na kukuonyeni makutano ya siku yenu hii?’ Watasema: ‘Kwa nini? Wametujia! Lakini limethibiti neno la adhabu juu ya wale waliowakanusha (nao ndio sisi).” (39:71)***

Na Amesema Aliyetukuka:

وَهُمْ يَصْطَرِحُونَ فِيهَا رَبَّنَا أَخْرِجْنَا نَعْمَلْ صَالِحًا غَيْرَ الَّذِي كُنَّا نَعْمَلُ ۗ أَوَلَمْ نُعَمِّرْكُم مَّا يَتَذَكَّرُ فِيهِ مَن تَذَكَّرَ وَجَاءَكُمُ النَّذِيرُ ۗ فَذُوقُوا فَمَا لِلظَّالِمِينَ مِن نَّصِيرٍ ﴿١٧﴾

***“Na humo watapiga makelele: ‘Mola wetu Mlezi! Tutoe Motoni uturejeze duniani, tutafanya vitendo vizuri visivyokuwa vile tulivyokuwa tukifanya’ Allah Awaambie: ‘Hatukukupeni umri wa kuweza kukumbuka mwenye kukumbuka? Na akakujieni muonyaji. Basi onjeni adhabu madhalimu hawana wa kuwanusuru.” (35: 37)***

Zipa Aya nyingine nyingi ambazo ni dalili kuwa Allah تعالى Hatamuingiza yeyote Motoni isipokuwa baada ya kumtuma Mtume kwao.

## Mas-ala ya Watoto Wadogo Wanaokufa

Hapa yapo masuala ambayo wanazuoni waliotangulia na wa sasa wametofautiana, Allah تعالى Awarehemu wote. Masuala yenyewe ni kuhusu watoto waliokufa wakiwa wachanga, ilhali wazazi wao ni makafiri: Je, ni ipi hukumu yao? Na hivyo hivyo, wendawazimu, viziwi, vikongwe na wanaokufa katika Fitrah, wakiwa hawajafikiwa na ujumbe, hukumu yao itakuwa ipi? Hadithi nyingi zimepokewa katika masuala haya, ambazo nitazitaja hapa kwa usaidizi na tawfiki ya Allah تعالى.

## Hadithi ya Kwanza kutoka kwa al-As'wad bin Sari' رضي الله عنه

Imaam Ahmad amepokea kutoka kwa Al-Aswad bin Sari' رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«أَرْبَعَةٌ يَخْتَجُونَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ: رَجُلٌ أَصَمٌ لَا يَسْمَعُ شَيْئًا، وَرَجُلٌ أَحْمَقٌ، وَرَجُلٌ حَرِيمٌ، وَرَجُلٌ مَاتَ فِي فِتْرَةٍ، فَأَمَّا الْأَصَمُ فَيَقُولُ: رَبِّ قَدْ جَاءَ الْإِسْلَامُ وَمَا أَسْمَعُ شَيْئًا، وَأَمَّا الْأَحْمَقُ فَيَقُولُ: رَبِّ قَدْ جَاءَ الْإِسْلَامُ وَالصَّيِّبَانُ يَخْدِفُونِي بِالْبَغْرِ، وَأَمَّا الْهَرِيمُ فَيَقُولُ: رَبِّ لَقَدْ جَاءَ الْإِسْلَامُ وَمَا أَغْقَلُ شَيْئًا، وَأَمَّا الَّذِي مَاتَ فِي الْفِتْرَةِ فَيَقُولُ: رَبِّ مَا أَتَانِي لَكَ رَسُولٌ. فَيَأْخُذُ مَوَانِقَهُمْ لِيُطِيعَهُ، فَيُرْسِلُ إِلَيْهِمْ أَنْ ادْخُلُوا النَّارَ، فَوَالَّذِي نَفْسُ مُحَمَّدٍ بِيَدِهِ، لَوْ دَخَلُوهَا لَكَانَتْ عَلَيْهِمْ بَرْدًا وَسَلَامًا»

*“Wapo watu aina nne wataleta kesi zao Siku ya Kiyama: Mtu kiziwi asiyesikia chochote, mwendawazimu, mzee dhaifu na aliyekufa katika Fitrah. Ama kiziwi, atasema: ‘Mola wangu Mlezi! Uislamu ulikuja na sikusikia chochote’. Ama mwendawazimu, atasema: ‘Mola wangu Mlezi! Uislamu ulikuja wakati watoto wananirushia kinyesi cha ngamia’. Ama mzee dhaifu, atasema: ‘Mola wangu Mlezi! Uislamu ulikuja nami sikufahamu chochote’. Na ama aliyekufa katika Fitrah, atasema: ‘Mola wangu Mlezi! Hakuja Mtume Wako kwangu’. Allah Atakubali ahadi za kumtii, Atawatumia ujumbe waingie motoni. Naapa kwa Aliyemiliki nafsi ya Muhammad, lau watauingia, utakuwa kwao baridi na salama”.*

Ipo Hadithi kama hii yenye Isnadi kutoka kwa Qataadah aliyepokea kutoka kwa Al-Hasan, naye kutoka kwa Abu Rafi' kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, lakini mwisho wake amesema:

«فَمَنْ دَخَلَهَا كَانَ عَلَيْهِ بَرْدًا وَسَلَامًا، وَمَنْ لَمْ يَدْخُلْهَا يُشْحَبُ إِلَيْهَا»

*“Yeyote atakayeingia ataukuta ukiwa baridi na salama, na yeyote asiyeuingia humo ataburuzwa kwayo.”<sup>1</sup>*

Hii pia ilinukuliwa na Ishaah bin Raahwayh kutoka kwa Mu'aadh bin Hishaam<sup>2</sup>, na Al-Bayhaqiy katika kitabu *Al-I'tiqaad*, akasema: “Isnadi yake ni sahihi”. Imenukuliwa na Ibn Jariir رحمه الله تعالى katika Hadithi ya Ma'mar kutoka kwa Hamaam kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, kwa ajili ya Hadithi “*Mauquuf*” yaani kauli ya Sahaba. Kisha Abu Hurayrah رضي الله عنه akasema: “Soma ukitaka:

وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّى تَبْعَثَ رَسُولًا ﴿١٧﴾

***‘Wala Sisi Hatuadhibu mpaka Tumpeleke Mtume’<sup>3</sup>***

Hii pia ilipokewa na Ma'mar kutoka kwa 'Abdallah bin Twaawus kutoka kwa babake, kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, lakini ni *Mawquuf* (haikunasibishwa moja kwa moja kwa Mtume ﷺ).<sup>4</sup>

**Hadithi ya Pili kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه**

Imepokewa na Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«كُلُّ مَوْلُودٍ يُوَلَّدُ عَلَى الْفِطْرَةِ، فَأَبَوَاهُ يُهَوِّدَانِهِ أَوْ يُنَصِّرَانِهِ أَوْ يُمَجْسَانِهِ، كَمَا تَنبُتُ  
الْبَيْهَمَةُ بِهَيْمَةِ جُمَعَاءَ، هَلْ تُجَسِّنُونَ فِيهَا مِنْ جَدْعَاءَ؟»

*“Kila kinachozaliwa kinazaliwa katika Fitrah (maumbile ya mwanadamu), ni wazazi wake ndio wanaomfanya awe Myahudi, Mkristo au Majusi. Kama hayawani wanavyozaa hayawani – je waona yeyote anayezaliwa akiwa ameatilika (akiwa hana kiungo kimoja au kingine)?”*

Katika riwaya moja, walisema: “Ewe Mtume wa Allah! Waonaje kuhusu wale wanaofariki wakiwa wachanga?” Akasema:

«اللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا كَانُوا عَامِلِينَ»

*“Allah Anajua zaidi kwa kile ambacho wangekifanya.”<sup>5</sup>*

<sup>1</sup> Ahmad 4:24.

<sup>2</sup> Tabarani 1:287.

<sup>3</sup> Tabari 17:403.

<sup>4</sup> Al-Qurtwubiy 10:232.

<sup>5</sup> Al-Bukhaariy 1385 na Muslim 2658.

Imaam Ahmad amepokea kutoka kwa Abu Hurayrah عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ kama ninavyojua – mpokezi hana hakika ikiwa ilinasibishwa kwa Musa – amesema:

«ذَرَارِيُّ الْمُسْلِمِينَ فِي الْجَنَّةِ يَكْفُلُهُمْ إِبْرَاهِيمُ عَلَيْهِ السَّلَامُ»

*“Watoto wa Waislamu wapo Peponi, wakiwa wanatizamwa na kulelewa na Ibraahim.”<sup>1</sup>*

Katika Sahihi Muslim imenukuliwa kutoka kwa ‘Iyaaadhw kutoka kwa Himari, kutoka kwa Mtume ﷺ, kutoka kwa Allah تعالى kuwa Amesema:

«إِنِّي خَلَقْتُ عِبَادِي حُتَمَاءَ»

*“Hakika Nimewaumba waja Wangu wakiwa Hunafaa”<sup>2</sup><sup>3</sup>. Kulingana na riwaya nyingine, neno lililotumika ni: “Muslimiina – Waislamu”.*

**Hadithi ya Tatu kutoka kwa Samurah** رضي الله عنه

Katika kitabu chake *Al-Mustakhraj Alal Bukhaariy*, Al-Haafidh Abubakar Al-Barqaaniy رحمه الله تعالى amenukuu Hadithi ya ‘Awf Al-A’rabiyy kutoka kwa Abu Rajaa’ Al-Utwaardi kutoka wa Samurah عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ amesema:

«كُلُّ مَوْلُودٍ يُوَلَّدُ عَلَى الْفِطْرَةِ»

*“Kila kinachozaliwa kinazaliwa katika Fitrah”.*

Watu walimuuliza: “Ewe Mtume wa Allah! Vipi Watoto wa washirikina (watakuaje)?” akasema:

«وَأَوْلَادُ الْمُشْرِكِينَ»

*“Na watoto wa washirikina pia”<sup>4</sup>.*

Amepokea Atw-Twabaraniyy kutoka kwa Samurah عنه رضي الله amesema: Tulimuuliza Mtume ﷺ kuhusu watoto wa washirikina, naye akasema,

«هُمْ خَدَمُ أَهْلِ الْجَنَّةِ»

*“Wao watakuwa watumishi wa watu wa Peponi”<sup>5</sup>.*

<sup>1</sup> Ahmad 2:326 na Al-Majma’ 7:219.

<sup>2</sup> Kuegemea katika kumpwekesha Allah تعالى.

<sup>3</sup> Muslim 2865. <sup>4</sup> Al-Bukhariy 7047. <sup>5</sup> Al-Mu’jam Al-Kabiir 7:244 na Al-Majma’ 7:219.

### Hadithi ya Nne kutoka kwa Ami wa Hasnaa'

Amepokea Ahmad kutoka kwa Hasnaa' bint Mu'awiyah, wa Bani Swuraym aliyesema: Amenihadithia ami yangu kuwa alisema: "Ewe Mtume wa Allah! Kina nani wapo Peponi?" Akasema:

«النَّبِيُّ فِي الْجَنَّةِ، وَالشَّهِيدُ فِي الْجَنَّةِ، وَالْمَوْلُودُ فِي الْجَنَّةِ، وَالزَّوْجِدُ فِي الْجَنَّةِ»

*"Manabii tayari wapo Peponi, mashahidi wapo Peponi, watoto wachanga wapo Peponi na wasichana wadogo waliozikwa hai wapo Peponi."*<sup>1</sup>

### Ukaraha wa Kuzungumzia Masuala Haya

Yalipokuwa mazungumzo kuhusu masuala haya yanahitaji dalili zilizo sahihi, nzuri na huenda wakazungumza wasiokuwa na elimu ya kisheria. Kwa ajili hiyo kikundi cha wanazuoni hawakupendelea kuzungumza kuhusu jambo hilo. Rai hiyo imepokewa kutoka kwa Ibn 'Abbaas, Al-Qaasim bin Muhammad bin Abubakar Asw-Swiddiq, Muhammad bin Al-Hanafiyyah na wengineo رضي الله عنهم<sup>2</sup>.

Imepokewa na Ibn Hibbaan رحمه الله تعالى katika Sahihi yake kutoka kwa Jariir bin Haazim: Nimemsikia Abu Rajaa' Al-Utwaaridi akisema kuwa amemsikia Ibn Abbaas رضي الله عنهما akisema: "Alipokuwa juu ya Mimbar, Mtume ﷺ amesema:

«لَا يَزَالُ أَمْرُ هَذِهِ الْأُمَّةِ مُرَاتِنًا - أَوْ مُقَارِبًا - مَا لَمْ يَتَكَلَّمُوا فِي الْوِلْدَانِ وَالْقَدَرِ»

*'Jambo la Ummah litaendelea kuwa zuri – au karibu na hilo – maadamu hawatazungumza kuhusu watoto na kudura (Qadar)'.*

Akasema Ibn Hibbaan رحمه الله تعالى: "Hii inamaanisha watoto wa washirikina"<sup>3</sup>. Hivyo ndivyo alivyopokea Abubakar Al-Bazaar رحمه الله تعالى kwa njia ya Jariir bin Haazim, kisha akasema: "Wamepokea kikundi kutoka kwa Abu Rajaa' kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما ikiwa ni *Mawquur*"<sup>4</sup>.

<sup>1</sup> Ahmad 5:58 na Fat'hul Al-Bari 3246.

<sup>2</sup> Ahmad 5:73.

<sup>3</sup> Ibn Hibbaan 8:256.

<sup>4</sup> Kashf Al-Astaar 3:35.



وَإِذَا أَرَدْنَا أَنْ نُهْلِكَ قَرْيَةً أَمَرْنَا مُتْرَفِيهَا فَفَسَقُوا فِيهَا فَحَقَّ عَلَيْنَا الْقَوْلُ فَندمَرْنَهَا تَدْمِيرًا ﴿١٦﴾

**16. Na pindi Tunapotaka Kuuangamiza mji Huwaamuru wale wenye starehe na taanusi. (Kumtii Allah pamoja na kusadikisha Mitume yake) lakini wao huendelea kutenda maovu humo. Basi hapo kauli huthibiti juu ya mji huo, Nasi Tukauangamiza kwa maangamizo makubwa.**

### Maana ya “Amarnaa”

Wafasiri wa Qur’ani wametofautiana kuhusu maana yake. Pakasemwa kuwa maana ya neno “Amarnaa”, Huwaamuru wale wanaoishi katika anasa na starehe. Hivyo, wanaendelea kutenda maovu na kuvuka mipaka. Maana yake ni kuwa amri hii ni ya Kadari ya Allah تعالى. Kama Alivyosema Allah تعالى sehemu nyengine:

أَتْنَهَا أَمْرًا لَيْلًا أَوْ نَهَارًا

**“Ikawajia Amri Yetu usiku au mchana.” (10:24)**

Haiwezi kuwa Amri Yetu kwani Allah تعالى Haamrishi mambo mabaya. Wapo wengine waliosema: Maana ni kuwa Allah تعالى Amewatiisha katika kufanya mabaya, hivyo wakastahiki kupata adhabu. Wapo pia waliosema: Maana yake ni ‘Tuliwaamuru kutii lakini wakafanya mabaya’, kwa hiyo wakastahiki kupata adhabu. Hii imepokewa na Ibn Jurayj kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما<sup>1</sup>, na hiyo ndiyo rai ya Sa’iid bin Jubayr<sup>2</sup>. Amesema ‘Aliy bin Twalhah kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuhusu kauli Yake Aliyetukuka:

أَمْرًا مُتْرَفِيهَا فَفَسَقُوا فِيهَا

**“Huwaamuru (kumtii Allah pamoja na kusadikisha Mitume yake) wale wenye starehe na taanusi, lakini wao huendelea kutenda maovu humo.”**

Kuwa ina maana ya Tuliwapatia nguvu na usultani watu wabaya ambao waliasi humo (ndani yake). Pindi walipofanya hivyo, Allah تعالى Aliwaangamiza kwa Kuwaadhibu”. Hii ni sawa na Aya inayosema:

وَكَذَلِكَ جَعَلْنَا فِي كُلِّ قَرْيَةٍ أَكْبَرًا مُجْرِمِيهَا

**“Na kadhalika Tulijaalia kila mji wakuu wao ndio waovu.” (6:123)<sup>3</sup>**

<sup>1</sup> Tabari 17:403.

<sup>2</sup> Tabari 17:403.

<sup>3</sup> Tabari 17:404.

Hii pia ndiyo iliyokuwa rai ya Abu Al-'Aliyah, Mujaahid na Ar-Rabi' bin Anas<sup>1</sup>.

Na amesema Al-'Awfi kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kuhusu Kauli ifuatayo ya Allah تعالى:

وَإِذَا أَرَدْنَا أَنْ نُهْلِكَ قَرْيَةً أَمَرْنَا مُتْرَفِيهَا فَفَسَقُوا فِيهَا

***“Na pindi Tunapotaka Kuungamiza mji huwaamuru (kumtii Allah pamoja na kusadikisha Mitume yake) wale wenye starehe na taanusi, lakini wao huendelea kutenda maovu humo...”***

Akasema: ‘Hii ina maana Tuliongeza idadi yao’<sup>2</sup>. Hii pia ndiyo iliyokuwa rai ya ‘Ikrimah, al-Hasan, adh-Dhahak na Qatadah<sup>3</sup>. Imepokewa na Maalik kutoka kwa az-Zuhriy kuwa, “Amarnaa” huwaamuru wale wenye starehe”, Yaani kukithiri.

وَكَمْ أَهْلَكْنَا مِنَ الْقُرُونِ مِنْ بَعْدِ نُوحٍ وَكَفَىٰ بِرَبِّكَ بِذُنُوبِ عِبَادِهِ خَبِيرًا بَصِيرًا ﴿١٧﴾

***17. Na kaumu ngapi Tumeziangamiza baada ya Nuuh! Na Mola wako Mlezi Anatosha kabisa kuwa ni Mwenye Kuzijua na Kuziona dhambi za waja Wake.***

### Vitisho kwa Makuraysh

Allah تعالى Anasema Kuwaonya makafiri wa Kikuraysh kwa kitendo cha kumkataa Mtume Wake Muhammad ﷺ, Allah تعالى Anatuambia kuwa Aliyaangamiza mataifa mengine waliokataa Mitume baada ya Nuuh عليه السلام. Hii inaonesha kuwa katika karne baina ya Adam عليه السلام na Nuuh عليه السلام, wanadamu walikuwa wanafuata Uislamu, kama alivyosema Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: “Baina Adam عليه السلام na Nuuh عليه السلام kulikuwa na vizazi kumi, wakati wote huo watu walikuwa wakifuata Uislamu.”<sup>4</sup> Maana ya ayah ni: “Enyi mnaokadhibisha (makafiri)! Nyinyi sio watukufu mbele ya Allah تعالى kuliko waliokuwa kabla yenu, nanyi mmekadhibisha Mtume aliye mtukufu zaidi na mbora wa viumbe. Hivyo, nyinyi mnastahiki zaidi adhabu”. Na Kauli Yake:

وَكَفَىٰ بِرَبِّكَ بِذُنُوبِ عِبَادِهِ خَبِيرًا بَصِيرًا ﴿١٧﴾

***“Na Mola wako Mlezi Anatosha kabisa kuwa ni Mwenye Kuzijua na Kuziona dhambi za waja Wake.”***

<sup>1</sup> Tabari 17:404.

<sup>2</sup> Tabari 17:404.

<sup>3</sup> Tabari 17:404, 405.

<sup>4</sup> Al-Majma' 6:318.

Maana yake: Yeye ni Mjuzi wa kila kitu mnachofanya, jema na baya, na hakuna kinachofichwa kutoka Kwake Aliyetukuka.

مَنْ كَانَ يُرِيدُ الْعَاجِلَةَ عَجَلْنَا لَهُ فِيهَا مَا نَشَاءُ لِمَنْ نُرِيدُ ثُمَّ جَعَلْنَا لَهُ جَهَنَّمَ يَصَلِّيَهَا  
مَذْمُومًا مَدْحُورًا ﴿١٨﴾ وَمَنْ أَرَادَ الْآخِرَةَ وَسَعَىٰ لَهَا سَعْيَهَا وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَأُولَٰئِكَ كَانَ  
سَعْيُهُمْ مَشْكُورًا ﴿١٩﴾

**18. Anayetaka Dunia, Tutafanya haraka kumletea hapa hapa Tunayoyataka kwa Tumtakaye. Kisha Tumemuekea Jahanamu; ataingia humo hali ya kuwa ni mwenye kulaumiwa na kufurushwa.**

**19. Na anayetaka Akhera, na akazifanyia juhudi amali zake, naye ni Muumini, basi hao juhudi yao itakuwa ni ya kushukuriwa.**

### Malipo na Jaza kwa Anayetaka Dunia hii na Akhera

Allah تعالی Anatufahamisha kuwa si kila anayetamani kupata ulimwengu huu na neema zake atakuwa ni mwenye kupata analotaka. Hilo linafikiwa kwa wale ambao Allah تعالی Anaotaka na Anachotaka wao wapate. Aya hii inafunga na kuzibana daima kauli za kijumla zilizokuja katika Aya nyingine.

Allah تعالی Anasema:

عَجَلْنَا لَهُ فِيهَا مَا نَشَاءُ لِمَنْ نُرِيدُ ثُمَّ جَعَلْنَا لَهُ جَهَنَّمَ

**“Tutafanya haraka Kumletea hapa hapa Tunayoyataka kwa Tumtakaye. Kisha Tumemuekea Jahanamu.”**

Kumaanisha katika nyumba ya Akhera.

يَصَلِّيَهَا

**“Atachomwa humo.”** Maana yake: Ataingia humo mpaka imzunguke kwa pande zake zote.

مَذْمُومًا

**“Hali ya kutwezwa.”** Maana yake: Kulaumiwa kwa tabia yake mbaya na matendo maovu, kwa sababu alichagua chenye kuisha juu ya chenye kudumu. Pia,

مَذْحُورًا ﴿١٧﴾

**“Kukataliwa.”**

Maana yake: Mbali na Rehema ya Allah تعالى, akiwa dhalili na kuaibishwa.

Na Kauli Yake:

وَمَنْ أَرَادَ الْآخِرَةَ

**“Na anayetaka Akhera.”**

Maana yake: Mwenye kutaka nyumba ya Akhera na zilizomo ndani yake katika neema na furaha. Kisha,

وَسَعَىٰ لَهَا سَعِيهَا

**“...Na Akazifanyia juhudi amali zake.”**

Maana yake: Akataka hayo kwa njia yake iliyo sawa, nayo ni kumfuata Mtume Muhammad ﷺ.

وَهُوَ مُؤْمِنٌ

**“Naye akiwa ni Muumini.”**

Kumaanisha moyo wake una Imani. Maana yake: anaamini kupata thawabu, jaza na adhabu. Hivyo,

فَأُولَٰئِكَ كَانَ سَعِيهِمْ مَّشْكُورًا ﴿١٨﴾

**“Basi hao juhudi yao itakuwa ni ya kushukuriwa.”**

\* \* \*

كُلًّا نُمِدُّ هُنُوْلًا ۖ وَهُنُوْلًا ۖ مِنْ عَطَاءِ رَبِّكَ ۗ وَمَا كَانَ عَطَاءُ رَبِّكَ مَحْظُورًا ﴿٢٠﴾ أَنْظِرْ كَيْفَ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَى بَعْضٍ ۗ وَلَآ خِرَّةٌ أَكْبَرُ دَرَجَتٍ ۖ وَأَكْبَرُ تَفْضِيلًا ﴿٢١﴾ لَا تَجْعَلْ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا ۖ آخَرَ فَتَقْعُدَ مَذْمُومًا مَحْدُولًا ﴿٢٢﴾ \* وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ ۚ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا ۗ إِمَّا يَبُلُغَنَّ عِنْدَكَ الْكِبَرَ أَحَدُهُمَا أَوْ كِلَاهُمَا فَلَا تَقُلْ لَهُمَا أُفٍّ وَلَا تَنْهَرهُمَا وَقُلْ لَهُمَا قَوْلًا كَرِيمًا ﴿٢٣﴾ وَأَخْفِضْ لَهُمَا جَنَاحَ الذُّلِّ مِنَ الرَّحْمَةِ وَقُلْ رَبِّ ارْحَمْهُمَا كَمَا رَبَّيَانِي صَغِيرًا ﴿٢٤﴾ رَبُّكُمْ أَعْلَمُ بِمَا فِي نُفُوسِكُمْ ۗ إِنْ تَكُونُوا صَالِحِينَ فَإِنَّهُ كَانَ لِلْأَوَّابِينَ غَفُورًا ﴿٢٥﴾ وَءَاتِ ذَا الْقُرْبَىٰ حَقَّهُ ۚ وَالْيَتَامَىٰ وَالسَّبِيْلَ وَلَا تُبْدِرْ تَبْدِيرًا ﴿٢٦﴾ إِنَّ الْمُبْدِرِينَ كَانُوا إِخْوَانَ الشَّيْطَانِ ۗ وَكَانَ الشَّيْطَانُ لِرَبِّهِ كَفُورًا ﴿٢٧﴾ وَإِمَّا تُعْرِضَنَّ عَنْهُمُ ابْتِغَاءَ رَحْمَةٍ مِنْ رَبِّكَ تَرْجُوهَا فَقُلْ لَهُمْ قَوْلًا مَيْسُورًا ﴿٢٨﴾ وَلَا تَجْعَلْ يَدَكَ مَغْلُولَةً إِلَىٰ عُنُقِكَ وَلَا تَبْسُطْهَا كُلَّ الْبَسْطِ فَتَقْعُدَ مَلُومًا مَحْسُورًا ﴿٢٩﴾ إِنَّ رَبَّكَ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَشَاءُ وَيَقْدِرُ ۗ إِنَّهُ كَانَ بِعِبَادِهِ خَبِيرًا بَصِيرًا ﴿٣٠﴾ وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ ۖ حَسِيَةً ۖ اِمْلَقِي ۗ نَحْنُ نَرِزُقُهُمْ وَإِيَّاكُمْ ۗ إِنْ قَتَلْتُمْ ۖ كَانَ خِطْئًا كَبِيرًا ﴿٣١﴾ وَلَا تَقْرُبُوا الرِّزْقَ ۗ إِنَّهُ كَانَ فَحِشَةً وَسَاءَ سَبِيلًا ﴿٣٢﴾

كُلًّا نُمِدُّ هُنُوْلًا ۖ وَهُنُوْلًا ۖ مِنْ عَطَاءِ رَبِّكَ ۗ وَمَا كَانَ عَطَاءُ رَبِّكَ مَحْظُورًا ﴿٢٠﴾ أَنْظِرْ كَيْفَ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَى بَعْضٍ ۗ وَلَآ خِرَّةٌ أَكْبَرُ دَرَجَتٍ ۖ وَأَكْبَرُ تَفْضِيلًا ﴿٢١﴾

**20. Wote hao Tunawa kunjulia - hawa na hao - katika Neema za Mola wako Mlezi. Wala neema za Mola wako Mlezi Hazizuiliki.**

**21. Angalia vipi Tulivyo wafadhili baadhi yao kuliko wengine. Na hakika Akhera ni yenye daraja kubwa zaidi na Fadhila kubwa zaidi.**

Allah تعالى Anasema:

كُلًّا

**“Wote hao.”** Kumaanisha kila mmoja kati ya makundi mawili hayo, wanaotaka dunia na wale wanaotaka Akhera Tunawakunjulia kwa yaliyo ndani yake. Hayo ni,

مِنْ عَطَاءِ رَبِّكَ

**“Katika Neema za Mola wako Mlezi”,**

Kumaanisha Yeye Ndiye wa Pekee Anayedhibiti kila kitu, Naye si dhalimu. Anampatia kila mmoja anachostahiki, ikiwa wema au uovu. Hukumu Yake haizuiliki, hakuna anayeweza kuzuia kwa Anachotoa au Kubadilisha kwa Analotaka. Kwa hiyo, Akasema:

﴿ وَمَا كَانَ عَطَاءُ رَبِّكَ مَحْظُورًا ﴾

***“Wala Neema za Mola wako Mlezi hazizuiliki.”***

Maana: Hawezi kuizuia mtu yeyote wala kuirudisha. Amesema Qatadah: Yaani hazipungui.<sup>1</sup>

﴿ وَمَا كَانَ عَطَاءُ رَبِّكَ مَحْظُورًا ﴾

***“Wala Neema za Mola wako Mlezi hazizuiliki.”***

Na amesema Al-Hasan na wengineo: “Inamaanisha hawatazuiliwa.”

Kisha Akasema Aliyetukuka:

﴿ أَنْظِرْ كَيْفَ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَى بَعْضٍ ﴾

***“Angalia vipi Tulivyowafadhili baadhi yao kuliko wenginewe.”***

Maana yake: Hapa duniani, miongoni mwao wapo walio matajiri, mafakiri na baina ya hao; mzuri, mbaya na baina yao hao; yupo atakayefariki akiwa mtoto mdogo, mwingine anaishi mpaka anakuwa mzee mkongwe na baina ya miaka hiyo. Hata hivyo,

﴿ وَلِلْآخِرَةِ أَكْبَرُ دَرَجَاتٍ وَأَكْبَرُ تَفْضِيلًا ﴾

***“Na hakika Akhera ni yenye daraja kubwa zaidi na Fadhila kubwa zaidi.”***

Maana yake: Tofauti baina yao Akhera itakuwa kubwa kuliko tofauti baina yao hapa duniani. Baadhi yao watakuwa katika daraja tofauti ndani ya Jahanamu (Moto), wakiwa wamefungwa na silsila (minyonyoro) na makongwa. Ilhali wengine watakuwa daraja za juu ndani ya Neema Zake na Furaha, nao

<sup>1</sup> At-Tabari 17:410.

watakuwa katika vidato vya fahari wakitofautiana baina yao. Kama vile watu wa daraja wanatofautiana, kwani Pepo ina daraja mia moja, baina ya kila daraja mbili (daraja moja na ile ya pili iliyo baada yake) kama baina ya mbingu na ardhi.<sup>1</sup>

Na katika Sahihi mbili kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ أَهْلَ الدَّرَجَاتِ الْعُلَى لَيَرَوْنَ أَهْلَ عِلِّيْنَ كَمَا تَرَوْنَ الْكَوْكَبَ الْغَابِرَ فِي أَفْقِ السَّمَاءِ»

*“Hakika watu wa daraja za juu kabisa Peponi watawaona watu wa ‘Illiyiin<sup>1</sup> kama vile wanatizama nyota zilizo mbali mbinguni.”<sup>2</sup>*

Kwa ajili hiyo Akasema Aliyetukuka:

وَلِلْآخِرَةِ أَكْبَرُ دَرَجَاتٍ وَأَكْبَرُ تَفْضِيلًا ﴿١٧﴾

*“Na hakika Akhera ni yenye daraja kubwa zaidi na Fadhila kubwa zaidi”.*

لَا تَجْعَلْ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا ءَاخَرَ فَتَقْعُدَ مَذْمُومًا مَّخْدُومًا ﴿١٨﴾

**22. Usimfanye mungu mwengine pamoja na Allah, usije ukawa wa kulaumiwa uliyetupika.**

**Usimshirikishe Allah تعالى na Chochote Katika Kumuabudu**

Allah تعالى Anasema, lengo likiwa ni kuwahutubia waliobebeshwa mzigo (waliopewa taklifu) katika Ummah huu: Msijaalie enyi mliokalifishwa mshirika katika kumuabudu kwenu Mola wenu Mlezi. Kwa sababu ukifanya hivyo:

فَتَقْعُدَ مَذْمُومًا

*“Usije ukakaa chini hali unalaumiwa”,*

Maana yake: Katika kumshirikisha Yeye. Na tena,

<sup>1</sup> Kwa maelezo na ufafanuzi tizama Suratul Mutwaffifiin 83: 18 – 21.

<sup>2</sup> Fat'h al-Baariy 6:386 na Muslim 4: 2177.



**“Uliyetupika.”**

Kwani Mola wako Mlezi Aliyetukuka, Hatakusaidia; Atakuacha kwa yule uliyemuabudu, naye hana, wala hatakuwa na uwezo wa kukusaidia (kukunufaisha) au kukudhuru. Sababu ni kuwa Anayemiliki na Mwenye uwezo wa Kukunufaisha na Kukudhuru ni Allah تعالى tu, asiye na mshirika. Amepokea Imaam Ahmad kutoka kwa 'Abdallah bin Mas'ud رضي الله عنه kuwa amesema: Mtume ﷺ amesema:

«مَنْ أَصَابَتْهُ فَاقَةٌ فَأَنْزَلَهَا بِالنَّاسِ لَمْ تُسَدَّ فَاقَتُهُ، وَمَنْ أَنْزَلَهَا بِاللَّهِ أُرْسَلَ اللَّهُ لَهُ بِالْغِنَى  
إِمَّا آجِلًا وَإِمَّا غِنَى عَاجِلًا»

*“Yeyote anayesibiwa na ufakiri, naye akawa anazunguka kutaka usaidizi wa watu, hataweza kuuondoa ufakiri huo. Na yeyote atakayetaka usaidizi kutoka kwa Allah, Allah Atampatia njia za kujitegemea (utajiri) kwa haraka au baadaye”<sup>1</sup>.*

Hii imenukuliwa na Abu Daawuud na At-Tirmidhiy, naye At-Tirmidhiy akasema kuwa hii ni Hadithi Hasan Sahih Gharib<sup>2</sup>.

\* وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا ۗ إِمَّا يَبُلُغَنَّ عِنْدَكَ الْكِبَرَ أَحَدُهُمَا أَوْ كِلَاهُمَا فَلَا تَقُلْ لَهُمَا أَلْفٌ وَلَا تَنْهَرُهُمَا وَقُلْ لَهُمَا قَوْلًا كَرِيمًا ﴿٢٣﴾  
وَأَخْفِضْ لَهُمَا جَنَاحَ الذَّلِيلِ مِنَ الرَّحْمَةِ وَقُلْ رَبِّ ارْحَمْهُمَا كَمَا رَبَّيَانِي صَغِيرًا ﴿٢٤﴾

**23. Na Mola wako Mlezi Ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu, na wazazi wawili muwatendee wema. Mmoja wao akifikia uzee, naye yuko kwako, au wote wawili, basi usimwambie hata: Ah! Wala usiwakemee. Na sema nao kwa msemo wa heshima.**

<sup>1</sup> Ahmad 1:407.

<sup>2</sup> Abu Daawuud 2:296 na Tuhfatul Ahwadhiy 6:617.



**24. Na uwainamishie bawa la unyenyekevu kwa kuwaonea huruma. Na useme: Mola wangu Mlezi! Warehemu kama walivyonilea utotoni.**

### **Amri ya Kumuabudu Allah تعالی Pekee na Kuwatendea Wema Wazazi**

Allah تعالی Anatuamuru sisi tumuabudu Yeye tu, wala tusimshirikishe Yeye na mwingine yeyote. Neno *Qadhwa* hapa linamaanisha “kuamrisha”. Mujaahid amesema:

﴿ وَقَصَىٰ ﴾

**“Na ameamuru.”**

Lina maana ya kuusia<sup>1</sup>. Hivi ndivyo pia alivyosoma Ubayy bin Ka’b, Ibn Mas’ud na Adh-Dhahhaak bin Muzaahim رضي الله عنهم. Ni kama Aya:

﴿ وَقَصَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ ﴾

**“Na Mola wako Mlezi Ameusia (Ameamuru) kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu.”<sup>2</sup>**

Wazo la kumuabudu Allah تعالی limefungamanishwa na kuwaheshimu wazazi. Allah تعالی Anasema:

﴿ وَيَأْتِ الْوَالِدِينَ إِحْسَانًا ﴾

**“Na wazazi wawili muwatendee wema.”**

Hapa Anaamrisha Kuwafanyia wema wazazi, kama Alivyosema mahali kwengineko:

﴿ أَنْ أَشْكُرَ لِي وَلِوَالِدَيْكَ إِلَىٰ الْمَصِيرِ ﴾

**“Upate kunishukuru Mimi na wazazi wako, Kwangu ndio marejeo yenu.” (31:14)**

Allah تعالی Anaendelea:

<sup>1</sup> At-Tabari 17:414.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:413, 414.

إِمَّا يَبْلُغَنَّ عِندَكَ الْكِبَرَ أَحَدُهُمَا أَوْ كِلَاهُمَا فَلَا تَقُلْ لَهُمَا أُفٍّ

**“Mmoja wao akifikia uzee, naye yuko kwako, au wote wawili, basi usimwambie hata: Ah!”**

Maana: Usiwaambie kauli yoyote ya matusi kutoka kwako, hata kuwaambia: “Uff (Ah!)”, ambayo ni neno jepesi zaidi la utovu wa adabu na heshima. Pia,

وَلَا تَنْهَرُهُمَا

**“Usiwakemee.”** Maana yake: Usiwafanyie kitu chochote kibaya.

وَلَا تَنْهَرُهُمَا

**“Na usiwakemee.”** Atwaa’ bin Rabaah amesema kuwa hiyo inamaanisha: “Usinyanyue mkono wako dhidi yao.”<sup>1</sup>

Pale Allah تعالى Alipokataza kuwatolea kauli mbaya na kuwatendea mambo mabaya, Aameamrisha kuzungumza nao na kuwatendea yaliyo mema na mazuri. Hivyo Akasema:

وَقُلْ لَهُمَا قَوْلًا كَرِيمًا ﴿١٧﴾

**“Na sema nao kwa msemu wa heshima.”**

Kumaanisha kwa upole, huruma, ulaini, ukarimu, kwa heshima na kushukuru. Mbali na hayo:

وَأَخْفِضْ لَهُمَا جَنَاحَ الذُّلِّ مِنَ الرَّحْمَةِ

**“Na uwainamishie bawa la unyenyekevu kwa kuwaonea huruma.”**

Maana: Nyenyekea kwao katika matendo yako. Na uwe ni mwenye kusema kwa kuwaombea:

وَقُلْ رَبِّ ارْحَمْهُمَا كَمَا رَبَّيَانِي صَغِيرًا ﴿١٨﴾

**“Na useme: Mola wangu Mlezi! Warehemu kama walivyonilea utotoni.”**

Hii ina maana yaseme haya wanapozeeka (wanapo kuwa wakongwe) na pindi wanapoaga dunia. Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Baadaye Allah تعالى Akateremsha:

<sup>1</sup> At-Tabari 17:417.

مَا كَانَتْ لِلنَّبِيِّ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا أَنْ يَسْتَغْفِرُوا لِلْمُشْرِكِينَ

**“Haimpasi Mtume na wale walioamini kuwatakia msamaha washirikina ijapokuwa ni jamaa zao.” (9:113)<sup>1</sup>**

Zipo Hadithi zinazozungumzia kuwaheshimu wazazi, kama ile Hadithi iliyopokewa kupitia kwa Isnadi nyingi ya masimulizi kutoka kwa Anas na wengineo رضي الله عنهم. Inayosema kuwa Mtume ﷺ alipopanda mimbari siku moja alisema: “Amin, Amin, Amin”. Aliulizwa: “Ewe Mtume wa Allah! Kwa nini umesema Amin?” Akajibu:

«أَتَانِي جِبْرِيلُ فَقَالَ: يَا مُحَمَّدُ رَغِمَ أَنْفُ رَجُلٍ ذُكِرَتْ عِنْدَهُ فَلَمْ يُصَلِّ عَلَيْكَ، قُلْ: آمِينَ، فَقُلْتُ: آمِينَ، ثُمَّ قَالَ: رَغِمَ أَنْفُ رَجُلٍ دَخَلَ عَلَيْهِ شَهْرُ رَمَضَانَ ثُمَّ خَرَجَ فَلَمْ يُغْفَرْ لَهُ، قُلْ: آمِينَ، فَقُلْتُ: آمِينَ، ثُمَّ قَالَ: رَغِمَ أَنْفُ رَجُلٍ أَدْرَكَ وَالِدَيْهِ أَوْ أَحَدَهُمَا فَلَمْ يُدْخِلْهُ الْجَنَّةَ، قُلْ: آمِينَ، فَقُلْتُ: آمِينَ»

*“Jibril alinjia na akaniambia: ‘Ewe Muhammad! Ameangamia anayesikia jina lako likitajwa, naye asikuswalia’. Akasema: “Sema, Amin”. Nami nikasema, ‘Amin.’ Kisha akasema: “Ameangamia yule anayeingiliwa na mwezi wa Ramadhani kisha ukapita bila kusamehewa madhambi yake”. Akasema: “Sema, Amin”. Nami nikasema: “Amin”. Kisha akasema: “Ameangamia yule aliyewakuta wazazi wake au mmoja wao asiwe ni mwenye kuingia Peponi (kwa kuwatumikia wao vizuri.)” Akasema: “Sema, Amin”. Nami nikasema: “Amin”<sup>2</sup>.*

## Hadithi Nyingine

Amepokea Imaam Ahmad kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«رَغِمَ أَنْفٌ، ثُمَّ رَغِمَ أَنْفٌ ثُمَّ رَغِمَ أَنْفٌ رَجُلٍ أَدْرَكَ أَحَدَ أَبْنَائِهِ أَوْ [كِلَيْهِمَا] عِنْدَ الْكَبِيرِ وَلَمْ يَدْخُلِ الْجَنَّةَ»

*“Ameangamia, kisha ameangamia, kisha ameangamia, mtu aliyemkuta mzazi wake (mmoja) au wote wawili akiwa mkongwe (wakiwa wakongwe), asiingie Peponi.”<sup>3</sup>*

<sup>1</sup> At-Tabari 17:421.

<sup>2</sup> Tuhfatul al-Ahwadhiy 5:550.

<sup>3</sup> Ahmad 2:346.



## Hadithi Nyingine

Amepokea Ahmad kuwa mtu mmoja kutoka katika ukoo wa Yarbu' (Banu Yarbu') alisema: "Nilikuja kwa Mtume ﷺ akiwa anazungumza na watu, nami nikamsikia akisema:

«يَدُ الْمُعْطِي الْعَلِيَا، أُمَّكَ وَأَبَاكَ، وَأُخْتِكَ وَأَخَاكَ، ثُمَّ أَدْنَاكَ أَدْنَاكَ»

*"Mkono unaotoa ni bora, mpe mamako na babako, dadako na kaka yako, kisha aliye karibu (kwa ujamaa) na anayefuata (kwa ukaribu)"<sup>1</sup>.*

رَبُّكُمْ أَعْلَمُ بِمَا فِي نُفُوسِكُمْ ۚ إِنَّ تَكُونُوا صَالِحِينَ فَإِنَّهُ كَانَ لِلْأَوَّابِينَ غُفُورًا ﴿٢٥﴾

**25. Mola wenu Anajua kabisa yaliyo nyoyoni mwenu. Ikiwa nyinyi mtakuwa wema, basi hakika Yeye ni Mwenye Kuwaghufiria wenye kurejea kwake kwa unyenyekevu.**

## Makosa Dhidi ya Wazazi Yanasamehewa kwa Kurudisha Mahusiano Mazuri na Kutubia kwa Allah تعالی

Amesema Said bin Jubayr: "Huyo ni mtu anayesema kitu anachodhania hakitakuwa kibaya kwa wazazi wake". Kulingana na riwaya nyingine: "Hakutaka ila kheri kwa hilo"<sup>2</sup>. Hivyo, Allah تعالی Akasema:

رَبُّكُمْ أَعْلَمُ بِمَا فِي نُفُوسِكُمْ ۚ إِنَّ تَكُونُوا صَالِحِينَ

**"Mola wenu Anajua kabisa yaliyo nyoyoni mwenu. Ikiwa nyinyi mtakuwa wema".**

Na Kauli Yake:

فَإِنَّهُ كَانَ لِلْأَوَّابِينَ غُفُورًا ﴿٢٥﴾

**"Basi hakika Yeye ni Mwenye Kuwaghufiria wanaotubia Kwake".**

Amesema Qataadah: "Kwa wenye kutii, watu wa Sala"<sup>3</sup>. Na amepokea Shu'bah kutoka kwa Yahya bin Said kutoka kwa Said bin Al-Musayyab kuhusu Kauli Yake تعالی:

<sup>1</sup> Ahmad 4:64.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:422.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:422.

فَإِنَّهُمْ كَانُوا لِالْآوَابِينَ غُفُورًا ﴿٢٠﴾

**“Basi hakika Yeye ni Mwenye Kuwaghufiria wanaotubia Kwake.”**

Kuwa ni, “Wale wenye kufanya dhambi kisha wakatubia na kufanya tena dhambi na kutubia”<sup>1</sup>. Na amesema ‘Atwaa’ bin Yasaar, Said bin Jubayr na Mujaahid: “Ni wale wenye kurudi katika kheri”<sup>2</sup>. Mujaahid amepokea kutoka kwa ‘Ubayd bin ‘Umayr, kuhusiana na Aya hii: “Huyu ni yule ambaye anapokumbuka dhambi aliyoifanya anapokuwa peke yake, anataka msamaha kutoka kwa Allah”. Mujaahid anakubaliana naye katika hilo<sup>3</sup>.

Ibn Jariir رحمه الله تعالى amesema: “Na muono ulio mzuri zaidi kuhusu suala hili ni kauli ya aliyesema: Huyo ni anayetubu kutokana na dhambi, mwenye kurudi kutoka katika maasi kwenda kwenye utiifu na mwenye kuacha analochukia Allah kufanya Alipendalo na Analoliridhia”<sup>4</sup>. Na hili alilosema ndilo la sawa, kwani “Al-Awaab” inatokana kwa “Al-Awbi” nayo ni kurudi. Katika lugha ya kiarabu husemwa: “Aaba fulani” yaani anaporudi. Amesema Aliyetukuka:

إِنَّ إِلَيْنَا إِيَابَهُمْ ﴿٢١﴾

**“Hakika marejeo yao ni Kwetu.” (88:25).**

Na kulingana na Hadithi iliyo Sahihi ni kuwa Mtume ﷺ alipokuwa anarudi kutoka safari alikuwa anasema:

«أَيُّونَ نَائِبُونَ، عَابِدُونَ لِرَبِّنَا حَامِدُونَ»

*“Tumerudi huku tunatubia, tunatekeleza Ibada na Mola wetu Mlezi tunamsifu na kumshukuru.”<sup>5</sup>*

وَأَاتِ ذَا الْقُرْبَىٰ حَقَّهُ وَالْمِسْكِينَ وَابْنَ السَّبِيلِ وَلَا تَبْذُرْ نَبْذِيرًا ﴿٢٢﴾ إِنَّ الْمُبْذِرِينَ

كَانُوا إِخْوَانَ الشَّيْطَانِ ۗ ط وَكَانَ الشَّيْطَانُ لِرَبِّهِ كَفُورًا ﴿٢٣﴾ وَإِذَا تَعْرَضْنَا عَنْهُمْ أَتْبَغَاءَ

رَحْمَةٍ مِّن رَّبِّكَ تَرْجُوهَا فَقُلْ لَهُمْ قَوْلًا مَّيْسُورًا ﴿٢٤﴾

<sup>1</sup> At-Tabari 17: 423.

<sup>2</sup> At-Tabari 17: 424, 425.

<sup>3</sup> At-Tabari 17: 424.

<sup>4</sup> At-Tabari 17: 425.

<sup>5</sup> Fat'h al-Baari 3: 724.

**26. Na mpe aliye jamaa yako haki yake, na masikini, na msafiri; wala usitumie ovyo kwa fujo.**

**27. Hakika wabadhirifu ni ndugu wa Mashetani. Na Shetani ni mwenye kumkufuru Mola wake Mlezi.**

**28. Na ikiwa unajikurupusha nao, nawe unatafuta Rehema ya Mola wako Mlezi unayoitaraji, basi sema nao maneno laini ya huruma.**

### **Amri ya Kudumisha Uhusiano wa Kindugu na Kukataza Ubadhirifu**

Pale Allah تعالى Alipotaja Kuwatendea wema wazazi, Alifuatisha hilo na amri ya kuwafanyia wema jamaa na kuenzi undugu. Na katika Hadithi:

«أُمَّكَ وَأَبَاكَ، ثُمَّ أَدْنَاكَ أَدْنَاكَ» وفي رواية «ثُمَّ الْأَقْرَبَ فَلَا اقْرَب»

“Mamako na babako, kisha walio chini yao (jamaa wa karibu) na wanaofuatia hao kwa ukaribu.”

Na katika riwaya nyingine: “Kisha walio karibu (kwa ujamaa), na walio karibu (baada yao)”<sup>1</sup>. Na katika Hadithi:

«مَنْ أَحَبَّ أَنْ يُسَاطَ لَهُ فِي رِزْقِهِ وَيُنْسَأَ لَهُ فِي أَجَلِهِ، فَلْيَجِئْ رَجِيمًا»

“Yeyote anayependa kupanuliwa riziki yake, umri wake kuongezwa, basi aunge kizazi”<sup>2</sup>.

Na Kauli ya Aliyetukuka:

وَلَا تُبَدِّرْ تَبْدِيرًا ﴿٦٧﴾

**“Wala usitumie ovyo kwa fujo”.**

Pindi Allah تعالى Alipoamrisha kutoa, Alikataza ubadhirifu kwayo. Bali utumiaji unatakiwa ufanywe kwa kiwango cha kati na kati kama Alivyosema katika Aya nyingine:

وَالَّذِينَ إِذَا أَنْفَقُوا لَمْ يُسْرِفُوا وَلَمْ يَقْتُرُوا

**“Na wale ambao wanapotumia hawatumii kwa fujo wala hawafanyi ubakhili, bali wanakuwa katikati baina ya hayo.” (25:67)**

<sup>1</sup> Ahmad 2:226.

<sup>2</sup> Muslim 4:1982.

Kisha Akasema, kukemea ubadhirifu na kufanya Israfu.

إِنَّ الْمُبَدِّرِينَ كَانُوا إِخْوَانَ الشَّيْطَانِ

**“Hakika wabadhirifu ni ndugu wa Mashetani”,**

Maana: Wameshabihiana nao katika hilo. Amesema Ibn Mas’ud رضي الله عنه: “Ubadhirifu ni kutumia katika njia isiyo ya haki”<sup>1</sup>. Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema hivyo hivyo<sup>2</sup>. Mujaahid amesema: “Iwapo mtu atatumia mali yake yote katika mambo ya sawa, hataingia katika sifa ya ubadhirifu, lakini akitumia hata kidogo kwa njia isiyo ya sawa, ataingia katika sifa hiyo.”<sup>3</sup> Qataadah amesema: “Ubadhirifu unaamanisha kutumia pesa katika kumuasi Allah Aliyetukuka, katika yasiyokuwa ya haki, ufisadi na uharibifu.”<sup>4</sup>

Na amepokea Ahmad kutoka kwa Anas bin Maalik رضي الله عنه kuwa amesema: Alikuwa mtu wa ukoo wa Tamiim kwa Mtume ﷺ akamuwambia: “Ewe Mtume wa Allah! Hakika mimi nina mali nyingi, mwenye familia, watoto na ustaarabu (wa maisha ya mjini). Nipashe habari nitumie vipi na nifanye nini?” Akasema Mtume ﷺ:

«تُخْرِجُ الزَّكَاةَ مِنْ مَالِكَ إِنْ كَانَ، فَإِنَّهَا طَهْرَةٌ تُطَهِّرُكَ، وَتَصِلُ أَقْرَبَاءَكَ، وَتَعْرِفُ حَقَّ السَّائِلِ وَالْجَارِ وَالْمَسْكِينِ»

*“Toa Zakah kwa mali yako ikiwa unadaiwa (hujalipa), kwani kufanya hivyo ni utakaso kwako ambao utakufanya uwe safi, unga kizazi na jamaa zako wa karibu, jua haki ya mwenye kuuliza (muombaji), jirani na masikini”.*

Akasema: “Nifanyie sahali na wepesi”. Akamsomea:

وَأَاتِ ذَا الْقُرْبَىٰ حَقَّهُ وَالْمَسْكِينِ وَالْأَسْبِيلَ وَلَا تَبَدِّرْ تَبْدِيرًا ﴿٢٦﴾

**“Na mpe aliye jamaa yako haki yake, na masikini, na msafiri; wala usitumie ovyo kwa fujo”. (17:26)**

Akasema: “Hiyo inatosha, Ewe Mtume ﷺ. Je, nikitoa Zakah kwa Mtume ﷺ,

<sup>1</sup> Tabari 17: 428.

<sup>2</sup> Tabari 17: 429.

<sup>3</sup> Tabari 17: 429.

<sup>4</sup> Tabari 17: 429.



nitasamehewa na jukumu hilo mbele ya Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ? Akasema Mtume ﷺ:

«نَعَمْ، إِذَا أَدَيْتَهَا إِلَى رَسُولِي فَقَدْ بَرَّتَ مِنْهَا وَلَكَ أَجْرُهَا، وَإِنَّمَا عَلَى مَنْ بَدَّلَهَا»

*“Ndio, ukimpatia mjumbe wangu, utakuwa umetekeleza wajibu wako na kutoka katika dhambi, nawe utapata ujira (na thawabu) na madhambi yatamuangukia aliyebadilisha”<sup>1</sup>.*

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

إِنَّ الْمُبْذِرِينَ كَانُوا إِخْوَانَ الشَّيْطَانِ

***“Hakika wabadhirifu ni ndugu wa Mashetani.”***

Maana: Ni ndugu zao katika ubadhirifu, ujinga, kushindwa kumtii Allah تعالى na kuasi. Allah تعالى Anasema:

وَكَانَ الشَّيْطَانُ لِرَبِّهِ كَفُورًا

***“Na Shetani ni mwenye kumkufuru Mola wake Mlezi.”***

Maana: Yeye hana shukrani wala fadhila kwa sababu alikataa neema za Allah تعالى juu yake, wala hakumtii bali aliendelea na maasi yake na kwenda kinyume Kwake. Na Kauli Yake:

وَأَمَّا تَعْرِضْنَ عَنْهُمْ أَبْتِغَاءَ رَحْمَةٍ مِنْ رَبِّكَ

***“Na ikiwa unajikurupusha nao, nawe unatafuta rehema ya Mola wako Mlezi.”***

Maana: Ikiwa jamaa zako wa karibu na wale Tuliokuamuru kuwasaidia watakuomba chochote, nawe huna chochote, ukageuka kwao kwa kukosa cha kuwapa kwa sababu ya kutokuwa nacho,

فَقُلْ هُمْ قَوْلًا مَيْسُورًا

***“Basi Sema nao maneno laini ya huruma.”***Maana: Kwa kuwaahidi kwa usahali na ulaini kuwa pindi itakapokuja riziki ya Allah تعالى tutawasiliana nanyi, Allah تعالى Akipenda. Hivi ndivyo alivyoifasiri Kauli Yake Aliyetukuka: “Basi sema

<sup>1</sup> Ahmad 3:136. Baadhi ya wanazuoni wanaichukulia Hadithi hii kuwa sahihi, japokuwa haijayakinishwa kwa mpokezi wake, Said bin Abi Hilaal alisikia kutoka kwa Anas bin Maalik.

nao maneno matamu”, kwa kuwaahidi. Hii ndio iliyokuwa rai ya Mujaahid, ‘Ikrimah, Said bin Jubayr, Al-Hasan, Qataadah na wengineo<sup>1</sup>.

وَلَا تَجْعَلْ يَدَكَ مَغْلُولَةً إِلَىٰ عُنُقِكَ وَلَا تَبْسُطْهَا كُلَّ الْبَسْطِ فَتَقْعُدَ مَلُومًا مَّحْسُورًا ﴿٢٧﴾

إِنَّ رَبَّكَ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَن يَشَاءُ وَيَقْدِرُ ۗ إِنَّهُ كَانَ بِعِبَادِهِ خَبِيرًا بَصِيرًا ﴿٢٨﴾

**29. Wala usiufanye mkono wako kama uliofungwa shingoni mwako, wala usiukunjue wote kabisa, utabaki ukilaumiwa muflisi (mahsu\_ran).**

**30. Hakika Mola wako Mlezi Humkunjulia riziki Amtakaye, na Humpimia Amtakaye. Hakika Yeye kwa waja Wake ni Mwenye Kuwajua na Kuwaona.**

### Kuwa Mtu wa Wastani katika Matumizi

Allah تعالیٰ Ameamuru kuwa na matumizi ya kati na kati katika maisha, Akaukemea ubakhili na Kukataza ubadhirifu. Akasema:

وَلَا تَجْعَلْ يَدَكَ مَغْلُولَةً إِلَىٰ عُنُقِكَ

**“Wala usiufanye mkono wako kama uliofungwa shingoni mwako.”**

Hii ina maana usiwe bakhili, mwenye kuzuia, usiyetoa chochote kwa yeyote, kama Mayahudi vile – laana ya Allah تعالیٰ iwe juu yao – waliposema: “Mkono wa Allah تعالیٰ Umefumba”, Maana: Hatoi, wakamnasibisha na ubakhili, Ametukuka Allah تعالیٰ na Utakaso ni Wake, Mwenye Ukarimu Mkubwa.

وَلَا تَبْسُطْهَا كُلَّ الْبَسْطِ

**“Wala usiukunjue wote kabisa.”**

Maana: Wala usifuje katika kutoa, ukatoa zaidi kuliko unachoweza, na ukatoa zaidi kuliko pato lako, kufanya hivyo huenda ikawa ni sababu ya wewe kufilisika, kulaumiwa na kujikuta umefukarika. Ukiwa bakhili, watu watakulaumu na kukushutumu, na hawawezi kukutegemea kabisa. Pia unapotumia kuliko uwezo wako, utajikuta katika hali ya kuwa na bila ya chochote cha kutumia, hivyo utabaki dhaifu kama mnyama asiyeweza kutembea. Mnyama huyo huwa dhaifu

<sup>2</sup> Tabari 17:431, 432.

na asiyeweza kufanya chochote (*al hasiir*). Mtu huyo amefananishwa na mnyama aliyelika, ambaye ni sawa katika maana, aliyechoka na kuishiwa nguvu kabisa na hivyo kuitwa *al Hasiir*. Kama Allah تعالى Alivyosema:

فَأَرْجِعِ الْبَصَرَ هَلْ تَرَىٰ مِنْ فُطُورٍ ﴿٦٧﴾ ثُمَّ أَرْجِعِ الْبَصَرَ كَرَّتَيْنِ يَنْقَلِبْ إِلَيْكَ الْبَصَرُ  
خَاسِئًا وَهُوَ حَسِيرٌ ﴿٦٨﴾

***“Kisha tizama tena: ‘Je unakuta mwanja wowote?’ Kisha tizama tena na tena, utizamaji wako utarudi kwako katika hali ya utwevu na kulika (Hasiir).” (67:3-4)***

Hii ina maana hutoweza kupata makosa yoyote. Hivyo hivyo, Ibn ‘Abbaas, Al-Hasan, Qataadah, Ibn Jurayj, Ibn Zayd na wengineo رضي الله عنهم wameifahamu Aya hii kuwa ni ubakhili na kufuja (israfu)<sup>1</sup>.

Imepokewa katika Sahihi mbili kutoka kwenye Hadithi ya Abi Az-Zinaad kutoka kwa Al-A'raj, naye kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume wa Allah ﷺ amesema:

«مَثَلُ الْبَخِيلِ وَالْمُنْفِقِ كَمَثَلِ رَجُلَيْنِ عَلَيْهِمَا جُبَّتَانِ مِنْ حَدِيدٍ مِنْ تُدْيِهِمَا إِلَى تَرَابِيهِمَا، فَأَمَّا الْمُنْفِقُ فَلَا يُنْفِقُ إِلَّا سَبَعَتْ - أَوْ وَفَرَتْ - عَلَى جِلْدِهِ حَتَّى تُخْفِي بَنَانَهُ وَتَعْفُو أَرْؤَهُ، وَأَمَّا الْبَخِيلُ فَلَا يُرِيدُ أَنْ يُنْفِقَ شَيْئًا إِلَّا لَزِقَتْ كُلُّ حَلْقَةٍ مِنْهَا مَكَانَهَا، فَهُوَ يُوسِمُهَا فَلَا تَسْبَعُ»

*“Mfano wa bakhili na mtoaji ni mfano wa watu wawili waliovaa majuba mawili ya chuma kuanzia kifuani mpaka kwenye mitulinga yao. Ama mtoaji anapotoa sadaka yake, juba lake hupanuka hadi linamuenea mwili mzima, kwa kiasi cha kufinika alama za vidole vyake na kusamehewa madhambi yake. Na ama bakhili huwa hataki kutoa chochote, hivyo lile juba la chuma hugandama, kila pete yake sehemu yake. Hujaribu kulipanua lakini wapi, halipanuki kabisa.”<sup>2</sup>*

Riwaya kwa lafdhi hii imenukuliwa na Al-Bukhaari katika Kitabu cha Zakaah.

Katika Sahihi mbili imepokewa kutoka kwa Mu'awiyah bin Abi Muzarrid kutoka kwa Said bin Yasaar kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema, Mtume ﷺ amesema:

<sup>1</sup> At-Tabari 17:434, 435.

<sup>2</sup> Fat'h Al-Baariy 3:358 na Muslim 2:708.

«مَا مِنْ يَوْمٍ يُضَيِّحُ الْعِبَادَ فِيهِ إِلَّا وَمَلَكَانِ يَنْزِلَانِ مِنَ السَّمَاءِ يَقُولُ أَحَدُهُمَا: اللَّهُمَّ  
أَعْطِ مُنِيفًا خَلْفًا، وَيَقُولُ الْآخَرُ: اللَّهُمَّ أَعْطِ مُسِيكًا تَلْفًا»

*“Hakuna siku yoyote anayopambazukiwa ndani yake mja isipokuwa wapo Malaika wawili wanateremka kutoka mbinguni. Mmoja wao husema: ‘Ewe Allah! Mlipe nyongeza mwenye kutoa (sadaka)’. Na mwengine husema: ‘Ewe Allah! Muangamize mwenye kuzuia (kutotoa)”.*

Muslim amepokea kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kwa njia ya *marfui*:

«مَا نَقَصَ مَالٌ مِنْ صَدَقَةٍ، وَمَا زَادَ اللَّهُ عَبْدًا أَنْفَقَ إِلَّا عِزًّا، وَمَنْ تَوَاضَعَ لِلَّهِ رَفَعَهُ  
اللَّهُ»

*“Mali haipungui kwa kuitoa katika njia ya sadaka. Allah Hamzidishii mja mwenye kutoa sadaka ila utukufu, na mwenye kunyenyekea kwa ajili ya Allah basi Allah Humnyanyua cheo chake.”<sup>1</sup>*

Na Imekuja Hadithi ya Abi Kathir kutoka kwa ‘Abdallah bin ‘Amr رضي الله عنهما kwa njia ya *marfui* (aliyeinasibisha kwa Mtume):

«إِيَّاكُمْ وَالشَّحَّ فَإِنَّهُ أَهْلَكَ مَنْ كَانَ قَبْلَكُمْ، أَمْرَهُمْ بِالْبُخْلِ فَبِخَلُوا، وَأَمْرَهُمْ بِالْقَطِيعَةِ  
فَقَطَعُوا، وَأَمْرَهُمْ بِالْفُجُورِ فَفَجَرُوا»

*“Tahadharini na ubahili kwani uliwaangamiza waliokuwa kabla yenu. Uliwaamuru kuwa mabakhili, nao wakawa na ubakhili; ukawaamuru kukata udugu, hivyo wakakata uhusiano wa kizazi; na ukawaamrisha wao kufanya uchafu, nao wakafanya hivyo”<sup>2</sup>.*

Na Kauli Yake:

إِنَّ رَبَّكَ يَبْسُطُ الرِّزْقَ لِمَنْ يَشَاءُ وَيَقْدِرُ<sup>3</sup>

***“Hakika Mola wako Mlezi Humkunjulia riziki Amtakaye, na Humpimia Amtakaye”.***

Aya hii inatupasha habari kuwa Allah Aliyetukuka Ndiye Mwenye Kutoa riziki,

<sup>1</sup> Muslim 4:2001.

<sup>2</sup> Ahmad 2:159.

Mwenye Kuzuia, Mwenye Kukunjua, Anayepeleka mambo ya viumbe Vyake Anavyotaka. Anampa utajiri Amtakaye, na Anamfanya masikini Amtakaye, kwani kuna hekima katika hayo. Kwa ajili hiyo Akasema:

إِنَّهُ كَانَ بِعِبَادِهِ خَبِيرًا بَصِيرًا ﴿١٧﴾

***“Hakika Yeye kwa waja Wake ni Mwenye Kuwajua na Kuwaona.”***

Maana yake: Ni Mjuzi, Mwenye Kuona yupi anayestahiki utajiri na mwenye kustahiki ufakiri.

Hakika ni kuwa inawezekana kuwa utajiri kwa baadhi ya watu ni kumtoa katika njia ya sawa (kumsahaulisha) na ufakiri ni adhabu. Tunajilinda na kutaka msaada wa Allah تعالى kwa hili na lile (mambo yote mawili).

وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ حَشِيَّةَ إِمْلَاقٍ ۖ لَنْ نَرْزُقَهُمْ وَإِيَّاكُمْ ۖ إِنَّ قَتْلَهُمْ كَانَ خِطْئًا كَبِيرًا ﴿٣١﴾

***31. Wala msiwauwe wana wenu kwa kuogopa umasikini. Sisi Tutawaruzuku wao na nyinyi. Hakika kuwau hao ni hatia kubwa.***

### **Makatazo ya Kuwau Watoto**

Aya hii tukufu ni dalili kuwa Allah تعالى ni Mwingi wa Rehema kwa waja Wake kuliko mzazi kwa mtoto wake. Kwani Yeye Amekataza kuuliwa kwa watoto kama Alivyowausia wazazi kuwatizama watoto wao katika masuala ya mirathi. Watu wa ujahiliya walikuwa hawawaruhusu mabinti zao kuwarithi, na wengine walikuwa hata wakiwau mabinti zao ili familia yake isiongezeke na wasizidi kuwa masikini. Hivyo, Allah تعالى Akakataza hilo, Akasema:

وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ حَشِيَّةَ إِمْلَاقٍ ۖ

***“Wala msiwauwe wana wenu kwa kuogopa umasikini.”***

Maana: Kwa hofu ya kuwatia wao katika ufukara katika mustakbali wao. Kwa hiyo, Allah تعالى Akataja mwanzo riziki za watoto, Akasema:

لَنْ نَرْزُقَهُمْ وَإِيَّاكُمْ ۖ

***“Sisi Tutawaruzuku wao na nyinyi.”***

Na katika Suratul An'aam (6), Allah تعالى Anasema:

وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ مِمَّنْ إِمْلَقِي<sup>ط</sup>

**“Wala musiwauwae wana wenu kwa ajili ya umasikini.” (6:151)**

Maana: Kwa sababu ya ufakiri,

نَحْنُ نَرْزُقُهُمْ وَإِنَّا كَرِيمُونَ<sup>ط</sup>

**“Sisi Tutawaruzuku nyinyi na wao.”** Na Kauli Yake Aliyetukuka:

إِن قَتَلْتُمْ كَانَ خَطْفًا كَبِيرًا ﴿١٧١﴾

**“Hakika kuwaua hao ni hatia kubwa.”**

Maana yake: Dhambi kubwa. Na wakasoma baadhi yao: “Kaana Khatwa’an Kabiiraa”, badala ya: “Kaana Khitw’an Kabiira”, na maana zao ni sawa. Na imenukuliwa katika Sahihi mbili kutoka kwa ‘Abdallah bin Mas’ud رضي الله عنه kuwa alisema: “Ewe Mtume wa Allah! Ni dhambi gani iliyo kubwa?” Akasema:

«أَنْ تَجْعَلَ لِلَّهِ بَدَأًا وَهُوَ خَلَقَكَ . قُلْتُ: نُمُّ أَيُّ؟ قَالَ: أَنْ تَقْتُلَ وَلَدَكَ خَشِيئَةً أَنْ يَطْعَمَ مَعَكَ . قُلْتُ: نُمُّ أَيُّ؟ قَالَ: أَنْ تُزَانِيَ بِحَلِيلَةِ جَارِكَ»

“Kumuekea Allah washirika wakati Yeye Ndiye Aliyekuumba”.  
Nikauliza: “Kisha lipi?” Akasema: “Kumuua mtoto wako kwa kuogopea kuwa atakula nawe”. Nikauliza: Kisha lipi?” Akasema: “Kuzini na mke wa jirani yako”<sup>1</sup>.

وَلَا تَقْرَبُوا الزَّوْجَ إِذْهُ<sup>ط</sup> كَانَ فَنَحِشَةً وَسَاءَ سَبِيلًا ﴿١٧٢﴾

**32. Wala msikaribie uzinzi. Hakika huo ni uchafu na njia mbaya.**

**Amri ya Kujiepusha na Zinaa na Kila Kitu Kinachokurubisha Zinaa**

Allah تعالى Anasema huku Akiwakataza waja Wake na kuikaribia na pamoja na kujiepusha na vishawishi vyake. Allah تعالى Anasema:

وَلَا تَقْرَبُوا الزَّوْجَ إِذْهُ<sup>ط</sup> كَانَ فَنَحِشَةً

**“Wala msikaribie uzinzi. Hakika huo ni uchafu.”** Maana: Ni dhambi kubwa.

<sup>1</sup> Fat’h Al-Baariy 8:13.

وَسَاءَ سَبِيلًا ﴿١٧﴾

**“Na ni njia mbaya.”** Maana: Ni njia mbaya sana kwa mtu kuifuata.

Imepokewa na Imaam Ahmad kutoka kwa Abi Umamah رضي الله عنه kuwa alikuja kwa Mtume ﷺ kijana mmoja, akamuambia: “Ewe Mtume wa Allah! Nipe ruhusa nikazini”. Watu walimjia na kumzunguka huku wanamkemea, na kumuambia, ‘We, funga mdomo wako!’ Wengine wakisema; ‘Shika adabu yako.” Mtume ﷺ akasema:

«أَذُنُهُ»

**“Mleteni karibu yangu.”** Yule kijana akaja karibu naye, akamuambia:

«الْخِلْسِ»

**“Kaa chini.”** Naye akakaa. Mtume ﷺ akasema :

«أَتُجِبُّهُ لِأُمِّكَ»

**“Je, utapendelea zinaa hiyo ifanywe kwa mama yako?”** Akajibu: “Hapana. Naapa kwa Allah تعالى Aliepushe mbali jambo hilo.” Mtume ﷺ akamuambia;

«وَلَا النَّاسُ يُجِيبُونَ لِأُمَّهَاتِهِمْ»

**“Wala watu hawapendelei wafanyiwe kwa mama zao.”** Mtume ﷺ akamuuliza:

«أَفَتُجِبُّهُ لِابْنَتِكَ؟»

**“Je, utapendelea zinaa hiyo ifanywe kwa binti yako?”** Akasema: “Hapana. Naapa kwa Allah تعالى Aliepushe mbali jambo hilo”. Mtume ﷺ akamuambia;

«وَلَا النَّاسُ يُجِيبُونَ لِبَنَاتِهِمْ»

**“Wala watu hawapendelei wafanyiwe kwa binti zao.”** Mtume ﷺ akamuuliza:

«أَفَتُجِبُّهُ لِأَخِيكَ؟»

**“Je, utapendelea zinaa hiyo ifanywe kwa dadako?”** Akasema: “Hapana. Naapa kwa Allah تعالى Aliepushe mbali jambo hilo”. Mtume ﷺ akamuambia;

«وَلَا النَّاسُ يُجِيبُونَ لِأَخْوَاتِهِمْ»

**“Wala watu hawapendelei wafanyiwe kwa dada zao.”** Mtume ﷺ akamuuliza:

«أَفْتَجِبُ لِعَمَّتِكَ؟»

“Je, utapendelea zinaa hiyo ifanywe kwa shangazi yako?” Akajibu: “Hapana. Naapa kwa Allah تعالی Aliepushe mbali jambo hilo”. Mtume ﷺ akamuambia;

«وَلَا النَّاسُ يُجْبُونَهُ لِعَمَاتِهِمْ»

“Wala watu hawapendelei wafanyiwe kwa mashangazi wao.” Mtume ﷺ akamuuliza:

«أَفْتَجِبُ لِيَخَالَتِكَ؟»

“Je, utapendelea zinaa ifanywe kwa halati (dadake mama) yako?” Akasema: “Kwa Allah تعالی hapana. Allah تعالی Anijaalie kujitolea fidia kwako”. Mtume ﷺ akamuambia:

«وَلَا النَّاسُ يُجْبُونَهُ لِعَمَاتِهِمْ»

“Wala watu hawapendelei zinaa ifanywe kwa halati zao”. Kisha Mtume ﷺ akamuekea mkono juu yake, akasema:

«اللَّهُمَّ اغْفِرْ ذَنْبَهُ، وَطَهِّرْ قَلْبَهُ، وَأَحْصِنْ فَرْجَهُ»

“Ewe Allah! Msamehe madhambi yake, Usafishe moyo wake na Uhifadhi tupu yake”. Akasema: “Hakuwa kijana huyo akitizama chochote baada ya hapo.”<sup>1</sup>.

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Ahmad 5: 256.



وَلَا تَقْتُلُوا النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ ۗ وَمَنْ قُتِلَ  
 مَظْلُومًا فَقَدْ جَعَلْنَا لَوْلِيَيْهِ سُلْطٰنًا فَلَا يُسْرِفُ فِي الْقَتْلِ ۗ  
 إِنَّهُ كَانَ مَنصُورًا ﴿٣٣﴾ وَلَا تَقْرَبُوا مَالَ الْيَتِيمِ إِلَّا بِالَّتِي  
 هِيَ أَحْسَنُ حَتَّىٰ يَبْلُغَ أَشُدَّهُ ۗ وَأَوْفُوا بِالْعَهْدِ ۗ إِنَّ الْعَهْدَ  
 كَاتِبٌ مُّسْتَوْفٍ ﴿٣٤﴾ وَأَوْفُوا الْكَيْلَ إِذَا كِلْتُمْ وَزِنْتُمْ  
 بِالْقِسْطَاسِ الْمُسْتَقِيمِ ۗ ذَلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٣٥﴾  
 وَلَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ ۗ إِنَّ السَّمْعَ وَالْبَصَرَ  
 وَالْأَفْئَادَ كُلُّ أُولَٰئِكَ كَانَ عَنْهُ مَسْئُولًا ﴿٣٦﴾ وَلَا تَمْشِ فِي  
 الْأَرْضِ مَرَحًا ۗ إِنَّكَ لَنْ تَخْرِقَ الْأَرْضَ وَلَا تَتَّبِعَ الْجِبَالَ  
 طُولًا ﴿٣٧﴾ كُلُّ ذَلِكَ كَانَ سَيِّئُهُمْ عِنْدَ رَبِّكَ مَكْرُوهًا ﴿٣٨﴾  
 ذَلِكَ بِمَا أَوْحَىٰ إِلَيْكَ رَبُّكَ مِنَ الْحِكْمَةِ ۗ وَلَا تَجْعَلْ مَعَ  
 اللَّهِ إِلَهًا ءَاخَرَ فَتَلْقَىٰ فِي جَهَنَّمَ مَلُومًا مَّدْحُورًا ﴿٣٩﴾  
 أَفَأَصْفِنَاكُمْ رَبُّكُم بِالْيَتِيمِ وَأَنْتُمْ مِنَ الْمَلَائِكَةِ إِنْتُمْ أَنْتُمْ  
 لَتَقُولُونَ قَوْلًا عَظِيمًا ﴿٤٠﴾ وَلَقَدْ صَرَّفْنَا فِي هٰذَا الْقُرْءَانِ  
 لِيَذْكُرُوا وَمَا يَزِيدُهُمْ إِلَّا نُفُورًا ﴿٤١﴾ قُلْ لَوْ كَانَ مَعَهُ  
 ءَاهَةٌ كَمَا يَقُولُونَ إِذًا لَّابْتَعَوْا إِلَىٰ ذِي الْعَرْشِ سَبِيلًا ﴿٤٢﴾  
 سُبْحٰنَهُ وَتَعَالَىٰ عَمَّا يَقُولُونَ عُلُوًّا كَبِيرًا ﴿٤٣﴾ تَسْبِيحٌ لَهُ  
 السَّمَوٰتُ السَّبْعُ وَالْأَرْضُ وَمَنْ فِيهِنَّ ۗ وَإِنْ مِنْ شَيْءٍ إِلَّا  
 يُسَبِّحُ بِحَمْدِهِ وَلٰكِن لَّا تَفْقَهُونَ تَسْبِيحَهُمْ ۗ إِنَّهُ كَانَ  
 حَلِيمًا غَفُورًا ﴿٤٤﴾

وَلَا تَقْتُلُوا النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا  
 بِالْحَقِّ ۗ وَمَنْ قُتِلَ مَظْلُومًا فَقَدْ  
 جَعَلْنَا لَوْلِيَيْهِ سُلْطٰنًا فَلَا يُسْرِفُ  
 فِي الْقَتْلِ ۗ إِنَّهُ كَانَ مَنصُورًا ﴿٣٣﴾

**33. Wala msiue nafsi  
 ambayo Allah Amekataza  
 isipokuwa kwa haki. Na  
 aliyeuliwa kwa kudhu-  
 lumiwa basi Tumempa  
 madaraka mrithi wake.  
 Lakini asipite mpaka katika  
 kuua. Kwani yeye anasa-  
 idiwa.**

**Katazo la Kuua Nafsi pasi  
 na Haki**

Allah تعالیٰ Anatakaza kuuliwa  
 nafsi yeyote pasi na haki ya  
 Kisheria, kama ilivyothibiti  
 Hadithi katika Sahihi mbili  
 kuwa Mtume ﷺ amesema:

«لَا يَحِلُّ دَمُ امْرِئٍ مُّسْلِمٍ بِشَهْدِ  
 أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ مُحَمَّدًا  
 رَسُولُ اللَّهِ، إِلَّا بِأَحَدِي ثَلَاثٍ:  
 النَّفْسُ بِالنَّفْسِ، وَالزَّانِي  
 الْمُحْضَرُّ، وَالتَّارِكُ لِذِيهِ  
 الْمَفَارِقِ لِلْجَمَاعَةِ»

*“Si halali damu ya mtu Muislamu anayeshuhudia kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah na kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah ila kwa moja kati ya mambo matatu: Nafsi kwa nafsi (yaani katika mauaji); mzinifu aliyeo (au kuolewa); na mwenye kuacha Dini yake na kutengana na Jama’ah.”<sup>1</sup>*

Na katika Sunan:

لَرَوَّالِ الدُّنْيَا عِنْدَ اللَّهِ أَهْوَنُ مِنْ قَتْلِ مُسْلِمٍ

*“Kuondoshwa (kuhilikishwa) kwa dunia mbele ya Allaah ni sahali zaidi kuliko kumuua Muislamu”<sup>2</sup>.*

Na Kauli Yake تعالی:

وَمَنْ قُتِلَ مَظْلُومًا فَقَدْ جَعَلْنَا لَوْلِيهِ سُلْطٰنًا

***“Na aliye uliwa kwa kudhulumiwa basi Tumempa madaraka mrithi wake.”***

Maana yake: Mamlaka juu ya aliyeua. Mrithi ana uchaguzi; akitaka, anaweza kuamuru naye pia auliwe kwa kisasi, au anaweza kumsamehe kwa kulipwa *Diyah* (fidia kwa damu iliyomwagwa), au anaweza kumsamehe bila malipo yoyote, kama ilivyonyukuliwa katika Sunna. Imamu na Mweledi na Mbobezi Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما, amefahamu maana ya kijumla ya Aya hii tukufu kuwa Mu’awiyah رضي الله عنه, achukue hatamu za uongozi, kwa sababu alikuwa mrithi wa ‘Uthmaan رضي الله عنه, aliyeuliwa kwa dhuluma. Hata hivyo, baadaye Mu’awiyah رضي الله عنه, alichukua hatamu za uongozi na mamlaka, kama alivyosema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما, kwa msingi wa Aya hii tukufu. Na hili ni katika jambo la ajabu na kushangaza.

Na Kauli Yake تعالی:

فَلَا يُسْرَفُ فِي الْقَتْلِ

***“Lakini asipite mpaka katika kuua”.***

<sup>1</sup> Fat’h al-Baariy 12:209 na Muslim 3:1302.

<sup>2</sup> Tuhfatul Al-Ahwadhiy 4:256, An-Nasaa’iy 7:82 na Ibn Maajah 2:874

Wamesema: “Maana yake ni kuwa mrithi asipitishie mpaka katika kumuua aliyeya, kama kumkatakata (kuukatakata mwili wa muuaji), au kuchukua kisasi kwa mtu mwingine asiyekuwa muuaji”. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

إِنَّهٗ كَانَ مَنصُورًا ﴿٣٣﴾

**“Kwani yeye anasaidiwa.”**

Maana yake: Mrithi anasaidiwa dhidi ya muuaji Kisheria na kwa Kudura.

وَلَا تَقْرُبُوا مَالَ الْيَتِيمِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ حَتَّىٰ يَبْلُغَ أَشُدَّهُ ۗ وَأَوْفُوا بِالْعَهْدِ ۗ إِنَّ الْعَهْدَ  
كَانَ مَسْئُولًا ﴿٣٤﴾ وَأَوْفُوا الْكَيْلَ إِذَا كِلْتُمْ وَزَنُوا بِالْقِسْطَاسِ الْمُسْتَقِيمِ ۗ ذَٰلِكَ خَيْرٌ  
وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٣٥﴾

**34. Wala msiikaribie mali ya yatima, isipokuwa kwa njia iliyo bora, mpaka afike balebhe yake. Na timizeni ahadi. Kwa hakika ahadi itaulizwa.**

**35. Na timizeni kipimo mpimapo. Na pimeni kwa mizani zilizo sawa. Hayo ni wema kwenu na hatimaye ndio bora.**

**Amri ya Kuitumia Vizuri Mali ya Yatima, Kutimiza Kipimo na Mizani**

Allah تعالى Anasema,

وَلَا تَقْرُبُوا مَالَ الْيَتِيمِ إِلَّا بِالَّتِي هِيَ أَحْسَنُ حَتَّىٰ يَبْلُغَ أَشُدَّهُ ۗ

**“Wala msiikaribie mali ya yatima, isipokuwa kwa njia iliyo bora, mpaka afike balebhe yake.”**

Maana: Usiitumie mali ya yatima isipokuwa kwa njia iliyo nzuri na bora. Pia,

وَلَا تَأْكُلُوهُمَا إِسْرَافًا وَبِدَارًا أَن يَكْبَرُوا ۗ وَمَن كَانَ غَنِيًّا فَلْيَسْتَعْفِفْ ۗ وَمَن كَانَ فَقِيرًا فَلْيَأْكُلْ  
بِالْمَعْرُوفِ ۗ

**“Wala usiile (mali ya mayatima) kwa ubadhirifu (israfu) na haraka ukichelea kukua kwao. Na yeyote miongoni mwa walezi aliye**

***tajiri, basi ahafifishe (asichukue ada yoyote) na ambaye ni fakiri, basi ale kwa wema na uadilifu (kulingana na kazi yake)."*** (4:6)

Imepokewa katika Sahihi Muslim kuwa Mtume ﷺ alimuambia Abi Dharr رضي الله عنه:

«يَا أَبَا ذَرٍّ إِنِّي أَرَاكَ ضَعِيفًا، وَإِنِّي أَحِبُّ لَكَ مَا أَحَبُّ لِنَفْسِي: لَا تَأْمُرَنَّ عَلَيَّ اثْنَيْنِ، وَلَا تَوَلِّبَنَّ مَالَ النَّبِيِّ»

*"Ewe Abu Dharr! Hakika nakuona wewe ni dhaifu, nami nakupendelea kama ninavyojipendelea nafsi yangu. Usiache kuchaguliwa Amiri (kiongozi) juu ya watu wawili wala usikubali mamlaka ya kutunza mali ya mayatima."*

Na Kauli Yake تعالى:

وَأَوْفُوا بِالْعَهْدِ

***"Na timizeni ahadi."***

Maana yake: Zile mnazoahidiana na watu na ahadi mnazokubali, sababu ni kuwa yeyote mwenye ahadi au mapatano atasailiwa juu yake. Anasema hayo Allah تعالى:

إِنَّ الْعَهْدَ كَانَ مَسْئُولًا

***"Kwa hakika ahadi itaulizwa."*** Maana: Juu yake.

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَأَوْفُوا الْكَيْلَ إِذَا كِلْتُمْ

***"Na timizeni kipimo mpimapo."***

Maana yake: Usijaribu kupunguza wala kuwapunja watu vitu vyao wenyewe.

وَزِنُوا بِالْقِسْطَاسِ

***"Na pimeni kwa Qistwaas."*** Inasomwa kwa Qaaf ikiwa na dhumma au kasra, nayo ni mizani. Na Kauli Yake Allah تعالى:

<sup>1</sup> Muslim 3:1458.

الْمُسْتَقِيمِ

**“Zilizo sawa”.**

Kumaanisha isiyo na udanganyifu wala kughushi (kuleta tatizo).

ذَلِكَ خَيْرٌ

**“Hayo ni wema.”**

Maana yake: Kwenu nyinyi katika maisha yenu ya kila siku na Akhera (mashukio) yenu. Hivyo, Akasema Allah تعالى:

وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا

**“Na hatimaye ndio bora.”**

Maana yake: Kwa mujibu wa mwisho wenu huko Akhera.

Amesema Said kutoka kwa Qataadah:

ذَلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا

**“Hayo ni wema kwenu na hatimaye ndio bora.”**

Maana yake: Kheri na bora katika thawabu na mwisho mwema<sup>1</sup>.

Na Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما alikuwa akisema: “Enyi watu! Mmepatiwa amana kwa vitu viwili ambavyo kwayo walihiliki waliokuwa kabla yenu – hiki kipimo cha ujazo na hii mizani.”<sup>2</sup>

وَلَا تَقْفُ مَا لَيْسَ لَكَ بِهِ عِلْمٌ إِنَّ السَّمْعَ وَالْبَصَرَ وَالْفُؤَادَ كُلُّ أُولَئِكَ كَانَ عَنْهُ

مَسْئُولًا

**36. Wala usiyafuate usiyo na ujuzi nayo. Hakika masikio, na macho, na moyo - hivyo vyote vitasailiwa.**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:446.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:446.

## Usizungumze bila Elimu

'Aliy bin Abi Twalhah amesema kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما aliyemsikia akisema: "Usiseme (chochote usichokuwa na elimu nacho)."<sup>1</sup> Na Al-Awfiy amesema: "Usimtuhumu yeyote kwa usilokuwa na elimu nalo."<sup>2</sup> Na amesema Muhammad Al-Hanafiyah: "Hiyo inamaanisha ushahidi wa uwongo."<sup>3</sup> Na Qataadah amesema: "Usiseme: 'Nimeona', wakati ambapo hujaona chochote, au 'Nimesikia', kumbe hujasikia lolote. Au kusema, 'Najua', ilhali hujui, kwani Allah تعالى Atakuuliza yote hayo."<sup>4</sup> Na muktadha wa yote hayo waliyoyataja ni kuwa Allah تعالى Amekataza kauli bila elimu kwani kufanya hivyo ni kujenga dhana, ambayo ni chanzo cha kutuhumu. Hayo ni kwa mujibu wa Kauli ya Allah تعالى:

أَجْتَنِبُوا كَثِيرًا مِّنَ الظَّنِّ إِنَّ بَعْضَ الظَّنِّ إِتْرٌ

**"Jiepusheni sana na dhana, bila shaka baadhi ya dhana ni madhambi." (49:12).** Na katika Hadithi:

«إِيَّاكُمْ وَالظَّنَّ فَإِنَّ الظَّنَّ أَكْذَبُ الْحَدِيثِ»

"Tahadharini sana na dhana, kwani dhana ni uwongo mbaya sana katika mazungumzo"<sup>5</sup>.

Na katika Sunan Abi Daawuud:

«بِئْسَ مَطِيئَةُ الرَّجُلِ: زَعَمُوا»

"Ni tabia mbaya sana kwa mtu kusema: wanadai."<sup>6</sup>

Na kulingana na Hadithi nyingine:

«إِنَّ أَقْرَى الْفِرَى أَنْ يُرَى الرَّجُلُ عَيْنَيْهِ مَا لَمْ تَرَيَا»

"Hakika uwongo ulio mbaya zaidi ni kwa mtu kudai ameona kitu ilhali hajaona."<sup>7</sup>

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Baariy 12:446.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:447.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:447.

<sup>4</sup> At-Tabari 17:446.

<sup>5</sup> Fat'hul Al-Baariy 9:106.

<sup>6</sup> Abu Daawuud 5:254.

<sup>7</sup> Fat'hulul Al-Baariy 12:446.

Na katika Sahihi:

«مَنْ تَحَلَّمَ حُلْمًا كُفِّفَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَنْ يَغْقَدَ بَيْنَ شَعِيرَتَيْنِ وَلَيْسَ بِفَاعِلٍ»

“Yeyote anayedai kuwa ameota (ilhali hakuota) ataambiwa Siku ya Kiyama kupiga fundo baina ya mbegu mbili za shayiri wala hataweza kufanya hilo”<sup>1</sup>.

Na Kauli Yake تعالى:

كُلُّ أَوْلِيَاكَ

“**Vyote hivyo.**” Maana yake: Sifa zote hizi, masikio, macho na moyo:

كَانَ عَنْهُ مَسْغُولًا

“**Vitasaliwa.**” Maana yake: Mja ataulizwa kuvihusu Siku ya Kiyama, na pia vitaulizwa kumhusu na alivitumia kwa njia gani.

وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا إِنَّكَ لَنْ تَخْرِقَ الْأَرْضَ وَلَنْ تَبْلُغَ الْجِبَالَ طُولًا ﴿٣٧﴾ كُلُّ

ذَلِكَ كَانَ سِيفُهُ عِنْدَ رَبِّكَ مَكْرُوهًا ﴿٣٨﴾

**37. Wala usitembee katika ardhi kwa maringo. Hakika wewe huwezi kuipasua ardhi wala kufikia urefu wa milima.**

**38. Haya yote ubaya wake ni wenye kuchukiza kwa Mola wako Mlezi.**

### Karipio la Kutembea kwa Maringo

Allah تعالى Amewakataza waja Wake kwenda kwa kutakabari na kutembea kwa maringo na kiburi. Allah تعالى Anasema :

وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا

“**Wala usitembee katika ardhi kwa maringo.**”

Maana yake: Kutembea kwa maringo na kiburi kama ulivyokuwa mwendo wa majabari wenye kiburi waliochupa mipaka. Hakika ni kuwa,

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Bari 12:1446

إِنَّكَ لَن تَخْرِقَ الْأَرْضَ

**“Wewe huwezi kuipasua ardhi.”** Inamaanisha kuwa huwezi kuipenya ardhi kwa matembezi yako. Hii ni rai ya Ibn Jariir رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى. Na Kauli Yake Allah تعالی:

وَلَنْ تَبْلُغَ الْجِبَالَ طُولًا ﴿١٧﴾

**“Wala kufikia urefu wa milima.”** Maana yake: Kwa kiburi, majivuno na kujiona kwako. Bila shaka, tabia hizo huenda zikaleta kinyume na mtazamo wa mwenye hulka hiyo. Kama ilivyonukuliwa katika Sahihi:

«بَيْنَمَا رَجُلٌ يَمْشِي فَمِنْ كَانَ قَبْلَكُمْ وَعَلَيْهِ بُرْدَانٌ يَتَخَرَّضُ فِيهِمَا، إِذْ خُفِيَ بِهِ الْأَرْضَ فَهُوَ يَتَجَلَّجَلُ فِيهَا إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ»

*“Wakati ambapo mtu mmoja aliyekuwa kabla yenu akitembea kwa maringo akiwa amevaa nguo, mara akamezwa na ardhi na bado anazama chini mpaka Siku ya Qiyama”<sup>1</sup>.*

Pia Allah تعالی Anatueleza kuhusu Qaarun, aliyetoka kwa watu wake akiwa na mapambo yake na hakika Allah تعالی Alimzamisha ardhini pamoja na nyumba yake. Na Kauli Yake Allah تعالی:

كُلُّ ذَلِكْ كَانَ سَيِّئُهُ عِنْدَ رَبِّكَ مَكْرُوهًا ﴿١٨﴾

**“Haya yote ubaya wake ni wenye kuchukiza kwa Mola wako Mlezi.”**

Ama kwa yule anayesoma: *“Sayyi’atan”* badala ya *“Sayyi’uhu”*, hilo neno la awali linamaanisha uchafu (matendo mabaya), maana yake ni kila jambo ambalo Tumelikataza (kila Tuliyojataja) kuanzia kwa Kauli Yake:

وَلَا تَقْتُلُوا أَوْلَادَكُمْ خَشْيَةَ إِمْلَاقٍ ۗ

**“Wala msiwaue wana wenu kwa kuogopa umasikini.” (17:31)**

Mpaka Aya hii ya 38. Hivyo, kila kilichotajwa hapa ni *Sayyi’ah* (matendo mabaya) huadhibiwa mtu kwa kutenda mambo hayo, na yanachukiza mbele ya Allah تعالی Hayapendi wala Hayaridhii.

<sup>1</sup> Muslim 3:1654.



Na ama kwa wale wenye kusoma: "Sayyi'uhu", Maana yake kwao, ni yote haya tuliyojataja kuanzia kwa Kauli Yake Allah تعالى:

﴿ وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ ﴾

**"Na Mola wako Mlezi Ameamrisha kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu." (17:23)**

Hadi aya hii (17:38). Maana yake: mabaya yote hayo yanachukiza mbele ya Allah تعالى. Hii ndiyo iliyokuwa rai ya Ibn Jariir رحمه الله تعالى.

ذَٰلِكَ مِمَّا أَوْحَىٰ إِلَيْكَ رَبُّكَ مِنَ الْحِكْمَةِ ۗ وَلَا تَجْعَلْ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا ءَاخَرَ فَتَلْقَىٰ فِي جَهَنَّمَ

مَلُومًا مَّدْحُورًا ﴿٣٨﴾

**39. Haya ni katika hekima alizokufunulia Mola wako Mlezi. Wala usimuweke pamoja na Allah mola mwengine, usije ukatupwa katika Jahanamu ukilaumiwa na kufurushwa.**

### Yote Yaliyopita ni Wahyi na Hekima

Allah تعالى Anasema: "Tuliyokuamrisha Kuyafanya ni maadili mema na Tuliyokukataza ni tabia mbaya. Tumekuteremshia, ewe Muhammad ﷺ, ili uweze kuwaamrisha watu hivyo". Allah تعالى Anasema:

﴿ وَلَا تَجْعَلْ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا ءَاخَرَ فَتَلْقَىٰ فِي جَهَنَّمَ مَلُومًا ﴾

**"Wala usimuweke pamoja na Allah mola mwengine, usije ukatupwa katika Jahanamu ukilaumiwa."**

Kumaanisha nafsi yako mwenyewe itakulaumu, Allah تعالى na viumbe Vyake. Ukiwa ni mwenye:

﴿ مَدْحُورًا ﴾ ﴿٣٩﴾

**"Kufurushwa."** Ina maana kuondoshewa vitu vyote vizuri. Ibn 'Abbaas na Qataadah wanasema: "(Ina maana) kutupwa nje"<sup>1</sup>.

Wanaosemeshwa katika Aya hii ni Umma wote kupitia kwa Mtume ﷺ, ambaye amelindwa na madhambi.

<sup>1</sup> At-Tabari 17:452.

أَفَأَصْفَنكُمْ رَبُّكُمْ بِالْبَيْنِ وَأَتَّخَذَ مِنَ الْمَلَائِكَةِ إِنْتًا ۗ إِنَّكُمْ لَتَقُولُونَ قَوْلًا عَظِيمًا ﴿٣٩﴾

**40. Je! Mola wenu Mlezi Amekuteulieni wavulana, na Yeye Akawafanya Malaika ni banati zake? Kwa hakika nyinyi mnasema usemi mkubwa.**

**Kukanushwa kwa Wanaodai kuwa Malaika ni Mabinti wa Allah** تعالی

Allah تعالی Anakanusha uwongo wa washirikina wanaodai, laana ya Allah تعالی iwe juu yao, kuwa Malaika ni mabinti wa Allah تعالی. Waliwafanya Malaika, ambao ni waja wa (Ar-Rahmaan) Allah تعالی, wanawake, na kuwaita wao kuwa ni mabinti wa Allah تعالی, kisha wakawaabudu wao. Walikosea sana katika sehemu zote tatu. Allah تعالی Anasema kupinga uzushi wao huo:

أَفَأَصْفَنكُمْ رَبُّكُمْ بِالْبَيْنِ

**“Je, Mola wenu Mlezi Amekuteulieni wavulana.”**

Kumaanisha kuwa je, Amewapatia wanaume nyinyi peke yenu.

وَأَتَّخَذَ مِنَ الْمَلَائِكَةِ إِنْتًا

**“Na Yeye Akawafanya Malaika ni mabinti zao.”**

Hiyo ni kumaanisha kuwa Yeye Amejichagulia, kama mnavyodai, wasichana? “Kwa hakika nyinyi mnasema usemi mkubwa”.

Kisha Allah تعالی Anawakana vikali sana, kwa Kusema:

إِنَّكُمْ لَتَقُولُونَ قَوْلًا عَظِيمًا ﴿٤٠﴾

**“Kwa hakika nyinyi mnasema usemi mkubwa”.**

Hii inamaanisha katika madai yenu ya kuwa Allah تعالی Alikuwa na watoto, kisha mnasema kuwa watoto Wake ni wasichana, ambao hamuwataki na hata huwaua kwa kuwazika wakiwa hai. Hakika huo ni mgao usio na uadilifu hata kidogo.

Allah تعالی Anasema:

وَقَالُوا اتَّخَذَ الرَّحْمَنُ وَلَدًا ﴿٣٣﴾ لَقَدْ جِئْتُمْ شَيْئًا إِدًّا ﴿٣٤﴾ تَكَادُ السَّمَوَاتُ يَتَفَطَّرْنَ  
 مِنْهُ وَتَنْشَقُّ الْأَرْضُ وَتَخِرُّ الْجِبَالُ هَدًّا ﴿٣٥﴾ أَنْ دَعَوْا لِلرَّحْمَنِ وَلَدًا ﴿٣٦﴾ وَمَا يَلْبِغِي  
 لِلرَّحْمَنِ أَنْ يَتَّخِذَ وَلَدًا ﴿٣٧﴾ إِنْ كُلُّ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ إِلَّا آتَى الرَّحْمَنِ  
 عَبْدًا ﴿٣٨﴾ لَقَدْ أَحْصَاهُمْ وَعَدَّهُمْ عَدًّا ﴿٣٩﴾ وَكُلُّهُمْ آتِيهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَرْدًا ﴿٤٠﴾

*“...Na makafiri husema: ‘Allah Mwingi wa Rehema Amejifanyia mtoto’. Bila shaka mmeleta jambo lichukizalo kabisa (kwa kusema hivyo). Zinakaribia mbingu kutatuka kwa tamko hilo na ardhi kupasuka na milima kuanguka ikatika vipande vipande. Kwa kule kudai kuwa Allah Mwingi wa Rehema Ana mtoto. Wala Haiwi kwa Allah Mwingi wa Rehema kuwa na mtoto. Hakuna yeyote aliyomo mbinguni na ardhini ila atafika kwa Allah, Mwingi wa Rehema hali ya kuwa ni mtumwa Wake. Amewadhibiti na Amewahesabu sawa sawa. Na kila mmoja katika wao atamjia Allah siku ya Kiyama peke Yake” (19:88-95).*

وَلَقَدْ صَرَّفْنَا فِي هَذَا الْقُرْآنِ لِيَذَكَّرُوا وَمَا يَزِيدُهُمْ إِلَّا نُفُورًا ﴿٤١﴾

**41. Na Tumekwisha bainisha katika Qur’ani hii ili wapate kukumbuka. Lakini haikuwazidisha ila kuwa mbali nayo.**

Allah تعالیٰ Anasema:

وَلَقَدْ صَرَّفْنَا فِي هَذَا الْقُرْآنِ

**“Na Tumekwisha bainisha katika Qur’ani.”**

Maana yake: Tumebainisha ndani yake adhabu Zetu ili wapate kukumbuka dalili zilizomo, bayana na mawaidha, hivyo kuacha ushirikina, udhalimu, uwongo na uzushi.

وَمَا يَزِيدُهُمْ

**“Lakini haikuwazidishia.”**

Maana yake: Madhalimu miongoni mwao,

إِلَّا نُفُورًا ﴿١٧﴾

**“ila kuwa mbali nayo.”**

Hiyo ina maana kukengeuka na ukweli, hivyo kwenda mbali zaidi nayo (yaani Qur’ani).

قُلْ لَوْ كَانَ مَعَهُ إِهْلَةٌ كَمَا يَقُولُونَ إِذَا لَأَبْتَغُوا إِلَيَّ ذِي الْعَرْشِ سَبِيلًا ﴿١٧﴾ سُبْحٰنَهُ  
وَتَعَالَىٰ عَمَّا يَقُولُونَ عُلُوًّا كَبِيرًا ﴿١٨﴾

**42. Sema: Lau kuwa wangelikuwa pamoja Naye miungu mingine kama wasemavyo, basi wangelitafuta njia ya kumfikia Mwenye Kiti cha Enzi.**

**43. Subhaanahu wa Ta’ala, Ametakasika na Ametukuka juu kabisa na hayo wasemayo, kwa uepukano mkubwa kabisa.**

Allah تعالیٰ Anasema: “Sema: Ewe Muhammad ﷺ, kuwaambia washirikina wanaodai kuwa Allah تعالیٰ Ana mshirika miongoni mwa viumbe Vyake, na wanaoabudu asiyekuwa Yeye kuwakurubisha Kwake. Lau hilo lingekuwa kama wanavyosema na kuwa wao wana mungu wanaemuabudu ili awakuribishe Kwake na kuwaombea mbele yake, basi wangemuabudu Yeye wenye kuabudiwa na wangetaka wasila na kujikurubisha. Basi muabuduni Yeye Peke Yake kama wanavyomuabudu munaowaabudu asiyekuwa Yeye. Wala hamuhitajii muabudiwa atakayekuwa baina yenu na Yeye, kwani Yeye Hapendi hilo wala Halimridhishi. Bali Anachukia na Kulikataa hilo. Naye Amekataza hilo kwa ulimi wa Manabii na Mitume Wake wote”. Kisha Akajitakasa na Kujitukuza mbali na hayo yote, Akasema:

سُبْحٰنَهُ وَتَعَالَىٰ عَمَّا يَقُولُونَ

**“Ametakasika na Ametukuka juu kabisa na hayo wasemayo.”**

Maana yake: Hawa washirikina madhalimu waliokiuka mipaka wanaodai kuwa wapo miungu mingine mbali na Yeye.

عُلُوًّا كَبِيرًا ﴿١٨﴾

**“Kwa uepukano mkubwa kabisa.”**

Maana yake: Juu kabisa. Bali Allah تعالى, ni Mmoja, Anayestahiki Kukusudiwa, Ambaye viumbe wote wanamuhitajia. Hakuzaa wala Hakuzaliwa wala Hana Anayefanana Naye hata mmoja.

تُسَبِّحُ لَهُ السَّمَوَاتُ السَّبْعُ وَالْأَرْضُ وَمَنْ فِيهِنَّ وَإِنْ مِنْ شَيْءٍ إِلَّا يُسَبِّحُ بِحَمْدِهِ وَلَكِنْ لَا تَفْقَهُونَ تَسْبِيحَهُمْ إِنَّهُ كَانَ حَلِيمًا غَفُورًا ﴿٣٤﴾

**44. Zinamtakasa mbingu zote saba na ardhi na vyote viliomo ndani yake. Na hapana kitu ila kinamtakasa kwa sifa Zake. Lakini nyinyi hamfahamu kutakasa Kwake. Hakika Yeye ni Mpole na Mwenye Maghufira.**

**Kila Kitu Kinamsabihi na Kumtakasa Allah تعالى**

Allah تعالى Anasema: Mbingu saba na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake, kumaanisha viumbe wote wanaoishi humo, vinamtakasa, kumsifu, kumtukuza na kumuadhimisha mbali na yote wanayosema washirikina. Wanashuhudia kuwa Yeye Yu peke Yake katika Uungu na Ubwana Wake. Katika kila kitu kuna ishara, Yenye kuonesha kuwa Yeye ni Mmoja. Kama Alivyosema تعالى:

تَكَادُ السَّمَوَاتُ يَتَفَطَّرْنَ مِنْهُ وَتَنْشَقُّ الْأَرْضُ وَتَخِرُّ الْجِبَالُ هَدًا ﴿٩٠﴾ أَنْ دَعَوْا لِلرَّحْمَنِ  
وَلَدًا ﴿٩١﴾

**“Zinakaribia mbingu kutatuka kwa tamko hilo na ardhi kupasuka na milima kuanguka ikatika vipande vipande. Kwa kule kudai kuwa Allah Mwingi wa Rehema Ana mtoto.” (19:90-91).**

Na Kauli Yake تعالى:

وَإِنْ مِنْ شَيْءٍ إِلَّا يُسَبِّحُ بِحَمْدِهِ

**“Na hapana kitu ila kinamtakasa kwa Sifa Zake.”**

Maana yake: Hakuna katika viumbe ila vinamtakasa kwa kumsifu Allah تعالى.

وَلَكِنْ لَا تَفْقَهُونَ تَسْبِيحَهُمْ

**“Lakini nyinyi hamfahamu kutakasa Kwake.”**

Maana yake: Nyinyi wanadamu hamfahamu jinsi vinavyomsabihi, kwa sababu lugha zao ni tofauti na zenu. Hii inajumlisha viumbe vyote kwa ujumla, hayawani (wanyama), viumbe visivyoyana uhai na mimea. Hii ndio kauli mashuhuri katika rai mbili zinazojulikana kama ilivyothibiti katika Sahihi Al-Bukhaari kutoka kwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه aliyesema: "Tulikuwa tunasikia tasbihi za chakula nacho kinaliwa."<sup>1</sup>

Imepokewa na Imaam Ahmad kutoka kwa Mu'adh bin Anas رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ aliingia kwa watu ambao baadhi yao walikuwa wameketi kwenye vipando vyao wakiwa wanazungumza. Aliwaambia:

«ارْكَبُوهَا سَالِمَةً وَدَعُوهَا سَالِمَةً، وَلَا تَتَّخِذُوهَا كَرَاسِيٍّ لِأَحَادِيثِكُمْ فِي الطَّرْفِ  
وَالْأَسْوَابِ، فَرُبَّ مَرْكُوبَةٍ خَيْرٌ مِنْ رَاكِبِهَا، وَأَكْثَرُ ذِكْرًا لِلَّهِ مِنْهُ»

*"Wapandeni kwa usalama na waacheni kwa salama. Msiwatumie kama viti kwa ajili ya mazungumzo yenu barabarani na masokoni. Huenda akawa mpandwa ni bora kuliko mpandaji, na mwenye kumdhukuru Allah zaidi kuliko yeye."*<sup>2</sup>

An-Nasaa'iy amenukuu katika Sunan yake kuwa 'Abdallah bin 'Amr رضي الله عنهما amesema: Mtume ﷺ alitukataza kuua vyura. Na amesema kukoroma kwa Chura ni Tasbihi.<sup>3</sup> Na Kauli Yake Allah تعالى،

إِنَّهُ كَانَ حَلِيمًا غَفُورًا ﴿١٧﴾

**"Hakika Yeye ni Mpole na Mwenye Maghufira."** Maana: Allah تعالى Hafanyi haraka Kumuadhibu aliyemuasi Yeye, bali anapatiwa muda na kungojewa. Ikiwa ataendelea na ukaidi wa ukafiri wake, Anampatiliza na adhabu kwa Nguvu Zake, Naye Ndiye Muweza. Imenukuliwa katika Sahihi mbili kuwa:

«إِنَّ اللَّهَ لَيَمْلِكُ لِلظَّالِمِ حَتَّىٰ إِذَا أَخَذَهُ لَمَّ يُغْلِبْهُ»

*"Hakika Allah Anamuacha dhalimu mpaka Anapomshika, Hamuachi kabisa."*<sup>4</sup> Kisha Mtume ﷺ akasoma:

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baariy 6:679.

<sup>2</sup> Ahmad 4:439. Isnadi yake ni dhaifu.

<sup>3</sup> An-Nasaa'iy 7:210. Mwandishi ametaja Hadithi isiy sahihi inayosema: "Kukoroma kwa chura ni Tasbihi".

<sup>4</sup> Fat'h Al-Baariy 8:205 na Muslim 4:1997.

وَكَذَلِكَ أَخَذُ رَبِّكَ إِذَا أَحَدَ أَلْفَرَىٰ وَهِيَ ظَالِمَةٌ

**“Na namna hivi ndivyo inavyokuwa kutesa kwa Mola wako Mlezi Anapowatesa (watu wa) miji wanapofanya dhuluma.” (11:102).**

Allah تعالى Anasema:

وَكَايْنٍ مِّن قَرْيَةٍ أَمَلَتْ هَا وَهِيَ ظَالِمَةٌ

**“Na (watu wa) miji mingapi Niliyowapa muda; na hali walikuwa wakidhulumu?” (22:45).**

Na Akasema:

فَكَأَيِّن مِّن قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَاهَا وَهِيَ ظَالِمَةٌ

**“Na miji mingapi Tuliangamiza iliyokuwa ikidhulumu.” (22:48)**

Yeyote mwenye kuacha ukafiri wake na uasi, na kurudi kwa kutubia kwa Allah تعالى, Allah تعالى Ataikubali toba yake, kwani Anasema:

وَمَنْ يَعْمَلْ سُوءًا أَوْ يَظْلِمْ نَفْسَهُ ثُمَّ يَسْتَغْفِرِ اللَّهَ

**“Na mwenye kutenda uovu au akajidhulumu nafsi yake; kisha akaomba msamaha (maghufira) kwa Allah.” (4:110).**

Hapa, Allah تعالى Anasema:

إِنَّهُ كَانَ حَلِيمًا غَفُورًا ﴿١١٠﴾

**“Hakika Yeye ni Mpole na Mwenye maghufira.”**

Kama Alivyosema mwisho wa Suratul Faatwir:

﴿ إِنَّ اللَّهَ يُمَسِّكُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ أَنْ تَزُولَا ۗ وَلَئِن زَالَتَا إِنْ أَمْسَكَهُمَا مِنْ أَحَدٍ مِنْ

بَعْدِهِ ۗ إِنَّهُ كَانَ حَلِيمًا غَفُورًا ﴿١١٠﴾

**“Hakika Allah Ndiye Anayezuilia mbingu na ardhi zisiondoke, na kama zikiondoka hakuna yeyote wa kuzizuia isipokuwa Yeye. Bila shaka, Yeye ni Mpole, Mwingi wa Kusamehe.” (35:41) Mpaka:**

وَلَوْ يُؤَاخِذُ اللَّهُ النَّاسَ

**“Na kama Allah Angaliwatesa watu.” (35:41-45),**

وَإِذَا قَرَأْتَ الْقُرْآنَ جَعَلْنَا بَيْنَكَ وَبَيْنَ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ  
 بِالْآخِرَةِ حِجَابًا مَّسْتُورًا ﴿٤٥﴾ وَجَعَلْنَا عَلَى قُلُوبِهِمْ أَكِنَّةً أَنْ  
 يَفْقَهُوهُ وَفِي آذَانِهِمْ وَقْرًا ۖ وَإِذَا ذَكَرْتَ رَبَّكَ فِي الْقُرْآنِ  
 وَحْدَهُ وَلَوْ عَلَىٰ أَدْبَارِهِمْ نُفُورًا ﴿٤٦﴾ نَحْنُ أَعْلَمُ بِمَا  
 يَسْتَمِعُونَ بِهِ إِذْ يَسْتَمِعُونَ إِلَيْكَ وَإِذْ هُمْ نَجْوَىٰ إِذْ يَقُولُ  
 الظَّالِمُونَ إِنْ تَتَّبِعُونَ إِلَّا رَجُلًا مَّسْحُورًا ﴿٤٧﴾ أَنْظِرْ كَيْفَ  
 صَرَبُوا لَكَ الْأَمْثَالَ فَضَلُّوا فَلَا يَسْتَطِيعُونَ سَبِيلًا ﴿٤٨﴾  
 وَقَالُوا أَإِذَا كُنَّا عِظْمًا وَرُفْنًا أَإِنَّا لَمَبْعُوثُونَ خَلْقًا  
 جَدِيدًا ﴿٤٩﴾ \* قُلْ كُونُوا حِجَارَةً أَوْ حَدِيدًا ﴿٥٠﴾ أَوْ  
 خَلْقًا مِمَّا يَكْبُرُ فِي صُدُورِكُمْ ۖ فَسَيَقُولُونَ مَنْ يُعِيدُنَا ۖ  
 قُلِ الَّذِي فَطَرَكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ ۖ فَسَيُنْغِضُونَ إِلَيْكَ رُءُوسَهُمْ  
 وَيَقُولُونَ مَتَىٰ هُوَ ۖ قُلْ عَسَىٰ أَنْ يَكُونَ قَرِيبًا ﴿٥١﴾  
 يَوْمَ يَدْعُوكُمْ فَتَسْتَجِيبُونَ بِحَمْدِهِ وَتَنْظُرُونَ أَنْ لَبِئْتُمْ  
 إِلَّا قَلِيلًا ﴿٥٢﴾ وَقُلْ لِعِبَادِي يَقُولُوا الَّتِي هِيَ أَحْسَنُ ۚ إِنَّ  
 الشَّيْطَانَ يَنْزِعُ بَيْنَهُمْ ۚ إِنَّ الشَّيْطَانَ كَانَ لِلْإِنْسَانِ عَدُوًّا  
 مُبِينًا ﴿٥٣﴾ رَبُّكُمْ أَعْلَمُ بِكُمْ ۗ إِنْ يَشَأْ يَرْحَمْكُمْ أَوْ إِنْ يَشَأْ  
 يُعَذِّبْكُمْ ۚ وَمَا أَرْسَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ وَكِيلًا ﴿٥٤﴾ وَرَبُّكَ أَعْلَمُ  
 بِمَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ۗ وَلَقَدْ فَضَّلْنَا بَعْضَ النَّبِيِّينَ  
 عَلَىٰ بَعْضٍ ۗ وَءَاتَيْنَا دَاوُدَ زَبُورًا ﴿٥٥﴾

وَإِذَا قَرَأْتَ الْقُرْآنَ جَعَلْنَا بَيْنَكَ وَبَيْنَ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ حِجَابًا مَّسْتُورًا ﴿٤٥﴾ وَجَعَلْنَا عَلَى قُلُوبِهِمْ أَكِنَّةً أَنْ يَفْقَهُوهُ وَفِي آذَانِهِمْ وَقْرًا ۖ وَإِذَا ذَكَرْتَ رَبَّكَ فِي الْقُرْآنِ وَحْدَهُ وَلَوْ عَلَىٰ أَدْبَارِهِمْ نُفُورًا ﴿٤٦﴾

**45. Na unaposoma Qur'ani Tunaweka baina yako na wale wasioiamini Akhera pazia linalowafunika.**

**46. Na Tunaweka vifuniko juu ya nyoyo zao wasije wakaifahamu, na Tunaweka kwenye masikio yao uziwi. Na unapomtaja katika Qur'ani Mola wako Mlezi Peke Yake, basi wao hugeuka nyuma wakenda zao.**

**Pazia kwenye Nyoyo za Washirikina**

Allah تعالى Anamuambia Mtume Wake Muhammad ﷺ: "Unapowasomea Qur'ani washirikina, Tunajaalia baina yao na wewe pazia linalowafinika".



Qatadah na Ibn Zayd wamesema: "Nachol ni kifuniko kwenye mioyo yao"<sup>1</sup>, kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَقَالُوا قُلُوبُنَا فِي أَكِنَّةٍ مِّمَّا تَدْعُونَا إِلَيْهِ وَفِي آذَانِنَا وَقْرٌ وَمِنْ بَيْنِنَا وَبَيْنَكَ حِجَابٌ

**"Na wakasema: 'Nyoyo zetu zi katika vifuniko kwa yale unayotuitia; na katika masikio yetu muna uzito; na baina yetu na yako kuna pazia...' (41:5),**

Maana: Kuna kitu ambacho kinazuia maneno yako kutufikia sisi. Na Kauli Yake:

حِجَابًا مَسْتُورًا ﴿٥٠﴾

**"Pazia linalowafunika."**

Kumaanisha kitu kinachofunika, au kisichoonekana, hivyo kuna kizuizi baina yao na uongofu. Na Ibn Jariir رحمه الله تعالى amependekeza kuwa tafsiri hii ndio iliyo sahihi na yenye nguvu zaidi.

Amepokea Al-Haafidh Abu Yaa'laa al-Mawswliy kutoka kwa Asmaa bint Abubakar رضي الله عنها kuwa amesema: Ilipoteremka:

تَبَّتْ يَدَا أَبِي لَهَبٍ وَتَبَّ ﴿١١١﴾

**"Kuangamia mikono miwili ya Abu Lahab, naye amekwisha angamia." (111:1),**

Alikuja mwanamke chongo, Ummu Jamiil (mke wa Abu Lahab) akiwa na jiwe mkononi mwake, akipiga kelele: "Aliyetumwa kwetu ni mtu wa kulaumiwa, au tunamkataa mtu anayelaumiwa (Abu Musa – mmoja miongoni mwa wapokezi wa Hadithi – alisema, ni mimi ambaye sina hakika kwa yaliyosemwa); tunaichukua dini yake na kuasi kila anachoamuru!" Mtume ﷺ alikuwa amekaa pamoja na Abubakar رضي الله عنه ubavuni mwake. Abubakar رضي الله عنه akasema: "Mwanamke huyu anakuja, nami nahofia kuwa atakuona". Mtume ﷺ alisema:

«إِنَّهَا لَنْ تَرَانِي»

**"Kwa hakika hataniona". Akasoma Qur'ani, ambayo kwayo alilindwa naye:**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:457.

وَإِذَا قَرَأْتَ الْقُرْآنَ فَاسْمِعْ أَنْ يَسْمِعَكَ رَبُّكَ وَأَنْتَ سَمِيعٌ ﴿٤٥﴾

***“Na unaposoma Qur’ani Tunaweka baina yako na wale wasioiamini Akhera pazia linalowafunika.”***

Alikuwa na kumuona Abubakar رضي الله عنه, lakini hakumuona Mtume ﷺ. Akasema: “Ewe Abubakar! Nimesikia kuwa sahibu yako ananishutumumu na kunifanyia istihzai”. Abubakar رضي الله عنه akasema: “Hapana, kwa Mola Mlezi wa Nyumba hii (yaani Ka’bah), hajakushutumumu kabisa”. Baada ya hapo akaenda zake, huku akisema: “Maqurayshi wanajua kuwa mimi ni binti ya bwana wao”<sup>1</sup>. Na Kauli Yake:

وَجَعَلْنَا عَلَى قُلُوبِهِمْ أَكِنَّةً

***“Na Tunaweka vifuniko juu ya nyoyo zao.”***

Nalo Akinnah ni jumla ya neno Kinaan ambayo inafunika moyo.

أَنْ يَفْقَهُوهُ

***“Wasiye wakaifahamu.”***

Maana yake: Wasiwe ni wenye kuifahamu Qur’ani. Pia,

وَفِي آدَانِهِمْ وَقْرًا

***“Na Tunaweka katika masikio yao uziwi.”***

Kitu ambacho kinawazuia kuisikia Qur’ani kwa njia ambayo wataifahamu na kuongoka kwayo. Amesema Allah تعالى,

وَإِذَا ذَكَرْتَ رَبَّكَ فِي الْقُرْآنِ وَحْدَهُ

***“Na unapomtaja katika Qur’ani Mola wako Mlezi Peke Yake.”***

Maana: Pindi unapompwekesha Allah تعالى Peke Yake katika kisomo chako, na ukasema: *Laa ilaaha illa Llaahu* (Hapana Mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Allah تعالى).

<sup>1</sup> Musnad Abu Ya’laa 1:53.

وَلَوْأ

**“Basi wao hugeuka.”** Maana yake: Wanageuka na kurudi,

عَلَىٰ أَدْبَارِهِمْ نُفُورًا ﴿٤٥﴾

**“Nyuma (kwa migongo yao) wakenda zao.”**

Na neno *Nufuur* ni wingi wa *Naafir*, na inajuzu kuwa ni mzizi wa neno usiokuwa na kitendo, na Allah تعالى Anajua zaidi. Kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَإِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَحْدَهُ اشْمَأَزَّتْ قُلُوبُ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِآخِرَةِ ۗ

**“Na anapotajwa Allah Peke Yake nyoyo za wale wasioamini Akhera huchukia.” (39:45)**

Amesema Qataadah katika Kauli Yake:

وَإِذَا ذُكِرَتِ رَبِّكَ فِي الْقُرْآنِ

**“Na unapomtaja katika Qur’ani Mola wako Mlezi Peke Yake.”**

Waislamu waliposema: *“Laa ilaaha illa Llaahu”*, washirikina walichukizwa sana na jambo hilo na kutoweza kuvumilia. Hivyo, Iblis na jeshi lake wakawaunga mkono, lakini Allah تعالى Akakataa hilo na Kuendelea Kulibakisha, Kulinyanyua, Kulinusuru na Kulidhihirisha dhidi ya wenye kulipinga. Yeyote mwenye kulitumia dhidi ya adui na mpinzani wake atashinda, na mwenye kulipigania basi atanusuriwa. Hakika ni Waislamu tu waliokuwa katika Bara Arabu, ndio wanaojua kalima hiyo, ambapo mpandaji (mnyama) anaweza kuitembea kwa masiku machache, na watu wengine, wakatembea dahari bila kuijua wala kukiri (kalima hio)<sup>1</sup>.

نَحْنُ أَعْلَمُ بِمَا يَسْتَمِعُونَ بِهِ إِذْ يَسْتَمِعُونَ إِلَيْكَ وَإِذْ هُمْ نَجْوَىٰ إِذْ يَقُولُ الظَّالِمُونَ إِن

تَتَّبِعُونَ إِلَّا رَجُلًا مَّسْحُورًا ﴿٤٦﴾ أَنْظِرْ كَيْفَ صَرَبُوا لَكَ الْأَمْثَالَ فَضَلُّوا فَلَا يَسْتَطِيعُونَ

سَبِيلًا ﴿٤٧﴾

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 17: 458.

**47. Sisi Tunajua vyema kabisa sababu wanayosikilizia wanapo kusikiliza, na wanaponong'ona. Wanaposema hao madhalimu: Nyinyi hamumfuati isipokuwa mtu aliyerogwa.**

**48. Tazama vipi wanavyokupigia mifano. Basi wamepotea. Kwa hivyo hawawezi kuipata njia.**

### Shura ya Siri ya Makuraishi baada ya Kuisikiliza Qur'ani

Allah تعالى Anamuambia Mtume Wake ﷺ kuhusu waliyoadili viongozi wa Kikurayshi walipokuja kusikiliza kisomo cha Qur'ani kwa siri bila ya watu wao kujua hayo. Walisema kuwa yeye ni *Mas'huri*, neno ambalo kulingana na kauli *Mas'huri* inamaanisha mtu aliyeathiriwa na sihiri (uchawi); huenda pia ikamaanisha mtu aliye na pafu (yaani mwanadamu), kama kwamba wanasema ukimfuata Muhammad utakuwa unamfuata mwanadamu tu anayekula chakula. Rai hii ya pili si sahihi. Wengine walikuwa wanasema kuwa alikuwa mshairi, au mtabiri, au mwendawazimu, au mchawi.

Allah تعالى Anasema:

أَنْظُرْ كَيْفَ ضَرَبُوا لَكَ الْأَمْثَالَ فَضَلُّوا فَلَا يَسْتَطِيعُونَ سَبِيلًا ﴿٤٨﴾

**“Tazama vipi wanavyokupigia mifano. Basi wamepotea. Kwa hivyo hawawezi kuipata njia.”**

Maana yake: Hawataongozwa katika ukweli wala hawataifikia njia. Muhammad bin Is'haaq رحمه الله تعالى amesema katika *As-Siirah*: “Muhammad bin Muslim bin Shihaab az-Zuhriy aliniambia kuwa ilitokea Abu Sufyaan bin Harb, Abu Jahli bin Hishaam na Al-Akhnas bin Sharaq bin 'Amr bin Wahb Ath-Thaqafiy, rafiki wa Bani Zahrah, walikwenda nje usiku mmoja ili kumsikiliza Mtume ﷺ alipokuwa akiswali nyumbani kwake. Kila mmoja wao alichukua nafasi ili aweze kusikiliza, na hakuna aliyejua kuwa wengine walikuwa hapo. Walibaki hapo wakimsikiliza usiku kucha mpaka karibu na Alfajiri. Walipoondoka, walikutana njiani kila mmoja wao akimlaumu mwenziwe, wakisemezana: ‘Msirudi tena, huenda mkatoa hisia tofauti (yaani mnapenda mnayosikia)’. Walikwenda zao mpaka ulipoingia usiku wa pili, kila mmoja wao akarudi tena mahali pake (pa kawaida) na kuutumia usiku akisikiliza. Alfajiri ilipofika waliondoka, nao

wakakutana tena barabarani, kila mmoja alimlaumu mwenziwe, wakasema yale yale waliyosema usiku uliopita. Walikwenda zao mpaka usiku wa tatu, ambapo kila mmoja alirudi sehemu yake ili apate kusikiliza kisomo usiku huo. Alfajiri ilipofika waliondoka, pindi walipokutana tena barabarani walisemezana: 'Tusiondoke mpaka tupeane ahadi kutorudi tena'. Hivyo, wakapeana ahadi kuhusiana na hilo, na kila mmoja akaenda njia yake. Asubuhi, al-Akhnas bin Shariq alichukua bakora yake na kuelekea nyumbani kwa Abu Sufyaan bin Harb, akamuambia: 'Niambie, ewe Abu Handhwalah (yaani Abu Sufyaan), unafikiria nini kuhusu uliyoyasikia kutoka kwa Muhammad?' Abu Sufyaan akasema: 'Ewe Abu Tha'labah (yaani Akhnas), naapa kwa Allah تعالیٰ, nimesikia vitu ninavyofahamu na kujua maana yake na nimesikia vitu nisivyofahamu wala kujua maana yake'. Al-Akhnas akasema: 'Hata mimi, naapa kwa Yule Mmoja uliyeapia Kwake'. Baada ya hapo aliondoka na kwenda kwa Abu Jahli, na kuingia nyumbani kwake. Akasema: 'Ewe Abul Hakam (yaani Abu Jahli), unafikiria nini kwa yale uliyosikia kutoka kwa Muhammad?' Akasema: 'Ulisikia nini?' Akasema (Abu Jahl): 'Sisi na Banu 'Abd Manaf tulishindania utukufu, hadhi na cheo: walikuwa wanawapatia chakula watu, nasi tukalisha; walishiriki katika vita, nasi pia; walitoa kiasi kadha nasi tukatoa, mpaka tukawa shingo kwa shingo (karibu sana), kama farasi washindanao. Kisha wakasema: Tuna Mtume miongoni mwetu, anayepata Wahyi kutoka mbinguni. Tutawezaje kushindana na hilo? Kwa Allah تعالیٰ, hatutamuamini'. Baada ya hapo Al-Akhnas aliinuka na kuondoka"<sup>1</sup>.

وَقَالُوا أَإِذَا كُنَّا عِظْمًا وَرُفْنًا أَإِنَّا لَمَبْعُوثُونَ خَلْقًا جَدِيدًا ﴿٤٥﴾ \* قُلْ كُونُوا حِجَارَةً  
 أَوْ حَدِيدًا ﴿٤٦﴾ أَوْ خَلْقًا مِّمَّا يَكْبُرُ فِي صُدُورِكُمْ ۖ فَسَيَقُولُونَ مَن يُعِيدُنَا ۖ قُلِ الَّذِي  
 فَطَرَكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ ۚ فَسَيُنْغِضُونَ إِلَيْكَ رُءُوسَهُمْ وَيَقُولُونَ مَتَىٰ هُوَ ۖ قُلْ عَسَىٰ أَن يَكُونَ  
 قَرِيبًا ﴿٤٧﴾ يَوْمَ يَدْعُوكُمْ فَتَسْتَجِيبُونَ بِحَمْدِهِ ۖ وَتَظُنُّونَ إِن لَّبِئْتُمْ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٤٨﴾

**49. Na walisema: Je! Tutapokuwa mifupa na mapande yaliyovurugika, tutafufuliwa kwa umbo jipya?**

**50. Sema: Kuweni hata mawe na chuma.**

<sup>1</sup> Ibn Hishaam, 1:337.

**51. Au umbo lolote mnaloliona kubwa katika vifua vyenu. Watasema: Nani atakayeturudisha tena? Sema: Yule yule Aliyekuumbeni mara ya kwanza! Watakutikisia vichwa vyao, na watasema: Lini hayo? Sema: Asaa yakawa karibu!**

**52. Siku Atakapokuiteni, na nyinyi mkamuitikia kwa kumshukuru, na mkadhani kuwa hamkukaa ila muda mdogo tu.**

### **Kuwaradi Wasioamini Maisha baada ya Mauti**

Allah تعالى Anatuelezea kuhusu makafiri wanaofikiria kuwa ni muhali kufufuliwa wakakanusha jambo hilo,

أءِذَا كُنَّا عِظْمًا وَّرُفْنًا

**“Je, Tunapokuwa mifupa na mapande yaliyovurugika.”**

Maana: Ardhi (mchanga). Hii ni kauli ya Mujaahid. ‘Aliy bin Abu Twalhah amepokea kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuwa inamaanisha vumbi<sup>1</sup>.

Allah تعالى Amesema:

أءِنَّا لَمَبْعُوثُونَ خَلْقًا جَدِيدًا ﴿١٠﴾

**“Tutafufuliwa kwa umbo jipya.”**

Maana yake: Siku ya Kiyama baada ya kuoza na kuwa si chochote na tumesahaulika. Allah تعالى Anatuelezea sehemu nyingine kuhusu wao:

يَقُولُونَ أءِنَّا لَمَرْدُودُونَ فِي الْحَافِرَةِ ﴿١١﴾ أءِذَا كُنَّا عِظْمًا نُخْرَةً ﴿١٢﴾ قَالُوا تِلْكَ إِذًا كَرَّةٌ

حَافِرَةٌ ﴿١٣﴾

**“Makafiri wanasema: Je! Kweli tutarudishwa katika hali yetu ya kwanza? Tutafufuliwa? Hata tukiwa mifupa mibovu. Wanasema: Basi marejeo haya ni yenye hasara.” (79:10-12)**

Na Kauli Yake Aliyetukuka,

<sup>1</sup> At-Tabari 17:464.

وَضَرَبَ لَنَا مَثَلًا وَنَسِيَ خَلْقَهُ ط

**“Na akatupigia mfano, na akasahau Kuumbwa kwake...”** Mpaka mwisho wa Aya (36:78-79)

Allah تعالی Alimuamuru Mtume Wake ﷺ kuwajibu, hivyo Akasema:

❖ قُلْ كُونُوا حِجَارَةً أَوْ حَدِيدًا ﴿٣٦﴾

**“Sema: Kuweni hata mawe na chuma.”**

Vitu ambavyo ni vigumu zaidi kuvirudisha katika hali yake ya awali kuliko mifupa na mapande yaliyovurugika,

أَوْ خَلَقًا مِّمَّا يَكْبُرُ فِي صُدُورِكُمْ ؕ

**“Au umbo lolote mnaloliona kubwa katika vifua vyenu.”**

Ibn Is'haq amepokea kutoka kwa Abu Najih kutoka kwa Mujaahid: “nilimuuliza Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kuhusu hilo, naye akasema: ‘Hiki ni kifo’. ‘Atwiyah amepokea kuwa Ibn Umar رضي الله عنهما aliifasiri Aya hii: ‘Ikiwa mungefariki bado Ningewafufua’<sup>1</sup>. Hiyo ndiyo iliyokuwa rai ya Said bin Jubayr, Abu Swalih, Al-Hasan, Qataadah, Adh-Dhahaak na wengineo<sup>2</sup>. Hii inamaanisha kuwa unapofikiria kuwa utakufa, ambayo ni kinyume na kuishi, Allah تعالی Atakufufua Anapopenda, kwani hakuna kitakachomzuilia Yeye Anapotaka kitu,

أَوْ خَلَقًا مِّمَّا يَكْبُرُ فِي صُدُورِكُمْ ؕ

**“Au umbo lolote mnaloliona kubwa katika vifua vyenu.”**

Mujaahid anasema: “Hii inamaanisha mbingu, ardhi na milima”. Kulingana na riwaya nyingine: “Chochote kile mnachotaka nyinyi muwe, Allah تعالی Atawafufua baada ya kufa kwenu”. Anasema Aliyetukuka:

فَسَيَقُولُونَ مَنْ يُعِيدُنَا ط

**“Watasema: Nani atakayeturudisha tena.”**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:463.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:463.

Maana: Nani atakayetufufua tukiwa mawe au chuma au vitu vingine vyenye nguvu vilivyoumbwa.

قُلِ الَّذِي فَطَرَكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ

**“Sema: Yule Yule Aliyekuumbeni mara ya kwanza.”** Maana yake: Yule Aliyewaumbeni mlipokuwa si chochote wala lolote, kisha mkawa wanadamu mliotawanyika, hakika Yeye ni Muweza Kuwarudisha hali ya awali, hata mkiwa hali yoyote ile.

وَهُوَ الَّذِي يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ

**“Na Yeye Ndiye Aliyeanzisha viumbe na Ndiye Atakayevirudisha mara nyingine, na jambo hilo ni rahisi kwake.” (30:27).**

فَسَيُنْغِضُونَ إِلَيْكَ رُءُوسَهُمْ

**“Watakutikisia vichwa vyao.”** Ibn ‘Abbaas na Qataadah wamesema: “Watatikisa vichwa vyao kwa istihzai”<sup>1</sup>. Rai hii ilitolewa na Ibn ‘Abbaas na Qataadah ni kama walivyoelewa Waarabu kutoka katika lugha yao, kwa sababu neno lililotumiwa *Fasayun-ghidhuun* linaashiria kutikisa juu na chini au chini na juu. Neno linalotokana na hilo, *Naghdh*, linatumika kwa mtoto wa mbuni kwa sababu anapotembea, anatembea haraka haraka na kutikisa kichwa chake. Neno hilo hilo linatumika kuelezea jino linapolegea na kung’oka kutoka sehemu yake. Na Kauli Yake:

وَيَقُولُونَ مَتَى هُوَ

**“Na watasema: Lini hayo?”** Hii inaonesha kuwa wanafikiria kuwa jambo hilo ni muhali kutokea (ni jambo lisilowezekana), kama Alivyosema Allah تعالى:

وَيَقُولُونَ مَتَى هَذَا الْوَعْدُ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ

**“Na wanasema: Ahadi hii (ya kuja Kiyama) itatokea lini, ikiwa mnasema kweli?” (36:48).**

Na Amesema Aliyetukuka:

يَسْتَعْجِلُ بِهَا الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِهَا

**“Wasioamini kwa stihzai zao hukuomba (Kiyama) kifike upesi...” (42:18)**

<sup>1</sup> At-Tabari 17: 467.



Na Kauli Yake:

قُلْ عَسَىٰ أَنْ يَكُونَ قَرِيبًا ﴿١٥﴾

**“Sema: Asaa kikawa karibu.”** Maana: Tahadhari nacho kwani kipo karibu na bila shaka kitakuja na kutokea kwenu na kila chenye kuja kipo karibu. Na Kauli Yake:

يَوْمَ يَدْعُوكُمْ

**“Siku Atakapo kuiteni.”** Maana yake: Bwana wenu Mlezi, Aliyetukuka:

إِذَا دَعَاكُمْ دَعْوَةً مِنَ الْأَرْضِ إِذَا أَنْتُمْ تَخْرُجُونَ ﴿٢٥﴾

**“Atakapokuiteni wito mmoja tu, nyote mtatoka ardhini.” (30:25),**

Maana: Atakapowaamuru mtoke ardhini hakuna kitakachompinga Yeye au kuzuia Amri Yake kutotimizwa. Bali, ni kama Alivyosema:

وَمَا أَمْرُنَا إِلَّا وَاحِدَةٌ كَلَّمَجٍ بِالْبَصْرِ ﴿٥٠﴾

**“Na hakukuwa kupitisha amri Yetu ila ni mara moja tu kama kupepesa jicho (kufumba na kufumbua).” (54:50)** Na,

إِنَّمَا قَوْلُنَا لِشَيْءٍ إِذَا أَرَدْنَاهُ أَنْ نَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٤٠﴾

**“Kauli Yetu kwa kitu Tunachokitaka kiwe, ni kukiambia: ‘Kuwa’, basi kinakuwa tu.” (16:40)** Na,

فَإِنَّمَا هِيَ زَجْرَةٌ وَاحِدَةٌ ﴿١٣﴾ فَإِذَا هُمْ بِالسَّاهِرَةِ ﴿١٤﴾

**“Kwa hakika hicho (Kiyama) kitakuwa kwa kupigwa ukelele mmoja tu. Mara wao viumbe wote watakuwa katika ardhi mpya.” (79:13-14)**

Maana: Hiyo itakuwa ni Amri moja tu ya uhakika, hapo watu watatoka ndani ya ardhi hadi juu yake. Hivyo ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

يَوْمَ يَدْعُوكُمْ فَتَسْتَجِيبُونَ بِحَمْدِهِ

**“Siku Atakapokuiteni, na nyinyi mkamuitikia kwa kumshukuru.”**

Maana: Nyote mtanyanyuka kwa kuitikia Amri Yake na kwa kutii Agizo na Matakwa Yake. Na Kauli Yake:

وَتَتَّظِنُونَ

**“Na mkadhani.”** Maana yake: Siku ambayo mtasimama kwenye makaburi yenu.

إِن لَّبِئْتُمْ

**"Kuwa hamkukaa."** Katika nyumba na makao haya ya ardhini,

إِلَّا قَلِيلًا ﴿٤٥﴾

**"Ila muda mdogo tu"**. Hii ni kama ile Aya inayosema:

كَأَنَّهُمْ يَوْمَ يَرَوْنَهَا لَمْ يَلْبَثُوا إِلَّا عَشِيَّةً أَوْ ضُحًى ﴿٤٦﴾

**"Siku watakapokiona watakuwa kama kwamba hawakukaa ulimwenguni ila jioni moja au mchana wake."** (79:46).

Na Amesema Aliyetukuka:

يَوْمَ يَنْفَخُ فِي الصُّورِ وَنَحْشُرُ الْمُجْرِمِينَ يَوْمَئِذٍ زُرْقًا ﴿٤٧﴾ يَتَخَفَتُونَ بَيْنَهُمْ إِنْ لَّبِئْتُمْ

إِلَّا عَشْرًا ﴿٤٨﴾ نَحْنُ أَعْلَمُ بِمَا يَقُولُونَ إِذْ يَقُولُ أَمْثَلُهُمْ طَرِيقَةً إِنْ لَّبِئْتُمْ إِلَّا يَوْمًا ﴿٤٩﴾

**"Siku itakapopigwa baragumu na Tukawakusanya wakosa siku hiyo, hali macho yao yatakuwa kibuluu kwa hofu. Watanong'onezana wao kwa wao wakisema: 'Hamkukaa ulimwenguni ila siku kumi tu hivi'. Sisi Tunajua sana watakayosema, watakaposema wabora wao katika mwendo: 'Nyinyi hamkukaa ila siku moja tu'"** (20:102-104).

وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ يُقْسِمُ الْمُجْرِمُونَ مَا لَبِثُوا غَيْرَ سَاعَةٍ كَذَلِكَ كَانُوا يُؤْفَكُونَ ﴿٥٠﴾

**"Na siku kitakaposimama Kiyama waovu wataapa ya kwamba hawakukaa ulimwenguni isipokuwa saa moja tu. Na namna hivi ndivyo walivyokuwa wakipotolewa."** (30:55).

Na Amesema Aliyetukuka:

قُلْ كَمْ لَبِئْتُمْ فِي الْأَرْضِ عَدَدَ سِنِينَ ﴿٥١﴾ قَالُوا لَبِئْنَا يَوْمًا أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ فَسَلِّ الْعَادِينَ

﴿٥٢﴾ قُلْ إِنْ لَّبِئْتُمْ إِلَّا قَلِيلًا لَوْ أَنَّكُمْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٥٣﴾

**"Atasema: 'Mlikaa muda gani katika ardhi kwa hesabu ya miaka?' Watasema: 'Tulikaa siku moja au sehemu ya siku. Basi waulize wafanyao hesabu'. Atasema: Nyinyi hamkukaa huko ulimwenguni ila kidogo tu; laiti mngalikuwa mmejua."** (23:112-114)

وَقُلْ لِعِبَادِي يَقُولُوا الَّتِي هِيَ أَحْسَنُ إِنَّ الشَّيْطَانَ يَنْزِعُ بَيْنَهُمْ إِنَّ الشَّيْطَانَ كَانَ  
لِلْإِنْسَانِ عَدُوًّا مُّبِينًا ﴿٥٥﴾

**53. Waambie waja Wangu waseme maneno mazuri, maana Shetani huchochea ugomvi baina yao. Hakika Shetani ni adui aliyedhahiri kwa mwanadamu.**

### Watu Wazungumze Maneno Mazuri na kwa Adabu

Allah تعالى Anamuamuru mja Muhammad ﷺ awaambie waja wa Allah تعالى wawe ni wenye kuzungumza na wenzao katika mijadala na mazungumzo kwa upole, ulaini na maneno mazuri zaidi. Hakika Waislamu wasipofanya hayo, Shetani atachochea ugomvi na shari baina yao. Bila shaka, Shetani ni adui wa Adam عليه السلام na wazawa wake, na ameendelea kukataa kumsujudia Adam عليه السلام. Uadui wake uko wazi na ni dhahiri kabisa. Kwa sababu hii, ni haramu kwa mwanadamu kumuelekeza nduguye Muislamu kifaa cha chuma, kwani huenda Shetani akamuhadaa ampige nacho nduguye.

Ampokea Imaam Ahmad kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ:

«لَا يُبِيرَنَّ أَحَدُكُمْ إِلَىٰ أَخِيهِ بِالسَّلَاحِ، فَإِنَّهُ لَا يَدْرِي أَحَدُكُمْ لَعَلَّ الشَّيْطَانَ أَنْ يَنْزِعَ فِي يَدِهِ قَبْعَةً فِي حُمْرَةٍ مِنَ النَّارِ»

*"Mmoja wenu asimuashirie nduguye na silaha kwani hatambui mmoja wenu huenda Shetani atamuhadaa na kumpiga nacho nduguye na hivyo kuingizwa shimo la Motoni."*<sup>1</sup>

Al-Bukhaariy na Muslim wameinukuu Hadithi hii kwa silsila ya mapokezi kutoka kwa 'Abdur-Razzaaq رحمه الله تعالى.<sup>2</sup>

رَبُّكُمْ أَعْلَمُ بِكُمْ ط إِنَّ يَشَأُ يَرْحَمَكُمُ أَوْ إِنْ يَشَأُ يُعَذِّبُكُمْ ط وَمَا أَرْسَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ وَكِيلاً ﴿٥٦﴾  
وَرَبُّكَ أَعْلَمُ بِمَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ ط وَلَقَدْ فَضَّلْنَا بَعْضَ النَّبِيِّينَ عَلَىٰ بَعْضٍ ط وَءَاتَيْنَا

دَاوُدَ زُورًا ﴿٥٧﴾

<sup>1</sup> Ahmad 2:317.

<sup>2</sup> Fat'h Al-Baariy 13:26 na Muslim 4:2020.

**54. Mola wenu Mlezi Anakujueni vilivyo. Akipenda Atakurehemuni, na Akipenda Atakuadhibuni. Na Hatukukutuma ili uwe mlinzi juu yao.**

**55. Na Mola wako Mlezi Anawajua waliomo mbinguni na katika ardhi. Na hakika Tumewafadhilisha baadhi ya Manabii kuliko wengine; na Daawuud Tulimpa Zaburi.**

Allah تعالیٰ Anasema:

رَبُّكُمْ أَعْلَمُ بِكُمْ<sup>ط</sup>

**“Mola wenu Mlezi Anakujueni vilivyo.”**

Enyi watu. Maana yake: Anawajua vilivyo nani kati yenu anastahiki uongofu na nani asiyestahiki. Hivyo:

إِنْ يَشَأْ يُرْحَمَكُمُ

**“Akipenda Atakurehemuni.”**

Kwa Kuwaafikisha na Kuwasaidia katika kumtii Yeye na kurudi Kwake. Pia,

أَوْ إِنْ يَشَأْ يُعَذِّبْكُمْ<sup>ع</sup> وَمَا أَرْسَلْنَاكَ

**“Au Akipenda Atakuadhibuni. Na Hatukukutuma.”**

Ewe Muhammad,

عَلَيْهِمْ وَكَيْلًا<sup>ح</sup>

**“Ili uwe mlinzi juu yao.”**

Maana yake: Tumekutuma wewe uwe muonyaji, yeyote atakayekutii ataingia Peponi na atakayekuasi ataingia Motoni.

Na Kauli Yake Allah تعالیٰ:

وَرَبُّكَ أَعْلَمُ بِمَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ<sup>د</sup>

**“Na Mola wako Mlezi Anawajua waliomo mbinguni na katika ardhi.”**

Maana yake: Kwa kiwango chao katika kutii na kuasi.

## Kufadhilishwa Baadhi ya Manabii juu ya Wengine

وَلَقَدْ فَضَّلْنَا بَعْضَ النَّبِيِّينَ عَلَىٰ بَعْضٍ<sup>ط</sup>

**“Na hakika Tumewafadhilisha baadhi ya Manabii kuliko wengine.”**

Kama Alivyosema Aliyetukuka:

﴿ تِلْكَ الْأَرْسُلُ فَضَّلْنَا بَعْضَهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ مِّنْهُمْ مِّنْ كَلِمَةِ اللَّهِ<sup>ط</sup> وَرَفَعَ بَعْضُهُمْ دَرَجَاتٍ<sup>ع</sup>﴾

**“Mitume hao Tumewafadhilisha baadhi yao zaidi kuliko wengine. Miongoni mwao wako ambao Allah Alisema nao; na wengine Akawapandisha vyeo vikubwa kabisa.” (2:253)**

Hii haipingani na ile Hadithi iliyothibiti katika Sahihi mbili kuwa Mtume ﷺ amesema:

«لَا تَفْضَلُوا بَيْنَ الْأَنْبِيَاءِ»

*“Msifadhilisha baina ya Manabii.”<sup>1</sup>*

Muradi wa Hadithi hii ni kufadhilisha kulingana na matamania, utaifa, taasubi na ulokole, sio kwa msingi wa dalili. Kukiwa na dalili ya wazi, tunalazimika kufuata. Hakuna tofauti kuwa Mitume ni bora kuliko baki ya Manabii, na kuwa Mitume waliopata taabu na misukosuko mikubwa ya hali ya juu ni bora kuliko wote. Mitume hao ni wale watano (5) waliotajwa katika Aya mbili za Qur’ani. Nazo ni kama zifuatazo:

وَإِذْ أَخَذْنَا مِنَ النَّبِيِّينَ مِيثَاقَهُمْ وَمِنْكَ<sup>ط</sup> وَمِن نُّوحٍ وَإِبْرَاهِيمَ وَمُوسَىٰ وَعِيسَىٰ ابْنِ مَرْيَمَ<sup>ع</sup>

**“Na wakumbushe Tulipochukua ahadi kwa Manabii wote na kwako wewe, na Nuuh na Ibrahim na Musa na ‘Isaa mwana wa Maryam.” (33:7)**

Na katika Kauli Yake:

﴿ شَرَعَ لَكُمْ مِنَ الدِّينِ مَا وَصَّىٰ بِهِ نُوحًا وَالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ وَمَا وَصَّيْنَا بِهِ إِبْرَاهِيمَ

﴿ وَمُوسَىٰ وَعِيسَىٰ أَنْ أَقِيمُوا الدِّينَ وَلَا تَتَفَرَّقُوا فِيهِ<sup>ع</sup>﴾

<sup>1</sup> Fat’h Al-Baariy 6:519 na Muslim 4:1844.

***“Amekupeni sharia ya Dini ile ile Aliyomuusia Nuuh na Tuli yokufunulia wewe na Tuli yowausia Ibraahim na Musa na ‘Isaa, kwamba simamisheni Dini wala msifarikiane kwayo.” (42:13)***

Hakuna ukinzani wala mzozano kuwa Muhammad ﷺ ni mbora kuliko wote, kisha ni Ibraahim عليه السلام, baadaye Musa عليه السلام, kishaa ‘Isaa عليه السلام, kulingana na kauli iliyo mashuhuri.

Tumejadili dalili za shauri hilo kwa urefu katika sehemu nyengine.

Na Allah تعالى Ndiye Mwenye Kuwafikisha. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَأَتَيْنَا دَاوُدَ زُبُورًا ﴿١٦٣﴾

***“Na Daud Tulimpa Zaburi.” (4:163)***

Hii ni kututanabahisha kuhusu ubora na utukufu wake.

Amepokea Al-Bukhaariy kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«خُفِّفَ عَلَى دَاوُدَ الْقُرْآنُ، فَكَانَ يَأْمُرُ بِدَوَابِهِ فَيُنْسِجُ، فَكَانَ يَقْرُؤُهُ قَبْلَ أَنْ يَبْرُغَ»

*“Zaburi ilifanywa sahali kwa Daud, hivyo alikuwa akiitisha kipando chake kuvikwa sogi (kutandikwa), na alikuwa akimaliza kisomo (Zaburi) kabla ya shughuli hiyo kumalizika.”<sup>1</sup>*

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baariy 6:522.

قُلِ ادْعُوا الَّذِينَ زَعَمْتُمْ مِنْ دُونِهِ فَلَا يَمْلِكُونَ كَشْفَ  
 الضُّرِّ عَنْكُمْ وَلَا تَحْوِيلًا ﴿٥٦﴾ أُولَئِكَ الَّذِينَ يَدْعُونَ  
 يَبْتَغُونَ إِلَىٰ رَبِّهِمْ الْوَسِيلَةَ أَيُّهُمْ أَقْرَبُ وَيَرْجُونَ رَحْمَتَهُ  
 وَيَخَافُونَ عَذَابَهُ ۗ إِنَّ عَذَابَ رَبِّكَ كَانَ مَحْذُورًا ﴿٥٧﴾  
 وَإِنْ مِنْ قَرْيَةٍ إِلَّا نَحْنُ مُهْلِكُوهَا قَبْلَ يَوْمِ الْقِيَامَةِ أَوْ  
 مُعَذِّبُوهَا عَذَابًا شَدِيدًا ۗ كَانَ ذَلِكَ فِي الْكِتَابِ مَسْطُورًا  
 ﴿٥٨﴾ وَمَا مَنَعَنَا أَنْ نُرْسِلَ بِالْآيَاتِ إِلَّا أَنْ كَذَّبَ بِهَا  
 الْأُولُونَ ۗ وَءَاتَيْنَا ثُمُودَ النَّاقَةَ مُبْصِرَةً فَظَلَمُوهَا ۗ وَمَا  
 نُرْسِلُ بِالْآيَاتِ إِلَّا تَحْوِيلًا ﴿٥٩﴾ وَإِذْ قُلْنَا لَكَ إِنَّ رَبَّكَ  
 أَحَاطَ بِالنَّاسِ ۗ وَمَا جَعَلْنَا آلَ رَأْيِنَا الْآلِيَّ أَرْبَابًا إِلَّا فِتْنَةً  
 لِلنَّاسِ وَالشَّجَرَةَ الْمَلْعُونَةَ فِي الْقُرْآنِ ۗ وَنُحُوتُهُمْ فَمَا  
 يَزِيدُهُمْ إِلَّا طُغْيَانًا كَبِيرًا ﴿٦٠﴾ وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ  
 اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ قَالَ أَأَسْجُدُ لِمَنْ  
 خَلَقْتُ طِينًا ﴿٦١﴾ قَالَ أَرَأَيْتَكَ هَذَا الَّذِي كَرَّمْتَ عَلَيَّ  
 لَئِنِ أَخَّرْتَنِي إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَأُحْتَنِكَنَّ ذُرِّيَّتَهُ إِلَّا قَلِيلًا  
 ﴿٦٢﴾ قَالَ أَذْهَبَ فَمَنْ تَبِعَكَ مِنْهُمْ فَإِنَّ جَهَنَّمَ جَزَاءُكُمْ  
 جَزَاءً مَوْفُورًا ﴿٦٣﴾ وَأَسْتَفْرِزَ مِنْ أَسْطَظَعَتْ مِنْهُمْ بِصَوْتِكَ  
 وَأَجْلِبَ عَلَيْهِمُ بِخَيْلِكَ وَرَجُلِكَ وَشَارِكُوهُمْ فِي الْأَمْوَالِ  
 وَالْأَوْلَادِ وَعَدَهُمْ ۗ وَمَا يَعِدُهُمُ الشَّيْطَانُ إِلَّا غُرُورًا ﴿٦٤﴾  
 إِنَّ عِبَادِي لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطَانٌ ۗ وَكَفَىٰ بِرَبِّكَ

وَكَيْلًا ﴿٦٥﴾

قُلِ ادْعُوا الَّذِينَ زَعَمْتُمْ مِنْ دُونِهِ  
 فَلَا يَمْلِكُونَ كَشْفَ الضُّرِّ عَنْكُمْ  
 وَلَا تَحْوِيلًا ﴿٥٦﴾ أُولَئِكَ الَّذِينَ  
 يَدْعُونَ يَبْتَغُونَ إِلَىٰ رَبِّهِمْ  
 الْوَسِيلَةَ أَيُّهُمْ أَقْرَبُ وَيَرْجُونَ  
 رَحْمَتَهُ وَيَخَافُونَ عَذَابَهُ ۗ إِنَّ  
 عَذَابَ رَبِّكَ كَانَ مَحْذُورًا ﴿٥٧﴾

56. Sema: Waombeni hao  
 mnaowadai badala yake  
 Yeye. Hawawezi kukuon-  
 doleeni madhara, wala  
 kuyaweka pengine.

57. Hao wanaowaomba,  
 wao wenyewe wanatafuta  
 njia ya kuendea kwa Mola  
 wao Mlezi - hata miongoni  
 mwao walio karibu mno - na  
 wanataraji Rehema Zake na  
 wanaikhofu Adhabu Yake.  
 Hakika Adhabu ya Mola  
 wako Mlezi yafaa kuta-  
 hadhari nayo.

## Miungu ya Washirikina Haiwezi Kunufaisha wala Kudhuru bali Hiyo Yenyewe Inahitaji Kujukurubisha

Anasema Aliyetukuka:

﴿ قُلْ ﴾

“Sema”,

Ewe Muhammad kwa hao washirikina wanaoabudu asiyekuwa Allah تعالى:

أَدْعُوا الَّذِينَ زَعَمْتُمْ مِّنْ دُونِهِ

**“Waombeni hao mnaowadaia badala yake Yeye.”**

Kama vile masanamu na wapinzani wa Allah تعالى. Hata ukiwarudia tambua kuwa:

فَلَا يَمْلِكُونَ كَشْفَ الضُّرِّ عَنْكُمْ

**“Hawawezi kukuondoleeni madhara.”**

Maana yake: Wao hawana uwezo huo. Pia,

﴿ وَلَا تَحْوِيلاً ﴾

**“Wala kuyaweka pengine.”**

Maana yake: Wayapeleke kwa wengine wasiokuwa nyinyi na maana yake ni kuwa hakika yule anayeweza hilo ni Allah تعالى Peke Yake, asiyekuwa na mshirika, ambaye Yeye Ndiye Muumbaji na Amri zote ni Zake. Amesema Al-'Awfiy kutoka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما kuhusu Kauli Yake:

﴿ قُلْ أَدْعُوا الَّذِينَ زَعَمْتُمْ مِّنْ دُونِهِ ﴾

**“Sema: Waombeni hao mnaowadaia badala yake...”**

Amesema: “Walikuwa washirikina wakisema ‘tunawaabudu Malaika, Masihi na ‘Uzayr’, ilhali hawa (Malaika, Masihi na ‘Uzayr) wenyewe wakimuabudu Allah تعالى<sup>1</sup>.”

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 17:471.



أُولَئِكَ الَّذِينَ يَدْعُونَ

**“Hao wanaowaomba...”.**

Amepokea Al-Bukhari kutoka kwa Hadithi ya Sulaymaan bin Mahraan Al-A'mash kutoka kwa Ibrahim kutoka kwa Abu Ma'mar kutoka kwa 'Abdallah katika Kauli Yake:

أُولَئِكَ الَّذِينَ يَدْعُونَ يَبْتَغُونَ إِلَىٰ رَبِّهِمُ الْوَسِيلَةَ

**“Hao wanaowaomba, wao wenyewe wanatafuta njia ya kuendea kwa Mola wao Mlezi’.**

Baadhi ya majini walikuwa wakiabudu hivyo, kisha wakasilimu. Kulingana na riwaya nyingine: “Baadhi ya wanadamu walikuwa wakiwaabudu baadhi ya majini, baadaye hao majini wakasilimu, lakini wale wanadamu walishikilia dini yao (ya kuwaabudu majini)”<sup>1</sup>. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَيَرْجُونَ رَحْمَتَهُ وَيَخَافُونَ عَذَابَهُ

**“Na wanataraji Rehema Zake na wanaikhofu Adhabu Yake”.**

‘Ibada haitimii wala kukamilika ila kwa khofu na matarajio. Khofu humzuilia mtu kufanya yaliyokatazwa na matarajio humfanya afanye mambo ya utiifu (na mema). Na Kauli Yake Aliyetukuka:

إِنَّ عَذَابَ رَبِّكَ كَانَ مَحْذُورًا

**“Hakika Adhabu ya Mola wako Mlezi yafaa kutahadhari nayo.”**

Maana: Inafaa mtu atahadhari nayo na akhofie kuingia ndani yake na kupatikana nayo. Tunajilinda kwa Allah تعالى kutokana na adhabu hiyo.

وَأَنَّ مِنَ قَرْيَةٍ إِلَّا نَحْنُ مُهْلِكُوهَا قَبْلَ يَوْمِ الْقِيَامَةِ أَوْ مُعَذِّبُوهَا عَذَابًا شَدِيدًا كَانَ

ذَلِكَ فِي الْكِتَابِ مَسْطُورًا

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baariy 8:249, 250.

**58. Na hapana mji wowote ila Sisi Tutauteketeza kabla ya Siku ya Kiyama, au Tutaupa adhabu kali. Haya yamekwishaandikwa katika Kitabu.**

### Maangamizi na Adhabu kwa Wasioamini Katika Miji Yao Kabla ya Kiama

Hii ni habari na maelezo kutoka kwa Allah تعالی kwamba Amepitisha na Kuamuru kwa Aliyonayo katika *Lawhul Mahfuudh* (Ubao Uliohifadhiwa): Hakuna kijiji ila kitahilikishwa (kuharibiwa) kwa Kuwafagia watu wake wote au kwa Kuwaadhibu,

عَذَابًا شَدِيدًا<sup>ط</sup>

**“Adhabu kali”.**

Adhabu hiyo itakuwa ima kwa kuwaua au kuwapatia mitihani kwa namna Apendavyo. Hakika hilo litakuwa kwa sababu ya dhambi zao na makosa yao, kama Alivyosema Aliyetukuka kuhusu kaumu zilizopita:

وَمَا ظَلَمْنَاهُمْ وَلَكِنْ ظَلَمُوا أَنفُسَهُمْ<sup>ط</sup>

**“Nasi Hatukuwadhulumu lakini wao wamejidhulumu wenyewe.” (11:101).**

Na Amesema Aliyetukuka:

فَذَاقَتْ وَبَالَ أَمْرِهَا وَكَانَ عِقَبَةُ أَمْرِهَا خُسْرًا<sup>ط</sup>

**“Basi ikauonja ubaya wa mambo yake; na mwisho wa mambo yao ilikuwa hasara.” (65:9).**

Na Amesema,

وَكَأَيِّن مِّن قَرْيَةٍ عَتَتْ عَن أَمْرِ رَبِّهَا وَرُسُلِهَا

**“Na miji mingapi iliyovunja Amri ya Mola wake na Mitume Yake.” (65:8).**

وَمَا مَنَعَنَا أَنْ نُرْسِلَ بِالْآيَاتِ إِلَّا أَنْ كَذَّبَ بِهَا الْأَوْلُونَ<sup>ط</sup> وَإِنَّا لَنُؤَدِّئُنَّكَمُودَ النَّاقَةِ مُبْصِرَةً

فَظَلَمُوا بِهَا<sup>ط</sup> وَمَا نُرْسِلُ بِالْآيَاتِ إِلَّا تَخْوِيفًا<sup>ط</sup>

**59. Na hapana kinachotuzuia kupeleka miujiza ila ni kuwa watu wa zamani waliikanusha. Na Tuliwapa Wathamudi ngamia jike**

***kuwa ni Ishara iliyo dhahiri, lakini walidhulumu kwaye. Nasi Hatupeleki Ishara ila kwa ajili ya kuhadharisha.***

### **Sababu za Allah ﷻ Kutotuma Ishara na Miujiza**

Amesema Said bin Jubayr: Washirikina walisema: “Ewe Muhammad, unadai ya kwamba kulikuwa na Manabii kabla yako, miongoni mwao alikuwepo yule ambaye upepo ulitiishwa kwake na mwingine ambaye aliweza kuhuisha wafu. Ikiwa wataka tukuamini, muombe Mola wako Mlezi Augeuze mlima wa Swafa uwe dhahabu kwa ajili yetu”. Allah ﷻ Alimteremshia Wahyi: “Nimesikia waliyosema. Ukitaka, Nitafanya wanayosema, lakini ikiwa hawataamini baada ya hapo, adhabu itawateremkia, kwa sababu baada ya ishara kuletwa hakuna tena nafasi ya kubahatisha. Au ukitaka, Nitawavumilia watu wako na Kuwapatia wakati zaidi”. Akasema:

«يَا رَبِّ اسْتَأْنِبْ بِهِمْ»

*“Ewe Mola wangu Mlezi! Wape wakati zaidi”<sup>1</sup>.*

Na hivyo ndivyo alivyosema Qataadah, Ibn Jurayj na wengineo<sup>2</sup>.

Amepokea Imaam Ahmad kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما: “Watu wa Makka walimtaka Mtume ﷺ augeuze mlima Swafa uwe dhahabu kwao wao, na aiondoe milima pembezoni mwa Makka ili waweze kulima ardhi”. Aliambiwa (na Allah ﷻ): “Ukitaka, Nitawavumilia na Kuwapatia muda zaidi, au ukitaka, Nitawafanyia wanayotaka, lakini baada ya hapo wakikufuru, wataangamizwa kama walivyoangamizwa watu waliokuwa kabla yao”. Akasema:

«لَا، بَلِ اسْتَأْنِبْ بِهِمْ»

*“Laa (Hapana), bali Wavumilie na Uwape muda zaidi.”*

Hapo Allah ﷻ Akateremsha:

وَمَا مَنَعَنَا أَنْ نُرْسِلَ بِالْآيَاتِ إِلَّا أَنْ كَذَّبَ بِهَا الْأَوَّلُونَ<sup>3</sup>

***“Na hapana kinachotuzuia kupeleka miujiza ila ni kuwa watu wa zamani waliikanusha”<sup>1</sup>. (17:59)***

<sup>1</sup> At-Tabari 17:477. Mapokezi haya yanaungwa mkono na Hadithi ya Ibn ‘Abbaas iliyonukuliwa na Ahmad. Tizama chini.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:477.

<sup>3</sup> Ahmad 1:258.

Pia an-Nasaa'iy ameipokea kutoka kwa Hadithi ya Jariir رحمته الله تعالى<sup>1</sup>.

Amepokea Imaam Ahmad kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: "Kuraysh walimuambia Mtume ﷺ: 'Muombe Mola wako Mlezi Atubadilishie mlima wa Swafa uwe ni dhahabu nasi tutakuamini'. Akasema:

«وَتَفْعَلُونَ؟»

*'Mtafanya kweli?'*

Wakasema: 'Ndio'. Hivyo, alimuomba Mola wake Mlezi, na Jibril alikuja kwake na kumuambia: 'Mola wako Mlezi Anakufikishia Salamu Zake kwako na Anakuambia: Ukitaka, Nitaubadilisha mlima Swafa uwe dhahabu kwa ajili yao, hivyo yeyote miongoni mwao atakayekufuru baada ya hapo, ataadhibiwa kwa adhabu ambayo mfano wake haujawahi kuonekana kwa viumbe; au ukitaka, Nitaifungua milango ya toba na rehema kwao'. Akasema:

«بَلْ بَابُ التَّوْبَةِ وَالرَّحْمَةِ»

*'Bali milango ya toba na rehema.'*<sup>2</sup>

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَمَا تُرْسِلُ بِالْآيَاتِ إِلَّا تَخْوِيفًا ﴿١٧﴾

***"Nasi Hatupeleki Ishara ila kwa ajili ya Kuhadharisha".***

Amesema Qataadah: "Allah تعالى Anawakhofisha watu kwa ishara zozote Atakazo, ili wapate kuzingatia, kukumbuka na kurudi. Tunaambiwa kuwa Kufah ilitetemeshwa wakati wa Ibn Mas'ud رضي الله عنه akasema: 'Enyi watu! Mola wenu Mlezi Anawakemea, basi zindukeni na mtanabahi'<sup>3</sup>.

Hivyo hivyo, imepokewa kuwa mji wa Madinah ulikumbwa na mitetemeko kadhaa wakati wa Umar bin Al-Khatwtwaab رضي الله عنه. 'Umar رضي الله عنه akasema: "Mmebadilika, naapa kwa Allah تعالى, na lau mitetemeko hiyo itakuja tena basi nitawafanya hivi na hivi."<sup>4</sup>

<sup>1</sup> An-Nasaa'iy katika Al-Kubraa 6:380 na atw-Twabariy 17:476.

<sup>2</sup> Ahmad 1:242.

<sup>3</sup> Atw-Twabariy 17:478.

<sup>4</sup> Ibn Abi Shaybah 2:473.

Na hivyo ndivyo alivyosema Mtume ﷺ katika Hadithi iliyonukuliwa na Al-Bukhaari na Muslim:

«إِنَّ الشَّمْسَ وَالْقَمَرَ آيَاتَانِ مِنْ آيَاتِ اللَّهِ وَإِنَّهُمَا لَا يَنْكَسِفَانِ لِمَوْتِ أَحَدٍ وَلَا لِحَيَاتِهِ، وَلَكِنَّ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ يُخَوِّفُ بِهِمَا عِبَادَهُ، فَإِذَا رَأَيْتُمْ ذَلِكَ فَافْرَعُوا إِلَى ذِكْرِهِ وَدُعَائِهِ وَاسْتِغْفَارِهِ ثُمَّ قَالَ: - يَا أُمَّةَ مُحَمَّدٍ وَاللَّهِ مَا أَحَدٌ أُغْيِرَ مِنْ اللَّهِ أَنْ يَزِيحَ عَبْدُهُ أَوْ تَزِيحَ أُمَّتُهُ، يَا أُمَّةَ مُحَمَّدٍ وَاللَّهِ لَوْ تَعْلَمُونَ مَا أَعْلَمُ لَفَضَحْتُمْ قَلِيلًا وَلَبَكَيْتُمْ كَثِيرًا»

*"Jua na mwezi ni ishara mbili miongoni mwa ishara za Allah, na hazipatwi kwa kupatwa kwa kufariki kwa yeyote wala uhai wake. Allaah Anatumia jua na mwezi Kuwakhofisha waja Wake, hivyo mukishaona, fanyeni haraka kumkumbuka Yeye, kumuomba na kumtaka msamaha". Kisha akasema: "Enyi Ummah wa Muhammad! Naapa kwa Allah, hakuna aliye na hisia ya wivu kuliko Allah Akimuona mja Wake au kijakazi Chake, akizini. Enyi Ummah wa Muhammad, lau mngejua ninayojua mngecheka kidogo na kulia sana"<sup>1</sup>.*

وَإِذْ قُلْنَا لَكَ إِنَّ رَبَّكَ أَحَاطَ بِالنَّاسِ وَمَا جَعَلْنَا آلَ رَبِّكَ الْبَاقِيَةَ إِلَّا فَتْنَةً لِّلنَّاسِ وَالشَّجَرَةَ الْمَلْعُونَةَ فِي الْقُرْآنِ وَخُوفُهُمْ مَّا يَزِيدُهُمْ إِلَّا طُغْيَانًا كَبِيرًا ﴿٦٠﴾

**60. Na Tulipokwambia: Hakika Mola wako Mlezi Amekwisha wazunguka hao watu. Na Hatukufanya muono (Ru'ya) Tuliokuonesha ila ni Kuwajaribu watu, na mti uliolaaniwa katika Qur'ani. Na Tunawahadharisha, lakini haiwazidishii ila uasi mkubwa kudhulumu na kutomtii Allah.**

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baari 2:615 na Muslim 2:618.

## Allah تعالى Kuwazunguka Watu na Kufanya Muono wa Mtume ni Mtihani kwao

Allah تعالى Anamuambia Mtume Wake ﷺ kwa Kumhimiza afikishe ujumbe (risala) na Kumpasha habari kuwa Atamlinda kutokana na watu. Hakika Yeye ni Muweza wa Kupambana nao na kuwa wapo Mikononi Mwake na chini ya Udhhibiti Wake.

Na amesema Mujaahid, 'Urwah bin az-Zubayr, Al-Hasan, Qataadah na wengineo katika Kauli Yake:

وَإِذْ قُلْنَا لَكَ إِنَّ رَبَّكَ أَحَاطَ بِالنَّاسِ<sup>٤</sup>

***“Na Tulipokuambia: Hakika Mola wako Mlezi Amekwisha wazunguka hao watu.”***

Maana: Atakulinda dhidi yao<sup>1</sup>. Na Kauli Yake:

وَمَا جَعَلْنَا آلَ رَأْيَا آلَئِي أَرَيْنَكَ إِلَّا فِتْنَةً لِّلنَّاسِ

***“Na Hatukufanya muono (Ru'ya) Tuliokuonesha ila ni Kuwajaribu watu”.***

Amepokea Al-Bukhari kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما:

وَمَا جَعَلْنَا آلَ رَأْيَا آلَئِي أَرَيْنَكَ إِلَّا فِتْنَةً لِّلنَّاسِ

***“Na Hatukufanya Muono (Ru'ya) Tuliokuonesha ila ni Kuwajaribu watu’,***

Akasema: ‘Hauo ni muono ambao Mtume ﷺ aliona kwa macho yake katika ile safari ya usiku (Israa’).’

وَالشَّجَرَةَ الْمَلْعُونَةَ فِي الْقُرْآنِ<sup>٤</sup>

***“Na mti uliolaaniwa katika Qur’ani”,***

Unamaanisha mti wa “Zaqquum”<sup>2</sup>.

<sup>1</sup> At-Tabari 17:479, 480.

<sup>2</sup> Fat’h Al-Baariy 8:250.

Hii pia ilinukuliwa na Ahmad, 'Abdur-Razzaaq na wengineo<sup>1</sup>. Pia imepokewa na al-'Awfiy kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما<sup>2</sup>.

Hii imefasiriwa kumaanisha usiku wa safari ya *Israa'* na Mujaahid, Sa'iid bin Jubayr, Al-Hasan, Masruuq, Ibraahim, Qataadah, Abdur-Rahman bin Zayd na wengine wengi<sup>3</sup>. Tayari tumetangulia kueleza kwa kina Hadithi kuhusu *Israa'* mwanzoni mwa Sura. Sifa zote njema Anastahiki Allah تعالى. Pia tulitaja kuwa baadhi ya Waislamu waliritadi baada ya kuufuata ukweli, kwa sababu nyoyo na akili zao hazikuweza kubeba na kufahamu hayo. Hivyo, walikataa yale ambayo elimu yao haikuweza kuelewa, lakini Allah تعالى Aliongeza na Kuimarisha Imani ya wengine. Kwa hiyo, Akasema:

إِلَّا فِتْنَةً

**"Ila ni Kuwajaribu"**, Maana: Mtihani. Ama kuhusu mti uliolaaniwa, huu ni mti wa *Zaqquum*<sup>4</sup>. Pale Mtume ﷺ alipowaambia kuwa ameiona Pepo na Moto, na kuuona mti wa *Zaqquum*, hawakumuamini, na Abu Jahl, laana ya Allah تعالى iwe juu yake, alisema: "Tuletee tende na siagi", akaanza kula huku anasema: "Wacha tule *Zaqquum*, kwani hatujui *Zaqquum* nyingine mbali na hii". Hii imepokewa na Ibn 'Abbaas, Maruzuq, Abu Maalik, Al-Hasan Al-Baswri na wengineo رضي الله عنهم. Kila alietafsiri Aya hii anasema inamaanisha usiku wa *Israa'*, pia wamefasiri kumaanisha mti wa *Zaqquum*<sup>5</sup>. Na Kauli Yake:

وَنُحُوفُهُمْ

**"Na Tunawahadharisha"**, Maana: Tunawakhofisha makafiri kwa kuwaonya, kwa kuwaeleza adhabu na mateso yanayowangojea. Hata hivyo:

فَمَا يَزِيدُهُمْ إِلَّا طُغْيَانًا كَبِيرًا ﴿٥٦﴾

**"Lakini haiwazidishii ila uasi mkubwa, kudhulumu na kutomtii Allah."**

Maana yake: Yanawasukuma wao zaidi katika ukafiri na upotevu, na hiyo ni kwa sababu ya kuachwa kwao na Allah تعالى.

<sup>1</sup> Ahmad 1:221 na 'Abdur-Razzaaq 2:380.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:481, 484.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:480, 481, 482.

<sup>4</sup> Tizama Surat Asw-Swaaffaat (37:62).

<sup>5</sup> Atw-Twabariy 17:484, 485, 486.

وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ قَالَ أَأَسْجُدُ لِمَنْ خَلَقْتَ طِينًا  
 ﴿٦١﴾ قَالَ أَرَأَيْتَكَ هَذَا الَّذِي كَرَّمْتَ عَلَيَّ لَئِنْ أُخِّرْتَنِّي إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَأَحْتَنِكَنَّ  
 ذُرِّيَّتَهُ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٦٢﴾

**61. Na pale Tulipowaambia Malaika: Msujudieni Adam. Wakamsujudia isipokuwa Iblisi. Akasema: Je! Nimsujudie uliyemuumba kwa udongo?**

**62. Akasema: Hebu nambie habari ya huyu uliyemtukuza juu yangu. Kama Ukinipa muda mpaka Siku ya Kiyama, hapana shaka nitawaangamiza kizazi chake wasipokuwa wachache tu.**

### Kisa cha Adam عليه السلام na Iblisi

Allah تعالى hapa Anataja kuhusu uadui wa Iblisi, laana ya Allah تعالى iwe juu yake, kwa Adam عليه السلام na kizazi chake. Huu ni uadui wa tangu zama za Kuumbwa kwa Adam عليه السلام, pale Allah تعالى Alipowaamuru Malaika wamsujudie Adam عليه السلام, wote walitii kwa kumsujudia ila Iblisi. Hakika yeye alitakabari na kukataa kusujudu. Alisema kwa njia ya kujikweza na kumdharau Adam عليه السلام,

﴿٦١﴾ قَالَ أَأَسْجُدُ لِمَنْ خَلَقْتَ طِينًا

**“Akasema: Je, nimsujudie uliyemuumba kwa udongo.”**

Kama Alivyosema katika Aya nyingine:

﴿٦٢﴾ أَنَا خَيْرٌ مِنْهُ خَلَقْتَنِي مِنْ نَّارٍ وَخَلَقْتَهُ مِنْ طِينٍ

**“Mimi ni bora kuliko yeye, Umeniumba kwa moto na Umemuumba kwa udongo.” (7:12)**

Na pia amesema, akizungumza na Mola Mlezi kwa kukufuru na jeuri, lakini Mola Mlezi Akamtizama katika hali ya upole:

﴿٦٢﴾ قَالَ أَرَأَيْتَكَ هَذَا الَّذِي كَرَّمْتَ عَلَيَّ

**“Akasema: Hebu nambie habari ya huyu uliyemtukuza juu yangu.”**

‘Aliy bin Abi Twalhah ameripoti kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema:



“Anasema: Nitaendelea kutawala vizazi vyake ila kidogo”. Na amesema Mujaahid: “Nitawazingira wao”. Ibn Zayd amesema (inamaanisha): “Nitawapoteza”<sup>1</sup>. Kauli zote hizo ziko karibu kwa maana, na maana ya Aya ni, “Je, wamuona huyu ambaye Umemtukuza na Kumfanya mkubwa kulikoni mimi? Ukinipatia muda, nitawapoteza vizazi vyake ila wachache.”

قَالَ أَذْهَبَ فَمَنْ تَبِعَكَ مِنْهُمْ فَإِنَّ جَهَنَّمَ جَزَاءُ مَوْفُورًا ﴿٥٦﴾ وَأَسْتَفْزِرُ مِنْ  
 أَسْتَطَعَتْ مِنْهُمْ بِصَوْتِكَ وَأَجْلَبَ عَلَيْهِمْ بِخَيْلِكَ وَرَجِلِكَ وَشَارِكِهِمْ فِي الْأَمْوَالِ وَالْأَوْلَادِ  
 وَعِدَّتِهِمْ وَمَا يَعِدُهُمُ الشَّيْطَانُ إِلَّا غُرُورًا ﴿٥٧﴾ إِنَّ عِبَادِي لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطَانٌ  
 وَكَفَىٰ بِرَبِّكَ وَكِيلًا ﴿٥٨﴾

**63. Akasema Allah: Ondokelea mbali! Atakayekufuata katika wao, basi Jahanamu itakuwa ndiyo malipo yenu, malipo ya kutimia.**

**64. Na wavute uwawezao katika wao kwa sauti yako, na wakusanyie jeshi lako la wapandao farasi na waendao kwa miguu. Na shirikiana nao katika mali na wana, na waahidi. Na Shetani hawapi ahadi ila ya udanganyifu.**

**65. Hakika waja Wangu huna mamlaka juu yao. Na Mola wako Mlezi Anatosha kuwa ni Mlinzi.**

Pale Iblisi alipoomba muda, Allah تعالى Alisema:

قَالَ أَذْهَبَ

“**Ondokea mbali**”, kwani tayari nimekupatia muda. Kulingana na Aya nyingine Allah تعالى Anasema:

قَالَ فَإِنَّكَ مِنَ الْمُنْتَضِرِينَ ﴿٨١﴾ إِلَىٰ يَوْمِ الْوَقْتِ الْمَعْلُومِ ﴿٨٢﴾

**“Allah Akamuambia: ‘Haya! Umekwisha kuwa miongoni mwa waliopewa nafasi ya kuishi. Mpaka wakati wa siku maalumu” (38:80-81).**

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 17:489.

Kisha Allah تعالى Alimuonya na wale watakaomfuata miongoni mwa dhuriya wa Wanadamu Jahanamu:

قَالَ أَذْهَبَ فَمَنْ تَبِعَكَ مِنْهُمْ فَإِنَّ جَهَنَّمَ جَزَاءُكُمْ

**“Akasema Allah: Ondokelea mbali! Atakayekufuata katika wao, basi Jahanamu itakuwa ndiyo malipo yenu.”**

Maana: Kwa amali zenu,

جَزَاءٌ مَّقْفُورًا

**“Malipo ya kutimia”.** Amesema Mujaahid: “Malipo ya kutosheleza”<sup>1</sup>. Amesema Qataadah: “Malipo mengi kwenu wala hayatapunguzwa”<sup>2</sup>. Na Kauli Yake تعالى:

وَأَسْتَفْزِرُ مَنْ أَسْتَطَعَتْ مِنْهُمْ بِصَوْتِكَ

**“Na wavute uwawezao katika wao kwa sauti yako”.**

Panasemwa: Hizo ni nyimbo. Amesema Mujaahid: “Kwa mambo ya upuuzi na nyimbo.”<sup>3</sup> Maana: kuwashawishi wao kwa wao. Na amesema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kwa Kauli Yake:

وَأَسْتَفْزِرُ مَنْ أَسْتَطَعَتْ مِنْهُمْ بِصَوْتِكَ

**“Na wachochee uwawezao katika wao kwa sauti yako’.**

Amesema: ‘Kila mlinganiaji anayewaita watu kumuasi Allah تعالى”<sup>4</sup>. Hiyo pia ndiyo iliyokuwa rai ya Qataadah<sup>5</sup> na akaichagua Ibn Jarir رحمه الله تعالى. Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَأَجَلِبْ عَلَيْهِمْ بِخَيْلِكَ وَرَجِلِكَ

**“Na wakusanyie jeshi lako la wapandao farasi na waendao kwa miguu”.**

Wakusanyie wao jeshi lako la askari farasi na miguu dhidi yao. Maana yake ni peleka kikosi chochote ulichonacho dhidi yao. Na hii ni Amri inayohusiana na Kudura ya Allah تعالى kama Alivyosema sehemu nyingine:

<sup>1</sup> At-Tabari 17:490.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:490.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:490.

<sup>4</sup> At-Tabari 17:491.

<sup>5</sup> At-Tabari 17:491.

﴿١٧﴾ أَلَمْ تَرَ أَنَا أَرْسَلْنَا الشَّيَاطِينَ عَلَى الْكَافِرِينَ تُوذُّهُمْ أَزْأًا

**“Je, huoni ya kwamba Tumewatuma mashetani juu ya makafiri, wanaowachochea kufanya mabaya?” (19:83),**

Maana yake: Kuwachochea katika kufanya maasiya. Na amesema Ibn ‘Abbaas na Mujaahid kwa Kauli Yake:

وَأَجَلِبْ عَلَيْهِم بِخَيْلِكَ وَرَجِلِكَ

**“Na wakusanyie jeshi lako la wapandao farasi na waendao kwa miguu”.**

Wakasema: Kila anayepanda (kipando) na mwenye kutembea kuelekea katika kumuasi Allah تعالى<sup>1</sup>. Na amesema Qataadah: “Hakika ana askari farasi na wa miguu miongoni mwa majini na wanadamu wanaomtii”<sup>2</sup>. Waarabu wanatumia kitendo *Ajlaba* wanapoelezea mtu anampigia kelele mwengine. Hivyo, hairuhusiwi katika mashindano kupigiana kelele baina yenu na kusukumana. Kutokana na asli hii linapatikana neno *Jalabah*, linalomaanisha kunyanyua sauti. Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَشَارِكْهُمْ فِي الْأَمْوَالِ وَالْأَوْلَادِ

**“Na shirikiana nao katika mali na wana”.** Amesema Ibn ‘Abbaas na Mujaahid: “Hii inamaanisha anayowaamuru wao kufanya katika kutumia pesa kumuasi Allah تعالى”<sup>3</sup>. Na Kauli Yake:

وَالْأَوْلَادِ

**“Na wana”**, Amesema Al-‘Awfiy kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما na Mujaahid na Adhw-Dhwahhak yaani ‘watoto wa zinaa’<sup>4</sup>. ‘Aliy bin Abi Twalhah amemnukuu Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما akisema: “Hii ina maana watoto waliokuwa wakiwaua kwa makosa, pasi na elimu.”<sup>5</sup> Qataadah رضي الله عنه amepokea kuwa Al-Hasan Al-Baswriy amesema: “Allah تعالى Amemfanya shetani achukue sehemu ya mali na watoto kwa kuwafanya wao Majusi, Mayahudi na Wakristo,

<sup>1</sup> At-Tabari 17:491, 492.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:491.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:493.

<sup>4</sup> At-Tabari 17:494.

<sup>5</sup> At-Tabari 17:495.

na kuwafanya wafuate dini nyingine yoyote isiyokuwa ya Uislamu. Pia kuwafanya watoe sehemu ya mali yao kwa shetani."<sup>1</sup> Qataadah amesema hivyo<sup>2</sup>. Wala haikuhusishwa kwa Kauli Yake:

وَشَارِكْهُمْ فِي الْأَمْوَالِ وَالْأَوْلَادِ

**"Na shirikiana nao katika mali na wana".**

Ile hakika kuwa ni mali na wana tu waliotajwa katika Aya hii, haimaanishi kuwa vimehusishwa vitu hivyo tu. Bali kila kitu ambacho kwayo mtu anamuasi Allah تعالی au kumtii shetani inamaanisha kuwa ushirika wa pamoja na shetani. Imethibiti katika Sahihi Muslim kutoka kwa 'Iyaadh bin Himaar عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ amesema:

«يَقُولُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ إِنِّي خَلَقْتُ عِبَادِي حَتَفَاءَ فَجَاءَتْهُمْ السَّيَاطِينُ فَاجْتَالَتْهُمْ عَنْ دِينِهِمْ وَحَرَّمَتْ عَلَيْهِمْ مَا أَخَلَّتْ لَهُمْ»

*"Amesema Allah Aliyetukuka: 'Hakika Mimi nimewaumba waja Wangu wakiwa Hunafaa' (wakimpwekesha Allaah), shetani aliwajia wao akawapoteza katika Dini yao na akawaharamishia Niliyowahalalishia kwao."*<sup>3</sup>

Na katika Sahihi mbili, Mtume ﷺ amesema:

«لَوْ أَنَّ أَحَدَهُمْ إِذَا أَرَادَ أَنْ يَأْتِيَ أَهْلَهُ قَالَ: بِسْمِ اللَّهِ اللَّهُمَّ جَنَّبْنَا الشَّيْطَانَ وَجَنَّبِ الشَّيْطَانَ مَا رَزَقْنَا فَإِنَّهُ إِنْ بَقِدَرَ بَيْنَهُمَا وَلَدَ فِي ذَلِكَ لَمْ يَضُرَّهُ الشَّيْطَانُ أَبَدًا»

*"Lau mmoja wao anapotaka kumjamii mkewe, akasema: 'Kwa jina la Allah! Ewe Allah tuepushe na shetani, na muepushe shetani na Ulichoturuzuku'. Hakika wanapokadiriwa baina yao mtoto hatadhuriwa na shetani milele."*<sup>4</sup> Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَعِدَّتْهُمْ وَمَا يَعِدُهُمُ الشَّيْطَانُ إِلَّا غُرُورًا

**"Na waahidi. Na Shetani hawapi ahadi ila ya udanganyifu."**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:495.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:495.

<sup>3</sup> Muslim 4:2197.

<sup>4</sup> Fat'hul al-Baariy 6: 386 na Muslim 2:1058.

Kama Alivyotupasha habari Aliyetukuka kuhusu Iblisi atakaposema pindi itakapodhihiri haki siku ya hukumu:

إِنَّ اللَّهَ وَعَدَكُمْ وَعَدَ الْحَقِّ وَوَعَدْتُكُمْ فَأَخْلَفْتُكُمْ ۗ

***“Hakika Allah Alikuahidini ahadi ya kweli, nami Nilikuahidini lakini sikukutimizieni.” (14:22).***

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

إِنَّ عِبَادِي لَيْسَ لَكَ عَلَيْهِمْ سُلْطَانٌ ۗ

***“Hakika wewe huna mamlaka juu ya waja Wangu”.***

Hapa Allah تعالی Anatueleza kuwa Anawasaidia waja Wake Waumini, Anawahifadhi na Kuwalinda kutokana na shetani aliyelaaniwa. Kwa ajili hiyo, Akasema Aliyetukuka:

وَكَفَىٰ بِرَبِّكَ وَكِيلًا ﴿٥٦﴾

***“Na Mola wako Mlezi Anatosha kuwa ni wa Kutegemewa.”***

Maana yake: Mwenye Kuhifadhi, Mlinzi, Mtegemewa na Msaidizi.

\* \* \*

رَبُّكُمْ الَّذِي يُزِيحُ لَكُمْ الْفَلَكَ فِي الْبَحْرِ لِيَتَّبِعُوا مِنْ فَضْلِهِ إِنَّهٗ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا ﴿٦٦﴾ وَإِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فِي الْبَحْرِ ضَلَّ مَنْ تَدْعُونَ إِلَّا إِلَاهُ ۗ فَلَمَّا خَجَدْتُمْ إِلَى الْإِثْرِ أَعْرَضْتُمْ ۗ وَكَانَ الْإِنْسَانُ كَفُورًا ﴿٦٧﴾ أَفَأَمِنْتُمْ أَنْ تَخْسِفَ بِكُمْ جَانِبَ الْإِثْرِ أَوْ يُرْسِلَ عَلَيْكُمْ حَاصِبًا ثُمَّ لَا تَجِدُوا لَكُمْ وُكَيْلًا ﴿٦٨﴾ أَمْ أَمِنْتُمْ أَنْ يُعِيدَكُمْ فِيهِ تَارَةً أُخْرَى فَيُرْسِلَ عَلَيْكُمْ قَاصِفًا مِنَ الرِّيحِ فَيُغْرِقَكُمْ بِمَا كَفَرْتُمْ ۗ ثُمَّ لَا تَجِدُوا لَكُمْ عَلَيْنَا بِهِ تَبِيعًا ﴿٦٩﴾ \* وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِي آدَمَ وَحَمَلْنَاهُمْ فِي الْإِثْرِ وَالْبَحْرِ وَرَزَقْنَاهُمْ مِنَ الطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَىٰ كَثِيرٍ مِمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِيلًا ﴿٧٠﴾ يَوْمَ نَدْعُوا كُلَّ أُنَاسٍ بِإِمْبِهِمْ ۗ فَمَنْ أُوتِيَ كِتَابَهُ بِيَمِينِهِ فَأُولَٰئِكَ يَقْرَءُونَ كِتَابَهُمْ وَلَا يُظْلَمُونَ فَتِيلًا ﴿٧١﴾ وَمَنْ كَانَ فِي هَذِهِ أَعْمَىٰ فَهُوَ فِي الْآخِرَةِ أَعْمَىٰ وَأَضَلُّ سَبِيلًا ﴿٧٢﴾ وَإِنْ كَادُوا لَيَفْتِنُونَكَ عَنِ الَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ لِتَفْتَرِيَ عَلَيْنَا غَيْرَهُ ۗ وَإِذَا لَا تَأْخُذُوكَ حَلِيلًا ﴿٧٣﴾ وَلَوْلَا أَنْ ثَبَّتْنَاكَ لَقَدْ كِدْتَ تَرْكُنُ إِلَيْهِمْ شَيْئًا قَلِيلًا ﴿٧٤﴾ إِذَا لَأَذْنُوكَ ضَعْفَ الْحَبِيرَةِ وَضَعْفَ الْأَمَمَاتِ ۗ ثُمَّ لَا تَجِدُ لَكَ عَلَيْنَا نَصِيرًا ﴿٧٥﴾

رَبُّكُمْ الَّذِي يُزِيحُ لَكُمْ الْفَلَكَ فِي الْبَحْرِ لِيَتَّبِعُوا مِنْ فَضْلِهِ إِنَّهٗ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا ﴿٦٦﴾

**66. Mola wenu Mlezi Ndiye Anayekuendesheeni marikebu katika bahari ili mtafute katika Fadhila Zake. Hakika Yeye ni Mwenye Kukurehemuni nyinyi.**

**Marikebu ni katika Ishara za Rehema ya Allah** تعالی

Allah تعالی Anatuarifu kuhusu ukarimu na wema Wake kwa waja Wake kwa kuwasahilishia marikebu baharini.

Anawafanyia wepesi kutumia marikebu kukidhi maslahi na mahitaji yao, huku wakitafuta fadhila Zake kwa kufanya biashara baina ya sehemu moja na nyengine. Anasema Aliye-tukuka:

إِنَّهٗ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا ﴿٦٦﴾

**“Hakika Yeye ni Mwenye Kukurehemuni nyinyi.”**

Maana yake: Anawafanyia haya kwa Ukarimu, Rehema na Huruma Yake kwenu.

وَإِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فِي الْبَحْرِ ضَلَّ مَنْ تَدْعُونَ إِلَّا إِلَهُهُ ۗ فَلَمَّا جَنَّكُمْ إِلَى الْعَبْرِ أَعْرَضْتُمْ ۗ وَكَانَ

الْإِنْسَانُ كَفُورًا ﴿٦٦﴾

**67. Na inapokufikieni taabu katika bahari, hao mnaowaomba wanapotea, isipokuwa Yeye tu. Na Anapokuvueni mkafika nchi kavu, mnageuka. Ama mwanadamu ni mwingi wa kukanusha.**

**Wanapofikiwa na Taabu, Wasioamini Hawamkumbuki Yeyote ila Allah** تعالی

Allah تعالی Anatuarifu kuwa pindi taabu inapowafikia wanadamu, wanamuita Yeye tu, kwa kurudi Kwake na kumuomba Yeye kwa ikhlasi. Hivyo, Allah تعالی Akasema:

وَإِذَا مَسَّكُمُ الضُّرُّ فِي الْبَحْرِ ضَلَّ مَنْ تَدْعُونَ إِلَّا إِلَهُهُ ۗ

**“Na inapokufikieni taabu katika bahari, hao mnaowaomba wanapotea, isipokuwa Yeye tu.”**

Maana: Kila walichokuwa wakiabudu mbali na Allah تعالی kinapotea kutoka nyoyoni na akilini mwao. 'Ikrimah bin Abi Jahl alifikiwa na jambo kama hilo alipomkimbua Mtume ﷺ huku akielekea Ethiopia baada ya kutekwa Makka. Hata hivyo, alikumbwa na kimbunga kikali kuwafanya watu waambizane: “Hakuna anayeweza kukuokoeni ila Allah تعالی Pekee”. 'Ikrimah akasema moyoni: “Naapa kwa Allah تعالی, ikiwa hakuna anayeweza kukuokoa baharini ila Allah تعالی, bila shaka pia hakuna anayeweza kukuokoa ardhini ila Allah تعالی. Ee Allah تعالی! Nakuahidi kuwa lau Utaniokoa katika hili na kunipeleka salama (kwenye ardhi), nitakwenda kumbai Muhammad, na bila shaka nitampata akiwa amejawa na huruma, ukarimu na rehema.” Walitoka katika msukosuko huo baharini salama salimini. Kisha 'Ikrimah alikwenda kwa Mtume ﷺ na kusilimu. Baada ya hapo akawa Muislamu mzuri, Allah تعالی Amuwie radhi<sup>1</sup>. Anasema Aliyetukuka:

فَلَمَّا جَنَّكُمْ إِلَى الْعَبْرِ أَعْرَضْتُمْ

**“Na Anapokuvueni mkafika nchi kavu, mnageuka.”** Maana yake: Mnasahau mliyoyakumbuka ya kumpwekesha Allah تعالی mlipokuwa baharini, na mnakengeuka katika kumuomba Yeye tu bila ya kumshirikisha.

<sup>1</sup> Al-Haakim 3:241.

وَكَانَ الْإِنْسَانُ كُفُورًا ﴿١٧﴾

**“Ama mwanadamu ni mwingi wa kukanusha.”** Maana yake: kimaumbile ni mwenye kusahau na kukataa Fadhila za Allah تعالى, isipokuwa wale waliohifadhiwa na Allah تعالى.

أَفَأَمِنْتُمْ أَنْ تَخْشِفَ بِكُمْ جَانِبَ الْبَرِّ أَوْ يُرْسِلَ عَلَيْكُمْ حَاصِبًا ثُمَّ لَا تَجِدُوا لَكُمْ

وَكَيْلًا ﴿١٨﴾

**68. Je! Mumeaminisha ya kuwa Hataku didimizeni upande wowote katika nchi kavu, au kwamba Hataku leteeni tufani la kokoto? Kisha msipate Mlinzi.**

Je, Hakuna Adhabu ya Allah تعالى Itakayokuja Duniani?

Allah تعالى Anasema, je mnadhani kwa kufika kwenye nchi kavu mtakuwa salama kutokana na kisasi na adhabu ya Allah تعالى.

أَفَأَمِنْتُمْ أَنْ تَخْشِفَ بِكُمْ جَانِبَ الْبَرِّ أَوْ يُرْسِلَ عَلَيْكُمْ حَاصِبًا

**“Je! Mumeaminisha ya kuwa Hataku didimizeni upande wowote katika nchi kavu, au kwamba Hataku leteeni tufani la kokoto?”**

Haasib – Aina ya mvua yenye kokoto? Hii ni kauli na rai ya Mujaahid na wengineo<sup>1</sup>. Kama Alivyosema Allah تعالى:

إِنَّا أَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ حَاصِبًا إِلَّا آلَ لُوطٍ لَّوَطٍ كُفَيْتُمْ بِسِحْرِ ۞ نِعْمَةٌ مِّنْ عِنْدِنَا

**“Hakika Sisi Tukawapelekea kimbunga cha vijiwe, isipokuwa wafuasi wa Lutw. Hao Tuliwaokoa karibu na alfajiri. Kwa neema inayotoka Kwetu.” (54:34-35).**

Anasema Allah تعالى katika sehemu nyingine:

وَأَمْطَرْنَا عَلَيْهَا حِجَابًا مِّنْ سَجِيلٍ مَّنْضُوبٍ ﴿١٩﴾

**“Na Tukawateremshia mvua ya changarawe za udongo mgumu uliokamatana wa Motoni.” (11:82).** Aidha, Amesema tena,

<sup>1</sup> At-Tabari 17:498, kutoka kwa Qataadah.



ءَأَمِنْتُمْ مِّن فِي السَّمَاءِ أَن تَخْسِفَ بِكُمْ الْأَرْضَ فَإِذَا هِيَ تَمُورُ ﴿٦٦﴾ أَمْ أَمِنْتُمْ مِّن فِي  
السَّمَاءِ أَن يُرْسِلَ عَلَيْكُمْ حَاصِبًا ۗ فَسَتَعْلَمُونَ كَيْفَ نَذِيرِ ﴿٦٧﴾

**“Mnadhani mko salama kwa Alioko juu kuwa Hataku didimizeni kwenye ardhi, na tahamaki hiyo inatikisika! Au mnadhani mko salama kwa Alioko juu ya kuwa Yeye Hakupelekeeni kimbunga chenye changarawe? Mtajua vipi maonyo yangu?” (67:16-17).**

ثُمَّ لَا تَجِدُوا لَكُمْ وَكَيلًا ﴿٦٨﴾

**“Kisha msipate wa kumtegemea.”** Maana yake: Msaidizi wa Kukuondoshea adhabu na Kukuokoa.

أَمْ أَمِنْتُمْ أَن يُعِيدَكُمْ فِيهِ تَارَةً أُخْرَىٰ ۖ فَيُرْسِلَ عَلَيْكُمْ قَاصِفًا مِّن الرِّيحِ فَيُغْرِقَكُم بِمَا  
كَفَرْتُمْ ۗ ثُمَّ لَا تَجِدُوا لَكُمْ عَلَيْنَا بِهِ تَبِيعًا ﴿٦٩﴾

**69. Au mmeaminisha ya kuwa Hatakurudisheni humo mara nyengine na Kukupelekeeni kimbunga cha upepo Akakuzamisheni kwa mlivyo kufuru, na kisha msipate wa Kukunusuruni Nasi.**

**Allah تعالیٰ Ana Uwezo wa Kuwarudisha Baharini**

Allah تعالیٰ Anasema:

أَمْ أَمِنْتُمْ

**“Au mmeaminisha.”** Enyi mnaokengeuka mbali na Sisi baada ya kutambua Upweke Wetu baharini pindi mnapofika nchi kavu.

أَن يُعِيدَكُم

**“Ya kuwa Hatakurudisheni humo mara nyengine.”** Maana: Baharini mara ya pili. Anasema Aliyetukuka:

فَيُرْسِلَ عَلَيْكُمْ قَاصِفًا مِّن الرِّيحِ

**“Na Kukupelekeeni kimbunga cha upepo.”** Kitakachoharibu milingoti na kuzamisha vyombo vyenu (marikebu, meli, dau, na kadhalika). Ibn ‘Abbaas na wengineo رضي الله عنهم wamesema: “Al-Qaasif ni upepo wa bahari unaoharibu vyombo vya usafiri na kuvizamisha”<sup>1</sup>. Hivyo,

<sup>1</sup> At-Tabari 17:500.

فَيَغْرِقْكُمْ بِمَا كَفَرْتُمْ<sup>١</sup>

**“Akakuzamisheni kwa mlivyokufuru.”**

Maana yake: Kwa sababu ya kukufuru, kukanusha na kukengeuka kwa yaliyokuja kutoka kwa Allah تعالى. Hatima yake,

ثُمَّ لَا تَجِدُوا لَكُمْ عَلَيْنَا بِهِ تَبِيعًا ﴿٦٦﴾

**“Na kisha msipate wa kukunusuruni Nasi.”**

Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema kuwa hiyo inamaanisha msaidizi<sup>1</sup>. Mujaahid amesema: “Msaidizi atakayelipa kisasi (Maana: mwenye kuchukua kisasi kwa niaba yako)”<sup>2</sup>. Na Qatadah amesema inamaanisha, “Hatuogopi kuwa yeyote yule Atatufuata na chochote cha kisasi.”<sup>3</sup>

\* وَلَقَدْ كَرَّمْنَا بَنِي آدَمَ وَحَمَلْنَاهُمْ فِي الْوُجُوهِ وَالْبَحْرِ وَرَزَقْنَاهُمْ مِنَ الطَّيِّبَاتِ وَفَضَّلْنَاهُمْ

عَلَى كَثِيرٍ مِّمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِيلًا ﴿٧٠﴾

**70. Na hakika Tumewatukuza wanadamu, na Tumewapa vya kupanda nchi kavu na baharini, na Tumewaruzuku vitu vizuri vizuri, na Tumewatukuza kuliko wengi miongoni mwa Tuliowaumba kwa utukufu ulio mkubwa kabisa.**

### Utukufu wa Kimaumbile wa Mwanadamu

Allah تعالى Anatarifu kuwa Amewatukuza wana wa Adam na Kuwapatia hadhi kwa Kuwaumba katika hali iliyo bora kabisa, kama Alivyosema:

لَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ فِي أَحْسَنِ تَقْوِيمٍ ﴿٧٠﴾

**“Bila ya shaka Tumemuumba mtu kwa umbo lilio bora kabisa.” (95:4).**

Anatembea wima kwa miguu yake miwili na kula kwa mkono wake, ilhali viumbe vyengine vinatembea kwa miguu minne na kula na midomo yao. Na hakika

<sup>1</sup> At-Tabari 17:500.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:500.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:500.

Amempa yeye masikio, macho na moyo wa kuweza kuelewa na kufahamu yote hayo, ili kufaidika nayo na kutofautisha baina ya vitu – vizuri na vibaya, katika masuala ya hapa duniani na ya kidini. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَحَمَلْنَهُمْ فِي الْوَجْدِ

**“Na Tumewapa vya kupanda nchi kavu.”**

Maana yake: Juu ya wanyama kama ng’ombe, farasi na nyumbu, na pia baharini kwa kutumia marikebu na mashua, kubwa na ndogo. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَرَزَقْنَهُمْ مِنَ الطَّيِّبَاتِ

**“Na Tumewaruzuku vitu vizuri vizuri.”**

Maana yake: Mazao ya kilimo, matunda, nyama na maziwa yenye utamu, rangi na mandhari aina tofauti. Pia nguo nzuri zenye rangi na vipimo tofauti, wanaojitengezea wenyewe au wananunuliwa na wengine kutoka sehemu nyengine. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَفَضَّلْنَاهُمْ عَلَىٰ كَثِيرٍ مِّمَّنْ خَلَقْنَا تَفْضِيلًا

**“Na Tumewatukuza kuliko wengi miongoni mwa Tuliowaumba kwa utukufu ulio mkubwa kabisa.”**

Maana yake: Juu ya viumbe hai vyote na aina nyengine ya viumbe. Ayah hii inatuashiria kuwa wanadamu wamefadhilishwa zaidi kuliko Malaika.

يَوْمَ نَدْعُوا كُلَّ أُنَاسٍ بِإِسْمِهِمْ ۗ فَمَنْ أُوتِيَ كِتَابَهُ بِيَمِينِهِ فَأُولَٰئِكَ يَقْرَءُونَ

كِتَابَهُمْ وَلَا يُظْلَمُونَ فَتِيلًا ﴿٧١﴾ وَمَنْ كَانَتْ فِي يَدَيْهِ أَعْمَىٰ فَهُوَ فِي الْآخِرَةِ أَعْمَىٰ

وَأَضَلُّ سَبِيلًا ﴿٧٢﴾

**71. Siku Tutapowaita kila kikundi cha watu kwa mujibu wa kitabu wakifuatacho - basi atakayepewa kitabu chake kwa mkono wake wa kulia, basi hao watasoma kitabu chao wala hawatadhulumiwa hata chembe.**

**72. Na aliyekuwa kipofu katika hii dunia, basi atakuwa kipofu Akhera, na atakuwa aliyeipotea zaidi njia.**

### Kila Mmoja Ataitwa na *Imaam* wake Siku ya Kufufuliwa (Kiyama)

Allah تعالى Anatuambia kuwa Siku ya Kiyama, Atawaita kila watu kwa hesabu na *Imaam* wake. Wanazuoni wametofautiana kuhusu maana ya Aya hii (yaani *Imaam*). Mujaahid na Qataadah wamesema: Inamaanisha kuwa kila taifa litaitwa kwa hesabu na Mtume wao. Baadhi ya watangu (*Salaḥ*) wema wamesema kuwa huu ni utukufu mkubwa kwa watu wa Hadithi, kwa sababu *Imaam* (kiongozi) wao ni Mtume Muhammad ﷺ.

Ibn Zayd amesema: "Ina maana huenda wakaitwa kwa hesabu kwa Kitabu chao kilichoteremshwa kwa Nabii wao pamoja na Sheria zao."

Hii ndiyo rai iliyochaguliwa na Ibn Jariir. Amesimulia Ibn Abi Najih kuwa Mujaahid amesema: "Pamoja na Vitabu vyao". Huenda ikawa kilichomaanishwa hapa ni ule upokezi wa Al-Awfi kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kuhusu Aya hii,

يَوْمَ نَدْعُوا كُلَّ أُنَاسٍ بِإِمَّتِهِمْ

**"Siku Tutapowaita kila kikundi cha watu kwa mujibu wa kitabu wakifuatacho."**

Maana yake: Kinahusishwa Kitabu (au kumbukumbu) cha amali zao<sup>1</sup>. Hii pia ndiyo rai ya Abu Al-Aaliyah, al-Hasan na Adhw-Dhwahhaak<sup>2</sup>.

Rai hii ndio sahihi zaidi, kwa sababu Allah تعالى Anasema:

وَكُلُّ شَيْءٍ أَحْصَيْنَاهُ فِي إِمَامٍ مُّبِينٍ ﴿٣٦﴾

**"Na kila kitu Tumekihifadhi katika daftari asli lenye kubainisha." (36:12).**

Na pia,

وَوُضِعَ الْكِتَابُ فَتَرَى الْمُجْرِمِينَ مُشْفِقِينَ مِمَّا فِيهِ

**"Na kitawekwa Kitabu. Basi utawaona wakosefu wanavyoogopa kwa yale yaliomo humo." (18:49)**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:502.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:502, 503.

وَتَرَى كُلَّ أُمَّةٍ جَائِيَةً كُلُّ أُمَّةٍ تُدْعَى إِلَى كِتَابِهَا الْيَوْمَ تُجْزَوْنَ مَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٦٦﴾ هَذَا  
 كِتَابُنَا يَنْطِقُ عَلَيْكُمْ بِالْحَقِّ إِنَّا كُنَّا نَسْتَنسِخُ مَا كُنتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٦٧﴾

***“Na utauona kila umma umepiga magoti, na kila umma utaitwa kwenda soma Kitabu chake: Leo mtalipwa muliyokuwa mukiyatenda. Hichi Kitabu chetu kinasema juu yenu kwa haki. Hakika Sisi Tulikuwa Tukiyaandika muliyokuwa mukiyatenda.”***  
 (45:28-29)

Hii haipingani na ile hakika kuwa Mtume ﷺ ataletwa mbele pindi Allah تعالى Atakapokuwa Anahukumu baina ya Umma wake, kwani yeye atakuwa ni shahidi dhidi ya Umma wake kwa amali zao. Kinachokusudiwa hapa kwa *Imaam* ni kitabu katika neno amali. Allah تعالى Anasema:

يَوْمَ نَدْعُوا كُلَّ أُنَاسٍ بِإِمْئِهِمْ فَمَنْ أُوْتِيَ كِتَابَهُ بِيَمِينِهِ فَأُولَئِكَ يَقْرَءُونَ  
 كِتَابَهُمْ

***“Siku Tutapowaita kila kikundi cha watu kwa mujibu wa wakifuatacho - basi atakayepewa kitabu chake kwa mkono wake wa kulia, basi hao watasoma kitabu chao.”***

Maana yake: Kwa ajili ya furaha yao kwa yale yaliyoandikwa ndani yake katika amali njema – watakisoma na watapenda kukisoma.

Hii ni kama Kauli Yake Aliyetukuka:

فَأَمَّا مَنْ أُوْتِيَ كِتَابَهُ بِيَمِينِهِ فَيَقُولُ هَذَا مَا أقرَأُ وَكُنْتُمْ تَكْتُمُونَ ﴿٦٨﴾

***“Basi ama yule atakayepewa daftari lake kwa mkono wake wa kuume atasema: ‘Haya! Someni daftari langu.’”***

Mpaka katika Kauli Yake Aliyetukuka:

وَأَمَّا مَنْ أُوْتِيَ كِتَابَهُ بِشِمَالِهِ

***“Walakini atakayepewa daftari lake kwa mkono wake wa kushoto.”*** (69:19-29)

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَلَا يُظَلِّمُونَ فَتِيلًا ﴿٦٦﴾

**“Wala hawatadhulumiwa hata chembe (ya uzi katika kokwa ya tende)”.**

Tumetangulia kutaja kuwa *Fatil* ni uzi mrefu uliopo katika mpasuko wa kokwa ya Tende. Al-Haafidh Abu Bakr Al-Bazaar رحمه الله تعالى amenukuu Hadithi kutoka kwa Abu Hurayrah عنه رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema kuhusiana na Aya hii,

يَوْمَ نَدْعُوا كُلَّ أُنَاسٍ بِإِيمَانِهِمْ

**“Siku Tutapowaita kila kikundi cha watu kwa mujibu wa kitabu wakifuatacho”.**

Akasema:

يُدْعَىٰ أَحَدُهُمْ فَيُعْطَىٰ كِتَابَهُ بِيَمِينِهِ، وَيُمَدُّ لَهُ فِي جَسَدِهِ، وَيَبْيَضُّ وَجْهُهُ، وَيُجْعَلُ عَلَىٰ رَأْسِهِ تَاجٌ مِنْ لَوْلُؤَةٍ يَتَلَاوَأُ، فَيَنْطَلِقُ إِلَىٰ أَصْحَابِهِ فَيَرَوْنَهُ مِنْ بَعِيدٍ، فَيَقُولُونَ: اللَّهُمَّ آتِنَا بِهَذَا، وَبَارِكْ لَنَا فِي هَذَا، فَيَأْتِيهِمْ فَيَقُولُ لَهُمْ: أَبْشِرُوا فَإِنَّ لِكُلِّ رَجُلٍ مِنْكُمْ مِثْلَ هَذَا، وَأَمَّا الْكَافِرُ فَيَسْوَدُ وَجْهُهُ، وَيُمَدُّ لَهُ فِي جَسَدِهِ، وَيَرَاهُ أَصْحَابُهُ فَيَقُولُونَ: نَعُوذُ بِاللَّهِ مِنْ هَذَا، أَوْ مِنْ شَرِّ هَذَا اللَّهُمَّ لَا تَأْتِنَا بِهِ فَيَأْتِيهِمْ فَيَقُولُونَ: اللَّهُمَّ أَخْرِهِ. فَيَقُولُ: أَبْعَدْكُمْ اللَّهُ فَإِنَّ لِكُلِّ رَجُلٍ مِنْكُمْ مِثْلَ هَذَا

*“Mmoja wenu ataitwa na kupatiwa Kitabu chake kwa mkono wake wa kuume. Atakuwa katika hali nzuri ya kimaumbile na uso wake utang'ara (mweupe), na atavikwa kichwani mwake taji la lulu inayo metameta. Atakwenda kwa sahibu wake, nao watamuona kutoka mbali, nao watasema: 'Ewe Allah! Tupe sisi na Utubariki katika hili'. Kisha atakuja kwao na kuwaambia: 'Pateni bishara njema, kwani kwa kila mtu miongoni mwenu atapata kama hii'. Ama kwa kafiri, uso wake utakuwa mweusi na mwili wake utafura. Sahibu wake watamuona kutoka mbali, nao watasema, 'Tunajilinda kwa Allah kutokana na hili, au kwa shari ya huyu. Ewe Allah! Usitupe sisi hilo'. Kisha atakuja kwao, nao watasema: 'Ewe Allah! Mdhaliishe'.*

Atasema: 'Allah Awaweke mbali, kila mmoja miongoni mwenu apate kama hivi'<sup>1</sup>.

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَمَنْ كَانَتْ فِي هَدِيمَةٍ أَعْمَىٰ

**"Na aliyekuwa hapa kipofu."**

Ibn 'Abbaas, Mujaahid, Qataadah na Ibn Zayd wamesema kuwa hii inamaanisha katika maisha ya hapa duniani.

أَعْمَىٰ

**"Kipofu."**

Maana yake: Kuwa na upofu kwa ishara, dalili, miujiza na ubainifu kutoka kwa Allah تعالى. Na Kauli Yake:

فَهُوَ فِي الْآخِرَةِ أَعْمَىٰ

**"Basi atakuwa kipofu Akhera."**

Kwa kuwa alikuwa kipofu katika maisha ya hapa, duniani na huko pia atakuwa katika hali hiyo. Aya inamalizikia:

وَأَضَلُّ سَبِيلًا ﴿٧٦﴾

**"Na atakuwa aliyeipotea zaidi njia."**

Maana yake: Atapotea zaidi kama alivyokuwa katika dunia hii. Tunajilinda kwa Allah تعالى kutokana na hilo<sup>1</sup>.

وَإِنْ كَادُوا لَيَفْتِنُونَكَ عَنِ الَّذِي أُوحِيَٰنَا إِلَيْكَ لِتَفْتَرِيَ عَلَيْنَا غَيْرَهُ ۗ وَإِذَا لَا تَأْخُذُوكَ

خَلِيلًا ﴿٧٧﴾ وَلَوْلَا أَنْ ثَبَّتْنَاكَ لَقَدْ كِدْتَ تَرْكَنُ إِلَيْهِمْ شَيْئًا قَلِيلًا ﴿٧٨﴾ إِذَا لَأُدْقَنَّكَ

ضِعْفَ الْحَيَوةِ وَضِعْفَ الْمَمَاتِ ثُمَّ لَا تَجِدُ لَكَ عَلَيْنَا نَصِيرًا ﴿٧٩﴾

<sup>1</sup> Mawaarid Adh-Dhamaan 2588, Sahiih Ibn Hibbaan 7349 na Sunan at-Tirmidhiy 3136.

**73. Na hakika walikaribia kukushawishi uache Tuli yokufunulia ili utuzulie mengineyo. Na hapo ndio wangelikufanya rafiki.**

**74. Na lau kuwa hatukukuweka imara ungelikaribia kuwaelekea kidogo.**

**75. Hapo basi bila ya shaka Tungelikuonjesha adhabu maradufu ya uhai, na adhabu maradufu ya kifo. Kisha usingepata mtu wa kukunusuru nasi.**

### **Adhabu kwa Mtume ﷺ Kama Angekubali Japo Kidogo Maombi ya Makafiri katika Kubadilisha Wahyi.**

Allah تعالی Anatupasha habari Alivyomsaidia Mtume Wake ﷺ, pia Kumlinda, Kumpatia msimamo na usalama dhidi ya vitimbi vibaya vya waovu, waliokengeuka. Allah تعالی Ndiye wa Pekee Aliyemsimamia mambo yake na Kumsaidia, na Hakumuacha kabisa kwa yeyote miongoni mwa viumbe Vyake. Bali Yeye Ndiye Mlinzi wake, Mwenye Kumhifadhi, Msaidizi wake, wa Pekee wa Kumsaidia Kupata ushindi na Kuifanya Dini yake kudhihiri dhidi ya wanaompinga na kumpiga vita, mashariki na magharibi ya ardhi, amani na baraka za Allah تعالی ziwe juu yake mpaka Siku ya Malipo.




---

<sup>1</sup> At-Tabari 17:504, 505.



وَإِن كَادُوا لَيَسْتَفِزُّوكَ مِنَ  
 الْأَرْضِ لِيُخْرِجُوكَ مِنْهَا <sup>ط</sup>  
 وَإِذَا لَا يَلْبُثُونَ خِلْفَكَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٧٦﴾ سُنَّةَ مَنْ قَدْ  
 أَرْسَلْنَا قَبْلَكَ مِنْ رُسُلِنَا <sup>ط</sup> وَلَا تَجِدُ لِسُنَّتِنَا تَحْوِيلًا ﴿٧٧﴾  
 أَمِرِ الصَّلَاةَ لِذُلُوكِ الشَّمْسِ إِلَى غَسَقِ اللَّيْلِ وَقُرْآنَ الْفَجْرِ  
 إِنَّ قُرْآنَ الْفَجْرِ كَانَ مَشْهُودًا ﴿٧٨﴾ وَمِنَ اللَّيْلِ فَتَهَجَّدْ  
 بِهِ نَافِلَةً لَكَ عَسَىٰ أَنْ يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُودًا ﴿٧٩﴾  
 وَقُلْ رَبِّ أَدْخِلْنِي مُدْخَلَ صِدْقٍ وَأَخْرِجْنِي مَخْرَجَ صِدْقٍ  
 وَأَجْعَلْ لِي مِنْ لَدُنْكَ سُلْطَانًا نَصِيرًا ﴿٨٠﴾ وَقُلْ جَاءَ الْحَقُّ  
 وَزَهَقَ الْبَاطِلُ <sup>ع</sup> إِنَّ الْبَاطِلَ كَانَ زَهُوقًا ﴿٨١﴾ وَنُنزِّلُ مِنَ  
 الْقُرْآنِ مَا هُوَ شِفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ <sup>ط</sup> وَلَا يَزِيدُ الظَّالِمِينَ  
 إِلَّا خَسَارًا ﴿٨٢﴾ وَإِذَا أَنْعَمْنَا عَلَى الْإِنْسَانِ أَعْرَضَ وَنَسَا  
 بِنَانِهِ <sup>ط</sup> وَإِذَا مَسَّهُ الشُّرُّ كَانَ يَئُوسًا ﴿٨٣﴾ قُلْ كُلُّ  
 يَعْمَلُ عَلَى شَاكِلَتِهِ فَرَبُّكُمْ أَعْلَمُ بِمَنْ هُوَ أَهْدَى سَبِيلًا  
 ﴿٨٤﴾ وَيَسْأَلُونَكَ عَنِ الرُّوحِ <sup>ط</sup> قُلِ الرُّوحُ مِنْ أَمْرِ رَبِّي وَمَا  
 أُوتِيتُمْ مِنَ الْعِلْمِ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٨٥﴾

وَإِن كَادُوا لَيَسْتَفِزُّوكَ مِنَ  
 الْأَرْضِ لِيُخْرِجُوكَ مِنْهَا <sup>ط</sup> وَإِذَا لَا  
 يَلْبُثُونَ خِلْفَكَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٧٦﴾  
 سُنَّةَ مَنْ قَدْ أَرْسَلْنَا قَبْلَكَ مِنْ  
 رُسُلِنَا <sup>ط</sup> وَلَا تَجِدُ لِسُنَّتِنَا تَحْوِيلًا ﴿٧٧﴾

**76. Na kwa hakika walikaribia kukufukuza nchi ili wakutoe humo. Na wasingalika baada yako ila kwa muda mchache tu.**

**77. Ndio desturi ya wale Tuliowatuma kabla yako katika Mitume Wetu. Wala hutapata mabadiliko katika desturi Yetu.**

**Sababu ya Kuteremshwa kwa Aya Hizi**

Aya Hii iliteremshwa kuhusu makafiri wa Quraysh, walipotaka kumfukuza Mtume ﷺ baina yao. Hivyo, Allah تعالی alitoa

onyo katika Aya hii, Akiwaambia kuwa lau watamfukuza, hawatakaa katika mji wa Makka kwa muda mrefu baada ya hapo. Na hivi ndivyo ilivyotokea baada ya kuhama kwao kutoka Makka pale mateso yalipozidi maradufu. Baada ya mwaka na nusu tu, Allah تعالی Aliwaleta pamoja katika uwanja wa vita wa Badr bila maagano yoyote, Akamfanya mwenye kuwashinda, hivyo kuwaua viongozi wao na kuwachukua mateka familia zao. Kwa hiyo, Allah تعالی Akasema:

سُنَّةَ مَنْ قَدْ أَرْسَلْنَا قَبْلَكَ مِنْ رُسُلِنَا<sup>ط</sup>

**“Ndio desturi ya wale Tuliowatuma kabla yako katika Mitume Wetu.”**

Maana yake: Haya ndiyo Tunayofanya kwa kawaida kwa wale wanaokataa Mitume Wetu na kuwatesa kwa kuwatoa Manabii miongoni mwao – adhabu inakuja kwao. Lau si kwa ile hakika kuwa Mtume ﷺ, ni wa rehema, adhabu na kisasi kingekuwa kwao kwa jinsi ambayo hakijawahi kuonekana kabla duniani. Hivyo, Allah تعالى Akasema:

وَمَا كَانَتْ أَلَّهُ لِيُعَذِّبَهُمْ وَأَنْتَ فِيهِمْ<sup>ع</sup>

**“Lakini Allah hakuwa wa Kuwaadhibu maadamu wewe (Nabii Muhammad) umo pamoja nao.” (8:33)**

أَقْرِ الصَّلَاةَ لِذُلُوكِ الشَّمْسِ إِلَى غَسَقِ اللَّيْلِ وَقُرْءَانَ الْفَجْرِ إِنَّ قُرْءَانَ الْفَجْرِ كَانَ  
مَشْهُودًا ﴿٧٨﴾ وَمِنَ اللَّيْلِ فَتَهَجَّدْ بِهِ نَافِلَةً لَكَ عَسَىٰ أَنْ يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَحْمُودًا

**78. Shika Sala jua linapopinduka mpaka giza la usiku, na Qur’ani ya Alfajiri. Hakika Qur’ani ya Alfajiri inashuhudiwa daima.**

**79. Na amka usiku kwa ibada; ni ziada ya Sunnah khasa kwako wewe. Huenda Mola wako Mlezi Akakunyanyua cheo kinachosifika.**

### **Amri ya Kusimamisha Sala katika Nyakati Zake Maalumu**

Allah تعالى Anasema Kumuamrisha Mtume Wake ﷺ kusimamisha Sala za faradhi kwa nyakati zake maalumu zilizowekwa:

أَقْرِ الصَّلَاةَ لِذُلُوكِ الشَّمْسِ

**“Shika Sala jua linapopinduka.”**

Amepokea Hushaym kutoka kwa Mughirah kutoka kwa Ash-Sha'biy kutoka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما: “Mchana yaani ni pale jua linapopinduka.”<sup>1</sup>

<sup>1</sup> At-Tabari 17:514.

Hii pia imepokewa na Naafi'iy kutoka kwa Ibn 'Umar رضي الله عنهما<sup>1</sup>, na kutoka kwa Maalik katika Tafsiri yake kutoka kwa Az-Zuhri kutoka kwa Ibn 'Umar رضي الله عنهما<sup>2</sup>. Hii pia ndio kauli na rai ya Abu Barzah Al-Aslamiy na Mujaahid, na Al-Hasan, Adh-dhahaak, Abu Ja'far al-Baaqir na Qataadah<sup>3</sup>.

Na inashuhudiwa hilo kwa aliyopokea Ibn Jariir رحمه الله تعالى kutoka kwa Jaabir bin 'Abdallah رضي الله عنه aliyesema: "Nilimualika Mtume ﷺ na anayewataka katika Masahaba wake, wakala kwangu, kisha wakatoka baada ya jua kupinduka. Akatoka Mtume ﷺ akasema: 'Toka, Ewe Abubakar'. Hii ni pale jua lilipopinduka."<sup>4</sup>

Kwa hiyo Aya hii inaingia katika nyakati za Sala tano. Na kwa Kauli Yake:

لِدُلُوكِ الشَّمْسِ إِلَىٰ عَسْقِ اللَّيْلِ

***"Jua linapopinduka mpaka giza la usiku."***

Kumaanisha kiza, au ilisemekana, machweo. Hii ilifahamika kumaanisha Dhuhr, 'Asr, Maghrib na 'Ishaa'. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَقُرْءَانَ الْفَجْرِ

***"Na Qur'ani ya Alfajiri."***

Maana: Sala ya Alfajiri. Sunna ya Mtume ﷺ imethibitisha kwa riwaya zilizopokewa na wengi (*Tawaatur*), kwa matendo yake ﷺ na kauli zake kwa kina kuhusu nyakati hizi kama walivyo Waislamu juu ya hilo leo. Wamelipokea hilo Waislamu wa leo kutoka kwa wale wa zamani, kizazi baada ya kizazi na karne baada ya karne kama ilivyotajwa mahali pake munasibu, sifa zote njema Anastahiki Allah تعالى tu.

<sup>1</sup> At-Tabari 17:515.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:515.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:515, 516.

<sup>4</sup> At-Tabraaniy 17:518. Ndani yake yupo mtu ambaye jina lake halikutajwa na mwengine ni dhaifu lakini asili ya kisa kimepokewa katika Sahihi mbili na wengineo.

## Kujumuika Malaika katika Sala ya Alfajiri na Alasiri

إِنَّ قُرْءَانَ الْفَجْرِ كَانَ مَشْهُودًا ﴿١٧٦﴾

**“Hakika Qur’ani ya Alfajiri inashuhudiwa daima”.**

Imepokewa na Ibn Mas’ud na Abu Hurayrah رضي الله عنهما kuwa Mtume ﷺ amesema yafuatayo kuhusu Aya hii:

وَقُرْءَانَ الْفَجْرِ إِنَّ قُرْءَانَ الْفَجْرِ كَانَ مَشْهُودًا ﴿١٧٦﴾

**“Na Qur’an ya Alfajiri: Hakika Qur’ani ya Alfajiri inashuhudiwa daima’.** Akasema:

«تَشْهَدُهُ مَلَائِكَةُ اللَّيْلِ وَمَلَائِكَةُ النَّهَارِ»

*‘Inashuhudiwa na Malaika wa usiku na mchana’<sup>1</sup>”.*

Amepokea Al-Bukhaariy kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«فَضْلُ صَلَاةِ الْجَمِيعِ عَلَى صَلَاةِ الْوَاحِدِ خَمْسٌ وَعِشْرُونَ دَرَجَةً، وَتَجْتَمِعُ مَلَائِكَةُ اللَّيْلِ وَمَلَائِكَةُ النَّهَارِ فِي صَلَاةِ الْفَجْرِ»

*“Fadhila (ubora) ya Sala ya jamaa juu ya Sala ya mtu binafsi (peke yake), ni daraja ishirini na tano (25), ‘Na wanajumuika Malaika wa usiku na mchana katika Sala ya Alfajiri’”.*

Abu Hurayrah رضي الله عنه akasema: Someni mkipenda,

وَقُرْءَانَ الْفَجْرِ إِنَّ قُرْءَانَ الْفَجْرِ كَانَ مَشْهُودًا ﴿١٧٦﴾

**“Na Qur’an ya Alfajiri: ‘Hakika Qur’ani ya Alfajiri inashuhudiwa daima<sup>2</sup>”.**

Amepokea Imaam Ahmad kutoka kwa Ibn Mas’ud na Abu Hurayrah رضي الله عنهما kuwa Mtume ﷺ amesema:

<sup>1</sup> At-Tabari 17:17:520.

<sup>2</sup> Fat’hul Al-Baariy 8:251.

«تَشْهَدُهُ مَلَائِكَةُ اللَّيْلِ وَمَلَائِكَةُ النَّهَارِ»

“Wanaishuhudia hiyo Malaika wa usiku na mchana.”<sup>1</sup>

Hadithi hii pia imenukuliwa na At-Tirmidhiy, An-Nasaa’iy na Ibn Maajah. At-Tirmidhiy akasema, “Hadithi hii ni *Hasan Swahih*”<sup>2</sup>. Na katika lafdhi ya Sahihi mbili kutoka kwa Abu Hurayrah رضى الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«يَتَعَابُونَ فِيكُمْ مَلَائِكَةُ بِاللَّيْلِ وَمَلَائِكَةُ بِالنَّهَارِ، وَيَجْتَمِعُونَ فِي صَلَاةِ الصُّبْحِ وَفِي صَلَاةِ الْعَصْرِ، فَيَعْرُجُ الَّذِينَ بَاتُوا فِيكُمْ فَيَسْأَلُهُمْ رَبُّهُمْ وَهُوَ أَعْلَمُ بِكُمْ كَيْفَ تَرَكْتُمْ عِبَادِي؟ فَيَقُولُونَ: أَتَيْنَاهُمْ وَهُمْ يُصَلُّونَ، وَتَرَكْنَاهُمْ وَهُمْ يُصَلُّونَ»

“Malaika wa usiku na Malaika wa mchana wanakuja miongoni mwenu kwa makundi (kwa zamu). Wanajumuika katika Swala ya Asubuhi na ‘Asr. Wale waliokaa pamoja nanyi wanapaa, na Mola wenu Mlezi Anawauliza, japokuwa Anajua vyema kuhusu nyinyi, “Mmewaacha vipi waja Wangu?” Wakasema: “Tuliwajia wakiwa wanaswali na tumewaacha wakiswali”<sup>3</sup>.

Na amesema Ibn Mas’ud رضى الله عنه wanajumuika walinzi wawili katika Sala ya Alfajiri, na kikundi kimoja kinapaa (kwenda juu mbinguni) ilhali kingine kinakaa papo hapo<sup>4</sup>. Na hivyo ndivyo alivyosema Ibraahim an-Nakha’iy, Mujaahid, Qataadah na wengineo katika kuifasiri Aya hii<sup>5</sup>.

### Amri ya Kuswali *Tahajjud*

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَمِنَ اللَّيْلِ فَتَهَجَّدْ بِهِ نَافِلَةً لَّكَ

“Na amka usiku kwa ibada; ni ziada ya Sunna khasa kwako wewe”.

<sup>1</sup> Ahmad 2:474.

<sup>2</sup> Tuhfatul Ahwadhiy 8:569, An-Nasaa’iy katika Al-Kubraa 6:381 na Ibn Maajah 1:220.

<sup>3</sup> Fat’hul Al-Baariy 2:41 na Muslim 1:439.

<sup>4</sup> At-Tabari 17:521.

<sup>5</sup> At-Tabari 17:521.

Aliamriwa Mtume kusali Sala ya usiku baada ya zile za faradhi kama ilivyonukuliwa katika Sahihi Muslim kutoka kwa Abu Hurayrah رضى الله عنه kuwa Mtume ﷺ aliulizwa: “Ni Swalah gani iliyo bora kabisa baada ya za faradhi?” Akasema:

صَلَاةُ اللَّيْلِ

“Sala ya usiku”<sup>1</sup>.

Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Amemuamuru Mtume Wake ﷺ asali Sala ya usiku baada ya zile za faradhi, na Tahajjud ni ile Sala inayoswaliwa baada ya kulala. Hii ndiyo rai ya Alqamah, Al-Aswad, Ibraahim, An-Nakha'iy na wengine wengi<sup>2</sup>. Na hiyo ni maarufu katika lugha ya Kiarabu. Na vivyo hivyo zimethibiti Hadithi kutoka kwa Mtume wa Allah ﷺ kuwa alikuwa akisali Tahajjud baada ya kulala. Hii imepokewa kutoka kwa Ibn 'Abbaas<sup>3</sup>, Aishah<sup>4</sup> na Maswahaba wengine رضى الله عنهم. Suala hili limeelezwa kwa kina katika mahali pengine munasibu, sifa zote njema Anastahiki Allah تعالى.

Na amesema Al-Hasan Al-Baswri رحمه الله تعالى: “Hii ni Sala inayokuja baada ya ‘Ishaa’, na huenda ikawa ni ile inayofanyika baada ya kulala”<sup>5</sup>.

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

نَافِلَةٌ لَّكَ

“Ni ziada ya Sunna khasa kwako wewe”,

Maana yake: Kisimamo cha usiku kimefanywa khasa kwako (Mtume ﷺ), kwani umesamehewa madhambi yaliyopita na yanayokuja. Ama kwa wafuasi wa Umma wake, kutekeleza Sala za Sunna, huenda ikawafutia wao madhambi yao kwa tofauti waliyoyafanya. Hii ni rai ya Mujaahid<sup>6</sup>, na imenukuliwa katika *Al-Musnad* kutoka kwa Abi Umamah Al-Baahiliy<sup>7</sup>. Na Kauli Yake:

<sup>1</sup> Muslim 2:821.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:524.

<sup>3</sup> Fat'hul Al-Baariy 8:83.

<sup>4</sup> Fat'hul Al-Baariy 3:39.

<sup>5</sup> At-Tabari 17:524.

<sup>6</sup> At-Tabari 17:525.

<sup>7</sup> Ahmad 5:255.

عَسَىٰ أَنْ يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُودًا ﴿٧٦﴾

**“Huenda Mola wako Mlezi Akakunyanyua cheo kinachosifika”,**

Maana yake: Fanya haya Niliyokuamuru, ili Tukunyanyue Siku ya Kiyama katika cheo kinachosifika, ambacho viumbe wote watakusifu, pamoja na Muumba wao Aliyetukuka. Ibn Jariir رحمه الله تعالى amesema: “Wafasiri wengi wamesema: Hicho ni cheo ambacho atakuwa nacho Muhammad ﷺ Siku ya Kiyama kuwaombea watu kwa Mola wao Mlezi ili Awaondolee shida waliyo nayo ya siku hiyo.”<sup>1</sup>

Imepokewa kutoka kwa Hudhayfah رضي الله عنه aliyesema: “Watakusanywa watu katika wangwa mmoja, ambamo kila mmoja atasikia mwito na wote wataonekana. Watasimama bila viatu na uchi kama walivyozaliwa, na hakuna atakayethubutu kuzungumza ila anayepewa ruhusa na Allah تعالى. Ataita: ‘Ewe Muhammad, naye ataitikia

«لَيْتَكَ وَسَعْدَيْكَ، وَالْخَيْرُ فِي يَدَيْكَ وَالشَّرُّ لَيْسَ إِلَيْكَ، وَالْمَهْدِيُّ مِنْ هَدَيْتِ،  
وَعَبْدُكَ بَيْنَ يَدَيْكَ، وَمِنْكَ وَإِلَيْكَ لَا مَنَجَى وَلَا مَلْجَأَ مِنْكَ إِلَّا إِلَيْكَ، تَبَارَكْتَ  
وَتَعَالَيْتَ سُبْحَانَكَ رَبَّ الْبَيْتِ»

*‘Nipo hapa kutekeleza Amri Yako, Mazuri yote yamo Mikononi Mwako na shari zote si za Kwako. Aliyeongoka ni yule Uliyemuongoza. Mja Wako yuko mbele Yako, kutoka Kwako na kuelekea Kwako, hakuna kuokoka wala kutaka hifadhi kutoka Kwako ila ipo Kwako. Baraka na Utukufu na Utakaso wote ni Wako, Mola Mlezi wa Nyumba (Al-Ka’bah)’.*

Hiki ndicho cheo cha utukufu chenye sifa (*Maqam Mahmud*) kilichotajwa na Allah تعالى<sup>2</sup>.

Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Cheo cha utukufu, kinachosifika ni ile fursa ya kuwaombea (waja)”<sup>3</sup>. Na hivyo ndivyo alivyosema Ibn Abi Najih kutoka kwa Mujaahid, na amesema hilo Al-Hasan Al-Baswriy رحمه الله تعالى<sup>4</sup>.

<sup>1</sup> At-Tabari 17:526.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:526.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:527.

<sup>4</sup> At-Tabari 17:527.

Qataadah amesema: “Yeye atakuwa wa kwanza ambaye ardhi itapasuka (kufunuliwa) Siku ya Kiyama na wa kwanza kuomba (kuwaombea waja)”<sup>1</sup>. Kwa hiyo, wanazuoni wameona kuwa hicho ni cheo kinachosifika ambacho kwacho, Amesema Allah تعالى،

عَسَىٰ أَنْ يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُودًا ﴿٧٦﴾

**“Huenda Mola wako Mlezi Akakunyanyua cheo kinachosifika”.**

Nikasema (yaani mimi, Ibn Kathir): Mtume ﷺ atakuwa na utukufu Siku ya Kiyama ambao hatakuwa nao mwingine yeyote, utukufu ambao hautafikiwa na yeyote yule. Atakuwa wa kwanza ambaye ardhi itafunguliwa na atakuja kwenye ardhi ya mkusanyiko na ufufuo akiwa amepanda (mnyama). Atakuwa na bendera, ambayo watu wote pamoja na Adam عليه السلام watakuwa nyuma yake, na pia *hawdh* (birika) ambayo yeye ndiye atakayeiliki kuliko mwengine yeyote. Naye atakuwa na ile fursa ya *shifaa* (uombezi mkubwa) kubwa mbele ya Allah تعالى Atakapokuja kuhukumu baina ya viumbe. Hii itakuwa baada ya watu kumuendea na kumuomba Adam عليه السلام, kisha Nuuḥ عليه السلام, baadaye Ibraahim عليه السلام, kisha Musa عليه السلام, na baadaye ‘Isa عليه السلام ili wawaombe na kila mmoja wao atasema, “Siwezi hilo”. Kisha watakuja kwa Muhammad ﷺ, naye atasema:

«أَنَا لَهَا أَنَا لَهَا»

**“Mimi ndiye mwenyewe, Mimi ndiye mwenyewe”.**

Tutataja hilo kwa kirefu baada ya muda mchache, Allah تعالى Akipenda.

Na kati ya hayo ni kuwaombea watu ambao wamehukumiwa kuingizwa Motoni, hivyo kurudishwa. Atakuwa Nabii wa kwanza ambaye Umma wake utahukumiwa, na wa kwanza kuwachukua Umma wake kuvuka sirati juu ya Moto, na wa kwanza kuwaombea Peponi, kama ilivyoripotiwa katika Sahihi Muslim<sup>2</sup>.

Na katika Hadithi kuhusu Baragumu, inasema kuwa Waumini hawataingia Peponi isipokuwa kwa *Shifaa*. Atakuwa wa kwanza kuingia Peponi, na Umma

<sup>1</sup> At-Tabari 17:528.

<sup>2</sup> Muslim 1:182.



wake utakuwa taifa la kwanza kuingia. Atawaombea watu wanyanyuliwe cheo chao na daraja yao, ambao amali zao zilikuwa haziwafikishi hapo. Yeye ni mmoja ya watakaofika *Al-Wasilah*, ambacho ni cheo cha juu zaidi Peponi, ambacho hakimfalii yeyote ila yeye. Pindi Allah تعالی Atakapotoa ruhusa kuombewa walioasi na wenye madhambi, Malaika, Manabii na Waumini watawaombea watu, naye pia atawaombea watu ambao idadi yao inajulikana na Allah تعالی tu. Hakuna atakayeombea watu mfano wake na hakuna atakayemfikia katika hilo<sup>1</sup>. Suala hili limeelezwa kwa kina na ukamilifu mwisho wa Kitabu cha Sira, katika mlango wa sifa mahususi, Sifa zote njema Anastahiki Allah تعالی. Sasa kwa msaada wa Allah تعالی tutazitaja Hadithi zilionukuliwa kuhusiana na cheo chenye hadhi kubwa *“Al-Maqaam al-Mahmuud”*. Imepokewa na Al-Bukhaariy kutoka kwa Ibn ‘Umar رضي الله عنهما kuwa alisema: “Hakika Siku ya Kiyama, watu wataelekea na kunyenyekea kwa magoti yao, kila taifa litamfuata Nabii wao, wakimuambia: ‘Ewe fulani, tuombe’ mpaka ile nguvu ya kuwaombea atakapopatiwa Muhammad ﷺ. Hiyo itakuwa ni siku ambayo Allah تعالی Atamnyanyua katika cheo na daraja inayosifika.”<sup>2</sup>

Amepokea Ibn Jariir رحمه الله تعالی kutoka kwa Ibn ‘Umar رضي الله عنهما akisema kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ الشَّمْسَ لَتَذُو حَتَّى يَبْلُغَ العَرَقُ نِصْفَ الأَذْنِ، فَيَبْتَئِمَا هُمْ كَذَلِكَ اسْتَعَانُوا بِأَدَمَ فَيَقُولُ: لَسْتُ بِصَاحِبِ ذَلِكَ، ثُمَّ بِمُوسَى فَيَقُولُ كَذَلِكَ، ثُمَّ بِمُحَمَّدٍ فَيَنْفَعُ بَيْنَ الخَلْقِ فَيَمُشِي حَتَّى يَأْخُذَ بِحَلَقَةِ بَابِ الجَنَّةِ، فَيُؤَمِّدُ بِعُنُقِهِ اللهُ مَقَامًا مَحْمُودًا»

*“Hakika jua litashuka chini mpaka jasho litawafikia watu katika nusu ya masikio yao, wakiwa katika hali hiyo, watamtaka msaada Adam, naye atasema: ‘Mimi si sahibu (mwenye) hilo’. Watakwenda kumtaka Musa msaada, naye atajibu hivyo hivyo. Kisha watamuendea Muhammad, atawaombea viumbe, Atakwenda hadi ashike kikuku cha mlango wa Peponi, na hiyo itakuwa ni siku ambayo Allah Atamnyanyua katika cheo kinachosifika.”<sup>3</sup>*

Na hivyo ndivyo alivyopokea Al-Bukhariy katika mlango wa Zakah na kuongeza:

<sup>1</sup> At-Tabrani katika Atw-Twiwaal na 36.

<sup>2</sup> Fat’h Al-Baariy 8:251.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:529.

«فَيَوْمَئِذٍ يَبْعَثُ اللَّهُ مَقَامًا مَّحْمُودًا، يَحْمَدُهُ أَهْلُ الْجَمْعِ كُلُّهُمْ»

*"Siku hiyo Allah Atamnyanyua kwenye cheo kinachosifika, na watu wote watamsifu."*<sup>1</sup>

Amepokea Abu Daawuud Atw-Twayaalisi رحمه الله تعالى kutoka kwa Abdallah amesema: "Kisha Allah تعالى Ataruhusu *Shifaa*. Hapo atasimama Roho Takatifu, Jibril عليه السلام, kisha Ibraahim عليه السلام Khaliil wa Allah تعالى (rafiki wa karibu wa Allah تعالى), kisha atasimama 'Isa عليه السلام au Musa عليه السلام. Akasema Abu az-Za'raa': 'Sijui ni yupi kati yao'. Akasema: 'Kisha atasimama Mtume wenu ﷺ kuomba, hakuna atakayeomba baada yake zaidi kwa aliyoomba'. Hicho ni cheo kinachosifika ambacho kwacho Allah تعالى Amesema:

عَسَىٰ أَنْ يَبْعَثَكَ رَبُّكَ مَقَامًا مَّحْمُودًا ﴿٧٦﴾

***'Huenda Mola wako Mlezi Akakunyanyua cheo kinachosifika.'***<sup>2</sup>

**Hadithi ya Abu Hurayrah رضي الله عنه**

Amepokea Imaam Ahmad kutoka kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema: "Nyama ililetwa kwa Mtume ﷺ, akapewa sehemu ya nyama ya mkono, ambayo alikuwa akipenda na kunyofoa kipande, kisha akasema:

«أَنَا سَيِّدُ النَّاسِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ، وَهَلْ تَذُرُونَ مِنِّي ذَاكَ؟ يَجْمَعُ اللَّهُ الْأَوْلِيَيْنَ وَالْآخِرِينَ فِي صَعِيدٍ وَاحِدٍ، يُسَمِعُهُمُ الدَّاعِيَ، وَيَتَفَذَّهُمُ الْبَصْرُ، وَتَذْنُو السَّمْسُ فَيَبْلُغُ النَّاسَ مِنَ النِّعَمِ وَالنَّكَرِ مَا لَا يُطِيقُونَ، وَلَا يَحْتَمِلُونَ فَيَقُولُ بَعْضُ النَّاسِ لِبَعْضٍ: أَلَا تَرَوْنَ مَا أَنْتُمْ فِيهِ وَمِمَّا قَدْ بَلَغَكُمْ، أَلَا تَنْظُرُونَ مَنْ يَشْفَعُ لَكُمْ إِلَىٰ رَبِّكُمْ؟ فَيَقُولُ بَعْضُ النَّاسِ لِبَعْضٍ: عَلَيْكُمْ بِآدَمَ، فَإِنَّا نَرَىٰ آدَمَ عَلَيْهِ السَّلَامُ فَيَقُولُونَ: يَا آدَمُ أَنْتَ أَبُو الْبَشَرِ خَلَقَكَ اللَّهُ بِيَدَيْهِ وَنَفَخَ فِيكَ مِنْ رُوحِهِ، وَأَمَرَ الْمَلَائِكَةَ فَسَجَدُوا لَكَ، فَاشْفَعْ لَنَا إِلَىٰ رَبِّكَ أَلَا تَرَىٰ مَا نَحْنُ فِيهِ، أَلَا تَرَىٰ مَا قَدْ بَلَغَنَا؟ فَيَقُولُ آدَمُ: إِنَّ رَبِّي قَدْ غَضِبَ الْيَوْمَ غَضَبًا لَمْ يَغْضَبْ قَبْلَهُ مِثْلَهُ وَلَنْ يَغْضَبَ بَعْدَهُ مِثْلَهُ، وَإِنَّهُ قَدْ نَهَانِي عَنِ الشَّجَرَةِ فَعَصَيْتُ، نَفْسِي نَفْسِي نَفْسِي، أَذْهَبُوا إِلَىٰ غَيْرِي أَذْهَبُوا إِلَىٰ نُوحٍ، فَإِنَّا نَرَىٰ نُوحًا فَيَقُولُونَ: يَا نُوحُ أَنْتَ أَوَّلُ الرُّسُلِ إِلَىٰ أَهْلِ الْأَرْضِ، وَقَدْ سَمَّاكَ اللَّهُ عَبْدًا شَكُورًا،

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baariy 3:396.

<sup>2</sup> Musnad Atw-Twayaalisi 51 na An-Nasaa'iy katika Al-Kubraa 11296.

اشْفَعْنَا لَنَا إِلَى رَبِّكَ أَلَا تَرَى مَا نَحْنُ فِيهِ، أَلَا تَرَى مَا قَدْ بَلَّغْنَا؟ فَيَقُولُ نُوحٌ: إِنَّ رَبِّي قَدْ غَضِبَ الْيَوْمَ غَضَبًا لَمْ يَغْضَبْ قَبْلَهُ مِثْلَهُ وَلَنْ يَغْضَبَ بَعْدَهُ مِثْلَهُ قَطُّ، وَإِنَّهُ قَدْ كَانَتْ لِي دَعْوَةٌ دَعَوْتُهَا عَلَى قَوْمِي نَفْسِي نَفْسِي نَفْسِي، اذْهَبُوا إِلَى غَيْرِي اذْهَبُوا إِلَى إِبْرَاهِيمَ، فَيَأْتُونَ إِبْرَاهِيمَ فَيَقُولُونَ: يَا إِبْرَاهِيمُ أَنْتَ نَبِيُّ اللَّهِ وَخَلِيلُهُ مِنْ أَهْلِ الْأَرْضِ، اشفَعْنَا لَنَا إِلَى رَبِّكَ أَلَا تَرَى مَا نَحْنُ فِيهِ، أَلَا تَرَى مَا قَدْ بَلَّغْنَا؟ فَيَقُولُ: إِنَّ رَبِّي قَدْ غَضِبَ الْيَوْمَ غَضَبًا لَمْ يَغْضَبْ قَبْلَهُ مِثْلَهُ، وَلَنْ يَغْضَبَ بَعْدَهُ مِثْلَهُ- فَذَكَرَ كَذَبَاتِهِ- نَفْسِي نَفْسِي نَفْسِي، اذْهَبُوا إِلَى غَيْرِي اذْهَبُوا إِلَى مُوسَى، فَيَأْتُونَ مُوسَى عَلَيْهِ السَّلَامُ فَيَقُولُونَ: يَا مُوسَى أَنْتَ رَسُولُ اللَّهِ اضْطَفَاكَ اللَّهُ بِرِسَالَاتِهِ وَبِكَلَامِهِ عَلَى النَّاسِ، اشفَعْنَا لَنَا إِلَى رَبِّكَ أَلَا تَرَى مَا نَحْنُ فِيهِ، أَلَا تَرَى مَا قَدْ بَلَّغْنَا؟ فَيَقُولُ لَهُمْ مُوسَى: إِنَّ رَبِّي قَدْ غَضِبَ الْيَوْمَ غَضَبًا لَمْ يَغْضَبْ قَبْلَهُ مِثْلَهُ، وَلَنْ يَغْضَبَ بَعْدَهُ مِثْلَهُ، وَإِنِّي قَدْ قَتَلْتُ نَفْسًا لَمْ أَوْمَرْ بِقَتْلِهَا، نَفْسِي نَفْسِي نَفْسِي، اذْهَبُوا إِلَى غَيْرِي اذْهَبُوا إِلَى عِيسَى، فَيَأْتُونَ عِيسَى فَيَقُولُونَ: يَا عِيسَى أَنْتَ رَسُولُ اللَّهِ وَكَلِمَتُهُ أَلْفَاها إِلَى مَرْيَمَ وَرُوحَ مِنْهُ، وَكَلَّمْتَ النَّاسَ فِي الْمَهْدِ صَبِيًّا، فَاشْفَعْنَا لَنَا إِلَى رَبِّكَ أَلَا تَرَى مَا نَحْنُ فِيهِ، أَلَا تَرَى مَا قَدْ بَلَّغْنَا؟ فَيَقُولُ لَهُمْ عِيسَى: إِنَّ رَبِّي قَدْ غَضِبَ الْيَوْمَ غَضَبًا لَمْ يَغْضَبْ قَبْلَهُ مِثْلَهُ، وَلَنْ يَغْضَبَ بَعْدَهُ مِثْلَهُ، وَلَمْ يَذْكُرْ ذَنْبًا، نَفْسِي نَفْسِي اذْهَبُوا إِلَى غَيْرِي اذْهَبُوا إِلَى مُحَمَّدٍ، فَيَأْتُونَ مُحَمَّدًا فَيَقُولُونَ: يَا مُحَمَّدُ أَنْتَ رَسُولُ اللَّهِ وَخَاتَمُ الْأَنْبِيَاءِ، وَقَدْ غَفَرَ اللَّهُ لَكَ مَا تَقَدَّمَ مِنْ ذَنْبِكَ وَمَا تَأَخَّرَ، فَاشْفَعْنَا لَنَا إِلَى رَبِّكَ أَلَا تَرَى مَا نَحْنُ فِيهِ، أَلَا تَرَى مَا قَدْ بَلَّغْنَا؟ فَأَقُولُ فَأَتَانِي تَحْتَ الْعَرْشِ، فَأَقَعُ سَاجِدًا لِرَبِّي عَزَّ وَجَلَّ، ثُمَّ يَفْتَحُ اللَّهُ عَلَيَّ وَيُلْهِمُنِي مِنْ مَحَامِدِهِ وَحُسْنِ الثَّنَاءِ عَلَيْهِ مَا لَمْ يَفْتَحْهُ عَلَيَّ أَحَدٌ قَبْلِي، فَيَقَالُ: يَا مُحَمَّدُ اذْفَعْ رَأْسَكَ وَسَلْ نَعْتَهُ، وَاشْفَعْنَا نُنْفَعُ، فَأَرْفَعُ رَأْسِي فَأَقُولُ: أُمَّتِي يَا رَبِّ، أُمَّتِي يَا رَبِّ، أُمَّتِي يَا رَبِّ، فَيَقَالُ: يَا مُحَمَّدُ أَدْخِلْ مِنْ أُمَّتِكَ مَنْ لَا حِسَابَ عَلَيْهِ مِنَ الْبَابِ الْأَيْمَنِ مِنْ أَبْوَابِ الْجَنَّةِ، وَهُمْ شُرَكَاءُ النَّاسِ فِيمَا سِوَى ذَلِكَ مِنَ الْأَبْوَابِ، ثُمَّ قَالَ: وَالَّذِي نَفْسُ مُحَمَّدٍ بِيَدِهِ إِنَّ مَا بَيْنَ الْمُضْرَاعَيْنِ مِنْ مَضَارِيعِ الْجَنَّةِ كَمَا بَيْنَ مَكَّةَ وَهَجَرَ، أَوْ كَمَا بَيْنَ مَكَّةَ وَبُصْرَى»

'Mimi ndiye bwana (kiongozi) wa wanadamu Siku ya Kiyama. Mnajua kwa nini iwe hivyo?' Allah Atawakusanya wa mwanzo na wa mwisho katika wangwa mmoja, nao watasikia sauti inayoita na

wote wataona. Jua litaletwa karibu sana mpaka ghamu, wasiwasi na mfadhaiko utakuwa haubebeki. Baadhi ya watu watasema kwa wengine: 'Je, hamuoni jinsi tunavyoteseka? Je, hamutizami kwa atakayewaombea kwa Mola wenu Mlezi?' Baadhi ya watu watawambia wengine: 'Nendeni kwa wengine'. Watakuja kwa Adam عليه السلام, watamuambia: 'Ewe Adam! Wewe ni baba wa viumbe, Amekuumba Allah kwa Mikono Yake na Kukupulizia roho Yake, Akawaamuru Malaika wakusujudie. Tuombee kwa Mola wako Mlezi. Je, huoni tuliyonayo? Je, huoni yaliyotufika?' Atasema Adam: 'Hakika Mola wangu Mlezi, Ameghadhibika sana leo Hajawahi Kukasirika kabla yake mfano wake wala Hataghadhibika baada yake mfano wake. Hakika Alinikataza kuukurubia mti, nikamuasi. Nafsi yangu, nafsi yangu, nafsi yangu, nendeni kwa mwengine asiyekuwa mimi. Nendeni kwa Nuuh'. Watakuja kwa Nuuh na kumuambia: 'Ewe Nuuh! Wewe ndiye Mtume wa kwanza kwa watu wa ardhini. Na hakika ni kuwa Allah Amekuita, mja mwenye kushukuru, tuombee nasi kwa Mola wako Mlezi. Je, huoni tuliyo nayo? Je, huoni yaliyotufika?' Atasema Nuuh: 'Hakika Mola wangu Mlezi, Ameghadhibika sana leo Hajawahi Kukasirika kabla yake mfano wake wala Hataghadhibika baada yake mfano wake. Na hakika niliomba dua juu ya kaumu zangu. Nafsi yangu, nafsi yangu, nafsi yangu. Nendeni kwa mwengine, nendeni kwa Ibraahim." Hivyo watakuja kwa Ibraahim, watamuambia: "Ewe Ibraahim! Wewe ni Nabii wa Allah na rafiki Yake katika watu wa ardhini. Twakuomba utuombee kwa Mola wako Mlezi. Je, huoni kwa yale tuliyonayo? Je, huoni yaliyotufika?" Atasema: "Hakika Mola wangu Mlezi, Ameghadhibika sana leo Hajawahi Kukasirika kabla yake mfano wake wala Hataghadhibika baada yake mfano wake. Akataja uwongo wake, nafsi yangu, nafsi yangu, nafsi yangu. Nendeni kwa mwengineo asiyekuwa mimi, nendeni kwa Musa." Watakwenda kwa Musa, na kumuambia: 'Ewe Musa! Wewe ni Mtume wa Allah, Allaah Amekuchagua kwa Kukupatia risala na Kuzungumza nawe moja kwa moja. Tuombee kwa Mola wako Mlezi. Je, huoni kwa yale tuliyonayo? Je, huoni yaliyotufika?" Atasema: "Hakika Mola wangu Mlezi, Ameghadhibika sana leo Hajawahi Kukasirika kabla yake

mfano wake wala Hataghadhibika baada yake mfano wake. Na hakika niliua nafsi ambayo sikuamrishwa kuiua, nafsi yangu, nafsi yangu, nafsi yangu. Nendeni kwa mwengine asiyekuwa mimi, nendeni kwa Isa". Watakwenda kwa 'Isa عليه السلام, na kumuambia: "Ewe 'Isa عليه السلام! Wewe ni Mtume wa Allah na Neno Lake Alilompatia Maryam na Roho kutoka Kwake na ukazungumza na watu ukiwa mtoto mchanga. Tuombe kwa Mola wako Mlezi. Je, huoni kwa yale tuliyonayo? Je, huoni yaliyotufika?" Isa atawaambia: "Hakika Mola wangu Mlezi, Ameghadhibika sana leo hajawahi Kukasirika kabla yake mfano wake wala Hataghadhibika baada yake mfano wake – wala hatataja dhambi lolote – nafsi yangu, nafsi yangu, nafsi yangu. Nendeni kwa mwengineo asiyekuwa mimi, nendeni kwa Muhammad ﷺ". Watakwenda kwa Muhammad ﷺ, na kumuambia: "Ewe Muhammad! Wewe ni Mtume wa Allah na mwisho wa Mitume. Na hakika Allah Amekusamehe madhambi yaliyopita na ya baadaye, tuombe kwa Mola wako Mlezi. Je, huoni kwa yale tuliyo nayo? Je, huoni yaliyotufika?" Nitasimama na kuja karibu na Kiti cha Enzi, hapo nitasujudu kwa Mola wangu Mlezi, Aliyetukuka. Kisha Allah Atanifunulia nizungumze kwa Kumhimidi kwa maneno mazuri, maneno ambayo hajafunuliwa yeyote kabla yangu. Kutasemwa: "Ewe Muhammad! Nyanyua kichwa chako na uombe, kwani hilo utapewa. Omba shifaa, shifaa yako itasikilizwa." Nitanyanyua kichwa changu, na kusema: "Umma wangu ewe Mola Mlezi, Umma wangu ewe Mola Mlezi, Umma wangu ewe Mola wangu Mlezi." Nitaambiwa: "Ewe Muhammad! Waingize katika Umma wako wale ambao hawatahesabiwa kwenye mlango wa kuume katika milango ya Pepo. Waliobaki katika Umma wako watashirikiana katika milango mingine pamoja na watu wengine." Kisha akasema: "Naapa kwa Yule ambaye nafsi ya Muhammad iko Mikononi Mwake, masafa baina ya vingi viwili vya milango ni baina ya Makka na Hajar au baina ya Makka na Buswraa (yaani Basra)"<sup>1</sup>. Hadithi hii imenukuliwa pia katika Sahihi mbili<sup>2</sup>.

---

<sup>1</sup> Ahmad 2:435.

<sup>2</sup> Al-Bukhaariy 4712 na Muslim 894.

وَقُلْ رَبِّ أَدْخِلْنِي مُدْخَلَ صِدْقٍ وَأَخْرِجْنِي مَخْرَجَ صِدْقٍ وَأَجْعَلْ لِي مِنْ أَلَدْنِكَ سُلْطٰنًا  
 نَصِيرًا ﴿٨٥﴾ وَقُلْ جَاءَ الْحَقُّ وَزَهَقَ الْبٰطِلُ إِنَّ الْبٰطِلَ كَانَ زَهُوقًا ﴿٨٦﴾

**80. Na sema: Mola wangu Mlezi! Niingize muingizo mwema, na Unitoe kutoka kwema. Na Unipe nguvu zitokazo Kwako zinisaidie.**

**81. Na sema: Kweli imefika, na uongo umetoweka. Hakika uongo lazima utoweke!**

### Amri ya Kuhama

Amepokea Imam Ahmad رحمه الله تعالى kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kuwa amesema: Mtume ﷺ alikuwa Makka, kisha akaamriwa kuhama, na Allah تعالى Akateremsha:

وَقُلْ رَبِّ أَدْخِلْنِي مُدْخَلَ صِدْقٍ وَأَخْرِجْنِي مَخْرَجَ صِدْقٍ وَأَجْعَلْ لِي مِنْ أَلَدْنِكَ سُلْطٰنًا  
 نَصِيرًا ﴿٨٥﴾

**“Na sema: Mola wangu Mlezi! Niingize muingizo mwema, na Unitoe kutoka kwema. Na Unipe nguvu zitokazo Kwako zinisaidie”<sup>1</sup>.**

At-Tirmidhiy amesema: Hadithi Hasan Swahiih<sup>2</sup>.

Na amesema Hasan Al-Baswriy رحمه الله تعالى katika kuifasiri Aya hii: Pale makafiri wa Makka walipopanga hila ya kutaka kumuua Mtume ﷺ, kumfukuza na kumtia kizuizini. Allah تعالى Alitaka apigane na watu wa Makkah, na Akamuamuru ahame kuelekea Madina. Naye Ndiye Ambaye Amesema:

وَقُلْ رَبِّ أَدْخِلْنِي مُدْخَلَ صِدْقٍ وَأَخْرِجْنِي مَخْرَجَ صِدْقٍ

**“Na sema: Mola wangu Mlezi! Niingize muingizo mwema na unitoe kutoka kwema”<sup>3</sup>. Na amesema Qataadah:**

وَقُلْ رَبِّ أَدْخِلْنِي مُدْخَلَ صِدْقٍ

**“Na sema: Mola wangu Mlezi! Niingize muingizo mwema.”**Maana: Madina.

<sup>1</sup> Ahmad 1:223.

<sup>2</sup> Tuhfat Al-Ahwadhiy 8:574. Sanadi yake ni dhaifu.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:533.

وَأُخْرِجْنِي مَخْرَجَ صِدْقٍ

**“Na Unitoe kutoka kwema”,**

Maana yake: Makka<sup>1</sup>. Hii ndiyo pia rai ya ‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam<sup>2</sup>. Na Kauli Yake:

وَأَجْعَلْ لِي مِنْ لَدُنْكَ سُلْطٰنًا نَّصِيْرًا ﴿٥٧﴾

**“Na Unipe nguvu zitokazo Kwako zinisaidie”.**

Amesema al-Hasan Al-Baswriy رحمه الله تعالى katika tafsiri yake: “Mola wake Mlezi Alimuahidi Kuuchukua ufalme na utukufu wa wafursi na Kumpatia yeye, na pia ufalme na utukufu wa Warumi na Kumpatia yeye.”<sup>3</sup>

Na amesema Qataadah kuhusu hilo: “Hakika Mtume ﷺ alijua kuwa hawezi kupata hilo bila ya kuwa na nguvu au mamlaka, hivyo akaomba mamlaka na nguvu za kumsaidia kukinyanyua Kitabu cha Allah تعالى, Sheria ya Allah تعالى, faradhi za Allah تعالى na kusimamisha Dini ya Allah تعالى. Mamlaka ni Rehema kutoka kwa Allah تعالى, ambayo Anaiweka juu ya migongo ya waja Wake. Lau kama si hivyo baadhi ya waja wangevamia wengine, na wenye nguvu wangewala wanyonge.”<sup>4</sup> Hapana budi pamoja na haki kuwa na nguvu na mamlaka ili kupambana na wenye kupinga na kumzuia, hivyo Allah تعالى Akasema:

لَقَدْ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا بِالْبَيِّنٰتِ

**“Kwa hakika Tuliwapeleka Mitume Wetu kwa dalili waziwazi.”**

Mpaka katika Kauli Yake,

وَأَنْزَلْنَا الْحَدِيْدَ

**“Na Tumekiteremsha chuma.” (57:25).**

<sup>1</sup> Ahmad 1:223.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:534.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:536.

<sup>4</sup> At-Tabari 17:536.

## Onyo kwa Wasioamini Katika Makuraishi

Na Kauli Yake:

وَقُلْ جَاءَ الْحَقُّ وَزَهَقَ الْبَاطِلُ<sup>٤٤</sup>

**“Na sema: Kweli imefika, na uongo umetoweka.”**

Hili ni onyo kwa makafiri wa Quraysh, kwani umekuja ukweli kutoka kwa Allah تعالى kuondoa tashwishi zozote na hawana nguvu za kuuzuia. Nayo ni yale aliyomtuma nayo katika Qur’ani, Imani na elimu yenye manufaa. Na uwongo wao ukatoweka, yaani ulipotea na kuhilikishwa, kwani batili haiwezi kuikatisha wala kubaki mbele ya haki.

بَلْ نَقْذِفُ بِالْحَقِّ عَلَى الْبَاطِلِ فَيَدْمَغُهُ فَإِذَا هُوَ زَاهِقٌ<sup>٤٥</sup>

**“Bali Tunaitupa haki juu ya batili ikalivunja bufuru (fuvu) la kichwa chake, na mara batili ikatoweka.” (21:18)**

Imepokewa na Al-Bukhaariy رضي الله عنهما kutoka kwa Ibn Mas’ud رحمه الله تعالى amesema: Aliingia Mtume ﷺ Makka (wakati wa kuifungua mwaka wa 8 Baada ya Hijra), na pembezoni mwa Al-Ka’bah yapo masanamu mia tatu na sitini (360). Alianza kuyagonga kwa fimbo iliyokuwa mkononi mwake, huku akisema:

وَقُلْ جَاءَ الْحَقُّ وَزَهَقَ الْبَاطِلُ<sup>٤٦</sup> إِنَّ الْبَاطِلَ كَانَ زَهُوقًا<sup>٤٧</sup>

**“Imekuja haki na batili kutoweka. Hakika batili ni lazima itoweke.”**

جَاءَ الْحَقُّ وَمَا يُبْدِي<sup>٤٨</sup> الْبَاطِلُ وَمَا يُعِيدُ<sup>٤٩</sup>

**“Haki imekuja batili haitaleta mapya tena wala haitarudi.” (34:49)**

وَنُنزِلُ مِنَ الْقُرْآنِ مَا هُوَ شِفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ<sup>٥٠</sup> وَلَا يَزِيدُ الظَّالِمِينَ إِلَّا خَسَارًا<sup>٥١</sup>

**82. Na Tunateremsha katika Qur’ani yaliyo ni matibabu na rehema kwa Waumini. Wala hayawazidishii madhalimu ila hasara.**



### Qur'ani ni Shifaa (Tiba) na Rehema

Allah تعالى Anatuambia kuwa Kitabu Chake, ambacho Amekiteremsha kwa Mtume Wake, Muhammad ﷺ, Qur'ani ambayo hakuna batili inayoweza kuikaribia mbele au nyuma yake, imeteremshwa na Mwenye Hekima, Mwenye Kuhimidiwa. Qur'ani ni shifaa na rehema kwa Waumini, yaani inaondoa yaliyo nyoyoni katika maradhi ya shaka, nifaki, ushirikina, kudang'anya na kumili kwenye uwongo. Qur'ani inatibu yote hayo. Nayo pia ni rehema, kupitia kwayo, mja anafikia kilele cha Imani na hekima na kutaka mema. Haya ni kwa wale wenye kuiamini na kuifuata, ni shifaa na rehema kwa watu hao tu. Ama kwa makafiri, anayejidhulumu kwa ukafiri wake, anapoisikia Qur'ani, inamsukuma mbali zaidi na ukweli na kumzidishia yeye ukafiri. Shida inatokana na kafiri mwenyewe, wala sio Qur'ani. Kama Allah تعالى Anavyosema:

قُلْ هُوَ لِلَّذِينَ آمَنُوا هُدًى وَشِفَاءً وَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ فِي آذَانِهِمْ وَقْرٌ وَهُوَ عَلَيْهِمْ عَمًى أُولَٰئِكَ يُنَادَوْنَ مِنْ مَّكَانٍ بَعِيدٍ ﴿٤٤﴾

**“Sema: Hii Qur'ani ni uwongofu na poza kwa wale walioamini; na wale wasioamini umo uzito katika masikio yao; na hiyo Qur'ani ni giza kwao. Kama kwamba hao wanaitwa, na hali ya kuwa wako mbali kabisa.” (41:44).**

Na Allah تعالى Amesema;

وَإِذَا مَا أَنْزَلْنَا سُورَةً فَمِنْهُمْ مَنْ يَقُولُ أَيُّكُمْ زَادَتْهُ هِدَايَةً إِيْمَانًا ۚ فَأَمَّا الَّذِينَ آمَنُوا فزَادَتْهُمْ إِيْمَانًا وَهُمْ يَسْتَبْشِرُونَ ﴿٤٥﴾ وَأَمَّا الَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ فزَادَتْهُمْ رِجْسًا إِلَىٰ رِجْسِهِمْ وَمَاتُوا وَهُمْ كَافِرُونَ ﴿٤٦﴾

**“Na inapoteremshwa sura mpya wako miongoni mwao (wanafiki) wasemao: ‘Ni nani miongoni mwenu ambaye surah hii imemzidishia Imani?’ Ama wale walioamini inawazidishia Imani,**

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baariy 8:252.

**nao wanafurahi. Ama wale wenye ugonjwa nyoyoni mwao, basi inawazidishia ubaya mpya juu ya ubaya waliokuwa nao; na wanakufa na hali ni makafiri.” (9:124-125).**

Na zipo Aya nyingi mfano wake. Amesema Qataadah katika Kauli Yake:

وَنُزِّلُ مِنَ الْقُرْآنِ مَا هُوَ شِفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِّلْمُؤْمِنِينَ<sup>٧</sup>

**“Na Tunateremsha katika Qur’ani yaliyo ni matibabu na rehema kwa Waumini...’ (17:82)**

Anaposikia Muumini hayo, anafaidika kutoka kwayo, anahifadhi na kuifahamu.

وَلَا يَزِيدُ الظَّالِمِينَ إِلَّا خَسَارًا ﴿٨٢﴾

**“...Wala hayawazidishii madhalimu ila hasara.”(17:82)**

Maana: Hawafaidiki madhalimu kwayo, au kuihifadhi, au kuifahamu, kwani Allah تعالى Ameifanya Qur’ani kuwa ni poza na rehema kwa Waumini.

وَإِذَا أُنْعَمْنَا عَلَى الْإِنْسَانِ أَعْرَضَ وَنَقَا بِيحَابِهِ<sup>٨</sup> وَإِذَا مَسَّهُ الشَّرُّ كَانَ يَئُوسًا ﴿٨٣﴾ قُلْ

كُلُّ يَعْمَلُ عَلَى شَاكِلَتِهِ فَرُبُّكُمْ أَعْلَمُ بِمَنْ هُوَ أَهْدَى سَبِيلًا ﴿٨٤﴾

**83. Na Tunapomneemesha mwanadamu hugeuka na kujitenga kando. Na inapomgusa shari hukata tamaa.**

**84. Sema: Kila mmoja anafanya kwa namna yake. Na Mola wenu Mlezi Anajua aliyeongoka katika njia.**

**Kugeuka kuwa Mbali na Allah تعالى Wakati wa Ukunjufu na Kukata Tamaa Wakati wa Shida**

Allah تعالى Anatarifu kuhusu maumbile ya udhaifu wa mwanadamu katika nyakati za raha na shida, ila kwa yule Aliyehifadhiwa. Pindi Allah تعالى Anapomneemesha mwanadamu kwa kumpatia mali, siha nzuri, wepesi na raha, riziki na usaidizi, na anapata anachotaka, hukengeuka kutoka katika utiifu na kumuabudu Allah تعالى na huwa mwenye kiburi.

Amesema Mujahid: "Hii inamaanisha anakengeuka kutoka Kwetu (anajitenga Nasi)"<sup>1</sup>. Nikasema, hii ni kama Kauli Yake Aliyetukuka:

فَلَمَّا كَشَفْنَا عَنْهُ صُورَهُ مَرَّ كَأَن لَّمْ يَدْعُنَا إِلَىٰ صُورٍ مِّسَّهُ<sup>٤</sup>

**"Lakini Tunapomuondolea dhara yake hupita (akafanya atakayo) kama kwamba hakuwa Akituomba Tumuondoshee dhara iliyompata." (10:12).**

Na Kauli Yake:

فَلَمَّا نَجَّيْنَاكَ إِلَى الْبَرِّ أَعْرَضْتُمْ<sup>٤</sup>

**"Lakini Anapokufikisheni salama nchi kavu, mnakengeuka." (17:67)**

Mwanadamu anapokumbwa na shari, nayo ni misiba, ajali na madhara,

كَانَ يَؤُوسًا

**"Hukata tamaa." Maana yake: Kukata tamaa anadhani kuwa hatapata kheri tena baada ya hayo. Hii ni kama Kauli Yake Aliyetukuka:**

وَلَيْنَ أَدَقْنَا آلَ نَسْرٍ مِنَّا رَحْمَةً نُّمَّ نَزَعْنَاهَا مِنْهُ إِنَّهُ لَيَؤُوسٌ كَفُورٌ ﴿١١﴾ وَلَيْنَ أَدَقْنَاهُ

نَعْمَاءَ بَعْدَ صِرَاءٍ مَسَّتُهُ لَيَقُولَنَّ ذَهَبَ السَّيِّئَاتُ عَنِّي<sup>٤</sup> إِنَّهُ لَفَرِحَ فَخُورٌ ﴿١٢﴾ إِلَّا الَّذِينَ

صَبَرُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أُولَٰئِكَ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ كَبِيرٌ ﴿١٣﴾

**"Na kama Tukimuonjesha mwanadamu rehemu inayotokana Nasi; kisha Tukaiondoa kwake, mara moja anakuwa mwenye kukata tama kabisa na asiyekuwa na shukrani. Na kama Tukimuonjesha neema baada ya dhara iliyompata mara husema: 'Taabu zimekwishaondoka kwangu'. Wala hashughuliki kufanya mema wala kumshukuru Allah. Basi huwa sasa ni mwenye kufurahi sana na mwenye kujivuna kabisa. Lakini wale wanaosubiri na kufanya vitendo vizuri, hao ndio watakaopata msamaha na ujira mkubwa." (11:9-11)**

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

<sup>1</sup> At-Tabari 17:539.

قُلْ كُلٌّ يَعْمَلُ عَلَيَّ شَاكِلِيَّةٍ

**“Sema: Kila mmoja anafanya kwa namna yake”.**

Amesema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما: “Kwa mujibu na mwelekeo wake”<sup>1</sup>. Mujaahid amesema: “Kulingana na mwelekeo na maumbile yake”<sup>2</sup>. Na Qataadah amesema: “Kulingana na nia yake”<sup>3</sup>. Na Ibn Zayd amesema: “Kulingana na Dini yake”<sup>4</sup>. Kauli zote hizi ziko karibu katika maana. Aya hii – na Allah تعالى Anajua zaidi – ni tishio na onyo kwa washrikina, kama ile ayah:

وَقُلْ لِلَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ أَعْمَلُوا عَلَيَّ مَكَانَتِكُمْ إِنَّا عَمِلُونَ ﴿١٢١﴾

**“Na waambie wale wasioamini: Fanyeni muyatakayo kwa tamkini yenu.” (11:121).** Kwa hiyo, Allah تعالى Amesema:

قُلْ كُلٌّ يَعْمَلُ عَلَيَّ شَاكِلِيَّةٍ فَرِيكُمُ أَعْلَمُ بِمَنْ هُوَ أَهْدَىٰ سَبِيلًا ﴿٨٥﴾

**“Sema: Kila mmoja anafanya kwa namna yake. Na Mola wenu Mlezi Anajua aliyeongoka katika njia.” (17:84)**

Maana yake: Sisi na nyinyi. Kila mmoja atalipwa kulingana na amali zake, kwani hakuna kinachofichwa na Allah تعالى.

وَسْئَلُونَكَ عَنِ الرُّوحِ ۗ قُلِ الرُّوحُ مِنْ أَمْرِ رَبِّي وَمَا أُوتِيتُمْ مِنَ الْعِلْمِ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٨٥﴾

**85. Na wanakuuliza habari za Roho. Sema: Roho ni katika mambo ya Mola wangu Mlezi. Nanyi hamkupewa katika elimu ila kidogo tu.**

### Kutajwa kwa Roho (Ruuh)

Amepokea Al-Bukhaariy katika kufasiri Aya kutoka kwa Abdallah bin Mas’ud رضي الله عنه amesema: Nilipokuwa natembea pamoja na Mtume ﷺ shambani akiwa ameegemea kwenye kigingi cha mtende, walipopita Mayahudi. Wakasema baadhi yao kwa wengine: “Muulizeni kuhusu Roho”. Wakasema: “Ni lipi linalowahimiza kumuuliza kuhusu hilo?” Wengine wakasema:

<sup>1</sup> At-Tabari 17:541.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:541.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:541.

<sup>4</sup> At-Tabari 17:541.

“Musimuulize asije akawapa jawabu msilolipenda”. Wakasema: “Muulizeni”. Hivyo wakamuuliza kuhusu Roho. Mtume ﷺ alinyamaza wala asiwajibu chochote, nikajua kuwa anapata wahyi, hivyo nikakaa nilipo. Uteremsho wa Wahyi ulipomalizika, Mtume ﷺ alisema:

وَسْئَلُونَكَ عَنِ الرُّوحِ قُلِ الرُّوحُ مِنْ أَمْرِ رَبِّي

**“Na wanakuuliza habari za Roho. Sema: Roho ni katika mambo ya Mola wangu Mlezi.”**

Na muktadha huu huenda ukaonesha kuwa Aya hii iliteremka Madinah, na kuwa iliteremshwa pindi Mayahudi walipomuuliza swali hilo huko Madinah, japokuwa Sura nzima iliteremka Makka. Hili linaweza kujibiwa kwa yale maoni kuwa Aya inaweza kuwa imeteremshwa Madina mara ya pili, baada ya kuwa tayari ilikuwa imeteremshwa Makka, au inawezekana kuwa alipatiwa Wahyi na alijibu swali lao kwa Aya ambayo ilikuwa tayari imeteremshwa, yaani Aya tunayoizungumzia.

Na imepokewa na Ibn Jariir رحمه الله تعالى kuwa ‘Ikrimah رضي الله عنه amesema: “Watu wa Kitabu walimuuliza Mtume ﷺ kuhusu Roho, na Allah تعالى Akateremsha:

وَسْئَلُونَكَ عَنِ الرُّوحِ

**‘Na wanakuuliza habari za Roho.’**

Wakasema: ‘Unadai kuwa hatukupatiwa elimu ila kidogo nasi tumepewa Taurati nayo ni Hikmah:

وَمَنْ يُؤْتَ الْحِكْمَةَ فَقَدْ أُوتِيَ خَيْرًا كَثِيرًا

**‘Na aliyepewa hekima bila shaka amepewa kheri nyingi.’ (2:269)**

Akasema: Kisha ikateremka,

وَلَوْ أَنَّمَا فِي الْأَرْضِ مِنْ شَجَرَةٍ أَقْلَمٌ وَالْبَحْرُ يَمُدُّهُ مِنْ بَعْدِهِ سَبْعَةُ أُخْرٍ

**‘Na lau kama miti yote iliyomo katika ardhi ingalikuwa kalamu, na bahari hii ikafanywa wino, na ikasaidiwa na bahari nyingine saba.’ (31:27)**

Akasema: ‘Hamkupatiwa katika elimu ambayo kwayo Allah تعالى Atawaokoa

na Moto, hiyo itakuwa ni kubwa na nzuri, lakini kulinganisha na elimu ya Allah تعالى ni kidogo sana<sup>1</sup>."

Amepokea Al-Awfiy kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema yafuatayo kuhusu Kauli Yake:

وَسْأَلُونَكَ عَنِ الرُّوحِ

**"Na wanakuuliza khabari za Roho."**

Na hiyo ni kuwa Mayahudi walimuambia Mtume ﷺ awaeleze kuhusu Roho na vipi Roho itaadhibiwa ndani ya mwili. Na hakika ni kwamba Roho inajulikana na Allah تعالى tu na hakukuwa na Wahyi kuihusu. Hakuwajibu kabisa, na baadae Jibril عليه السلام alikuja, akamuambia:

قُلِ الرُّوحُ مِنْ أَمْرِ رَبِّي وَمَا أُوتِيتُمْ مِنَ الْعِلْمِ إِلَّا قَلِيلًا ﴿١٧٠﴾

**"Sema: Roho ni katika mambo ya Mola wangu Mlezi. Nanyi hamkupewa katika elimu ila kidogo tu".**

Mtume ﷺ akawajulisha kuhusu hilo. Wakasema: "Ni nani aliyekujia (aliyekuambia) na hilo?" Akasema:

«جَاءَنِي بِهِ جِبْرِيلُ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ»

**"Ameniletea Jibril kutoka kwa Allah".**

Wakasema: "Kwa Allah تعالى, hakuna aliyekuambia isipokuwa adui wetu (Maana yake: Jibril عليه السلام)". Allah تعالى Akateremsha:

قُلْ مَنْ كَانَ عَدُوًّا لِجِبْرِيلَ فَإِنَّهُ نَزَّلَهُ عَلَى قَلْبِكَ بِإِذْنِ اللَّهِ مُصَدِّقًا لِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ

**"Sema: 'Anayemfanyia ushinde (uadui) Jibril (mwache afe na hasira zake); kwani yeye ameiteremsha Qur'ani moyoni mwako kwa idhini ya Allah; Qur'ani inayosadikisha yale yaliyokuwa kabla yake." (2:97)<sup>2</sup>.**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:542.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:543. Zipo riwaya nyingi kuhusu hili. Mapokezi kutoka kwa 'Ikrimah ni Mursal. Sanadi yake ni dhaifu.

## Roho na Nafsi

As-Suhayliy رحمه الله تعالى ametaja tofauti baina ya wanazuoni kuhusu Roho kama ni sawa na Nafsi au ni nyengineyo (au ni tofauti). Amesema kuwa Roho ni nyepesi na laini kama hewa, inapita ndani ya mwili kama maji yanavyopita katika mishipa ya miti. Na amesema kuwa Roho inayopulizwa na Malaika katika kijusi ni Nafsi, kwa sharti iungane na mwili na kupata sifa fulani kwa sababu yake, sifa hiyo ima nzuri au mbaya. Kwa hiyo, inakuwa ima ni Nafsi iliyotulia au Nafsi inayoamrisha maovu, kama vile maji ni uhai kwa miti, kwa kuchang'anyika nayo, inatoa kitu chengine kabisa. Hivyo, ikichang'anyika na zabibu, na zabibu zikakamuliwa, unapata juisi au pombe. Hapo haitaitwa tena maji, isipokuwa kiistiari. Hivyo, tunafaa tufahamu haiitwi Nafsi, Roho isipokuwa kwa njia hii. Yapo mafungamano baina ya Nafsi na Roho: Roho haiitwi Nafsi ila inapoungana na mwili na kuathiriwa nayo. Kwa kuhitimisha tunaweza kusema: Roho ndio asili na kiini, na Nafsi imeungana na Roho na mafungamano yake na mwili. Hivyo, hulingana sawa katika njia moja lakini sio njia zote. Na hii ni maana nzuri, na Allah تعالى Anajua zaidi<sup>1</sup>. Ninasema: Huenda watu wakazungumza kuhusu kiini cha Roho na hukumu zake, na vitabu vingi vimeandikwa kuhusu mada hii. Na bora aliyezungumzia kuhusu hili ni Al-Haafidh Ibn Mandah رحمه الله تعالى katika Kitabu tulichokisikia kuhusu Roho.




---

<sup>1</sup> Ar-Rawdh Al-Anf 2:62.

وَلَيْنَ شِعْرَانَا لَنَنْذَرَنَّهُ بِالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ ثُمَّ لَا يَجِدُ لَكَ  
 بِهِ عَلَيْنَا وَكَيْلًا ﴿٨٦﴾ إِلَّا رَحْمَةً مِن رَّبِّكَ ۗ إِنَّ  
 فَضْلَهُ كَانَ عَلَيْكَ كَظِيمًا ﴿٨٧﴾ قُل لِّئِنِ اجْتَمَعَتِ  
 الْإِنْسُ وَالْجِنُّ عَلَىٰ أَنْ يَأْتُوا بِمِثْلِ هَذَا الْقُرْآنِ لَا يَأْتُونَ  
 بِمِثْلِهِ وَلَوْ كَانَ بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ ظَهِيرًا ﴿٨٨﴾ وَلَقَدْ  
 صَرَّفْنَا لِلنَّاسِ فِي هَذَا الْقُرْآنِ مِنْ كُلِّ مَثَلٍ فَأَبَىٰ أَكْثَرُ  
 النَّاسِ إِلَّا كُفُورًا ﴿٨٩﴾ وَقَالُوا لَنْ نُؤْمِنَ بِكَ حَتَّىٰ  
 تَفْجُرَ لَنَا مِنَ الْأَرْضِ يَدْعُوبًا ﴿٩٠﴾ أَوْ تَكُونَ لَكَ جَنَّةٌ  
 مِّنْ نَّحِيلٍ وَعِنَبٍ فَتُفَجَّرَ الْأَنْهَارُ خِلْفَهَا تَفْجِيرًا ﴿٩١﴾ أَوْ  
 تُسْقِطَ السَّمَاءَ كَمَا زَعَمَتِ عَلَيْنَا كَيْفًا أَوْ تَأْتِيَنَا بِاللَّهِ  
 وَالْمَلَائِكَةِ قَبِيلًا ﴿٩٢﴾ أَوْ يَكُونُ لَكَ بَيْتٌ مِّن رُّحُوفٍ أَوْ  
 تَرْقَىٰ فِي السَّمَاءِ وَلَنْ نُؤْمِنَ لِرُؤْيَاكَ حَتَّىٰ تُنَزَّلَ عَلَيْنَا كِتَابًا  
 نَّقْرُؤُهُ ۗ قُلْ سُبْحَانَ رَبِّيَ هَلْ كُنْتُ إِلَّا بَشَرًا رَسُولًا ﴿٩٣﴾  
 وَمَا مَنَعَ النَّاسَ أَنْ يُؤْمِنُوا إِذْ جَاءَهُمُ الْهُدَىٰ إِلَّا أَنْ قَالُوا  
 أَبْعَثَ اللَّهُ بَشَرًا رَسُولًا ﴿٩٤﴾ قُلْ لَوْ كَانَتْ فِي الْأَرْضِ  
 مَلَائِكَةٌ يَّمشُونَ مُطْمَئِنِينَ لَنَزَلْنَا عَلَيْهِمْ مِن  
 السَّمَاءِ مَلَكًا رَسُولًا ﴿٩٥﴾ قُلْ كَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِدًا بَيْنِي  
 وَبَيْنَكُمْ ۗ إِنَّهُ كَانَ بِعِبَادِهِ خَبِيرًا بَصِيرًا ﴿٩٦﴾

وَلَيْنَ شِعْرَانَا لَنَنْذَرَنَّهُ بِالَّذِي أَوْحَيْنَا  
 إِلَيْكَ ثُمَّ لَا يَجِدُ لَكَ بِهِ عَلَيْنَا  
 وَكَيْلًا ﴿٨٦﴾ إِلَّا رَحْمَةً مِن رَّبِّكَ  
 ۗ إِنَّ فَضْلَهُ كَانَ عَلَيْكَ كَظِيمًا  
 ﴿٨٧﴾ قُل لِّئِنِ اجْتَمَعَتِ الْإِنْسُ  
 وَالْجِنُّ عَلَىٰ أَنْ يَأْتُوا بِمِثْلِ هَذَا  
 الْقُرْآنِ لَا يَأْتُونَ بِمِثْلِهِ وَلَوْ كَانَتْ  
 بَعْضُهُمْ لِبَعْضٍ ظَهِيرًا ﴿٨٨﴾  
 وَلَقَدْ صَرَّفْنَا لِلنَّاسِ فِي هَذَا الْقُرْآنِ مِنْ  
 كُلِّ مَثَلٍ فَأَبَىٰ أَكْثَرُ النَّاسِ إِلَّا  
 كُفُورًا ﴿٨٩﴾

**86. Na Tungelipenda  
 Tungeliyaondoa Tuliyo  
 kufunulia. Kisha usunge-  
 lipata mwakilishi wa  
 kukupigania Kwetu kwa  
 haya.**

**87. Isipokuwa iwe rehema  
 itokayo kwa Mola wako  
 Mlezi. Hakika Fadhila Yake  
 kwako ni kubwa.**

**88. Sema: Wangeliku-  
 sanyika watu na majini ili  
 walete mfano wa Qur'ani  
 hii basi hawaleti mfano  
 wake, hata wakisaidiana  
 wao kwa wao.**



**89. Na hakika Tumewaeleza watu katika Qur'ani hii kwa kila mfano. Lakini watu wengi wanakataa isipokuwa kukanusha tu.**

### Angetaka Allah تعالی Angeichukua Qur'ani

Allah تعالی Anataja ile Neema na Fadhila Aliyompatia mja na Mtume Wake ﷺ kwa Kumteremshia Qur'ani, Kitabu ambacho batili haiwezi kukikaribia kabisa mbele au nyuma yake, ni ufunuo kutoka kwa Mwenye Hekima, Mwenye Kuhimidiwa. Amesema Ibn Mas'ud رضي الله عنه: "Utawajia watu upepo mwekundu, kumaanisha mwisho wa wakati (karibu sana na Kiyama) kutoka Shaam (Syria). Wakati huo hautabakia Msahafu wala Aya katika moyo wa mtu." Kisha Ibn Mas'ud رضي الله عنه akasoma:

وَلَيْنَ شِعْنَا لَنَذْهَبَنَّ بِالَّذِي أَوْحَيْنَا إِلَيْكَ

**"Na Tungelipenda Tungeliyaondoa Tuli yokufunulia".**

### Changamoto ya Qur'ani

Kisha Allah تعالی Anatutanabahisha utukufu na ubora wa Qur'ani, na Akatuambia kuwa lau wanadamu na Majini wote wakaafikiana kuleta sawa na Aliyoteremsha Allah تعالی kwa Mtume Wake, hawataweza hilo hata ikiwa ni kusaidiana. Hili ni jambo ambalo haliwezekani. Vipi yatakuwa maneno ya viumbe yawe kama ya Muumba asiye na mshirika, marafiki wala mfano wake na hakuna yeyote anayefanana Naye. Na Kauli Yake:

وَلَقَدْ صَرَّفْنَا لِلنَّاسِ

**"Na hakika Tumewaeleza watu."**

Maana yake: Tumewapatia ishara na hoja za wazi, na kuwaonesha na kuwaelezea wao haki kwa njia nyepesi. Pamoja na hayo, "Lakini watu wengi wanakataa isipokuwa kukanusha tu." Maana yake: Kuipinga haki na kuyakataa na kuyarudisha yaliyo sahihi.

<sup>1</sup> At-Tabari 17:546.

وَقَالُوا لَنْ نُؤْمِنَ بِكَ حَتَّىٰ تَفْجُرَ لَنَا مِنَ الْأَرْضِ يَنْبُوعًا ﴿٩٦﴾ أَوْ تَكُونَ لَكَ جَنَّةٌ مِّنْ  
 خَيْلٍ وَعِجْبٍ فَتَفْجُرَ الْأَنْهَارَ حَلَالَهَا تَفْجِيرًا ﴿٩٧﴾ أَوْ تُسْقِطَ السَّمَاءَ كَمَا زَعَمَتْ عَلَيْنَا  
 كِسْفًا أَوْ تَأْتِيَ بِاللَّهِ وَالْمَلَائِكَةِ قَبِيلًا ﴿٩٨﴾ أَوْ يَكُونَ لَكَ بَيْتٌ مِّنْ زُخْرَفٍ أَوْ تَرْقَىٰ فِي  
 السَّمَاءِ وَلَنْ نُؤْمِنَ بِكَ حَتَّىٰ تُنَزِّلَ عَلَيْنَا كِتَابًا نَّقْرُؤُهُ ۗ قُلْ سُبْحَانَ رَبِّيَ هَلْ كُنْتُ  
 إِلَّا بَشَرًا رَسُولًا ﴿٩٩﴾

**90. Na walisema: Hatutakuamini mpaka ututimbulie chemchem katika ardhi hii.**

**91. Au uwe na kitalu cha mitende na mizabibu, na utububujishie mito kati yake ikimiminika.**

**92. Au utuangushie mbingu vipande vipande kama ulivyo dai; au utuletee Allah na Malaika uso kwa uso.**

**93. Au uwe na nyumba ya dhahabu<sup>1</sup>, au upae mbinguni. Wala hatutaamini kupaa kwako mpaka ututeremshie kitabu tukisome. Sema: Subhana Rabbi, Ametakasika Mola wangu Mlezi! Kwani mimi ni nani isipokuwa ni mwanadamu na Mtume?**

## Matakwa ya Makuraysh ya Kuoneshwa Ishara Maalumu na Kukataliwa Kwao

Ibn Jariir رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Muhammad bin Is'haaq رحمه الله تعالى, amenihadithia mkongwe kati ya watu wa Misri aliyekuja kwetu kiasi cha miaka arobaini na ushei<sup>1</sup>, kutoka kwa 'Ikrimah kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kuwa 'Utbah na Shaybah – watoto wawili wa Rabi'ah, Abu Sufyaan bin Harb, mtu kutoka katika ukoo wa 'Abd Ad-Daar, Abu al-Bakhtariy – ndugu wa Bani Asad, Al-Aswad bin Al-Muttwalib bin Asad, Zam'ah bin Al-Aswad, Waliyd bin Al-Mughirah, Abu Jahl bin Hishaam, Abdallah bin Abi Umayyah, Umayyah bin Khalaf, Al-Aasw bin Wa'il, Nabiih na Munabbih – watoto wawili wa Al-Hajjaaj As-Sahmin, walikusanyika wote au baadhi yao baada ya machweo nyuma ya Ka'bah. Baadhi yao walisema kwa wengine: "Tumeni mtu kwa Muhammad

<sup>1</sup> Ni baina ya tatu hadi tisa.

akamuite, mzungumze na jadilieni naye, ili wasifikirie watu kuwa sisi ndio wa kulaumiwa". Walituma mtu kwenda kumuita, akamuambia: "Watukufu wa watu wako wamekusanyika ili uzungumze nao." Kwa ajili hiyo Mtume ﷺ alikuja haraka haraka, akidhania kuwa huenda wakabadilisha mawazo yao, kwani alikuwa na hamu sana waongoke, na alikuwa anahuzunishwa sana kuona ukaidi wao. Hivyo alikuja na akakaa nao, wakasema: "Ewe Muhammad! Tumetuma uitwe ili asidhanie yeyote kuwa sisi ndio wa kulaumiwa. Kwa Allah تعالى, hakuna mtu miongoni mwa Waarabu aliyeleta kwa watu wake kama wewe. Umewakashifu mababu, ukaikosoa dini yetu, ukatutusi, ukawakashifu miungu yetu na ukaleta mfarakano. Hakuna uovu wowote uliobaki isipokuwa umeuleta baina yetu na yako. Ikiwa umekuja na mambo haya kwa kuwa unataka mali, tutakukusanyia mali yetu mpaka uwe wewe ndiye mwenye mali nyingi kuliko sote. Na ikiwa unataka utukufu baina yetu kwayo, tutakufanya kiongozi wetu. Na ikiwa unataka ufalme, tutakupatia. Na ikiwa yanayokujia ni aina ya Jini aliyekushinda, na huenda ikawa una shida hiyo, basi tutatumia mali yetu ili tukupatie tiba mpaka akuondokee ili tusilaumiwe." Mtume ﷺ akasema:

«مَا بِي مَا تَقُولُونَ، مَا جِئْتُكُمْ بِمَا جِئْتُكُمْ بِهِ أَطْلُبُ أَمْوَالَكُمْ، وَلَا الشَّرَفَ فِيكُمْ، وَلَا الْمُلْكَ عَلَيْكُمْ، وَلَكِنَّ اللَّهَ بَعَثَنِي إِلَيْكُمْ رَسُولًا وَأَنْزَلَ عَلَيَّ كِتَابًا، وَأَمَرَنِي أَنْ أَكُونَ لَكُمْ بَشِيرًا وَنَذِيرًا، فَبَلَّغْتُكُمْ رَسُولَاتِ رَبِّي وَنَصَحْتُ لَكُمْ، فَإِنْ تَقَبَّلُوا مِنِّي مَا جِئْتُكُمْ بِهِ فَهُوَ حَظُّكُمْ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ، وَإِنْ تَرُدُّوهُ عَلَيَّ أُضِيزْ لِأَمْرِ اللَّهِ حَتَّى يَخُذَكُمْ اللَّهُ بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ»

*"Mimi sina yote mlioyasema. Sikuja na niliokuja nayo nikitaka wala kutarajia mali yenu, wala utukufu baina yenu, wala ufalme juu yenu, lakini Allah Amenituma mimi kuwa Mtume kwenu na Akaniteremshia Kitabu, na Akaniamuru niwe mwenye kuwaletea bishara njema na kuwaonya. Nimefikisha ujumbe wa Mola wangu Mlezi na nimewanasihi vilivyo. Ikiwa mtayakubali niliyokuja nayo, hiyo itakuwa ni bahati yenu nzuri hapa duniani na Kesho Akhera, na mkipinga nitasubiri Amri ya Allah mpaka Atuhukumu baina yangu na yenu." au kama alivyosema Mtume Muhammad ﷺ.*

Wakasema: "Ewe Muhammad! Ikiwa hutakubali tuliyokupatia, unajua kuwa hakuna watu wenye ardhi ndogo, mali kidogo na wenye hali ngumu kama sisi,

hivyo muombe Mola wako Mlezi Aliyekutuma kwa alichokutuma Kuisukuma milima ambayo inatubana na Kuipanua ardhi yetu na Aijaalie mito kama ile mito ya Shaam na Iraq, na Kuwafufua babu zetu waliokufa. Wawe miongoni watakaofufuliwa ni Ousayy bin Kilaab. Kwani yeye alikuwa mzee mkweli, nasi tutamuuliza kama unasema kweli au uwongo. Ukifanya tunayoyataka, na waliofufuliwa wakasema kuwa unasema ukweli. Hapo tutakuamini na kuikubali hadhi na cheo chako mbele ya Allah تعالیٰ na tutaamini kuwa Amekutuma Mtume kama ulivyosema." Mtume ﷺ akawaambia:

«مَا بِهَذَا بُعِثُ، إِنَّمَا جِئْتُكُمْ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ بِمَا بَعَثَنِي بِهِ، فَقَدْ بَلَّغْتُكُمْ مَا أُرْسِلْتُ بِهِ إِلَيْكُمْ، فَإِنْ تَقْبَلُوهُ فَهُوَ حَظُّكُمْ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ، وَإِنْ تَرُدُّوهُ عَلَيَّ أَصِيبَ لِأَمْرِ اللَّهِ حَتَّى يَحْكُمَ اللَّهُ بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ»

*"Sikutumwa kwa ajili hii. Nimekuleteeni kutoka kwa Allah kwa Alichonituma, nami nimefikisha risala niliyotumwa nayo. Mkikubali niliyowaleteeni hiyo itakuwa ni bahati nzuri kwenu hapa duniani na Kesho Akhera, lakini mkikataa, nitangojea kwa uvumilivu Amri ya Allaah mpaka Allah Ahukumu baina yangu na nyinyi."*

Wakasema: "Ukitufanyia haya, fanya kwa ajili ya nafsi yako. Muombe Mola wako Mlezi Amtume Malaika kuyakinisha kwamba unayoyasema ni kweli na azungumze kwa niaba yako. Muombe Akupe bustani, hazina, makasri ya dhahabu na fedha, na Akufanye wewe si muhitajia wa yeyote ili usiwe ni mwenye kufanya unayofanya, kwani wewe unasimama masokoni ukitafuta riziki kama sisi. Hapo tutajua fadhila na ubora wa cheo chako mbele ya Mola wako Mlezi na kama wewe ni Mtume kama unavyodai". Mtume ﷺ akawaambia:

«مَا أَنَا بِفَاعِلٍ، مَا أَنَا بِالَّذِي يَسْأَلُ رَبَّهُ هَذَا، وَمَا بُعِثْتُ إِلَيْكُمْ بِهَذَا، وَلَكِنَّ اللَّهَ بَعَثَنِي بَشِيرًا وَنَذِيرًا، فَإِنْ تَقْبَلُوا مَا جِئْتُكُمْ بِهِ، فَهُوَ حَظُّكُمْ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ، وَإِنْ تَرُدُّوهُ عَلَيَّ أَصِيبَ لِأَمْرِ اللَّهِ حَتَّى يَحْكُمَ اللَّهُ بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ»

*"Sitafanya hivyo, wala sitamuuliza Mola wangu Mlezi hilo. Mimi sikutumwa kwa sababu hiyo, lakini Allah Amenituma kwenu kuwapatia bishara njema na kuwaonya. Mkikubali niliyowaletea, hiyo itakuwa bahati nzuri kwenu hapa duniani na Kesho Akhera, na*

*mkiikataa, nitasubiri huku nikingojea Amri ya Allah mpaka Ahukumu baina yangu na nyinyi."*

Wakasema: "Fanya mbingu zituangukie, kama unavyodai kuwa Mola wako Mlezi Akitaka Anaweza fanya. Hatutakuamini mpaka ufanye hilo". Mtume ﷺ akawaambia:

«ذَلِكَ إِلَى اللَّهِ، إِنْ شَاءَ فَعَلَ بِكُمْ ذَلِكَ»

*"Hilo ni juu ya Allah Kuamua, Akitaka Atakufanyieni".*

Wakasema: "Ewe Muhammad! Mola wako Mlezi Hakujuu kuwa tutakaa nawe na kukuuliza tuliyokuuliza na kukupatia maombi yetu tuliyokupatia? Angekuambia kabla na Kukufundisha namna gani utatujibu, na pia Kukufahamisha Atakavyotufanya ikiwa hatutakubali wito wako. Tumesikia kuwa anayekufundisha haya ni mtu wa Al-Yamaamah anayelitwa Ar-Rahman. Nasi twaapa kwa Allah تعالی, hatutamuamini Ar-Rahman. Tunakuonya, ewe Muhammad, hatutakuacha ufanye unayofanya mpaka wewe au sisi tuangamizwe." Mmoja wao akasema: "Tunawaabudu Malaika, nao ni mabinti wa Allah". Mwingine akasema: "Hatutakuamini mpaka utuletee Allah na Malaika uso kwa uso". Waliposema haya, Mtume ﷺ aliinuka na kuondoka. 'Abdallah bin Abi Umayyah bin Al-Mughirah bin 'Abdallah bin 'Umar bin Makhzum, mtoto wa shangazi yake, 'Atikah bint 'Abdul-Muttwalib, alinyanyuka pia na kumfuata. Alimuambia: "Ewe Muhammad! Watu wako wamekuahidi waliyokuahidi, nawe hukukubali hayo. Kisha wakakuomba vitu, ili wapate kujua cheo chako mbele ya Allah تعالی, nawe hukuwafanyia. Kisha wakakutaka uharakishe adhabu juu yao kwa unayowakhofisha. Naapa kwa Allah تعالی! Sitakuamini mpaka upande ngazi kuelekea mbinguni, ilhali ninakutizama, baada ya hapo ulete Kitabu kilichofunuliwa na Malaika wanne kushuhudia kuwa unayosema ni kweli. Naapa kwa Allah تعالی! Hata ukifanya hayo, nadhani sitakuamini." Kisha akaondoka kwa Mtume ﷺ, na Mtume ﷺ akaelekea nyumbani kwa familia yake, akiwa amehuzunika kuwa amekosa fursa ambayo alitizamia pale watu wake walipomuita, kwa sababu aliona kuwa wanazidi kuwa mbali naye"<sup>1</sup>.

<sup>1</sup> At-Tabari 17:557. Kisa hiki si sahihi.

### Sababu ya Kukataliwa Matakwa ya Washirikina

Na katika kikao hiki ambacho Makuraysh walikuja pamoja ili kuzungumza na Mtume ﷺ, lau Allah تعالى Angejua kuwa wanafanya maombi hayo kwa ajili ya kutaka uongofu, wangekubaliwa, lakini Alijua kuwa wanataka hayo kwa ukafiri, inadi na ukaidi. Mtume ﷺ aliambiwa: "Ukitaka Tutawapatia watakacho, lakini wakikufuru baada ya hapo, Nitawaadhibu kwa adhabu ambayo sijawahi Kumpatia yeyote hapa duniani; au Nikitaka, Nitawafungulia mlango wa tauba na rehema." Akasema:

﴿بَلْ تَفْتَحْ عَلَيْهِمْ بَابَ التَّوْبَةِ وَالرَّحْمَةَ﴾

*"Bali, wafungulie mlango wa toba na rehema"*<sup>1</sup>.

Na hii ni kama Kauli Yake Aliyetukuka:

وَمَا مَنَعَنَا أَنْ نُرْسِلَ بِالْآيَاتِ إِلَّا أَنْ كَذَّبَ بِهَا الْأَوْلُونَ ۖ وَءَاتَيْنَا ثُمُودَ النَّاقَةَ مُبْصِرَةً فَظَلَمُوا بِهَا ۗ وَمَا نُرْسِلُ بِالْآيَاتِ إِلَّا تَخْوِيفًا ﴿٥٨﴾

***"Na hapana kinachotuzuia Kupeleka miujiza ila ni kuwa watu wa zamani waliikanusha. Na Tuliwapa Wathamudi ngamia jike kuwa ni Ishara iliyo dhahiri, lakini walidhulumu kwaye. Nasi Hatupeleki Ishara ila kwa ajili ya kuhadharisha."* (17:59).**

Na Amesema Aliyetukuka:

وَقَالُوا مَالِ هَذَا الرَّسُولِ يَأْكُلُ الطَّعَامَ وَيَمْشِي فِي الْأَسْوَاقِ لَوْلَا أَنْزَلَ إِلَيْهِ مَلَكٌ فَيَكُونُ مَعَهُ نَذِيرًا ﴿٦٧﴾ أَوْ يُلْقَىٰ إِلَيْهِ كَنْزٌ أَوْ تَكُونُ لَهُ جَنَّةٌ يَأْكُلُ مِنْهَا وَقَالَ الظَّالِمُونَ إِنْ تَتَّبِعُونَ إِلَّا رَجُلًا مَسْحُورًا ﴿٦٨﴾ أَنْظِرْ كَيْفَ ضَرَبُوا لَكَ الْأَمْثَلَ فَضَلُّوا فَلَا يَسْتَطِيعُونَ سَبِيلًا ﴿٦٩﴾ تَبَارَكَ الَّذِي إِنْ شَاءَ جَعَلَ لَكَ خَيْرًا مِنْ ذَلِكَ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ وَيَجْعَلُ لَكَ قُصُورًا ﴿٧٠﴾ بَلْ كَذَّبُوا بِالسَّاعَةِ ۖ وَأَعْتَدْنَا لِمَنْ كَذَّبَ بِالسَّاعَةِ سَعِيرًا ﴿٧١﴾

<sup>1</sup> Ahmad 1:242.

***“Na wakasema: ‘Mtume gani huyu anayekula chakula na anayekwenda sokoni! Mbona hakuteremshiwa Malaika awe muonyaji pamoja naye? Au mbona hakuangushiwa hazina, au kwa nini asiwe na bustani ale katika hiyo’. Na madhalimu wakasema tena: ‘Nyinyi hamumfuati ila mtu aliyerogwa’. Tazama jinsi wanavyokupigia mifano isiyokuelekea, basi wamepotea wala hawataweza kushika njia iliyonyooka. Ni mwenye kuleta baraka kweli kweli yule ambaye akitaka atakufanyia bora kuliko hivyo; atakupu bustani ya Peponi zipitazo mito mbele yake na akujaalie na majumba ya kifalme huko. Bali wanakadhibisha Kiyama; na Tumewaandalia wanaokadhibisha Kiyama Moto mkali kabisa.”***  
(25:7-11).

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

حَتَّى تَفْجُرَ لَنَا مِنَ الْأَرْضِ يَنْبُوعًا ﴿١٧﴾

***“Mpaka ututimbulie chemchem katika ardhi hii.”***

*Al-Yanbuu'* ina maana ya chemchem ya maji yanayobubujika.

Walimtaka awatolee chemchem ya maji tamu katika ardhi ya Hijjaz, hapa na pale. Hili ni jambo sahali sana kwa Allah تعالی Akitaka, Anaweza kufanya hilo. Angewajibu kwa yote waliyoomba na kutaka, lakini Alijua kuwa hawataongoka kwa hayo, kama Alivyosema:

إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٨﴾ وَلَوْ جَاءَتْهُمْ كُلُّ آيَةٍ حَتَّى

يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿١٩﴾

***“Hakika wale ambao neno la Mola wako Mlezi limekwisha wathibitika juu yao, hawataamini. Ijapokuwa kila ishara itawajia; mpaka waone adhabu inayoumiza.”*** (10:96-97).

Na Amesema Aliyetukuka:

\* وَلَوْ أَنَّا نَزَّلْنَا إِلَهُمُ الْمَلٰٓئِكَةَ وَكَلَّمَهُمُ الْمَوْتَىٰ وَحَشَرْنَا عَلَيْهِمْ كُلَّ شَيْءٍ قُبُلًا مَا كَانُوا

لِيُؤْمِنُوا

***“Na lau Tungewateremshia Malaika, na wafu wakazungumza nao (kuwa haya ni kweli), na Tukawakusanyia kila kitu mbele yao, wasingeamini.” (6:111)***

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

أَوْ تُسْقِطَ السَّمَاءَ كَمَا زَعَمَت

***“Au utuangushie mbingu vipande vipande kama ulivyo dai.”***

Maana yake: Umetuahidi kuwa Siku ya Kiyama mbingu zitapasuka, zitavunjwa na kuraruliwa, baadhi ya sehemu zake zikianguka chini, hivyo fanya hivyo hapa duniani kwa kufanya ianguke vipande vipande.

Hii ni kama Kauli Yake:

اللَّهُمَّ إِن كَانَتْ هَذَا هُوَ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِكَ فَأَمْطِرْ عَلَيْنَا حِجَابًا مِنَ السَّمَاءِ

***“Ee Allaah! Kama haya ni haki itokayo Kwako, basi tupige kwa mvua ya mawe yanayotoka mbinguni.” (8:32)***

Na hivyo hivyo, watu wa Shu'ayb عليه السلام walidai hilo, kwa kusema:

فَأَسْقِطْ عَلَيْنَا كِسْفًا مِنَ السَّمَاءِ إِنْ كُنْتَ مِنَ الصَّادِقِينَ

***“Basi tuangushie vipande vya mbingu ikiwa ni miongoni mwa wasemao kweli.” (26:187)***

Hivyo, Allah تعالی Akawaadhibu kwa adhabu ya siku ya kivuli, ambayo ilikuwa ni adhabu ya siku kubwa. Ama Mtume wa Rehema na Nabii anayewataka watu walete toba, aliyetumwa kama Rehema kwa walimwengu wote, alimuomba Allah تعالی Acheleweshe adhabu yao kwa matarajio na matumaini kuwa Allah تعالی Atatoa kutoka katika vizazi vyao watu watakaomuabudu Allah تعالی tu, bila kumshirikisha. Hili ndilo lililotokea, kwani miongoni mwa wale waliokuwepo wapo waliosilimu na wakawa Waislamu wazuri wenye ikhlasi. Hata ‘Abdallah bin Abi Umayyah, aliyemfuata Mtume ﷺ [baada ya mkutano] na kuzungumza naye kwa namna hiyo, alikuja kusilimu, akawa Muislamu mwenye ikhlasi na kurudi kwa Allah تعالی kwa kutubia. Na Kauli Yake Aliyetukuka:



أَوْ يَكُونُ لَكَ بَيْتٌ مِّنْ زُكْرَفٍ

**“Au uwe na nyumba ya zukhruf”.**

Amesema Ibn ‘Abbaas, Mujaahid na Qataadah: “Hiyo ni ya dhahabu”<sup>1</sup>. Na hivyo ndivyo ilivyosemwa katika kisomo cha Ibn Mas’ud رضي الله عنه, “Au uwe na nyumba ya dhahabu”<sup>2</sup>.

أَوْ تَرَقَّىٰ فِي السَّمَاءِ

**“Au upae mbinguni.”**

Maana yake: Upae juu ya ngazi ilhali tunakutizama.

وَلَنْ نُؤْمِنَ بِرُؤْيَاكَ حَتَّىٰ تَنْزِلَ عَلَيْنَا كِتَابًا نَّقْرُؤُهُ<sup>3</sup>

**“Wala hatutaamini kupaa kwako mpaka ututeremshie Kitabu tukisome.”**

Amesema Mujaahid: “Yaani kila mmoja awe na sahifa moja iliyoandikwa ndani yake: Hiki ni Kitabu kutoka kwa Allah تعالى kwa fulani bin Fulani ambacho atakipata kwenye kichwa chake atakapoamka asubuhi.”<sup>3</sup>

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

قُلْ سُبْحَانَ رَبِّيَ هَلْ كُنْتُ إِلَّا بَشَرًا رَسُولًا

**“Sema: Subhana Rabbi, Ametakasika Mola wangu Mlezi! Kwani mimi ni nani isipokuwa ni mwanadamu na Mtume?”**

Maana yake: Utakaso ni Wake Aliye Mtukufu, hatangulizwi yeyote juu ya jambo lolote lile kuhusiana na Mamlaka na Ufalme Wake. Yeye ni Mwenye Kufanya Atakalo. Akitaka Atawajibu kwa mliyomuuliza, na Akipenda Hatawajibu. Mimi ni Mtume kwenu nyinyi, nimetumwa kuwafikishia ujumbe wa Mola wangu Mlezi na kuwanasihii. Nimefanya hivyo na majibu yenu kwa mliyoyauliza yataamuliwa na Allah تعالى.

<sup>1</sup> At-Tabari 17:553.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:553.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:554.

وَمَا مَنَعَ النَّاسَ أَنْ يُؤْمِنُوا إِذْ جَاءَهُمُ الْهُدَىٰ إِلَّا أَنْ قَالُوا أَبَعَثَ اللَّهُ بَشَرًا رَسُولًا ﴿١٧٦﴾  
 قُلْ لَوْ كَانَتْ فِي الْأَرْضِ مَلَائِكَةٌ يَمْشُونَ مُطْمَئِنِّينَ لَنَزَّلْنَا عَلَيْهِم مِّنَ السَّمَاءِ  
 مَلَكًَا رَسُولًا ﴿١٧٧﴾

**94. Na nini kilichowazuilia watu kuamini ulipowajia uongofu isipokuwa walisema: Je! Allah Humtuma mwanadamu kuwa ni Mtume?**

**95. Sema: Ingelikuwa duniani wapo Malaika wanatembea kwa utulivu wao, basi bila ya shaka Tungeliwateremshia Malaika kuwa ni Mtume wao.**

**Kukataa Washirikina Kuamini kwa kuwa Mtume ni Mwanadamu na Kujibiwa Kwao**

Amesema Aliyetukuka:

وَمَا مَنَعَ النَّاسَ

**“Na nini kilichowazuilia watu.”** Maana yake: Wengi wao,

أَنْ يُؤْمِنُوا

**“Kuamini.”** Na kuwafuata Mitume, ila ile hakika kuwa waliona ajabu na jambo geni sana kuwa wanadamu watatumwa kama Mitume. Kama Alivyosema Aliyetukuka:

أَكَانَ لِلنَّاسِ عَجَبًا أَنْ أَوْحَيْنَا إِلَىٰ رَجُلٍ مِّنْهُمْ أَنْ أَنْذِرِ النَّاسَ وَبَشِّرِ الَّذِينَ ءَامَنُوا أَنَّ لَهُمْ قَدَمَ صِدْقٍ عِنْدَ رَبِّهِمْ ۗ

**“Je, ni ajabu kwa watu ya kwamba Tumemfunulia mtu miongoni mwao kuwa: ‘Waonye watu na wape walioamini habari njema ya kwamba watakuwa na cheo kikubwa mbele ya Mola wao Mlezi?’” (10:2).**

Na Amesema Aliyetukuka:

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُ كَانَتْ تَأْتِيهِمْ رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ فَقَالُوا أَبَشَرًا يَّهْدُونَنَا

**“Hayo ni kwa sababu Mitume wao walikuwa wakiwajia kwa hoja**

**waziwazi; lakini wakisema: 'Oh, watu wenzetu ndio watuongoze?'**  
(64:6).

Na Firauni na watu wake walisema:

فَقَالُوا أَتُؤْمِنُ لِبَشَرَيْنِ مِثْلِنَا وَقَوْمُهُمَا لَنَا عِبَادُونَ ﴿٦٤﴾

**"Oh! Tuwaamini watu walio mfano wetu na ambao jamaa zao ni watumwa wetu?" (23:47).**

Hivyo ndivyo walivyosema watu tofauti kwa Mitume wao:

إِن أَنْشَرْنَا إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُنَا تُرِيدُونَ أَنْ تَصُدُّونَا عَمَّا كَانَتْ يَعْبُدُ ءَابَاؤُنَا فَأَنْتُونَا بِسُلْطَنٍ

مُتَّبِعِينَ ﴿١٠﴾

**"Hamkuwa nyinyi ila ni watu kama sisi. Mnataka tu kutuzuilia na yale waliyokuwa wakiyaabudu baba zetu. Basi tulateeni hoja zilizo wazi." (14:10).** Na Aya katika mlango huu ni nyingi.

Kisha Anasema Allah تعالی, Akiashiria Upole na Rehema Yake kwa waja Wake, kuwa Anawatumia Mitume kutoka katika jinsi yao ili wafahamu anayosema na wanaweza kuzungumza nao moja kwa moja. Lau Angetuma kwa wanadamu Mtume kutoka katika jinsi ya Malaika, hawangeweza kukabiliana wala kujifunza kutoka kwao. Kama Alivyosema Allah تعالی:

لَقَدْ مَنَّ اللَّهُ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ إِذْ بَعَثَ فِيهِمْ رَسُولًا مِّنْ أَنفُسِهِمْ

**"Hakika Allah Amewafanyia hisani kubwa Waislamu Alipowaletea Mtume miongoni mwao." (3:164).**

Na Amesema Aliyetukuka:

كَمَا أَرْسَلْنَا فِيكُمْ رَسُولًا مِّنكُمْ يَتْلُوا عَلَيْكُمْ ءَايَاتِنَا وَيُزَكِّيكُمْ وَيُعَلِّمُكُمُ الْكِتَابَ

وَالْحِكْمَةَ وَيُعَلِّمُكُم مَّا لَمْ تَكُونُوا تَعْلَمُونَ ﴿١٧١﴾ فَادْكُرُوا لِي وَالْآيَاتِ

نَكْفُرُونَ ﴿١٧٢﴾

**"Kama Tulivyomleta Mtume kwenu anayetokana na nyinyi, anakusomeeni Aya Zetu na kukutakaseni na kukufundisheni Kitabu**

**na hekima na kukufundisheni mliyokuwa hamyajui. Basi Nikumbukeni, Nitawakumbuka; na Nishukurini wala msinikufuru.”**  
(2:151-152)

Kwa ajili hiyo, Akasema hapa:

قُلْ لَوْ كَانَتْ فِي الْأَرْضِ مَلَائِكَةٌ يَمْشُونَ مُطْمَئِنِّينَ

**“Sema: Ingelikuwa duniani wapo Malaika wanatembea kwa utulivu wao.”**

Maana yake: Kama mlivyo ndani yake,

لَنَزَّلْنَا عَلَيْهِمْ مِنَ السَّمَاءِ مَلَكًا رَسُولًا ﴿١٦﴾

**“Basi bila ya shaka Tungeliwateremshia Malaika kuwa ni Mtume wao.”**

Maana: Mmoja miongoni mwao (jinsia moja nao). Na mlipokuwa nyinyi ni wanadamu, Tukawatamia Mitume miongoni mwenu kama huruma na rehema kwenu.

قُلْ كَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ ۗ إِنَّهُ كَانَ بِعِبَادِهِ خَبِيرًا بَصِيرًا ﴿١٧﴾

**96. Sema: Allah Anatosha kuwa Shahidi baina yangu na nyinyi. Hakika Yeye Anawajua vyema waja Wake na Anawaona.**

Anasema Aliyetukuka Kumuongoza Mtume Wake ﷺ jinsi ya kuwatolea hoja na ishara kaumu yake kwa ukweli aliokuja nao, kwamba: “Allah تعالى ni Shahidi wake yeye na nyinyi, Naye Anajua niliyokuja nayo kwenu. Lau ningewadanganya basi Angenipatiliza kwa Kuniadhibu kwa adhabu kali kabisa”. Kama Anavyosema Allah تعالى:

وَلَوْ تَقَوَّلَ عَلَيْنَا بَعْضَ الْأَقَاوِيلِ ﴿١٨﴾ لَأَخَذْنَا مِنْهُ بِالْيَمِينِ ﴿١٩﴾ ثُمَّ لَقَطَعْنَا مِنْهُ

الْوَتِينَ ﴿٢٠﴾

**“Na kama Mtume Angelizua juu Yetu baadhi ya maneno tu, bila shaka Tungelimshika kwa Mkono wa Kuume, kisha kwa hakika Tungalimkata mshipa wake mkubwa wa moyo (wa uhai)....”(69:44-46).**

Na Kauli Yake:

إِنَّهُ كَانَ بِعِبَادِهِ خَبِيرًا بَصِيرًا ﴿١٦﴾

***“Hakika Yeye Anawajua vyema waja Wake na Anawaona.”***

Maana yake: Anajua barabara nani miongoni mwao anayestahiki neema, ihsani na uongofu, na nani anayestahiki maangamivu na upotevu. Kwa hiyo Akasema:

\* \* \*

وَمَنْ يَهْدِ اللَّهُ فَهُوَ الْمُهْتَدِ ۖ وَمَنْ يُضِلِلْ فَلَنْ تَجِدَ لَهُمْ أَوْلِيَاءَ  
 مِنْ دُونِهِ ۗ وَنَحْشُرُهُمْ ۖ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ عُمِيَآ  
 وَنُكَمَا وَصُمَّآ ۖ مَا أُولَهُمْ جَهَنَّمَ ۖ كُلَّمَا حَبَتِ زِدْنَهُمْ  
 سَعِيرًا ﴿٧٧﴾ ذَٰلِكَ جَزَاؤُهُمْ بِأَنَّهُمْ كَفَرُوا بِبَايِعَتِنَا وَقَالُوا  
 أَإِذَا كُنَّا عِظْمًا وَرُفَاتًا أَيْنَا لِمَبْعُوثُونَ خَلْقًا جَدِيدًا ﴿٧٨﴾  
 \* أَوْلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ قَادِرٌ  
 عَلَىٰ أَنْ يَخْلُقَ مِثْلَهُمْ وَجَعَلَ لَهُمْ أَجَلًا لَا رَيْبَ فِيهِ فَأَبَى  
 الظَّالِمُونَ إِلَّا كُفُورًا ﴿٧٩﴾ قُلْ لَوْ أَنْتُمْ تَمْلِكُونَ خَزَائِنَ  
 رَحْمَةِ رَبِّي إِذًا لَأَمْسَكْتُمْ خَشْيَةَ الْإِنْفَاقِ ۗ وَكَانَ الْإِنْسَانُ  
 قَتُورًا ﴿٨٠﴾ وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَىٰ بَسَمًا ۖ آتَيْنَاهُ بَيْتًا ۖ فَسَقَلَ  
 بِبَنِي إِسْرَائِيلَ إِذْ جَاءَهُمْ فَقَالَ لَهُ فِرْعَوْنُ إِنِّي لَأَظُنُّكَ  
 يَمُوسَىٰ مَسْحُورًا ﴿٨١﴾ قَالَ لَقَدْ عَلِمْتُمَا أَنزَلَ هَٰؤُلَاءِ  
 إِلَّا رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ بِصَآئِرٍ وَإِنِّي لَأَظُنُّكَ  
 يَفِرْعَوْنُ مَثْبُورًا ﴿٨٢﴾ فَأَرَادَ أَنْ يَسْتَفِيزَهُمْ مِنَ الْأَرْضِ  
 فَأَغْرَقْنَاهُ وَمَنْ مَعَهُ جَمِيعًا ﴿٨٣﴾ وَقُلْنَا مِنْ بَعْدِهِ لِبَنِي  
 إِسْرَائِيلَ أَسْكُنُوا الْأَرْضَ فَإِذَا جَاءَ وَعْدُ الْآخِرَةِ جِئْنَا بِكُمْ  
 لَفِيفًا ﴿٨٤﴾ وَيَا لِحَقِّ أَنْزَلْنَاهُ وَبِالْحَقِّ نَزَّلَهُ ۗ وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا  
 مُبَشِّرًا وَنَذِيرًا ﴿٨٥﴾ وَوَقَرْنَا أَنَا فَرَقْنَاهُ لِتَقْرَأَهُ عَلَى النَّاسِ  
 عَلَىٰ مَكْثٍ وَنَزَّلْنَاهُ تَنزِيلًا ﴿٨٦﴾

وَمَنْ يَهْدِ اللَّهُ فَهُوَ الْمُهْتَدِ ۖ وَمَنْ يُضِلِلْ فَلَنْ تَجِدَ لَهُمْ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِهِ ۗ وَنَحْشُرُهُمْ ۖ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ عُمِيَآ وَنُكَمَا وَصُمَّآ ۖ مَا أُولَهُمْ جَهَنَّمَ ۖ كُلَّمَا حَبَتِ زِدْنَهُمْ سَعِيرًا ﴿٧٧﴾

**97. Na ambaye Allah Amemuongoa basi yeye ndiye aliyeongoka. Na Anayewaachia kupotea basi wewe hutowapatia walinzi wasiokuwa Yeye. Na Tutawakusanya Siku ya Kiyama hali wakikokotwa juu ya nyuso zao, nao ni vipofu, mabubu na viziwi. Na makazi yao ni Jahanamu. Kila moto ukifanya kusinzia Tutazidi kuuchochea uwake kwa nguvu.**

**Uongofu na Upotevu uko Mikononi mwa Allah** تعالى

Allah تعالى Anatuelezea jinsi Anavyowapeleka viumbe Vyake na Hukumu Yake inavyofuatwa. Hakuna

anayeweza kuirudisha Hukumu Yake, kwani yeyote Anayemuongoza hakuna anayeweza kumpoteza, pia:

وَمَنْ يُضِلِّ فَلَنْ تَجِدَ لَهُمْ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِهِ<sup>ط</sup>

**“Na Anaowaachia kupotea basi wewe hutawapa walinzi wasiokuwa Yeye.”**

Maana yake: Wa kuwaongoza. Kama Alivyosema:

مَنْ يَهْدِ اللَّهُ فَهُوَ الْمُهْتَدِ وَمَنْ يُضِلِّ فَلَنْ تَجِدَ لَهُ وَلِيًّا مُرَشِدًا<sup>ط</sup>

**“Ambaye Allah Amemuongoza basi Yeye Ndiye aliyeongoka; na Anayemuachia kupotea, basi hutampatia mlinzi mwongozi.” (18:17)**

**Adhabu kwa Watu Walioongoza Kinyume na Maagizo ya Allah** تعالى

Na Kauli Yake:

وَنَحْشُرُهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ

**“Na Tutawakusanya Siku ya Kiyama hali wakikokotwa juu ya nyuso zao.”**

Amepokea Imaam Ahmad kuwa Anas bin Maalik رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ aliulizwa: “Vipi watu watakusanywa juu ya nyuso zao?” Akasema:

«الَّذِي أَمْسَاهُمْ عَلَىٰ أَرْجُلِهِمْ قَادِرٌ عَلَىٰ أَنْ يُنْشِيَهُمْ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ»

**“Yule Aliyewafanya watembe kwa miguu yao ni Muweza wa Kuwafanya watembe juu ya nyuso zao.”<sup>1</sup>**

Imenukuliwa pia katika Sahihi mbili (Al-Bukhaariy na Muslim)<sup>2</sup>. Na Kauli Yake:

عَمِيًّا

**“Nao ni vipofu.”** Maana yake: hawaoni,

وَتُكْمًا

**“Na mabubu.”** Maana yake: hawasemi,

<sup>1</sup> Ahmad 3:167.

<sup>2</sup> Fat'h Al-Baariy 8:350 na Muslim 4:2161.

وَصِمًا<sup>ط</sup>

**“Na viziwi.”**

Maana yake: Hawasikii. Watakuwa katika hali hii kama adhabu kwa jinsi walivyokuwa katika dunia hii. Hii itakuwa ni jaza yao watakapokusanywa Siku ya Kiyama, wakati ambao watahitaji sana viungo hivyo. Na Kauli Yake:

مَأْوَاهُمْ

**“Makazi yao.”**

Maana yake: Mashukio na hatima yao,

جَهَنَّمَ كُلَّمَا خَبَتْ

**“Ni Jahanamu. Kila moto ukifanya kusinzia.”**

Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Unapotulia”<sup>1</sup>. Na amesema Mujaahid: “Unapozimika”.

زِدْنَهُمْ سَعِيرًا

**“Tutazidi kuchochea uwake kwa nguvu.”**

Maana yake: Kuuzidisha mwako, mvuke, hari na makaa. Kama Alivyosema Aliyetukuka:

فَذُوقُوا فَلَنْ نَزِيدَكُمْ إِلَّا عَذَابًا

**“Basi onjeni (leo adhabu). Nasi Hatutakuzidishieni ila adhabu (juu ya adhabu).” (78:30)**

ذَٰلِكَ جَزَاؤُهُمْ بِأَنَّهُمْ كَفَرُوا بِعَايَتِنَا وَقَالُوا أَإِذَا كُنَّا عِظْمًا وَرُفُنَا أَإِنَّا لَمَبْعُوثُونَ خَلْقًا

جَدِيدًا ﴿٧٨﴾ \* أَوَلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ قَادِرٌ عَلَىٰ أَنْ يَخْلُقَ

مِثْلَهُمْ وَجَعَلَ لَهُمْ أَجَلًا لَا رَيْبَ فِيهِ فَإِنَّ الظَّالِمُونَ إِلَّا كُفُورًا ﴿٧٩﴾

<sup>1</sup> At-Tabari 17:561.



**98. Hayo ni malipo yao kwa sababu walizikataa Ishara Zetu, na wakasema: Hivyo tukisha kuwa mifupa na mapande yaliyovurugika tutafufuliwa kwa umbo jipya?**

**99. Kwani hawakuona ya kwamba Allah Aliyeumba mbingu na ardhi ni Mwenye Kuweza Kuumba mfano wao? Na Yeye Amewawekea muda usio na shaka yoyote. Lakini madhalimu hawataki ila ukafiri.**

Anasema Aliyetukuka: "Adhabu hii, kule kufufuliwa vipofu, bubu na viziwi, ni waliyostahiki, kwa sababu ya kukufuru kwao,

بِعَايِنَتِنَا

**"Kwa ishara Zetu."** Maana yake: "Dalili na Hoja Zetu, na wakadhani ufufuo hautatokea." Usemi wao ulikuwa:

وَقَالُوا أَءِذَا كُنَّا عِظْمًا وَرُفُنَا

**"Hivyo tukishakuwa mifupa na mapande yaliyovurugika."**

Maana yake: Tutakapokuwa tumechanganuka na miili yetu imeoza,

أَيْنَا لَمَبْعُوثُونَ خَلْقًا جَدِيدًا ﴿٥٧﴾

**"Tutafufuliwa kwa umbo jipya?."**

Maana yake: Baada sehemu zetu kutenganika, kupotea na kufyonzwa na ardhi, tutarudishwa tena mara ya pili? Allah تعالى Akatoa dalili na hoja dhidi yao na Kuwaambia kuwa Yeye ni Muweza wa Kufanya hilo, kwani Yeye Ndiye Aliyeumba mbingu na ardhi, hivyo Kuwafufua wao mara nyengine ni sahali zaidi, kama Alivyosema:

لَخَلْقُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ أَكْبَرُ مِنْ خَلْقِ النَّاسِ

**"Kwa yakini umbo la mbingu na ardhi ni kubwa kuliko umbo la wanadamu." (40:57).**

Na Amesema:

أُولَئِكَ يَرَوْنَ أَنَّ اللَّهَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ وَلَمْ يَعْزُبْ عَنْهُمُ خَلْقُهُمْ بَقْدِيرٍ عَلَىٰ أَنْ يُحْيِيَ

الْمَوْتَىٰ ۗ

***“Je, hawaoni ya kwamba Allah – Aliyeziumba mbingu na ardhi na Hakuchoka kwa Kuziumba – Ana uweza wa Kuwafufua wafu?....” (46:33).***

Na Amesema:

أَوَلَيْسَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ بِقَدِيرٍ عَلَيَّ أَنْ يَخْلُقَ مِثْلَهُمْ ۗ بَلَىٰ وَهُوَ الْخَلَّاقُ  
الْعَلِيمُ ﴿٣٣﴾ إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَنْ يَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٣٤﴾

***“Je, yule Aliyeziumba mbingu na ardhi (mnaona) hana uweza wa Kuumba mara ya pili mfano wao (wanadamu)? Kwa nini? Naye ni Muumbaji Mkuu, Mjuzi wa kila jambo. Hakika Amri Yake Anapotaka chochote ni kukiambia: ‘Kuwa’, basi mara huwa.” (36:81-82)***

Na Amesema hapa:

﴿ أَوْلَمْ يَرَوْا أَنَّ اللَّهَ الَّذِي خَلَقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ قَادِرٌ عَلَيَّ أَنْ يَخْلُقَ مِثْلَهُمْ ﴾

***“Kwani hawakuona ya kwamba Allah Aliyeumba mbingu na ardhi ni Mwenye Kuweza Kuumba mfano wao?.”***

Maana yake: Siku ya Kiyama, Atawaumba tena na Kuirudisha miili yao, kama Alivyowaumba mara ya kwanza. Na Kauli Yake:

وَجَعَلْ لَهُمْ أَجَلًا لَا رَيْبَ فِيهِ

***“Na Yeye Amewawekea muda usio na shaka yoyote.”***

Maana yake: Ameweka wakati Kuwaumba tena upya na Kuwatoa kutoka katika makaburi, wakati maalumu ambao hauna budi kufika.

Kama Alivyosema Allah تعالیٰ:

وَمَا نُؤَخِّرُهُ إِلَّا لِأَجَلٍ مُّعَدَّدٍ ﴿١٠٤﴾

***“Na Hatuiakhirishi ila kwa muda unaohesabiwa (na mwenyewe Allah).” (11:104).***

Na Kauli Yake:

قَالَى الظِّلْمُونَ

**“Lakini madhalimu hawataki.”**

Maana yake: Baada ya kusimamishiwa hoja na dalili,

إِلَّا كُفُورًا

**“Ila ukafiri.”**

Isipokuwa wanaendelea kwa ukaidi na inadi katika batili na upotevu wao.

قُلْ لَوْ أَنْتُمْ تَمْلِكُونَ خَزَائِنَ رَحْمَةِ رَبِّي إِذًا لَأَمْسَكْتُمْ خَشْيَةَ الْإِنْفَاقِ ۗ وَكَانَ الْإِنْسَانُ

فَتُورًا

**100. Sema: Lau kuwa nyinyi mnazimiliki khazina za Rehema za Mola wangu Mlezi, basi hapana shaka mngelizuia kwa kuogopa kuzitumia. Na mwanadamu tabia yake ni mchoyo mno!**

### Kuzuia ni katika Silka ya Mwanadamu

Allah تعالى Anamuambia Mtume Wake ﷺ: “Waambie, ewe Muhammad, hata kama mungekuwa na mamlaka juu ya hazina za Allah تعالى mngekataa kutoa kwa hofu ya kumalizika”. Ibn ‘Abbaas na Qataadah wamesema: “Hii inamaanisha hofu ya umasikini na ufukara”<sup>1</sup>, huenda kikamalizika, mbali na ile hakika kuwa haiwezi kumalizika au kufikia kikomo. Hii ni kwa sababu ni sehemu ya maumbile yenu. Hivyo, Allah تعالى Akasema:

وَكَانَ الْإِنْسَانُ فَتُورًا

**“Na mwanadamu tabia yake ni mchoyo mno!”**

Ibn ‘Abbaas na Qataadah wamesema: “Hii inamaanisha kuwa yeye ni bakhili na mwenye kuzuia”<sup>2</sup>. Allah تعالى Anasema:

<sup>1</sup> At-Tabari 17:563.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:563.

أَمْ هُمْ نَصِيبٌ مِّنَ الْمَلِكِ إِذْ لَا يُؤْتُونَ النَّاسَ نَقِيرًا ﴿٥٣﴾

**“Au wanayo sehemu ya utawala? Basi hapo wasingewapa watu hata tundu ya kokwa ya tende.” (4:53),**

Kumaanisha hata kama wangekuwa na ushirika katika Mamlaka ya Allah تعالى, hawangetoa chochote kwa kumpa yeyote, hata kwa ile sehemu ya *naqiira* (tundu ya kokwa ya tende). Allah تعالى Anamuelezea mwanadamu kama alivyo, ila kwa wale wenye Kusaidiwa na Kuongozwa na Allah تعالى. Ubakhli, kutoridhia, papatiko na kutokuwa na subira ni katika sifa za mwanadamu.

Kama Alivyosema Allah تعالى:

\* إِنَّ الْإِنْسَانَ خُلِقَ هَلُوعًا ﴿٦٠﴾ إِذَا مَسَّهُ الشَّرُّ جَزُوعًا ﴿٦١﴾ وَإِذَا مَسَّهُ الْخَيْرُ مَنُوعًا ﴿٦٢﴾

إِلَّا الْمُصَلِّينَ ﴿٦٣﴾

**“Hakika mtu ameumbwa na papara. Inapomgusa shari hupapatika. Na inapomgusa kheri huizuilia. Isipokuwa wanaoswali.” (70:19-22)**

Na zipo Aya nyingi kama hizo katika Qur’ani. Hii ni ishara ya ukarimu na huruma ya Allah تعالى. Katika Sahihi mbili, yapo maneno yafuatayo: *“Mkono wa Allah Umejaa na Haupungui kwa sababu ya Yeye Kutoa usiku na mchana. Je, huoni ni ngapi Alizotoa kuanzia Aumbe mbingu na ardhi, hata hivyo, zilizo Mkononi Mwake wa Kuume Hazipungui kabisa.”*<sup>1</sup>

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَىٰ تِسْعَ آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ ۖ فَسَأَلَ بَنِي إِسْرَائِيلَ إِذْ جَاءَهُمْ فَقَالَ لَهُ فِرْعَوْنُ

إِنِّي لَأَظُنُّكَ يَمُوسَىٰ مَسْحُورًا ﴿٦٤﴾ قَالَ لَقَدْ عَلِمْتُمَا أَنزَلَ هَٰؤُلَاءِ إِلَّا رَبُّ

السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ بِصَآئِرٍ وَإِنِّي لَأَظُنُّكَ بِفِرْعَوْنِ مُثَبَّرًا ﴿٦٥﴾ فَأَرَادَ أَن يَسْتَفِزَّهُمْ

مِّنَ الْأَرْضِ فَأَغْرَقْنَاهُ وَمِن مَّعَهُ جَمِيعًا ﴿٦٦﴾ وَقُلْنَا مِن بَعْدِهِ لِبَنِي إِسْرَائِيلَ آسْكُنُوا

الْأَرْضَ فَإِذَا جَاءَ وَعْدُ الْآخِرَةِ جِئْنَا بِكُمْ لَفِيفًا ﴿٦٧﴾

<sup>1</sup> Fat’h Al-Baariy 8:202 na Muslim 2:691.

**101. Na kwa yakini Tulimpa Musa ishara tisa zilizo wazi. Waulize Wana wa Israili alipowafikia, na Firauni akawaambia: Hakika mimi nakuona wewe Musa umerogwa!**

**102. Akasema: Bila shaka Wewe unajua kuwa haya hakuyateremsha ila Mola Mlezi wa mbingu na ardhi ili kuwa ni ushahidi wa kuonekana. Na hakika mimi bila ya shaka nakuona wewe, Firauni, kuwa umekwishaangamia.**

**103. Basi Firauni akataka kuwafukuza katika nchi. Kwa hivyo Tukamzamisha yeye na waliokuwa pamoja naye wote.**

**104. Na Tukawaambia baada yake Wana wa Israili: Kaeni katika nchi. Itapokuja ahadi ya Akhera Tutakuleteni nyote pamoja.**

#### **Ishara Tisa za Nabii Musa عليه السلام**

Allah تعالى Anatuarifu kuwa Alimtuma Musa عليه السلام na ishara tisa zilizo wazi kabisa, zilizotoa dalili za wazi kuwa utume wake ni wa kweli na kwamba aliyokuwa akiyabalighisha ni kutoka kwa Yule Aliyemtuma yeye kwa Firauni ni kweli. Ishara hizi za wazi zilikuwa: Fimbo yake, mkono wake, miaka ya ukame, bahari, tufani, nzige, chawa, vyura na damu. Hii ndiyo iliyokuwa rai ya Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما<sup>1</sup>. Muhammad bin Ka'b amesema: "Ishara hizo zilikuwa ni mkono wake na fimbo yake, ishara tano zilizotajwa katika Suratul A'raaf, kuteketezwa mali<sup>2</sup> na jabali"<sup>3</sup>. Ibn 'Abbaas, Mujaahid, 'Ikrimah, Ash-Sha'biy na Qataadah رضي الله عنهم wamesema: "Hizo ni mkono wake, fimbo yake, miaka ya ukame, mazao kutomea, tufani, nzige, chawa, vyura na damu"<sup>4</sup>. Hata hivyo,

فَأَسْتَكْبِرُوا وَكَانُوا قَوْمًا مُّجْرِمِينَ ﴿١٣٣﴾

**"Nao wakapanda kiburi, na wakawa watu wakosefu."(7:133),**

Maana yake: Mbali na ishara zote hizi walizozishuhudia, walikufuru, japokuwa walikinaika nazo, lakini hazikuwaathiri hata kidogo. Kwa namna hiyo hiyo,

<sup>1</sup> At-Tabari 17:564.

<sup>2</sup> Tizama tafsiri ya Surah Yunus 10: 88.

<sup>3</sup> At-Tabari 17: 565.

<sup>4</sup> At-Tabari 17: 565, 566.

(Allah تعالی Anamuambia Mtume Wake ﷺ hapa), “Ingekuwa Tuwajibu hawa kwa matakwa yao waliyoyauliza, waliosema kuwa hawataamini mpaka uwatolee chemchemu sehemu zote za ardhi kwa ajili yao, hawataamini ila anapotaka Allah تعالی”. Kama Firauni alimuambia Musa عليه السلام, baada ya kushuhudia ishara zote hizo alizoleta:

إِنِّي لَأَظُنُّكَ يَا مُوسَىٰ مَسْحُورًا ﴿١٠٦﴾

**“Hakika mimi nakuona wewe Musa umerogwa!”**

Inasemekana kuwa hii inamaanisha kuwa alikuwa mchawi, lakini Allah تعالی Anajua zaidi. Hizi ishara tisa zilizotajwa na wanazuoni zilionukuliwa hapo juu ni zile zinazoashiriwa hapa, na katika Aya:

وَأَلْقَىٰ عَصَاكَ فَلَمَّا رَءَاهَا تَهْتَزُّ كَأَنَّهَا جَانٌّ وَلَّىٰ مُدَبِّرًا ۖ وَلَمْ يَعْقِبْ يَمُوسَىٰ لَّا تَخَفْ

**“Na itupe fimbo yako! Alipoiona ikitikisika kama nyoka, aligeuka nyuma wala hakungoja. Ewe Musa, usikhofu!”**

Hadi Maneno Yake,

فِي تِسْعِ آيَاتٍ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَقَوْمِهِ ۖ إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمًا فَسِيقِينَ ﴿١٠٧﴾

**“Ni katika Ishara tisa za kumpelekea Firauni na kaumu yake. Hakika hao walikuwa watu waovu.” (27:10-12)**

Ishara hizi zinataja fimbo na mkono, na zile ishara zilizobakia zimetajwa kwa urefu katika Suratul A'raaf. Musa عليه السلام alipatiwa ishara nyengine nyingi kama kulipiga jabali na fimbo yake na hapo maji yakaanza kutoka kwayo, kule kufunikwa na mawingu, *manna* na *salwa* na ishara nyengine walizopatiwa Wana wa Israili baada ya kuondoka Misri. Lakini hapa Allah تعالی Anataja ishara tisa zilizoshuhudiwa na watu wake Misri. Hizi zikawa dalili dhidi yao, kwa sababu ya kuzikataa kwa inadi na ukaidi kwa ajili ya kukufuru kwao.

Hivyo Musa عليه السلام alimuambia Firauni:

<sup>1</sup> Tizama tafsiri ya Surah Yunus 10: 88.

<sup>2</sup> At-Tabari 17: 565.

<sup>3</sup> At-Tabari 17: 565, 566.

لَقَدْ عَلِمْتُمْ مَا أَنْزَلَ هَتُؤُلَاءِ إِلَّا رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ بِصَآئِرٍ

**“Wewe unajua bila ya shaka kuwa haya hakuyateremsha ila Mola Mlezi wa mbingu na ardhi ili kuwa ni ushahidi wa kuonekana.”**

Maana yake: Kama dalili na hoja ya ukweli kwa niliyokuletea.

وَإِنِّي لَأَظُنُّكَ يَا فِرْعَوْنُ مَثْبُورًا ﴿١٧٠﴾

**“Na hakika mimi bila ya shaka nakuona wewe, Firauni, kuwa umekwisha angamia.”**

Maana yake: Utaangamizwa. Hii ilikuwa rai ya Mujaahid na Qataadah<sup>1</sup>. Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Inamaanisha kulaaniwa”<sup>2</sup>. Ibn ‘Abbaas na adhw-Dhwahhaak wamesema:

مَثْبُورًا ﴿١٧١﴾

**“Mathbuuraa – umekwisha angamia.”**

Maana yake: umeshindwa<sup>3</sup>. Kama alivyosema Mujaahid, “Hii inajumlisha maana zote hizi”.

### Kuangamizwa kwa Firauni na Watu Wake

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

فَأَرَادَ أَنْ يَنْتَفِيزَهُمْ مِنَ الْأَرْضِ

**“Basi Firauni akataka kuwafukuza katika nchi.”**

Maana yake: Alitaka kuwafukuza na kuwatoa nje (ya Misri). Hata hivyo,

فَأَغْرَقْنَاهُ وَمَنْ مَعَهُ جَمِيعًا ﴿١٧٢﴾ وَقُلْنَا مِنْ بَعْدِهِ لِبَنِي إِسْرَائِيلَ اسْكُنُوا الْأَرْضَ

**“Tukamzamisha yeye na waliokuwa pamoja naye wote. Na Tukawaambia baada yake Wana wa Israili: Kaeni katika nchi.”**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:571.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:570.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:570.

Hii ni habari njema kwa Muhammad ﷺ, utabiri wa kutekwa kwa Makka, mbali na kuwa Sura imeteremshwa Makka kabla ya Hijra (kuhama kuelekea Madina). Vivyo hivyo, watu wa Makka walitaka kumfukuza na kumtoa Mtume ﷺ kutoka katika mji huo,

Kama Alivyosema Allah تعالی katika Aya,

وَإِنْ كَادُوا لَيَسْتَفِزُّوكَ مِنَ الْأَرْضِ لِيُخْرِجُوكَ مِنْهَا

**“Na walitaka kukukera ili uitoke nchi ...” (17:76-77).**

Hivyo Allah تعالی Alimfanya Mtume Wake ﷺ kuirithi Makka, akaingia katika mji huo kwa nguvu, kulingana na kauli moja mashuhuri kati ya kauli mbili zinazofahamika.

Aliwashinda watu wake, kisha kwa huruma na ukarimu, aliwaachilia, kama vile Allah تعالی Alivyowafanya Wana wa Israili, waliokuwa wamenyanyaswa, kurithi ardhi, mashariki na magharibi, na kuirithi ardhi ya watu wa Firauni, pamoja na mashamba yake, mazao na hazina (mali),

Kama Alivyosema Allah تعالی:

كَذَلِكَ وَأَوْرَثْنَاهَا بَنِي إِسْرَائِيلَ

**“Kadhalika; na Tukawarithisha hayo Wana wa Israili.” (26:59)**

Hapa Allah تعالی Anasema:

وَقُلْنَا مِنْ بَعْدِهِ لِبَنِي إِسْرَائِيلَ أَكُنُوا الْأَرْضَ فَإِذَا جَاءَ وَعْدُ الْآخِرَةِ جَعَلْنَا بِكُمْ لَفِيفًا

**“Na Tukawaambia baada yake Wana wa Israili: Kaeni katika nchi. Itapokuja Ahadi ya Akhera Tutakuleteni nyote pamoja.”**

Maana yake: Nyote, nyinyi na maadui zenu. Ibn ‘Abbaas, Qataadah na adhw-Dhwahhaa wamesema: “Inamaanisha nyote pamoja.”<sup>1</sup>

<sup>1</sup> At-Tabari 17: 572, 573.



وَبِالْحَقِّ أَنْزَلْنَاهُ وَبِالْحَقِّ نَزَّلَهُ وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا مُبَشِّرًا وَنَذِيرًا ﴿١٠٥﴾ وَقُرْءَانًا فَرَقْنَاهُ لِتَقْرَأَهُ  
عَلَى النَّاسِ عَلَى مَكْثٍ وَنَزَّلْنَاهُ تَنْزِيلًا ﴿١٠٦﴾

**105. Na kwa Haki Tumeiteremsha, na kwa Haki imeteremka. Na Hatukukutuma ila uwe mtoaji wa habari na mwonyaji.**

**106. Na Qur'ani Tumeigawanya sehemu mbali mbali ili uwasomee watu kwa kituo, na Tumeiteremsha kidogo kidogo.**

### Kuteremshwa Qur'ani Kidogo Kidogo

Allah تعالی Anatufahamisha kuwa Kitabu Chake, Qur'ani Tukufu, kimeteremshwa kwa haki. Maana yake: kina ukweli mtupu ndani yake. Kama Anavyosema Allah تعالی:

لَكِنَّ اللَّهَ يَشْهَدُ بِمَا أَنْزَلَ إِلَيْكَ أَنْزَلَهُ بِعِلْمِهِ وَالْمَلَكُ يَشْهَدُونَ

**“Lakini Allah Anayashuhudia Aliyokuteremshia wewe. Ameyateremsha kwa Kujua Kwake na Malaika pia wanashuhudia.”  
(4:166)**

Maana yake: Ina elimu ambayo Allah تعالی Alitaka Kuwafundisha, pamoja na Hukumu Zake, Maamrishi na Makatazo. Na Kauli Yake:

وَبِالْحَقِّ نَزَّلَهُ

**“Na kwa Haki imeteremka.”**

Maana yake: Imeteremshwa kwako, ewe Muhammad ﷺ, ikiwa imehifadhiwa, inalindwa, haijachang'anyika na chochote, wala hakuna kilichoongezwa wala kupunguzwa. Kimeteremshwa kwako kwa ukweli na haki, imeteremshwa na aliye na nguvu, muaminifu, anayetiwa na Malaika.

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ

**“Na Hatukukutuma.”** Ewe Muhammad ﷺ, ila,

إِلَّا مُبَشِّرًا وَنَذِيرًا ﴿١٠٦﴾

**“Uwe mtoaji wa habari na mwonyaji.”**

Mwenye kuleta bishara njema kwa Waumini wanaokutii na kuwaonya makafiri wanaokuasi. Na Kauli Yake:

وَقُرْءَانًا فَرَقْنَاهُ

**“Na Qur’ani Tumeigawanya”.**

Neno limefasiriwa hapa kama, ‘Tumeigawanya’, linaweza kusomwa kwa njia mbili. Ikisomwa: “*Faraqnaahu*, bila ya *Shaddah*, maana itakuwa: ‘Tumeifanya iteremke kutoka *Al-Lawhul Mahfudh* hadi *Baytil ‘Izzah*, iliyo katika uwingu wa chini kabisa, kisha ikateremshwa kidogo kidogo kwa Mtume wa Allah, kulingana na matukio, kwa kipindi cha miaka ishirini na tatu (23)”. Hii imepokewa na ‘Ikrimah kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما<sup>1</sup>. Pia imepokewa kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما alikuwa akiisoma kama: “*Farraqnaahu*, pamoja na *Shaddah*, yenye maana: ‘Tuliiteremsha Aya moja baada ya nyengine, na Tukaeleza na Kuibainisha (Kuiweka wazi)<sup>2</sup>”. Hivyo, Allah تعالى Akasema:

لِتَقْرَأَهُ عَلَى النَّاسِ

**“Ili uwasomee watu”,**

Maana yake: ubalighishe (ufikishe) ujumbe wake kwa watu na pia kuwasomea,

عَلَى مَكْتَبٍ

**“Kwa kituo”,**

Kumaanisha pole pole. Na pia,

وَنَزَّلْنَاهُ تَنْزِيلًا ﴿١٧٦﴾

**“Tumeiteremsha kidogo kidogo.”**

Maana yake: aya baada ya aya, au kwa mafungu ya aya.

\* \* \*

<sup>1</sup> At-Tabari 17:574.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:573, 574.

قُلْ ءَامِنُوا بِمِةٍ أَوْ لَا تُؤْمِنُوا ۚ إِنَّ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ مِنْ قَبْلِهِ إِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ يَخِرُّونَ لِلْأَذْقَانِ سُجَّدًا ﴿١٠٧﴾ وَيَقُولُونَ سُبْحٰنَ رَبِّنَا إِن كَانَ وَعْدُ رَبِّنَا لَمَفْعُولًا ﴿١٠٨﴾ وَيَخِرُّونَ لِلْأَذْقَانِ يَسْكُوتُونَ وَيَزِيدُهُمْ خُشُوعًا ﴿١٠٩﴾ قُلِ ادْعُوا اللَّهَ أَوْ ادْعُوا الرَّحْمٰنَ ۗ أَيًّا مَا تَدْعُوا فَلَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ ۗ وَلَا تَجْهَرُوا بِصَلَاتِكُمْ وَلَا تَخَافُتْ بِهَا وَابْتَغِ بَيْنَ ذَلِكَ سَبِيلًا ﴿١١٠﴾ وَقُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي لَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا وَلَمْ يَكُن لَّهُ شَرِيكٌ فِي الْمَلِكِ وَلَمْ يَكُن لَّهُ وِليٌّ مِنَ الدُّنْيَا ۗ وَكَبِيرَةٌ تَكْبِيرًا ﴿١١١﴾

قُلْ ءَامِنُوا بِمِةٍ أَوْ لَا تُؤْمِنُوا ۚ إِنَّ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ مِنْ قَبْلِهِ إِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ يَخِرُّونَ لِلْأَذْقَانِ سُجَّدًا ﴿١٠٧﴾ وَيَقُولُونَ سُبْحٰنَ رَبِّنَا إِن كَانَ وَعْدُ رَبِّنَا لَمَفْعُولًا ﴿١٠٨﴾ وَيَخِرُّونَ لِلْأَذْقَانِ يَسْكُوتُونَ وَيَزِيدُهُمْ خُشُوعًا ﴿١٠٩﴾

107. Sema: laminini au msiiamini. Hakika wale waliopewa elimu kabla yake, wanaposomewa hii,

huanguka kifudifudi wanasujudu.

108. Na wanasema: Ametakasika Mola wetu Mlezi! Hakika Ahadi ya Mola wetu Mlezi lazima itimizwe!

109. Na huanguka kifudifudi na huku wanalia, na inawazidisha unyenyekevu.

### Wale Waliopewa Elimu Kabla kwa Ukweli na Dhati Waliikubali Qur'an

Allah تعالیٰ Anamuambia Mtume Wake ﷺ:

قُلْ

“Sema”, Ewe Muhammad ﷺ kwa hawa makafiri kuhusu ulichowaletea, kwa hii Qur’ani Tukufu:

ءَامِنُوا بِمِةٍ أَوْ لَا تُؤْمِنُوا ۚ

“laminini au msiiamini”, Maana yake: Ni sawa kama mtaiamini au la, kwani ni ya kweli. Allah تعالیٰ Ameiteremsha, na Akaitaja hapo mbeleni katika Vitabu Alivyoteremsha kwa Mitume wengine. Kwa ajili hiyo Akasema:

إِنَّ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ مِنْ قَبْلِهِ

**“Hakika wale waliopewa ilimu kabla yake.”**

Maana yake: Miongoni mwa watu wema waliopewa Kitabu, walioshikilia kufuata Vitabu vyao na kuvisimamisha bila kuvibadilisha. Hao,

إِذَا يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ

**“Wanaposomewa.”**

Maana yake: Qur’ani hii, inawaathiri,

يَخْرُونَ لِلْأَذْقَانِ سُجَّدًا

**“Huanguka kifudifudi.”**

Nayo ni sehemu ya chini ya uso.

Maana yake: Kwa ajili ya Allah تعالیٰ kwa kushukuru kwa kile walichoneemeshwa kwayo. Neema ya kuwa Allah تعالیٰ Amewajaalia kukutana na Mtume huyu aliyeteremshiwa Kitabu hiki. Kwa hiyo wakasema:

سُبْحَانَ رَبِّنَا

**“Ametakasika Mola wetu Mlezi.”**

Maana yake: Wanamtukuza na Kumtakasa kwa Uweza Wake uliotimia, na kwa kuwa Yeye Havunji Ahadi Yake Aliyoahidi kupitia kwa Manabii waliotangulia, kuwa Atamtuma Muhammad ﷺ. Hivyo wakasema:

سُبْحَانَ رَبِّنَا إِنْ كَانَ وَعْدُ رَبِّنَا لَمَفْعُولًا

**“Ametakasika Mola wetu Mlezi! Hakika Ahadi ya Mola wetu Mlezi lazima itimizwe!”**

Na Kauli Yake Allah تعالیٰ,

وَيَخْرُونَ لِلْأَذْقَانِ يَسْكُوبُونَ

**“Na huanguka kifudifudi na huku wanalia.”** Maana yake: Kwa kunyenyekea kwa Allah تعالیٰ, kwa Imani na kukisadiki Kitabu Chake na Mtume Wake ﷺ. Mbali na hayo,

وَيَزِيدُهُمْ حُشُوعًا ۝

**“Na inawazidishia unyenyekevu.”**

Maana yake: Kwa Imani, kunyenyekea na kujisalimisha, kama Alivyosema:

وَالَّذِينَ أَهْتَدُوا زَادَهُمْ هُدًى وَآتَاهُمْ تَقْوَاهُمْ ۝

**“Na wale walioongoka Anawazidishia uongofu na Anawapa uchamungu wao.” (47:17)**

Na Kauli Yake Allah,

وَيَحْزُونَ

**“Na huanguka.”**

Maana yake: Haya ni maelezo ya ziada kwa unyenyekevu wao kama ilivyoelezwa katika Aya 107; wala haimaanishi kuwa wanasujudu mara mbili.

قُلْ أَدْعُوا اللَّهَ أَوْ ادْعُوا الرَّحْمَنَ أَيُّمَا مَا تَدْعُوا فَلَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ ۚ وَلَا تَجْهَرُوا بِصَلَاتِكُمْ  
وَلَا تَخَافَتْ بِهَا وَابْتَغِ بَيْنَ ذَلِكَ سَبِيلًا ۝ وَقُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي لَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا وَلَمْ  
يَكُنْ لَهُ شَرِيكٌ فِي الْمُلْكِ وَلَمْ يَكُنْ لَهُ وِليٌّ مِنَ الذُّلِّ ۗ وَكَبِيرُهُ تَكْبِيرًا ۝

**110. Sema: Muombeni Allah (Mwenyezi Mungu), au Muombeni Rahman (Mwingi wa Rehema), kwa jina lolote mnalomuita. Kwani Yeye Ana Majina Mazuri Mazuri. Wala usitangaze Swala yako kwa sauti kubwa, wala usiifiche kwa sauti ndogo, bali shika njia ya kati na kati ya hizo.**

**111. Na sema: Alhamdulillah, Himdi zote ni za Allaah Ambaye Hana mwana, wala Hana mshirika katika Ufalme, wala Hana rafiki wa kumsaidia kwa sababu ya Udhaifu Wake. Na Mtukuze kwa Utukufu Mkubwa.**

**Allah تعالی Ndiye Mwenye Majina Mazuri Kabisa**

Anasema Aliyetukuka:

قُلْ

"Sema."

Ewe Muhammad ﷺ, kuwaambia hawa makafiri wanaokataa kuwa Allah تعالی Ana Sifa ya *Ar-Rahman* na kukataa kumuita kwa Jina hilo.

أَدْعُوا اللَّهَ أَوْ ادْعُوا الرَّحْمَنَ أَيُّمَا مَا تَدْعُوا فَلَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ

***"Muombeni Allah (Mwenyezi Mungu), au Muombeni Rahman (Mwingi wa Rehema), kwa jina lolote mnalomuita. Kwani Yeye Ana Majina mazuri mazuri."***

Maana yake: Hakuna tofauti katika kumuita kwenu kwa Jina la Allah تعالی au kwa Jina la *Ar-Rahman*, kwa sababu Yeye Ana Majina yaliyo Mazuri kabisa, kama Anavyosema:

هُوَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ عَلِيمٌ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ هُوَ الرَّحْمَنُ الرَّحِيمُ ﴿٢١﴾

***"Yeye Ndiye Allah ambaye hakuna aabudiwaye kwa haki isipokuwa Yeye tu. Anayeyajua yaliyofichikana na yaliyo dhahiri, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu."*** (59:22)

Mpaka pale Aliposema:

لَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ يُسَبِّحُ لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

***"Mwenye Majina (sifa) mazuri. Kinamtukuza kila kilichomo mbinguni na ardhini."*** (59:24).

Na imepokewa kutoka kwa Makhul kuwa mtu mmoja miongoni mwa washrikina alimsikia Mtume ﷺ akiwa katika sijdah: "Ee, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu". Yule mshrikina akasema: "Anadai kuwa anamuabudu Mmoja, naye anawaomba na kuwaabudu wawili". Hapo Allah تعالی Akateremsha Aya hii. Na hivyo ndivyo ilivyopokewa kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما, na pia kwa Ibn Jariir <sup>1</sup> رحمه الله تعالی.

<sup>1</sup> At-Tabari 17:580. Sanadi yake si sahihi.

## Amri ya Kusoma kwa Sauti ya Kati na Kati (Sio kwa Sauti Kubwa wala Ndogo Sana)

Na Kauli Yake:

وَلَا تَجْهَرُ بِصَلَاتِكَ

***“Wala usitangaze Sala yako kwa sauti kubwa”.***

Amepokea Imam Ahmad kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Aya hii iliteremka kwa Mtume ﷺ akiwa anahubiri kwa uficho akiwa Makka:

وَلَا تَجْهَرُ بِصَلَاتِكَ وَلَا تُخَافِتُ بِهَا

***“Wala usitangaze Sala yako kwa sauti kubwa, wala usiifiche kwa sauti ndogo.”***

Akasema: ‘Alipokuwa akiswali pamoja na Maswahaba wake, alikuwa akisoma Qur’ani kwa sauti kubwa’, washirikina waliposikia hicho kisomo, waliitusi Qur’ani na aliyeiteremsha na aliyeileta’. Kwa hiyo, Allah تعالى Alimuambia Mtume Wake ﷺ:

وَلَا تَجْهَرُ بِصَلَاتِكَ

***‘Wala usitangaze Sala yako kwa sauti kubwa’,***

Maana yake: Usiisome kwa sauti kubwa wakaisikia washirikina na hivyo kuitukana Qur’ani,

وَلَا تُخَافِتُ بِهَا

***‘Wala usiifiche kwa sauti ndogo’,***

Maana yake: Wala usiisome kwa sauti ndogo sana kiasi ambacho hata Maswahaba wako hawaisikii Qur’ani na kujifunza kutoka kwako. Hivyo,

وَأَبْتَعِ بَيْنَ ذَلِكَ سَبِيلًا ﴿١٠٧﴾

***‘Bali shika njia ya kati na kati ya hizo.’<sup>1</sup>***

Hadithi hii pia ilinukuliwa katika Sahihi mbili<sup>2</sup>. Adhw-Dhwahhaak amesimulia mfano wa Hadithi hii kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما, na kuongeza: “Pindi alipohamia Madina, kanuni hiyo ilifutika ikawa Mtume anasoma anavyotaka”<sup>3</sup>.

<sup>1</sup> Ahmad 1:23.

<sup>2</sup> Fat’h Al-Baariy 8:257 na Muslim 1:329.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:584.

Na amepokea Muhammad bin Is'haaq رحمه الله تعالى kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: "Alikuwa Mtume ﷺ akisoma Qur'ani kwa sauti wakati akiswali, (washirikina) walikuwa wakitawanyika na kukataa kumsikiliza; mmoja wao alipokuwa anataka kusikiliza baadhi ya Aya alizokuwa akisoma katika Swala, alikuwa akimsikiliza bila ya yeyote kumuona, kwa sababu alikuwa anawaogopa. Anapotambua kuwa kuna mtu anayejua kusikiliza kwake, alikuwa anaondoka ili asidhuriwe, hivyo hasikii. Pale Mtume ﷺ alipohafifisha sauti yake, wale waliokuwa wanataka kukisikiliza kisomo chake walikuwa hawawezi kusikia chochote. Hivyo, Allah تعالى Akateremsha:

وَلَا تَجْهَرْ بِصَلَاتِكَ

**'Wala usitangaze Swala yako kwa sauti kubwa.'**

Maana yake: Usisome kwa sauti, ili wale wanaotaka kusikiliza wasitawanyike kwa hofu kutoka hadhira yako,

وَلَا تُخَافِتْ بِهَا

**'Wala usiifiche kwa sauti ndogo.'**

Hivyo wasiweze kusikia wanaotaka kusikiza. Huenda akamaanika kwa anayosikia na kufaidika kwayo.

وَأَتَّبِعْ بَيْنَ ذَلِكَ سَبِيلًا ﴿١٠٧﴾

**'Bali shika njia ya kati na kati ya hizo.'**<sup>1</sup>

Hii ndiyo rai ya Ikrimah, Al-Hasan Al-Baswriy na Qataadah kuwa Aya hii iliteremka kuhusiana na kisomo katika Swala<sup>2</sup>. Na imepokewa kutoka kwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه kuwa: "Wala usiifiche kwa sauti ndogo" kwa jinsi ambayo hakuna atakayesikia ila wewe mwenyewe<sup>3</sup>.

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 17: 585.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 17:587.

<sup>3</sup> Atw-Twabariy 17:589.



**Tamko la Dhati la Kumpwekesha Allah (Tauhid)**

Na Kauli Yake:

وَقُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي لَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا

**“Na sema: Alhamdulillah, Himdi zote ni za Allah Ambaye Hana mwana.”**

Kwa sababu Allah تعالى Amethibitisha kwa Nafsi Yake kuwa Majina yaliyo Mazuri kabisa ni Yake, na Akajitangaza kuwa Hana kasoro wala mapungufu ya aina yoyote. Akasema Aliyetukuka:

وَقُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي لَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا وَلَمْ يَكُنْ لَهُ شَرِيكٌ فِي الْمَلَكِ

**“Na sema: Himdi zote ni za Allah Ambaye Hana mwana, wala Hana mshirika katika Ufalme.”**

Bali Yeye ni Mmoja, Mwenye Kustahiki Kucusudiwa, Hakuzaa wala Hakuzaliwa, wala Hakuna Anayefanana Naye hata mmoja.

وَلَمْ يَكُنْ لَهُ وِليٌّ مِّنَ الدُّنْيَا

**“Wala hana rafiki wa kumsaidia kwa sababu ya udhaifu wake.”**

Maana: Yeye si dhalili wa kuhitajia kuwa na msaidizi au mshauri, bali Yeye Pekee, asiyekuwa na mshirika, Aliyetukuka, Ndiye Muumba wa vitu vyote na Yeye Ndiye Mwenye Kuendesha na Kudhibiti kwa Matakwa Yake, pasi na kuwa na mshirika. Amesema Mujaahid kuhusu Kauli Yake:

وَلَمْ يَكُنْ لَهُ وِليٌّ مِّنَ الدُّنْيَا

**“Wala hana rafiki wa kumsaidia kwa sababu ya udhaifu Wake.”**

Haundi muungano na yeyote, wala Hataki usaidizi wa yeyote.”<sup>1</sup>

---

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 17:590.

Na Kauli Yake:

وَكَبِيرَةٌ تَأْكِبُ

**“Na Mtukuze kwa Utukufu Mkubwa.”**

Maana yake: Mtukuze na Mtakase kwa kiasi kikubwa zaidi dhidi ya wale wanayosema madhalimu waliokengeuka wenye kutakabari kukubwa.

Amepokea Ibn Jariir رحمه الله تعالى kuwa Al-Quradhiy alikuwa akisema yafuatayo kuhusu Aya hii:

وَقُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي لَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا

**“Na sema: Himdi zote ni za Allah Ambaye Hana mwana’.**

Akasema: ‘Hakika Mayahudi na Manasara (Wakristo) walisema kuwa Allah تعالى Amejifanyia mtoto; na Waarabu wakasema: ‘Tunakuitikia, huna mshirika isipokuwa mshirika uliye Naye, Unammiliki na vyote alivyonavyo’. Na wakasema Wasabai na Majusi: ‘Lau si kwa wasaidizi na marafiki wa Allah تعالى, Angekuwa dhaifu’. Allah تعالى Akateremsha Aya hii:

وَقُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي لَمْ يَتَّخِذْ وَلَدًا وَلَمْ يَكُنْ لَهُ شَرِيكٌ فِي الْمُلْكِ وَلَمْ يَكُنْ لَهُ وِليٌّ مِّنَ

الدُّنْيَا وَكَبِيرَةٌ تَأْكِبُ

**“Na sema: Himdi zote ni za Allah Ambaye Hana mwana, wala Hana mshirika katika Ufalme, wala Hana rafiki wa kumsaidia kwa sababu ya udhaifu Wake. Na Mtukuze kwa Utukufu Mkubwa”<sup>1</sup>.**

Mwisho wa Tafsiri ya Sura *Subhaana* (Suratul Israa’). Na Allah تعالى Ndiye Mwenye Kustahiki Sifa zote njema na ihsani.

\* \* \*

<sup>1</sup> At-Tabari 17:590.

## Tafsiri ya Suratul Kahf

### Sura ya 18

### Iliteremshwa Makkah

**Yaliyotajwa kuhusu Fadhila za Sura hii, Aya Kumi za Mwanzo na za Mwisho, Zinazomlinda Mtu kutokana na Vitimbi vya Dajjaal**

Amepokea Imam Ahmad kutoka kwa Al-Baraa' amesema: "Mtu mmoja alisoma Al-Kahf na kulikuwa na mnyama nyumbani aliyeingiwa na wahaka. Alitizama na kuona ukungu au kiwingu kilichofunika juu." Akamtajia hilo Mtume ﷺ. Naye akamuambia:

«أَفْرَأَ فَلَانٌ، فَإِنَّهَا السَّكِينَةُ نَزَلُ عِنْدَ الْقُرْآنِ أَوْ نَزَلَتْ لِلْقُرْآنِ»

*'Fulani, endelea kusoma, kwani hiyo ni sakina (utulivu) inayoteremka mmoja wenu anaposoma Qur'ani au inateremka kwa sababu ya kusoma Qur'ani'*<sup>1</sup>.

Imenukuliwa katika Sahihi mbili.<sup>2</sup> Na huyu mtu aliyesoma ni Usayd bin Al-Hudhwayr رضي الله عنه kama tulivyotangulia kueleza katika Tafsiri ya *Suratul Baqarah*.

Na amepokea Imaam Ahmad kutoka kwa Abu Dardaa رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«مَنْ حَفِظَ عَشْرَ آيَاتٍ مِنْ أَوَّلِ سُورَةِ الْكَهْفِ عُصِمَ مِنَ الدَّجَالِ»

*"Mwenye kuhifadhi Aya kumi (10) za mwanzo wa Suratil Kahf atalindwa na (mitihani na vitimbi) vya Dajjaal."*<sup>3</sup>

Hii pia imenukuliwa na Muslim, Abu Daawuud, An-Nasaa'iy na At-Tirmidhiy. Kulingana na riwaya ya At-Tirmidhiy:

<sup>1</sup> Ahmad 4:281.

<sup>2</sup> Fat'h Al-Baariy 6:719 na Muslim 1:548.

<sup>3</sup> Ahmad 5:196.

«مَنْ حَفِظَ ثَلَاثَ آيَاتٍ مِنْ أَوَّلِ الْكَهْفِ»

*"Mwenye kuhifadhi Aya tatu za mwanzo wa Al-Kahf".*

Akasema ni Hadith Hasan Sahih<sup>4</sup>.

Katika *Al-Mustadrak* wake, Al-Haakim amepokea kutoka kwa Abu Said عنه رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ akisema:

«مَنْ قَرَأَ سُورَةَ الْكَهْفِ فِي يَوْمِ الْجُمُعَةِ أَضَاءَ لَهُ مِنَ النُّورِ مَا بَيْنَهُ وَبَيْنَ الْجُمُعَتَيْنِ»

*"Yeyote mwenye kusoma Suratal Kahf siku ya Ijumaa, atamulikiwa mwangaza kutoka Ijumaa moja hadi nyingine".*

Kisha akasema: "Hadithi hii ina silsila (Isnadi) iliyo sahihi, lakini wao (Al-Bukhaariy na Muslim) hawakuinukuu."<sup>1</sup> Al-Haafidh Abukakar Al-Bayhaqiy رحمه الله تعالى pia ameinukuu katika *Sunan* yake kutoka kwa Al-Haakim, kisha akapokea kwa Isnadi yake kutoka kwa Mtume ﷺ kuwa amesema:

«مَنْ قَرَأَ سُورَةَ الْكَهْفِ كَمَا نَزَلَتْ، كَانَتْ لَهُ نُورًا يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

*"Mwenye kusoma Suratal Kahf kama ilivyoteremka, atakuwa na nuru Siku ya Kiyama"<sup>2</sup>*

\* \* \*

<sup>1</sup> Muslim 1:555, Abu Daawuud 4:497, An-Nasaa'iy katika Al-Kubraa 6:236 na Tuhfat Al-Ahwadhiy 8:195.

<sup>2</sup> Al-Haakim 2:368.

<sup>3</sup> Al-Bayhaqiy 3:249.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْكَافِرَاتِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَنْزَلَ عَلَىٰ عَبْدِهِ الْكِتَابَ وَلَمْ يَجْعَلْ لَهُ عِوَجًا ﴿١﴾  
 قِيمًا يُنذِرَ بِأَسَا شَدِيدًا مِّنْ لَّدُنْهُ وَيُبَشِّرَ  
 الْمُؤْمِنِينَ الَّذِينَ يَعْمَلُونَ الصَّالِحَاتِ أَنَّ لَهُمْ أَجْرًا  
 حَسَنًا ﴿٢﴾ مَّكِينٍ فِيهِ أَبَدًا ﴿٣﴾ وَيُنذِرَ الَّذِينَ  
 قَالُوا اتَّخَذَ اللَّهُ وَلَدًا ﴿٤﴾ مَا هُمْ بِهِ مِنْ عِلْمٍ وَلَا  
 لِأَبَائِهِمْ كَبُرَتْ كَلِمَةً تَخْرُجُ مِنْ أَفْوَاهِهِمْ ۖ إِنَّ يَقُولُونَ  
 إِلَّا كَذِبًا ﴿٥﴾ فَلَعَلَّكَ بِنِعْمَتِ اللَّهِ عَلَيْهِمْ إِنْ لَمْ  
 يُؤْمِنُوا بِهِذَا الْحَدِيثِ أَسَفًا ﴿٦﴾ إِنَّا جَعَلْنَا مَا عَلَى  
 الْأَرْضِ زِينَةً لِّهَا لِنَبْلُوهُمْ أَيُّهُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ﴿٧﴾ وَإِنَّا  
 لَجَاعِلُونَ مَا عَلَيْهَا صَعِيدًا جُرُزًا ﴿٨﴾ أَمْ حَسِبْتَ أَنَّ  
 أَصْحَابَ الْكَهْفِ وَالرَّقِيمِ كَانُوا مِنْ آيَاتِنَا عَجَبًا ﴿٩﴾ إِذْ  
 أَوَى الْفِتْيَةُ إِلَى الْكَهْفِ فَقَالُوا رَبَّنَا آتِنَا مِن لَّدُنكَ رَحْمَةً  
 وَهَيِّئْ لَنَا مِنْ أَمْرِنَا رَشَدًا ﴿١٠﴾ فَضَرَبْنَا عَلَىٰ آذَانِهِمْ فِي  
 الْكَهْفِ سِنِينَ عَدَدًا ﴿١١﴾ ثُمَّ بَعَثْنَاهُمْ لِنَعْلَمَ أَيُّ  
 الْحِزْبَيْنِ أَحْصَىٰ لِمَا لَبِئُوا أَمَدًا ﴿١٢﴾

الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَنْزَلَ عَلَىٰ عَبْدِهِ  
 الْكِتَابَ وَلَمْ يَجْعَلْ لَهُ عِوَجًا ﴿١﴾  
 قِيمًا يُنذِرَ بِأَسَا شَدِيدًا مِّنْ لَّدُنْهُ  
 وَيُبَشِّرَ الْمُؤْمِنِينَ الَّذِينَ يَعْمَلُونَ  
 الصَّالِحَاتِ أَنَّ لَهُمْ أَجْرًا حَسَنًا ﴿٢﴾  
 مَّكِينٍ فِيهِ أَبَدًا ﴿٣﴾ وَيُنذِرَ  
 الَّذِينَ قَالُوا اتَّخَذَ اللَّهُ وَلَدًا ﴿٤﴾  
 مَا هُمْ بِهِ مِنْ عِلْمٍ وَلَا لِأَبَائِهِمْ  
 كَبُرَتْ كَلِمَةً تَخْرُجُ مِنْ أَفْوَاهِهِمْ ۖ  
 إِنَّ يَقُولُونَ إِلَّا كَذِبًا ﴿٥﴾

1. Sifa zote njema Anastahiki Allah, Ambaye Amemte-remshia mja Wake Kitabu, wala hakukifanya kina upogo.

2. Amekifanya kimenyooka sawa, ili kitoe onyo kali kutoka Kwake, na kiwabashirie Waumini watendao mema kwamba watapata ujira mzuri.

3. Wakae humo milele.

**4. Na kiwaonye wanaosema: Allah ana mwana.**

**5. Wao hawana ujuzi wa jambo hili, wala baba zao. Ni neno kuu hilo litokalo vinywani mwao. Hawasemi ila uongo tu.**

### Wahyi wa Qur'ani unaleta Bishara Njema na Onyo

Mwanzo wa tafsiri hii, tumetaja kuwa Allah تعالى, Anaitukuza Nafsi Yake Tukufu mwanzoni na mwisho wa mambo, kwani Yeye Ndiye wa Kuhimidiwa katika hali zote. Sifa zote njema na Shukurani Anastahiki Yeye, mwanzoni na mwishoni pia. Anajisifu Mwenyewe kwa Kuteremsha Kitabu Chake kikuu kwa Mtume Wake, Muhammad ﷺ, ambacho ni neema kubwa ambayo Allah تعالى Amewatunukia watu wa ardhi hii. Kupitia kwa Qur'ani, Anawatoa gizani Kuelekea kwenye mwangaza. Amekifanya (Kitabu) chenye kufunza (moja kwa moja), bila kupotoka wala kukanganya ndani yake. Kinaongoza kwa uwazi kabisa katika njia nyoofu, iliyo wazi na bayana, kikiwaonya makafiri na kuwapa bishara Waumini.

Hii ndiyo sababu ya Allah تعالى Kusema:

وَلَمْ يَجْعَلْ لَهُ عِوَجًا ۝

**“Wala Hakukifanya kina upogo.”**

Maana yake: Hakuna utata wala upotofu au upogo. Hata hivyo, Amekifanya kuwa chenye mizani na ubayana. Kama Alivyosema:

قِيمًا

**“...Kimenyooka sawa...”**

Maana yake: Waziwazi na nyoofu.

لِيُنذِرَ بَأْسًا شَدِيدًا مِّن لَّدُنْهُ

**“...Ili kitoe onyo kali kutoka Kwake...”**

Maana yake: Kwa wale wenye kumpinga Mtume Wake na kukikanusha Kitabu Chake, Anatoa onyo kwa adhabu kali inayoharakishwa katika dunia hii na kuahirishwa hadi katika ulimwengu mwengine, Akhera.

مِنْ لَدُنْهُ

**“...Kutoka Kwake...”**

Maana yake: Kutoka kwa Allah تعالى. Hakuna anayeweza kuadhibu kama Anavyoadhibu na hakuna aliye na nguvu au mwenye kuaminika kuliko Yeye. Pia,

وَيُبَشِّرُ الْمُؤْمِنِينَ

**“...Kiwabashirie Waumini...”**

Maana yake: Wale wenye kuiamini Qur’ani hii na kuithibitisha Imani yao kwa matendo mema. Natija yao,

أَنْ لَهُمْ أَجْرًا حَسَنًا

**“...Kwamba watapata ujira mzuri...”**

Maana yake: Zawadi na ujira mzuri sana kutoka kwa Allah تعالى.

مَكِينٍ فِيهِ

**“...Wakae humo...”** Maana yake: Kwa ujira utokao kwa Allah تعالى, nayo ni Pepo, ambamo wataishi humo daima.

أَبَدًا

**“Milele.”**

Maana yake: Daima, usiokuwa na mwisho au kusimama. Na Kauli Yake:

وَيُنذِرَ الَّذِينَ قَالُوا اتَّخَذَ اللَّهُ وَلَدًا

**“Na kiwaonye wanaosema: Allah Ana mwana.”**

Ibn Is’haaq رحمه الله تعالى amesema: “Hawa ni wapagani (washirikina) wa Kiarabu, waliosema: ‘Tunawaabudu Malaika ambao ni mabinti wa Allah’<sup>1</sup>”

Na Kauli Yake:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 17: 595.

مَا هُمْ بِمِنَ عِلْمٍ

“...*Wao hawana ujuzi wa jambo hili...*”Maana yake: Kuhusu jambo hili walilozua na kulitunga.

وَلَا لِأَبَائِهِمْ

“...*Wala baba zao...*”Maana yake: Waliotangulia. Hakika ni kuwa,

كَبُرَتْ كَلِمَةً

“...*Ni neno kuu hilo...*”

Hii inaashiria ukuu na uzito wa uwongo walioutunga. Allah تعالى Anasema:

كَبُرَتْ كَلِمَةً تَخْرُجُ مِنْ أَفْوَاهِهِمْ

“*Ni neno kuu hilo litokalo vinywani mwao.*”

Maana yake: Hauna msingi mbali na wanayoyasema, nao hawana dalili yoyote isipokuwa uongo wao wenyewe na uzushi wao. Hivyo Allah Aliyetukuka Akasema:

إِنْ يَقُولُونَ إِلَّا كَذِبًا

“*Hawasemi ila uwongo tu.*”

### Sababu ya Kuteremshwa Sura hii

Muhammad bin Is’haaq رحمه الله تعالى ametaja sababu ya kuteremshwa Sura hii. Amesema kuwa mtu mkongwe miongoni mwa watu wa Misri alikuja kwao miaka arobaini na ushei iliyopita na kuwaambia, kutoka kwa Ikrimah kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Makureshi walimtuma An-Nadhr bin Al-Haarith na ‘Uqbah bin Abi Mu’it kwa wanazuoni wa Kiyahudi Madina, na kuwaambia: Waulizeni (wanazuoni) kuhusu Muhammad, na wafahamisheni kumhusu, na waambieni anayosema. Hakika wao ni watu wa kitabu cha mwanzo, nao wana ujuzi zaidi wa manabii kuliko sisi.”

Hivyo, walifunga safari na walipofika Madina, waliwauliza wanazuoni wa Kiyahudi kuhusu Mtume ﷺ. Walimuelezea kwao na kuwaambia baadhi ya kauli zake. Wakasema: ‘Nyinyi ni watu wa Taurati, nasi tumekuja kwenu ili mtueleze kuhusu sahibu wetu huyu’.



Wao (wanazuoni) walisema: 'Muulizeni kuhusu mambo matatu ambayo tutakuambieni, akiwajibu basi yeye ni Nabii wa kweli aliyetumwa na Allah تعالى: asipowajibu basi atakuwa anasema vitu visivyokuwa kweli. Katika hali hiyo mtakavyomfanya itakuwa ni juu yenu. Muulizeni kuhusu baadhi ya vijana wa kale, kisa chao kilikuwaje? Kwani kisa chao ni cha ajabu. Muulizeni kuhusu mtu aliyesafiri sana na akafika mashariki na magharibi ya dunia. Kisa chake kilikuwa kipi? Na muulizeni kuhusu Roho – hiyo ni nini?. Akiwaambieni kuhusu haya matatu, basi yeye ni Nabii, hivyo mfuateni, lakini akishindwa kuwajibu hayo, atakuwa ni mtu mwenye kuzua mambo, katika hali hiyo mfanyeni mnavyoona sawa'. Hivyo, An-Nadhr na 'Uqbah walirudi kwa Makureshi na kuwaambia: 'Enyi Makureshi! Tumekuja kwenu na suluhisho muafaka kabisa ambalo litamaliza shida baina yenu na Muhammad. Wanazuoni wa Kiyahudi wametuaambia tumuulize kuhusu baadhi ya mambo', Na wakawaambia mambo yenyewe. Kisha wakaja kwa Mtume ﷺ na kumuambia: 'Ewe Muhammad! Tuambie', na wakamuuliza kuhusu yale mambo waliyoambiwa wayaulize. Mtume ﷺ akawaambia:

«أَخْبِرْكُمْ غَدًا عَمَّا سَأَلْتُمْ عَنْهُ»

*'Nitawaambieni kesho mliyo yauliza',*

Lakini hakusema, 'Insha' Allah - Allah تعالى Akipenda' Hivyo, walikwenda zao, na Mtume ﷺ akakaa kwa siku kumi na tano (15) bila ya wahyi wowote kutoka kwa Allah تعالى kuhusu hayo, pia Jibril عليه السلام hakuja kwake. Watu wa Makka walianza kumshuku, na kusema, Muhammad ametuahidi kutujibu siku ya pili, na sasa siku kumi na tano zimepita na hajatuambia chochote katika kutujibu maswali tuliyomuuliza'.

Mtume ﷺ alihuzunika kwa sababu ya kuchelewa kuja kwa Wahyi, na akahuzunishwa kwa yale waliokuwa wakiyasema watu wa Makkah kumhusu. Kisha Jibril عليه السلام alikuja kwake kutoka kwa Allah تعالى na Sura kuhusu vijana wa pangoni, pia ikawa ni kemeo kwa kuhisi huzuni kuhusu wapagani. Sura pia ilimhadithia kuhusu mambo waliyomuuliza, vijana na msafiri. Suala la Roho lilijibiwa katika Aya:

وَسْأَلُونَكَ عَنِ الرُّوحِ قُلِ الرُّوحُ

***"Na wanakuuliza habari ya Roho. Sema: 'Roho...' (17:85)"***<sup>1</sup>.

<sup>1</sup> At-Tabari 17:592. Isnadi yake ni dhaifu, kwa kutojulikana mtu mzima aliyetoka Misri.

فَلَعَلَّكَ بِنِعْمِ نَفْسِكَ عَلَىٰ ءَاثَرِهِمْ إِن لَّمْ يُؤْمِنُوا بِهَذَا الْحَدِيثِ أَسَفًا ﴿١٨﴾ إِنَّا جَعَلْنَا  
 مَا عَلَى الْأَرْضِ زِينَةً لِّهَا لِنَبْلُوهُمْ أَيُّهُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ﴿١٩﴾ وَإِنَّا لَجَاعِلُونَ مَا عَلَيْهَا صَعِيدًا  
 جُرُزًا ﴿٢٠﴾

**6. Huenda ukajihiliki nafsi yako kwa ajili yao, kuwasikitikia kwa kuwa hawayaamini mazungumzo haya!**

**7. Kwa hakika Tumevifanya vilioko juu ya ardhi kuwa ni pambo lake ili Tuwafanyie mtihani, ni nani kati yao wenye vitendo vizuri zaidi.**

**8. Na hakika Sisi Tutavifanya vyote vilio juu ya ardhi kuwa kama nchi iliopigwa na ukame.**

### Usisikitike na Kuona Vibaya kwa kuwa Washirikina Hawaamini

Allah تعالیٰ Anamliwaza Mtume Wake kwa huzuni aliyokuwa nayo kuhusu wapagani kwa sababu ya kutoamini kwao na kujitenga naye. Pia Alisema Aliyetukuka:

فَلَا تَذْهَبْ نَفْسُكَ عَلَيْهِمْ حَسْرَتٍ ۗ

**“Basi roho yako isitoke kwa majonzi juu yao.” (35:8).** Na pia, Amesema,

وَلَا تَحْزَنْ عَلَيْهِمْ

**“Wala usihuzunike kwa ajili yao.” (16:127).** Na Amesema tena:

لَعَلَّكَ بِنِعْمِ نَفْسِكَ أَلَّا يَكُونُوا مُؤْمِنِينَ ﴿٢٦﴾

**“Huenda (wewe Nabii Muhammad) utaangamiza nafsi yako kwa sababu hawawi Waumini.” (26:3),**

Maana yake: Huenda ukajiangamiza kwa huzuni na masikitiko yako kwa ajili yao. Anasema Aliyetukuka:

فَلَعَلَّكَ بِنِعْمِ نَفْسِكَ عَلَىٰ ءَاثَرِهِمْ إِن لَّمْ يُؤْمِنُوا بِهَذَا الْحَدِيثِ

**“Huenda ukajihiliki nafsi yako kwa ajili yao, kwa kuwa hawayaamini mazungumzo haya.”**

Maana: Qur'ani.



***“Kwa kuwasikitikia”.***

Allah تعالى Anasema hapa, “Usijiangamize kwa majuto” Qataadah amesema: “Kuiua nafsi yako kwa hasira na huzuni juu yao.”<sup>1</sup> Mujaahid amesema: “Kwa hamu”<sup>2</sup>. Hizi zinafanana, hivyo maana itakuwa: “Usiwasikitikie, bali fikisha ujumbe wa Allah تعالى kwao. Yeyote atakayeongoka na kufuata njia ya sawa, hivyo atafuata njia ya sawa kwa faida yake mwenyewe. Ne yeyote mwenye kupotoka, hivyo anakwenda kombo kwa hasara yake mwenyewe. Kwa hiyo usijiangamize kwa kuwahuzunikia.”

**Dunia ni Mahali pa Majaribio**

Kisha Allah تعالى Anatuambia Ameiumba dunia hii kuwa makazi ya muda, iliyopambwa na uzuri wa kupita, na Akaifanya kuwa ni mahali pa mitihani na majaribio, sio mahali pa makao ya maisha. Hivyo Akasema:

إِنَّا جَعَلْنَا مَا عَلَى الْأَرْضِ زِينَةً لَهَا لِنَبْلُوهُمْ أَيُّهُمْ أَحْسَنُ عَمَلًا ﴿١٣١﴾

***“Kwa hakika Tumevifanya vilioko juu ya ardhi kuwa ni pambo lake ili Tuwafanyie mtihani, ni nani kati yao wenye vitendo vizuri zaidi”.***

Abu Maslamah amepokea kutoka kwa Abu Nadhrah naye kutoka kwa Abu Said رضي الله عنه kutoka Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ الدُّنْيَا حُلُوهٌ خَصِرَةٌ، وَإِنَّ اللَّهَ مُسْتَخْلِفُكُمْ فِيهَا فَنَظِرٌ مَّاذَا تَعْمَلُونَ، فَاتَّقُوا الدُّنْيَا، وَاتَّقُوا النَّسَاءَ، فَإِنَّ أَوَّلَ فِتْنَةٍ بَنِي إِسْرَائِيلَ كَانَتْ فِي النِّسَاءِ»

*“Hakika dunia ni tamu na kijani, na hakika Allah Atawafanya makhalifa ndani yake, kizazi baada ya kizazi, Naye Anakutizameni kwa mtakayofanya. Tahadharini na dunia na wanawake, kwani fitnah ya kwanza iliyowakumba Banu (Wana) Israili ilikuwa kwa wanawake.”<sup>3</sup>*

<sup>1</sup> At-Tabari 17:597-598.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:598.

<sup>3</sup> Ahmad 3:22.

Kisha Allah تعالى Anatuambia kuwa dunia hii itapita na kufika kikomo kama Anavyosema:

وَإِنَّا لَجَاعِلُونَ مَا عَلَيْهَا صَعِيدًا جُرُزًا ﴿١٧﴾

**“Na hakika Sisi Tutavifanya vyote vilio juu ya ardhi kuwa kama nchi iliopigwa na ukame”**

Maana: Baada ya kuipamba, Tutaihiliki na kufanya kila kitu ndani yake kuwa kitupu na kikavu, bila ya mimea au faida yoyote ile.

Amepokea Al-Awfiy kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuwa hii inamaanisha kila kitu juu yake kitaangamizwa na kuharibiwa.<sup>1</sup> Mujaahid amesema: “Tambarare, kavu na kame.”<sup>2</sup> Na Qataadah amesema: “Tambarare ambayo haitakuwa na miti au mimea.”<sup>3</sup>

أَمْ حَسِبْتَ أَنَّ أَصْحَابَ الْكَهْفِ وَالرَّقِيمِ كَانُوا مِنْ آيَاتِنَا عَجَبًا ﴿١٨﴾ إِذْ أَوَى الْفِتْيَةُ إِلَى الْكَهْفِ فَقَالُوا رَبَّنَا آتِنَا مِنْ لَدُنْكَ رَحْمَةً وَهَيِّئْ لَنَا مِنْ أَمْرِنَا رَشَدًا ﴿١٩﴾ فَضَرَبْنَا عَلَى آذَانِهِمْ فِي الْكَهْفِ سِنِينَ عَدَدًا ﴿٢٠﴾ ثُمَّ بَعَثْنَاهُمْ لِنَعْلَمَ أَيُّ الْحِزْبَيْنِ أَحْصَى لِمَا لَبِئُوا أَمَدًا ﴿٢١﴾

**9. Bali unadhani ya kwamba wale Watu wa Pangoni na Raqim walikuwa ni ajabu miongoni mwa ishara Zetu?**

**10. Vijana hao walipokimbilia kwenye pango walisema: Mola wetu Mlezi! Tupe rehema itokayo Kwako, na Tutengezee uongofu katika jambo letu.**

**11. Tukayaziba masikio yao kuwalaza humo pangoni kwa muda wa miaka kadhaa wa kadhaa.**

**12. Kisha Tukawazindua ili Tujue ni lipi katika makundi mawili lilio hisabu sawa muda waliokaa.**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:599.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:599.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:600.

## Kisa cha Watu wa Pangoni

Hapa Allah تعالى Anatuelezea kisa cha watu wa pangoni kwa muhtasari na ujumla, kisha Anaeleza kwa kina. Anasema Aliyetukuka:

أَمْرٌ حَسِبْتِ

*“Bali mnadhani”, Ewe Muhammad,*

أَنْ أَصْحَبَ الْكَهْفِ وَالرَّقِيمِ كَانُوا مِنْ آيَاتِنَا عَجَبًا ﴿١٧﴾

***“Ya kwamba wale Watu wa Pangoni na Raqiim walikuwa ni ajabu miongoni mwa ishara Zetu?”***

Maana: Kisa chao sio cha ajabu kikilinganishwa na Nguvu na Uwezo Wetu, wa Kuumba mbingu na ardhi, mabadiliko ya usiku na mchana na Kutiishwa kwa jua, mwezi na sayari nyengine. Na ishara nyengine inaonesha nguvu kuu ya Allah تعالى na yaonesha kuwa Yeye ni Muweza wa Kufanya Atakalo. Yeye Hashindwi Kufanya mambo ya ajabu kuliko Kisa cha watu wa Pangoni. Vivyo hivyo, Ibn Jurayj amemnukuu Mujaahid kuwa alisema,

أَمْرٌ حَسِبْتِ أَنْ أَصْحَبَ الْكَهْفِ وَالرَّقِيمِ كَانُوا مِنْ آيَاتِنَا عَجَبًا ﴿١٧﴾

***“Bali mnadhani ya kwamba wale Watu wa Pangoni na Raqiim walikuwa ni ajabu miongoni mwa ishara Zetu?”***

“Miongoni mwa ishara Zetu kuna vitu vya ajabu zaidi kuliko hili.”<sup>1</sup>

Amepokea Al-Awfiy kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema:

أَمْرٌ حَسِبْتِ أَنْ أَصْحَبَ الْكَهْفِ وَالرَّقِيمِ كَانُوا مِنْ آيَاتِنَا عَجَبًا ﴿١٧﴾

***“Bali mnadhani ya kwamba wale Watu wa Pangoni na Raqiim walikuwa ni ajabu miongoni mwa ishara Zetu?”***

‘Niliyokupa katika elimu, Sunna na Kitabu ni bora zaidi kuliko kisa cha watu wa Pangoni na *Ar-Raqiim*.”<sup>2</sup> Muhammad bin Is’haaq رحمه الله تعالى amesema: “Inamaanisha ya kuwa niliyowaonesha viumbe Vyangu miongoni mwa ishara Zangu ni ya ajabu zaidi kuliko Kisa cha watu wa Pangoni na *Ar-Raqiim*.”<sup>3</sup>

<sup>1</sup> At-Tabari 17:601.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:601.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:601.

*Al-Kahf* ina maana ya pango katika mlima, ambamo vijana waliotajwa walitafuta himaya na ukimbizi humo. Ama kuhusu neno *ar-Raqiim*, Al-Awfiy amepokea kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kuwa ni bonde karibu na Aylah.<sup>1</sup> Hii pia ilisemwa (katika riwaya nyengine) ya Atwiyah Al-Awfiy na Qatadah. Adh-Dhahaak amesema: "Ama kuhusu *Al-Kahf*, ni pango katika bonde<sup>2</sup>, na *Ar-Raqiim* ni jina la bonde lenyewe". Mujaahid amesema: "*Ar-Raqiim* inahusisha majumba yao". Wengine wasema kuwa ina maana ya bonde ambalo pango lilikiwemo ndani yake.<sup>3</sup>

'Abdur-Razzaaq amenukuu kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema yafuatayo kuhusu *Ar-Raqiim*: "Ka'b alikuwa akisema kuwa ulikuwa ni mji". Amepokea Ibn Jurayj kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: "*Ar-Raqiim* ni mlima uliokuwa na pango."<sup>4</sup> Said bin Jubayr amesema, "*Ar-Raqiim* ni ubao wa jiwe ambao waliandika Kisa cha watu wa pango, kisha wakaliweka katika mlango wa pango lenyewe."<sup>5</sup> Na Kauli Yake Aliyetukuka:

إِذْ أَوَى الْفِتْيَةُ إِلَى الْكَهْفِ فَقَالُوا رَبَّنَا آتِنَا مِن لَّدُنكَ رَحْمَةً وَهَيِّئْ لَنَا مِنْ أَمْرِنَا رَشَدًا ﴿١٨﴾

***"Vijana hao walipokimbilia kwenye pango walisema: Mola wetu Mlezi! Tupe rehema itokayo Kwako, na Tutengezee uwongofu katika jambo letu."***

Hapa Allah تعالى Anatuambia kuhusu vijana waliowakimbia watu wao kwa ajili ya Dini yao, huku wakiogopa kunyanyaswa. Hivyo, walikimbia kutafuta himaya kwenye pango lililokuwa kwenye mlima, ambamo walijificha kutoka kwa watu wao. Walipoingia ndani ya pango, walimuomba Allah تعالى Awarehemu na Kuwahurumia wao:

رَبَّنَا آتِنَا مِن لَّدُنكَ رَحْمَةً

***"Mola wetu Mlezi! Tupe rehema itokayo Kwako."***

Maana yake: Tupe rehema itokayo Kwako na Utusitiri na watu wetu. Na Kauli Yake:

<sup>1</sup> At-Tabari 17:602.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:602.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:602.

<sup>4</sup> At-Tabari 17:602.

<sup>5</sup> Sanadi yake ni dhaifu, isitoshe Ibn Jurayj hakupokea kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما.

وَهَيَّءْ لَنَا مِنْ أَمْرِنَا رَشَدًا ﴿١٧﴾

**“Na Tutengezee uongofu katika jambo letu.”**

Maana yake: Tuongoze katika jambo letu (tupe mwisho mwema). Kama ilivyopokewa katika Hadithi:

«وَمَا قَضَيْتُ لَنَا مِنْ قَضَاءٍ فَاجْعَلْ عَاقِبَتَهُ رَشَدًا»

*“Lolote Ulilotuamulia, Ufanye mwisho wake uwe mwema.”<sup>1</sup>*

Na Kauli Yake:

فَضَرْتَنَا عَلَىٰ آذَانِهِمْ فِي الْكَهْفِ سِنِينَ عَدَدًا ﴿١٨﴾

**“Tukayaziba masikio yao kuwalaza humo pangoni kwa muda wa miaka kadhaa wa kadhaa.”**

Maana yake: Tuliwafanya kulala walipoingia pangoni, nao wakalala kwa miaka mingi.

ثُمَّ بَعَثْنَاهُمْ

**“Kisha Tukawazindua.”**

Kutoka katika usingizi, na mmoja wao alitoka nje na Dirham yake (pesa za aina ya madini ya fedha) ili kuwanunulia chakula, kama itakavyozungumzwa kwa kina chini. Allah تعالى Anasema:

ثُمَّ بَعَثْنَاهُمْ لِنَتَلَمَّرَ أَيُّ الْحَزِينِ

**“Kisha Tukawazindua ili Tujue ni lipi katika makundi mawili.”**

Maana yake: makundi mawili yazozanayo kuhusu wao,

أَحْصَىٰ لِمَا لَبِثُوا أَمَدًا ﴿١٩﴾

**“Lilio hisabu sawa muda waliokaa.”**

Imesemwa kuwa hii ina maana ni muda gani waliokaa pangoni.

\* \* \*

<sup>1</sup> Ahmad 6:147.

نَحْنُ نَقُصُّ عَلَيْكَ نَبَأَهُم بِالْحَقِّ إِنَّهُمْ فِتْنَةٌ ءَامَنُوا بِرَبِّهِمْ  
 وَزِدْنَاهُمْ هُدًى ﴿١٣﴾ وَرَبَطْنَا عَلَى قُلُوبِهِمْ إِذْ قَامُوا فَقَالُوا  
 رَبُّنَا رَبُّ الْأَرْضِ لَنْ نَدْعُوَ مِنْ دُونِهِ ءِالِهَةً  
 لَقَدْ قُلْنَا إِذَا شَطَطًا ﴿١٤﴾ هَتُولَاءِ قَوْمَنَا أَلْتَّخَذُوا مِنْ دُونِهِ  
 ءِالِهَةً لَوْلَا يَأْتُونَ عَلَيْهِم بِسُلْطَانٍ بَيِّنٍ فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّن  
 أَفْتَرَى عَلَى اللَّهِ كَذِبًا ﴿١٥﴾ وَإِذْ أَعْرَضْتُمُوهُمْ وَمَا  
 يَعْبُدُونَ إِلَّا اللَّهَ فَأَوْرَأْنَا إِلَى الْكَهْفِ يَنْشُرُ لَكُمْ رَبُّكُمْ مِنْ  
 رَحْمَتِهِ وَيُهَيِّئْ لَكُمْ مِنْ أَمْرِكُمْ مِزْفَقًا ﴿١٦﴾ \* وَتَرَى  
 الشَّمْسَ إِذَا طَلَعَتْ تَرَاوُرُ عَنْ كَهْفِهِمْ ذَاتَ الْيَمِينِ وَإِذَا  
 غَرَبَتْ تَقْرِضُهُمْ ذَاتَ الشِّمَالِ وَهُمْ فِي فَجْوَةٍ مِنْهُ ؕ ذَلِكَ  
 مِنْ ءَايَاتِ اللَّهِ مَنْ يَهْدِ اللَّهُ فَهُوَ الْمُهْتَدِ ؕ وَمَنْ يُضِلِلْ  
 فَلَنْ يَجِدَ لَهُ وَلِيًا مُرْشِدًا ﴿١٧﴾ وَتَحْسَبُهُمْ آيِقَاطًا وَهُمْ رُقُودٌ  
 ؕ وَنُقَلِّبُهُمْ ذَاتَ الْيَمِينِ وَذَاتَ الشِّمَالِ ؕ وَكَلْبُهُمْ بَاسِطٌ  
 ذِرَاعَيْهِ بِالْوَصِيدِ ؕ لَوِ اطَّلَعْتَ عَلَيْهِمْ لَوَلَّيْتَ مِنْهُمْ فِرَارًا  
 وَلَمَلَأْتَ مِنْهُمْ رُعبًا ﴿١٨﴾

نَحْنُ نَقُصُّ عَلَيْكَ نَبَأَهُم بِالْحَقِّ إِنَّهُمْ فِتْنَةٌ ؕ  
 ءَامَنُوا بِرَبِّهِمْ وَزِدْنَاهُمْ هُدًى ﴿١٣﴾  
 وَرَبَطْنَا عَلَى قُلُوبِهِمْ إِذْ قَامُوا فَقَالُوا  
 رَبُّنَا رَبُّ الْأَرْضِ لَنْ نَدْعُوَ مِنْ دُونِهِ ءِالِهَةً  
 لَقَدْ قُلْنَا إِذَا شَطَطًا ﴿١٤﴾ هَتُولَاءِ  
 قَوْمَنَا أَلْتَّخَذُوا مِنْ دُونِهِ ءِالِهَةً لَوْلَا  
 يَأْتُونَ عَلَيْهِم بِسُلْطَانٍ بَيِّنٍ فَمَنْ  
 أَظْلَمُ مِمَّنْ أَفْتَرَى عَلَى اللَّهِ كَذِبًا ﴿١٥﴾  
 وَإِذْ أَعْرَضْتُمُوهُمْ وَمَا يَعْبُدُونَ إِلَّا  
 اللَّهَ فَأَوْرَأْنَا إِلَى الْكَهْفِ يَنْشُرُ لَكُمْ رَبُّكُمْ  
 مِنْ رَحْمَتِهِ وَيُهَيِّئْ لَكُمْ مِنْ أَمْرِكُمْ  
 مِزْفَقًا ﴿١٦﴾

**13. Sisi Tunakusimulia habari zao kwa kweli. Hakika wao walikuwa ni vijana waliomuamini Mola**

**wao Mlezi. Na Sisi Tukawazidisha uongofu.**

**14. Na Tukazitia nguvu nyoyo zao waliposimama na wakasema: Mola wetu Mlezi ni Mola Mlezi wa mbingu na ardhi. Hatutamuita mwengineuwe kabisa badala Yake kuwa ni Mungu. Hivyo itakuwa tumesema jambo la kuvuka mpaka.**

**15. Hawa watu wetu wameshika miungu mingine badala Yake Yeye. Kwa nini basi hawatolei uthibitisho uliodhahiri? Na nani aliyedhalimu zaidi kuliko anayemzulia uongo Allah?**



**16. Na mkijitenga nao na vile wanavyoviabudu badala ya Allaah, basi kimbilieni pangoni, Akufungulieni Mola wenu Mlezi Rehema Yake, na Akutengenezeeni ya kukufaeni katika mambo yenu.**

### **Kumuamini Kwao Allah ﷻ na Kujitenga Mbali na Jamaa Zao**

Kuanzia hapa Allah ﷻ Anaanza kutueleza Kisa kwa kina. Anatueleza kuwa hao walikuwa vijana, waliokubali ukweli na haki na walioongoka zaidi kuliko wazee walioshikilia njia zao kwa ukaidi na kukamata dini ya uwongo na batili. Kwa sababu hiyo hiyo, wengi wa wale walioitikia wito wa Allah ﷻ na Mtume Wake ﷺ walikuwa ni vijana. Ama kuhusu wazee wa Kikureshi, wengi wao walijikita katika dini yao na wachache ndio waliosilimu.

Hivyo, Allah ﷻ Anatuambia kuwa watu wa pango walikuwa ni vijana. Mujaahid amesema: “Nimejulishwa kuwa baadhi yao walikuwa wamevaa hereni, kisha Allah ﷻ Akawaongoza na kuwapatia ilhamu wamuogope Yeye, hivyo wakatambua Upweke Wake, na kushuhudia kuwa hapana Mola apasaye kuabudiwa ila Yeye.”<sup>1</sup>

وَزِدْنَهُمْ هُدًى

**“Na Sisi Tukawazidishia uongofu.”**

Kutokana na Aya hii na nyengine mfano wake, wanazuoni wengi, kama vile al-Bukhaariy na wengine, wamefahamu kuwa Imani huzidi na kupungua.

Na kwa ajili hiyo Allah ﷻ Anasema:

وَزِدْنَهُمْ هُدًى

**“Na Sisi Tukawazidishia uongofu.”**

Kama Alivyosema kwengineko:

وَالَّذِينَ آهْتَدَوْا زَادَهُمْ هُدًى وَءَاتَيْنَهُمْ تَقْوَانَهُمْ

**“Na wale wanaokubali kuongoka Anawazidishia uongofu na Anawapa jaza ya ucha Mungu wao.” (47:17).**

<sup>1</sup> Fat’h Al-Baariy 1:60.

Na pia Amesema,

فَأَمَّا الَّذِينَ ءَامَنُوا فَزَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَهُمْ يَسْتَبْشِرُونَ ﴿١٣﴾

**“...Ama wale walioamini inawazidishia Imani, nao wanafurahi.”  
(9:124).**

Aidha Amesema,

لِيَزِدَادُوا إِيمَانًا مَعَ إِيمَانِهِمْ ۗ

**“Ili waongezeke Imani juu ya Imani yao...” (48:4)**

Zipo Aya nyengine zinazoashiria suala hilo hilo.

Imetajwa kuwa wao walikuwa ni wafuasi wa Dini ya Masihi, 'Isaa bin Maryam عليه السلام, lakini Allah تعالى Ndiye Anayejua zaidi. Inaonekana kuwa waliishi kabla ya Ukristo, kwa sababu kama wangekuwa Wakristo, wanazuoni wa Kiyahudi hawangejali kuhifadhi kisa chao kwa sababu ya tofauti zao. Tumetaja hapo juu mapokezi kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kuwa Makuraishi walituma ujumbe kwa wanazuoni wa Kiyahudi waliokuwa Madina kuwauliza mambo ambayo wangeweza kumjaribu nayo Mtume ﷺ, nao waliwaambia wamuulize kuhusu hawa vijana, na kuhusu Dhul Qarnayn (mtu aliyesafiri sana) na kuhusu Roho.

Hii inaashiria kuwa kisa hichi kimehifadhiwa na kunukuliwa katika vitabu vya Watu wa Kitabu, na kuwa kilikuja kabla ya Ukristo. Na Allah تعالى Anajua zaidi. Na Kauli Yake:

وَرَبَطْنَا عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ إِذْ قَامُوا فَقَالُوا رَبُّنَا رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ

**“Na Tukazitia nguvu nyoyo zao waliposimama na wakasema: Mola wetu Mlezi ni Mola Mlezi wa mbingu na ardhi.”**

Hapa Allah تعالى Anasema: ‘Tuliwapatia uvumilivu kwa kupingana na watu wa mji wao, na kuacha maisha ya anasa na starehe waliyokuwa wakiishi jamaa zao.’ Wanazuoni kadhaa wa Tafsiri wa zamani na wa baadaye wametaja kuwa hao walikuwa vijana wa wafalme na viongozi wa Warumi (Bizanta), na kuwa walikwenda siku moja katika moja ya sherehe za watu wao. Walikuwa wakikusanyikana mara moja kila mwaka nje ya mji wao, na hapo waliabudu masanamu na kuwachinjia.

Watu hao walikuwa na mfalme mwenye kiburi na dikteta aliyekuwa akiitwa Decianus, aliyekuwa akihimiza na kuamuru watu kufanya hilo. Watu walipokwenda kuhudhuria sherehe hiyo, hawa vijana walikwenda na baba zao na watu wao. Na walipowaona watu wao wakifanya amali hiyo mbele ya macho yao. Walitambua kuwa kusujudu na watu kuchinja kwa ajili ya masanamu kitendo hicho anatakiwa afanyiwe Allah تعالی tu, Aliyeumba mbingu na ardhi. Kila mmoja wao alianza kujitenga na watu wake na kujiweka mbali nao. Wa kwanza aliyejitenga kivyake alikwenda kukaa kwenye kivuli cha mti, kisha mwengine alikuja kukaa naye, kisha wa tatu alikuja kukaa pamoja nao, kisha wane wengine walifuata mmoja baada ya mwengine. Hakuna aliyemjua mwenziwe, lakini waliletwa pamoja na Mmoja Aliyeingiza Imani nyoyoni mwao.

Kama inavyosema Hadithi iliyonukuliwa na Al-Bukhaari *mu'allaq* (iliyotundikwa kwa kukosekana kwa mpokeaji au wapokeaji katika Isnadi au silsila ya wapokezi kutotimia) kutoka kwa 'Aishah رضي الله عنها aliyesema kuwa Mtume ﷺ amesema:

«الْأَزْوَاجُ جُنُودٌ مُجَنَّدَةٌ، فَمَا تَعَارَفَ مِنْهَا اتَّكَلَفَ وَمَا تَنَاقَرَ مِنْهَا اخْتَلَفَ»

*"Roho ni kama maaskari. Zile zinazotambuana zinakuja pamoja, na zile zisizotambuana miongoni mwazo hutofautiana (kugeuka moja kwa nyengine)."*<sup>1</sup>

Na amepokea Muslim katika Sahihi yake kutoka kwa Hadithi ya Suhayl kutoka kwa babake kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ<sup>2</sup>. Watu wasema kuwa sifa zinazofanana ndizo zinazowaleta watu pamoja.

Hivyo kila mmoja katika vijana hao alikuwa anajaribu kujificha kwa alichokuwa akiamini kutoka kwa wenziwe, kwa kuwaogopa, bila kujua ya kwamba walikuwa kama yeye. Kisha mmoja wao alisema: "Enyi watu, mnajua kwa Allah تعالی kuwa kitu kimoja pekee ndicho kinachowafanya nyinyi kuwaacha watu wenu na kujitenga nao, hivyo kila mmoja wenu adhihirishe jambo lake."

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baariy 6:426.

<sup>2</sup> Muslim 4:2031.

Mwengine akasema: “Ama mimi, niliwaona watu wangu wanavyofanya na nikatambua huo ni uongo, na kuwa anayefaa kuabudiwa kwa haki ni Mmoja Pekee wala hashirikishwi na chochote, naye ni Allah تعالی Aliyeumba kila kitu: mbingu na ardhi na vilivyomo baina yake.” Akasema mwengine: “Na mimi, Wallahi, jambo hilo hilo limenitokea.” Wengine wakasema hivyo hivyo, na wote wakakubaliana kuwa wawe ndugu katika Imani. Wakachukua sehemu moja maalumu kama mahali pa Ibada na wakaanza kumuabudu Allah تعالی hapo, lakini wakajua watu wao kuhusu wao na hivyo kumuambia mfalme wao kuwahusu vijana hao. Mfalme aliamuru kuwa waje mbele yake, naye akawauliza kuhusu waliokuwa nayo katika mambo yao. Walimuambia ukweli mtupu pamoja na kumuita yeye aifate njia ya Allah تعالی kama Alivyosema Allah تعالی kuhusu wao:

وَرَبَطْنَا عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ إِذْ قَامُوا فَقَالُوا رَبُّنَا رَبُّ الْأَرْضِ لَن نَّدْعُوهُ مِن دُونِهِ  
إِلَهًا

**“Na Tukazitia nguvu nyoyo zao waliposimama na wakasema: Mola Wetu Mlezi ni Mola Mlezi wa mbingu na ardhi. Hatutamuita mwenginewe kabisa badala Yake kuwa ni Mungu.”**

Na herufi ya *Lan* katika sarufi ya kiarabu ina maana (hapana) ni kukataa milele, kumaanisha kuwa hili halitokea, na lau ingekuwa ni wa kufanya hivyo itakuwa ni uwongo na batili. Kwa hivyo, Akasema kuwahusu:

لَقَدْ قُلْنَا إِذًا شَطَطًا

**“Lau tutafanya, itakuwa tumesema jambo la kuvuka mpaka.”**

Maana yake: Batili na uwongo wa dhahiri.

هَؤُلَاءِ قَوْمُنَا اتَّخَذُوا مِن دُونِهِ ءَالِهَةً لَّوْلَا يَأْتُونَ عَلَيْهِم بِسُلْطٰنٍ بَيِّنٍ

**“Hawa watu wetu wameshika miungu mingine badala Yake Yeye. Kwa nini basi hawawatolei uthibitisho ulio dhahiri?”**

Maana yake: Kwa nini hawatoi hapo hapo dalili za wazi na dhahiri na sahihi kwa wanayoyaamini?

﴿فَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنِ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا﴾

**“Na nani aliye dhalimu zaidi kuliko anayemzulia uongo Allah?”**

Wakasema: “Bali wao kwa kusema hayo ni madhalimu waongo”. Kulisemwa kuwa walipomlingania mfalme wao amuamini Allah تعالی, alikataa, aliwaonya na kuwatisha. Aliamuru wavuliwe nguo zao zilizokuwa na mapambo ya watu wao, kisha akawapa muda wa kutafakari kuhusu hali yao, akitarajia kuwa watarudi katika dini yao ya awali. Hii ni njia ambayo kwayo Allah تعالی Aliwahurumia, kwa sababu wakati huo waliweza kukimbia kutoka kwake na kukimbia kwa ajili ya dini yao kutokana na fitnah.

Hii ndio iliyofaradhiwa katika sheria katika wakati wa majaribio na mitihani na kutokea kwa fitnah kwa watu, hivyo kumfanya mja kukimbia akihofia Dini yake, kama ilivyokuja katika Hadithi:

«يُوشِكُ أَنْ يَكُونَ خَيْرُ مَالٍ أَحَدِكُمْ عِنَّمَا يَتَّبِعْ بِهَا شَعْفَ الْجِبَالِ وَمَوَاقِعَ الْقَطْرِ يَفِرُّ  
بِدِينِهِ مِنَ الْفِتَنِ»

*“Huenda zikaja zama ambamo mali bora atakayomiliki mmoja wenu ni kondoo, anaoweza kuwafuata hadi kilele cha mlima na sehemu ambazo mvua hunyesha, kukimbia kwa ajili ya Dini yake kutokana na fitnah.”<sup>1</sup>*

Katika hali hiyo, inajuzu kujitenga na watu, lakini hiyo haijaruhusiwa katika hali nyengine yoyote, kwa sababu katika kujitenga huko mtu anakosa fadhila na faida ya Sala za jamaa na Sala ya Ijumaa.

Vijana hawa walikuwa na bidii ya kuwakimbia watu wao, na Allah تعالی Akapitisha hilo kwao, kama Alivyosema kuwahusu:

﴿وَإِذْ أَعْرَضْنَا عَنْهُمْ وَمَا يَعْبُدُونَ إِلَّا اللَّهَ﴾

**“Na mkijitenga nao na vile wanavyo viabudu badala ya Allah.”**

Maana yake: Mlipotengana nao na mkatofautiana nao katika Dini (mkafuata Dini nyengine) na katika Ibada yao ya kuabudu asiyekuwa Allah تعالی, jitengeni nao kimwili pia.

<sup>1</sup> Fat’h Al-Baariy 1:87.

فَأُوتُوا إِلَى الْكَهْفِ يَنْشُرْ لَكُمْ رَبُّكُمْ مِّن رَّحْمَتِهِ

**“Basi kimbilieni pangoni, Akufungulieni Mola wenu Mlezi rehema Yake.”**

Maana yake: Atawapatieni rehema ambayo itawawezesha kujificha kwayo na watu wenu.

وَيُهَيِّئْ لَكُمْ مِّنْ أَمْرِكُمْ مِّرْفَقًا ﴿١٦﴾

**“Na Atakutengenezeeni ya kukufaeni katika mambo yenu.”**

Maana yake: Atawapatia muyatakayo.

Hivyo waliondoka na kukimbilia kwenye pango ambapo walitafuta hifadhi. Baada ya hapo watu wao walitambua kuwa hawapo, na mfalme akaanza kuwatafuta, na pakasemwa kuwa walishindwa kuwapata, kwa kuwa Allah تعالى Amewaficha. Hivyo kutoweza kuwapata au kupata habari zao, kama vile Allah تعالى Alivyomficha Mtume Wake ﷺ pamoja na sahibu wake (Abu Bakr) Asw-Swiddiq رضي الله عنه, walipotafuta hifadhi katika pango la *Thawr*. Washirikina wa Kikureshi waliwatafuta, lakini hawakuwapata japokuwa walipita karibu yake kabisa. Pale Mtume ﷺ alipomuona Abubakr Asw-Swiddiq رضي الله عنه akiwa na wasiwasi, na akasema: “Ewe Mtume ﷺ! Lau mmoja wao atatizama miguuni mwake, atatuona.” Mtume ﷺ alimuambia:

« يَا أَبَا بَكْرٍ مَا ظَنَنْتُكَ بِأَنْتَيْنِ اللَّهُ نَالُهُمَا؟ »

*“Ewe Abubakr! Una dhana gani kwa wawili ambao Allah ni watatu wao?”<sup>1</sup>*

Na hakika Amesema Allah تعالى:

إِلَّا تَنْصُرُوهُ فَقَدْ نَصَرَهُ اللَّهُ إِذْ أَخْرَجَهُ الَّذِينَ كَفَرُوا ثَانِيَ اثْنَيْنِ إِذْ هُمَا فِي الْغَارِ إِذْ يَقُولُ لِصَاحِبِهِ لَا تَحْزَنْ إِنَّ اللَّهَ مَعَنَا ۗ فَأَنْزَلَ اللَّهُ سَكِينَتَهُ عَلَيْهِ وَأَيَّدَهُ بِجُنُودٍ لَّمْ تَرَوْهَا وَجَعَلَ كَلِمَةَ الَّذِينَ كَفَرُوا السُّفْلَى ۗ وَكَلِمَةُ اللَّهِ هِيَ الْعُلْيَا ۗ وَاللَّهُ عَزِيزٌ

حَكِيمٌ ﴿١٦﴾

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baariy 7:11.

***“Kama hamtamnusuru (Mtume), basi Allah Alimnusuru walipomtoa wale waliokufuru; alipokuwa (mmoja tu na mwenziwe) wa pili wake; walipokuwa wote wawili katika pango; alipomuambia sahibu yake: ‘Usihzunike, kwa yakini Allaah Yu pamoja nasi’. Allah Akamteremshia Utulivu Wake, na Akamnusuru kwa majeshi msiyoyaona, na Akafanya neno la waliokufuru kuwa chini; na Neno la Allaah ndilo la juu. Na Allah Ndiye Anayeshinda na Ndiye Mwenye Hekima.” (9:40)***

Kisa cha pango hili la ‘*Thawr*’ ni kitukufu, adhimu na cha ajabu kuliko cha watu wa pango - ‘*Aswahaabul Kahf*’.

✽ وَتَرَى السَّمْسَ إِذَا طَلَعَتْ تَزَاوَرُ عَنْ كَهْفِهِمْ ذَاتَ الْيَمِينِ وَإِذَا غَرَبَتْ تَقْرِضُهُمْ ذَاتَ الشِّمَالِ وَهُمْ فِي فَجْوَةٍ مِنْهُ ذَلِكَ مِنْ آيَاتِ اللَّهِ لَعَلَّ مَنْ يَهْدِي اللَّهُ فَهُوَ الْمُهْتَدِ وَمَنْ يُضِلِّ فَلَنْ يَجِدَ لَهُ وَلِيًّا مُرْشِدًا ﴿١٧﴾

***17. Na unaliona jua linapochomoza linainamia kuliani mwao kutoka hapo pangoni; na linapokuchwa linawakwepa kushotoni, na wao wamo katika uwazi wa pango. Hizo ni katika ishara za Allah. Ambaye Allah Anamuongoa basi huyo ni mwenye kuongoka. Na Anayemuacha kupotea basi hutampatia mlinzi wala mwongozi.***

### **Mahali pa Pango**

Na huu ni ushahidi ya kuwa mlango wa pango hili ulikuwa upande wa kaskazini, kwa sababu Allah تعالیٰ Anatuambia kuwa linapochomoza jua, mwangaza wake ulikuwa unaingia,

ذَاتَ الْيَمِينِ

***“Kuliani mwao.”*** Maana yake: Kivuli kilikuwa kikipungua kuelekea kuliani. Kama walivyosema Ibn ‘Abbaas, Sa’id bin Jubayr na Qataadah:

تَزَاوَرُ

***“Linainamia.”*** Maana yake: Kuegemea.<sup>1</sup> Kila wakati wa kuchomoza kwa jua

<sup>1</sup> Tabari 17:620.

kwenye mbingu, miale yake ilikuwa inainamika mpaka kusibaki chochote mahali hapo linapofika katikati. Hivyo, Allah تعالى Akasema:

وَإِذَا غَرَبَت تَّقَرُّظُهُمْ ذَاتَ الشَّمَالِ

**“Na linapokuchwa linawakwepa kushotoni.”**

Maana: Lilikuwa likiingia pangoni kushotoni mwa mlango wake, kumaanisha kutoka magharibi. Hii ni dalili kwa tunayosema, na ni wazi kwa kila mmoja anayedhania au kufikiria kuhusu jambo hili na ana elimu ya falaki na njia za jua, mwezi na nyota. Lau mlango wa pango ungekuwa umekabili mashariki, hakuna kitakachoringia wakati wa kuchwa kwa jua, na kama ingeelekea Qiblah (katika hali hii, kusini), hakuna mwangaza wowote ungeingia wakati wa kuchomoza na kuchwa kwa jua, na vivuli havingeinamia kuliani wala kushotoni. Ikiwa ingeelekea magharibi, hakuna cha kuingia wakati wa kuchomoza jua, mpaka jua lipite katikati (*zawaa*), na ingebaki hadi kuchwa kwake. Hii inaunga mkono tuliyoyasema, na Allah تعالى Ndiye Mwenye Kuhimidiwa.

Ibn ‘Abbaas, Mujaahid na Qatadah wamesema kuwa, “*Linawakwepa*”, Maana: linawang’aria kisha kuwaacha.<sup>1</sup> Allah تعالى Ametuambia hayo, na Anatutaka tufahamu na kuzingatia maana yake, lakini hakutuambia sehemu iliyokuwa pango hilo (lipo nchi gani katika hii dunia). Kwa sababu hakuna faida kwetu kujua hilo na wala hakuna malengo ya kisheria nyuma yake. Lau kama kungekuwa na maslahi ya kiroho au kidini ambayo yangepatikana kwa kujua kwetu hilo, Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ wangetufundisha kuhusu hilo, kama alivyosema Mtume ﷺ:

«مَا تَرَكْتُ شَيْئًا يُقَرِّبُكُمْ إِلَى الْجَنَّةِ وَيُبَاعِدُكُمْ مِنَ النَّارِ إِلَّا وَقَدْ أُغْلَمْتُكُمْ بِهِ»

*“Sikuacha kitu chochote kinachowakurubisha nyinyi na Pepo na kuwaweka mbali na Moto ila nimewafundisha.”<sup>2</sup>*

Allah تعالى Ametujulisha sifa zake, lakini Hakutujulisha mahali pa pango hilo. Akasema:

• وَتَرَى الشَّمْسَ إِذَا طَلَعَتْ تَزَوُّرًا عَنْ كَهْفِهِمْ

**“Na unaliona jua linapochomoza linainamia kutoka hapo pangoni”.**

<sup>1</sup> Tabari 17:621, 622.

<sup>2</sup> ‘Abdur-Razzaaq 11:125.



Maalik amesema aliyopokea kutoka kwa Zayd bin Aslam, "Kuegemea".

ذَاتَ الْيَمِينِ وَإِذَا عَزَبْتَ تُقْرِضُهُمْ ذَاتَ الشِّمَالِ وَهُمْ فِي فَجْوَةٍ مِنْهُ<sup>٤</sup>

***"Kuliani mwao, na linapokuchwa linawakwepa kushotoni, na wao wamo katika uwazi wa pango."***

Maana yake: Jua lilikuwa linaingia pangoni bila kuwagusa, kwa sababu lau lingewagusa lingewachoma miili na nguo zao. Hii ilikuwa ni rai ya Ibn 'Abbaas رضي الله عنه<sup>1</sup>.

ذَٰلِكَ مِنْ ءَايَاتِ اللَّهِ<sup>٥</sup>

***"Hizo ni katika ishara za Allah."***

Jinsi Alivyowaongoza kwenye pango mahali Alipowaweka katika uhai, na jua pamoja na upepo ilikuwa ikiingia pangoni ili ibaki miili yao. Kwa ajili hiyo Akasema Aliyetukuka:

ذَٰلِكَ مِنْ ءَايَاتِ اللَّهِ<sup>٥</sup>

***"Hizo ni katika ishara za Allah."***

Kisha Akasema:

مَنْ يَهْدِ اللَّهُ فَهُوَ الْمُهْتَدِ<sup>٦</sup>

***"Ambaye Allah Anamuongoa basi huyo ni mwenye kuongoka."***

Maana yake: Yeye Ndiye Aliyewaongoa vijana hawa katika njia ya uongofu kati ya watu wao, kwani yeyote Anayeongolewa na Allah تعالى, Ameongoka na Anayemuacha kupotea hatapata wa kumuongoza.

وَحَسْبُهُمْ أَيْقَاطًا وَهُمْ رُقُودٌ<sup>٧</sup> وَنُقَلِّبُهُمْ ذَاتَ الْيَمِينِ وَذَاتَ الشِّمَالِ<sup>٨</sup> وَكَلْبُهُمْ بَنِي سَيْدٍ ذِرَاعِيهِ

بِالْوَصِيدِ<sup>٩</sup> لَوِ اطَّلَعْتَ عَلَيْهِمْ لَوَلَّيْتَ مِنْهُمْ فِرَارًا وَلَمُلِئْتَ مِنْهُمْ رُغْبًا<sup>١٠</sup>

***18. Nawe utawadhania wamacho, na hali wamelala. Nasi Tunawageuza kulia na kushoto. Na mbwa wao amenyoosha miguu yake ya mbele kizingitini. Kama ungeliwatokea hapana shaka ungeligeuka kuwakimbia, nawe umejaa khofu.***

<sup>1</sup> At-Tabari 17:620.

### Kulala kwao Pangoni

Baadhi ya wanazuoni wametaja kuwa pale Allah تعالى Alipowafanya walale, vigubiko vyao vya macho havikufumba, ili wasichanguke. Lau macho yao yangukuwa wazi kwa hewa, hii ingekuwa bora kwa ajili ya kuhifadhika kwao. Kwa hiyo, Akasema Aliyetukuka:

وَتَحْسَبُهُمْ آيِقَاطًا وَهُمْ رُقُودٌ

**“Nawe utawadhania wamacho, na hali wamelala”.**

Imetajwa kuwa mbwa mwitu anapolala, anafumba jicho lake moja na kuliwacha jengine likiwa wazi, kisha anabadilisha (kwa kufumbua hili na kufumba jengine kwa kubadilisha) ilhali amelala. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَنُقَلِّبُهَا ذَاتَ الْيَمِينِ وَذَاتَ الشِّمَالِ

**“Nasi Tunawageza kulia na kushoto”.**

Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Lau kama hawangegeuka, ardhi ingewameza (ingewala).”<sup>1</sup> Kauli Yake:

وَكَلْبُهُمْ بَنَسِطٌ ذِرَاعِيهِ بِالْوَصِيدِ

**“Na mbwa wao amenyoosha miguu yake”.**

Amesema Ibn ‘Abbaas, Mujaahid, Said bin Jubayr na Qataadah: “Waswiid ina maana ya ukumbini.”<sup>2</sup> Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Mlangoni.”<sup>3</sup> Na pamesemwa: “Kwa mchanga (chini kwenye ardhi).” Na kauli iliyo sahihi ni kuwa maana yake ni kizingiti, nao ni mlango. Na miongoni mwao ni Kauli ya Allah تعالى:

إِنَّا عَلَّمِمْ مَوْصِدَةً

**“Hakika huo moto watafungiwa wawemo ndani yake.” (104:8),**

Maana yake: Ikiwa na tabaka, iliyofungwa.

<sup>1</sup> At-Tabari 17:620.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:624, 625.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:625.

Mbwa wao amejinyoosha chini mlangoni, kama ada ya mbwa. Amesema Ibn Jurayj: "Alikuwa akilinda mlango kwa ajili yao."<sup>1</sup> Ilikuwa ni maumbile yake kujinyoosha mlangoni pao kama kwamba anawalinda. Alikuwa amekaa nje ya mlango, kwa sababu Malaika hawaingii nyumba ambayo ina mbwa, kama ilivyopokewa katika Hadithi Sahihi, wala katika nyumba yenye picha, kwa mwenye janaba na kafiri, kama ilivyopokewa katika Hadithi Hasan.<sup>2</sup>

Baraka waliyotunukiwa ikamjumuisha na mbwa wao pia, hivyo ule usingizi uliowakuta ulimkuta na yeye pia. Hii ndio faida ya kusuhubiana na wateule na watu wema, na hivyo mbwa huyu akapata umaarufu, kujulikana na hadhi. Hakika imesemekana kuwa alikuwa mbwa wa kuwinda wa mmoja wa watu wa pangoni, na hii ndio rai iliyo sawa na kuafiki. Na panasemwa: Ni mbwa wa mpishi wa mfalme, aliyeafikiana nao katika Dini, akamchukua mbwa wake. Na Allah تعالى Anajua zaidi. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

لَوْ أَطَّلَعْتَ عَلَيْهِمْ لَوَلَّيْتَ مِنْهُمْ فِرَارًا وَكَلَمْتَهُمْ مِنْهُمْ رُعْبًا ﴿١٤﴾

***"Kama ungeliwatokea hapana shaka ungeligeuka kuwakimbia, nawe umejaa khofu."***

Maana yake: Allah تعالى Aliwafanya waonekane wenye kuogopesha, ili iwe hakuna anayeweza kuwatizama bila ya kuingiwa na khofu, kwa sababu ya kupatiwa sura ya kutisha.

Hii ilikuwa hivyo ili asikaribie yeyote wala kuwagusa mpaka wakati uliopangiwa ufike, wakati ambapo usingizi wao utamalizika kama Alivyopenda Allah تعالى, kwa sababu katika hilo pana hekima, dalili ya wazi, hoja thabiti na rehema pana na kubwa.

\* \* \*

<sup>1</sup> At-Tabari 17:625.

<sup>2</sup> Abu Daawuud 2:192-193.

وَكَذَلِكَ بَعَثْنَاهُمْ لِيَتَسَاءَلُوا بَيْنَهُمْ ۚ قَالَ قَائِلٌ مِّنْهُمْ  
 كَمْ لَبِثْتُمْ ۗ قَالُوا لَبِثْنَا يَوْمًا أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ ۗ قَالُوا رَبُّكُمْ  
 أَعْلَمُ بِمَا لَبِثْتُمْ فَابْعَثُوا أَحَدَكُمْ بِوَرِقِكُمْ هَذِهِ إِلَى  
 الْمَدِينَةِ فَلْيَنْظُرْ أَيُّهَا أَزْكَى طَعَامًا فَلْيَأْتِكُمْ بِرِزْقٍ مِّنْهُ  
 وَلْيَتَلَطَّفْ وَلَا يُشْعِرَنَّ بِكُمْ أَحَدًا ﴿١٩﴾ إِنَّهُمْ إِنْ يَظْهَرُوا  
 عَلَيْكُمْ يَرْجُمُوكُمْ أَوْ يُعِيدُوكُمْ فِي مِلَّتِهِمْ وَلَنْ تُفْلِحُوا إِذَا  
 أَبَدًا ﴿٢٠﴾ وَكَذَلِكَ أَعْرَضْنَا عَنْهُمْ لِيَعْلَمُوا أَنَّهُ وَعد  
 اللَّهِ حَقٌّ وَأَنَّ السَّاعَةَ لَا رَيْبَ فِيهَا إِذْ يَتَنَزَّعُونَ بَيْنَهُمْ  
 أَمْرَهُمْ ۗ فَقَالُوا ابْنُوا عَلَيْهِم بُنْيَانًا ۗ رَبُّهُمْ أَعْلَمُ بِهِمْ ۗ قَالَ  
 الَّذِينَ غَلَبُوا عَلَىٰ أَمْرِهِمْ لَنَتَّخِذَنَّ عَلَيْهِم مَّسْجِدًا  
 ﴿٢١﴾ سَيَقُولُونَ لَوْلَا رَبُّنَا كَلَّمَهُمْ وَيَقُولُونَ خَمْسَةٌ  
 سَادِسُهُمْ كَلِّمَهُم بِآلِغَيْبٍ ۗ وَيَقُولُونَ سَبْعَةٌ وَنَابِئُهُمْ  
 كَلِّمَهُمْ ۗ قُلْ رَبِّي أَعْلَمُ بِعَدَّتِهِمْ مَّا يَعْلَمُهُمْ إِلَّا قَلِيلٌ ۗ فَلَا  
 تُمَارِ فِيهِمْ إِلَّا مِرَاءً ظَهَرَ وَلَا تَشْهَدَ فِيهِمْ مِّنْهُمْ أَحَدًا  
 ﴿٢٢﴾ وَلَا تَقُولَنَّ لِشَايٍ إِنِّي فَاعِلٌ ذَٰلِكَ غَدًا ﴿٢٣﴾ إِلَّا  
 أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ ۗ وَادْكُرْ رَبَّكَ إِذَا نَسِيتَ وَقُلْ عَسَىٰ أَنْ  
 يَهْدِيَنِّي رَبِّي لِأَقْرَبٍ مِّنْ هَٰذَا رَشْدًا ﴿٢٤﴾

وَكَذَلِكَ بَعَثْنَاهُمْ لِيَتَسَاءَلُوا بَيْنَهُمْ ۚ قَالَ قَائِلٌ مِّنْهُمْ  
 كَمْ لَبِثْتُمْ ۗ قَالُوا لَبِثْنَا يَوْمًا أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ ۗ قَالُوا رَبُّكُمْ  
 أَعْلَمُ بِمَا لَبِثْتُمْ فَابْعَثُوا أَحَدَكُمْ  
 بِوَرِقِكُمْ هَذِهِ إِلَى الْمَدِينَةِ فَلْيَنْظُرْ  
 أَيُّهَا أَزْكَى طَعَامًا فَلْيَأْتِكُمْ بِرِزْقٍ مِّنْهُ  
 وَلْيَتَلَطَّفْ وَلَا يُشْعِرَنَّ بِكُمْ أَحَدًا  
 ﴿١٩﴾ إِنَّهُمْ إِنْ يَظْهَرُوا  
 عَلَيْكُمْ يَرْجُمُوكُمْ أَوْ يُعِيدُوكُمْ فِي مِلَّتِهِمْ  
 وَلَنْ تُفْلِحُوا إِذَا أَبَدًا ﴿٢٠﴾

19. Na kwa namna hii  
 Tuliwainua usingizini wapate  
 kuulizana wao kwa wao.  
 Alisema msemaji katika  
 wao: Mmekaa muda gani?  
 Wakasema: Tumekaa siku  
 moja au sehemu ya siku.  
 Wakasema: Mola Wenu  
 Mlezi Anajua zaidi muda  
 mliokaa. Hebu mtumeni  
 mmoja wenu na hizi fedha  
 zenu ende mjini, akatazame

chakula chake kipi kilicho bora kabisa akuleteeni cha kukila. Naye afanye mambo hayo kwa busara, wala asikutajeni kabisa kwa yeyote.

20. Kwani wao wakikutambueni watakupigeni mawe, au watakurudisheni katika dini yao; na hapo hamtafanikiwa kabisa!

### **Kuamka Kwao na Kumtuma Mmoja wao kwenda Kununua Chakula**

Allah تعالى Anasema: “Kama Tulivyowapatia usingizi, Tuliwafufua pamoja na miili yao, nywele na ngozi zikiwa kama zilivyokuwa wala hakuna kilichopungua katika hali na maumbile yao.” Hii ilikuwa baada ya miaka mia tatu na tisa (309). Na hivyo waliulizana:

كَمْ لَبِئْتُمْ

**“Mmekaa muda gani?”**

Maana yake: Mmelala muda gani?

قَالُوا لَبِئْنَا يَوْمًا أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ

**“Wakasema: Tumekaa siku moja au sehemu ya siku.”**

Kwa sababu kuingia kwao pangoni kulikuwa mwanzo wa asubuhi na waliinuka mwisho wa siku, hivyo walipatiliza kwa kusema:

أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ قَالُوا رَبُّكُمْ أَعْلَمُ بِمَا لَبِئْتُمْ

**“Au sehemu ya siku. Wakasema: Mola wenu Mlezi Anajua zaidi muda mliokaa.”**

Maana yake: Allah تعالى Anajua zaidi kuhusu hali yenu. Inaonesha kuwa hawakuwa na yakini kuhusu ule muda waliolala, na Allah تعالى Anajua zaidi. Baada ya hapo walijishughulisha kwa mambo muhimu zaidi, kama mahitaji yao ya chakula na kinywaji, hivyo wakasema:

فَاتَّبَعُوا أَحَدَكُمْ بِوَرِقِكُمْ

**“Hebu mtumeni mmoja wenu na hizi fedha zenu.”**

Walikuwa wamekuja na baadhi ya *Dirham* (fedha) kutoka majumbani mwao, kununua kila walichohitajia, na walikuwa wametoa baadhi yake sadaka na kubakisha baadhi. Hivyo wakasema:

فَاتَّبَعُوا أَحَدَكُمْ بِوَرِقِكُمْ هَذِهِ إِلَى الْمَدِينَةِ

**“Hebu mtumeni mmoja wenu na hizi fedha zenu ende mjini.”**

Maana yake: Mji wao, waliotoka. Na *Alif* na *Laam* inahusisha mji maalumu. Na huko,

فَلْيَنْظُرْ إِلَيْهَا أَزْجَىٰ طَعَامًا

**“Akatazame chakula kilicho bora kabisa.”**

Maana yake: Chakula kilicho kizuri kabisa, kama ilivyo katika Kauli Yake:

وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ مَا زَكَا مِنكُمْ مِّنْ أَحَدٍ أَبَدًا

**“Na lau si Fadhila za Allah na Rehema Yake juu yenu asingali-takasika miongoni mwenu hata mmoja.” (24:21).**

Na Kauli Yake Allah تعالى،

قَدْ أَفْلَحَ مَن تَزَكَّىٰ ﴿٨٧﴾

**“Hakika amekwisha faulu aliyejitakasa.” (87:14)**

Na kutoka katika mzizi wa neno hilo “masdar” hiyo hiyo linapatikana neno *Zaka*, inayofanya mali ya mtu kuwa nzuri na kuitakasa. Na Kauli Yake:

وَلْيَتَلَطَّفْ

**“Naye awe mwangalifu (afanye mambo kwa busara).”**

Maana yake: Anapotoka kwenda kununua chakula na kurudi. Walikuwa wanamuambia ajifiche kwa upeo anaoweza. Sababu ya kufanya hivyo ni kuwa,

وَلَا يُشْعِرَنَّ بِكُمْ أَحَدًا ﴿٨٨﴾ إِنَّهُمْ إِن يَظْهَرُوا عَلَيْكُمْ يَرْجُمُوكُمْ

**“Wala asikutajeni kabisa kwa yeyote. Kwani wao wakikutambueni watakupigeni mawe.”**

Maana yake: Wakijua mlipo.

يَرْجُمُوكُمْ أَوْ يُعِيدُوكُمْ فِي مِلَّتِهِمْ

**“Watakupigeni mawe, au watakurudisheni katika dini yao.”**

Walikuwa wanamaanisha watu wa *Decianus*. Walikuwa wana khofu naye kuwa anaweza kujua walipo na hivyo kuwaadhibu kwa adhabu za aina zote mpaka

awafanye warudi katika dini yao ya zamani, au wafe. Kwani lau watakubali kurudi katika dini yao ya zamani, hawatafaulu hapa duniani na Kesho Akhera. Kwa hiyo wakasema:

وَلَنْ تَفْلِحُوا إِذَا أَبَدًا ﴿٢١﴾

**“Na hapo hamtafanikiwa kabisa!”**

وَكَذَلِكَ أَعْتَرْنَا عَلَيْهِمْ لِيَعْلَمُوا أَنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ وَأَنَّ السَّاعَةَ لَا رَيْبَ فِيهَا إِذْ يَتَنَزَّعُونَ بَيْنَهُمْ أَمْرَهُمْ فَقَالُوا ابْنُوا عَلَيْهِم بُنْيَانًا رَبُّهُمْ أَعْلَمُ بِهِمْ قَالَ الَّذِينَ غَلَبُوا عَلَىٰ أَمْرِهِمْ لَنَتَّخِذَنَّ عَلَيْهِم مَّسْجِدًا ﴿٢٢﴾

**21. Na namna hivi Tuliwajulisha kwa watu wapate kujua ya kwamba ahadi ya Allah ni ya kweli, na kwamba Saa haina shaka. Walipokuwa wakigombania jambo lao wao kwa wao walisema: Jengeni jengo juu yao. Mola wao Mlezi Anawajua vyema. Wakasema walioshinda katika shauri yao: Bila ya shaka tutawajengea Msikiti juu yao.**

**Vipi Watu wa Mji Walipowajua na Kujenga Ukumbusho juu ya Pango**

Anasema Aliyetukuka:

وَكَذَلِكَ أَعْتَرْنَا عَلَيْهِمْ

**“Na namna hivi Tuliwajulisha kwa watu.”**

Maana yake: Tulifanya watu kuwajua walipo.

لِيَعْلَمُوا أَنَّ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ وَأَنَّ السَّاعَةَ لَا رَيْبَ فِيهَا

**“Wapate kujua ya kwamba ahadi ya Allah ni ya kweli, na kwamba Saa haina shaka”.**

Wanazuoni wengi waliotangulia (*Salaḥ*) wametaja kuwa watu wa wakati huo hawakuwa ni wenye kuamini ufufuo (kufufuliwa watu baada ya kufa). 'Ikrimah amesema: “Kulikuwa na kikundi miongoni mwao waliokuwa wakisema kuwa

roho zitafufuliwa lakini sio miili, hivyo Allah تعالی Akawafufua watu wa pango kama ishara na dalili ya ufufuo.”<sup>1</sup>

Wametaja kuwa walipokuwa wanataka kumtuma mtu wao mmoja mjini kuwanunulia chakula, alijibadilisha na kutembea kwa njia nyengine mpaka akafika mjini, ambao wamesema ulikuwa ukiitwa *Daqsus*. Alikuwa anafikiria kuwa sio muda mrefu kuanzia waondoke, lakini hakika ni kuwa karne baada ya karne zimepita, na vizazi baada ya vizazi, na Ummah baada ya Ummah umepita, na nchi yenyewe na watu wake wamebadilika. Hakuona alama yoyote ya mahali hapo ambayo alikuwa anaifahamu, wala hakumtambua yeyote miongoni mwa watu wake, si mabwana wao wala watu wa kawaida.

Alianza kujihisi kama amechanganyikiwa na kujisemeza, “Huenda nikawa nimeshikwa na wazimu au nimechanganyikiwa au ninaota”. Kisha akasema: “Wallahi, sina lolote katika hayo, ninayoyajua kwa niliyoyaona usiku wa jana ni tofauti na haya”. Kisha akaenda kwa mmoja wa watu aliyekuwa akiuza chakula, akampa pesa alizokuwa nazo na kumtaka amuuzie chakula.

Mtu yule alipoiona ile fedha hakuitambua wala chapa yake hakuitambua, hivyo akampa jirani yake na wote wakaanza kuipitisha kwa wenziwao, huku wakisema: “Huenda ikawa mtu huyu amepata hazina”. Walimuuliza yeye ni nani na amepata wapi pesa hiyo.

Je, amepata hazina? Yeye ni nani? Akasema: “Mimi ni mtu wa mji huu, nilikuwa naishi hapa jana na *Decianus* ndiye aliyekuwa mfalme”. Walimshutumu kuwa na wazimu na wakampeleka kwa liwali ambaye alianza kumuuliza kuhusu hali yenyewe, naye akamueleza. Akawa amechanganyikiwa kuhusu hali yenyewe. Alipowaelezea kuhusu jambo hilo, mfalme na watu wa mji – walikwenda naye pangoni, hapo akawaambia, “Niwacheni niingie mwanzo ili niwajulishe sahibu zangu”.

Inasemekana kuwa watu hawakujua alivyoingia na Mwenyezi Mungu Aliwaficha kisa chao, na watu pia hawakujua kuhusu kisa chao. Pia yasemekana kuwa waliingia pangoni na kuwaona, na kuwa mfalme aliwasalimia na kuwakumbatia. Mfalme alikuwa ni Muislamu, akiitwa *Tedosis*. Walifurahi

---

<sup>1</sup> Taarikh at-Tabari 2:9.



kumuona na kuzungumza naye, kisha walimuaga na kurudi tena kulala, na hapo Allah تعالى Akawafisha. Na Allah تعالى Anajua zaidi<sup>1</sup>.

Na Kauli Yake:

وَكَذَلِكَ أَعْتَرْنَا عَلَيْهِمْ

**“Na namna hivi Tuliwajulisha kwa watu.”**

Maana yake: Kama Tulivyowafanya walale, Tuliwaamsha kimwili na miili yao ikiwa barabara, na kukifanya kisa chao kujulikana na watu wa zama zao.

لِيَعْلَمُوا أَنَّهُ وَعْدَ اللَّهِ حَقٌّ وَأَنَّ السَّاعَةَ لَا رَيْبَ فِيهَا إِذْ يَتَنَزَّعُونَ بَيْنَهُمْ أَمْرُهُمْ

**“Wapate kujua ya kwamba ahadi ya Allah ni ya kweli, na kwamba Saa haina shaka. Walipokuwa wakigombania jambo lao wao kwa wao.”**

Maana yake: Kuhusu Kiyama. Baadhi yao walikuwa wanaamini na wengine kukataa, hivyo Allah تعالى Aliwadhihirisha watu wa pangoni wawe ni dalili ima kwao au dhidi yao. Wakasema:

فَقَالُوا أَبْنَاؤُا عَلَيْهِمْ بُنِينًا رَبُّهُمْ أَعْلَمُ بِهِمْ

**“Jengeni jengo juu yao”, Mola wao Mlezi Anawajua vyema.**

Maana yake: Uzibeni mlango wa pango lao juu yao, na waacheni kama walivyo.

قَالَ الَّذِينَ غَلَبُوا عَلَىٰ أَمْرِهِمْ لَنَتَّخِذَنَّ عَلَيْهِم مَّسْجِدًا ﴿٢٠﴾

**“Wakasema walioshinda katika shauri lao: Bila ya shaka tutawajengea Msikiti juu yao”.**

Wale waliosema haya, ni watu wenye kusikilizwa na ushawishi, lakini walikuwa ni watu wazuri au wabaya? Yapo majadiliano kuhusu nukta hii, kwani Mtume ﷺ amesema:

<sup>1</sup> Taarikh at-Tabari 2:9.

«لَعَنَ اللَّهُ الْيَهُودَ وَالنَّصَارَى اتَّخَذُوا قُبُورَ أَنْبِيَائِهِمْ وَصَالِحِيهِمْ مَسَاجِدَ»

*“Allah Awalaani Mayahudi na Manasara waliochukua makaburi ya Manabii na wema wao kuwa Misikiti”<sup>1</sup>.*

Akionya dhidi ya walioyafanya. Na hakika tumepokea kutoka kwa Amiri wa Waumini, ‘Umar bin Al-Khattwab رضي الله عنه alipolipata kaburi la *Daniel* katika zama zake huko Iraq aliamuru habari hiyo isitolewe (ifichwe) kwa watu. Pia aliagiza kuwa yale maandishi yaliyotaja kuhusu mambo mbali mbali ya kivita na kadhalika walioyafanya yafukiwe.<sup>2</sup>

سَيَقُولُونَ ثَلَاثَةٌ رَابِعُهُمْ كَلْبُهُمْ وَيَقُولُونَ خَمْسَةٌ سَادِسُهُمْ كَلْبُهُمْ رَجْمًا بِالْغَيْبِ  
وَيَقُولُونَ سَبْعَةٌ وَثَامِنُهُمْ كَلْبُهُمْ قُل رَّبِّي أَعْلَمُ بِعَدَّتِهِمْ مَا يَعْلَمُهُمْ إِلَّا قَلِيلٌ فَلَا تُمَارِ  
فِيهِمْ إِلَّا مِرَاءً ظَهْرًا وَلَا تَسْتَفْتِ فِيهِمْ مِنْهُمْ أَحَدًا ﴿١٧﴾

**22. Watasema: Walikuwa watatu, wa nne wao ni mbwa wao. Na wanasema: Walikuwa watano, wa sita wao ni mbwa wao. Wanavurumisha ovyo. Na wanasema: Walikuwa saba, na wa nane wao ni mbwa wao. Sema: Mola wangu Mlezi ndiye anayejua sawa sawa hisabu yao. Hawawajui ila wachache tu. Basi usibishane juu yao ila kwa mabishano ya juu juu tu hivi. Wala usiulize khabari zao kwa yeyote yule.**

## Idadi Yao

Allah تعالی Anatupasha habari juu ya tofauti za watu katika idadi ya watu wa pangoni. Aya inataja rai tatu, kutoa hoja kuwa hakukuwa na rai ya nne kuhusu hilo. Allah تعالی Anaashiria kuwa rai mbili za mwanzo ni dhaifu, hivyo Akasema:

رَجْمًا بِالْغَيْبِ

**“Wanavurumisha ovyo.”**

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baariy 1:634.

<sup>2</sup> Al-Bidaayah wan-Nihaayah 7:88.

Maana yake: Wamezungumza bila elimu wala ujuzi, kama anayelenga pasipojulikana – ni muhali kwake kulenga, na anapofanikiwa, haikuwa ndio lengo wala matlaba yake. Kisha Allah تعالى Anazungumzia rai ya tatu na Akanyamaza au Akayakinisha na Kupitisha kwa Kusema:

وَأَنذَرْتَهُمْ كَلِمَةً

**“Na wa nane wao ni mbwa wao.”**

Kuashiria kuwa hii ndiyo sahihi na hilo ndilo lililotokea. Na Kauli Yake:

قُلْ رَبِّيَ أَعْلَمُ بِعِبَادَتِهِمْ

**“Sema: Mola wangu Mlezi Ndiye Anayejua sawa sawa hisabu yao.”**

Kuelekezwa kuwa lililo bora la kufanya katika mambo kama haya ni kuirudisha elimu kwa Allah تعالى, kwa sababu hakuna haja kujadili mambo haya bila elimu. Tunapopatiwa elimu ya jambo, tunaweza kulizungumzia, kinyume na hivyo tunatakiwa tusimame tuliposimama (tujiepushe nalo). Na Kauli Yake:

مَا يَعْلَمُهُمْ إِلَّا قَلِيلٌ

**“Hawawajui ila wachache tu.”**

Maana yake: Miongoni mwa wanadamu. Qataadah amepokea kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Mimi ni miongoni mwa wachache niliotajwa katika Aya hii; walikuwa saba.”<sup>1</sup> Hivyo hivyo amepokea Ibn Jurayj kutoka kwa ‘Atwaa’ Al-Khuraasaani aliyekuwa akisema: “Mimi ni miongoni mwa wale waliohusishwa katika Aya hii”, na alikuwa akisema: “Idadi yao ilikuwa saba.”<sup>1</sup> Na amepokea Ibn Jariir رحمه الله تعالى kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema:

مَا يَعْلَمُهُمْ إِلَّا قَلِيلٌ

**“Hawawajui ila wachache tu.”**

“Mimi ni miongoni mwa wale wachache, na idadi yao ilikuwa ni saba”. Isnadi za riwaya zote hizi zilizopokewa kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما zinazosema

<sup>1</sup> At-Tabari 17:642.

kuwa walikuwa saba, ni sahihi, na hii ni kulingana na tuliyoyasema hapo awali. Amesema Aliyetukuka:

فَلَا تُمَارِ فِيهِمْ إِلَّا مِرَاءً ظَهْرًا

**“Basi usibishane juu yao ila kwa mabishano ya juu juu tu hivi.”**

Maana yake: Kwa usahali, upole na ulaini, kwani hakuna faida kubwa utakayopata katika kujua hilo. Pia,

وَلَا تَسْتَفْتِ فِيهِمْ مِنْهُمْ أَحَدًا

**“Wala usiulize khabari zao kwa yeyote yule.”**

Maana yake: Wao hawana elimu yoyote kuhusu hilo isipokuwa kwa wanayotunga na kuvurumisha ovyo, bila kuwa na dalili kutoka kwenye chimbuko thabiti na lisilokosea. Hakika ni kuwa Allah تعالى Amekujuzi wewe, ewe Muhammad ﷺ, kwa ukweli usio na shaka wala kuchanganyikiwa ndani yake. Na hiyo ni lazima itangulizwe na kupatiwa kipaumbele juu ya vitabu vyote vya mbeleni (awali).

Na Kauli yake Allah تعالى:

وَلَا تَقُولَنَّ لِشَايٍ إِنِّي فَاعِلٌ ذَٰلِكَ غَدًا ۚ ﴿١٧﴾ إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ ۗ وَأَذْكُرَنَّ رَبَّكَ إِذَا

نَسِيتَ وَقُلْ عَسَىٰ أَنْ يَهْدِيَنِّي رَبِّي لِأَقْرَبَ مِنْ هَٰذَا رَشْدًا ﴿١٨﴾

**23. Wala usiseme kamwe kwa jambo lolote lile: Hakika nitalifanya hilo kesho.**

**24. Isipokuwa Allah Akipenda. Na mkumbuke Mola wako Mlezi pale unaposahau, na sema: Huenda Mola wangu Mlezi Ataniongoa kwenye uongozi ulio karibu zaidi kuliko huu.**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:642.

### Sema *Insha'Allah* Unapoazimia Kufanya Jambo katika Mustakbali

Hapa Allah تعالى, Anatoa muongozo kwa Mtume Wake kwa adabu sahihi na ya sawa pale anapotaka kufanya jambo katika mustakbali; alirudishe katika Utashi wa Allah تعالى. Yeye Ndiye Mjuzi wa ghaibu, Anayejua yaliokuwa na yatakayokua na yasiokuwa na jinsi itakavyokuwa lau itakuwa. Imenukuliwa katika Sahihi mbili kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema, Mtume ﷺ amesema:

«قَالَ سُلَيْمَانُ بْنُ دَاوُدَ عَلَيْهِمَا السَّلَامُ: لَأُطَوِّقَنَّ اللَّيْلَةَ عَلَى سَبْعِينَ امْرَأَةً - وَفِي رِوَايَةٍ: تَسْعِينَ امْرَأَةً، وَفِي رِوَايَةٍ: مِائَةَ امْرَأَةٍ - تَلِدُ كُلُّ امْرَأَةٍ مِنْهُنَّ عَلَامًا يُقَاتِلُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ، فَيَقِيلُ لَهُ - وَفِي رِوَايَةٍ قَالَ لَهُ الْمَلَكُ: - قُلْ إِنْ شَاءَ اللَّهُ، فَلَمْ يَقُلْ، فَطَافَ بِهِمْ فَلَمْ تَلِدْ مِنْهُنَّ إِلَّا امْرَأَةً وَاحِدَةً بَضْفَ إِنْسَانٍ، فَقَالَ رَسُولُ اللَّهِ ﷺ: وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ، لَوْ قَالَ إِنْ شَاءَ اللَّهُ لَمْ يَخْتَفِ، وَكَانَ دَرَكًا لِحَاجَتِيهِ» وَفِي رِوَايَةٍ: «وَلَقَاتَلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فُرْسَانًا أَجْمَعُونَ»

*“Sulaymaan bin Daawuud alisema: ‘Usiku wa leo nitawapitia wake wangu wote sabiini (kulingana na riwaya nyengine wake tisiini, na katika riwaya nyengine wake mia) kila mmoja atazaa kijana atakayepigana katika njia ya Allaah’. Akaambiwa – na katika riwaya nyengine, Malaika alimuambia: ‘Sema: Insha’Allah’, lakini hakusema. Aliwaendea wake zake wote lakini hakuna aliyezaa ila mke wake mmoja aliyezaa mtoto ambae hakuwa na viungo vyake vingine. Mtume ﷺ akasema: ‘Naapa kwa yule ambaye nafsi yangu iko Mikononi Mwake, lau angesema Insha’Allah, hangevunja kiapo chake, na hilo lingemsaidia kupata alichotaka.’ Kulingana na riwaya nyengine: ‘Wote wangepigana kama wapanda farasi katika njia ya Allah.’”<sup>1</sup>*

Na tumetangulia kutaja sababu ya kuteremshwa kwa Aya hii mwanzo wa Sura katika kauli ya Mtume ﷺ alipoulizwa kuhusu kisa cha watu wa Pangoni, alisema: “Nitawajibu kesho”. Hivyo, Wahyi ulichelewa kwa siku kumi na tano.<sup>2</sup>

<sup>1</sup> Fat’h Al-Baariy 6:41 na Muslim 3:1275.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:592.

Kwa vile tulieleza kwa kirefu mwanzo wa Sura, hapana haja kurudia tena hapa. Na Kauli Yake:

وَأَذْكُرُّ رَبِّكَ إِذَا نَسِيتَ

**“Na mkumbuke Mola wako Mlezi pale unaposahau”.**

Panasemwa: “Maana yake ni kuwa unaposahau kusema, *Insha’Allaah*, hivyo iseme pindi unapokumbuka.” Hii ni rai ya Abu Al-’Aaliyah na Al-Hasan Al-Baswriy<sup>1</sup>. Amepokea Hushaym kutoka kwa Al-A’ mash kutoka kwa Mujahid kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema yafuatayo kuhusu mtu anayekula kiapo: “Ni juu yake kusema, *Insha’Allaah* hata kama ni baada ya mwaka”. Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما alikuwa akiifasiri Aya hii:

وَأَذْكُرُّ رَبِّكَ إِذَا نَسِيتَ

**“Na mkumbuke Mola wako Mlezi unaposahau.”**

Kwa njia hii. Al-A’ mash aliulizwa, “Je, ulisikia haya kwa Mujaahid?” Akasema: “Layth bin Abi Saliim ameniambia”<sup>2</sup>. Maana ya rai ya Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما, ni kuwa mtu anaweza kusema, “*Insha’Allah*”, hata baada ya mwaka, ni pale anaposahau kusema anapoapa au anapozungumza, na akakumbuka baadaye, hata kama baada ya mwaka, Sunna ni aseme, ili awe katika kuifuata Sunnah ya kusema, “*Insha’Allah*”, hata ikiwa hiyo ni baada ya kuvunja kiapo chake. Hii pia ndiyo iliokuwa rai ya Ibn Jariir رحمه الله تعالى<sup>3</sup>, lakini akasema kuwa kufanya hivyo hakulipi kuvunja yamini na kuondoa kafara (yaani kafara haihitajiki tena, hapana kafara inahitajika kutekelezwa). Aliyosema Ibn Jariir رحمه الله تعالى ni sahihi na ni sawa zaidi kuyafahamu maneno ya Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kwa njia hii. Na Allah تعالى Anajua zaidi.

Na imepokewa na At-Tabaraaniy kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema yafuatayo kuhusu Kauli Yake Aliyetukuka:

وَلَا تَقُولَنَّ لِشَيْءٍ إِنِّي فَاعِلٌ ذَٰلِكَ غَدًا ﴿١٨﴾ إِلَّا أَن يَشَاءَ اللَّهُ ۗ وَأَذْكُرُّ رَبِّكَ إِذَا

**“Wala usiseme kamwe kwa jambo lolote lile: Hakika nitalifanya hilo kesho - Isipokuwa Allah Akipenda. Na mkumbuke Mola wako Mlezi pale unaposahau”,**

<sup>1</sup> At-Tabari 17:645.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:645. Sanadi yake ina dosara.

<sup>3</sup> At-Tabari 17:646.

Inamaanisha kusema, "Insha'Allah"<sup>1</sup>. Na Kauli Yake:

وَقُلْ عَسَىٰ أَن يَهْدِيَنِي رَبِّي لِأَقْرَبَ مِن هَذَا رَشَدًا ﴿١٩﴾

***"Na sema: Huenda Mola wangu Mlezi Ataniongoa kwenye uongozi ulio karibu zaidi kuliko huo."***

Maana yake: Ukiulizwa (ewe Nabii) kuhusu jambo usilolijua, muombe Allah تعالیٰ kuhusu hilo, muelekee Yeye ili Akuongoe (Akuongoze) katika njia nyoofu katika hilo. Na Allah تعالیٰ Anajua zaidi

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Atw-Twabaraaniy katika Al-Awsatw 7:4545. Sanadi yake ni dhaifu.

وَلَبِثُوا فِي كَهْفِهِمْ ثَلَاثَ مِائَةٍ سِنِينَ وَازْدَادُوا تِسْعًا ﴿٢٥﴾  
 قُلِ اللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا لَبِثُوا لَهُ غَيْبُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ  
 أَبْصَرَ بِهِ وَأَسْمِعُ مَا لَهُمْ مِنْ دُونِهِ مِنْ وَلِيٍّ وَلَا يُشْرِكُ  
 فِي حُكْمِهِ أَحَدًا ﴿٢٦﴾ وَأَتْلُ مَا أُوحِيَ إِلَيْكَ مِنْ كِتَابِ  
 رَبِّكَ لَا مُبَدِّلَ لِكَلِمَاتِهِ وَلَنْ تَجِدَ مِنْ دُونِهِ مُلْتَحَدًا  
 ﴿٢٧﴾ وَأَصْبِرْ نَفْسَكَ مَعَ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ بِالْغَدْوَةِ  
 وَالْعَشِيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُ وَلَا تَعْدُ عَيْنَاكَ عَنْهُمْ تُرِيدُ زِينَةَ  
 الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَلَا تَطْعَمَنْ مَنْ أَعْفَلْنَا قَلْبَهُ عَنْ ذِكْرِنَا وَاتَّبَعَ  
 هَوَاهُ وَكَانَ أَمْرُهُ فُرُطًا ﴿٢٨﴾ وَقُلِ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكُمْ  
 فَمَنْ شَاءَ فَلْيُؤْمِنْ وَمَنْ شَاءَ فَلْيُكْفِرْ إِنَّا أَعْتَدْنَا  
 لِلظَّالِمِينَ نَارًا أَحَاطَ بِهِمْ سُرَادِقُهَا وَإِنْ يَسْتَغِيثُوا يُغَاثُوا  
 بِمَاءٍ كَالْمُهْلِ يَشْوِي الْوُجُوهَ بِئْسَ الشَّرَابُ وَسَاءَتْ  
 مُرْتَفَقًا ﴿٢٩﴾ إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ إِنَّا  
 لَا نُضِيعُ أَجْرَ مَنْ أَحْسَنَ عَمَلًا ﴿٣٠﴾ أُولَئِكَ هُمُ جَنَّاتُ  
 عَدْنٍ يَدْخِلُونَهَا يُخْرَجُونَ مِنْهَا فِيهَا مِنْ أَسَاوِرَ مِنْ  
 ذَهَبٍ وَيَلْبَسُونَ ثِيَابًا خُضْرًا مِنْ سُنْدُسٍ وَإِسْتَبْرَقٍ مُتَّكِنِينَ  
 فِيهَا عَلَى الْأَرَائِكِ نِعْمَ الثَّوَابُ وَحَسُنَتْ مُرْتَفَقًا ﴿٣١﴾

وَلَبِثُوا فِي كَهْفِهِمْ ثَلَاثَ مِائَةٍ  
 سِنِينَ وَازْدَادُوا تِسْعًا ﴿٢٥﴾ قُلِ  
 اللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا لَبِثُوا لَهُ غَيْبُ  
 السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ أَبْصَرَ بِهِ  
 وَأَسْمِعُ مَا لَهُمْ مِنْ دُونِهِ مِنْ وَلِيٍّ  
 وَلَا يُشْرِكُ فِي حُكْمِهِ أَحَدًا ﴿٢٦﴾

25. Na walikaa katika pango lao miaka mia tatu, na wakazidisha tisa.

26. Sema: Allah Anajua zaidi muda waliokaa. Ni Zake tu siri za mbingu na ardhi. Kuona kulioje na Kusikia Kwake! Hawana mlinzi isipokuwa Yeye, wala hamshirikishi yeyote katika hukumu Yake.

### Muda Waliokaa Pangoni

Hii ni habari kutoka kwa Allah تعالیٰ kwa Mtume Wake muda waliokaa pangoni watu wa pango, kuanzia wakati Alipowapatia

usingizi mpaka Alipowafufua na Kuwafanya watu wa zama hizo kuwakuta. Muda ni miaka mia tatu na tisa za mwandamo wa mwezi, ambazo ni miaka mia tatu kwa mahesabu ya miaka ya jua. Tofauti baina ya miaka mia moja kwa mahesabu ya mwandamo wa mwezi na miaka mia moja ya jua ni miaka



mitatu. Hiyo ndiyo sababu baada ya kutaja miaka mia tatu, Allah تعالى Akasema, “Na wakazidisha tisa”. Na Kauli Yake:

قُلِ اللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا لَبِثُوا<sup>ط</sup>

**“Sema: Allaah Anajua zaidi muda waliokaa.”**

Maana yake: Unapoulizwa kuhusu muda waliokaa, nawe huna elimu ya hilo na hujapata Wahyi kutoka kwa Allah تعالى kuhusu hilo, usiseme chochote. Bali sema mfano wa hivi:

اللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا لَبِثُوا<sup>ط</sup> لَهُ غَيْبُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ<sup>ط</sup>

**“Allah Anajua zaidi muda waliokaa. Ni Zake tu siri za mbingu na ardhi.”**

Maana yake: Hakuna mwenye kujua hayo ila Yeye, na yeyote miongoni mwa viumbe Vyake Anayemchagua Kumuambia. Tuliyoasema hapa ni rai ya wanazuoni wengi wa tafsiri, kama vile Mujaahid na wengineo miongoni mwa *Salaf* (waliotangulia) na wa baadae. Na amesema Qataadah katika Kauli Yake:

وَلَبِثُوا فِي كَهْفِهِمْ ثَلَاثَ مِائَةٍ سِنِينَ

**“Na walikaa katika pango lao miaka mia tatu.”**

Hii ni kauli ya waliopewa Kitabu, na Allah تعالى Akairudi (Akaikosoa) kwa Kauli Yake:

قُلِ اللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا لَبِثُوا<sup>ط</sup>

**“Sema: Allaah Anajua zaidi muda waliokaa.”**

Akasema: Na katika kisomo cha ‘Abdallah: “*Wa qaalu, wa Labithuu* – Na wakasema: Na walikaa,” Maana: Hivyo ndivyo wanavyosema watu<sup>1</sup>. Na hivyo ndivyo alivyosema Mutwarraf bin ‘Abdallah<sup>2</sup>. Hata hivyo, rai hii inayodaiwa na Qataadah inafaa itizamwe na kujadiliwa, kwa sababu pale watu wa Kitabu waliposema kuwa walikaa pangoni kwa miaka mia tatu, bila ya nyongeza au

<sup>1</sup> At-Tabari 17:647.

<sup>2</sup> At-Tabari 17:648.

ziada ya miaka tisa, walikuwa wanatumia mahesabu ya jua, na ikiwa Allah تعالى Alikuwa tu Akisimulia yale waliyosema, Hangesema,

وَأَزْدًا دُونَ تِسْعًا ﴿١٧﴾

**“Na wakazidisha tisa”.**

Maana dhahiri ya Aya hii ni kuwa Allah تعالى Anatupa habari ya uhakika sio hekaya kuwahusu. Na huu ni uchaguzi na rai ya Ibn Jariir رحمه الله تعالى. Na Allah تعالى Anajua zaidi. Na Kauli Yake:

أَبْصِرْ بِهِ وَأَسْمِعْ

**“Kuona kulioje na Kusikia Kwake”.**

Maana yake: Anawaona na Kuwasikia. Ibn Jariir رحمه الله تعالى amesema: “Lugha iliyotumika fasaha kabisa katika kusifu.”<sup>1</sup>

Kama kwamba panasemwa: “Ni kiasi gani Anachoona na Kusikia.”<sup>2</sup> Ibara hii inaweza kueleweka: Ni kiasi gani ambacho Allah تعالى Anaona kila kitu kilicho kuwepo na ni kiasi gani Allah تعالى Anasikia kila kitu cha kusikiwa, kwani hakuna kinachofichikana Naye!. Kisha imepokewa kutoka kwa Qataadah katika Kauli Yake:

أَبْصِرْ بِهِ وَأَسْمِعْ

**“Kuona kulioje na Kusikia Kwake”.**

Maana yake: Hakuna anayesikia wala kuona zaidi ya Allah تعالى<sup>3</sup>. Na Kauli Yake:

مَا لَهُمْ مِنْ دُونِهِ مِنْ وَلِيٍّ وَلَا يُشْرِكُ فِي حُكْمِهِ أَحَدًا ﴿١٨﴾

**“Hawana mlinzi isipokuwa Yeye, wala hamshirikishi yeyote katika Hukumu Yake.”**

Maana yake: Yeye Aliyetukuka, Ndiye Mwenye Nguvu ya Kuumba na Kuamrisha, Ambaye Hukumu Yake Haiwezi kupinduliwa; Hana waziri wala mshauri, wala msaidizi, wala mshirika, Ametukuka na Mtakatifu.

<sup>1</sup> At-Twabari 17:650.

<sup>2</sup> At-Twabari 17:650.

<sup>3</sup> At-Twabari 17:650.

وَأَتْلُ مَا أُوحِيَ إِلَيْكَ مِنْ كِتَابِ رَبِّكَ ۗ لَا مُبَدِّلَ لِكَلِمَاتِهِ وَلَنْ تَجِدَ مِنْ دُونِهِ  
 مُلتَحَدًا ﴿٢٧﴾ وَأَصْبِرْ نَفْسَكَ مَعَ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ بِالْغَدَاةِ وَالْعَشِيِّ يُرِيدُونَ  
 وَجْهَهُ ۗ وَلَا تَعْدُ عَيْنَاكَ عَنْهُمْ تُرِيدُ زِينَةَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۗ وَلَا تُطِعْ مَنْ أَغْفَلْنَا قَلْبَهُ عَنِ  
 ذِكْرِنَا وَاتَّبَعَ هَوَاهُ وَكَانَ أَمْرُهُ فُرُطًا ﴿٢٨﴾

**27. Na soma uliyofunuliwa katika Kitabu cha Mola wako Mlezi. Hapana wa kubadilisha Maneno Yake. Wala nawe hutapata makimbilio isipokuwa Kwake.**

**28. Na isubirisha nafsi yako pamoja na wanaomuomba Mola wao Mlezi asubuhi na jioni, hali ya kuwa wanataka Radhi Yake. Wala macho yako yasiwaruke kwa kutaka pambo la maisha ya dunia. Wala usimtii Tuliymghafilisha moyo wake asitukumbuke, na akafuata matamano yake yakawa yamepita mpaka.**

### Amri ya Kusoma Qur'ani na Kuwa na Subra pamoja na Waumini

Allah تعالیٰ Anasema Akimuamuru Mtume Wake kusoma Kitabu Chake Kitukufu na kukifikisha kwa watu:

مُبَدِّلَ لِكَلِمَاتِهِ

**“Hapana wa kubadilisha Maneno Yake.”**

Maana yake: Hakuna anayeweza kubadilisha wala kuyageuza Maneno ndani yake wala kuyapindisha kwa kufasiri sivyo. Na,

وَلَنْ تَجِدَ مِنْ دُونِهِ مُلتَحَدًا ﴿٢٧﴾

**“Wala nawe hutapata makimbilio isipokuwa Kwake.”**

Imepokewa kuwa Mujaahid amesema: “Makazi au makimbilio.”<sup>1</sup> Na Qatadah naye amesema: “Msaidizi wala rafiki.”<sup>2</sup> Amesema Ibn Jariir رحمه الله تعالیٰ: “Allah

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 17:651.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 17:651.

تعالى Anasema, 'Ewe Muhammad! Ikiwa hutasoma uliyoteremshiwa katika Kitabu cha Mola wako Mlezi, hutakuwa na makimbilio au ulinzi kutoka kwa Allah تعالى<sup>1</sup>". Hii ni kama Kauli ya Aliyetukuka:

﴿ يَتَأْتِيهَا الرَّسُولُ بَلِّغْ مَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ وَإِنْ لَمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَغْتَ رَسُولَهُ ۗ وَاللَّهُ يَعَصْمُكَ مِنَ النَّاسِ ۗ ﴾

***"Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi; na kama hutafanya, basi hukufikisha ujumbe Wake. Na Allah Atakulinda na watu."*** (5:67)

Na Amesema:

﴿ إِنَّ الَّذِي فَرَضَ عَلَيْكَ الْقُرْآنَ لَرَأْدُكَ إِلَىٰ مَعَادٍ ۗ ﴾

***"Hakika Yeye Aliyekulazimisha kufuata Qur'ani kwa yakini Atakurudisha mahali pa kurejea."*** (28:85),

Maana yake: Atakuuliza kwa Aliyokufaradhishia katika kufikisha ujumbe. Na Kauli Yake:

﴿ وَأَصْبِرْ نَفْسَكَ مَعَ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ بِالْغَدْوَةِ وَالْعِشِيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُ ۗ ﴾

***"Na isubirisha nafsi yako pamoja na wanaomuomba Mola wao Mlezi asubuhi na jioni, hali ya kuwa wanataka Radhi Yake."***

Maana yake: Kukaa pamoja na wale wanaomdhukuru Allah تعالى, wanaoleta *Tahlili (Laa ilaaha illa Llaahu)*, na *Tahmid (Alhamdulillah)*, na *Tasbih (Subhaanallaah)* na kuleta *Takbiri (Allahu Akbar)* na kumuomba asubuhi na jioni, waja wote wa Allah تعالى, wakiwa matajiri au masikini, wenye nguvu au dhaifu. Inasemekana kuwa Aya hii iliteremshwa kwa mabwana (mabwanyenye) wa Kikureshi walipomtaka Mtume akae nao peke yao wala asiwalete wale wanyonge miongoni mwa Maswahaba wake, kama Bilaal, 'Ammaar, Suhayb, Khabbaab na Ibn Mas'ud رضي الله عنهم. Walitaka akae nao peke yao, lakini Allah تعالى Alimkataza kufanya hivyo, na Kumwambia,

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 17:651.

وَلَا تَطْرُدِ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ بِالْغَدَاةِ وَالْعَشِيِّ

**“Wala usiwafukuze wale wanaomuabudu Mola wao Mlezi, asubuhi na jioni...” (6:52).**

Allah تعالى Alimuamuru aisubirisha nafsi yake kwa kukaa na hawa (Waumini wanyonge). Akasema:

وَأَصْبِرْ نَفْسَكَ مَعَ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ بِالْغَدَاةِ وَالْعَشِيِّ

**“Na isubirisha nafsi yako pamoja na wanaomuomba Mola wao asubuhi na jioni”.**

Na amepokea Imaam Muslim katika Sahihi yake kutoka kwa Sa’ad bin Abi Waqqaasw amesema: “Tulikuwa kikundi cha watu sita pamoja na Mtume.” Washirikina wakasema: ‘Waambie watu hawa waondoke ili wasituudhi’. Nilikuwa mimi, Ibn Mas’ud, mtu kutoka katika ukoo wa Hudhayl, Bilaal na watu wawili ambao nimewasahau majina yao. Ikaja fikra katika nafsi ya Mtume ﷺ Alivyopenda Allah تعالى afikirie, hivyo akaihadithia nafsi yake. Hapo Allah تعالى Akateremsha:

وَلَا تَطْرُدِ الَّذِينَ يَدْعُونَ رَبَّهُمْ بِالْغَدَاةِ وَالْعَشِيِّ يُرِيدُونَ وَجْهَهُ<sup>ط</sup>

**‘Wala usiwafukuze wale wanaomuabudu Mola wao Mlezi, asubuhi na jioni kwa kutaka Radhi Yake.’ (6:52)**

Muslim peke yake ndiye aliyenukuu bila al-Bukhaariy.<sup>1</sup> Na Kauli Yake:

وَلَا تَعْدُ عَيْنَاكَ عَنْهُمْ تُرِيدُ زِينَةَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا<sup>ط</sup>

**“Wala macho yako yasiwaruke kwa kutaka pambo la maisha ya dunia.”**

Amesema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما: “Wala usiwapendeleo wengine juu yao”<sup>2</sup>, kumaanisha kutaka badali yao watu wenye vyeo, hadhi, utukufu, na utajiri. Pia,

<sup>1</sup> Muslim 4:1878.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:6.

وَلَا تُطِيعَنَّ مَنْ أَغْفَلْنَا قَلْبَهُ عَن ذِكْرِنَا

**“Wala usimtii Tuliye mghafilisha moyo wake asitukumbuke.”**

Maana yake: Wale walioshughulishwa na dunia hivyo wasiwe ni wenye kufuata Dini na kufanya Ibada. Hivyo,

وَكَانَ أَمْرُهُ فُرْطًا ﴿٢٥﴾

**“Yakawa yamepita mpaka.”**

Maana yake: Amali zake na matendo yake yakawa ni ya kipuuzi na kupoteza wakati tu. Wala usiwe ni mwenye kumtii wala kupenda njia zake wala kumhusudu kwa aliyenayo.

Kama Alivyosema Aliyetukuka mahali pengine:

وَلَا تَمُدَّنَّ عَيْنَيْكَ إِلَىٰ مَا مَتَّعْنَا بِهِ أَزْوَاجًا مِنْهُمْ زَهْرَةَ الدُّنْيَا لِنَفْتِنَهُمْ فِيهِ ۚ وَرِزْقٌ

رَبِّكَ خَيْرٌ وَأَبْقَىٰ ﴿٢٦﴾

**“Wala usivikodolee macho yako Tulivyowastereheshea baadhi ya watu miongoni mwao, hao wabaya. Hivyo ni mapambo ya maisha ya dunia tu, ili Tuwafanyie mtihani kwavyo. Na riziki ya Mola wako Mlezi ni bora mno na iendeleayo.” (20:131)**

وَقُلِ الْحَقُّ مِن رَّبِّكُمْ ۚ فَمَن شَاءَ فَلْيُؤْمِن وَمَن شَاءَ فَلْيُكْفُرْ ۚ إِنَّا أَعْتَدْنَا لِلظَّالِمِينَ نَارًا

أَحَاطَ بِهِنَّ سُرَادِقُهَا ۚ وَإِن يَسْتَغِيثُوا يُغَاثُوا بِمَاءٍ كَالْمُهْلِ يَشْوِي الْوُجُوهَ ۚ بِئْسَ الشَّرَابُ

وَسَاءَتٌ مُّرْتَفَقًا ﴿٢٧﴾

**29. Na sema: Hii ni kweli itokayo kwa Mola wako Mlezi. Basi atakaye aamini, na atakaye, akatae. Hakika Sisi Tumewaandalia wenye kudhulumu Moto ambao utawazunguka kama hema. Na wakiomba msaada watasaidiwa kwa kupewa maji kama mafuta yaliyotibuka. Yatayowababua nyuso zao. Kinywaji hicho ni kiovu mno! Na matandiko hayo ya kupumzikia ni maovu mno!**

## Ukweli Watoka kwa Allah تعالى na Adhabu kwa Wale Wasioamini

Allah تعالى Anamuambia Mtume Wake ﷺ: “Na sema ewe Muhammad kwa watu! Haya niliyokuja nayo kutoka kwa Mola wenu Mlezi ni ukweli usio na shaka ndani yake”.

فَمَنْ شَاءَ فَلْيُؤْمِنْ وَمَنْ شَاءَ فَلْيُكْفُرْ<sup>٤</sup>

**“Basi atakaye, aamini. Na atakaye, akatae.”**

Hii ni aina ya onyo kali, kwa hivyo Akasema:

إِنَّا أَعْتَدْنَا

**“Hakika Sisi Tumewaandalia.”**

Maana yake: Tumeweka tayari,

لِلظَّالِمِينَ

**“Kwa wenye kudhulumu.”**

Nao ni makafiri wanaomkanusha Allah تعالى, na Mtume Wake ﷺ na Kitabu Chake:

نَارًا أَحَاطَ بِهَا<sup>٥</sup> سُرَادِقُهَا

**“Moto ambao utawazunguka kama hema.”**

Maana yake: Ngome. Na amesema Ibn Jurayj kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema:

أَحَاطَ بِهَا<sup>٥</sup> سُرَادِقُهَا

**“Utawazunguka kama hema.”**

“Ukuta wa moto.”<sup>1</sup> Na Kauli Yake:

وَإِنْ يَسْتَعِثُّوا يُعَاثُوا بِمَاءٍ كَالْمُهْلِ يَشْوِي آلُجُوهَ<sup>٦</sup>

**“Na wakiomba msaada watasaidiwa kwa kupewa maji kama mafuta yaliyotibuka yatakayowababua nyuso zao.”**

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18: 11.

Amesema Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: "Al-Muhl ni maji mazito mfano wa mashapo ya mafuta."<sup>1</sup> Mujaahid amesema: "Ni kama mfano wa damu na usaha."<sup>2</sup> Na amesema 'Ikrimah: "Ni kitu kilichofikia kilele cha uharara." Wengine wamesema: "Ni kitu chochote kilichoyeyuka."<sup>3</sup> Na amesema Qataadah: "Ibn Mas'ud رضي الله عنه aliyeyusha dhahabu katika tanuri, na ilikuwa maji na povu likapanda mpaka juu, alisema, hiki ni kitu kinachofanana na Al-Muhl."<sup>4</sup> Na amesema Adh-Dhahaak: "Maji ya Jahanamu ni meusi, na wenyewe ni mweusi na watu wake ni weusi."<sup>5</sup> Na hizi kauli zote hazipingani, kwani Al-Muhl inajumlisha sifa zote hizi mbaya, ni nyeusi, inanuka, nzito na moto. Kama Alivyosema Allah تعالى:

يَشْوَى الْوُجُوهُ

**"Yatayowababua nyuso zao."**

Maana yake: Kwa ajili ya moto na uharara wake. Atakapotaka kafiri kuyanywa, hivyo kuyaleta karibu na uso wake, yataibabua ngozi kuifanya idondoke ndani yake (ndani ya kinywaji).

Amesema Sa'id bin Jubayr: "Pindi watakaposikia njaa watu wa Motoni, watataka afueni kutoka kwayo, na watapatiwa mti wa *Zaqquum* ambao watakula. Mti utararua ngozi ya nyuso zao, na lau yeyote anaewajua atapita karibu nao, atatambua ngozi ya nyuso zao kwenye mti. Kisha watasikia kiu, hivyo wataomba kinywaji, na watapatiwa maji mfano wa Al-Muhl, hayo ni yale yaliyochemshwa mpaka kilele cha uharara. Kitakapoletwa karibu na midomo yao, nyama ya nyuso zao ambazo kwayo ngozi imeraruliwa itachomwa."<sup>6</sup> Baada ya kukielezea kinywaji hiki kwa sifa hizi za kutisha, Allah تعالى Anasema:

بِقَسْرِ الْأَشْرَابِ

**"Kinywaji hicho ni kiovu mno."** Maana yake: Ni kinywaji kiovu sana. Vivyo hivyo, Anasema katika Aya nyengine:

<sup>1</sup> At-Tabari 18:13.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:13.

<sup>3</sup> At-Tabari 18:12.

<sup>4</sup> At-Tabari 18:13.

<sup>5</sup> At-Tabari 18:13.

<sup>6</sup> At-Tabari 18:14.



وَسُقُوا مَاءً حَمِيمًا فَقَطَّعَ أَمْعَاءَهُمْ ﴿٤٧﴾

**“...Na kunyweshwa maji yachemkayo yatakayokata chango zao?”  
(47:15)**

Na Amesema Aliyetukuka:

تُسْقَى مِنْ عَيْنٍ آتِيَةٍ ﴿٤٨﴾

**“Watanyweshwa humo katika chemchem zichemkazo barabara.” (88:5)**

Maana: Uharara na moto wake. Kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَيَبِّئْ حَمِيمٍ ءَانٍ ﴿٤٩﴾

**“Na baina ya maji ya moto yachemkayo.” (55:44)**

Na Kauli Yake:

وَسَاءَتْ مُرْتَفَقًا ﴿٥٠﴾

**“Na matandiko hayo ya kupumzikia ni maovu mno.”**

Maana yake: Ni mahali paovu sana Motoni kuwa ndiyo nyumba, makao ya kupumzika na kukusanyika. Kama Alivyosema Allah تعالى katika Aya nyengine:

إِنَّهَا سَاءَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا ﴿٥١﴾

**“Hakika hiyo Jahanamu ni kituo kibaya na mahali pabaya sana pa kukaa.” (25:66)**

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ إِنَّا لَا نُضِيعُ أَجْرَ مَنْ أَحْسَنَ عَمَلًا ﴿٥٢﴾

أُولَئِكَ هُمْ جَنَّاتُ عَدْنٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ يُتْلَوْنَ فِيهَا مِنْ أَسْوَرَ مِنْ ذَهَبٍ

وَيَلْبَسُونَ ثِيَابًا خُضْرًا مِنْ سُنْدُسٍ وَإِسْتَبْرَقٍ مُتَّكِينَ فِيهَا عَلَى الْأَرَائِكِ ۗ نِعْمَ الْأَثْوَابُ

وَحَسَنَتُ مُرْتَفَقًا ﴿٥٣﴾

**30. Hakika wale walioamini na wakatenda mema - hakika Sisi Hatupotezi ujira wa anayetenda mema.**

<sup>1</sup> At-Tabari 18:14.

**31. Hao watapata Bustani za milele, zinazopita mito kati yake. Humo watapambwa kwa mavazi ya mikononi ya dhahabu, na watavaa nguo za kijani za Sundus na Istabraq, huku wakiwa Muttakiin humo juu ya makochi. Ni malipo bora hayo! Na matandiko mazuri mno ya kupumzikia!**

### Malipo na Jaza ya Walioamini na Kutenda Matendo Mema

Pale Allah تعالی Alipotaja hali ya ya watu waovu, Anafuatisha kwa kutaja hali ya watu wema, waliomuamini Allah تعالی na yaliyokuja na Mitume Wake, walifanya amali njema walizoamrisha. Wao watakuwa na *Jannatu 'Adn*. 'Adn inamaanisha yenye kudumu.

تَجْرِي مِنَ تَحْتِهِمُ الْأَنْهَارُ

**“Zinazopita mito kati yake.”**

Maana yake: Mbele ya vyumba na makaazi yao. Firauni alisema:

وَهَذِهِ الْأَنْهَارُ تَجْرِي مِن تَحْتِي

**“...na hii mito ipitayo mbele yangu...” (43:51)**

يُحَلِّوْنَ

**“Humo watapambwa.”**

Maana yake: Na mapambo ya vito.

فِيهَا مِنْ أَسَاوِرَ مِنْ ذَهَبٍ

**“Kwa mavazi ya mikononi ya dhahabu.”**

Allah تعالی Anasema kwengineko:

وَلَوْلَوْأَ وَ لِبَاسُهُمْ فِيهَا حَرِيرٌ ﴿٢٣﴾

**“Na lulu na mavazi yao humo yatakuwa hariri.” (22:23)**

Hii imeelezwa kwa kina hapa, ambapo Allah تعالی Anasema:

وَيَلْبَسُونَ ثِيَابًا خُضْرًا مِّنْ سُندُسٍ وَإِسْتَبْرَقٍ

**“Na watavaa nguo za kijani za sundus na Istabraq”.**

Sundus ni nguo nzuri, kama shati na mfano wake na *Istabraq* ni mahameli nene inayong’aa. Na Kauli Yake:

مُتَّكِئِينَ فِيهَا عَلَى الْأَرَائِكِ

**“Huku wakiwa Muttaki’iin humo juu ya makochi”.**

Neno *Muttaki’iin* ina maana ya kujinyoosha chini, au inasemwa inamaanisha kukaa kimarufaa, ambayo iko karibu na maana yake hapa. Katika Hadithi Sahihi, Mtume ﷺ amesema:

أَنَا أَنَا فَلَا أَكُلُ مُتَّكِئًا

**“Ama kwangu mimi, sikai kimarufaa wakati wa kula.”<sup>1</sup>**

*Araa’ik* ni wingi wa *Ariikah*, ambacho ni kitanda chini ya kipaa kilichoningi’izwa (*Bashkhanah*). Na Allah تعالیٰ Anajua zaidi. Na Kauli Yake:

نِعْمَ الثَّوَابُ وَحَسُنَتْ مُرْتَفَقًا

**“Ni malipo bora hayo! Na matandiko mazuri mno ya kupumzikia!”**

Maana: Ni neema iliyoje ya kupatiwa Pepo kama jaza na zawadi kwa amali zao njema. Na *Murtafaq* nzuri sana ina maana ya makazi na nyumba njema ya kupumzika, kama Alivyosema hapo awali kuhusiana na Moto:

بئسَ الشَّرَابُ وَسَاءَتْ مُرْتَفَقًا

**“Kinywaji hicho ni kiovu mno! Na matandiko hayo ya kupumzikia ni maovu mno!” (18:29).**

Kwa njia hiyo hiyo, Analinganisha (Pepo na Moto) katika *Suratul Furqaan* katika Kauli Yake:

إِنَّهَا سَاءَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا

**“Hakika hiyo Jahanamu ni kituo kibaya na mahali pabaya kabisa pa kukaa.” (25:66).**

<sup>1</sup> Tuhfat Al-Ahwadhiy 5:557.

Kisha Akataja sifa za Waumini, Akasema:

أُولَئِكَ مُجْرَمُونَ الْغُرَفَةَ بِمَا صَبَرُوا وَيُلَقَّوْنَ فِيهَا تَحِيَّةً وَسَلَامًا ﴿٧٥﴾ خَالِدِينَ  
فِيهَا حَسَنَتٌ مُّسْتَقَرًّا وَمُقَامًا ﴿٧٦﴾

***“Hao ndio watakaolipwa ghorofa za Peponi kwa kuwa walisubiri, na watakuta humo heshima na amani; Wakae humo milele: kituo kizuri na mahali pazuri kabisa pa kukaa.” (25:75-76).***

\* \* \*

\* وَأَضْرِبْ لَهُم مَّثَلًا رَّجُلَيْنِ جَعَلْنَا لِأَحَدِهِمَا جَنَّتَيْنِ مِنْ  
 أَعْنَابٍ وَخَفَفْنَاهَا بِنَخْلٍ وَجَعَلْنَا بَيْنَهُمَا زُرْعًا ﴿٣٢﴾ كِلْتَا  
 الْجَنَّتَيْنِ ءَاتَتْ أَكْثَرًا وَأَلْهَىٰ أَكْثَرًا لِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٣٣﴾ وَكَانَ لِمَنْ  
 أَهْرَأَهُمْ نَهْرًا ﴿٣٤﴾ وَكَانَ لَهُ ثَمَرٌ فَقَالَ لِصَاحِبِهِ وَهُوَ  
 يُخَاوِرُهُ أَنَا أَكْثَرُ مِنْكَ مَالًا وَأَعَزُّ نَفَرًا ﴿٣٥﴾ وَدَخَلَ جَنَّتَهُ  
 وَهُوَ ظَالِمٌ لِنَفْسِهِ قَالَ مَا أَظُنُّ أَن تَبِيدَ هَذِهِ أَبَدًا ﴿٣٦﴾  
 وَمَا أَظُنُّ السَّاعَةَ قَائِمَةً وَلَئِن رُّدِدْتُ إِلَىٰ رَبِّي لَأُجِدَنَّ خَيْرًا  
 مِنْهَا مُنْقَلَبًا ﴿٣٧﴾ قَالَ لَهُ صَاحِبُهُ وَهُوَ يُخَاوِرُهُ أَكَفَرْتَ  
 بِالَّذِي خَلَقَكَ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ مِنْ نُطْفَةٍ ثُمَّ سَوَّكَ رَجُلًا ﴿٣٨﴾  
 لَنُكُنَّا هُوَ اللَّهُ رَبِّي وَلَا أُشْرِكُ بِرَبِّي أَحَدًا ﴿٣٩﴾ وَلَوْلَا  
 إِذْ دَخَلْتَ جَنَّتَكَ قُلْتَ مَا شَاءَ اللَّهُ لَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ إِن تَرَنِ  
 أَنَا أَقَلُّ مِنْكَ مَالًا وَوَلَدًا ﴿٤٠﴾ فَعَسَىٰ رَبِّي أَن يُؤْتِيَنِي خَيْرًا  
 مِنْ جَنَّتِكَ وَيُرْسِلَ عَلَيْهَا حُسْبَانًا مِنَ السَّمَاءِ فَتُصْبِحَ  
 صَعِيدًا زَلَقًا ﴿٤١﴾ أَوْ يُصْبِحَ مَأْوَاهَا غَوْرًا فَلَن تَسْتَطِيعَ  
 لَهُ طَلَبًا ﴿٤٢﴾ وَأُحِيطَ بِثَمَرِهِ فَأَصْبَحَ يُقَلِّبُ كَفَّيْهِ عَلَىٰ  
 مَا أَنفَقَ فِيهَا وَهِيَ خَاوِيَةٌ عَلَىٰ عُرُوشِهَا وَيَقُولُ يَا لَيْتَنِي لَمْ  
 أُشْرِكْ بِرَبِّي أَحَدًا ﴿٤٣﴾ وَلَمْ تَكُن لَّهُ فِئَةٌ يَنْصُرُونَهُ مِنْ  
 دُونِ اللَّهِ وَمَا كَانَ مُنتَصِرًا ﴿٤٤﴾ هُنَالِكَ الْوَلَايَةُ لِلَّهِ الْحَقِ  
 هُوَ خَيْرٌ ثَوَابًا وَخَيْرٌ عُقْبًا ﴿٤٥﴾

\* وَأَضْرِبْ لَهُم مَّثَلًا رَّجُلَيْنِ جَعَلْنَا  
 لِأَحَدِهِمَا جَنَّتَيْنِ مِنْ أَعْنَابٍ  
 وَخَفَفْنَاهَا بِنَخْلٍ وَجَعَلْنَا بَيْنَهُمَا  
 زُرْعًا ﴿٣٢﴾ كِلْتَا الْجَنَّتَيْنِ ءَاتَتْ أَكْثَرًا  
 وَأَلْهَىٰ أَكْثَرًا لِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٣٣﴾  
 وَكَانَ لِمَنْ أَهْرَأَهُمْ نَهْرًا ﴿٣٤﴾ وَكَانَ لَهُ  
 ثَمَرٌ فَقَالَ لِصَاحِبِهِ وَهُوَ يُخَاوِرُهُ أَنَا  
 أَكْثَرُ مِنْكَ مَالًا وَأَعَزُّ نَفَرًا ﴿٣٥﴾  
 وَدَخَلَ جَنَّتَهُ وَهُوَ ظَالِمٌ لِنَفْسِهِ  
 قَالَ مَا أَظُنُّ أَن تَبِيدَ هَذِهِ أَبَدًا ﴿٣٦﴾  
 وَمَا أَظُنُّ السَّاعَةَ قَائِمَةً وَلَئِن  
 رُّدِدْتُ إِلَىٰ رَبِّي لَأُجِدَنَّ خَيْرًا مِنْهَا  
 مُنْقَلَبًا ﴿٣٧﴾

32. Na wapigie mfano wa watu wawili: mmoja wao Tulimpa vitalu viwili vya mizabibu, na Tukavizungushia mitende, na kati yake Tukatia mimea ya nafaka.

33. Na hivyo vitalu viwili vikitoa mazao yake, wala hapana kitu katika hayo kilichotindikia. Na ndani yake Tukapasua mito.

**34. Naye alikuwa na mazao mengi. Basi akamuambia mwenzake naye akibishana naye: Mimi nimekushinda wewe kwa mali na nguvu za watu!**

**35. Na akaingia kitaluni kwake, naye hali anajidhulumu nafsi yake. Akasema: Sidhani kabisa kuwa haya yataharibika.**

**36. Wala sidhani kuwa hiyo Saa (ya Kiyama) itatokea. Na ikiwa nitarudishwa kwa Mola wangu Mlezi, bila ya shaka nitapata marejeo bora zaidi kuliko haya.**

### Mfano wa Washirikina Matajiri na Waislamu Mafakiri

Baada ya Allah تعالى kutaja washirikina waliotakabari, hivyo kukataa kukaa pamoja na masikini na wanyonge miongoni mwa Waislamu, wakiwaonesha mbele yao kwa ile mali walionayo na utukufu wao katika kizazi. Allah تعالى Anawapigia mfano wa watu wawili. Mmoja wao alineemeshwa na Allah تعالى kwa kupatiwa bustani mbili za zabibu, zilizozungukwa na mitende, naye alikuwa akivuna mwaka mzima. Mimea na miti yote ilikuwa ikitoa mazao mazuri, yaliyokuwa yakipatikana kwa usahali na hivyo kupata mavuno mazuri.

Allah تعالى Akasema:

كَلَّمْنَا الْجَنَّتَيْنِ ءَاتَتْ أُكُلَهَا

**“Na hivyo vitalu viwili vikitoa mazao yake.”**

Maana yake: Yakitoa mazao na matunda yake,

وَلَمْ تَظَلِمِ مِنْهُ شَيْئًا

**“Wala hapana kitu katika hayo kilicho tindikia.”**

Maana yake: Hakuna chochote katika hizo kilichopungua.

وَفَجَّرْنَا خِلْفَهُمَا نَهْرًا

**“Na ndani yake Tukapasua mito.”**

Maana yake: Mito ilikuwa ikipita kati yake hapa na pale.

وَكَانَ لَهُ ثَمَرٌ

**“Naye alikuwa na mazao mengi”.**

Pamesemwa: Makusudio hapa ni mali, na pamesemwa: Ni mazao na matunda, ambayo ndio maana iliyo dhahiri hapa. Na hii inatiliwa nguvu na kisomo chengine: *“Wa kaana lahu thumrun (Thaa ikiwa na Dhumma, Miim ikiwa na Sakna)”*. Hivyo kuwa ni wingi wa neno *Thamarah*. Na wakasoma wengine: *Thamarun – Thaa na Miim zikiwa na Fatha*<sup>1</sup>.

فَقَالَ

**“Akasema.”**

Maana yake: Yule sahibu wa bustani mbili:

لصاحبيه وهو شاوره

**“Mwenzake naye akibishana naye.”**

Maana yake: Akijadiliana naye, huku akijifakhiri na kujionesha,

أَنَا أَكْثَرُ مِنْكَ مَالًا وَأَعَزُّ نَفَرًا ﴿١٧﴾

**“Mimi nimekushinda wewe kwa mali na nguvu za watu!”**

Maana yake: Nina watumishi na wahudumu wengi na watoto, hadhi na heshima kubwa. Amesema Qataadah: “Hii, Wallahi, ni matumaini ya kila muovu kuwa na mali nyingi na msafara mkubwa.”<sup>1</sup> Na Kauli Yake:

وَدَخَلَ جَنَّتَهُ وَهُوَ ظَالِمٌ لِّنَفْسِهِ

**“Na akaingia kitaluni kwake, naye hali anajidhulumu nafsi yake.”**

Maana yake: Kwa kukanusha na kukengeuka kwake, kiburi chake na kukataa kwake Akhera.

<sup>1</sup> At-Tabari 18:21.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:22.

قَالَ مَا أَظُنُّ أَنْ تَبِيدَ هَذِهِ أَبَدًا ﴿٣٢﴾

**“Akasema: Sidhani kabisa kuwa haya yataharibika.”**

Hivyo, alikubali kuhadaika kwa sababu ya mimea, miti na matunda aliyoyaona, na mito iliyokuwa ikipita katika sehemu tofauti za bustani yake. Alidhania kuwa hayo hayatakuwa na ukomo wala kuharibika. Hii ilitokana na ukosefu wa ufahamu na uhaba wa akili yake na udhaifu wa Imani na yakini yake kwa Allah تعالى. Na pia kwa sababu ya kustaajabia maisha ya hapa duniani na mapambo yake na kukanusha kwake Akhera. Kwa ajili hiyo akasema:

وَمَا أَظُنُّ السَّاعَةَ قَائِمَةً

**“Wala sidhani kuwa hiyo Saa (ya Kiyama) itatokea.”**

Maana yake: Hakitatokea milele,

وَلَئِنْ رُدِدْتُ إِلَىٰ رَبِّي لَأَجِدَنَّ خَيْرًا مِّنْهَا مُنْقَلَبًا ﴿٣٣﴾

**“Na ikiwa nitarudishwa kwa Mola Wangu Mlezi, bila ya shaka nitapata marejeo bora zaidi kuliko haya.”**

Maana yake: ikiwa kutakuwa na Akhera na kurudi kwa Allah تعالى, basi nitakuwa na sehemu nzuri zaidi kuliko hii kwa Mola Wangu Mlezi. Na lau si kwa sababu mimi napendwa Naye sana basi Hangenipatia yote haya. Kama Alivyosema Aliyetukuka katika Aya nyengine:

وَلَئِنْ رُجِعْتُ إِلَىٰ رَبِّي إِنَّ لِي عِنْدَهُ لَلْحُسْنَىٰ

**“Na kama nikirudishwa kwa Mola Wangu Mlezi bila shaka nina mema yangu Kwake.” (41:50)**

Na Amesema:

أَفَرَأَيْتَ الَّذِي كَفَرَ بِعَائِبَتِنَا وَقَالَ لَأُوتِينَ مَالًا وَوَلَدًا ﴿٣٤﴾

**“Je, umemuona yule aliyezikanusha Aya Zetu na akasema: ‘Kwa hakika nitapewa huko Akhera mali na watoto kama nilivyopewa hapa.’ (19:77)**



Maana yake: Aliapa na kujipatia dhamana kuwa Allah تعالى Atampatia haya bila ya dalili sahihi kuhusu hayo. Sababu ya kuteremshwa Aya hii ni kuwa Al-Aasw bin Waa'il, kama tutakavyobainisha hilo mahali muafaka kabisa, Allah تعالى Akipenda. Na Kwake tuna Imani na Yeye Ndiye tunayemtegemea.

قَالَ لَهُ صَاحِبُهُ وَهُوَ يُحَاوِرُهُ أَكَفَرْتَ بِالَّذِي خَلَقَكَ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ مِنْ نُطْفَةٍ ثُمَّ سَوَّكَ  
رَجُلًا ﴿٣٧﴾ لَنَكُنَّا هُوَ اللَّهُ رَبِّي وَلَا أُشْرِكُ بِرَبِّي أَحَدًا ﴿٣٨﴾ وَلَوْلَا إِذْ دَخَلْتَ جَنَّتَكَ قُلْتَ  
مَا شَاءَ اللَّهُ لَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ إِن تَرَنِ أَنَا أَقَلُّ مِنْكَ مَالًا وَوَلَدًا ﴿٣٩﴾ فَعَسَى رَبِّي أَنْ يُؤْتِيَنِي  
خَيْرًا مِّنْ جَنَّتِكَ وَيُرْسِلَ عَلَيْهَا حُسْبَانًا مِّنَ السَّمَاءِ فَتُصْبِحُ صَعِيدًا زَلَقًا ﴿٤٠﴾ أَوْ يُصْبِحَ  
مَأْوَاهَا غَوْرًا فَلَن تَسْتَطِيعَ لَهُ طَلَبًا ﴿٤١﴾

**37. Mwendake akamuambia kwa kubishana naye: Je! Unamkufuru Aliyekuumba kutokana na udongo, tena kutokana na tone la manii, kisha Akakufanya mtu kamili?**

**38. Lakini Yeye Allah Ndiye Mola Wangu Mlezi. Wala simshirikishi na yeyote.**

**39. Na lau kuwa ulipoingia kitaluni kwako ungelisema: Maashaallah! Alitakalo Allah huwa! Hapana nguvu ila kwa Allaah. Ikiwa unaniona mimi nina mali kidogo na watoto kuliko wewe,**

**40. Basi huenda Mola wangu Mlezi Akanipa kilicho bora kuliko kitalu chako, naye Akapitisha Kudra Yake kutoka mbinguni kukiletea hicho chako, na kikageuka ardhi tupu inayoteleza.**

**41. Au maji yake yakadidimia wala usiweze kuyagundua.**

### Majibu ya Muumini Fakiri

Allah تعالى Anatueleza vipi sahibu Muumini wa tajiri alivyo mjibu, kwa kumpatia mawaidha na kumuonya kwa aliyokuwa nayo kwa kumkufuru Allah تعالى na kujidanganya:

أَكَفَرْتَ بِالَّذِي خَلَقَكَ مِنْ تُرَابٍ

**“Je! Unamkufuru Aliyekuumba kutokana na udongo”.**

Na huku ni kukataa na kukuza kule kumkanusha kwake Mola wake Mlezi Aliyemuumba na Kumuanzisha mwanadamu kutokana na udongo, naye ni Adam عليه السلام, kisha Akakijaalia kizazi chake kutokana na maji dhalili,

Kama Alivyosema Aliyetukuka:

كَيْفَ تَكْفُرُونَ بِاللَّهِ وَكُنْتُمْ أُمَمًا قَدْ حَيَّيْنَاكُمْ

**“...Vipi mnamkanusha Allah, na hali mlikuwa wafu, Akaku-huisheni...” (2:28),**

Maana yake: Vipi mtamkanusha Mola wenu Mlezi na dalili za Kuwepo kwake zipo wazi kabisa kwa kila mmoja kuziona. Hakuna hata mmoja katika viumbe Vyake asiyejua kuwa yeye hakuwa chochote, kisha akaja ulimwenguni, na kuwepo kwake si kwa sababu yake au kwa kiumbe mwengine. Anajua kuwa kuwepo kwake hapa ni kwa sababu ya Muumba Wake, Naye ni Allah تعالى, hapana Mola apasaye kuabudiwa ila Yeye, Muumba wa kila kitu. Kwa ajili hiyo, akasema Muumini:

لَيْكِنَّا هُوَ اللَّهُ رَبِّي

**“Lakini Yeye Allaah Ndiye Mola Wangu Mlezi”,**

Maana: Ama kwangu mimi sitasema kama ulivyosema, bali ninatambua Upweke na Ubwana wa Allah تعالى,

وَلَا أُشْرِكُ بِرَبِّي أَحَدًا ﴿٢٨﴾

**“Wala simshirikishi na yeyote.”**

Hii ina maana kuwa bali Yeye ni Allah تعالى Anayeabudiwa Peke Yake, Hana mshirika na yeyote. Kisha akasema:

وَلَوْلَا إِذْ دَخَلْتَ جَنَّتَكَ قُلْتَ مَا شَاءَ اللَّهُ لَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ ۗ إِنَّ تَرِنَ أَنَا أَقَلُّ مِنكَ مَالًا

وَوَلَدًا ﴿٢٩﴾

**“Na lau kuwa ulipoingia kitaluni kwako ungelisema: Maashaallah! Alitakalo Allah huwa! Hapana nguvu ila kwa Allah. Ikiwa unaniona mimi nina mali kidogo na watoto kuliko wewe”.**

Huku ni kumhimiza na kumshawishi kusema hayo, kama kwamba alikuwa anasema: “Unapoinjia kwenye bustani lako na kuliangalia kwa kulipenda, kwa nini humshukuru Allah تعالیٰ kwa neema hiyo na pia kwa mali na watoto Aliokupa wewe na sio wengine? Kwa nini hukusema: ‘Maasha’Allaah! Hakuna nguvu ila kwa Allah تعالیٰ?” Kwa ajili hii baadhi ya *Salaf* (watangu) wamesema: “Mwenye kustaajabu kwa chochote katika hali yake au mali au watoto, basi asema: ‘Maashaallah! Alitakalo Allah huwa! Hapana nguvu ila kwa Allah’”. Hii imechukuliwa kutoka kwa Aya hii tukufu. Imethibiti katika Sahihi kutoka kwa Abu Musa رضي الله عنه Mtume ﷺ amesema:

«أَلَا أَدُلُّكَ عَلَىٰ كَثْرٍ مِّنْ مَّا كُنْتُمْ الْجَنَّةِ؟ لَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ»

*“Je, niwaambie nyinyi hazina miongoni mwa hazina za Peponi? (nayo ni) Laa Hawla walaa Quwwata illaa Billaahi (Hapana hila wala nguvu ila kwa kuwezesha na Allah).”<sup>1</sup>*

Na Kauli Yake:

فَعَسَىٰ رَبِّي أَن يُؤْتِيَنِي خَيْرًا مِّنْ جَنَّتِكَ

***“Basi huenda Mola Wangu Mlezi Akanipa kilicho bora kuliko kitalu chako.”***

Maana yake: Katika nyumba ya Akhera.

وَيُرْسِلْ عَلَيْهَا

***“Naye Akapitisha kudra Yake.”***

Maana yake: Kwa kitalu (bustani) chako hapa duniani, ambacho unadhania hakitakwisha au kufikia kikomo,

حُسْبَانًا مِّنَ السَّمَاءِ

***“Husbaanan kutoka mbinguni (kukiletea hicho chako).”***

Amesema Ibn ‘Abbaas, Adh-Dhahaak na Qatadah<sup>2</sup>, na Maalik kutoka kwa Az-Zuhriy: Yaani: hiyo ni adhabu kutoka mbinguni.” Hata hivyo, maana iliyo dhahiri

<sup>1</sup> Fat’hul-Baariy 11:217 na Muslim 4:2076.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:25.

ni mvua kubwa itakayovuruga kitalu chake na kung'oa mimea na miti iliyomo ndani yake. Kama Alivyosema:

﴿٤٤﴾ فَتُصْبِحُ صَعِيدًا زَلَقًا

**“Na kikageuka ardhi tupu inayoteleza.”**

Maana yake: Ardhi yenye udongo unaoteleza ambao hakuna awezae kuithibitisha miguu yake. Na amesema Ibn Abbaas رضي الله عنهما: “Ni ardhi bila mimea, ambamo hakuna kinachomea.”<sup>1</sup> Na Kauli Yake:

﴿٤٥﴾ أَوْ يُصْبِحَ مَأْوَهَا غَوْرًا

**“Au maji yake yakadididmia.”**

Maana yake: Yakapotea kwenye ardhi, ambayo ni kinyume na yanayopita yakiwa yako juu ya ardhi. Hivyo, *Gha'ir* ni kwenda chini. Kama Alivyosema Allah تعالى:

﴿٤٦﴾ قُلْ أَرَأَيْتُمْ إِنْ أَصْبَحَ مَأْوُكُمْ غَوْرًا فَمَنْ يَأْتِيكُمْ بِمَاءٍ مَّعِينٍ

**“Sema: Mnaonaje, kama maji yenu yakiwa yamezama (yamedididimia chini), basi nani Atakuleteeni maji safi yatiririkao?” (67:30),**

Maana yake: Maji yanayotiririka kila upande. Na hapa Allah تعالى Anasema:

﴿٤٧﴾ أَوْ يُصْبِحَ مَأْوَهَا غَوْرًا فَلَنْ تَسْتَطِيعَ لَهُدَّ طَلَبًا

**“Au maji yake yakadididmia wala usiweze kuyagundua”.**

Neno “*Ghawr*” katika sarufi ya kiarabu ni kutoka mzizi wa neno “*maswdar*” (chimbuko) moja na *Gha'ir* na ina maana moja, lakini yenye nguvu na kutilia mkazo zaidi.

﴿٤٨﴾ وَأُحِيطَ بِشَمْرِهِ، فَأَصْبَحَ يُقَلِّبُ كَفَيْهِ عَلَىٰ مَا أَنفَقَ فِيهَا وَهِيَ خَاوِيَةٌ عَلَىٰ عُرُوشِهَا وَيَقُولُ

﴿٤٩﴾ يَلَيْتَنِي لَمْ أَشْرِكْ بِرَبِّي أَحَدًا ۚ وَلَمْ تَكُنْ لَهُدًى فِتْنَةٌ يَنْصُرُونَهُ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَمَا كَانَ

﴿٥٠﴾ مُنْتَصِرًا ۚ هُنَالِكَ الْوَلَايَةُ لِلَّهِ الْحَقِّ ۚ هُوَ خَيْرٌ نَوَابًا وَخَيْرٌ عُقْبًا

<sup>1</sup> At-Tabari 18:26.

**42. Yakateketezwa matunda yake, akabaki akipindua pindua viganja vyake, kwa vile alivyoyagharimia, na miti imebwagika juu ya chanja zake. Akawa anasema: Laiti nisingelimshiriki Mola wangu Mlezi na yeyote!**

**43. Wala hakuwa nacho kikundi cha kumsaidia badala ya Allah, wala mwenyewe hakuweza kujisaidia.**

**44. Huko ulinzi ni wa Allah wa Haki tu. Yeye Ndiye Mbora wa malipo, na Mbora wa matokeo.**

### Matokeo Mabaya ya Ukafiri

Anasema Aliyetukuka:

وَأُحِيطَ بِثَمَرِهِ

**“Yakateketezwa matunda yake.”**

Maana yake: Mali yake, au kulingana na kauli nyengine, mazao na matunda yake. Kusudio ni kuwa yale aliyoyahofia kafiri huyu na aliyotishwa na Muumini yule ndio yaliyotokea. Kimbunga kilipiga kwenye bustani lake, ambalo kimakosa alidhania litabakia daima dawamu, hivyo bustani hilo likamuhadaa na kumzuia yeye kumfikiria Allah تعالى. Hivyo,

فَأَصْبَحَ يُقَلِّبُ كَفَّيْهِ عَلَىٰ مَا أَنفَقَ

**“Akabaki akipindua pindua viganja vyake, kwa vile alivyoyagharimia”.**

Na amesema Qataadah: “Alikuwa akifumbata mikono yake kwa ishara ya majuto na huzuni kwa mali iliyopotea.”

وَيَقُولُ يَلَيْتَنِي لَمْ أُشْرِكْ بِرَبِّي أَحَدًا ﴿٣٧﴾ وَلَمْ تَكُن لَّهُ فِئَةٌ

**“Akawa anasema: Laiti nisingelimshiriki Mola wangu Mlezi na yeyote! Wala hakuwa nacho kikundi.”<sup>1</sup>**

Maana yake: Ukoo au watoto, kama alivyokuwa akijifakhiri,

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:27.

يَنْصُرُونَهُ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَمَا كَانَ مُنتَصِرًا ﴿٤٣﴾ هُنَالِكَ الْوَلِيَّةُ لِلَّهِ الْحَقِّ

**“Cha kumsaidia badala ya Allah, wala mwenyewe hakuweza kujisaidia. Huko Ulinzi ni wa Allaah wa Haki tu.”**

Hapa wametofautiana wasomi wa Qur’ani ‘Maqari’ katika kisomo. Wapo miongoni mwao wanaosimama, kwa kufanya kituo pindi wanaposoma:

وَمَا كَانَ مُنتَصِرًا ﴿٤٣﴾ هُنَالِكَ

**“Wala mwenyewe hakuweza kujisaidia. Huko.”**

Maana yake: Katika wakati huo, pale Allah تعالى Anapoleta adhabu juu yake, hakuna atakayemnusuru. Kisha wanaanza tena kusoma kwa Kauli Yake:

الْوَلِيَّةُ لِلَّهِ الْحَقِّ

**“Ulinzi ni wa Allah wa Haki tu”.**

Wengine wanasimama kwa kufanya kituo pindi wanaposoma kwenye ibara:

وَمَا كَانَ مُنتَصِرًا ﴿٤٣﴾

**“Wala mwenyewe hakuweza kujisaidia.”**

Na anaanza kwa Kauli Yake:

هُنَالِكَ الْوَلِيَّةُ لِلَّهِ الْحَقِّ

**“Huko Ulinzi ni wa Allaah wa Haki tu.”**

Kisha wakatofautiana katika kulisoma neno, “Al-Walaayah”, hivyo maana ikawa Utiifu kwa Allah تعالى. Maana: Siku ya Kiyama, kila mmoja, Muumini na Kafari atarudi kwa Allah تعالى, kwa utiifu na unyenyekevu Kwake pindi adhabu itakapotolewa, kama ilivyo katika Kauli Yake:

فَلَمَّا رَأَوْا بَأْسَنَا قَالُوا ءَامَنَّا بِاللَّهِ وَحَدَّهُ وَكَفَرْنَا بِمَا كُنَّا بِهِ مُشْرِكِينَ ﴿٤٤﴾

**“Walipoiona Adhabu Yetu walisema: ‘Tunamuamini Allah kuwa ni wa Peke Yake na tunaikanusha miungu tuliokuwa tukiishirikisha Naye.’ (40:84)**

Na kama ilivyo katika Kauli Yake katika Kutupa habari ya Firauni:

حَتَّىٰ إِذَا أَدْرَكَهُ الْغَرَقُ قَالَ ءَأَمِنْتُ أَنَّهُ لَآ إِلَهَ إِلَّا الَّذِي ءَأَمَنْتُ بِهِم بَنُو إِسْرَائِيلَ  
وَأَنَا مِنَ الْمُسْلِمِينَ ﴿٩١﴾ ءَأَلْفَنُ وَقَدْ عَصَيْتَ قَبْلُ وَكُنْتَ مِنَ الْمُفْسِدِينَ ﴿٩٢﴾

**“Hata kulikomfikia Firauni kuzama alisema: ‘Naamini ya kwamba hakuna aabudiwaye kwa haki ila Yule wanayemuamini wana wa Israili, na mimi ni miongoni mwa wanaotii’. Malaika wakamuambia: ‘Sasa, hali uliasi kabla ya hapo na ukawa miongoni mwa waharibifu.” (10:90-91).**

Na wengine wanaisoma kama *Al-Wilaayah*, kumaanisha kuwa siku hiyo Hukumu itakuwa kwa Allah تعالى tu, Allah تعالى wa Kweli. Na wengine wenye kuisoma *Al-Haqqu*, kumaanisha *Al-Wilaayah*, kama katika Kauli ya Aliyetukuka:

الْمَلِكُ يَوْمَئِذٍ الْحَقُّ لِلرَّحْمَنِ ؕ وَكَانَ يَوْمًا عَلَى الْكَافِرِينَ عَسِيرًا ﴿٢٦﴾

**“Ufalme wa haki siku hiyo utakuwa wa Mwingi wa Rehema, na itakuwa ni siku ngumu kwa makafiri.” (25:26).**

Na wengine wakaisoma kama *Al-Haqqi*, kumaanisha Allah تعالى, Ndiye Anayekusudiwa. Kama katika Kauli Yake:

ثُمَّ رُدُّوْا إِلَى اللَّهِ مَوْلَاهُمُ الْحَقِّ ؕ

**“Kisha watarudishwa kwa Allah, Mola wao wa Haki.” (6:62).**

Kwa hiyo Akasema تعالى:

هُوَ خَيْرٌ ثَوَابًا

**“Yeye Ndiye Mbora wa malipo.”** Maana yake: Jaza na malipo.

وَخَيْرٌ عُقْبًا ﴿٤٤﴾

**“Na mbora wa matokeo.”** Maana yake: Amali ambazo zimefanywa kwa ajili ya Allah تعالى, thawabu zake zitakuwa nzuri, na hatima yake pia itakuwa njema. Zote ni kheri.

وَأَضْرَبَ لَهُمْ مَثَلًا الْحَيَاةِ الدُّنْيَا كَمَا أَنْزَلْنَاهُ مِنَ السَّمَاءِ  
 فَاخْتَلَطَ بِهِ نَبَاتُ الْأَرْضِ فَأَصْبَحَ هَشِيمًا تَذْرُوهُ  
 وَالرِّيحُ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ مُّقْتَدِرًا ﴿٤٥﴾ أَمْالُ  
 وَالْبُنُونَ زِينَةُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۗ وَالْبَاقِيَاتُ الصَّالِحَاتُ خَيْرٌ  
 عِندَ رَبِّكَ ثَوَابًا وَخَيْرٌ أَمَلًا ﴿٤٦﴾ وَيَوْمَ نُسَيِّرُ الْجِبَالَ وَتَرَى  
 الْأَرْضَ بَارِزَةً وَحَشَرْنَاهُمْ فَلَمْ نُغَادِرْ مِنْهُمْ أَحَدًا ﴿٤٧﴾  
 وَعَرَضُوا عَلَىٰ رَبِّكَ صَفًا لَقَدْ جِئْتُمُونَا كَمَا خَلَقْنَاكُمْ أَوَّلَ  
 مَرَّةٍ ۗ بَلْ زَعَمْتُمْ أَلَّنْ نَجْعَلَ لَكُمْ مَوْعِدًا ﴿٤٨﴾ وَوَضِعَ  
 الْكِتَابَ فَتَرَى الْمُجْرِمِينَ مُشْفِقِينَ مِمَّا فِيهِ وَيَقُولُونَ  
 يَا وَيْلَتَنَا مَالِ هَذَا الْكِتَابِ لَا يُغَادِرُ صَغِيرَةً وَلَا كَبِيرَةً  
 إِلَّا أَحْصَاهَا ۗ وَوَجَدُوا مَا عَمِلُوا حَاضِرًا ۗ وَلَا يَظْلِمُ رَبُّكَ  
 أَحَدًا ﴿٤٩﴾ وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا  
 إِبْلِيسَ كَانَ مِنَ الْجِنِّ فَفَسَقَ عَنْ أَمْرِ رَبِّهِ ۗ أَفَتَتَّخِذُونَهُ  
 وَذُرِّيَّتَهُ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِي وَهُمْ لَكُمْ عَدُوٌّ بِئْسَ لِلظَّالِمِينَ  
 بَدَلًا ﴿٥٠﴾ \* مَا أَشْهَدُكُمْ خَلْقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلَا  
 خَلْقِ أَنْفُسِهِمْ وَمَا كُنْتُمْ مُتَّخِذِ الْمُضِلِّينَ عَضُدًا ﴿٥١﴾  
 وَيَوْمَ يَقُولُ نَادُوا شُرَكَاءِيَ الَّذِينَ زَعَمْتُمْ فَدَعَوْهُمْ فَلَمْ  
 يَسْتَجِيبُوا لَهُمْ وَجَعَلْنَا بَيْنَهُمْ مَوْبِقًا ﴿٥٢﴾ وَرَأَى الْمُجْرِمُونَ  
 النَّارَ فَظَنُّوا أَنَّهُمْ مُوَافِعُوهَا وَلَمْ يَجِدُوا عِنْدَهَا مَصْرَفًا ﴿٥٣﴾

وَأَضْرَبَ لَهُمْ مَثَلًا الْحَيَاةِ الدُّنْيَا  
 كَمَا أَنْزَلْنَاهُ مِنَ السَّمَاءِ فَاخْتَلَطَ  
 بِهِ نَبَاتُ الْأَرْضِ فَأَصْبَحَ هَشِيمًا  
 تَذْرُوهُ الرِّيحُ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ  
 شَيْءٍ مُّقْتَدِرًا ﴿٤٥﴾ أَمْالُ  
 وَالْبُنُونَ زِينَةُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۗ  
 وَالْبَاقِيَاتُ الصَّالِحَاتُ خَيْرٌ  
 عِندَ رَبِّكَ ثَوَابًا  
 وَخَيْرٌ أَمَلًا ﴿٤٦﴾

**45. Na wapigie mfano wa maisha ya dunia. Hayo ni kama maji Tunayoya-teremsha kutoka mbinguni, yakachanganyika na mimea ya ardhi, kisha hiyo mimea ikawa vibuwa vina-vyopeperushwa na upepo. Na Allah ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu.**

**46. Mali na wana ni pambo la maisha ya dunia. Na mema yanayobakia ni bora mbele ya Mola Wako Mlezi kwa malipo, na bora kwa matumaini.**



**Hadithi inayofundisha Maadili Mema katika Maisha ya Dunia**

Anasema Aliyetukuka:

وَأَضْرَبَ لَهُمُ

**“Na wapigie.”**

Kwa watu, ewe Muhammad ﷺ,

مَثَلِ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا

**“Mfano wa maisha ya dunia.”**

Katika maumbile yake kupita, kumalizika na kufikia kikomo (mwisho). Mfano wake,

كَمَا أَنْزَلْنَاهُ مِنَ السَّمَاءِ فَاخْتَلَطَ بِهِ نَبَاتُ الْأَرْضِ

**“Hayo ni kama maji Tunayoyateremsha kutoka mbinguni, yakachanganyika na mimea ya ardhi.”**

Maana yake: Inachanganyika na nafaka (chembe chembe) zilizomo katika ardhi, hivyo zikamea na kuwa nzuri na zikatoa maua yanayong’aa na katika hali nzuri (freshi), kisha baada ya hapo,

فَأَصْبَحَ هَشِيمًا

**“Hiyo mimea ikawa vibuwa.”** Kavu na kunyauka.

تَذُوقُهُ الرِّيحِ

**“Vinapeperushwa na upepo.”**

Maana yake: Kusukika sukika kuliani na kushotoni, na hakika ni kuwa:

وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ مُّقْتَدِرًا ﴿٥٣﴾

**“Na Allah ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu.”**

Maana yake: Yeye Ana Uweza na Nguvu ya Kufanya haya na yale. Na mara nyingi Allah تعالیٰ Anatupigia mifano ya maisha ya duniani kwa mfano huu, Kama Alivyosema Aliyetukuka katika *Suratu Yunus*:

إِنَّمَا مَثَلُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا كَمَاءٍ أَنْزَلْنَاهُ مِنَ السَّمَاءِ فَاخْتَلَطَ بِهِ نَبَاتُ الْأَرْضِ مِمَّا يَأْكُلُ  
النَّاسُ وَالْأَنْعَامُ

***“Hakika mfano wa maisha ya dunia ni kama maji Tuliyoateremsha kutoka mbinguni; kisha mimea ya ardhi wanayoila watu na wanyama ikachanganyika nayo.” (10:24).***

Na Akasema katika *Suratu Zumar*:

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَسَلَكَهُ يَنْبِيعَ فِي الْأَرْضِ ثُمَّ يُخْرِجُ بِهِ زَرْعًا  
مُخْتَلِفًا أَلْوَانُهُ

***“Je, huoni kwamba Allah Ameteremsha maji kutoka mbinguni. Kisha Akayapitisha chini kwa chini, yakawa chemchem katika ardhi, tena Akaotesha kwayo mimea ya rangi mbali mbali?” (39:21).***

Na Akasema katika *Suratul Hadid*:

اعْلَمُوا أَنَّمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا لَعِبٌ وَهُوَ زِينَةٌ وَتَفَاخُرٌ بَيْنَكُمْ وَتَكَاثُرٌ فِي الْأَمْوَالِ وَالْأَوْلَادِ  
كَمَثَلِ غَيْثٍ أَعْجَبَ الْكُفَّارَ نَبَاتُهُ

***“Jueni ya kwamba maisha ya dunia ni mchezo, na pumbao, na pambo, na kujifakhirisha baina yenu na kushindana kwa wingi wa mali na watoto. Mfano wake ni kama mvua ambayo huwafurahisha wakulima mimea yake...” (57:20).***

Na katika Hadithi Sahihi:

«الدُّنْيَا حُلْوَةٌ خَضِرَةٌ»

*“Dunia ni tamu na kijani.”<sup>1</sup>*

<sup>1</sup> Muslim 4:2098.

**Baina ya Mali, Watoto na Amali Njema**

Na Kauli Yake:

أَمْالٌ وَأَلْبُنُونَ زِينَةُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا

**“Mali na wana ni pambo la maisha ya dunia.”**

Kama Kauli Yake:

زُيِّنَ لِلنَّاسِ حُبُّ الشَّهَوَاتِ مِنَ النِّسَاءِ وَالْبَنِينَ وَالْقَنَاطِيرِ الْمُقَنْطَرَةِ مِنَ الذَّهَبِ

**“Watu wametiwa huba ya kupenda wanawake na watoto na mirundi ya dhahabu...” (3:14).**

Na Amesema Aliyetukuka:

إِنَّمَا أَمْوَالُكُمْ وَأَوْلَادُكُمْ فِتْنَةٌ وَاللَّهُ عِنْدَهُ أَجْرٌ عَظِيمٌ

**“Bila shaka mali zenu na watoto wenu ni jaribio kwenu. Na kwa Allah kuna ujira mkubwa kabisa.” (64:15),**

Maana: Kuelekea kwa Allah تعالى na kuwa faragha kwa ajili ya kumuabudu Yeye ni bora kwenu kuliko kujishughulisha nao na kukusanya mali kwa ajili yao na kuchupa mipaka katika kuwaonea huruma. Kwa ajili hiyo Akasema:

وَأَلْبَقَيْتُ الصَّلَاحَتُ حَيْرٌ عِنْدَ رَبِّكَ ثَوَابًا وَحَيْرٌ أَمَلًا

**“Na mema yanayobakia ni bora mbele ya Mola wako Mlezi kwa malipo, na bora kwa matumaini.”**

Amesema Ibn ‘Abbaas, Said bin Jubayr na wengine miongoni mwa *Salaf*: “Na mema yanayobakia”, Swala tano<sup>1</sup>. Na amesema ‘Atwaa’ bin Abi Rabaah na Sa’id bin Jubayr kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Amali njema inayodumu ni kuleta *Tasbiyh* (*Subhaanallaah*), *Tahmiyd* (*Alhamdulillaah*), *Tahliyl* (*Laa ilaaha ilaa Llaah*) na *Takbiyr* (*Allahu Akbar*)”<sup>2</sup>. Amiri wa Waumini,

<sup>1</sup> At-Tabari 18:32.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:33.

'Uthmaan bin 'Affaan رضي الله عنه aliulizwa, "Ni amali gani njema inayo dumu?" Alijibu: "Ni *Tahliyl, Tasbiyh, Tahmiyd, Takbiyr* na *Laa hawla wa laa quwwata illaa billaah al-'Aliyyil 'Adhiym.*" (Imepokewa na Imaam Ahmad)<sup>1</sup>.

Na amepokea Imaam Ahmad kutoka kwa mwachwa huru wa Mtume kuwa Mtume ﷺ amesema:

«بِخِ بَيْحِ لِحْمِيسٍ مَا أَثْقَلَهُنَّ فِي الْجِيزَانِ: لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاللَّهُ أَكْبَرُ، وَسُبْحَانَ اللَّهِ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ، وَالْوَلَدُ الصَّالِحُ يُتَوَفَّى فَيُخْتَبِئُهُ وَالِدُهُ - وَقَالَ: - بَيْحُ بَيْحِ لِحْمِيسٍ مَنْ لَقِيَ اللَّهَ مُسْتَيْقِنًا بِهِمْ دَخَلَ الْجَنَّةَ: يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ، وَبِالْجَنَّةِ وَالنَّارِ، وَبِالْبَغْتِ بَعْدَ الْمَوْتِ، وَبِالْحِسَابِ»

*"Fanyeni haraka (fanyeni vizuri)! Fanyeni haraka kwa mambo matano! Ni mazito yalioje katika mizani: Laa ilaaha illaa Llaahu Wallaahu Akbar wa Subhaanallaahu wal Hamdulillaahi, na mtoto mwema anayekufa na wazazi wake wakatarajia thawabu kutoka kwa Allah". Na akasema: "Fanyeni haraka! Fanyeni haraka kwa mambo matano! Yeyote atakayekutana na Allaah akiwa na yakini na Imani kwayo basi ataingia Peponi: Kumuamini Allah, Siku ya Mwisho, Pepo na Moto, kufufuliwa baada ya umauti na Malipo."*<sup>2</sup>

Amepokea 'Aliy bin Abi Twalhah kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema kuhusu Kauli ya Aliyetukuka:

وَالْبَقِيَّةُ الصَّلِيحَةُ

***"Na mema yanayobakia",***

Ni kumdhukuru Allah (kumtaja Allah); *Laa ilaaha illaa Llaahu, Allaahu Akbar, Subhaanallaah, na Alhamdulillaah, Tabaarakallaahu walaa Hawla walaa Quwwata illaa Billaah, na Astaghfirullaah*, kumswalia Mtume, Kufunga, Kuswali, Kuhiji, Sadaka, kuacha huru watumwa, Jihadi, kueneza udugu na amali zote njema. Haya ni mema yaliyobakia ambayo yatabakia na watu wake Peponi maadamu mbingu na ardhi zitabakia.<sup>3</sup> Amepokea Al-Awfi kuwa Ibn 'Abbas

<sup>1</sup> Ahmad 1:71.

<sup>2</sup> Ahmad 4:237.

<sup>3</sup> At-Tabari 18:35.

amesema: "Hayo ni maneno mazuri."<sup>1</sup> Na amesema 'Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam: "Hizo ni amali njema zote."<sup>2</sup> Hii pia ndiyo rai iliyochaguliwa na Ibn Jariir رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى Allah تعالى Amrehemu.

وَيَوْمَ نُسِيرُ الْجِبَالَ وَتَرَى الْأَرْضَ بَارِزَةً وَحَشَرْنَاهُمْ فَلَمْ نُغَادِرْ مِنْهُمْ أَحَدًا ﴿٤٧﴾ وَعَرَضُوا  
عَلَى رَبِّكَ صَفًا لَقَدْ جِئْتُمُونَا كَمَا خَلَقْنَاكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ بَلْ زَعَمْتُمْ أَلَّنْ نَجْعَلَ لَكُمْ مَوْعِدًا  
﴿٤٨﴾ وَوَضَعَ الْكِتَابَ فَفَتَى الْمُجْرِمِينَ مُشْفِقِينَ مِمَّا فِيهِ وَيَقُولُونَ يَا وَيْلَتَنَا مَالِ هَذَا  
الْكِتَابِ لَا يُغَادِرُ صَغِيرَةً وَلَا كَبِيرَةً إِلَّا أَحْصَاهَا وَوَجَدُوا مَا عَمِلُوا حَاضِرًا وَلَا يَظُنُّرُ  
رُبُّكَ أَحَدًا ﴿٤٩﴾

**47. Na siku Tutapoiondoa milima na ukaiona ardhi iwazi, na Tukawafufua - wala hatutamuacha hata mmoja kati yao.**

**48. Na wakahudhurishwa mbele ya Mola wako Mlezi kwa safu (wakaambiwa): Mmetujia kama Tulivyokuumbeni mara ya kwanza! Bali mlidai kwamba Hatutakuwekeeni miadi.**

**49. Na kitawekwa kitabu. Basi utawaona wakosefu wanavyoogopa kwa yale yaliomo humo. Na watasema: Ole wetu! Kitabu hichi kina nini! Hakiachi dogo wala kubwa ila huliandika? Na watayakuta yote waliyoyatenda yamehudhuria hapo. Na Mola wako Mlezi Hamdhulumu yeyote.**

### Vitisho Vikubwa vya Siku Kiyama

Allah تعالى Anatuelezea kuhusu hali za Siku ya Kiyama na yaliyomo katika mambo makubwa, kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَيَوْمَ تَمُورُ السَّمَاءُ مَوْرًا ﴿٥١﴾ وَتُسِيرُ الْجِبَالَ سِيرًا ﴿٥٢﴾

**"Siku zitakapotikisika mbingu kwa mtikiso. Na milima iwe inakwenda kwa mwendo mkubwa." (52:9-10)**

<sup>1</sup> At-Tabari 18:35. Sanadi yake ni dhaifu.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:35.

Maana yake: Wataondoka kutoka katika sehemu zao na kupotea. Hii ni kama Alivyosema Allah تعالى:

وَتَرَى الْجِبَالَ تَحْسِبُهَا جَamِدَةً وَهِيَ تَمُرُّ مَرَّ السَّحَابِ

**“Na unaiona milima unaidhania imetulia; nayo inakwenda kama mwendo wa mawingu.” (27:88)**

Na Amesema Aliyetukuka:

وَتَكُونُ الْجِبَالُ كَالْعِهْنِ الْمَنْفُوشِ

**“Na milima itakuwa kama sufi zilizochambuliwa!” (101:5).**

وَسَعَلُونَاكَ عَنِ الْجِبَالِ فَقُلْ يَنْسِفُهَا رَبِّي نَسْفًا

فَيَذَرُهَا قَاعًا صَفْصَفًا

لَا

تَرَى فِيهَا عِوَجًا وَلَا أَمْتًا

**“Na wanakuuliza khabari za milima. Waambie: Mola wangu Mlezi Ataivurugavuruga. Na Ataiacha tambarare, uwanda. Hutaona humo mdidimio wala muinuko.” (20:105-107).**

Allah تعالى Anatutajia kuwa Ataifanya milima ipotee na kusawazishwa (kuwa tambarare), na ardhi itaachwa kuwa, “Tambarare, uwanja mtupu.” Maana: itasawazishwa kabisa kusiwe na mididimiko wala miinuko. Hakutakuwa na mabonde wala milima.

Kwa hiyo, Akasema Aliyetukuka:

وَتَرَى الْأَرْضَ بَارِزَةً

**“Na ukaiona ardhi iwazi.”**

Maana yake: Bariza iliyo wazi, hakuna kabisa sehemu muhimu ambazo zinaweza kutambulikana na hakuna chochote cha kujifichia nyuma yake. Viumbe vyote vitaonekana na Mola wao Mlezi, na hakuna yeyote atakayeweza kujificha Kwake. Amesema Qataadah na Mujaahid:

وَتَرَى الْأَرْضَ بَارِزَةً

**“Na ukaiona ardhi iwazi.”**

‘Hakuna atakayejificha wala kukosekana.’<sup>1</sup> Na amesema Qataadah: ‘Hakutakuwa na majengo wala mimea.’<sup>2</sup> Na Kauli Yake:

وَحَشَرْنَاهُمْ فَلَمْ نُغَادِرْ مِنْهُمْ أَحَدًا ﴿٤٧﴾

**“Na Tukawafufua - wala hatutamuacha hata mmoja kati yao.”**

Maana yake: Tutawakusanya wote pamoja, wa mwanzo na wa mwisho, na hatutamuacha yeyote nyuma, mdogo wala mkubwa.

Kama Alivyosema Aliyetukuka:

قُلْ إِنَّ الْأَوَّلِينَ وَالْآخِرِينَ ﴿٤٩﴾ لَمَجْمُوعُونَ إِلَىٰ مِيقَاتِ يَوْمٍ مَّعْلُومٍ ﴿٥٠﴾

**“Sema: Hakika wa zamani na wa mwisho. Bila ya shaka watakusanywa kwa wakati wa siku maalumu.” (56:49-50).** Na,

ذَٰلِكَ يَوْمٌ مَّجْمُوعٌ لَّهُ النَّاسُ وَذَٰلِكَ يَوْمٌ مَّشْهُودٌ ﴿٥١﴾

**“Hakika katika haya ipo ishara kwa yule anayeogopa adhabu ya Akhera. Hiyo ndiyo Siku itakayokusanyiwa watu, na hiyo ndiyo Siku itakayoshuhudiwa.” (11:103)**

Na Kauli Yake:

وَعَرَّضُوا عَلَىٰ رَبِّكَ صَفًّا

**“Na wakahudhurishwa mbele ya Mola Wako Mlezi kwa safu.”**

Hii inaweza kumaanisha kuwa viumbe vyote watasimama mbele ya Allah Aliyetukuka katika safu moja. Kama Alivyosema Aliyetukuka:

يَوْمَ يَقُومُ الرُّوحُ وَالْمَلَائِكَةُ صَفًّا ۗ لَّا يَتَكَلَّمُونَ إِلَّا مَنْ أذِنَ لَهُ الرَّحْمَنُ وَقَالَ صَوَابًا ﴿٣٨﴾

**“Siku atakaposimama Roho na Malaika kwa safu. Hawatasema ila Mwingi wa rehema Aliyemruhusu, na atasema yaliyo sawa tu.” (78:38).**

<sup>1</sup> At-Tabari 18:36.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:36.

Na huenda pia ikawa watasimama safu kwa safu, kama Alivyosema:

وَجَاءَ رُؤُكَ وَالْمَلَكُ صَفًا صَفًا ﴿٤٧﴾

**“Na Akaja Mola wako Mlezi na Malaika safu safu.” (89:22).**

Na Kauli Yake:

لَقَدْ جَعَلْنَاكُمْ آوَّلَ مَرَّةٍ

**“Hakika mmetujia kama Tulivyokuumbeni mara ya kwanza!”**

Hili ni karipio kwa wenye kukataa Siku ya Mwisho (miadi), kemeo mbele ya viumbe wote.

Hii ndio sababu ya Allah تعالى Kuwaambia:

بَلْ زَعَمْتُمْ أَن لَّنْ نَّجْعَلَ لَكُم مَّوْعِدًا ﴿٤٨﴾

**“Bali mlidai kwamba Hatutakuwekeeni miadi.”**

Maana yake: Hamkudhania kuwa hili litatokea kwenu au litakuja kupita. Na Kauli Yake:

وَوُضِعَ الْكِتَابُ

**“Na kitawekwa kitabu.”**

Maana yake: Kitabu cha amali, kilicho na kumbukumbu ya kila kitu, mtukufu na dhalili, muhimu na isiyo na thamani, mdogo na mkubwa.

فَتَرَى الْمُجْرِمِينَ مَشْفِقِينَ مِمَّا فِيهِ

**“Basi utawaona wakosefu wanavyoogopa kwa yale yaliomo humo.”**

Maana yake: Katika amali mbaya na matendo maovu.

وَيَقُولُونَ يَا وَيْلَتَنَا

**“Na watasema: Ole wetu!”**

Maana yake: Ni hasara gani kwetu na ole wetu kwa kupoteza maisha yetu.



مَالٍ هَذَا أَلَكْتَبِ لَا يُغَادِرُ صَغِيرَةً وَلَا كَبِيرَةً إِلَّا أَحْصَاهَا<sup>٤</sup>

**“Kitabu hichi kina nini! Hakiachi dogo wala kubwa ila huliandika?”**

Maana: Hakiachi dhambi dogo, wala kubwa, wala amali yoyote ile hata iwe ndogo namna gani, “Ila huliandika.” Maana: limeshibitiwa na kuhifadhiwa.

وَوَجَدُوا مَا عَمِلُوا حَاضِرًا<sup>٥</sup>

**“Na watayakuta yote waliyoyatenda yamehudhuria hapo.”**

Maana yake: Ya kheri na shari. Kama Alivyosema Aliyetukuka:

يَوْمَ تَجِدُ كُلُّ نَفْسٍ مَّا عَمِلَتْ مِنْ خَيْرٍ مُّحْضَرًا

**“Siku ambayo kila nafsi itakuta mema iliyoyafanya yamehudhurishwa...” (3:30).**

Na Amesema Aliyetukuka:

يُنَبِّئُوا آلَ نَسْنُ يَوْمَئِذٍ بِمَا قَدَّمُوا وَآخِرًا ﴿١٣﴾

**“Siku hiyo ataambiwa aliyoyatanguliza na aliyoyaakhirisha.” (75:13).**

Na Amesema Aliyetukuka:

يَوْمَ تُبْلَى السَّرَائِرُ ﴿١٤﴾

**“Siku zitakapodhihirishwa siri.” (86:9)**

Maana yake: Kila kilichofichamana katika nyoyo za wanadamu kitajulikana. Amepokea Imaam Ahmad kutoka kwa Anas رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«لِكُلِّ غَادِرٍ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ يُعْرَفُ بِهِ»

**“Kila haini atakuwa na bendera Siku ya Kiyama, atakayojulikana nayo.”<sup>1</sup>**

Imepokewa katika Sahihi mbili, na katika lafudhi:

<sup>1</sup> Ahmad 3:142.

أُزْفَعُ لِكُلِّ غَادِرٍ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ عِنْدَ اسْتِهِ بِقَدْرِ غَدْرَتِهِ، يُقَالُ: هَذِهِ غَدْرَةُ فُلَانِ بْنِ فُلَانٍ،

*"Itanyanyuliwa Siku ya Kiyama kwa kila haini, bendera nyuma yake, kulingana na uhaini wake na kutasemwa, 'Huyu ni haini wa fulani bin fulani'<sup>1</sup>."*

Na Kauli Yake:

وَلَا يَظْلِمُ رَبُّكَ أَحَدًا ﴿٤٥﴾

***"Na Mola Wako Mlezi Hamdhulumu yeyote."***

Maana: Atawahukumu waja Wake kwa amali zao zote wala Hatamdholumu yeyote miongoni mwa viumbe Vyake. Bali Husamehe, Hughufiri madhambi na Huhurumia, na pia Anamuadhibu Amtakaye kwa Kudra, Hekima Yake na Uadilifu Wake, na Ataujaza Moto kwa makafiri na watu wa maasi. Kisha Atawatoa watu wa maasi na Kuwabakisha daima dawamu makafiri. Naye Ndiye Hakimu Ambaye Asiyedholumu wala Kunyanyasa. Amesema Aliyetukuka:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ وَإِنْ تَكَ حَسَنَةً يُّضَعِفْهَا

***"Hakika Allah Hadholumu hata uzito wa chembe moja. Na ikiwa ni jambo jema basi Yeye Hulizidisha." (4:40).***

Na Amesema:

وَنَضَعُ الْمَوَازِينَ الْقِسْطَ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ فَلَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا

***"Nasi Tutaweka mizani za uadilifu Siku ya Kiyama. Basi nafsi haitadhulumiwa kitu chochote..."*** Mpaka Kauli Yake:

حَسِبِينَ ﴿٤٧﴾

***"Washika hesabu." (21:47).***

Na Aya kuhusu suala hili ni nyingi sana.

Na amepokea Imam Ahmad kutoka kwa 'Abdallah bin Muhammad bin 'Aqil kuwa alimsikia Jaabir bin 'Abdallaah akisema: "Nilielezewa kuhusu Hadithi kutoka kwa mtu aliyemsikia Mtume ﷺ, hivyo nikanunua ngamia, nikamuweka sogi, kisha nikasafiri kwa mwezi mzima mpaka nikafika Shaam<sup>2</sup>, hapo

<sup>1</sup> Fat'hul-Baariy 12:354 na Muslim 3:1361.

<sup>2</sup> Syria Kubwa.

nikakutana na 'Abdallaah bin Unays. Nikamuambia mlinzi mlangoni: 'Muambia kuwa Jaabir yu mlangoni'. Akasema: 'Jaabir bin 'Abdallah?' Nikasema: 'Ndio'. Hivyo, akaja nje huku bado anavaa nguo yake, na kunikumbatia, nami nikamkumbatia, akasema: 'Imenifikia Hadithi iliyopokewa nawe, kuwa umemsikia Mtume ﷺ akizungumza kuhusu kisasi. Nikahofia nisije nikaaga dunia au nikafa kabla kuisikia'. Akasema: 'Nimemsikia Mtume ﷺ akisema:

«يُخْسِرُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ النَّاسَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ - أَوْ قَالَ: الْعِبَادَ - عُرَاءَ غُرْلًا بُهْمًا»

*'Allah Aliyetukuka Atawakusanya watu – au waja Wake – Siku ya Kiyama, wakiwa uchi, hawajatahiriwa na Buhman'. Nikauliza: 'Buhman ni nini?' Akasema:*

لَيْسَ مَعَهُمْ شَيْءٌ، ثُمَّ يُتَادِيهِمْ بِصَوْتٍ يَسْمَعُهُ مَنْ بَعْدَ كَمَا يَسْمَعُهُ مَنْ قَرُبَ: أَنَا الْمَلِكُ، أَنَا الدَّيَّانُ لَا يَتَّبِعِي لِأَحَدٍ مِنْ أَهْلِ النَّارِ أَنْ يَدْخُلَ النَّارَ وَلَهُ عِنْدَ أَحَدٍ مِنْ أَهْلِ الْجَنَّةِ حَقٌّ حَتَّى أُقِصَّهُ مِنْهُ، وَلَا يَتَّبِعِي لِأَحَدٍ مِنْ أَهْلِ الْجَنَّةِ أَنْ يَدْخُلَ الْجَنَّةَ وَلَهُ عِنْدَ رَجُلٍ مِنْ أَهْلِ النَّارِ حَقٌّ حَتَّى أُقِصَّهُ مِنْهُ حَتَّى اللَّطْمَةُ،

*'Hawatakuwa na chochote. Kisha sauti itawaita itakayosikika na hata walio mbali kwa usahali kabisa kama na wale walio karibu: Mimi Ndiye Mfalme, Nami Ndiye Hakimu. Haifalii kwa mtu wa Motoni kuingia Motoni, ikiwa anadaiwa na mmoja wa watu wa Peponi, mpaka Nichukue haki yake kutoka kwake. Na hakuna mtu yeyote wa Peponi ataingia Peponi ikiwa adaiwa na mmoja kati ya watu wa Motoni mpaka Nichukue haki kutoka kwake, hata likiwa ni kofi.'*

Tukasema: 'Itakuwaje hivyo, ikiwa tumekuja mbele ya Allah تعالى tukiwa hatukuvaa viatu, uchi, hatujatahiriwa na Buhman?' Akasema:

«بِالْحَسَنَاتِ وَالسَّيِّئَاتِ»

*'Kwa (ustahili) wa matendo mema na maovu.'*<sup>1</sup>

Na imepokewa na Shu'bah kutoka kwa A-'Awwaam bin Muzaahim kutoka kwa Abu 'Uthmaan kutoka kwa 'Uthman bin 'Affan رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

<sup>1</sup> Ahmad 3:495.

«إِنَّ الْجَمَاءَ لَتَنْتَصُرُنَّ مِنَ الْفِرْنَاءِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

*“Hakika mnyama aliyekosa pembe atamlipiza kisasi mwenye nayo Siku ya Kiyama.”<sup>1</sup>*

Amepokea ‘Abdallaah, mwana wa Imaam Ahmad, na zipo riwaya zinazoshuhudia kwa njia nyengine (Isnadi tofauti).

وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلٰٓئِكَةِ اسْجُدُوْا لِاٰدَمَ فَسَجَدُوْۤا اِلَّاۤ اِبْلِيسَ كَانَ مِنَ الْجٰنِّ فَفَسَقَ عَنۢۢ اَمْرِ رَبِّهٖۤ

۞ اَفَتَتَّخِذُوْنَہٗ وَاٰوِيٰٓتَہٗۤ اَوْلِيَآءَ مِنْ دُوْنِیْ وَہُمْ لَکُمْ عَدُوٌّۭۤ اَبْسَ لِلظَّٰلِمِیْنَۤ بَدَلًاۙ

**50. Na Tulipowaambia Malaika: Msujudieni Adam! Walimsujudia isipokuwa Iblisi. Yeye alikuwa miongoni mwa majini, na akavunja Amri ya Mola Wake Mlezi. Je! Mnamshika yeye na dhuriya zake kuwa marafiki badala Yangu, hali wao ni adui zenu? Ni ovu mno badala hii kwa wenye kudhulumu.**

**Kisa cha Adam عليه السلام na Ibilisi**

Allah تعالیٰ Anawatanabahisha wana wa Adam عليه السلام kuhusu uadui wa Iblisi kwao na baba yao kabla yao, na Kuwakemea wale wanaomfuata na kwenda kinyume na Muumba na Bwana wao. Yeye Ndiye Aliyewaumba na Kuwaanzisha pasi na chochote, Kuwadumisha na Kuwaruzuku kwa Huruma Yake, hata hivyo wakamchukua Ibilisi kuwa rafiki yao na kutangaza uadui wao kwa Allah تعالیٰ. Hivyo Akasema Aliyetukuka:

وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلٰٓئِكَةِ

**“Na Tulipowaambia Malaika.”**

Maana: Malaika wote, kama ilivyotajwa mwanzo wa *Suratul Baqarah*<sup>2</sup>,

اسْجُدُوْا لِاٰدَمَ

**“Msujudieni Adam.”**

Maana yake: Sijda ya heshima, kumkirimu na utukufu. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

<sup>1</sup> Zawaa'id Al-Musnad 1:12.

<sup>2</sup> Tizama mjalada wa kwanza, Tafsiri ya Suratul Baqarah, 2:36.

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَائِكَةِ إِنِّي خَلِيقٌ بَشَرًا مِّنْ صَلْصَلٍ مِّنْ حَمَلٍ مَّسْنُونٍ ﴿٢٨﴾ فَإِذَا سَوَّيْتُهُ  
وَنَفَخْتُ فِيهِ مِن رُّوحِي فَقَعُوا لَهُ سَاجِدِينَ ﴿٢٩﴾

**“Na Mola Wako Mlezi Alipowaambia Malaika: Hakika Mimi Nitamuumba mtu kwa udongo unaotoa sauti, unaotokana na matope yaliyotiwa sura. Basi Nitakapomkamilisha na Nikampulizia roho Yangu, basi mumuangukie kumsujudia.” (15:28-29)**

Na Kauli Yake:

فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ كَانَ مِنَ الْجِنِّ

**“Walimsujudia isipokuwa Iblisi. Yeye alikuwa miongoni mwa majini.”**

Maana: Alikhiniwa na asili yake. Alikuwa ameumbwa kutokana na moto usiokuwa na moshi, ilhali Malaika wameumbwa na nuru, kama ilivyothibiti katika Sahihi Muslim kutoka kwa ‘Aishah رضي الله عنها kuwa Mtume ﷺ amesema:

«خُلِقَتِ الْمَلَائِكَةُ مِنْ نُورٍ، وَخُلِقَ إِبْلِيسُ مِنْ مَّارِجٍ مِنْ نَّارٍ، وَخُلِقَ آدَمُ مِمَّا وُصِفَ لَكُمْ»

**“Malaika wameumbwa na nuru na Iblisi ameumbwa na moto usio na moshi na Adam naye ameumbwa kama mlivyosifiwa.”<sup>1</sup>**

Wakati wa haja, na mambo yakawa katika hali ngumu, kila chombo kinavuja kilicho nacho na kinakhiniwa na maumbile ya kweli. Iblisi alikuwa anafanya wanayofanya Malaika na akafanana nao katika kufanya Ibadah tofauti, hivyo akajumlishwa walipoagizwa (walipohutubiwa), lakini aliasi na kwenda kinyume na alichambiwa. Hivyo, Allah تعالى Anatuashiria hapa kuwa yeye alikuwa miongoni mwa majini, yaani ameumbwa na moto. Kama Alivyosema:

أَنَا خَيْرٌ مِنْهُ خَلَقْتَنِي مِنْ نَّارٍ وَخَلَقْتَهُ مِنْ طِينٍ ﴿٣٨﴾

**“Akasema: Mimi ni bora kuliko yeye. Umeniumba kwa moto, na yeye Umemuumba kwa udongo.” (38:76).**

Al-Hasan Al-Baswriy رحمه الله تعالى amesema : “Iblisi hakuwa mmoja wa Malaika kabisa hata kwa upepeso wa jicho. Yeye alikuwa na asili ya Kijini kama vile Adam عليه السلام, alivyo na asili ya wanadamu”. Imepokewa na Ibn Jariir رحمه الله تعالى kwa Isnadi iliyo Sahihi<sup>2</sup>.

<sup>1</sup> Muslim 4:2294.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:506.

Na Kauli Yake:

فَفَسَقَ عَنْ أَمْرِ رَبِّهِ ۗ

**“Na akavunja amri ya Mola wake Mlezi.”**

Maana: Akatoka, katika utii wa Allah تعالى, kwani neno ufasiki lina maana ya kutoka. Panasemwa: *Fasaqat Rutwbah* ina maana ya tende zinapotoka kutoka katika ua lake; na *Fasaqat Al-Fa'arah*, pindi panya anapotoka katika shimo lake kwa ajili ya kutafuta chakula na kufanya uharibifu.

Kisha Akasema Aliyetukuka, kwa Kukejeli na Kuwakemea wenye kumfuata na kumtii Iblisi:

أَفَتَتَّخِذُونَهُ وَذُرِّيَّتَهُ أَوْلِيَاءَ مِنْ دُونِي

**“Je! Mnamshika yeye na dhuriya zake kuwa marafiki badala Yangu.”**

Maana yake: Badala Yangu. Kwa hiyo Akasema:

بئسَ لِلظَّالِمِينَ بَدَلًا

**“Ni ovu mno badala hii kwa wenye kudhulumu.”**

Hii ni kama Aya katika *Surat Yaasin*, ambapo baada ya kutaja Kiyama na hali zake za utisho na hatima ya kila moja katika makundi mawili, waliofaulu na waliohasirika.

Allah تعالى Anasema:

وَأَمْتَرُوا الْيَوْمَ أَيُّهَا الْمَجْرُمُونَ ﴿٥٩﴾

**“Na enyi wakosefu! Jitengeni leo!”** Hadi,

أَفَلَمْ تَكُونُوا تَعْقِلُونَ ﴿٦٠﴾

**“Je, hamkuwa mkifikiri?” (36:59-62).**

\* مَا أَشْهَدُهُمْ خَلْقَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَلَا خَلْقَ أَنْفُسِهِمْ وَمَا كُنْتُمْ مُتَّخِذَ الْمُضِلِّينَ

عَضُدًا ﴿٦١﴾

**51. Sikuwashuhudisha Kuumbwa kwa mbingu na ardhi, wala Kuumbwa kwa nafsi zao. Wala Sikuwafanya wapotezao kuwa ni wasaidizi.**

## Miungu ya Washirikina Hawakushuhudia Uumbaji wa Chochote hata Wao Wenyewe

Anasema Aliyetukuka: “Hawa ambao mmewachukua kuwa ndio wasaidizi wenu badala Yangu ni viumbe kama nyinyi. Hawamiliki chochote, hata hawakushuhudia Uumbaji wa mbingu na ardhi, kwani hawakuwepo wakati huo”. Anasema Aliyetukuka: “Mimi ni Peke Yangu Ndiye Niliyesimamia Uumbaji wa vitu vyote na Ndiye Ninayevidhibiti vitu vyote na Kuvikadiria Peke Yangu. Sina katika hayo mshirika, waziri wala mshauri”. Hii ni kama Alivyosema:

قُلِ ادْعُوا الَّذِينَ زَعَمْتُمْ مِّنْ دُونِ اللَّهِ لَا يَمْلِكُونَ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ فِي السَّمَوَاتِ  
وَلَا فِي الْأَرْضِ وَمَا هُمْ فِيهِمَا مِنْ شِرْكٍَ وَمَا لَهُ مِنْ ظَهِيرٍ ﴿٤٥﴾ وَلَا تَنْفَعُ الشَّفَعَةُ  
عِنْدَهُ إِلَّا لِمَنْ أَذِنَ لَهُ ۗ

**“Sema: Waite mnaowadaia kuwa ni badala ya Allah. Hawamiliki hata uzito wa chembe hichi katika mbingu wala ardhi. Wala hawana ushirika wowote humo. Wala Yeye hana msaidizi miongoni mwao. Wala uombezi mbele yake hautafaa kitu, isipokuwa kwa Aliyempa Idhini.” (34:22-23).**

Kwa hivyo Akasema:

وَمَا كُنْتُمْ تُخِذُ الْمُضِلِّينَ عَضُدًا ﴿٤٦﴾

**“Wala sikuwafanya wapotezao kuwa ni wasaidizi.”**

Maalik amesema: “Wasaidizi”.

وَيَوْمَ يَقُولُ نَادُوا شُرَكَاءِيَ الَّذِينَ زَعَمْتُمْ فَدَعَوْهُمْ فَلَمْ يَسْتَجِيبُوا لَهُمْ وَجَعَلْنَا بَيْنَهُمْ  
مُؤَبِّقًا ﴿٤٧﴾ وَرءَا الْمَجْرُمُونَ النَّارَ فَظَنُّوا أَنَّهُمْ مُوَاقِعُوهَا وَلَمْ يَجِدُوا عِنَّا مَصْرِفًا ﴿٤٨﴾

**52. Na siku Atakaposema (Allah): Waiteni hao mliodai kuwa ni washirika Wangu. Basi watawaita, na wao hawatowaitikia. Nasi Tutaweka baina yao maangamio.**

**53. Na wakhalifu watauona Moto na watajua ya kwamba wao lazima wataingia humo; wala hawatapata pa kuuepuka.**

**Washirika wao Wameshindwa kujibu na Kuhudhurishwa Wahalifu Motoni**

Allah تعالى Anasema Akitupasha habari Atakavyowahutubia washirikina Siku ya Kiyama mbele ya viumbe wote kwa Kuwakamea na Kuwakaripia,

نَادُوا شُرَكَآئِيَ الَّذِينَ زَعَمْتُمْ

**“Waiteni hao mlidai kuwa ni washirika Wangu”,**

Maana yake: Ulimwenguni. Waiteni leo waje kuwasaidieni katika hali mliyomo ndani yake. Kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَلَقَدْ جِئْتُمُونَا فَرَادَى كَمَا خَلَقْنَاكُمْ أَوَّلَ مَرَّةٍ وَتَرَكْتُمْ مَا خَوَّلْنَاكُمْ وَرَاءَ ظُهُورِكُمْ<sup>ط</sup>  
وَمَا نَرَى مَعَكُمْ شُفَعَاءَكُمُ الَّذِينَ زَعَمْتُمْ أَنَّهُمْ فِيكُمْ شُرَكَؤُا<sup>ع</sup> لَقَدْ نَقَطَعَ بَيْنَكُمْ وَضَلَّ  
عَنْكُمْ مَا كُنْتُمْ تَزْعُمُونَ ﴿٦٩﴾

**“Nanyi mlitujia wapweke kama Tulivyokuumbeni mara ya kwanza. Na mkayaacha nyuma yenu yote Tuliyokupeni, na wala hatuwaoni hao waombezi wenu, ambao mlidai kuwa ni washirika wa Allaah kwenu. Yamekatika mahusiano baina yenu, na yamekupoteeni mliyokuwa mkidai.” (6:94).** Na Kauli Yake:

فَدَعَوْهُمْ فَلَمْ يَسْتَجِيبُوا لَهُمْ

**“Basi watawaita, na wao hawatowaitikia.”** Kama Alivyosema:

وَقِيلَ ادْعُوا شُرَكَآءَكُمْ فَدَعَوْهُمْ فَلَمْ يَسْتَجِيبُوا لَهُمْ

**“Na itasemwa: Waiteni hao miungu wa kishirikina wenu! Basi watawaita, lakini hawatowaitikia...” (28:64).** Amesema:

وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّن يَدْعُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ مَنْ لَا يَسْتَجِيبُ لَهُمْ

**“Na nani mpotofu mkubwa kuliko hao wanaowaomba, badala ya Allah, ambao hawatowaitikia...” (46:5)**

Mpaka mwisho wa Aya mbili. Na Amesema Aliyetukuka:

وَاتَّخَذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ إِلَهَةً لِيَكُونُوا لَهُمْ عِزًّا ﴿٧٠﴾ كَلَّا سَيَكْفُرُونَ بِعِبَادَتِهِمْ وَيَكُونُونَ

عَلَيْهِمْ ضِدًّا ﴿٧١﴾



***“Na wamechukua miungu mingine badala ya Allah ili ati iwape nguvu. Sivyo kabisa! Wataikataa hiyo ibada yao, na watakuwa ndio dhidi yao.” (19:81-82).***

Na Kauli Yake:

﴿٨١﴾ وَجَعَلْنَا بَيْنَهُم مَّوْبِقًا

***“Nasi Tutaweka baina yao maangamio.”***

Amesema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما, Qatadah na wengineo: “Maangamivu”.<sup>1</sup> Na maana ni kuwa Allah تعالى Amebaini kuwa hakuna njia kabisa kwa hawa washirikina wala hawatawafikia miungu yao waliokuwa wakidai hapa duniani. Hakika ni kuwa Atawatenganisha Akhera na hakuna atakayekuwa na uwezo wa kumfikia mwenziwe. Bali baina yao kutakuwa na maangamio, vituko na vitisho vikubwa na mambo makubwa. Ama kiwakilishi kilichopo katika Kauli Yake: ***“Baina yao”***, Kinarudi kwa Waumini na makafiri kama alivyosema ‘Abdallah bin ‘Amr, na kuwa watatenganishwa baina ya watu waongofu na wapotevu kwayo<sup>2</sup>. Hii ni kama Kauli ya Aliyetukuka:

﴿١٤﴾ وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ يُومِنُونَ يَتَفَرَّقُونَ

***“Na siku itaposimama Saa, siku hiyo watagawanyika.” (30:14)***

Na Amesema:

﴿٤٣﴾ يُومِنُونَ يَصِدُّونَ

***“Siku hiyo watatengana (watu wazuri wende Paponi na wabaya wende Motoni.” (30:43)***

Na Amesema Aliyetukuka:

﴿٥٩﴾ وَأَمْتَنُوا الْيَوْمَ أَيُّهَا الْمَجْرُمُونَ

***“Na enyi wakosefu! Jitengeni leo!” (36:59).***

Na Amesema Aliyetukuka:

﴿٣٠﴾ وَضَلَّ عَنْهُمْ مَا كَانُوا يَفْتُرُونَ

***“Na yote waliyokuwa wakiyazua yatawapotea.” (10:28-30).***

<sup>1</sup> At-Tabari 18:46.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:46.

Na Kauli Yake:

وَرَاءَ الْمُجْرِمُونَ النَّارَ فَظَنُّوا أَنَّهُمْ مُوَاقِعُوهَا وَلَمْ يَجِدُوا عَنْهَا مَصْرِفًا ۝

**“Na wakhalifu watauona Moto na watajua ya kwamba wao lazima wataingia humo; wala hawatapata pa kuuepuka.”**

Maana yake: Watakapouona Moto kwa macho yao, itakuwa inavutwa na hatamu elfu sabiini, kila hatamu ikivutwa na Malaika elfu sabiini.

وَرَاءَ الْمُجْرِمُونَ النَّارَ

**“Na wakhalifu watauona Moto.”**

Watahakikisha hilo bila wasiwasi, na kuwa wao wataingizwa ndani yake, na hilo litazidisha mfadhaiko, huzuni, wasiwasi na dhiki, kwa sababu ya hofu ya kutiwa adhabu kabla ya kutuka, ni adhabu kihakika. Na Kauli Yake:

وَلَمْ يَجِدُوا عَنْهَا مَصْرِفًا ۝

**“Wala hawatapata pa kuuepuka.”**

Maana yake: Hawatakuwa na njia ya kukimbia, hapana budi wakumbane nayo,

\* \* \*

وَلَقَدْ صَرَّفْنَا فِي هَذَا الْقُرْآنِ لِلنَّاسِ مِنْ كُلِّ مَثَلٍ ۚ  
 وَكَانَ الْإِنْسَانُ أَكْثَرَ شَيْءٍ جَدَلًا ۗ وَمَا مَنَعَ النَّاسَ  
 أَنْ يُؤْمِنُوا إِذْ جَاءَهُمُ الْهُدَىٰ وَيَسْتَغْفِرُوا رَبَّهُمْ إِلَّا أَنْ  
 تَأْتِيَهُمْ سُنَّةُ الْأَوَّلِينَ أَوْ يَأْتِيَهُمُ الْعَذَابُ قُبُلًا ۗ وَمَا  
 نُرْسِلُ الْمُرْسَلِينَ إِلَّا مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ ۚ وَيُجَادِلُ الَّذِينَ  
 كَفَرُوا بِالْبَاطِلِ لِيُدْحِضُوا بِهِ الْحَقَّ ۗ وَاتَّخَذُوا آيَاتِي وَمَا  
 أُنذِرُوا هُزُوًا ۗ وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ دُكِرَ بِآيَاتِ رَبِّهِ  
 فَأَعْرَضَ عَنْهَا وَنَسِيَ مَا قَدَّمَتْ يَدَاهُ ۗ إِنَّا جَعَلْنَا عَلَىٰ  
 قُلُوبِهِمْ أَكِنَّةً أَنْ يَفْقَهُوهُ وَفِي آذَانِهِمْ وَقْرًا ۗ وَإِنْ تَدْعُهُمْ  
 إِلَى الْهُدَىٰ فَلَنْ يَهْتَدُوا إِذًا أَبَدًا ۗ وَرَبُّكَ الْغَفُورُ ذُو  
 الرَّحْمَةِ ۗ لَوْ يُؤَاخِذُهُمْ بِمَا كَسَبُوا لَعَجَلْ لَهُمْ  
 الْعَذَابُ ۗ بَلْ لَهُمْ مَوْعِدٌ لَنْ يَجِدُوا مِنْ دُونِهِ مَوْعِدًا ۗ  
 وَتِلْكَ الْأَقْرَبُ ۗ أَهْلَكْنَهُمْ لَمَّا ظَنَّمُوا وَجَعَلْنَا لِمَهْلِكِهِمْ  
 مَوْعِدًا ۗ

وَلَقَدْ صَرَّفْنَا فِي هَذَا الْقُرْآنِ  
 لِلنَّاسِ مِنْ كُلِّ مَثَلٍ ۚ وَكَانَ  
 الْإِنْسَانُ أَكْثَرَ شَيْءٍ جَدَلًا ۗ

**54. Na bila ya shaka Tume-  
 waelezea watu katika  
 Qur’ani hii kila namna ya  
 mfano. Lakini mwanadamu  
 amezidi kuliko kila kitu kwa  
 ubishi.**

**Mifano Iliyopewa Kipau-  
 mbele Katika Qur’an**

Allah تعالیٰ Anasema:  
 “Hakika Tumewabainishia  
 watu katika Qur’ani hii, na  
 Tukawawekea wazi mambo  
 ili wasipotee kutoka katika  
 njia ya haki na kutoka katika  
 njia ya uongofu. Na pamoja  
 na bayana hii na kipamba-  
 nuzi, mwanadamu amekuwa  
 mwingi wa kujadili na kuwa

mbishi, kupinga ukweli kwa batili, isipokuwa kwa aliyeongozwa na Allah تعالیٰ  
 na Akampatia uoni kwa njia ya ufanisi na kufaulu. Amepokea Imaam Ahmad  
 kuwa ‘Ali bin Abi Twalib رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ aliwatembelea, yeye  
 na Fatima رضي الله عنها binti ya Mtume ﷺ usiku, akasema:

«أَلَا تَضَلَّان؟»

“Je, nyinyi hamuswali?”

Nikasema: “Ewe Mtume wa Allah تعالیٰ! Hakika nafsi zetu ziko Mikononi mwa  
 Allah تعالیٰ, Akitaka Kutuamsha Atatuamsha”. Aliondoka niliposema hayo wala

asinirudishie chochote. Kisha nikamsikia akiwa anatembea zake, akipiga paja lake, huku akisema:

وَكَانَ الْإِنْسَانُ أَكْثَرَ شَيْءٍ جَدَلًا ﴿١٨٧﴾

**“Lakini mwanadamu amezidi kuliko kila kitu kwa ubishi.”<sup>1</sup>**

Imepokewa katika Sahihi mbili<sup>2</sup>.

وَمَا مَنَعَ النَّاسَ أَنْ يُؤْمِنُوا إِذْ جَاءَهُمُ الْهُدَىٰ وَدَسْتَفَرُّوهُ رَبَّهُمْ إِلَّا أَنْ تَأْتِيَهُمْ سُنَّةٌ  
الْأُولَىٰ أَوْ يَأْتِيَهُمُ الْعَذَابُ قُبُلًا ﴿١٨٨﴾ وَمَا نُرْسِلُ الْمُرْسَلِينَ إِلَّا مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ ۗ وَمُجَادِلُ  
الَّذِينَ كَفَرُوا بِالْبَاطِلِ لِيُدْحِضُوا بِهِ الْحَقَّ ۗ وَاتَّخَذُوا آيَاتِي وَمَا أُنذِرُوا هُزُوًا ﴿١٨٩﴾

**55. Na hapana kilichowazuia watu kuamini ulipowajia uwongofu na wakaomba maghufira kwa Mola wao Mlezi, isipokuwa yawafikie ya wale wa zamani, au iwafikie adhabu jahara.**

**56. Na Hatuwatumi Mitume ila wawe wabashiri na waonyaji. Na waliokufuru wanabishana kwa uwongo, ili kwa uwongo huo waivunje kweli. Na wanazifanya Ishara Zangu na yale waliyoonywa kuwa ni mzaha.**

## Uasi wa Wasioamini

Allah تعالى Anatueleza kuhusu uasi wa makafiri, wa zamani na wa sasa, na kuikadhibisha kwao haki hata walipoona ishara na dalili za wazi kabisa. Hakuna kilichowakataza kufuata haki isipokuwa dai lao la kutaka kushuhudia kwa macho yao adhabu waliokuwa wakionywa nayo. Kama walivyosema hivyo kwa Mtume wao:

فَأَسْقِطْ عَلَيْنَا كِسْفًا مِّنَ السَّمَاءِ ۖ إِن كُنتَ مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿١٨٧﴾

**“Hebu tuangushie vipande kutoka mbinguni ikiwa wewe ni miongoni mwa wasemao kweli.” (26:187)**

<sup>1</sup> Ahmad 1:112.

<sup>2</sup> Fat’hul-Baariy 3:13 na Muslim 1:538.

Na wengine wakasema:

أَتَيْنَا بِعَذَابِ اللَّهِ إِنْ كُنْتَ مِنَ الصّٰدِقِينَ ﴿٢٩﴾

**“Tuletee adhabu hiyo ya Allah ikiwa wewe ni katika wasemao kweli.” (29:29)**

Na Makureshi wakasema:

اللَّهُمَّ إِنْ كَانَ هَذَا هُوَ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِكَ فَأَمْطِرْ عَلَيْنَا حِجَابًا مِنَ السَّمَاءِ أَوْ آتِنَا بِعَذَابِ الْيَمِّ ﴿٣٢﴾

**“...Ee Mwenyezi Mungu! Ikiwa haya ni kweli itokayo kwako basi tunyeshee mawe kutoka mbinguni, au tuletee adhabu yoyote iliyo chungu.” (8:32)**

وَقَالُوا يَا أَيُّهَا الَّذِي نُزِّلَ عَلَيْهِ الذِّكْرُ إِنَّكَ لَمَجْنُونٌ ﴿٦٧﴾

**“Na walisema: Ewe uliyeteremshiwa Ukumbusho! Hakika wewe ni mwendawazimu.” (15:6 -7)**

Na nyingine nyingi zisizokuwa hizo miongoni mwa Aya ambazo ni dalili katika hilo.

Kisha Akasema:

إِلَّا أَنْ تَأْتِيَهُمْ سُنَّةٌ الْأَوَّلِينَ

**“Isipokuwa yawafikie ya wale wa zamani.”**

Maana yake: Kufunikwa na adhabu, hivyo Kuwaangamiza kila mmoja wao hadi wa mwisho.

أَوْ يَأْتِيَهُمُ الْعَذَابُ قُبُلًا ﴿٦٨﴾

**“Au iwafikie adhabu jahara.”**

Maana yake: Wakaiona kwa macho yao wenyewe, wakikabiliana nayo uso kwa uso.

Kisha Akasema Aliyetukuka:

وَمَا تُرْسِلُ الْمُرْسَلِينَ إِلَّا مُبَشِّرِينَ وَمُنذِرِينَ ۚ

**“Na Hatuwatumi Mitume ila wawe wabashiri na waonyaji.”**

Maana yake: Kabla ya adhabu wanatoa bishara njema kwa wale wenye kuamini na kuwafuata, na onyo pamoja na tahadhari kwa wenye kukataa na kukanusha na kwenda kinyume nao.

Kisha Akatupasha habari kuhusu makafiri kwamba wao wanajali uwongo:

بِالْبَطِيلِ لِيُدْحِضُوا بِهِ الْحَقَّ ۚ

**“Ili kwa uwongo huo waivunje kweli.”**

Maana yake: Wajaribu kuidhoofisha haki iliyoletwa na Manabii, lakini hawawezi kufanikiwa katika hilo kabisa. Kisha Akasema Aliyetukuka:

وَأَخَذُوا آيَاتِي وَمَا أُنذِرُوا هُرُوءًا ﴿٥٧﴾

**“Na wanazifanya Ishara Zangu na yale waliyoonywa kuwa ni mzaha.”**

Maana yake: Wanachukulia dalili, ushahidi na miujiza iliyoletwa na Manabii kuwaonya na kuwahofisha wao juu ya adhabu.

هُرُوءًا ﴿٥٧﴾

**“Mzaha.”** Maana yake: Wanazifanyia dhihaka kuhusu hilo, ambayo ni aina mbaya kabisa ya kukadhibisha.

وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ دُكِرَ بِعَآيَتِ رَبِّهِ فَأَعْرَضَ عَنْهَا وَنَسِيَ مَا قَدَّمَتْ يَدَاهُ ۗ إِنَّا جَعَلْنَا عَلَىٰ

قُلُوبِهِمْ أَكِنَّةً أَنْ يَفْقَهُوهُ وَفِي آذَانِهِمْ وَقْرًا ۗ وَإِنْ تَدْعُهُمْ إِلَى الْهُدَىٰ فَلَنْ يَهْتَدُوا إِذًا

أَبَدًا ﴿٥٨﴾ وَرَبُّكَ الْغَفُورُ ذُو الرَّحْمَةِ ۗ لَوْ يُؤَاخِذُهُمْ بِمَا كَسَبُوا لَعَجَلْ لَهُمُ الْعَذَابَ

بَلْ لَهُمْ مَوْعِدٌ لَنْ يَجِدُوا مِنْ دُونِهِ مَوْيلًا ﴿٥٩﴾ وَتِلْكَ الْقُرَىٰ ۖ أَهْلَكْنَاهُمْ لَمَّا ظَمَمُوا

وَجَعَلْنَا لِمَهْلِكِهِمْ مَوْعِدًا ﴿٥٩﴾

**57. Na ni nani dhalimu mkubwa zaidi kuliko yule anayekumbushwa Ishara za Mola Wake Mlezi, naye akazipuuza na akasahau**

*yaliyotangulizwa na mikono yake? Hakika Sisi Tumeweka vifuniko juu ya nyoyo zao ili wasifahamu, na uziwi kwenye masikio yao. Na ukiwaita kwenye uwongofu hawakubali kabisa kuongoka.*

**58. Na Mola Wako Mlezi ni Msamehevu Mwenye Rehema. Lau Angeliwachukulia kwa mujibu kwa waliyoyachuma, bila ya shaka Angeliwafanyia haraka Kuwaadhibu. Lakini wanayo miadi ambayo hawatapata makimbilio yoyote ya kuepukana nayo.**

**59. Na miji hiyo Tuliwaangamiza watu wake walipodhulumu. Na Tukawawekea miadi ya maangamizo yao.**

### **Watu Wabaya Zaidi na Waliodhulumu Zaidi ni Wenye Kukengeuka baada ya Kukumbushwa**

Anasema Aliyetukuka: Na ni waja Wangu wapi wenye kujidhulumu zaidi kuliko yule mwenye kukumbushwa Ishara za Allah تعالى na akakengeuka. Maana: anazipuuza na kuzipa nyongo wala hazitilii maanani,

وَنَسِيَ مَا قَدَّمَتْ يَدَاهُ

**“Na akasahau yaliyotangulizwa na mikono yake?”**

Maana yake: Miongoni mwa amali mbaya na matendo maovu.

إِنَّا جَعَلْنَا عَلَى قُلُوبِهِمْ

**“Hakika Sisi Tumeweka juu ya nyoyo zao.”**

Maana yake: Mioyo ya watu hawa,

أَكِنَّةٌ

**“Vifuniko.”**

Maana yake: kufunika.

أَنْ يَفْقَهُوهُ

**“Ili wasifahamu.”**

Maana yake: Ili wasiweze kuifahamu Qur’ani na ujumbe wake ulio wazi kabisa.

وَفِي آذَانِهِمْ وَقْرًا ط

**“Na uziwi kwenye masikio yao.”**

Maana yake: Watakuwa viziwi kimaana kwa uongofu.

وَإِنْ تَدْعُهُمْ إِلَى الْهُدَى فَلَنْ يَهْتَدُوا إِذًا أَبَدًا ﴿٥٤﴾

**“Na ukiwaita kwenye uongofu hawakubali kabisa kuongoka.”**

Na Kauli Yake:

وَرَبُّكَ الْغَفُورُ ذُو الرَّحْمَةِ ط

**“Na Mola wako Mlezi ni Msamehevu Mwenye Rehema.”**

Maana yake: Mola wako Mlezi, ewe Muhammad ﷺ ni Msamehevu Mwenye Rehema pana na kubwa.

لَوْ يُؤَاخِذُهم بِمَا كَسَبُوا لَعَجَل لَهُمُ الْعَذَابُ ؕ

**“Lau Angeliwachukulia kwa mujibu waliyoyachuma, bila ya shaka Angeliwafanyia haraka Kuwaadhibu.”**

Kama Alivyosema:

وَلَوْ يُؤَاخِذُ اللهُ النَّاسَ بِمَا كَسَبُوا مَا تَرَكَ عَلَى ظَهْرهَا مِنْ دَابَّةٍ

**“Na lau kuwa Allah Angeliwachukulia watu kwa waliyoyachuma, basi Asingelimuacha juu ya ardhi hata kiumbe kimoja.” (35:45)**

Na Akasema:

وَإِنَّ رَبَّكَ لَذُو مَغْفِرَةٍ لِلنَّاسِ عَلَى ظُلْمِهِمْ ط وَإِنَّ رَبَّكَ لَشَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٥٥﴾

**“Mola wako Mlezi ni Mwenye Msamaha kwa watu juu ya udhalimu wao. Na hakika Mola wako Mlezi ni Mkali wa Kuadhibu.” (13:6)**

Na Aya katika hili ni nyingi sana. Kisha Aliyetukuka Anatupasha habari kuwa Yeye ni Mpole, Anaficha makosa na Anasamehe madhambi. Huenda Akawaongoza baadhi yao kutoka katika upotevu kuelekea kwenye uongofu. Na yeyote atakayeendelea katika njia za uovu, itamjia yeye siku ambayo watoto



wachanga watabadilika kuwa vizee (wenye mvi) na kila mjamzito kubwagwa mzigo wake (kuzaa kabla ya muda wake). Na hivyo Akasema:

بَلْ لَهُمْ مَوْعِدٌ لَّنْ يَجِدُوا مِنْ دُونِهِ مَوْيَلًا ﴿٥٤﴾

***“Lakini wanayo miadi ambayo hawatapata makimbilio yoyote ya kuepukana nayo.”***

Maana yake: Hawatapata njia yoyote ile. Na Kauli Yake:

وَتِلْكَ الْقُرَىٰ ۖ أَهْلَكْنَاهُمْ لَمَّا ظَلَمُوا

***“Na miji hiyo Tuliwaangamiza watu wake walipodhulumu.”***

Maana yake: Ummah zilizotangulia katika nyakati za awali; ‘Tuliwaangamiza kwa sababu ya ukafiri wao na inadi yao’.

وَجَعَلْنَا لِمَهْلِكِهِمْ مَوْعِدًا ﴿٥٥﴾

***“Na Tukawawekea miadi ya maangamizo yao.”***

Maana yake: Tuliwajaalia kuwa na muda na wakati maalumu, haizidi wala kupungua. Hivyo ndivyo mtakavyopatikana enyi washirikina, kwa hiyo tahadharini kwani yaliowafikia wao yatawafikia nyinyi pia, kwani mumemkanusha Mtume Mtukufu na Nabii mkubwa. Na fahamuni kuwa nyinyi si bora wala vipenzi Vyetu kuliko wao, hivyo ogopeni adhabu na maonyo Yangu.

\* \* \*

وَإِذْ قَالَ مُوسَى لِفَتْنِهِ لَآ أَبْرُحُ حَتَّىٰ ۚ أَبْلُغَ مَجْمَعَ  
 الْبَحْرَيْنِ أَوْ أَمْضِيَ حُقُبًا ﴿٦٠﴾ فَلَمَّا بَلَغَا مَجْمَعَ بَيْنَهُمَا  
 نَسِيَا حُوتَهُمَا فَاتَّخَذَ سَبِيلَهُ فِي الْبَحْرِ سَرَبًا ﴿٦١﴾ فَلَمَّا  
 جَاوَزَا قَالَ لِفَتْنِهِ ءَإِنَّا غَدَاءُنَا لَقَدْ لَقِينَا مِنْ سَفَرِنَا هَذَا  
 نَصَبًا ﴿٦٢﴾ قَالَ أَرَأَيْتَ إِذْ أَوَيْنَا إِلَى الصَّخْرَةِ فَإِنِّي نَسِيتُ  
 الْحُوتَ وَمَا أَنسِيهِ إِلَّا الشَّيْطَانُ أَنْ أَذْكُرَهُ ۗ وَاتَّخَذَ سَبِيلَهُ  
 فِي الْبَحْرِ عَجَبًا ﴿٦٣﴾ قَالَ ذَلِكَ مَا كُنَّا نَبِغُ ۗ فَارْتَدَّا عَلَىٰ  
 ءَانَارِهِمَا قَصَصًا ﴿٦٤﴾ فَوَجَدَا عَبْدًا مِنْ عِبَادِنَا ءَاتَيْنَاهُ  
 رَحْمَةً مِنْ عِنْدِنَا وَعَلَّمْنَاهُ مِنْ لَدُنَّا عِلْمًا ﴿٦٥﴾ قَالَ لَهُ  
 مُوسَىٰ هَلْ أَتَيْكَ عَلَىٰ أَنْ تُعَلِّمَ مِمَّا عَلَّمْتَ رُسُلَنَا ﴿٦٦﴾  
 قَالَ إِنَّكَ لَنْ تَسْتَطِيعَ مَعِيَ صَبْرًا ﴿٦٧﴾ وَكَيْفَ تَصْبِرُ عَلَىٰ  
 مَا لَمْ تُحِطْ بِهِ خُبْرًا ﴿٦٨﴾ قَالَ سَتَجِدُنِي إِنْ شَاءَ اللَّهُ  
 صَابِرًا وَلَا أَعْصِي لَكَ أَمْرًا ﴿٦٩﴾ قَالَ فَإِنِ اتَّبَعْتَنِي فَلَا  
 تَسْأَلْنِي عَنْ شَيْءٍ حَتَّىٰ أُحَدِّثَ لَكَ مِنْهُ ذِكْرًا ﴿٧٠﴾  
 فَانطَلَقَا حَتَّىٰ إِذَا رَكِبَا فِي السَّفِينَةِ خَرَقَهَا ۗ قَالَ أَخْرَقَهَا  
 لِثَغْرِ قِ أَهْلِهَا لَقَدْ جِئْتُمْ شَيْئًا إِمْرًا ﴿٧١﴾ قَالَ أَلَمْ أَقُلْ  
 إِنَّكَ لَنْ تَسْتَطِيعَ مَعِيَ صَبْرًا ﴿٧٢﴾ قَالَ لَا تُؤَاخِذْنِي بِمَا  
 نَسِيتُ وَلَا تُرْهِقْنِي مِنْ أَمْرِي عُسْرًا ﴿٧٣﴾

وَإِذْ قَالَ مُوسَى لِفَتْنِهِ لَآ أَبْرُحُ  
 حَتَّىٰ ۚ أَبْلُغَ مَجْمَعَ الْبَحْرَيْنِ أَوْ  
 أَمْضِيَ حُقُبًا ﴿٦٠﴾ فَلَمَّا بَلَغَا مَجْمَعَ  
 بَيْنَهُمَا نَسِيَا حُوتَهُمَا فَاتَّخَذَ سَبِيلَهُ  
 فِي الْبَحْرِ سَرَبًا ﴿٦١﴾ فَلَمَّا جَاوَزَا  
 قَالَ لِفَتْنِهِ ءَإِنَّا غَدَاءُنَا لَقَدْ لَقِينَا  
 مِنْ سَفَرِنَا هَذَا نَصَبًا ﴿٦٢﴾ قَالَ  
 أَرَأَيْتَ إِذْ أَوَيْنَا إِلَى الصَّخْرَةِ فَإِنِّي  
 نَسِيتُ الْحُوتَ وَمَا أَنسِيهِ إِلَّا  
 الشَّيْطَانُ أَنْ أَذْكُرَهُ ۗ وَاتَّخَذَ سَبِيلَهُ  
 فِي الْبَحْرِ عَجَبًا ﴿٦٣﴾ قَالَ ذَلِكَ مَا  
 كُنَّا نَبِغُ ۗ فَارْتَدَّا عَلَىٰ ءَانَارِهِمَا  
 قَصَصًا ﴿٦٤﴾ فَوَجَدَا عَبْدًا مِنْ  
 عِبَادِنَا ءَاتَيْنَاهُ رَحْمَةً مِنْ  
 عِنْدِنَا وَعَلَّمْنَاهُ مِنْ لَدُنَّا عِلْمًا ﴿٦٥﴾

60. Na pale Musa alipo-  
 muambia kijana wake:  
 Sitoacha kuendelea mpaka  
 nifike zinapokutana bahari  
 mbili, au nitaendelea kwa  
 muda mrefu.

**61. Basi wawili hao walipofika zinapokutana bahari mbili walimsahau samaki wao, naye akashika njia yake kaporonyokea baharini.**

**62. Walipokwishapita alimuambia kijana wake: Tupe chakula chetu cha mchana. Kwa hakika tumepata machofu kweli kwa safari yetu hii.**

**63. Akasema (kijana): Waona! Pale tulipopumzika penye jabali basi mimi nilimsahau samaki yule. Na hapana aliyenisahaulisha nisimkumbuke ila Shetani tu. Naye akashika njia yake baharini kwa ajabu.**

**64. (Musa) akasema: Hayo ndiyo tuliyokuwa tunayataka. Basi wakarudi nyuma kwa kufuata njia waliyojia.**

**65. Basi wakamkuta mja katika waja Wangu Tuliempa rehema kutoka Kwetu, na Tukamfunza mafunzo yaliyotoka Kwetu.**

### Kisa cha Musa عليه السلام na Al-Khidhwr

Sababu ya kauli ya Musa عليه السلام kwa kijana wake, Yusha' bin Nuun, ni kuwa alikuwa ameambiwa kuhusu mmoja wa waja wa Allah تعالى katika makutano ya bahari mbili, ambaye ana elimu asiyokuwa nayo yeye (Musa عليه السلام), hivyo alitaka kusafiri ili kukutana naye. Kwa hiyo, alimuambia kijana wake hilo:

لَا أُبْرِحُ

**“Sitoacha kuendelea.”**

Maana yake: Nitaendelea kusafiri,

حَتَّىٰ آتِبُلُغَ مَجْمَعِ الْبَحْرَيْنِ

**“Mpaka nifike zinapokutana bahari mbili.”**

Maana yake: Mahali ambapo bahari mbili zinakutana. Na Kauli Yake:

أَوْ أَمْضَىٰ حُقُبًا

**“Au nitaendelea kwa muda mrefu.”**

Maana yake: Hata kama nitahitajika kusafiri kwa muda mrefu sana. Amesema Ibn Jariir رحمه الله تعالى: “Baadhi ya wanazuoni wa lugha ya Kiarabu wanasema kuwa *Huqub* ina maana ya mwaka katika lahaja ya kabila la Qays”<sup>1</sup>. Kisha akapokea kutoka kwa ‘Abdallaah bin ‘Amr kuwa amesema: “*Huqub* ni miaka themanini”<sup>2</sup>. Na amesema Mujaahid: “Miaka sabiini”<sup>3</sup>. Na amepokea ‘Aliy bin Abi Twalhah kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuhusu Kauli Yake: ‘*Au nitaendelea kwa muda mrefu*’, akasema: “Dahari (maisha yote)”<sup>4</sup>. Qataadah na Ibn Zayd wamesema mfano wa hayo<sup>5</sup>. Na Kauli Yake:

فَلَمَّا بَلَغَا مَجْمَعَ بَيْنَهُمَا نَسِيَا حُوتَهُمَا

**“Basi wawili hao walipofika zinapokutana bahari hizo mbili walimsahau samaki wao...”**

Hiyo ni kuwa aliamriwa abebe samaki aliyetiwa chumvi pamoja naye, na akaambiwa, pindi unapomkosa samaki, hiyo itakuwa ndio ishara na alama ya kuwa umefika mahali unapopahitajia. Hivyo, waliondoka na kusafiri mpaka wakafika kwenye makutano ya bahari mbili, kulipokuwa na chemchemi inayoitwa ‘*Ayn Al-Hayaat* (Chemchemi ya Maisha). Walilala hapo, na hapo samaki akahisi matone ya maji hayo, hivyo akapata uhai kwa mara nyingine. Alikuwa amewekwa kwenye chombo na Yusha’, naye akaruka kutoka katika hicho chombo kuelekea baharini. Yusha’ aliamka na samaki akaanguka kwenye maji na kuanza kuogelea kwenye maji, na kuacha mkokoto (alama) nyuma yake. Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Anasema:

فَاتَّخَذَ سَبِيلَهُ فِي الْبَحْرِ سَرَبًا ﴿٦٠﴾

**“Naye akashika njia yake kaporonyokea baharini.”**

Maana: Mfano wa kuchimba upenyo kwenye ardhi. Amesema Ibn Jurayj kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Iliacha alama kama kwamba ni juu ya jiwe”.

<sup>1</sup> At-Tabari 18:56.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:56.

<sup>3</sup> At-Tabari 18:56.

<sup>4</sup> At-Tabari 18:57.

<sup>5</sup> At-Tabari 18:57.

<sup>6</sup> At-Tabari 18:58. Isnadi yake ina dosari.

Na imepokewa na Muhammad bin Is'haaq رحمه الله تعالى kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kutoka kwa Ubayi bin Ka'b kuwa Mtume ﷺ pindi alipokumbuka Hadithi hiyo alisema: "Maji hayajasimama kuanzia kuwepo kwa watu isipokuwa sehemu zile alizozipita samaki wa Musa عليه السلام, yakasimama yakawa kama njia pana mpaka aliporudi Musa عليه السلام akaona njia aliyopitia." Akasema: "*Hayo ndiyo tuliyokuwa tunayataka*".<sup>1</sup> Na Kauli Yake:

فَلَمَّا جَاوَزَا

**"Walipokwisha pita."** Maana yake: Mahali walipomsahau samaki. Na sahu imenasibishwa kwa wote wawili japokuwa kwa hakika ilikuwa ni Yusha' ndiye aliyesahau. Hii ni kama ilivyo katika Kauli ya Aliyetukuka:

يَخْرُجُ مِنْهَا اللَّوْلُؤُ وَالْمَرْجَانُ

**"Katika hizo bahari mbili hutoka lulu na marijani."** (55:22), Japokuwa lulu zinatoka kutoka katika maji ya chumvi (bahari) kulingana na moja ya kauli mbili. Walipopita kituo kimoja mahali ambapo walimsahau samaki, "Alisema", Maana: Musa عليه السلام:

لِفَتْهُ إِاتِنَا عِدَاءَنَا لَقَدْ لَقِينَا مِنْ سَفَرِنَا هَذَا

**"Kumuambia kijana wake tupe chakula chetu cha mchana. Kwa hakika tumepata kweli, katika safari yetu hii."**

Maana yake: Katika safari ambamo wamepita mahali walipotaka kusimama.

نَصَبًا

**"Naswaban."** Maana yake: Machofu na taabu.

قَالَ أَرَأَيْتَ إِذْ أُوِينَا إِلَى الصَّخْرَةِ فَإِنِّي نَسِيتُ الْحَوْتَ وَمَا أَنَسِيَهُ إِلَّا الشَّيْطَانُ أَنْ أَذْكُرَهُ

**"Akasema (kijana): Waona! Pale tulipopumzika penye jabali basi mimi nilimsahau samaki yule. Na hapana aliyenisahaulisha nisimkumbuke ila Shetani tu."** Na hivyo akasema:

وَأَتَّخَذَ سَبِيلَهُ

**"Na akashika njia yake."** Maana yake: Njia aliyochukua (ndani ya bahari),

<sup>1</sup> At-Tabari (23195) Sanadi yake ni dhaifu.

فِي الْبَحْرِ عَجَبًا ﴿٦٠﴾ قَالَ ذَلِكَ مَا كُنَّا نَبْغُ

**“Baharini kwa ajabu. (Musa) akasema: Hayo ndiyo tuliyokuwa tunayataka...”**

Maana yake: Hili ndilo tulilokuwa tunalitaka.

فَارْتَدَّا

**“Basi wakarudi nyuma.”** Maana yake: Wakarejea,

عَلَىٰ آثَارِهِمَا

**“Kwa kufuata njia.”** Maana yake: njia yao.

**“Waliojia”,** Maana yake: Wakafuata nyayo zao kwa kurudi walikotaka.

فَوَجَدَا عَبْدًا مِّنْ عِبَادِنَا آتَيْنَاهُ رَحْمَةً مِّنْ عِنْدِنَا وَعَلَّمْنَاهُ مِن لَّدُنَّا عِلْمًا ﴿٦١﴾

**“Basi wakamkuta mja katika waja wangu Tuliyeempa Rehema kutoka Kwetu, na Tukamfunza mafunzo yaliyotoka Kwetu.”**

Na huyu ndiye Al-Khidhwr, kama zilivyoashiria Hadithi Sahihi za Mtume ﷺ. Al-Bukhaariy amepokea kuwa Sa'id bin Jubayr amesema, “Nilimuambia Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: Nawf Al-Bikaaliy anadai kuwa Musa, sahibu wa Al-Khidhwr sio Musa wa Wana wa Israili”. Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما akasema: “Adui wa Allah تعالى amesema uongo”. Amepokea Ubayy bin Ka'b رضي الله عنه amemsikia Mtume ﷺ akisema:

«إِنَّ مُوسَى قَامَ خَطِيئًا فِي بَنِي إِسْرَائِيلَ فَسُئِلَ: أَيُّ النَّاسِ أَعْلَمُ؟ قَالَ: أَنَا، فَعَتَبَ اللَّهُ عَلَيْهِ إِذْ لَمْ يَرُدَّ الْعِلْمَ إِلَيْهِ، فَأَوْحَى اللَّهُ إِلَيْهِ إِنَّ لِي عَبْدًا بِمَجْمَعِ الْبَحْرَيْنِ هُوَ أَعْلَمُ مِنْكَ. قَالَ مُوسَى: يَا رَبِّ وَكَيْفَ لِي بِهِ؟ قَالَ: تَأْخُذُ مَعَكَ حُوتًا فَتَجْعَلُهُ بِمِكْتَلٍ، فَحَيْثُمَا فَقَدْتَ الْحُوتَ فَهُوَ نَمٌّ، فَأَخْذُ حُوتًا فَجَعَلَهُ بِمِكْتَلٍ، ثُمَّ انْطَلَقَ وَانْطَلَقَ مَعَهُ فَتَاهُ يُرْسِعُ بَنُ نُونٍ عَلَيْهِ السَّلَامُ، حَتَّى إِذَا أَتَى الصَّخْرَةَ وَضَمَا رُؤُسَهُمَا فَتَامَا، وَاضْطَرَبَ الْحُوتُ فِي الْمِكْتَلِ، فَخَرَجَ مِنْهُ فَسَقَطَ فِي الْبَحْرِ فَاتَّخَذَ سَبِيلَهُ فِي الْبَحْرِ سَرِيًّا، وَأَمْسَكَ اللَّهُ عَنِ الْحُوتِ جِزْيَةَ الْمَاءِ، فَصَارَ عَلَيْهِ مِثْلُ الطَّاقِ، فَلَمَّا اسْتَيْقَطَ، نَسِيَ صَاحِبَهُ أَنْ يُخْبِرَهُ بِالْحُوتِ، فَانْطَلَقَا بِقِيَّةِ يَوْمِهِمَا وَلَيْلَتُهُمَا حَتَّى إِذَا كَانَ مِنَ الْعَدِ قَالَ مُوسَى لِفَتَاهُ: ﴿يَا بَنِي عَدَاءِنَا لَقَدْ لَقِينَا مِنْ سَفَرِنَا هَذَا نَصَبًا﴾

"Musa alisimama kutoa khutbah mbele ya Wana wa Israili, naye akaulizwa: 'Ni nani aliye na elimu zaidi miongoni mwa watu?' Musa akajibu: 'Mimi'. Allah Akamlaumu kwa sababu hakuirudisha elimu hiyo kwa Allah. Hivyo, Allah Akamteremshia: 'Hakika Ninaye mja Wangu katika makutano ya bahari ambaye ana elimu zaidi kukuliko wewe'. Musa akauliza: 'Ee Mola Wangu Mlezi! Nitawezaje kukutana naye?' Allah Alimuambia: 'Chukua samaki na mtie katika chombo na mahali utakapomkosa samaki utamkuta (mtu huyo)'. Hivyo, Musa akamchukua samaki, akamtia katika chombo na kuanza safari pamoja na kijana, Yusha' bin Nuun, hadi wakafika kwenye jabali ambalo kwalo walijipumzisha na kulala.

Samaki akatingishika na kugeuka geuka katika chombo, akatoka ndani yake na kuanguka baharini, na huko akaanza kutembea ndani yake kama katika upenyo. Allah Akasimamisha utembeaji wa maji katika sehemu zote mbili za maji, hivyo hiyo ikawa kama shimo. Musa alipoamka, sahibu wake alisahau kumueleza kuhusu samaki, na hivyo waliendelea na safari yao katika baki ya mchana na usiku kucha. Asubuhi ya pili, Musa alimuambia kijana wake, '**Tupe chakula chetu cha mchana. Kwa hakika tumepata machofu kweli kwa hii safari yetu.**'

وَلَمْ يَجِدْ مُوسَى النَّصَبَ حَتَّى جَاوَزَ الْمَكَانَ الَّذِي أَمَرَهُ اللَّهُ بِهِ، قَالَ لَهُ فَتَاهُ:  
 ﴿أَرَأَيْتَ إِذْ أَوَّانَا إِلَى الصَّخْرَةِ فَإِنِّي نَبِئْتُ الْمَوْتِ وَمَا أُنْسِينِي إِلَّا السَّيْطَانَ أَن أَدْكُرَهُ وَأَتَخَذَ  
 سَبِيلَهُ فِي الْبَحْرِ عَجَبًا﴾ قَالَ: فَكَانَ لِلْحَوْبِ سَرَبًا، وَلِمُوسَى وَفَتَاهُ عَجَبًا، فَقَالَ:  
 ﴿ذَلِكَ مَا كُنَّا نَبِئُ فَارْتَدًّا عَلَيَّ مَا نَاهَيْتَا قَصَصًا﴾ قَالَ: فَرَجَعَا يَقْضَانِ أَثْرَهُمَا حَتَّى انْتَهَيَا  
 إِلَى الصَّخْرَةِ، فَإِذَا رَجُلٌ مُسَجًى بِنُوبٍ، فَسَلَّمَ عَلَيْهِ مُوسَى فَقَالَ الْخَضِرُ: وَأَنْتَى  
 بِأَرْضِكَ السَّلَامُ. فَقَالَ: أَنَا مُوسَى. فَقَالَ: مُوسَى بَنِي إِسْرَائِيلَ؟ قَالَ: نَعَمْ، قَالَ:  
 أَتَيْتُكَ لِتُعَلِّمَنِي مِمَّا عَلَّمْتَ رُشْدًا ﴿قَالَ إِنَّكَ لَنْ تَسْتَطِيعَ مَعِيَ صَبْرًا﴾ يَا مُوسَى إِنِّي  
 عَلَى عِلْمٍ مِّنْ عِلْمِ اللَّهِ عَلَّمَنِيهِ لَا تَعْلَمُهُ أَنْتَ وَأَنْتَ عَلَى عِلْمٍ مِّنْ عِلْمِ اللَّهِ عَلَّمَكَهُ اللَّهُ  
 لَا أَعْلَمُهُ.

Musa hakuchoka mpaka alipopita mahali alipoagizwa na Allah kupatizama. Kijana wake hapo alimuambia:

**'Waona! Pale tulipopumzika penye jabali basi mimi nilimsahau samaki yule. Na hapana aliyenisahaulisha nisimkumbuke ila Shetani tu. Naye akashika njia yake baharini kwa ajabu'.** Akasema: 'Kulikuwa na upenyo wa samaki.' Musa na kijana wake wakaona ajabu (kwa hilo). Musa akasema: **'Hayo ndiyo tuliyokuwa tunayataka. Basi wakarudi nyuma kwa kufuata njia waliyojia'.** Akasema: 'Hivyo, wakarudi wakifuata nyayo zao mpaka wakafika kwenye jabali. Hapo walimkuta mtu aliyejifunika na nguo. Musa alimsalimia. Al-Khidhwr akasema: 'Je, kuna salamu kama hizi katika ardhi hii?' Musa akasema: 'Mimi ni Musa'. Akasema: 'Je, wewe ni Musa wa Wana wa Israili?' Musa akasema: 'Ndio', na kuongeza: 'Nimekuja kwako ili unifunze elimu uliyofunzwa katika uongofu'. Al-Khidhwr akasema: **'Hakika wewe hutaweza kuvumilia kuwa pamoja nami.'** Ewe Musa! Nina elimu niliyopewa na Allah lakini wewe huna; nawe pia una elimu uliyopewa na Allah lakini mimi sina.'

فَقَالَ مُوسَى: ﴿سَتَجِدُنِي إِِنْ شَاءَ اللَّهُ صَابِرًا وَلَا أَعْصِي لَكَ أَمْرًا﴾ قَالَ لَهُ الْخَازِئِرُ: ﴿إِنِ اتَّبَعْتَنِي فَلَا تَسْأَلْنِي عَنْ شَيْءٍ حَتَّى أُحَدِّثَ لَكَ مِنْهُ ذِكْرًا﴾ فَاَنْطَلَقَا يَمْشِيَانِ عَلَى سَاحِلِ الْبَحْرِ فَمَرَّتْ سَفِينَةٌ، فَكَلَّمُوهُمْ أَنْ يَحْمِلُوهُمْ، فَعَرَفُوا الْخَازِئِرَ فَحَمَلُوهُمْ بِغَيْرِ نَوْلٍ، فَلَمَّا رَكِبَا فِي السَّفِينَةِ لَمْ يَفْجَأْ إِلَّا وَالْخَازِئِرُ قَدْ قَلَعَ لَوْحًا مِنَ الْأَوْجِ السَّفِينَةَ بِالنَّوْمِ، فَقَالَ لَهُ مُوسَى: قَدْ حَمَلُونَا بِغَيْرِ نَوْلٍ، فَعَمَدْتَ إِلَى سَفِينَتِهِمْ فَحَرَقْتَهَا لِتُغْرِقَ أَهْلَهَا؟ لَقَدْ جِئْتَ شَيْئًا إِمْرًا ﴿قَالَ أَلَمْ أَقُلْ إِنَّكَ لَنْ تَسْتَطِيعَ مَعِيَ صَبْرًا﴾ قَالَ لَا تُؤَاخِذْنِي بِمَا نَسِيتُ وَلَا تَرَهْتَنِي مِنْ أَمْرِي عَسَىٰ أَن يَأْتِيَنَّكَ السَّيْرُ ﴿٦٣﴾

Akasema Musa: **"Insha'Allah, Allah Akipenda, utaniona mvumilivu, wala sitoasi amri yako'.** Al-Khidhwr akamuambia: **'Basi ukunifuata usiniulize kitu mpaka mimi nianze kukutajia'.** Hivyo walianza kutembea kwenye ufuo wa bahari, mpaka safina (jahazi) ilipopita karibu yao, nao wakamuomba nahodha awasaidie kuwabeba. Nahodha alimtambua Al-Khidhwr, naye akawaruhusu kupanda bure.

Walipoingia ndani, mara tu Musa alimuona Al-Khidhwr akitoa mbao miongoni mwa mbao za safina kwa kutumia tezo. Musa



akamuambia, "Watu hawa wametupandisha bure, nawe umeivunja safina yao ili watu wake wazame! Hakika umefanya jambo baya sana'. Akasema: '**Sikukuambia hutaweza kuvumilia kuwa pamoja nami?**' (Musa) akasema: '**Usinichukulie kwa niliyosahau, wala usinipe uzito kwa jambo langu.'**

Mtume ﷺ akasema :

فَكَانَتْ الْأُولَىٰ مِنْ مُوسَىٰ بَنِيَانَا، قَالَ: وَجَاءَ عُضْفُورٌ فَوَقَعَ عَلَىٰ حَرْبِ السَّفِينَةِ، فَتَقَرَّرَ فِي الْبَحْرِ نَقْرَةً أَوْ تَقَرَّتَيْنِ فَقَالَ لَهُ الْخَضِيرُ: مَا عَلِمِي وَعَلِمْتُكَ فِي عِلْمِ اللَّهِ إِلَّا بِمِثْلِ مَا نَقَصَ هَذَا الْعُضْفُورُ مِنْ هَذَا الْبَحْرِ ثُمَّ خَرَجَا مِنْ السَّفِينَةِ فَيَتَمَّا هُمَا يَمْشِيَانِ عَلَى السَّاحِلِ إِذْ أَبْصَرَ الْخَضِيرُ غُلَامًا يَلْعَبُ مَعَ الْعِلْمَانِ، فَأَخَذَ الْخَضِيرُ رَأْسَهُ فَأَقْتَلَهُ بِيَدِهِ فَقَتَلَهُ، فَقَالَ لَهُ مُوسَى: ﴿أَقْتَلْتَ نَفْسًا زَكِيَّةً بِغَيْرِ نَفْسٍ لَقَدْ جِئْتَ شَيْئًا نُكْرًا ﴿٧٦﴾ قَالَ أَتَىٰ أَقْلَ لَكَ إِنَّكَ لَنْ تَسْتَطِيعَ مَعِيَ صَبْرًا ﴿٧٧﴾﴾

"Katika hali hiyo ya mwanzo, Musa alimuuliza Al-Khidhwr kwa sababu alisahau ahadi yake. Kisha alikuja ndege na akakaa pembezoni mwa safina, akatia mdomo wake na kudonoa baharini mara moja au mbili. Al-Khidhwr akamuambia Musa: 'Elimu yangu na yako, kulinganisha na elimu ya Allah, ni kama ndege huyu na alichochukua baharini'. Kisha walitoka kwenye safina, na walipokuwa wakitembea kwenye ufuo, Al-Khidhwr alimuona kijana akicheza na vijana wengine. Al-Khidhwr alimshika kijana kichwa chake na kuking'oa kwa mikono yake, na hivyo kumuua. Musa akamuambia:

**"Ala! Umemuua mtu asiye na kosa, na wala hakuua! Ama hakika umefanya jambo baya kabisa!" Akasema: 'Je! Sikukwambia kwamba hakika wewe huwezi kuvumilia kuwa pamoja nami?'**

قَالَ: وَهَذِهِ أَشَدُّ مِنَ الْأُولَىٰ، ﴿قَالَ إِنْ سَأَلْتَكَ عَنْ شَيْءٍ بَعْدَهَا فَلَا تُصْنِجْنِي فَدَّ بَلَنْتَ مِنْ لَدُنِّي عَذَابًا﴾ فَأَطْلَقَهَا حَتَّىٰ إِذَا آتَىٰ أَهْلَ قَرْيَةٍ اسْتَظَلَمَ أَهْلُهَا فَأَبْرَأَ أَنْ يُضَيَّفُوهُمَا فَوَجَدَا فِيهَا حِدَارًا يُرِيدُ أَنْ يَنْقَضَ ﴿أَي مَائِلًا، فَقَالَ الْخَضِيرُ بِيَدِهِ ﴿فَأَقَامَهُ﴾ فَقَالَ مُوسَى: قَوْمٌ أَتَيْنَاهُمْ فَلَمْ يُطْعِمُونَا وَلَمْ يُضَيَّفُونَا ﴿لَوْ شِئْتَ لَتَّخَذْتَ عَلَيْهِ أَجْرًا﴾ ﴿٧٧﴾ قَالَ هَذَا فِرَاقُ بَيْنِي وَبَيْنَكَ سَأَيْتَكَ بِأَوَّلِ مَا لَمْ تَسْتَطِيعَ عَلَيْهِ صَبْرًا ﴿٧٨﴾﴾

Mpokezi akasema, 'Kosa la pili lilikuwa kubwa kabisa kuliko la mwanzo'.

**Musa akasema: 'Nikikuuliza kitu chochote baada ya haya usifuatane nami, kwani umekwishapata udhuru kwangu. Basi wakatoka mpaka wakawafikia watu wa mji mmoja. Wakawaomba watu wake wawape chakula, nao wakakataa kuwakaribisha. Hapo wakakuta ukuta unataka kuanguka.'** Maana: Umeinama. Al-Khidhwr akasimamisha kwa mikono yake.

Musa akasema: 'Tuliwajia watu hawa, nao hawakutupatia chakula wala kutukaribisha hivyo, 'Ungelitaka ungelichukua ujira kwa haya.' (Mtu yule) akasema: 'Huku ndio kufarikiana baina yangu na wewe. Sasa nitakueleza maana ya yale uliyokuwa huwezi kuyastahamia'".

Mtume ﷺ akasema:

«وَوَدِدْنَا أَنَّ مُوسَىٰ كَانَ صَبِيرًا حَتَّىٰ يَقْضَىٰ اللَّهُ عَلَيْنَا مِنْ خَيْرِهِمَا»

"Tulitamani kuwa Musa angesubiri ili Allah Atuelezee mengi kuhusu wao wawili."

Said bin Jubayr amesema: "Ibn 'Abbas رضي الله عنهما alikuwa akisoma (Aya ya 79):

(وَكَانَ أَمَامَهُمْ مَلِكٌ يَأْخُذُ كُلَّ سَفِينَةٍ صَالِحَةٍ عَشَبًا)

'Na alikuwa mbele yao mfalme ambaye anaghusubu kwa nguvu kila safina iliyo katika hali nzuri'.

Na pia (Aya ya 80):

(وَأَمَّا الْعُلَامُ فَكَانَ كَافِرًا وَكَانَ أَبَوَاهُ مُؤْمِنِينَ)

'Na ama kijana alikuwa kafiri na wazazi wake walikuwa Waumini'<sup>1</sup>.

Kisha Al-Bukhaariy amepokea mfano wake, na ndani yake:

فَخَرَجَ مُوسَىٰ وَمَعَهُ قَتَاهُ يُوشَعَ بْنِ نُونٍ وَمَعَهُمَا الْحُوْتُ، حَتَّىٰ انْتَهَبَا إِلَى الصَّخْرَةِ، فَتَرَا عِنْدَهَا، قَالَ: فَوَضَعَ مُوسَىٰ رَأْسَهُ قَتَامَ، قَالَ: وَفِي أَصْلِ الصَّخْرَةِ عَيْنٌ يُقَالُ

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baariy 8:262.

لَهَا الْحَيَاةُ لَا يُصِيبُ مِنْ مَائِهَا شَيْءٌ إِلَّا حَيٌّ فَأَصَابَ الْحُوتَ مِنْ مَاءِ تِلْكَ الْعَيْنِ،  
فَتَحَرَّكَ وَانْسَلَّ مِنَ الْمِكْتَلِ فَدَخَلَ الْبَحْرَ، فَلَمَّا اسْتَبْقَطَ قَالَ مُوسَى لِفَتَاهُ: ﴿هَآئِنَا  
غَدَاءَنَا﴾

*"Alitoka Musa akiwa na kijana wake Yusha' bin Nuun, na walikuwa na samaki pamoja nao. Walipofika kwenye jabali, walipiga kambi hapo, Musa akaweka kichwa chake na hapo hapo akalala. Akasema: 'Chini ya jabali kulikuwa na chemchemi inayoitwa Al-Hayaat; maji yake hayagusi chochote ila hukipatia uhai. Samaki akaguswa na maji yatokayo katika chemchemi hiyo, na hapo akaanza kutaharaki na kuruka nje ya chombo na kuingia kwenye bahari. Alipoamka, Musa alimuambia kijana wake:*

**'Tupe chakula chetu cha asubuhi'.**

Kisha akanukuu baki ya Hadithi.

Kisha alikuja ndege na kukaa pembezoni mwa safina, akatia mdomo wake na kudonoa baharini mara moja au mbili. Al-Khidhwr akamuambia Musa عليه السلام: 'Elimu yangu na yako na elimu ya viumbe wote, kulinganisha na elimu ya Allah تعالى, ni kama ndege huyu na alichochukua baharini.'" Kisha akataja baki ya ripoti<sup>1</sup>.

قَالَ لَهُ مُوسَى هَلْ أَتَّبِعُكَ عَلَيَّ أَنْ تُعَلِّمَنِي مِمَّا عَلَّمْتَ رُشْدًا ﴿٦٦﴾ قَالَ إِنَّكَ لَنْ  
تَسْتَطِيعَ مَعِيَ صَبْرًا ﴿٦٧﴾ وَكَيْفَ تَصْبِرُ عَلَيَّ مَا لَمْ تُحِطْ بِهِ خُبْرًا ﴿٦٨﴾ قَالَ سَتَجِدُنِي  
إِنْ شَاءَ اللَّهُ صَابِرًا وَلَا أَعْصِي لَكَ أَمْرًا ﴿٦٩﴾ قَالَ فَإِنْ أَتَّبَعْتَنِي فَلَا تَسْأَلْنِي عَنْ شَيْءٍ  
حَتَّى أُحَدِّثَ لَكَ مِنْهُ ذِكْرًا ﴿٧٠﴾

**66. Musa akamuambia: Nikufuate ili unifunze katika ule uwongofu uliofunzwa wewe?**

**67. Akasema: Hakika wewe hutaweza kuvumilia kuwa pamoja nami.**

**68. Na utawezaje kuvumilia yale usiyoyajua vilivyo undani wake?**

<sup>1</sup> Fat'hul-Baariy 8:276.

**69. Akasema: Insha'Allaah, Allah Akipenda, utaniona mvumilivu, wala sitoasi amri yako.**

**70. Akasema: Basi ukinifuata usiniulize kitu mpaka mimi nianze kukutajia.**

### Musa عليه السلام Kukutana na Al-Khidhwr na Kuongozana Naye

Allah تعالى Anatuambia jinsi Musa عليه السلام alivyomuambia yule mwanachuoni, ambaye ni al-Khidhwr. Alikuwa ni mmoja ambaye alipatiwa elimu na Allah تعالى ambayo hakupatiwa Musa عليه السلام, kama vile Allah تعالى Alivyompatia Mussa عليه السلام elimu ambayo hakumpatia Al-Khidhwr.

قَالَ لَهُ مُوسَىٰ هَلْ أَتَّبِعُكَ

**“Musa akamuambia: Je, nikufuate?”** Hili ni swali la upole, sio katika njia ya ulazima wala nguvu. Hii ndio njia ambayo mtafutaji elimu anafaa kumsemesha mwanachuoni. Na Kauli Yake:

أَتَّبِعُكَ

**“Nikufuate.”** Maana yake: Niwe sahibu yako na niwe nawe.

عَلَىٰ أَنْ تُعَلِّمَنِي مِمَّا عَلَّمْتَ رُشْدًا ﴿٦٠﴾

**“Ili unifunze katika ule uongofu uliofunzwa wewe.”**

Maana yake: Unifunze katika aliyokufundisha Allah تعالى ili nipate kuongoka kwayo na nijifunze yenye faida na nifanye amali njema. Hapo,

قَالَ

**“Akasema.”** Maana yake: Al-Khidhwr alimuambia Musa عليه السلام,

إِنَّكَ لَنْ تَسْتَطِيعَ مَعِيَ صَبْرًا ﴿٦١﴾

**“Hakika wewe hutaweza kuvumilia kuwa pamoja nami.”**

Maana yake: Hutaweza kufuatana nami utakapoona nikifanya kinachokwenda kinyume na sheria yako, kwani nina elimu kutoka kwa Allah تعالى ambayo Hajakufunza, nawe una elimu kutoka kwa Allah تعالى ambayo Hajanifunza mimi. Kila mmoja wetu ana majukumu mbele ya Allah تعالى, na hutaweza kusuhubiana nami.

وَكَيْفَ تَصْبِرُ عَلَىٰ مَا لَمْ تُحِطْ بِهِ خُبْرًا ﴿٦٨﴾

**“Na utawezaje kuvumilia yale usiyoyajua vilivyo undani wake?”**

Hakika najua utakanusha ninayoyafanya ambayo wewe una udhuru kwayo, lakini nina elimu ya hekima na maslahi ya kindani kutoka kwa Allah تعالى ambayo naweza kuona, nawe huwezi.

قَالَ

**“Akasema”,** Maana yake: Musa عليه السلام alisema:

سَتَجِدُنِي إِنْ شَاءَ اللَّهُ صَابِرًا

**“Insha’Allah, Allah Akipenda, utaniona mvumilivu.”** Maana yake: Kwa kila kitu unachofanya katika mambo yako,

وَلَا أَعْصِي لَكَ أَمْرًا ﴿٦٩﴾

**“Wala sitoasi amri yako.”** Maana yake: Sitakwenda kinyume nawe kwa chochote. Hapa, Al-Khidhwr, aliweka sharti:

قَالَ فَإِنِ اتَّبَعْتَنِي فَلَا تَسْأَلْنِي عَنْ شَيْءٍ

**“Akasema: Basi ukunifuata usiniulize kitu chochote.”** Maana yake: Usianzishe mazungumzo yoyote katika jambo kuanzia mwanzo,

حَتَّىٰ أَحْدِثَ لَكَ مِنْهُ ذِكْرًا ﴿٧٠﴾

**“Mpaka mimi nianze kukutajia.”** Maana yake: Mpaka nianze mazungumzo kuhusu hilo kabla hujaniuliza.

فَأَنْطَلَقَا حَتَّىٰ إِذَا رَكِبَا فِي السَّفِينَةِ خَرَقَهَا ۖ قَالَ أَخْرَقْتُهَا لِتُفْرَقَ أَهْلُهَا لَقَدْ جِئْتُمْ شَيْئًا

إِمْرًا ﴿٧١﴾ قَالَ أَلَمْ أَقُلْ إِنَّكَ لَنْ تَسْتَطِيعَ مَعِيَ صَبْرًا ﴿٧٢﴾ قَالَ لَا تُؤَاخِذْنِي بِمَا نَسِيتُ

وَلَا تُرْهِقْنِي مِنْ أَمْرِي عُسْرًا ﴿٧٣﴾

**71. Basi wawili hao wakatoka, hata walipopanda safina/ jahazi (mtu yule) akaitoboa. (Musa) akasema: Unaitoboa uwazamishe watu wake? Hakika umefanya jambo baya.**

**72. Akasema: Sikukwambia hutaweza kuvumilia kuwa pamoja nami?**

**73. (Musa) akasema: Usinichukulie kwa niliyosahau, wala usinipe uzito kwa jambo langu.**

### **Kisa cha Kuiharibu Safina**

Allah تعالیٰ Anatuambia kuwa Musa عليه السلام na sahibu yake, Al-Khidhwr walitoka baada ya kuafikiana na kufahamiana katika hilo. Al-Khidhwr aliweka sharti kwa Musa عليه السلام kuwa asimuulize kuhusu chochote anachochukua mpaka yeye mwenyewe amuelezee kuhusu hilo. Hivyo walipanda kwenye safina, kama ilivyoelezwa katika Hadithi tuliyonukuu iliyotangulia – nahodha alimtambua Al-Khidhwr na kuwaacha kupanda bure, kama heshima kwa A-Khidhwr. Safina ilipoanza kwenda baharini na wakawa mbali kutoka ufuoni, Al-Khidhwr alinyanyuka na kuiharibu safina kwa kung’oa ubao na kisha kuurudisha. Musa (عليه السلام), hakuweza kuizuilia nafsi yake akawa ni mwenye kusema kwa kumsuta:

أَحْرَقْتَهَا لِتُغْرِقَ أَهْلَهَا

**“Unaitoboa uwazamishe watu wake?”**

Na katika sarufi ya kirabu *Laam* hii hapa ni *Laam* ya matokeo yake sio lengo la amali yake.

لَقَدْ جِئْتِ شَيْئًا إِمْرًا ﴿٧٦﴾

**“Hakika umefanya jambo baya”.**

Amesema Mujaahid: “Jambo baya”<sup>1</sup>. Na amesema Qataadah: “Jambo la ajabu”<sup>2</sup>. Hapo Al-Khidhwr alimuambia kwa kumkumbusha ahadi na sharti walilokubaliana:

أَلَمْ أَقُلْ إِنَّكَ لَنْ تَسْتَطِيعَ مَعِيَ صَبْرًا ﴿٧٧﴾

**“Sikukwambia hutaweza kuvumilia kuwa pamoja nami?”**

Maana yake: Kwa hili nililofanya kwa makusudi ni moja kati ya mambo niliyokuekea kama sharti kwa sababu hujui habari kamili, na ipo sababu na lengo kwa hilo ambalo wewe hujajui.

<sup>1</sup> At-Tabari 18:72.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:72.

قَالَ

“Akasema”,

Maana yake: Musa عليه السلام akasema:

لَا تُؤَاخِذْنِي بِمَا نَسِيتُ وَلَا تُرْهِقْنِي مِنْ أَمْرِي عُسْرًا ﴿٦٧﴾

**“Usinichukulie kwa niliyosahau, wala usinipe uzito kwa jambo langu.”**

Maana yake: Usinibane wala usiwe mkali nami. Kwa hiyo, tumetangulia kutaja katika Hadithi ya Mtume ﷺ kuwa alisema:

«كَانَتْ الْأُولَى مِنْ مُوسَى نَسْيَانًا»

*“Katika hali hiyo ya mwanzo, Musa alisahau ahadi yake.”<sup>1</sup>*

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Fat’hul-Baariy 8:262.

فَانْطَلَقَا حَتَّىٰ إِذَا لَقِيَا غُلَامًا فَقَتَلَهُ قَالَ أَقْتَلْتَنِي نَفْسًا زَكِيَّةً  
 بِغَيْرِ نَفْسٍ لَّقَدْ جِئْتَ شَيْئًا نُّكْرًا ﴿٧٤﴾ \* قَالَ أَلَمْ أَقُلْ  
 لَكَ إِنَّكَ لَنْ تَسْتَطِيعَ مَعِيَ صَبْرًا ﴿٧٥﴾ قَالَ إِنْ سَأَلْتُكَ  
 عَنْ شَيْءٍ بَعْدَهَا فَلَا تُصَحِّبْنِي ۖ قَدْ بَلَغْتَ مِنَ لُدُنِي عُذْرًا  
 ﴿٧٦﴾ فَانْطَلَقَا حَتَّىٰ إِذَا أَتَيَا أَهْلَ قَرْيَةٍ اسْتَطَعَمَا أَهْلَهَا  
 فَأَبَوْا أَنْ يُضَيِّفُوهُمَا فَوَجَدَا فِيهَا جِدَارًا يُرِيدُ أَنْ يَنْقَضَ  
 فَأَقَامَهُ ۖ قَالَ لَوْ شِئْتَ لَتَّخَذْتَ عَلَيْهِ أَجْرًا ﴿٧٧﴾ قَالَ  
 هَذَا فِرَاقُ بَنِي وَيَسَّكَ ۚ سَأُنبِتُكَ مِنَّا بِتَأْوِيلٍ مَا لَمْ تَسْتَطِعْ  
 عَلَيْهِ صَبْرًا ﴿٧٨﴾ أَمَّا السَّفِينَةُ فَكَانَتْ لِمَسْكِينٍ يَعْمَلُونَ  
 فِي الْبَحْرِ فَأَرَدْتُ أَنْ أَعِيبَهَا وَكَانَ وَرَاءَهُمْ مَلِكٌ يَأْخُذُ كُلَّ  
 سَفِينَةٍ غَصْبًا ﴿٧٩﴾ وَأَمَّا الْعُلَمَاءُ فَكَانَ أَبُوهُمَا مُؤْمِنِينَ  
 فَخَشِينَا أَنْ يُرْهِقَهُمَا طُغْيَانًا وَكُفْرًا ﴿٨٠﴾ فَأَرَدْنَا أَنْ  
 يُبَدِّلَهُمَا رَبُّهُمَا خَيْرًا مِنْهُ زَكَاةً وَأَقْرَبَ رُحْمًا ﴿٨١﴾ وَأَمَّا  
 الْجِدَارُ فَكَانَ لِغُلَامَيْنِ يَتِيمَيْنِ فِي الْمَدِينَةِ وَكَانَ تَحْتَهُ  
 كَنْزٌ لَهُمَا وَكَانَ أَبُوهُمَا صَالِحًا فَأَرَادَ رَبُّكَ أَنْ يَبْلُغَا  
 أَشُدَّهُمَا وَيَسْتَخْرِجَا كَنْزَهُمَا رَحْمَةً مِنْ رَبِّكَ ۗ وَمَا فَعَلْتُهُ  
 عَنْ أَمْرِ رَبِّي ۗ ذَلِكَ تَأْوِيلُ مَا لَمْ تَسْطِعْ عَلَيْهِ صَبْرًا ﴿٨٢﴾

فَانْطَلَقَا حَتَّىٰ إِذَا لَقِيَا غُلَامًا فَقَتَلَهُ  
 قَالَ أَقْتَلْتَنِي نَفْسًا زَكِيَّةً بِغَيْرِ نَفْسٍ  
 لَّقَدْ جِئْتَ شَيْئًا نُّكْرًا ﴿٧٤﴾ \* قَالَ  
 أَلَمْ أَقُلْ لَكَ إِنَّكَ لَنْ تَسْتَطِيعَ مَعِيَ  
 صَبْرًا ﴿٧٥﴾ قَالَ إِنْ سَأَلْتُكَ عَنْ  
 شَيْءٍ بَعْدَهَا فَلَا تُصَحِّبْنِي ۖ قَدْ  
 بَلَغْتَ مِنَ لُدُنِي عُذْرًا ﴿٧٦﴾

74. Basi wakatoka wawili hao mpaka wakamkuta kijana, akamuua. (Musa) akasema: Ala! Umemuua mtu asiye na kosa, na wala hakuua! Ama hakika umefanya jambo baya kabisa!

75. Akasema: Je! Siku-kwambia kwamba hakika wewe huwezi kuvumilia kuwa pamoja nami?

76. Akasema: Nikikuuliza kitu chochote baada ya haya usifuatane nami, kwani umekwisha pata udhuru kwangu.



**Kisa cha Kuuliwa Kijana**

Allah تعالى Anasema:

فَأَنْطَلَقَا

**“Basi wakatoka hao wawili.”**

Maana yake: Baada ya tukio la mwanzo,

حَتَّىٰ إِذَا لَقِيَا غُلَامًا فَقَتَلَهُ.

**“Mpaka wakamkuta kijana, akamuua.”**

Tayari tumetaja hapo awali kuwa kijana mmoja alikuwa anacheza na vijana wenziwe katika kijiji miongoni mwa vijiji, na Al-Khidhwr alimchagua na kumkusudia kati ya wenziwe. Alikuwa ndiye mzuri wao na mwenye sura na umbile zuri zaidi kuliko wote, na Al-Khidhwr akamuua. Musa عليه السلام alipoona hilo alishutumumu kwa ukali zaidi kuliko wa mwanzo, na kwa haraka akasema:

أَقْتَلْتُ نَفْسًا زَكِيَّةً

**“Ala! Umemuua mtu asiye na kosa.”**

Maana yake: Kijana mdogo ambaye hajafanya kosa lolote, hata hivyo umemuua,

بِغَيْرِ نَفْسٍ

**“Na wala hakuua.”**

Maana yake: Hakukuwa na sababu ya kumuua.

لَقَدْ جِئْتُمْ شَيْئًا نُّكْرًا ﴿٧٤﴾

**“Ama hakika umefanya jambo baya kabisa!”** Maana: Jambo ambalo kwa uwazi na dhahiri ni ovu na baya.

﴿٧٤﴾ قَالَ أَلَمْ أَقُلْ لَّكَ إِنَّكَ لَنْ تَسْتَطِيعَ مَعِيَ صَبْرًا

**“Akasema: Je! Sikukwambia kwamba hakika wewe huwezi kuvumilia kuwa pamoja nami?”**

Kwa mara nyengine tena, Al-Khidhwr akamkumbusha sharti na ahadi waliowekeana kuanzia mwanzo, hivyo Musa عليه السلام akamuambia:

إِنْ سَأَلْتُكَ عَنْ شَيْءٍ بَعْدَهَا

**“Nikikuuliza kitu chochote baada ya haya.”** Maanae: Nikipinga lolote utakalo fanya baada ya hili,

فَلَا تُصَحِّبْنِي ۖ قَدْ بَلَغْتَ مِنْ لَدُنِّي عُذْرًا ﴿٧٧﴾

**“Usifuatane nami, kwani umekwishapata udhuru kwangu.”**

Maana: Umekubali udhuru wangu mara mbili. Amepokea Ibn Jariir رحمه الله تعالى kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuwa Ubayy bin Ka’b رضي الله عنه amesema: “Mtume ﷺ alipomtaja yeyote na kumuomba (Du’aa) basi alikuwa akianza na nafsi yake. Akasema siku hiyo (siku moja):

«رَحِمَهُ اللهُ عَلَيْنَا وَعَلَى مُوسَى، لَوْ لَبِثَ مَعَ صَاحِبِهِ لَأَبْصَرَ الْعَجَبَ، وَلَكِنَّهُ قَالَ:

‘Rehema ya Allaah iwe juu yetu na juu ya Musa. Lau angebaki na sahibu yake angeona maajabu zaidi, lakini alisema:

إِنْ سَأَلْتُكَ عَنْ شَيْءٍ بَعْدَهَا فَلَا تُصَحِّبْنِي ۖ قَدْ بَلَغْتَ مِنْ لَدُنِّي عُذْرًا ﴿٧٧﴾

**“Nikikuuliza kitu chochote baada ya haya usifuatane nami, kwani umekwisha pata udhuru kwangu.”<sup>1</sup>**

فَانْطَلَقَا حَتَّى إِذَا أَتَيَا أَهْلَ قَرْيَةٍ اسْتَطَعَمَا أَهْلَهَا فَأَبَوْا أَنْ يُضَيِّفُوهُمَا فَوَجَدَا فِيهَا

جِدَارًا يُرِيدُ أَنْ يَنْقُضَ فَأَقَامَهُ ۗ قَالَ لَوْ شِئْتَ لَتَّخَذْتَ عَلَيْهِ أَجْرًا ﴿٧٨﴾ قَالَ هَذَا فِرَاقُ

بَيْنِي وَبَيْنِكَ ۚ سَأُنَبِّئُكَ بِتَأْوِيلِ مَا لَمْ تَسْتَطِعْ عَلَيْهِ صَبْرًا ﴿٧٩﴾

**77. Basi wakatoka mpaka wakawafikia watu wa mji mmoja. Wakawaomba watu wake wawape chakula, nao wakakataa kuwakaribisha. Hapo wakakuta ukuta unataka kuanguka, (mja yule mwema) akasimamisha. (Musa) akasema: Ungelitaka ungelichukua ujira kwa haya.**

**78. (Mtu yule) akasema: Huku ndio kufarikiana baina yangu na wewe. Sasa nitakueleza maana ya yale uliyokuwa huwezi kuyastahamia.**

<sup>1</sup> At-Tabari 18:77. Isnadi yake ni dhaifu.

**Kisa cha Kukarabati Ukuta**

Allah تعالیٰ Anatupa habari kuhusu wao wawili kuwa,

فَانْطَلَقَا

**“Basi wakatoka.”**

Baada ya matukio mawili ya awali,

حَتَّىٰ إِذَا أَتَيَا أَهْلَ قَرْيَةٍ

**“Mpaka wakawafikia watu wa mji mmoja.”**

Amepokea Ibn Jariir رحمه الله تعالى kutoka kwa Ibn Siriin رحمه الله تعالى amesema: “Huo ni mji wa *Al-Aylah*”<sup>1</sup>. Na katika Hadithi:

«حَتَّىٰ إِذَا أَتَيَا أَهْلَ قَرْيَةٍ لِنَامَا»

**“Hata walipowajja watu wa kijiji li’ama.”**<sup>2</sup>

Maana yake: Mabakhili.

أَسْتَطَعَمَا أَهْلَهَا فَأَبَوْا أَنْ يُضَيِّفُوهُمَا فَوَجَدَا فِيهَا جِدَارًا يُرِيدُ أَنْ يَنْقَضَ

**“Wakawaomba watu wake wawape chakula, nao wakakataa kuwakaribisha. Hapo wakakuta ukuta unataka kuanguka.”**

Hapa kumekuja matumizi ya kutaka “*irada*” ya ukuta njia ya kiistiari. Hakika *irada* katika matukio yana maana ya kuinama. Na maana ya *Inqidhwaadhwni* kuanguka. Na Kauli Yake:

فَأَقَامَهُ

**“Akausimamisha.”**

Maana yake: Aliusimamisha peke yake. Na tumetangulia kutaja Hadithi kuwa alirudisha yeye peke yake katika hali ya kuusimamisha sawa sawa (kama ulivyokuwa hapo awali) na hili lilikuwa jambo lisilo la kawaida. Wakati huo, Musa عليه السلام alimuambia:

<sup>1</sup> At-Tabari 18:78.

<sup>2</sup> Ahmad 5:119.

لَوْ شِئْتُمْ لَتَّخَذْتُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا ﴿٧٤﴾

**“Ungelitaka ungelichukua ujira kwa haya.”**

Maana yake: Kwa sababu wao walikataa kutukaribisha, hivyo haikuwa sawa kuwafanyia kazi bure.

قَالَ هَذَا فِرَاقُ بَيْنِي وَبَيْنِكَ ۗ

**“(Mtu yule) akasema: Huku ndio kufarikiana baina yangu na wewe.”**

Maana yake: Wewe uliweka sharti baada ya kuuliwa kijana lau utaniuliza chochote baada ya hapo hutafuatana nami kabisa. Hivyo, hapa ndipo kutengana baina yangu na wewe.

سَأُنَبِّئُكَ بِتَأْوِيلِ

**“Sasa nitakueleza maana.”**

Maana yake: Tafsiri,

مَا لَمْ تَسْتَطِعْ عَلَيْهِ صَبْرًا ﴿٧٥﴾

**“Yale uliyokuwa huwezi kuyastahamia.”**

أَمَّا السَّفِينَةُ فَكَانَتْ لِمَسْكِينٍ يَعْمَلُونَ فِي الْبَحْرِ فَأَرْدَتْ أَنْ أُعْيِبَهَا وَكَانَ وِرَاءَهُمْ مَلِكٌ

يَأْخُذُ كُلَّ سَفِينَةٍ غَصْبًا ﴿٧٦﴾

**79. Ama jahazi ile ilikuwa ya masikini wafanyao kazi baharini. Nilitaka kuiharibu, kwani nyuma yao alikuwako mfalme anaghusubu safina (majahazi) yote.**

### Tafsiri ya Kwanini Safina Iliharibiwa

Hii ndiyo tafsiri ya yale ambayo hayakufahamika na Musa عليه السلام, na kukemea kwake matukio hayo. Allah تعالى Alimuonesha Al-Khidhwr hekima zilizofichana, hivyo akasema: “Hakika niliiharibu safina ili kuitia aibu kwani wao watapita kwa mfamle aliye dhalimu:

يَأْخُذُ كُلَّ سَفِينَةٍ

**'Ambaye anachukua kila safina.'** Iliyo nzuri.

غَضَبًا

**'Kwa kuighusubu.'** "Hivyo nilitaka kuitia dosari ili asiwe ni mwenye kuichukua, kwa hiyo, mwenye safina huyo aliye masikini asiyekuwa na chochote ataweza bado kufaidika nayo". Na panasemwa kuwa walikuwa mayatima.

وَأَمَّا الْغُلَامُ فَكَانَ أَبَوَاهُ مُؤْمِنَيْنِ فَخَشِينَا أَنْ يُرْهِقَهُمَا طُغْيَانًا وَكُفْرًا ﴿٨٠﴾ فَأَرَدْنَا أَنْ

يُبَدِّلَهُمَا رَبُّهُمَا خَيْرًا مِنْهُ زَكَاةً وَأَقْرَبَ رُحْمًا ﴿٨١﴾

**80. Na ama kijana yule, wazazi wake walikuwa ni Waumini. Tukakhofu asije watia mashakani kwa uasi na ukafiri.**

**81. Basi tulitaka Mola Wao Mlezi Awabadilishie aliye bora zaidi kuliko huyo kwa kutakasika, na aliye karibu zaidi kwa huruma.**

### Tafsiri ya Sababu za Kuuliwa Mtoto

Ibn 'Abbaas رضي الله عنه amepokea kutoka kwa Ubayy bin Ka'b رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«الغلام الذي قتله الخضر طبع يوم طبع كافرا»

*"Kijana aliyeuliwa na Al-Khidhr alikuwa ameshakadiriwa kuanzia kuumbwa kwake kuwa kafiri."*

Imepokewa na Ibn Jariir رحمه الله تعالى kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنه<sup>1</sup>. Kwa hivyo akasema:

فَكَانَ أَبَوَاهُ مُؤْمِنَيْنِ فَخَشِينَا أَنْ يُرْهِقَهُمَا طُغْيَانًا وَكُفْرًا ﴿٨٠﴾

**"Wazazi wake walikuwa ni Waumini. Tukakhofu asije watia mashakani kwa uasi na ukafiri."**

Maana yake: Huenda ikawapeleka wao kumfuata mtoto wao katika ukafiri kwa ajili ya mahaba yao kwake. Qataadah amesema: "Hakika ni kuwa wazazi wake walifurahi sana kwa kuzaliwa kwake na kuhuzunika sana alipouliwa, na

<sup>1</sup> At-Tabari 18:85.

lau angebakia angewapelekea katika maangamivu yao. Hivyo, mwanadamu anatakiwa aridhie Kudura ya Allah تعالى, kwani Kudura ya Allah تعالى kwa yale Muumini kwa anayochukia, ni bora kwake kuliko Kudura Yake kwa jambo analopenda”<sup>1</sup>. Na imesihi katika Hadithi:

«لَا يَفْضِي اللهُ لِلْمُؤْمِنِ مِنْ قَضَاءٍ إِلَّا كَانَ خَيْرًا لَهُ»

*“Allah Hamkadirii chochote Muumini kwa Kadari isipokuwa huwa kheri kwake.”<sup>2</sup>*

Na Amesema Aliyetukuka:

وَعَسَىٰ أَنْ تَكْرَهُوا شَيْئًا وَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ

*“Na huenda mkachukia kitu, nacho ni kheri kwenu.” (2:216)*

Na Kauli Yake:

فَارْدَنَّا أَنْ يُبَدِّلَهُمَا رَبُّمَا خَيْرًا مِنْهُ زَكَاةً وَأَقْرَبَ رُحْمًا ﴿٨٢﴾

*“Basi tulitaka Mola Wao Mlezi Awabadilishie aliye bora zaidi kuliko huyo kwa kutakasika, na aliye karibu zaidi kwa huruma.”*

Maana: Mtoto aliye bora kuliko huyu, nao watakuwa na huruma zaidi kuliko yeye. Hii ilikuwa rai ya Ibn Jurayj<sup>3</sup>.

وَأَمَّا الْجِدَارُ فَكَانَ لِغُلَامَيْنِ يَتِيمَيْنِ فِي الْمَدِينَةِ وَكَانَ تَحْتَهُ كَنْزٌ لَهُمَا وَكَانَ أَبُوهُمَا

صَالِحًا فَأَرَادَ رَبُّكَ أَنْ يَبْلُغَا أَشُدَّهُمَا وَيَسْتَخْرِجَا كَنْزَهُمَا رَحْمَةً مِنْ رَبِّكَ ۗ وَمَا فَعَلْتُهُ

عَنْ أَمْرِي ۗ ذَٰلِكَ تَأْوِيلُ مَا لَمْ تَسْطِعْ عَلَيْهِ صَبْرًا ﴿٨٢﴾

**82. Na ama ukuta, huo ulikuwa ni wa vijana wawili mayatima kule mjini. Na chini yake ilikuwako khazina yao; na baba yao alikuwa ni mtu mwema. Basi Mola wako Mlezi Alitaka wafikie utu uzima na wajitolee khazina yao wenyewe, kuwa ni rehema itokayo kwa Mola wako Mlezi. Wala mimi sikutenda hayo kwa amri yangu. Hiyo ndiyo tafsiri ya hayo ambayo wewe hukuweza kuyasubiria.**

<sup>1</sup> At-Tabari 18:86.

<sup>2</sup> Ahmad 3:117.

<sup>3</sup> At-Tabari 18:86-87.

### Tafsiri ya Kwanini Ukuta Ulijengwa Bila Ujira

Na katika Aya hii kuna dalili kuwa neno *Qaryah* (kijiji) inaweza kutumika kumaanisha mji (*Madinah*), kwa sababu Allah تعالى mwanzo Anasema.

حَتَّىٰ إِذَا أَتَىٰ أَهْلَ قَرْيَةٍ

**“Mpaka wakawafikia watu wa mji (Qaryah) mmoja.” (18:77).**

Na hapa Amesema:

فَكَانَ لِغُلَامَيْنِ يَتِيمَيْنِ فِي الْمَدِينَةِ

**“Huo ulikuwa ni wa vijana wawili mayatima kule mjini (al-Madinah)”.**

Hii ni kama Aya:

وَكَايِنٍ مِّن قَرْيَةٍ هِيَ أَشَدُّ قُوَّةً مِّن قَرْيَتِكَ الَّتِي أَخْرَجْتِكَ

**“Na watu wa miji (Qaryah) mingapi iliyokuwa yenye nguvu zaidi kuliko watu wa mji wako uliokutoa.” (47:13)**

وَقَالُوا لَوْلَا نُزِّلَ هَذَا الْقُرْآنُ عَلَىٰ رَجُلٍ مِّنَ الْقَرْيَتَيْنِ عَظِيمٍ ﴿٤٣﴾

**“Na walisema: Kwa nini Qur’ani hii haikuteremshwa juu ya mtu mkubwa katika miji miwili (Al-Qaryatan) mikubwa.” (43:31),**

Maana yake: Makkah na Ta’if.

Maana ya Aya (18:82), “Nimeutengeneza ukuta huu kwa sababu ni wa vijana wawili mayatima katika mji, na chini yake kuna khazina yao”. Amesema ‘Ikrimah, Qatadah na wengineo: “Chini yake kulikuwa na mali iliyofukiwa kwa ajili yao.”<sup>1</sup> Na maana hii iko wazi kutokana na mtiririko wa Aya, na hii ndiyo rai ya Ibn Jariir (Allah تعالى Amrehemu). Na Kauli Yake:

وَكَانَ أَبُوهُمَا صَالِحًا

**“Na baba yao alikuwa ni mtu mwema”.** Ndani yake kuna dalili kuwa watoto wa mtu mwema wanatizamwa, na kuwa baraka za ‘Ibada yake inawajumuisha wao (watoto) hapa duniani na Kesho Akhera. Hii itatukia kupitia kwa maombi yake kwao. Na vile vile hadhi yao kunyanyuliwa hadi kufikia daraja ya juu

<sup>1</sup> At-Tabari 18:90.

peponi, ili yaweze kutulia macho yake kwao, kama ilivyokuja katika Qur'ani na kunukuliwa katika Sunna. Amepokea Sa'id bin Jubayr kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: "Walitizamwa (na kuhifadhiwa) kwa sababu ya wema wa baba yao, japokuwa haijatajwa kuwa wao pia walikuwa wema."<sup>1</sup> Na Kauli Yake:

فَأَرَادَ رَبُّكَ أَنْ يَبْلُغَا أَشُدَّهُمَا وَيَسْتَخْرِجَا كَنْزَهُمَا

***"Basi Mola wako Mlezi Alitaka wafikie utu uzima na wajitolee khazina yao wenyewe."***

Hapa katika "Irada" imerudishwa kwa Allah تعالى, kwani kufikia makamu ya kubaleghe kunamtegemea Allah تعالى Peke Yake (hakuna mwengine anayeweza kuwafikisha makamu hayo). Kinyume na ilivyosemwa kuhusu kijana:

فَأَرَدْنَا أَنْ يُبَدِّلَهُمَا رَبُّهُمَا خَيْرًا مِنْهُ زَكَاةً

***"Basi tulitaka Mola Wao Mlezi Awabadilishie aliye bora zaidi kuliko huyo kwa kutakasika...", (18:81)***

Na kuhusu safina,

فَأَرَدْتُ أَنْ أَعِيبَهَا

***"Nilitaka kuiharibu".***

Na Allah تعالى Anajua zaidi.

### **Jee Al-Khidhwr Alikuwa Nabii?**

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

رَحْمَةً مِنْ رَبِّكَ وَمَا فَعَلْتُهُ عَنْ أَمْرِي

***"Kuwa ni rehema itokayo kwa Mola wako Mlezi Mimi sikufanya hayo kwa amri yangu..."***

Maana: Mambo haya matatu niliyoyafanya yanatokana na rehema kutoka kwa Allah تعالى kwa yale tuliyotaja, sahibu wa safina, wazazi wa mtoto na watoto wawili wa mtu mwema. Mimi sikufanya hayo kwa amri yangu. Lakini niliamriwa kuyafanya nami nikayatekeleza (bila kurudi nyuma). Hii ni dalili ya kuunga mkono wale wanaosema kuwa Al-Khidhwr alikuwa Nabii, pamoja na Aya tuliyoinukuu hapo mbeleni:

<sup>1</sup> At-Tabari 18:90.



﴿ فَوَجَدَا عَبْدًا مِّنْ عِبَادِنَا ءَاتَيْنَاهُ رَحْمَةً مِّنْ عِنْدِنَا وَعَلَّمْنَاهُ مِمَّا لَدُنَّا عِلْمًا ﴾

***“Basi wakamkuta mja katika waja Wangu Tuliyeempa Rehema kutoka Kwetu, na Tukamfunza mafunzo yaliyotoka Kwetu.”(18:65).***

### **Kwa Nini Akaitwa Al-Khidhwr?**

Amepokea Imaam Ahmad kutoka kwa Abu Hurayrah عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ amesema yafuatayo kuhusu Al-Khidhwr:

﴿ إِنَّمَا سُمِّيَ خَضِرًا لِأَنَّهُ جَلَسَ عَلَى فَرْوَةٍ بَيْضَاءَ، فَإِذَا هِيَ نَهْتَزُ مِنْ تَحْتِهِ خَضِرَاءَ ﴾

*“Hakika aliitwa Al-Khidhwr kwa sababu ya kuketi kwenye nyasi kavu “Farwah” nyeupe, kisha ikageuka kuwa kijani (khadhwraa) chini yake”<sup>1</sup>.*

Imam Ahmad pia amenukuu hili kutoka kwa ‘Abdur-Razzaaq<sup>2</sup>. Pia imenukuliwa katika Swahili Al-Bukhaariy kutoka kwa Hamaam kutoka kwa Abu Hurayrah عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ amesema:

﴿ إِنَّمَا سُمِّيَ الْخَضِرَ لِأَنَّهُ جَلَسَ عَلَى فَرْوَةٍ، فَإِذَا هِيَ نَهْتَزُ مِنْ تَحْتِهِ خَضِرَاءَ ﴾

*“Hakika aliitwa al-Khidhwr kwa sababu ya kuketi kwenye nyasi kavu “Farwah” nayo ikageuka kijani (khadhwraa) chini yake”<sup>3</sup>.*

*Farwah* hapa ina maana ya vijishehemu vya mimea iliyokauka. Hii ilikuwa rai ya ‘Abdur-Razzaaq<sup>4</sup>. Pia palisemwa kuwa maana yake ni uso wa ardhi.

Na Kauli Yake:

﴿ ذَلِكَ تَأْوِيلُ مَا لَمْ تَسْطِعْ عَلَيْهِ صَبْرًا ﴾

***“Hiyo ndiyo tafsiri ya hayo ambayo wewe hukuweza kuyasubiria.”***

Maana: Hii ndiyo tafsiri katika mambo ambayo hukuweza kusubiri kwayo mpaka nikachukua fursa ya kukuelezea. Na pindi alipomfasiria na kumbainishia na kumuekea wazi mushkeli huo uliondoka, akasema:

<sup>1</sup> Ahmad 2:312.

<sup>2</sup> Ahmad 2:318.

<sup>3</sup> Fat’hul-Baariy 6:499.

<sup>4</sup> Ahmad 2:318.

مَا لَمْ تَسْتَطِعْ

**“Ambayo wewe hukuweza”.**

Na kabla ya hapo mushkeli ulikuwa na nguvu na ulikuwa mzito, akasema:

سَأُنَبِّئُكَ بِتَأْوِيلِ مَا لَمْ تَسْتَطِعْ عَلَيْهِ صَبْرًا ﴿٧٨﴾

**“...Sasa nitakueleza maana ya yale uliyokuwa huwezi kuyastahamia.” (18:78).**

Uzito unakabiliana na uzito zaidi, na hafifu kwa hafifu zaidi, kama Alivyosema:

فَمَا اسْتَطَعُوا أَنْ يَظْهَرُوهُ

**“Basi hawakuweza kuukwea...” (18:97),**

Nayo ni kupanda kuelekea juu (kileleni).

وَمَا اسْتَطَعُوا لَهُمْ نَقْبًا ﴿٩٧﴾

**“Wala hawakuweza kuutoboa.” (18:97)**

Ambayo ni ngumu zaidi kuliko ya awali. Kukabiliana kila moja kwa inayonasibiana kwa lafudhi na maana. Na Allah تعالى Anajua zaidi.

Pakisemwa: Je, kumetokea nini kwa kijana yule wa Musa عليه السلام aliyetajwa mwanzo wa kisa kisha hakutajwa baada ya hapo? Jawabu ya hilo ni kuwa makusudio ya kisa ni yale yaliyotokea baina ya Musa عليه السلام na Al-Khidhwr. Kijana wa Musa عليه السلام alikuwa pamoja naye, akimfuata katika yote hayo.

Imetajwa kwa uwazi kabisa katika Hadithi Sahihi iliyotajwa huko nyuma, kuwa alikuwa Yusha' bin Nuun, ambaye alikuwa kiongozi wa Wana wa Israili baada ya Musa عليه السلام.

\* \* \*

وَسْأَلُونَكَ عَنِ ذِي الْقَرْيَيْنِ <sup>ط</sup> قُلْ سَأَلْتُوْا عَلَیْكُمْ مِنْهُ  
 ذِكْرًا ﴿٨٣﴾ إِنَّا مَكَّنَّا لَهُ فِي الْأَرْضِ وَءَاتَيْنَاهُ مِنْ كُلِّ  
 شَيْءٍ سَبَبًا ﴿٨٤﴾ فَاتَّبَعَ سَبَبًا ﴿٨٥﴾ حَتَّىٰ إِذَا بَلَغَ مَغْرِبَ  
 الشَّمْسِ وَجَدَهَا تَغْرُبُ فِي عَيْنٍ حَمِئَةٍ وَوَجَدَ عِنْدَهَا  
 قَوْمًا <sup>ط</sup> قُلْنَا يَنْدَا الْقَرْيَتَيْنِٰ إِنَّمَا أَنْ تَعَذَّبَ وَإِنَّمَا أَنْ تَتَّخِذَ فِيهِمْ  
 حُسْنًا ﴿٨٦﴾ قَالَ أَمَا مَنْ ظَلَمَ فَسَوْفَ نَعَذِّبُهُ ثُمَّ يُرَدُّ إِلَىٰ  
 رَبِّهِ فَيُعَذِّبُهُ عَذَابًا نَكْرًا ﴿٨٧﴾ وَأَمَا مَنْ ءَامَنَ وَعَمِلَ  
 صَالِحًا فَلَهُ جَزَاءٌ الْحَسَنَىٰ <sup>ط</sup> وَسَأْتُولُ لَهُ مِنْ أَمْرِنَا يُسْرًا  
 ﴿٨٨﴾ ثُمَّ اتَّبَعَ سَبَبًا ﴿٨٩﴾ حَتَّىٰ إِذَا بَلَغَ مَطْلِعَ الشَّمْسِ  
 وَجَدَهَا تَطْلُعُ عَلَىٰ قَوْمٍ لَمْ يَجْعَلْ لَهُمْ مِنْ دُونِهَا سِتْرًا ﴿٩٠﴾  
 كَذَٰلِكَ وَقَدْ أَحَطْنَا بِمَا لَدَيْهِ خُبْرًا ﴿٩١﴾ ثُمَّ اتَّبَعَ سَبَبًا  
 ﴿٩٢﴾ حَتَّىٰ إِذَا بَلَغَ بَيْنَ السَّدَّيْنِ وَجَدَ مِنْ دُونِهِمَا قَوْمًا  
 لَّا يَكَادُونَ يَفْقَهُونَ قَوْلًا ﴿٩٣﴾ قَالُوا يَنْدَا الْقَرْيَتَيْنِٰ إِن  
 بَأْسُجُوجٍ وَمَأْجُوجٍ مُّفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ فَهَلْ نَجْعَلُ لَكَ  
 خَرْجًا عَلَیٰ أَنْ نَجْعَلَ بَيْنَنَا وَبَيْنَهُمْ سَدًّا ﴿٩٤﴾ قَالَ مَا  
 مَكَّنِّي فِيهِ رَبِّي خَيْرٌ فَأَعِينُونِي بِقُوَّةٍ أَجْعَلْ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُمْ  
 رَدْمًا ﴿٩٥﴾ ءَاتُونِي زُبَرَ الْحَدِيدِ <sup>ط</sup> حَتَّىٰ إِذَا سَاوَىٰ بَيْنَ  
 الصَّدَفَيْنِ قَالَ أَنْفُخُوا <sup>ط</sup> حَتَّىٰ إِذَا جَعَلَهُ نَارًا قَالَ ءَاتُونِي  
 أُفْرِغْ عَلَيْهِ قِطْرًا ﴿٩٦﴾

وَسْأَلُونَكَ عَنِ ذِي الْقَرْيَتَيْنِ <sup>ط</sup> قُلْ  
 سَأَلْتُوْا عَلَیْكُمْ مِنْهُ ذِكْرًا ﴿٨٣﴾ إِنَّا  
 مَكَّنَّا لَهُ فِي الْأَرْضِ وَءَاتَيْنَاهُ مِنْ كُلِّ  
 شَيْءٍ سَبَبًا ﴿٨٤﴾

**83. Na wanakuuliza khabari za Dhul Qarnayn. Waambie: Nitakusimulieni baadhi ya Hadithi yake.**

**84. Sisi Tulimtilia nguvu katika ardhi na Tukampa njia za kila kitu.**

**Kisa cha Dhul Qarnayn**

Allah تعالى Anamuambia Mtume Wake:

وَسْأَلُونَكَ

“Na wanakuuliza”,

Ewe Muhammad,

عَنِ ذِي الْقَرْيَتَيْنِ <sup>ط</sup>

“Khabari za Dhul Qarnayn”,

Maana yake: Kuhusu khabari zake. Tayari tumeshaeleza jinsi gani makafiri wa Makka walituma ujumbe kwa Ahl Al-Kitaab (walio-pewa Kitabu) na kuwauliza baadhi ya khabari ambayo

kwayo wanaweza kumjaribu Mtume. Wao (watu wa Kitabu) walisema: “Muulizeni kuhusu mtu aliyezunguka (kutembea sana) katika ardhi, na vijana ambao hakuna ajuao waliyoyafanya, na kuhusu Roho”. Hapo Suratul Kahf ikateremshwa.

### Dhul Qarnayn Alikuwa Mwenye Nguvu Kubwa

Na Kauli Yake:

إِنَّا مَكِّنَّا لَهُ فِي الْأَرْضِ

**“Sisi Tulimtilia nguvu katika ardhi.”**

Maana yake: Tulimpatia ufalme na nguvu kubwa iliyowezekana, hivyo akawa na kila kitu walichokuwa nacho wafalme, katika nguvu, jeshi, silaha na vifaa vya kuuzingira mji (kwa ajili ya kuuteka). Hivyo, akawa na mamlaka juu ya mashariki na magharibi ya ardhi, nchi zote pamoja na wafalme wote walinyenyekea kwake, na mataifa yote, ya Kiarabu na ya Kiajemi (yasiyokuwa ya Kiarabu) yalimtumikia. Baadhi yao wanasema kuwa aliitwa Dhul Qarnayn (mwenye pembe mbili) kwa sababu alifika ‘Pembe’ mbili za jua, mashariki na magharibi, linapochomoza na linapo zama.

وَأَتَيْنَاهُ مِنْ كُلِّ شَيْءٍ سَبَبًا

**“Na Tukampa njia za kila kitu.”**

Ibn ‘Abbaas, Mujaahid, Sa’id bin Jubayr, ‘Ikrimah, As-Suddiy, Qataadah, Adh-Dhahaak na wengine رضي الله عنهم wamesema: “Hiyo ina maana ya elimu”<sup>1</sup>. Pia amesema Qataadah katika Kauli Yake:

وَأَتَيْنَاهُ مِنْ كُلِّ شَيْءٍ سَبَبًا

**“Na Tukampa njia za kila kitu.”**

Maana yake: “Sehemu tofauti za ardhi na sehemu muhimu.”<sup>1</sup>Hakika Allah تعالى Amesema yafuatayo kuhusu Bilqis:

<sup>1</sup> Al-Bidaayah wan Nihaayah 2:106 na At-Tabari 18:94-95.

وَأُوتِيَتْ مِنْ كُلِّ شَيْءٍ

**“Na amepewa kila kitu.” (27:23),**

Maana yake: Vitu vyote ambavyo wafalme mfano wake wanapatiwa.

Hivyo pia ndivyo alivyokuwa Dhul Qarnayn: Allah تعالى Alimsahilishia sababu, maana njia na nguvu za kuteka sehemu zote, maeneo na nchi, kuwashinda maadui, kuwakomesha wafalme wa ardhi na kuwadhalilisha washirikina. Alipatiwa kila kitu ambacho mtu kama yeye atahitajia. Na Allah تعالى Anajua zaidi.

فَأَتَّبَعَ سَبَبًا ﴿٢٧﴾ حَتَّىٰ إِذَا بَلَغَ مَغْرِبَ الشَّمْسِ وَجَدَهَا تَغْرُبُ فِي عَيْنٍ حَمِئَةٍ وَوَجَدَ  
عِنْدَهَا قَوْمًا قُلْنَا يَنْدُوا الْقَرْيَتَيْنِ ۖ إِمَّا أَنْ تُعَذِّبَ وَإِمَّا أَنْ تَتَّخِذَ فِيهِمْ حُسْنًا ﴿٢٨﴾ قَالَ أَمَّا  
مَنْ ظَلَمَ فَسَوْفَ نُعَذِّبُهُ ثُمَّ يُرَدُّ إِلَىٰ رَبِّهِ فَيُعَذِّبُهُ عَذَابًا نُكْرًا ﴿٢٩﴾ وَأَمَّا مَنْ ءَامَنَ  
وَعَمِلَ صَالِحًا فَلَهُ جَزَاءٌ أَحْسَنٌ ۖ وَسَنَقُولُ لَهُ مِنْ أَمْرِنَا يُسْرًا ﴿٣٠﴾

**85. Basi akaifuata njia.**

**86. Hata alipofika machwea-jua alilionga linatua katika chemchem yenye matope meusi. Na hapo akawakuta watu. Tukasema: Ewe Dhul Qarnayn! Ama uwaadhibu au watwae kwa wema.**

**87. Akasema: Ama aliye dhulumu basi tutamuadhibu, na kisha atarudishwa kwa Mola Wake Mlezi Amuadhibu adhabu isiyo julikana.**

**88. Na ama aliyeamini na akatenda mema basi atapata malipo mazuri. Nasi tutamuambia lilio jepesi katika amri yetu.**

<sup>1</sup> Al-Bidaayah wan Nihaayah 2:106 na at-Tabari 18:94-95.

**Kusafiri na Kufika Kwake Machweo ya Jua (Magharibi)**

Amesema Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما:

فَأْتِيعَ سَبِيًّا

**"Basi akaifuata njia."** Maana yake: Alifuata njia tofauti kufikia alikotaka<sup>1</sup>. Na amesema Mujaahid:

فَأْتِيعَ سَبِيًّا

**"Basi akaifuata njia."** Maana yake: Alifuata njia tofauti, mashariki na magharibi<sup>2</sup>. Na katika riwaya nyingine ya Mujaahid:

سَبِيًّا

**"Njia."** Maana yake: Njia katika ardhi.<sup>3</sup> Qataadah amesema: "Inamaanisha alifuata njia na alama katika ardhi"<sup>4</sup>. Na Kauli Yake:

حَتَّىٰ إِذَا بَلَغَ مَغْرِبَ الشَّمْسِ

**"Hata alipofika machwea-jua."**

Maana: Alipita njia mpaka akafika sehemu ya mbali kabisa ambayo inawezafikiwa katika sehemu ya machweo ya jua, ambayo ni magharibi ya ardhi. Na ama kufika kwake mbinguni, magharibi ya jua ni jambo lisilowezekana, na visa vinavyotolewa na wasimulizi wa hekaya kuwa alisafiri sana magharibi kiasi cha jua kuzama nyuma yake si kweli kabisa. Visa vingi kati ya hivi ni visa vilivyobuniwa na watu wa Kitabu, na ni miongoni mwa uzushi na uongo wa waasi wao. Na Kauli Yake:

وَجَدَهَا تَغْرُبُ فِي عَيْنٍ حَمِئَةٍ

**"Aliliona linatua katika chemchem yenye matope meusi."**

Maana: Aliliona jua kama kwamba linatua baharini. Hili ni jambo ambalo kila mmoja anayekwenda baharini anaweza kuona: Inaonekana kana kwamba jua linatua ndani ya bahari, lakini hakika ni kuwa halikuacha njia yake lili lowekewa.

<sup>1</sup> At-Tabari 18:99.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:95.

<sup>3</sup> At-Tabari 18:95.

<sup>4</sup> At-Tabari 18:99.

*Hami'ah* ni, kulingana na kisomo kimoja kati ya viwili, inatokana na neno *Hama'ah*, inayomaanisha udongo. Hii ni kama ilivyo katika Kauli Yake:

إِنِّي خَلَقْتُ بَشَرًا مِّنْ صَلْصَلٍ مِّنْ حَمَلٍ مَّسْنُونٍ ﴿٢٨﴾

***“Hakika Mimi Nitamuumba mtu kwa udongo mkavu unaotoa sauti, wenye kutokana na matope meusi yaliyovunda.” (15:28)***

Maana: Udongo laini (telezi), kama tulivyobainisha hapo awali. Na Kauli Yake:

وَوَجَدَ عِنْدَهَا قَوْمًا

***“Na hapo akawakuta watu.”***

Maana yake: Ummah kati ya Ummah. Wakataja kuwa walikuwa taifa kubwa miongoni mwa binadamu. Na Kauli Yake:

فَلَمَّا يَدْعَا الْقَرْيَتَيْنِ إِمَّا أَنْ تُعَذِّبَ وَإِمَّا أَنْ تَتَّخِذَ فِيهِمْ حُسْنًا ﴿٢٩﴾

***“Tukasema: Ewe Dhul Qarnayn! Ama uwaadhibu au watwae kwa wema.”***

Maana ya Aya hii ni kuwa Allah تعالی Alimmakinisha (Alimpa nguvu) juu yao na Kumpatia uchaguzi: akitaka aweza kuwaua wanaume na kuwachukua wanawake na watoto mateka, au akitaka, aweza kuwaacha huru, kwa kutoa fidia (malipo ya kujikomboa) au bila ya fidia. Uadilifu wake na Imani yalijitokeza katika hukumu aliyoitamka:

أَمَّا مَنْ ظَلَمَ

***“Ama aliyedhulumu.”***

Maana yake: Aliyeendelea katika ukafiri wake na kumshirikisha Mola wake Mlezi,

فَسَوْفَ نُعَذِّبُهُ

***“Basi tutamuadhibu.”***

Qataadah amesema kwa kumuua<sup>1</sup>. Na Kauli Yake:

<sup>1</sup> At-Tabari 18:98.

ثُمَّ يُرَدُّ إِلَىٰ رَبِّهِ فَيُعَذِّبُهُ عَذَابًا نُّكْرًا ﴿٨٧﴾

**“Na kisha atarudishwa kwa Mola wake Mlezi Amuadhibu adhabu isiyojulikana.”**

Maana yake: Adhabu iliyo kali yenye kuumiza. Na katika hili kuna ushuhuda na thibitisho la Akhera na jaza'a (malipo) pamoja na adhabu. Na Kauli Yake:

وَأَمَّا مَنْ ءَامَنَ

**“Na ama aliyeamini.”**

Maana yake: Kwa kufuata yale tunayowaitia kwayo katika kumuabudu Allah تعالى Peke Yake asiyekuwa na mshirika. Basi huyo,

فَلَهُ جَزَاءٌ أَحْسَنُ ۗ

**“Atapata malipo mazuri.”**

Maana yake: Katika nyumba ya Akhera kwa Allah تعالى Aliyetukuka. Pia,

وَسَنَقُولُ لَهُ مِن أَمْرِنَا يُسْرًا ﴿٨٨﴾

**“Nasi tutamwambia lilio jepesi katika amri yetu.”**

Amesema Mujaahid “Maneno ya huruma”<sup>1</sup>.

ثُمَّ أَتْبَعَ سَبَبًا ﴿٨٩﴾ حَتَّىٰ إِذَا بَلَغَ مَطْلِعَ الشَّمْسِ وَجَدَهَا تَطَّلُعُ عَلَىٰ قَوْمٍ لَّمْ يَجْعَلْ لَهُم

مِّن دُونِهَا سِتْرًا ﴿٩٠﴾ كَذَٰلِكَ وَقَدْ أَحَطْنَا بِمَا لَدَيْهِ خُبْرًا ﴿٩١﴾

**89. Kisha akaifuata njia.**

**90. Hata alipofika matokeo ya jua aliliona linawachomozea watu Tusiowawekea pazia la kuwakinga nalo.**

**91. Ndio hivyo hivyo. Na Sisi Tulizijua vilivyo khabari zake zote.**

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:99.



### Safari Yake Upande wa Mashariki

Allah تعالى Anasema kuwa Dhul Qarnayn kisha alisafiri kutoka magharibi ya ardhi kuelekea mashariki. Kila alipopita katika taifa, aliwatenza nguvu na kuwashinda na kuwaita wao kwa Allah تعالى. Wakimtii. Kila kitu kilikuwa sawa na vyema, kinyume na hivyo huwadhalilisha kwa kuchukua mali yao, vyombo na samani zao. Alikuwa akitumia kutoka kila taifa kile kinachohitajiwa na jeshi lake ili kuweza kupigana na taifa linalofuata. Alipofika matokeo ya jua katika ardhi, kama Alivyosema Allah تعالى,

وَجَدَهَا تَطَّلُعُ عَلَى قَوْمٍ

**“Aliliona linawachomozea watu.”** Maana: Taifa,

لَمْ يَجْعَلْ لَهُمْ مِّنْ دُونِهَا سِتْرًا ﴿١٨٠﴾

**“Tusiowawekea pazia la kuwakinga nalo.”**

Maana yake: Hawakuwa na majumba wala miti ya kuwapatia kivuli na kuwasitiri kutokana na uharara wa jua.

Na amesema Qataadah: “Tumetajiwa kuwa walikuwa katika ardhi isiyomea chochote, hivyo jua lilipochomoza walikuwa wakiingia mashimoni mpaka linapopinduka ndipo walipotoka ili kufanya kazi zao za kila siku na kutafuta maisha yao.”<sup>1</sup> Na Kauli Yake:

كَذَلِكَ وَقَدْ أَحَطْنَا بِمَا لَدَيْهِ خُبْرًا ﴿١٨١﴾

**“Ndio hivyo hivyo. Na Sisi Tulizijua vilivyo khabari zake zote”.**

Amesema Mujaahid na As-Suddiy: “Hii inamaanisha kuwa Allah تعالى Anajua kila kitu kumhusu yeye na jeshi lake, na hakuna kilichofichamana Naye, japokuwa walikuwa wanatoka kutoka mataifa mengi tofauti. Kwani Yeye Aliyetukuka:

لَا يَخْفَىٰ عَلَيْهِ شَيْءٌ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ ﴿١٨٢﴾

**‘Hakifichiki chochote kilichomo ardhini wala kilichomo mbinguni.’ (3:5)<sup>2</sup>**

<sup>1</sup> At-Tabari 18:100.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:101.

ثُمَّ اتَّبَعَ سَبَبًا ﴿٣٣﴾ حَتَّىٰ إِذَا بَلَغَ بَيْنَ السَّدَّيْنِ وَجَدَ مِنْ دُونِهِمَا قَوْمًا لَّا يَكَادُونَ  
 يَفْقَهُونَ قَوْلًا ﴿٣٤﴾ قَالُوا يَبْنَؤُا الْقَرْيَتَيْنِ إِنَّ يَا جُوجَ وَمَأْجُوجَ مُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ فَهَلْ  
 تَجْعَلُ لَكَ خَرْجًا عَلَيَّ أَنْ تَجْعَلَ بَيْنَنَا وَبَيْنَهُمْ سَدًّا ﴿٣٥﴾ قَالَ مَا مَكَّنِّي فِيهِ رَبِّي خَيْرٌ  
 فَأَعِينُونِي بِقُوَّةٍ أَجْعَلْ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُمْ رَدْمًا ﴿٣٦﴾ ءَاتُونِي زُبَرَ الْحَدِيدِ ۗ حَتَّىٰ إِذَا سَاوَىٰ بَيْنَ  
 الصَّدَفَيْنِ قَالَ أَنْفُخُوا ۗ حَتَّىٰ إِذَا جَعَلَهُ نَارًا قَالَ ءَاتُونِي أُفْرِغْ عَلَيْهِ قِطْرًا ﴿٣٧﴾

**92. Kisha akaifuata njia.**

**93. Hata alipofika baina ya milima miwili, alikuta nyuma yake watu ambao takriban hawakuwa wanafahamu lolote.**

**94. Wakasema: Ewe Dhul Qarnayn! Hakika Juju wa majuju wanafanya uharibifu katika nchi. Basi je, tukulipe ujira ili utujengee baina yetu na wao ngome?**

**95. Akasema: Yale Mola wangu Aliyoniwezesha ni bora zaidi. Lakini nyinyi nisaidieni kwa nguvu zenu. Nitakujengeeni kizuizi baina yenu na wao.**

**96. Nileteeni vipande vya chuma. Hata alipoijaza nafasi iliyo kati ya milima miwili, akasema: Vukuteni. Hata alipokifanya (chuma) kama moto akasema: Nileteeni shaba iliyoyayuka niimwagie.**

**Safari Yake katika Ardhi ya Juju (Ya'ajuuj) na Majuju (Ma'ajuuj) , na Kujenga Kwake Kizuizi**

Allah تعالیٰ Anasema kuhusu Juju na Majuju:

ثُمَّ اتَّبَعَ سَبَبًا ﴿٣٣﴾

**“Kisha akaifuata njia.”** Maana yake: Kisha akasafiri kutoka mashariki ya ardhi mpaka akafika baina ya vizuizi viwili, nayo ni milima miwili iliyokuwa karibu, ikiwa na bonde baina yao. Watatoka kwayo Juju na Majuju kuelekea katika ardhi ya Waturuki na kueneza ndani yake ufisadi, kuharibu mimea, mazao na watu (kizazi). Juju na Majuju ni miongoni mwa kizazi cha Adam عليه السلام , kama ilivyonukuliwa katika Sahihi mbili:

«إِنَّ اللَّهَ تَعَالَى يَقُولُ: يَا آدَمُ قَبُولُ: لَيْتَكَ وَسَعْدَيْكَ قَبُولُ: ابْتِثْ بَعَثَ النَّارَ، قَبُولُ: وَمَا بَعَثَ النَّارِ؟ قَبُولُ: مِنْ كُلِّ أَلْفٍ تَسْعِمَائِهِ وَتِسْعَةً وَتِسْعُونَ إِلَى النَّارِ وَوَاحِدٌ إِلَى الْجَنَّةِ، فَحِينِيذٍ تَبِيْبُ الصَّغِيرُ وَتَضَعُ كُلُّ ذَاتِ حَمَلٍ حَمْلَهَا. فَقَالَ: إِنَّ لِيكُمْ أُمَّتَيْنِ مَا كَانَا فِي شَيْءٍ إِلَّا كُنَّا نَأْتِيهِ بِأَجُوجَ وَمَأْجُوجَ»

*“Hakika Allah Aliyetukuka Anasema: ‘Ewe Adam!’ Atasema: ‘Nipo hapa kukuhudumikia’. Allah Atasema: ‘Lete kikundi cha Motoni’. Atasema Adam: ‘Ni lipi kundi la Motoni?’ Atasema: ‘Kwa kila elfu, mia tisa tisini na tisa watakwenda Motoni na mmoja Peponi’. Wakati huo vijana watabadilika kumea mvi na kuzeeka na kila mwanamke mwenye mimba kuzaa. Akasema: ‘Hakika miongoni mwenu mataifa mawili ambayo hawatafikia chochote ila watakishinda kwa idadi yao kubwa, ni Juju na Majuju.’”<sup>1</sup>*

وَجَدَ مِنْ دُونِهِمَا قَوْمًا لَا يَكَادُونَ يَفْقَهُونَ قَوْلًا ﴿١٧﴾

***“Alikuta nyuma yake watu ambao takriban hawakuwa wanafahamu lolote.”***

Maana: Hakufahamu mazungumzo yao kwa kuwa walijitenga na watu wengine.

قَالُوا يَبْدَأُ الْفَرْقَيْنِ إِنْ يَأْجُوجَ وَمَأْجُوجَ مُفْسِدُونَ فِي الْأَرْضِ فَهَلْ نَجْعَلُ لَكَ خَرْجًا

***“Wakasema: Ewe Dhul Qarnayn! Hakika Juju wa Majuju wanafanya uharibifu katika nchi. Basi je, tukulipe ujira.”***

Amepokea Ibn Jurayj kutoka kwa ‘Atwaa’ kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما: “Ujira mkubwa.”<sup>2</sup> Maana: Walikuwa wanataka kukusanya mali baina yao wampe ili aweze kuwajengea kizuizi baina yao na Juju na Majuju. Dhul Qarnayn akasema hali ya kuwa na huruma, ucha Mungu na nia nzuri,

مَا مَكَّنِي فِيهِ رَبِّي حَيْرٌ

***“Yale Mola Wangu Aliyoniwzesha ni bora zaidi.”***

Maana yake: Nguvu na mamlaka Aliyonipa Allah تعالى ni bora kwangu kuliko mlizokusanya. Hii ni kama alivyosema Sulaymaan عليه السلام:

<sup>1</sup> Fat’hul-Baariy 8:295 na Muslim 1:201.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:112. Sanadi yake ni dhaifu.

أَتُمِدُّونَ بِمَالٍ فَمَا آتَيْنَاهُ اللَّهُ خَيْرٌ مِمَّا آتَاكُمْ

**“Je, nyinyi mnanisaidia kwa mali? Aliyonipa Allah ni bora zaidi kuliko Aliyokupeni nyinyi.” (27:36)**

Na hivyo hivyo ndivyo alivyosema Dhul Qarnayn: “Niliyonayo ni bora zaidi kuliko mnazotaka kunipatia, lakini nisaidieni nguvu zenu.” Maana: Kwa amali yenu (vibarua) na ala za ujenzi,

أَجْعَلْ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُمْ رَدْمًا ﴿٣٦﴾ ءَاتُونِي زُبَرَ الْحَدِيدِ

**“Nitakujengeeni kizuizi baina yenu na wao. Nileteeni vipande vya chuma”.**

Zubar ni wingi wa Zubrah, inayomaanisha vipande vya vitu. Hii ilikuwa rai ya Ibn ‘Abbaas, Mujaahid na Qataadah<sup>1</sup> رضي الله عنهم.

Vipande hivi vilikuwa kama matofali, na palisemwa kuwa kila tofali lilikuwa na wizani wa *Qintar* moja ya Dimishq<sup>2</sup> (Damascus) au zaidi.

حَتَّىٰ إِذَا سَاوَىٰ بَيْنَ الصَّدَفَيْنِ

**“Hata alipojaza nafasi iliyo kati ya milima miwili.”**

Maana yake: Aliweka moja juu ya jingine kuanzia chini mpaka akafika juu ya milima, kwa kuijaza mapana yake na urefu wake wa bonde hilo (baina milima hiyo miwili). Wanazuoni wametofautiana hasa katika upana na urefu wake kwa kauli kadhaa.

قَالَ أَنْفُخُوا

**“Akasema: Vukuteni”,**

Maana yake: Aliwasha moto mpaka ikawa sehemu yote hiyo imeshika moto. Hapo,

<sup>1</sup> At-Tabari 18:114.

<sup>2</sup> *Qintar* ni wizani uliosawa na kilogramu 256.4. Tizama maelezo na tafsiri ya Suratul ‘Imraan, 3:14.

قَالَ أَتُونِي أَفْرَغَ عَلَيْهِ قَطْرًا ﴿٣٦﴾

**“Akasema: Niteeni shaba iliyoyayuka niimwagie”.**

Amesema Ibn ‘Abbaas, Mujaahid, ‘Ikrimah, Adh-Dhahaak, Qataadah na As-Suddiy رضي الله عنهم: “Hiyo ni shaba. Baadhi wameongezea iliyoyayuka”<sup>1</sup>. Inatolewa ushahidi kwa Kauli Yake Aliyetukuka:

وَأَسَلْنَا لَهُ عَيْنَ الْقِطْرِ ط

**“Na Tukamyayushia chemchem ya shaba.” (34:12)**

Hivyo inafanana na joho lenye mistari.

Kisha Allah تعالى Akasema:

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:116-117 na Ad-Durr Al-Manthuur 5:460.

فَمَا اسْتَطَعُوا أَنْ يَظْهَرُوهُ وَمَا اسْتَطَعُوا لَهُ نَقْبًا ﴿٧٧﴾  
 قَالَ هَذَا رَحْمَةٌ مِنْ رَبِّي ۖ فَإِذَا جَاءَ وَعْدُ رَبِّي جَعَلَهُ دَكَّاءَ ۗ  
 وَكَانَ وَعْدُ رَبِّي حَقًّا ﴿٧٨﴾ \* وَتَرَكْنَا بَعْضَهُمْ يَوْمَئِذٍ يَمُوجُ  
 فِي بَعْضٍ ۗ وَنُفِخَ فِي الصُّورِ لَجْمَعَنَّهُمْ جَمْعًا ﴿٧٩﴾ وَعَرَضْنَا  
 جَهَنَّمَ يَوْمَئِذٍ لِلْكَافِرِينَ عَرَضًا ﴿٨٠﴾ الَّذِينَ كَانَتْ أَعْيُنُهُمْ فِي  
 غِطَاءٍ عَنِ ذِكْرِي وَكَانُوا لَا يَسْتَطِيعُونَ سَمْعًا ﴿٨١﴾  
 أَفَحَسِبَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنْ يَتَّخِذُوا عِبَادِي مِنْ دُونِي  
 أَوْلِيَاءَ ۗ إِنَّا أَعْتَدْنَا جَهَنَّمَ لِلْكَافِرِينَ نُزُلًا ﴿٨٢﴾ قُلْ هَلْ  
 نُنَبِّئُكُمْ بِالْأَخْسَرِينَ أَعْمَالًا ﴿٨٣﴾ الَّذِينَ ضَلَّ سَعْيُهُمْ فِي  
 الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَهُمْ يُحْسِبُونَ أَنَّهُمْ يُحْسِنُونَ صُنْعًا ﴿٨٤﴾  
 أُولَئِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا بِآيَاتِ رَبِّهِمْ وَلِقَائِهِمْ فَحَبِطَتْ  
 أَعْمَالُهُمْ فَلَا نُقِيمُ لَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ زَنًّا ﴿٨٥﴾ ذَلِكَ  
 جَزَاءُ هُمُومِهِمْ بِمَا كَفَرُوا وَأَتَّخِذُوا آيَاتِي وَرُسُلِي هُزُوعًا ﴿٨٦﴾  
 إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ كَانَتْ لَهُمْ جَنَّاتُ  
 الْفِرْدَوْسِ نُزُلًا ﴿٨٧﴾ خَالِدِينَ فِيهَا لَا يَبْغُونَ عَنْهَا حِوَلًا  
 ﴿٨٨﴾ قُلْ لَوْ كَانَ الْبَحْرُ مِدَادًا لِكَلِمَاتِ رَبِّي لَنَفِدَ الْبَحْرُ  
 قَبْلَ أَنْ تَنْفَدَ كَلِمَاتُ رَبِّي وَلَوْ جِئْتَنَا بِمِثْلِهِ مَدَدًا ﴿٨٩﴾  
 قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِثْلُكُمْ يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَهُكُمُ اللَّهُ وَاحِدٌ ۗ  
 فَمَنْ كَانَ يَرْجُوا لِقَاءَ رَبِّهِ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَالِحًا وَلَا  
 يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِ ۗ أَحَدًا ﴿٩٠﴾

فَمَا اسْتَطَعُوا أَنْ يَظْهَرُوهُ وَمَا  
 اسْتَطَعُوا لَهُ نَقْبًا ﴿٧٧﴾ قَالَ هَذَا  
 رَحْمَةٌ مِنْ رَبِّي ۖ فَإِذَا جَاءَ وَعْدُ رَبِّي  
 جَعَلَهُ دَكَّاءَ ۗ وَكَانَ وَعْدُ رَبِّي حَقًّا  
 ﴿٧٨﴾ \* وَتَرَكْنَا بَعْضَهُمْ يَوْمَئِذٍ  
 يَمُوجُ فِي بَعْضٍ ۗ وَنُفِخَ فِي الصُّورِ  
 لَجْمَعَنَّهُمْ جَمْعًا ﴿٧٩﴾

97. Basi hawakuweza kuukwea, wala hawakuweza kuutoboa.

98. Akasema: Hii ni rehema itokayo kwa Mola Wangu Mlezi. Na itapofika ahadi ya Mola Wangu Mlezi Atauvunjavunja. Na ahadi ya Mola Wangu Mlezi ni kweli tu.

99. Na siku hiyo Tutawaacha wakisongana wao kwa wao. Na baragumu litapulizwa, na wote watakusanywa pamoja.

### Kizuizi Kinawazuia lakini Kitavunjwa Karibu na Kiyama

Allah تعالیٰ Anatupasha habari kuwa Juju na Majuju hawakuweza kukwea kizuizi wala kutoboa na kupita chini yake. Mfumo tofauti wa kitendo umetumika hapa katika andiko la Kiarabu kuonesha na kudhihirisha ugumu wa amali inayohusishwa. Akasema:

﴿فَمَا اسْتَبَعُوا أَنْ يَظْهَرُوهُ وَمَا اسْتَبَعُوا لَهُ نَقَابًا﴾

**“Basi hawakuweza kuukwea, wala hawakuweza kuutoboa”.**

Na hii ni dalili kuwa wao hawawezi kabisa kuutoboa au kufukua chini yake.

Imaam Ahmad ameripoti kuwa Zaynab bint Jahsh رضي الله عنها, mke wa Mtume ﷺ amesema: Mtume ﷺ aliamka kutoka usingizini huku uso wake ukiwa mwekundu na kusema.

«لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَبِئْسَ لِلْعَرَبِ مِنْ شَرِّ قَدٍ اقْتَرَبَ فُتِحَ الْيَوْمَ مِنْ رِذْمِ يَأْجُوجَ وَمَأْجُوجَ  
مِثْلُ حَظَا»

*“Laa ilaaha illa Llaahu (Hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah)! Kuna balaa kubwa kwa Waarabu kutokana na shari inayokaribia. Leo umefunguliwa ukuta wa Juju na Majuju kama hivi”.*

Akatengeneza mduara (kwa kidole gumba na kilichofuatia). Nikasema: ‘Ewe Mtume wa Allah! Tutahiliki hali ya kuwa kati yetu mna watu wema?’ Akanijibu:

«نَعَمْ إِذَا كَثُرَ الْخَبَثُ»

‘Ndiyo, kama watu waovu watazidi’<sup>1</sup>. Hii ni Hadithi iliyo sahihi, iliyonukuliwa na Al-Bukhaari na Muslim<sup>2</sup>. Na Kauli Yake:

«قَالَ هَذَا رَحْمَةٌ مِنْ رَبِّي»

**“Akasema: Hii ni rehema itokayo kwa Mola wangu Mlezi.”**

Maana yake: Ya kujengwa na Dhul Qarnayn.

<sup>1</sup> Ahmad 6:428.

<sup>2</sup> Fat’hul-Baariy 6:440 na Muslim 4:2208.

قَالَ هَذَا رَحْمَةٌ مِّن رَّبِّي ط

**“Akasema: Hii ni rehema itokayo kwa Mola Wangu Mlezi.”**

Kwa watu, alipoweka kizuizi baina yao na Juju na Majuju, kuwazuilia kueneza uchafu, uovu na uharibifu katika ardhi.

فَإِذَا جَاءَ وَعْدُ رَبِّي ط

**“Na itapofika ahadi ya Mola wangu Mlezi.”**

Maana yake: Itakapokaribia ahadi ya kweli,

جَعَلَهُ دَكَّاءَ ط

**“Ataufanya kuwa Dakkaa.”**

Maana yake: Atausawazisha na ardhi. Waarabu walikuwa wakielezea *Dakkaa'* kuwa ni ngamia jike aliye na maungo yaliyo sawasawa na bila ya nundu. Na Amesema Aliyetukuka:

فَلَمَّا تَخَلَّىٰ رَبُّهُ لِلْجَبَلِ جَعَلَهُ دَكًّا

**“Basi Mola Wako Mlezi Alipojionesha kwa jabali Alilifanya ni lenye kuvunjika vunjika.” (7:143)**

Maana yake: likawa sawasawa na ardhi.

وَكَانَ وَعْدُ رَبِّي حَقًّا ﴿١٧﴾

**“Na ahadi ya Mola Wangu Mlezi ni kweli tu.”**

Maana yake: Itakujatokea bila ya shaka yoyote ile. Na Kauli Yake:

✦ وَتَرْكْنَا بَعْضَهُمْ

**“Na siku hiyo Tutawaacha wao.”** Maana yake: Wanadamu, siku hiyo, siku ambayo kizuizi kitavunjwa na hawa watu (Juju na Majuju) watatoka nje na kusonga mbele kuwaelekea watu ili kuharibu mali yao na kuharibu vitu vyao. Na hivi ndivyo alivyosema As-Suddiy katika Kauli Yake:



﴿ وَتَرَكْنَا بَعْضَهُمْ يَوْمَئِذٍ يَمُوجُ فِي بَعْضٍ ۗ ۝٩٧﴾

**“Na siku hiyo Tutawaacha wakizongana wao kwa wao.”**

Akasema: “Hapo ni pale watakapowatokea watu”<sup>1</sup>. Na yote haya yatatokea kabla ya Kiyama na baada ya kuja Dajjaal, kama yatakavyokuja maelezo yake katika Kauli Yake:

حَتَّىٰ ۚ إِذَا فُتِحَتْ يَأْجُوجُ وَمَأْجُوجُ وَهُمْ مِّن كُلِّ حَدَبٍ يَنْسِلُونَ ﴿٩٧﴾ وَأَقْتَرَبَ  
الْوَعْدُ الْحَقُّ

**“Hata watakapofunguliwa Juju na Majuju wakawa wanateremka kutoka kila mlipo (hapo Kiyama kitakuwa tayari). Na itafika ile ahadi ya haki.” (21:96-97).**

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَنُفِخَ فِي الصُّورِ

**“Na Suur litapulizwa.”**

Na As-Suur ni kama ilivyoelezwa katika Hadithi, ni pembe inayopulizwa. Na atakayeipuliza ni Israa'fiil, kama ilivyotangulia kuelezwa kwa kirefu, na zipo Hadithi nyingi katika mada hii<sup>2</sup>.

Kulingana na Hadithi ya 'Atwiyah kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما<sup>3</sup> na Abu Sa'id رضي الله عنه, iliyonasibishwa kwa Mtume ﷺ:

«كَيْفَ أَنْعَمُ وَصَاحِبُ الْقُرْنِ قَدْ أَنْعَمَ الْقُرْنُ وَحَنَى جَبْهَتَهُ وَاسْتَمَعَ مَتَى يُؤْمَرُ؟»

**“Nawezaje kupumzika ilhali sahibu wa pembe (baragumu) ameitia mdomoni na kupiga magoti, huku akingojea amri kutolewa?”**

Wakasema: “Je, tuseme nini?” Akasema:

<sup>1</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 4:454.

<sup>2</sup> Tuhfatul al-Ahwadhiy 9:116.

<sup>3</sup> Tabari 18:122. Sheikh Al-Bani amesema ni sahihi Taz. “Assahiha” (1079)

«قُولُوا: حَسْبُنَا اللَّهُ وَنِعْمَ الْوَكِيلُ عَلَى اللَّهِ تَوَكَّلْنَا»

"Semeni: Allah تعالى Anatutosha (Atatukifia), Naye ni Mlinzi bora kabisa, nasi tumemtegemea Yeye."<sup>1</sup>

Na Kauli Yake:

﴿جَمَعْنَهُمْ جَمْعًا﴾

**"Na wote watakusanywa pamoja",**

Maana yake: Tutawaleta wote kwa ajili ya hesabu.

﴿قُلْ إِنَّ الْأَوَّلِينَ وَالْآخِرِينَ﴾ ﴿لَمَجْمُوعُونَ إِلَىٰ مِيقَاتِ يَوْمٍ مَّعْلُومٍ﴾

**"Sema: Bila shaka wa kwanza na wa mwisho. Watakusanywa kwa wakati uliowekwa katika siku maalumu." (56:49-50).**

Na pia,

﴿وَحَشَرْنَهُمْ فَلَمْ نُغَادِرْ مِنْهُمْ أَحَدًا﴾

**"Nasi siku hiyo Tutawafufua viumbe wote wala Hatutamuacha hata mmoja katika wao." (18:47).**

﴿وَعَرَضْنَا جَهَنَّمَ يَوْمَئِذٍ لِلْكَافِرِينَ عَرْضًا﴾ ﴿الَّذِينَ كَانَتْ أَعْيُنُهُمْ فِي غِطَاءٍ عَنِ ذِكْرِي وَكَانُوا لَا يَسْتَطِيعُونَ سَمْعًا﴾ ﴿أَفَحَسِبَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنْ يَتَّخِذُوا عِبَادِي مِنْ دُونِ أَوْلِيَاءَ إِنََّّا أَعْتَدْنَا جَهَنَّمَ لِلْكَافِرِينَ نُزُلًا﴾

**100. Na siku hiyo Tutawadhihirishia wazi Jahanamu makafiri waione.**

**101. Wale ambao kwamba macho yao yalikuwa paziani hayanikumbuki, na wakawa hawawezi kusikia.**

**102. Je, wanadhani waliokufuru ndio wawafanye waja Wangu ndio walinzi wao badala Yangu Mimi? Hakika Sisi Tumeiandaa Jahanamu iwe ndipo mahala pa kuteremkia makafiri.**

<sup>1</sup> Tuhfatul Al-Ahwadhyy 7:117.

### Jahanamu Itaoneshwa kwa Makafiri Siku ya Kufufuliwa (Kiyama)

Allah تعالی Anatueleza yale Atakayowafanya makafiri Siku ya Kiyama. Atawaonesha Jahanamu, kumaanisha Ataileta mbele yake waone adhabu kabla ya kutiwa ndani yake. Hili litawazidishia majonzi na huzuni. Imenukuliwa katika Sahih Muslim kutoka kwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«يُؤْتَى بِجَهَنَّمَ تَفَادُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ بِسَبْعِينَ أَلْفَ زِمَامٍ، مَعَ كُلِّ زِمَامٍ سَبْعُونَ أَلْفَ مَلَكٍ»

*“Jahanamu italetwa mbele Siku ya Kiyama, ikivutwa na hatamu elfu sabiini, kila mojawapo ikishikwa na Malaika elfu sabiini”<sup>1</sup>.*

Kisha Allah تعالی Anatuambia kuwahuu wao:

الَّذِينَ كَانَتْ أَعْيُنُهُمْ فِي غِطَاءٍ عَنِ ذِكْرِي

***“Wale ambao kwamba macho yao yalikuwa paziani hayanikumbuki.”***

Maana yake: Wameghafilika, wakafumba macho na kuziba masikio, huku wakikataa kukubali uongofu na kufuata ukweli. Amesema Allah تعالی kuhusu hilo:

وَمَنْ يَعِشْ عَنِ ذِكْرِ الرَّحْمَنِ نُقِصْ لَهُ شَيْطَانًا فَهُوَ لَهُ قَرِينٌ ﴿٤٣﴾

***“Anayeyafanyia upofu maneno ya Mwingi wa Rehema Tunamuekea Shetani kuwa rafiki yake.” (43:36)***

Na hapa Allah تعالی Anasema:

وَكَانُوا لَا يَسْتَطِيعُونَ سَمْعًا ﴿٤٤﴾

***“Na wakawa hawawezi kusikia.”***

Maana yake: Hawakufahamu amri na makatazo ya Allah تعالی. Kisha Akasema:

أَفَحَسِبَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنْ يَتَّخِذُوا عِبَادِي مِنْ دُونِي أَوْلِيَاءَ

***“Je, wanadhani waliokufuru ndio wawafanye waja Wangu ndio walinzi wao badala Yangu Mimi?.”***

<sup>1</sup> Muslim 4:2184.

Kumaanisha, je wanadhani kuwa hili ni sawa na kuwa litawasaidia wao?

كَلَّا سَيَكْفُرُونَ بِعِبَادِهِمْ وَيَكُونُونَ عَلَيْهِمْ ضِدًّا ﴿١٠٣﴾

**“Wapi! Watakanusha Ibada yao na watakuwa makhasimu zao.”**  
(19:82).

Na kwa ajili hii Allah تعالى Ametupasha habari kuwa Yeye Amewaandalia Jahanamu Siku ya Kiyama kuwa makazi yao.

قُلْ هَلْ نُنَبِّئُكُمْ بِالْأَخْسَرِينَ أَعْمَالًا ﴿١٠٣﴾ الَّذِينَ ضَلَّ سَعْيُهُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَهُمْ  
يَحْسَبُونَ أَنَّهُمْ مُحْسِنُونَ صُنْعًا ﴿١٠٤﴾ أُولَئِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا بِآيَاتِ رَبِّهِمْ وَلِقَائِهِمْ فَحَبِطَتْ  
أَعْمَالُهُمْ فَلَا نُقِيمُ لَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَزَنًا ﴿١٠٥﴾ ذَلِكَ جَزَاءُهُمْ بِمَا كَفَرُوا وَآخَذُوا  
ءَايَاتِي وَرُسُلِي هُزُؤًا ﴿١٠٦﴾

**103. Sema: Je, Tukutajieni wenye khasara mno katika vitendo vyao?**

**104. Ni wale ambao juhudi yao katika maisha ya dunia imepotea bure, nao wanadhani kwamba wanafanya kazi nzuri.**

**105. Hao ni wale waliozikanusha Ishara za Mola Wao Mlezi na kukutana Naye. Kwa hivyo vitendo vyao vimepotea bure, na wala Siku ya Kiyama Hatutawathamini kitu.**

**106. Hiyo Jahanamu ni malipo yao kwa walivyokufuru na wakafanyia kejeli Ishara Zangu na Mitume Wangu.**

### **Waliokhasirika Mno kwa Matendo Yao na Malipo Wanayostahili**

Amepokea Al-Bukhaariy kutoka kwa ‘Amr kutoka kwa Musw’ab ambaye amesema: “Nilimuuliza babangu, yaani Sa’d bin Abi Waqqaasw رضي الله عنه kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

قُلْ هَلْ نُنَبِّئُكُمْ بِالْأَخْسَرِينَ أَعْمَالًا ﴿١٠٣﴾

**‘Sema: Je, Tukutajieni wenye khasara mno katika vitendo vyao?’**

"Je, wao ni *Haruuriyyah*?" Akasema: "Hapana, wao ni Mayahudi na Manasara. Ama kuhusu Mayahudi, wamemkanusha Muhammad ﷺ na ama Manasara, wamekanusha Pepo na wakasema kuwa hakuna chakula wala kinywaji huko, na *Haruuriyyah* ni wale wenye kuvunja ahadi baada ya kuiridhia". Sa'd رضي الله عنه alikuwa akiwaita *al-Faasiqun* (mafasiiki/ waasi)<sup>1</sup>. 'Ali bin Abi Twaalib<sup>2</sup>, Adh-Dhahaak na wengine رضي الله عنهم wamesema: "Hao ni *Haruuriyyah*". Hivyo hii inamaanisha, kulingana na 'Ali, Aya hii inajumuisha *Haruuriyyah*, kama inavyowajumlisha Mayahudi, Manasara na wengineo. Hii haimanishi kuwa aya hii iliteremshwa kuhusiana khasa na pote lolote lile; hakika ni kuwa Aya yenyewe ni ya jumla sana kuliko hivyo, kwa sababu aya yenyewe iliteremshwa Makka, kabla ya Qur'ani kuwazungumzia Mayahudi na Manasara, na kabla ya kuanzishwa kwa kundi la Khawarij. Hivyo, aya kwa ujumla inamhusisha kila mmoja anayemuabudu Allah تعالى kwa njia isiyokubalika, akidhania kuwa yuko sawa katika kufanya hilo na kuwa amali yake itakubaliwa, lakini amekosea sana na amali yake itakataliwa. Kama Anavyosema Allah تعالى:

وَجُوهٌ يَوْمَئِذٍ خَشِيعَةٌ ﴿٢٤﴾ عَامِلَةٌ نَّاصِبَةٌ ﴿٢٣﴾ تَصَلَّىٰ نَارًا حَامِيَةً ﴿٢٢﴾

**"Nyuso siku hiyo ni zenye kudhalilika. Ni zenye kufanya kazi ngumu kabisa, zichoke. Waingie katika moto uwakao kweli kweli." (88:2-4).**

Na Amesema Aliyetukuka:

وَقَدِمْنَا إِلَىٰ مَا عَمِلُوا مِنَّ عَمَلٍ فَجَعَلْنَاهُ هَبَاءً مَّنثُورًا ﴿٢٣﴾

**"Na Tutayaendea yale waliyoyatenda katika amali; Tuzifanye kama mavumbi yaliyotapanywa." (25:23).**

Na Amesema Aliyetukuka:

وَالَّذِينَ كَفَرُوا أَعْمَلُهُمْ كَسَرَابٍ بِقِيَعَةٍ مَّحْسَبُهُ الظَّمْثَانُ مَاءٌ حَتَّىٰ إِذَا جَاءَهُ لَمْ يَجِدْهُ  
شَيْعًا

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baari 8:278.

<sup>2</sup> Tabari 18:128.

***“Na wale waliokufuru, vitendo vyao ni kama mazigazi, jangwani, mwenye kiu huyadhani ni maji, akiyaendea hayaoni chochote...”***  
(24:39)

Na Akasema Allah تعالى katika Aya hii Tukufu:

قُلْ هَلْ نُنَبِّئُكُمْ

***“Sema: Je, Tukutajieni.”***

Maana yake: Tukupasheni habari,

بِأَلْحَسْرِينَ أَعْمَلَاءَ

***“Wenye khasara mno katika vitendo vyao?.”***

Kisha Allah تعالى Akaifasiri kwa Kusema:

الَّذِينَ ضَلَّ سَعْيُهُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا

***“Ni wale ambao juhudi yao katika maisha ya dunia imepotea bure.”***

Maana yake: Walifanya amali ya batili, amali iliyokwenda kinyume na njia ya sheria, inayoridhiwa na kukubaliwa na Allah تعالى. Hata hivyo,

وَهُمْ يَحْسَبُونَ أَنَّهُمْ مُحْسِنُونَ صُنْعًا

***“Nao wanadhani kwamba wanafanya kazi nzuri.”***

Maana yake: Wanaitakidi kuwa wao wanafanya jambo lenye msingi na kuwa wanakubaliwa na kupendwa. Na Kauli Yake:

أُولَئِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا بِآيَاتِ رَبِّهِمْ وَلِقَائِهِمْ

***“Hao ni wale waliozikanusha Ishara za Mola wao Mlezi na kukutana naye.”***

Maana yake: Walikanusha Ishara za Allah تعالى duniani, dalili Alizoziweka zinazothibitisha ya kuwa Yeye ni Mmoja na ukweli wa Mitume Wake, na kukataa kuwepo kwa Akhera.

فَلَا تُقِيمُ هُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَرَنَا ﴿١٠٧﴾

**“Na wala Siku ya Kiyama Hatutawathamini kitu.”**

Maana yake: Hatutazifanya mizani zao kuwa nzito kwa sababu hazina mema yoyote yale. Amepokea Al-Bukhaariy kutoka kwa Abu Hurayrah عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّهُ لَيَأْتِي الرَّجُلُ الْعَظِيمُ السَّمِينُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ لَا يَزِنُ عِنْدَ اللَّهِ جَنَاحَ بُعُوضَةٍ - وَقَالَ: - اقْرَأُوا إِنَّ شِئْنَكُمْ: ﴿فَلَا تُقِيمُ هُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَرَنَا﴾»

*“Hakika atakuja mtu Siku ya Kiyama aliye mkubwa na mnene, lakini wizani wake mbele ya Allah hautazidi ule wa bawa la mbu. Akasema, soma ukitaka: ‘Na wala Siku ya Kiyama Hatutawathamini kitu.’*

Pia imenukuliwa na Muslim.<sup>1</sup> Na Kauli Yake:

ذَلِكَ جَزَاءُ هُمْ جَهَنَّمَ بِمَا كَفَرُوا

**“Hiyo Jahanamu ni malipo yao kwa walivyokufuru.”**

Maana yake: Hakika Tutawaadhibu kwa hilo kwa sababu ya kufuru yao na kuwa wamechukua Ishara na Miujiza ya Allah تعالى na Mitume Wake kama stihzai, wakiwadhihaki na kuwakejeli na kuwakanusha kabisa.

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ كَانَتْ هُمْ جَنَّتِ الْفِرْدَوْسِ نُزُلًا ﴿١٠٨﴾ خَالِدِينَ فِيهَا

لَا يَبْغُونَ عَنْهَا حِوَلًا ﴿١٠٩﴾

**107. Hakika wale walioamini na wakatenda mema mashukio yao yatakuwa kwenye Pepo za Firdausi.”**

**108. Watadumu humo; hawatataka kuondoka.”**

<sup>1</sup> Fat’hul-Baariy 8:279 na Muslim 4:2147.

## Jaza ya Waumini Wema

Allah تعالى Anatupasha habari ya waja Wake walio wema, waliomuamini Allah na Mitume Wake na kuukubali ukweli ulioletwa na Mitume. Anatuambia kuwa hao watapata bustani ya *Al-Firdaws* (Pepo). Amesema Abu Umaamah: “*Al-Firdaws* ni katikati ya Pepo.”<sup>1</sup> Na Qataadah amesema: “*Al-Firdaws* ni mlima Peponi, ulio katikati na bora mno (kuliko sehemu nyengine)”<sup>2</sup>. Hakika hii imepokewa *Marfuu* kutoka kwa Samurah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«الْفِرْدَوْسُ رُبُّهُ الْجَنَّةِ أَوْسَطُهَا وَأَحْسَنُهَا»

“*Al-Firdaws* ni kilima Peponi, kilicho katikati na bora mno”.

Na imepokewa na Qataadah kutoka kwa Anas bin Maalik رضي الله عنه *Marfuu* kama hivyo. Riwaya zote hizi zimepokewa na Ibn Jariir (Allah Amrehemu)<sup>3</sup>. Na katika Sahihi:

«إِذَا سَأَلْتُمْ اللَّهَ الْجَنَّةَ، فَاسْأَلُوهُ الْفِرْدَوْسَ فَإِنَّهُ أَعْلَى الْجَنَّةِ وَأَوْسَطُ الْجَنَّةِ، وَمِنْهُ تَمَجَّرُ أَنْهَارُ الْجَنَّةِ»

“Mnapomuomba Allah Pepo, basi muombeni *Al-Firdaws*, kwani hiyo ndiyo sehemu ya juu kabisa Peponi na iliyo katikati na kutoka kwayo mito ya Peponi itatokea.”<sup>4</sup>

Na Kauli Yake:

تَوَلَّأَ

“**Mashukio yao (pumbao lao).**” Maana: Ugeni na kukirimiwa katika mashukio ya ugeni. Na Kauli Yake:

خَلِيدِينَ فِيهَا

“**Wataadumu humo.**” Maana yake: Watakaa humo milele na hawataondoka.

لَا يَتُغَوَّنَ عَنْهَا حَوْلًا

“**Hawatataka kuondoka.**” Maana yake: Hawatachagua au kutaka kitu chengine chochote.

<sup>1</sup> Tabari 18:130.

<sup>2</sup> Tabari 18:130.

<sup>3</sup> Tabari 18:134.

<sup>4</sup> Fat'hul Al-Baariy 13:415.



Aya hii inatuelezea jinsi gani wataipenda na kuitamani, japokuwa huenda mtu akadhania kuwa yeyote atakayekaa mahali pamoja daima dawamu atachoka kwayo. Lakini Allah تعالى Anatuambia kuwa mbali na kukaa huku milele, hawatachagua kubadilisha sehemu hiyo yao kwa kuondoka wala safari au badali.

قُلْ لَوْ كَانَ الْبَحْرُ مَدَادًا لَكَلِمَتِ رَبِّي لَنَفِدَ الْبَحْرُ قَبْلَ أَنْ تَنفِدَ كَلِمَتُ رَبِّي وَلَوْ جِئْنَا

بِمِثْلِهِ مَدَدًا ﴿١٠٩﴾

**109. Sema: Lau kuwa bahari ndio wino kwa Maneno ya Mola Wangu Mlezi, basi bahari ingelimalizika kabla ya kumalizika Maneno ya Mola Wangu Mlezi, hata Tungeliileta mfano wa hiyo kuongezea.**

### Maneno ya Mola Mlezi Hayamaliziki

Anasema Aliyetukuka: “Sema, ewe Muhammad, lau maji ya bahari yangekuwa wino kwa kalamu iandike Maneno ya Allah تعالى, Hekima Zake na Ishara zilizo na dalili ya kuwepo Yeye, bahari ingemalizika kabla ya kumalizika kuandikwa yote hayo.”

وَلَوْ جِئْنَا بِمِثْلِهِ

**“Hata Tungeliileta mfano wa hiyo.”** Maana: Mfano wa bahari kama hiyo ya awali, kisha nyengine, na kadhalika, bahari nyengine zitakazotumiwa kuandikia. Maneno ya Allah تعالى hayatamalizika kabisa. Kama Alivyosema:

وَلَوْ أَنَّمَا فِي الْأَرْضِ مِنْ شَجَرَةٍ أَقْلَمٌ وَالْبَحْرُ يَمُدُّهُ مِنْ بَعْدِهِ سَبْعَةُ أَبْحُرٍ مَا نَفِدَتْ

كَلِمَتُ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿١٠٩﴾

**“Na lau kama miti yote iliyomo katika ardhi ingalikuwa kalamu, na bahari hii (ikafanywa wino), na ikasaidiwa na bahari nyingine saba, Maneno ya Allah yasingalikwisha. Bila shaka Allah ni Mwenye Nguvu na Mwenye Hekima.” (31:27).**

Na amesema Ar-Rabi’ bin Anas: “Mfano wa elimu ya wanadamu wote kulinganisha na Elimu ya Allah تعالى, ni kama tone la maji kulinganisha na bahari zote”. Na hakika Allah تعالى Ameteremsha hiyo:

قُلْ لَوْ كَانَ الْبَحْرُ مِدَادًا لِكَلِمَاتِ رَبِّي لَنَفِدَ الْبَحْرُ قَبْلَ أَنْ تَنفَدَ كَلِمَاتُ رَبِّي

**“Lau kuwa bahari ndio wino kwa Maneno ya Mola Wangu Mlezi, basi bahari ingelimalizika kabla ya kumalizika Maneno ya Mola Wangu Mlezi”.**

Allah Aliyetukuka Anasema, “Kuwa lau bahari hizo zingekuwa wino kwa Maneno ya Allah تعالى, na miti yote ikawa kalamu, kalamu zitavunjika na maji ya bahari yatakauka, na Maneno ya Allah تعالى yatabaki, kwani Maneno Yake hayamalizwi na chochote wala lolote. Hakika ni kuwa hakuna anayeweza kufahamu Ukubwa Wake wala Kumsifu kama Anavyostahiki Kusifiwa, ila Yeye Anajisifu Mwenyewe. Hakika Mola Wetu Mlezi kama Anavyosema na Yu juu kwa tunayosema. Mfano wa neema za dunia hii, ya mwanzo na mwisho wake, kulinganisha na neema za Akhera ni kama mfano wa mbegu ya haradali ikilinganishwa na ulimwengu mzima.

قُلْ إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَهُكُمُ اللَّهُ وَاحِدٌ ۖ فَمَن كَانَ يَرْجُوا لِقَاءَ رَبِّهِ

فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَالِحًا وَلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِ ۚ أَحَدًا ﴿١١٠﴾

**110. Sema: Mimi ni mwanadamu kama nyinyi. Ninaletewa Wahyi kwamba Mungu wenu ni Mungu Mmoja. Mwenye kutaraji kukutana na Mola Wake Mlezi basi na atende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola Wake Mlezi.**

**Muhammad ﷺ ni Mwanadamu na Mtume, na Mungu ni Mmoja**

Allah تعالى Anamuambia Mtume Wake, Muhammad ﷺ:

قُلْ

**“Sema.”** Kuwaambia hawa washirikina wanaokanusha Utume wako kwao,

إِنَّمَا أَنَا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ

**“Hakika mimi ni mwanadamu kama nyinyi.”** Hivyo, yeyote anayedai kuwa mimi ni muongo basi aje na kama niliyokuja nayo. Hakika ni kuwa mimi sijui ghaibu, mambo yaliyopita mlioniuliza, nami nikawaambia miongoni mwa hayo ni kisa cha watu wa pangoni na habari za Dhul Qarnayn, visa vya kweli ambavyo sikuvijua ila kwa Aliyonijulisha Allah تعالى. Nami nawaambia,

أَنَّمَا إِلَهُكُمُ

**“Kwamba Mungu wenu.”** Ambaye ninakuiteni katika kumuabudu Yeye tu,

إِلَهُهُ وَاحِدٌ

**“Ni Mungu Mmoja.”** Naye hana mshirika.

فَمَنْ كَانَ يَرْجُوا لِقَاءَ رَبِّهِ

**“Mwenye kutaraji kukutana na Mola wake Mlezi.”** Maana yake: Thawabu na jaza za nzuri,

فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَالِحًا

**“Basi na atende vitendo vyema.”** Maana yake: Vinavyoafikiana na sheria ya Allah تعالى.

وَلَا يُشْرِكْ بِعِبَادَةِ رَبِّهِ أَحَدًا

**“Wala asimshirikishe yeyote katika ibada ya Mola Wake Mlezi.”**

Hayo ni kwa yule anayetaka Radhi ya Allah تعالى Peke Yake asiye na mshirika na yeyote yule. Na hizi mbili ni nguzo muhimu kwa amali inayokubaliwa: Hapana budi amali hiyo ifanywe kwa ikhlasi na nia nzuri kwa ajili ya Allah تعالى, na pia iende sanjari na njia na sheria ya Mtume ﷺ.

Amepokea Imaam Ahmad kutoka kwa Mahmuud bin Labiid رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ أَخْوَفَ مَا أَخَافَ عَلَيْكُمُ الشِّرْكَ الْأَضْعَرُ»

**“Hakika ninachowahofia nyinyi sana ni shirki ndogo”.**

Wakasema: “Na shirki ndogo ni nini, ewe Mtume wa Allah?” Akasema:

«الرِّيَاءُ، يَقُولُ اللَّهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ إِذَا جَزَى النَّاسَ بِأَعْمَالِهِمْ: اذْهَبُوا إِلَى الَّذِينَ كُنتُمْ تُرَاءُونَ فِي الدُّنْيَا، فَانظُرُوا هَلْ تَجِدُونَ عِنْدَهُمْ جَزَاءً؟»

**“Ar-Riyaa’ (kujionesha). Allah Atasema Siku ya Kiyama, watu wanapolipwa kwa amali zao: Nendeni kwa wale mliokuwa mkijionesha duniani, mtizame ikiwa mtapata malipo yoyote kwao”<sup>1</sup>.**

<sup>1</sup> Ahmad 5:428.

Amepokea Imaam Ahmad kutoka kwa Abi Said bin Abi Fadhwaalah Al-Answaariy رضي الله عنه, naye alikuwa miongoni mwa Maswahaba amesema: Nimemsikia Mtume ﷺ akisema:

«إِذَا جَمَعَ اللَّهُ الْأَوَّلِينَ وَالْآخِرِينَ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ لِيَوْمٍ لَا رَيْبَ فِيهِ نَادَى مُنَادٍ: مَنْ كَانَ أَشْرَكَ فِي عَمَلٍ عَمِلَهُ اللَّهُ أَحَدًا فَلْيَطْلُبْ ثَوَابَهُ مِنْ عِنْدِ غَيْرِ اللَّهِ، فَإِنَّ اللَّهَ أَعْتَى الشُّرَكَاءَ عَنِ الشُّرِكِ»

*“Pindi Allah Atakapowajumuisha Siku ya Kiyama, wa mwanzo na wa mwisho, Siku ambayo haina shaka. Ataita muitaji: ‘Yeyote aliyekuwa akimshirikisha Allah katika amali aliyokuwa akiifanya, atake thawabu zake kutoka kwa asiyekuwa Allah, kwani Allah Hana haja ya mshirika au msaidizi.”<sup>1</sup>*

Hii pia imeripotwa na at-Tirmidhi na Ibn Maajah<sup>2</sup>.

Mwisho wa Tafsiri ya *Suratul Kahf*.




---

<sup>1</sup> Ahmad 4:215.

<sup>2</sup> Tuhfat Al-Ahwadhiy 8:599 na Ibn Maajah 2:1406.

## Tafsiri ya Suratu Maryam

### Sura ya 19

#### Iliteremshwa Makkah

Muhammad bin Is-haaq رحمه الله تعالى amepokea Hadithi kutoka kwa Umm Salamah رضي الله عنها<sup>1</sup> katika Siirah, na Imaam Ahmad bin Hambal رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه, kisa cha Hijrah (kuhama) ya kuelekea Habashah (Ethiopia) kutoka Makkah. Mapokezi yanataja kuwa Ja'far bin Abi Twaalib رضي الله عنه alimsomea Mfalme Najaashi na watu wake sehemu ya kwanza ya Sura hii.<sup>2</sup>



---

<sup>1</sup> Ibn Hishaam, 1:357.

<sup>2</sup> Ahmad 1:201, 461.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُوْرَةُ الْمَرْيَمِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

كَهَيْعَصَ ۝ ذُكِّرَ رَحْمَتَ رَبِّكَ عَبْدَهُ زَكْرِيَّا ۝ إِذْ نَادَى رَبَّهُ نِدَاءً خَفِيًّا ۝ قَالَ رَبِّ إِنِّي وَهَنَ الْعَظْمُ مِنِّي وَأَشْتَعَلَ الرَّأْسُ شَيْبًا وَلَمْ أَكُنْ بِدُعَائِكَ رَبِّ شَقِيًّا ۝ وَإِنِّي خِفْتُ الْمَوَالِيَ مِنْ وَرَائِي وَكَانَتِ امْرَأَتِي عَاقِرًا فَهَبْ لِي مِنْ لَدُنْكَ وَلِيًّا ۝ يَرِثُنِي وَيَرِثُ مِنْ آلِ يَعْقُوبَ ۝ وَاجْعَلْهُ رَبِّ رَضِيًّا ۝ بِنَزَكِرْيَا إِنَّا نُبَشِّرُكَ بِغُلَامٍ اسْمُهُ يَحْيَىٰ لَمْ نَجْعَلْ لَهُ مِنْ قَبْلُ سَمِيًّا ۝ قَالَ رَبِّ أَنَّى يَكُونُ لِي غُلَامٌ وَكَانَتِ امْرَأَتِي عَاقِرًا وَقَدْ بَلَغْتُ مِنَ الْكِبَرِ عِتِيًّا ۝ قَالَ كَذَلِكَ قَالَ رَبُّكَ هُوَ عَلَيَّ هَيِّنٌ وَقَدْ خَلَقْتُكَ مِنْ قَبْلُ وَلَمْ تَكُ شَيْئًا ۝ قَالَ رَبِّ اجْعَلْ لِي آيَةً ۝ قَالَ آيَتُكَ أَلَّا تُكَلِّمَ النَّاسَ ثَلَاثَ لَيَالٍ سَوِيًّا ۝ فَخَرَجَ عَلَى قَوْمِهِ مِنَ الْمِحْرَابِ فَأَوْحَىٰ إِلَيْهِمْ أَنْ سَبِّحُوا بِكُرَّةٍ وَعَشِيًّا ۝

كَهَيْعَصَ ۝ ذُكِّرَ رَحْمَتَ رَبِّكَ  
عَبْدَهُ زَكْرِيَّا ۝ إِذْ نَادَى  
رَبَّهُ نِدَاءً خَفِيًّا ۝ قَالَ رَبِّ إِنِّي  
وَهَنَ الْعَظْمُ مِنِّي وَأَشْتَعَلَ الرَّأْسُ  
شَيْبًا وَلَمْ أَكُنْ بِدُعَائِكَ رَبِّ  
شَقِيًّا ۝ وَإِنِّي خِفْتُ الْمَوَالِيَ مِنْ  
وَرَائِي وَكَانَتِ امْرَأَتِي عَاقِرًا فَهَبْ  
لِي مِنْ لَدُنْكَ وَلِيًّا ۝ يَرِثُنِي  
وَيَرِثُ مِنْ آلِ يَعْقُوبَ ۝ وَاجْعَلْهُ رَبِّ  
رَضِيًّا ۝

1. Kaf Ha Ya 'Ayn Swaad.

2. Huu ni Ukumbusho wa rehema ya Mola wako Mlezi kwa mja Wake, Zakariyya.

3. Alipomuita Mola wake Mlezi kwa siri.

4. Akasema: Mola wangu Mlezi! Mifupa yangu imedhoofika, na kichwa kinameremeta kwa mvi; wala sikuwa mwenye bahati mbaya, (mwenye kukhasirika) Mola wangu, kwa kukuomba Wewe.

5. Na hakika mimi nawakhofia jamaa zangu baada yangu. Na mke wangu ni tasa. Basi nipe mrithi kutoka Kwako.

**6. Atakaye nirithi mimi na awarithi ukoo wa Ya'qub. Ewe Mola wangu Mlezi! Na umjaalie awe mwenye kuridhisha.**

**Kisa cha Zakaria عليه السلام na Kuomba Kwake Mtoto**

Ama mazungumzo kuhusu herufi *Muqatwa'ah* (zilizo katwa au zilizo mbali mbali) yameshatangulia mwanzo wa Suratul Baqarah. Na Kauli Yake:

ذِكْرُ رَحْمَتِ رَبِّكَ

***"Huu ni Ukumbusho wa rehema ya Mola wako Mlezi",***

Maana yake: Huu ni ukumbusho wa rehema ya Allah تعالى juu ya mja Wake, Zakariyya عليه السلام<sup>1</sup>. Yahya bin Ya'mur aliisoma,

(ذَكَرَ رَحْمَةَ رَبِّكَ عَبْدَهُ زَكَرِيَّا)

"Amekukumbusha kuhusu rehema ya Mola wako Mlezi kwa mja Wake Zakariyya".

Neno Zakariyya عليه السلام katika Aya linasomwa kwa kuvuta (kurefusha) na kufupisha. Visomo vyote vinajulikana na ni mashuhuri. Alikuwa ni Mtume miongoni mwa Mitume wa Bani Israili. Katika Sahihi Al - Bukhaari, imeripotiwa kuwa Mtume alisema kuhusu Zakariyya عليه السلام kuwa alikuwa seremala aliyekuwa akila kwa alichochuma kwa mikono yake kwa ufundi seremala<sup>2</sup>. Na Kauli Yake:

إِذْ نَادَى رَبَّهُ نِدَاءً خَفِيًّا ﴿١٩٠﴾

***"Alipomuita Mola wake Mlezi kwa siri".***

Hakika yeye aliomba kwa siri kwa kuwa kufanya hivyo kunapendwa zaidi na Allah تعالى. Hii ni sawa na vile alivyosema Qataadah kuhusu Aya hii,

إِذْ نَادَى رَبَّهُ نِدَاءً خَفِيًّا ﴿١٩٠﴾

***"Alipomuita Mola wake Mlezi kwa siri".***

Hakika Allah تعالى Anajua na kuufahamu moyo wenye kumcha Mungu, na Anasikia mwito wa siri<sup>3</sup>.

<sup>1</sup> Al-Qurtwubiy 11:75.

<sup>2</sup> Muslim 4:1847. Hatukuweza kuipata katika Al-Bukhaari.

<sup>3</sup> Atw-Twabariy 18:142.

قَالَ رَبِّ إِنِّي وَهَنَ الْعَظْمُ مِنِّي

**“Akasema: Mola wangu Mlezi! Mifupa yangu imedhoofika”,**

Maana yake: Nimedhoofika na nguvu zimepungua.

وَأَشْتَعَلَ الرَّأْسُ شَيْبًا

**“Na kichwa kinameremeta kwa mvi.”**

Maana: Weusi wa nywele zangu umeshaondoka. Lengo kuu ni kufahamisha udhaifu wake na ukongwe, kwa dalili za nje na ndani. Na Kauli Yake:

وَلَمْ أَكُنْ بِدُعَائِكَ رَبِّ شَقِيًّا

**“wala sikuwa mwenye bahati mbaya, Mola wangu, kwa kukuomba Wewe.”**

Maana yake: Sijapata kuomba kitu Kwako ila Unanijibu na Kunikubalia dua zangu na Hutanikatalia kile ninacho kuomba”. Na Kauli Yake:

وَلِيَّ خِيفَتُ الْمَوْلَىٰ مِن وَّرَائِي

**“Na hakika mimi nawakhofia jamaa zangu baada yangu”.**

Amesema Mujaahid, Qatadah na As-Suddiy: “Katika kusema neno *Mawaali*, yeye (Zakariyya عليه السلام) inamaanisha jamaa wanaokuja baada yake.”<sup>1</sup> Sababu ya khofu yake ni kuwa alihofia kuwa kizazi kitakachomfuata kitakuwa kizazi kibaya. Hivyo, akamuomba Allah تعالى Ampe mtoto atakaye kuwa Mtume baada yake, atakayewaongoza kwa utume wake na kile alichoteremshiwa.

Kujibu haya ningependa kufafanua kuwa hakuogopa kurithiwa mali yake. Hakika ni kuwa daraja ya Nabii ni kubwa sana na hadhi ya juu kuliko kujuta juu ya mali kwa hali hii. Mtume hatachukia kuacha mali yake kwa jamaa zake wanaomfuata, na hivyo akaomba kupata kijana atakayepata urithi badala yao. Hii ni hoja moja.

Ya pili ni kuwa Allah تعالى hakutaja kuwa yeye (Zakariyya عليه السلام) alikuwa tajiri. Kinyume na hivyo, alikuwa seremala aliyekuwa akila kwa mapato ya kufanya kazi kwa mikono yake. Mtu wa aina hii kwa kawaida hana mali nyingi. Kukusanya mali si jambo la kawaida kwa Manabii, hakika ni kuwa wao walikuwa ni wenye kujinyima sana katika maisha ya hapa duniani.

<sup>1</sup> At-Tabari 18:144.



Hoja ya tatu ni kuwa imeripotwa katika Sahihi mbili, katika mapokezi zaidi ya moja kuwa Mtume ﷺ amesema,

«لَا نُورُتُ، مَا تَرَكْنَا فَهُوَ صَدَقَةٌ»

*“Sisi (Mitume) haturithiwi, tunachoacha (katika mali) ni sadaka.”*<sup>1</sup>

Na katika riwaya ya At-Tirmidhiy ikiwa na Isnadi iliyo Sahihi, amesema,

«نَحْنُ مَعَسَرُ الْأَنْبِيَاءِ لَا نُورُتُ»

*“Sisi kongamano la Manabii haturithiwi (hatuachi mali ya kurithiwa).”*<sup>2</sup>

Kwa hiyo, maana ya Hadithi hizi zinabainisha kauli ya Zakariyya عليه السلام,

فَهَبْ لِي مِنْ لَدُنْكَ وَلِيًّا ﴿١٩٦﴾ يَرِثُنِي

***“Basi nipe mrithi kutoka Kwako. Atakayenirithi mimi...”***

Urithi wa unabii. Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Amesema:

وَوَيْرِثُ مِنْ آءَالٍ يَعْقُوبُ ﴿١٩٧﴾

***“Na awarithi ukoo wa Ya’qub.”***

Hii ni sawa na Kauli ya Allah تعالى:

وَوَيْرِثُ سُلَيْمَنُ دَاوُدَ ﴿١٩٨﴾

***“Na Sulaymaan alimrithi Daawuud.” (27:16).***

Hii ina maana kuwa alirithi Unabii kutoka kwake. Lau maana hii ingemaanisha mali (na utajiri), asingemuhusisha yeye peke yake na kuwaacha ndugu zake wengine.

Pia isingekuwa na faida ya kulitaja jambo hilo lau ungekuwa utajiri ndio unaokusudiwa. Ni maarufu na inajulikana katika sheria zote zilizopita na itikadi ya ufunuo unaotoka kwa Allah, kuwa mtoto anarithi mali ya babake. Kwa hivyo, ‘lau’ hii haihusishi aina maalumu ya urithi, Allah تعالى Hangeitaja. Yote haya yanaungwa mkono na kuyakinishwa na Hadithi Sahihi:

<sup>1</sup> Fat’h Al-Baariy 6:227 na Muslim 3:1383.

<sup>2</sup> Tuhfat Al-Ahwadhyy 5:234.

نَحْنُ مَعَاشِرَ الْأَنْبِيَاءِ لَا نُورِثُ، مَا تَرَكْنَا فَهُوَ صَدَقَةٌ

*“Sisi, kongamano la Manabii hatuachi urithi wowote (haturithiwi). Tunayoacha ni sadaka”<sup>1</sup>.*

Mujaahid amesema kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

يَرِثُنِي وَيَرِثُ مِنْ آلِ يَعْقُوبَ

***“Atakayenirithi mimi na awarithi ukoo wa Ya’qub.”***

Maana: Urithi wake ni elimu, na Zakariyya عليه السلام alikuwa ni miongoni mwa ukoo wa Ya’qub عليه السلام<sup>2</sup>. Hushaym amesema: “Ismaa’il bin Abi Khaalid ametufahamisha kuwa Abu Swaalih amefasiri Aya hii:

يَرِثُنِي وَيَرِثُ مِنْ آلِ يَعْقُوبَ

***“Atakayenirithi mimi na awarithi ukoo wa Ya’qub.”***

Maana yake: Atakuwa Nabii kama mababu zake waliokuwa pia ni Manabii<sup>3</sup>. Na Kauli Yake:

وَأَجْعَلُهُ رَبِّ رَضِيًّا

***“Ewe Mola wangu Mlezi! Na Umjaalie awe mwenye kuridhiwa.”***

Maana yake: Mfanye ni mwenye kuridhiwa Nawe (Allah تعالى) na viumbe Vyako. Mpende na mfanye ni mwenye kupendwa na viumbe Vyako, katika Dini yake, maadili na tabia zake.

يَنزَكِينَا إِنَّا نُبَشِّرُكَ بِغُلَامٍ اسْمُهُ يَحْيَى لَمْ نَجْعَلْ لَهُ مِنْ قَبْلُ سَمِيًّا

**7. (Akaambiwa): Ewe Zakariyya! Hakika Sisi Tunakubashiria mwana; jina lake ni Yahya. Hatujapata kumpa jina hilo yeyote kabla yake.**

<sup>1</sup> Tuhfat Al-Ahwadhiy 5:234.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:146.

<sup>3</sup> At-Tabari 18:146.

**Kuitikiwa kwa Dua Yake**

Maneno haya yanamaanisha kuwa dua yake imekubaliwa. Akaambiwa:

يَنْزَكِرِيَا إِنَّا نُبَشِّرُكَ بِغُلْمٍ أَسمُهُ سَيِّحِي

**“Ewe Zakariyya! Hakika Sisi Tunakubashiria mwana; jina lake ni Yahya”.**

Hivyo hivyo, Allah تعالى Amesema:

هُنَالِكَ دَعَا زَكَرِيَّا رَبَّهُ ۖ قَالَ رَبِّ هَبْ لِي مِنْ لَدُنْكَ ذُرِّيَّةً طَيِّبَةً ۗ إِنَّكَ سَمِيعُ الدُّعَاءِ ﴿٦٨﴾ فَنَادَتْهُ الْمَلَائِكَةُ وَهُوَ قَائِمٌ يُصَلِّي فِي الْمِحْرَابِ أَنَّ اللَّهَ يُبَشِّرُكَ بِيَحْيَىٰ مُصَدِّقًا بِكَلِمَةٍ مِنَ اللَّهِ وَسَيِّدًا وَحَصُورًا وَنَبِيًّا مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٦٩﴾

**“Pale pale Zakariyya akamuomba Mola wake Mlezi, akasema: Mola wangu Mlezi! Nipe kutoka kwako uzao mwema. Wewe Ndiye Unayesikia maombi. Alipokuwa kasimama chumbani akiswali, Malaika kamnadia: Hakika Allah Anakubashiria Yahya, atayekuwa mwenye kusadikisha neno litokalo kwa Allah, na ni bwana na mtawa na Nabii kwa watu wema.” (3:38-39).**

Na Kauli Yake:

لَمْ نَجْعَلْ لَهُ مِنْ قَبْلُ سَمِيًّا ﴿٧٠﴾

**“Hatujapata Kumpa jina hilo yeyote kabla yake.”**

Qatadah, Ibn Jurayj na Ibn Zayd wamesema: “Hii inamaanisha kuwa hakukuwa na yeyote mwenye jina hilo kabla yake”<sup>1</sup>. Ibn Jariir رحمه الله تعالى aliifadhilisha tafsiri hii, Allah تعالى Amrehemu.

قَالَ رَبِّ أَنَّى يَكُونُ لِي غُلْمٌ وَكَانَتِ امْرَأَتِي عَاقِرًا وَقَدْ بَلَغْتَ مِنَ الْكِبَرِ عِتِيًّا ﴿٧٠﴾  
قَالَ كَذَلِكَ قَالَ رَبُّكَ هُوَ عَلَيَّ هَيِّنٌ وَقَدْ خَلَقْتُكَ مِنْ قَبْلُ وَلَمْ تَكُ شَيْئًا ﴿٧١﴾

<sup>1</sup> At-Tabari 18:148.

**8. Akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Vipi nitakuwa na mwana na hali mke wangu ni tasa, na mimi nimeshafikia ukongwe katika uzee?**

**9. Akasema: Ndio hivyo hivyo Amesema Mola wako Mlezi: Haya ni mepesi Kwangu. Na hakika Mimi Nilikwisha Kukuumba wewe zamani na hali hukuwa kitu.**

### **Kustaajabu Kwake Baada ya Kujibiwa Dua Yake**

Zakariyya عليه السلام alistaajabu pale Dua yake ilipojibiwa na kupewa bishara njema ya kupata mtoto wa kiume. Alifurahi sana na kuuliza kijana huyo atazaliwa namna gani, na atakuja kwa njia gani. Hili lilikuwa ni jambo la kustaajabisha kwa kuwa mkewe alikuwa ajuza na tasa na hakuwahi kupata mtoto katika maisha yake yote. Hata Zakariyya عليه السلام mwenyewe alikuwa tayari amekuwa mzee, mifupa yake imedhoofika na membamba na hakuwa na mbegu (manii) zilizokuwa zenye uwezo (wa kuzalisha) na nguvu ya kujimai.

### **Jibu la malaika**

قَالَ

**“Akasema”,**

Maana yake: Malaika, kumjibu Zakariyya عليه السلام kwa kustaajabu kwake,

كَذَلِكَ قَالَ رَبُّكَ هُوَ عَلَيَّ هَيِّنٌ

**“Ndio hivyo hivyo Amesema Mola wako Mlezi: Haya ni mepesi Kwangu”.**

Kumaanisha kuzaliwa kwa mtoto kutatokea kwako na mkeo huyu, na sio kutoka kwa mwengine (mke mwengine). Na Kauli Yake:

هَيِّنٌ

**“Wepesi”,**

Maana: Ni sahali na wepesi sana kwa Allah تعالى Kufanya hivyo. Kisha yeye (Malaika) akamtajia yeye (Zakaria) kilichokuwa cha kustaajabisha zaidi kuliko alichouliza. Malaika alimuambia kuwa Mola Mlezi Amesema:

وَقَدْ خَلَقْتَلِك مِنْ قَبْلُ وَلَمْ تَكُ شَيْئًا ﴿١١﴾

**“Na hakika Mimi Nilikwisha Kukuumba wewe zamani na hali hukuwa kitu”.**

Hii ni kauli iliyo sawa na Kauli Yake, Allah تعالى:

هَلْ أَتَى عَلَى الْإِنْسَانِ حِينٌ مِّنَ الدَّهْرِ لَمْ يَكُنْ شَيْئًا مَّذْكُورًا ﴿١١﴾

**“Hakika kilimpitia binadamu kipindi fulani katika dahari ambapo hakuwa kitu kinachotajwa.” (76:1).**

قَالَ رَبِّ اجْعَلْ لِي آيَةً ۚ قَالَ آيَاتُكَ أَلَّا تُكَلِّمَ النَّاسَ ثَلَاثَ لَيَالٍ سَوِيًّا ﴿١٠﴾ فَخَرَجَ عَلَى قَوْمِهِ مِنَ الْمِحْرَابِ فَأَوْحَى إِلَيْهِمْ أَنْ سَبِّحُوا بُكْرَةً وَعَشِيًّا ﴿١١﴾

**10. Akasema: Mola wangu Mlezi nijaalie Ishara. Akasema Ishara yako ni kuwa hutasema na watu kwa siku tatu, na hali ni mzima.**

**11. Basi akawatokea watu wake kutoka mihirabuni. Akawaashiria: Msabihini Allah asubuhi na jioni.**

## Alama ya Ujauzito

Allah عليه السلام, Anatuarifu kuhusu alichosema Zakariyya

قَالَ رَبِّ اجْعَلْ لِي آيَةً

**“Akasema: Mola wangu Mlezi nijaalie Ishara”.**

Nipe ishara na dalili za kuwepo kwa kile Ulichoniahidi, ili roho yangu itulie na moyo wangu pia uwe katika hali ya utulivu kwa ahadi Yako. Hivyo hivyo, Ibrahim عليه السلام alisema:

رَبِّ أَرِنِي كَيْفَ تُحْيِي الْمَوْتَى ۗ قَالَ أُولَئِمُتُؤْمِنٌ ۗ قَالَ بَلَىٰ وَلَئِن لِّيَطْمِئِنَّ قُلُوبِي ۗ

**“Na aliposema Ibraahim: Mola wangu Mlezi! Nioneshe vipi unavyofufua wafu. Allah Akasema: Kwani huamini? Akasema: Hasha! Lakini ili moyo wangu utue.” (2:260).**

Kisha Allah تعالى Akasema:

قَالَ ءَايَتُكَ

**“Akasema Ishara yako.”**

Maana yake: Ishara yako itakuwa,

أَلَّا تُكَلِّمَ النَّاسَ ثَلَاثَ لَيَالٍ سَوِيًّا ﴿٤١﴾

**“Ni kuwa hutasema na watu kwa siku tatu, na hali ni mzima”.**

Hii inamaanisha, ulimi wako utazuiliwa kuzungumza kwa siku tatu ilhali wewe ni mzima kabisa, bila ya kuwa mgonjwa. Ibn ‘Abbaas, Mujaahid, Ikrimah, Wahb, As-Suddiy, Qatadah na wengineo wamesema: “Ulimi wake ulizuiliwa bila ya maradhi au ugonjwa wowote”<sup>1</sup>. ‘Abdur- Rahman bin Zayd bin Aslam amesema: “Alikuwa akisoma na kumtakasa Allah تعالى, lakini hakuweza kuzungumza na watu wake isipokuwa kwa ishara”<sup>2</sup>. Amepokea Al-‘Awfiy kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema:

ثَلَاثَ لَيَالٍ سَوِيًّا ﴿٤١﴾

**“Kwa siku tatu, na hali ni mzima’.**

Siku hizo zilikuwa zinafuatana”. Hata hivyo, kauli ya kwanza iliyonukuliwa kutoka kwake na jamhuri (walio wengi) ni sahihi zaidi. Aya hii ni sawa na ile Aliyosema Allah تعالى, katika Suratul Al- ‘Imraan:

قَالَ رَبِّ اجْعَلْ لِي آيَةً ۗ قَالَ ءَايَتُكَ ۗ أَلَّا تُكَلِّمَ النَّاسَ ثَلَاثَةَ أَيَّامٍ إِلَّا رَمًا ۗ وَادُّكُرْ رَبَّكَ

كَثِيرًا وَسَبِّحْ بِالْعَشِيِّ وَالْإِبْكَرِ ﴿٤١﴾

**“Akasema: Mola wangu Mlezi! Niwekee alama. Akasema: Alama yako ni kuwa hutasema na watu kwa siku tatu, isipokuwa kwa kuashiria tu. Na mdhukuru Mola Mlezi wako kwa wingi na mtakase jioni na asubuhi.” (3:41).**

<sup>1</sup> At-Tabari 18:152.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:152.

Hii ni dalili kuwa hakuzungumza na watu wake kwa siku tatu na mchana wake. Uzungumzi wake ulikuwa,

إِلَّا رَمَزًا

**“Ila kwa ishara.”**

Maana yake: Kwa kutumia ishara za kimwili, hii ndiyo sababu kwa Allah تعالى Kusema katika Aya Tukufu:

خَرَجَ عَلَى قَوْمِهِ مِنَ الْمِحْرَابِ

**“Basi akawatokea watu wake kutoka mihirabuni.”**

Kumaanisha ile sehemu ambayo alipatiwa hiyo bishara njema ya kupata mtoto. Na Kauli Yake:

فَأَوْحَىٰ إِلَيْهِمْ

**“Akawaashiria.”**

Maana yake: kwa kutumia ishara kwao ambayo ilikuwa ya ustadi na ya haraka.

أَنْ سَبَّحُوا بُكْرَةً وَعَشِيًّا ﴿١٩﴾

**“Msabihini Allah asubuhi na jioni.”**

Maana yake: Wanatakiwa wakubali kwa aliyoamrisha kufanya katika siku tatu hizo, kuongeza amali zake na shukrani zake kwa Allah تعالى kwa Aliyompa. Mujaahid amesema:

فَأَوْحَىٰ إِلَيْهِمْ

**“Akawaashiria.”**

Alitoa ishara<sup>1</sup>. Wahb na Qataadah wamesema hivyo hivyo<sup>2</sup>.

\* \* \*

<sup>1</sup> At-Tabari 18:153.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:154.

يَبْحَثُ خُذِ الْكِتَابَ بِقُوَّةٍ ۗ وَءَاتَيْنَاهُ الْحَكْمَ صَبِيًّا ۗ  
 وَحَنَانًا مِّن لَّدُنَّا وَزَكَاةً ۗ وَكَانَ تَقِيًّا ۗ  
 وَلَمْ يَكُن جَبَّارًا عَصِيًّا ۗ وَسَلَّمٌ عَلَيْهِ يَوْمَ وُلِدَ وَيَوْمَ  
 يَمُوتُ وَيَوْمَ يُبْعَثُ حَيًّا ۗ وَأذْكُرْ فِي الْكِتَابِ مَرْيَمَ إِذِ  
 انْتَبَذَتْ مِنْ أَهْلِهَا مَكَانًا شَرِيًّا ۗ فَاتَّخَذَتْ مِنْ دُونِهِمْ  
 حِجَابًا فَأَرْسَلْنَا إِلَيْهَا رُوحَنَا فَتَمَثَّلَ لَهَا بَشَرًا سَوِيًّا ۗ  
 قَالَتْ إِنِّي أَعُوذُ بِالرَّحْمَنِ مِنْكَ إِنْ كُنْتَ تَقِيًّا ۗ قَالَتْ  
 إِنَّمَا أَنَا رَسُولُ رَبِّكِ لِأَهَبَ لَكِ غُلَامًا زَكِيًّا ۗ قَالَتْ  
 أَنَّى يَكُونُ لِي غُلَامٌ وَلَمْ يَمَسِّنِي بَشَرٌ وَلَمْ أَكُ بَغِيًّا ۗ  
 قَالَ كَذَلِكَ قَالَ رَبُّكَ هُوَ عَلَىٰ هَيِّئٍ ۗ وَلَنَجْعَلَ لَآيَةً  
 لِلنَّاسِ وَرَحْمَةً مِنَّا ۗ وَكَانَ أَمْرًا مَّقْضِيًّا ۗ فَحَمَلَتْهُ  
 فَانْتَبَذَتْ بِهِ مَكَانًا قَصِيًّا ۗ فَأَجَاءَهَا الْمَخَاضُ إِلَىٰ  
 جِذْعِ النَّخْلَةِ قَالَتْ يَلَيْتَنِي مِتُّ قَبْلَ هَذَا وَكُنْتُ نَسِيًّا  
 مِّنْسِيًّا ۗ فَوَدَّعْنَاهَا مِنْ تَحْتِهَا أَلَّا تَحْزَنِي قَدْ جَعَلَ رَبُّكِ  
 تَحْتَكِ سَرِيًّا ۗ وَهَزِيءَ إِلَيْكِ بِجِذْعِ النَّخْلَةِ تُسَاقِطُ  
 عَلَيْكَ رُطْبًا جَنِيًّا ۗ فَكُلِي وَاشْرَبِي وَعَيْنًا مُّنِيًّا ۗ فَإِمَّا  
 تَرَيْنَ مِنَ الْبَشَرِ أَحَدًا فَقُولِي إِنِّي نَذَرْتُ لِلرَّحْمَنِ صَوْمًا فَلَنْ  
 أُكَلِّمَ الْيَوْمَ إِنْسِيًّا ۗ

يَبْحَثُ خُذِ الْكِتَابَ بِقُوَّةٍ ۗ  
 وَءَاتَيْنَاهُ الْحَكْمَ صَبِيًّا ۗ وَحَنَانًا  
 مِّن لَّدُنَّا وَزَكَاةً ۗ وَكَانَ تَقِيًّا ۗ  
 وَلَمْ يَكُن جَبَّارًا عَصِيًّا ۗ وَسَلَّمٌ عَلَيْهِ يَوْمَ وُلِدَ وَيَوْمَ  
 يَمُوتُ وَيَوْمَ يُبْعَثُ حَيًّا ۗ

**12. Ewe Yahya! Kishike Kitabu kwa nguvu! Nasi Tulimpa hekima angali mtoto.**

**13. Na Tukampa huruma itokayo Kwetu, na utakaso, na akawa mchamungu.**

**14. Na akawa mwema kwa wazazi wake, wala hakuwa jabari muasi.**

**15. Na amani iwe juu yake siku ya kuzaliwa, na siku ya kufa, na siku ya kufufuliwa.**

**Kuzaliwa kwa Kijana na Sifa Zake na Tabia Zake**

Hii pia inamaanisha kwa yasiyotajwa, kuwa kijana aliyehidiwa alizaliwa na

ndiye aliyekuwa Yahya عليه السلام. Pia kuna kidokezi kuwa Allah تعالی Alimfundisha Kitabu, Tawrati ambacho walikuwa wakikisoma baina yao. Manabii waliotumwa kwa Mayahudi walikuwa waki hukumu kulingana na Tawrati, kama



walivyokuwa wanazuoni na waalimu miongoni mwao. Alikuwa bado mdogo Allah تعالى Alipompata elimu hii. Hii ndiyo sababu ambayo Allah تعالى Ameitaja. Kwa sababu ya vipi Allah تعالى Alimneemesha pamoja na wazazi wake, Anasema:

يَنْحَيِّ حُدِّ الْكِتَابِ بِقُوَّةٍ

***“Ewe Yahya! Kishike Kitabu kwa nguvu!”***

Maana yake: Jifunze Kitabu kwa nguvu. Kwa maneno mengine, kisome vizuri na vyema kabisa, kwa makini na bidii ya juu. Na Kauli Yake:

وَأَتَيْنَهُ الْحُكْمَ صَبِيًّا

***“Nasi Tulimpa hekima angali mtoto.”***

Hii inamaanisha alipatiwa ufahamu, elimu, ushupavu, uvumilivu, juhudi na ari katika mambo ya kheri na utafutaji mazuri. Alibarikiwa na sifa hizi kemkemu japokuwa alikuwa kijana mdogo. Allah تعالى Anasema:

وَحَنَانًا مِّن لَّدُنَّا

***“Na Tukampa hanaan itokayo Kwetu.”***

Amepokea ‘Aliy bin Abi Twalhah kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema:

وَحَنَانًا مِّن لَّدُنَّا

***“Na Tukampa hanaan itokayo Kwetu.”***

Maana yake: ‘Rehema na Huruma kutoka Kwetu’<sup>1</sup>. ‘Ikrimah, Qataadah na Adh-Dhahaak wote wamesema hivyo hivyo.

Adh- Dhahaak ameongeza, “Rehema na Huruma ambayo hakuna awezaye kumpatia ila Sisi (Yeye, Allah تعالى).”

Qataadah ameongeza: “Kwayo, Allah تعالى Alikuwa na Huruma na Zakariyya عليه السلام<sup>2</sup>. Mujaahid amesema:

<sup>1</sup> At-Tabari 18:156.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:156.

وَحَنَانًا مِّن لَّدُنَّا

**“Na Tukampa hanaan itokayo Kwetu.”**

‘Huu ni ule upole kutoka kwa Mola wake Mlezi juu yake’. Maana ya dhahiri ni kuwa Kauli ya Allah تعالى ‘Hanaan’ (huba, huruma, kite) inakwenda sambamba na Kauli Yake,

وَأَتَيْنَاهُ الْحِكْمَ صَبِيًّا

**“Nasi Tulimpa hekima angali mtoto.”**

Maana yake: Tulimpa hekima, huruma na utakaso. Hii inamaanisha kuwa alikuwa mtu mwenye huruma, mchamngu. *Hanaan* ina maana upendo huba na ulaini (kwa wengine).

Kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

وَزَكَاةً

**“Na Zakatan.”**

Hii inahusiana na Kauli Yake:

وَحَنَانًا

**“Na Hanaan.”**

Neno *Zakaah* lina maana utakaso kutokana na uchafu, uovu na madhambi. Qataadah amesema: “Neno *Zakaah* lina maana ya matendo mema.”<sup>1</sup>

Adhw-Dhwahhaak na Ibn Jurayj wamesema: “Tendo jema ni amali safi (*Zakaah*).”<sup>2</sup> Al-‘Awfiy amepokea kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuwa amesema:

وَزَكَاةً

**“Na Zakatan.”**

Maana yake: Alikuwa ni wa baraka. Pia,

<sup>1</sup> At-Tabari 18:159.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:159.

وَكَانَ تَقِيًّا ﴿١٢﴾

**“Na akawa mchamungu.”**

Maana yake: Alikuwa twahara, safi na hakuegemea kufanya madhambi<sup>2</sup>. Allah تعالی Amesema:

وَبَرًّا بِوَالِدَيْهِ وَلَمْ يَكُنْ جَبَّارًا عَصِيًّا ﴿١٣﴾

**“Na akawa mwema kwa wazazi wake, wala hakuwa jabari muasi.”**

Baada ya Allah تعالی kutaja utiifu wa Yahya عليه السلام kwa Mola wake Mlezi na kuwa Allah تعالی Amemuumba akiwa amejawa na huruma, utakaso na uchamungu, Aliufungamanisha kwa utiifu wake kwa wazazi wake na kuwatendea wema. Allah تعالی Ametaja kuwa alijitenga na kujiweka mbali na kuwaasi wao (wazazi) katika maneno, vitendo, amri na makatazo.

Kwa ajili hii, Allah تعالی Anasema:

وَلَمْ يَكُنْ جَبَّارًا عَصِيًّا ﴿١٤﴾

**“Wala hakuwa jabari muasi.”**

Baada ya kutaja sifa hizi nzuri, Allah تعالی Anataja malipo Yake kwayo,

وَسَلَّمْ عَلَيْهِ يَوْمَ وُلِدَ وَيَوْمَ يَمُوتُ وَيَوْمَ يُبْعَثُ حَيًّا ﴿١٥﴾

**“Na amani iwe juu yake siku ya kuzaliwa, na siku ya kufa, na siku ya kufufuliwa.”**

Hii inamaanisha kuwa yeye ana usalama na hifadhi katika hali hizi tatu. Sufyaan bin ‘Uyaynah amesema: “Upweke kabisa ambao mtu anaweza kuhisi ni katika hali tatu. Hali ya kwanza ni anapozaliwa, anapojiona anatoka kule alikokuwa. Hali ya pili, ni siku anayokufa, anapowaona watu ambao hatawaona tena. Na hali ya tatu, ni siku anapofufuliwa, anapojiona akiwa katika mkusanyiko mkubwa. Allah تعالی Amempa Yahya عليه السلام, mtoto wa Zakariyya عليه السلام, hadhi ya kipekee, kwa Kumpa amani katika hali hizi. Allah تعالی Anasema:

<sup>1</sup> At-Tabari 18:159 na Ad-Durr Al-Manthuur 5:486.

وَسَلَّمْ عَلَيْهِ يَوْمَ وُلِدَ وَيَوْمَ يَمُوتُ وَيَوْمَ يُبْعَثُ حَيًّا ﴿٢٦﴾

**'Na amani iwe juu yake siku ya kuzaliwa, na siku ya kufa, na siku ya kufufuliwa'.**

Riwaya hii imepokewa na Ibn Jariir رحمه الله تعالى kutoka kwa Ahmad bin Manswuur Al-Marwazi, kutoka kwa Swadaqah bin Al-Fadhwi, kutoka kwa Sufyaan bin 'Uyaynah.

وَأَذْكُرُ فِي الْكِتَابِ مَرْيَمَ إِذِ انْتَبَدَتْ مِنْ أَهْلِهَا مَكَانًا شَرْقِيًّا ﴿٢٧﴾ فَأَخَذَتْ مِنْ دُونِهِمْ حِجَابًا فَأَرْسَلْنَا إِلَيْهَا رُوحَنَا فَتَمَثَّلَ لَهَا بَشَرًا سَوِيًّا ﴿٢٨﴾ قَالَتْ إِنِّي أَعُوذُ بِالرَّحْمَنِ مِنْكَ إِنْ كُنْتَ تَقِيًّا ﴿٢٩﴾ قَالَ إِنَّمَا أَنَا رَسُولُ رَبِّكِ لِأَهَبَ لَكِ غُلَامًا زَكِيًّا ﴿٣٠﴾ قَالَتْ أَنَّى يَكُونُ لِي غُلَامٌ وَلَمْ يَمَسِّنِي بَشَرٌ وَلَمْ أَكُ بَغِيًّا ﴿٣١﴾ قَالَ كَذَلِكَ قَالَ رَبُّكَ هُوَ عَلَىٰ هَيِّئٍ وَلِنَجْعَلَكَ آيَةً لِلنَّاسِ وَرَحْمَةً مِنَّا وَكَاتِبٌ أَمْرًا مَّقْضِيًّا ﴿٣٢﴾

**16. Na mtaje Maryam katika Kitabu, pale alipojitenga na jamaa zake mahali upande wa mashariki;**

**17. Na akaweka pazia kujikinga nao. Tukampelekea Roho wetu, akajifananisha kwake sawa na mtu.**

**18. (Maryam) akasema: Hakika mimi najikinga kwa Mwingi wa Rehema aniepushe nawe, ukiwa ni mchamungu.**

**19. (Malaika) akasema: Hakika mimi ni mwenye kutumwa na Mola wako Mlezi ili nikubashirie tunu ya mwana aliyetakasika.**

**20. Akasema: Nitampataje mwana hali mwanadamu yeyote hajanigusa, wala mimi si kahaba?**

**21. (Malaika) akasema: Ndio hivyo hivyo! Mola wako Mlezi Amesema: Haya ni mepesi Kwangu! Na ili Tumfanye kuwa ni Ishara kwa watu, na Rehema itokayo Kwetu, na hilo ni jambo lililokwisha hukumiwa.**

### Kisa cha Maryam na Al-Masih (Isa عليه السلام)

Baada ya Allah تعالى, Kutaja kisa cha Zakariyya عليه السلام, na kuwa Alimbariki na Kumneemsha mtoto mchamungu, twahara na mwenye baraka hata uzeeni mwake ilhali mkewe alikuwa tasa, kisha Anataja kisa cha Maryam. Allah تعالى Anatupasha kumpatia yeye mtoto aliyelitwa Isa عليه السلام bila ya kupitia baba (katika mimba yake). Kwa visa hivi viwili tunapata mahusiano sawa na muafaka. Kwa ajili ya ukaribu baina yao katika maana, Allah تعالى Amevitaja hapa pamoja, vile vile katika Surah Al-'Imraan na Al-Anbiyaa'. Allah تعالى Ametaja visa hivi kuwaonesha waja Wake Uweza Wake, Nguvu za Mamlaka Yake na kuwa Yeye Ana Nguvu juu ya kila kitu. Allah تعالى Anasema:

وَأَذْكُرُ فِي الْكِتَابِ مَرْيَمَ

**“Na mtaje Maryam katika Kitabu”.**

Yeye alikuwa Maryam bint 'Imraan kutoka katika familia na ukoo wa Nabii Dawuud عليه السلام. Alitoka katika familia nzuri iliyokamilika katika Wana wa Israili. Allah تعالى Alitutajia kisa cha uzazi wa mama yake katika Suratul 'Imraan, na kuwa yeye (mama wa Maryam) alimtoa kumtumikia Allah تعالى. Hii inamaanisha kuwa alimtoa mtoto (Maryam) kuwa wakfu kuuhudumia Msikiti Mtukufu. Na walikuwa wanajikurubisha katika hilo.

فَتَقَبَّلَهَا رَبُّهَا بِقَبُولٍ حَسَنٍ وَأَنْبَتَهَا نَبَاتًا حَسَنًا

**“Tena Mola wake Mlezi Akampokea kwa mapokeo mema na Akamkuza makuzo mema.” (3:37).**

Hivyo, Maryam alilelewa kati ya Wana wa Israili kwa njia nzuri, ya heshima. Alikuwa mmoja wa wanawake waliokuwa wakiabudu, aliyejulikana kwa amali zake njema za 'Ibaadah, aliyeshika Dini na mvumilivu. Aliishi chini ya uangalizi na ulezi wa shemeji yake, Zakariyya عليه السلام, aliyekuwa Nabii wa Wana wa Israili wakati huo. Alikuwa mtu mkubwa miongoni mwao, waliokuwa wakimuuliza mambo yao ya kidini. Zakariyya عليه السلام aliona miujiza na mambo ya ajabu kutoka kwake yaliyomstaajabisha sana.

كُلَّمَا دَخَلَ عَلَيْهَا زَكَرِيَّا الْمِحْرَابَ وَجَدَ عِنْدَهَا رِزْقًا قَالَ يَمْرُؤُا أَنَّى لَكَ هَذَا قَالَتْ

هُوَ مِنْ عِنْدِ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٣٧﴾

***“Kila mara Zakariyya alipoingia chumbani kwake alimkuta na vyakula. Basi alimuambia: Ewe Maryam! Unavipata wapi hivi? Naye akasema: Hivi vinatoka kwa Allah; na Allah Humruzuku Amtakaye bila ya hesabu.” (3:37).***

Imeelezwa kuwa alikuwa akimkuta na matunda ya wakati wa baridi katika siku za joto na yale ya wakati wa joto siku za baridi. Haya tayari yameelezwa katika Suratul ‘Imraan. Kisha, pale Allah تعالى Alipotaka Kumpa mja na Mtume Wake, Isa عليه السلام, mmoja kati ya Mitume mitano watukufu na wakubwa.

إِذْ أَنْتَبَدْتِ مِنْ أَهْلِهَا مَكَانًا شَرْقِيًّا ﴿١٦﴾

***“Pale alipojitenga na jamaa zake mahali upande wa mashariki.”***

Maana yake: Alitoka na kujitenga na watu wake. Alikwenda upande wa mashariki wa Msikiti Mtukufu (uliopo Al-Quds). Imeripotwa kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuwa amesema: “Hakika, mimi ni mjuzi zaidi katika viumbe wa Allah تعالى hivi ni kwa nini Wakristo walichukua mashariki kuwa sehemu yao ya kuelekea katika ‘Ibaadah zao.

Walifanya hilo kwa ajili ya Kauli ya Allah تعالى,

إِذْ أَنْتَبَدْتِ مِنْ أَهْلِهَا مَكَانًا شَرْقِيًّا ﴿١٦﴾

***‘Pale alipojitenga na jamaa zake mahali upande wa mashariki.’***

Hivyo, wamechukua alipozaliwa Isa عليه السلام kuwa ndio sehemu ya kuelekea katika ‘Ibaadah”<sup>1</sup>. Na Kauli Yake Allah تعالى,

فَأَخَذَتْ مِنْ دُونِهِمْ حِجَابًا

***“Na akaweka pazia kujikinga nao.”***

Maana yake: Alijificha na kujisitiri kutokana nao. Kisha, Allah تعالى Alimtuma Jibril رحمه الله تعالى kwake:

فَتَمَثَّلَ لَهَا بَشَرًا سَوِيًّا ﴿١٧﴾

***“Akajifananisha kwake sawa na mtu.”***

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:162.

Maana yake: Alikuwa kwake kama mwanadamu aliye sawa kabisa. Mujaahid, Adh-Dhahaak, Qatadah, Ibn Jurayj, Wahbi bin Munabbih na As - Suddiy wote wamefasiri Kauli ya Allah تعالى:

فَأَرْسَلْنَا إِلَيْهَا رُوحَنَا ﴿١٥﴾

**“Tukampelekea Roho wetu.”**

Maana yake: Malaika Jibril رحمه الله تعالى.<sup>1</sup> Na Kauli Yake:

قَالَتْ إِنِّي أَعُوذُ بِالرَّحْمَنِ مِنْكَ إِنْ كُنْتَ تَقِيًّا ﴿١٦﴾

**“(Maryam) akasema: Hakika mimi najikinga kwa Mwingi wa Rehema Aniepushe nawe, ukiwa ni mchamungu.”**

Maana yake: Pindi Malaika Jibril عليه السلام alipojitokeza kwake kama mwanadamu, alipokuwa katika maficho yake yaliyokuwa na sitara baina yake na watu wake, aliogopa na kudhania kuwa mtu huyo anataka kumnajisi (kumbaka). Hivyo, akasema:

إِنِّي أَعُوذُ بِالرَّحْمَنِ مِنْكَ إِنْ كُنْتَ تَقِيًّا ﴿١٦﴾

**“Hakika mimi najikinga kwa Mwingi wa Rehema Aniepushe nawe, ukiwa ni mchamungu.”**

Kwa kusema hivyo, alimaanisha: “Ikiwa unamcha Allah تعالى”, kama njia ya kumkumbusha yeye na Allah تعالى. Hili ndilo jambo lililowekwa katika sheria ya kumlinda na kumhifadhi mtu dhidi ya uovu, ili liweze kuepukwa kwa usahali. Kwa hiyo, jambo la kwanza alilofanya ni kujaribu kumhofisha na Allah تعالى, Mwenye Nguvu na Shani. Amepokea Ibn Jariir رحمه الله تعالى kutoka kwa ‘Aswim kuwa Abu Wa’il amesema alipotaja kisa cha Maryam, “Alijua kuwa mchamungu (mtu mwema) atajiepusha (kutenda baya) aliposema,

إِنِّي أَعُوذُ بِالرَّحْمَنِ مِنْكَ إِنْ كُنْتَ تَقِيًّا ﴿١٦﴾ قَالَ إِنَّمَا أَنَا رَسُولُ رَبِّكِ

**‘Hakika mimi najikinga kwa Mwingi wa Rehema Aniepushe nawe, ukiwa ni mchamungu. (Malaika) akasema: Hakika mimi ni mwenye kutumwa na Mola wako Mlezi’.**

<sup>1</sup> At-Tabari 18:163.

Hii inamaanisha kuwa Malaika alimjibu, na ili kuondosha hofu aliyokuwa akihisi ndani yake, 'Sivyo unavyodhanika, lakini mimi ni mjumbe wa Mola wako Mlezi'. Kwa hili alimaanisha, Allah تعالى Amenituma kwako<sup>1</sup>".

Panasemwa kuwa pindi tu alipotaja jina la *Ar-Rahman* (Mwingi wa Rehema), Jibril عليه السلام alipomoka na kurudi katika umbile lake (la Malaika). Hapo akamjibu,

(إِنَّمَا أَنَا رَسُولُ رَبِّكِ لِیَهَبَ لَكِ غُلَامًا زَكِيًّا)

"Hakika mimi ni mwenye kutumwa na Mola wako Mlezi ili nikubashirie tunu ya mwana aliyetakasika".

Na Kauli Yake:

قَالَتْ أَنَّى يَكُونُ لِي غُلَامٌ

**"Akasema: Nitampataje mwana."**

Hii inamaanisha kuwa Maryam alishangazwa na hilo. Akasema: "Vipi nitapata mtoto?" Alisema hayo kumaanisha, "Kwa njia gani mtoto atazaliwa na mimi ilhali mimi sina mume wala sijafanya kitendo chochote kibaya (yaani kuzini)?"

Kwa sababu hiyo, alisema:

وَلَمْ يَمَسَّ سِنِيَّ بِشَرٍّ وَلَمْ أَكُ بَغِيًّا

**"Hali mwanadamu yeyote hajanigusa, wala mimi si Baghiyya?."**

*Baghiyy*ni mwanamke mzinifu.

Kwa ajili hii, Hadithi imeripotiwa kuharamisha pesa zinazochumwa kutokana na uzinzi<sup>2</sup>.

Na Kauli Yake:

قَالَ كَذَلِكَ قَالَ رَبُّكَ هُوَ عَلَيَّ هَيِّنٌ

**"(Malaika) akasema: Ndio hivyo hivyo! Mola wako Mlezi Amesema: Haya ni mepesi Kwangu!."**

<sup>1</sup> At-Tabari 18:164.

<sup>2</sup> Ahmad 1:235



Hii ina maana kuwa Malaika alimuambia kumjibu swali lake, “Hakika, Allah تعالى Ameshasema kuwa mtoto wa kiume atazaliwa nawe japokuwa huna mume wala hukufanya uasherati. Bila shaka, Yeye ni Muweza kufanya Alitakalo”. Kwa ajili hii, yeye (Jibril) alifikisha ujumbe wa Maneno ya Allah تعالى:

وَلَتَجْعَلَنَّ آيَةً لِلنَّاسِ

**“Na ili Tumfanye kuwa ni Ishara kwa watu.”**

Maana yake: dalili na ishara kwa watu kwa nguvu za Mtengenezaji na Muumba, Aliyefanya anuwai katika maumbile yao. Alimuumba baba yao, Adam عليه السلام, bila ya mwanaume (baba) wala mwanamke (mama). Kisha, Akamuumba Hawa (mke wa Adam) kwa baba bila mwanamke (mama). Kisha, Akawaumba vizazi vyao kutokana na mwanamme na mwanamke, isipokuwa Isa عليه السلام. Alimfanya Isa عليه السلام kuzaliwa na mwanamke bila mwanamme. Hivyo, Allah تعالى Alikamilisha aina nne za Uumbaji (wa wanadamu), zinazoonesha Ukamilifu wa Nguvu Zake na Utukufu wa Mamlaka Yake. Hapana mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Yeye tu na hakuna Mola Mlezi wa kweli ila Yeye. Ama kuhusu Kauli Yake:

وَرَحْمَةً مِنَّا

**“Na Rehema itokayo Kwetu.”**

Maana yake: Tutamfanya kijana huyu rehema kutoka kwa Allah تعالى na pia atakuwa Nabii miongoni mwa Manabii. Atawaita watu wamuabudu Allah تعالى na Imani ya kumpwekesha Yeye. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka katika Aya nyengine:

إِذْ قَالَتِ الْمَلَأِكَةُ يَمْزِمْ إِنَّ اللَّهَ يُبَشِّرُكَ بِكَلِمَةٍ مِّنْهُ اسْمُهُ الْمَسِيحُ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ

وَجِيهًا فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَمِنَ الْمُقَرَّبِينَ ﴿١٩﴾ وَيُكَلِّمُ النَّاسَ فِي الْمَهْدِ وَكَهْلًا وَمِنَ

الصَّالِحِينَ ﴿٢٠﴾

**“Na pale Malaika waliposema: Ewe Maryam! Hakika Allah Anakubashiria (mwana) kwa neno litokalo Kwake. Jina lake ni Masihi Isa mwana wa Maryam, mwenye heshima katika dunia na Akhera, na miongoni mwa waliokaribishwa (kwa Allah). Naye**

***atazungumza na watu katika utoto wake na katika utuuzima wake, na atakuwa katika watu wema.” (3:45-46).***

Hii inamaanisha kuwa yeye atawaita katika kumuabudu Mola wake Mlezi katika utoto wake na pia akiwa mtu mzima. Na Kauli Yake:

وَكَانَ أَمْرًا مَّقْضِيًّا ﴿١٦﴾

***“Na hilo ni jambo liliokwisha hukumiwa”.***

Huu ndio mwisho wa mazungumzo baina ya Jibril عليه السلام na Maryam. Alimjulisha kuwa jambo hili tayari limepitishwa na Nguvu na Matakwa ya Allah تعالى. Muhammad bin Is-haaq رحمه الله تعالى amesema:

وَكَانَ أَمْرًا مَّقْضِيًّا ﴿١٦﴾

***“Na hilo ni jambo liliokwisha hukumiwa”.***

Hii inamaanisha kuwa Allah تعالى Aliazimia kufanya hilo, kwa hivyo hakuna njia ya kuliepuka”<sup>1</sup>.

﴿١٦﴾ فَحَمَلَتْهُ فَانْتَبَدَتْ بِهِ مَكَانًا قَصِيًّا ﴿١٧﴾ فَأَجَاءَهَا الْمَخَاضُ إِلَىٰ جِذْعِ النَّخْلَةِ

قَالَتْ يَلَيْتَنِي مِثُّ قَبَلِ هَذَا وَكُنْتُ نَسِيًّا مَّنْسِيًّا ﴿١٨﴾

***22. Basi akachukua mimba yake, na akaondoka nayo mpaka mahali pa mbali.***

***23. Kisha uchungu ukampeleka kwenye shina la mtende; akasema: Laiti ningelikufa kabla ya haya, na nikawa niliyesahaulika kabisa!***

### **Kubeba Mimba na Kujifungua**

Allah تعالى Anatumjulisha kuhusu Maryam kuwa pindi Jibril عليه السلام alipozungumza naye kwa Idhini ya Allah تعالى, alikubali Kudra ya Allah تعالى. Wanazuoni wengi waliotangulia (salafu) wametaja kuwa Malaika aliyemjia Maryam ni Jibril عليه السلام, akampuliza katika mfuko wa nguo yake, mpulizo huo ukaenda hadi katika mfuko wake wa uzazi, hivyo basi, akashika ujauzito kwa Idhini ya Allah تعالى.

<sup>1</sup> At-Tabari 18:165.

Muhammad bin Is-haaq رحمه الله تعالى amesema: "Alipotunga mimba na kujaza kigudulia chake kwa maji (kutoka katika kisima), alirudi kwa watu wake. Baada ya hapo, damu yake ya ada ilisimama na kupatikanwa na yale wanaoyapata wanawake wenye mimba miongoni mwa ugonjwa, njaa, kubadilika rangi na hata alikuwa na mabadiliko katika mazungumzo yake. Tukio hilo lilienea miongoni mwa Wana wa Israili, na watu wakawa wanasema: 'Hakika, mwenzi wake (katika zinaa) ni Yusuf kwa sababu hakuna aliyekuwa katika Msikiti pamoja naye ila yeye. Hivyo, alijificha kwa watu na kuweka sitara baina yake na wao. Hakuna aliyemuona, naye hakumuona yeyote". Allah تعالى Anasema:

فَأَجَاءَهَا الْمَخَاضُ إِلَى جِذْعِ النَّخْلَةِ

***"Kisha uchungu ukampeleka kwenye shina la mtende."***

Maana yake: Uchungu wa uzazi ulimlazimisha kwenda kwenye shina la mtende ambao ulikuwa mahali alipojitenga. Wanazuoni wametofautiana kuhusu sehemu yenyewe. Asuddiy amesema: "Mahali pakujitenga kwake kulikuwa ni mashariki na hapo ndipo alipokuwa akiswali katika Nyumba Tukufu iliyopo Qudsi"<sup>1</sup>. Wahab bin Munabbih amesema: "Alikimbia na alipofika sehemu baina ya Sham<sup>2</sup> na Misri, alijiwa na uchungu uliomshinda"<sup>3</sup>. Riwaya nyingine kutoka kwa Wahb, amesema: "Tukio hili lilifanyika maili nane<sup>4</sup> kutoka Nyumba Tukufu ya al-Quds katika kijiji kinachojulikana kama *Bayt Lahm*<sup>5</sup> (Bethlehem)". Ninasema, zipo Hadithi kuhusu Israa' safari ya usiku ya Mtume iliyonukuliwa na An-Nasaa'i kutoka kwa Anas رضي الله عنه<sup>6</sup>, na Al-Bayhaqiy kutoka kwa Shaddaad bin Aws رضي الله عنه<sup>7</sup>, kuwa jambo hili lilitokea *Bayt Lahm*<sup>7</sup>. Allah تعالى Anajua zaidi. Hili ndilo mashuhuri kuwa watu wote wanasimuliana mmoja kwa mwengine. Wakristo bila shaka wamechukulia kuwa hii ndio sehemu ya tukio hilo na inasimuliwa na watu wote. Pia imepokewa katika Hadithi ikiwa Hadithi hii ni sahihi.

<sup>1</sup> At-Tabari 18:161.

<sup>2</sup> Syria kubwa.

<sup>3</sup> At-Tabari 18:170.

<sup>4</sup> Kwa sasa huu ni mji uliyopo Ukingo wa Magharibi wa mto Jordan.

<sup>5</sup> At-Tabari 18:170.

<sup>6</sup> An-Nasaa'iy katika Al-Kubraa 1:221.

<sup>7</sup> Dalaa'il An-Nubuwwah 2:355.

Allah تعالى Anasema kutujulisha kuhusu yeye:

قَالَتْ يَلَيْتَنِي مِتُّ قَبْلَ هَذَا وَكُنْتُ نَسِيًّا مَّسِيًّا ﴿١٩﴾

**“Akasema: Laiti ningelikufa kabla ya haya, na nikawa niliyesahaulika kabisa!”**

Katika hili kuna ruhusa ya mtu kutamani mauti anapokumbwa na majanga. Alijua kuwa atajaribiwa kwa kuzaa, watu hawatamsaidia, na wala hawataamini kisa chake. Baada ya kujulikana kama mwenye Dini na ‘Ibaadah miongoni mwao, sasa watadhania kuwa alikuwa kahaba. Akasema:

يَلَيْتَنِي مِتُّ قَبْلَ هَذَا

**“Laiti ningelikufa kabla ya haya.”**

Alisema haya kumaanisha kabla ya tukio hilo.

وَكُنْتُ نَسِيًّا مَّسِيًّا ﴿٢٠﴾

**“Na nikawa niliyesahaulika kabisa!”**

Hiyo ni kumaanisha: “Natamani nisingeumbwa wala nisingekuwa chochote”. Hili lilitajwa na Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما<sup>1</sup>. Qataadah amesema:

وَكُنْتُ نَسِيًّا مَّسِيًّا ﴿٢١﴾

**“Na nikawa niliyesahaulika kabisa!”**

Maana: Kitu kisichojulikana, kilichosahaulika na hakuna aliyejua mimi nani.”

فَنَادَاهَا مِنْ تَحْتِهَا أَلَا مَحْزَنِي قَدْ جَعَلَ رَبُّكِ تَحْتَكِ سَرِيًّا ﴿٢٢﴾ وَهَزَيْتُ إِلَيْكَ بِجِذْعِ النَّخْلَةِ

تُسْقِطُ عَلَيْكَ رَطْبًا جَبِيًّا ﴿٢٣﴾ فَكُلِي وَاشْرَبِي وَقَرِّي عَيْنًا ۖ فَإِمَّا تَرِينِ مِنَ الْبَشَرِ أَحَدًا

فَقُولِي إِنِّي نَذَرْتُ لِلرَّحْمَنِ صَوْمًا فَلَنْ أُكَلِّمَ الْيَوْمَ إِنْسِيًّا ﴿٢٤﴾

**24. Pakatangazwa kutoka chini yake: Usihuzunike! Hakika Mola wako Mlezi Amejaalia chini yako kijito kidogo cha maji!**

**25. Na litikise kwako hilo shina la mtende, utakuangushia tende nzuri zilizo mbivu.**

<sup>1</sup> At-Tabari 18:172.

**26. Basi kula, na kunywa, na litue jicho lako. Na pindi ukimuona mtu yeyote basi sema: Hakika mimi nimeweka nadhiri kwa Ar-Rahman ya kufunga; kwa hivyo leo sitasema na mtu.**

### **Alichambiwa baada ya Kujifungua**

Baadhi ya wasomaji wanaisoma Aya:

(مَنْ تَحْتَهَا)

(Man Tahtahaa) Maana yake: Aliyekuwa chini yake alimuita. Wengine wanaisoma:

مِنْ تَحْتِهَا

**“Min Tahtihaa – kutoka chini yake”.**

Kwa maana ya kiunganishi (*Min* - kutoka) badala ya kiwakilishi nomino (*Man* – nani). Wanazuoni wa Tafsiri wametofautiana juu ya tafsiri kuhusu nani aliyeita. Awfiy na wengine wamenukuu kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuwa alisema:

فَنَادَاهَا مِنْ تَحْتِهَا

**“Pakatangazwa kutoka chini yake”.**

Maana: Jibril<sup>1</sup> عليه السلام kwa sababu ‘Isa عليه السلام hakuzungumza mpaka alipompeleka kwa watu wake”. Sa’id bin Jubayr, Adh-Dhwahaak, ‘Amr bin Maymun, as-Suddiy na Qataadah wamesema: “Hakika, hii inamhusisha Malaika Jibril عليه السلام”<sup>2</sup>. Hii inamaanisha kuwa yeye (Jibril عليه السلام) alimuita kutoka chini ya bonde. Mujaahid amesema:

فَنَادَاهَا مِنْ تَحْتِهَا

**“Pakatangazwa kutoka chini yake”.**

Hii inamkusudia ‘Isa bin Maryam عليه السلام”. Hivyo hivyo, ‘Abdur-Razzaaq ameripoti kutoka kwa Ma’mar kutoka kwa Qatadah, kutoka kwa Hasan amesema: “Hii inamkusudia mtoto wake (‘Isa عليه السلام)”. Hii pia ndio rai moja kati ya mbili zilizoripotiwa kutoka kwa Sa’id bin Jubayr – kuwa alikuwa mtoto wake, ‘Isa عليه السلام, aliyezungumza.’ Sa’id amesema: “Je hujamsikia Allah تعالى Akisema:

<sup>1</sup> Tabari 18:173.

<sup>2</sup> Tabari 18:173.

فَأَشَارَتْ إِلَيْهِ<sup>ط</sup>

**'Akawaashiria yeye'.**

Ibn Zayd na Ibn Jariri wamechagua rai hii katika tafsiri yake.

Allah تعالی Anasema:

أَلَا تَحْزَنِي

**"Usihuzunike!"**

Alimuita akimuambia: "Usihuzunike." Kwa nini asifanye hivyo,

قَدْ جَعَلَ رَبُّكَ تَحْتِكَ سَرِيًّا ﴿١٨﴾

**"Hakika Mola wako Mlezi Amejaalia chini yako kijito kidogo cha maji!"**

Sufyaan Ath-Thawriy رحمه الله تعالى na Shu'bah رحمه الله تعالى wamepokea kutoka kwa Abu Is-haaq رحمه الله تعالى kuwa Al-Baraa' bin 'Azib رضي الله عنه amesema,

قَدْ جَعَلَ رَبُّكَ تَحْتِكَ سَرِيًّا ﴿١٨﴾

**"Hakika Mola wako Mlezi Amejaalia (kijito cha maji) 'sariyya' chini yako"**

Maana yake: "Kijito kidogo"<sup>1</sup>. Hivyo hivyo, 'Aliy bin Abi Twalhah ameripoti kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: "Sariy ni mto"<sup>2</sup>. 'Amr bin Maymuun amechukua rai hiyo hiyo, kama alivyosema: "Inamaanisha mto ambao maji yake hunywewa"<sup>3</sup>. Mujaahid amesema: "Inamaanisha mto katika lugha ya Syria"<sup>4</sup>. Sa'id bin Jubayr amesema: "Sariy ni mto mdogo unaomiminika."<sup>5</sup> Wengine wamesema kuwa Sariy inamhusisha 'Isa عليه السلام. Rai hii ilisemwa na Hasan, Rabi' bin Anas, Muhammad bin 'Abbaad bin Ja'far, na pia ni rai moja kati ya mbili zilizonukuliwa kutoka kwa Qataadah. Pia hiyo ni rai ya 'Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam. Hata hivyo, rai ya kwanza ni dhahiri zaidi. Kwa sababu hii, Allah تعالی Anasema baada yake:

<sup>1</sup> Tabari 18:175.

<sup>2</sup> Tabari 18:176.

<sup>3</sup> Tabari 18:176.

<sup>4</sup> Tabari 18:176.

<sup>5</sup> Tabari 18:176.

وَهَزِي إِلَيْكَ بِجَذَعِ النَّخْلَةِ

**“Na litikise kwako hilo shina la mtende.”**

Maana yake: Likamate shina la mtende na litikise kwako. Hivyo, Allah تعالى Alimbariki na Kumneemesha kwa Kumpatia chakula na kinywaji. Kisha Akasema:

تُسْقِطُ عَلَيْكَ رُطْبًا جَنِيًّا ﴿١٩﴾ فَكُلْ وَاشْرَبْ وَقَرِّ عَيْنًا

**“Utakuangushia tende nzuri zilizo mbivu. Basi kula, na kunywa, na litue jicho lako.”**

Maana: Kuwa na furaha. Hii ndio sababu ya ‘Amr bin Maymuun akasema, “Hakuna kilicho bora kwa mwanamke baada ya kuzaa kuliko tende kavu na mbichi kisha akasoma Aya hii tukufu.”<sup>1</sup> Kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

فَأِمَّا تَرِينَ مِنْ الْبَشَرِ أَحَدًا

**“Na pindi ukimuona mtu yeyote.”**

Maana yake: Mtu yeyote unayemuona,

فَقُولِي إِنِّي نَذَرْتُ لِلرَّحْمَنِ صَوْمًا فَلَنْ أُكَلِّمَ الْيَوْمَ إِنْسِيًّا ﴿٢٠﴾

**“Basi sema: Hakika mimi nimeweka nadhiri kwa Ar-Rahman ya kufunga.”**

Maana yake: Kwa kumuashiria, sio kwa kuzungumza. Hii ni kwa ajili ya kuondoa kupingana na maneno yake ya mwanzo,

فَلَنْ أُكَلِّمَ الْيَوْمَ إِنْسِيًّا ﴿٢٠﴾

**“Kwa hivyo leo sitasema na mtu.”**

Anas bin Maalik رضي الله عنه amefasiri,

إِنِّي نَذَرْتُ لِلرَّحْمَنِ صَوْمًا

**“Hakika mimi nimeweka nadhiri ya kufunga kwa Mwingi wa Rehema.”**

<sup>1</sup> At-Tabari 18:179.

Amesema: “Nadhiri ya kukaa kimya”<sup>1</sup>. Hivyo ndivyo walivyosema Ibn ‘Abbaas na Adh-Dhahaak.<sup>2</sup>

Maana hapa ni kuwa katika Sheria yao, ukiwa umefunga, ilikuwa haifai kwao kula na kuzungumza. As-Suddiy, Qataadah na ‘Abdur-Rahman bin Zayd wote wamechukua rai hii. ‘Abdur-Rahman bin Zayd amesema: “Pale Isa عليه السلام alipomuambia Maryam,

أَلَّا تَحْزَنِي

**“Usihuzunike.”**

Alisema: ‘Itakuwaje nisihuzinike nawe uko pamoja nami, nami sina mume wala sijamilikiwa kama kijakazi? Nina udhuru gani wa kuwapatia watu wangu? Ole wangu, lau ningekuwa nimekufa kabla ya hili, na nikawa ni kitu kilichosahaulika kabisa na nisiyejulikana’.

Hapo Isa عليه السلام akamuambia, ‘Nitakutosheleza na kauli,

فَأِمَّا تَرِينَ مِنْ الْبَشَرِ أَحَدًا فَقُولِي إِنِّي نَذَرْتُ لِلرَّحْمَنِ صَوْمًا فَلَنْ أُكَلِّمَ الْيَوْمَ إِنْسِيًّا ﴿١٩﴾

**“Na pindi ukimuona mtu yeyote basi sema: Hakika mimi nimeweka nadhiri kwa Allah ya kufunga; kwa hivyo leo sitasema na mtu.”**

Yote haya ni katika mazungumzo ya Isa عليه السلام kwa mamake”. Wahab amesema kama hivyo.

\* \* \*

<sup>1</sup> At-Tabari 18:182-183.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:182-183.



فَأَتَتْ بِهِ قَوْمَهَا تَحْمِلُهُ ۗ قَالُوا يَمْرَأَتُ لَقَدْ جِئْتِ شَيْئًا فَرِيًّا ﴿٢٧﴾  
 يَتَأَخَذَتِ هُنَّ مَا كَانَ أَبُوكِ أَمْرًا سَوًّا وَمَا كَانَتْ أُمُّكِ بَغِيًّا ﴿٢٨﴾ فَأَشَارَتْ إِلَيْهِ ۗ قَالُوا كَيْفَ نُكَلِّمُ مَنْ كَانَ فِي الْأَمْهِدِ صَبِيًّا ﴿٢٩﴾ قَالَ إِنِّي عَبْدُ اللَّهِ ءَاتَنِي الْكِتَابَ وَجَعَلَنِي نَبِيًّا ﴿٣٠﴾ وَجَعَلَنِي مُبَارَكًا أَيْنَ مَا كُنْتُ وَأَوْصَانِي بِالصَّلَاةِ وَالزَّكَاةِ مَا دُمْتُ حَيًّا ﴿٣١﴾ وَبِرَأْسِ بُولَدِي وَلَمْ يُجْعَلِنِي جَبَّارًا شَقِيًّا ﴿٣٢﴾ وَالسَّلَامُ عَلَيَّ يَوْمَ وُلِدْتُ وَيَوْمَ أُمُوتُ وَيَوْمَ أُبْعَثُ حَيًّا ﴿٣٣﴾ ذَلِكَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ ۗ قَوْلَ الْحَقِّ الَّذِي فِيهِ يَمْتَرُونَ ﴿٣٤﴾ مَا كَانَ لِلَّهِ أَنْ يَتَّخِذَ مِنْ وَلَدٍ ۗ سُبْحَانَ اللَّهِ إِنِّي رَبُّ رَبُّكُمْ فَاَعْبُدُوهُ ۗ يَقُولُ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٣٥﴾ وَإِنَّ لِلَّهِ رَبِّي وَرَبُّكُمْ فَاَعْبُدُوهُ ۗ هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ ﴿٣٦﴾ فَاتَّخَذَ الْأَحْزَابُ مِنْ بَيْنِهِمْ فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ مَشْهَدِ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿٣٧﴾ أَسْمِعْ يَوْمَ وَأَبْصِرْ يَوْمَ يَأْتُونَنَا لَكِنِ الظَّالِمُونَ الْيَوْمَ فِي ضَلَالٍ مُبِينٍ ﴿٣٨﴾ وَأَنْذِرْهُمْ يَوْمَ الْحَسْرَةِ إِذْ قُضِيَ الْأَمْرُ وَهُمْ فِي غَفْلَةٍ وَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٣٩﴾ إِنَّا نَحْنُ رَبُّ الْأَرْضِ وَمَنْ عَلَيْنَا وَإِلَيْنَا يُرْجَعُونَ ﴿٤٠﴾

فَأَتَتْ بِهِ قَوْمَهَا تَحْمِلُهُ ۗ قَالُوا  
 يَمْرَأَتُ لَقَدْ جِئْتِ شَيْئًا فَرِيًّا ﴿٢٧﴾  
 يَتَأَخَذَتِ هُنَّ مَا كَانَ أَبُوكِ أَمْرًا  
 سَوًّا وَمَا كَانَتْ أُمُّكِ بَغِيًّا ﴿٢٨﴾  
 فَأَشَارَتْ إِلَيْهِ ۗ قَالُوا كَيْفَ نُكَلِّمُ مَنْ  
 كَانَ فِي الْأَمْهِدِ صَبِيًّا ﴿٢٩﴾ قَالَ  
 إِنِّي عَبْدُ اللَّهِ ءَاتَنِي الْكِتَابَ وَجَعَلَنِي  
 نَبِيًّا ﴿٣٠﴾ وَجَعَلَنِي مُبَارَكًا أَيْنَ مَا  
 كُنْتُ وَأَوْصَانِي بِالصَّلَاةِ وَالزَّكَاةِ  
 مَا دُمْتُ حَيًّا ﴿٣١﴾ وَبِرَأْسِ بُولَدِي وَلَمْ  
 يُجْعَلِنِي جَبَّارًا شَقِيًّا ﴿٣٢﴾ وَالسَّلَامُ  
 عَلَيَّ يَوْمَ وُلِدْتُ وَيَوْمَ أُمُوتُ وَيَوْمَ  
 أُبْعَثُ حَيًّا ﴿٣٣﴾

27. Akenda naye (mwanawe)  
 kwa jamaa zake amembeba.  
 Wakasema: Ewe Maryam!  
 Hakika umeleta kitu cha  
 ajabu!

28. Ewe dada yake Haarun! Baba yako hakuwa mtu muovu, wala mama yako hakuwa kahaba.

29. Akawaashiria (mtoto). Wakasema: Vipi tumsemeze aliye bado mdogo yumo katika malezi?

**30. (Mtoto) akasema: Hakika mimi ni mtumwa wa Allah. Amenipa Kitabu, na Amenifanya kuwa Nabii.**

**31. Na Amenijaalia ni mwenye kubarikiwa popote pale niwapo. Na Ameniusia Sala na Zakah maadamu ni hai,**

**32. Na nimtendee wema mama yangu. Wala Hakunifanya niwe jeuri, muovu.**

**33. Na amani iko juu yangu siku niliyozaliwa, na siku nitakayokufa, na siku nitakayofufuliwa kuwa hai.**

### **Maryam Akiwa na Masihi Mbele ya Watu Wake Kumkataa Kwao na Majibu Yake Kwao**

Allah تعالی Anatufahamisha kuhusu hali ya Maryam Alipoamriwa kufunga siku hiyo na asizungumze na mtu yeyote. Kwa hakika, jambo lake litatazamwa na kutolewa ufumbuzi wake. Hivyo, alikubali Amri ya Allah تعالی mara moja na Kudura Yake. Hivyo alimchukua mtoto wake na kumleta kwa watu wake, akiwa amembeba. Walipomuona katika hali hii walilichukulia kuwa ni jambo kubwa sana na wakapinga kwa ukali dhidi ya hilo, na,

قَالُوا يَنْمَرِيْمُ لَقَدْ جِئْتِ شَيْئًا فَرِيًّا ﴿٢٧﴾

**“Wakasema: Ewe Maryam! Hakika umeleta kitu Fariy!.”**

Fariy inamaanisha kitu kikubwa cha ajabu. Hii imesemwa na Mujaahid, Qataadah, As-Suddiy na wengineo<sup>1</sup>. Amepokea Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالی kuwa Nawf Al-Bikaaliy amesema: “Watu wake walitoka kumtafuta, alikuwa katika familia iliyobarikiwa kwa unabii na utukufu. Hata hivyo hawakumuona kabisa. Walikutana na mchungaji wa ng’ombe na wakamuuliza: ‘Je, umemuona msichana ambaye sifa zake ni kadha na kadha?’ Akajibu, ‘Hapana, lakini usiku wa leo nimewaona ng’ombe wangu wakifanya kitu ambacho sijawaona wakifanya kabla.’ Wakauliza: ‘Umeona nini?’ Akasema: ‘Usiku niliwaona wakisujudu kuelekea sehemu ya bonde lile’<sup>2</sup>”.

<sup>1</sup> At-Tabari 18:185.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:187.

'Abdallah bin Ziyaad amesema (akiongezea katika riwaya), "Nimehifadhi kutoka kwa Sayyaar kuwa huyo (mchungaji) alisema: "Niliona mwangaza ung'aao". Hivyo walielekea sehemu hiyo waliyoambiwa, Maryam alielekea upande wao. Alipowaona alikaa chini akiwa amepakata mtoto wake mapajani kwake. Walimjia mpaka wakasimama juu yake.

قَالُوا يَنْمِرِمُرٌ لَقَدْ جِئْتِ شَيْئًا فَرِيًّا ﴿٢٧﴾

**"Wakasema: Ewe Maryam! Hakika umeleta kitu Fariy!."**

Hii ina maana kuwa jambo hilo alilolileta lilikuwa kubwa.

يَتَأَخَّتْ هَارُونَ

**"Ewe dada yake Haarun!"** Maana yake: Ewe unayefanana na Haarun عليه السلام katika 'Ibadah.

مَا كَانَ أَبُوكَ أَمْرًا سَوْءَ وَمَا كَانَتْ أُمُّكَ بَغِيًّا ﴿٢٨﴾

**"Baba yako hakuwa mtu muovu, wala mama yako hakuwa kahaba."**

Walimaanisha: "Wewe watoka katika familia nzuri safi, inayojulikana katika uchamungu, 'Ibadah na kujiepusha katika mambo machafu. Vipi utafanya kitendo hicho?" 'Aliy bin Abi Twalhah na As-Suddiy wote wamesema, "Aliambiwa,

يَتَأَخَّتْ هَارُونَ

**"Ewe dada yake Haarun!"**

Kumaanisha ndugu wa Musa عليه السلام, kwa sababu alitoka katika kizazi hicho. Hii ni sawa na kauli, 'Ewe ndugu wa Tamiim', kwa anayetoka katika kabila la Tamimiy, na 'Ewe ndugu wa Mudar', kwa anayetoka katika kabila la Mudar. Pia pamesemwa kuwa alikuwa anahusiana na mtu mwema miongoni mwao ambaye jina lake ni Haarun na alifananishwa naye kwa kujitenga kwake na kwa 'Ibadah zake". Kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

فَأَشَارَتْ إِلَيْهِ قَالُوا كَيْفَ نُكَلِّمُ مَنْ كَانَ فِي الْأَمْتِدِ صَبِيًّا ﴿٢٩﴾

**"Akawaashiria (mtoto). Wakasema: Vipi tumsemeze aliye bado mdogo yumo katika malezi?."**

Hili lilitokea walipokuwa na shaka kuhusu hali yake, walimshutumu na kusema walichotaka kusema. Wakati huo walikuwa wakimkashifu na kumshutumu kwa uwongo kwa kitendo hicho kibaya. Siku hiyo alikuwa amefunga na kunyamaza. Kwa hiyo, aliwaashiria kuwa mazungumzo yote yapite kwa kijana na kuwaunganisha wao na hotuba yake. Walimkejeli kwa sababu walidhania alikuwa anawafanyia dhahaka na kucheza nao tu. Wakasema:

كَيْفَ تُكَلِّمُ مَنْ كَانَ فِي الْمَهْدِ صَبِيًّا ﴿٢٧﴾

***“Vipi tumsemeze aliye bado mdogo yumo katika malezi?.”***

Maymuun bin Mahraan amesema,

فَأَشَارَتْ إِلَيْهِ ۗ

***“Akawaashiria.”***

Aliashiria, ‘Zungumzeni naye’. Hapo wakasema: ‘Baada ya kuja kwetu na janga hili, sasa anatuamuru tuzungumze na mtoto aliye mchanga!’<sup>1</sup> Suddiy amesema: “Alipomuashiria yeye (mtoto) walikasirika na kusema, ‘Anatudhahiki, kwa jinsi ambayo anatuamuru tuzungumze na mtoto huyu. Bila shaka hilo ni baya zaidi hata kuliko uzinifu wake’.

قَالُوا كَيْفَ تُكَلِّمُ مَنْ كَانَ فِي الْمَهْدِ صَبِيًّا ﴿٢٨﴾

***“Wakasema: Vipi tumsemeze aliye bado mdogo yumo katika malezi?.”***<sup>2</sup>

Hii ina maana, “Vipi tutazungumza na mtoto mchanga, katika hali ya utoto?” Isa عليه السلام alijibu kwa kusema:

قَالَ إِنِّي عَبْدُ اللَّهِ

***“Hakika mimi ni mtumwa wa Allah.”***

Kitu cha kwanza alichosema ni kutangaza heshima ya juu ya Mola Mlezi na kuwa Yeye Yu mbali sana na kuwa na mtoto. Pia, aliyakinisha kuwa yeye ni mja na mwenye kumuabudu Mola wake Mlezi. Allah تعالى Amesema:

<sup>1</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 5:508.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:189.

ءَاتِنِي الْكِتَابَ وَجَعَلِي نَبِيًّا ﴿٢٧﴾

***“Amenipa Kitabu, na Amenifanya kuwa Nabii.”***

Hili ni tangazo la kutokuwa na hatia kwa mamake kutokana na uasherati ulio nasibishwa naye. Nawf Bikaaliy amesema, “Waliposema walioyasema kwa mamake, Isa عليه السلام alikuwa ananyonya. Kwa kauli yao hiyo alilitoa titi mdomoni mwake na kujitegemeza kushotoni mwake akisema,

إِنِّي عَبْدُ اللَّهِ ءَاتِنِي الْكِتَابَ وَجَعَلِي نَبِيًّا ﴿٢٨﴾

***“Hakika mimi ni mtumwa wa Allah. Amenipa Kitabu, na Amenifanya Nabii.”***

Na aliendelea kuzungumza hadi alipofika,

مَا دُمْتُ حَيًّا ﴿٢٩﴾

***“Maadamu ni hai.”***

Kuhusu Kauli yake,

وَجَعَلَنِي مُبَارَكًا أَيْنَ مَا كُنْتُ

***“Na Amenijaalia ni mwenye kubarikiwa popote pale niwapo.”***

Mujaahid, ‘Amri bin Qays na Thawriy wote wamesema kuwa hii inamaanisha, “Alinifanya kuwa mwalimu wa mema na mazuri.”<sup>1</sup> Na katika riwaya nyingine kutoka kwa Mujaahid, amesema: “Mtu wa faida kubwa.”<sup>2</sup> Ibn Jariir رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Wuhayb bin Wardiy, mwachwa huru wa Bani Makhzuum kuwa alisema: “Mwanachuoni alikutana na mwanachuoni mwingine aliyekuwa na elimu kuliko yeye. Hivyo akamuambia, ‘Allah تعالى Akurehemu, ni amali yangu gani ninayotakiwa kuifanya wazi?’ Mwingine akajibu, ‘Kuamrisha mema na kukataza mabaya, kwa hakika hiyo ndio Dini ya Allah تعالى Aliyowatuma nayo Manabii kwa waja Wake’. Kwa hakika, wanazuoni wamekubaliana kuhusu Kauli ya Allah تعالى,

<sup>1</sup> At-Tabari 18:191.

<sup>2</sup> Rejeo la nyuma.

وَجَعَلَنِي مُبَارَكًا أَيْنَ مَا كُنْتُ

**“Na Amenijaalia ni mwenye kubarikiwa popote pale niwapo.”**

Kisha pakasemwa: ‘Baraka yake ilikuwa ipi?’ Yeye (Wuhayb) alijibu: ‘Kuamrisha mema na kukataza mabaya popote alipokuwa.’<sup>1</sup> Kauli Yake:

وَأَوْصِنِي بِالصَّلَاةِ وَالزَّكَاةِ مَا دُمْتُ حَيًّا ﴿١١﴾

**“Na Ameniusia Sala na Zakah maadamu ni hai.”**

Hii inafanana na Kauli ya Allah تعالى kwa Muhammad ﷺ

وَأَعْبُدْ رَبَّكَ حَتَّىٰ يَأْتِيَكَ الْيَقِينُ ﴿١٢﴾

**“Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ikufikie yakini (mauti).”**  
(15:99).

‘Abdur-Rahman bin Qaasim amepokea kutoka kwa Maalik bin Anas kuwa alifasiri Kauli ya Allah تعالى:

وَأَوْصِنِي بِالصَّلَاةِ وَالزَّكَاةِ مَا دُمْتُ حَيًّا ﴿١١﴾

**“Na Ameniusia Sala na Zakah maadamu ni hai.”**

Akasema: ‘Allah تعالى Alimjulisha mambo yake mpaka atakapoaga dunia. Hii ni dalili yenye nguvu dhidi ya watu wenye kukanusha Qadar (kudura).’<sup>2</sup>

Na Kauli Yake:

وَبِرًّا بِوَالِدَيْ

**“Na nimtendee wema mama yangu.”**

Maana yake: Ameniamuru (Allah تعالى) kumtendea mema na mazuri mama yangu. Ametaja hili baada ya kutaja utiifu wake kwa Mola wake Mlezi, Allah تعالى. Hii ni kuwa mara nyingi Allah تعالى Anajumuisha Amri ya kuabudiwa Yeye na utiifu kwa wazazi. Hii ni sawa na Kauli Yake Aliyetukuka:

<sup>1</sup> At-Tabari 18:191.

<sup>2</sup> Al-Qurtwubiy 11:103.

﴿ وَقَضَىٰ رَبُّكَ أَلَّا تَعْبُدُوا إِلَّا إِيَّاهُ وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا ۗ ﴾

**“Na Mola wako Mlezi Amehukumu kuwa msimuabudu yeyote ila Yeye tu na kuwafanyia wema wazazi.” (17:23)**

Na Amesema:

﴿ أَنْ أَشْكُرَ لِي وَلِوَالِدَيْكَ إِلَيَّ الْمَصِيرُ ۗ ﴾

**“Ya kwamba unishukuru Mimi na wazazi wako; marejeo yenu ni Kwangu.” (31:14).**

Na Kauli Yake:

﴿ وَلَمْ يَجْعَلْنِي جَبَّارًا شَقِيًّا ۗ ﴾

**“Wala Hakunifanya niwe jeuri, muovu.”**

Maana yake: Wala Hakunijaalia kuwa jeuri, mwenye kiburi katika kumuabudu Yeye na kumtii. Na nikawa si mwenye kumtendea wema mama yangu, na hivyo kutobarikiwa. Na Kauli Yake:

﴿ وَالسَّلَامُ عَلَيَّ يَوْمَ وُلِدْتُ وَيَوْمَ أَمُوتُ وَيَوْمَ أُبْعَثُ حَيًّا ۗ ﴾

**“Na amani iko juu yangu siku niliyozaliwa, na siku nitakayokufa, na siku nitakayo fufuliwa kuwa hai.”**

Huu ni uthibitisho kuwa yeye ni mwenye kumuabudu Allah تعالى, na kwamba yeye ni kiumbe aliyeumbwa na Allah تعالى. Isa عليه السلام ataishi, kufa na kufufuliwa, kama viumbe vyengine vilivyoyumbwa na Allah تعالى. Hata hivyo, atakuwa na amani katika hali tatu hizo, ambazo ni hali ngumu sana kwa viumbe vya Allah تعالى. Sala na salamu za Allah تعالى ziwe juu yake.

﴿ ذَٰلِكَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ ۗ قَوْلَ الْحَقِّ الَّذِي فِيهِ يَمْتَرُونَ ۗ ﴾ مَا كَانَ لِلَّهِ أَنْ يَتَّخِذَ مِنْ

وَلِدٍ ۗ سُبْحٰنَهُ ۗ إِذَا قَضَىٰ أَمْرًا فَإِنَّمَا يَقُولُ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ۗ ﴿ وَإِنَّ اللَّهَ رَبِّي وَرَبُّكُمْ

فَاعْبُدُوهُ ۗ هٰذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ ۗ ﴿ فَاخْتَلَفَ الْأَحْزَابُ مِنْ بَيْنِهِمْ ۗ فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ كَفَرُوا

مِنْ مَّشْهَدِ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿

**34. Huyo ndiye Isa mwana wa Maryam. Ndiyo kauli ya haki ambayo wanaifanyia shaka.**

**35. Haiwi kwa Allah kuwa na mwana, Subhanahu, Yeye Ametakasika! Anapolihukumia jambo basi huliambia tu: Kuwa! Likawa.**

**36. Na hakika Allah ni Mola wangu Mlezi, na Mola wenu Mlezi. Basi muabuduni Yeye. Hii ndiyo njia Iliyonyooka.**

**37. Lakini makundi yakakhitalifiana wao kwa wao. Basi ole wao hao waliokufuru kwa kuhudhuria Siku iliyo kuu!**

Isa عليه السلام ni mja wa Allah تعالى, sio mtoto Wake

Allah تعالى Anamuambia Mtume Wake, Muhammad ﷺ, 'Hicho ni kisa ambacho Tumekusimulia wewe kuhusu Isa عليه السلام':

قَوْلِكَ الْحَقِّ الَّذِي فِيهِ يَمْتَرُونَ ﴿٦٠﴾

**“Ndiyo kauli ya haki ambayo wanaifanyia shaka”.**

Maana yake: Wametofautiana baina ya watu wa batili na watu wa ukweli, na wale wenye kuamini na waliokufuru. Kwa sababu hii wasomaji (*Quraa'*) wengi wameisoma Aya hii *Qawlul Haqq* 'kauli ya kweli', ikimhusisha Isa عليه السلام mwenyewe. 'Aswim na 'AbdAllah bin 'Amir, wote wameisoma *Qawlul Haqq* 'kauli ya kweli', ikihusisha kisa chote ambacho watu wametofautiana. Imepokewa kuwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه alisoma *Qawlul Haqq*,<sup>1</sup> inayomaanisha kuwa Isa عليه السلام alisema kweli. Kisomo cha Aya kwa njia hii, *Qawlul Haqq*, inayomhusisha Isa عليه السلام, ndio maana ya dhahiri kabisa kilugha. Nayo inaungwa mkono na Kauli ya Aliyetukuka:

الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ فَلَا تَكُنْ مِنَ الْمُمْتَرِينَ ﴿٦٠﴾

**“Hii ni kweli itokayo kwa Mola wako Mlezi. Basi usiwe miongoni mwa wanaofanya shaka.” (3:60).**

<sup>1</sup> At-Tabari 18:194.



Allah تعالى Alipotaja kuwa Alimuumba yeye kama mja na Nabii, Alijituza Mwenyewe, Aliye Mtukufu, kwa Kusema:

مَا كَانَ لِلَّهِ أَنْ يَتَّخِذَ مِنْ وَاٰلِهٖ سُبْحٰنَهُ

**“Haiwi kwa Allah kuwa na mwana, Subhanahu, Yeye Ametakasika!”** Maana yake: Kwa wanayosema watu hawa wajinga, madhalimu na waliochupa mipaka kwa kutakabari kukubwa.

إِذَا قَضَىٰ أَمْرًا فَإِنَّمَا يَقُولُ لَهُ كُن فَيَكُونُ ﴿٦٥﴾

**“Anapolihukumia jambo basi huliambia tu: Kuwa! Likawa.”** Maana yake: Anapotaka chochote kile, hakika Huamuru na hivyo kikawa kama Alivyotaka, kama Alivyosema Aliyetukuka:

إِنَّ مَثَلَ عِيسَىٰ عِنْدَ اللَّهِ كَمَثَلِ آدَمَ ۖ خَلَقَهُ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ قَالَ لَهُ كُن فَيَكُونُ ﴿٦٦﴾  
الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ فَلَا تَكُن مِنَ الْمُمْتَرِينَ ﴿٦٧﴾

**“Hakika mfano wa Isa kwa Allah ni kama mfano wa Aadam; Alimuumba kwa udongo kisha Akamuambia: Kuwa! Basi akawa. Hii ni kweli itokayo kwa Mola wako Mlezi. Basi usiwe miongoni mwa wanaofanya shaka.”** (3:59-60).

Isa عليه السلام Aliamuru Kupwekeshwa Allah تعالى, kisha Watu Wakatofautiana Baada Yake

Na Kauli Yake Allah تعالى:

وَإِنَّ اللَّهَ رَبِّي وَرَبُّكُمْ فَأَعْبُدُوهُ هٰذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ ﴿٦٨﴾

**“Na hakika Allah ni Mola wangu Mlezi, na Mola wenu Mlezi. Basi muabuduni Yeye. Hii ndiyo njia Iliyonyooka.”**

Maana yake: Kwa yale aliyoaamuru Isa عليه السلام watu, akiwa katika rika la ulezi kwa kuwaambia wakati huo: ‘Hakika Allah تعالى ni Mola wake Mlezi na Mola wao na Akawaamuru wamuabudu Yeye’. Akasema:

فَأَعْبُدُوهُ هٰذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ ﴿٦٩﴾

**“Basi muabuduni Yeye. Hii ndiyo njia Iliyonyooka.”** Maana yake: Haya niliyokuja nayo kutoka kwa Allah تعالى ni njia iliyonyooka, njia ya sawa.

Yeyote atakayeifuata ataongoka na atakayekwenda kinyume nayo atapotea na kukengeuka. Na Kauli Yake:

فَاخْتَلَفَ الْأَحْزَابُ مِنْ بَيْنِهِمْ

**“Lakini makundi yakakhitalifiana wao kwa wao”,**

Maana yake: Rai za Watu wa Kitabu zilitofautiana kuhusu Isa عليه السلام hata baada ya kubainishiwa kwa uwazi jambo lake na hali yake. Na kuwa yeye ni mja na Mtume Wake na Neno Lake Aliloteremshiwa Maryam na roho kutoka Kwake. Hivyo, kundi miongoni mwao – ambao ni wengi kati ya Mayahudi (Allah تعالى Awalaani) – walipitisha kuwa yeye ni mtoto wa zinaa, na wakasema: Kuzungumza kwake akiwa mchanga ni uchawi. Na kikundi kingine kikasema: Hakika ni Allah تعالى Aliyezungumza (sio Isa عليه السلام). Na wengine wakasema: Bali yeye ni mtoto wa Allah تعالى. Na wengine wakasema: Yeye ni mmoja katika utatu (pamoja na Allah تعالى). Na wengine wakasema: Bali yeye ni mja wa Allah تعالى na Mtume wake. Na hii kauli ya mwisho ndio iliyo ya sawa, ambayo Allah تعالى Amewaongoza Waumini. Na hakika imepokewa mfano wa haya kwa ‘Amri bin Maymuun, Ibn Jurayj, Qataadah na wengine miongoni mwa watangulizi wema na waliokuja baadaye. Na Kauli Yake:

فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ مَّشْهَدِ يَوْمٍ عَظِيمٍ

**“Basi ole wao hao waliokufuru kwa kuhudhuria Siku iliyo kuu!”**

Hili ni tisho na onyo kali kwa wenye kuongopa juu ya Allah تعالى, kuzua uongo na kudai kuwa Allah تعالى Ana mtoto. Hata hivyo, Allah تعالى Amewapatia muda na Kuwaachilia mpaka Siku ya Kiyama, na Kuwacheleweshea muda wao kwa Upole Wake na Imani ya Kudura Yake juu yao. Hakika, Allah تعالى Haharakishi Amri Yake kwa wenye kumuasi. Hili limepokewa katika Hadithi iliyonukuliwa katika Sahihi mbili:

«إِنَّ اللَّهَ لَيُمْلِي لِلظَّالِمِ حَتَّى إِذَا أَخَذَهُ لَمْ يُقْلِتْهُ»

**“Hakika, Allah Anamuachilia dhalimu mpaka Anapomshika hataweza kukimbia’.**

Kisha Mtume ﷺ akasoma Aya:

وَكَذَلِكَ أَخَذَ رَبُّكَ إِذَا أَخَذَ الْقُرَىٰ وَهِيَ ظَالِمَةٌ إِنَّ أَخَذَهُدْ أَلِيمٌ شَدِيدٌ ﴿٢٧﴾

**'Na namna hivi ndivyo inavyokuwa kutesa kwa Mola wako Mlezi Anapowatesa (watu wa) miji wanapokuwa wameacha mwendo walioambiwa. Hakika Kutesa Kwake kunaumiza na kukali kabisa.'**  
(11:102)<sup>1</sup>

Na pia imepokewa katika Sahihi mbili kuwa Mtume ﷺ wamesema:

«لَا أَحَدٌ أَصْبِرُ عَلَىٰ أَدَىٰ سَمِعَهُ، مِنْ اللَّهِ، إِنَّهُمْ يَجْعَلُونَ لَهُ وَلَدًا وَهُوَ يَرْزُقُهُمْ وَيُعَافِيهِمْ»

*"Hakuna aliye na subira zaidi kwa maudhi anayosikia kuliko Allah. Hakika wao wanamjaalia kuwa na mtoto, Naye Ndiye Mwenye Kuwaruzuku na Kuwapatia siha njema."*<sup>2</sup>

Na hakika Allah تعالى Amesema:

وَكَأَيِّن مِّن قَرْيَةٍ أَمَلَيْتُهَا وَهِيَ ظَالِمَةٌ نُّرُ أَخَذْتَهَا وَإِلَى الْمَصِيرِ ﴿٢٨﴾

**"Na (watu wa) miji mingapi niliyowapa muda; na hali walikuwa wakidhulumu? Kisha Niliwatia Mkononi; na Kwangu ndiko marudio."** (22:48).

Na Amesema Aliyetukuka:

وَلَا تَحْسَبَنَّ اللَّهَ غَفِيلاً عَمَّا يَعْمَلُ الظَّالِمُونَ ۗ إِنَّمَا يُؤَخِّرُهُمْ لِيَوْمٍ تَشْخَصُ فِيهِ  
الْأَبْصَارُ ﴿٢٩﴾

**"Wala usidhani Allah Ameghafilika na haya wanayoyafanya madhalimu. Hakika Yeye Anawaakhirisha tu mpaka siku ambayo macho yao yatakodoka."** (14:42).

Na kwa hivyo hapa Akasema:

فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ مَّشْهَدِ يَوْمٍ عَظِيمٍ ﴿٣٠﴾

**"Basi ole wao hao waliokufuru kwa kuhudhuria Siku iliyo kuu!"**

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baariy 08:205 na Muslim 4:1997.

<sup>2</sup> Fat'h Al-Baariy 10:527 na Muslim 4:2160.

Maana: Siku ya Kiyama. Na hakika imepokewa Hadithi Sahihi iliyonukuliwa na Al-Bukhaariy na Muslim kutoka kwa 'Ubaadah bin Swaamit رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«مَنْ شَهِدَ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، وَأَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ، وَأَنَّ عِيسَى عَبْدُ اللَّهِ وَرَسُولُهُ وَكَلِمَتُهُ أَلْفَاهَا إِلَىٰ مَرْيَمَ وَرُوحٌ مِنْهُ، وَأَنَّ الْجَنَّةَ حَقٌّ وَالنَّارَ حَقٌّ، أَدْخَلَهُ اللَّهُ الْجَنَّةَ عَلَىٰ مَا كَانَ مِنَ الْعَمَلِ»

*“Yeyote anayeshuhudia kuwa hapana apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah, Peke Yake asiye na mshirika na kuwa Muhammad ni mja na Mtume Wake, na kuwa Isa ni mja wa Allah na Mtume Wake na ni Neno Lake Alilomteremshia Maryam na roho kutoka Kwake, na hakika Pepo na Moto ni kweli, hakika Allah Atamuingiza peponi bila kujali amali aliyofanya.”<sup>1</sup>*

أَسْمِعْ بِهِمْ وَأَبْصِرْ يَوْمَ يَأْتُوتَنَّا لَنَكِنَ الظَّالِمُونَ الْيَوْمَ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٢٧﴾ وَأَنْذِرْهُمْ يَوْمَ الْحَسْرَةِ إِذْ قُضِيَ الْأَمْرُ وَهُمْ فِي غَفْلَةٍ وَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٢٨﴾ إِنَّا نَحْنُ نَرِثُ الْأَرْضَ وَمَنْ عَلَيْهَا وَإِلَيْنَا يُرْجَعُونَ ﴿٢٩﴾

**38. Watasikia na wataona vizuri vilioje Siku watakayotufikia! Lakini madhalimu sasa wamo katika upotofu uliodhahiri.**

**39. Na waonye siku ya majuto itapokatwa amri. Nao wamo katika ghafla, wala hawaamini.**

**40. Hakika Sisi Tutairithi ardhi na walio juu yake. Na Kwetu watarejeshwa.**

### Kuwaonya Makafiri Siku ya Majuto

Allah تعالیٰ Anatufahamisha kuhusu makafiri Siku ya Kiyama kuwa watafanywa wenye kusikia barabara na kuona vyema. Kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الْمُجْرِمُونَ نَاكِسُوا رُءُوسِهِمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ رَبَّنَا أَبْصَرْنَا وَسَمِعْنَا

**“Na ungaliwaona waovu wakiinamisha vichwa vyao mbele ya**

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baariy 6:546 na Muslim 1:57.

***Mola wao Mlezi, na kusema: Mola wetu! Tumekwisha kuona na kusikia.” (32:12).***

Watasema hayo wakati ambapo hakutawasaidia chochote, wala haitakuwa na maana yoyote. Lau wangetumia hisia hizo sawasawa kabla ya kuona adhabu hiyo, ingekuwa imewapatia faida na kuwaokoa kutokana na adhabu ya Allah تعالى. Na kwa hiyo Allah تعالى Amesema:

أَسْمِعْ يَوْمَ وَأُبْصِرْ

***“Watasikia na wataona vizuri vilioje.”*** Maana yake: Hakuna atakayesikia na kuona zaidi yao.

يَوْمَ يَأْتُونَنَا

***“Siku watakatufikia.”*** Maana yake: Siku ya Kiyama.

لَنْ كُنِ الظَّالِمُونَ الْيَوْمَ

***“Lakini madhalimu sasa.”*** Maana yake: Katika dunia.

فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ

***“Wamo katika upotofu uliodhahiri.”***

Maana yake: Hawasikii, hawaoni wala hawafikirii. Wanapotakiwa kufuata uwongofu, hawaongoki na wanatii wakati halitawafalia lolote hilo. Kisha Akasema Aliyetukuka:

وَأَنْذِرْهُمْ يَوْمَ الْحَسْرَةِ

***“Na waonye siku ya majuto.”*** Maana: Waonye viumbe kwa siku ya majuto.

إِذْ قُضِيَ الْأَمْرُ

***“Itapokatwa Amri.”***

Maana yake: Kupambanuliwa baina ya watu wa Peponi na watu wa Motoni, na kila mmoja akapelekwa sehemu ya makazi yake ya daima.

وَهُمْ

***“Nao wamo.”*** Maana yake: Leo, katika maisha ya hapa duniani,

فِي غَفْلَةٍ

**“Katika pumbao.”**

Kwa walioonywa kwayo kwa siku ya majuto na huzuni.

وَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٢٧﴾

**“Wala hawaamini”.** Maana: Hawataamini kuwa hilo ni kweli.

Imaam Ahmad amepokea kutoka kwa Abu Sa’id رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِذَا دَخَلَ أَهْلُ الْجَنَّةِ الْجَنَّةَ وَأَهْلُ النَّارِ النَّارَ، بُجَاءَ بِالْمَوْتِ كَأَنَّهُ كَبَشْرٌ أَمْلَحُ فَيُوقَفُ بَيْنَ الْجَنَّةِ وَالنَّارِ، فَيَقَالُ: يَا أَهْلَ الْجَنَّةِ هَلْ تَعْرِفُونَ هَذَا، قَالَ: فَيَسْرِيُونَ وَيَنْظُرُونَ وَيَقُولُونَ: نَعَمْ هَذَا الْمَوْتُ - قَالَ: - فَيَقَالُ: يَا أَهْلَ النَّارِ، هَلْ تَعْرِفُونَ هَذَا؟ قَالَ: فَيَسْرِيُونَ وَيَنْظُرُونَ وَيَقُولُونَ: نَعَمْ هَذَا الْمَوْتُ - قَالَ: - فَيُؤْمَرُ بِهِ فَيُذْبَحُ، قَالَ: وَيَقَالُ: يَا أَهْلَ الْجَنَّةِ، خُلُودٌ وَلَا مَوْتٌ، وَيَا أَهْلَ النَّارِ، خُلُودٌ وَلَا مَوْتٌ»

*“Pindi watakapoingia Peponi watu wa Peponi na watakapoingia Motoni watu wa Motoni, umauti utaletwa kama kwamba ni kondoo mzuri na atawekwa baina ya Pepo na Moto. Kisha patasemwa: ‘Enyi watu wa Peponi! Je, mwamjua huyu?’ Watageuza mtizamo wao na kutizama, na watasema: ‘Ndio, huu ni umauti’. Akasema: Patasemwa: ‘Enyi watu wa Motoni! Je, mwamjua huyu?’ Akasema: Watageuza mtizamo wao na kutizama, na watasema: ‘Ndio, huu ni umauti’. Akasema: “Kutatolewa amri ya kuchinjwa, naye atachinjwa.” Akasema: Na kutasemwa: ‘Enyi watu wa Peponi! Daima (milele) na hakuna tena umauti. Enyi watu wa Motoni! Daima na hakuna tena umauti’.*

Kisha Mtume ﷺ akasoma Aya:

وَأَنْذِرْهُمْ يَوْمَ الْحَسْرَةِ إِذْ قُضِيَ الْأَمْرُ وَهُمْ فِي غَفْلَةٍ وَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٢٨﴾

**“Na waonye siku ya majuto itapokatwa Amri. Nao wamo katika ghafla, wala hawaamini.”**

Na akaashiria kwa mkono wake, kisha akasema:

«أَهْلُ الدُّنْيَا فِي غَفْلَةٍ الدُّنْيَا»

*“Watu wa duniani wamezama katika pumbao la maisha ya dunia”<sup>1</sup>.*

Hivi ndivyo ilivyopokewa na Imaam Ahmad na pia imetolewa na Al- Bukhaariy na Muslim katika Sahihi zao<sup>2</sup>, na lafudhi zipo karibu sana na hiyo. Na imepokewa kutoka kwa ‘Abdallah bin Mas’ud رضى الله عنه katika kisa alichokitaja, akasema: “Hakuna nafsi ila itatazama makazi yake Peponi na makazi yake Motoni, na hii itakuwa katika siku ya majuto. Kwa hiyo, watu wa Motoni wataona makazi yao waliyotayarishiwa na Allah تعالى kama wangeamini.” Kisha wataambiwa: ‘Lau mngeamini na mkafanya amali njema, mngepata hii, mnayoona Peponi’. Kisha, watashikwa na majuto na huzuni. Hivyo hivyo, watu wa Peponi wataona makazi yao yaliyo Motoni, na wataambiwa: ‘Lau Allah تعالى Hakuwaneemesha (haya yangukuwa makazi yenu)...’<sup>3</sup> Na Kauli Yake:

إِنَّا نَحْنُ نَرِثُ الْأَرْضَ وَمَنْ عَلَيْهَا وَإِلَيْنَا يُرْجَعُونَ ﴿٢٧﴾

***“Hakika Sisi Tutairithi ardhi na walio juu yake. Na Kwetu watarejeshwa”.***

Allah تعالى Anatupa habari kuwa Yeye Ndiye Muumba, Mmiliki na Mwenye Kuendesha mambo yote. Viumbe wote wataangamia. Ni Yeye tu, Aliye juu na Mtukufu, Atabaki. Hakuna anayeweza kudai umiliki wowote wala kupeleka na kuendesha mambo mbali na Yeye. Yeye Ndiye Mrithi wa viumbe Vyake vyote. Yeye Ndiye Atakayebaki milele, Atakayebaki baada ya kila mmoja kuondoka na Yeye Ndiye Hakimu wa mambo yote. Hivyo, hakuna nafsi itakayo dhulumiwa hata wizani wa bawa la mbu au atomu. Amepokea Ibn Abi Haatim kutoka kwa Hazm bin Abi Haazim Al-Qutwa’iy aliyesema: ‘Umar bin ‘Abdul-‘Aziz رحمه الله تعالى alimuandikia ‘Abdul-Hamid bin ‘Abdur-Rahman, aliyekuwa liwali wa Kufah: Ama baada ya hayo: Hakika Allah تعالى Amefaradhisha kwa viumbe Vyake mauti Alipowaumba, naye Akajaalia hatima yao. Akasema hayo ni katika jumla ya Alivyoteremsha katika Kitabu Chake cha kweli, Alichokihifadhi kwa Elimu Yake na Akawafanya Malaika Zake kushuhudia kuhifadhiwa kwake. Naye Atarithi ardhi na wote walio juu yake, na wote watarudi Kwake<sup>4</sup>.

<sup>1</sup> Ahmad 3:9.

<sup>2</sup> Fat’h Al-Baariy 8: 282 na Muslim 4:2188.

<sup>3</sup> Atw-Twabariy 8:344.

<sup>4</sup> Ibn Abi Haatim 7:2410.

وَأَذْكُرُ فِي الْكِتَابِ إِبْرَاهِيمَ ۚ إِنَّهُ كَانَ صِدِّيقًا نَبِيًّا ﴿٤١﴾ إِذْ  
 قَالَ لِأَبِيهِ يَا أَبَتِ لِمَ تَعْبُدُ مَا لَا يَسْمَعُ وَلَا يُبْصِرُ وَلَا  
 يُغْنِي عَنْكَ شَيْئًا ﴿٤٢﴾ يَا أَبَتِ إِنِّي قَدْ جَاءَنِي مِنَ الْعِلْمِ مَا  
 لَمْ يَأْتِكَ فَاتَّبِعْنِي أَهْدِكَ صِرَاطًا سَوِيًّا ﴿٤٣﴾ يَا أَبَتِ لَا  
 تَعْبُدِ الشَّيْطَانَ ۗ إِنَّ الشَّيْطَانَ كَانَ لِلرَّحْمَنِ عَصِيًّا ﴿٤٤﴾  
 يَا أَبَتِ إِنِّي أَخَافُ أَنْ يَمَسَّكَ عَذَابٌ مِنَ الرَّحْمَنِ فَتَكُونَ  
 لِلشَّيْطَانِ وَلِيًّا ﴿٤٥﴾ قَالَ أَرَأَيْتَ أَنْتَ عَنِ الْهَيْبَةِ بَلِإِبْرَاهِيمَ  
 ۗ لَنْ لَمْ نَنْتَه لِأَرْحَمْنِكَ ۗ وَأَهْجُرْنِي مَلِيًّا ﴿٤٦﴾ قَالَ سَلِمْتُ  
 عَلَيْكَ ۗ سَأَسْتَغْفِرُ لَكَ رَبِّي ۗ إِنَّهُ كَانَ بِي حَفِيًّا ﴿٤٧﴾  
 وَأَعْتَرَلَكُمْ وَمَا تَدْعُونَ مِنَ دُونِ اللَّهِ وَأَدْعُوا رَبِّي عَسَى  
 أَلَّا أَكُونَ بِدُعَاءِ رَبِّي شَقِيًّا ﴿٤٨﴾ فَلَمَّا أَعْتَرَهُمْ وَمَا  
 يَعْبُدُونَ مِنَ دُونِ اللَّهِ وَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ ۗ كُلًّا  
 جَعَلْنَا نَبِيًّا ﴿٤٩﴾ وَوَهَبْنَا لَهُم مِّن رَّحْمَتِنَا وَجَعَلْنَا هُمْ  
 لِسَانَ صِدْقٍ عَلِيًّا ﴿٥٠﴾ وَأَذْكُرُ فِي الْكِتَابِ مُوسَى ۚ إِنَّهُ كَانَ  
 مُخْلَصًا وَكَانَ رَسُولًا نَّبِيًّا ﴿٥١﴾ وَنَسَدَيْنَاهُ مِنَ جَانِبِ الطُّورِ  
 الْأَيْمَنِ وَقَرَّبْنَاهُ نَجِيًّا ﴿٥٢﴾ وَوَهَبْنَا لَهُ مِنْ رَّحْمَتِنَا أَخَاهُ  
 هَارُونَ نَبِيًّا ﴿٥٣﴾ وَأَذْكُرُ فِي الْكِتَابِ إِسْمَاعِيلَ ۚ إِنَّهُ كَانَ  
 صَادِقَ الْوَعْدِ وَكَانَ رَسُولًا نَّبِيًّا ﴿٥٤﴾ وَكَانَ يَأْمُرُ أَهْلَهُ  
 بِالصَّلَاةِ وَالزَّكَاةِ وَكَانَ عِنْدَ رَبِّهِ مَرْضِيًّا ﴿٥٥﴾

وَأَذْكُرُ فِي الْكِتَابِ إِبْرَاهِيمَ ۚ إِنَّهُ كَانَ  
 صِدِّيقًا نَبِيًّا ﴿٤١﴾ إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ  
 يَا أَبَتِ لِمَ تَعْبُدُ مَا لَا يَسْمَعُ وَلَا  
 يُبْصِرُ وَلَا يُغْنِي عَنْكَ شَيْئًا ﴿٤٢﴾  
 يَا أَبَتِ إِنِّي قَدْ جَاءَنِي مِنَ الْعِلْمِ مَا  
 لَمْ يَأْتِكَ فَاتَّبِعْنِي أَهْدِكَ صِرَاطًا  
 سَوِيًّا ﴿٤٣﴾ يَا أَبَتِ لَا تَعْبُدِ الشَّيْطَانَ  
 ۗ إِنَّ الشَّيْطَانَ كَانَ لِلرَّحْمَنِ عَصِيًّا  
 ﴿٤٤﴾ يَا أَبَتِ إِنِّي أَخَافُ أَنْ يَمَسَّكَ  
 عَذَابٌ مِنَ الرَّحْمَنِ فَتَكُونَ لِلشَّيْطَانِ  
 وَلِيًّا ﴿٤٥﴾

41. Na mtaje katika Kitabu Ibraahim. Hakika yeye alikuwa mkweli, Nabii.

42. Alipomuambia baba yake: Ewe baba yangu! Kwa nini unaabudu visivyosikia, na visivyoona, na visivyo-kufaa chochote?

43. Ewe baba yangu! Kwa yakini imenifikia elimu isiyokufikia wewe. Basi nifuate mimi, nami nitakuo-ngoza njia iliyo sawa.



**44. Ewe baba yangu! Usimuabudu Shetani. Hakika Shetani ni mwenye kumuasi Mwingi wa Rehema.**

**45. Ewe baba yangu! Hakika mimi naogopa isikupate adhabu inayotoka kwa Mwingi wa Rehema ukaja kuwa mwenziwe Shetani.**

### Mawaidha ya Ibrahim عليه السلام kwa Baba Yake

Anasema Aliyetukuka kumuambia Mtume Wake, Muhammad ﷺ:

وَأَذْكُرْ فِي الْكِتَابِ إِبْرَاهِيمَ

**“Na mtaje katika Kitabu Ibraahim.”**

Wasomee haya watu wako wanaoabudu masanamu na watajije yaliyomfikia Ibraahim عليه السلام, aliye rafiki wa karibu wa *ar-Rahman* (Khalil Ar-Rahman). Ambao wao (Maquraysh) ni katika kizazi chake, nao wanadai kuwa wanafuata Dini yake. Waeleze kuwa yeye alikuwa Nabii mkweli. Waambie yaliyotokea na baba yake na jinsi gani alivyomkataza kuabudu masanamu.

Akasema Ibraahim عليه السلام:

يَتَأْتِيَ لِمَ تَعْبُدُ مَا لَا يَسْمَعُ وَلَا يُبْصِرُ وَلَا يُغْنِي عَنْكَ شَيْئًا ﴿١٩﴾

**“Ewe baba yangu! Kwa nini unaabudu visivyosikia, na visivyoona, na visivyokufaa chochote?”**

Maana yake: Hawawezi kukunufaisha wala kukuinga na madhara yoyote.

يَتَأْتِيَ إِيَّيْ قَدْ جَاءَنِي مِنَ الْعِلْمِ مَا لَمْ يَأْتِكَ

**“Ewe baba yangu! Kwa yakini imenifikia elimu isiyokufikia wewe”.**

Akasema: “Japokuwa natoka katika uti wa mgongo wako na unaniona ni mdogo kwako kwa kuwa ni mtoto wako, jua kuwa nimepata elimu kutoka kwa Allah تعالی ambayo hujui na haijakufikia”. Hivyo,

فَاتَّبَعْنِي أَهْدِكَ صِرَاطًا سَوِيًّا ﴿٢٠﴾

**“Basi nifuate mimi, nami nitakuongoza njia iliyo sawa.”**

Maana yake: Njia nyoofu ambayo itakufikisha katika lengo linalo tarajiwa na kukuokoa kwa kinachoogopewa (Moto).

يَتَأْتِي لَا تَعْبُدِ الشَّيْطَانَ

**“Ewe baba yangu! Usimuabudu Shetani.”**

Maana: Usimtii kwa kuabudu masanamu. Hakika yeye anaita kwa hilo na anaridhia sana kufanywa jambo hilo. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

﴿ أَلَمْ أَعْهَدْ إِلَيْكُمْ يَبْنَىءَ آدَمَ أَن لَّا تَعْبُدُوا الشَّيْطَانَ إِنَّهُ لَكُمُ عَدُوٌّ مُّبِينٌ ﴾

**“Je, sikukuagizeni (sikukuusieni) enyi wanadamu kuwa msimuabudu Shetani? Hakika yeye ni adui aliye dhahiri kwenu.” (36:60).**

Na Amesema:

﴿ إِن يَدْعُونَ مِن دُونِهِ إِلَّا إِنْتَا وَإِن يَدْعُونَ إِلَّا شَيْطَنَا مَرِيدَا ﴾

**“Hawaabudu baada ya kumwacha Allah ila waungu wanawake; wala hawamwabudu ila Shetani aliye asi.” (4:117).**

Na Kauli Yake:

﴿ إِنَّ الشَّيْطَانَ كَانَ لِلرَّحْمَنِ عَصِيَا ﴾

**“Hakika Shetani ni mwenye kumuasi Mwingi wa Rehema.”**

Maana yake: mkaidi, mweye kiburi kwa kumuasi Mola wake Mlezi. Kwa hiyo, Allah تعالى Alimfukuza na kumueka mbali. Hivyo, usimfuata ili usije ukawa kama yeye.

يَتَأْتِي إِنِّي أَخَافُ أَن يَمَسَّكَ عَذَابٌ مِّنَ الرَّحْمَنِ

**“Ewe baba yangu! Hakika mimi naogopa isikupate adhabu inayotoka kwa Mwingi wa Rehema.”**

Maana yake: Kwa ajili ya kumshirikisha Allah تعالى kumuasi kwa ninayokuamuru. Hatima yake:

﴿ فَتَكُونُ لِلشَّيْطَانِ وَلِيَا ﴾

**“Ukaja kuwa mwenziwe Shetani.”**

Maana yake: Hakuna atakayekulinda wala kukusaidia wala kukuokoa ukimfuata Ibilisi. Hakuna anayeweza kukusaidia, si yeye wala mwengine yeyote. Hakuna

atakayekuwa na amri ya lolote siku hiyo isipokuwa Allah تعالى tu. Bali kumfuata yeye itakufanya uwe ni mwenye kuzungukwa na adhabu ya Allah تعالى, kama Anavyosema Aliyetukuka:

تَاللَّهِ لَقَدْ أَرْسَلْنَا إِلَىٰ أُمَمٍ مِّن قَبْلِكَ فَزَيَّنَ لَهُمُ الشَّيْطَانُ أَعْمَالَهُمْ فَهُوَ وَلِيُّهُمُ الْيَوْمَ وَهُمْ  
عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٦٣﴾

**“Wallahi! Sisi Tulituma (Mitume) kwa Ummah zilizokuwa kabla yako; lakini Shetani aliwapambia vitendo vyao. Kwa hivyo yeye (shetani) ni rafiki yao, nao watapata adhabu iumizayo.” (16:63)**

قَالَ أَرَأَيْتَ أَنْتَ عَنْ ءَالِهَتِي يَتَّبِعُهُمْ لَئِن لَّمْ تَنْتَه لَأَرْجُمَنَّكَ وَأَهْجُرَنِي مَلِيًّا ﴿٦٤﴾ قَالَ  
سَلِّمْ عَلَيَّ سَأَسْتَغْفِرُ لَكَ رَبِّي إِنَّهُ كَانَ بِي حَفِيًّا ﴿٦٥﴾ وَأَعْتَرِلَكُمْ وَمَا تَدْعُونَ  
مِن دُونِ اللَّهِ وَأَدْعُوا رَبِّي عَسَىٰ أَلَّا أَكُونَ بِدُعَاءِ رَبِّي شَقِيًّا ﴿٦٦﴾

**46. (Baba) akasema: Unaichukia miungu yangu, ewe Ibraahim? Kama huachi, basi lazima nitakupiga mawe. Na niondokelee mbali Maliyan! (milele).**

**47. (Ibraahim) akasema: Salamun ‘alayka! Amani iwe juu yako! Mimi nitakuomba msamaha kwa Mola wangu Mlezi. Hakika Yeye Ananihurumia sana.**

**48. Nami najitenga nanyi na hayo mnayoyaabudu badala ya Allah. Na ninamuomba Mola wangu Mlezi; asaa nisiwe mwenye kukosa bahati kwa kumuomba Mola wangu Mlezi.**

**Jawabu la Babake Ibrahim عليه السلام**

Allah تعالى Anasema Akituelezea jawabu la babake Ibrahim عليه السلام kwa mtoto wake, Ibraahim عليه السلام kwa alilomuitia. Akasema:

قَالَ أَرَأَيْتَ أَنْتَ عَنْ ءَالِهَتِي يَتَّبِعُهُمْ

**“Unaichukia miungu yangu, ewe Ibraahim?”** Maana yake: Ikiwa hutaki kuwaabudu (masanamu) wala huwaridhii, basi kwa uchache wacha kuwaalani, kuwatusi na kuwabeza na kuwakejeli. Hakika,

usipoacha, nitakuadhibu, kukulaani na kukukejeli. Na hiyo ni kauli yake:

لَأَرْحَمَنَّكَ ط

**“Nitakupiga mawe”.** Wamesema hayo Ibn ‘Abbaas, As-Suddiy, Ibn Jurayj, Adh-Dhahaak na wengineo رضي الله عنهم<sup>1</sup>. Na Kauli Yake:

وَأَهْجُرَنِي مَلِيًّا ﴿٤١﴾

**“Na niondokelee mbali milele.”** Mujaahid, ‘Ikrimah, Sa’id bin Jubayr na Muhammad bin Is-haaq رحمه الله تعالى wamesema: *“Maliyan”* ina maana milele.”<sup>2</sup> Hasan Al-Baswriy amesema, “Kwa muda mrefu”<sup>3</sup>. Asuddiy amesema,

وَأَهْجُرَنِي مَلِيًّا ﴿٤٢﴾

**“Na niondokelee mbali!”** Hii ina maana ya daima (milele)<sup>4</sup>. Na wamepokea ‘Aliy bin Abi Twalhah na Al-‘Awfiy kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuwa amesema:

وَأَهْجُرَنِي مَلِيًّا ﴿٤٣﴾

**“Na niondokelee mbali!”** Ina maana nenda zako kwa amani na usalama kabla sijakuadhibu”. Adh-Dhahaak, Qatadah, ‘Atwiyyah Al-Jadaliy, Maalik na wengineo wamesema hivyo hivyo. Hii pia ndiyo rai iliyochaguliwa na Ibn Jariir رحمه الله تعالى.

**Jawabu la Ibrahim** تعالى عليه السلام Rafiki wa Allah

Hapo Ibrahim عليه السلام alimuambia babake:

سَلَّمَ عَلَيْكَ ط

**“Amani iwe juu yako!”** Kama Alivyosema Aliyetukuka Kuelezea sifa za Waumini,

وَإِذَا خَاطَبَهُمُ الْجَاهِلُونَ قَالُوا سَلَامًا ﴿٤٤﴾

**“Na wajinga wakisema nao (maneno mabaya) huwajibu maneno ya salama (amani).” (25:63).**

<sup>1</sup> At-Tabari 18:205.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:205, 206.

<sup>3</sup> At-Tabari 18:205.

<sup>4</sup> At-Tabari 18:206.

Na Anasema Aliyetukuka:

وَإِذَا سَمِعُوا اللَّغْوَ أَعْرَضُوا عَنْهُ وَقَالُوا لَنَا أَعْمَلُنَا وَلَكُمْ أَعْمَلُكُمْ سَلَمٌ عَلَيْكُمْ لَا نَبْتَغِي

الْجَاهِلِينَ ﴿٢٥﴾

**“Na wanaposikia upuuzi hujitenga nao na husema: Sisi tuna vitendo vyetu na nyinyi muna vitendo vyenu; amani juu yenu. Sisi hatutaki kujibizana na watu wajinga.” (28:55).**

Na maana ya kauli ya Ibrahim عليه السلام kwa babake:

سَلَمٌ عَلَيْكَ

**“Amani iwe juu yako!”** Maana yake: Hutasikia matusi kutoka kwangu wala madhara. Hii ni kwa ajili ya heshima na hadhi ya ubaba.

سَأَسْتَغْفِرُ لَكَ رَبِّي

**“Mimi nitakuombea msamaha kwa Mola wangu Mlezi”.**

Lakini nitamuomba Allah تعالى Akuongoze na Akughufirie dhambi zako.

إِنَّهُ كَانَ بِي حَفِيًّا ﴿٢٦﴾

**“Hakika Yeye ni Hafiyya kwangu”.**

Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما na wengineo wamesema kuwa maana ya “Hafiyya” ni, “Huruma”<sup>1</sup>. Maana: Kwangu mimi, kwa kuniongoza kumuabudu Yeye tu na kumtakasia Dini yangu. Amesema As-Suddiy: “Al-Hafiyy ni Yule Anayetilia umuhimu mkubwa sana mambo yake (Ibrahim عليه السلام).” Hakika, Ibrahim عليه السلام alimuomba msamaha babake kwa muda mrefu, hata baada ya kuhamia Shaam. Aliendelea kumuomba msamaha hata baada ya kujenga Msikiti Mtukufu (Makkah) na baada ya kuzaliwa kwa watoto wake wawili, Ismaa’il عليه السلام na Is-haaq عليه السلام. Hii inapatikana katika Kauli Yake Aliyetukuka:

رَبَّنَا اغْفِرْ لِي وَلِوَالِدَيَّ وَلِلْمُؤْمِنِينَ يَوْمَ يَقُومُ الْحِسَابُ ﴿٢٧﴾

**“Mola wetu Mlezi! Unighufirie mimi na wazazi wangu wote wawili na wanaoamini, siku ya kusimama hesabu (Kiyama).” (14:41).**

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:207.

Hakika Waislamu waliwaombea maghufira jamaa zao wa karibu na familia zao miongoni mwa washirikina mwanzoni wa ujumbe wa Mtume wa Allah تعالى (mwanzo wa Uislamu), na hiyo ni kufuata kielelezo cha Ibrahim Khalil katika hilo mpaka Allah تعالى Akateremsha:

قَدْ كَانَتْ لَكُمْ أُسْوَةٌ حَسَنَةٌ فِي إِبْرَاهِيمَ وَالَّذِينَ مَعَهُ إِذْ قَالُوا لِقَوْمِهِمْ إِنَّا بُرَءُؤُا مِنْكُمْ  
وَمِمَّا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ

**“Hakika nyinyi mna mfano mzuri kwa Nabii Ibrahim na wale waliokuja pamoja naye; walipowaambia jamaa zao makafiri: ‘Kwa yakini sisi tu mbali nanyi, na mbali na hayo mnayoyaabudu kinyume cha Allah.’ (60:4)**

Mpaka kwa Kauli Yake,

إِلَّا قَوْلَ إِبْرَاهِيمَ لِأَبِيهِ لَأَسْتَغْفِرَنَّ لَكَ وَمَا أَمْلِكُ لَكَ مِنَ اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ

**“Ila katika usemi wake Ibrahim kumuambia baba yake: ‘Hakika nitakuombea msamaha, wala sina uweza wa chochote kwa ajili yako mbele ya Allah...’ (60:4),**

Maana: Ila kwa kauli hii, hivyo msiifuate. Kisha Allah تعالى Alibainisha kuwa Ibrahim عليه السلام aliwacha kauli hii na kuiondoa (kuifuta kauli hiyo). Akasema Aliyetukuka:

مَا كَانَ لِلنَّبِيِّ وَالَّذِينَ ءَامَنُوا أَنْ يَسْتَغْفِرُوا لِلْمُشْرِكِينَ

**“Haimpasii Mtume na wale walioamini kuwatakia samahani washirikina.” (9:113) Mpaka Kauli Yake,**

وَمَا كَانَ لِأَسْتِغْفَارِ إِبْرَاهِيمَ لِأَبِيهِ إِلَّا عَن مَّوْعِدَةٍ وَعَدَهَا إِيَّاهُ فَلَمَّا تَبَيَّنَ لَهُ أَنَّهُ عَدُوٌّ

لِلَّهِ تَبَرَّأَ مِنْهُ إِنَّ إِبْرَاهِيمَ لَأَوَّاهٌ حَلِيمٌ ﴿١١٤﴾

**“Wala haikuwa Ibrahim kumtakia samahani baba yake ila kwa sababu ya ahadi aliyofanya naye. Lakini ilipo mbainikia kwamba yeye ni adui wa Dini ya Allah (kwa ukaidi tu sio kwa ujinga), alijiepusha naye. Kwa yakini Ibraahim alikuwa mwingi wa kurejea kwa Mungu na mvumilivu.” (9:114).**

Na Kauli Yake:

وَأَعْتَرُكُمْ وَمَا تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ

**“Nami najitenga nanyi na hayo mnayoyaabudu badala ya Allah.”**

Maana yake: Najitenga mbali nanyi pamoja na miungu yenu ambayo mnaiabudu pasina Allah تعالى.

وَأَدْعُوا رَبِّي

**“Na ninamuomba Mola wangu Mlezi.”**

Maana yake: Nimuabudu Mola wangu Mlezi Peke Yake hana mshirika.

عَسَىٰ آلَٰ أَكُونَ بِدُعَاءِ رَبِّي شَقِيًّا

**“Asaa nisiwe mwenye kukosa bahati kwa kumuomba Mola wangu Mlezi.”**

Na Asaa, ni neno lenye maana ya matumaini (au huenda); nalo limetumika kumaanisha lile ambalo litatokea na sio lile ambalo linatumainiwa kutokea bila kizuizi. Hakika, yeye (Ibrahim عليه السلام) ni kiongozi na mkuu wa Manabii baada ya Muhammad ﷺ.

فَلَمَّا أَعْتَرَهُمْ وَمَا يَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ وَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ ۗ وَكُلًّا جَعَلْنَا نَبِيًّا

وَوَهَبْنَا لَهُمْ مِنْ رَحْمَتِنَا وَجَعَلْنَا لَهُمْ لِسَانَ صِدْقٍ عَلِيًّا

**49. Basi alipojitenga nao na yale waliyokuwa wakiyaabudu badala ya Allah, Tulimpa Is-haaq na Ya'quub, na kila mmoja Tukamfanya Nabii.**

**50. Na Tukawapa Rehema Zetu na Tukawajaalia kupewa sifa za kweli tukufu.**

**Allah** عليه السلام Kumtunukia Ibrahim عليه السلام, Is-haaq عليه السلام na Ya'quub عليه السلام

Anasema Aliyetukuka: Pindi Rafiki wa Allah تعالى (Ibrahim عليه السلام) alipojitenga na baba yake na watu wake kwa ajili ya Allah تعالى, Allah تعالى Alimpatia badala yake walio bora kuliko wao. Alimpatia Is-haaq عليه السلام na Ya'quub عليه السلام, kumaanisha mtoto wake, na mtoto wa Is-haaq عليه السلام, yaani Ya'quub عليه السلام.

Hii ni kama Alivyosema Allah تعالى katika sehemu nyingine,

وَيَعْقُوبَ نَافِلَةً<sup>ط</sup>

**“Na Ya’quub kuwa mjukuu...” (21:72).**

Na Akasema:

وَمِنْ وَرَاءِ إِسْحَاقَ يَعْقُوبَ ﴿٧٢﴾

**“Na baada ya Is-haaq, watapata mjukuu wamuite Ya’quub.” (11:71).**

Hakuna tofauti yoyote kuwa Is-haaq عليه السلام ni baba yake Ya’quub عليه السلام, kwani lipo andiko kwenye Qur’ani katika Suratul Baqarah:

أَمْ كُنْتُمْ شُهَدَاءَ إِذْ حَضَرَ يَعْقُوبَ الْمَوْتُ إِذْ قَالَ لِبَنِيهِ مَا تَعْبُدُونَ مِنْ بَعْدِي قَالُوا نَعْبُدُ  
إِلَهَكَ وَإِلَهَ آبَائِكَ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ وَإِسْحَاقَ

**“Je, mlikuwapo yalipomfikia Ya’quub mauti, alipowaambia wanawe: ‘Je, mtamuabudu nani baada yangu’. Wakasema: ‘Tutamuabudu Mola wako Mlezi na Mola wa baba zako, Ibraahim, Ismaa’il na Is-haaq.’ (2:133).**

Allah تعالى Amemtaja Is-haaq عليه السلام na Ya’quub عليه السلام hapa kuwa Aliwafanya Manabii miongoni mwa kizazi na makhalifa kwa ajili ya kumpatia liwazo, faraja na furaha katika maisha yake. Hii ndiyo sababu ya Allah تعالى Kusema:

وَكُلًّا جَعَلْنَا نَبِيًّا ﴿٤٩﴾

**“Na kila mmoja Tukamfanya Nabii”. (19:49)**

Lau Ya’quub عليه السلام hakuwa Nabii katika uhai wa Ibraahim عليه السلام, Allah تعالى Hangeibana Ahadi Yake ya unabii kwake, lakini Angetaja na Mtoto wake Yusuf عليه السلام pia. Kwa hakika, Yusuf عليه السلام pia alikuwa Nabii, kama alivyosema Mtume ﷺ katika Hadithi iliyoafikiwa katika usahihi wake, pale alipoulizwa nani aliye bora miongoni mwa watu. Akasema:

«يُوسُفُ نَبِيٌّ اللَّهِ ابْنُ يَعْقُوبَ نَبِيِّ اللَّهِ ابْنِ إِسْحَاقَ نَبِيِّ اللَّهِ ابْنِ إِبْرَاهِيمَ خَلِيلِ اللَّهِ»

**“Nabii wa Allah, Yusuf, mtoto wa Nabii wa Allah, Ya’quub, mtoto wa Nabii wa Allah, Is-haaq, mtoto wa Rafiki wa Allah, Ibraahim”<sup>1</sup>.**

<sup>1</sup> Fat’h Al-Baariy 8:212.





**Kutajwa kwa Musa عليه السلام na Haarun عليه السلام.**

Baada ya Allah تعالى Kututajia kuhusu Ibrahim عليه السلام, Rafiki wa Allah na Kumsifu, Alimtaja *Al-Kaliim* (aliyezungumza moja kwa moja na Allah تعالى). Allah تعالى Anasema:

وَأَذْكُرْ فِي الْكِتَابِ مُوسَىٰ إِنَّهُ كَانَ مُخْلَصًا

**“Na mtaje Musa katika Kitabu. Hakika yeye alikuwa ni Mukhlaswan.”**

Imepokewa na Thawriy kutoka kwa ‘Abdul-‘Aziz bin Rafi’ kuwa Abu Lubabah amesema: “Wanafunzi (wa Isa عليه السلام) walisema: ‘Ee Roho wa Allah! Tujulishe kuhusu aliye **Mukhlaswan** wa Allah تعالى’. Akasema: ‘Ni yule anayefanya kitendo kwa ajili ya Allah تعالى tu wala hataki watu wamtukuze au wamsifu’”. Wengine wakasoma kwa *fat’ha, Mukhlasw*, inayomaanisha aliyechaguliwa. Kama Alivyosema Allah تعالى:

إِنِّي اصْطَفَيْتُكَ عَلَى النَّاسِ

**“Mimi nimekuchagua juu ya watu wote” (7:144).**

وَكَانَ رَسُولًا نَّبِيًّا

**“Alikuwa Mtume, Nabii.”**

Allah تعالى Amemtunuku sifa hizo mbili. Hakika alikuwa miongoni mwa Mitume wakubwa na mmoja kati ya wale Mitume watano wenye azma kubwa, nao ni Nuuh, Ibraahim, Musa, Isa na Muhammad, Sala na salamu za Allah تعالى ziwashukie wote hao pamoja na Manabii wote. Na Kauli Yake:

وَتَنْدِيئُهُ مِنْ جَانِبِ الطُّورِ

**“Na Tulimuita upande wa Twuur.”** Maana yake: Jabali (mlima).

الْأَيْمَنِ

**“Wa kulia.”** Huo ulikuwa upande wa kulia wa Musa عليه السلام pale alipokwenda kutaka kuchukua kipande cha moto. Alikiona kiking’aa kutoka mbali, hivyo alikwenda na kukikuta kipo upande wa kulia wa mlima kutoka kwake, pembezoni mwa bonde alilokuwemo. Hapo ndipo Allah تعالى Alipozungumza naye na kumuita. Allah تعالى Alimtaka aje karibu na Kuzungumza naye. Na Kauli Yake:

وَوَهَبْنَا لَهُ مِنْ رَحْمَتِنَا أَخَاهُ هَارُونَ نَبِيًّا ﴿٤١﴾

**“Nasi kwa Rehema Zetu Tukampa nduguye, Haarun, awe Nabii.”**

Maana: Tulimuitikia ombi lake kwa niaba ya nduguye na Tukamfanya yeye kuwa Nabii. Hii ni kama Alivyosema Allah تعالى katika Aya nyingine:

وَأَخِي هَارُونُ هُوَ أَفْصَحُ مِنِّي لِسَانًا فَأَرْسَلَهُ مَعِيَ رِدْءًا يُصَدِّقُنِي ۗ إِنِّي أَخَافُ أَنْ يُكَدِّبُونَ ﴿٤٢﴾

**“Na ndugu yangu Haarun ni fasihi zaidi kuliko mimi kwa usemi, basi mtume pamoja nami awe msaidizi, kunisadikisha; hakika mimi naogopa ya kwamba watanikadhibisha.” (28:34).**

Na Akasema:

قَالَ قَدْ أُوتِيتَ سُؤْلَكَ يَا مُوسَىٰ ﴿٤٣﴾

**“Akasema: Hakika umepewa maombi yako, ewe Musa!” (20:36).**

Na Akasema:

فَأَرْسَلْنَا إِلَىٰ هَارُونَ ﴿٤٤﴾ وَهُمْ عَلَىٰ ذَنْبٍ فَأَخَافُ أَنْ يَقْتُلُونِ ﴿٤٥﴾

**“Basi upeleke ujumbe huu kwa Haarun. Nao wanalo kosa, kisasi kwangu. Basi naogopa wasije wakaniua.” (26:13-14).**

Kwa sababu ya hili, baadhi ya wema waliotangulia wamesema: “Hakuna katika maisha haya aliyemuomba yeyote kama Musa عليه السلام alivyomuomba nduguye awe Nabii”. Allah تعالى Anasema:

وَوَهَبْنَا لَهُ مِنْ رَحْمَتِنَا أَخَاهُ هَارُونَ نَبِيًّا ﴿٤٦﴾

**“Nasi kwa Rehema Zetu Tukampa nduguye, Haarun, awe Nabii”.**

وَأَذْكُرُ فِي الْكِتَابِ إِسْمَاعِيلَ ۚ إِنَّهُ كَانَ صَادِقَ الْوَعْدِ وَكَانَ رَسُولًا نَبِيًّا ﴿٤٧﴾ وَكَانَ يَأْمُرُ أَهْلَهُ بِالصَّلَاةِ وَالزَّكَاةِ وَكَانَ عِنْدَ رَبِّهِ مَرْضِيًّا ﴿٤٨﴾

**54. Na mtaje katika Kitabu Ismaail. Bila ya shaka yeye alikuwa ni mkweli wa ahadi, na alikuwa Mtume, Nabii.**

**55. Na alikuwa akiwaamrisha watu wake Sala na Zaka, na alikuwa mbele ya Mola wake Mlezi mwenye kuridhiwa.**

**Kumtaja Ismail** عليه السلام

Hii ni sifa kutoka kwa Allah تعالى kwa Ismail عليه السلام, mtoto wa Ibrahim عليه السلام, Rafiki wa Allah تعالى. Yeye (Ismail عليه السلام) ni baba wa Waarabu wote wa Hijaz kwa sababu alikuwa mkweli kwa aliyokuwa akiahidi. Ibn Jurayj amesema: “Hakufanya ahadi yoyote kwa Mola wake Mlezi isipokuwa aliitekeleza”<sup>1</sup>. Hakujilazimisha kufanya kitendo chochote cha ‘Ibadah kwa nadhiri, ila aliitekeleza kwa kuipatia haki yake. Wamesema baadhi yao, “Hakika aliambiwa,

صَادِقَ الْوَعْدِ

**‘Alikuwa mkweli wa ahadi.’**

Kwa kuwa alimuambia baba yake:

سَتَجِدُنِي إِنْ شَاءَ اللَّهُ مِنَ الصَّابِرِينَ ﴿١٠٢﴾

**“Utanikuta Insha’Allah (Allah Akipenda) miongoni mwa wanaosubiri.” (37:102).**

Akawa mkweli katika hilo la kuwa mkweli katika ahadi, na ni katika sifa nzuri za kusifiwa. Kama ilivyo kuvunja na kutotekeleza ahadi ni katika sifa mbaya inayochukiza. Allah تعالى Anasema:

يَأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لِمَ تَقُولُونَ مَا لَا تَفْعَلُونَ ﴿٦١﴾ كَبُرَ مَقْتًا عِنْدَ اللَّهِ أَنْ تَقُولُوا مَا

لَا تَفْعَلُونَ ﴿٦٢﴾

**“Enyi Mlioamini! Mbona munasema musiyoyatenda? Ni chukizo kubwa mbele ya Allah kusema musiyoyatenda.” (61:2-3)**

Na amesema Mtume ﷺ:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:211.

«آيَةُ الْمُنَافِقِ ثَلَاثٌ: إِذَا حَدَّثَ كَذَبَ، وَإِذَا وَعَدَ أَخْلَفَ، وَإِذَا اتَّخَذَ خَانَ»

*“Alama za mnafiki ni tatu: Akizungumza anadanganya, akiahidi hatekelezi na akiaminiwa hufanya hiyana.”<sup>1</sup>*

Zilipokuwa hizi ni sifa za wanafiki, kadhalika na sifa zilizo kinyume na hizi ni katika sifa za Waumini wa kweli. Kwa ajili hii, Allah تعالی Alimsifu mja Wake na Mtume Ismail عليه السلام kwa kuwa mkweli katika kutekeleza ahadi. Hivyo hivyo, Mtume ﷺ alikuwa mkweli katika ahadi. Hakumuahidi yeyote isipokuwa alitekeleza ahadi yake kwa mtu huyo. Alimsifu Abul ‘Asw bin Ar-Rabi’, mume wa binti yake, Zaynab رضي الله عنها kwa kusema:

«حَدَّثْتِي فَصَدَّقْتَنِي، وَوَعَدْتَنِي فَأَوْفَى لِي»

*“Alizungumza nami, akasema ukweli; na aliniahidi naye akatekeleza ahadi hiyo kwangu.”<sup>2</sup>*

Alipoaga dunia Mtume ﷺ, Khalifah Abubakar Asw-Swiddiq رضي الله عنه alisema: “Yeyote aliyeahidiwa na Mtume ﷺ au anam dai, aje kwangu nami nitatekeleza hayo kwa niaba yake”. Hivyo Jaabir bin ‘AbdAllah رضي الله عنهما alikuja na kumuambia kuwa Mtume ﷺ aliniambia:

«لَوْ قَدْ جَاءَ مَالُ الْبَحْرَيْنِ أُعْطَيْتَكَ هَكَذَا وَهَكَذَا وَهَكَذَا»

*“Lau mali ya Bahrain yatakuja (kwangu), basi nitakupatia hivi na hivi na hivi.”*

Maana yake: Atamjazia mali kwenye mikono yake. Mali hayo ya Bahrain yalipofika, Asw-Swiddiq رضي الله عنه aliamuru Jaabir رضي الله عنه aje na kujaza mikono yake kwa mali hiyo. Kisha, akamuamuru afanye tena, jumla yake zikawa ni Dirham mia tano (500). Kisha Abubakar رضي الله عنه akampatia tena mfano wake mara mbili<sup>3</sup> (yaani Dirham elfu moja zaidi). Na Kauli Yake:

<sup>1</sup> Al-Bukhaariy 33, 2682, 2749 na 6095.

<sup>2</sup> Fat’h Al-Baariy 5:380.

<sup>3</sup> Fat’h Al-Baariy 4:554.

وَكَانَ رَسُولًا نَّبِيًّا ﴿٤١﴾

**“Na alikuwa Mtume, Nabii”.**

Katika hili kuna dalili ya cheo na hadhi kubwa ya Ismail عليه السلام kwa nduguye Is-haaq عليه السلام. Is-haaq عليه السلام alielezwa kuwa ni Nabii pekee, ilhali Ismail عليه السلام amesifiwa kwa Unabii na Utume. Na imethibiti katika Sahihi Muslim kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ اللَّهَ اضْطَفَىٰ مِنْ وَلَدِ إِبْرَاهِيمَ إِسْمَاعِيلَ»

*“Hakika Allah Amemchagua Ismaail katika watoto wa Ibraahim”<sup>1</sup>.*

Kisha Imam Muslim ametaja Hadithi yote kwa ukamilifu wake na hii ni dalili kwa tuliyoasema. Na Kauli Yake:

وَكَانَ يَأْمُرُ أَهْلَهُ بِالصَّلَاةِ وَالزَّكَاةِ وَكَانَ عِنْدَ رَبِّهِ مَرْضِيًّا ﴿٤٢﴾

**“Na alikuwa akiwaamrisha watu wake Swala na Zakah, na alikuwa mbele ya Mola wake Mlezi mwenye kuridhiwa.”**

Hii pia ni sifa njema, inayopendeza, yenye kujenga na ya haki. Aliamriwa katika njia hii kwa sababu ya kujikita kwake katika kumtii Mola wake Mlezi na kuiamrisha familia yake kutekeleza hayo. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka kwa Mtume Wake ﷺ:

وَأْمُرْ أَهْلَكَ بِالصَّلَاةِ وَاصْطَبِرْ عَلَيْهَا

**“Na waamrishe watu wako kuswali na uendelee mwenyewe kwa hayo.”(20:132).**

Na Akasema:

يَتَأْتِيهِمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا قُوًا أَنفُسِكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَارًا وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ عَلَيْهَا مَلَائِكَةٌ

غَلَاطٌ شِدَادٌ لَا يَعْصُونَ اللَّهَ مَا أَمَرَهُمْ وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمَرُونَ ﴿٤٣﴾

<sup>1</sup> Muslim 4:1782.

***“Enyi Mlioamini! Jiokoeni nafsi zenu na watu wenu, na Moto ambao kuni zake ni watu na mawe. Wanausimamia Malaika wakali, wenye nguvu, hawamuasi Allah kwa Amri Zake; na wanatenda wanayoamrisha yote.” (66:6)***

Maana yake: Waamrishe kufanya mema, wakataze mabaya wala usiwapuuze. Ukifanya hivyo, nao wakakutii katika maamrisha yako, Moto wa Jahanamu hautawala (hautawagusa) Siku ya Kiyama. Na imekuja katika Hadithi kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«رَجِمَ اللهُ رَجُلًا قَامَ مِنَ اللَّيْلِ فَصَلَّى وَأَبْقَطَ امْرَأَتَهُ، فَإِنْ أَبَتْ نَضَحَ فِي وَجْهِهَا الْمَاءَ. رَجِمَ اللهُ امْرَأَةً قَامَتْ مِنَ اللَّيْلِ فَصَلَّتْ وَأَبْقَطَتْ زَوْجَهَا، فَإِنْ أَبَى نَضَحَتْ فِي وَجْهِهِ الْمَاءَ»

*“Allah Amrehemu mtu aliyeamka kusali usiku na kumuamsha mkewe, anapokataa kuamka, akamnyunyizia maji usoni mwake. Allah Amrehemu mwanamke anayeamka kuswali usiku akaswali na kumuamsha mumewe, na anapokataa, akamnyunyizia maji usoni mwake.”*

Hadithi imepokewa na Abu Daawuud na Ibn Maajah.<sup>1</sup>

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Abu Daawuud 2:73 na Ibn Maja 1:424.

وَأَذْكُرْ فِي الْكِتَابِ إِدْرِيْسَ ۗ إِنَّهُ كَانَ صِدِّيقًا نَبِيًّا ﴿٥٦﴾  
 وَرَفَعْنَاهُ مَكَانًا عَلِيًّا ﴿٥٧﴾ أُولَئِكَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ  
 مِنَ النَّبِيِّينَ مِن ذُرِّيَّةِ آدَمَ وَمِمَّنْ حَمَلْنَا مَعَ نُوحٍ وَمِن  
 ذُرِّيَّةِ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْرَائِيلَ وَمِمَّنْ هَدَيْنَا وَاجْتَبَيْنَا ۗ إِذَا تُتْلَىٰ  
 عَلَيْهِمْ آيَاتُ الرَّحْمَنِ خَرُّوا سُجَّدًا وَسُكُوتًا ﴿٥٨﴾ \* خَلَقَ  
 مِنْ بَعْدِهِمْ خَلْفًا أَضَاعُوا الصَّلَاةَ وَاتَّبَعُوا الشَّهْوَةَ ۗ  
 فَسَوْفَ يَلْقَوْنَ غِيًّا ﴿٥٩﴾ إِلَّا مَنْ تَابَ وَآمَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا  
 فَأُولَئِكَ يُدْخِلُونَ الْجَنَّةَ وَلَا يُظْلَمُونَ شَيْئًا ﴿٦٠﴾ جَنَّتٍ  
 عَدْنٍ الَّتِي وَعَدَ الرَّحْمَنُ عِبَادَهُ بِالْغَيْبِ ۗ إِنَّهُ كَانَ وَعْدُهُ  
 مَأْتِيًّا ﴿٦١﴾ لَا يَسْمَعُونَ فِيهَا لَغْوًا إِلَّا سَلَامًا ۗ وَهُمْ فِيهَا  
 فِيهَا بِكْرَةٌ وَعِشْيًا ﴿٦٢﴾ تِلْكَ الْجَنَّةُ الَّتِي نُورِثُ مِنَ عِبَادِنَا  
 مَنْ كَانَ تَقِيًّا ﴿٦٣﴾ وَمَا نَنْزِلُ إِلَّا بِأَمْرِ رَبِّكَ ۗ لَهُ مَا بَيْنَ  
 أَيْدِينَا وَمَا خَلْفَنَا وَمَا بَيْنَ ذَلِكَ ۗ وَمَا كَانَ رَبُّكَ نَسِيًّا ﴿٦٤﴾  
 رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا فَاعْبُدْهُ وَاصْطَبِرْ  
 لِعِبَادَتِهِ ۗ هَلْ تَعْلَمُ لَهُ سَمِيًّا ﴿٦٥﴾ وَيَقُولُ الْإِنْسَانُ أَإِذَا  
 مَا مِتُّ لَسَوْفَ أُخْرَجُ حَيًّا ﴿٦٦﴾ أَوْ لَا يَذْكُرُ الْإِنْسَانُ أَنَا  
 خَلَقْنَاهُ مِن قَبْلُ وَلَمْ يَكُ شَيْئًا ﴿٦٧﴾ فَوَرَبِّكَ لَنَحْشُرَنَّهُمْ  
 وَالشَّيَاطِينَ ثُمَّ لَنُحْضِرَنَّهُمْ حَوْلَ جَهَنَّمَ جِثًّا ﴿٦٨﴾ ثُمَّ  
 لَنَنْزِعَنَّ مِنَ كُلِّ شِيعَةٍ أَيُّهُمْ أَشَدُّ عَلَى الرَّحْمَنِ عِتِيًّا ﴿٦٩﴾  
 ثُمَّ لَنَحْنُ أَعْلَمُ بِالَّذِينَ هُمْ أَوْلَىٰ بِهَا صِلِيًّا ﴿٧٠﴾

وَأَذْكُرْ فِي الْكِتَابِ إِدْرِيْسَ ۗ إِنَّهُ كَانَ  
 صِدِّيقًا نَبِيًّا ﴿٥٦﴾ وَرَفَعْنَاهُ مَكَانًا  
 عَلِيًّا ﴿٥٧﴾

56. Na mtaje katika Kitabu Idris. Hakika yeye alikuwa ni mkweli Nabii.

57. Na Tulimuinua daraja ya juu.

Kumtaja Idris عليه السلام.

Ametajwa Idris عليه السلام kwa Kumsifu kwa kuwa alikuwa mkweli, Nabii. Na hakika Allah Aliinyanyua daraja yake ikawa ya juu. Na imetajwa huko nyuma katika Sahihi kuwa Mtume ﷺ alikutana na Idris عليه السلام katika usiku wa Israa', naye (Idris) alikuwa katika uwingu wa nne (4). Amepokea Sufyaan kutoka kwa Mujaahid kuwa amesema:

﴿٥٧﴾ وَرَفَعْنَاهُ مَكَانًا عَلِيًّا

“Na Tulimuinua daraja ya juu.”

Uwingu wa nne<sup>1</sup>. Na amesema Al-Hasan na wengineo kuhusu Kauli Yake:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:213.



وَرَفَعْنَاهُ مَكَانًا عَلِيًّا ﴿٥٧﴾

*“Na Tulimuinua daraja ya juu.”* Maana yake: Pepo.

أُولَئِكَ الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنَ النَّبِيِّينَ مِن ذُرِّيَّةِ آدَمَ وَمِمَّنْ حَمَلْنَا مَعَ نُوحٍ وَمِن  
ذُرِّيَّةِ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْرَائِيلَ وَمِمَّنْ هَدَيْنَا وَاجْتَبَيْنَا إِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ آيَاتُ الرَّحْمَنِ خَرُّوا

سُجَّدًا وَسُبَّحًا ﴿٥٨﴾

**58. Hao ndio Aliowaneemesha Allah miongoni mwa Manabii katika uzao wa Adam, na katika uzao wa wale Tuliowapandisha pamoja na Nuuh, na katika uzao wa Ibraahim na Israil, na katika wale Tuliowaongoa na Tukawateua. Wanaposomewa Ayah za Mwingi wa Rehema huanguka kusujudu na kulia.**

### Manabii Hao ni Wateule

Allah تعالى Anasema: **‘Manabii hawa’** – na lengo sio waliotajwa katika Sura hii tu bali inawahusisha Manabii wote. Allah تعالى Anabadili tu mazungumzo kutoka kwa watu makhsusi kwa kikundi chote cha Manabii.

الَّذِينَ أَنْعَمَ اللَّهُ عَلَيْهِمْ مِنَ النَّبِيِّينَ مِن ذُرِّيَّةِ آدَمَ

**“Ndio Aliowaneemesha Allah miongoni mwa Manabii katika uzao wa Adam.”**

Amesema As-Suddiy na Ibn Jariir, Allah تعالى Awarehemu: “Kilichokusudiwa kwa uzao wa Adam عليه السلام ni Idris عليه السلام, na kinachomaanishwa na uzao wa wale Tuliowachukua pamoja na Nuuh عليه السلام ni Ibraahim عليه السلام. Na wale maana ya uzao wa Ibraahim عليه السلام ni Is-haaq عليه السلام, Ya’quub عليه السلام na Ismaail عليه السلام, na kinachomaanishwa kwa uzao wa Israili ni Musa عليه السلام, Haarun عليه السلام, Zakariyya عليه السلام, Yahya عليه السلام na Isa bin Maryam عليه السلام”. Ibn Jariir رحمه الله تعالى amesema: “Na hiyo ndiyo tofauti ya nasaba zao, japokuwa Adam عليه السلام amewakusanya wote hao (kama baba yao wa asili). Sababu ni kuwa miongoni mwao kuna yule ambaye hakuwa katika uzao wa wale waliokuwa katika safina pamoja na Nuhu عليه السلام, naye ni Idris عليه السلام. Hakika yeye alikuwa ni babu wa Nuhu عليه السلام”. Nasema kuwa hii ndio maana ya dhahiri zaidi kuwa Idris عليه السلام ndiye nguzo kwa nasaba ya Nuhu عليه السلام<sup>1</sup>.

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:214.

Na inayotilia nguvu kuwa muradi na lengo la Aya hii ni kujumuisha Manabii wote, ni kama Kauli ya Aliyetukuka katika Suratul An'aam:

وَتِلْكَ حُجَّتُنَا آتَيْنَاهَا إِبْرَاهِيمَ عَلَىٰ قَوْمِهِ ۚ نَرْفَعُ دَرَجَاتٍ مِّنْ ذُنُوبِهِ إِنَّا بِرَبِّكَ حَكِيمٌ  
 عَلَيْهِ ۝ وَوَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ ۚ كُلًّا هَدَيْنَا ۚ وَنُوحًا هَدَيْنَا مِن قَبْلُ ۚ وَمِن  
 ذُرِّيَّتِهِ دَاوُدَ وَسُلَيْمَانَ وَأَيُّوبَ وَيُوسُفَ وَمُوسَىٰ وَهَارُونَ ۚ وَكَذَٰلِكَ نَجْزِي الْمُحْسِنِينَ  
 ۝ وَذَكَرْنَا وَيْحَىٰ وَعِيسَىٰ وَإِلْيَاسَ ۚ كُلًّا مِّنَ الصَّالِحِينَ ۝ وَإِسْمَاعِيلَ وَالْيَسَعَ  
 وَيُوشَعَ ۚ وَلُوطًا ۚ وَكُلًّا فَضَّلْنَا عَلَىٰ الْعَالَمِينَ ۝ وَمِنَ آبَائِهِمْ وَذُرِّيَّاتِهِمْ وَإِخْوَانِهِمْ  
 وَاجْتَبَيْنَاهُمْ وَهَدَيْنَاهُمْ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ۝

*“Na hizi ndizo baadhi ya hoja Zetu Tulizompa Ibraahim juu ya watu wake. Tunamnyanyua katika vyeo yule Tumtakaye. Hakika Mola wako Mlezi Ndiye Mwenye Hekima na Ndiye Ajuaye. Na Tukampa (Ibraahim mtoto anayeitwa) Is-haaq na (mjukuu anayeitwa) Ya'quub, wote Tukawaongoa. Na Nuuh Tulimuongoa zamani. Na katika kizazi chake (Nuuh, Tulimuongoa) Daawuud, Sulaymaan, Ayyub, Yusuf, Musa na Haarun. Na hivi ndivyo Tuwalipavyo wafanyao mema. Na Tukamuongoa Zakariyya, Yahya, Isa na Ilyas wote walikuwa miongoni mwa watu wema. Na Tukamuongoa Ismaail, Alyasa', Yunus na Luutw. Na wote Tukawafadhilisha juu ya walimwengu. Na Tukawaongoa baadhi ya baba zao na vizazi vyao na ndugu zao. Na Tukawachagua na Kuwaongoza katika njia ilinyooka.” (6:83-87) Mpaka kwa Kauli Yake,*

أُولَٰئِكَ الَّذِينَ هَدَىٰ اللَّهُ ۖ فَبِهُدُنَاهُمْ أَقْتَدِهٖ ۚ

*“Hao ndio ambao Allah Amewaongoa. Basi fuata uwongofu wao....” (6:90). Na Amesema Aliyetukuka:*

مَنْ قَصَصْنَا عَلَيْكَ وَمِنْهُمْ مَّن لَّمْ نَقْصُصْ عَلَيْكَ

*“Wengine (Mitume) katika hao Tumekusimulia habari zao, na wengine hatukukusimulia.” (40:78).*

Na katika Sahihi Al-Bukhari kutoka kwa Mujaahid kuwa alimuuliza Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: "Je, kuna *Sijdah* katika *Swaad*?" Akasema: "Ndio, kisha akasoma Aya hii,

أُولَئِكَ الَّذِينَ هَدَى اللَّهُ فَبِهِدَاهُمُ آقَّتَدِرُهُ

**"Hao ndio ambao Allah Amewaongoa. Basi fuata uwongofu wao..." (6:90).**

Kisha Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما akasema, "Hivyo, Mtume wenu ni mmoja kati ya wale walioamrisha kuwafuata. Naye ni kati ya wanaofaa kufuatwa", Maana: Daawud.<sup>2</sup> Na amesema Allah تعالى katika Aya hii Tukufu:

إِذَا تَتَلَىٰ عَلَيْهِمْ آيَاتُ الرَّحْمَنِ خَرُّوا سُجَّدًا وَبُكِيًّا ﴿٥٨﴾

**"Wanaposomewa Aya za Mwingi wa Rehema huanguka kusujudu na kulia." (19:58)**

Maana yake: Wanaposikia maneno ya Allah تعالى yanayotaja hoja na dalili Zake, wanasujudu kwa unyenyekevu, utulivu, kwa kumhimidi na kumshukuru Mola wao Mlezi kwa walio nayo katika neema kubwa.

Na neno *Bukiyyan* mwisho wa Aya ni wingi neno *Baki* lenye maana wale wenye kulia. Kwa ajili hii wanazuoni wamekubali kuwa ni sheria kusujudu kwa kuisoma Aya hii, kwa kuwafuata wao na kushikamana na njia zao za Ibadah.

﴿٥٩﴾ خَلَّفَ مِنْ بَعْدِهِمْ خَلْفٌ أَضَاعُوا الصَّلَاةَ وَاتَّبَعُوا الشَّهْوَاتِ فَسُوفَ يَلْقَوْنَ غِيًّا ﴿٥٩﴾

إِلَّا مَنْ تَابَ وَآمَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا فَأُولَئِكَ يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ وَلَا يُظْلَمُونَ شَيْئًا ﴿٦٠﴾

**59. Lakini wakaja baada yao walio wabaya, wakaacha Sala, na wakafuata matamano. Basi watakujakuta malipo ya ubaya.**

<sup>1</sup> Surah ya Qur'ani namba 38 – Mfasiri.

<sup>2</sup> Fat'h Al-Baariy 8:144. Aya inayokusudiwa ni ya 24, katika Surah Swaad (38) ambamo ku-metajwa Daawud عليه السلام kuwa alisujudu. Kwa vile Allah Aliyetukuka Aameamuru kufuata kwa waliyongozwa katika Aya hizi za Suratul An'aam, hivyo pia tunahitajika kusujudu kwa kutajwa kusujudu kwa Manabii, kulingana na Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما.

**60. Isipokuwa waliotubu, wakaamini, na wakatenda mema. Hao, basi, wataingia Peponi wala hawatadhulumiwa chochote.**

### **Wakarithiwa Baada Yao na Watu Wabaya na Wazuri**

Baada ya Allah تعالى kutaja kundi la watu wema lililofaulu, nao ni Manabii عليه السلام na waliowafuata kwa kusimama imara katika mipaka ya Allah تعالى na maamrisha Yake, kutekeleza waliyoamrisha na Allah تعالى na kuepuka makatazo Yake Ametaja,

(خَلَفَ مِنْ بَعْدِهِمْ خَلْفٌ)

(kuwa baada ya hao walifuatiwa na kizazi). Hii ina maana ya vizazi vilivyofuata baadaye:

أَضَاعُوا الصَّلَاةَ

**“Wakaacha Sala.”**

Na wanapoiacha Sala hiyo hufahamika kwamba kisichokuwa Sala katika mambo mengine ya wajibu kitapotea zaidi, kwa sababu Sala ni nguzo na msingi wa Dini. Hii ni amali iliyo njema kwa mja kuitekeleza. Hivyo, watu hawa watajishughulisha na matamania, ladha na utamu wa kidunia na wakaridhia maisha ya dunia. Watakuwa katika utulivu na katika raha na utamu wa duniani. Kwa hiyo, watu hawa wanakutana na Ghayy, inayo maanisha hasara Siku ya Kiyama. Al-Awzaa'iy رحمه الله تعالى Amepokea kutoka kwa Musa bin Sulaymaan, kutoka kwa Qaasim bin Mukhaymirah kuwa alisema yafuatayo kuhusu Kauli ya Aliyetukuka:

✽ خَلَفَ مِنْ بَعْدِهِمْ خَلْفٌ أَضَاعُوا الصَّلَاةَ

**“Lakini wakaja baada yao walio wabaya, wakaacha Sala”**

Maana: “Hawatunzi wakati maalumu uliowekewa Sala, kwa sababu lau ingemaanisha kuacha kabisa Sala, ingekuwa ni ukafiri”<sup>1</sup>. Na imepokewa kwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه kuwa aliambiwa: “Allah mara nyingi Ametaja Sala katika Qur'ani.”<sup>2</sup> Akasema:

الَّذِينَ هُمْ عَنْ صَلَاتِهِمْ سَاهُونَ

**‘Ambao wanapuuza Swala zao.’ (107:5).**

<sup>1</sup> At-Tabari 18:215.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:216.

الَّذِينَ هُمْ عَلَى صَلَاتِهِمْ دَائِمُونَ ﴿٢٣﴾

**Na, 'Ambao wanadumisha Sala zao.'** (70:23). Na pia,

وَالَّذِينَ هُمْ عَلَى صَلَاتِهِمْ يُحَافِظُونَ ﴿٢٤﴾

**'Na ambao Sala zao wanazihifadhi.'** (23:9)

Akasema Ibn Mas'ud رضي الله عنهما: "Kwa wakati wake". Watu wakasema: "Tulidhani kuwa huko ni kuacha Sala kabisa". Akajibu: "Kufanya hivyo ni ukafiri"<sup>1</sup>. Masruq amesema: "Hakuna yeyote anayehifadhi Sala tano kisha akaandikiwa kuwa yu miongoni mwa walioghafilika. Na katika kuzipuuza kuna maangamivu. Na kuzipuuza ni kuzichelewesha na kuziswali nje ya muda wake."<sup>2</sup> Amepokea Al-Awzaa'iy رحمه الله تعالى kutoka kwa Ibraahim bin Zayd kuwa 'Umar bin 'Abdul-Aziz رحمه الله تعالى alisoma Aya hii:

﴿٢٥﴾ خَلَفَ مِنْ بَعْدِهِمْ خَلْفٌ أَضَاعُوا الصَّلَاةَ وَاتَّبَعُوا الشَّهْوَاتِ فَسَوْفَ يَلْقَوْنَ غَيًّا

**"Lakini wakaja baada yao walio wabaya, wakaacha Sala, na wakafuata matamano. Basi watakujakuta malipo ya ubaya."** (19:59)

Kisha akasema: 'Haikuwa kuacha Sala kabisa bali ilikuwa ni kuziswali nje ya wakati wake"<sup>3</sup>. Na Kauli Yake:

﴿٢٦﴾ فَسَوْفَ يَلْقَوْنَ غَيًّا

**"Basi watakujakuta Ghayy."**

Amepokea 'Aliy bin Abi Twalhah kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema:

﴿٢٧﴾ فَسَوْفَ يَلْقَوْنَ غَيًّا

**"Basi watakujakuta Ghayy."**

Maana: 'Hasara"<sup>4</sup> Na amesema Qatadah: "Shari."<sup>5</sup> Na amepokea Sufyaan Ath-Thawriy, Shu'bah na Muhammad bin Is-haaq kutoka kwa Abi Is-haaq As-Sabi'iy, kutoka kwa Abi 'Ubaydah, kuwa 'Abdallah bin Mas'ud رضي الله عنه amesema:

<sup>1</sup> At-Tabari 18:216.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:216.

<sup>3</sup> At-Tabari 18:216.

<sup>4</sup> At-Tabari 18:219.

<sup>5</sup> At-Tabari 18:218.

﴿ فَسَوْفَ يَلْقَوْنَ غَيًّا ﴾

**“Basi watakujakuta Ghayy.”**

Maana: “Hilo ni bonde katika Jahanamu lenye kina kirefu na chakula chake ni kibaya”. Na amepokea Al-A'mash kutoka kwa Ziyaad kuwa Abi 'Iyaadhw amesema kuhusu Kauli Yake:

﴿ فَسَوْفَ يَلْقَوْنَ غَيًّا ﴾

**“Basi watakujakuta Ghayy.”**

Maana yake: ‘Ni bonde katika Jahanamu lenye usaha na damu’. Na Kauli Yake:

﴿ إِلَّا مَنْ تَابَ وَآمَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا ﴾

**“Isipokuwa waliotubu, wakaamini, na wakatenda mema.”**

Maana: Isipokuwa kwa wanaorudi kusimamisha Sala na kuacha kufuata matamania, hakika ni kuwa Allah تعالی Atakubali toba yake, kufanya hatima yao kuwa nzuri na kuwafanya warithi Pepo ya Neema. Kwa ajili hii, Allah تعالی Anasema:

﴿ فَأُولَئِكَ يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ وَلَا يُظَلَّمُونَ شَيْئًا ﴾

**“Hao, basi, wataingia Peponi wala hawatadhumiwa chochote.”**

Na hiyo ni kuwa toba inafuta yale yaliyokuwa kabla yake. Na katika Hadithi nyingine,

﴿التَّائِبُ مِنَ الذَّنْبِ كَمَنْ لَا ذَنْبَ لَهُ﴾

**“Mwenye kutubia kutokana na dhambi ni kama asiyekuwa na dhambi”<sup>1</sup>.**

Kwa sababu hiyo, wenye kutubia hawatapoteza chochote kwa amali njema walizofanya. Wala hawatapatilizwa kwa waliyoyafanya kabla ya toba yao, hivyo kupunguza thawabu zao kwa amali wanazofanya baada ya toba yao. Hiyo ni kuwa kila waliyofanya kabla ya toba yanapotea, kusahuliwa na kutotiwa hesabuni. Huu ni Ukarimu wa Aliye Mkarimu na Huruma ya Aliye Mpole. Na huku ni kuvuliwa kulikofanywa kwa watu hawa, sawa na Kauli ya Allah تعالی katika Suratul Furqaan,

<sup>1</sup> Ibn Maajah 2:1420.

وَالَّذِينَ لَا يَدْعُونَ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ وَلَا يَقْتُلُونَ النَّفْسَ الَّتِي حَرَّمَ اللَّهُ إِلَّا بِالْحَقِّ

**“Na wale wasiomuomba mungu mwingine pamoja na Allah, wala hawai nafsi aliyoiharamisha Allah ila kwa haki...”**

Mpaka Kauli Yake,

وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٧٠﴾

**“Na Allah ni Mwingi wa Kusamehe na Mwingi wa Kurehemu.”**  
(25:68-70).

جَنَّاتٍ عَدْنٍ الَّتِي وَعَدَ الرَّحْمَنُ عِبَادَهُ بِالْغَيْبِ ۗ إِنَّهُ كَانَ وَعْدُهُ مَأْتِيًا ﴿٦٩﴾ لَا يَسْمَعُونَ فِيهَا لَغْوًا إِلَّا سَلَامًا ۗ وَهُمْ فِيهَا رِزْقُهُمْ فِيهَا بُكْرَةٌ وَعِشْيًا ﴿٧٠﴾ تِلْكَ الْجَنَّةُ الَّتِي نُورِثُ مِنْ عِبَادِنَا مَنْ كَانَ تَقِيًّا ﴿٧١﴾

**61. Bustani za milele alizowaahidi Rahmani waja Wake katika siri. Hakika Ahadi Yake hapana shaka itafika.**

**62. Humo hawatasikia upuuzi, ila salama tu. Na watapata humo riziki zao asubuhi na jioni.**

**63. Hiyo ndiyo Pepo Tutayowarithisha katika waja Wetu waliokuwa wachamungu.**

### Maelezo na Ufafanuzi wa Bustani (Pepo) la Waongofu na Wale Waliotubia

Anasema Aliyetukuka: Pepo ambayo wataingia wenye kutubia kutokana na madhambi yao - hiyo ni Pepo 'Adn, yenye maana ya milele. Hizi ni Pepo ambazo *Rahmaan* Amewaahidi waja Wake kwa mambo ya ghaibu. Hii inamaanisha kuwa Pepo hizi ni katika vitu visivyoonekana ambazo wanaamini japokuwa hawajazona. Wanaamini ghaibu kwa ile yakini yao na nguvu za Imani zao. Na Kauli Yake:

إِنَّهُ كَانَ وَعْدُهُ مَأْتِيًا ﴿٦٩﴾

**“Hakika Ahadi Yake hapana shaka itafika.”**

Hii ni kutilia nguvu na kuyakinisha ile hakika kuwa itatokea nalo ni jambo lililopitishwa. Allah تعالی Havunji Ahadi Yake wala Haibadilishi. Hii ni sawa na Kauli Yake:

كَانَ وَعْدُهُ مَفْعُولًا ﴿٧٣﴾

**“Ahadi Yake (Allah) itatekelezwa tu.” (73:18).**

Maana yake: Itatokea bila pingamizi aina yoyote. Na Kauli Yake hapa:

مَأْتِيًا ﴿٧٤﴾

**“Itafika”.** Maana yake: Itakuja na kuwafikia waja Wake wanaojitahidi na kuiendea na bila shaka wataifikia. Wapo wafasiri wanaosema:

مَأْتِيًا ﴿٧٥﴾

**“Itafika”.** Kwa maana inakuja, kwa kuwa kila kitu kinachokujia, nawe wakifikia. Hii ni kama wanavyosema Waarabu: “Miaka hamsini ilikuja kwangu, nami nikaiendea miaka hamsini”. Ibara zote mbili zina maana moja (kuwa mimi nina miaka hamsini). Na Kauli Yake:

لَا يَسْمَعُونَ فِيهَا لَغْوًا

**“Humo hawatasikia upuuzi”.**

Maana yake: Katika bustani (na Pepo) hiyo hakutakuwa na mazungumzo ya upuuzi, ya kijinga yasiyo na maana, kama yanavyopatikana hapa duniani. Na Kauli Yake:

إِلَّا سَلَامًا ۗ

**“Ila salama”.** Huku ni kuvua (isipokuwa) kwa kutohusisha kama katika Kauli Yake:

لَا يَسْمَعُونَ فِيهَا لَغْوًا وَلَا تَأْتِيًا ﴿٧٦﴾ إِلَّا قِيلًا سَلَامًا سَلَامًا ﴿٧٧﴾

**“Hawatasikia humo mambo ya upuuzi wala maneno ya dhambi. Isipokuwa maneno ya salama na amani.” (56:25-26).**

Na Kauli Yake:

وَهُمْ رَزَقُهُمْ فِيهَا بُكْرَةً وَعَشِيًّا ﴿٧٨﴾

**“Na watapata humo riziki zao asubuhi na jioni.”**

Maana: Kwa inayofanana na wakati wa asubuhi na jioni. Hii haimaanishi kuwa kutakuwa na usiku na mchana (Peponi), lakini wataishi katika nyakati zinazobadilika. Watajua nyakati zenye mwangaza kwa mwangaza na nuru yake.



Hii ni kama alivyonyukuu Imaam Ahmad kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«أَوَّلُ زُمْرَةٍ تَلِجُ الْجَنَّةَ صُورُهُمْ عَلَى صُورَةِ الْقَمَرِ لَيْلَةَ الْبَدْرِ لَا يَنْصُقُونَ فِيهَا، وَلَا يَتَمَخَّطُونَ فِيهَا. وَلَا يَتَعَوَّطُونَ، آيَتُهُمْ وَأَمْسَاطُهُمُ الذَّهَبُ وَالْفِضَّةُ وَمَجَابِرُهُمُ الْأَلْوَةُ، وَرَشْحُهُمُ الْمِسْكُ وَلِكُلِّ وَاحِدٍ مِنْهُمْ زَوْجَتَانِ، يُرَى مَخَّ سَاقِهَا مِنْ وَرَاءِ اللَّحْمِ مِنَ الْحُسْنِ، لَا اخْتِلَافَ بَيْنَهُمْ وَلَا تَبَاغُضَ، قُلُوبُهُمْ عَلَى قَلْبِ رَجُلٍ وَاحِدٍ، يُسَبِّحُونَ اللَّهَ بُكْرَةً وَعَشِيًّا»

*“Kundi la kwanza litakaloingia Peponi litakuwa na sura kama sura ya mwezi wa usiku ulio kamili. Hawatatema mate wala kupuliza pua zao wala kwenda haja. Vyombo na vichana vyao ni vya dhahabu na fedha na vitezo vyao ni vya kipande cha mshubiri. Jasho lao litakuwa na harufu ya miski na kila mmoja wao atakuwa na wake wawili. Misuli ya miguu yao itaonekana chini ya ngozi kwa uzuri wake. Hawatazozana baina yao wala kuchukiana. Mioyo yao itaunganishwa kama moyo wa mtu mmoja. Watamtakasa Allah asubuhi na jioni.”<sup>1</sup> Imenukuliwa katika Sahihi mbili<sup>2</sup>.*

Na imepokewa na Imaam Ahmad رحمه الله تعالى kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuwa Mtume ﷺ amesema:

«الشُّهَدَاءُ عَلَى بَارِقِ نَهْرِ بِيَابِ الْجَنَّةِ فِي قَبَائِعِ خَضْرَاءَ، يَخْرُجُ عَلَيْهِمْ رِزْقُهُمْ مِنَ الْجَنَّةِ بُكْرَةً وَعَشِيًّا»

*“Mashahidi watakuwa juu ya ukingo wa mto mlangoni mwa Pepo. Juu yao kutakuwa na kuba la kijani. Riziki zao zitatoka Peponi, asubuhi na jioni”.*

Upokezi huu ni wa Ahmad peke yake. Amepokea Adh-Dhahaak kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema:

﴿وَهُمْ رِزْقُهُمْ فِيهَا بُكْرَةً وَعَشِيًّا﴾

***“Na watapata humo riziki zao asubuhi na jioni”.***

<sup>1</sup> Ahmad 2:316.

<sup>2</sup> Fat’h Al-Baariy 6:367 na Muslim 4:2180.

Kiasi cha wakati ulio sawa na usiku na asubuhi. Na Kauli Yake:

تِلْكَ الْحِجَّةُ الَّتِي نُورِثُ مِنْ عِبَادِنَا مَنْ كَانَ تَقِيًّا ﴿٥٦﴾

***“Hiyo ndiyo Pepo Tutayowarithisha katika waja Wetu waliokuwa wachamungu.”***

Maana yake: Pepo hii Tuliyoisifia kwa sifa hizi kubwa na tukufu, ndio Tutakayo warithisha waja Wetu walio wachamungu. Hao ni wale wanaomtii Allah تعالى katika nyakati za furaha, wasaa na dhiki, wazuiyao ghadhabu na wenye kusamehe watu.

Hii ni kama Alivyosema Allah تعالى mwanzo wa Suratul Mu’miniin:

قَدْ أَفْلَحَ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ الَّذِينَ هُمْ فِي صَلَاتِهِمْ خَاشِعُونَ ﴿٢﴾

***“Hakika wamefuzu Waumini. Ambao katika Sala zao huwa na unyenyekevu.”***

Mpaka Aliposema,

أُولَئِكَ هُمُ الْوَارِثُونَ ﴿١١﴾ الَّذِينَ يَرِثُونَ الْفِرْدَوْسَ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿١٢﴾

***“Hao ndio warithi. Ambao watarithi Pepo; wakae humo milele.”***  
(23:10-11).

وَمَا نَنْزِلُ إِلَّا بِأَمْرِ رَبِّكَ لَهُ مَا بَيْنَ أَيْدِينَا وَمَا خَلْفَنَا وَمَا بَيْنَ ذَلِكَ وَمَا كَانَ رَبُّكَ

دَسِيسًا ﴿٦٦﴾ رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا فَاعْبُدْهُ وَاصْطَبِرْ لِعِبَادَتِهِ هَلْ تَعْلَمُ لَهُ

سَمِيًّا ﴿٦٧﴾

**64. (Nao watasema:) Wala hatuteremki ila kwa Amri ya Mola wako Mlezi. Ni Yake Yeye yaliyoko mbele yetu na yaliyoko nyuma yetu, na yaliyomo katikati ya hayo. Na Mola wako Mlezi si Mwenye Kusahau.**

**65. Mola Mlezi wa mbingu na ardhi na vilivyo baina yake. Basi muabudu Yeye tu, na udumu katika ibadah Yake. Je, mnamjua Mwenye jina kama Lake?**

**Malaika Hawateremki ila kwa Amri ya Allah** تعالى

Imaam Ahmad رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kuwa Mtume ﷺ alimuuliza Jibril عليه السلام:

«مَا يَمْتَنِعُكَ أَنْ تَزُورَنَا أَكْثَرَ مِمَّا تَزُورُنَا؟»

*“Ni kitu gani kinachokuzuia kututembelea mara nyingi zaidi kuliko unavyotuzuru?”*

Akasema: Ikateremka Aya hii:

وَمَا نَنْتَهِزُ إِلَّا بِأَمْرِ رَبِّكَ<sup>ط</sup>

***“Wala hatuteremki ila kwa Amri ya Mola wako Mlezi.”***

Mpaka mwisho wa Aya. Bukhari ameipokea hadithi hii peke yake, na akaisimulia katika kuifasiri ayah hii<sup>2</sup>. Na amepokea Awfiy kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kuwa amesema: “Jibril عليه السلام alizuiliwa kumzuru Mtume ﷺ, hivyo akababaika na kuhuzunika kwa sababu ya hilo. Kisha, Jibril عليه السلام alikuja na kumuambia: ‘Ewe Muhammad,

وَمَا نَنْتَهِزُ إِلَّا بِأَمْرِ رَبِّكَ<sup>ط</sup>

***“Wala hatuteremki ila kwa Amri ya Mola wako Mlezi”<sup>3</sup>.***

Na Kauli Yake:

لَهُدَا مَا بَيْنَ أَيْدِينَا وَمَا خَلْفَنَا

***“Ni Yake Yeye yaliyoko mbele yetu na yaliyoko nyuma yetu”.***

Panasemwa: Muradi wa “yaliyoko mbele yetu”, ni mambo ya kidunia, na “Yaliyoko nyuma yetu”, ni mambo ya Akhera.

وَمَا بَيْنَ يَدَيْكَ<sup>ع</sup>

***“Na yaliyomo katikati ya hayo”.*** Maana: Baina ya kupulizwa baragumu mara mbili. Hii ni kauli ya Abil 'Aliyah, 'Ikrimah, Mujaahid, Sa'id bin Jubayr, Qataadah katika moja ya kauli zake, as-Suddiy na Ar-Rabi bin Anas<sup>4</sup>. Na panasemwa:

<sup>1</sup> Ahmad 1:231.

<sup>2</sup> Fat'h Al-Baariy 8:282.

<sup>3</sup> At-Tabari 18:222.

<sup>4</sup> At-Tabari 18:224.

مَا بَيْنَ أَيْدِينَا

**“Na yaliyoko mbele yetu.”**

Maana yake: Mambo ya mustakbali ya Akhera.

وَمَا خَلْفَنَا

**“Na yaliyoko nyuma yetu.”**

Maana yake: Yale yaliyotokea katika maisha ya duniani.

وَمَا بَيْنَ ذَلِكَ

**“Na yaliyomo katikati ya hayo.”**

Maana: Baina ya dunia na Akhera. Na imepokewa mfano wa hayo kutoka kwa Ibn ‘Abbaas, Sa’id bin Jubayr, Adh-Dhahaak, Qatadah, Ibn Jurayj na Ath-Thawriy. Na imechaguliwa na Ibn Jarir رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى, na Allah تَعَالَى Anajua zaidi<sup>1</sup>. Na Kauli Yake:

وَمَا كَانَ رَبُّكَ نَسِيًّا

**“Na Mola wako Mlezi si Mwenye Kusahau.”**

Amesema Mujaahid: “Maana yake ni kuwa Mola wako Mlezi Hajakusahau.”<sup>2</sup>  
Na Kauli Yake:

رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا

**“Mola Mlezi wa mbingu na ardhi na vilivyo baina yake.”**

Maana yake: Muumba wa vyote hivyo, Mwenye Kupelekesha mambo Yake, Hakimu, Mwenye Kudhibiti kila kitu, hakuna anayeweza kupinga Maamuzi Yake.

فَأَعْبُدْهُ وَأَصْطَبِرْ لِعِبَادَتِهِ هَلْ تَعْلَمُ لَهُ سَمِيًّا

**“Basi muabudu Yeye tu, na udumu katika ibadah Yake. Je, munamjua mwenye jina kama Lake?”**

<sup>1</sup> At-Tabari 18:224 na Al-Qurtwubiy 11:129.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:225.

Amepokea 'Aliy bin Abi Twalhah kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: "Je, wamjua Mola aliye mfano Wake au anayefanana Naye?"<sup>1</sup>

Na hivyo ndivyo alivyosema Mujaahid, Sa'id bin Jubayr, Qataadah, Ibn Jurayj na wengineo<sup>2</sup>.

Na Ikrimah amepokea kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kuwa amesema: "Hakuna hata mmoja anayelitwa *ar-Rahman* (Mwingi wa Rehema) mbali na Yeye Aliyetukuka na limetakasika Jina Lake"<sup>3</sup>.

وَيَقُولُ الْإِنْسَانُ أَإِذَا مَا مِتُّ لَسَوْفَ أُخْرَجُ حَيًّا ﴿٦٦﴾ أَوْلَا يَذْكُرُ الْإِنْسَانُ أَنَا خَلَقْتُهُ  
 مِنْ قَبْلُ وَلَمْ يَكُ شَيْئًا ﴿٦٧﴾ فَوَرَبِّكَ لَنَحْشُرَنَّهُمْ وَالشَّيَاطِينَ ثُمَّ لَنُحْضِرَنَّهُمْ حَوْلَ  
 جَهَنَّمَ جِثِيًّا ﴿٦٨﴾ ثُمَّ لَنَنْزِعَنَّ مِنْ كُلِّ شِيعَةٍ أَيُّهُمْ أَشَدُّ عَلَى الرَّحْمَنِ عِتِيًّا ﴿٦٩﴾ ثُمَّ  
 لَنَخُنُّ أَعْلَمُ بِالَّذِينَ هُمْ أَوْلَىٰ بِهَا صِلِيًّا ﴿٧٠﴾

**66. Na mwanadamu husema: Hivyo, nitakapokufa, ni kweli nitafululiwa niwe hai tena?**

**67. Je! Hakumbuki mwanadamu ya kwamba Tulimuumba kabla, na hali hakuwa chochote?**

**68. Basi naapa kwa Mola wako Mlezi! Kwa yakini Tutawakusanya wao pamoja na mashetani; kisha Tutawahudhurisha kuizunguka Jahanamu, nao wamepiga magoti!**

**69. Kisha kwa yakini Tutawatoa katika kila kundi wale miongoni mwao waliozidi kumuasi Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema.**

**70. Tena hakika Sisi Tunawajua vyema zaidi wanaostahiki kuunguzwa humo.**

<sup>1</sup> At-Tabari 18: 226.

<sup>2</sup> At-Tabari 18: 226.

<sup>3</sup> Al-Qurtwubiy 11: 130.

## Kustaajabu kwa Mwanadamu Kufufuliwa baada ya Kufa na Majibu ya Mshangao Wake

Allah تعالى Anatujuulisha kuwa mwanadamu anastaajabu kuwa atarudishwa katika maisha ya uhai baada ya kufa kwake naye anadhania kuwa hili ni jambo ambalo haliwezekani.

Hii ni kama Anavyosema Aliyetukuka:

﴿ وَإِنْ تَعَجَّبْتَ فَعَجَبْتَ قَوْلَهُمْ أَءِذَا كُنَّا تُرَابًا أَعْنَاءُ لِمِى خَلْقٍ جَدِيدٍ ۝﴾

**“Na kama ukistaajabu, basi cha ajabu zaidi ni usemi wao: ‘Je, tutakapokwisha kuwa udongo, kweli tutakuwa katika umbo jipya?’ (13:5).**

Na Akasema:

﴿ أَوَلَمْ يَرَ الْإِنْسَانُ أَنَّا خَلَقْنَاهُ مِنْ نُطْفَةٍ فَإِذَا هُوَ خَصِيمٌ مُّبِينٌ ﴿٧٧﴾ وَضَرَبَ لَنَا مَثَلًا وَنَسِيَ خَلْقَهُ قَالَ مَنْ يُحْيِي الْعِظْمَ وَهِيَ رَمِيمٌ ﴿٧٨﴾ قُلْ يُحْيِيهَا الَّذِي أَنْشَأَهَا أَوَّلَ مَرَّةٍ وَهُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيمٌ ﴿٧٩﴾﴾

**“Je, mwanadamu hatambui ya kwamba Tumemuumba kwa tone la manii? Amekuwa hasimu Yetu aliye dhahiri! Na akatupigia mfano, na akasahau Kuumbwa kwake – akasema: ‘Nani atakayeihusha mifupa na hali imesagika?’ Sema: ‘Ataihusisha Yule Aliyeiumba mara ya kwanza, Naye ni Mjuzi wa kila namna ya Kuumba.’ (36:77-79).**

Na hapa Amesema,

﴿ وَيَقُولُ الْإِنْسَانُ أَءِذَا مَا مِتُّ لَسَوْفَ أُخْرَجُ حَيًّا ﴿٧٦﴾ أَوْ لَا يَذْكُرُ الْإِنْسَانُ أَنَّا خَلَقْنَاهُ مِنْ قَبْلُ وَلَمْ يَكُ شَيْئًا ﴿٧٧﴾﴾

**“Na mwanadamu husema: Hivyo, nitakapokufa, ni kweli nitafufuliwa niwe hai tena? Je! Hakumbuki mwanadamu ya kwamba Tulimuumba kabla, na hali hakuwa chochote?”**

Allah تعالى Anatomia mwanzo wa Kuumba kama dalili ya kuweza kurudiwa tena. Hii inamaanisha Yeye, Aliyetukuka, Amemuumba mwanadamu ilhali hakuwa chochote. Je, hawezi tena kurudisha maumbile yake kwa mara nyingine baada ya kuwa si kitu kinachoonekana.

Hii ni kama Alivyosema:

وَهُوَ الَّذِي يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ

**“Na Yeye Ndiye Aliyeanzisha viumbe na Ndiye Atakayevirudisha mara nyingine, na jambo hili ni rahisi zaidi Kwake.” (30:27).**

Na katika Sahihi imenukuliwa kuwa Mtume ﷺ amesema:

«يَقُولُ اللهُ تَعَالَى: كَذَّبَنِي ابْنُ آدَمَ وَلَمْ يَكُنْ لَهُ أَنْ يُكَذِّبَنِي، وَأَذَانِي ابْنُ آدَمَ وَلَمْ يَكُنْ لَهُ أَنْ يُؤَذِّنَنِي، أَمَا تَكْذِيبُهُ إِيَّايَ فَقَوْلُهُ لَنْ يُعِيدَنِي كَمَا بَدَأَنِي، وَلَيْسَ أَوَّلُ الْخَلْقِ بِأَهْوَنَ عَلَيَّ مِنْ آخِرِهِ، وَأَمَا أَذَاهُ إِيَّايَ فَقَوْلُهُ إِنَّ لِي وَلَدًا وَأَنَا الْأَخْدُ الصَّمَدُ الَّذِي لَمْ يَلِدْ وَلَمْ يُولَدْ وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُوًا أَحَدٌ»

*“Anasema Allah Aliyetukuka: Amenikadhibisha (na Kunikataa) mwanadamu, ilhali hana haki ya kunikataa. Na mwanadamu Ananiudhi, naye hana haki ya Kuniudhi. Ama Kunikataa ni ile kauli yake kuwa hatanirudisha (katika uhai) kama Alivyoniumba mara ya kwanza. Na Kuumbwa kwake mara ya pili si kugumu zaidi Kwangu kuliko ile ya kwanza. Na ama Kuniudhi kwake ni kauli yake kuwa Mimi Nina mtoto, nami ni Mmoja, Anayekusudiwa (Anayehitajiwa na viumbe vyote). Ambaye kwamba Hakuzaa wala Hakuzaliwa, wala Hakuna anayefanana Naye hata mmoja”<sup>1</sup>.*

Na Kauli Yake:

فَوَرَبِّكَ لَنَحْشُرَنَّهُمْ وَالشَّيَاطِينَ

**“Basi naapa kwa Mola wako Mlezi! Kwa yakini Tutawakusanya wao pamoja na mashetani”.**

Mola Mlezi, Aliyetukuka Anaapa kwa nafsi ya Jina Lake Tukufu kuwa bila ya shaka Atawakusanya wote binaadamu pamoja na mashetani walioabudu mbali ya Yeye.

<sup>1</sup> Ahmad 2:350.

ثُمَّ لَنُحْضِرَنَّ لَهُمْ حَوْلَ جَهَنَّمَ جِثِيًّا ﴿٥٧﴾

**“Kisha Tutawahudhurisha kuizunguka Jahanamu, wamesimama (Jithiyaa!)”**

Amepokea Al-'Awfiy kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kuwa amesema: “Hii ina maana amekaa.” Nayo ni kama Kauli Yake:

وَتَرَى كُلَّ أُمَّةٍ جَائِيَةً

**“Na utaona kila Umma Ja-thiyah (umepiga magoti).”<sup>1</sup> (45:28).**

As-Suddiy amesema kuhusu neno *Ja-thiyaa*: “Lina maana ya kusimama”. Imepokewa kutoka kwa Murrah kuwa Ibn Mas'uud رضي الله عنه amesema mfano wake. Na Kauli Yake:

ثُمَّ لَنَنْزِعَنَّ مِنْ كُلِّ شِيعَةٍ

**“Kisha kwa yakini Tutawatoa katika kila kundi.”**

Maana yake: Kutoka katika kila Ummah. Amesema hilo Mujaahid<sup>2</sup>.

أَيُّهُمْ أَشَدُّ عَلَى الرَّحْمَنِ عِتِيًّا ﴿٥٨﴾

**“Wale miongoni mwao waliozidi kumuasi Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema”.**

Amepokea Ath-Thawriy kutoka kwa 'Aliy bin Al-Aqmar kutoka kwa Abu Al-Ahwasw kuwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه amesema: “Watafungwa wa mwanzo hadi wa mwisho mpaka idadi yao ikamilike.” Kisha wataletwa wote pamoja. Kisha Allah تعالى Ataanza na wale wakubwa

ثُمَّ لَنَنْزِعَنَّ مِنْ كُلِّ شِيعَةٍ أَيُّهُمْ أَشَدُّ عَلَى الرَّحْمَنِ عِتِيًّا ﴿٥٨﴾

**“Kisha kwa yakini Tutawatoa katika kila kundi wale miongoni mwao waliozidi kumuasi Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema.”<sup>3</sup>**

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:227.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:228.

<sup>3</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 5:533.



Na hii ni kama Kauli Yake:

حَتَّىٰ إِذَا آذَرَكُوا فِيهَا جَمِيعًا قَالَتْ أُخْرِنُهُمْ لِأَوْلَادِهِمْ رَبَّنَا هَتُّوْنَا أَضْلُوْنَا فَفَاتِهِمْ عَذَابًا  
ضِعْفًا مِّنَ النَّارِ ۗ

***“Mpaka watakapokusanyika wote humo, wa nyuma wao watasema kwa ajili ya wa kwanza wao: ‘Mola wetu Mlezi! Hawa ndio waliotupoteza; basi wape adhabu ya Moto maradufu.”***

Mpaka Kauli Yake:

بِمَا كُنْتُمْ تَكْسِبُونَ ﴿٣٩﴾

***“Kwa sababu ya yale maasi muliyokuwa mukiyachuma.” (7:38-39).***

Na Kauli Yake:

ثُمَّ لَنَحْنُ أَعْلَمُ بِالَّذِينَ هُمْ أَوْلَىٰ بِهَا صِلِيًّا ﴿٤٠﴾

***“Tena hakika Sisi Tunawajua vyema zaidi wanaostahiki kuunguzwa humo”.***

Kisha, hapa Allah تعالى Anaunganisha habari moja kwa nyingine. Na muradi wake hapa ni kuwa Aliyetukuka ni Mjuzi kabisa kwa anayestahiki katika waja Wake Kuingizwa katika Moto wa Jahanamu na kubaki humo milele. Na pia kwa yule anayestahiki adhabu maradufu. Kama Alivyosema katika Aya iliyotangulia:

قَالَ لِكُلِّ ضِعْفٌ وَلٰكِنْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٣٨﴾

***“Atasema: Itakuwa kwenu nyinyi nyote adhabu maradufu, lakini nyinyi hamjui.” (7:38).***

\* \* \*

وَإِنْ مِنْكُمْ إِلَّا وَارِدُهَا كَانَ عَلَى رَبِّكَ حَتْمًا مَقْضِيًّا ﴿٧١﴾  
 ثُمَّ نُنَجِّي الَّذِينَ اتَّقَوْا وَنَذَرُ الظَّالِمِينَ فِيهَا جِثًا ﴿٧٢﴾  
 وَإِذَا تَتَلَوْا عَلَيْهِمْ ءَايَاتُنَا بَيِّنَاتٍ قَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلَّذِينَ  
 ءَامَنُوا أَيُ الْفَرِيقَيْنِ خَيْرٌ مَقَامًا وَأَحْسَنُ نَدْبًا ﴿٧٣﴾ وَكَمْ  
 أَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِنْ قَرْنٍ هُمْ أَحْسَنُ أَثْنًا وَرِءْيَا ﴿٧٤﴾ قُلْ  
 مَنْ كَانَ فِي الضَّلَالَةِ فَلْيَمْدُدْ لَهُ الرَّحْمَنُ مَدًّا حَتَّىٰ إِذَا رَأَوْا  
 مَا يُوعَدُونَ إِمَّا الْعَذَابَ وَإِمَّا السَّاعَةَ فَسَيَعْلَمُونَ مَنْ  
 هُوَ شَرٌّ مَكَانًا وَأَضْعَفُ جُنْدًا ﴿٧٥﴾ وَزَيْدُ اللَّهِ الَّذِينَ  
 أَهْتَدَوْا هُدًى ۗ وَالْبَقِيَّةُ الضَّالِّحَتُ خَيْرٌ عِنْدَ رَبِّكَ  
 ثَوَابًا وَخَيْرٌ مَرَدًّا ﴿٧٦﴾ أَفَرَأَيْتَ الَّذِي كَفَرَ بِآيَاتِنَا وَقَالَ  
 لَأُوتِينَ مَالًا وَّوَلَدًا ﴿٧٧﴾ أَطَّلَعَ الْغَيْبَ أَمِ اتَّخَذَ عِنْدَ  
 الرَّحْمَنِ عَهْدًا ﴿٧٨﴾ كَلَّا ۚ سَنَكْتُبُ مَا يَقُولُ وَنَمُدُّ لَهُ  
 مِنَ الْعَذَابِ مَدًّا ﴿٧٩﴾ وَنَرِيهِ مَا يَقُولُ وَيَأْتِينَا فَرْدًا ﴿٨٠﴾  
 وَاتَّخَذُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ ءَالِهَةً لِيَكُونُوا هُمْ عِزًّا ﴿٨١﴾ كَلَّا ۚ  
 سَيَكْفُرُونَ بِعِبَادِهِمْ وَيَكُونُونَ عَلَيْهِمْ ضِدًّا ﴿٨٢﴾ أَلَمْ تَرَ أَنَا  
 أَرْسَلْنَا الشَّيَاطِينَ عَلَى الْكَافِرِينَ تَوَهُمَ آزًا ﴿٨٣﴾ فَلَا  
 تَعْجَلْ عَلَيْهِمْ ۗ إِنَّمَا نَعُدُّ لَهُمْ عَدًّا ﴿٨٤﴾

وَإِنْ مِنْكُمْ إِلَّا وَارِدُهَا كَانَ عَلَى رَبِّكَ حَتْمًا مَقْضِيًّا ﴿٧١﴾ ثُمَّ نُنَجِّي الَّذِينَ اتَّقَوْا وَنَذَرُ الظَّالِمِينَ فِيهَا جِثًا ﴿٧٢﴾

71. Wala hapana yeyote katika nyinyi ila ni mwenye kuifikia. Hiyo ni hukumu ya Mola wako Mlezi ambayo lazima itimizwe.

72. Kisha Tutawaokoa wale waliomchamungu; na Tutawaacha madhalimu humo wamepiga magoti.

Kila mmoja Ataletwa motoni, kisha Wataokolewa Waadilifu (Wachamungu)

Amepokea Ibn Jariir رحمه الله تعالى kutoka kwa 'Abdallah juu ya Kauli Yake:

وَإِنْ مِنْكُمْ إِلَّا وَارِدُهَا

"Wala hapana yeyote katika nyinyi ila ni mwenye kuifikia."

Akasema: "Ni daraja juu ya Moto mfano wa upande wa makali ya upanga. Kikundi cha kwanza kitapita kama radi. Kikundi cha pili kitapita hapo kama upepo. Kikundi cha tatu kitapita kama farasi anayekwenda mbio sana. Kikundi cha nne kitapita kama ng'ombe mwenye kwenda mbio sana. Kisha, wengine

wote watapita katika daraja hiyo ilhali Malaika watakuwa wanasema, 'Ee Allah تعالى, waokoe wao.'<sup>1</sup>".

Hadithi hii inatiliwa nguvu kwa ushahidi wa Hadithi nyingine iliyomo katika Sahihi mbili na wengineo kwa riwaya ya Anas, Abi Sa'id, Abi Hurayrah, Jaabir na wengineo miongoni mwa Maswahaba رضي الله عنهم.

Na amepokea tena Ahmad kutoka kwa Umm Mubashir رضي الله عنها, mke wa Zayd bin Haarithah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alikuwa katika nyumba ya Hafswah رضي الله عنها akasema:

«لَا يَدْخُلُ النَّارَ أَحَدٌ شَهِدَ بَدْرًا وَالْحُدَيْبِيَّةَ»

*"Hataingia Motoni yeyote aliyehudhuria Vita vya Badr na Hudaibiyah (miongoni mwa Waislamu)."*

Kisha, Hafswah رضي الله عنها akasema: "Je, si Allah تعالى Amesema:

«وَأِنْ مِّنكُمْ إِلَّا وَارِدُهَا»

*"Wala hapana yeyote katika nyinyi ila ni mwenye kuifikia".*

Mtume ﷺ akasema:

«ثُمَّ نُنَجِّي الَّذِينَ اتَّقَوْا»

*"Kisha Tutawaokoa wale waliomchamungu..."<sup>2</sup>*

Na katika Sahihi mbili kutoka kwa Hadithi ya Zuhriy, kutoka kwa Sa'id kuwa Abuu Hurayrah رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema:

«لَا يَمُوتُ لِأَحَدٍ مِنَ الْمُسْلِمِينَ ثَلَاثَةٌ مِنَ الْوَلَدِ تَمَسُّهُ النَّارُ إِلَّا تَجَلَّتْ الْقَسَمِ»

*"Hakuna yeyote atakayeguswa na Moto miongoni mwa Waislamu aliye na watoto watatu, waliokufa wote, isipokuwa kwa kiapo anachotakiwa kukitimiza."<sup>3</sup>*

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:232.

<sup>2</sup> Ahmad 6: 362. Hadithi hii pia imenukuliwa na Muslim (namba 2496) ikiwa na tofauti kidogo katika riwaya.

<sup>3</sup> Fat'h Al-Baariy 3: 142 na Muslim 4:2028.

Na 'Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam amesema kuhusu Kauli Yake:

وَإِنْ مِّنكُمْ إِلَّا وَارِدُهَا

**“Wala hapana yeyote katika nyinyi ila ni mwenye kuifikia.”**

Akasema: “Kupita kwa Waislamu (juu ya Moto) kunamaanisha kupita juu ya daraja iliyopo juu yake (Moto). Na kupita kwa washirikina juu ya Moto kunamaanisha kuingizwa ndani yake.” Amepokea Asuddiy kutoka kwa Murrah kuwa Ibn Mas’ud رضي الله عنه amesema yafuatayo kuhusu Kauli Yake:

كَانَ عَلَىٰ رَبِّكَ حَتْمًا مَّقْضِيًّا ﴿٧١﴾

**“Hiyo ni hukumu ya Mola wako Mlezi ambayo lazima itimizwe.”**

Maana: Kiapo kinachohitajika kutimizwa (wajibu)<sup>1</sup>. Na amesema Mujaahid: “Hatman ina maana kudura”<sup>2</sup>. Na hivyo ndivyo alivyosema Ibn Jurayj.<sup>3</sup> Na Kauli Yake:

ثُمَّ تُنَجِّي الَّذِينَ اتَّقَوْا

**“Kisha Tutawaokoa wale waliomchamungu...”**

Maana: Wanapopita viumbe vyote juu ya Moto, na makafiri na walioasi wakawa wanaanguka mmoja baada ya mwingine kwa ajili ya maasia yao, Allah تعالى Atawaokoa Waumini na wachamungu kutoka kwayo kwa sababu ya amali zao. Kwa hiyo, kupita kwao juu ya daraja na kasi yao itategemea amali zao walizofanya hapa duniani. Kisha, Waumini waliofanya madhambi makubwa wataombewa. Malaika, Manabii na Waumini wote wataruhusiwa kuwaombea watu, hivyo kufanya kundi kubwa kutolewa Motoni baada ya kuliwa na Moto kwa sehemu kubwa ya miili yao, ila sehemu ya kusujudu kwenye nyuso zao. Kutolewa kwao Motoni kutakuwa ni kwa ajili ya Imani nyoyoni mwao. Wa kwanza kutolewa atakuwa ni yule mwenye Imani yenye wizani ndogo ya dinari moyoni mwake. Kisha, ni yule aliye baada yake katika Imani. Kisha, ni yule aliye chini yake katika Imani, na kadhalika. Hii itaendelea mpaka yule mwenye wizani ndogo sana ya Imani katika moyo wake, chenye wizani wa atomu. Kisha Allah تعالى Atamtoa Motoni kila aliyesema, “Laa ilaaha illa Llaahu”, hata kama

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:237.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:237.

<sup>3</sup> Atw-Twabariy 18:237.

kwa siku moja ya maisha yake yote, hata kama hakufanya amali yeyote. Baada ya hapa, hakuna atakayebaki Motoni, ila wale waliowajibika kubaki Motoni milele. Hii imenukuliwa katika Hadithi Sahihi nyingi za Mtume ﷺ. Hii ndio sababu ya Allah تعالیٰ Kusema:

ثُمَّ نُنجِي الَّذِينَ اتَّقَوْا وَنُذِرُ الظَّالِمِينَ فِيهَا جِثًّا ﴿٧١﴾

***“Kisha Tutawaokoa wale waliomchamungu; na Tutawaacha madhalimu humo, Jithiyya (wamepiga magoti).”<sup>1</sup>***

وَإِذَا تَتَلَىٰ عَلَيْهِمْ ءَايَاتُنَا بَيِّنَاتٍ قَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلَّذِينَ ءَامَنُوا أَيُّ الْفَرِيقَيْنِ خَيْرٌ مَّقَامًا

وَأَحْسَنُ نَدِيًّا ﴿٧٢﴾ وَكَمْ أَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِّن قَرْنٍ هُمْ أَحْسَنُ أَثْنًا وَرِءْيَا ﴿٧٣﴾

***73. Na wanaposomewa Ayah Zetu zilizo wazi, waliokufuru huwaambia walioamini: Lipi katika makundi mawili lenye makao mema na mazuri na lilio Nadiyyan bora?***

***74. Na kaumu ngapi Tuliziangamiza zilizo kuwa na mapambo mazuri zaidi na wazuri zaidi kwa kuwatazama!***

### **Makafiri Wanajivuna kwa Hadhi yao Nzuri hapa Duniani**

Allah تعالیٰ Anatufahamisha kuwa pindi makafiri wanaposomewa Aya za Allah تعالیٰ zilizo na dalili dhahiri na hoja za wazi kabisa, wanazikataa na kukengeuka. Wanasema yafuatayo kuhusu Waumini, huku wakijifakhiri kwao na kutoa hoja kwa usahihi wa waliyo nayo kwa dini yao ya batili kuwa wao,

خَيْرٌ مَّقَامًا وَأَحْسَنُ نَدِيًّا ﴿٧٢﴾

***“Lipi katika makundi mawili lenye makao mema na mazuri na lilio Nadiyyan bora?”***

Maana: Majumba mazuri na bora, yaliyonyanyuliwa ghorofa na mabaraza bora. Hivyo, hii ina maana kuwa vyumba vya kukutana vimejaa watu wengi waliokuja kuhudhuria. Katika hili walikuwa wakisema, “Tutakuwa vipi katika uongo na batili ilhali sisi tuko katika hali hii ya ufanisi katika maisha yetu?” Watu hawa kwa hakika walikuwa ni wale waliojificha katika nyumba ya Al-Arqam bin Abi

<sup>1</sup> Fat’h Al-Baariy 13:48.

Al-Arqam na mfano wake katika nyumba nyingine. Hii ni kama Kauli ya Allah تعالى:

وَقَالَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِلَّذِينَ آمَنُوا لَوْ كَانَ خَيْرًا مَا سَبَقُونَا إِلَيْهِ

**“Na waliokufuru waliwaambia Waislamu: Lau ingalikuwa Dini hii ni ya kheri, hao (madhaifu na masikini) wasingetutangulia katika hilo.” (46:11).**

Na wamesema kaumu ya Nuuh عليه السلام:

أَتُؤْمِنُ لَكَ وَاتَّبَعَكَ الْأَرْذَالُونَ ﴿١١١﴾

**“Wakasema: Je, tukuamini wewe, hali ya kuwa wanyonge ndio wanaokufuata.” (26:111).**

Na Amesema Aliyetukuka:

وَكَذَلِكَ فَتَنَّا بَعْضَهُم بِبَعْضٍ لِيَقُولُوا أَهْتُوا لَنَا مِنْ بَيْنِنَا أَلَيْسَ اللَّهُ

بِأَعْلَمَ بِالشَّاكِرِينَ ﴿٥٣﴾

**“Na namna hii Tumewafanyia mtihani baadhi yao kwa baadhi yao wengine ili waseme: Je hao ndio Allah Amewafanyia ihsani miongoni mwetu pasina kutufanyia sisi? Basi Allah Akasema: Je, Allah Hawajui wanaomshukuru?” (6:53).**

Na kwa ajili hiyo Allah تعالى Akawajibu kwa kuondoa shaka, dhana na ufahamu wao mbaya kwa kusema:

وَكَمْ أَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِنْ قَرْنٍ

**“Na kaumu ngapi Tuliziangamiza kabla yao.”**

Maana: Ni Ummah na vizazi vingapi kwa ajili ya kukadhibisha kwao Tuliviangamiza kwa ukafiri wao.

هُم أَحْسَنُ أُمَّتِنَا وَرِءْيَا ﴿٧٦﴾

**“Zilizokuwa na mapambo mazuri zaidi na wazuri zaidi kwa kuwatazama!”**

Maana yake: Walikuwa ni bora kuliko hao watu wa sasa kwa mali, miliki walizokuwa nazo, hali na umbile. Amepokea A'mash kutoka kwa Abu Dhibyaan kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema yafuatayo kuhusu Aya hii:

حَيْرٌ مَّقَامًا وَأَحْسَنُ نَدِيًّا ﴿٧٢﴾

**“Makao mema na mazuri na lilio Nadiyyan bora.”**

Amesema: ‘*Al-Maqaam* ina maana ya nyumba na *An-Nadiyy* ina maana ya mahali pa kukutana (baraza), *Ath-Thaath* ina maana miliki ya mada na umbile lao la nje ni vile walivyo na wanavyoonekana kimwili”<sup>1</sup>. Na amepokea al-‘Awfiy kuwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما amesema: “*Al-Maqaam* ni maskani, *An-Nadiyy* ni mahali pa kukutana (baraza), na baraka na furaha kwa waliokuwa ndani yake”. Nayo ni kama Anavyosema Allah تعالى kwa kaumu ya Firauni pale walipoangamizwa na kuelezwa kisa cha hali yao katika Qur’ani:

كَمْ تَرَكُوا مِنْ جَنَّاتٍ وَعُيُونٍ ﴿٢٥﴾ وَزُرُوعٍ وَمَقَامٍ كَرِيمٍ ﴿٢٦﴾

**“Bustani ngapi na chemchemi ngapi waliziacha baada ya kugharikishwa. Na mimea na mahali pazuri!” (44:25-26)**

Hivyo, *Al-Maqaam* ina maana ya maskani na neema na *An-Nadiyy* ina maana ya mahali pa kukusanyika na kukutana ambapo walikuwa wakikusanyika hapo. Na Amesema Aliyetukuka katika Kuelezea kisa kwa Mtume ﷺ kwa yaliyotokea kwa kaumu ya Lutwi عليه السلام:

وَتَاتُونَ فِي نَادِيكُمْ الْمُنْكَرَ ۗ

**“Na mnafanya maovu katika mikusanyiko yenu?” (29:29).**

Na Waarabu wanaiita sehemu ya mkusanyiko kuwa ni *Naadiy*.<sup>2</sup>

قُلْ مَنْ كَانَ فِي الضَّلَالَةِ فَلْيَمْدُدْ لَهُ الرَّحْمَنُ مَدًّا ۗ حَتَّىٰ إِذَا رَأَوْا مَا يُوعَدُونَ إِمَّا الْعَذَابَ

وَإِمَّا السَّاعَةَ فَسَيَعْلَمُونَ ۗ مَنْ هُوَ شَرٌّ مَكَانًا وَأَضْعَفُ جُنْدًا ﴿٧٥﴾

**75. Sema: Walio katika upotofu basi Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema Atawapururia muda mpaka wayaone waliyoonywa – ama**

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:239, 241.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:239.

***ni adhabu au ni Saa. Hapo ndipo watapojua ni nani mwenye makao mabaya na mwenye askari dhaifu.***

### **Muovu Anapatiwa Muda lakini Hajasahuliwa**

Anasema Aliyetukuka:

قُلْ

**“Sema”.** Ewe Muhammad ﷺ, kwa hawa wanaomshirikisha Mola wao Mlezi, ilhali wanadai kuwa wanafuata haki, na nyinyi mko katika batili.

مَنْ كَانَ فِي الضَّلَالَةِ

**“Walio katika upotofu”.** Maana yake: Kati yetu na nyinyi.

فَلْيَمْدُدْ لَهُ الرَّحْمَنُ مَدًّا

**“Basi Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema Atawapupuria muda”.**

Maana: Ar-Rahman Atawapatia muda kwa aliyoko ndani yake mpaka atakapo kutana na Mola wake Mlezi na wakati Aliomchagulia utakapofika.

حَتَّىٰ إِذَا رَأَوْا مَا يُوعَدُونَ إِمَّا الْعَذَابَ

**“Mpaka wayaone waliyoonywa – ama ni adhabu”.** Itakayomfikia.

وَأِمَّا السَّاعَةَ

**“Au ni Saa”.** Itakayokuja kwa ghafula.

فَسَيَعْلَمُونَ

**“Hapo ndipo watapojua”.** Wakati huo.

مَنْ هُوَ شَرٌّ مَّكَانًا وَأَضْعَفُ جُنْدًا

**“Ni nani mwenye makao mabaya na mwenye askari dhaifu”.**

Huku ni kukanusha hoja yao kuhusu maskani zao nzuri na mabaraza yao ya kukusanyika. Hii ni changamoto dhidi ya washirikina wanaodai kuwa wanafuata uongofu kwa wanayofanya. Hii ni sawa na changamoto Aliyoitaja Allah تعالى kuhusu Mayahudi pale Aliposema:



قُلْ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ هَادُوا إِن زَعَمْتُمْ أَنَّكُمْ أَوْلِيَاءُ لِلَّهِ مِن دُونِ النَّاسِ فَتَمَنَّوْا الْمَوْتَ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٦٦﴾

**“Sema: Enyi Mayahudi! Kama mnadai ya kuwa nyinyi ni wapenzi wa Allah pasipokuwa watu wengine, basi yatamanini mauti, ikiwa mnasema kweli.” (62:6)**

Maana yake: Ombeni mauti yawajjie, wale wenye kufuata batili miongoni mwenu ikiwa kweli mnadai mko juu ya haki, dua haitawadhuru. Lakini walikataa kufanya hivyo. Mazungumzo ya kina kuhusu hilo tayari tushayaelezea katika Suratul Baqarah, na kwa Allah تعالى Ndiye Mwenye Kustahiki sifa zote njema. Kama vile Alivyotaja Allah تعالى changamoto waliyopewa Wakristo katika Suratul 'Imraan, waliposhikilia ukafiri wao na kuendelea katika utwaghuti. Walikataa kuacha dai lao la kuchupa mipaka kuwa 'Isa alikuwa mtoto wa Allah تعالى. Hivyo, Allah تعالى Anataja Hoja Zake na Dalili dhidi ya kumuabudu Isa عليه السلام na kuwa yeye alikuwa ni kiumbe kama Adam عليه السلام. Akasema Allah تعالى baada ya hapo:

فَمَنْ حَاجَّكَ فِيهِ مِن بَعْدِ مَا جَاءَكَ مِنَ الْعِلْمِ فَقُلْ تَعَالَوْا نَدْعُ أَبْنَاءَنَا وَأَبْنَاءَكُمْ وَنِسَاءَنَا وَنِسَاءَكُمْ وَأَنْفُسَنَا وَأَنْفُسَكُمْ ثُمَّ نَبْتَهِلْ فَنَجْعَل لَّعْنَتَ اللَّهِ عَلَى الْكٰذِبِينَ ﴿٦٧﴾

**“Watakaokuhoji sasa katika haya baada ya kukufikia elimu, waambie: Njooi tuwaite watoto wetu na watoto wenu; na wanawake wetu na wanawake wenu, na sisi na nyinyi; kisha tuombe kwa unyenyekevu tutake laana ya Allah iwashukie waongo.” (3:61).**

Hata hivyo, wao (Wakristo) walirudi nyuma kutoka kwa changamoto hii.

وَيَزِيدُ اللَّهُ الَّذِينَ الَّذِينَ أَهْتَدُوا هُدًى ۖ وَالْبَاقِيَتُ الصَّٰلِحَتُ حٰخِرٌ عِنْدَ رَبِّكَ ثَوَابًا وَحٰخِرٌ مَّرَدًّا ﴿٦٨﴾

**76. Na Allah Huwazidishia uwongofu wenye kushika uwongofu. Na mema yenye kudumu ni bora katika malipo mbele ya Mola wako Mlezi na yana mwisho mwema.”**

## Kuongozeka Uongofu kwa Walioongoka na Wale Walioongozwa

Baada ya Allah تعالى Kutaja kuongezeka kwa wakati na muda wa ziada uliokubaliwa kwa waliopotea na Kuwazidishia upotevu. Aliwafahamisha kuzidi kwa wale walioongoka. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَإِذَا مَا أَنْزَلَتْ سُورَةً فَمِنْهُمْ مَنْ يَقُولُ أَيُّكُمْ زَادَتْهُ هَذِهِ إِيمَانًا

**“Na inapoteremshwa Surah (mpya ya Qur’ani) wako miongoni mwao (wanafiki) wasemao: Ni nani miongoni mwenu ambaye Imani imezidi.” (9:124).** Na Aya inayofuata inaonesha hilo.

وَالْبَقِيَّةُ الْصَّالِحَاتُ

**“Na mema yenye kudumu”.** Tayari tumeifasiri katika Suratul Kahf iliyotangulia, pamoja na maelezo ya kina kuhusiana nayo na kutaja Hadithi zinazohusiana na maudhui hiyo.

خَيْرٌ عِنْدَ رَبِّكَ ثَوَابًا

**“Ni bora katika malipo mbele ya Mola wako Mlezi”**, Maana yake: Malipo na thawabu.

وَخَيْرٌ مَرَدًا

**“Na yana mwisho mwema.”** Maana yake: Hatima na mwisho kwa mtendaji.

أَفْرَأَيْتَ الَّذِي كَفَرَ بِآيَاتِنَا وَقَالَ لَأُوتِيَنَّ مَالًا وَوَلَدًا ﴿٧٦﴾ أَطَّلَعَ الْغَيْبَ أَمِ اتَّخَذَ

عِنْدَ الرَّحْمَنِ عَهْدًا ﴿٧٧﴾ كَلَّا ۚ سَنَكْتُبُ مَا يَقُولُ وَنَمُدُّ لَهُ مِنَ الْعَذَابِ مَدًّا ﴿٧٨﴾

وَنُرِثُهُ مَا يَقُولُ وَيَأْتِينَا فَرْدًا ﴿٧٩﴾

**77. Je, umemuona aliyelikana Ishara Zetu na akasema: Kwa hakika mimi nitapewa mali na wana!**

**78. Kwani yeye amepata khabari za ghaibu, au amechukua ahadi kwa Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema?**

**79. Hasha! Tutaandika Anayoyasema, Tutamkunjulia muda wa adhabu.**

**80. Na Tutamrithi hayo Anayoyasema, na Atatufikia mtupu peke yake!**

## Kuwarudi Wasioamini Wale Wanaodai Watapewa huko Akhera Mali na Watoto

Amepokea Imaam Ahmad kuwa Khabbaab bin Al-Aratt رضي الله عنه amesema: “Nilikuwa mfua chuma, nami nilikuwa namdai Al-‘Asw bin Waa’il. Hivyo nilikwenda kwake siku moja kuchukua deni langu kutoka kwake. Akaniambia, ‘Naapa kwa Allah تعالى, sitakulipa deni lako mpaka umkanushe Muhammad’. Nilimjibu: ‘Hapana, Naapa kwa Allah تعالى, sitamkufuru wala kumkanusha Muhammad mpaka ufe na ufufuliwe tena’. Kisha akaniambia, ‘Hakika, nikifa kisha nikafufuliwa, nawe ukaja kwangu, pia nitakuwa na mali nyinyi pamoja na watoto na wakati huo nitakulipa’. Allah تعالى Akateremsha:

﴿٧١﴾ أَفْرَأَيْتَ الَّذِي كَفَرَ بِآيَاتِنَا وَقَالَ لَأُوتِينَ مَالًا وَّوَلَدًا

***‘Je, umemuona aliyelikana Ishara Zetu na akasema: Kwa hakika mimi nitapewa mali na wana.’*** Hadi Kauli ya Allah تعالى,

﴿٧٢﴾ وَيَأْتِينَا فَرْدًا

***“Na Atatufikia mtupu peke yake.”***

Hii imepokewa na wanazuoni wawili wa Hadithi katika Sahihi zao mbili na wengineo. Na katika lafudhi ya Bukhaariy: “Nilikuwa mfua chuma katika mji wa Makkah, nikamtengenezea upanga Al-Asw bin Waa’il. Hivyo, nilikwenda kwake kuchukua pesa (kwa kazi yangu hiyo)”. Kisha akataja kipande kilichobaki cha Hadithi, akasema:

﴿٧٣﴾ أَمْ أَرْحَمُ عَبْدًا عِنْدَ الرَّحْمَنِ عَهْدًا

***“Au amechukua Ahadi kwa Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema?”***

Akasema: “Makubaliano”<sup>2</sup>. Na Kauli Yake:

﴿٧٤﴾ أَطَّلَعَ الْغَيْبَ

***“Kwani yeye amepata khabari za ghaibu.”*** Hii ni kumkataa mtu anayesema,

﴿٧٥﴾ لَأُوتِينَ مَالًا وَّوَلَدًا

***“Kwa hakika mimi nitapewa mali na wana.”***

<sup>1</sup> Ahmad 5:111.

<sup>2</sup> Fat’h Al-Baariy 4:372 na Muslim 4:2153.

Maana yake: Siku ya Kiyama. Kwa maneno mengine, “Je, anajua atakayopata Akhera, kwa kiasi ambacho anaweza kulia kiapo?”

أَمِ اتَّخَذَ عِنْدَ الرَّحْمَنِ عَهْدًا ﴿٧١﴾

**“Au amechukua ahadi kwa Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema?”**

Au amepata ahadi kutoka kwa Allah تعالى kuwa atapatiwa vitu hivi? Tayari tumetangulia kuitaja Hadithi iliyonukuliwa na Al-Bukhaariy kuwa maana yake ni makubaliano<sup>1</sup>. Na Kauli Yake:

كَلَّا

**“Hasha (Sivyo hivyo)!”** Hili ni neno linalokanusha kauli ya nyuma na papohapo kutilia mkazo kwa kinachofuatia.

سَنَكْتُبُ مَا يَقُولُ

**“Tutaandika Anayoyasema.”** Kwa anachotaka, na ile rai yake kuwa amejitoa kwa aliyo na matumaini kwayo, na kumkanusha kwake Allah تعالى, Aliye Mkubwa na Mtukufu. Na Kauli Yake:

وَنَمُدُّ لَهُ مِنَ الْعَذَابِ مَدًّا ﴿٧٢﴾

**“Tutamkunjulia muda wa adhabu.”** Maana yake: Katika nyumba ya Akhera, kwa ile kauli yake hiyo na kumkanusha kwake Allah تعالى hapa duniani.

وَنَرْتُدُّهُ مَا يَقُولُ

**“Na Tutamrithi hayo Anayoyasema.”**

Maana yake: Kwa mali na watoto. Tutachukua vyote hivyo kutoka kwake, kinyume cha madai yake kuwa atazidishiwa katika mali na watoto huko Akhera kuliko alivyokuwa navyo hapa duniani.

Kinyume na hivyo, ina maana Akhera vitachukuliwa alivyokuwa navyo hapa duniani. Kwa ajili hiyo, Akasema Allah تعالى:

وَيَأْتِينَا فَرْدًا ﴿٧٣﴾

**“Na Atatufikia mtupu peke yake!”** Maana yake: Bila ya mali wala wana.

<sup>1</sup> Fat’h ul-Baariy 4:372.

وَأَتَّخِذُوا مِن دُونِ اللَّهِ إِلَهَةً لِّيَكُونُوا لَهُمْ عِزًّا ۖ كَلَّا سَيَكْفُرُونَ بِبِعَادِهِمْ وَيَكُونُونَ عَلَيْهِمْ ضِدًّا ۖ أَلَمْ تَرَ أَنَا أَرْسَلْنَا الشَّيَاطِينَ عَلَى الْكَافِرِينَ تَوْزِعُهُمْ آزًّا ۖ فَلَا تَعَجَلْ عَلَيْهِمْ ۗ إِنَّمَا نَعُدُّ لَهُمْ عَدًّا ۖ

**81. Na wamechukua miungu mingine badala ya Allah ili ati iwape nguvu.**

**82. Sivyoy kabisa! Wataikataa hiyo Ibadah yao, na watakuwa ndio dhidi yao.**

**83. Kwani huoni ya kwamba Tumewatuma mashetani kwa makafiri wawachochee kwa uchochezi?**

**84. Basi usiwafanyie haraka. Sisi Tunawahisabia idadi ya siku zao.**

### Miungu ya Washirikina Itakataa Ibadah zao

Allah تعالی Anatupasha habari juu ya makafiri washirikina kwa Mola wao Mlezi, kuwa wamechukua miungu badala ya Allah تعالی, ili miungu hawa wawe ni chimbuko la, "Nguvu". Wanadhani kuwa miungu hawa wanawapa nguvu na kuwapa ushindi. Kisha, Akatupasha khabari kuwa suala hilo sio kama wanavyodai, na wala haitakuwa kama wanavyotamani. Akasema:

كَلَّا سَيَكْفُرُونَ بِبِعَادِهِمْ

**"Sivyo kabisa! Wataikataa hiyo Ibadah yao."** Maana yake: Siku ya Kiyama.

وَيَكُونُونَ عَلَيْهِمْ ضِدًّا ۖ

**"Na watakuwa ndio dhidi yao."** Maana: Watakuwa maadui kinyume na wanavyodhania kuhusu miungu hiyo. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَمَنْ أَضَلُّ مِمَّن يَدْعُوا مِن دُونِ اللَّهِ مَن لَّا يَسْتَجِيبُ لَهُ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَهُمْ عَن

دُعَائِهِمْ غَافِلُونَ ۖ وَإِذَا حُيِّرَ النَّاسُ كَانُوا لَهُمْ أَعْدَاءً وَكَانُوا بِبِعَادِهِمْ كَافِرِينَ ۖ

**"Na wapotofu wakubwa ni nani kuliko wale wanaowaomba asiyekuwa Allah ambao hawatawajibu mpaka Siku ya Kiyama, na**

***hawatambui dua zao. Na ambao watakapokusanywa watu watakuwa maadui zao, na wataikataa Ibadah yao.” (46:5-6).***

Na Assuddi amesema;

كَلَّا سَيَكْفُرُونَ بِعِبَادَتِهِمْ

***“Sivyo kabisa! Wataikataa hiyo Ibadah yao.”***

Maana yake: kwa kuabudu masanamu<sup>1</sup>. Na Kauli Yake:

وَيَكُونُونَ عَلَيْهِمْ ضِدًّا

***“Na watakuwa ndio dhidi yao.”***

Kinyume na matumaini yao kutoka kwa miungu hii (yao). Na amesema As-Suddiy:

وَيَكُونُونَ عَلَيْهِمْ ضِدًّا

***“Na watakuwa ndio dhidi yao.”***

Maana yake: Watakuwa mahasimu, wakiwa na utesi mkali sana. Na amesema Adh-Dhahaak:

وَيَكُونُونَ عَلَيْهِمْ ضِدًّا

***“Na watakuwa ndio dhidi yao.”*** Maana yake: Maadui<sup>2</sup>.

### **Uchochezi wa Mashetani kwa Makafiri**

Na Kauli Yake:

أَلَمْ تَرَ أَنَا أَرْسَلْنَا الشَّيَاطِينَ عَلَى الْكَافِرِينَ تَوَضَّعُوا لَهُمْ أَرَأَيْتُمْ

***“Kwani huoni ya kwamba Tumewatuma mashetani kwa makafiri wawachochee kwa uchochezi?”***

Amepokea Aliy bin Abi Twalhah kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Watawapoteza wao kwa kuwashawishi na kuwadanganya”<sup>3</sup>. Na amepokea

<sup>1</sup> At-Tabari 18:251.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:250.

<sup>3</sup> At-Tabari 18:251.

al-Awfiy kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kuwa amesema: "Watawachochea wao dhidi ya Muhammad na Maswahaba wake"<sup>1</sup>. Na amesema Qatadah: "Watawabughudhi na kuwasumbua mpaka wamuasi Allah تعالى."<sup>2</sup> Na amesema Abdur-Rahman bin Zayd: "Hii ni kama Kauli Yake Aliyetukuka:

وَمَنْ يَعِشْ عَنْ ذِكْرِ الرَّحْمَنِ نُقِضَ لَهُ شَيْطَانًا فَهُوَ لَهُ قَرِينٌ ﴿٦٦﴾

**'Anayeyafanyia upofu maneno ya Mwingi wa Rehema Tunamuwekea Shetani kuwa rafiki yake, kuwa mwenziwe.'** (43:36).<sup>3</sup>

Na Kauli Yake:

فَلَا تَعْجَلْ عَلَيْهِمْ <sup>ط</sup> إِنَّمَا نَعُدُّ لَهُمْ عَدًّا ﴿٦٧﴾

**"Basi usiwafanyie haraka. Sisi Tunawahisabia idadi ya siku zao."**

Maana yake: Usiwe na haraka katika kuwafikia adhabu, ewe Muhammad juu yao.

إِنَّمَا نَعُدُّ لَهُمْ عَدًّا ﴿٦٨﴾

**"Sisi Tunawahisabia idadi ya siku zao."**

Maana yake: Hakika Tunawacheleweshea kwa muda maalumu waliowekewa. Wamekadiriwa juu ya hilo, na hawana njia ya kukimbia Adhabu ya Allah تعالى na Kutesa Kwake. Allah تعالى Anasema:

وَلَا تَحْسَبَنَّ اللَّهَ غَفْلًا عَمَّا يَعْمَلُ الظَّالِمُونَ ﴿٦٩﴾

**"Wala usidhani Allah Ameghafilika na haya wanayoyafanya madhalimu."** (14:42).

Na Amesema:

فَمَهْلِكِ الْكَافِرِينَ آمَهُلَّهُمْ زُرُودًا ﴿٧٠﴾

**"Basi wape makafiri muda – wape muda kidogo."** (86:17).

<sup>1</sup> Ad-Durr Al-Manthur 5:538.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:252.

<sup>3</sup> Atw-Twabariy 18:252.

Na Amesema:

إِنَّمَا نُمَلِّئُهُمْ لِيُزَادُوا إِتْمَاعًا

**“Hakika Tunawapa muda na wanazidi madhambi.” (3:178).**

تُمَتِّعُهُمْ قَلِيلًا ثُمَّ نَضْطَرُّهُمْ إِلَىٰ عَذَابٍ غَلِيظٍ ﴿٣١﴾

**“Tunawastarehesha kidogo, kisha Tutawasukuma katika adhabu ngumu.” (31:24).**

قُلْ تَمَتَّعُوا فَإِنَّ مَصِيرَكُمْ إِلَىٰ النَّارِ ﴿١٤﴾

**“Sema: Jifurahisheni kidogo tu, kisha marejeo yenu ni katika Moto.” (14:30).**

Na amesema as-Suddiy:

إِنَّمَا نَعُدُّ لَهُمْ عَدًّا ﴿٢٠﴾

**“Sisi Tunawahisabia idadi ya siku zao.”**

Maana yake: Miaka, miezi, siku na masaa.

\* \* \*



يَوْمَ نَحْشُرُ الْمُتَّقِينَ إِلَى الرَّحْمَنِ وَفَدًا ﴿٨٥﴾ وَنَسُوقُ  
 الْمُجْرِمِينَ إِلَىٰ جَهَنَّمَ وَرَدًا ﴿٨٦﴾ لَا يَمْلِكُونَ الشَّفْعَةَ إِلَّا  
 مَنِ اتَّخَذَ عِنْدَ الرَّحْمَنِ عَهْدًا ﴿٨٧﴾ وَقَالُوا اتَّخَذَ الرَّحْمَنُ  
 وَلَدًا ﴿٨٨﴾ لَقَدْ جِئْتُمْ شَيْئًا إِدًّا ﴿٨٩﴾ تَكَادُ السَّمَوَاتُ  
 يَتَفَطَّرْنَ مِنْهُ وَتَنْشَقُّ الْأَرْضُ وَتَخِرُّ الْجِبَالُ هَدًّا ﴿٩٠﴾ أَنْ  
 دَعَوْا لِلرَّحْمَنِ وَلَدًا ﴿٩١﴾ وَمَا يَنْبَغِي لِلرَّحْمَنِ أَنْ يَتَّخِذَ وَلَدًا  
 ﴿٩٢﴾ إِنْ كُلُّ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ إِلَّا آتِي  
 الرَّحْمَنِ عَبْدًا ﴿٩٣﴾ لَقَدْ أَحْصَاهُمْ وَعَدَّهُمْ عَدًّا ﴿٩٤﴾  
 وَكُلُّهُمْ آتِيهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَرْدًا ﴿٩٥﴾ إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا  
 وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ سَيَجْعَلُ لَهُمُ الرَّحْمَنُ وُدًّا ﴿٩٦﴾ فَإِنَّمَا  
 يَسْرَنَّهُ بِلِسانِكَ لِتُبَشِّرَ بِهِ الْمُتَّقِينَ وَتُنذِرَ بِهِ قَوْمًا  
 لُدًّا ﴿٩٧﴾ وَكَمْ أَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِنْ قَوْمٍ هَلْ نَحْسُبُ مِنْهُمْ مِّنْ  
 أَحَدٍ أَوْ تَسْمَعُ لَهُمْ رِكْرًا ﴿٩٨﴾

يَوْمَ نَحْشُرُ الْمُتَّقِينَ إِلَى الرَّحْمَنِ وَفَدًا  
 وَنَسُوقُ الْمُجْرِمِينَ إِلَىٰ جَهَنَّمَ  
 وَرَدًا ﴿٨٦﴾ لَا يَمْلِكُونَ الشَّفْعَةَ إِلَّا  
 مَنِ اتَّخَذَ عِنْدَ الرَّحْمَنِ عَهْدًا ﴿٨٧﴾

**85. Siku Tutayowakusanya wachamungu kuwapeleka kwa Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema kuwa ni wageni Wake.**

**86. Na Tukawachunga wakhalifu kuwapeleka Jahanamu hali ya kuwa wana kiu.**

**87. Hawatakuwa na mamlaka ya uombezi ila wale waliochukua ahadi kwa Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema.**

### Hali ya Wachamungu na Hali ya Wahalifu Siku ya Kufufuliwa

Allah تعالى Anatupa khabari kuhusu marafiki Zake wachamungu ambao walimuogopa hapa duniani, wakafuata Mitume wake na wakaamini waliokuja nayo Mitume. Waliwatii kwa waliyoamuru na kujitenga kwa waliyokataza. Allah تعالى Anatueleza kuwa Atawakusanya watu hawa Siku ya Kiyama kama wajumbe waliokuja Kwake. *Wafd* ni kikundi cha watu waliofika wakiwa juu ya kipando. Neno hilo limepatikana kutokana na neno *Wufuud* (kufika). Watakuja wakiwa wamepanda farasi bora wa nuru kutoka kwa vipando vya Akhera. Watafika mbele ya Mbora, Mwenye Kuwapokea wajumbe katika nyumba Yake

ya heshima na radhi. Ama kuhusu wahalifu, waliowakadhibisha Mitume na kwenda kinyume nao, watapelekwa kwa nguvu Motoni. Anasema Aliyetukuka:

وَرَدًا

**“Kuwa wana kiu.”**

Maana yake: Wamekauka na wakihitajia kinywaji kwa ajili ya kiu. Amesema hayo ‘Atwaa’, Ibn ‘Abbaas, Mujaahid, Al-Hasan, Qataadah na wengine wengi.<sup>1</sup> Na hapa patasemwa:

أَيُّ الْفَرِيقَيْنِ خَيْرٌ مَّقَامًا وَأَحْسَنُ نَدِيًّا

**“Lipi katika makundi mawili lenye makao mema na mazuri na lilio Nadiyyan bora?” (19:73).**

Na imepokewa kwa Ibni Abii Haatim kutoka kwa ‘Amr bin Qays Malaa’i aliye ripoti kutoka kwa Ibn Marzuuq aliyesema:

يَوْمَ نَحْشُرُ الْمُتَّقِينَ إِلَى الرَّحْمَنِ وَفَدًا

**“Siku Tutakayowakusanya wachamungu kuwapeleka kwa ar-Rahman, Mwingi wa Rehema kuwa ni wageni Wake.”**

Pindi Muumini atakapotoka kaburini, atakutana na sura nzuri ambayo hajawahi kuiona na itakuwa na harufu nzuri sana. Atasema, ‘Wewe ni nani?’ Atajibu, ‘Je, hunijui wala hunitambui mimi?’ Muumini atasema, ‘Hapana, lakini Allah تعالی Amekufanya uwe na harufu nzuri na uso wako mzuri’. Huyu atasema, ‘Mimi ni amali yako njema. Hivi ndivyo ulivyokuwa duniani ukifanya amali njema nzuri. Nilikupanda katika maisha yako yote ya duniani, hivyo nipande mimi leo.’ Muumini atakipanda kiumbe hicho. Hii ndio maana ya Kauli Yake:

يَوْمَ نَحْشُرُ الْمُتَّقِينَ إِلَى الرَّحْمَنِ وَفَدًا

**‘Siku Tutayowakusanya wachamungu kuwapeleka kwa Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema kuwa ni wageni Wake.’**

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:253 na Durr Al-Manthuur 5:541.

Na amepokea 'Aliy bin Abi Twalhah kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema yafuatayo kuhusu Aya hii:

يَوْمَ نَحْشُرُ الْمُتَّقِينَ إِلَى الرَّحْمَنِ وَفَدًا ﴿٨٥﴾

**“Siku Tutayowakusanya wachamungu kuwapeleka kwa Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema kuwa ni wageni Wake.”**

Kwa kipando.<sup>1</sup> Na Kauli ya Allah تعالى،

وَنُسُوقُ الْمُجْرِمِينَ إِلَىٰ جَهَنَّمَ وَرِدًا ﴿٨٦﴾

**“Na Tukawachunga wakhalifu kuwapeleka Jahanamu hali ya kuwa wana kiu.”**

Maana yake: Wanahitajia kinywaji kwa ajili ya kiu kikali.

لَا يَمْلِكُونَ الشَّفْعَةَ

**“Hawatakuwa na mamlaka ya uombezi.”**

Hakuna atakayekuwa na uwezo wa kuwaombea kama Waumini watakaombeana. Allah تعالى Anasema kuwa:

فَمَا لَنَا مِن شَافِعِينَ ﴿١٠٠﴾ وَلَا صَدِيقٍ حَمِيمٍ ﴿١٠١﴾

**“Basi hatuna waombezi. Wala rafiki khalisi.” (26:100-101).**

Na Kauli Yake:

إِلَّا مَن آتَّخَذَ عِندَ الرَّحْمَنِ عَهْدًا ﴿٨٧﴾

**“Ila wale waliochukua ahadi kwa ar-Rahman, Mwingi wa Rehema.”**

Huku ni kutolewa katika hukumu iliyopita. Maana:, Wale waliochukua ahadi kutoka kwa Ar-Rahman. Ahadi hii ni kule kushuhudia kuwa hakuna anayepasa kuabudiwa ila Allah تعالى، na kutekeleza haki Zake. Amesema 'Aliy bin Abi Twalhah kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema:

إِلَّا مَن آتَّخَذَ عِندَ الرَّحْمَنِ عَهْدًا ﴿٨٧﴾

**“Ila wale waliochukua ahadi kwa Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema.”**

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 8:380.

Ahadi. Nayo ni kushuhudia kuwa hakuna anayepasa kuabudiwa kwa haki ila Allah تعالى, na kukubali kuwa hila na nguvu zote Anastahiki Allah تعالى, na asiwe na matumaini ila kwa Allah تعالى tu.”<sup>1</sup>

وَقَالُوا اتَّخَذَ الرَّحْمَنُ وَلَدًا ﴿١٨﴾ لَقَدْ جِئْتُمْ شَيْئًا إِدًّا ﴿١٩﴾ تَكَادُ السَّمَوَاتُ يَتَفَطَّرْنَ مِنْهُ وَتَنْشَقُّ الْأَرْضُ وَتَخِرُّ الْجِبَالُ هَدًّا ﴿٢٠﴾ أَنْ دَعَوْا لِلرَّحْمَنِ وَلَدًا ﴿٢١﴾ وَمَا يَنْبَغِي لِلرَّحْمَنِ أَنْ يَتَّخِذَ وَلَدًا ﴿٢٢﴾ إِنْ كُلُّ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ إِلَّا آتِي الرَّحْمَنِ عَبْدًا ﴿٢٣﴾ لَقَدْ أَحْصَيْنَاهُمْ وَعَدَّهُمْ عَدًّا ﴿٢٤﴾ وَكُلُّهُمْ آتِيهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَرْدًا ﴿٢٥﴾

**88. Na wao ati husema kuwa Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema ana mwana!**

**89. Hakika mumeleta jambo la kuchusha mno!**

**90. Zinakaribia mbingu kutatuka kwa hilo, na ardhi kupasuka, na milima kumegeka vipande vipande.**

**91. Kwa kudai kwao kuwa Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema ana mwana.**

**92. Wala hahitajii Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema kuwa na mwana.**

**93. Hapana yeyote aliomo mbinguni na ardhini ila atafika kwa Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema kuwa ni mtumwa Wake.**

**94. Yeye hakika Amewadhibiti na Amewahisabu sawa sawa.**

**95. Na kila mmoja katika wao Atamfikia Siku ya Kiyama peke yake.**

**Kukataliwa Kabisa Kumnasibishia Allah تعالى kuwa ana mtoto**

Allah تعالى Alipokariri katika Sura hii Tukufu kuwa 'Isa عليه السلام ni mja mwenye kumuabudu Allah تعالى na Kutaja kuzaliwa kwake kutoka kwa Maryam bila ya baba, Alianza Kukanusha na Kukataa yale madai ya kuwa Ana mwana. Ametukuka na Ametakasika na sifa hizo, Naye Ametakabari kukubwa. Akasema:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:257.

وَقَالُوا اتَّخَذَ الرَّحْمَنُ وَلَدًا ۗ لَقَدْ جِئْتُمْ

**“Na wao ati husema kuwa Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema ana mwana! Hakika mmeleta.”**

Maana: Katika kauli yenu hii,

شَيْئًا إِذَا

**“Jambo la kuchusha mno!”**

Ibn ‘Abbaas, Mujaahid, Qataadah na Maalik رضي الله عنهم wamesema: Maana: Jambo kubwa. Na neno: *Idda*, hutamkwa kwa *Hamzah* kuwa na irabu ya *kasrah* (*Idda*), au *Fathah* (*Adda*) na pamoja na kuwa na *Madd* (*Adda*), ni lugha na matamko aina tatu neno ambalo ni mashuhuri ni la kwanza. Na Kauli Yake:

تَكَادُ السَّمَوَاتُ يَتَفَطَّرْنَ مِنْهُ وَتَنْشَقُّ الْأَرْضُ وَتَخِرُّ الْجِبَالُ هَدًّا ۗ أَنْ دَعَوْا لِلرَّحْمَنِ

وَلَدًا ۗ

**“Zinakaribia mbingu kutatuka kwa hilo, na ardhi kupasuka, na milima kuanguka vipande vipande. Kwa kudai kwao kuwa ar-Rahman, Mwingi wa Rehema ana mwana.”**

Maana yake: Kwa kumtukuza Mola Mlezi kwa kiasi kikubwa, Mbingu na ardhi zinakaribia kuwa hivyo, kwa kusikia maneno haya maovu kutoka kwa mwanadamu. Sababu mbingu na ardhi ni viumbe vya Allah تعالى na vimeanzishwa katika Tawhidi Yake na ile hakika kuwa hakuna mungu anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Yeye. Hana washirika, wala wenzi walio sawa Naye, wala mwana, wala rafiki, wala aliye sawa Naye. Bali Yeye ni Mmoja, Anayefaa Kukusudiwa (na viumbe Vyake vyote kwa kumuabudu na kumtegemea). Amepokea Ibn Jariir رحمه الله تعالى kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema haya kwa Kauli Yake Aliyetukuka:

تَكَادُ السَّمَوَاتُ يَتَفَطَّرْنَ مِنْهُ وَتَنْشَقُّ الْأَرْضُ وَتَخِرُّ الْجِبَالُ هَدًّا ۗ أَنْ دَعَوْا لِلرَّحْمَنِ

وَلَدًا ۗ

**“Zinakaribia mbingu kutatuka kwa hilo, na ardhi kupasuka, na milima kuanguka vipande vipande. Kwa kudai kwao kuwa ar-Rahman, Mwingi wa Rehema ana mwana.”**

Hakika mbingu, ardhi, majabali na viumbe vyote – ila kwa wanadamu na majini – vinatishika kushirikishwa kwa Allah تعالى. Na vinakaribia kuondoka na kutokuwepo kwa kushirikishwa kwa ule Utukufu na Ukubwa wa Allah تعالى. Na kama vile mshirikina hafaidiki kwa amali zake njema kwa sababu ya kumshirikisha Allah تعالى, tunatumai kuwa Allah تعالى Atatusamehe madhambi ya wale wanaoamini na kumpwekesha kwa kumuabudu Yeye Peke Yake. Mtume ﷺ amesema:

«لَقُمُوا مَوْتَكُمْ شَهَادَةً أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، فَمَنْ قَالَهَا عِنْدَ مَوْتِهِ وَجَبَتْ لَهُ الْجَنَّةُ»

*“Wahimizeni wenye kukata roho miongoni mwenu washuhudie kuwa hapana anayepasa kuabudiwa ila Allah, kwani yeyote mwenye kusema (maneno hayo) wakati wa kukata roho, amewajibika kuingia Peponi”.*

Watu wakasema: “Ewe Mtume wa Allah! Je, itakuwaje kwa mwenye kusema akiwa na afya yake?” Akasema:

«تِلْكَ أَوْجِبُ وَأَوْجِبُ»

*“Huyo amewajibika kuingia Peponi kwa kiwango kikubwa zaidi”.*

Kisha akasema:

«وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ لَوْ جِئَءَ بِالسَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِينَ، وَمَا فِيهِنَّ وَمَا بَيْنَهُنَّ وَمَا تَحْتَهُنَّ، فَوَضَعْنِي فِي كِفَّةِ الْمِيزَانِ، وَوَضِعْتَ شَهَادَةً أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ فِي الْكِفَّةِ الْأُخْرَى لَرَجَحْتُ بِهِنَّ»

*“Naapa kwa Yule Ambaye nafsi yangu iko Mkononi Mwake, lau mbingu, ardhi, zilizomo ndani yake na baina na chini yake, zitaletwa na kutiwa kwenye mizani na shahada ya Laa ilaaha illa Llaahu kuwekwa upande mwingine wa mizani, shahada itakuwa nzito zaidi”*

Hivi ndivyo alivyonukuu Ibn Jariir رحمه الله تعالى<sup>1</sup>, na inatiliwa nguvu na Hadithi ya kisa cha Kadi<sup>2</sup>. Na Allah تعالى Anajua zaidi.

Na amesema Adh-Dhwahaak:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:258.

<sup>2</sup> Tuhfat Al-Ahwadhyy 7:395. Na Ahmad 213 na Albani amesema ni sahihi.

تَكَادُ السَّمَوَاتُ يَتَفَطَّرْنَ مِنْهُ

**“Zinakaribia mbingu kutatuka kwa hilo.”**

Maana yake: Itapasuka vipande vipande kwa hofu ya Utukufu wa Allah تعالی. Na amesema ‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam:

وَتَنَشِقُّ الْأَرْضُ

**“Na ardhi kupasuka”,**

Maana: Kwa ajili ya ghadhabu kwa niaba ya Allah تعالی,

وَتَخْرُ الْجِبَالُ هَدًّا ﴿٤٦﴾

**“Na milima kuanguka vipande vipande.”**

Amesema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما: “Kupasuka pasuka”. Na akasema Said bin Jubayr: “Haddan” Maana yake: “Litavunjika vipande vipande mtawalia.”

Na amepokea Imaam Ahmad kutoka kwa Abi Musa رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«لَا أَحَدٌ أَضْبِرُ عَلَى أَدَى سَمِعَهُ مِنَ اللَّهِ إِنَّهُ يُشْرِكُ بِهِ وَيُجْعَلُ لَهُ وَلَدًا، وَهُوَ يُعَافِيهِمْ وَيَذْفَعُ عَنْهُمْ وَيَرْزُقُهُمْ»

*“Hakuna aliye na subira zaidi kuliko Allah kuhusu adha Anayosikia. Hakika Anashirikishwa na kujaaliwa kuwa na mtoto, ilhali Yeye Ndiye Mwenye Kuwapatia afya nzuri, Anawalinda na Kuwaruzuku”<sup>1</sup>.*

Hadithi hii pia imepokewa katika Sahihi mbili. Na katika lafudhi nyingine:

«إِنَّهُمْ يَجْعَلُونَ لَهُ وَلَدًا وَهُوَ يَرْزُقُهُمْ وَيُعَافِيهِمْ»

*“Hakika wao wanamjaalia kuwa ana mtoto, ilhali Yeye Ndiye Anaye waruzuku na Kuwapatia afya nzuri.”<sup>2</sup>*

Na Kauli Yake:

وَمَا يُلْبِغِي لِلرَّحْمَنِ أَنْ يَتَّخِذَ وَلَدًا ﴿٤٧﴾

**“Wala hahitajii Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema kuwa na mwana.”**

<sup>1</sup> Ahmad 4:405.

<sup>2</sup> Fat’h Al-Baariy 10:527 na Muslim 4:2160.

Maana: Haisihi wala haifai Kwake kwa Utukufu na Ukubwa Wake. Hakuna anayefanana Naye katika viumbe Vyake, kwani viumbe vyote ni waja Wake.

Na kwa hiyo Akasema:

إِنْ كُلُّ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ إِلَّا آتَى الرَّحْمَنِ عَبْدًا ﴿٨٥﴾ لَقَدْ أَحْصَاهُمْ  
وَعَدَّهُمْ عَدًّا ﴿٨٦﴾

***“Hapana yeyote aliomo mbinguni na ardhini ila atafika kwa ar-Rahman, Mwingi wa Rehema kuwa ni mtumwa Wake. Yeye hakika Amewadhibiti na Amewahisabu sawa sawa.”***

Maana yake: Anajua idadi yao kuanzia wakati Alipowaumba mpaka Siku ya Kiyama, wanaume na wanawake, watoto miongoni mwao na wakubwa.

وَكُلُّهُمْ آتِيهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَرْدًا ﴿٨٧﴾

***“Na kila mmoja katika wao Atamfikia Siku ya Kiyama peke yake.”***

Maana yake: Hatakuwa na msaidizi wala wa kumuokoa ila Allah تعالى Peke Yake asiyekuwa na mshirika. Atawahukumu viumbe Vyake kama Anavyotaka, Naye ni Muadilifu wala Hadhulumu hata wizani wa atomu, wala Hamdhulumu yeyote.

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ سَيَجْعَلُ لَهُمُ الرَّحْمَنُ وُدًّا ﴿٨٨﴾ فَإِنَّمَا يَسْرُنَهُ  
بِلِسَانِكَ لِنُبَشِّرَ بِهِ الْمُتَّقِينَ وَتُنذِرَ بِهِ قَوْمًا لُدًّا ﴿٨٩﴾ وَكَمْ أَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِّن قَرْنٍ  
هَلْ نُحِيسُ مِنْهُمْ مِّنْ أَحَدٍ أَوْ تَسْمَعُ لَهُمْ رِكْرًا ﴿٩٠﴾

**96. Hakika walioamini na wakatenda mema Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema Atawajaalia mapenzi.**

**97. Na hakika Tumeifanya nyepesi kwa ulimi wako, ili uwabashirie kwayo wachamungu, na uwaonye kwayo watu wabishi.**

**98. Na kaumu ngapi Tumezihiliki kabla yao. Je! Unawaona hata mmoja katika wao au unasikia hata mchakato wao?**



## Allah تعالى Anajaalia Mapenzi ya Watu Wema Nyoyoni

Allah تعالى Anatupasha habari ya kuwa Yeye Ndiye Anayestawisha kwa waja Wake Waumini ambao wanafanya mema, amali ambazo zinamridhisha Allah تعالى kwa kuwa zinakwenda sambamba na Sheria aliyokuja nayo Muhammad ﷺ – hivyo kupanda mapenzi kwao nyoyoni mwa waja Wake wema. Na hili ni jambo lililo muhimu sana na hakuna kulikwepa.

Na hakika imepokewa kuhusu hilo Hadithi Sahihi kutoka kwa Mtume ﷺ katika njia tofauti. Amepokea Imaam Ahmad kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ اللَّهَ إِذَا أَحَبَّ عَبْدًا دَعَا جِبْرِيْلَ، فَقَالَ: يَا جِبْرِيْلُ، إِنِّي أُحِبُّ فُلَانًا فَأَجِبْهُ قَالَ: فَيَجِبُهُ جِبْرِيْلُ، قَالَ: ثُمَّ يُنَادِي فِي أَهْلِ السَّمَاءِ: إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ فُلَانًا فَأَجِيبُوهُ، قَالَ: فَيَجِبُهُ أَهْلُ السَّمَاءِ، ثُمَّ يُوَضَّعُ لَهُ الْقَبُولُ فِي الْأَرْضِ، وَإِنَّ اللَّهَ إِذَا أَبْغَضَ عَبْدًا دَعَا جِبْرِيْلَ فَقَالَ: يَا جِبْرِيْلُ إِنِّي أَبْغِضُ فُلَانًا فَأَبْغِضْهُ، قَالَ: فَيَبْغِضُهُ جِبْرِيْلُ، ثُمَّ يُنَادِي فِي أَهْلِ السَّمَاءِ: إِنَّ اللَّهَ يَبْغِضُ فُلَانًا فَأَبْغِضُوهُ، قَالَ: فَيَبْغِضُهُ أَهْلُ السَّمَاءِ، ثُمَّ يُوَضَّعُ لَهُ الْبُغْضَاءُ فِي الْأَرْضِ»

*“Hakika Allah Anapompenda mja Wake, Anamuita Jibril, na Kumuambia: ‘Ewe Jibril! Hakika Mimi nampenda Fulani, hivyo nawe mpende’. Hivyo, Jibril anampenda. Akasema: Kisha, ataita (Jibril) kwa wakaazi wa mbinguni: ‘Hakika Allah Anampenda Fulani, kwa hivyo mpendeni’. Akasema: ‘Wakaazi wa mbinguni wataanza kumpenda. Kisha atatiliwa kabuli katika ardhi.’ Na hakika pindi Allah Anapomchukia mja Wake, Humuita Jibril na Kumuambia: ‘Ewe Jibril! Hakika Mimi Namchukia Fulani, hivyo mchukie’. Akasema: Jibril anamchukia, kisha naye atawatangazia wakaazi wa mbinguni: ‘Hakika Allah Anamchukia Fulani, nanyi mchukieni’. Akasema: Hivyo wakaazi wa mbinguni watamchukia. Kisha inawekwa juu yake chuki katika ardhi.”<sup>1</sup>*

Na imepokewa mfano wake katika Al-Bukhaariy na Muslim<sup>2</sup>.

<sup>1</sup> Ahmad 2:413 na 514.

<sup>2</sup> Fat’h Al-Baariy 1:476 na Muslim 4:2030.

Amepokea Ibn Abi Haatim kutoka kwa Abi Hurayrah عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِذَا أَحَبَّ اللَّهُ عَبْدًا نَادَى جِبْرِيلَ: إِنِّي قَدْ أَحْبَبْتُ فَلَانًا فَأَجِبْهُ، فَيُنَادِي فِي السَّمَاءِ، ثُمَّ يُنَزِّلُ لَهُ الْمَحَبَّةَ فِي أَهْلِ الْأَرْضِ، فَذَلِكَ قَوْلُ اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ: ﴿إِنَّ الْأَبْرَارَ مَشَٰوِرًا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ سَيَجْعَلُ لَهُمُ الرَّحْمَنُ وُدًّا﴾»

*“Pindi Allah Anapompenda mja Wake yeyote, Anamuita Jibril: ‘Hakika Mimi nampenda Fulani, hivyo nawe mpende’. Kisha, ataita (Jibril) mbinguni na mapenzi atateremshiwa kwa watu ardhini. Na hiyo ni Kauli ya Allah تعالى: “Hakika walioamini na wakatenda mema Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema Atawajaalia mapenzi.”<sup>1</sup>*

Imepokewa na Muslim na At-Tirmidhiy, na akasema At-Tirmidhiy: Hadithi Hasan Sahih<sup>2</sup>.

### Qur’ani Imeteremka Kutoa Bishara Njema na Kuonya

Na Kauli Yake:

فَإِنَّمَا يَسَّرْنَاهُ

*“Na hakika Tumeifanya nyepesi.”*

Maana yake: Qur’ani.

بِلِسَانِكَ

*“Kwa ulimi wako.”*

Maana: Ewe Muhammad ﷺ, nayo ni lugha ya Kiarabu safi, fasaha na kamili.

لِنُبَشِّرَ بِهِ الْمُتَّقِينَ

*“Ili uwabashirie kwayo wachamungu.”*

Maana yake: Wenye kumuitikia Allah تعالى na kumsadiki Mtume Wake.

وَتُنذِرَ بِهِ قَوْمًا لُدًّا

*“Na uwaonye kwayo watu wabishi.”*

Maana yake: Waliopotoka juu ya haki, wakiegemea katika batili na uwongo.

<sup>1</sup> Abdur-Razzaq 10:450.

<sup>2</sup> Muslim 4:1031 na Tuhfatul al-Ahwadhiy 8:608.

Na Kauli Yake:

وَكَمْ أَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِّن قَرْنٍ

**“Na kaumu ngapi Tumezihiliki kabla yao”,**

Maana yake: Miongoni mwa Ummah zilizokufuru Ishara za Allah تعالى na kuwakadhibisha Mitume.

هَلْ تُحِسُّ مِنْ أَحَدٍ أَوْ تَسْمَعُ لَهُمْ رِكْرًا

**“Je! Unawaona hata mmoja katika wao au unasikia hata mchakato wao?”**

Maana yake: Je, unamuona yeyote miongoni mwao au hata kusikia mnong’ono kutoka kwao. Na amesema Ibn ‘Abbaas, Abul ‘Aliyah, ‘Ikrimah, Hasan Baswriy, Sa’id bin Jubayr, Adh-Dhwahhaak na Ibn Zayd: “Hiyo ina maana ya sauti yoyote ile”<sup>1</sup>. Na amesema Hasan na Qataadah: “Je, waona kwa jicho lako au kusikia sauti?”<sup>2</sup> Na *Ar-Riqz*, katika asili ya lugha ya Kiarabu ni sauti ndogo sana.

Huu ndio mwisho wa Tafsiri ya Sura Maryam. Sifa zote njema na Shukrani Anastahiki Allah تعالى. Inayofuatia ni Tafsiri Sura Twaha Insha’Allah.’

\* \* \*

<sup>1</sup> At-Tabari 18:265.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:265.



## Tafsiri ya Suratu Twaha

### Sura ya 20

#### Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ طه  
سورة طه

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

طه ﴿١﴾ مَا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْقُرْآنَ لِتَشْقَى ﴿٢﴾ إِلَّا

تَذْكَرَةً لِمَنْ يَخْشَى ﴿٣﴾ تَنْزِيلًا مِمَّنْ خَلَقَ الْأَرْضَ

وَالسَّمَوَاتِ الْعُلَى ﴿٤﴾ الرَّحْمَنُ عَلَى الْعَرْشِ اسْتَوَى ﴿٥﴾

لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا وَمَا تَحْتَ

الترى ﴿٦﴾ وَإِنْ تَجَهَّرَ بِالْقَوْلِ فَإِنَّهُ يَعْلَمُ الْبَيْرَ وَأَخْفَى ﴿٧﴾

اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ لَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَى ﴿٨﴾ وَهَلْ أُنْتَك

حَدِيثُ مُوسَى ﴿٩﴾ إِذْ رَأَى نَارًا فَقَالَ لِأَهْلِهِ امْكُثُوا إِنِّي

ءَانَسْتُ نَارًا لَعَلِّي آتِيكُمْ مِنْهَا بِقَبَسٍ أَوْ أَجْدُ عَلَى النَّارِ

هُدًى ﴿١٠﴾ فَلَمَّا أَتَاهَا نُودِيَ يَمْوَسَى ﴿١١﴾ إِنِّي أَنَا رَبُّكَ

فَاخْلَعْ نَعْلَيْكَ ۗ إِنَّكَ بِالْوَادِ الْمُقَدَّسِ طُوًى ﴿١٢﴾ وَأَنَا

أَخْتَرْتُكَ فَاسْتَمِعْ لِمَا يُوحَى ﴿١٣﴾ إِنَّنِي أَنَا اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا

أَنَا فَاعْبُدْنِي وَأَقِمِ الصَّلَاةَ لِذِكْرِي ﴿١٤﴾ إِنَّ السَّاعَةَ

ءَاتِيَةٌ أَكَادُ أُخْفِيهَا لِشِجْرَى كُلِّ نَفْسٍ بِمَا تَسْعَى ﴿١٥﴾ فَلَا

يَصُدُّكَ عَنْهَا مَنْ لَا يُؤْمِنُ بِهَا وَاتَّبَعَ هَوْلَهُ فتردى ﴿١٦﴾

طه ﴿١﴾ مَا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْقُرْآنَ

لِتَشْقَى ﴿٢﴾ إِلَّا تَذْكَرَةً لِمَنْ

يَخْشَى ﴿٣﴾ تَنْزِيلًا مِمَّنْ خَلَقَ

الْأَرْضَ وَالسَّمَوَاتِ الْعُلَى ﴿٤﴾

الرَّحْمَنُ عَلَى الْعَرْشِ اسْتَوَى ﴿٥﴾

لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ

وَمَا بَيْنَهُمَا وَمَا تَحْتَ التَّرَى ﴿٦﴾

وَإِنْ تَجَهَّرَ بِالْقَوْلِ فَإِنَّهُ يَعْلَمُ الْبَيْرَ

وَأَخْفَى ﴿٧﴾ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۗ لَهُ

الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَى ﴿٨﴾

1. Twaha!

2. Hatukukuteremshia Qur'ani ili upate mashaka.

3. Bali ni mawaidha kwa wenye kunyenyekea.

4. Materemsho yatokayo kwa Aliyeumba ardhi na mbingu zilizo juu.

5. *Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema, Aliyekaa juu ya Kiti cha Enzi.*

6. *Ni Vyake vyote viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi, na viliomo baina yao, na viliomo chini ya ardhi.*

7. *Na ukinyanyua sauti kwa kusema, basi hakika Yeye Anajua siri na duni kuliko siri.*

8. *Allah! Hapana mola isipokuwa Yeye. Yeye Ana Majina mazuri kabisa.*

**Qur'ani ni Ukumbusho na Uteremsho kutoka kwa Allah تعالى**

Tumetangulia kueleza kuhusu herufi zilizoachana mwanzo wa Suratul Baqarah, hivyo hakuna haja ya kurudia maelezo hayo hapa. Na Kauli Yake:

مَا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْقُرْآنَ لِتَشْقَىٰ ﴿١٠٠﴾

***“Hatukukuteremshia Qur’ani ili upate mashaka”.***

Amepokea Juwaybir kuwa Adhw-Dhwahaak amesema: “Pindi Allaah تعالى Alipo mteremshia Mtume Wake Qur’ani, yeye na Maswahaba wake walishikamana nayo. Hapo washirikina wa Quraysh wakasema ‘Haikuteremshwa hii Qur’ani kwa Muhammad ila kupata mashaka’.

Allah تعالى Akateremsha:

طه ﴿١٠١﴾ مَا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْقُرْآنَ لِتَشْقَىٰ ﴿١٠٢﴾ إِلَّا تَذَكُّرَةً لِّمَن يَخْشَىٰ ﴿١٠٣﴾

***‘Twaha! Hatukukuteremshia Qur’ani ili upate mashaka. Bali ni mawaidha kwa wenye kunyenyekea’<sup>1</sup>.***

Jambo hili si kama walivyodai waongo. Bali, yeyote anayepatiwa elimu na Allah تعالى, hakika Ametakiwa (na Allah تعالى) kheri nyingi. Hii ni kama ilivyothibiti katika Sahihi mbili kutoka kwa Mu’aawiyah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

<sup>1</sup> Al-Qurtwubiy 11:167.

«مَنْ يُرِدِ اللَّهُ بِهِ خَيْرًا يُفَقِّهْهُ فِي الدِّينِ»

*“Anayetakiwa kheri na Allah Anampatia ufahamu wa Dini.”<sup>1</sup>*

Na amesema Mujaahid kuhusu Kauli Yake Aliyetukuka:

﴿ مَا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْقُرْآنَ لِتَشْقَى ﴾

*“Hatukukuteremshia Qur’ani ili upate mashaka.”*

Hiyo ni kama Kauli Yake:

﴿ فَأَقْرَأُوا مَا تيسَّرَ مِنْهُ ﴾

*“Kwa hivyo someni kilicho sahali humo.” (73:20)*

Watu walikuwa wakifunga kamba vifuani mwao (kujitungika wakiwa wamechoka) katika Sala<sup>2</sup>. Na amesema Qatadah:

﴿ مَا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْقُرْآنَ لِتَشْقَى ﴾

*“Hatukukuteremshia Qur’ani ili upate mashaka.”*

Hapana, Naapa kwa Allah تعالى, Hakuifanya Qur’an kuwa ni taabu na mashaka. Bali, Ameifanya kuwa rehema, nuru, uongofu na njia ya kumpeleka mtu Peponi<sup>3</sup>. Allah تعالى Anasema:

﴿ إِلَّا تَذَكَّرَ لِمَنْ يَخْشَى ﴾

*“Bali ni mawaidha kwa wenye kunyenyekea.”*

Hakika Allah تعالى Ameteremsha Kitabu Chake na Akamtuma Mtume Wake kama rehema kwa waja Wake, ili akumbuke mwenye kukumbuka na afaidike mtu kwa anayoyasikia kutoka katika Kitabu cha Allah تعالى, nao ni ukumbusho Aliouteremsha Allah تعالى, ndani yake, yapo ya halali na haramu. Na Kauli Yake:

﴿ تَنْزِيلًا مِمَّنْ خَلَقَ الْأَرْضَ وَالسَّمَوَاتِ الْعُلَى ﴾

*“Materemsho yatokayo kwa Aliyeumba ardhi na mbingu zilizo juu.”*

Maana yake: Hii Qur’ani, ulioletewa, ewe Muhammad ﷺ, ni uteremsho kutoka

<sup>1</sup> Fat’hi Al-Baariy 1:197 na Muslim 2:719).

<sup>2</sup> At-Tabari 18:269.

<sup>3</sup> At-Tabari 18:269.

kwa Mola wako Mlezi. Yeye ni Mola Mlezi wa kila kitu, Mfalme wao. Muweza kwa Anayoyataka. Yeye Ndiye Aliyeumba ardhi kwa vina vyake vidogo na sehemu zilizo banana. Yeye Ndiye Aliyeumba mbingu zilizo juu kwa kunyanyuka na kwa ustadi. Na Kauli Yake:

الرَّحْمَنُ عَلَى الْعَرْشِ اسْتَوَى ﴿١٠﴾

**“Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema, Aliyekaa juu ya Kiti cha Enzi.”**

Tumetangulia kuelezea kuhusu hilo katika Suratul A’raaf, hivyo hakuna haja ya kurudia tena hapa. Njia iliyo salama kabisa kutumiwa katika kuifahamu Aya hii, ni njia ya watangu wema (*salafu swalih*). Njia yao ilikuwa ni kukubali kile kilichonukuliwa kuhusiana nacho katika Kitabu na Sunnah bila kuelezea vipi (*min ghayri takyiyfin*), wala kupindisha maneno (*wala tahriyfin*), wala kukishabihisha (*wala tashbiyhin*), wala kukataa (*wala ta’twiylin*) na wala kufananisha na kiumbe chochote kile (*wala tamthiylin*). Na Kauli Yake:

لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا وَمَا تَحْتَ الثَّرَى ﴿١١﴾

**“Ni Vyake vyote viliomo mbinguni na viliomo katika ardhi, na viliomo baina yao, na viliomo chini ya ardhi.”**

Maana: Vyote vinamilikiwa na Yeye na vimo Mkononi Mwake. Vyote vimo chini ya Udhhibiti Wake, Kutaka Kwake, na Hukumu Yake. Ameumba vyote hivi, Anavimiliki, Naye Ndiye Mola Muabudiwa wa vyote hivyo. Hakuna Mola muabudiwa mbali na Yeye wala Mola Mlezi asiyekuwa Yeye. Na Kauli Yake:

وَمَا تَحْتَ الثَّرَى ﴿١٢﴾

**“Na viliomo chini ya ardhi”.**

Amesema Muhammad bin Ka’b: “Maana: Viliomo chini ya ardhi saba.”<sup>1</sup>

Na Kauli Yake:

وَإِنْ مَجْهَرٌ بِالْقَوْلِ فَإِنَّهُ يَعْلَمُ السِّرَّ وَأَخْفَى ﴿١٣﴾

**“Na ukinyanyua sauti kwa kusema, basi hakika Yeye Anajua siri na lililo zaidi kuliko siri.”**

Maana yake: Ameiteremsha Qur’ani hii, na pia Ameumba ardhi na mbingu zilizo juu, na Anajua siri na iliyofichakana kuliko siri. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

<sup>1</sup> At-Tabari 18:271.



قُلْ أَنْزَلَهُ الَّذِي يَعْلَمُ السِّرَّ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ إِنَّهُ كَانَ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٦﴾

**“Sema: Ameyateremsha haya Yule Ajuaye siri za mbinguni na ardhini; bila shaka Yeye ni Mwingi wa Msamaha na Mwingi wa Rehema.” (25:6)**

Amepokea ‘Aliy bin Abi Twalhah kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuhusu Aya hii:

يَعْلَمُ السِّرَّ وَأَخْفَى ﴿٧﴾

**“Yeye Anajua siri na duni kuliko siri.”**

Maana yake: Siri ni ile ambayo mwanadamu ameificha katika nafsi yake, na

وَأَخْفَى ﴿٧﴾

**“Na duni kuliko siri.”**

Ni ile amali ambayo mwanadamu ameificha kabla ya kuifanya. Allah تعالى Anajua yote hayo. Elimu Yake Yeye inakusanya kila kitu, kilichopita na kinachokuja katika mustakbali wake na yote ni elimu kamili.

Katika hili wanadamu wote ni kama roho moja Kwake. Hiyo ndio maana ya Kauli Yake:

مَا خَلَقْنَاكُمْ وَلَا بَعَثْنَاكُمْ إِلَّا كَنَفْسٍ وَاحِدَةٍ ﴿٢٨﴾

**“Hakukuwa Kuumbwa kwenu wala Kufufuliwa kwenu ila kama nafsi moja.” (31:28)<sup>1</sup>**

Na Kauli Yake:

اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ ۖ لَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ ﴿٨٠﴾

**“Allah! Hapana mola isipokuwa Yeye. Yeye Ana Majina mazuri kabisa.”**

Maana yake: Yeye Ndiye Aliyeteremsha Qur’ani kwako (ewe Muhammad ﷺ), Yeye ni Allah تعالى, hapana mungu ila Yeye. Yeye Ndiye Mmiliki wa Majina mazuri kabisa na Sifa zilizo njema na bora.

<sup>1</sup> At-Tabari 18:272.

وَهَلْ أَتَاكَ حَدِيثُ مُوسَى ﴿١٠﴾ إِذْ رَأَى نَارًا فَقَالَ لِأَهْلِهِ امْكُثُوا إِنِّي آنَسْتُ نَارًا لَّعَلِّي  
 آتِيكُمْ مِنْهَا بِقَبَسٍ أَوْ أَجْدٍ عَلَى النَّارِ هُدًى ﴿١١﴾

**9. Na je! Imekufikia hadithi ya Musa?**

**10. Alipouona moto, akawaambia watu wake: Ngojeni! Mimi nimeuona moto, huenda nikakuleteeni kijinga kutoka moto huo, au nikapata uongofu kwenye moto.**

**Majadiliano kuhusu Ujumbe wa Musa عليه السلام**

Kutoka hapa, Allah تعالى Anatutajia kisa cha Musa عليه السلام, na vipi alianza kuteremshiwa Wahyi na Allah تعالى Kuzungumza naye moja kwa moja. Hii ilitokea baada ya Musa عليه السلام kumaliza muda walioagana baina yake na baba mkwe kuwa atachunga kondoo. Alikuwa anasafiri na familia yake, na panasemwa kuwa alikuwa akielekea Misri, baada ya kuwa nje kwa muda wa zaidi ya miaka kumi (10). Alikuwa na mkewe, akapotea njiani wakati wa baridi, katika usiku wa majira ya baridi. Hivyo, alikaa chini na kupiga kambi katika njia ya baadhi ya milima iliyofunikwa na theluji, kunyesha mvua ya theluji, mawingu mazito, kiza na ukungu. Alijaribu kuwasha moto kwa vifaa vya kuwashia alivyokuwa navyo, ili atoe mwangaza, kama ilivyokuwa ada na desturi. Hata hivyo, haikuwasha chochote japo hata kutoa cheche. Alipokuwa katika hali hii, aliona moto pembezoni mwa mlima. Ilionekana kwake kuwa ni moto unaong'aa upande wa kulia wa mlima kutoka pale alipokuwa. Hapo akawapatia familia yake bishara njema:

إِنِّي آنَسْتُ نَارًا لَّعَلِّي آتِيكُمْ مِنْهَا بِقَبَسٍ

**“Mimi nimeuona moto, huenda nikakuleteeni kijinga kutoka huo moto.”**

Maana yake: Mwale wa moto. Na katika Aya nyingine:

أَوْ جَذْوَةٍ مِنَ النَّارِ

**“Au kijinga cha moto.” (28:29)**

Na hilo ni kaa lenye miale ya moto (linalowaka),

لَعَلَّكُمْ تَصْطَلُونَ ﴿١٦﴾

“*Ili muote.*” (28:29). Hii ni dalili ya kuonesha kuwa huo ulikuwa ni wakati wa baridi. Na Kauli Yake:

بِقَبْسٍ

“*Kijinga cha moto.*”

Hii ni dalili ya kuwepo kiza. Na Kauli Yake:

أَوْ أَجِدُ عَلَى النَّارِ هُدًى ﴿١٧﴾

“*Au nikapata uongofu kwenye moto.*”

Maana yake: Wa kuniongoza njia. Hii inaonesha kuwa alipotea kutoka katika njia ya sawa, kama alivyosema Ath-Thawriy رحمه الله تعالى kutoka kwa Abi Said Al-A'war kutoka kwa 'Ikrimah kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema kuhusu Aya hii:

أَوْ أَجِدُ عَلَى النَّارِ هُدًى ﴿١٧﴾

“*Au nikapata uongofu kwenye moto.*”

Atakayeniongoza njia ya sawa. Walikuwa wanasikia baridi na wamepotea njia. Pindi Musa عليه السلام alipouona moto alisema, ‘Ima nitamkuta atakayetuongoza njia ya sawa, au kwa uchache nitawaletea moto ambao mtaweza kuuwasha’<sup>1</sup>.

فَلَمَّا أَتَاهَا نُودِيَ يَمُوسَى ﴿١٨﴾ إِنِّي أَنَا رَبُّكَ فَاخْلَعْ نَعْلَيْكَ إِنَّكَ بِالْوَادِ الْمُقَدَّسِ طُوًى

﴿١٩﴾ وَأَنَا آخِزَتُكَ فَاسْتَمِعْ لِمَا يُوحَى ﴿٢٠﴾ إِنبَى أَنَا اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدْنِي وَأَقِمِ

الصَّلَاةَ لِذِكْرِي ﴿٢١﴾ إِنَّ السَّاعَةَ آتِيَةٌ أَكَادُ أُخْفِيهَا لِتُجْزَى كُلُّ نَفْسٍ بِمَا تَسْعَى ﴿٢٢﴾

فَلَا يَصُدُّكَ عَنْهَا مَنْ لَّا يُؤْمِنُ بِهَا وَاتَّبَعَ هَوَاهُ فَتَرْدَى ﴿٢٣﴾

**11. Basi alipoufikia akaitwa: Ewe Musa!**

**12. Hakika Mimi Ndiye Mola wako Mlezi! Basi vua viatu vyako. Kwani upo katika bonde takatifu la Tuwa.**

**13. Nami Nimekuteua wewe; basi sikiliza unayofunuliwa.**

<sup>1</sup> At-Tabari 18:277.

**14. Hakika Mimi Ndiye Allah. Hapana mungu ila Mimi tu. Basi Niabudu Mimi, na ushike Swala kwa ajili ya kunikumbuka Mimi.**

**15. Hakika Saa itakuja bila ya shaka. Nimekaribia kuificha, ili kila nafsi ilipwe kwa iliyoyafanya.**

**16. Kwa hivyo asikukengeushe nayo yule ambaye haiamini na akafuata pumbao lake ukaja kuhiliki.**

**Wahyi wa Kwanza kwa Musa عليه السلام**

Anasema Aliyetukuka:

فَلَمَّا أَتَتْهَا

**“Basi alipoufikia.”** Maana yake: Moto alipoukaribia.

نُودِيَ يَمُوسَى

**“Akaitwa: Ewe Musa!”** Na katika Aya nyingine:

نُودِيَ مِنْ سَنْطِي الْوَادِ الْأَيْمَنِ فِي الْبُقْعَةِ الْمُبْرَكَةِ مِنَ الشَّجَرَةِ أَنْ يَمُوسَى إِنْ  
أَنَا اللَّهُ

**“Aliitwa kutoka upande wa kuliani wa bonde hilo, katika kiwanja kilichobarikiwa, kutoka mtini, ‘Ewe Musa! Bila shaka Mimi Ndiye Allah.” (28:30)**

Na hapa Akasema:

إِنِّي أَنَا رَبُّكَ

**“Hakika Mimi Ndiye Mola wako Mlezi!”**

Maana yake: Yule Anayezungumza nawe na Kukuhutubia.

فَاخْلَعْ نَعْلَيْكَ

**“Basi vua viatu vyako.”** ‘Aliy bin Abi Twaalib, Abu Dharr, Abu Ayyub na Salaf wengine رضي الله عنهم wamesema: “Viatu vyake vilitengenezwa na ngozi ya punda aliyekuwa hakuchinjwa (kisheria)”. Pia panasemwa: ‘Aliamriwa tu kuvua viatu vyake ili kupaheshimu mahali hapo patakatifu.<sup>1</sup>

<sup>1</sup> At-Tabari 18:278.

Na Kauli Yake:

طُوًى

**“Tuwa”**. Amepokea ‘Aliy bin Abi Twalhah kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Hilo ni jina la bonde”<sup>1</sup>. Na wengine wamesema hivyo hivyo. Hii imetajwa tu kama ubainifu wa sehemu hiyo. Pia imesemwa kuwa hii ni tamathali ya usemi, ambayo ni Amri ya kuweka miguu yake chini. Na panasemwa: kuwa sehemu hiyo imetakaswa, na *Tuwa* ni kitu chenye baraka yenye kukariri. Hata hivyo, rai ya kwanza ndio iliyo sahihi zaidi. Hii ni kama Kauli Yake:

إِذْ نَادَاهُ رَبُّهُ بِالْوَادِ الْمُقَدَّسِ طُوًى

**“Mola wake Mlezi Alipomuita katika bonde Takatifu la Tuwa.” (79:16).**

Na Kauli Yake:

وَأَنَا آخَرَتُكَ

**“Nami Nimekuteua wewe”**. Hii ni kama Kauli Yake:

إِنِّي أَصْطَفَيْتُكَ عَلَى النَّاسِ بِرِسَالَتِي وَبِكَلِمِي

**“Mimi Nimekuchagua juu ya watu wote kwa ujumbe Wangu na kwa Kusema nawe Kwangu.” (7:144)**

Maana yake: Kwa watu wote wa wakati huo. Na panasemwa: “Hakika Allah تعالى Amesema: ‘Ewe Musa! Je, wajua kwa nini Nimekuchagua Kuzungumza nawe moja kwa moja kati ya watu wote?’ Musa عليه السلام alisema: “Hapana”. Hapo Allah تعالى Akamuambia: “Sababu ni kuwa sijamfanya yeyote kunyenyekea kama ulivyonyenyekea”. Na Kauli Yake:

فَاسْتَمِعْ لِمَا يُوحَى

**“Basi sikiliza unayofunuliwa.”** Maana yake: Sikiliza sasa Ninayokwambia na Kukuteremshia Wahyi.

إِنِّي أَنَا اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا

**“Hakika Mimi Ndiye Allah. Hapana mungu ila Mimi tu”**.

Huu ni wajibu wa kwanza kwa watu wote waliobaleghe kujua kuwa hapana mungu wa kuabudiwa kwa haki ila Allah تعالى tu, asiyekuwa na mshirika kabisa.

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:281.

Na Kauli Yake:

فَاعْبُدْنِي

**“Basi Niabudu Mimi.”**

Maana yake: Peke Yangu, na simamisha ‘Ibada Yangu bila ya kunishirikisha.

﴿وَأَقِمِ الصَّلَاةَ لِذِكْرِي﴾

**“Na ushike Sala kwa ajili ya kunikumbuka Mimi”.**

Pamesemwa: Maana yake ni Sala kwa ajili ya kunikumbuka Mimi. Na pamesemwa: Maana yake ni simamisha Sala kila unaponikumbuka. Na hii maana ya pili inashuhudiwa na Hadithi iliyonukuliwa na Imaam Ahmad kutoka kwa Anas رضي الله عنه Mtume ﷺ amesema:

«إِذَا رَفَدَ أَحَدُكُمْ عَنِ الصَّلَاةِ أَوْ غَفَلَ عَنْهَا، فَلْيُصَلِّهَا إِذَا ذَكَرَهَا، فَإِنَّ اللَّهَ تَعَالَى قَالَ: ﴿وَأَقِمِ الصَّلَاةَ لِذِكْرِي﴾»

*“Pindi mmoja wenu anapolala na kupitiliwa na Sala au akaghafilika nayo, aiswali pindi anapokumbuka. Hakika ni kuwa Allah Aliyetukuka Amesema: ‘Na ushike Sala kwa ajili ya kunikumbuka Mimi’”.*

Na imenukuliwa katika Sahihi mbili kutoka kwa Anas رضي الله عنه Mtume ﷺ amesema:

«مَنْ نَامَ عَنِ صَلَاةٍ أَوْ نَسِيَهَا فَكَفَّارَتُهَا أَنْ يُصَلِّيَهَا إِذَا ذَكَرَهَا، لَا كَفَّارَةَ لَهَا إِلَّا ذَلِكَ»

*“Yeyote anayelala mpaka Sala ikampita au akasahau, kafara yake ni kuiswali pindi anapokumbuka. Hakuna kafara nyingine ila hiyo.”<sup>2</sup>*

Na Kauli Yake:

إِنَّ السَّاعَةَ آتِيَةٌ

**“Hakika Saa itakuja bila ya shaka.”**

Maana yake: Kiama kitasimama na hakuna njia ya kukiepuka. Na kitafika hapana budi. Na Kauli Yake:

<sup>1</sup> Ahmad 3:84.

<sup>2</sup> Fat’h al-Baariy 2:84 na Muslim 1:477.

أَكَادُ أَحْفِيهَا

**“Nimekaribia kuificha”.**

Amepokea Adh-Dhahaak kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما alikuwa akiisoma hivi, “Nimekaribia kuificha na Nafsi Yangu”<sup>1</sup>. Alikuwa akisema: “Sababu ni kuwa hakuna kabisa kinachojificha kutoka kwa Nafsi Yake”<sup>2</sup>. Amepokea ‘Aliy bin Abi Twalhah kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema:

أَكَادُ أَحْفِيهَا

**“Nimekaribia kuificha.”**

Maana yake: Hakuna mwenye kujua wakati wake isipokuwa Mimi (Allah تعالى)<sup>3</sup>. Na Amesema:

ثُقُلْتُ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ لَا تَأْتِيكُمْ إِلَّا بَغْتَةً

**“...Ni nzito katika mbingu na ardhi. Haitakufikieni ila kwa ghafla...”**  
(7:187),

Maana yake: Elimu yake ni nzito sana kwa wakazi wa mbinguni na ardhini. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

لِتُجْزَى كُلُّ نَفْسٍ بِمَا تَسْعَى ﴿٧٠﴾

**“Ili kila nafsi ilipwe kwa iliyoyafanya.”**

Maana yake: Nitaisimamisha na hakuna njia ya kuiepuka. Bila shaka Nitamlipa kila mtu anayefanya, kulingana na anayofanya:

فَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ خَيْرًا يَرَهُ ﴿٧١﴾ وَمَنْ يَعْمَلْ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ شَرًّا يَرَهُ ﴿٧٢﴾

**“Basi anayefanya wema hata kiasi cha uzito wa atomu ataona jaza yake. Na anayefanya uovu hata kiasi cha uzito wa atomu ataona jaza yake.”** (99:7-8).

<sup>1</sup> Fat’h Al-Qadiir 3:361. Sanadi yake ina dosari, Adh-Dhahhak hakupokea kutoka kwa Ibn Abbasi.

<sup>2</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 5:563.

<sup>3</sup> At-Tabari 18:285.

Na pia:

إِنَّمَا تُجْزَوْنَ مَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿١٦﴾

***“Munalipwa mliyokuwa mukiyatenda.” (52:16)***

Na Kauli Yake:

فَلَا يَصُدُّكَ عَنْهَا مَنْ لَا يُؤْمِنُ بِهَا

***“Kwa hivyo asikukengeushe nayo yule ambaye haiamini.”***

Muradi wa wito hapa umeelekezwa kwa watu wote waliokalifishwa (wenye uwezo wa kuzingatia ujumbe). Hii ina maana, “Usifuate njia ya wenye kukanusha Kiyama, anayefuata matamanio yake tu katika maisha ya hapa duniani. Anamuasi Mola wake Mlezi na kufuata matamanio yake tu. Yeyote mwenye kuafikiana na hao basi amefeli na kupata hasara.”

فَتَرَدَّى ﴿١٧﴾

***“Ukaja hiliki.”***

Maana yake: Utahiliki na kuangamia. Amesema Allah تعالیٰ:

وَمَا يُغْنِي عَنْهُ مَالُهُ إِذَا تَرَدَّى ﴿١٧﴾

***“Na mali yake hayatamfaa atakapokuwa anadidimia.” (92:11)***

\* \* \*



وَمَا تِلْكَ بِبِمِينِكَ يَمْوَسَى ﴿١٧﴾ قَالَ هِيَ عَصَايَ  
 أَنْتَوَكَّؤُا عَلَيَّهَا وَأَهْمَشُ بِهَا عَلَى غَنَمِي وَلِيَ فِيهَا مَفَارِثُ  
 أُخْرَى ﴿١٨﴾ قَالَ أَلْقِهَا يَمْوَسَى ﴿١٩﴾ فَأَلْقَاهَا فَإِذَا هِيَ  
 حَيَّةٌ تَسْعَى ﴿٢٠﴾ قَالَ خُذْهَا وَلَا تَخَفْ ۗ سُنُعَيْدُهَا سِيرَتَهَا  
 الْأُولَى ﴿٢١﴾ وَأَضْمُمْ يَدَكَ إِلَى جَنَاحِكَ تَخْرُجْ بَيْضَاءَ مِنْ  
 غَيْرِ سُوءٍ ؕ آيَةٌ أُخْرَى ﴿٢٢﴾ لِئَرْيَا مِنْ ءَايَاتِنَا أَكْثَرَ جِزَى ﴿٢٣﴾  
 أَذْهَبَ إِلَى فِرْعَوْنَ إِنَّهُ طَغَى ﴿٢٤﴾ قَالَ رَبِّ اشْرَحْ لِي  
 صَدْرِي ﴿٢٥﴾ وَبَيِّرْ لِي أَمْرِي ﴿٢٦﴾ وَأَحْلِلْ عُقْدَةَ مِنْ  
 لِسَانِي ﴿٢٧﴾ يَفْقَهُوا قَوْلِي ﴿٢٨﴾ وَاجْعَلْ لِي وَزِيرًا مِنْ أَهْلِي  
 ﴿٢٩﴾ هَارُونَ أَخِي ﴿٣٠﴾ اشْدُدْ بِهِ أَزْرِي ﴿٣١﴾ وَأَشْرِكُهُ فِي  
 أَمْرِي ﴿٣٢﴾ كَيْ نُسَبِّحَكَ كَثِيرًا ﴿٣٣﴾ وَنَذْكُرَكَ كَثِيرًا ﴿٣٤﴾  
 إِنَّكَ كُنْتَ بِنَا بَصِيرًا ﴿٣٥﴾ قَالَ قَدْ أُوتِيتَ سُؤْلَكَ يَمْوَسَى  
 ﴿٣٦﴾ وَلَقَدْ مَنَّا عَلَيْكَ مَرَّةً أُخْرَى ﴿٣٧﴾ إِذْ أَوْحَيْنَا إِلَى  
 أُمِّكَ مَا يُوحَى ﴿٣٨﴾ أَنْ أَقْذِفِيهِ فِي الْكَنَابُوتِ فَأَقْذِفِيهِ فِي  
 الْيَمِّ فَلْيُلْقِهِ الْيَمُّ بِالسَّاحِلِ يَأْخُذْهُ عَدُوٌّ لِي وَعَدُوٌّ لَهُ ۗ  
 وَأَلْقَيْتُ عَلَيْكَ مَحَبَّةً مِنِّي وَلِتُصْنَعَ عَلَى عَيْنِي ﴿٣٩﴾ إِذْ  
 تَمْشِي أُخْتُكَ فَتَقُولُ هَلْ أَدُلُّكُمْ عَلَىٰ مَن يَكْفُلُهُ ۗ  
 فَرَجَعْنَاكَ إِلَىٰ أُمِّكَ كَيْ تَقَرَّ عَيْنُهَا وَلَا تَحْزَنَ ۗ وَقَتَلْتَ نَفْسًا  
 فَنَجَّيْنَاكَ مِنَ الْغَمِّ وَفَتَنَّاكَ فُتُونًا ۗ فَلَبِثْتَ سِنِينَ فِي أَهْلِ  
 مَدْيَنَ ثُمَّ جِئْتَ عَلَىٰ قَدَرٍ يَمْوَسَى ﴿٤٠﴾

وَمَا تِلْكَ بِبِمِينِكَ يَمْوَسَى ﴿١٧﴾  
 قَالَ هِيَ عَصَايَ أَنْتَوَكَّؤُا عَلَيَّهَا  
 وَأَهْمَشُ بِهَا عَلَى غَنَمِي وَلِيَ فِيهَا  
 مَفَارِثُ أُخْرَى ﴿١٨﴾ قَالَ أَلْقِهَا  
 يَمْوَسَى ﴿١٩﴾ فَأَلْقَاهَا فَإِذَا هِيَ  
 حَيَّةٌ تَسْعَى ﴿٢٠﴾ قَالَ خُذْهَا وَلَا تَخَفْ ۗ  
 سُنُعَيْدُهَا سِيرَتَهَا الْأُولَى ﴿٢١﴾

17. Na nini hicho kilichomo mkononi mwako wa kulia, ewe Musa?

18. Akasema: Hii ni fimbo yangu; naiegemea na ninawaangushia majani kondoo na mbuzi wangu. Tena inanifaa kwa matumizi mengine.

19. Akasema: Itupe, ewe Musa!

20. Akaitupa. Mara ikawa nyoka anayekwenda mbio.

21. Akasema: Ikamate, wala usiogope! Tutai-rudisha hali yake ya kwanza.

## Fimbo ya Musa عليه السلام Kugeuka na kuwa Nyoka

Hii ni dalili kutoka kwa Allah تعالى kwa Musa عليه السلام na muujiza mkubwa. Hili ni jambo lililovunja mipaka kwa yanayojulikana kuwa ni mambo ya kawaida, ilikuwa ni dalili nzuri kuwa hapana anayeweza kufanya hivyo ila Allah تعالى. Pia hiyo ni dalili kuwa hakuna anayeweza kuja na mfano wake (katika wanadamu) ila Mtume aliyetumwa na Allah تعالى. Na Kauli Yake:

﴿ وَمَا تِلْكَ بِيَمِينِكَ يَا مُوسَىٰ ﴾

***“Na nini hicho kilichomo mkononi mwako wa kulia, ewe Musa?”***

Wamesema baadhi ya wanazuoni wa Tafsiri, “Allah تعالى Alisema haya kwake kwa njia ya kumvutia Kwake”. Pia panasemwa: “Kwa hakika Alimuambia hilo kwa njia ya Kumfariji, yaani ama hicho ambacho kipo katika mkono wako wa kuume ni fimbo ambayo waifahamu vyema. Utaona yale ambayo Tutayafanya hivi sasa.”

﴿ وَمَا تِلْكَ بِيَمِينِكَ يَا مُوسَىٰ ﴾

***“Na nini hicho kilichomo mkononi mwako wa kulia, ewe Musa?”***

Hii ni ibara ya kusaili kwa lengo la kuyakinisha.

﴿ قَالَ هِيَ عَصَايَ أَتَوَكَّؤُا عَلَيَّهَا ﴾

***“Akasema: Hii ni fimbo yangu; naiegemea.”***

Maana yake: Naiegemea katika hali ya kutembea. Pia,

﴿ وَأَهْشُ بِهَا عَلَىٰ غَنَمِي ﴾

***“Na ninawaangushia majani kondoo na mbuzi wangu.”***

Maana yake: Naitumia kutingisha matawi ya miti kwa ajili ya kuangusha majani kwa kondoo na mbuzi wangu kula kwayo. Amepokea ‘Abdur-Rahman bin Al-Qaasim kuwa Imaam Maalik amesema: “Hapo ni pale mtu anapoweka fimbo yake kwenye tawi la mti na kuitingisha ili majani na matunda yake yawe ni yenye kuanguka bila kuivunja fimbo. Hii si sawa kama kupiga.”<sup>1</sup> Maymuun bin Mahraan amesema kama hivyo. Na Kauli Yake:

<sup>1</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 5:564.

وَلِي فِيهَا مَقَارِبٌ أُخْرَى ﴿١٧﴾

**“Tena inanifaa kwa matumizi mengine.”**

Maana yake: Maslahi, manufaa na mahitajio mengine yasiyokuwa hayo. Baadhi ya wanazuoni wamechukua mzigo juu ya nafsi zao wa kutaja matumizi mengi yasiyoeleweka vizuri. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

قَالَ أَلْقَهَا يَنُوسَىٰ ﴿١٨﴾

**“Akasema: Itupe, ewe Musa!”**

Maana yake: Ewe Musa عليه السلام itupe fimbo iliyo mkononi mwako.

فَأَلْقَهَا فَإِذَا هِيَ حَيَّةٌ تَسْعَىٰ ﴿١٩﴾

**“Akaitupa. Mara ikawa nyoka anayekwenda mbio.”**

Maana yake: Fimbo ilibadilika kuwa nyoka mkubwa, kama chatu mkubwa, aliyetembea kwa haraka. Alitembea haraka sana kana kwamba ni sampuli ya nyoka mdogo, mbali na kuwa alikuwa aina ya nyoka mkubwa sana, ilhali anakwenda kwa kasi sana.

تَسْعَىٰ ﴿٢٠﴾

**“Anayekwenda mbio.”** Maana yake: anatembea na mwenye wahaka. Na Kauli Yake:

سَتُعِيدُهَا سِيرَتَهَا الْأُولَىٰ ﴿٢١﴾

**“Tutairudisha hali yake ya kwanza.”** Maana yake: Hali unayoifahamu iliyokuwa nayo kabla.

وَأَضْمَمْنَا يَدَكَ إِلَىٰ جَنَاحِكَ تَخْرُجُ بَيْضَاءَ مِنْ غَيْرِ سُوءٍ ؕ آيَةٌ أُخْرَىٰ ﴿٢٢﴾ لِئَرْيَاكَ مِنْ

ءَايَاتِنَا الْكُبْرَىٰ ﴿٢٣﴾ أَذْهَبَ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ إِنَّهُ طَغَىٰ ﴿٢٤﴾ قَالَ رَبِّ اشْرَحْ لِي صَدْرِي ﴿٢٥﴾

وَبَيِّرْ لِي أَمْرِي ﴿٢٦﴾ وَأَحْلِلْ عُقْدَةَ مِنِّ لِسَانِي ﴿٢٧﴾ يَفْقَهُوا قَوْلِي ﴿٢٨﴾ وَأَجْعَلْ لِي وَزِيرًا

مِّنْ أَهْلِي ﴿٢٩﴾ هُنُونَ أُنجَىٰ ﴿٣٠﴾ أَشَدُّ بِهِمْ أَزْرَىٰ ﴿٣١﴾ وَأَشْرِكُهُ فِي أَمْرِي ﴿٣٢﴾ كَيْ

نُسَبِّحَكَ كَثِيرًا ﴿٣٣﴾ وَنَذْكُرَكَ كَثِيرًا ﴿٣٤﴾ إِنَّكَ كُنْتَ بِنَا بَصِيرًا ﴿٣٥﴾

22. Na uambatishe mkono wako kwenye ubavu. Utatoka mweupe pasipo kuwa na madhara yoyote. Hiyo ni ishara nyengine.

23. Ili Tukuoneshe baadhi ya Ishara Zetu kubwa.

24. Nenda kwa Firauni; kwani hakika yeye amepindukia mipaka.

25. (Musa) akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Nikunjulie kifua changu,

26. Na Unifanyie nyepesi kazi yangu,

27. Na Ulifungue fundo lililo katika ulimi wangu,

28. Wapate kufahamu maneno yangu.

29. Na Nipe waziri katika watu wangu,

30. Haarun, ndugu yangu.

31. Kwake yeye niongeze nguvu zangu.

32. Na Umshirikishe katika kazi yangu.

33. Ili tukutakase sana.

34. Na tukukumbuke sana.

35. Hakika Wewe Unatuona.

### Mkono wa Musa عليه السلام Kubadilika kuwa mweupe bila Maradhi

Hii ni ishara ya pili ya Musa عليه السلام. Hiyo ni kuwa Allah تعالى Alimuamuru aingize mkono wake katika mfuko wake, kama ilivyoelezewa katika Aya nyingine. Hapa imetajwa hilo, Kwa Kauli Yake Allah تعالى:

وَأَضْمُمْ يَدَكَ إِلَىٰ جَنَاحِكَ

*“Na uambatishe mkono wako kwenye ubavu”.*

Na Amesema katika sehemu nyingine:

وَأَضْمُمْ إِلَيْكَ جَنَاحَكَ مِنَ الرَّهْبِ ۖ فَذٰلِكَ بُرْهٰنَانِ مِنْ رَبِّكَ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ

وَمَلٰئِكَتِهِ

***“Na jiambatishе mkono wako ukihisi khofu. Basi hizi ni dalili mbili zitokazo kwa Mola wako Mlezi kumpelekea Firauni na wakuu wa umma wake.” (28:32).***

Na amesema Mujaahid:

وَأَضْمَمَ يَدَكَ إِلَى جَنَاحِكَ

***“Na uambatishe mkono wako kwenye ubavu.”***

Maana yake: Weka kiganja chako chini ya kwapa lako<sup>1</sup>. Pindi Musa عليه السلام alipotia mkono wake katika mfuko wake na kuutoa, ulitoka uking'aa kama ni nusu mwezi. Na Kauli Yake:

تَخْرُجُ بَيْضَاءَ مِنْ غَيْرِ سُوءٍ

***“Utatoka mweupe pasipo kuwa na madhara yoyote.”***

Maana yake: Bila ukoma, ugonjwa na bila kuumbua. Amesema hilo Ibn 'Abbaas, Mujaahid, 'Ikrimah, Qatadah, Adh-Dhahaak, As-Suddiy na wengineo<sup>2</sup>. Al-Hasan Al-Baswriy amesema: “Aliutoa, na kwa Allah تعالى, ulikuwa kama taa”. Kutoka kwa haya Musa عليه السلام alijua ule uhakika kuwa amekutana na Mola wake Mlezi Aliyetukuka. Na kwa ajili hiyo Amesema Allah تعالى:

لِنُرِيكَ مِنْ آيَاتِنَا الْكُبْرَى

***“Ili Tukuoneshe baadhi ya ishara Zetu kubwa.”***

Allah تعالى Anamuamuru Musa عليه السلام Kwenda kwa Firauni Kupeleka Ujumbe

Na Kauli Yake:

أَذْهَبَ إِلَى فِرْعَوْنَ إِنَّهُ طَغَى

***“Nenda kwa Firauni; kwani hakika yeye amepindukia mipaka.”***

Maana yake: Nenda kwa Firauni, mfalme wa Misri, ambaye ulitoka kwa kumkimbia na ukitoroka, umuite katika kumuabudu Allah تعالى Peke Yake,

<sup>1</sup> At-Tabari 18:297.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:297, 298.

asiyekuwa na mshirika. Muamuru awafanyie wema wana wa Israilli wala asiwaadhibu. Hakika amechupa na kupindukia mipaka na kufanya uovu, na akachagua maisha ya dunia na kumsahau Mola Mlezi Aliye juu.

**Dua ya Musa** عليه السلام.

قَالَ رَبِّ اشْرَحْ لِي صَدْرِي ۖ وَيَسِّرْ لِي أَمْرِي ﴿١٧﴾

**“(Musa) akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Nikunjulie kifua changu, Na Unifanyie nyepesi kazi yangu.”**

Musa عليه السلام alimuomba Mola wake Mlezi Akipanue na Kukikunjua kifua chake apate wepesi kutekeleza majukumu Aliyompa. Hakika, Alimuamuru kwa jambo kubwa na zito. Alimtuma kwa mfalme mwenye nguvu sana ulimwenguni wakati huo. Alikuwa mwenye kiburi na ukafiri kushinda wote, naye alikuwa na jeshi kubwa na ufalme wenye nguvu. Alikuwa dhalimu katili na mwenye kukengeuka kwa inadi miongoni mwa wafalme. Alifikia hatua kudai kuwa hamjui Allah تعالى kabisa, na hamjui Mungu yeyote mwingine kwa raia wake mbali na yeye. Na zaidi ya hayo, Musa عليه السلام alikuwa katika nyumba yake kwa muda alipokuwa mtoto. Alikaa katika chumba cha Firauni mwenyewe na kulala kwenye kitanda chake. Baada ya hayo, alimuua mmoja wa watu wake na alihofia kuwa watalipiza kisasi kwa kumuua. Kisha, alikimbia kutoka kwao na kubakia kama mkimbizi kwa muda wote huo. Baada ya yote hayo, Mola wake Mlezi Alimtuma kama muonyaji akiwaita kumuabudu Allah تعالى tu, bila kumshirikisha pamoja Naye. Hii ndio sababu akasema:

قَالَ رَبِّ اشْرَحْ لِي صَدْرِي ۖ وَيَسِّرْ لِي أَمْرِي ﴿١٧﴾

**“(Musa) akasema: Ewe Mola wangu Mlezi! Nikunjulie kifua changu, na Unifanyie nyepesi kazi yangu.”**

Maana yake: Siwezi kutekeleza kazi hii usiponisaidia na kuniunga mkono.

وَأَحَلَّلْ عُقْدَةً مِّنْ لِّسَانِي ۖ يَفْقَهُوا قَوْلِي ﴿١٨﴾

**“Na Ulifungue fundo lililo katika ulimi wangu, Wapate kufahamu maneno yangu.”**

Na hilo ni kutokana na tatizo alilokuwa nalo katika mdomo wake, kwa tukio lililotokea baada ya kupatiwa tende na kaa la moto, naye alichukua kaa la moto na kulitia mdomoni badala ya tende. Kisa hiki kitaelezewa kwa kina katika Surah zinazofuatia. Hata hivyo, hakumuomba Allah تعالی Amuondoshee hilo kabisa. Bali, aliomba kuondoshewa kithembe alichokuwa nacho ili watu wapate kumuelewa anachozungumza. Aliomba lile linalohitajika kufikisha ujumbe kiasi cha haja tu. Lau angeomba kuondoshwa hilo kabisa basi angeondoshewa kabisa, lakini Manabii hawaombi chochote ila kwa kadiri ya haja. Hivyo, alibakishwa na mabaki ya tukio hilo lililoathiri mdomo wake. Allah تعالی Anatufahamisha alichosema Firauni,

﴿أَمْ أَنَا خَيْرٌ مِّنْ هَٰذَا الَّذِي هُوَ مَهِينٌ وَلَا يَكَادُ يُبِينُ﴾

***“Au mimi ni bora kuliko huyu (Musa) aliye mnyonge wala hawezi kusema waziwazi?” (43:52),***

Maana yake: Si fasaha katika mazungumzo. Na Kauli Yake:

﴿وَأَجْعَلِ لِي وَزِيرًا مِّنْ أَهْلِي﴾ ﴿هٰرُونَ أَخِي﴾

***“Na nipe waziri katika watu wangu, Haarun, ndugu yangu”.***

Hili pia lilikuwa ni ombi la Musa عليه السلام kuhusu kutaka usaidizi. Aliomba apewe nduguye, Haarun عليه السلام amsaidie. Amepokea Ath-Thawriy رحمه الله تعالی kutoka kwa Abu Sa'id kutoka kwa 'Ikrimah kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Harun عليه السلام alifanywa kuwa Nabii wakati ule ule Musa عليه السلام alipofanywa Nabii”<sup>1</sup>. Amepokea Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالی kuwa mama Aishah رضي الله عنها alitoka akiwa na nia ya kufanya 'Umrah na akasimama kupiga kambi kati ya Mabedui. Alipokuwa pamoja nao alimsikia mtu akisema, “Ni ndugu gani katika maisha haya (duniani) alikuwa ni mwenye manufaa zaidi kwa nduguye?” Watu wakajibu, “Hatujui”. Mtu yule akasema: “Naapa kwa Allah تعالی najua”. Mama Aisha رضي الله عنها alisema: “Nikasema katika nafsi yangu kuhusu kuapa kwake kuwa asiape kiapo, kujichagua yeye kuwa anajua mtu aliyekuwa na manufaa makubwa kwa nduguye”. Huyo mtu akasema: “Huyo ni

<sup>1</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 5:567.

Musa عليه السلام, pale alipoomba kwa nduguye apewe Unabii". Hapo, Aishah رضي الله عنها akasema, "Naapa kwa Allah تعالى, amesema kweli". Nikasema: "Na kuhusu hili amesema Allah تعالى katika Kumsifu Musa عليه السلام:

وَكَانَ عِنْدَ اللَّهِ وَجِيهًا ﴿٣٣﴾

**'Naye alikuwa mwenye heshima mbele ya Allah.'** (33:69)

Na Kauli Yake:

أَشْدُدْ يَمَّةَ أَزْرَى ﴿٣٤﴾

**"Kwake yeye niongeze nguvu zangu".** Amesema Mujaahid: "Mgongo wangu (yaani ufanye uwe na nguvu)".

وَأَشْرِكُهُ فِي أَمْرِي ﴿٣٥﴾

**"Na Umshirikishe katika kazi yangu."** Maana: Kunishauri katika jambo hili.

كَيْ تَسْبَحَكَ كَثِيرًا ﴿٣٦﴾ وَتَذُكَّرَ كَثِيرًا ﴿٣٧﴾

**"Ili tukutakase sana. Na tukukumbuke sana".**

Amesema Mujaahid: "Mja wa Allah تعالى hawezi wala hachukuliwi kuwa ni mwenye kumtaja Allah تعالى kwa wingi mpaka amkumbuke Allah تعالى kwa kusimama, kukaa na kwa kulala."<sup>1</sup> Na Kauli Yake:

إِنَّكَ كُنْتَ بِنَا بَصِيرًا ﴿٣٨﴾

**"Hakika Wewe Unatuona."**

Maana yake: Kwa kutuchagua, Kutupatia Utume na Kututuma kwa adui Yako, Firauni. Sifa zote njema Unastahiki Wewe kwa hilo.

قَالَ قَدْ أُوتِيتَ سُؤْلَكَ يَا مُوسَى ﴿٣٩﴾ وَلَقَدْ مَنَّا عَلَيْكَ مَرَّةً أُخْرَى ﴿٤٠﴾ إِذْ أَوْحَيْنَا إِلَىٰ  
أُمِّكَ مَا يُوحَىٰ ﴿٤١﴾ أَنْ أَقْذِفِيهِ فِي الْتَابُوتِ فَأَقْذِفِيهِ فِي الْيَمِّ فَلْيُلْقِهِ الْيَمُّ بِالسَّاحِلِ  
يَأْخُذْهُ عَدُوٌّ لِي وَعَدُوٌّ لَهُ ۗ وَأَلْقَيْتُ عَلَيْكَ حَبَابًا مِّنِّي وَلَتُضْنَعُ عَلَىٰ عَيْنِي ﴿٤٢﴾ إِذْ تَمْشِي  
أَخْتُكَ فَتَقُولُ هَلْ أَدُلُّكُمْ عَلَىٰ مَن يَكْفُلُهُ ۗ فَرَجَعْنَاكَ إِلَىٰ أُمِّكَ كَيْ تَقَرَّ عَيْنُهَا وَلَا تَحْزَنَ ۗ

<sup>1</sup> Al-Qurtwubiy 14:186.



وَقَتَلْتَ نَفْسًا فَنَجَّيْنَاكَ مِنَ الْغَمِّ وَفَتَنَّاكَ فُتُونًا فَلَبِثْتَ سِتِينَ فِيْ أَهْلِ مَدْيَنَ ثُمَّ جِئْتَ

عَلَىٰ قَدَرٍ يَمُوسَىٰ ﴿٤٠﴾

**36. Akasema: Hakika Umepewa maombi yako, ewe Musa!**

**37. Na hakika Tulikwisha kufanyia hisani mara nyengine...**

**38. Pale Tulipomfunulia mama yako yaliyofunuliwa,**

**39. Ya kuwa mtie katika kibanduku, na kisha kitie mtoni, na mto utamfikisha ufukweni. Atamchukua adui Yangu naye ni adui yake. Na Nimekutulia mapenzi yanayotoka Kwangu, na ili ulelewe machoni Mwangu.**

**40. Dada yako alipokwenda na akasema: Je! Nikujulisheni mtu wa kuweza kumlea? Basi Tukakurejesha kwa mama yako ili macho yake yaburudike, wala asihuzunike. Na ulimua mtu, Nasi Tukakuokoa katika dhiki, na Tukakujaribu kwa majaribio mengi. Ukakaa miaka kwa watu wa Madyan. Kisha ukaja kama ilivyokadiriwa, ewe Musa!**

### Kukubaliwa Dua ya Musa عليه السلام na Kukumbushwa Neema za Awali

Jawabu hili kutoka kwa Allah تعالى kwa Mtume Wake, Musa عليه السلام kwa aliyoomba kutoka kwa Mola Wake Aliyetukuka. Ndani yake upo ukumbusho kwa kuneemeshwa kwake hapo mbeleni. Wa kwanza ulikuwa ni kupatiwa ilhamu mama yake alipokuwa akimnyonyesha huku akiogopa kuwa Firauni na wakuu wake watamua. Musa عليه السلام alizaliwa ule mwaka ambao wao (watu wa Firauni) walikuwa wakiua watoto wote wa kiume waliozaliwa. Hivyo, alimtia kwenye kibanduku, ambacho alikitia mtoni. Mto ulimchukua, kumfanya (mama yake Musa عليه السلام) kuwa na huzuni na mfidhaiko mkubwa, kama Alivyotaja Allah تعالى kumhusu Aliposema,

وَأَصْبَحَ فُؤَادُ أُمِّ مُوسَىٰ فَرِغًا ۗ إِن كَادَتْ لَتُبْدِي بِهِ لَوْلَا أَن رَّبَّنَا عَلَي قَلْبِهَا

**“Na moyo wa mamake Musa ukawa mtupu, alikuwa karibu kudhihirisha siri kama Tusingeutia nguvu moyo wake...” (28:10).**

Mto ulimchukua mpaka kwenye nyumba ya Firauni.

فَأَلْتَقَطَهُ ءِالُ فِرْعَوْنَ لِيَكُونَ لَهُمْ عَدُوًّا وَحَزَنًا<sup>4</sup>

**“...Basi wakamuokota watu wa Firauni. Ili awe adui kwao na huzuni...” (28:8)**

Maana: Hiyo ilikuwa ni Kudura, iliyopitishwa na Allah تعالى. Walikuwa wakiwaua watoto wa kiume wa wana wa Israili kwa kuhofia ujio wa Musa عليه السلام. Hivyo, Allah تعالى Akahukumu na Kupitisha, Naye Ndiye Mwenye Mamlaka makubwa na Uwezo uliotimia. Alipitisha kuwa Musa عليه السلام hatalelewa isipokuwa katika godoro na kitanda cha Firauni, naye atalishwa chakula na kinywaji chake (Firauni), akipata mapenzi yake (Firauni) na mkewe. Kwa hiyo, Akasema Aliyetukuka:

يَأْخُذُهُ عَدُوِّي وَعَدُوُّ لَهُ<sup>5</sup> وَأَلْقَيْتُ عَلَيْكَ مَحَبَّةً مِّنِّي

**“Atamchukua adui Yangu naye ni adui yake. Na Nimekutilia mapenzi yanayotokana Kwangu...”**

Maana yake: Nilimfanya adui yako akupende. Amesema Salamah bin Kuhayl:

وَأَلْقَيْتُ عَلَيْكَ مَحَبَّةً مِّنِّي

**“Na Nimekutilia mapenzi yanayotokana Kwangu...”** Maana yake: Niliwafanya waja wangu wakupende.

وَلِتُضَنَّ عَلَيَّ عَيْنِي<sup>6</sup>

**‘Na ili ulelewe machoni Mwangu!’**

Amesema Abu Imraan Al-Jawniy: Utalelewa chini ya Uangalizi wa Allah تعالى<sup>2</sup>.

Na Kauli Yake:

إِذْ تَمْشِي أُحْتَلِكُ فَتَقُولُ هَلْ أَذْلُكُمْ عَلَيَّ مَن يَكْفُلُهُ<sup>7</sup> فَرَجَعْتَنكَ إِلَىٰ أُمِّكَ كَيْ تَقَرَّ عَيْنُهَا

**“Dada yako alipokwenda na akasema: Je! Nikujuulisheni mtu wa kuweza kumlea? Basi Tukakurejesha kwa mama yako ili macho yake yaburudike”.**

Alipokubaliwa katika nyumba ya Firauni, wanawake waliletwa katika jaribio

<sup>1</sup> At-Tabari 18:303.

<sup>2</sup> Fat’h Al-Qadiir 3:367.

la kumtafuta atakayemnyonyesha, lakini alikataa kunyonyeshwa na yeyote kati ya hao. Akasema Allah تعالى:

﴿ وَحَرَّمْنَا عَلَيْهِ الْمَرَاضِعَ مِنْ قَبْلُ ﴾

**“Na Tukamharimishia wanyonyeshaji tangu mwanzo...” (28:12).**

Hapo akaja dada yake, akasema:

﴿ هَلْ أَدُلُّكُمْ عَلَىٰ أَهْلِ بَيْتٍ يَكْفُلُونَهُ لَكُمْ وَهُمْ لَهُ نَصْحُورٌ ﴾

**“Je, nikuonesheni watu wa nyumba watakaomlea kwa ajili yenu, na pia watakuwa wema kwake?” (28:12).**

Alikuwa anamaanisha, je, nikuonesheni atakayemnyonyesha kwa ajili yenu kwa ujira? Hivyo, alimchukua na akaenda nao mpaka kwa mama yake. Alipompatia titi lake, alinyonya (bila shida), nao watu wa Firauni walifurahi sana kwa hilo. Kwa hiyo, walimuajiri ili amnyonyeshe, na kwa sababu hiyo akapata furaha, starehe na raha hapa duniani na furaha zaidi Akhera. Na hapa Akasema Aliyetukuka:

﴿ فَرَجَعْنَكَ إِلَىٰ أُمِّكَ كَيْ تَقَرَّ عَيْنُهَا وَلَا تَحْزَنَ ۗ ﴾

**“Basi Tukakurejesha kwa mama yako ili macho yake yaburudike, wala asihuzunike”,** Maana yake: Asihuzunike juu yako.

﴿ وَقَتَلْتَ نَفْسًا ﴾

**“Na ulimuua mtu.”** Maana yake: Mkibiti (mwananchi miongoni mwa watu wa Firauni).

﴿ فَتَجِيئُكَ مِنَ الْعَمْرِ ﴾

**“Nasi Tukakuokoa katika dhiki”.**

Na hilo ndilo alilokuwa akihisi kwa sababu ya familia ya Firauni kutaka kumuua. Hivyo, alikimbia kutoka kwao mpaka akafika kwenye maji ya watu wa Madyan. Na huko akamuambia yeye mtu mwema:

﴿ لَا تَخَفْ ۗ نَجَّيْنَاكَ مِنَ الْغَمِّ مِنَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴾

**“Usiogope umekwisha kuokoka na watu madhalimu.” (28:25).**

وَأَصْطَفَيْتَكَ لِنَفْسِي ﴿٤١﴾ أَذْهَبَ أَنْتَ وَأَخُوكَ بِمَا بَيْنِي وَلا  
 تَبَيَّنَا فِي ذِكْرِي ﴿٤٢﴾ أَذْهَبَا إِلَى فِرْعَوْنَ إِنَّهُ طَغَى ﴿٤٣﴾  
 فَقُولَا لَهُ قَوْلًا لَيْتِنَا لَعَلَّهُ يَتَذَكَّرُ أَوْ يَخْشَى ﴿٤٤﴾ قَالَ رَبَّنَا  
 إِنَّا نَخَافُ أَنْ يُفْرِطَ عَلَيْنَا أَوْ أَنْ يَطْغَى ﴿٤٥﴾ قَالَ لَا تَخَافَا  
 إِنِّي مَعَكُمْ أَسْمَعُ وَأَرَى ﴿٤٦﴾ فَأَتِيَاهُ فَقُولَا إِنَّا  
 رَسُولَا رَبِّكَ فَأَرْسِلْ مَعَنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ وَلا تُعَذِّبْهُمْ قَدْ  
 جَعَلْنَاكَ بِمَا بَيْنَ يَدَيْهِ مِنَ رَحْمَتِنَا عَلَى مَنْ أَتْبَعَ أَهْدَى ﴿٤٧﴾  
 إِنَّا قَدْ أُوحِيَ إِلَيْنَا أَنَّ الْعَذَابَ عَلَى مَنْ كَذَّبَ وَتَوَلَّى ﴿٤٨﴾  
 قَالَ فَمَنْ رُبُّكُمْ يَا مُوسَى ﴿٤٩﴾ قَالَ رَبُّنَا الَّذِي  
 أَعْطَى كُلَّ شَيْءٍ حَلْقَهُ ثُمَّ هَدَى ﴿٥٠﴾ قَالَ فَمَا بَالُ  
 الْقُرُونِ الْأُولَى ﴿٥١﴾ قَالَ عَلِمَهَا عِنْدَ رَبِّي فِي كِتَابٍ لا  
 يَضِلُّ رَبِّي وَلا يَنْسَى ﴿٥٢﴾ الَّذِي جَعَلَ لَكُمْ الْأَرْضَ  
 مَهْدًا وَسَلَكَ لَكُمْ فِيهَا سُبُلًا وَأَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً  
 فَأَخْرَجْنَا بِهِ أَزْوَاجًا مِنْ نَبَاتٍ شَتَّى ﴿٥٣﴾ كُلُوا وَارْزُقُوا  
 أَتَعْمَلُونَ إِنِّي فِي ذَلِكَ لِأَيُّمٌ لِأُولِي الْأَلْبَابِ ﴿٥٤﴾ \* مِنْهَا  
 خَلَقْنَاكُمْ وَفِيهَا نُعِيدُكُمْ وَمِنْهَا نُخْرِجُكُمْ تَارَةً أُخْرَى ﴿٥٥﴾  
 وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا إِبْرَاهِيمَ إِذْ يَبْنِي كَعْبَةَ اللَّهِ كَالْحُرِيِّ ﴿٥٦﴾  
 لِيُخْرِجَنَا مِنْ أَرْضِنَا بِسِحْرِكَ يَا مُوسَى ﴿٥٧﴾ فَلَمَّا تَبَيَّنَكَ  
 بِسِحْرِ مِثْلِهِ فَأَجْعَلْ بَيْنَنَا وَبَيْنَكَ مَوْعِدًا لا نُخْلِفُهُ نَحْنُ  
 وَلا أَنْتَ مَكَانًا سَوِيًّا ﴿٥٨﴾ قَالَ مَوْعِدُكُمْ يَوْمَ الزَّيْنَةِ وَأَنْ  
 تُخَشِّرَ النَّاسَ ضُحًى ﴿٥٩﴾

وَأَصْطَفَيْتَكَ لِنَفْسِي ﴿٤١﴾ أَذْهَبَ  
 أَنْتَ وَأَخُوكَ بِمَا بَيْنِي وَلا تَبَيَّنَا فِي  
 ذِكْرِي ﴿٤٢﴾ أَذْهَبَا إِلَى فِرْعَوْنَ إِنَّهُ  
 طَغَى ﴿٤٣﴾ فَقُولَا لَهُ قَوْلًا لَيْتِنَا  
 لَعَلَّهُ يَتَذَكَّرُ أَوْ يَخْشَى ﴿٤٤﴾

41. Na Nimekuteua kwa ajili ya Nafsi Yangu.

42. Nenda, wewe na ndugu yako, pamoja na ishara Zangu, wala msichoke kunikumbuka.

43. Nendeni kwa Firauni. Hakika yeye amepindukia mipaka.

44. Mwambieni maneno laini, huenda akazingatia au akaogopa.

Kuchaguliwa Musa عليه السلام Kwenda kwa Firauni na Kuamrisha Alinganie kwa maneno mazuri

Anasema Aliyetukuka Akimuambia Musa عليه السلام kuwa ameishi kati ya watu wa Madyan, akimkimbia Firauni na wakuu wake. Akafanya kazi ya kuchunga wanyama wa baba mkwe

mpaka muda walioagana kumalizika. Kisha akafikwa na Kudura ya Allah تعالى na *Irada* Yake bila ya yeye kuwa na miadi. Jambo hilo lilikuwa chini ya Uwezo na Udhhibiti wa Allah تعالى. Naye Ndiye Mwenye Kufanya wepesi kwa waja Wake na viumbe Vyake kwa Analotaka. Kwa sababu hiyo Akasema:

ثُمَّ جِئْتَنَا عَلَىٰ قَدَرٍ يَمُوسَىٰ ﴿٤١﴾

**“Kisha ukaja kama ilivyo kadiriwa, ewe Musa!”**

Amesema Mujaahid: “Maana: Kwa miadi (waliyoafikiana)”<sup>1</sup>. Amepokea Abdur-Razzaaq kutoka kwa Ma’mar kutoka kwa Qataadah kuwa amesema yafuatayo kuhusu Kauli Yake:

ثُمَّ جِئْتَنَا عَلَىٰ قَدَرٍ يَمُوسَىٰ ﴿٤١﴾

**“Kisha ukaja kama ilivyokadiriwa, ewe Musa!”**

Kwa Kudura (*Qadar*) ya unabii na utume”<sup>2</sup>. Na Kauli Yake:

وَأَصْطَفَيْنَاكَ لِنَفْسِي ﴿٤٢﴾

**“Na Nimekuteua kwa ajili ya Nafsi Yangu.”**

Maana yake: Nimekuteua na Kukuchagua ili uwe Mtume Wangu. Hili ndilo Ninalotaka na Kulipendelea. Na amepokea Al-Bukhaari kuhusu tafsiri ya Aya hii kuwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kutoka kwa Mtume ﷺ amesema:

«النَّفِيُّ آدَمُ وَمُوسَىٰ فَقَالَ مُوسَىٰ: أَنْتَ الَّذِي أَشَقَيْتَ النَّاسَ وَأَخْرَجْتَهُمْ مِنَ الْجَنَّةِ، فَقَالَ آدَمُ: وَأَنْتَ الَّذِي اضْطَفَاكَ اللهُ بِرِسَالَتِي وَاضْطَفَاكَ لِنَفْسِي، وَأَنْزَلَ عَلَيْكَ التَّوْرَةَ؟ قَالَ: نَعَمْ، قَالَ: فَوَجَدْتَهُ مَكْتُوبًا عَلَيَّ قَبْلَ أَنْ يَخْلُقَنِي؟ قَالَ: نَعَمْ، فَحَجَّ آدَمُ مُوسَىٰ»

*“Adam na Musa walikutana, na Musa akamuambia, ‘Wewe ndiye uliyefanya mambo kuwa ya shida kwa wanadamu na kuwatoa Peponi’. Adam akasema: “Je, wewe ni yule ambaye Allah*

<sup>1</sup> At-Tabari 18:311.

<sup>2</sup> Abdur-Razzaaq 3:17.

*Alikuchagua kwa ajili ya Ujumbe Wake kwa Nafsi Yake na Kukuteremshia Taurati". Musa akajibu: "Ndio". Kisha, Adam akasema, "Ulinikuta limeandikiwa hilo kwangu hata kabla ya Kuumbwa kwangu?" Musa akasema: "Ndio". Hapo Adam alimshinda Musa kwa hoja<sup>1</sup>.*

Upokezi huu umenukuliwa na Al-Bukhaari na Muslim. Na Kauli Yake:

أَذْهَبَ أَنْتَ وَأَخُوكَ بِمَا بَيْنِي

***"Nenda, wewe na ndugu yako, pamoja na ishara Zangu."***

Maana yake: Kwa hoja, dalili na miujiza,

وَلَا تَبَيَّنَا فِي ذِكْرِي

***"Wala msichoke kunikumbuka".***

Amepokea 'Aliy bin Abi Twalhah kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: "Usiwe goi goi"<sup>2</sup>. Na amesema Mujaahid kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: "Usiwe dhaifu". Maana hapa ni kuwa wasirudi nyuma (wala kusita) katika kumtaja Allah تعالى. Bali, wote wawili wanatakiwa wamdhukuru Allah تعالى katika mikutano yao na Firauni ili kumtaja kwao Allah تعالى kusaidie dhidi yake (Firauni). Kumdhukuru Allah تعالى ndio itakuwa ngao na nguvu kwao itakayowafanya wamshinde. Na Kauli Yake:

أَذْهَبَا إِلَىٰ فِرْعَوْنَ إِنَّهُ طَغَىٰ

***"Nendeni kwa Firauni. Hakika yeye amepindukia mipaka."***

Maana yake: Amekengeuka, amekuwa na kiburi na kujifakhiri dhidi ya Allah تعالى na kumuasi.

فَقُولَا لَهُ قَوْلًا لَّيِّنًا لِّعَلَّهِ يَتَذَكَّرُ أَوْ يَحْشَىٰ

***"Muambieni maneno laini, huenda akazingatia au akaogopa".***

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baariy 8:288 na Muslim 4:2043, 2044

<sup>2</sup> At-Tabari 18:312.

Aya hii ina fundisho kubwa sana. Japokuwa Firauni alikuwa wakati huo ni mwenye kujiona na mwenye kiburi miongoni mwa watu, na Musa عليه السلام ndiye rafiki na mteule wa Allah تعالى kati ya viumbe Vyake wakati huo, bado Musa عليه السلام aliamriwa azungumze na Firauni kwa upole na ulaini. Hivyo, wito wao kwake ulikuwa kwa ulaini na mazungumzo ya upole na usahali kama yanayotumika kwa rafiki wa karibu. Ili ujumbe huo uwe na athari kubwa zaidi nyoyoni, na ukite ndani na utoe natija nzuri. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

أَدْعُ إِلَى سَبِيلِ رَبِّكَ بِالْحُكْمَةِ وَالْمَوْعِظَةِ الْحَسَنَةِ ۗ وَجَدِلْ لَهُم بِآيَاتِي هِيَ أَحْسَنُ

**“Waite watu katika njia ya Mola wako Mlezi kwa hekima na mawaidha mema na jadiliano nao kwa namna iliyo bora.” (16:125)**

Na Kauli Yake:

لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ أَوْ يَخْشَوْنَ ﴿١٢٥﴾

**“Huenda akazingatia au akaogopa.”**

Maana yake: Huenda akarudi nyuma kwa aliyokuwa nayo katika upotevu na maangamivu,

أَوْ يَخْشَوْنَ ﴿١٢٥﴾

**“Au akaogopa.”**

Hii ina maana atarudi katika utiifu kwa kumuogopa Allah تعالى. Kama Alivyosema Aliyetukuka:

لِمَنْ أَرَادَ أَنْ يَذْكَرَ أَوْ أَرَادَ شُكُورًا ﴿١٢٦﴾

**“Kwa anayetaka kukumbuka au anayetaka kushukuru.” (25:62)**

Kwa hiyo, kukumbuka ni kurudi kutokana na hatari na kuogopa ni kufikia utiifu. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

قَالَ لَا تَخَافَا إِنِّي مَعَكُمَا

أَسْمَعُ وَأَرَى ﴿١٢٧﴾ فَأَتِيَاهُ فَقُولَا إِنَّا رَسُولَا رَبِّكَ فَأَرْسِلْ مَعَنَا بَنِي إِسْرَائِيلَ وَلَا

تُعَذِّبِهِمْ ۗ قَدْ جِئْنَاكَ بِبَيِّنَةٍ مِّنْ رَبِّكَ ۗ وَالسَّلَامُ عَلَيَّ مَنِ اتَّبَعَ الْهُدَىٰ ﴿١٢٨﴾ إِنَّا قَدْ أُوحِيَ

إِلَيْنَا أَنَّ الْعَذَابَ عَلَيَّ مَنِ كَذَّبَ وَتَوَلَّىٰ ﴿١٢٩﴾

**45. Wakasema: Ewe Mola wetu Mlezi! Hakika sisi tunaogopa asije akapindukia mipaka juu yetu au kufanya jeuri.**

**46. Akasema: Msiogope! Hakika Mimi ni pamoja nanyi. Nasikia na Ninaona.**

**47. Basi muendeeni, na mwambieni: Hakika sisi ni Mitume wa Mola wako Mlezi! Basi waache Wana wa Israili watoke nasi, wala usiwaadhibu. Sisi tumekuletea ishara itokayo kwa Mola wako Mlezi. Na amani itakuwa juu ya aliyefuata uwongofu.**

**48. Hakika tumefunuliwa sisi kwamba hapana shaka adhabu itamsibu anayekadhibisha na akapuuza.**

**Khofu ya Musa عليه السلام kwa Firauni na Kutiliwa Nguvu na Allah تعالى**

Allah تعالى Anatupasha habari kuhusu Musa عليه السلام na Haarun عليه السلام walimuomba Allah تعالى huku wakimlilia kwa kumuambia:

إِنَّا نَخَافُ أَنْ يُفْرِطَ عَلَيْنَا أَوْ أَنْ يَطَّغَىٰ ﴿٥٥﴾

**“Hakika sisi tunaogopa asije akapindukia mipaka juu yetu au kufanya jeuri.”**

Wakimaanisha kuwa huenda Firauni akawashika kwa ghafla kwa adhabu, au kuchupa mipaka dhidi yao kwa kuwaadhibu, ilhali hawastahiki hilo. Amepokea Adh-Dhahaak kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “‘Au kufanya ujeuri’ ina maana ya kuvuka mipaka”<sup>1</sup>.

قَالَ لَا تَخَافَا إِنِّي مَعَكُمَا أَسْمَعُ وَأَرَىٰ ﴿٥٦﴾

**“Akasema: Msiogope! Hakika Mimi ni pamoja nanyi. Nasikia na Ninaona.”**

Maana yake: Msimuogope, kwani Mimi Niko pamoja nanyi, Nasikia mazungumzo yenu na yake pia. Nawaona mlipo na sehemu alipo. Hakuna chochote katika mambo yenu ambayo Siyajui (Najua mambo yenu yote). Jueni kuwa paji lake la uso liko Mkononi Mwangu, na hazungumzi, kupumua au

<sup>1</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 5:580.



kutumia nguvu yoyote ile isipokuwa kwa Ruhusa na Amri Yangu. Niko pamoja nanyi kwa Ulinzi, Hifadhi na Usaidizi Wangu.

فَأْتِيَاهُ فَقُولَا إِنَّا رَسُولَا رَبِّكَ

**“Basi muendeeni, na mwambieni: Hakika sisi ni Mitume wa Mola wako Mlezi!”**

**Waadhi wa Musa عليه السلام mbele ya Firauni**

Na Kauli Yake:

قَدْ جِئْنَاكَ بِبَيِّنَاتٍ مِنْ رَبِّكَ

**“Sisi tumekuletea ishara itokayo kwa Mola wako Mlezi”,**

Maana: Pamoja na dalili na miujiza kutoka kwa Mola wako Mlezi,

وَأَسَلْتُمُ عَلِيَّ مَنِ اتَّبَعَ الْهُدَىٰ ﴿١٧﴾

**“Na amani itakuwa juu ya aliyefuata uongofu.”**

Maana yake: Amani iwe juu yako ukiwa utafuata uongofu. Kwa ajili hiyo pale Mtume ﷺ alipomuandikia barua Hiraql (Heraclius), mfalme wa Roma, alianza na,

«بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ، مِنْ مُحَمَّدٍ رَسُولِ اللَّهِ إِلَىٰ هِرَقْلَ عَظِيمِ الرُّومِ، سَلَامٌ عَلَيَّ مَنِ اتَّبَعَ الْهُدَىٰ، أَمَّا بَعْدُ، فَإِنِّي أَدْعُوكَ بِدَعَايَةِ الْإِسْلَامِ، فَأَسَلِمُ تَسْلِمًا يُؤْتِنُكَ اللَّهُ أَجْرَكَ مَرَّتَيْنِ»

*“Kwa jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu. Kutoka kwa Muhammad, Mtume wa Allah, hadi kwa Heraclius, mfalme wa Roma. Amani iwe juu ya mwenye kufuata uongofu. Ama baada ya hayo: Hakika, nakuita kwa wito wa Uislamu. Silimu utasalimika, na Allah Atakupa ujira mara mbili”<sup>1</sup>.*

Kwa hiyo, Musa عليه السلام na Haarun عليه السلام walimuambia Firauni:

وَأَسَلْتُمُ عَلِيَّ مَنِ اتَّبَعَ الْهُدَىٰ ﴿١٧﴾ إِنَّا قَدْ أُوحِيَ إِلَيْنَا أَنَّ الْعَذَابَ عَلَىٰ مَنْ كَذَّبَ

وَتَوَلَّى ﴿١٨﴾

<sup>1</sup> Fat'h al-Baariy 1:42.

**“Na amani itakuwa juu ya aliyefuata uongofu. Hakika tumefunuliwa sisi kwamba hapana shaka adhabu itamsibu anayekadhibisha na akapuuza.”**

Maana yake: Ametuelezea kwa Aliyotuteremshia katika Wahyi kuwa adhabu imeandaliwa hasa kwa wale wenye kukataa Aya na Ishara za Allah تعالى na kukengeuka katika utiifu Wake, kama Alivyosema Aliyetukuka:

فَأَمَّا مَنْ طَغَى ﴿٣٧﴾ وَءَاثَرَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ﴿٣٨﴾ فَإِنَّ الْجَحِيمَ هِيَ الْمَأْوَى ﴿٣٩﴾

**“Ama yule aliyeeasi. Na akapenda zaidi maisha ya dunia. Basi kwa hakika Jahanamu ndiyo itakayokuwa makazi yake.” (79:37-39)**

Na Amesema Aliyetukuka:

فَأَنْذَرْتُكُمْ نَارًا تَلَظَّى ﴿٩٢﴾ لَا يَصْلَاهَا إِلَّا الْأَشْقَى ﴿٩٣﴾ الَّذِي كَذَّبَ وَتَوَلَّى ﴿٩٤﴾

**“Basi nakuhadharisheni na Moto uwakao kwa nguvu. Hatauingia ila muovu. Anayekadhibisha na kuipa mgongo Dini hii ya haki.” (92:14-16).**

Na Amesema Aliyetukuka:

فَلَا صَدَقَ وَلَا صَلَّى ﴿٧٥﴾ وَلَكِنْ كَذَّبَ وَتَوَلَّى ﴿٧٦﴾

**“Hakusadiki wala hakuswali. Bali alikadhibisha na akarudi nyuma.” (75:31- 32).**

Hii inamaanisha alikadhibisha kwa moyo wake na akakengeuka kwa vitendo vyake.

قَالَ فَمَنْ رَبُّكُمْ يَا مُوسَى ﴿٤٩﴾ قَالَ رَبُّنَا الَّذِي أَعْطَى كُلَّ شَيْءٍ خَلْقَهُ ثُمَّ هَدَى ﴿٥٠﴾

قَالَ فَمَا بَالُ الْقُرُونِ الْأُولَى ﴿٥١﴾ قَالَ عِلْمُهَا عِنْدَ رَبِّي فِي كِتَابٍ لَا يَضِلُّ رَبِّي وَلَا

يَنْسَى ﴿٥٢﴾

**49. (Firauni) akasema: Basi Mola wenu Mlezi ni nani, ewe Musa?**

**50. Akasema: Mola wetu Mlezi ni yule aliyekipa kila kitu umbo lake, kisha akakiongoa.**

**51. Akasema: Nini hali ya karne za kwanza?**

**52. Akasema: Ilimu yake iko kwa Mola wangu Mlezi katika Kitabu.  
Mola wangu Mlezi Hapotei wala Hasahau.**

**Mjadala Baina ya Musa عليه السلام na Firauni**

Allah تعالى Anatupa habari za Firauni kuwa alimuambia Musa عليه السلام katika kukataa kwake kuwepo kwa Muumba, ambaye ni Mola wake Mlezi na Mwenye Kumiliki kila kitu. Akasema:

فَمَنْ رَبُّكُمَْا يَمُوسَىٰ ﴿٥٢﴾

***“Basi Mola wenu Mlezi ni nani, ewe Musa?”***

Maana yake: Nani aliyekuita na kukutuma? Hakika mimi simjui wala sikukujuzua mungu mwengine yeyote asiyekuwa mimi.

قَالَ رَبُّنَا الَّذِي أَعْطَىٰ كُلَّ شَيْءٍ خَلْقَهُ ثُمَّ هَدَىٰ ﴿٥٣﴾

***“Akasema: Mola wetu Mlezi ni Yule Aliyekipa kila kitu umbo lake,  
kisha Akakiongoa”.***

Amepokea ‘Aliy bin Abi Twalhah kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما: “Anasema kuwa Ameumba jozi kwa kila kitu”<sup>1</sup>. Na amepokea Adh-Dhahaak kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Alimjaalia mwanadamu kuwa mwanadamu, na punda kuwa ni punda na kondoo kuwa kondoo”. Amepokea Layth bin Abi Sulaym kutoka kwa Mujaahid amesema: “Alikipatia kila kitu sura yake”. Amepokea Ibn Abi Najih kuwa Mujaahid amesema: “Akalinganisha umbile la kila mnyama”. Na amesema Sa’id bin Jubayr kuhusu Kauli Yake:

أَعْطَىٰ كُلَّ شَيْءٍ خَلْقَهُ ثُمَّ هَدَىٰ ﴿٥٣﴾

***“Yule Aliyekipa kila kitu umbo lake, kisha Akakiongoa”.***

Akasema: ‘Akakipatia kila kiumbe Chake kinachostahiki kwa umbo lake”<sup>2</sup>. Kwa hiyo, Hakumpa mwanadamu umbile la mnyama, wala mnyama umbile la mwanadamu. Hivyo hivyo, umbile la mbwa si kama la kondoo. Pia Akakipa kila kitu kinachostahiki katika ndoa, na Akakiathiri kila kitu katika hilo. Hakuna kitu miongoni mwayo kinachofanana na kiumbe chengine katika vitendo vyake

<sup>1</sup> At-Tabari 18:316.

<sup>2</sup> Al-Qurtwubiy 11:204.

kwa umbile, riziki na kuingiliana kimwili. Wakasema baadhi ya wafasiri: **‘Yule Aliyekipa kila kitu umbile lake, kisha Akakiongoa’**, kama Kauli Yake Aliyetukuka:

وَالَّذِي قَدَّرَ فَهَدَىٰ ﴿٢٠﴾

**“Na Akakikadiria na Akakiongoa.” (87:3),**

Maana yake: Alikadiria kipimo kilichoandikwa na kuongoza viumbe, wakitembea bila kuweza kuepuka hilo wala hakuna anayeweza kutoka kwayo. Anasema Mola wetu Mlezi ambaye Ameumba viumbe na Aliyekadiria vipimo kwa kila mmoja na Kuvilazimisha viumbe kila Alitakalo.

قَالَ فَمَا بَالُ الْقُرُونِ الْأُولَىٰ ﴿٢١﴾

**“Akasema: Nini hali ya karne za kwanza?”**

Kauli iliyo sahihi kabisa kwa maana ya hilo ni kuwa pindi Musa عليه السلام alipomjulisha Firauni kuwa Mola wake Mlezi Aliyemtuma ni yule Anayeumba, Mwenye Kuruzuku, Anayekadiria na Kuongoa. Firauni alianza kujadili hayo kutumia mfano vizazi vilivyopita kama dalili yake. Alikuwa akikusudia vile vizazi vya zamani na awali waliomshirikisha Allah تعالى.

Kwa maana nyingine ni kuwa ikiwa jambo lao ni hilo, hawakumuabudu Mola wako Mlezi bali waliabudu asiyekuwa Yeye? Musa عليه السلام akamuambia yafuatayo katika kumjibu: Wao mbali na kuwa hawakumuabudu elimu yao iko pamoja na Allah تعالى, Anayejua hakika yao kwa yaliyotokea kwao, Naye Atawapatia jaza na ujira kwa matendo yao kama yalivyoandikwa katika Kitabu cha Allah تعالى. Nacho kinaitwa *Al-Lawhul Mahfuudh* (Ubao Uliohifadhiwa) na Kitabu (cha amali).

لَا يَضِلُّ رَبِّي وَلَا يَنسَىٰ ﴿٢٢﴾

**“Mola wangu Mlezi Hapotei wala Hasahau.”**

Maana yake: Hakuna kinachomkwepa wala hakimpiti kidogo wala kikubwa. Hasahau chochote na Eimu Yake Aliyetukuka inazunguka kila kitu. Na hakika Hasahau chochote, Aliyetukuka na Mtakatifu Asiye na kasoro yoyote ile. Bila shaka elimu ya viumbe ina dosari mbili. Ya kwanza, haizunguki kikamilifu chochote, na ya pili ni usahaulivu wake baada ya kuwa na elimu. Hivyo, Allah تعالى Ameitakasa Nafsi Yake juu ya kasoro hizo.

الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ الْأَرْضَ مَهْدًا وَسَلَكَ لَكُمْ فِيهَا سُبُلًا وَأَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجْنَا  
بِهِ أَزْوَاجًا مِنْ نَبَاتٍ شَتَّى ﴿٥٣﴾ كُلُوا وَارْزُقُوا أَنْعَمَكُمْ ۗ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ  
﴿٥٤﴾ \* مِنْهَا خَلَقْنَاكُمْ وَفِيهَا نُعِيدُكُمْ وَمِنْهَا نُخْرِجُكُمْ تَارَةً أُخْرَى ﴿٥٥﴾ وَلَقَدْ أَرَيْنَاهُ  
آيَاتِنَا كُلَّهَا فَكَذَّبَ وَأُولَى ﴿٥٦﴾

**53. Ambaye Amekufanyieni ardhi kuwa tandiko, na Akakupitishieni humo njia, na Akakuteremshieni kutoka mbinguni maji. Na kwa hayo Tukatoa namna mbali mbali za mimea.**

**54. Kuleni, na mchunge wanyama wenu. Hakika katika hayo zipo ishara kwa wenye akili.**

**55. Kutokana nayo (ardhi) Tumekuumbeni, na humo Tunakurudisheni, na kutoka humo Tutakutoeni mara nyengine.**

**56. Na hakika Tulimuonesha ishara Zetu zote. Lakini alikadhibisha na akakataa.**

### Kukamilika Jawabu la Musa عليه السلام kwa Firauni

Huu ni katika ukamilifu wa maneno ya Musa عليه السلام kama alivyomsifu Mola wake Mlezi pale Firauni alipomuuliza kuhusu Yeye (Allah تعالى). Musa عليه السلام akasema:

الَّذِي أَعْطَىٰ كُلَّ شَيْءٍ خَلْقَهُ ثُمَّ هَدَىٰ ﴿٥٧﴾

**“Yule aliyekipa kila kitu umbo lake, kisha Akakiongoa”.**

Kisha, Firauni akajaribu kupinga kwa kumrudi Musa عليه السلام. Kisha akasema: **“Ambaye Amekufanyieni ardhi kuwa kitanda kwa ajili yenu”**. Na katika kisomo cha baadhi yao, wanasoma: *“Mahdan”*, yenye maana ya sehemu ya mapumziko ambamo mnajituliza. Pia inaweza kumaanisha kile mnachosimama kwacho na kulala juu yake au kusafiri juu ya mgongo wake.

وَسَلَكَ لَكُمْ فِيهَا سُبُلًا

**“Na Akakupitishieni humo njia”**, Maana yake: Amejaalia njia mnazotembea katika pande zake kama Alivyosema Allah تعالى:

وَجَعَلْنَا فِيهَا فِجَاجًا سُبُلًا لَّعَلَّهُمْ يَهْتَدُونَ ﴿٣١﴾

**“Na Tukaweka humo mabarabara, waziwazi ili wapate kuongoza njia.” (21:31).**

وَأَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَأَخْرَجْنَا بِهِ أَزْوَاجًا مِّن نَّبَاتٍ شَتَّىٰ ﴿٣٢﴾

**“Na Akakuteremshieni kutoka mbinguni maji. Na kwa hayo Tukatoa namna mbali mbali za mimea.”**

Maana: Aina tofauti za miti, kama mimea na matunda. Mengine kati ya hayo ni chachu baadhi yao tamu na baadhi yao tena ni chungu na aina nyingine.

كُلُوا وَارْزُقُوا أَتَعْمَكُمُ ۗ

**“Kuleni, na mchunge wanyama wenu.”**

Maana yake: Ni chakula kwenu pamoja na matunda yanayoliwa, na baadhi yake ni chakula kwa wanyama wenu, yaliyo kijani na yaliokauka.

إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ

**“Hakika katika hayo zipo ishara.”**

Maana yake: Dalili na hoja,

لَأُولَىٰ الْآلِهَةِ ﴿٣٣﴾

**“Kwa wenye akili.”** Maana yake: Kwa wale wenye akili ya sawa na timamu wakitambua kuwa hakuna mungu anayepasa kuabudiwa ila Allah تعالى, na hakuna Mola Mlezi wa kweli isipokuwa Yeye.

﴿٣٤﴾ مِمَّا خَلَقْنَاكُمْ فِيهَا نُعِيدُكُمْ وَمِمَّا نُخْرِجُكُمْ تَارَةً أُخْرَىٰ ﴿٣٥﴾

**“Kutokana nayo (ardhi) Tumekuumbeni, na humo Tunakurudisheni, na kutoka humo Tutakutoeni mara nyengine.”**

Maana yake: Ardhi ndio chanzo chenu. Kwani baba yenu Adam عليه السلام, aliumbwa kutokana na mchanga wa juu ya ardhi. Nanyi pia mtarudishwa mchangani. Hii inamaanisha kuwa mtakuwa mchanga pindi mnapokufa na kuoza. Na kutoka humo Tutakutoeni mara nyengine tena.

يَوْمَ يَدْعُوكُمْ فَتَسْتَجِيبُونَ بِحَمْدِهِ وَتَظُنُّونَ إِن لَّبِئْتُمْ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٥٧﴾

**“Siku Atakapokuiteni, na nyinyi mkamuitikia kwa kumshukuru, na mkadhani kuwa hamkukaa ila muda mdogo tu.” (17:52).**

Na Aya hii ni sawa na Kauli Yake Aliyetukuka:

قَالَ فِيهَا تَحْيَوْنَ وَفِيهَا تَمُوتُونَ وَمِنهَا تُخْرَجُونَ ﴿٧﴾

**“Akasema (Allah): Mtaishi humo na mtafia humo na mtatolewa humo.” (7:25).**

**Firauni Alioneshwa Kila miujiza lakini Hakuamini**

Na Kauli Yake:

وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا آيَاتِنَا كُلَّهَا فَكَذَّبَ وَأَبَىٰ ﴿٥٨﴾

**“Na hakika Tulimuonesha ishara Zetu zote. Lakini alikadhibisha na akakataa.”**

Maana yake: Hoja, ishara na dalili zilisimamishwa dhidi ya Firauni, naye akazona kwa macho yake, lakini hata hivyo alizikadhibisha na kuzikataa kwa ukafiri na inadi na kwa kukengeuka, kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَجَحَدُوا بِهَا وَاسْتَيْقَنَتْهَا أَنفُسُهُمْ ظُلْمًا وَعُلُوًّا ﴿٥٩﴾

**“Na wakazikanusha, na hali ya kuwa nafsi zao zina yakini nazo kwa dhuluma na kujivuna.” (27:14).**

قَالَ أَجَعَلْتَنَا لِتُخْرِجَنَا مِنْ أَرْضِنَا بِسِحْرِكَ يَا مُوسَىٰ ﴿٦٠﴾ فَلَنَأْتِيَنَّكَ بِسِحْرِ مِثْلِهِ

فَأَجْعَلْ بَيْنَنَا وَبَيْنَكَ مَوْعِدًا لَا نُخْلَفُهُ نَحْنُ وَلَا أَنْتَ مَكَانًا سُوًى ﴿٦١﴾ قَالَ مَوْعِدُكُمْ

يَوْمَ الزَّيْنَةِ وَأَنْ تُحْشَرَ النَّاسُ ضُحًى ﴿٦٢﴾

**57. Akasema: Ewe Musa! Hivyo umetujia kututoa katika nchi yetu kwa uchawi wako?**

**58. Basi sisi hakika tutakuletea uchawi kama huo. Basi weka miadi baina yetu na wewe, ambayo tusiivunje sisi wala wewe, mahali patapokuwa sawa.**

**59. Akasema: Miadi yenu ni siku ya Sikukuu; na watu wakusanywe kabla ya adhuhuri.**

### **Firauni Anaelezea Miujiza ya Musa عليه السلام kuwa ni Uchawi**

Allah تعالى, Anatufahamisha yale aliyosema Firauni kumuambia Musa عليه السلام alipomuonesha muujiza mkubwa. Muujiza huu mkubwa ulikuwa ni ule wa Musa عليه السلام kwa Firauni kwa kutupa chini fimbo yake, nayo ikabadilika kuwa nyoka mkubwa na kuutoa mkono wake ubavuni mwake, ilhali unang'aa kwa weupe pasi na ugonjwa. Kwa haya, Firauni alisema: "Huu ni uchawi uliotuletea kuturoga na kuwateka watu ili wakufuate. Baada ya hapo mutatuzidi kwa idadi". Firauni hapo alisema: "Mkakati wako utaruka patupu. Tuna uchawi kama wako, hivyo usidanganyike kwa unayoyafanya". Hivyo,

فَأَجْعَلْ بَيْنَنَا وَبَيْنَكَ مَوْعِدًا

**"Basi weka miadi baina yetu na wewe."**

Maana yake: Siku ambayo tutakuja pamoja ili kuonesha uchawi wetu dhidi ya wako. Hilo litafanyika katika sehemu na wakati maalumu. Kwa haya, Musa عليه السلام aliwaambia:

مَوْعِدُكُمْ يَوْمَ الزَّيْنَةِ

**"Miadi yenu ni siku ya Sikukuu".**

Hiyo ilikuwa ni siku yao ya sherehe na sikukuu yao ya mwaka mpya. Ilikuwa ni sikukuu yao walipokuwa wanachukua likizo kwa kutofanya kazi na kuja pamoja kwa mkusanyiko mkubwa. Siku hii ilichaguliwa ili watu wote waweze kushuhudia Nguvu za Allah تعالى za Kuweza Kufanya Atakalo. Wataweza kuona miujiza ya Manabii na kutofua dafu uchawi katika kushindana na uwezo usiokuwa wa kawaida wa nguvu za unabii.

Hii ndio sababu ya Musa عليه السلام kusema:



وَأَنْ تُحَشِّرَ النَّاسُ

**“Na watu wakusanywe.”**

Maana yake: Watu wote.

ضُحًى

**“Kabla ya Adhuhuri.”**

Maana yake: Asubuhi, kabla ya mchana (Adhuhuri). Kwa njia hii mashindano hayo yataonekana kwa uwazi kabisa, dhahiri na kuonekana kwa wazi kabisa. Hii ndio njia ya Manabii. Kazi yao kwa wakati wote ni wazi, dhahiri na yenye kuonekana wala si kitu kilichofichika, au chenye mazingaombwe. Hii ndio sababu hakusema mkutano huo ufanyike usiku, bali, ulikuwa ufanyike sehemu ya asubuhi yenye muangaza. Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Siku yao ya sherehe ilikuwa ni siku ya Ashuraa”<sup>1</sup>. As-Suddiy, Qataadah na Ibn Zayd wamesema: “Ilikuwa ni siku yao ya sherehe kubwa”. Sa’id bin Jubayr amesema: “Ilikuwa ni siku yao kubwa ya soko”. Kauli hizi hazigongani. Nasema kuwa Allah تعالى Alimuangamiza Firauni na jeshi lake kwa siku sawa na hii kama ilivyoyakinishwa katika Hadithi Sahihi<sup>2</sup>.

‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam amesema: “Hiyo ilikuwa ni sehemu tambarare, mahali ambapo watu wote walikuwa katika usawa mmoja uliolingana wa kuweza kuona tukio linaloendelea sawasawa. Hakukuwa na chochote ambacho kingeweza kukingwa kuona kwa baadhi ya watu dhidi ya wengine.”<sup>3</sup>

\* \* \*

<sup>1</sup> Ad-Durr al-Manthuur 4:540, Nayo ni tarehe 10 katika mwezi wa kwanza katika kalenda ya Kiislamu (*Muharram*).

<sup>2</sup> Fat’h Al-Baariy 8:288.

<sup>3</sup> At-Tabari 18:323.

فَتَوَلَّى فِرْعَوْنُ فَجَمَعَ كَيْدَهُ ثُمَّ أَتَى ﴿٦٠﴾ قَالَ لَهُمُ مُوسَى وَيْلَكُمْ لَا تَفْتَرُوا عَلَى اللَّهِ كَذِبًا فَيُسْحِتَكُمْ بِعَذَابٍ ۗ وَقَدْ خَابَ مَنِ افْتَرَى ﴿٦١﴾ فَتَنَزَّعُوا أَمْرَهُمُ بَيْنَهُمْ وَأَسْرُوا النَّجْوَى ﴿٦٢﴾ قَالُوا إِنْ هَذَا لَسِحْرَانِ يُرِيدَانِ أَنْ يُخْرِجَاكُم مِّنْ أَرْضِكُمْ بِسِحْرِهِمَا وَيَذْهَبَا بِطَرِيقَتِكُمُ الْمُثَلَّى ﴿٦٣﴾ فَأَجْمَعُوا كَيْدَكُمْ ثُمَّ اتُّوُوا صَفًّا ۖ وَقَدْ أَفْلَحَ الْيَوْمَ مَنِ اسْتَعْلَى ﴿٦٤﴾ قَالُوا يَا مُوسَى إِمَّا أَنْ تُلْفَىٰ وَإِمَّا أَنْ نَكُونَ أَوَّلَ مَنْ أَلْفَىٰ ﴿٦٥﴾ قَالَ بَلْ أَلْفَوْا ۗ وَإِذَا حِينَاهُمْ وَعَصِيَّهُمْ يَخْتَلُ إِلَيْهِ مِنْ سِحْرِهِمْ إِنَّمَا تَسْعَىٰ ﴿٦٦﴾ فَأَوْجَسَ فِي نَفْسِهِ خِيفَةً مُّوسَى ﴿٦٧﴾ قُلْنَا لَا تَخَفْ إِنَّكَ أَنْتَ الْأَعْلَىٰ ﴿٦٨﴾ وَأَلْقِ مَا فِي يَمِينِكَ تَلْقَفْ مَا صَنَعُوا ۗ إِنَّمَا صَنَعُوا كَيْدٌ سَاحِرٌ وَلَا يُفْلِحُ السَّاحِرُ حَيْثُ أَتَىٰ ﴿٦٩﴾ فَأَلْفَى السَّحْرَةَ سَجْدًا قَالُوا ءَامَنَّا بِرَبِّ هَارُونَ وَمُوسَى ﴿٧٠﴾ قَالَ ءَامَنُمْ لَهُ قَبْلَ أَنْ ءَاذَنَ لَكُمْ ۗ إِنَّهُ لَكَبِيرِكُمْ الَّذِي عَلَّمَكُمُ السِّحْرَ ۗ فَلَا تُقْطِعْ أَيْدِيَكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ مِّنْ خَلْفٍ وَلَا صَلِّبِكُمْ فِي جُدُوعِ النَّخْلِ وَلِتَعْلَمَنَّ أَنِنَّا أَشَدُّ عَذَابًا وَأَبْقَىٰ ﴿٧١﴾ قَالُوا لَنْ نُؤْذِرَكَ عَلَىٰ مَا جَاءَنَا مِنَ الْيَقِينِ وَالَّذِي فَطَرَنَا فَاقْضِ مَا أَنْتَ قَاضٍ ۗ إِنَّمَا تَقْضِي هَذِهِ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ﴿٧٢﴾ إِنَّا ءَامَنَّا بِرَبِّنَا لِيَغْفِرَ لَنَا خَطِيئَاتِنَا وَمَا أَكْرَهْتَنَا عَلَيْهِ مِنَ السِّحْرِ ۗ وَاللَّهُ خَبِيرٌ وَأَبْقَىٰ ﴿٧٣﴾

فَتَوَلَّى فِرْعَوْنُ فَجَمَعَ كَيْدَهُ ثُمَّ أَتَى ﴿٦٠﴾ قَالَ لَهُمُ مُوسَى وَيْلَكُمْ لَا تَفْتَرُوا عَلَى اللَّهِ كَذِبًا فَيُسْحِتَكُمْ بِعَذَابٍ ۗ وَقَدْ خَابَ مَنِ افْتَرَى ﴿٦١﴾ فَتَنَزَّعُوا أَمْرَهُمُ بَيْنَهُمْ وَأَسْرُوا النَّجْوَى ﴿٦٢﴾ قَالُوا إِنْ هَذَا لَسِحْرَانِ يُرِيدَانِ أَنْ يُخْرِجَاكُم مِّنْ أَرْضِكُمْ بِسِحْرِهِمَا وَيَذْهَبَا بِطَرِيقَتِكُمُ الْمُثَلَّى ﴿٦٣﴾ فَأَجْمَعُوا كَيْدَكُمْ ثُمَّ اتُّوُوا صَفًّا ۖ وَقَدْ أَفْلَحَ الْيَوْمَ مَنِ اسْتَعْلَى ﴿٦٤﴾

60. Basi Firauni akarudi na akatengeneza hila yake, kisha akaja.

61. Musa akawaambia: Ole wenu! Msimzulie Allah uwongo, Asije akakufutilieni mbali kwa adhabu. Na mwenye kuzua lazima ashindwe!

62. Basi wakazozana kwa shauri yao wenyewe kwa wenyewe, na wakano-ng'ona kwa siri.

**63. Wakasema: Hakika hawa wawili ni wachawi, wanataka kukutoeni katika nchi yenu kwa uchawi wao, na waondoe mila zenu zilizo bora kabisa.**

**64. Kwa hivyo kusanyeni hila zenu zote, kisha mfike kwa kujipanga safu, na kwa yakini atafuzu kweli kweli leo atakayeshinda.**

### **Pande Mbili Zakutana na Wito wa Musa عليه السلام kwa Wachawi**

Allah تعالى Anatufahamisha kuwa pale Firauni na Musa عليه السلام walipokubaliana kukutana katika mahali maalumu na wakati maalum, Firauni alianza kuwakusanya baadhi ya wachawi kutoka katika miji ya ufalme wake. Mtu yeyote aliyekuwa na ujuzi wa uchawi wakati huo aliitwa, uchawi wakati huo ulikuwa umeenea na kuhitajika sana.

Hii ni sawa na Kauli ya Aliyetukuka:

وَقَالَ فِرْعَوْنُ أَتَأْتُونِي بِكُلِّ سِحْرِ عَلَيْهِ ۝٧٩

**“Na Firauni akasema: Nileteeni kila mchawi hodari.” (10:79).**

Kisha, siku hiyo ikafika. Hiyo ilikuwa ni siku iliyojulikana ambapo watu wote walikuwa wanakusanyika, ikiwa ni siku ya sherehe. Firauni alikuwa amekaa juu ya kiti chake cha enzi akiwa amezungukwa na wakuu miongoni mwa tabaka la juu katika watu wa ufalme wake. Wananchi wote walikuwa wamesimama kuliani na kushotoni mwake. Kisha, Musa عليه السلام alikuja mbele akiwa ameegemea fimbo yake akiwa amefuatana na nduguye, Haarun عليه السلام. Wachawi walikuwa wamesimama mbele ya Firauni kwa safu, naye (Firauni) alikuwa anawachochea, kuwashawishi na kuwahimiza kufanya vyema siku hiyo. Walitaka kumridhisha, naye (Firauni) aliwaahidi na kuwatia hima. Wakasema:

أَلَيْسَ لَنَا لَأَجْرًا إِنْ كُنَّا نَحْنُ الْغَالِبِينَ ۝ قَالَ نَعَمْ وَإِنِّكُمْ إِذَا لَمِنَ الْمُقْرَبِينَ ۝٨٠

**“Je, tutapata ujira tukiwa sisi ndio tulioshinda? Akasema: Ndio, na pia mtakuwa miongoni mwa wale wanaowekwa mbele (katika dola yangu).” (26:41-42).**

قَالَ لَهُم مُوسَى وَيَلِكُمْ لَا تَفْتَرُوا عَلَى اللَّهِ كَذِبًا

**“Musa akawaambia: Ole wenu! Msimzulie Allah uongo.”**

Maana yake: Msilete uongo mbele ya watu kwa kitu kisichokuwa cha kweli, kufanya kionekane kama ni kiumbe, ilhali si kiumbe. Hakika mkifanya hivyo, mtakuwa mnamzulia uongo Allah تعالى.

فَيَسْجِتْكُمْ بَعْدَآبِ

**“Asije Akakufutilieni mbali kwa adhabu.”**

Maana yake: Atawaangamiza kwa adhabu iangamizayo ambayo haitaacha chochote wala yeyote.

وَقَدْ خَابَ مَنْ أَفْتَرَى ﴿٦٠﴾ فَتَنْزَعُوا أَمْرَهُم بَيْنَهُمْ

**“Na mwenye kuzua lazima ashindwe! Basi wakazozana kwa shauri yao wenyewe kwa wenyewe”.**

Panasemwa kuwa hii inamaanisha walibishana baina yao. Hivyo, mmoja wao akasema: “Haya si mazungumzo ya mchawi, bali ni maneno ya Nabii”. Mwingine akasema: “Hapana, yeye ni mchawi tu”. Zipo rai nyingine ambazo zimetajwa kuhusu waliyozungumza. Na Allah تعالى Anajua zaidi. Na Kauli Yake:

وَأَسْرُوا النَّجْوَى ﴿٦١﴾

**“Na wakanong’ona kwa siri.”** Maana yake: Walifanya mashauri ya siri baina yao kuhusu jambo hili.

قَالُوا إِنَّ هَذَا لَسَجْرَانِ

**“Wakasema: Hakika hawa wawili ni wachawi.”**

Hii ni njia ya uzungumzi kwa baadhi ya Waarabu na Aya hii imesomwa kulingana na sarufi ya lahaja yao. Wapo wengine wanaoisoma:

(إِنَّ هَذَيْنِ لَسَاجِرَانِ)

“Inna Haadhayni lasaahiraani”

Ambayo ina maana sawa, **“Hakika, hawa ni wachawi wawili”**. Huu ndio muundo maarufu wa sarufi ya lugha ya Kiarabu. Waliobobea katika sarufi wamekuwa na mjadala na mazungumzo ya kina kujibu kisomo cha kwanza na maelezo yake ya kisarufi, lakini hapa si mahali pa mazungumzo hayo. Nukta muhimu ni kuwa wachawi walisememzana: “Nyote mwajua kuwa mtu huyu na nduguye (Musa عليه السلام na Haarun عليه السلام) ni wachawi wawili walio wajuzi (na elimu) walio na uzoefu na utaalumu wa uchawi. Wanataka kukushindeni nyinyi na watu wenu leo na kuwatawala watu, hivyo kuwafanya raia kuwafuata wao. Wanataka kupigana dhidi ya Firauni na jeshi lake, nao wanataka ushindi juu yake. Na hakika lengo lao ni kuwatoa nyinyi nchini mwenu”. Kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

وَيَذْهَبَا بِطَرِيقَتِكُمُ الْمُتْلَىٰ ﴿٦٠﴾

**“Na waondoe mila zenu zilizo bora kabisa.”**

Maana yake: Wanataka kuzifuta desturi zenu waziwazi, ambazo ni uchawi. Kwa hakika, wanatambulika kuwa wakubwa kwa sababu ya uchawi wao. Walikuwa na mali na riziki kwa sababu ya uchawi. Kwa hakika walikuwa wanasema: “Ikiwa hawa wawili (Musa عليه السلام na Haarun عليه السلام) watashinda, watakuangamizeni na kukutoeni kutoka nchini kwenu. Kwa kufanya hivyo, watakuwa watu wa kwanza kufanya hivyo, nao watapewa uwezo mkubwa wa uongozi bila nyinyi”. Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما ametaja yafuatayo kuhusu Kauli ya Allah تعالى:

وَيَذْهَبَا بِطَرِيقَتِكُمُ الْمُتْلَىٰ ﴿٦٠﴾

**“Na waondoe mila zenu zilizo bora kabisa.”**

Maana yake: Ufalme wao, waliokuwa ndani yake na maisha yao<sup>1</sup>. ‘Abdur-Rahman bin Zayd amesema: “Njia hii bora inamaanisha yale waliokuwa juu yake (waliokuwa wakiyatenda)”.

فَأَجْمِعُوا كَيْدَكُمْ ثُمَّ آتُوا صَفَاً

**“Kwa hivyo kusanyeni hila zenu zote, kisha mfike kwa kujipanga safu...”**

<sup>1</sup> An-Nasaa’iy katika Al-Kubraa 6:396.

Maana yake: Nyote njooni katika safu moja, na tupeni fimbo zilizokuwa mikononi mwenu kwa wakati mmoja kwa ajili ya kuduwaza macho (ya watu) na kumshinda mtu huyu na nduguye.

وَقَدْ أَفْلَحَ الْيَوْمَ مَنْ أَسْتَعْلَىٰ ﴿٦٥﴾

**“Na kwa yakini atafuzu kweli kweli leo atakayeshinda.”**

Maana yake: baina yako na sisi. Ama kuhusu sisi (wachawi), tumeahidiwa kupatiwa nguvu nyingi na utawala. Na ama kuhusu yeye (Musa عليه السلام), atapata uongozi mkubwa.

قَالُوا يَمُوسَىٰ إِمَّا أَنْ تُلْقَىٰ وَإِمَّا أَنْ نَكُونَ أَوْلَ مَنْ أَلْقَىٰ ﴿٦٥﴾ قَالَ بَلْ أَلْقُوا ۗ فَإِذَا  
 حِبَاهُمْ وَعَصِيْبُهُمْ مُّخَيَّلٌ إِلَيْهِ مِنْ سِحْرِهِمْ أَنهَا تَسْعَىٰ ﴿٦٦﴾ فَأَوْجَسَ فِي نَفْسِهِ خِيفَةً  
 مُّوسَىٰ ﴿٦٧﴾ قُلْنَا لَا تَخَفْ إِنَّكَ أَنْتَ الْأَعْلَىٰ ﴿٦٨﴾ وَأَلْقِ مَا فِي يَمِينِكَ تَلْقَفْ مَا صَنَعُوا  
 ۗ إِنَّمَا صَنَعُوا كَيْدٌ سَاحِرٌ ۗ وَلَا يُفْلِحُ السَّاحِرُ حَيْثُ أَتَىٰ ﴿٦٩﴾ فَأَلْقَى السَّحْرَةَ سُجُودًا قَالُوا  
 ءَأَمْنَا بِرَبِّ هَارُونَ وَمُوسَىٰ ﴿٧٠﴾

**65. Wakasema: Ewe Musa! Je! Utatupa wewe, au tutakuwa sisi wa kwanza kutupa?**

**66. Akasema: Bali tupeni nyinyi! Tahamaki kamba zao na fimbo zao zikaonekana mbele yake, kwa uchawi wao, kuwa zinapiga mbio.**

**67. Basi Musa akaingia khofu nafsi yake.**

**68. Tukasema: Usikhofu! Hakika wewe ndiye utakayeshinda.**

**69. Na kitupe kilicho katika mkono wako wa kulia; kitavimeza walivyoviunda. Hakika walivyounda ni hila za mchawi tu, na mchawi hafanikiwi popote afikapo.**

**70. Basi wachawi wakaanguka wanasujudu. Wakasema: Tumemuamini Mola Mlezi wa Haarun na Musa!**

**Mpambano, Ushindi wa Musa عليه السلام na Imani ya Wachawi**

Allah تعالى Anatarifu kuhusu wachawi walipokutana na Musa عليه السلام, nao walimuambia Musa عليه السلام,

إِمَّا أَنْ تُتْلَىٰ

*“Je, utatupa wewe mwanzo.”* Maana yake: Anza wewe mwanzo.

وَإِمَّا أَنْ نَكُونَ أَوَّلَ مَنْ أَلْقَىٰ ﴿٢٠﴾ قَالَ بَلْ أَلْقَوُا

*“Au tutakuwa sisi wa kwanza kutupa? Akasema: Bali tupeni nyinyi!”*

Maana yake: Nyinyi anzeni mwanzo ili tupate kuona uchawi wenu mtakaotuoonesha na ili hali khalisi wa jambo lao liwe wazi kwa watu.

فَإِذَا حِبَاهُمْ وَعَصِيئُهُمْ تُخِيلُ إِلَيْهِ مِنْ سِحْرِهِمْ أَنهَاسَعَىٰ ﴿٢١﴾

*“Tahamaki kamba zao na fimbo zao zikaonekana mbele yake, kwa uchawi wao, kuwa zinapiga mbio.”*

Na katika Aya nyingine inasema kuwa pindi waliporusha,

وَقَالُوا بِعِزَّةِ فِرْعَوْنَ إِنَّا لَنَحْنُ الْغَالِبُونَ ﴿٢٢﴾

*“Na wakasema: Kwa nguvu za Firauni sisi tutakuwa ndio wenye kushinda.” (26:44)*

Na Amesema Aliyetukuka:

سَحَرُوا أَعْيُنَ النَّاسِ وَأَسْتَرَهُبُهُمْ وَجَاءُوا بِسِحْرِ عَظِيمٍ ﴿٢٣﴾

*“Waliyazuga macho ya watu na wakawaogopesha, na wakaleta uchawi mkubwa.” (7:116).*

Na hapa Anasema:

فَإِذَا حِبَاهُمْ وَعَصِيئُهُمْ تُخِيلُ إِلَيْهِ مِنْ سِحْرِهِمْ أَنهَاسَعَىٰ ﴿٢٤﴾

*“Tahamaki kamba zao na fimbo zao zikaonekana mbele yake, kwa uchawi wao, kuwa zinapiga mbio.”*

Walikuwa ni kundi kubwa na kila mmoja wao alirusha fimbo na kamba hadi uwanja huo ukajaa nyoka mmoja juu ya mwengine. Na Kauli Yake:

﴿ فَأَوْجَسَ فِي نَفْسِهِ خِيفَةً مُّوسَىٰ ﴾

***“Basi Musa akaingia khofu nafsi yake.”***

Maana: Alikhofia kuwa watu watajaribiwa na kudanganywa na uchawi wao kabla yake kuweza hata kuwa na nafasi ya kutupa alichokuwa nacho kwenye mkono wake wa kulia. Hivyo, Allah تعالی Alimfunulia kwa wakati mnasibu.

﴿ وَأَلْقَىٰ مَا فِي يَمِينِكَ ﴾

***“Na kitupe kilicho katika mkono wako wa kulia...”***

Nayo ilikuwa ni fimbo. Alipofanya hivyo.

﴿ تَلَقَّفَ مَا صَنَعُوا ﴾

***“Kitavimeza walivyoviunda...”***

Na fimbo hiyo ikageuka kuwa kiumbe mkubwa sana, mwenye miguu, shingo, kichwa na chonge. Lilifuata kamba na fimbo hizo mpaka haikubakia hata moja isipokuwa zilimezwa na mnyama huyo. Wakati huo huo, wachawi na watu walikuwa wakitizama kwa macho yao, wakiona tukio hili la ajabu mchana wa muangaza. Hivyo, muujiza ulifanywa na dalili pamoja na ishara ilikuwa wazi na dhahiri kabisa. Haki ikashinda na uongo wa uchawi ukadhihiri. Na kwa hiyo, Allah تعالی Akasema:

﴿ إِنَّمَا صَنَعُوا كَيْدٌ سَجِرٌ ۖ وَلَا يُفْلِحُ السَّاجِرُ حَيْثُ أَتَىٰ ﴾

***“Hakika walivounda ni hila za mchawi tu, na mchawi hafanikiwi popote afikapo.”***

Hivyo, pindi wachawi walipoliona tukio hilo na kulishuhudia kwa macho yao, ilhali walikuwa ni wajuzi kwa aina tofauti ya hila na njia za sayansi ya uchawi walijua kwa yakini kuwa aliyoyafanya Musa عليه السلام si uchawi au hila. Walitambua kuwa hilo ni kweli bila ya shaka yoyote. Walijua kuwa hakuna mwenye nguvu na uwezo kufanya hilo ila Yule Anayekiambia kitu: “Kuwa”, nacho kikawa. Kwa hiyo, lilipotokea hili, walianguka na kumsujudia Allah تعالی.



Hapo wakasema: ***“Tunamuamini Mola wa walimwengu wote. Mola Mlezi wa Musa عليه السلام na Haarun عليه السلام.”*** (26:47-48). Kwa ajili hiyo alisema Ibn ‘Abbaas na ‘Ubayd bin ‘Umayr: “Mwanzo wa siku walikuwa ni wachawi na mwisho wa siku wakawa ni mashahidi wema wa Imani.”<sup>1</sup>

### Idadi ya Wachawi

Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى amepokea kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Wachawi walikuwa ni watu sabiini asubuhi yake walikuwa wachawi lakini jioni wakawa ni mashahidi wa Imani.”<sup>2</sup> Imepokewa na Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى kutoka kwa Al-Awzaa’iy رحمه الله تعالى amesema: “Pindi wachawi walipoanguka kusujudu, Pepo ilinyanyuliwa mbele yao mpaka wakawa wanaitizama.”<sup>3</sup> Na pia imepokewa kutoka kwa Sa’id bin Jubayr kuhusu Kauli Yake:

فَأَلْقَى السَّحْرَةَ سُجَّدًا

***“Basi wachawi wakaanguka wanasujudu.”*** Waliona wazi kabisa mahali (pao Peponi) wakiwa katika sijda. Na hivyo ndivyo walivyosema ‘Ikrimah na Al-Qaasim bin Abi Bizzah<sup>4</sup>.

قَالَ ءَامَنَّمْ لَهُ قَبْلَ أَنْ ءَاذَنَ لَكُمْ إِنَّهُ لَكَبِيرٌ كُمُ الَّذِي عَلَّمَكُمُ السِّحْرَ فَلَأَقْطِعَنَّ  
 أَيْدِيَكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ مِمَّنْ خَلَفَ وَلَاصَلْبَتِكُمْ فِي جُدُوعِ النَّخْلِ وَلِتَعْلَمَنَّ أَيُّنَا أَشَدُّ عَذَابًا  
 وَأَتَقَى ﴿٦٦﴾ قَالُوا لَنْ نُؤْتِرَكَ عَلَىٰ مَا جَاءَنَا مِنَ الْبَيِّنَاتِ وَالَّذِي فَطَرَنَا فَاقْضِ مَا أَنْتَ  
 قَاضٍ إِنَّمَا تَقْضِي هَذِهِ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ﴿٦٧﴾ إِنَّا ءَامَنَّا بِرَبِّنَا لِيَغْفِرَ لَنَا خَطِيئَتَنَا وَمَا  
 أَكْرَهْتَنَا عَلَيْهِ مِنَ السِّحْرِ ۗ وَاللَّهُ خَبِيرٌ وَأَتَقَى ﴿٦٨﴾

**71. (Firauni) akasema: Oh! Mmemuamini kabla sijakupeni ruhusa? Hakika yeye ndiye mkubwa wenu aliyekufundisheni uchawi. Basi kwa yakini nitakukateni mikono yenu na miguu yenu kwa kutafautisha. Na nitakutundikeni misalabani katika vigogo vya mitende, na hapo kwa yakini mutajua ni nani katika sisi aliye mkali wa kuadhibu na kuiendeleza adhabu yake.**

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:340, 13:36.

<sup>2</sup> Ibn Abi Haatim 7:2428.

<sup>3</sup> Ibn Abi Haatim 7:2428.

<sup>4</sup> Atw-Twabariy 18:334.

**72. Wakasema: Hatutokukhiari wewe kuliko ishara waziwazi zilizotujia, na kuliko yule aliyetuumba. Basi hukumu utavyo hukumu; kwani wewe unahukumu haya ya maisha ya duniani tu.**

**73. Hakika sisi tumemuamini Mola wetu Mlezi ili atusamehe makosa yetu na uchawi uliotulazimisha kuufanya. Na Allah Ndiye Mbora na Mwenye kudumu zaidi.**

### **Firauni Kuwageukia Wachawi, Kuwatisha na Jawabu lao Kwake**

Allah تعالى Anatuieleza kuhusu ukafiri wa Firauni, inadi yake, kuchupa mipaka na kiburi dhidi ya haki na ukweli kwa kufuata uongo. Alipoona kwa muujiza na ishara kubwa, na akawaona wale aliotaka usaidizi wake wamesilimu na kufuata njia ya Imani mbele ya watu wote, naye akiwa ameshindwa kabisa, hapo alionesha kiburi chake na kuanza kushutumu. Alianza kutumia cheo chake na nguvu zake dhidi ya wachawi. Aliwaonya na kuwatisha kwa kuwaambia:

ءَامَنَّمْ لَهُد

**“Mnamuamini yeye.”** Maana yake: Mmemsadikisha yeye?

قَبْلَ أَنْ ءَاذَنَ لَكُمْ

**“Kabla sijakupeni ruhusa.”** Maana: Nami sijawaamuru kufanya hivyo, kwa njia hiyo mumeniasi. Baada ya hapo, alisema kauli ambayo yeye mwenyewe, wachawi na viumbe vyote walitambua kuwa huo ni uongo na uzushi.

إِنَّهُ لَكَبِيرُكُمْ الَّذِي عَلَّمَكُمُ السِّحْرَ

**“Hakika yeye ndiye mkubwa wenu aliyekufundisheni uchawi.”**

Maana yake: Nyote mmejifunza uchawi kutoka kwa Musa عليه السلام, nanyi mumepatana naye dhidi yangu na watu wangu, ili mumsaidie yeye apate kushinda. Allah تعالى Anatuambia katika Aya nyingine:

إِنَّ هَذَا لَمَكْرٌ مَّكْرَتُمُوهُ فِي الْمَدِينَةِ لِتُخْرِجُوا مِنْهَا أَهْلَهَا فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿١٢٣﴾

**“Hii ndiyo hila muliyoifanya mjini (nyinyi na Musa) ili muwatoe humo wenyewe (ili mubakie nyinyi) lakini mtajua nini nitakufanyieni.” (7:123)**

Kisha akaanza kuwatisha, akawaambia:

فَلَا قُطِّعَ أَيْدِيكُمْ وَأَرْجُلُكُمْ مِّنْ خَلْفٍ وَلَا صَلِّبَتْكُمْ فِي جُدُوعِ النَّخْلِ

***“Basi kwa yakini nitakukateni mikono yenu na miguu yenu kwa kutafautisha. Na nitakutundikeni msalabani katika vigogo vya mitende.”***

Maana yake: Bila shaka nitafanya mfano kutoka kwenu, nami nitawaua hadharani. Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Hivyo, akawa mtu wa kwanza kua hadharani (kusulubu)”. Hii imeripotiwa na Ibn Abi Haatim <sup>1</sup>رحمته الله تعالى.

وَلَتَعْلَمَنَّ أَيُّنَا أَشَدُّ عَذَابًا وَأَبْقَى ﴿٦٧﴾

***“Na hapo kwa yakini mtajua ni nani katika sisi aliye mkali wa kuadhibu na kuiendeleza adhabu yake.”***

Maana yake: Munasema kuwa watu wangu na mimi mwenyewe tumepotea, na kuwa nyinyi (wachawi), Musa عليه السلام na watu wake wanafuata uongofu wa kweli, lakini mtakuja jua nani atakayeadhibiwa na kubaki kuadhibiwa. Hivyo alipowashambulia na hili na kuwatisha, roho zao zilitulia kwa sababu ya Imani yao kwa Allah تعالى. Hapo walimaka,

قَالُوا لَنْ نُؤْثِرَكَ عَلَيَّ مَا جَاءَنَا مِن بَيْنِ أَيْدِيكَ

***“Wakasema: Hatutokukhiari wewe kuliko ishara waziwazi zilizotujia.”***

Maana yake: Hatukuchagui wewe juu ya uongofu na ukweli uliotujia.

وَالَّذِي فَطَرَنَا

***“Na kuliko Yule Aliyetuumba”.***

Huenda wakawa wanaapa, “Kwa Yule Aliyetuumba sisi”. Pia huenda ikawa inahusiana na miujiza ya wazi yaliyotajwa kabla yake. Kwa hali hii itamaanisha, “Hatukufadhilishi wewe juu ya Muanzilishi na Muumba, Aliyetuumba kuanzia mwanzo tulipokuwa si chochote. Ametuumba kutokana na udongo. Kwa hiyo, Yeye Ndiye Anayestahiki kuabudiwa na Kunyenyekeka na sio wewe (Firauni).

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 13:34.

فَأَقْضِ مَا أَنْتَ قَاضٍ<sup>ط</sup>

**“Basi hukumu utavyohukumu”.**

Fanya utakalo na lolote ambalo laweza kufanywa na mikono yako.

إِنَّمَا تَقْضِي هَذِهِ الْحَيَاةَ الدُّنْيَا ﴿٧٧﴾

**“Kwani wewe unahukumu haya ya maisha ya duniani tu.”**

Maana: Wewe una uwezo na nguvu hapa duniani tu, na hii dunia itafika kikomo chake. Hakika sisi tuna matumaini ya nyumba ya milele ya Kesho Akhera.

إِنَّا ءَامَنَّا بِرَبِّنَا لِيَغْفِرَ لَنَا خَطْبَيْنَا

**“Hakika sisi tumemuamini Mola wetu Mlezi ili Atusamehe makosa yetu”.**

Kwa makosa yoyote tuliyofanya. Hii hasa inamaanisha, “ambayo ulitulazimisha kutekeleza uchawi, ili kupinga ishara na dalili za Allah تعالى na muujiza wa Mtume Wake”. Amepokea Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema yafuatayo kuhusu Kauli Yake Aliyetukuka:

وَمَا أَكْرَهْتَنَا عَلَيْهِ مِنَ السِّحْرِ<sup>ط</sup>

**“Na uchawi uliotulazimisha kuufanya’.**

Firauni alichukua vijana arobaini (40) kutoka kwa wana wa Israili na kuamrisha wafundishwe uchawi Al-Farama<sup>1</sup>. Akasema: ‘Wafundisheni wao elimu ambayo haijulikani na yeyote katika ardhi’. Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kisha akasema: ‘Hao walikuwa wale waliomuamini Musa عليه السلام, na ndio waliosema,

ءَامَنَّا بِرَبِّنَا لِيَغْفِرَ لَنَا خَطْبَيْنَا وَمَا أَكْرَهْتَنَا عَلَيْهِ مِنَ السِّحْرِ<sup>ط</sup>

**‘Hakika sisi tumemuamini Mola wetu Mlezi ili Atusamehe makosa yetu. Na uchawi uliotulazimisha kuufanya.’<sup>2</sup>”**

<sup>1</sup> Ni ngome ufukoni mwa bahari, Misri, baina Al-Arish, ambao ni mji kaskazini mwa Misri, kwenye Bahari ya Mediterenia na Al-Fustat. Na huu ni mji wa Kiislamu mkongwe kusini mwa Cairo ya sasa.

<sup>2</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 5:587.

'Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam amesema hivyo hivyo<sup>1</sup>. Na Kauli ya Aliyetukuka:

وَاللَّهُ خَيْرٌ وَأَبْقَىٰ

***“Na Allah Ndiye Mbora na Mwenye kudumu zaidi.”***

Maana yake: Yeye ni Mbora kwetu kuliko wewe.

وَأَبْقَىٰ

***“Na Mwenye kudumu zaidi.”***

Maana yake: Inadumu zaidi katika ujira na thawabu kuliko uliyoahidi na kutufanya sisi tutamani. Ni dhahiri kuwa Firauni (Allah تعالیٰ Amlaani) aliazimia kuwaadhibu, na yale aliyowafanyia ni kwa Rehema ya Allah تعالیٰ kwao. Hii ndio sababu kwa Ibn 'Abbaas na wengine miongoni mwa watangu wema kusema: “Waliamka asubuhi wakiwa wachawi, lakini wakawa mashahidi (wa Imani) jioni.”

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:341.

إِنَّهُ مَن يَأْتِ رَبَّهُ مُجْرِمًا فَإِنَّ لَهُ جَهَنَّمَ لَا يَمُوتُ فِيهَا وَلَا يَحْيَىٰ ﴿٧٤﴾ وَمَن يَأْتِهِ مُؤْمِنًا قَدْ عَمِلَ الصَّالِحَاتِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الدَّرَجَاتُ الْعُلَىٰ ﴿٧٥﴾ جَنَّاتُ عَدْنٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ۗ وَذَٰلِكَ جَزَاءُ مَن تَزَكَّىٰ ﴿٧٦﴾ وَلَقَدْ أَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ أَن أَسْرِ بِعِبَادِي فَاصْرَبْ لَهُم مَّطَرِبًا فِي الْبَحْرِ يَبَسًا لَا تَخَفُ دَرَكًا وَلَا تَخْشَىٰ ﴿٧٧﴾ فَأَتَيْنَهُم فِرْعَوْنُ بِجُنُودِهِ فَغَشِيَهُم مِّنَ اللَّيْلِ مَا عَاشَيْهِمْ ﴿٧٨﴾ وَأَصْلًا فِرْعَوْنُ قَوْمَهُ وَمَا هَدَىٰ ﴿٧٩﴾ يَبْنَئِي إِسْرَاءِيلَ قَدْ أَنْجَيْنَاكَم مِّنْ عَدُوِّكُمْ وَوَعَدْنَاكُمْ جَانِبَ الطُّورِ الْأَيْمَنِ وَنَزَّلْنَا عَلَيْكُمُ الْمَنَّانَ وَالسَّلْوَىٰ ﴿٨٠﴾ كُلُوا مِن طَيِّبَاتِ مَا رَزَقْنَاكُمْ وَلَا تَطْغَوْا فِيهِ فَيَحِلَّ عَلَيْكُمْ غَضَبِي ۗ وَمَن يَحْلِلْ عَلَيْهِ غَضَبِي فَقَد هَوَىٰ ﴿٨١﴾ وَإِنِّي لَغَفَّارٌ لِّمَن تَابَ وَآمَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا ثُمَّ اهْتَدَىٰ ﴿٨٢﴾

إِنَّهُ مَن يَأْتِ رَبَّهُ مُجْرِمًا فَإِنَّ لَهُ جَهَنَّمَ لَا يَمُوتُ فِيهَا وَلَا يَحْيَىٰ ﴿٧٤﴾ وَمَن يَأْتِهِ مُؤْمِنًا قَدْ عَمِلَ الصَّالِحَاتِ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الدَّرَجَاتُ الْعُلَىٰ ﴿٧٥﴾ جَنَّاتُ عَدْنٍ تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا ۗ وَذَٰلِكَ جَزَاءُ مَن تَزَكَّىٰ ﴿٧٦﴾

**74. Hakika atayemjia Mola wake Mlezi naye ni mkhalifu, basi kwa yakini, yake huyo ni Jahanamu. Hafi humo wala haishi.**

**75. Na atakayemjia naye ni Muumini aliyetenda mema, basi hao ndio wenye vyeo vya juu.**

**76. Bustani za milele zipitazo mito kati yake, wadumu humo. Na hayo ni malipo ya mwenye kujitakasa.**

### Wachawi Wanampa Nasaha Firauni

Dhahiri ya mtiririko wa haya ni kukamilisha yale wachawi waliyomnasahi Firauni kwayo. Walimuonya na kisasi cha Allah تعالى na adhabu Yake ya daima na milele. Pia walimuhimiza atafute na kutaka thawabu za daima zisizomalizika kutoka kwa Allah تعالى. Walisema:

إِنَّهُ مَن يَأْتِ رَبَّهُ مُجْرِمًا

**“Hakika atayemjia Mola wake Mlezi naye ni mkhalifu.”**

Maana yake: Yeyote atakayekutana na Allah Siku ya Kiyama ilhali yeye ni mkhalifu.

﴿٧٤﴾ فَإِنَّ لَهُ جَهَنَّمَ لَا يَمُوتُ فِيهَا وَلَا يَحْيَىٰ

**“Basi kwa yakini, yake huyo ni Jahanamu. Hafi humo wala haishi”.**

Hii ni sawa kama ile Kauli Yake Aliyetukuka:

﴿٣٥﴾ لَا يُقْضَىٰ عَلَيْهِمْ فَيَمُوتُوا وَلَا يُحْيَوْنَ عَنْهُمْ مِّنْ عَذَابِهَا كَذَلِكَ نَجْزِي كُلَّ كَافِرٍ

**“Hawatahukumiwa kufa, wala hawatapunguziwa adhabu yake. Hivi ndivyo Tunavyomlipa kila asiye na shukrani.” (35:36).**

Na Amesema tena:

﴿٨٧﴾ وَيَتَجَنَّبُهَا الْأَشْقَى ﴿٨٨﴾ الَّذِي يَصْلَى النَّارَ الْكُبْرَى ﴿٨٩﴾ ثُمَّ لَا يَمُوتُ فِيهَا وَلَا يَحْيَىٰ ﴿٩٠﴾

**“Na mwingi wa mateso atajitenga mbali nayo hayo. Ambaye atauingia Moto mkubwa. Kisha humo hatakufa wala hatakuwa hai.” (87:11-13).**

Na Amesema Aliyetukuka,

﴿٧٧﴾ وَنَادَوْا يَمْلِكُ لِيَقْضِ عَلَيْنَا رَبُّكَ قَالَ إِنَّكُمْ مِكْتُوبٌ

**“Nao watapiga kelele: ‘Ee Maalik! Na atufishe Mola wako Mlezi’. Maalik (Malaika mlinzi wa Moto) atasema: ‘Bila shaka mtakaa humu humu.’” (43:77).**

Imepokewa na Imaam Ahmad bin Hambal رحمه الله تعالى kutoka kwa Abi Said Al-Khudriy رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«أَمَّا أَهْلُ النَّارِ الَّذِينَ هُمْ أَهْلُهَا، فَإِنَّهُمْ لَا يَمُوتُونَ فِيهَا وَلَا يَحْيَوْنَ، وَلَكِنْ أَنَا سَ تُصِيبُهُمُ النَّارُ بِذُنُوبِهِمْ فَتَمِيتُهُمْ إِمَانَةً حَتَّىٰ إِذَا صَارُوا نَحْمًا أَذِنَ فِي السَّفَاعَةِ فَجِيءَ بِهِمْ ضَبَائِرُ ضَبَائِرَ، فَثَبُّوا عَلَىٰ أَنْهَارِ الْجَنَّةِ، فَيَقَالُ: يَا أَهْلَ الْجَنَّةِ أَيْضُوا عَلَيْهِمْ، فَيَبْتُونَ نَبَاتَ الْجَبَّةِ تَكُونُ فِي حَمِيلِ السَّبِيلِ»

**“Ama watu wa Motoni, ambao wanastahiki, hawatakufa ndani yake**

*wala hawataishi. Bali watakuwa ni watu watakaoadhibiwa na Moto kwa sababu ya madhambi yao. Kwa Pole Pole (Moto) utakuwa unawaua na kuwameza mpaka wawe makaa yalioungua. Baada ya hapo, maombezi (shifaa) yatakubaliwa, nao watatolewa (nje ya Moto) kikundi baada ya kikundi, nao watatawanywa kwenye mito ya Peponi. Kisha kutasemwa: 'Enyi watu wa Peponi! Wamwagieni maji juu yao'. Hapo wataanza kumea kama kumea kwa mbegu kwenye tope ukingoni mwa mto unaomiminika".*

Akasema mtu miongoni mwa watu: "Kama kwamba Mtume wa Allah تعالى alikuwa akiishi jangwani.<sup>1</sup>"

Hivi ndivyo alivyoipokea Muslim katika Kitabu chake cha Sahih<sup>2</sup>.

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَمَنْ يَأْتِهِ مُؤْمِنًا قَدْ عَمِلَ الصَّالِحَاتِ

**"Na atakayemjia naye ni Muumini aliyetenda mema."**

Maana yake: Yeyote atakayekutana na Mola wake Mlezi Siku ya Malipo akiwa Muumini, basi kwa hakika, dhamiri yake moyoni itakuwa imeyakinishwa kuwa ni kweli kwa kauli zake na matendo yake.

فَأُولَئِكَ هُمُ الدَّرَجَاتُ الْعُلَى

**"Basi hao ndio wenye vyeo vya juu."**

Maana yake: Pepo, yenye daraja ya juu kabisa, ghorofa za usalama na utulivu na nyumba zilizo nzuri sana. Amepokea Imaam Ahmad kutoka kwa 'Ubadah bin asw-Swaamit رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«الْجَنَّةُ مِائَةٌ دَرَجَةٍ مَا بَيْنَ كُلِّ دَرَجَتَيْنِ كَمَا بَيْنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ، وَالْفِرْدَوْسُ أَعْلَاهَا دَرَجَةٌ، وَمِنْهَا تُخْرَجُ الْأَنْهَارُ الْأَرْبَعَةُ، وَالْعَرْشُ فَوْقَهَا، فَإِذَا سَأَلْتُمُ اللَّهَ فَاسْأَلُوهُ الْفِرْدَوْسَ»

<sup>1</sup> Ahmad 3:11. Kutajwa jangwa hapa ina maana kuwa maelezo yake ni kama ya mtu asiye-toka mjini.

<sup>2</sup> Muslim 1:172, 173.



*"Pepo ina daraja mia moja, baina ya kila daraja mbili ni masafa yaliyo baina ya mbingu na ardhi. Al-Firdaws ndiyo jina la daraja ya juu kabisa. Na kutoka kwayo kunatoka mito mine na kiti cha Enzi juu yake. Hivyo, mkimuomba Allah, basi muombeni Al-Firdaws<sup>1</sup>".*

Na pia At-Tirmidhiy ameipokea Hadithi hiyo<sup>2</sup>. Na katika Sahihi mbili:

«إِنَّ أَهْلَ عَلِيٍّ لَيَرَوْنَ مَنْ فَوْقَهُمْ كَمَا تَرَوْنَ الْكَوْكَبَ الْعَايِرَ فِي أَفْقِ السَّمَاءِ لَتَفَاضِلِ مَا بَيْنَهُمْ - قَالُوا: يَا رَسُولَ اللَّهِ! تِلْكَ مَنَازِلُ الْأَنْبِيَاءِ قَالَ: - بَلَى، وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ رَجَالَ آمَنُوا بِاللَّهِ وَصَدَّقُوا الْمُرْسَلِينَ»

*"Hakika watu wa 'Illiyin watawaona wale walio juu yao kama unavyoiona nyota inayofifia katika maeneo ya mbali mbinguni, kwa vile vyeo vyao vilivyo tofauti baina yao'. Watu wakasema: 'Ewe Mtume wa Allah! Hayo yatakuwa ni makazi ya Manabii'. Akasema: 'Ndio! Naapa kwa Yule Ambaye nafsi yangu iko Mikononi Mwake, ni kwa watu wenye kumuamini Allah na kuwasadiki pamoja na kuwaamini Mitume<sup>3</sup>".*

Na katika as-Sunan:

«وَإِنَّ أَبَا بَكْرٍ وَعُمَرَ لَمِنْهُمْ وَأَنْعَمًا»

*"Na hakika Abubakar na 'Umar ni miongoni mwao na watafadhilishwa (kwa kupatiwa neema)."<sup>4</sup>*

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

جَنَّتُ عَدْنٍ

**"Bustani 'Adn."**

Maana yake: Makazi yaliyoimarishwa. Hapa imetumiwa kama badali ya, **"Vyeo vya juu"** (iliyotajwa hapo mbeleni).

<sup>1</sup> Ahmad 5:316.

<sup>2</sup> Tuhfat ul Al-Ahwadhiy 7:238.

<sup>3</sup> Fat'h Al-Baariy 6:368 na Muslim 4:2177.

<sup>4</sup> Abu Daawuud 4:287, Tuhfatul Al-Ahwadhiy 10:141 na Ibn Maajah 1:37.

تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا

*“Zipitazo mito kati yake, wadumu humo.”*

Maana yake: Wataishi humo daima dawamu na milele.

وَذَلِكَ جَزَاءُ مَنْ تَزَكَّى

*“Na hayo ni malipo ya mwenye kujitakasa.”*

Maana: Aliyeitwahirisha nafsi yake na madoa, uchafu, ushirikina. Huyu ni mtu anayemuabudu Allah تعالى Peke Yake bila kumshirikisha Yeye na yeyote au chochote na akawafuata Mitume kwa waliokuja nayo katika mambo ya kheri.

وَلَقَدْ أَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ أَنْ أَسْرِ بِعِبَادِي فَاصْرَبْ لَهُمْ طَرِيقًا فِي الْبَحْرِ يَبَسًا لَا تَخَفُ

دَرْكًا وَلَا تَخَفْ ۗ فَاتَّبَعَهُمْ فِرْعَوْنُ بِجُنُودِهِ ۖ فَغَشِيَهُمْ مِنَ اللَّيْلِ مَا عَشِيَهُمْ ۗ وَأَصْلٌ

فِرْعَوْنُ قَوْمَهُ وَمَا هَدَىٰ

**77. Na Tulimfunulia Musa: Toka usiku na waja Wangu, na uwapigie njia kavu baharini. Usikhofu kukamatwa, wala usiogope.**

**78. Firauni akawafuata pamoja na majeshi yake. Basi kiliwafudikiza humo baharini kilichowafudikiza.**

**79. Na Firauni aliwapoteza watu wake wala hakuwaongoa.**

## Wana wa Israili Wanaondoka Misri

Allah تعالى Anatueleza kuwa Alimuamrisha Musa عليه السلام kutoka usiku pamoja na Wana wa Israili, pale Firauni alipokataa kuwaachilia. Na Musa عليه السلام. Alikuwa anataka kuwaweka mbali na utumwa wa Firauni. Allah تعالى Amelifafanua hili katika Sura mbali na Sura hii. Musa عليه السلام alitoka pamoja na Wana wa Israili, na pindi watu wa Misri walipoamka asubuhi walikuta kuwa hakuna hata mtu mmoja aliyebaki Misri. Firauni alikasirika sana. Aliwatuma katika miji wapiga mbiu kukusanya jeshi lake kutoka katika nchi na mikoa yake yote. Aliwaambia:

<sup>1</sup> Abu Daawuud 4:287, Tuhfat ul Al-Ahwadhiy 10:141 na Ibn Maajah 1:37.

إِنَّ هَؤُلَاءِ لَشِرْذِمَةٌ قَلِيلُونَ ﴿٥٥﴾ وَإِنَّهُمْ لَنَا لَغَائِظُونَ ﴿٥٤﴾

**“Hakika hawa (Mayahudi) ni kikosi kidogo. Nao wanatukasirisha.”**  
(26:54-55)

Baada ya kukusanya jeshi lake na kulipanga barabara, alianza kuwafuatia, “Basi wakawafuatia lilipotoka jua.” Maana: Wakati wa alfajiri jua linachomoza.

فَلَمَّا تَرَاءَا الْجَمْعَانِ

**“Na yalipoonana majeshi mawili.”** (26:61)

Maana yake: Yakatizamana makundi hayo mawili.

قَالَ أَصْحَابُ مُوسَىٰ إِنَّا لَمُدْرِكُونَ ﴿٦٢﴾ قَالَ كَلَّا إِنَّ مَعِيَ رَبِّي سَيَهْدِينِ ﴿٦١﴾

**“Wakasema watu wa Musa: Hakika tutakamatwa. Musa akasema: La, kwa yakini Mola wangu Mlezi Yu pamoja nami, bila shaka Ataniongoza (tuokoke sote).”** (26:61-62)

Musa عليه السلام alisimama pamoja na Wana wa Israili na bahari ilikuwa mbele yao na Firauni nyuma yao. Kisha, wakati huo, Allah تعالى Alimfunulia Musa عليه السلام:

فَأَضْرَبَ لَهُمْ طَرِيقًا فِي الْبَحْرِ يَبَسًا

**“Na uwapigie njia kavu baharini.”**

Hivyo, Musa عليه السلام aliipiga bahari na fimbo yake, na kusema: “Pasuka kwa ajili yangu, kwa Idhini ya Allah تعالى”. Kwa hiyo, ilipasuka (kugawanyika) na kila sehemu ya maji ilikuwa kama mlima mkubwa sana. Baada ya hapo, Allah تعالى Akautuma upepo kwenye ardhi ya bahari, hivyo kuuchoma mchanga mpaka ukawa mkavu kama ile sehemu ya ardhi. Kwa ajili hii Akasema:

فَأَضْرَبَ لَهُمْ طَرِيقًا فِي الْبَحْرِ يَبَسًا لَا تَخَافُ دَرَكًا

**“Na uwapigie njia kavu baharini. Usikhofu kukamatwa.”**

Maana yake: Kushikwa na Firauni.

وَلَا تَخْشَىٰ

**“Wala usiogope.”**

Maana yake: Usikhofu bahari kuwaangamiza watu wako. Kisha, Allah تعالى Akatuambia:

فَاتَّبَعَهُمْ فِرْعَوْنُ بِجُنُودِهِ فَغَشِيَهُمْ مِنَ اللَّيْلِ

**“Firauni akawafuata pamoja na majeshi yake. Basi kiliwafudikiza humo baharini.”**

Maana yake: Al-Yammi ni bahari.

مَا غَشِيَهُمْ

**“Kilichowafudikiza.”** Maana yake: Iliwafunika kwa kitu ambacho walikuwa wamekizowea sana katika hali hiyo, kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَأَلْمُؤْتَفِكَةَ أَهْوَىٰ ۖ فَغَشَّاهَا مَا غَشَّىٰ

**“Na miji iliyopinduliwa (juu chini) Ameipindua (yeye hivyo). Vikaifunika miji hiyo vilivyoifunika.” (53:53-54).**

Firauni aliwafuatia baharini, akawapoteza watu wake na hakuwaongoza katika njia ya uongofu, hivyo hivyo,

يَقْدُمُ قَوْمَهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فَأَوْرَدَهُمُ النَّارَ ۖ وَبِئْسَ الْوَرْدُ الْمَوْرُودُ

**“Siku ya Kiyama atawatangulia watu wake na atawaingiza Motoni. Na muingio muovu ulioje huo!”**

يَبْنِي إِسْرَائِيلَ ۖ فَذُحِّبَتْ لَكُمْ مِنْ عَدُوِّكُمْ ۖ وَعَدْنَاكُمْ جَانِبَ الطُّورِ الْأَيْمَنِ وَنَزَّلْنَا عَلَيْكُمُ  
الْمَنَّاءَ وَالسَّلْوَٰئِي ۖ كُلُوا مِنْ طَيِّبَاتِ مَا رَزَقْنَاكُمْ وَلَا تَطْغَوْا فِيهِ فَيَحِلَّ عَلَيْكُمْ غَضَبِي ۖ  
وَمَنْ يَحْلِلْ عَلَيْهِ غَضَبِي فَقَدْ هَوَىٰ ۖ وَإِنِّي لَغَفَّارٌ لِّمَنْ تَابَ وَءَامَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا ثُمَّ

أَهْتَدَىٰ

**80. Enyi Wana wa Israili! Hakika Tulikuoeni na adui yenu, na Tukuahidini upande wa kulia wa mlima. Na Tulikuteremshieni Manna na Salwa.**

**81. Kuleni katika vitu vizuri hivyo Tulivyokuruzukuni, wala msiruke mipaka katika hayo, isije ikakushukieni Ghadhabu Yangu. Na inaye mshukia Ghadhabu Yangu basi huyo ameangamia.**

**82. Na hakika Mimi ni Mwingi wa Kusamehe kwa anayetubia, na akaamini, na akatenda mema, tena akaongoka.**

### **Kuwakumbusha Wana wa Israili Neema ya Allah تعالى Juu Yao**

Allah تعالى Anawakumbusha Neema Zake kubwa na nyingi juu ya Wana wa Israili. Aliwaokoa kutoka kwa adui yao, Firauni, na kutuliza macho yao kwa kumgharikisha yeye na watu wake kwa wakati mmoja ilhali wanatizama kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَأَغْرَقْنَا آلَ فِرْعَوْنَ وَأَنْتُمْ تَنْظُرُونَ ﴿٢٠٠﴾

**“Na Tukawazamisha watu wa Firauni na hali mkitizama.”**

Amepokea al-Bukhaari kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Pale Mtume ﷺ alipofika Madinah, aliwakuta Mayahudi wakifunga siku ya ‘Ashuraa’. Hivyo, aliwauliza kuhusu hilo, nao wakasema: ‘Hii ni siku ambayo Allah تعالى Alimpatia ushindi Musa dhidi ya Firauni’. Akasema Mtume ﷺ:

«نَحْنُ أَوْلَىٰ بِمُوسَىٰ فَصَوِّمُوهُ»

*‘Sisi tuna haki zaidi kwa Musa (kuliko wao), hivyo fungeni’<sup>1</sup>”.*

Muslim pia amenukuu mapokezi haya katika Sahihi yake<sup>2</sup>.

Kisha, Allah تعالى Akachukua ahadi nzito kutoka kwa Musa عليه السلام na Wana wa Israili upande wa kulia wa mlima, baada ya kuangamizwa kwa Firauni. Huu ndio mlima ambao Allah تعالى Alizungumza na Musa عليه السلام na Aliwaambia

<sup>1</sup> Fat’h al-Baariy 8:288.

<sup>2</sup> Muslim 1:795.

watu wa Musa عليه السلام kuuangalia walipoomba kumuona Allah تعالى. Na huo ndio mlima ule ule ambapo Musa عليه السلام alipatiwa Taurati, ilhali wakati huo huo wana wa Israili walianza kuabudu king'ombe kama Anavyoelezea Allah تعالى katika Aya inayofuatia. Ama kuhusu *Manna* na *Salwa* tayari zishaelezwa katika maelezo kwenye *Suratul Baqarah* na nyenginezo. *Manna* ni kitu tamu (halwa) iliyokuwa ikiteremka kutoka mbinguni na *Salwa* ni aina ya ndege waliokuwa wakianguka kwa ajili yao. Waliweza kujaza kila chungu kwa vitu hivyo kama riziki ya kutosha mpaka siku ya pili. Hii ni dhahiri ya ihsani nzuri kutoka kwa Allah تعالى kwao. Kwa sababu hii Allah تعالى Anasema:

كُلُوا مِنْ طَيِّبَاتِ مَا رَزَقْنَاكُمْ وَلَا تَطْغَوْا فِيهِ فَيَحِلَّ عَلَيْكُمْ غَضَبِي

***“Kuleni katika vitu vizuri hivyo Tulivyokuruzukuni, wala msiruke mipaka katika hayo, isije ikakushukieni Ghadhabu Yangu.”***

Maana yake: Kuleni kutoka katika riziki hii ambayo Nimekuruzukuni, wala msiruke mipaka katika riziki Yangu, hivyo mkachukua bila ya haja yoyote au mtakuwa mumekwenda kinyume kwa Niliyokuamrisheni.

فَيَحِلَّ عَلَيْكُمْ غَضَبِي

***“Isije ikakushukieni Ghadhabu Yangu.”***

Maana yake: Nitawakasirikia.

وَمَنْ يَحْلِلْ عَلَيْهِ غَضَبِي فَقَدْ هَوَىٰ

***“Na inayemshukia Ghadhabu Yangu basi huyo ameangamia”***

Amepokea 'Aliy bin Abi Twalhaf kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Hii ina maana kuwa bila shaka atataabika.”<sup>1</sup> Na Kauli Yake:

وَإِنِّي لَغَفَّارٌ لِّمَن تَابَ وَءَامَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا ثُمَّ اهْتَدَىٰ

***“Na hakika Mimi ni Mwingi wa Kusamehe kwa anayetubia, na akaamini, na akatenda mema.”***

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:347.

Maana yake: Yeyote anayerudi kwa kutubia Kwangu, kisha Nitaikubali toba yake bila kujali dhambi alilofanya. Allah تعالى Alikubali hata toba ya Wana wa Israili walioabudu king'ombe. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

تَابَ

**“Kwa anayetubia.”**

Maana yake: Ameacha kwa aliyokuwa nayo miongoni mwa ukafiri, au kumshirikisha Allah تعالى au kumuasi Allah تعالى au unafiki. Na Kauli Yake:

وَأَمِنَ

**“Na akaamini.”** Maana yake: Moyoni mwake.

وَعَمِلَ صَالِحًا

**“Na akatenda mema.”** Maana yake: Kwa viungo vyake. Na Kauli Yake:

ثُمَّ أَهْتَدَى

**“Tena akaongoka.”**

Amepokea ‘Aliy bin Abi Twalhah kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Maana: kisha asiwe ni mwenye kuwa na shaka”<sup>1</sup>. Na amesema Qataadah:

ثُمَّ أَهْتَدَى

**“Tena akaongoka.”**

Hii inamaanisha anashikamana na Uislamu hadi kufariki. Na neno hili, **“Kisha”**, tunaona hapa kuna mpangilio wa habari juu ya habari, kama katika Kauli Yake:

ثُمَّ كَانَ مِنَ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ وَتَوَاصَوْا بِالْمَرْحَمَةِ ﴿١٧﴾

**“Kisha awe miongoni mwa walioamini na wakausiana kusubiri na wakausiana kuhurumiana.” (90:17)**

\* \* \*

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:347.

\* وَمَا أَعْجَلَكَ عَنْ قَوْمِكَ يَمُوسَى ﴿٨٣﴾ قَالَ هُمْ  
 أَوْلَاءٌ عَلَيَّ أَتْرَى وَعَجَلْتُ إِلَيْكَ رَبِّ لِتَرْضَى ﴿٨٤﴾ قَالَ  
 فَإِنَّا قَدْ فَتَنَّا قَوْمَكَ مِنْ بَعْدِكَ وَأَضَلَّهُمُ السَّامِرِيُّ ﴿٨٥﴾  
 فَرَجَعَ مُوسَى إِلَى قَوْمِهِ غَضْبَانَ أَسِفًا قَالَ يَقَوْمِ أَلَمْ  
 يَعِدْكُمْ رَبُّكُمْ وَعَدًّا حَسَنًا أَفَطَالَ عَلَيْكُمْ الْعَهْدُ أَمْ  
 أَرَدْتُمْ أَنْ يَحِلَّ عَلَيْكُمْ غَضَبٌ مِنْ رَبِّكُمْ فَأَخْلَفْتُمْ  
 مَوْعِدِي ﴿٨٦﴾ قَالُوا مَا أَخْلَفْنَا مَوْعِدَكَ بِمَلِكِنَا وَلِنَكُنَّا  
 حُمَلَاءَ أَوْزَارًا مِنْ زِينَةِ الْقَوْمِ فَقَدَفْتَنَاهَا فَكَذَلِكَ أَلْقَى  
 السَّامِرِيُّ ﴿٨٧﴾ فَأَخْرَجَ لَهُمْ عِجْلًا جَسَدًا لَهُ خُورًا  
 فَقَالُوا هَذَا إِلَهُكُمْ وَإِلَهُ مُوسَى فَنَسِيَ ﴿٨٨﴾ أَفَلَا  
 يَرَوْنَ أَلَّا يَرْجِعُ إِلَيْهِمْ قَوْلًا وَلَا يَمْلِكُ لَهُمْ صَرًّا وَلَا نَفْعًا  
 ﴿٨٩﴾ وَلَقَدْ قَالَ لَهُمْ هَارُونُ مِنْ قَبْلُ يَقَوْمِ إِنَّمَا فُتِنْتُمْ  
 بِهِ وَإِنَّ رَبَّكُمُ الرَّحْمَنُ فَاتَّبِعُونِي وَأَطِيعُوا أَمْرِي ﴿٩٠﴾  
 قَالُوا لَنْ نَبْرَحَ عَلَيْهِ عَنكِيفِينَ حَتَّىٰ يَرْجِعَ إِلَيْنَا مُوسَى ﴿٩١﴾  
 قَالَ يَبْهَرُونَ مَا مَنَعَكَ إِذْ رَأَيْتَهُمْ ضَلُّوا ﴿٩٢﴾ أَلَّا  
 تَتَّبِعَنِ أَفَعَصَيْتَ أَمْرِي ﴿٩٣﴾ قَالَ يَبْتَنُوْا لَا تَأْخُذْ  
 بِرِجْلِي وَلَا بَرَأْسِي ۖ إِنِّي خَشِيتُ أَنْ تَقُولَ فَرَّقْتَ بَيْنَ بَنِي  
 إِسْرَائِيلَ وَلَمْ تَرْقُبْ قَوْلِي ﴿٩٤﴾

\* وَمَا أَعْجَلَكَ عَنْ قَوْمِكَ يَمُوسَى  
 ﴿٨٣﴾ قَالَ هُمْ أَوْلَاءٌ عَلَيَّ أَتْرَى  
 وَعَجَلْتُ إِلَيْكَ رَبِّ لِتَرْضَى ﴿٨٤﴾  
 قَالَ فَإِنَّا قَدْ فَتَنَّا قَوْمَكَ مِنْ بَعْدِكَ  
 وَأَضَلَّهُمُ السَّامِرِيُّ ﴿٨٥﴾ فَرَجَعَ  
 مُوسَى إِلَى قَوْمِهِ غَضْبَانَ أَسِفًا قَالَ  
 يَقَوْمِ أَلَمْ يَعِدْكُمْ رَبُّكُمْ وَعَدًّا  
 حَسَنًا أَفَطَالَ عَلَيْكُمْ الْعَهْدُ أَمْ  
 أَرَدْتُمْ أَنْ يَحِلَّ عَلَيْكُمْ غَضَبٌ مِنْ  
 رَبِّكُمْ فَأَخْلَفْتُمْ مَوْعِدِي ﴿٨٦﴾ قَالُوا  
 مَا أَخْلَفْنَا مَوْعِدَكَ بِمَلِكِنَا وَلِنَكُنَّا  
 حُمَلَاءَ أَوْزَارًا مِنْ زِينَةِ الْقَوْمِ  
 فَقَدَفْتَنَاهَا فَكَذَلِكَ أَلْقَى السَّامِرِيُّ  
 ﴿٨٧﴾ فَأَخْرَجَ لَهُمْ عِجْلًا جَسَدًا لَهُ  
 خُورًا فَقَالُوا هَذَا إِلَهُكُمْ وَإِلَهُ  
 مُوسَى فَنَسِيَ ﴿٨٨﴾ أَفَلَا يَرَوْنَ أَلَّا  
 يَرْجِعُ إِلَيْهِمْ قَوْلًا وَلَا يَمْلِكُ لَهُمْ  
 صَرًّا وَلَا نَفْعًا ﴿٨٩﴾

83. Na nini kilichokutia haraka ukawaacha watu wako, ewe Musa?

84. Akasema: Hao wapo nyuma yangu wananifuatia. Na nimefanya haraka kukujia, Mola wangu Mlezi, ili uridhike.



**85. (Allah) Akasema: Sisi Tumewatia mtihani watu wako baada yako, na Samiri amewapoteza.**

**86. Musa akarudi kwa watu wake kwa ghadhabu na kusikitika. Akasema: Enyi watu wangu! Kwani Mola wenu Mlezi Hakukuahidini ahadi nzuri? Je, umekuwa muda mrefu kwenu au mumetaka ikushukieni Ghadhabu ya Mola wenu Mlezi, ndio maana mkavunja miadi yangu?**

**87. Wakasema: Sisi hatukuvunja miadi yako kwa khiari yetu, lakini tulibebeshwa mizigo ya mapambo ya watu, basi tukaitupa. Na hivyo ndivyo alivyotoa shauri Samiri.**

**88. Na akawaundia ndama, kiwiliwili chenye sauti. Na wakasema: Huyu ndiye mungu wenu, na mungu wa Musa, lakini alisahau.**

**89. Je! Hawakuona kuwa hakuwarudishia neno, wala hakuweza kuwadhuru wala kuwafaa?**

**Musa عليه السلام Kwenda katika Miadi ya Allah تعالى na Kuingia Wana wa Israili Kwenye Kuabudu Ndama**

Alipokuwa Musa عليه السلام akisafiri na Wana wa Israili baada kuangamizwa kwa Firauni.

فَأْتَوْا عَلَىٰ قَوْمٍ يَعْكُفُونَ عَلَىٰ أَصْنَامِهِمْ ۖ قَالُوا يَا مُوسَىٰ اجْعَلْ لَنَا إِلَهًا كَمَا لَهُمْ آلِهَةٌ ۚ  
 قَالَ إِنَّكُمْ قَوْمٌ تَجْهَلُونَ ﴿٧٣﴾ إِنَّ هَٰؤُلَاءِ مُتَّبِعُونَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٧٤﴾

**“Na wakawafikia watu waliokuwa wakiabudu masanamu yao. Wakasema: Ewe Musa! Tufanyie waungu na sisi kama wao walivyo na miungu. Akasema: Hakika nyinyi ni watu mfanyao ujinga. Hawa yataangamia haya waliyonayo na ni bure waliokuwa wakiyafanya.” (7:138-139)**

Na Mola wake Mlezi Akamuahidi siku thelathini, kisha akafuatisha kwa siku kumi, ikatimu siku arobaini. Maana: Akiwa anafunga mchana na usiku. Hivyo, Musa عليه السلام alifanya haraka kwenda kwenye mlima na akamuacha nduguye,

Haarun عليه السلام kuwa muangalizi wa Wana wa Israili. Kwa hiyo, Akasema Aliyetukuka:

﴿٨٣﴾ وَمَا أَعْجَلَكَ عَنْ قَوْمِكَ يَمُوسَىٰ ۖ قَالَ هُمْ أَوْلَاءٌ عَلَيَّ أَنْزَىٰ

**“Na nini kilichokutia haraka ukawaacha watu wako, ewe Musa?  
Akasema: Hao wapo nyuma yangu wananifuatia”**

Maana yake: Wanakuja, nao wamefika karibu na mlima.

﴿٨٤﴾ وَعَجِلْتُ إِلَيْكَ رَبِّ لِتَرْضَىٰ

**“Na nimefanya haraka kukujia, Mola wangu Mlezi, ili Uridhike.”**

Maana yake: Ili Uzidi Kuniridhia.

﴿٨٥﴾ قَالَ فَإِنَّا قَدْ فَتَنَّا قَوْمَكَ مِنْ بَعْدِكَ وَأَضَلَّهُمُ السَّامِرِيُّ

**“(Allah) Akasema: Sisi Tumewatia mtihani watu wako baada yako,  
na Samiri amewapoteza”.**

Aliyetukuka Alimpasha habari Nabii Wake, Musa عليه السلام, kwa tukio lililotokea baada yake kwa Wana wa Israili kwa kuabudu kwao king’ombe walichofanyiwa na Samiri. Katika muda huu Allah تعالى Alimuandikia Musa عليه السلام ubao uliokuwa na Taurati kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَكَتَبْنَا لَهُ فِي الْأَلْوَابِ مِنْ كُلِّ شَيْءٍ مَوْعِظَةً وَتَفْصِيلًا لِكُلِّ شَيْءٍ فَخَذَهَا بِقُوَّةٍ وَأَمَرَ

﴿٨٦﴾ قَوْمَكَ بِأَخْذِهَا بِحَسَنَةٍ ۖ سَآوِرِكُمْ دَارَ الْفَاسِقِينَ

**“Na Tukamuwandikia katika ubao kila kitu – mawaidha ya kila namna na maelezo ya kila jambo. Basi yashike kwa imara na uwaamrishe watu wako wayashike bora haya. Karibuni Nitakuonesheni miji ya wavunjao amri.” (7:145),**

Maana yake: Nitawaonesha hatima kwa yatakayotokea kwa wale wenye kuacha Utii Wangu na kupinga Amri Zangu.

Na Kauli Yake:

فَرَجَعَ مُوسَىٰ إِلَىٰ قَوْمِهِ غَضْبَانَ أَسِفًا

***“Musa akarudi kwa watu wake kwa ghadhabu na kusikitika.”***

Maana yake: Baada ya Allah تعالیٰ Kumpasha habari kuhusu hayo akafikia upeo wa ghadhabu, hasira na kufadhaishwa sana nao. Alikuwa na wasiwasi mkubwa juu yao. Wakati huu alipewa Taurati, iliyokuwa na Shari’ah yao, na jambo hili lilikuwa ni heshima kubwa sana kwao. Hali ya kuwa wao walikuwa ni watu waliokuwa wakiabudu asiyekuwa Allah تعالیٰ. Kila mtu mwenye akili ataona kuwa yale waliyokuwa wakifanya ni ya uongo kwa waliyokuwa nayo na ujinga wao. Kwa ajili hiyo akasema: Akarudi kwao

غَضْبَانَ أَسِفًا

***“Kwa ghadhabu na kusikitika.”***

Na neno *Asaf* ni ghadhabu ya hali ya juu. Na amesema Mujaahid: “Katika hali ya ghadhabu na huzuni (kusikitika), yaani kufadhaika”<sup>1</sup>. Qatadah na As-Suddiy wamesema: “*Asifan*, akiwa na huzuni kwa waliyofanya watu wake baada yake”<sup>2</sup>.

قَالَ يَنْقُورِ آلَمْ يَعِدْكُمْ رَبُّكُمْ وَعَدَّٰ حَسَنًا

***“Akasema: Enyi watu wangu! Kwani Mola wenu Mlezi hakukuhidini ahadi nzuri?”***

Maana yake: Je, Hajawaahidi Yeye kwa yale ambayo nimewazungumzia, kila jema katika maisha haya na maisha ya baadaye, na pia hatima njema ya mambo? Tayari mmeshuhudia jinsi Alivyowasaidia kumshinda adui yenu (Firauni) na Akawafanya kumshinda na Akawaneemesha kwa neema nyingine kwa Usaidizi Wake.

أَفْطَالَٰ عَلَيْكُمْ ٱلْعَهْدُ

***“Je, umekuwa muda mrefu kwenu.”*** Maana yake: Katika kungojea kwa Aliyowaahidi Allah تعالیٰ na kusahau Fadhila Zake za mbeleni na Ahadi Aliyofanya nanyi kabla.

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:350.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:350.

أَمْ أَرَدْتُمْ أَنْ يَحِلَّ عَلَيْكُمْ غَضَبٌ مِّن رَّبِّكُمْ

**“Au mmetaka ikushukieni Ghadhabu ya Mola wenu Mlezi.”**

**Ama** (au) hapa imekuja kumaanisha ‘bali’, nayo inatumika hapa kupambanua baina ya neno la kwanza na linalokuja. Kama kwamba anasema: “Bali mnataka kwa matendo yenu haya kuhalalika juu yenu Ghadhabu kutoka kwa Mola wenu Mlezi, ndio maana mkavunja Miadi Yangu.”

قَالُوا

**“Wakasema.”**

Maana yake: Wana wa Israeli kwa kumjibu Musa عليه السلام baada ya kuwalaumu na kuwakaripia.

مَا أَخْلَفْنَا مَوْعِدَكَ بِمَلِكِنَا

**“Sisi hatukuvunja miadi yako kwa khiari yetu.”**

Maana yake: Kwa uwezo na kutaka kwetu. Kisha wakaanza kutoa nyudhuru zisizofaa na kuwaambia jinsi walivyotoa vito walivyochukua kutoka kwa Makibiti walizoazima kutoka kwao walipotoka Misri.

فَقَدَّفْنَاهَا

**“Basi tukaitupa.”** Maana yake: Wakaitupa kando.

Na katika mapokezi ya Assuddi kutoka kwa Abu Malik, kutoka kwa Ibn Abbasi رضي الله عنهما: Hakika si vingine Harun عليه السلام alitaka mapambo na vito vyote vya thamani vya dhahabu kuvikusanya pamoja na kuvizika katika shimo moja na kisha juu yake kuweka jiwe kama alama, hadi hapo atakaporudi Musa عليه السلام na kutoa maamuzi yake vile atakavyoona.

Kisha ndio akafika Samiri, akatupa katika mapambo na vito hivyo fumba la mchanga ambapo alikanyaga juu yake Malaika Jibril عليه السلام. Na akamtaka Harun عليه السلام kumuomba Allah تعالى kumkubalia maombi yake.

Hivyo akaomba bila ya kujua dhamira aliyokuwa nayo Samiri, hivyo maombi yake yakakubaliwa. Hapo Samiri akasema: “Ninamuomba Allah تعالى yawe ndama wa Ng’ombe.”

Hapo hapo kikawa king’ombe (ndama) chenye sauti, sauti ya kupiga kite, iliyokuwa ikiongezeka. Ndama huyu alikuwa ni majaribio, kikazwo na mtihani.

Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Anasema:

فَكَذَّبَكَ الَّذِي لَمْ يَكُنْ لَكَ الْبَدِينُ ﴿٨٧﴾ فَأَخْرَجَ لَهُمْ عِجْلًا جَسَدًا لَهُ خُورٌ

**“Na hivyo ndivyo alivyotoa shauri Samiri. Na akawaundia ndama, kiwiliwili chenye sauti...”<sup>1</sup>.**

Na amepokea Muhammad bin Ishaq رحمه الله تعالى kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema:

هَذَا إِلَهُكُمْ وَإِلَهُ مُوسَىٰ

**“Huyu ndiye mungu wenu, na mungu wa Musa.”**

Hivyo wakanyenyekela kidini kwa ndama huyu, nao wakakipenda mapenzi ambayo hawajawahi kupenda chochote mbali nacho kabla.

Kisha Allah تعالى Akasema:

فَنَسِيَ ﴿٨٨﴾

**“Lakini alisahau.”**

Maana yake: Aliacha kile alichokuwa akifuata katika Dini ya Uislamu, yaani huyo ni Samiri<sup>2</sup>.

Akasema Allah تعالى Kuwajibu na Kuwakemea, na pia Kuwaeleza makosa yao na ujinga waliofanya:

أَفَلَا يَرَوْنَ أَنَّهُمْ إِذْ يُضَاعِفُونَ لِيهِمْ وَقُولاً وَمَا يَكْفُرُونَ بِهِمْ فَأَبْهَتُوا بِهَا صُورَهُمْ فَأَنجَاهُ

**“Je! Hawakuona kuwa hakuwarudishia neno, wala hakuweza kuwadhuru wala kuwafaa?”**

<sup>1</sup> An-Nasaa’iy katika Al-Kubraa 6:396.

<sup>2</sup> Taarikh Atw-Twabariy 1:422 na atw-Twabariy 18:355. Isnadi yake ni dhaifu.

Hii ni kuhusu ndama. Je, hawaoni kuwa hakiwajibu wanapokiomba na wanapozungumza nacho?

وَلَا يَمْلِكُ هُمْ ضَرًّا وَلَا نَفْعًا ﴿٨٣﴾

**“Wala hakuweza kuwadhuru wala kuwafaa?”**

Maana yake: Katika mambo ya duniani na Akhera.

Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “La! Naapa kwa Allah تعالى haikuwa kupiga kwake kite ya ndama ila ni upepo ulioingia katika tupu yake ya nyuma na kutoka mdomoni, hivyo kutoa sauti yenye kusikika”<sup>1</sup>.

Na katika Hadithi ya Al- Fituun Imekuja kutoka kwa al-Hasan Al-Baswri رحمه الله تعالى, imetajwa kuwa jina la ndama huyu ni *Buhmut*<sup>2</sup>.

Katika kutaja udhuru wao hawa watu wajinga, walidai kuwa walikuwa wakiziondoshwa tu vile vito vya Wakibti walivyotoka navyo Misri.

Katika kufanya hilo, walizitupa vito (kwenye shimo la moto), na wakamalizikia kuabudu ndama.

Hivyo, walitaka kujiondolea kitu kichukizacho, lakini walifikia kufanya lililo baya zaidi.

Kama ilivyokuwa katika Hadithi sahihi Kutoka kwa Abdillah bin Umar رضي الله عنهما, kwamba mtu mmoja katika watu wa Iraq alimuuliza kuhusu damu ya mbu iwapo itaingia katika nguo, kwa maana nguo hiyo anaweza kuswalia au la? Ibn Umar رضي الله عنهما akasema: “Hebu yaoneni maajabu ya watu wa Iraq, wamemuua mjukuu wa Mtume ﷺ, kwa maana ya Husain رضي الله عنه, halafu eti wanauliza kuhusu damu ya mbu.”<sup>3</sup>

وَلَقَدْ قَالَ لَهُمْ هَارُونُ مِنْ قَبْلُ يَنْقَوْمِ إِنَّمَا فُتِنْتُمْ بِهِ وَإِنَّ رَبَّكُمُ الرَّحْمَنُ فَاتَّبِعُونِي

وَأَطِيعُوا أَمْرِي ﴿٩٠﴾ قَالُوا لَنْ نَبْرَحَ عَلَيْهِ عَنكِفِينَ حَتَّىٰ يَرْجِعَ إِلَيْنَا مُوسَىٰ ﴿٩١﴾

**90. Na hakika Haarun alikwisha waambia kabla yake: Enyi watu wangu! Hakika nyinyi mumetiwa mtihanini tu kwa kitu hiki. Na**

<sup>1</sup> Taarikh Atw-Twabariy 1:424, 425.

<sup>2</sup> An-Nasaa’iy katika al-Kubraa 6:396. Ibara hii inachukuliwa kuwa si Sahihi.

<sup>3</sup> Fat’h-Al-Bari 10:440.

*kwa yakini Mola wenu Mlezi ni ar-Rahman, Mwingi wa Rehema. Basi nifuateni mimi, na tiini amri yangu!*

**91. Wakasema: Hatutaacha kumuabudu mpaka Musa ataporejea kwetu.**

### Harun عليه السلام Anawakataza Wana wa Israili Kuabudu Ndama

Allah تعالی Anatueleza kuhusu jitihada ya Haarun عليه السلام kuwakataza kuabudu ndama na kuwaambia kuwa huu ni mtihani kwao. Aliwaambia kuwa Mola wao Mlezi Ndiye Mwingi wa Rehema, Aliyeumba kila kitu na Kukikadiria kila kitu kwa kipimo. Yeye Ndiye Mmiliki wa kiti cha Enzi, Yule Anayefanya Atakalo. Hivyo,

فَاتَّبِعُونِي وَأَطِيعُوا أَمْرِي ﴿٩١﴾

**“Basi nifuateni mimi, na tiini amri yangu!”**

Maana yake: Nifuateni mimi kwa ninayokuamuruni na acheni yale niliyowakatazeni. Hata hivyo walijibu:

قَالُوا لَنْ نَبْرَحَ عَلَيْهِ عَنكِفِينَ حَتَّىٰ يَرْجِعَ إِلَيْنَا مُوسَىٰ ﴿٩٢﴾

**“Wakasema: Hatutaacha kumuabudu mpaka Musa ataporejea kwetu.”**

Maana yake: Hatutaacha katika kumuabudu ndama huyu mpaka tumsikie Musa عليه السلام atasema nini kuhusu hilo. Hivyo walimpinga Haarun عليه السلام katika hili na wakapigana naye, hata kukaribia kumuua.

قَالَ يَهْرُونَ مَا مَنَعَكَ إِذْ رَأَيْتَهُمْ ضَلُّوا ﴿٩٣﴾ أَلَّا تَتَّبِعَ أَفَعَصَيْتَ أَمْرِي ﴿٩٤﴾ قَالَ

يَبْتُؤُمْ لَا تَأْخُذْ بِلِحْيَتِي وَلَا بِرَأْسِي ﴿٩٥﴾ إِنِّي خَشِيتُ أَنْ تَقُولَ فَرَّقْتَ بَيْنَ بَنِي إِسْرَائِيلَ وَلَمْ

تَرْقُبْ قَوْلِي ﴿٩٦﴾

**92. (Musa) akasema: Ewe Haarun! Ni nini kilichokuzuia, ulipowaona wamepotea.**

**93. Hata usinifuate? Je, umeasi amri yangu?**

**94. Akasema: Ewe mwana wa mama yangu! Usinishike ndevu zangu, wala kichwa changu. Kwa hakika naliogopa usije sema: Umewafarikisha Wana wa Israili, na hukungojea kauli yangu.**

**Yaliyotokea Baina ya Musa عليه السلام na Haarun عليه السلام baada ya Kurudi kwa Musa عليه السلام**

Allah تعالیٰ Anatueleza yaliyotokea pale Musa عليه السلام aliporudi kwa watu wake na kuona tukio hilo kubwa lililotokea baina yao. Kwa hilo alijawa na hasira na akautupa ubao uliokuwa mkononi mwake. Kisha, akamshika nduguye, Haarun عليه السلام kichwani mwake na kumvuta kwake.

Tulielezea kwa kina kuhusu jambo hili katika Suratul A'raaf, pale tulipoitaja Hadithi:

«لَيْسَ الْخَبْرُ كَالْمُعَايَنَةِ»

“Kusikia Habari si sawa kama kuona”<sup>1</sup>

Kisha, alianza kumlaumu nduguye, Haarun عليه السلام, kwa kusema:

مَا مَنَعَكَ إِذْ رَأَيْتَهُمْ ضَلُّوا ﴿١٤٣﴾ أَلَّا تَتَّبِعَ ۗ

**“Ni nini kilichokuzuia, ulipowaona wamepotea, Hata usinifuate?”**

Maana yake: Ugeniarifu kuhusu jambo hili pindi tu lilipotokea hilo.

أَفَعَصَيْتَ أَمْرِي ﴿١٤٤﴾

**“Je, umeasi amri yangu?”**

Katika jambo ambalo nimekuamini kwalo, ikihusishwa ile kauli ya Musa عليه السلام,

أَخْلَفْنِي فِي قَوْمِي وَأَصْلَحَ وَلَا تَتَّبِعْ سَبِيلَ الْمُفْسِدِينَ ﴿١٤٥﴾

**“Shika mahali pangu katika kuwaendesha watu wangu na utengeneze wala usifuate njia ya waharibifu.” (7:142).**

<sup>1</sup> Ahmad 1:271.



قَالَ يَبْنَؤُمَّ

***“Akasema: Ewe mwana wa mama yangu!”***

Huku kumtaja mama ni njia aliyotumia Harun عليه السلام kupunguza hasira za Musa عليه السلام, kwani yeye alikuwa ni ndugu wa Musa kwa kizazi na wazazi wao walikuwa wamoja. Kutajwa kwa mama hapa ni kumvutia na kwenye uzito katika kuleta upole na ulaini. Hiyo ndio sababu ya yeye kusema:

لَا تَأْخُذْ بِلِحْيَتِي وَلَا بِرَأْسِي ط

***“Usinishike ndevu zangu, wala kichwa changu.”***

Huu ndio udhuru wa Harun عليه السلام kwa Musa عليه السلام katika kuchelewa kumuendea na kumueleza juu ya maafa makubwa yaliyotokea. Alimuambia:

إِنِّي حَشِيئَةٌ

***“Kwa hakika niliogopa.”***

Maana: Nilihofia kukujia ili kukueleza kuhusu jambo hili, kwa kuwa nilifikiria utanishutumu kuwaacha wao peke yao na kuleta mfarakano baina yao. Pia,

وَلَمْ تَرْقُبْ قَوْلِي ﴿٢٠﴾

***“Na hukungojea kauli yangu.”***

Maana yake: Wala hukutizama niliyokuamuru ufanye nilipokuacha kuwa mwangalizi wao. Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Harun عليه السلام alikuwa akimuheshimu na mtiifu sana kwa Musa عليه السلام<sup>1</sup>.”

\* \* \*

قَالَ فَمَا حَطْبُكَ يَسْمِيرِي ﴿٩٥﴾ قَالَ بَصُرْتُ بِمَا لَمْ  
 يَبْصُرُوا بِهِ فَقَبَضْتُ قَبْضَةً مِّنْ أَثَرِ الرَّسُولِ فَنَبَذْتُهَا  
 وَكَذَلِكَ سَوَّلَتْ لِي نَفْسِي ﴿٩٦﴾ قَالَ فَاذْهَبْ فَإِنَّ  
 لَكَ فِي الْحَيَاةِ أَنْ تَقُولَ لَا مِسَاسٌ وَإِنَّ لَكَ مَوْعِدًا لَّن  
 تُخَلَّفَهُ ط<sup>ط</sup> وَأَنْظُرَ إِلَىٰ إِلْهِكَ الَّذِي ظَلْتَ عَلَيْهِ عَاكِفًا ط  
 لَنْحَرِقْنَهُ ثُمَّ لَنَنْسِفَنَّهُ فِي الْيَمِّ نَسْفًا ﴿٩٧﴾ إِنَّمَا إِلَهُكُمُ  
 اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ وَسِعَ كُلَّ شَيْءٍ عِلْمًا ﴿٩٨﴾  
 كَذَلِكَ نَقُصُّ عَلَيْكَ مِنْ أَنْبَاءِ مَا قَدْ سَبَقَ وَقَدْ آتَيْنَاكَ  
 مِنْ لَدُنَّا ذِكْرًا ﴿٩٩﴾ مَنْ أَعْرَضَ عَنْهُ فَإِنَّهُ يَحْمِلُ يَوْمَ  
 الْقِيَامَةِ وِزْرًا ﴿١٠٠﴾ خَلْدَيْنَ فِيهِ وَسَاءَ لَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ  
 حِمْلًا ﴿١٠١﴾ يَوْمَ يُنْفَخُ فِي الصُّورِ وَنَحْشُرُ الْمُجْرِمِينَ  
 يَوْمَئِذٍ زُرْقًا ﴿١٠٢﴾ يَتَخَفَتُونَ بَيْنَهُمْ إِنْ لَبِثْتُمْ إِلَّا  
 عَشْرًا ﴿١٠٣﴾ نَحْنُ أَعْلَمُ بِمَا يَقُولُونَ إِذْ يَقُولُ أَمْثَلُهُمْ  
 طَرِيقَةً إِنْ لَبِثْتُمْ إِلَّا يَوْمًا ﴿١٠٤﴾ وَسَعَلُونَكَ عَنِ الْجِبَالِ  
 فَقُلْ يَنْسِفُهَا رَبِّي نَسْفًا ﴿١٠٥﴾ فَيَذَرُهَا قَاعًا صَفْصَفًا  
 ﴿١٠٦﴾ لَا تَرَىٰ فِيهَا عِوَجًا وَلَا أَمْتًا ﴿١٠٧﴾ يَوْمَئِذٍ  
 يَتَّبِعُونَ الدَّاعِيَ لَا عِوَجَ لَهُ ط وَخَشَعَتِ الْأَصْوَاتُ  
 لِلرَّحْمَنِ فَلَا تَسْمَعُ إِلَّا هَمْسًا ﴿١٠٨﴾

قَالَ فَمَا حَطْبُكَ يَسْمِيرِي ﴿٩٥﴾ قَالَ بَصُرْتُ بِمَا لَمْ يَبْصُرُوا بِهِ  
 فَقَبَضْتُ قَبْضَةً مِّنْ أَثَرِ الرَّسُولِ فَنَبَذْتُهَا  
 وَكَذَلِكَ سَوَّلَتْ لِي نَفْسِي ﴿٩٦﴾ قَالَ فَاذْهَبْ فَإِنَّ  
 لَكَ فِي الْحَيَاةِ أَنْ تَقُولَ لَا مِسَاسٌ ط  
 وَإِنَّ لَكَ مَوْعِدًا لَّن تُخَلَّفَهُ ط وَأَنْظُرَ  
 إِلَىٰ إِلْهِكَ الَّذِي ظَلْتَ عَلَيْهِ عَاكِفًا ط  
 لَنْحَرِقْنَهُ ثُمَّ لَنَنْسِفَنَّهُ فِي الْيَمِّ نَسْفًا  
 ﴿٩٧﴾ إِنَّمَا إِلَهُكُمُ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ  
 إِلَّا هُوَ وَسِعَ كُلَّ شَيْءٍ عِلْمًا ﴿٩٨﴾

95. (Musa) akasema: Ewe Samiri! Unataka nini?

96. Akasema: Niliona wasiyo yaona wao, nikashika gao katika unyao wa Mtume. Kisha nikautupa. Na hivi ndivyo ilivyonielekeza nafsi yangu.

97. (Musa) akasema: Basi ondoka! Na kwa yakini utakuwa katika maisha ukisema: Usiniguse. Na

hakika una ahadi kwako isiyovunjwa. Na mtazame huyo mungu wako

***uliyeeendelea kumuabudu - Sisi kwa hakika tutamchoma moto, kisha tutamtawanya baharini atawanyike.***

***98. Hakika Mungu wenu ni Allah, Mwenyezi Mungu, tu. Hapana Mungu isipokuwa Yeye. Ujuzi Wake Umeenea kila kitu.***

### **Jinsi Samiri Alivyomtengeneza Ndama**

Musa عليه السلام alimuambia Samiri: “Ni kitu gani kilichokufanya ufanye uliyofanya? Ni kipi kilichokujia kikakufanya ufanye hili?” Amepokea Muhammad bin Ishaq رحمه الله تعالى kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Samiri alikuwa mtu miongoni mwa watu wa Baajarma, watu waliokuwa wakiabudu ng’ombe. Bado alikuwa na mapenzi makubwa ya kuabudu ng’ombe katika nafsi yake. Hata hivyo, alijifanya kama kwamba amesilimu pamoja na Wana wa Israili. Jina lake lilikuwa ni Musa bin Zafar”<sup>2</sup>. Qatadah amesema: “Alitoka katika kijiji cha *Samarra*.”<sup>3</sup>

قَالَ بَصُرْتُ بِمَا لَمْ يَبْصُرُوا بِهِ

***“Akasema: Niliona wasiyoyaona wao...”***

Maana yake: Nilimuona Jibril عليه السلام alipokuja kumuangamiza Firauni.

فَقَبِضْتُ قَبْضَةً مِّنْ أَثَرِ الرَّسُولِ

***“Nikashika gao katika unyao wa Mtume...”***

Maana yake: Kutoka kwa nyayo ya kwato ya farasi wake (Jibril عليه السلام)<sup>4</sup>. Hii ni kauli iliyo mashuhuri na maarufu kwa wanazuoni wengi wa tafsiri, bali wengi zaidi. Mujaahid amesema:

فَقَبِضْتُ قَبْضَةً مِّنْ أَثَرِ الرَّسُولِ

***“Nikashika gao katika unyao wa Mtume...”***

<sup>1</sup> At-Twabariy 18:359.

<sup>2</sup> Taarikh At-Tabari 1:424.

<sup>3</sup> At-Tabari 18:363.

<sup>4</sup> At-Tabari 18:362.

“Kutoka chini ya kwato ya farasi wa Jibril عليه السلام”. Pia alisema: “Neno *Qabdhwah* lina maana ya mkono tele, na pia ni kile kinachoshikwa na ncha za vidole”. Mujaahid amesema: “Samiri alirusha kilichokuwa mkononi mwake kwenye vito vya Wana wa Israili na vikafinyangika kuwa mwili wa ndama, aliyefanya sauti ya kite hafifu. Upepo uliopuliza ndani yake ndio uliotoa sauti.”<sup>1</sup> Hivyo akasema:

فَنَبَذْتُهَا

**“Kisha nikautupa.”**

Maana yake: Nikautupa pamoja na wale waliokuwa wakitupa vito.

وَكَذَلِكَ سَأَلْتِ لِي نَفْسِي ﴿٦٦﴾

**“Na hivi ndivyo ilivyonielekeza nafsi yangu.”**

Maana yake: Nafsi yake iliona kuwa hilo ni jambo jema na lilimridhisha ndani ya nafsi yake.

### **Kuadhibiwa Samiri na Kuchomwa kwa Ndama**

Hapo,

قَالَ فَأَذْهَبَ فِإِيَّكَ لَكَ فِي الْحَيَاةِ أَنْ تَقُولَ لَا مِسَاسَ

**“(Musa) akasema: Basi ondoka! Na kwa yakini utakuwa katika maisha ukisema: Usiniguse.”**

Maana yake: Kama vile ulivyochukua na kugusa kisichokuwa chako katika nyayo ya kwato ya Mtume, hiyo ndio itakuwa adhabu yako katika maisha haya, nawe utakuwa unasema, ‘Usiniguse’. Hii ina maana, “Hutawagusa watu, nao hawatakugusa.”

وَإِنَّ لَكَ مَوْعِدًا

**“Na hakika una ahadi kwako.”**

Maana: Siku ya Kiyama,

---

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:362.

لَنْ تُخَلَّفَهُ<sup>ط</sup>

**“Isiyovunjwa.”**

Kwani hutakuwa na njia ya kukwepa. Qataadah amesema:

أَنْ تَقُولَ لَا مِسَاسَ<sup>ط</sup>

**“Ukisema: Usiniguse.”**

Hii inahusisha adhabu kwao na waliobaki miongoni mwao (walio na maradhi kama yao) leo bado wanasema, ‘Usiniguse.’

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَإِنَّ لَكَ مَوْعِدًا لَنْ تُخَلَّفَهُ<sup>ط</sup>

**“Na hakika una ahadi kwako isiyovunjwa.”**

Hasan, Qataadah na Abu Nahik wamesema: “Hutakosekana kwayo.”<sup>1</sup>

وَأَنْظُرْ إِلَىٰ إِلٰهِكَ

**“Na mtazame mungu wako huyo.”**

Uliyekuwa ukimuabudu.

الَّذِي ظَلَّتْ عَلَيْهِ عَآكِفًا<sup>ط</sup>

**“Uliyeendelea kumuabudu.”**

Yule uliyemuanzisha kwa ajili ya kumuabudu, naye ni ndama.

﴿٢٠﴾ إِنَّمَا إِلٰهُكُمُ اللّٰهُ الَّذِي لَا إِلٰهَ إِلَّا هُوَ وَسِعَ كُلَّ شَيْءٍ عِلْمًا

**“Hakika Mungu wenu ni Allah, Mwenyezi Mungu, tu. Hapana Mungu isipokuwa Yeye. Ujuzi Wake Umeenea kila kitu.”**

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:364.

Musa عليه السلام alikuwa anawaambia: “Huyu si mungu wenu. Mungu wenu ni Allah تعالى Peke Yake, Yule ambaye hakuna mungu wa kweli ila Yeye. Ibada haifalii kufanyiwa yeyote isipokuwa Yeye. Kila kitu kinamuhitajia na kila kitu ni mtumishi Wake. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَسِعَ كُلَّ شَيْءٍ عِلْمًا ﴿١٧﴾

**“Ujuzi Wake Umeenea kila kitu.”**

Neno *Ilm* (elimu/ ujuzi) hapa linamaanisha kuwa Yeye ni Mjuzi wa kila kitu.

أَحَاطَ بِكُلِّ شَيْءٍ عِلْمًا ﴿١٨﴾

**“Amekizunguka kila kitu Kukijua (vilivyo kwa Elimu Yake)” (65:12).**

Na Anasema,

وَأَحْصَىٰ كُلَّ شَيْءٍ عَدَدًا ﴿١٩﴾

**“Na Ameidhibiti idadi ya kila kitu.” (72:28).**

Hivyo,

لَا يَعْزُبُ عَنْهُ مِثْقَالُ ذَرَّةٍ

**“Hakifichikani Kwake kitu chochote hata kilicho na uzito wa atomu.” (34:3).**

Pia Amesema:

وَمَا تَسْقُطُ مِنْ وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٍ فِي ظُلْمَتِ الْأَرْضِ وَلَا رَطْبٍ وَلَا يَابِسٍ إِلَّا فِي

كِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿٢٠﴾

**“Na halianguki jani ila Analijua. Wala haianguki punje katika giza la ardhi ila Anaijua. Wala hakianguki kilichorutubika ila Anakijua. Hapana chochote, ila kimo katika Kitabu kidhihirishacho kila jambo.” (5:59).**

Na pia Anasema:

\* وَمَا مِنْ دَابَّةٍ فِي الْأَرْضِ إِلَّا عَلَى اللَّهِ رِزْقُهَا وَيَعْلَمُ مُسْتَقَرَّهَا وَمُسْتَوْدَعَهَا كُلٌّ فِي

كِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿٢١﴾

***“Na hakuna kiumbe yoyote katika ardhi ila riziki yake iko juu ya Allah. Na Anajua makao yake ya milele na mahali pake pa kupita tu. Yote yamo katika Kitabu kinachodhihirisha (kila kitu. Kitabu Chake Allah Anachokijua Mwenyewe hakika yake).” (11:6)***

Aya zinazoelezea na kutaja kuhusu hili ni nyingi.

كَذَلِكَ نَقُصُّ عَلَيْكَ مِنْ أَنْبَاءِ مَا قَدْ سَبَقَ وَقَدْ آتَيْنَاكَ مِنْ لَدُنَّا ذِكْرًا ﴿١١﴾ مَنْ  
أَعْرَضَ عَنْهُ فَإِنَّهُ يَحْمِلُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وِزْرًا ﴿١٢﴾ خَلْدَيْنَ فِيهِ ۗ وَسَاءَ لَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ  
حِمْلًا ﴿١٣﴾

**99. Namna hivi Tunakuhadithia katika khabari za yaliyotangulia. Na hakika Tumekuletea kutoka Kwetu mawaidha ya kukumbukwa.**

**100. Atakayejitenga nayo, basi kwa yakini Siku ya Kiyama atabeba mzigo.**

**101. Wadumu humo. Na ni mzigo muovu kwao kuubeba Siku ya Kiyama!**

**Qur’ani Yote ni Utajo wa Allah تعالى na Ubainifu wa Adhabu ya Wenye Kuikengeuka**

Allah تعالى Anamuambia Mtume Muhammad ﷺ, “Tumekwambia, (ewe Muhammad) kisa cha Musa عليه السلام na yaliyomfikia Firauni na jeshi lake kwa uwazi kama ilivyotokea. Tumekueleza habari zilizotangulia kama zilivyotokea, bila kuongeza au kupunguza.”

وَقَدْ آتَيْنَاكَ مِنْ لَدُنَّا

***“Na hakika Tumekuletea kutoka Kwetu.”*** Maana yake: Tumekupa Sisi.

ذِكْرًا ﴿١١﴾

***“Mawaidha ya kukumbukwa.”***

Pia Tumekupatia ukumbusho kutoka Kwetu, (Qur’ani Tukufu).

لَا يَأْتِيهِ الْبَطْلُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِ ط تَنْزِيلٌ مِّنْ حَكِيمٍ حَمِيدٍ ﴿٤٢﴾

**“Hautakifikia upotovu mbele yake wala nyuma yake.  
Kimeteremshwa na Mwenye Hikima, Msifiwa.” (41:42)**

“Hakuna batili inayojia kutoka mbele wala nyuma yake”. Qur’ani ni ufunuo kutoka kwa Aliye na Hekima, Mwenye Kuhimidiwa.

Hakuna Mtume yeyote aliyepatiwa Kitabu mfano wake au kilicho kamilika kuliko hicho (Qur’ani), kuanzia wakati wa Mitume waliotangulia waliotumwa mpaka kufungwa kwa kuja kwa Mtume ﷺ.

Hakuna Mtume wala Nabii aliyepewa Kitabu kilicho na elimu na habari kuliko Qur’ani kwa yaliyopita na yanayokuja.

Hukumu kuhusu tofauti baina ya mwanadamu imechukuliwa kwayo.

Allah تعالی Anasema yafuatayo kuhusu Qur’ani:

مَنْ أَعْرَضَ عَنْهُ

**“Atakaye jitenga nayo.”**

Maana: Yeyote atakayekikana na kukengeuka katika kufuata maamrishi na maagizo yake, ilhali wanatafuta uongofu kutoka kwa vitabu vingine mbali na Qur’ani, Allah تعالی Atampoteza mtu huyo na kumuacha katika njia ya kuelekea Motoni.

Hii ndio sababu ya Allah تعالی Kusema:

مَنْ أَعْرَضَ عَنْهُ فَإِنَّهُ سَحْمِلٌ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَرَرًا ﴿٤٣﴾

**“Atakayejitenga nayo, basi kwa yakini Siku ya Kiyama atabeba mzigo.”**

Mzigo hapa inamaanisha madhambi ambayo ni sawa na Kauli ya Aliyetukuka:

وَمَنْ يَكْفُرْ بِهِ مِنَ الْأَحْزَابِ فَالنَّارُ مَوْعِدُهُ ﴿٤٤﴾

**“Na atakayemkataa katika makundi basi Moto ndio mahali pa miadi yao.” (11:17)**



Hii inajumlisha kila aliyefikiwa na Qur'ani miongoni mwa Waarabu, Waajemi, Watu wa Kitabu na wengineo.

Hii ni kama Kauli ya Aliyetukuka:

لَأُنذِرْكُمْ بِهِ وَمَنْ بَلَغَ

**“Kwa hiyo (Qur’ani) nikuonyeni nyinyi na kila imfikiayo.” (6:19).**

Qur’ani ni onyo la mwisho kwa kila mmoja imfikiayo. Yeyote mwenye kuifuata, ataongoka na yeyote mwenye kwenda kinyume nayo na kukengeuka na mafunzo yake, atapotea.

Huyo atakuwa na maisha ya dhiki hapa duniani na anaahidiwa kuwa Siku ya Kiyama makazi yake yatakuwa Motoni.

Kwa sababu hii Allah تعالى Anasema:

مَنْ أَعْرَضَ عَنْهُ فَإِنَّهُ يَحْمِلُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ وِزْرًا ﴿١٠٠﴾ خَلِيدِينَ فِيهِ ط

**“Atakayejitenga nayo, basi kwa yakini Siku ya Kiyama atabeba mzigo. Wadumu humo.”**

Hawataweza kuikwepa siku hiyo.

وَسَاءَ لَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ حِمْلًا ﴿١٠١﴾

**“Na ni mzigo muovu kwao kuubeba Siku ya Kiyama!”**

يَوْمَ يُنْفَخُ فِي الصُّورِ ۚ وَنَحْشُرُ الْمُجْرِمِينَ يَوْمَئِذٍ زُرْقًا ﴿١٠٢﴾ يَتَخَفَتُونَ بَيْنَهُمْ إِنْ لَبِثْتُمْ

إِلَّا عَشْرًا ﴿١٠٣﴾ نَحْنُ أَعْلَمُ بِمَا يَقُولُونَ إِذْ يَقُولُ أَمْثَلُهُمْ طَرِيقَةً إِنْ لَبِثْتُمْ إِلَّا يَوْمًا ﴿١٠٤﴾

**102. Siku litakapopulizwa barugumu, na Tukawakusanya wakhalifu Siku hiyo, hali macho yao ya kibuluu.**

**103. Watanong’onezana wao kwa wao: Hamkukaa ila siku kumi tu.**

**104. Sisi Tunajua zaidi watakayoyasema, atakaposema mbora wao katika mwendo: Nyinyi hamkukaa ila siku moja tu.**

## Kupulizwa Parapanda na Siku ya Ufufuo (Kiyama)

Imeelezwa katika Hadithi kuwa Mtume wa Allah ﷻ aliulizwa kuhusu *Swuur* (baragumu), naye akajibu:

«قَرْنٌ يُنْفَخُ فِيهِ»

“Ni pembe itakayopulizwa”<sup>1</sup>.

Imeelezwa katika Hadithi kuhusu *Swuur*, kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa hiyo ni pembe kubwa yenye ukubwa wenye umbali sawa na mbingu na ardhi. Malaika Israfil عليه السلام ndiye atakaye puliza (*Swuur* hiyo)<sup>2</sup>. Hadithi nyingine inayoelezea kuwa Mtume ﷻ amesema:

«كَيْفَ أَنْعَمُ وَصَاحِبُ الْقَرْنِ قَدِ اتَّقَمَ الْقَرْنَ وَحَسَىٰ جَبْهَتُهُ، وَانْتَظَرَ أَنْ يُؤَدَّنَ لَهُ»

“Vipi nitakuwa na raha ilhali mwenye pembe ameishika (pembe hiyo) kwenye mdomo wake na paji lake la uso limeegemea mbele, akingoja kupewa ruhusa (ya kupuliza)”.

Watu wakasema: “Ewe Mtume wa Allah! Je, tuseme nini?” Akasema: “Semeni:

«قُولُوا: حَسْبُنَا اللَّهُ وَنِعْمَ الْوَكِيلُ عَلَى اللَّهِ تَوَكَّلْنَا»

“Allah Anatutosha (Atatukifia). Naye ni Mlinzi bora kabisa. Na Allah, Ndiye tunayemtegemea.”<sup>3</sup>

Ama kuhusu Kauli Yake:

﴿وَنَحْشُرُ الْمُجْرِمِينَ يَوْمَئِذٍ زُرْقًا﴾

“Na Tukawakusanya wakhalifu Siku hiyo, hali macho yao ya kibuluu.”

Pamesemwa kuwa hii ina maana kuwa na macho ya kibuluu kwa ile hali ngumu sana yenye kutisha watakatayokumbana nayo.

يَتَخَلَّفُونَ بَيْنَهُمْ

“Watanong’onezana wao kwa wao”.

<sup>1</sup> Tuhfatul Ahwadhiy 9:116.

<sup>2</sup> Atw-Twabaraniy katika Atw-Twiwaal Namba 36.

<sup>3</sup> Tuhfatul Ahwadhiy 9:117.

Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: "Hii ina maana kunong'onezana baina yao"<sup>1</sup>. Hii inamaanisha kuwa baadhi yao watakuwa wakiwaambia wengine,

إِن لَّبِئْتُمْ إِلَّا عَشْرًا ﴿٣٧﴾

**"Hamkukaa ila siku kumi tu."**

Maana yake: Katika makazi yenu duniani, mulikaa humo kwa muda mchache tu. Wakati huo ulikuwa sawa na siku kumi au mfano wake. Allah تعالى Anasema baada ya hapo:

نَحْنُ أَعْلَمُ بِمَا يَقُولُونَ

**"Sisi Tunajua zaidi watakayoyasema."**

Maana yake: Katika hali yao ya kuzungumza kati yao (baina yao).

إِذْ يَقُولُ امْتَلَهُمْ طَرِيقَةً

**"Atakaposema mbora wao katika mwenendo."**

Maana yake: Yule mwenye akili barabara miongoni mwao,

إِن لَّبِئْتُمْ إِلَّا يَوْمًا ﴿٣٨﴾

**"Nyinyi hamkukaa ila siku moja tu."**

Hii ni kwa kuwa Siku ya Kiyama watahisi ufupi wa maisha ya duniani ndani ya nafsi zao. Hakika maisha ya duniani, na nyakati zake za kurudia na siku zinazofuatana, siku na saa, ni kama kwamba ni siku moja tu. Kwa sababu hii, Siku ya Kiyama makafiri watadhani kuwa maisha ya duniani yalikuwa mafupi sana. Kwa haya wanamaanisha kukwamisha kusimamishia hoja dhidi yao kwa ajili ya ufupi wa muda waliokuwa nao. Kwa ajili hiyo, Allah تعالى Anasema:

وَيَوْمَ تَقُومُ السَّاعَةُ يُقْسِمُ الْمُجْرِمُونَ مَا لَبِثُوا غَيْرَ سَاعَةٍ

**"Na siku kitakaposimama Kiyama waovu wataapa ya kwamba hawakukaa ulimwenguni isipokuwa saa moja tu."** Mpaka Kauli Yake,

وَلَكِنَّكُمْ كُنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٣٩﴾

**"Lakini nyinyi mulikuwa hamjui." (30:55-56).**

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:371.

Na Amesema Aliyetukuka:

أَوَلَمْ نُعَمِّرْكُمْ مَا يَتَذَكَّرُ فِيهِ مَنْ تَذَكَّرَ وَجَاءَكُمْ مِنَ الْأَنْذِيرِ

**“Hatukukupeni umri wa kuweza kukumbuka mwenye kukumbuka?  
Na akakujieni muonyaji...” (35:37)**

Na Amesema Aliyetukuka:

قَالَ كَمْ لَبِئْتُمْ فِي الْأَرْضِ عَدَدَ سِنِينَ ﴿١١٢﴾ قَالُوا لَبِئْنَا يَوْمًا أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ فَسَلِ الْعَادِينَ ﴿١١٣﴾ قُلْ إِنْ لَبِئْتُمْ إِلَّا قَلِيلًا لَوْ أَنْتُمْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١١٤﴾

**“Mulikaa muda gani katika ardhi kwa hesabu ya miaka?  
Watasema: Tulikaa siku moja au sehemu ya siku. Basi waulize wafanyao hesabu. Atasema: Nyinyi hamkukaa ila kidogo tu; laiti mungalikuwa mumejua!” (23:112-114)**

Maana: Kuwa mulibaki humo (ardhini) kwa muda mchache. Lau mungalijua mungalichagua maisha ya milele juu ya yale yenye kumalizika (ya muda). Hata hivyo, mlijiweka katika maisha na mwendo muovu. Mliyapatia kipau mbele maisha ya mpito ya hapa duniani juu ya yenye kudumu ya Akhera.

وَدَسَّلُونَاكَ عَنِ الْجِبَالِ فَقُلْ يَنْسِفُهَا رَبِّي نَسْفًا ﴿١١٥﴾ فَيَذَرُهَا قَاعًا صَفْصَفًا ﴿١١٦﴾ لَا تَرَى فِيهَا عِوَجًا وَلَا أَمْتًا ﴿١١٧﴾ يَوْمَئِذٍ يَتَّبِعُونَ الدَّاعِيَ لَا عِوَجَ لَهُ ۖ وَخَشَعَتِ الْأَصْوَاتُ لِلرَّحْمَنِ فَلَا تَسْمَعُ إِلَّا هَمْسًا ﴿١١٨﴾

**105. Na wanakuuliza khabari za milima. Waambie: Mola wangu Mlezi ataivuruga vuruga.**

**106. Na Ataiacha tambarare, uwanda.**

**107. Hutaona humo mdidimio wala muinuko.**

**108. Siku hiyo watamfuata muitaji asiye na upotofu. Na sauti zote zitamnyenyekea ar-Rahman, Mwingi wa Rehema. Basi husikii ila Minong’ono.**

**Kuvurugwa kwa Milima na Kuachwa Ardhi Uwanda Tambarare**

Anasema Aliyetukuka:

وَسْئَلُونَكَ عَنِ الْجِبَالِ

**“Na wanakuuliza khabari za milima.”**

Maana yake: Je, itabakia Siku ya Kiyama au itaondoka?

فَقُلْ يَنْسِفُهَا رَبِّي نَسْفًا

**“Waambie: Mola wangu Mlezi ataivuruga vuruga.”**

Maana: Ataiondosha katika sehemu zake (iliyokuwepo), kuifuta na kuiondosha.

فَيَذُرُهَا

**“Na Ataiacha”,** Maana yake: Ardhi;

قَاعًا صَفْصَفًا

**“Uwanda tambarare.”**

Maana yake: Imetandazwa moja kwa moja. Neno *Qa'a* lililotumika hapa linamaanisha sehemu ya ardhi iliyo tambarare na neno *Swafswafaa* limetumika kutilia mkazo maana hiyo. Pia imesemwa kuwa inamaanisha ardhi isiyo na mimea, inayomea ndani yake. Maana ya kwanza ndiyo iliyochaguliwa, japokuwa maana ya pili pia inatumwiwa kwa haja. Na kwa hiyo Akasema:

لَا تَرَىٰ فِيهَا عِوَجًا وَلَا أَمْتًا

**“Hutaona humo mdidimio wala muinuko.”**

Maana yake: Hutaona siku hiyo kwenye ardhi mabonde, milima au sehemu nyingine yoyote, si ya chini wala ya juu iliyonyanyuka. Hivyo ndivyo alivyosema Ibn 'Abbaas, 'Ikrimah, Mujaahid, Al-Hasan Al-Baswriy, Adh - Dhahaak, Qatadah na wengine wengi miongoni mwa *salaf*<sup>1</sup>.

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:372 na ad-Durr Al-Manthuur 5:598-599.

## Watu Watafanya Haraka Kuelekea Sauti ya Muitaji

يَوْمَئِذٍ يَتَّبِعُونَ الدَّاعِيَ لَا عِوَجَ لَهُ<sup>ط</sup>

**“Siku hiyo watamfuata muitaji asiye na upotofu.”**

Maana yake: Siku watakapoona hali hii na mambo yenye kutisha, watafanya haraka kuitikia wito wa muitaji. Popote watakapoamriwa kwenda, watakwenda haraka. Lau wangukuwa hivi katika maisha ya dunia, ingekuwa ni manufaa kwao, lakini kufanya hivyo hakutawasaidia.

أَسْمِعْ بِهِمْ وَأَبْصِرْ يَوْمَ يَأْتُوتُنَا<sup>ط</sup>

**“Watasikia na wataona vizuri ilioje Siku watakayotujia...” (19:38).**

Na Akasema tena:

مُهْطِعِينَ إِلَى الدَّاعِ<sup>ط</sup>

**“Wanamkimbilia muitaji...” (54:8).**

Na Kauli Yake:

وَحَشَعَتِ الْأَصْوَاتُ لِلرَّحْمَنِ

**“Na sauti zote zitamnyenyekea ar-Rahman, Mwingi wa Rehema”.**

Amesema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما: “Watanyamaza kabisa”<sup>1</sup>. Na hivyo ndivyo alivyosema As-Suddiy.

فَلَا تَسْمَعُ إِلَّا هَمْسًا ﴿٥٥﴾

**“Basi husikii ila minong’ono”.**

Sa’id bin Jubayr amemsikia Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما akisema: “Hizo ni hatua za miguu”<sup>2</sup>. Na hivyo ndivyo walivyosema ‘Ikrimah, Mujaahid, Adh-Dhahaak, Ar-Rabi’ bin Anas, Qataadah, Ibn Zayd na wengineo<sup>3</sup>. Na amepokea ‘Aliy bin Abi Twalhah kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:374.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:374.

<sup>3</sup> Atw-Twabariy 18:375.

فَلَا تَسْمَعُ إِلَّا هَمْسًا ﴿١٨﴾

***"Basi husikii ila minong'ono."***

"Sauti ndogo, ya mnong'ono"<sup>1</sup>. Na hiyo ni riwaya kutoka kwa 'Ikrimah na Adh-Dhahaak. Na amesema Sa'id bin Jubayr:

فَلَا تَسْمَعُ إِلَّا هَمْسًا ﴿١٨﴾

***"Basi husikii ila Hamsa."***

Ina maana ya mazungumzo ya siri (mnong'ono) na hatua za miguu.

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:375.

يَوْمَئِذٍ لَا تَنْفَعُ الشَّفَعَةُ إِلَّا مَنْ أَذِنَ لَهُ الرَّحْمَنُ وَرَضِيَ  
لَهُ قَوْلًا ﴿١٠٩﴾ يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَلَا  
يُحِيطُونَ بِهِ عِلْمًا ﴿١١٠﴾ \* وَعَنَتِ الْوُجُوهُ لِلْحَيِّ  
الْقَيُّومِ ۖ وَقَدْ خَابَ مَنْ حَمَلَ ظُلْمًا ﴿١١١﴾ وَمَنْ يَعْمَلْ  
مِنَ الصَّالِحَاتِ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَا يَخَافُ ظُلْمًا وَلَا  
هَضْمًا ﴿١١٢﴾ وَكَذَلِكَ أَنْزَلْنَاهُ قُرْآنًا عَرَبِيًّا وَصَرَّفْنَا فِيهِ  
مِنَ الْوَعِيدِ لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ أَوْ يُحَدِّثُ هُمْ ذِكْرًا ﴿١١٣﴾  
فَتَعَلَّى اللَّهُ الْمَلِكُ الْحَقُّ ۖ وَلَا تَعْجَلْ بِالْقُرْآنِ مِنْ قَبْلِ  
أَنْ يُقْضَىٰ إِلَيْكَ وَحْيُهُ ۗ وَقُلْ رَبِّ زِدْنِي عِلْمًا ﴿١١٤﴾  
وَلَقَدْ عَهِدْنَا إِلَىٰ آدَمَ مِنْ قَبْلِ فَتَسَىٰ وَلَمْ يَجِدْ لَهُ عِزْمًا  
﴿١١٥﴾ وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا  
إِبْلِيسَ أُوِيَ ﴿١١٦﴾ فَقُلْنَا يَا آدَمُ إِنَّ هَذَا عَدُوٌّ لَكَ  
وَلِزَوْجِكَ فَلَا يُخْرِجَنَّكَ مِنَ الْجَنَّةِ فَتَشْقَىٰ ﴿١١٧﴾ إِنَّ  
لَكَ أَلَّا تَجُوعَ فِيهَا وَلَا تَعْرَىٰ ﴿١١٨﴾ وَأَنَّكَ لَا تَظْمَأُ فِيهَا  
وَلَا تَضْحَىٰ ﴿١١٩﴾ فَوَسَّوَسَ إِلَيْهِ الشَّيْطَانُ قَالَ يَا آدَمُ  
هَلْ أَدُلُّكَ عَلَىٰ شَجَرَةِ الْخُلْدِ وَمُلْكٍ لَّا يَبْلَىٰ ﴿١٢٠﴾  
فَأَكَلَا مِنْهَا فَبَدَتَ هُمَا سَوْءَ نُهْمًا وَطَفِقَا يَخْصِفَانِ  
عَلَيْهِمَا مِنْ وَرَقِ الْجَنَّةِ ۗ وَعَصَىٰ آدَمُ رَبَّهُ فَغَوَىٰ ﴿١٢١﴾  
ثُمَّ اجْتَبَاهُ رَبُّهُ فَتَابَ عَلَيْهِ وَهَدَىٰ ﴿١٢٢﴾

يَوْمَئِذٍ لَا تَنْفَعُ الشَّفَعَةُ إِلَّا مَنْ أَذِنَ  
لَهُ الرَّحْمَنُ وَرَضِيَ لَهُ قَوْلًا ﴿١٠٩﴾  
يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَلَا  
يُحِيطُونَ بِهِ عِلْمًا ﴿١١٠﴾ \*  
وَعَنَتِ الْوُجُوهُ لِلْحَيِّ الْقَيُّومِ ۖ وَقَدْ  
خَابَ مَنْ حَمَلَ ظُلْمًا ﴿١١١﴾ وَمَنْ  
يَعْمَلْ مِنَ الصَّالِحَاتِ وَهُوَ مُؤْمِنٌ  
فَلَا يَخَافُ ظُلْمًا وَلَا هَضْمًا ﴿١١٢﴾

109. Siku hiyo uombezi haufai kitu, ila wa aliyemruhusu ar - Rahman, Mwingi wa Rehema na Akamridhia kusema.

110. Yeye Anajua yaliyo mbele yao, na yaliyo nyuma yao. Wala wao hawawezi kumjua Yeye vilivyo.

111. Na zitadhalilika nyuso mbele ya Aliye Hai Milele, Muangalizi Mkuu. Na atakuwa ameharibikiwa mwenye kubeba dhulma.

112. Na anayetenda mema, naye ni Muumini, basi hatakhofu kudhulumiwa wala kupunjwa.



**Uombezi na malipo**

Anasema Aliyetukuka:

يَوْمَئِذٍ

**“Siku hiyo.”** Maana yake: Siku ya Kiyama,

لَا تَنْفَعُ الشَّفَعَةُ

**“Uombezi haufai kitu.”** Maana yake: Kutoka Kwake (Allah تعالى).

إِلَّا مَنْ أَدْنَىٰ لَهُ الرَّحْمَنُ وَرَضِيَ لَهُ قَوْلًا ﴿١١﴾

**“Ila wa aliyemruhusu ar-Rahman, Mwingi wa Rehema na Akamridhia kusema.”**

Hii ni kama Kauli Yake:

مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِنْدَهُ إِلَّا بِإِذْنِهِ ۗ

**“Na nani huyo awezaye kuombea mbele Yake (Allah) bila ya Idhini Yake?” (2:255).**

Na pia Kauli Yake:

\* وَكَرَّمْنَا فِي السَّمَاءِ لَا تُغْنِي شَفَاعَتُهُمْ شَيْئًا إِلَّا مِنْ بَعْدِ أَنْ يَأْذَنَ اللَّهُ لِمَنْ يَشَاءُ

وَبَرَّضْنَا ﴿١٦﴾

**“Na wako Malaika wangapi mbinguni, ambao uombezi wao hautafaa chochote isipokuwa baada ya Allah kutoa Idhini kwa Amtakaye na kumridhia.” (53:26)**

Na Amesema:

وَلَا يَشْفَعُونَ إِلَّا لِمَنْ آرْتَضَىٰ وَهُمْ مِنْ خَشِيَّتِهِ مُشْفِقُونَ ﴿٢١﴾

**“Na (Malaika) hawamuombi yeyote ila yule anayemridhia (Mwenyewe Allah), nao kwa ajili ya kumuogopa wananyenyekea.” (21:28)** Na Amesema,

وَلَا تَنْفَعُ الشَّفَعَةُ عِنْدَهُ إِلَّا لِمَنْ أَدْنَىٰ لَهُ ۗ

**“Wala hautafaa uombezi mbele Yake (Allaah) ila kwa yule Aliyempa Idhini.” (34:23)**

Na Amesema:

يَوْمَ يَقُومُ الرُّوحُ وَالْمَلَائِكَةُ صَفًّا لَا يَتَكَلَّمُونَ إِلَّا مَنْ أُذِنَ لَهُ الرَّحْمَنُ وَقَالَ صَوَابًا ﴿٣٨﴾

***“Siku ambayo zitasimama roho (za viumbe wote) na Malaika safu safu; hatasema siku hiyo ila yule ambaye (Allah) Mwingi wa Rehema Amempa Idhini na atasema yaliyo sawa.” (78:38)***

Na katika Sahihi mbili kwa njia zaidi ya moja kutoka kwa Mtume wa Allah تعالى, naye ni bwana na kiongozi wa wana wa Adam na mtukufu zaidi juu ya viumbe vyote vya Allah تعالى, amesema:

«آتَى نَحْتِ الْعَرْشِ، وَأَجْرُ اللَّهِ سَاجِدًا، وَيَفْتَحُ عَلَيَّ بِمَحَامِدٍ لَا أَحْصِيهَا الْآنَ، فَيَدْعُنِي مَا شَاءَ أَنْ يَدْعُنِي، ثُمَّ يَقُولُ: يَا مُحَمَّدُ، ازْفَعِ رَأْسَكَ وَقَلَّ يُسْمَعُ، وَاشْفَعِ تُسْمَعُ - فَيُحَدِّثُ لِي حَدًّا، فَأُدْخِلُهُمُ الْجَنَّةَ ثُمَّ أَعُودُهُ»

*“Nitakuja chini ya Kiti cha Enzi (Arshi), na hapo nitaporomoka kwa kusujudu. Na nitafunguliwa (kwa Wahyi) Kumuhimidi (Kumsifu) Allah sifa ambazo siwezi kuzikumbuka sasa. Allah Ataniacha muda Atakao kuniacha katika hali hiyo. Kisha, Atasema: ‘Ee, Muhammad! Nyanyua kichwa chako, zungumza nawe utasikilizwa, omba na uombezi wako utakubaliwa’. Baada ya hapo, kikundi maalumu kitaruhusiwa kwangu (kuwaombea kwa niaba yao). Allah Atawaingiza Peponi, kisha nitarudi tena (kuwaombea wengine)”<sup>1</sup>.*

Mtume ﷺ ametaja kuwa alifanya hilo mara nne na Manabii wengine wote pia. Katika Hadithi nyingine imetaja kuwa alisema,

«يَقُولُ تَعَالَى: أَخْرِجُوا مِنَ النَّارِ مَنْ كَانَ فِي قَلْبِهِ مِثْقَالُ حَبَّةٍ مِنْ إِيْمَانٍ، فَيُخْرِجُونَ خَلْقًا كَثِيرًا، ثُمَّ يَقُولُ: أَخْرِجُوا مِنَ النَّارِ مَنْ كَانَ فِي قَلْبِهِ نِصْفُ مِثْقَالٍ مِنْ إِيْمَانٍ، أَخْرِجُوا مِنَ النَّارِ مَنْ كَانَ فِي قَلْبِهِ مَا يَزِنُ دَرَّةً، مَنْ كَانَ فِي قَلْبِهِ أَذْنَى أَذْنَى مِثْقَالٍ دَرَّةً مِنْ إِيْمَانٍ»

*“Allah Aliyetukuka Atasema: ‘Mtoeni Motoni yeyote mwenye wizani wa punje (mbegu) moyoni mwake wa Imani’. Hivyo, kundi kubwa la*

<sup>1</sup> Fat'h al-Baariy 8:247 na Muslim 1:184.

watu litatolewa (Motoni). Kisha Atasema: 'Mtoeni Motoni kila mwenye wizani wa nusu punje moyoni mwake ya Imani.' 'Mtoeni Motoni kila mwenye wizani wa atomu ya Imani.' 'Mtoeni Motoni kila mwenye wizani wa imani mdogo zaidi kuliko atomu moyoni mwake' <sup>1</sup>.

Na Kauli Yake:

يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ

**“Yeye Anajua yaliyo mbele yao, na yaliyo nyuma yao.”**

Maana: Anavijua viumbe Vyake vyote kwa Elimu Yake.

وَلَا يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِنْ عِلْمِهِ إِلَّا بِمَا شَاءَ

**“Wala wao hawawezi kumjua Yeye vilivyo.”**

Hii ni kama Kauli Yake:

وَلَا يُحِيطُونَ بِشَيْءٍ مِنْ عِلْمِهِ إِلَّا بِمَا شَاءَ

**“Wala (hao viumbe) hawalijui lolote katika yaliyo katika Elimu Yake (Allah) ila kwa Alipendalo.” (2:255).**

Na Kauli Yake:

وَعَنْتَ أَلْوَجْوهُ لِلْحَيِّ الْقَيُّومِ

**“Na zitadhalilika nyuso mbele ya Aliye Hai Milele, Muangalizi Mkuu.”**

Amesema Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما na wengineo: “Hii inamaanisha kuwa viumbe wote watanyenyekea, watadhalilika na watasalimu amri, kwa Aliye Jabari, Mwenye Uhai wa maisha, Asiye kufa, Msimamia kila jambo wala Halali<sup>2</sup>. Ndiye Mwenye Kusimamia, Kupelekesha na Kuhifadhi kila kitu. Yeye Ndiye Aliyekamilika Pekee, ambaye kila kitu kinamtegemea Yeye na hakuna maisha na uhai bila Yeye. Na Kauli Yake:

وَقَدْ خَابَ مَنْ حَمَلَ ظُلْمًا

**“Na atakuwa ameharibikiwa mwenye kubeba dhulma.”**

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baariy 13:481.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:377, 378.

Maana yake: Siku ya Kiyama. Hakika Allah تعالى Atampatia kila mmoja haki yake anayostahiki. Hata yule kondoo aliyekosa pembe atapatiwa nafasi ya kulipiza kisasi dhidi ya yule aliyekuwa na pembe. Na katika Hadithi: *“Anasema Allah Aliyetukuka: Na kwa Nguvu Zangu, Jaha Yangu na Utukufu Wangu! Sitaachilia kabisa leo dhulma ya dhalimu.”* Na katika Hadithi Sahihi, imenukuliwa kuwa Mtume ﷺ amesema:

﴿إِيَّاكُمْ وَالظُّلْمَ، فَإِنَّ الظُّلْمَ ظُلَمَاتٌ يَوْمَ الْقِيَامَةِ﴾

*“Tahadharini sana na dhulma, kwani hakika ni kuwa dhulma ni giza nene (giza totoro) Siku ya Kiyama”<sup>1</sup>.*

Na aliyefeli kikweli kweli ni yule atakayekutana na Allah تعالى ilhali amemshirikisha Yeye (Allah). Hakika Allah تعالى Anasema:

﴿إِنَّ الشِّرْكَ لَظُلْمٌ عَظِيمٌ﴾

***“Hakika ushirikina ndiyo dhulma kubwa.” (31:13).***

Na Kauli Yake,

﴿وَمَنْ يَعْمَلْ مِنَ الصَّالِحَاتِ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَا يَخَافُ ظُلْمًا وَلَا هَضْمًا﴾

***“Na anayetenda mema, naye ni Muumini, basi hatakhofu kudhulumiwa wala kupunjwa.”***

Baada ya Allah تعالى kutaja waovu na vitisho vyao, Anawapongeza watu wema na kutaja hukumu watakayopata. Hukumu yao ni kuwa hawatadhulumiwa wala kunyanyaswa. Hii ina maana kuwa maovu yao hayataongezwa wala mazuri yao hayatapunguzwa. Hii ni rai ya Ibn ‘Abbaas, Mujaahid, Adh-Dhahaak, Al-Hasan, Qataadah na wengineo<sup>2</sup>. *“Dhulm”* ina maana ni ziada inayotokana na madhambi ya wengine anayobebeshwa mtu, na *“Hadhman”* inamaanisha upungufu.

﴿وَكَذَلِكَ أَنْزَلْنَاهُ قُرْآنًا عَرَبِيًّا وَصَرَّفْنَا فِيهِ مِنَ الْوَعِيدِ لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ أَوْ يُحَدِّثُ هُمْ ذِكْرًا

﴿فَتَعَلَى اللَّهِ الْمَلِكُ الْحَقُّ وَلَا تَعْجَلْ بِالْقُرْآنِ مِنْ قَبْلِ أَنْ يُقْضَىٰ إِلَيْكَ وَحْيُهُ

﴿وَقُلْ رَبِّ زِدْنِي عِلْمًا﴾

<sup>1</sup> Muslim 4:1996.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:379-380.

**113. Na namna hivi Tumeiteremsha Qur'ani kwa Kiarabu, na Tumekariri humo maonyo ili wapate kuogopa na iwe (kila wakati) inawapa makumbusho (mapya).**

**114. Ametukuka Allah, Mfalme wa Haki. Wala usiifanyie haraka Qur'ani hii, kabla haujamalizika ufunuo wake. Na sema: Mola wangu Mlezi! Nizidishie elimu.**

### **Qur'ani Imeteremshwa ili Watu Wawe na Uchamungu na Kutafakari**

Baada ya Allah تعالى, Kutaja kuwa Siku hiyo ya Kiyama, watu wazuri na wabaya watalipwa na hakuna cha kuepukana nacho, kisha Anaeleza kuwa Qur'ani imeteremshwa kuleta bishara njema na kuonya kwa uwazi katika lugha ya Kiarabu fasaha kabisa. Hakuna utata wala upungufu ndani yake

وَصَرَّفْنَا فِيهِ مِنَ الْوَعِيدِ لَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ

**“Na Tumekariri humo maonyo ili wapate kuogopa.”**

Maana yake: Ili waache madhambi, vitu vilivyokatanzwa na uchafu mbaya.

أَوْ تُحَدِّثُ لَهُمْ ذِكْرًا

**“Na iwe (kila wakati) inawapa makumbusho.”**

Nayo ni kuleta utiifu na vitendo ambavyo vitamleta karibu na Allah تعالى.

فَتَعَلَى اللَّهِ الْمَلِكُ الْحَقُّ

**“Ametukuka Allah, Mfalme wa Haki.”**

Maana yake: Mtukufu, Muadhama, Mfalme wa Haki, Ambaye Yeye Mwenyewe Ndiye Ukweli na Ahadi Yake ni ya kweli.

Hivyo hivyo, Adhabu Yake ni kweli, Manabii Wake ni haki, Pepo na Moto zipo (ukweli na haki), kila kitu kinachotoka Kwake ni haki na kweli.

Na Uadilifu Wake ni Kutowaadhibu watu kabla ya Kuwaonya, Kuwatuma Manabii kwao na Kuwapatia nyudhuru kwa viumbe Vyake, ili asipate yeyote hoja wala udhuru au shaka Siku ya Kiyama.

## Amri kwa Mtume ﷺ Kuisikiliza Qur'ani Ilipotaremshwa bila Kufanya Haraka katika Kuisoma

Na Kauli Yake:

وَلَا تَعْجَلْ بِالْقُرْآنِ مِنْ قَبْلِ أَنْ يُقْضَىٰ إِلَيْكَ وَحْيُهُ

**“Wala usiifanyie haraka Qur’ani hii, kabla haujamalizika ufunuo wake”.**

Hii ni kama Kauli Yake katika Suratul Qiyaamah:

لَا تُحْرِكْ بِهِ لِسَانَكَ لِتَعْجَلَ بِهِ ۚ إِنَّ عَلَيْنَا جَمْعَهُ وَقُرْآنَهُ ۚ فَإِذَا قَرَأْتَهُ فَاتَّبِعْ  
قُرْآنَهُ ۚ ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا بَيَانَهُ ۚ

**“Usiutikise ulimi wako kwa kuufanyia haraka wahyi unapoteremka. Kwa hakika ni juu Yetu Kuukusanya na Kukusomesha. Wakati Tunapokusomea, basi fuata kusomwa kwake. Kisha ni juu Yetu Kuubainisha.”(75:16-19).**

Imethibiti katika Hadithi Sahihi kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuwa Mtume wa Allah تعالى alikuwa akipata shida sana katika kuudhibiti Wahyi. Kwa hiyo, alikuwa akiutikisa ulimi wake kwa haraka pamoja na kisomo chake. Allah تعالى Akateremsha Aya hii<sup>1</sup>. Hii inamaanisha kuwa pindi Jibril عليه السلام alipokuwa akimteremshia Aya za Qur’an, Mtume ﷺ alikuwa akiisoma pamoja naye (Jibril عليه السلام) kwa ile hamu yake ya kuihifadhi. Kisha, Allah تعالى Alimuongoza kwa lililo jepesi, rahisi na sahali katika jambo hilo, Kumtoa katika shida hiyo. Akasema:

لَا تُحْرِكْ بِهِ لِسَانَكَ لِتَعْجَلَ بِهِ ۚ إِنَّ عَلَيْنَا جَمْعَهُ وَقُرْآنَهُ ۚ

**“Usiutikise ulimi wako kwa kuufanyia haraka wahyi unapoteremka. Kwa hakika ni juu Yetu Kuukusanya na Kukusomesha.”(75:16-17)**

Maana: Tutaikusanya kifuani mwako, kisha utawasomea watu bila ya kusahau chochote.

فَإِذَا قَرَأْتَهُ فَاتَّبِعْ قُرْآنَهُ ۚ ثُمَّ إِنَّ عَلَيْنَا بَيَانَهُ ۚ

**“Wakati Tunapokusomea, basi fuata kusomwa kwake. Kisha ni juu Yetu Kuubainisha.”(75:16-19).**

<sup>1</sup> Fat’h Al-Baariy 1:39.

Na Anasema katika Aya hii:

وَلَا تَعْجَلْ بِالْقُرْآنِ مِنْ قَبْلِ أَنْ يُقْضَىٰ إِلَيْكَ وَحْيُهُ

**“Wala usiifanyie haraka Qur’ani, hii kabla haujamalizika ufunuo wake.”**

Maana yake: Bali anyamaze (na kusikiliza kwa makini). Pindi Malaika anapomaliza kukusomea, soma baada yake.

وَقُلْ رَبِّ زِدْنِي عِلْمًا

**“Na sema: Mola wangu Mlezi! Nizidishie elimu”.**

Maana yake: Nizidishie kutoka Kwako elimu. Ibn ‘Uyaynah amesema: “Mtume ﷺ aliendelea kuzidisha elimu yake mpaka Allah تعالى Alipomfisha”.

وَلَقَدْ عَهِدْنَا إِلَىٰ آدَمَ مِنْ قَبْلُ فَنَسِيَ وَلَمْ نَجِدْ لَهُ عَزْمًا ﴿١١٥﴾ وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ فَسَجَدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ أَبَىٰ ﴿١١٦﴾ فَقُلْنَا يَا آدَمُ إِنَّ هَذَا عَدُوٌّ لَكَ وَارْزُقْكَ فَلَا يُخْرِجُكَ مِنَ الْجَنَّةِ فَتَشْقَىٰ ﴿١١٧﴾ إِنَّ لَكَ أَلَّا تَجُوعَ فِيهَا وَلَا تَعْرَىٰ ﴿١١٨﴾ وَأَنَّكَ لَا تَظْمَأُ فِيهَا وَلَا تَصْحَىٰ ﴿١١٩﴾ فَوَسْوَسَ إِلَيْهِ الشَّيْطَانُ قَالَ يَا آدَمُ هَلْ أَدُلُّكَ عَلَىٰ شَجَرَةِ الْخُلْدِ وَمُلْكٍ لَّا يَبُلَىٰ ﴿١٢٠﴾ فَأَكَلَا مِنْهَا فَبَدَتَ هُمَا سَوْءَ تَهْمَا وَطَفِيقَا يَخْصِفَانِ عَلَيْهِمَا مِنْ رِزْقِ الْجَنَّةِ وَعَصَىٰ آدَمُ رَبَّهُ فَغَوَىٰ ﴿١٢١﴾ ثُمَّ آجَبْتَهُ رَبُّهُ فَتَابَ عَلَيْهِ وَهَدَىٰ ﴿١٢٢﴾

**115. Na hapo zamani Tuliagana na Adam, lakini alisahau, wala hatukuona kwake azma kubwa.**

**116. Na Tulipowaambia Malaika: Msujudieni Adam! Wakasujudu, isipokuwa Iblisi, alikataa.**

**117. Tukasema: Ewe Adam! Hakika huyu ni adui yako na wa mkeo. Basi asikutoeni katika Bustani hii, mkaingia mashakani.**

**118. Hakika humo hutakuwa na njaa wala hutakuwa uchi.**

**119. Na kwa yakini hutapata kiu humo wala hutapata joto.**

**120. Lakini Shetani alimtia wasiwasi, akamuambia: Ewe Adam! Je, nikujulishe mti wa umilele na wa ufalme usiokoma.**

**121. Basi wakaula wote wawili, na uchi wao ukawadhihirikia na wakaanza kujibandika majani ya Peponi. Na Adam akamkosea Mola wake Mlezi, na akapotea kidogo njia.**

**122. Kisha Mola wake Mlezi Akamchagua na Akamkubalia toba yake na Akamuongoa.**

### **Kisa cha Adam عليه السلام na Ibilisi**

Ampokea Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: "Hakika ameitwa *Insaan* (mwanadamu) kwa kuwa alichukua ahadi, lakini akasahau"<sup>1</sup>. Na hivyo ndivyo alivyopokea Aliy bin Abi Twalhah kutoka kwake (Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما)<sup>2</sup>. Na wamesema Al-Hasan na Mujaahid: "Aliacha"<sup>3</sup>. Na Kauli Yake:

وَإِذْ قُلْنَا لِلْمَلَائِكَةِ اسْجُدُوا لِآدَمَ

**"Na Tulipowaambia Malaika: Msujudieni Adamu!"**

Allah تعالى Anatutajia vipi Adam عليه السلام alivyotukuzwa na kukirimiwa kwake. Ametutajia vipi alivyofadhilishwa juu ya wale Aliowaumba. Mazungumzo juu ya kisa hiki tayari tumetangulia kuyaeleza katika Suratul Baqarah (2), Suratul A'raaf (7), Suratul Hijr (15) na Suratul Kahf (18). Na maelezo yake bado yatakuja tena katika mwisho wa Sura ya Swaad (38). Katika kisa hiki, Allah تعالى Anataja Kuumbwa kwa Adam عليه السلام na kuwa Aliwaamrisha Malaika kumsujudia Adam عليه السلام kama ishara ya utukufu, heshima na kumkirimu. Pia Ametaja uadui wa Ibilisi kwa Wana wa Adam عليه السلام na kwa baba yao, Adam عليه السلام, kabla yao. Kwa ajili ya hiyo, Allah تعالى Anasema

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:383.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:383.

<sup>3</sup> Atw-Twabariy 18:383.



فَسَجِدُوا إِلَّا إِبْلِيسَ أَبَى ﴿١٠٩﴾

**“Wakasujudu, isipokuwa Iblisi, alikataa.”**

Maana yake: Alikataa kusujudu na kutakabari (kuwa na kiburi).

فَقُلْنَا يَتَّادَمُ إِنَّ هَذَا عَدُوٌّ لَكَ وَلِزَوْجِكَ

**“Tukasema: Ewe Adam! Hakika huyu ni adui yako na wa mkeo...”**

Maana yake: Mke wake Hawwaa’.

فَلَا يُخْرِجَنَّكَ مِنَ الْجَنَّةِ فَتَشْقَى ﴿١١٠﴾

**“Basi asikutoeni katika Bustani hii, mkaingia mashakani.”**

Maana yake: Usifanye haraka katika kufanya kitu ambacho kitakufanya utolewe Peponi, hivyo utapata taabu, utakosa raha na utaingia mashakani katika kupata riziki yako. Lakini hapa (Peponi), utaishi maisha ya raha na starehe, bila ya kuwa na mzigo, taklifu wala mashaka.

إِنَّ لَكَ أَلَّا تَجُوعَ فِيهَا وَلَا تَعْرَى ﴿١١١﴾

**“Hakika humo hutakuwa na njaa wala hutakuwa uchi.”**

Sababu ya Allah تعالى hapa kuchang’anya njaa na uchi ni kuwa njaa ni kudhalilishwa ndani (kusikoonekana) na uchi ni kudhalilishwa kidhahiri.

وَأَنَّكَ لَا تَظْمَأُ فِيهَا وَلَا تَصْحَى ﴿١١٢﴾

**“Na kwa yakini hutapata kiu humo wala hutapata joto.”**

Na mambo haya mawili pia ni kinyume. Kiu ni joto la ndani, nayo ni ukosefu wa maji ilhali uharara wa jua joto la nje. Na Kauli Yake:

فَوَسَّوَسَ إِلَيْهِ الشَّيْطَانُ قَالَ يَتَّادَمُ هَلْ أَدُلُّكَ عَلَى شَجَرَةِ الْخَالِدِ وَمُلْكٍ لَا يَبْئَلُ ﴿١١٣﴾

**“Lakini Shetani alimtia wasiwasi, akamuambia: Ewe Adam! Je, nikujulisha mti wa umilele na wa ufalme usiokoma.”**

Tumetangulia kueleza kuwa Iblisi aliwafanya (wote wawili) kuanguka kwa udanganyifu.

وَقَاسَمُهُمَا إِيَّيْ لَكُمْآ لَمِنَ النَّصِيحِينَ ﴿٢١﴾

**“Naye akawaapia: Kwa yakini mimi ni mmoja wa watowao ushauri mzuri kwenu.” (7:21).**

Tumetangulia kuelezea kuwa Allah تعالى Alichukua ahadi kutoka kwa Adam عليه السلام na mkewe kuwa japokuwa wanaweza kula kila aina ya tunda, wasiwe ni wenye kuukaribia mti fulani Peponi.

Hata hivyo, Iblisi, aliendelea kuwaghuri mpaka wote wawili wakala kutoka kwa mti huo. Huo ulikuwa ni mti wa umilele, yaani yeyote mwenye kula kwayo ataishi milele na atakuwa ni mwenye kubakia daima. Kuna Hadithi iliyonukuliwa ambayo imetaja Mti wa Umilele.

Abu Daawud Atw-Twayaalisiy رحمه الله تعالى amempokea Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ فِي الْجَنَّةِ شَجْرَةَ بَيْسِرُ الرَّائِبِ فِي ظِلِّهَا مِائَةٌ عَامٍ مَا يَنْقُطُهَا، وَهِيَ شَجْرَةُ الْخُلْدِ»

*“Hakika Peponi kuna mti ambao mpandaji atasafiri chini ya kivuli chake kwa miaka mia moja na bado hajaumaliza. Nao ni Mti wa Umilele”<sup>1</sup>.*

Na Imaam Ahmad pia ameipokea Hadithi hii<sup>2</sup>.

Na Kauli Yake:

فَأَكَلَا مِنْهَا فَبَدَّتْ هُمَا سَوْءَاتُهُمَا

**“Basi wakaula wote wawili, na uchi wao ukawadhihirikia.”**

Ampokea Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى kutoka kwa Ubayy bin Ka'b رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

<sup>1</sup> Musnad At-Tayalis na. 332.

<sup>2</sup> Ahmad 2:455.

«إِنَّ اللَّهَ خَلَقَ آدَمَ رَجُلًا طَوَالًا كَثِيرَ شَعْرِ الرَّأْسِ، كَأَنَّهُ نُخْلَةٌ سَحُوقِي، فَلَمَّا ذَاقَ الشَّجَرَةَ سَفَطَ عَنْهُ لِبَاسُهُ، فَأَوَّلُ مَا بَدَأَ مِنْهُ عَوْرَتُهُ، فَلَمَّا نَظَرَ إِلَى عَوْرَتِهِ جَمَلَ يَشْتَدُّ فِي الْجَنَّةِ، فَأَخَذَتْ شَعْرُهُ شَجَرَةَ فَتَارَعَهَا، فَتَادَاهُ الرَّحْمَنُ: يَا آدَمُ مِنِّي نَجْرٌ، فَلَمَّا سَمِعَ كَلَامَ الرَّحْمَنِ قَالَ: يَا رَبِّ لَا، وَلَكِنِ اسْتِخْيَاءٌ، أَرَأَيْتَ إِنْ نُبْتُ وَرَجَعْتُ أَغَايِدِي إِلَى الْجَنَّةِ؟ قَالَ: نَعَمْ»

*“Hakika Allah Alimuumba Adam akiwa mtu mrefu mwenye nywele nyingi kichwani mwake. Alionekana kama mtende uliovaa nguo. Pindi alipoonja (tunda) la mti, nguo zake zilianguka. Kitu cha kwanza kilichodhihiri ni uchi wake. Hivyo, pindi alipouona uchi wake, alijaribu kukimbia kurudi Peponi. Hata hivyo, katika hali hiyo mti ulimshika nywele zake, naye akaziondoa. Hapo akamuita yeye, Mwingi wa Rehema: ‘Ewe Adam! Unanikimbia Mimi?’ Aliposikia Maneno ya Mwingi wa Rehema, alisema: ‘Hapana, Ewe Mola wangu Mlezi! Lakini naona haya. Waonaje nikitubia na nikarudi tena katika Njia Yako, Utanirudisha Peponi?’ Akasema: ‘Ndio’”<sup>1</sup>.*

Hii ni kama Kauli Yake:

فَتَلَقَّى آدَمُ مِنْ رَبِّهِ كَلِمَاتٍ فَتَابَ عَلَيْهِ<sup>٢</sup>

**“Kisha Adam akapokea maneno kwa Mola wake Mlezi, na Mola wake Mlezi Akapokea toba yake.” (2:37).**

Hata hivyo, riwaya hii imekatika baina ya Al-Hasan na Ubayy bin Ka'b.

Na Kauli Yake:

وَطَفِيفًا مَخْضِفَانِ عَلَيْهِمَا مِنْ وَرَقِ الْجَنَّةِ<sup>٣</sup>

**“Na wakaanza kujibandika majani ya Peponi.” (7:22)**

Amesema Mujahid: “Walibandika majani mwilini mwao kwa muundo wa nguo”. Na hivyo ndivyo alivyosema Qataadah na as-Suddiy<sup>2</sup>. Na Kauli Yake:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 12:354. Kama mwandishi alivyoeleza kuwa Hadithi hii ni dhaifu. Imenuku-liwa na Isnadi iliyokamilika na Al-Haakim, aliyesema kuwa ni Sahihi. Adh-Dhahabiy akakub-aliana naye. Hata hivyo, katika Isnadi yake yupo Yahya bin Damrah, ambaye maisha yake hayajulikani. Al-Hasan hakuwahi kusikia kutoka kwa Ubayy bin Ka'b. Na hata katika kuinyanyua hadi kwa Mtume ﷺ pia kuna utata, yaani haiwezi kunasibishwa kwa Mtume.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:388.

وَعَصَىٰ آدَمُ رَبَّهُ فَغَوَىٰ ﴿١٠٩﴾ ثُمَّ أَجْتَبَهُ رَبُّهُ فَتَابَ عَلَيْهِ وَهَدَىٰ ﴿١١٠﴾

***“Na Adam akamkosea Mola wake Mlezi, na akapotea kidogo njia. Kisha Mola wake Mlezi Akamchagua na Akamkubalia toba yake na Akamuongoa.”***

Amepokea Al-Bukhaari kutoka kwa Abu Hurayrah عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ amesema:

«حَاجَّ مُوسَىٰ آدَمَ، فَقَالَ لَهُ: أَنْتَ الَّذِي أَخْرَجْتَ النَّاسَ مِنَ الْجَنَّةِ بِذَنْبِكَ وَأَشَقَّيْتَهُمْ؟ قَالَ آدَمُ: يَا مُوسَى، أَنْتَ الَّذِي اضْطَنَّاكَ اللَّهُ بِرِسَالَاتِهِ وَبِكَلَامِهِ، أَتَلْمِزُنِي عَلَىٰ أَمْرِ كَتَبَهُ اللَّهُ عَلَيَّ قَبْلَ أَنْ يَخْلُقَنِي أَوْ قَدَّرَهُ اللَّهُ عَلَيَّ قَبْلَ أَنْ يَخْلُقَنِي؟ - قال رسول الله ﷺ: - فَحَجَّ آدَمُ مُوسَىٰ»

*“Musa alihojiana na Adam, akamuambia: ‘Wewe ndiye uliyewatoa watu Peponi kwa sababu ya dhambi yako na ukawatia mashakani’. Akasema Adam: ‘Ewe Musa! Wewe ndiye uliyechaguliwa na Allah kwa Kukupatia ujumbe Wake na Kuzungumza nawe. Je, unanilaumu mimi kwa jambo ambalo Allah tayari Ameniandikia kabla Hajaniumba?’ Kisha, Mtume wa Allah akasema: ‘Hapo, Adam akamshinda Musa kwa hoja<sup>1</sup>”.*

Na Hadithi hii ina njia nyingi katika Sahihi mbili na vitabu vingine vinavyojulikana kama Musnad<sup>2</sup>.

\* \* \*

<sup>1</sup> Fat’h Al-Baariy 8:288.

<sup>2</sup> Fat’h al-Baariy 6:508 na 11:513, Muslim 4:2042 na 2043 na Ahmad 2:287, 314.

قَالَ أَهْبِطَا مِنْهَا جَمِيعًا ۖ بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ ۖ فِيمَا  
 يَأْتِيَنَّكُمْ مِنِّي هُدًى فَمَنِ اتَّبَعَ هُدَايَ فَلَا يَضِلُّ وَلَا  
 يَشْقَى ﴿١٢٣﴾ وَمَنْ أَعْرَضَ عَن ذِكْرِي فَإِنَّ لَهُ مَعِيشَةً  
 ضَنْكًا وَنَحْشُرُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَعْمَى ﴿١٢٤﴾ قَالَ رَبِّ لِمَ  
 حَشَرْتَنِي أَعْمَى وَقَدْ كُنْتُ بَصِيرًا ﴿١٢٥﴾ قَالَ كَذَلِكَ  
 أَتَتْكَ آيَاتُنَا فَنَسِيهَا ۖ وَكَذَلِكَ الْيَوْمَ تُنسى ﴿١٢٦﴾  
 وَكَذَلِكَ نَجْزِي مَنْ أَسْرَفَ وَلَمْ يُؤْمِنْ بِآيَاتِ رَبِّهِ ۗ  
 وَلَعَذَابُ الْآخِرَةِ أَشَدُّ وَأَبْقَى ﴿١٢٧﴾ أَفَلَمْ يَهْدِ لَهُمْ كَمْ  
 أَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِنَ الْقُرُونِ يَمْشُونَ فِي مَسْجِدِهِمْ ۗ إِنَّ فِي  
 ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّأُولِي الْأَلْبَابِ ﴿١٢٨﴾ وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِن  
 رَبِّكَ لَكَانَ لِزَامًا وَأَجَلٌ مُّسْمًى ﴿١٢٩﴾ فَاصْبِرْ عَلَىٰ مَا  
 يَقُولُونَ وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ قَبْلَ طُلُوعِ الشَّمْسِ وَقَبْلَ  
 غُرُوبِهَا ۖ وَمِنَ اللَّيْلِ فَسَبِّحْ وَأَطْرَافَ النَّهَارِ لَعَلَّكَ  
 تَرْضَىٰ ﴿١٣٠﴾

قَالَ أَهْبِطَا مِنْهَا جَمِيعًا ۖ بَعْضُكُمْ  
 لِبَعْضٍ عَدُوٌّ ۖ فِيمَا يَأْتِيَنَّكُمْ مِنِّي  
 هُدًى فَمَنِ اتَّبَعَ هُدَايَ فَلَا يَضِلُّ  
 وَلَا يَشْقَى ﴿١٢٣﴾ وَمَنْ أَعْرَضَ عَن  
 ذِكْرِي فَإِنَّ لَهُ مَعِيشَةً ضَنْكًا  
 وَنَحْشُرُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَعْمَى ﴿١٢٤﴾  
 قَالَ رَبِّ لِمَ حَشَرْتَنِي أَعْمَى وَقَدْ  
 كُنْتُ بَصِيرًا ﴿١٢٥﴾ قَالَ كَذَلِكَ  
 أَتَتْكَ آيَاتُنَا فَنَسِيهَا ۖ وَكَذَلِكَ  
 الْيَوْمَ تُنسى ﴿١٢٦﴾

**123. Allah Akasema:**  
*Ondokeni humu nyote, hali  
 ya kuwa ni maadui nyinyi  
 kwa nyinyi. Na ukikufikieni  
 kutoka Kwangu uongofu,  
 basi atakayeufuata uongofu  
 Wangu huo hatapotea wala  
 hatataabika.*

**124. Na atakayejeipusha na mawaidha Yangu hayo, basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki, na Siku ya Kiyama Tutamfufua hali ya kuwa kipofu.**

**125. Aseme: Ewe Mola wangu Mlezi! Mbona umenifufua kipofu na hali nilikuwa nikiona?**

**126. Allah Atasema: Ndiyo vivyo hivyo. Zilikuja Aya Zetu ukazisahau (ukazipuza), na kadhalika leo utasahauliwa?**

## Adam عليه السلام Kuteremshwa Ardhini na Ahadi ya Kheri kwa Watu Waongofu na Waovu

Allah تعالى Anawaambia Adam عليه السلام, Hawa' na Iblisi: "Ondokeni humu nyote, yaani kutoka Peponi nyote pamoja". Hakika tumeeleza hilo kwa kina katika Tafsiri ya Suratul Baqara.

بَعْضُكُمْ لِبَعْضٍ عَدُوٌّ

**"Hali ya kuwa ni maadui nyinyi kwa nyinyi." (2:36)**

Akasema (Allah تعالى): Adam عليه السلام na kizazi chake na pia Iblisi na vizazi vyake. Na Kauli Yake:

فَأِمَّا يَأْتِيَنَّكُمْ مِنِّي هُدًى

**"Na ukikufikieni kutoka Kwangu uwongofu."**

Amesema Abul 'Aaliyah: "Manabii, Mitume na bayana (ujumbe)."<sup>1</sup>

فَمَنِ اتَّبَعَ هُدَايَ فَلَا يَضِلُّ وَلَا يَشْقَى

**"Basi atakayeufuata uongofu Wangu huo hatapotea wala hatataabika".**

Amesema Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: "Hatapotea duniani wala hatataabika Akhera"<sup>2</sup>.

وَمَنْ أَعْرَضَ عَن ذِكْرِي

**"Na atakayejepusha na mawaidha Yangu hayo."** Maana yake: Mwenye kwenda kinyume na Maamrishi Yangu na yale Niliyoteremsha kwa Mtume Wangu, basi akawa amejepusha nao, amepuuza na kuchukua uongofu mwengine usiokuwa Wangu.

فَإِنَّ لَهُ مَعِيشَةً ضَنْكًا

**"Basi kwa yakini atapata maisha yenye dhiki."**

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 1:549.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:389.

Maana yake: Dhiki hapa duniani, hatapata utulivu wala kupanuka kifua chake. Bali kifua chake kitadhikika kwa uzito wa upotevu hata akionekana kuwa na raha kwa nje, anavaa na anakula anachotaka na anaishi anapotaka. Mbali na hayo yote, moyo wake hautakuwa na utohara wa yakini na uongofu. Hakika ni kuwa atakuwa katika wasiwasi, utatanishi na shaka na atabaki katika hali ya kutojifahamu na ugeugeu. Na hizi ni dhiki za kimaisha. Na Kauli Yake:

وَنَحْشُرُهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ أَعْمَى ﴿١٢٤﴾

**“Na Siku ya Kiyama Tutamfufua hali ya kuwa kipofu.”**

Amesema Mujaahid, Abu Swaalih na As-Suddiy: “Hatakuwa na hoja (yoyote ile)”<sup>1</sup>.

Na amesema ‘Ikrimah: “Atafanywa kipofu kwa kila kitu isipokuwa Moto”. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَنَحْشُرُهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَلَىٰ وُجُوهِهِمْ عُمْيًا وَبُكْمًا وَصُمًّا مَأْوَاهُمْ جَهَنَّمُ ﴿١٢٥﴾

**“Na Tutawakusanya Siku ya Kiyama, hali ya kuwa wanakokotwa juu ya nyuso zao, na hali ya kuwa vipofu na mabubu na viziwi. Makazi yao ni Jahanamu...” (17:97)**

Kwa hiyo Akasema:

رَبِّ لِمَ حَشَرْتَنِي أَعْمَىٰ وَقَدْ كُنْتُ بَصِيرًا ﴿١٢٦﴾

**“Ewe Mola wangu Mlezi! Mbona umenifufua kipofu na hali nilikuwa nikiona?”**

Maana yake: Duniani.

قَالَ كَذَلِكَ أَتَتْكَ آيَاتُنَا فَنَسِيتَهَا ۖ وَكَذَلِكَ الْيَوْمَ تُنْسَىٰ ﴿١٢٧﴾

**“Allah Atasema: Ndiyo vivyo hivyo. Zilikuja Aya Zetu ukazisahau (ukazipuza), na kadhalika leo utasahauliwa?”**

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:394, 395.

Maana yake: Ulipokengeuka Aya za Allah تعالى na ukazifanya kama huzikumbuki baada ya kufikishwa kwako. Ulizipuuzwa, ukakengeuka kwayo na hukuzitilia maanani. Kwa hiyo, leo Tutakuchukulia na kuamiliana nawe muamala wa aliyekusahau kabisa.

فَأَلْيَوْمَ نَنْسَهُمْ كَمَا نَسُوا لِقَاءَ يَوْمِهِمْ هَذَا

***“Basi leo Sisi Tunawasahau kama walivyosahau mkutano wa Siku yao hii.” (7:51)***

Hakika, adhabu itakwenda sambamba na amali iliyofanywa. Hata hivyo, kusahau maneno ya Qur’ani, ilhali unafahamu maana yake na kusimama juu ya hukumu zake, haijumlishwi katika tishio hili maalumu (hasa). Japokuwa, kusahau maneno ya Qur’ani kumeonywa dhidi yake kwa njia nyingine. Hakika imenukuliwa katika Sunna kuwa haifai kabisa na pia adhabu kali kwa anayesahau Qur’ani baada ya kuihifadhi.

وَكَذَلِكَ نَجْزِي مَنْ أَسْرَفَ وَلَمْ يُؤْمِنْ بِعَائِدَةِ رَبِّهِ ۗ وَلَعَذَابُ الْآخِرَةِ أَشَدُّ وَأَبْقَى ۗ

***127. Na hivi ndivyo Tutakavyomlipa kila apitaye kiasi, na asiyeamini Aya za Mola wake Mlezi; na bila shaka adhabu ya Akhera ni kali zaidi na iendeleayo sana.***

### **Adhabu Kali kwa Mwenye Kuvuka Mipaka**

Anasema Aliyetukuka: “Na hivi ndivyo Tutavyowalipa waliovuka mipaka, waliokadhibisha na kukanusha Aya na Ishara za Allah تعالى duniani na Akhera.”

هُمَّ عَذَابٌ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۗ وَلَعَذَابُ الْآخِرَةِ أَشَقُّ ۗ وَمَا لَهُم مِّنَ اللَّهِ مِن وَّاقٍ ۗ

***“Wanayo adhabu katika maisha ya dunia; na bila shaka adhabu ya Akhera ni ngumu zaidi wala hawatakuwa na mlinzi kwa Allah.” (13:34)***

Na kwa hiyo Akasema:

وَلَعَذَابُ الْآخِرَةِ أَشَدُّ وَأَبْقَى ۗ

***“Na bila shaka adhabu ya Akhera ni kali zaidi na iendeleayo sana.”***

Maana: Ina maumivu makali na makubwa zaidi kuliko adhabu ya duniani na pia itakuwa ni yenye kudumu milele, kwani watabaki humo daima dawamu



katika maisha yao hayo. Kwa ajili hiyo, Mtume ﷺ aliwaambia wote wenye kulaaniana (mume na mke) pale wanapokula kiapo<sup>1</sup>:

﴿إِنَّ عَذَابَ الدُّنْيَا أَهْوَنُ مِنْ عَذَابِ الْآخِرَةِ﴾

*"Hakika adhabu ya duniani ni nyepesi (na ndogo zaidi) kuliko adhabu ya Akhera"<sup>2</sup>.*

أَفَلَمْ يَهْدِ لَهُمْ كَمْ أَهْلَكْنَا قَبْلَهُمْ مِنَ الْقُرُونِ يَمْشُونَ فِي مَسْجِدِهِمْ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِّأُولِي  
الْأَلْبَابِ ﴿١٢٨﴾ وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِنْ رَبِّكَ لَكَانَ لِزَامًا وَأَجَلٌ مُّسَمًّى ﴿١٢٩﴾ فَاصْبِرْ عَلَىٰ  
مَا يَقُولُونَ وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ قَبْلَ طُلُوعِ الشَّمْسِ وَقَبْلَ غُرُوبِهَا وَمِنْ آنَاءِ اللَّيْلِ فَسَبِّحْ  
وَأَطْرَافَ النَّهَارِ لَعَلَّكَ تَرْضَىٰ ﴿١٣٠﴾

**128.** Je, haikuwabainikia tu kama karne ngapi Tuliziangamiza kabla yao? Na hawa makafiri wanatembeatembea katika maskani yao. Bila shaka katika hayo zimo Ishara kwa wenye akili.

**129.** Na kama si neno lililotangulia kutoka kwa Mola wako Mlezi na muda uliowekwa, bila shaka ingefika sasa hivi adhabu kwao.

**130.** Yavumilie wasemayo, na umtukuze Mola wako Mlezi pamoja na kumsifu kabla halijatoka jua na kabla halijatua, na nyakati za usiku pia umtukuze, na katikati ya mchana ili upate ya kukuridhisha.

**Kuangamizwa Ummah Zilizopita Pana Mafunzo kwa Wenye Kuzingatia**

Anasema Aliyetukuka:

أَفَلَمْ يَهْدِ

*"Je, haikuwabainikia tu?"*

Kwa hawa wenye kukadhibisha kwa uliyokuja nayo, ewe Muhammad kuwa,

<sup>1</sup> Pale mume anapomshutumu mkewe kuwa amezini – Mfasiri.

<sup>2</sup> Muslim 2:1131.

“Tuliwaangamiza wale waliokataa Mitume Wetu katika Ummah zilizopita kabla yao. Walionesha uadui wa dhahiri, kwa hiyo hakukubaki alama yao na hakuna miongoni mwao aliyebaki.”

“Ushahidi kuhusu hilo ni majumba yao matupu waliyoyaacha, ambayo yamerithiwa na wengine, wakitembea katika makazi na maskani za wale waliotangulia (kabla yao)”.

﴿١٢٤﴾ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ لِّأُولِي الْأَلْبَابِ

**“Bila shaka katika hayo zimo Ishara kwa wenye akili.”**

Maana yake: Akili iliyo timamu na sahihi na ufahamu wa kweli. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ فَتَكُونَ لَهُمْ قُلُوبٌ يَعْقِلُونَ بِهَا أَوْ آذَانٌ يَسْمَعُونَ بِهَا فَإِنَّهَا لَا تَعْمَى الْأَبْصَارُ وَلَكِن تَعْمَى الْقُلُوبُ الَّتِي فِي الصُّدُورِ ﴿١٢٤﴾

**“Je, hawatembe katika ardhi ili wapate nyoyo, (akili) za kufahamia, au masikio ya kusikia? Kwa hakika macho hayapofoki, lakini nyoyo ambazo zimo vifua ni ndizo zinazopofoka.” (22:46).**

Na Akasema katika Sura ya Aliif Laam Miim Sajdah:

أَوَلَمْ يَهْدِ لَهُمْ كَمْ أَهْلَكْنَا مِن قَبْلِهِم مِّنَ الْقُرُونِ يَمْشُونَ فِي مَسْجِدِهِمْ

**“Je, haijawabainikia kuwa Ummah ngapi Tuliziangamiza kabla yao, na wao wanapita katika maskani yao hayo?” (32:26).**

Kisha Akasema Aliyetukuka:

﴿١٢٥﴾ وَلَوْلَا كَلِمَةٌ سَبَقَتْ مِن رَّبِّكَ لَكَانَ لِزَامًا وَأَجَلٌ مُّسَمًّى

**“Na kama si neno lililotangulia kutoka kwa Mola wako Mlezi na muda uliowekwa, bila shaka ingefika sasa hivi adhabu kwao.”**

Maana yake: Lau kama si neno lililotangulia kutoka kwa Allah تعالى, nalo ni Kutomuadhibu yeyote ila baada ya kusimamishiwa hoja juu yake na muda

maalumu uliowekwa Naye kwa wenye kukanusha na kukadhibisha – adhabu ingekuwa ni yenye kuwafikia kwa ghafla.

### Amri ya Kusubiri na Kutekeleza Sala Tano

Kwa hiyo Allah تعالى Anamuambia Mtume Wake kwa Kumliwaza:

فَأَصْبِرْ عَلَىٰ مَا يَقُولُونَ

*“Yavumilie wasemayo.”*

Maana yake: Katika kukukadhibisha kwao.

وَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ قَبْلَ طُلُوعِ الشَّمْسِ

*“Na umtukuze Mola wako Mlezi pamoja na kumsifu kabla halijatoka jua.”*

Maana yake: Sala ya Alfajiri.

وَقَبْلَ غُرُوبِهَا

*“Na kabla halijatua.”*

Maana yake: Sala ya Alasiri, kama ilivyokuja katika Sahihi mbili kutoka kwa Jariir bin Abdallaah Al-Bajaliy رضي الله عنه aliyesema: “Tulikuwa tumekaa pamoja na Mtume ﷺ alipoutizama mwezi usiku uliokuwa umekamilika. Akasema:

«إِنَّكُمْ سَتَرُونَ رَبَّكُمْ كَمَا تَرُونَ هَذَا الْقَمَرَ، لَا تَصَامُونَ فِي رُؤْيَيْهِ، فَإِنْ اسْتَطَعْتُمْ أَنْ لَا تُغْلِبُوا عَلَىٰ صَلَاةِ قَبْلِ طُلُوعِ الشَّمْسِ وَقَبْلِ غُرُوبِهَا فَافْعَلُوا»

*‘Hakika nyinyi mtamuona Mola wenu Mlezi (Siku ya Kiyama) kama mnavyouna mwezi huu na wala hamtahitajika kuzongana pamoja ili kuona. Kwa hiyo, ikiwa mtaweza msikose kusali Sala kabla ya kuchomoza jua (Alfajiri) na kabla kuchwa (Alasiri), basi fanyeni hivyo.’*

Kisha akasoma Aya hii<sup>1</sup>.

<sup>1</sup> Fat’h Al-Baariy 2:40 na Muslim 1:439.

Na amepokea Imaam Ahmad kutoka kwa 'Umarah bin Ru'aybah رضي الله عنه kuwa amemsikia Mtume ﷺ akisema:

«لَنْ يَلِجَ النَّارَ أَحَدٌ صَلَّى قَبْلَ طُلُوعِ الشَّمْسِ وَقَبْلَ غُرُوبِهَا»

*"Hataingia Motoni yule mwenye kusali kabla kuchomoza na kabla ya kuchwa jua"<sup>1</sup>.*

Hadithi hii pia imenukuliwa na Muslim<sup>2</sup>. Na Kauli Yake:

وَمِنْ آتَايَ اللَّيْلِ فَسَبِّحْ

***"Na nyakati za usiku pia umtukuze."***

Maana yake: Katika wakati wake tekeleza Sala ya *Tahajjud* (Sala ya usiku). Baadhi ya wanazuoni wamesema kuwa maana yake ni Sala ya Magharibi na Isha'.

وَاطْرَافَ النَّهَارِ لَعَلَّكَ تَرْضَى ﴿١٢٤﴾

***"Na katikati ya mchana."***

Maana yake: Hii ni kinyume na nyakati za usiku.

لَعَلَّكَ تَرْضَى ﴿١٢٥﴾

***"Ili upate ya kukuridhisha."***

Kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَلَسَوْفَ يُعْطِيكَ رَبُّكَ فَتَرْضَى ﴿١٢٦﴾

***"Na Mola wako Mlezi Atakupa mpaka uridhike." (93:5).***

Na imekuja katika Hadithi sahihi.

<sup>1</sup> Ahmad 4:136.

<sup>2</sup> Muslim 1:440.

«يَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى يَا أَهْلَ الْجَنَّةِ، قَيُّوْلُوْنَ: لَيْتَكَ رَبَّنَا وَسَعْدَيْكَ، قَيُّوْلُوْنَ: خَلِّ رَضِيْمٌ؟ قَيُّوْلُوْنَ: رَبَّنَا وَمَا لَنَا لَا نَرْضَى وَقَدْ أُعْطِينَا مَا لَمْ نُعْطِ أَحَدًا مِنْ خَلْقِكَ، قَيُّوْلُوْنَ: إِنِّي أُعْطِيكُمْ أَفْضَلَ مِنْ ذَلِكَ، قَيُّوْلُوْنَ: وَأَيُّ شَيْءٍ أَفْضَلُ مِنْ ذَلِكَ؟ قَيُّوْلُوْنَ: أَجَلٌ عَلَيْكُمْ رِضْوَانِي فَلَا أَسْخَطُ عَلَيْكُمْ بَعْدَهُ أَبَدًا»

*"Allah Aliyetukuka Anasema: 'Enyi watu wa Peponi'. Watajibu: 'Tuko hapa, ewe Mola wetu Mlezi, kukutumikia'. Atawaambia: 'Je, mumeridhia?' Watajibu: 'Kwa nini tusiridhie, ewe Mola wetu Mlezi, ilhali Umetupatia yale ambayo Hujampatia yeyote miongoni mwa viumbe Vyako?' Hapo, Allah Aliyetukuka Atasema: 'Hakika, Nitawapa kilicho bora kuliko hilo'. Watauliza: 'Ni kitu gani kitakachokuwa bora kuliko hilo?' Atasema: "Nimewapa Ridhaa Yangu, hivyo Sitawakasirikia tena baada ya hapo milele"<sup>1</sup>.*

Na katika Hadithi nyingine:

«يَا أَهْلَ الْجَنَّةِ، إِنَّ لَكُمْ عِنْدَ اللَّهِ مَوْعِدًا يُرِيدُ أَنْ يُنْجِزَكُمُوهُ: قَيُّوْلُوْنَ: وَمَا هُوَ؟ أَلَمْ يَبَيِّنْ وَجْوهَنَا وَيُنْفِلْ مَوَازِينَنَا وَيُرْزُقِنَا عَنِ النَّارِ وَيُدْخِلَنَا الْجَنَّةَ، قَيُّوْلُوْنَ: فَكَيْفَ الْجَنَابُ قَيُّوْلُوْنَ: إِلَيْهِ، فَوَاللَّهِ مَا أُعْطَاهُمْ خَيْرًا مِنَ النَّظَرِ إِلَيْهِ، وَهِيَ الزِّيَادَةُ»

*"Enyi watu wa Peponi! Hakika nyote muna miadi na Allah ambayo Anataka kuwatimizia'. Watasema: 'Na hilo ni nini? Je, si tayari Ushazifanya nyuso zetu kuwa nyeupe, na Kufanya mizani zetu kuwa nzito, na Ukatuokoa na Moto na Kutuingiza Peponi?' Kisha, pazia itanyanyuliwa, nao watamtizama Yeye (Allah). Naapa kwa Allah! Hakuwapa lolote lililo bora kuliko ile fursa ya kumtizama, na hiyo ndiyo ziada (ya neema)"<sup>2</sup>.*

\* \* \*

<sup>1</sup> Fat'h al-Baariy 11:423.

<sup>2</sup> Ahmad 4:332.

وَلَا تَمُدَّنْ عَيْنِيَكَ إِلَىٰ مَا مَتَّعْنَا بِهِ أَزْوَاجًا مِنْهُمْ زَهْرَةَ  
 الْحَيَاةِ الدُّنْيَا لِنَفْتِنَهُمْ فِيهِ ۚ وَرَزَقْنَا رِيكَ خَيْرًا وَأَتَقَىٰ ﴿١٣١﴾  
 وَأُمِرَ أَهْلَكَ بِالصَّلَاةِ وَاصْطَبِرْ عَلَيْهَا لَا نَسْأَلُكَ رِزْقًا نَحْنُ  
 نَرْزُقُكَ ۗ وَالْعَاقِبَةُ لِلتَّقْوَىٰ ﴿١٣٢﴾ وَقَالُوا لَوْلَا يَأْتِينَا بِآيَةٍ  
 مِنْ رَبِّهِ ۗ أَوَلَمْ تَأْتِهِم بَيِّنَةٌ مَا فِي الصُّحُفِ الْأُولَىٰ ﴿١٣٣﴾  
 وَلَوْ أَنَّا أَهْلَكْنَاهُمْ بِعَذَابٍ مِنْ قَبْلِهِ لَقَالُوا رَبَّنَا لَوْلَا  
 أَرْسَلْتَ إِلَيْنَا رَسُولًا فَنَتَّبِعَ آيَاتِكَ مِنْ قَبْلِ أَنْ نَذِلَّ  
 وَنُحْزَىٰ ﴿١٣٤﴾ قُلْ كُلٌّ مُتَرَبِّصٌ فَتَرَبَّصُوا ۗ فَسَتَعْلَمُونَ  
 مَنْ أَصْحَابُ الصِّرَاطِ السَّوِيِّ وَمَنِ اهْتَدَىٰ ﴿١٣٥﴾

وَلَا تَمُدَّنْ عَيْنِكَ إِلَىٰ مَا مَتَّعْنَا بِهِ  
 أَزْوَاجًا مِنْهُمْ زَهْرَةَ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا  
 لِنَفْتِنَهُمْ فِيهِ ۚ وَرَزَقْنَا رِيكَ خَيْرًا وَأَتَقَىٰ  
 ﴿١٣١﴾ وَأُمِرَ أَهْلَكَ بِالصَّلَاةِ وَاصْطَبِرْ  
 عَلَيْهَا لَا نَسْأَلُكَ رِزْقًا نَحْنُ نَرْزُقُكَ ۗ  
 وَالْعَاقِبَةُ لِلتَّقْوَىٰ ﴿١٣٢﴾

*131. Wala usivikodolee macho yako Tulivyowastareheshea baadhi ya watu miongoni mwao. Hivyo, ni mapambo ya maisha ya dunia tu, ili*

*Tuwafanyie mtihani kwavyo. Na riziki ya Mola wako Mlezi ni bora mno na iendeleayo.*

*132. Na waamrishe watu wako kusali, na uendelee mwenyewe kwa hayo. Hatukuombi riziki bali Sisi ndio Tunakuruzuku. Na mwisho mwema utawathibitikia wamchao Mungu.*

**Usitizame Starehe za Watu na Subiri katika Ibada ya Allah تعالى**

Allah تعالى Anamuambia Mtume ﷺ, "Usitizame walio nayo hawa watu walio matajiri na mfano wake, na starehe walizo nazo. Kwa hakika, ni raha na starehe za muda mchache na neema ndogo, ambayo Tunatumia kuwajaribu kwayo. Na ni wachache miongoni mwa waja Wangu wanaoshukuru kweli kweli".

Na amesema Mujaahid:

أَزْوَاجًا مِنْهُمْ

*"Baadhi ya watu miongoni mwao."*

Maana yake: “Matajiri”<sup>1</sup>. Hakika Allah تعالى Amekupa vizuri zaidi kuliko walivyopewa wao, kama Alivyosema katika Aya nyingine:

وَلَقَدْ آتَيْنَاكَ سَبْعًا مِّنَ الْمَثَانِي وَالْقُرْآنَ الْعَظِيمَ ﴿١٧٧﴾ لَا تَمُدَّنَّ عَيْنَيْكَ

**“Na Tumekupa hizi ayah saba zisomwazo mara kwa mara, na Tumekupa Qur’ani Tukufu. Usinyooshe macho yako...” (15:87-88).**

Na hasa yale Allah تعالى Aliyomuwekea Mtume Wake siku ya kiama Akhera ni jambo kubwa sana. Ni malipo yasiyo na kikomo ambayo hayawezi kuelezeka, kama Alivyoeleza Aliyetukuka:

وَلَسَوْفَ يُعْطِيكَ رَبُّكَ فَتَرْضَىٰ ﴿٩٣﴾

**“Na Mola wako Mlezi Atakupa mpaka uridhike.” (93:5)**

Kwa sababu hii Allah تعالى Amesema:

وَرَزَقْنَاكَ حَيْرًا وَأَبْقَىٰ ﴿١٠٠﴾

**“Na riziki ya Mola wako Mlezi ni bora mno na iendeleayo”.**

Na katika Hadithi Sahihi imenukuliwa kuwa pindi ‘Umar bin Al-Khatwtwaab رضي الله عنه alipoingia katika chumba kidogo cha Mtume ﷺ alipokuwa amejitenga na wakeze alipokula kiapo kukaa mbali nao. Alipoingia (‘Umar رضي الله عنه), alimuona (Mtume ﷺ) amejinyoosha kwenye kijamvi juu ya mchanga. Hakukuwa na kitu kingine chochote chumbani humo ila mkusanyiko wa maganda ya mti na vifaa vingine vilivyotundikwa. Macho ya ‘Umar رضي الله عنه yalidondokwa na machozi (kwa kuona hayo), hivyo Mtume ﷺ alimuuliza,

«مَا يُبْكِيكَ يَا عُمَرُ؟»

**“Ewe ‘Umar! Ni lipi linalokuliza?”**

Akajibu: Ewe Mtume wa Allah! Hakika Kisra na Kaisari wanaishi maisha ya starehe na raha, ilhali wewe ni Mteule na Rafiki wa Allah تعالى miongoni mwa viumbe Vyake?” Mtume ﷺ alimjibu:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 17:141.

«أَوْ فِي شَكِّ أَنْتَ يَا ابْنَ الْخَطَّابِ؟ أَوْلَيْكَ قَوْمٌ عَجَلَتْ لَهُمْ طِبَابُهُمْ فِي حَيَاتِهِمْ  
الدُّنْيَا»

*“Je, una shaka, ewe mtoto wa Al-Khatwtwaab? Watu hao wamefanyiwa haraka kupatiwa mazuri yao hapa duniani”<sup>1</sup>.*

Hivyo, Mtume ﷺ alikuwa msitari wa mbele katika kuupa nyongo ulimwengu, japokuwa alikuwa na uwezo wa kupata starehe hizo. Hata alipokuwa akipata mali ya duniani alikuwa akiigawa kwa waja wa Allah تعالى. Hakuwa ni mwenye kuweka akiba ya kitu chochote (kwa ajili yake yeye mwenyewe) kwa ajili ya kesho. Amepokea Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى kutoka kwa Abi Said Al-Khudriy رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ أَخْوَفَ مَا أَخَافَ عَلَيْكُمْ مَا يَفْتَحُ اللَّهُ لَكُمْ مِنْ زَهْرَةِ الدُّنْيَا»

*“Hakika, kitu ninachowahofia sana, ni mutakachofunguliwa na Allah katika mapambo ya Dunia”.*

Wakasema: “Na ni nini mapambo ya dunia, ewe Mtume wa Allah?” Akasema:

«بَرَكَاتُ الْأَرْضِ»

*“Baraka na neema za ardhi”<sup>2</sup>.*

Na wamesema Qataadah na As-Suddiy: “Mapambo ya maisha ya dunia”<sup>3</sup>, Maana: Mapambo mazuri ya maisha ya dunia. Na amesema Qataadah:

لِنَفْتِيَهُمْ فِيهِ

*“Ili Tuwafanyie mtihani kwavyo.”*

Tuwajaribu kwa kuwapatia mtihani<sup>4</sup>.

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baariy 5:137.

<sup>2</sup> Ibn Abi Haatim 7:2442.

<sup>3</sup> Atw-Twabariy 18:404.

<sup>4</sup> Atw-Twabariy 18:405.



Na Kauli Yake:

وَأْمُرْ أَهْلَكَ بِالصَّلَاةِ وَاصْطَبِرْ عَلَيْهَا<sup>ط</sup>

***“Na waamrishe watu wako kuswali, na uendelee mwenyewe kwa hayo.”***

Maana yake: Kuwaokoa wao na adhabu ya Allah kwa kusimamisha Sala, na wewe mwenyewe usubiri katika kutekeleza Sala hiyo.

Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا قَوْا أَنفُسَكُمْ وَأَهْلِيكُمْ نَارًا

***“Enyi Mlioamini! Jiokoeni nafsi zenu na watu wenu na Moto.”***  
**(66:6).**

Na amepokea Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى kutoka kwa Zayd bin Aslam kutoka kwa babake kuwa alikuwa yeye na Yarfaa' wakitumia usiku kwenye nyumba ya 'Umar bin Khatwtwaab رضي الله عنه. 'Umar رضي الله عنه alikuwa na wakati kila usiku ambamo aliamka na kuswali. Hata hivyo, siku nyingine alikuwa haamki. Kisha, tulikuwa tukisema: “Hataamka kama kawaida yake”. Alipokuwa akiamka alikuwa akiyamsha familia yake. Wakati huo alikuwa akisema:

وَأْمُرْ أَهْلَكَ بِالصَّلَاةِ وَاصْطَبِرْ عَلَيْهَا<sup>ط</sup>

***“Na waamrishe watu wako kuswali, na uendelee mwenyewe kwa hayo.”<sup>1</sup>***

Na Kauli Yake:

لَا نَسْأَلُكَ رِزْقًا نَحْنُ نَرْزُقُكَ<sup>ط</sup>

***“Hatukuombi riziki bali Sisi ndio Tunakuruzuku.”***

Maana yake: unaposimamisha Swala, basi riziki hukujia kwa njia usiyo idhania, kama Alivyosema Aliyetukuka:

<sup>1</sup> At-Tabari 18:406. Isnadi yake ni dhaifu. Taz. “Al-Ilali” 2:45

وَمَنْ يَتَّقِ اللَّهَ يَجْعَلْ لَهُ مَخْرَجًا ۖ وَيَرْزُقْهُ مِنْ حَيْثُ لَا يَحْتَسِبُ ۗ

**“Na anayemuogopa Allah, Humtengenezea njia ya kuokoka. Na Humpa riziki kwa namna asiyoitazamia.” (66:2-3).**

Na Amesema Aliyetukuka:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّ وَالْإِنْسَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ ﴿٥١﴾

**“Sikuwaumba majini na watu ila wapate Kuniabudu.” Mpaka:**

إِنَّ اللَّهَ هُوَ الرَّزَّاقُ ذُو الْقُوَّةِ الْمَمِينُ ﴿٥٨﴾

**“Kwa yakini Allah ndiye Mtoaji wa riziki, Mwenye Nguvu, Madhubuti.” (51: 56-58).**

Kwa hiyo hapa Akasema:

لَا نَسْأَلُكَ رِزْقًا نَحْنُ نَرْزُقُكَ ۗ

**“Hatukuombi riziki bali Sisi ndio Tunaokuruzuku”.**

Na hakika imepokewa na At-Tirmidhiy na Ibn Maajah kutoka kwa Abu Hurayrah عنه رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«يَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى: يَا ابْنَ آدَمَ فَفَرِّغْ لِعِبَادَتِي أَمْلَأُ صَدْرَكَ غِنًى وَأَسُدُّ فَتْرَكَ، وَإِنْ لَمْ تَفْعَلْ، مَلَأْتُ صَدْرَكَ شُغْلًا وَلَمْ أَسُدِّ فَتْرَكَ»

**“Anasema Allah تعالى: ‘Ewe mwana wa Adam, jitenge kwa ajili ya kuniabudu, Nami nitajaza kifua chako utajiri na Kukuondolea ufukara. Na ikiwa hutafanya hivyo, basi Nitajaza kifua chako shughuli wala sitakuondolea ufukara”<sup>1</sup>.**

Na pia imepokewa kutoka kwa Zayd bin Thaabit عنه رضي الله عنه kuwa alimsikia Mtume ﷺ akisema:

«مَنْ كَانَتْ الدُّنْيَا هَمَّهُ فَرَّقَ اللَّهُ عَلَيْهِ أَمْرَهُ، وَجَعَلَ فَتْرَهُ بَيْنَ عَيْنَيْهِ، وَلَمْ يَأْتِهِ مِنَ الدُّنْيَا إِلَّا مَا كُتِبَ لَهُ، وَمَنْ كَانَتْ الْآخِرَةُ نِيَّتَهُ، جَمَعَ لَهُ أَمْرُهُ وَجَعَلَ غِنَاهُ فِي قَلْبِهِ، وَأَتَتْهُ الدُّنْيَا وَهِيَ رَاعِمَةٌ»

<sup>1</sup> Tuhfatul Al-Ahwadhiy 7:166 na Ibn Maajah 2:1376.

“Mwenye kuifanya dunia ndio hamu yake, Allah Humfanyia ugumu mambo yake na ufukara wake utawekwa baina ya macho yake. Na hatapata chochote duniani ila alichandikiwa. Na yeyote mwenye kuweka nia yake kwa ajili ya Akhera, hali yake itakuwa nzuri na sahali na utajiri wake utakuwa moyoni mwake. Hata hivyo, maisha ya duniani yatamjia (mbali na kuwa hayataki)”<sup>1</sup>.

Na Kauli Yake:

وَالْعِقَبَةُ لِلتَّقْوَىٰ

“Na mwisho mwema utawathubutikia wamchao Mungu.”

Maana: Mwisho mwema hapa duniani na Kesho Akhera. Na mwisho mwema Akhera ni kuingizwa Peponi kwa wamchao Allah تعالیٰ. Na katika Hadithi Sahihi, Mtume ﷺ amesema:

«رَأَيْتُ الذَّبِيلَةَ كَأَنَّهَا فِي دَارِ عُقْبَةَ بْنِ رَافِعٍ، وَأَنَا أُتِينَا بِرُطَبٍ مِنْ رُطَبِ ابْنِ طَابٍ، فَأَوَّلْتُ ذَلِكَ أَنَّ الْعَاقِبَةَ لَنَا فِي الدُّنْيَا وَالرَّافِعَةَ، وَأَنَّ دِينَنَا قَدْ طَابَ»

“Niliona ndoto usiku wa leo kama kwamba tuko nyumbani kwa ‘Uqbah bin Raafi’, na humo tukapatiwa tende mbivu za Ibn Twaab. Kwa hiyo, nimeifasiri ndoto hiyo kumaanisha kuwa mwisho mwema ni wetu pamoja na kunyanyuliwa daraja kubwa, na kuwa Dini yetu ni nzuri”<sup>2</sup>.

وَقَالُوا لَوْلَا يَأْتِينَا بِغَايَةِ مَن رَّبِّهِمْ أَوْلَمَ تَأْتِيهِمْ بَيِّنَةٌ مَّا فِي الصُّحُفِ الْأُولَىٰ ۗ وَلَوْ أَنَّا  
 أَهْلَكْنَاهُمْ بِعَذَابٍ مِّن قَبْلِهِ لَقَالُوا لَوْلَا أَرْسَلْتَ إِلَيْنَا رَسُولًا فَنَتَّبِعَ آيَاتِكَ مِن قَبْلِ  
 أَنْ نُنذَلَ وَنُخْزَىٰ ۗ قُلْ كُلُّ مُتَرَبِّصٍ فَتَرَبُّصُوا ۗ فَسَتَعْلَمُونَ مَن أَصْحَابُ الصِّرَاطِ  
 السَّوِيِّ وَمَنِ اهْتَدَىٰ

**133. Na makafiri walisema: Kwa nini hakutuletea Miujiza kutoka kwa Mola wake Mlezi? Je, hazikuwajia dalili wazi zilizomo katika Vitabu vya kale?**

<sup>1</sup> Ibn Maajah 2:1375.

<sup>2</sup> Muslim 4:1779. Ibn Twaab ni jina la tende zilizo maarufu sana.

**134. Na lau kama Tungaliwaangamiza kwa adhabu kabla ya kuja huyo (Mtume), wangesema: Ewe Mola wetu Mlezi! Kwa nini Usituletee Mtume tukazifuata Aya Zako kabla kudhilika hivi na kufedheheka?**

**135. Sema: Kila mmoja (katika sisi) anangoja jaza yake. Basi ngojeni, Nasi Tunangoja! Hivi karibuni mtajua ni nani mwenye njia iliyo sawa na ni nani aliyongoka.**

### Ombi la Washirikina Kutaka Muujiza ilihali Qur'ani Yenyewe ni Muujiza

Allah تعالی Anatupasha habari kuhusu makafiri kwa kauli yao:

لَوْلَا

**“Kwa nini?”** Maana yake: Kwa nini Muhammad ﷺ hatuletei dalili na muujiza kutoka kwa Mola wake Mlezi? Walimaanisha alama itakayokuwa dalili ya ukweli kuwa yeye ni Mtume? Anasema Allah تعالی:

أَوْلَمْ تَأْتِهِمْ بَيِّنَةٌ مَّا فِي الصُّحُفِ الْأُولَىٰ ﴿١٣١﴾

**“Je, hazikuwajia dalili wazi zilizomo katika Vitabu vya kale?”**

Maana: Qur'ani Tukufu ambayo ameteremshiwa na Allah تعالی, naye ni *Ummiy* (hajui kusoma wala kuandika) wala hakusoma pamoja na Watu wa Kitabu. Hata hivyo, Qur'ani inayo maalumati kuhusu watu waliotangulia (wa awali) kwa kuelezea matukio yao kwa nyakati zilizopita na hayo yanakubaliana na maelezo sahihi katika Vitabu vilivyotangulia kuhusu mambo haya. Qur'ani inavihukumia Vitabu vyengine, kinasadikisha yaliyo sahihi na kubainisha makosa yaliyozuliwa. Na hii ni kama Kauli ya Aliyetukuka katika Suratul Ankaboot:

وَقَالُوا لَوْلَا أُنزِلَ عَلَيْهِ آيَاتٌ مِّن رَّبِّهِ ۗ قُلْ إِنَّمَا الْآيَاتُ عِندَ اللَّهِ وَإِنَّمَا أَنَا نَذِيرٌ

مُّبِينٌ ﴿١٣٢﴾ أَوْلَمْ يَكْفِهِمْ أَنَا أَنْزَلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ يُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ ۗ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ

لَرَحْمَةً وَذِكْرَىٰ لِقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿١٣٣﴾

**“Na walisema: Mbona hakuteremshiwa miujiza kutoka kwa Mola wake Mlezi? Sema: Miujiza iko Kwake Allah tu, nami hakika ni**

**muonyaji mbainishaji dhahiri tu. Je, hayakuwatosha ya kwamba Tumekuteremshia Kitabu hiki wanachosomewa? Bila shaka katika hayo muna rehema na mawaidha kwa watu wanaoamini.” (29: 50-51).**

Na katika Sahihi mbili, Mtume ﷺ amesema:

«مَا مِنْ نَبِيٍّ إِلَّا وَقَدْ أُوتِيَ مِنَ الْآيَاتِ مَا آمَنَ عَلَىٰ مِثْلِهِ الْبَشَرُ، وَإِنَّمَا كَانَ الَّذِي أُوتِيَهُ وَحْيًا أَوْحَاهُ اللَّهُ إِلَيَّ، فَأَرْجُو أَنْ أَكُونَ أَكْثَرَهُمْ تَابِعًا يَوْمَ الْقِيَامَةِ»

*“Hakuna Nabii (Mtume) yeyote ila alipewa miujiza iliyowafanya watu waamini. Na hakika kile nilichopewa ni Wahyi Alioniteremshia Allah, nataraji kuwa nitakuwa na wafuasi wengi (miongoni mwa Manabii) Siku ya Kiyama”<sup>1</sup>.*

Katika Hadithi hii, Mtume ﷺ ametaja tu muujiza mkubwa kabisa aliopewa, nao ni Qur’ani. Hata hivyo, alikuwa na miujiza mengine isiyoweza kuhesabika, kama vile ambavyo miujiza hiyo imeandikwa katika vitabu vinavyozungumzia hilo. Kisha Akasema Aliyetukuka:

وَلَوْ أَنَا أَهْلَكْتَهُمْ بَعْدَ أَنْ مَنَ قَبْلِهِمْ لَقَالُوا رَبَّنَا لَوْلَا أَرْسَلْتَ إِلَيْنَا رَسُولًا

**“Na lau kama Tungaliwaangamiza kwa adhabu kabla ya kuja huyo (Mtume), wangesema: Ewe Mola wetu Mlezi! Kwa nini Usituletee Mtume...”,**

Maana: Lau Tungewaangamiza hawa watu waliokataa na kukadhibisha kabla ya Kuwapelekea Mtume ﷺ Mtukufu na Kuwateremshia Kitabu kitukufu, wangesema,

رَبَّنَا لَوْلَا أَرْسَلْتَ إِلَيْنَا رَسُولًا

**“Ewe Mola wetu Mlezi! Kwa nini Usituletee Mtume.”**

Maana: Kabla ya kutuagamiza, ili tupate kumuamini na kumfuata. Kama Walivyosema:

فَتَتَّبِعْ آيَاتِكَ مِنْ قَبْلِ أَنْ نُنزِلَ وَنُحْزِمَ ﴿١٣٥﴾

**“Tukazifuata ayah Zako kabla kudhilika hivi na kufedheheka?”**

<sup>1</sup> Fat’h ul Al-Baariy 8:619 na Muslim 1:134.

Anatubainishia Aliyetukuka kuwa hawa waliokadhibisha ni wakaidi wenye inadi wala hawataamini.

وَلَوْ جَاءَهُمْ كُلُّ آيَةٍ حَتَّى يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٩٧﴾

**“Japokuwa kila ishara itawajia; mpaka waone adhabu iumizayo.”**  
(10:97).

Ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَهَذَا كِتَابٌ أَنْزَلْنَاهُ مُبَارَكٌ فَاتَّبِعُوهُ وَاتَّقُوا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿٩٨﴾

**“Na hii Qur’ani ni Kitabu Tulichokiteremsha kwenu, kilicho na baraka nyingi. Basi kifuateni na muwe wachamungu ili murehemewe.”**

Mpaka Kauli Yake,

بِمَا كَانُوا يَصْدِفُونَ ﴿٩٩﴾

**“Kwa sababu ya kule kujitenga kwao.”** (6:155-157).

Na Amesema:

وَأَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ لَئِن جَاءَهُمْ نَذِيرٌ لَّيَكُونُنَّ أَهْدَىٰ مِنْ إِحْدَى الْأُمَمِ ﴿٤٢﴾

**“Na (hawa makafiri hapo zamani) waliapa kwa Allah kiapo chao kilicho kikubwa wakasema: Akiwajia Muonyaji, bila shaka watakuwa waongofu zaidi kuliko taifa jingine lolote.”** (35:42).

Na Amesema:

وَأَقْسَمُوا بِاللَّهِ جَهْدَ أَيْمَانِهِمْ لَئِن جَاءَهُمْ آيَةٌ لَّيُؤْمِنُنَّ بِهَا ﴿١٠٩﴾

**“Na (makafiri) waliapa kwa Allah kwa viapo vyenye nguvu, kama ikiwafikia miujiza wataiamini.”** (6:109).

Kisha Akasema Aliyetukuka:

قُلْ

**“Sema”,** Maana yake: Ewe Muhammad ﷺ, kwa yeyote mwenye kukukadhibisha, akaenda kinyume nawe na akaendelea kukufuru (au kukanusha) na inadi pamoja na ukaidi wake,

كُلُّ مُتَرَيِّصٍ

**“Kila mmoja anangoja jaza yake...”**

Maana yake: Kati yetu.

فَتَرْتَضُوا

**“Basi ngojeni...”**

Maana yake: Hii ni Amri ya kuwa wasubiri kwa kungojea.

فَسَتَعْلَمُونَ مَنْ أَصْحَابُ الصِّرَاطِ السَّوِيِّ

**“Hivi karibuni mutajua ni nani mwenye njia iliyo sawa...”**

Maana yake: Njia nyoofu.

وَمَنْ أَهْتَدَى

**“Na ni nani aliyeongoka.”**

Katika haki na njia ya uongofu. Na hii ni kama Kauli Yake Aliyetukuka:

وَسَوْفَ يَعْلَمُونَ حَيْثُ يَرَوْنَ الْعَذَابَ مَنْ أَضَلُّ سَبِيلًا

**“Karibu watajua, watakapoiona adhabu, ni nani aliyepotea njia.”**

(25:42)

Na Amesema:

سَيَعْلَمُونَ غَدًا مِّنَ الْكَذَّابِ الْأَشْرُرِ

**“Watajua kesho ni nani muongo anayejiona.” (54:26)**

Mwisho wa Tafsiri ya Sura Twaha. Na Allah تعالیٰ, Ndiye Mwenye Kustahiki Sifa zote njema na Ihsani. Inayofuatia Anapopenda Allah تعالیٰ ni Tafsiri ya Suratul-Ambiyaa’.

\* \* \*





## Tafsiri ya Suratul Anbiyaa

### Sura ya 21

#### Iliteremshwa Makkah

#### Fadhila za Suratul-Anbiyaa

Bukhaariy Amepokea kutoka kwa 'Abdur-Rahman bin Yazid kuwa 'Abdallaah amesema: "Banu Israa'il<sup>1</sup>, Al-Kahf, Maryam, Twaha na Al- Anbiyaa – ni miongoni mwa Sura za mwanzo (kuteremshwa), nazo ni katika Sura nzuri sana na ni hazina yangu."<sup>2</sup>



---

<sup>1</sup> Suratul Israa' (17).

<sup>2</sup> Fat'hul Al-Baariy 4:289.

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْأَنْبِيَاءِ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

أَقْرَبَ لِلنَّاسِ حِسَابُهُمْ وَهُمْ فِي غَفْلَةٍ مُّعْرِضُونَ ﴿١﴾ مَا يَأْتِيهِمْ مِنْ ذِكْرٍ مِنْ رَبِّهِمْ مُحَدَّثٍ إِلَّا أَسْتَمِعُوهُ وَهُمْ يَلْعَبُونَ ﴿٢﴾ لَاهِيَةً قُلُوبُهُمْ ۗ وَأَسْرَأُ النَّجْوَى الَّذِينَ ظَلَمُوا هَلْ هُنَا إِلَّا بَشْرٌ مِثْلُكُمْ ۗ أَفَتَأْتُونَ السَّحْرَ وَأَنْتُمْ تُبْصِرُونَ ﴿٣﴾ قَالَ رَبِّي يَعْلَمُ الْقَوْلَ فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۗ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٤﴾ بَلْ قَالُوا أَضْغَثٌ أَحْلَمَ بَلِ افْتَرَاهُ بَلْ هُوَ شَاعِرٌ فَلْيَأْتِنَا بِآيَةٍ كَمَا أُرْسِلَ الْأَوْلُونَ ﴿٥﴾ مَا ءَامَنَتْ قَبْلَهُمْ مِنْ قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَاهَا ۗ أَفَهُمْ يُؤْمِنُونَ ﴿٦﴾ وَمَا أَرْسَلْنَا قَبْلَكَ إِلَّا رِجَالًا نُوْحِي إِلَيْهِمْ ۗ فَسَلُوا أَهْلَ الذِّكْرِ إِنْ كُنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٧﴾ وَمَا جَعَلْنَاهُمْ جَسَدًا لَا يَأْكُلُونَ الطَّعَامَ وَمَا كَانُوا خَالِدِينَ ﴿٨﴾ ثُمَّ صَدَقْنَاهُمُ الْوَعْدَ فَأَنْجَيْنَاهُمْ وَمَنْ نَشَاءُ وَأَهْلَكْنَا الْمُسْرِفِينَ ﴿٩﴾

أَقْرَبَ لِلنَّاسِ حِسَابُهُمْ وَهُمْ فِي غَفْلَةٍ مُّعْرِضُونَ ﴿١﴾ مَا يَأْتِيهِمْ مِنْ ذِكْرٍ مِنْ رَبِّهِمْ مُحَدَّثٍ إِلَّا أَسْتَمِعُوهُ وَهُمْ يَلْعَبُونَ ﴿٢﴾ لَاهِيَةً قُلُوبُهُمْ ۗ وَأَسْرَأُ النَّجْوَى الَّذِينَ ظَلَمُوا هَلْ هُنَا إِلَّا بَشْرٌ مِثْلُكُمْ ۗ أَفَتَأْتُونَ السَّحْرَ وَأَنْتُمْ تُبْصِرُونَ ﴿٣﴾ قَالَ رَبِّي يَعْلَمُ الْقَوْلَ فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۗ وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٤﴾ بَلْ قَالُوا أَضْغَثٌ أَحْلَمَ بَلِ افْتَرَاهُ بَلْ هُوَ شَاعِرٌ فَلْيَأْتِنَا بِآيَةٍ كَمَا أُرْسِلَ الْأَوْلُونَ ﴿٥﴾ مَا ءَامَنَتْ قَبْلَهُمْ مِنْ قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَاهَا ۗ أَفَهُمْ يُؤْمِنُونَ ﴿٦﴾

1. Imewakaribia watu hesabu yao, nao wamo katika pumbao wanapuuza.

2. Hayawafikilii mawaidha mapya kutoka kwa Mola wao Mlezi ila huyasikiliza na huku wanafanya mchezo.

**3. Zimeghafilika nyoyo zao. Na wale waliodhulumu hunong'onezana kwa siri: Ni nani ati huyu isipokuwa ni binadamu tu kama nyinyi! Munauwendea uchawi hali nanyi mnaona?**

**4. Alisema: Mola wangu Mlezi anayajua yasemwayo mbinguni na katika ardhi. Na Yeye ni Mwenye Kusikia Mwenye Kujua.**

**5. Lakini wao walisema: Hizo ni ndoto za ovyo ovyo, bali amezizua tu, bali huyo ni mtunga mashairi. Basi atuletee miujiza kama walivyotumwa wale wa mwanzo.**

**6. Hawakuamini kabla yao watu wa mji Tuliouangamiza. Basi, je, wataamini hawa?**

### Saa Ipo Karibu na Watu Wameghafilika

Hili ni onyo kutoka kwa Allah تعالیٰ kuwa Kiyama kimekaribia sana, na hakika watu wameghafilika nacho. Maana: Hawafanyi amali kwa ajili yake wala kujitayarisha nacho. Na imepokewa na An-Nasaa'iy kutoka kwa Abi Sa'id kuwa Mtume ﷺ amesema:

عَفَلَةٌ مُّعْرَضُونَ ﴿١٦﴾

**“Nao wamo katika pumbao wanapuuza.”** Akasema ﷺ:

«فِي الدُّنْيَا»

Yaani duniani<sup>3</sup>.

Na Amesema Aliyetukuka:

أَتَىٰ أَمْرُ اللَّهِ فَلَا تَسْتَعْجِلُوهُ ۗ ﴿١٦﴾

**“Amri ya Allah itafika tu; basi msiihimize...” (16:1).**

أَقْرَبَتِ السَّاعَةُ وَانْشَقَّ الْقَمَرُ ﴿١٧﴾ وَإِنْ يَرَوْا آيَةً يُعْرَضُوا وَيَقُولُوا سِحْرٌ مُّسْتَمِرٌّ ﴿١٨﴾

**“Saa ya kufika Kiyama imekaribia; na mwezi umepasuka. Na wakiona muujiza hugeuka upande mwingine.” (54:1-2).**

<sup>1</sup> An-Nasaa'iy katika Al-Kubraa 6:407.

Kisha Allah تعالی Anatueleza kuwa hao watu hawasikilizi Wahyi Aliouteremsha kwa Mtume Wake, unaowahutubia Quraysh na makafiri kama wao.

مَا يَأْتِيهِمْ مِّنْ ذِكْرٍ مِّن رَّبِّهِمْ مُّحَدَّثٍ

**“Hayawafikilii mawaidha mapya kutoka kwa Mola wao Mlezi.”**

Maana yake: Kuteremshwa upya,

إِلَّا أَسْتَمِعُوهُ وَهُمْ يَلْعَبُونَ ﴿٢٠﴾

**“Ila huyasikiliza na huku wanafanya mchezo.”**

Hii ni kama alivyosema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما: “Kwa nini munawauliza Watu wa Kitabu kwa walicho nacho, ambacho kimebadilishwa na kugeuzwa, wameongeza na kupunguza vitu, ilhali Kitabu chenu ndicho kimeteremshwa upya kutoka kwa Allah تعالی, nanyi munakisoma kikiwa safi bila kughushiwa?” Al-Bukhaari amenukuu mfano wa riwaya hii<sup>1</sup>.

وَأَسْرُوا النَّجْوَى الَّذِينَ ظَلَمُوا

**“Na wale waliodhulumu hunong’onezana kwa siri.”**

Maana yake: Wanasemezana kwa siri baina yao.

هَلْ هَذَا إِلَّا بَشْرٌ مِّثْلَكُمُ

**“Ni nani ati huyu isipokuwa ni binadamu tu kama nyinyi!”**

Maana yake: Mtume ﷺ. Hawakuamini kuwa anaweza kuwa Nabii (Mtume) kwa kuwa alikuwa mwanadamu kama wao, vipi atachaguliwa yeye kupata Wahyi, na sio wao? Wakasema:

أَفَتَأْتُونَ السَّحَرَ وَالنَّجْمَ تُبْصِرُونَ ﴿٢١﴾

**“Munauwendea uchawi hali nanyi munaona?”**

Maana yake: Je, mutamfuata yeye, muwe kama yule anayenyenyekea uchawi anayejua kuwa huo ni uchawi? Allah تعالی Anawajibu kwa ule uzushi na uongo wao:

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Baariy 13:505.

قَالَ رَبِّي يَعْلَمُ الْقَوْلَ فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ط

**“Alisema: Mola wangu Mlezi Anayajua yasemwayo mbinguni na katika ardhi.”**

Hakuna kilichofichikana kutoka kwa Yule Anayejua hayo, Naye Ndiye Aliyeteremsha Qur’ani hii iliyo na habari ya vizazi vya mwanzo na baadaye. Hakuna anayeweza kuleta mfano wake ila Yule Mwenye Kujua siri za mbinguni na ardhini.

وَهُوَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ ﴿٢١﴾

**“Na Yeye ni Mwenye Kusikia Mwenye Kujua.”**

Maana yake: Anasikia yote wasemayo na Anajua hali zao zote. Hili ni onyo na tishio kwao.

**Mawazo na Dhana za Makafiri kwa Qur’ani na Mtume na Kutaka Muujiza na Kuthibitishwa Kwao**

بَلْ قَالُوا أَضْغَثٌ أَحْلَمَ بَلْ أَفْتَرْتَهُ

**“Lakini wao walisema: Hizo ni ndoto za ovyo ovyo.”**

Hapa Anatueleza Allah تعالی juu ya ukaidi na uasi wa makafiri, na mambo chungu nzima waliyosema kuhusu Qur’ani na vipi walivyochanganyikiwa na kupotea kuhusu hilo. Wakati mwingine walielezea kuwa ni uchawi, na wakati mwingine walisema kuwa ni mashairi, au mchanganyiko wa ndoto za uwongo, au uzushi. Hii ni kama Alivyosema Allah تعالی:

أَنْظُرْ كَيْفَ ضَرَبُوا لَكَ الْأَمْثَالَ فَضَلُّوا فَلَا يَسْتَطِيعُونَ سَبِيلًا ﴿٤٨﴾

**“Tazama vipi wanavyokupigia mifano. Basi wamepotea. Kwa hivyo hawawezi kuipata njia”. (17:48).**

Na Kauli Yake Allah تعالی,

فَلْيَأْتِنَا بَيِّنَاتٍ كَمَا أُرْسِلَ الْأَوَّلُونَ ﴿٥٠﴾

**“Basi atuletee miujiza kama walivyotumwa wale wa mwanzo.”**

Walikuwa wanakusudia mfano wa ngamia wa Nabii Swaalih عليه السلام, na muujiza wa Musa عليه السلام na 'Isa عليه السلام. Na Allah تعالى Akasema:

وَمَا مَنَعَنَا أَنْ نُرْسِلَ بِالْآيَاتِ إِلَّا أَنْ كَذَّبَ بِهَا الْأَوَّلُونَ

**“Na hapana kinachotuzuia kupeleka miujiza ila ni kuwa watu wa zamani waliikanusha.” (17:59)**

Hivyo, hapa Allah تعالى Anasema:

مَا آمَنَتْ قَبْلَهُمْ مِنْ قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَاهَا أَفَهُمْ يُؤْمِنُونَ ﴿٦١﴾

**“Hawakuamini kabla yao watu wa mji Tuliouangamiza. Basi, je, wataamini hawa?”**

Hakuna miongoni mwa kaumu zilizopita isipokuwa walipelekewa Mitume, walipatiwa miujiza mikononi mwa Manabii hao. Kinyume na hivyo, walikanusha, Nasi Tukawaangamiza kwa sababu ya hilo. Je, watu hawa wataamini muujiza wanapouona? Hawawezi kabisa! Hakika ni kuwa,

إِنَّ الَّذِينَ حَقَّتْ عَلَيْهِمْ كَلِمَتُ رَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٦٢﴾ وَلَوْ جَاءَهُمْ كُلُّ آيَةٍ حَتَّى يَرَوْا الْعَذَابَ الْأَلِيمَ ﴿٦٣﴾

**“Hakika wale ambao Neno la Mola wako Mlezi limekwi shathibitika juu yao, hawataamini. Ijapokuwa kila ishara itawajia; mpaka waone adhabu inayoumiza.” (10:96-97)**

Hakika, walishuhudia ishara na muujiza dhahiri kabisa kutoka kwa Mtume ﷺ, miujiza na ishara zilizokuwa wazi na kuyakinisha zaidi kuliko zilizoshuhudiwa kutoka kwa Mtume mwingine yeyote.

وَمَا أَرْسَلْنَا قَبْلَكَ إِلَّا رِجَالًا نُوْحِي إِلَيْهِمْ فَسَلُّوا أَهْلَ الذِّكْرِ إِنْ كُنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٦٤﴾ وَمَا جَعَلْنَاهُمْ جَسَدًا لَا يَأْكُلُونَ الطَّعَامَ وَمَا كَانُوا خَالِدِينَ ﴿٦٥﴾ ثُمَّ صَدَقْنَاهُمُ الْوَعْدَ فَأَنْجَيْنَاهُمْ وَمَنْ نَشَاءُ وَأَهْلَكْنَا الْمُسْرِفِينَ ﴿٦٦﴾

**7. Na kabla yako hatukuwatuma ila watu wanaume Tuliowapa wahyi (ufunuo). Basi waulizeni wenye elimu ikiwa nyinyi hamjui.**

**8. Wala hatukuwafanya miili isiyokula chakula, wala hawakuwa wenye kuishi milele.**

**9. Kisha Tukawatimizia miadi, na Tukawaokoa wao na Tuliowataka, na Tukawateketeza waliopita mipaka.**

### Mitume ni Binadamu

Hapa Allah تعالى Anapinga madai ya kuwa Mitume wanadamu hawawezi kutumwa:

وَمَا أَرْسَلْنَا قَبْلَكَ إِلَّا رِجَالًا نُوْحِي إِلَيْهِمْ

**“Na kabla yako hatukuwatuma ila watu wanaume Tuliowapa wahyi.”**

Maana yake: Mitume wote waliotumwa kabla yako walikuwa wanaume, wanadamu. Hakukuwa na Malaika miongoni mwao. Kama Alivyosema katika Aya nyingine:

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ إِلَّا رِجَالًا نُوْحِي إِلَيْهِمْ مِنْ أَهْلِ الْقُرَىٰ

**“Na Hatukutuma kabla yako isipokuwa wanaume Tuliowafunulia katika watu wa miji...” (12:109).**

Na Amesema Aliyetukuka:

قُلْ مَا كُنْتُ بِدَعَاٍ مِنَ الرُّسُلِ

**“Sema: Mimi si kiroja (mpya) katika Mitume...” (46:9).**

Na Amesema Aliyetukuka kuwa Umati zilizotangulia zilikataa hilo, wakasema:

أَبَشَرٌ مِّمَّنْ دُونَنَا

**“Oh! Watu wenzetu ndio watuongoze?” (64:6).** Hivyo, hapa Anasema:

فَسْأَلُوا أَهْلَ الذِّكْرِ إِنْ كُنْتُمْ لَا تَعْلَمُونَ ﴿٧﴾

**“Basi waulizeni wenye elimu ikiwa nyinyi hamujui.”**

Maana yake: Waulizeni wenye elimu miongoni mwa mataifa, kama vile Mayahudi, Manasara na makundi mengine: ‘Je, Mitume waliotumwa kwao walikuwa wanadamu au Malaika?’ Bila shaka walikuwa wanadamu. Na huu ni ule ukamilifu wa Neema ya Allah تعالى kwa viumbe Vyake: Aliwatumia Mitume miongoni mwao ili waweze kupata *risala* (ujumbe) na kujifundisha kutoka kwao. Na Kauli Yake:

وَمَا جَعَلْنَاهُمْ جَسَدًا لَّا يَأْكُلُونَ الطَّعَامَ

**“Wala hatukuwafanya miili isiyokula chakula.”**

Maana yake: Bali walikuwa na miili, wakila chakula (kama wanadamu wengine). Kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَمَا أَرْسَلْنَا قَبْلَكَ مِنَ الْمُرْسَلِينَ إِلَّا إِنَّهُمْ لَيَأْكُلُونَ الطَّعَامَ وَيَمْشُونَ فِي الْأَسْوَاقِ<sup>٤</sup>

**“Na Hatukupeleka kabla yako Mitume ila bila shaka walikuwa wakila chakula na wakenda masokoni.” (25:20),**

Maana yake: Walikuwa wanadamu waliokuwa wakila chakula na kunywa kama wanadamu wengine. Na pia walikuwa wakenda masokoni ili wapate chumo pamoja na kufanya biashara; bila shaka kufanya hivyo, hakukuwaathiri wala kuteremsha hadhi na cheo chao kwa njia yoyote ile, kama walivyodhania washirikina. Washirikina walikuwa wanasema:

‘ مَا لِهَذَا الرَّسُولِ يَأْكُلُ الطَّعَامَ وَيَمْشِي فِي الْأَسْوَاقِ<sup>٥</sup> لَوْلَا أَنْزَلَ إِلَيْهِ مَلَكٌ

فَيَكُونُ مَعَهُ نَذِيرًا ﴿٥﴾ أَوْ يُلْقَىٰ إِلَيْهِ كَنْزٌ أَوْ تَكُونُ لَهُ جَنَّةٌ يَأْكُلُ مِنْهَا

**“Mtume gani huyu anayekula chakula na anayekwenda masokoni! Mbona hakuteremshiwa Malaika awe muonyaji pamoja naye? Au mbona hakuangushiwa hazina; au kwa nini asiwe na bustani ale katika hiyo?” (25:7-8).**

Na Kauli Yake:

وَمَا كَانُوا خَالِدِينَ ﴿٦﴾

**“Wala hawakuwa wenye kuishi milele.”**

Maana yake: Hapa duniani, bali walikuwa wakiishi, kisha wakifariki dunia.



﴿٣٤﴾ وَمَا جَعَلْنَا لِبَشَرٍ مِّن قَبْلِكَ الْخُلْدَ أَفَإِن مِّن مَّتَّ فَهُمْ يَحْنَلُونَ ﴿٣٤﴾

***“Nasi Hatukumjaalia mwanadamu yeyote kabla yako kuwa na maisha ya milele.” (21:34)***

Tofauti yao (Mitume) na wanadamu wengine ni kuwa wao walikuwa wakiteremshiwa Wahyi kutoka kwa Allah تعالى, na Malaika walikuwa wakileta hukumu kwao kutoka kwa Allah تعالى kuhusu viumbe Vyake, Aliyoyaamuru na Aliyotakataza. Na Kauli ya Aliyetukuka:

ثُمَّ صَدَقْنَاهُمُ الْوَعْدَ

***“Kisha Tukawatimizia miadi.”***

Maana yake: Ile ahadi ya kuwa Mola wao Mlezi Atawaangamiza madhalimu. Allah تعالى Alitekeleza hilo kwa Kuwaangamiza. Kwa hiyo, Akasema hapa:

فَأَجْبَيْنَاهُمْ وَمَن نَّشَاءُ

***“Na Tukawaokoa wao na Tuliowataka.”***

Maana yake: Wafuasi wao miongoni mwa Waumini,

﴿٣٥﴾ وَأَهْلَكْنَا الْمُسْرِفِينَ ﴿٣٥﴾

***“Na Tukawateketeza waliopita mipaka.”***

Maana yake: Waliokanusha yale waliyokuja nayo Mitume.

\* \* \*

لَقَدْ أَنْزَلْنَا إِلَيْكُمْ كِتَابًا فِيهِ ذِكْرُكُمْ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿١٠﴾  
 وَكَمْ قَصَمْنَا مِنْ قَبْلِكَ ذِكْرًا فَكَانَتْ ظَالِمَةً وَأَنْشَأْنَا بَعْدَهَا قَوْمًا  
 آخَرِينَ ﴿١١﴾ فَلَمَّا أَحْسَسُوا بِأَسَاسِنَا إِذَا هُمْ مِنْهَا يَرْكُضُونَ  
 ﴿١٢﴾ لَا تَرْكُضُوا وَارْجِعُوا إِلَى مَا أُتْرِفْتُمْ فِيهِ وَمَسْكِنِكُمْ  
 لَعَلَّكُمْ تُشْعَلُونَ ﴿١٣﴾ قَالُوا يَبْوِئَلَنَا إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿١٤﴾  
 فَمَا زَالَتْ تِلْكَ دَعْوَاهُمْ حَتَّى جَعَلْنَاهُمْ حَصِيدًا  
 خَامِدِينَ ﴿١٥﴾ وَمَا خَلَقْنَا السَّمَاءَ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا  
 لَعِبِينَ ﴿١٦﴾ لَوْ أَرَدْنَا أَنْ نَتَّخِذَ لَهْوًا لَأَتَّخِذْنَاهُ مِنْ لَدُنَّا إِنْ  
 كُنَّا فَعِلِينَ ﴿١٧﴾ بَلْ نَقْذِفُ بِالْحَقِّ عَلَى الْبَاطِلِ  
 قَيْدًا مَغْمُورًا فِإِذَا هُوَ زَاهِقٌ وَلَكُمُ الْوَيْلُ مِمَّا تَصِفُونَ ﴿١٨﴾  
 وَاللَّهُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَنْ عِنْدَهُ لَا يَسْتَكْبِرُونَ  
 عَنْ عِبَادَتِهِ وَلَا يَسْتَحْسِرُونَ ﴿١٩﴾ يُسْحِرُونَ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ  
 لَا يَفْتُرُونَ ﴿٢٠﴾

لَقَدْ أَنْزَلْنَا إِلَيْكُمْ كِتَابًا فِيهِ  
 ذِكْرُكُمْ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿١٠﴾ وَكَمْ  
 قَصَمْنَا مِنْ قَبْلِكَ ذِكْرًا فَكَانَتْ ظَالِمَةً  
 وَأَنْشَأْنَا بَعْدَهَا قَوْمًا آخَرِينَ ﴿١١﴾  
 فَلَمَّا أَحْسَسُوا بِأَسَاسِنَا إِذَا هُمْ مِنْهَا  
 يَرْكُضُونَ ﴿١٢﴾ لَا تَرْكُضُوا  
 وَارْجِعُوا إِلَى مَا أُتْرِفْتُمْ فِيهِ  
 وَمَسْكِنِكُمْ لَعَلَّكُمْ تُشْعَلُونَ ﴿١٣﴾  
 قَالُوا يَبْوِئَلَنَا إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿١٤﴾  
 فَمَا زَالَتْ تِلْكَ دَعْوَاهُمْ حَتَّى  
 جَعَلْنَاهُمْ حَصِيدًا خَامِدِينَ ﴿١٥﴾

10. Na hakika Tumekute-remshieni Kitabu ambacho ndani yake yamo maku-

mbusho yenu. Je! Hamuzingatii?

11. Na mingapi katika miji iliyokuwa ikidhulumu Tumeiteketeza, na Tukawasimamisha baada yao watu wengine.

12. Basi walipoihisi Adhabu Yetu, mara wakaanza kukimbia.

13. Msikimbie! Na rejeeni kwenye zile zile starehe zenu, na maskani zenu, mpate kusailiwa!

14. Wakasema: Ole wetu! Hakika sisi tulikuwa madhalimu.

15. Hakikuacha hicho kuwa kilio chao mpaka Tukawafanya kama waliofyekwa, wamezimika.

## Fadhila za Qur'ani

Anasema Aliyetukuka kutuashiria hapa hadhi na cheo cha Qur'ani Tukufu na Kuwahimiza kutambua thamani yake:

لَقَدْ أَنْزَلْنَا إِلَيْكُمْ كِتَابًا فِيهِ ذِكْرُكُمْ<sup>ط</sup>

***“Na hakika Tumekuteremshieni Kitabu ambacho ndani yake yamo makumbusho yenu.”***

Amesema Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: “Ni utukufu kwenu.”<sup>1</sup>

أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٤٤﴾

***“Je, hamuzingatii?”***

Maana yake: Je, nyinyi hamuifahamu neema hii na kuikubali? Hii ni kama Kauli Yake Aliyetukuka:

وَإِنَّهُمْ لَذِكْرُ لَكَ وَلِقَوْمِكَ<sup>ط</sup> وَسَوْفَ تُسْأَلُونَ ﴿٤٤﴾

***“Na kwa yakini haya ni ukumbusho kwako na kwa watu wako, na karibuni hivi mutaulizwa.” (43:44)***

## Vipi Madhalimu Walivyoangamizwa?

Na Kauli Yake:

وَكَمْ قَصَمْنَا مِنْ قَرْيَةٍ كَانَتْ ظَالِمَةً

***“Na mingapi katika miji iliyokuwa ikidhulumu Tumeiteketeza.”***

Hii ni ibara ya kuonesha kuwa ilikuwa ni miji mingi. Hii ni kama Alivyosema:

وَكَمْ أَهْلَكْنَا مِنَ الْقُرُونِ مِنْ بَعْدِ نُوحٍ<sup>ط</sup>

***“Na kaumu ngapi Tumeziangamiza baada ya Nuuh!” (17:17).***

Na Amesema Aliyetukuka:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 21:611.

فَكَأَيُّ مِّنْ قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَاهَا وَهِيَ ظَالِمَةٌ فِيهَا خَاوِيَةٌ عَلَىٰ عُرُوشِهَا

**“Miji mingapi Tuliangamiza iliyokuwa ikidhulumu, ikawa imebaki magofu.” (22:45).**

Na Kauli Yake:

وَأَنْشَأْنَا بَعْدَهَا قَوْمًا آخَرِينَ ﴿٢١﴾

**“Na Tukawasimamisha baada yao watu wengine.”**

Maana yake: Ummah mwingine uliokuja baada yao.

فَلَمَّا أَحْسَوْا بِآسَاتِنَا

**“Basi walipoihisi Adhabu Yetu.”**

Maana yake: Walipoyakinisha kuwa adhabu itawafikia bila shaka yoyote, kama alivyowaahidi Nabii wao,

إِذَا هُمْ مِّنْهَا يَرْكُضُونَ ﴿٢٢﴾

**“Mara wakaanza kukimbia.”**

Maana yake: Walijaribu kukimbia.

لَا تَرْكُضُوا وَأَرْجِعُوا إِلَىٰ مَا أُتْرِفْتُمْ فِيهِ وَمَسْكِنِكُمْ

**“Msikimbie! Na rejeeni kwenye zile zile starehe zenu, na maskani zenu”.**

Hii ni njia ya kuwakejeli. Maana yake: Wataambiwa kwa njia ya kuwakejeli: “Msikimbie kutokana na adhabu inayokuja; rudini kwa yale mliokuwa nayo katika neema, furaha, maisha mazuri na maskani nzuri”. Amesema Qataadah: “Kuwapanyia stihzai wao:

لَعَلَّكُمْ تَسْأَلُونَ ﴿٢٣﴾

**“Mpate kusailiwa!”**

Maana yake: Kama mulikuwa mukishukuru neema (mliyopatiwa).

قَالُوا يَبْوِلْنَا إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿١٠﴾

**“Wakasema: Ole wetu! Hakika sisi tulikuwa madhalimu”.**

Wametambua dhambi zao wakati hilo halitawafalia chochote.

فَمَا زَالَتْ تِلْكَ دَعْوَاهُمْ حَتَّىٰ جَعَلْنَاهُمْ حَصِيدًا خَمِيدِينَ ﴿١١﴾

**“Hakikuacha hicho kuwa kilio chao mpaka Tukawafanya kama waliofyekwa, wamezimika.”**

Maana yake: Wataendelea kusema hayo, nayo ni kukiri dhulma waliyofanya, mpaka Tuwafyeke na kuzima mwendo wao na sauti zao kwa kuzizima kabisa.

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَاءَ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا لِعَيْنٍ ﴿١٢﴾ لَوْ أَرَدْنَا أَنْ نَتَّخِذَ لَهْوًا لَّاتَّخَذْتَهُ

مِن لَّدُنَّا إِنْ كُنَّا فَعَلِينَ ﴿١٣﴾ بَلْ نَقْذِفُ بِالْحَقِّ عَلَى الْبَاطِلِ فَيَدْمَغُهُ فَإِذَا هُوَ زَاهِقٌ ﴿١٤﴾

وَلَكُمْ الْوَيْلُ مِمَّا تَصِفُونَ ﴿١٥﴾ وَاللَّهُ مَن فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَنْ عِنْدَهُ لَا

يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِهِ وَلَا يَسْتَحْسِرُونَ ﴿١٦﴾ يُسَبِّحُونَ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ لَا يَفْتُرُونَ ﴿١٧﴾

**16. Na Hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyo baina yao kwa mchezo.**

**17. Kama Tungelitaka kufanya mchezo Tungejifanyia Sisi wenyewe, lau kwamba Tungelikuwa ni wafanyao mchezo.**

**18. Bali Tunaitupa haki juu ya batili ikavunja na mara ikatoweka. Na ole wenu kwa munayoyazua.**

**19. Na ni Vyake Yeye tu Allah vilivyomo mbinguni na katika ardhi. Na walioko Kwake hawafanyi kiburi wakaacha kumuabudu, wala hawachoki.**

**20. Wanamtakasa usiku na mchana, wala hawanyong'onyei.**

## Uumbaji Ulifanywa kwa Uadilifu na Hekima

Allah تعالى Anatuambia kuwa Ameumba mbingu na ardhi kwa haki. Maana: Kwa uadilifu.

لِيَجْزِيَ الَّذِينَ أَسْتَوُوا بِمَا عَمِلُوا وَيَجْزِيَ الَّذِينَ أَحْسَنُوا بِالْحُسْنَى ﴿٣١﴾

***“Ili Awalipe wabaya kwa hayo wanayoyatenda, na Kuwalipa mema wale wanaofanya mema.” (53:31).***

Na hakika Hakuumba vyote hivyo kwa upuuzi na mchezo. Kama Alivyosema:

وَمَا خَلَقْنَا السَّمَاءَ وَالْأَرْضَ وَمَا بَيْنَهُمَا بَطْلًا ۚ ذَٰلِكَ ظَنُّ الَّذِينَ كَفَرُوا ۚ فَوَيْلٌ لِلَّذِينَ  
كَفَرُوا مِنَ النَّارِ ﴿٣٧﴾

***“Na Hatukuziumba mbingu na ardhi na vilivyomo ndani yake bure. Hii ni dhana ya wale waliokufuru. Basi adhabu kali ya Moto itawathibitikia wale waliokufuru.” (38:27).***

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

لَوْ أَرَدْنَا أَنْ نَتَّخِذَ هَٰؤُلَاءِ لَاتَّخِذْنَهُ مِنْ لَدُنَّا إِنْ كُنَّا فَعَالِينَ ﴿٤٧﴾

***“Kama Tungelitaka kufanya mchezo Tungejifanyia Sisi wenyewe, lau kwamba Tungelikuwa ni wafanyao mchezo”.***

Ampokea Ibn Abi Najiih kuwa Mujaahid amesema:

لَوْ أَرَدْنَا أَنْ نَتَّخِذَ هَٰؤُلَاءِ لَاتَّخِذْنَهُ مِنْ لَدُنَّا

***“Kama Tungelitaka kufanya mchezo Tungejifanyia Sisi wenyewe.”***

Maana yake: Kutoka Kwetu. Anasema: Na Hatungeumba Pepo, Moto, Umauti, Ufufuo na Hesabu”<sup>1</sup>. Na Kauli Yake:

إِنْ كُنَّا فَعَالِينَ ﴿٤٧﴾

***“Lau kwamba Tungelikuwa ni wafanyao mchezo”.***

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:421.

Amesema Qataadah<sup>1</sup>, As-Suddiy, Ibraahim An-Nakhaa'iy na Mughirah bin Miqsam: "Hiyo ina maana, 'Hatutafanya hivyo".

Na amesema Mujaahid: "Kila mara neno hili linapokuja katika Qur'ani:

إِنْ

**"Lau."**

Huwa lina maana ya "kukataa"<sup>2</sup>.

Na Kauli Yake:

بَلْ نَقْذِفُ بِالْحَقِّ عَلَى الْبَاطِلِ

**"Bali Tunaitupa haki juu ya batili."**

Maana yake: Tunaibainisha haki, hivyo kuushinda uwongo. Kwa hiyo Akasema:

فَيَدْمَغُهُ فَإِذَا هُوَ زَاهِقٌ

**"Ikaivunja na mara ikatoweka."**

Maana yake: ikafifia na kutoweka.

وَلَكُمْ أَلْوِيلٌ

**"Na ole wenu."**

Maana yake: Enyi wenye kusema kuwa Allah تعالی Ana mtoto.

مِمَّا تَصِفُونَ

**"Kwa mnayoyazua."**

Maana yake: Mnayoyasema na kuyazua.

Kisha Anatupasha habari Aliyetukuka kuhusu utumwa wa Malaika, na jinsi gani wanavyodumu na kusubiri katika Ibada usiku na mchana. Akasema:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:420.

<sup>2</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 5:620.

Kila Kitu ni Miliki ya Allah تعالى na Kinamtumikia Yeye

وَلَهُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَنْ عِنْدَهُ

**“Na ni Vyake Yeye tu Allah vilivyomo mbinguni na katika ardhi. Na walioko Kwake.”**

Maana yake: Malaika.

لَا يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِهِ

**“Hawafanyi kiburi wakaacha kumuabudu.”**

Maana yake: Hawana kiburi wala hawakatai kumuabudu Yeye. Hii ni kama Aya ifuatayo:

لَنْ يَسْتَنْكِفَ الْمَسِيحُ أَنْ يَكُونَ عَبْدًا لِلَّهِ وَلَا الْمَلَائِكَةُ الْمُقَرَّبُونَ وَمَنْ يَسْتَنْكِفْ عَنْ عِبَادَتِهِ وَيَسْتَكْبِرْ فَسَيَحْشُرُهُمْ إِلَيْهِ جَمِيعًا ﴿١٧٦﴾

**“Masihi hataona unyonge kuwa mja wa Allah, wala Malaika waliokurubishwa (na Allah). Na watakaouona unyonge uja wa Mungu na kutakabari, basi Atawakusanya wote Kwake (Awatie Motoni).” (4:172)**

Na Kauli Yake:

وَلَا يَسْتَحْسِرُونَ ﴿١٧٧﴾

**“Wala hawachoki.”** Maana yake: Hawachoki wala hawahisi usumbufu.

يُسَبِّحُونَ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ لَا يَفْتُرُونَ ﴿١٧٨﴾

**“Wanamtakasa usiku na mchana, wala hawanyong’onyei.”**

Wao wanaendelea bila kusita katika Ibada zao usiku na mchana, wakimtii Allah تعالى kwa kukusudia na kwa amali, na wanaweza kufanya hivyo. Kama Alivyosema Aliyetukuka:

لَا يَعْصُونَ اللَّهَ مَا أَمَرَهُمْ وَيَفْعَلُونَ مَا يُؤْمَرُونَ ﴿١٧٩﴾

**“Hawamuasi Allah kwa Amri Zake; na wanatenda wanayoamrisha.”(66:6).**



أَمِ اتَّخَذُوا إِلَهًا مِّنَ الْأَرْضِ هُمْ يُنشِرُونَ ﴿٢١﴾ لَوْ كَانَ  
 فِيهَا إِلَهَةٌ إِلَّا اللَّهُ لَفَسَدَتَا ۗ فَسُبْحَانَ اللَّهِ رَبِّ الْعَرْشِ  
 عَمَّا يُصِفُونَ ﴿٢٢﴾ لَا يُسْأَلُ عَمَّا يَفْعَلُ وَهُمْ يُسْأَلُونَ  
 ﴿٢٣﴾ أَمِ اتَّخَذُوا مِن دُونِهِ إِلَهًا ۗ قُلْ هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ ۗ  
 هَذَا ذِكْرٌ مِّن مَّعَىٰ وَذِكْرٌ مِّن قَبْلِي ۗ بَلْ أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ  
 الْحَقَّ ۗ فَهُمْ مُّعْرِضُونَ ﴿٢٤﴾ وَمَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ مِن  
 رَّسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ ﴿٢٥﴾  
 وَقَالُوا اتَّخَذَ الرَّحْمَنُ وَلَدًا ۗ سُبْحٰنَهُ ۗ بَلْ عِبَادٌ مُّكْرَمُونَ  
 ﴿٢٦﴾ لَا يَسْـَٔفُونَہُ بِالْقَوْلِ ۗ وَهُمْ بِأَمْرِهِ يَعْمَلُونَ ﴿٢٧﴾  
 يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَلَا يَشْفَعُونَ إِلَّا لِمَنِ  
 أَرْتَضَىٰ وَهُمْ مِّن خَشْيَتِهِ مُشْفِقُونَ ﴿٢٨﴾ \* وَمَن يَقُلْ  
 مِنْهُمْ إِنَّيَ إِلَهٌ مِّن دُونِهِ ۗ فَذٰلِكَ نَجْزِيہُ جَهَنَّمَ ۗ كَذٰلِكَ  
 نَجْزِي الظَّٰلِمِينَ ﴿٢٩﴾ أَوَلَمْ يَرَ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنَّ السَّمٰوٰتِ  
 وَالْأَرْضَ كَانَتَا رَتْقًا فَفَتَقْنَاهُمَا ۗ وَجَعَلْنَا مِنَ الْمَآءِ كُلَّ  
 شَيْءٍ حَيًّا ۗ أَفَلَا يُؤْمِنُونَ ﴿٣٠﴾ وَجَعَلْنَا فِي الْأَرْضِ رَوَاسِي  
 أَن تَمِيدَ بِهِمْ وَجَعَلْنَا فِيهَا فِجَاجًا سُبُلًا لَّعَلَّهُمْ يَهْتَدُونَ  
 ﴿٣١﴾ وَجَعَلْنَا السَّمَآءَ سَفْعًا مَّحْفُوظًا ۗ وَهُمْ عَن آيٰتِنَا  
 مُّعْرِضُونَ ﴿٣٢﴾ وَهُوَ الَّذِي خَلَقَ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ وَالشَّمْسَ  
 وَالْقَمَرَ ۗ كُلٌّ فِي فَلَكٍ يَسْبَحُونَ ﴿٣٣﴾

أَمِ اتَّخَذُوا إِلَهًا مِّنَ الْأَرْضِ هُمْ  
 يُنشِرُونَ ﴿٢١﴾ لَوْ كَانَ فِيهَا إِلَهَةٌ إِلَّا  
 اللَّهُ لَفَسَدَتَا ۗ فَسُبْحَانَ اللَّهِ رَبِّ  
 الْعَرْشِ عَمَّا يُصِفُونَ ﴿٢٢﴾ لَا يُسْأَلُ  
 عَمَّا يَفْعَلُ وَهُمْ يُسْأَلُونَ ﴿٢٣﴾

**21. Au wamepata miungu katika ardhi inayofufua?**

**22. Lau wangelikuwamo humo miungu wengine isipokuwa Allah basi bila ya shaka hizo mbingu na ardhi zingelifisidika. Subhana Llaah, Ametakasika Allah, Bwana wa Arshi (Kiti cha Enzi), na hayo wanayo-yazua.**

**23. Yeye Hahojiwi kwa Ayatendayo, na wao ndio wanaohojiwa kwa waya-tendayo.**

**Kukanusha miungu ya Uongo**

Allah تعالى Anawasuta wale wenye kuabudu miungu mingine mbali na Yeye, Akasema:

أَمْ اتَّخَذُوا إِلَهًا مِّنَ الْأَرْضِ هُمْ يُنشِرُونَ ﴿٢١﴾

**“Au wamepata miungu katika ardhi inayofufua?”**

Maana yake: Je, wanaweza kuwafufua wafu na kuwatoa ardhini? Hawawezi lolote kati ya hayo, vipi basi wamemfanyia Allah تعالى mshirika na kuwaabudu pamoja Naye?

Kisha Allah تعالى Anatufahamisha kuwa lau kungekuwa na mungu mwingine mbali na Yeye, mbingu na ardhi zingefisidika:

لَوْ كَانَ فِيهِمَا آلِهَةٌ

**“Lau wangelikuwamo humo miungu wengine.”**

Maana yake: Mbinguni na katika ardhi,

لَفَسَدَتَا

**“Zingefisidika (zote mbili)”.**

Hii ni kama Kauli Yake Aliyetukuka:

مَا اتَّخَذَ اللَّهُ مِنْ وَلَدٍ وَمَا كَانَ مَعَهُ مِنْ إِلَهٍ إِذًا لَّذَهَبَ كُلُّ إِلَهٍ بِمَا خَلَقَ وَلَعَلَّا

بَعْضُهُمْ عَلَى بَعْضٍ سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يُصِفُونَ ﴿٢١﴾

**“Allah Hakujiptatia mtoto wala hakuwa pamoja Naye mungu mwingine. Ingekuwa hivyo basi kila mungu angaliwachukua aliowaumba; na baadhi yao wangaliwashinda wengine. Allah Ameepukana na sifa wanazomsifu nazo.” (23:91)**

Na Akasema hapa:

فَسُبْحَانَ اللَّهِ رَبِّ الْعَرْشِ عَمَّا يُصِفُونَ ﴿٢٢﴾

**“Ametakasika Allah, Bwana wa Arshi (Kiti cha Enzi), na hayo wanayoyazua.”**

Maana yake: Kwa wanayosema kuwa Yeye Ana mtoto au mshirika; Ametakasika Naye Yuko mbali sana na uongo wanaomzulia. Na Kauli Yake:

لَا يُسْئَلُ عَمَّا يَفْعَلُ وَهُمْ يُسْئَلُونَ ﴿٣٣﴾

**“Yeye Hahojiwi kwa Ayatendayo, na wao ndio wanahojiwa kwa wayatendayo.”**

Maana yake: Yeye Ndiye Hakimu, Ambaye Hukumu Yake Haipinduliwi wala kupingwa na yeyote, kwa Nguvu Zake, Utukufu Wake, Kiburi Chake, Elimu na Hekima Yake, Uadilifu na Upole Wake.

وَهُمْ يُسْئَلُونَ ﴿٣٣﴾

**“Na wao ndio watakaoulizwa.”** Maana yake: Yeye Ndiye Atakayewauliza viumbe Vyake kwa waliyoyafanya. Hii ni kama Kauli Yake Aliyetukuka:

فَوَرَبِّكَ لَنَسْئَلَنَّهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٣٤﴾ عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٣٣﴾

**“Basi ndivyo Wallaahi Tutakavyowauliza wote. Juu ya yale waliokuwa wakiyatenda.” (15:92-93).**

Na hii ni kama Kauli Yake Aliyetukuka:

وَهُوَ يُجِيرُ وَلَا يُجَارُ عَلَيْهِ

**“Naye Ndiye Alindaye, na hakilindwi kinyume Naye...” (23:88).**

أَمْ اتَّخَذُوا مِنْ دُونِهِ ءَالِهَةً ۗ قُلْ هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ ۗ هَذَا ذِكْرٌ مَنْ مَعِيَ وَذِكْرٌ مَنْ قَبْلِي ۗ بَلْ

أَكْثَرُهُمْ لَا يَعْلَمُونَ الْحَقَّ ۗ فَهُمْ مُعْرِضُونَ ﴿٣٥﴾ وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا

نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ ﴿٣٥﴾

**24. Au wanawaabudu miungu mingine badala Yake? Sema: Leteni ushahidi wenu! Haya ni ukumbusho wa hawa walio Nami, na ukumbusho wa walio kabla Yangu. Lakini wengi wao hawajui kweli, na kwa hivyo wanapuuza.**

**25. Na Hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila Tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipokuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu.**

Anasema Aliyetukuka:

أَمِرًا تَخَذُوا مِنْ دُونِهِ ءِالِهَةً قُلْ

**“Au wanawaabudu miungu mingine badala yake?”**

“Sema” – ee Muhammad.

هَاتُوا بُرْهَانَكُمْ

**“Leteni ushahidi wenu.”**

Maana yake: Dalili yenu kwa munayoyasema.

هَذَا ذِكْرٌ مِنْ مَعِيَ

**“Haya ni ukumbusho wa hawa walio nami.”**

Maana yake: Qur’ani.

وَذِكْرٌ مِنْ قَبْلِي

**“Na ukumbusho wa walio kabla yangu.”**

Maana yake: Vitabu vilivyotangulia kinyume na wanavyosema na kudai. Kila Kitabu kilichoteremshwa kwa kila Mtume aliyetumwa na kulikuwa na *risala* kuwa, “Hapana apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah تعالى tu”, lakini nyinyi washirikina hamjui haki, hivyo mnakengeuka (na kupa nyongo).

Kwa hiyo, Akasema:

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ ﴿٢١﴾

**“Na Hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila Tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipokuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu”.**

Hii ni kama Kauli Yake:

وَسْئَلٌ مِمَّنْ أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رُسُلِنَا أَجَعَلْنَا مِنْ دُونِ الرَّحْمَنِ ءِالِهَةً يُعْبَدُونَ ﴿٤٣﴾

**“Na kawaulize Mitume Wetu Tuliowaleta kabla yako: Je, Tulifanya miungu mingine iabudiwe badala ya Mwingi wa Rehema.” (43: 45).**

Na Amesema:

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الطَّاغُوتَ ط

**“Na bila shaka Tulimpeleka Mtume katika kila Umma ya kwamba: Muabuduni Allah na muepukeni Taghuti (miungu yote ya uongo)...” (16:36).**

Kila Mtume aliyetumwa na Allah تعالى, aliwaita watu wamuabudu Allah تعالى tu, bila ya mshirika. Na pia maumbile (*Fitrah*) ya mwanadamu yanashuhudia hayo. Washirikina hawana dalili kabisa na hoja zao hazitakuwa na faida yoyote mbele ya Mola wao Mlezi; ghadhabu iko juu yao na watakuwa na adhabu iumizayo.

وَقَالُوا اتَّخَذَ الرَّحْمَنُ وَلَدًا ۗ سُبْحٰنَهُ ۗ بَلْ عِبَادٌ مُّكْرَمُونَ ﴿٢٦﴾ لَا يَسْبِقُونَهُ بِالْقَوْلِ  
وَهُمْ بِأَمْرِهِ يَعْمَلُونَ ﴿٢٧﴾ يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ وَلَا يَشْفَعُونَ إِلَّا لِمَنِ  
أَرْتَضَىٰ وَهُمْ مِنَ خَشْيَتِهِ مُشْفِقُونَ ﴿٢٨﴾ \* وَمَنْ يُقْلَ مِنْهُمْ إِنَّ إِلَهَ مِنْ دُونِهِ فَذٰلِكَ  
نَجْزِيهِ جَهَنَّمَ ۗ كَذٰلِكَ نَجْزِي الظَّٰلِمِينَ ﴿٢٩﴾

**26. Na wanasema: Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema, Ana mwana! Subhanahu, Ametakasika na hayo! Bali hao (wanaowaita wana) ni watumwa waliotukuzwa.**

**27. Hawamtangulii kwa neno, nao wanafanya Amri Zake.**

**28. Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao. Wala hawamuombi yeyote ila yule anayemridhia Yeye, nao kwa ajili ya kumuogopa wananyenyekoa.**

**29. Na yeyote kati yao atakayesema: Mimi ni mungu, badala Yake, basi huyo Tutamlipa malipo yake Jahanamu. Hivyo ndivyo Tuwalipavyo wenye kudhulumu.**

## Kuwarudi Wenye Kudai kuwa Malaika ni Mabinti wa Allah تعالی na Ubainifu wa Amali na Daraja Zao

Anasema Aliyetukuka Kuwarudi wenye kudai kuwa Yeye Aliyetukuka Ana mtoto miongoni mwa Malaika. Waarabu walikuwa wakisema hayo kuwa Malaika ni mabinti wa Allah تعالی. Akasema Aliyetukuka:

سُبْحٰنَهُۥٓ ۙ بَلَّ عِبَادٌ مُّكْرَمُوۡنَ ﴿٢١﴾

***“Ametakasika na hayo! Bali hao ni watumwa waliotukuzwa.”***

Maana yake: Malaika ni waja wa Allah تعالی waliotukuzwa Naye na watakuwa na vyeo na hadhi kubwa. Na wao wanamtii (Allah تعالی) upeo wa kumtii, kwa maneno na vitendo.

لَا يَسْقُوۡنَهُۥٓ بِالْقَوْلِ وَّهُم بِأَمْرِهٖ يَعْمَلُوۡنَ ﴿٢٢﴾

***“Hawamtangulii kwa neno, nao wanafanya Amri Zake.”***

Maana yake: Hawatangulizi jambo lolote mbele Yake wala hawaendi kinyume na waliyoamriwa Naye, bali wanafanya haraka kutekeleza. Naye Aliyetukuka Anawazunguka kwa Elimu Yake, na hakuna chohote kilichofichwa Kwake.

يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ

***“Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao”. (2:255)***

Na Kauli Yake:

وَلَا يَشْفَعُوۡنَ إِلَّا لِمَنْ أَرَادَۙ

***“Wala hawamwombi yeyote ila yule anayemridhia Yeye”.***

Hii ni kama Kauli Yake:

مَنْ ذَا الَّذِي يَشْفَعُ عِنْدَهُٓ إِلَّا بِإِذْنِهٖۙ

***“Na nani huyo awezaye kuombea mbele Yake bila ya Idhini Yake?...” (2:255).***

وَلَا تَنْفَعُ الشَّفَاعَةُ عِنْدَهُٓ إِلَّا لِمَنْ أُذِنَ لَهُۥٓ

***“Wala hautafaa uombezi mbele Yake ila kwa yule Aliyempa Idhini...” (34:23).***

Na zipo Aya nyingi zenye maana hiyo.

وَهُمْ مِّنْ حَشِيَّتِهِ

**“Nao kwa ajili ya kumwogopa”,** Maana: kwa kumuogopa na kuwa na hofu.

مُشْفِقُونَ ﴿٢١﴾ \* وَمَنْ يُقَلِّمْ مِنْهُمْ لِيْلَٰهٍ مِّنْ دُونِهِ

**“Wananyenyekea. Na yeyote kati yao atakayesema: Mimi ni mungu, badala Yake.”**

Maana yake: Mwenye kudai kuwa yeye ni mungu badala ya Allah تعالى au pamoja na Allah تعالى.

فَذَٰلِكَ نَجْزِيهِ جَهَنَّمَ ۚ كَذَٰلِكَ نَجْزِي الظَّٰلِمِينَ ﴿٢٢﴾

**“Basi huyo Tutamlipa malipo yake Jahanamu. Hivyo ndivyo Tuwalipavyo wenye kudhulumu.”**

Maana yake: Kila anayesema hayo. Na hili ni sharti, na sharti si lazima litokee. Hii ni kama Kauli Yake:

قُلْ إِنْ كَانَ لِلرَّحْمٰنِ وَلَدٌ فَأَنَا أَوَّلُ الْعٰبِدِينَ ﴿٢٣﴾

**“Sema: (Allah) Mwingi wa Rehema angalikuwa na mtoto ningekuwa wa kwanza wa kumuabudu.” (43:81).**

Na Kauli Yake:

إِنْ أَشْرَكَتَ لَيَحْبَطَنَّ عَمَلُكَ وَلَتَكُونَنَّ مِنَ الْخٰسِرِينَ ﴿٢٤﴾

**“Kama ukimshirikisha (Allah) bila shaka amali zako zitaruka patupu; na lazima utakuwa miongoni mwa wenye kula hasara.” (39:65).**

أَوَلَمْ يَرِ الَّذِينَ كَفَرُوا أَنَّ السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضَ كَانَتَا رَتْقًا فَفَتَقْنَاهُمَا ۗ وَجَعَلْنَا مِنَ الْمَآءِ

كُلَّ شَيْءٍ حَيٍّ ۖ أَفَلَا يُؤْمِنُونَ ﴿٢٥﴾ وَجَعَلْنَا فِي الْأَرْضِ رَوٰسِي ۙ أَنْ تَمِيدَ بِهِمْ وَجَعَلْنَا فِيهَا

فِجَاجًا سُبُلًا لَّعَلَّهُمْ يَهْتَدُونَ ﴿٢٦﴾ وَجَعَلْنَا السَّمٰءَ سَفَافًا مَّحْفُوظًا ۗ وَهُمْ عَنْ ءَايٰتِنَا

مُعْرِضُونَ ﴿٢٧﴾ وَهُوَ الَّذِي خَلَقَ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ ۗ كُلٌّ فِي فَلَكٍ يَسْبَحُونَ

**30. Je! Hao waliokufuru hawakuona kwamba mbingu na ardhi zilikuwa zimeambatana, kisha Sisi Tukazibandua? Na Tukajaalia kwa maji kila kilicho hai? Basi je, hawaamini?**

**31. Na Tukaweka katika ardhi milima iliyothibiti ili isiwayumbishe, na Tukaweka humo njia pana ili wapate kuongoka.**

**32. Na Tukaifanya mbingu kuwa dari iliyohifadhiwa, lakini wanazipuuza Ishara Zake.**

**33. Na Yeye Ndiye Aliyeumba usiku na mchana na jua na mwezi, vyote katika anga vinaogelea.**

**Ishara za Allah تعالی mbinguni na katika Ardhi na Usiku na mchana**

Hapa Anasema Aliyetukuka Kutuelezea kuhusu Uwezo Wake uliotimia na Umiliki Wake katika Kuumba vitu na Kutenza Nguvu viumbe Vyake vyote. Akasema:

أُولَٰمِرِ الَّذِينَ كَفَرُوا

**“Je, hao waliokufuru hawakuona kwamba.”** Maana yake: Wale wenye kukanusha Uungu Wake, hivyo kuabudu wengine wasiokuwa Yeye. Je, hawatambui kuwa Allah تعالی ni Yule Mwenye Uhuru katika Nguvu Zake za Uumbaji na Anapelekesha mambo yote kwa Nguvu Zake? Itakuwaje basi kuabudu asiyekuwa Yeye au kumshirikisha katika Ibada? Je, hawaoni?

أَنَّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ كَانَتَا رَتْقًا فَفَتَقْنَاهُمَا

**“Hawakuona kwamba mbingu na ardhi zilikuwa zimeambatana, kisha Sisi Tukazibandua?”**

Kuwa mbingu na ardhi zilikuwa zimeambatana. Maana: kilikuwa ni kipande kimoja hapo mwanzoni, zikiwa zimeshikana kimoja juu ya kingine, kisha Akazibandua moja kutoka kwa nyengine. Kutokana nayo, Akafanya mbingu saba na ardhi saba, na Akaweka hewa baina ya ardhi na wingu wa chini (ulio karibu na ardhi, wingu wa ardhi). Kisha, Akaifanya mvua kunyesha kutoka mawinguni na mimea kumea kutoka katika ardhi. Akasema:

وَجَعَلْنَا مِنَ الْمَاءِ كُلَّ شَيْءٍ حَيٍّ أَفَلَا يُؤْمِنُونَ

**“Na Tukajaalia kwa maji kila kilicho hai? Basi je, hawaamini?”**

Maana yake: Wanaona kwa macho yao jinsi viumbe vinavyokua hatua kwa hatua. Yote hayo ni dalili ya kuwepo kwa Muumba, Mwenye Kudhibiti kila kitu na Ana Uwezo wa Kufanya Atakalo.



### Katika Kila Kitu Kuna Alama za Allah تعالی Kwamba Yeye ni Mmoja

Amepokea Sufyaan Thawriy رحمه الله تعالی kutoka kwa baba yake, aliyepokea kutoka kwa Ikrimah kuwa, “Aliulizwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما: ‘Je, usiku ulikuja kabla ya mchana au vipi?’ Akasema: “Mnaonaje pale mbingu na ardhi zilipokuwa zimeambatana, je, kulikuwa na chochote baina yao, isipokuwa kiza? Hilo ili mupate kujua kuwa usiku ulikuwepo kabla mchana.”<sup>1</sup>

Na amepokea Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالی kutoka kwa Ibn ‘Umar رضي الله عنهما amesema alikuja mtu kwake akimuuliza kuhusu mbingu na ardhi,

كَأَتَا رَتْقًا فَفَتَقْنَهُمَا

**“Zilikuwa zimeambatana kisha Sisi Tukazibandua?”** Akasema: “Nenda kamuulize yule shaikh (mzee), kisha rudi unieleze aliyokuambia”. Akasema: Akaenda kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما na kumuuliza (kuhusu hilo). Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما akasema: “Ndio, mbingu zilikuwa zimeambatana, wala hainyeshi mvua, na ardhi zilikuwa zimeambatana, hakuna kilichokuwa kikimea. Pindi viumbe vilipoumbwa ili kuijaza dunia, mvua ilianza kunyesha kutoka mbinguni na mimea kuanza kumea”. Mtu yule alirudi na kumueleza Ibn ‘Umar رضي الله عنهما jawabu hilo. Ibn ‘Umar رضي الله عنهما alisema: “Sasa nimejua kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amepatiwa elimu ya Qur’ani. Amesema kweli, na hivi ndivyo ilivyokuwa”. Akasema Ibn ‘Umar رضي الله عنهما: “Hakika nilikuwa sipendezwi na ujasiri wa Ibn ‘Abbaas katika kuifasiri Qur’ani, lakini sasa nimejua kuwa amepatiwa yeye (Ibn ‘Abbaas) elimu ya Qur’ani”<sup>2</sup>. Na Hasan na Qatadah wamesema: “Zilikuwa zote zimeshikana pamoja, kisha zikabanduliwa na hii hewa”. Na Kauli Yake:

وَجَعَلْنَا مِنَ الْمَاءِ كُلَّ شَيْءٍ حَيٍّ

**“Na Tukajaalia kwa maji kila kilicho hai?”** Maana yake: Asili na chanzo kwa kila uhai ni maji.

Amepokea Imaam Ahmad kuwa Abi Hurayrah عنه رضي الله عنهما amesema: “Nilisema: Ewe Mtume wa Allah! Pindi ninapokuona ninakuwa na furaha na jicho langu kutulia na kuridhia, hivyo nieleze mimi kuhusu kila kitu”. Akasema:

«كُلُّ شَيْءٍ خُلِقَ مِنْ مَاءٍ»

“Kila kitu kimeumbwa kutokana na maji”.

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:433.

<sup>2</sup> Ibn Abi Haatim 8:2450.

“Nikasema: Nijulishe jambo lau nitalifanya nitaingia Peponi”. Akasema:

«أَفْشِ السَّلَامَ، وَأَطْعِمِ الطَّعَامَ، وَصِلِ الْأَرْحَامَ، وَقُمْ بِاللَّيْلِ وَالنَّاسُ نِيَامٌ، ثُمَّ  
ادْخُلِ الْجَنَّةَ بِسَلَامٍ»

“Toleaneni salamu, walisheni wengine chakula, ungeni udugu na simama (kuswali) usiku, ilhali watu wamelala. Hapo utaingia Peponi kwa amani”<sup>1</sup>. Na Kauli Yake:

وَجَعَلْنَا فِي الْأَرْضِ رَوَاسِيَ

“**Na Tukaweka katika ardhi milima.**” Maana: Majabali yameikalia juu ardhi na Kuidhibiti pamoja na Kuipa wizani (mzito) ili isitetemeke na watu. Hiyo ina maana kutetemeka na kutaharaki hivyo kutoweza kusimama imara juu yake – kwa kuwa imefunikwa na maji, ila kipimo cha robo yake. Hivyo, ardhi imefunuka na kujichomoza hewani na kwenye jua, ili watu wake wapate kuona mbingu na ishara zake kabambe, hekima na dalili za wazi. Kwa hiyo Akasema:

أَنْ تَمِيدَ بِهِمْ

“**Iliyothibiti ili iswayumbishe.**” Maana yake: Ili isiyumbe pamoja nao.

وَجَعَلْنَا فِيهَا فِجَاجًا سُبُلًا

“**Na Tukaweka humo njia pana.**” Maana yake: Njia zilizo milimani kupitia kwayo wanaweza kusafiri kutoka eneo moja hadi eneo jengine, nchi hadi nchi. Kama inavyoshuhudiwa katika ardhi, kunakuwa na milima mikubwa baina ya ardhi hii na nyingine, hivyo Allah تعالى Akaweka ndani yake upenyo, njia, ili watu wapate kusafiri kutoka hapa hadi pale. Kwa hiyo Akasema:

لَعَلَّهُمْ يَهْتَدُونَ ﴿٢١﴾

“**Ili wapate kuongoka.**”

وَجَعَلْنَا السَّمَاءَ سَقْفًا مَحْفُوظًا

“**Na Tukaifanya mbingu kuwa dari iliyohifadhiwa.**”

Maana yake: Inayofunika ardhi kama kuba juu yake. Hii ni kama usemi Wake:

<sup>1</sup> Ahmad 2:295, 323, 324.

وَالسَّمَاءَ بَنَيْنَاهَا بِأَيْمٍ وَإِنَّا لَمُوسِعُونَ ﴿٤٧﴾

**“Na mbingu Tumezifanya kwa Kudura Yetu; na hakika Sisi ndio wenye Uweza wa Kuipanua.” (51:47).** Aidha Amesema,

وَالسَّمَاءِ وَمَا بَنَاهَا ﴿٩١﴾

**“Na kwa mbingu na kwa Aliyezijenga.” (91:5).**

أَفَلَمْ يَنْظُرُوا إِلَى السَّمَاءِ فَوْقَهُمْ كَيْفَ بَنَيْنَاهَا وَزَيَّنَّاهَا وَمَا لَهَا مِنْ فُرُوجٍ ﴿٥٠﴾

**“Je, hawazioni mbingu zilizo juu yao! Tumezijengaje na Tumezipambaje. Wala hazina nyufa.” (50:6).**

Jengo na kutengeneza kulikoelezwa hapa ni kule kunyanyua kuba, kama alivyosema Mtume ﷺ:

«بُنِيَ الْإِسْلَامُ عَلَى خَمْسٍ»

**“Uislamu umejengwa juu ya mambo matano.”<sup>1</sup>**

Maana yake: Nguzo tano. Na hili haliwezi kuwa isipokuwa katika hema, kama ilivyojulikana na Waarabu.

مَحْفُوظًا

**“Iliyohifadhiwa”,** Maana yake: Iko juu sana na kulindwa isiwe ni yenye kufikiwa na chochote. Mujaahid amesema: **“Iliyonyanyuliwa”<sup>2</sup>.** Na Kauli Yake:

وَهُمْ عَنْ آيَاتِنَا مُعْرِضُونَ ﴿١٠٥﴾

**“Lakini wanazipuza Ishara Zake”.** Hii ni kama Kauli Yake:

وَكَايِنٍ مِّنْ آيَاتِنَا فِي السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ يَمُرُونَ عَلَيْهَا وَهُمْ عَنْهَا مُعْرِضُونَ ﴿١٠٥﴾

**“Na ishara ngapi katika mbingu na ardhi wanazozipitia, na hali ya kuwa wanazipuza.” (12:105)**

Maana yake: hawafikirii jinsi Alivyoiumba Allah تعالى ndani yake, pana sana na Kunyanyuliwa juu kabisa pamoja na Kupambwa na sayari zilizotulia na zile zenye kutembea usiku na mchana. Mfano wa hizo ni jua ambalo linazunguka

<sup>1</sup> Fat’h Al-Baariy 1:64.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:436.

kwa ukamilifu wake mara moja kwa mchana na usiku mmoja (masaa 24), mpaka linapomaliza muda wake, ambao hakuna aujuae ila Allah تعالى, ambaye Amelikadiria, Aliyeliumba, Aliyeliitiisha na Kulielekeza. Kisha Akasema huku Anatutanabahisha kwa baadhi ya ishara:

وَهُوَ الَّذِي خَلَقَ اللَّيْلَ وَالنَّهَارَ

**“Na Yeye Ndiye Aliyeumba usiku na mchana.”**

Maana yake: Usiku una giza lake na utulivu wake na mchana una mwangaza wake na maingiliano ya wanadamu; wakati mwengine mmoja wapo ni mrefu kuliko nyengine kisha unakuwa mfupi mwengine na kinyume chake.

وَالشَّمْسِ وَالْقَمَرِ

**“Na jua na mwezi.” (7:54)**

Jua likiwa na mwangaza wake lenyewe, mapitio yake, muda uliowekewa, mwendo (harakati) na msogeo wake maalumu. Na mwezi ukimulikwa mwangaza, ukiwa na mapitio tofauti, msogeo mwingine na muda wake.

كُلٌّ فِي فَلَكٍ يَسْبَحُونَ

**“Vyote katika anga vinaogelea.”**

Maana yake: Zinazunguka. Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Zinazunguka kama gurudumu la kusokota nyuzi, katika duara.”<sup>1</sup> Hii ni kama Kauli Yake Aliyetukuka:

فَالِقُ الْإِصْبَاحِ وَجَعَلَ اللَّيْلَ سَكَنًا وَالشَّمْسَ وَالْقَمَرَ حُسْبَانًا ۚ ذَلِكَ تَقْدِيرُ الْعَزِيزِ

الْعَلِيمِ

**“Ndiye Anayepambazua muangaza asubuhi; na Ameufanya usiku kuwa mapumziko na jua na mwezi kwenda kwa hesabu. Hicho ndicho kipimo cha Mwenye Nguvu na Ajuaye.” (6:96).**

\* \* \*

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 20:520-521.

وَمَا جَعَلْنَا لِبَشَرٍ مِّن قَبْلِكَ الْخُلْدَ ۗ أَفَلَا يَن مِّتَ فَهَمُ ۗ  
 الْخَالِدُونَ ﴿٣٤﴾ كُلُّ نَفْسٍ ذَائِقَةُ الْمَوْتِ ۗ وَنَبَلَّوْكُمْ بِالشَّرِّ  
 وَالْخَيْرِ فِتْنَةً ۗ وَإِلَيْنَا تُرْجَعُونَ ﴿٣٥﴾ وَإِذَا رَأَى الَّذِينَ  
 كَفَرُوا إِن يَتَّخِذُونَكَ إِلَّا هُزُوًا أَهَذَا الَّذِي يَذْكُرُ  
 آلِهَتَكُمْ وَهُمْ يَذْكُرِ الرَّحْمَنَ هُمْ كَافِرُونَ ﴿٣٦﴾  
 خَلِقَ الْإِنْسَانَ مِن عَجَلٍ ۗ سَأُورِيكُمْ آيَاتِي فَلَا  
 تَسْتَعْجِلُونَ ﴿٣٧﴾ وَيَقُولُونَ مَتَى هَذَا الْوَعْدُ إِن  
 كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٣٨﴾ لَوْ يَعْلَمُ الَّذِينَ كَفَرُوا حِينَ لَا  
 يَكْفُرُونَ عَن وُجُوهِهِمُ النَّارَ وَلَا عَن ظُهُورِهِمْ وَلَا هُمْ  
 يُنصَرُونَ ﴿٣٩﴾ بَلْ تَأْتِيهِم بَغْتَةً فَتَبْهَتُهُمْ فَلَا  
 يَسْتَطِيعُونَ رَدَّهَا وَلَا هُمْ يُنظَرُونَ ﴿٤٠﴾ وَلَقَدْ أَسْرَفْنَا  
 بِرُسُلٍ مِّن قَبْلِكَ فَحَاقَ بِالَّذِينَ سَخِرُوا مِنْهُمْ مَا كَانُوا  
 بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ ﴿٤١﴾ قُلْ مَن يَكْلُؤْكُمْ بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ  
 مِنَ الرَّحْمَنِ ۗ بَلْ هُمْ عَن ذِكْرِ رَبِّهِمْ مُعْرِضُونَ ﴿٤٢﴾  
 أَمْرَهُمُ إِلَهَةٌ تَمْنَعُهُمْ مِّن دُونِنَا ۗ لَا يَسْتَطِيعُونَ نَصْرَ  
 أَنفُسِهِمْ وَلَا هُمْ مِنَّا يُصْحَبُونَ ﴿٤٣﴾

وَمَا جَعَلْنَا لِبَشَرٍ مِّن قَبْلِكَ الْخُلْدَ ۗ  
 أَفَلَا يَن مِّتَ فَهَمُ الْخَالِدُونَ ﴿٣٤﴾ كُلُّ  
 نَفْسٍ ذَائِقَةُ الْمَوْتِ ۗ وَنَبَلَّوْكُمْ بِالشَّرِّ  
 وَالْخَيْرِ فِتْنَةً ۗ وَإِلَيْنَا تُرْجَعُونَ ﴿٣٥﴾

**34. Nasi Hatukumjaalia mwanadamu yeyote kabla yako kuwa na maisha ya milele. Basi je! Ukifa wewe, wao wataishi milele?**

**35. Kila nafsi itaonja mauti; na Tunakujaribuni kwa mtihani wa shari na kheri. Na Kwetu Sisi mtarejeshwa.**

**Hakuna Atakayepewa Uhai wa Kuishi Milele Hapa Duniani**

Anasema Aliyetukuka:

وَمَا جَعَلْنَا لِبَشَرٍ مِّن قَبْلِكَ

**“Nasi Hatukumjaalia mwanadamu yeyote kabla yako”**

Maana: Ewe Muhammad ﷺ

الْخُلْدَ ۗ

**“Kuwa na maisha ya milele.”**

Maana yake: Katika hii dunia, bali,

كُلُّ مَنْ عَلَيْهَا فَانٍ ﴿٢٦﴾ وَيَبْقَىٰ وَجْهَ رَبِّكَ ذُو الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ ﴿٢٧﴾

**“Kila kilicho juu yake (ardhi na mbingu) kitatoweka. Itabaki dhati ya Mola wako Mlezi Mwenye Utukufu na Heshima.” (55:26-27).**

Na Kauli Yake:

أَفَلَيْنَ مِتَّ

**“Basi je! Ukifa wewe.”**

Maana yake: Ewe Muhammad ﷺ,

فَهُمُ الْخَالِدُونَ ﴿٢٨﴾

**“Wao wataishi milele?”**

Maana yake: Wanataraji kuwa wao watabaki milele katika maisha baada yako, lakini hilo halitatokea; kila kitu kitaondoka. Hivyo, Akasema Aliyetukuka:

كُلُّ نَفْسٍ ذَائِقَةُ الْمَوْتِ ﴿٢٩﴾

**“Kila nafsi itaonja mauti.”**

Na imepokewa kutoka kwa Imamu Shafi رحمه الله تعالى kwamba yeye alisoma kasida yake kwa kusema, “watu wanatamani nife, na hata nikifa, hiyo sio safari ya peke yangu.”

وَتَبْلُوكُمْ بِالشَّرِّ وَالْخَيْرِ فِتْنَةً ﴿٣٠﴾

**“Na Tunakujaribuni kwa mtihani wa shari na kheri.”**

Maana yake: Tutawaonjeni kwa baadhi ya shida na neema wakati mwingine, kutizama atakayeshukuru na atakayekufuru, pia atakayesubiri. Hii ni kama alivyopokea ‘Aliy bin Abi Twalhah kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuwa amesema:

وَتَبْلُوكُمْ

**“Na Tunakujaribuni.”** Maana yake: Tutawaonjeni.

بِالشَّرِّ وَالْخَيْرِ فِتْنَةً ﴿٣١﴾

**“Kwa mtihani wa shari na kheri.”**

Kwa shida na raha, siha na ugonjwa, utajiri na umasikini, halali na haramu, utiifu na maasi na uwongofu na upotevu. Na Kauli Yake:

وَإِلَيْنَا تُرْجَعُونَ ﴿٣٤﴾

**“Na Kwetu Sisi mtarejeshwa.”** Maana yake: Kuwalipa jaza kwa amali zenu (mulizofanya).<sup>1</sup>

وَإِذَا رَأَى الَّذِينَ كَفَرُوا إِنْ يَتَّخِذُونَكَ إِلَّا هُزُوءًا أَهْذَى الَّذِي يَذْكُرُ ءِالِهَتِكُمْ  
وَهُمْ بِذِكْرِ الرَّحْمَنِ هُمْ كَافِرُونَ ﴿٣٥﴾ خُلِقَ الْإِنْسَانُ مِنْ عَجَلٍ ؕ سَأُورِيكُمْ ءَايَاتِي  
فَلَا تَسْتَعْجِلُونِ ﴿٣٦﴾

**36. Na wakikuona waliokufuru hawakufanyi wewe ila ni kitu cha maskhara tu, (wakisema): Je! Ndiye huyu anayeitaja miungu yenu? Na hali wao wanakataa kumkumbuka ar- Rahman, Mwingi wa Rehema!**

**37. Mwanadamu ameumbwa na haraka. Nitakuonesheni Ishara Zangu. Basi musinihimize.**

**Washirikina Kumfanyia Istihzai Mtume** ﴿٣٧﴾

Allah تعالیٰ Anamuambia Mtume Wake ﴿٣٧﴾:

وَإِذَا رَأَى الَّذِينَ كَفَرُوا

**“Na wakikuona waliokufuru.”** Maana yake: Makafiri wa Quraysh kama Abu Jahl na mfano wake.

إِنْ يَتَّخِذُونَكَ إِلَّا هُزُوءًا

**“Hawakufanyi wewe ila ni kitu cha maskhara tu.”** Maana yake: Wanakufanyia istihzai (masikhara) na kukutusi, wakisema:

أَهْذَى الَّذِي يَذْكُرُ ءِالِهَتِكُمْ

**“Je! Ndiye huyu anayeitaja miungu yenu?”** Wanamaanisha, je ni huyu anawatukana miungu yenu na kuwachezea akili zenu? Amesema Aliyetukuka:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:440.

وَهُمْ بِذِكْرِ الرَّحْمَنِ هُمْ كَنُفُورًا ﴿٣٤﴾

**“Na hali wao wanakataa kumkumbuka ar-Rahman, Mwingi wa Rehema.”**

Maana yake: Wenye kumkanusha Allah تعالى pamoja na hilo wanamfanyia maskhara Mtume ﷺ, kama Alivyosema katika Aya nyingine:

وَإِذَا رَأَوْكَ إِن يَتَّخِذُونَكَ إِلَّا هُزُؤًا أَهْذًا الَّذِي بَعَثَ اللَّهُ رَسُولًا ﴿٣٥﴾ إِن كَادَ لَيُضِلَّنَا  
عَنِ الْهَيْتِنَا لَوْلَا أَن صَبَرْنَا عَلَيْهَا ۚ وَسَوْفَ يَعْلَمُونَ حِينَ يَرَوْنَ الْعَذَابَ مَن أَضَلُّ  
سَبِيلًا ﴿٣٦﴾

**“Na wanapokuona hawakufanyi ila ni kufanyiwa mzaha tu (wanasema): Je, huyo ndiye Allah Aliyemtuma kuwa Mtume! Kwa hakika alikuwa karibu kutupoteza na miungu yetu. Kama Tusingalikazana juu yao. Karibu watajua, watakapoiona adhabu, ni nani aliyepotea njia.” (25:41-42).**

Na Kauli Yake:

خُلِقَ الْإِنْسَانُ مِنْ عَجَلٍ ۗ

**“Mwanadamu ameumbwa na haraka.”**

Hii ni kama ile Aya:

وَكَانَ الْإِنْسَانُ عَجُولًا ﴿١٧﴾

**“Na mwanadamu amekuwa ni mwenye pupa.” (17:11),**

Maana yake: Katika mambo yote. Sababu ya kutajwa kwa haraka ya mwanadamu hapa ni kule kutajwa masikhara yaliyofanywa dhidi ya Mtume ﷺ, (waumini) watataka kulipa kisasi cha haraka, na hilo litatokea karibuni. Akasema Allah تعالى:

خُلِقَ الْإِنْسَانُ مِنْ عَجَلٍ ۗ

**“Mwanadamu ameumbwa na haraka.”**

Kwa sababu Anamcheleweshea (adhabu) mpaka wakati Anapomshika Hatomuacha kabisa. Anaichelewesha, kisha Anaiharakisha; Anangojea, kisha Hacheleweshi kabisa. Kwa hiyo Akasema:



سَأُورِيكُمْ آيَاتِي

**“Nitakuonesheni Ishara Zangu.”**

Maana yake: Adhabu na Hukumu Yangu na Nguvu Zangu juu ya walioniasi.

فَلَا تَسْتَعْجِلُونِ

**“Basi musinihimize”.**

وَيَقُولُونَ مَتَى هَذَا الْوَعْدُ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٣٨﴾ لَوْ يَعْلَمُ الَّذِينَ كَفَرُوا حِينَ  
لَا يَكْفُونَ عَنْ وُجُوهِهِمُ النَّارَ وَلَا عَنْ ظُهُورِهِمْ وَلَا هُمْ يُنصَرُونَ ﴿٣٩﴾ بَلْ  
تَأْتِيهِمْ بَغْتَةً فَتَبْهَتُهُمْ فَلَا يَسْتَطِيعُونَ رَدَّهَا وَلَا هُمْ يُنظَرُونَ ﴿٤٠﴾

**38. Na wanasema: Ahadi hii itatokea lini, ikiwa nyinyi munasema kweli?**

**39. Lau wangelijua wale waliokufuru wakati ambao hawatauzuia Moto kwenye nyuso zao wala migongo yao, na wala hawatanusuriwa!**

**40. Bali utawafikia kwa ghafla, na utawashitua na wala hawataweza kuurudisha, wala hawatapewa muhula!**

### Washirikina Kutaka Waharakishiwe Adhabu

Allah تعالی Anatupasha habari kuwa washirikina wanataka waharakishiwe kufika adhabu yao juu ilihali wanaikanusha, wanaikataa, wanaikufuru, kwa inadi na ukaidi pamoja na kuitakidi kuwa hilo halitatokea kabisa.

Akasema:

وَيَقُولُونَ مَتَى هَذَا الْوَعْدُ إِن كُنْتُمْ صَادِقِينَ ﴿٣٨﴾

**“Na wanasema: Ahadi hii itafika lini ikiwa nyinyi mnasema kweli?”**

Amesema Allah تعالی:

لَوْ يَعْلَمُ الَّذِينَ كَفَرُوا حِينَ لَا يَكْفُوفُونَ عَنْ وُجُوهِهِمُ النَّارَ وَلَا عَنْ ظُهُورِهِمْ

**“Lau wangelijua wale waliokufuru wakati ambao hawatauzuia Moto kwenye nyuso zao wala migongo yao.”**

Maana yake: Lau wangelijua kwa yakini kuwa bila shaka tukio hilo litafika, wasingelitaka adhabu iletwe kwa haraka. Laiti wangejua jinsi adhabu hiyo itakavyowafunika juu yao na chini ya nyayo zao.

هُمْ مِّنْ فَوْقِهِمْ ظُلَلٌ مِّنَ النَّارِ وَمِنْ تَحْتِهِمْ ظُلَلٌ

**“Yatawekwa juu yao mawingu ya Moto na chini yao mawingu (ya Moto vile vile).” (39:16).** Na pia,

هُمْ مِّنْ جَهَنَّمَ مِهَادٌ وَمِنْ فَوْقِهِمْ غَوَاشٍ

**“Watakuwa na magodoro ya moto wa Jahanamu; na juu yao nguo za moto za kujifunika.” (7:41).**

Na Akasema katika Aya hii:

حِينَ لَا يَكْفُوفُونَ عَنْ وُجُوهِهِمُ النَّارَ وَلَا عَنْ ظُهُورِهِمْ

**“Wakati ambao hawatauzuia Moto kwenye nyuso zao wala migongo yao.”**

Na Akasema:

سَرَابِيلُهُمْ مِّنْ قَطِرَانٍ وَتَغْشَىٰ وُجُوَّهُمُ النَّارُ ﴿٥٠﴾

**“Nguo zao zitakuwa za lami, na Moto utazijia nyuso zao (uzibabue).” (14:50)**

Adhabu hiyo itawazunguka pande zote,

وَلَا هُمْ يُنصَرُونَ ﴿٥١﴾

**“Na wala hawatanusuriwa!”** Maana yake: Hakuna wa kuwasaidia wala kuwanusuru. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَمَا هُمْ مِّنَ اللَّهِ مِن وَّاقٍ ﴿٣٤﴾

**“Wala hawatakuwa na mlinzi kwa Allah.” (13:34).**

Na Kauli Yake:

بَلْ تَأْتِيهِمْ بَغْتَةً

**“Bali utawafikia kwa ghafla.”** Maana yake: Moto utawajia na kuwafikia kwa ghafla, utawachukua wao kwa kuwashitusha, bila ishara yoyote ile.

فَتَبْتَهُمْ

**“Na utawashitua.”** Maana yake: Utawaogofya, na hawatakuwa na budi ila kusalimu amri bila kujua wafanye nini.

فَلَا يَسْتَطِيعُونَ رَدَّهَا

**“Na wala hawataweza kuurudisha.”**

Maana: Hawatakuwa na hila wala njia katika hilo.

وَلَا هُمْ يُنظَرُونَ ﴿٤١﴾

**“Wala hawatapewa muhula!”**

Maana yake: Wala haitacheleweshwa kwao hiyo adhabu hata kwa saa moja (muda mchache).

وَلَقَدْ آسَفْنَاهُ بِرُسُلِهِمْ مِنْ قَبْلِكَ فَحَاقَ بِالَّذِينَ سَخِرُوا مِنْهُمْ مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِئُونَ

﴿٤١﴾ قُلْ مَنْ يَكْفُرْكُمْ بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ مِنَ الرَّحْمَنِ ۗ بَلْ هُمْ عَنْ ذِكْرِ رَبِّهِمْ

مُعْرِضُونَ ﴿٤٢﴾ أَمْ لَهُمْ آلِهَةٌ تَمْنَعُهُمْ مِنْ دُونِنَا لَا يَسْتَطِيعُونَ نَصْرَ أَنْفُسِهِمْ وَلَا

هُم مِّنَّا يُصْحَبُونَ ﴿٤٣﴾

**41. Na Mitume walio kabla yako walikwishadhihakiwa. Kwa hivyo wale waliowafanyia masikhara yaliwafika yale waliyokuwa wakiyafanyia dhihaka.**

**42. Sema: Nani anayekulideni usiku na mchana na Ar-Rahmani, Mwingi wa Rehema? Bali wao wanapuuza kumkumbuka Mola wao Mlezi.**

**43. Au wao wanao miungu wataoweza kuwakinga nasi? Hao hawawezi kujinusuru nafsi zao, wala hawatalindwa Nasi!**

### Mafunzo Tunayopata kwa Wale Waliowafanyia Mzaha Mitume Iliyopita

Anasema Aliyetukuka kwa Kumliwaza Mtume Wake kutokana na maudhi anayofanyiwa na washirikina miongoni mwa istihzai na kukadhibishwa washirikina,

وَلَقَدْ آسَفْتُمُوعِي بِرُسُلِي مِّن قَبْلِكَ فَحَاقَ بِالَّذِينَ سَخِرُوا مِنْهُمْ مَا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِءُونَ

***“Na Mitume walio kabla yako walikwisha dhihakiwa. Kwa hivyo wale walio wafanyia maskhara yaliwafika yale waliyokuwa wakiyafanyia dhihaka.”***

Maana yake: Adhabu waliodhania kuwa haitafika. Hii ni kama Aya ifuatayo:

وَلَقَدْ كُذِّبَتْ رُسُلٌ مِّن قَبْلِكَ فَصَبَرُوا عَلَىٰ مَا كُذِّبُوا وَأَوْدُوا حَتَّىٰ أَتَاهُمْ نَصْرُنَا وَلَا

مُبَدِّلَ لِكَلِمَاتِ اللَّهِ ۗ وَلَقَدْ جَاءَكَ مِن نَّبِإِ الْمُرْسَلِينَ ﴿٤٤﴾

***“Na hakika walikadhibishwa Mitume wote kabla yako, wakavumilia kwa kule kukadhibishwa na kuudhiwa mpaka ikawafikia Nusura Yetu. Na hakuna abadilishaye Maneno ya Allah. Na bila shaka zimekufikia habari za Mitume wao.”*** (6:34).

Kisha Allah تعالى Anataja Neema Zake kwa viumbe Wake; Anawalinda usiku na mchana, kwa Kuwatunza na Kuwatizama kwa Jicho Lake Lisilolala wala Kusinzia. Akasema:

قُلْ مَن يَكْلُؤْكُمْ بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ مِنَ الرَّحْمَنِ ۗ

***“Sema: Nani anayekulindeni usiku na mchana na Ar-Rahmani, Mwingi wa Rehema?”*** (21:42)

Maana yake: Badala ya Ar-Rahman Mwenyewe?

بَلْ هُمْ عَن ذِكْرِ رَبِّهِمْ مُّعْرِضُونَ ﴿٤٥﴾

***“Bali wao wanapuuza kumkumbuka Mola wao Mlezi.”***

Maana yake: Hawatambui neema na Ihsani za Allah تعالى kwao; wanakengeuka na Ishara na Baraka Zake. Kisha Akasema:

أَمْ لَهُمْ ءَالِهَةٌ تَمْنَعُهُمْ مِّنْ دُونِنَا

***“Au wao wanao miungu wataoweza kuwakinga Nasi?”***

Hili ni swali la balagha lenye lengo la kukanusha na kushutumu. Maana yake ni, je wao wana miungu wowote wanaoweza kuwalinda, kuwatumza mbali na Yeye? Sio kama wanavyodhania au wanavyodai. Kwa hiyo Akasema:

لَا يَسْتَطِيعُونَ نَصْرَ أَنفُسِهِمْ

***“Hao hawawezi kujinusuru nafsi zao.”***

Hawa miungu wanayoitegemea badala ya Allah تعالى hawawezi hata kujisaidia wao wenyewe.

وَلَا هُمْ مِنَّا يُصْحَبُونَ ﴿٤٣﴾

***“Wala hawatalindwa Nasi!”***

Amepokea Al-'Awfiy kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema:

وَلَا هُمْ مِنَّا يُصْحَبُونَ ﴿٤٣﴾

***“Wala hawatalindwa Nasi!”***

Maana yake: Hawataweza kulindwa kutoka na adhabu Yetu.<sup>1</sup>

\* \* \*

<sup>1</sup> Atw-Twabariy, 18:448. Isnadi yake ina dosari.

بَلْ مَتَّعْنَا هَٰؤُلَاءِ وَءَابَاءَهُمْ حَتَّىٰ طَالَ عَلَيْهِمُ الْعُمُرُ أَفَلَا يَرَوْنَ أَنَا نَأْتِي الْأَرْضَ نَنْقُصُهَا مِنْ أَطْرَافِهَا أَفَهُمُ الْغَالِبُونَ ﴿٤٤﴾ قُلْ إِنَّمَا أُنذِرُكُم بِالْوَحْيِ وَلَا يَسْمَعُ الصُّمُّ الدُّعَاءَ إِذَا مَا يُنذَرُونَ ﴿٤٥﴾ وَلَئِن مَّسَّتْهُمُ نَفْحَةٌ مِّنْ عَذَابِ رَبِّكَ لَيَقُولُنَّ يَا وَيْلَتَنَا إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿٤٦﴾ وَنَضَعُ الْمَوَازِينَ الْقِسْطَ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ فَلَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا وَإِن كَانَ مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِّنْ حَرْدَلٍ أَتَيْنَا بِهَا وَكَفَىٰ بِنَا حَٰسِبِينَ ﴿٤٧﴾ وَلَقَدْ ءَاتَيْنَا مُوسَىٰ الْوَحْيَ وَإِن يُؤْتِيكَ مِنْ بَدَلٍ مِّثْقَالَ ذَرَّةٍ شَاكَ وَكُنَّا بِكُمْ مُّشَفِقِينَ ﴿٤٨﴾ وَكَذَٰلِكَ نُفَصِّلُ الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ ﴿٤٩﴾ وَإِن يُؤْتِيكَ مِنْ بَدَلٍ مِّثْقَالَ ذَرَّةٍ شَاكَ وَكُنَّا بِكُمْ مُّشَفِقِينَ ﴿٥٠﴾ وَإِن يُؤْتِيكَ مِنْ بَدَلٍ مِّثْقَالَ ذَرَّةٍ شَاكَ وَكُنَّا بِكُمْ مُّشَفِقِينَ ﴿٥١﴾ وَإِن يُؤْتِيكَ مِنْ بَدَلٍ مِّثْقَالَ ذَرَّةٍ شَاكَ وَكُنَّا بِكُمْ مُّشَفِقِينَ ﴿٥٢﴾ وَإِن يُؤْتِيكَ مِنْ بَدَلٍ مِّثْقَالَ ذَرَّةٍ شَاكَ وَكُنَّا بِكُمْ مُّشَفِقِينَ ﴿٥٣﴾ وَإِن يُؤْتِيكَ مِنْ بَدَلٍ مِّثْقَالَ ذَرَّةٍ شَاكَ وَكُنَّا بِكُمْ مُّشَفِقِينَ ﴿٥٤﴾ وَإِن يُؤْتِيكَ مِنْ بَدَلٍ مِّثْقَالَ ذَرَّةٍ شَاكَ وَكُنَّا بِكُمْ مُّشَفِقِينَ ﴿٥٥﴾ وَإِن يُؤْتِيكَ مِنْ بَدَلٍ مِّثْقَالَ ذَرَّةٍ شَاكَ وَكُنَّا بِكُمْ مُّشَفِقِينَ ﴿٥٦﴾

بَلْ مَتَّعْنَا هَٰؤُلَاءِ وَءَابَاءَهُمْ حَتَّىٰ طَالَ عَلَيْهِمُ الْعُمُرُ أَفَلَا يَرَوْنَ أَنَا نَأْتِي الْأَرْضَ نَنْقُصُهَا مِنْ أَطْرَافِهَا أَفَهُمُ الْغَالِبُونَ ﴿٤٤﴾ قُلْ إِنَّمَا أُنذِرُكُم بِالْوَحْيِ وَلَا يَسْمَعُ الصُّمُّ الدُّعَاءَ إِذَا مَا يُنذَرُونَ ﴿٤٥﴾ وَلَئِن مَّسَّتْهُمُ نَفْحَةٌ مِّنْ عَذَابِ رَبِّكَ لَيَقُولُنَّ يَا وَيْلَتَنَا إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿٤٦﴾ وَنَضَعُ الْمَوَازِينَ الْقِسْطَ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ فَلَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا وَإِن كَانَ مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِّنْ حَرْدَلٍ أَتَيْنَا بِهَا وَكَفَىٰ بِنَا حَٰسِبِينَ ﴿٤٧﴾

44. Bali Tuliwastarehesha hawa na baba zao mpaka umri ukawa mrefu kwao. Je, hawaoni ya kwamba Sisi Tunaifikia ardhi Tukii-punguza ncha zake? Basi je! Hao ni wenye kushinda?

45. Sema: Mimi nakuonyeni

kwa Wahyi. Na viziwi hawasikii wito wanapoonywa.

46. Na wanapoguswa na mpulizo mmoja tu wa adhabu itokayo kwa Mola

**wako Mlezi, bila ya shaka wao husema: Ole wetu! Hakika tulikuwa wenye kudhulumu.**

**47. Nasi Tutaweka mizani za uadilifu kwa Siku ya Kiyama. Basi nafsi haitadhulumiwa kitu chochote. Hata ikiwa ni uzito wa chembe ya khardali Tutaiteta. Nasi Tunatosha kuwa washika hesabu.**

**Kudanganyika Washirikina kwa muda wao mrefu wa Kustarehe Duniani, na Kuwabainishia Wao Haki**

Allah تعالی Anatupasha habari za washirikina jinsi walivyodanganywa na kupotezwa kwa starehe walizo nazo duniani na maisha yao marefu waliyopewa. Kwa ajili ya hilo wakaamini kuwa wanafuata njia ya sawa na nzuri. Kisha Akawaonya Aliyetukuka kwa Kusema:

أَفَلَا يَرَوْنَ أَنَا نَأْتِي الْأَرْضَ نَنْقُصُهَا مِنْ أَطْرَافِهَا

**“Je, hawaoni ya kwamba Sisi Tunaifikia ardhi Tukiipunguza ncha zake?”**

Hii ni kama ile Aya:

وَلَقَدْ أَهْلَكْنَا مَا حَوْلَكُمْ مِنَ الْقَرْيِ وَصَرَّفْنَا الْآيَاتِ لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُونَ ﴿٢٧﴾

**“Na hakika Tuliangamiza miji iliyokuzungukeni, na Tuliwabainishia Aya Zetu ili warejee.” (46:27)**

Na amesema Al-Hasan Al-Baswriy: “Hii inamaanisha ushindi wa Uislamu dhidi ya ukafiri”<sup>1</sup>. Na maana ya ibara hii ni kuwa je, hawazingatii nusura ya Allah تعالی kwa waumini (marafiki/ walii Wake) dhidi ya maadui zao. Allah تعالی Aliyaangamiza mataifa yaliyokufuru na miji iliyodhulumu na kuwaokoa waja Wake Waumini Kwa hiyo Akasema:

أَفَهُمْ أَغْلِبُونَ ﴿٢٨﴾

**“Basi je! Hao ni wenye kushinda?”** Maana yake: Bali wao watashindwa, watakuwa chini, watahasirika na kudhalilishwa.

<sup>1</sup> Atw-Twabariy, 1:494.

Na Kauli Yake:

قُلْ إِنَّمَا أُنذِرُكُمْ بِالْوَحْيِ ۗ

**“Sema: Mimi nakuonyeni kwa Wahyi”**, Maana yake: Hakika mimi nafikisha tu onyo la adhabu na kisasi kutoka kwa Allah تعالی, na hii si zaidi kwa yale Aliyoniteremshia Allah تعالی. Hata hivyo, hilo halina faida kwa aliyefanywa kipofu na Allah تعالی na Akaweka kizibo kwenye masikio yake na moyo wake. Kwa hiyo, Akasema:

وَلَا يَسْمَعُ الصُّمُّ الدُّعَاءَ إِذَا مَا يُنذَرُونَ ﴿٥٦﴾

**“Na viziwi hawasikii wito wanapoonywa”.**

Na Kauli Yake:

وَلَيْنَ مَسْتَهْمَرٍ نَفْحَةٌ مِّنْ عَذَابِ رَبِّكَ لَيَقُولُنَّ يَا وَيْلَتَنَا إِنَّا كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿٥٧﴾

**“Na wanapoguswa na mpulizo mmoja tu wa adhabu itokayo kwa Mola wako Mlezi, bila ya shaka wao husema: Ole wetu! Hakika tulikuwa wenye kudhulumu.”**

Maana: Inapowagusa hawa waliokadhibisha adhabu duni na ya chini zaidi kutoka kwa Allah تعالی, watatambua madhambi yao waliyoyafanya na kukubali kuwa wao walikuwa wakizidhulumu nafsi zao duniani. Na Kauli Yake:

وَنَضَعُ الْمَوَازِينَ الْقِسْطَ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ فَلَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا ۗ

**“Nasi Tutaweka mizani za uadilifu kwa Siku ya Kiyama. Basi nafsi haitadhulumiwa kitu chochote.”**

Maana: Tutaweka kwa uadilifu mizani Siku ya Kiyama. Wanazuoni wengi wanaeleza kuwa mizani ni moja, na ibara ya wingi imetumiwa kuonesha idadi kubwa ya amali itakayopimwa. Na Kauli Yake:

فَلَا تُظْلَمُ نَفْسٌ شَيْئًا ۗ وَإِنْ كَانَ مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِّنْ حَرْدَلٍ أَتَيْنَا بِهَا ۗ وَكَفَىٰ بِنَا

حَلِيبِينَ ﴿٥٨﴾

**“Basi nafsi haitadhulumiwa kitu chochote. Hata ikiwa ni uzito wa chembe ya khardali Tutaileta. Nasi Tunatosha kuwa washika hisabu”.**



Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَلَا يَظْلِمُ رُبُّكَ أَحَدًا ﴿٤٩﴾

**“Na Mola wako Mlezi hamdhulumu yeyote.” (18:49)**

Na Amesema:

إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ ۖ وَإِنْ تَكَ حَسَنَةً يُّضْعِفْهَا وَيُؤْتِ مِنْ لَدُنْهُ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٤٠﴾

**“Hakika Allah Hawadhulumu viumbe Vyake uzito wa atomu (dharrah); na kama likiwa ni jambo jema Atalizidisha na Kutoa ujira mkubwa unaotoka Kwake.” (4:40)**

Na amesema Luqmaan:

يَبْنِيْ إِيَّاهَا إِنْ تَكُ مِثْقَالَ حَبَّةٍ مِّنْ حَرْدَلٍ فَتَكُنْ فِي صَخْرَةٍ أَوْ فِي السَّمَوَاتِ أَوْ فِي الْأَرْضِ يَأْتِيهَا اللَّهُ إِنْ اللَّهُ لَطِيفٌ خَبِيرٌ ﴿١٦﴾

**“Ewe mwanangu! Kwa hakika jambo lolote lijapokuwa na uzito wa chembe ya hardali, likawa ndani ya jabali au mbinguni au katika ardhi, Allah Atalileta (Amlipe aliyefanya); bila shaka Allah ni Mjuzi wa mambo yaliyofichikana, na Mjuzi wa mambo yaliyodhahiri.” (31:16)**

Na katika Sahihi mbili kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«كَلِمَتَانِ خَفِيفَتَانِ عَلَى اللِّسَانِ، ثَقِيلَتَانِ فِي الْمِيزَانِ، حَبِيبَتَانِ إِلَى الرَّحْمَنِ: سُبْحَانَ اللَّهِ وَبِحَمْدِهِ، سُبْحَانَ اللَّهِ الْعَظِيمِ»

**“Maneno mawili yaliyo hafifu ulimini, lakini mazito kwenye mizani na yanayompendeza Ar-Rahman (Mwingi wa Rehema): (Ametakasika Allah na Sifa zote ni Zake, Ametakasika Allah Aliye Mtukufu na Ndiye Mkubwa)<sup>1</sup>”.**

Pia amepokea Imaam Ahmad kutoka kwa mama Aishah رضي الله عنها amesema kuwa mmoja wa Maswahaba wa Mtume ﷺ alikaa mbele yake, akasema: “Ewe

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baariy 13:547 na Muslim 4:2072.

Mtume wa Allah! Nina watumishi wawili walionidang'anya, wakanifanyia hiyana na kuniasi. Kwa ajili hiyo nikawapiga na kuwatusi. Je, nasimama wapi na wao?" Mtume ﷺ akasema:

«يُحْسَبُ مَا خَانُوكَ وَعَصَوْتَ وَكَذَّبُوكَ وَعِقَابُكَ إِيَّاهُمْ، فَإِنْ كَانَ عِقَابُكَ إِيَّاهُمْ بِقَدْرِ دُنُوبِهِمْ، كَانَ كَفَافًا لَكَ وَلَا عَلَيْكَ، وَإِنْ كَانَ عِقَابُكَ إِيَّاهُمْ دُونَ دُنُوبِهِمْ، كَانَ فَضْلًا لَكَ، وَإِنْ كَانَ عِقَابُكَ إِيَّاهُمْ فَوْقَ دُنُوبِهِمْ، اقْتَصَّ لَهُمْ مِنْكَ الْفَضْلُ الَّذِي بَقِيَ تَبْلُكَ»

*"Kunahesabiwa waliyokuhini, kukuasi na kukudang'anya dhidi ya adhabu uliyowapatia. Ikiwa adhabu uliyowapatia ni sawa na madhambi yao, basi hakuna utakachohesabiwa wala kitakachokuwa dhidi yako. Na adhabu yako kwao ikiwa ni duni kuliko madhambi yao, hilo litakuwa bora kwako. Na ikiwa adhabu yako kwao ni zaidi ya madhambi yao, Allah Atachukua haki yao kutoka kwao".*

Hapo mtu yule akaanza kulia kwa sauti mbele ya Mtume ﷺ. Mtume ﷺ akasema:

«مَا لَهُ لَا يَفْرَأُ كِتَابَ اللَّهِ ﴿وَتَضَعُ الْمَوَازِينَ الْقِسْطَ لِيَوْمِ الْقِيَامَةِ فَلَا تُخْلَفُ﴾ نَسْرَ شَيْئًا وَإِنْ كَانَتْ يَمْشِي حَكِيمًا مِنْ حَرْدَلٍ أَيْنَا بِهَا وَكَفَى بِنَا حَسِيبًا ﴿٤٧﴾»

*"Ana nini huyo (mtu) kwani yeye hasomi Kitabu cha Allah, "Nasi Tutaweka mizani za uadilifu kwa Siku ya Kiyama. Basi nafsi haitadhulumiwa kitu chochote. Hata ikiwa ni uzito wa chembe ya khardali Tutaileta. Nasi Tunatosha kuwa washika hesabu".*

Akasema mtu yule: "Ewe Mtume wa Allah! Sipati kitu kilicho bora kuliko kutengana na hao – yaani watumishi wake – ninakushuhudisha kuwa wote ni huru sasa"<sup>1</sup>.

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَىٰ وَهَارُونَ الْفُرْقَانَ وَضِيَاءً وَذِكْرًا لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٤٨﴾ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُم بِالْغَيْبِ وَهُمْ مِنْ السَّاعَةِ مُشْفِقُونَ ﴿٤٩﴾ وَهَذَا ذِكْرٌ مُّبَارَكٌ أَنْزَلْنَاهُ أَفَأَنْتُمْ لَهُ مُنْكَرُونَ ﴿٥٠﴾

<sup>1</sup> Ahmad 6:280 na at-Tirmidhiy 3165. Isnadi yake ni dhaifu.

**48. Na kwa yakini Tuliwapa Musa na Haarun kipambanuzi, na mwangaza, na makumbusho kwa wachamngu,**

**49. Ambao wanamkhofu Mola wao Mlezi faraghani, na wanaiogopa Saa ya Kiyama.**

**50. Na haya ni makumbusho yaliyobarikiwa, Tuliyoyateremsha. Basi je! Mnayakataa?**

### Kuteremshwa Taurati na Qur'ani

Tayari tumetaja kuwa Allah تعالى mara nyingi Anamtaja Musa عليه السلام na Muhammad ﷺ pamoja, na mara nyingi Anataja Vitabu vyao pamoja pia. Kwa hiyo Akasema:

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَىٰ وَهَارُونَ الْفُرْقَانَ

**“Na kwa yakini Tuliwapa Musa na Haarun kipambanuzi.”**

Amesema Mujaahid: “Hii inamaanisha Kitabu”<sup>1</sup>. Na amesema Abu Swalih: “Hiyo ni Taurati”. Na amesema Qatadah: “Yaliyoruhusiwa na kukatazwa na Taurati na jinsi gani Allah تعالى Alivyopambanua haki na batili”<sup>2</sup>. Alhasili ni kuwa Vitabu vyote vya mbinguni vimekusanya kipambanuzi baina ya haki na batili, uongofu na upotevu, kuvuka mipaka na njia nyoofu, halali na haramu, na yote yenye kujaza muangaza, uongofu, hofu, kutubu na kurudi kwa Allah تعالى na kuwa na unyenyekevu moyoni. Kwa hiyo Allah تعالى Akasema:

الْفُرْقَانَ وَضِيَاءً وَذِكْرًا لِّلْمُتَّقِينَ ﴿٥٠﴾

**“Kipambanuzi, na muangaza, na makumbusho kwa wachamungu.”**

Maana: Ni ukumbusho na mawaidha kwao. Kisha Akawaelezea kwa Kusema:

الَّذِينَ تَخْشَوْنَ رَبَّهُم بِالْغَيْبِ

**“Ambao wanamkhofu Mola wao Mlezi kwa ghaibu.”**

Hii ni kama Aya ifuatayo:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:453.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:453.

مَنْ حَشِيَ الرَّحْمَنَ بِالْغَيْبِ وَجَاءَ بِقَلْبٍ مُنِيبٍ ﴿٣٣﴾

**“Na anayemuogopa Allah, Mwingi wa Rehema, na akaja kwa moyo ulioelekea.” (50:33).**

Na kama Kauli Yake:

إِنَّ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ رَبَّهُم بِالْغَيْبِ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ كَبِيرٌ ﴿١٢﴾

**“Hakika wale wanao muogopa Mola wao Mlezi, na hali ya kuwa hawamuoni watapata msamaha na malipo makubwa.” (67:12).**

وَهُمْ مِنَ السَّاعَةِ مُشْفِقُونَ ﴿١١﴾

**“Na wanaiogopa Saa ya Kiyama.”**

Maana yake: Wakiwa na hofu na kuogopa. Kisha Akasema Aliyetukuka:

وَهَذَا ذِكْرٌ مُّبَارَكٌ أَنْزَلْنَاهُ

**“Na haya ni makumbusho yaliyobarikiwa, Tuliyoysteremsha.”**

Maana yake: Qur’ani Tukufu ambayo haifikiwi na batili mbele wala nyuma yake, imeteremshwa na Mwingi wa Hekima na Mwenye Kustahiki Kusifiwa.

أَفَأَنْتُمْ لَهُ مُنْكَرُونَ ﴿١٠﴾

**“Basi je! Munyakataa?.”**

Maana yake: Je, munalikataa hilo ilhali ipo katika upeo wa ukweli?

﴿٩﴾ \* وَلَقَدْ آتَيْنَا إِبْرَاهِيمَ رُشْدَهُ مِن قَبْلُ وَكُنَّا بِهِ عَالِمِينَ ﴿٩﴾ إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ مَا

هَذِهِ التَّمَاثِيلُ الَّتِي أَنْتُمْ لَهَا عَاكِفُونَ ﴿١٠﴾ قَالُوا وَجَدْنَا آبَاءَنَا لَهَا عِبَادِينَ ﴿١٠﴾

قَالَ لَقَدْ كُنْتُمْ أَنْتُمْ وَآبَاؤُكُمْ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿١١﴾ قَالُوا أَجِئْتَنَا بِالْحَقِّ أَمْ أَنْتَ مِنَ

الضَّالِّينَ ﴿١٢﴾ قَالَ بَلْ رَبُّكُمْ رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ الَّذِي فَطَرَهُمْ وَأَنَا عَلَىٰ ذَٰلِكُمْ

مِنَ الشَّاهِدِينَ ﴿١٣﴾

**51. Na hakika Tulikwishampa Ibrahimu uongofu wake zamani, na Tulikuwa Tunamjua.**

**52. Alipomuambia baba yake na watu wake: Ni nini haya masanamu haya mnayoyashughulikia kuyaabudu?**

**53. Wakasema: Tumewakuta baba zetu wakiyaabudu.**

**54. Akasema: Bila ya shaka nyinyi na baba zenu mumekuwa katika upotofu uliodhahiri.**

**55. Wakasema: Je! Umetujia kwa maneno ya kweli au wewe ni katika wachezao tu?**

**56. Akasema: Bali Mola wenu Mlezi ni Mola Mlezi wa mbingu na ardhi Ambaye Ndiye Aliyeziumba. Na mimi ni katika wenye kuyashuhudia hayo.**

### Kisa cha Ibrahimu عليه السلام na Watu Wake

Allah تعالى Anatuelezea kuhusu Rafiki Yake wa karibu, Ibrahimu عليه السلام, na jinsi gani Alivyomtunukia uongofu hapo zamani, yaani kuanzia utoto wake. Alimfunulia ukweli na dalili dhidi ya watu wake. Kama Anavyosema Allah تعالى katika Aya nyingine:

وَتِلْكَ حُجَّتُنَا آتَيْنَاهَا إِبْرَاهِيمَ عَلَىٰ قَوْمِهِ ۗ

**“Na hizi ndizo baadhi ya hoja Zetu Tulizompa Ibrahimu juu ya watu wake...” (6:83).**

Nukta iliyo hapa ni kuwa Allah تعالى Anatuambia Amempa Ibrahimu عليه السلام uongofu zamani, yaani tayari Amemuongoa akiwa mdogo.

وَكُنَّا بِمِهِ عَلِيمِينَ ﴿٨٣﴾

**“Na Tulikuwa Tunamjua.”** Maana yake: Alikuwa ni mwenye kustahiki hayo. Kisha Akasema Aliyetukuka:

إِذْ قَالَ لِأَبِيهِ وَقَوْمِهِ مَا هَذِهِ التَّمَاثِيلُ الَّتِي أَنْتُمْ لَهَا عَاكِفُونَ

**“Alipomuambia baba yake na watu wake: Ni nini haya masanamu mnayoyashughulikia kuyaabudu?”**

Huu ni uongofu aliopatiwa akiwa kijana: Kukataa kwake Ibada ya masanamu ya watu wake badala ya kumuabudu Allah تعالى. Ibrahimu عليه السلام akasema:

مَا هَذِهِ التَّمَاثِيلُ الَّتِي أَنْتُمْ لَهَا عَاكِفُونَ ﴿٤٤﴾

***“Ni nini haya masanamu mnayoyashughulikia kuyaabudu?”***

Maana yake: Munayoyaabudu kwa kuyanyenyekea kabisa.

قَالُوا وَجَدْنَا آبَاءَنَا لَهَا عَابِدِينَ ﴿٤٥﴾

***“Wakasema: Tumewakuta baba zetu wakiyaabudu.”***

Maana yake: Hawakuwa na hoja nyingine mbali na vitendo vya upotevu vya babu zao. Ibraahim عليه السلام akasema:

قَالَ لَقَدْ كُنْتُمْ أَنْتُمْ وَآبَاؤُكُمْ فِي ضَلَالٍ مُّبِينٍ ﴿٤٦﴾

***“Bila ya shaka nyinyi na baba zenu mumekuwa katika upotofu ulio dhahiri.”***

Maana yake: Kuzungumza na baba zenu ambao mumetoa dalili na hoja kwa amali zao ni sawa na kuzungumza nanyi. Nyote nyinyi na wao mumepotea na hamfuati njia nyoofu. Na pindi alipovunja ndoto zao na upotevu wa baba zao na kudharau miungu yao,

قَالُوا أَجِئْتَنَا بِالْحَقِّ أَمْ أَنْتَ مِنَ اللَّاعِبِينَ ﴿٤٧﴾

***“Wakasema: Je! Umetujia kwa maneno ya kweli au wewe ni katika wachezao tu?”***

Wakasema (kumuambia Ibrahimu عليه السلام): “Je, haya maneno yatokayo kwako, unayasema kwa mzaha au ni ya kweli?”

Kwani hatujasikia maneno kama hayo kabla”.

قَالَ بَلْ رَبُّكُمْ رَبُّ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ الَّذِي فَطَرَهُمْ ۚ

***“Akasema: Bali Mola wenu Mlezi ni Mola Mlezi wa mbingu na ardhi Ambaye Ndiye Aliyeziumba.”***

Maana yake: Mola wenu Mlezi, hakuna mola asiyekuwa Yeye. Naye ni Yule Aliyeumba mbingu na ardhi na vyote vilivyomo ndani yake; Yeye Ndiye Aliyeanzisha Kuviumba; Yeye ni Muumba wa kila kitu.

وَأَنَا عَلَىٰ ذَٰلِكُمْ مِنَ الشَّاهِدِينَ ﴿٤٤﴾

***“Na mimi ni katika wenye kuyashuhudia hayo.”***

Maana yake: Nami nashuhudia kuwa hapana anayepasa kuabudiwa mbali na Yeye, wala hakuna Mola Mlezi mwengine.

\* \* \*

وَتَاللَّهِ لَأَكِيدَنَّ أَصْنَمَكُمْ بَعْدَ أَنْ تُوَلُّوا مُدْبِرِينَ ﴿٥٧﴾  
 فَجَعَلَهُمْ جُذَدًا إِلَّا كَبِيرًا هُمْ لَعَلَّهُمْ إِلَيْهِ يَرْجِعُونَ ﴿٥٨﴾  
 قَالُوا مَنْ فَعَلَ هَذَا بِآلِهَتِنَا إِنَّهُ لَمِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٥٩﴾  
 قَالُوا سَمِعْنَا فَتَى يَذُكُرُهُمْ يُقَالُ لَهُ إِبْرَاهِيمُ ﴿٦٠﴾  
 قَالُوا فَأَتُوا بِهِ عَلَى أَعْيُنِ النَّاسِ لَعَلَّهُمْ يَشْهَدُونَ ﴿٦١﴾  
 قَالُوا ءَأَنْتَ فَعَلْتَ هَذَا بِآلِهَتِنَا يَا إِبْرَاهِيمُ ﴿٦٢﴾ قَالَ بَلْ  
 فَعَلَهُ كَبِيرُهُمْ هَذَا فَسَتَلُوهُمْ إِنْ كَانُوا يَنْطِقُونَ ﴿٦٣﴾  
 فَرَجَعُوا إِلَى أَنْفُسِهِمْ فَقَالُوا إِنَّكُمْ أَنْتُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٦٤﴾  
 ثُمَّ نَكَسُوا عَلَى رُءُوسِهِمْ لَقَدْ عَلِمْتُمْ مَا هَؤُلَاءِ  
 يَنْطِقُونَ ﴿٦٥﴾ قَالَ أَفَتَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ مَا لَا  
 يَنْفَعُكُمْ شَيْئًا وَلَا يَضُرُّكُمْ ﴿٦٦﴾ أَفِي لَكُمْ وَلِمَا  
 تَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٦٧﴾ قَالُوا  
 حَرِّقُوهُ وَانصُرُوا آلِهَتَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ فَعِلِينَ ﴿٦٨﴾ قُلْنَا  
 يَبْنَازُ كُونِي بَرْدًا وَسَلَامًا عَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ ﴿٦٩﴾ وَأَرَادُوا بِهِ  
 كَيْدًا فَجَعَلْنَاهُمُ الْأَخْسَرِينَ ﴿٧٠﴾

وَتَاللَّهِ لَأَكِيدَنَّ أَصْنَمَكُمْ بَعْدَ أَنْ  
 تُوَلُّوا مُدْبِرِينَ ﴿٥٧﴾ فَجَعَلَهُمْ جُذَدًا  
 إِلَّا كَبِيرًا هُمْ لَعَلَّهُمْ إِلَيْهِ  
 يَرْجِعُونَ ﴿٥٨﴾ قَالُوا مَنْ فَعَلَ  
 هَذَا بِآلِهَتِنَا إِنَّهُ لَمِنَ الظَّالِمِينَ  
 ﴿٥٩﴾ قَالُوا سَمِعْنَا فَتَى يَذُكُرُهُمْ  
 يُقَالُ لَهُ إِبْرَاهِيمُ ﴿٦٠﴾ قَالُوا  
 فَأَتُوا بِهِ عَلَى أَعْيُنِ النَّاسِ لَعَلَّهُمْ  
 يَشْهَدُونَ ﴿٦١﴾ قَالُوا ءَأَنْتَ فَعَلْتَ  
 هَذَا بِآلِهَتِنَا يَا إِبْرَاهِيمُ ﴿٦٢﴾ قَالَ  
 بَلْ فَعَلَهُ كَبِيرُهُمْ هَذَا فَسَتَلُوهُمْ  
 إِنْ كَانُوا يَنْطِقُونَ ﴿٦٣﴾

57. Na Wallahi! Nitayafanyia vitimbi masanamuyenu haya baada ya mkishageuka kwenda zenu.

58. Basi akayavunja vipande vipande, ila mkubwa wao, ili wao wamrudie.

59. Wakasema: Nani aliyei-

fanyia haya miungu yetu? Hakika huyu ni katika waliodhulumu.

60. Wakasema: Tumemsikia kijana mmoja akiwataja. Anaitwa Ibrahimu.

61. Wakasema: Mleteni mbele ya macho ya watu, wapate kumshuhudia!

62. Wakasema: Je! Wewe umefanya haya kwa miungu yetu, ewe Ibrahimu?

63. Akasema: Bali amefanya hayo huyu mkubwa wao. Basi waulizeni ikiwa wanaweza kutamka.



### Ibrahim عليه السلام Ayavunja masanamu

Kisha Ibrahimu عليه السلام alikula kiapo, kilichosikiwa na baadhi ya watu wake, kuyafanyia vitimbi masanamu yao, yaani kuyavunja na kuyaharibu baada ya kuondoka kwao na kuyapa mgongo, watakapokwenda kwenye sherehe zao. Walikuwa na Idi (sherehe) waliyokuwa wakitoka kusherehekea. Amepokea Abu Is-haaq رحمه الله تعالى kutoka kwa Abii Ahwasw kuwa 'Abdallah (bin Mas'ud) رضى الله عنه alisema: "Pindi watu wa Ibrahimu عليه السلام walipotoka kwenda kusherehekea Idi yao, walipita kwake na kusema: 'Ewe Ibrahimu, je huji pamoja nasi?' Akasema: 'Mimi ni mgonjwa'". Ilikuwa ni siku moja tu kabla yake aliposema:

﴿وَتَأْتِيهِمْ لَأَكِيدَنَّ أَصْنَمَكُم بَعْدَ أَنْ تُولُوا مُدْبِرِينَ﴾

***"Na Wallahi! Nitayafanyia vitimbi masanamu yenu haya baada ya mkishageuka kwenda zenu."***

Na baadhi ya watu walimsikia akisema hayo. Na Kauli Yake:

﴿فَجَعَلَهُمْ جُودًا﴾

***"Basi akayavunja vipande vipande."*** Maana yake: Aliyavunja yote, "Ila kubwa lao", Maana: Isipokuwa lile sanamu lao kubwa. Hii ni kama ile Aya:

﴿فَرَاغَ عَلَيْهِمْ صَرْبًا يَأْتِمِينُ﴾

***"Kisha akawageukia kuwapiga kwa mkono wa kulia."*** (37:93).

Na Kauli Yake:

﴿لَعَلَّهُمْ إِلَيْهِ يَرْجِعُونَ﴾

***"Ili wao wamrudie"***. Kumetajwa kuwa aliweka nyundo kwenye mikono ya sanamu kubwa ili watu wadhania kuwa limesikia wivu lenyewe na kukataa kuabudiwa pamoja naye masanamu wadogo, hivyo likawavunja.

﴿قَالُوا مَنْ فَعَلَ هَذَا بِغَالِبَتِنَا إِنَّهُ لَمِنَ الظَّالِمِينَ﴾

***"Wakasema: Nani aliyefanya haya kwa miungu yetu? Hakika huyu ni katika waliodhulumu."***

Maana yake: Pindi waliporudi na kushuhudia aliyofanya Ibrahimu عليه السلام kwa kuyatweza na kuyadhaliisha, kumaanisha kuwa hayana sifa ya uungu ni dalili ya upumbavu na ujinga kwa wenye kuyaabudu.

قَالُوا مَنْ فَعَلَ هَذَا بِآلِهَتِنَا إِنَّهُ لَمِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٥٧﴾

**“Wakasema: Nani aliyefanya haya kwa miungu yetu? Hakika huyu ni katika walio dhulumu.”**

Maana yake: Kwa kitendo chake hicho.

قَالُوا سَمِعْنَا فَتَىٰ يَدُكُرُهُمْ يُقَالُ لَهُٗٓ إِنْبِرَاهِيمُ

**“Wakasema: Tumemsikia kijana mmoja akiwataja. Anaitwa Ibrahimu.”**

Maana: Wale waliomsikia akiapa kuyafanyia vitimbi masanamu hayo walisema, Tulimsikia kijana mmoja akiwazungumzia, na walisema kuwa anaitwa Ibrahimu. Na Kauli Yake:

قَالُوا فَآتُوا بِهِ عَلَىٰ أَعْيُنِ النَّاسِ

**“Wakasema: Mleteni mbele ya macho ya watu.”**Maana yake: Mbele ya umati mkubwa wa watu ili watu wote wawepo. Hili ndilo lililokuwa lengo la Ibrahimu عليه السلام, ili auambie umati huo mkubwa daraja ya upumbavu wao na jinsi gani wapo katika ujinga wa kuabudu masanamu ambayo hayawezi hata kujitetea kutokana na madhara au kujisaidia. Hivyo, vipi watawataka msaada?

قَالُوا ءَأَنْتَ فَعَلْتَ هَذَا بِآلِهَتِنَا يَا إِبْرَاهِيمُ ﴿٥٨﴾ قَالَ بَلْ فَعَلَهُ كَبِيرُهُمْ هَذَا

**“Wakasema: Je! Wewe umefanya haya kwa miungu yetu, ewe Ibrahimu? Akasema: Bali amefanya hayo huyu mkubwa wao.”**

Maana yake: Yule aliyemuacha bila ya kumvunja.

فَسَعَلُوهُمْ إِنْ كَانُوا يَنْطِقُونَ ﴿٥٩﴾

**“Basi waulizeni ikiwa wanaweza kutamka”.**

Kwa hilo alikuwa anataka wakubali kwa hiari yao kuwa haya masanamu hayawezi kuzungumza na kuwa hili sanamu halitasema lolote kwa sababu halina uhai.

Na katika Sahihi mbili kutoka kwa Abi Hurayrah رضي الله عنه Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ إِبْرَاهِيمَ عَلَيْهِ السَّلَامُ لَمْ يَكْذِبْ غَيْرَ ثَلَاثٍ: يَثْنَيْنِ فِي ذَاتِ اللَّهِ قَوْلُهُ:

“*Hakika Ibraahim* عليه السلام *hakudanganya ila mara tatu, mbili kwa ajili ya Allah – pale aliposema:*

بَلْ فَعَلَهُمْ كَيْدُهمْ هَذَا

‘*Bali amefanya hayo huyu mkubwa wao.*’ Na:

فَقَالَ إِنِّي سَقِيمٌ

‘*Hakika mimi ni mgonjwa.*’ (37:89).

قَالَ: وَبَيْنَا هُوَ يَسِيرُ فِي أَرْضِ جَبَّارٍ مِنَ الْجَبَابِرَةِ وَمَعَهُ سَارَةٌ، إِذْ نَزَلَ مِنْزِلًا فَأَتَى الْجَبَّارَ رَجُلٌ فَقَالَ: إِنَّهُ قَدْ نَزَلَ هَهُنَا رَجُلٌ بِأَرْضِكَ مَعَهُ امْرَأَةٌ أَحْسَنُ النَّاسِ، فَأَرْسَلَ إِلَيْهِ فَجَاءَ، فَقَالَ: مَا هَذِهِ الْمَرْأَةُ مِنْكَ؟ قَالَ: هِيَ أُخْتِي. قَالَ: فَادْهَبْ فَأَرْسِلْ بِهَا إِلَيَّ، فَانْطَلَقَ إِلَى سَارَةَ فَقَالَ: إِنَّ هَذَا الْجَبَّارَ قَدْ سَأَلَنِي عَنْكَ، فَأَخْبَرْتُهُ أَنَّكَ أُخْتِي، فَلَا تُكْذِبِينِي عِنْدَهُ، فَإِنَّكَ أُخْتِي فِي كِتَابِ اللَّهِ، وَإِنَّهُ لَيْسَ فِي الْأَرْضِ مُسْلِمٌ غَيْرِي وَغَيْرِكَ، فَانْطَلَقَ بِهَا إِبْرَاهِيمُ ثُمَّ قَامَ يُصَلِّي، فَلَمَّا أَنْ دَخَلَتْ عَلَيْهِ قَرَأَهَا أَهْوَى إِلَيْهَا فَتَنَّاوَلَهَا فَأَخِذَ أَخِذًا شَدِيدًا، فَقَالَ: ادْعِي اللَّهَ لِي وَلَا أَضْرِكِ، فَدَعَتْ لَهُ، فَأَرْسَلَ فَأَهْوَى إِلَيْهَا، فَتَنَّاوَلَهَا فَأَخِذَ بِمِثْلِهَا أَوْ أَشَدَّ، فَمَعَلَ ذَلِكَ الثَّلَاثَةَ، فَأَخِذَ فَذَكَرَ مِثْلَ الْمَرَّتَيْنِ الْأُولَتَيْنِ، فَقَالَ: ادْعِي اللَّهَ فَلَا أَضْرِكِ، فَدَعَتْ لَهُ فَأَرْسَلَ، ثُمَّ دَعَا أَدْنَى حُجَابِهِ فَقَالَ: إِنَّكَ لَمْ تَأْتِنِي بِإِنْسَانٍ، وَلَكِنَّكَ أَتَيْتَنِي بِسَبْطَانٍ، أَخْرَجْتَهَا وَأَعْطَيْتَهَا هَاجِرًا. فَأَخْرَجْتَ وَأَعْطَيْتَ هَاجِرًا، فَأَقْبَلْتُ، فَلَمَّا أَحْسَسَ إِبْرَاهِيمُ بِمَجِيئِهَا، انْفَتَلَ مِنْ صَلَاتِهِ، وَقَالَ: مَهَيْمٌ. قَالَتْ: كَفَى اللَّهُ كَيْدَ الْكَافِرِ الْفَاجِرِ، وَأَخَذَنِي هَاجِرًا.

*Akasema: Ibrahimu Alipokuwa akisafiri katika ardhi ya mmoja wa wababe pamoja na Saara; akapiga kambi, mtu mmoja alifika kwa mbabe na kumuambia: ‘Kuna mtu aliyepiga kambi katika ardhi yako na yuko pamoja na mwanamke mzuri kabisa katika watu’. Mbabe huyo alituma aitwe Ibrahimu, na kumuuliza: ‘Mwanamke huyu ana uhusiano gani nawe?’ Akasema: ‘Yeye ni dada yangu’. Akamuambia: ‘Nenda ukaniletee’. Hivyo, alikwenda kwa Saara na kumuambia: ‘Huyu mbabe ameniuliza kuhusu wewe, na nimemuambia kuwa*

wewe ni dada yangu, hivyo usimuache kudhania kuwa nimemuambia uongo. Kwani kwa hakika wewe ni dada yangu kulingana na Kitabu cha Allah, na hakuna Waislamu katika hii dunia ila wewe na mimi'. Kwa hivyo, Ibrahimu alimleta kwake, kisha akasimama kuswali. Pindi Saara alipoingia kwa mbabe huyo, naye akamuona alimkimbilia kwa matamano lakini akakamatwa mkamato mkubwa na mshtuko wa moyo. Akasema: 'Niombe kwa Allah nami sitakudhuru.' Akamuomba, naye akawa ni mwenye kupona. Kisha akamuendea tena kwa matamano, naye akakumbwa kama mara ya kwanza au zaidi. Hili liliendelea mara tatu, na kila wakati alikuwa akisema maneno hayo hayo kama alivyosema mara ya kwanza. Baada ya hapo alimuita mlinzi wake wa karibu na kumuambia, 'Hujaniletea mwanadamu, umeniletea shetani! Mtoe hapa na umpatie Haajar'. Hivyo, alitolewa nje na kupatiwa Haajar, naye (Saara) akenda zake. Ibrahimu alipohisi kuwa amerudi, alimaliza Swala yake na kugeuka. Akasema: 'Kumetokea nini?' Akamjibu: 'Allah Amenitosheleza kwa vitimbi vya kafiri huyu muovu na amenipatia Haajar kuwa kijakazi wangu'".

Muhammad bin Sirin رحمه الله تعالى amesema: "Abu Hurayrah رضي الله عنه alipokuwa akihadithia Hadithi hii, alisema: 'Huyu ni mama yenu, enyi watoto wa maji ya mbinguni'<sup>1</sup>.

فَرَجَعُوا إِلَىٰ أَنفُسِهِمْ فَقَالُوا إِنَّكُمْ أَنْتُمُ الظَّالِمُونَ ﴿٦٤﴾ ثُمَّ نَكَسُوا عَلَىٰ رُءُوسِهِمْ لَقَدْ عَلِمْتُمْ مَا هَٰؤُلَاءِ يَنْطِقُونَ ﴿٦٥﴾ قَالَ أَفَتَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَنْفَعُكُمْ شَيْئًا وَلَا يَضُرُّكُمْ ﴿٦٦﴾ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٦٧﴾

**64. Basi wakajirudi nafsi zao, wakasema: Hakika nyinyi mulikuwa madhalimu!**

**65. Kisha wakarejea kwenye ule ule upotovu wao wakasema: Wewe unajua kwamba hawa hawasemi.**

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Baariy 6:447 na Muslim 4:1840.

**66. Akasema: Basi nyinyi munawaabudu asiyekuwa Allah wasio kufaini kitu wala kukudhuruni?**

**67. Aibu yenu nyinyi na hivyo munavyoviabudu badala ya Allah! Basi nyinyi hamutii akilini?**

**Watu wa Ibrahimu عليه السلام Kukubali Udhaifu wa Miungu Yao, na Mawaidha ya Ibrahimu عليه السلام.**

Anasema Aliyetukuka Kutupasha habari pindi Ibrahim عليه السلام alipowaambia watu wake aliyowaambia,

فَرَجَعُوا إِلَىٰ أَنفُسِهِمْ

**“Basi wakajirudi nafsi zao.”**

Maana yake: Walijilaumu wenyewe kwa kutochukua tahadhari na kuwalinda miungu yao. Wakasema:

إِنَّكُمْ أَنْتُمْ الظَّالِمُونَ ﴿٦٦﴾

**“Hakika nyinyi mulikuwa madhalimu!”**

Maana yake: Kwa sababu ya kuwaacha na hamkuwalinda.

ثُمَّ نَكُسُوا عَلَىٰ رُءُوسِهِمْ

**“Kisha wakarejea kwenye ule ule upotovu wao.”**

Maana yake: Kisha wakatizama chini (kwenye ardhi), wakasema:

لَقَدْ عَلِمْتُمْ مَا هَٰؤُلَاءِ يَنطِقُونَ ﴿٦٧﴾

**“Wewe unajua kwamba hawa hawasemi.”**

Qataadah amesema: “Watu walikiri makosa yao, kwa hiyo wakasema:

لَقَدْ عَلِمْتُمْ مَا هَٰؤُلَاءِ يَنطِقُونَ ﴿٦٧﴾

**“Wewe unajua kwamba hawa hawasemi.”**

Kwa hiyo, vipi watutaka sisi kuwauliza wao, ikiwa hawawezi kusema na unajua hilo, kuwa hawawezi kuzungumza?

Katika hilo, Ibrahimu عليه السلام akawaambia pindi walipokubali:

قَالَ أَفَتَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَنْفَعُكُمْ شَيْئًا وَلَا يَضُرُّكُمْ ﴿٦٦﴾

**“Basi nyinyi mnawaabudu asiyekuwa Allah wasiokufaeni kitu wala kukudhuruni?”**

Maana yake: Ikiwa hawawezi kuzungumza, na pia hayawezi kuwanufaisha wala kuwadhuru, kwa nini mnayaabudu badala ya Allah تعالیٰ?

أَفِ لَكُمْ وَ لِمَا تَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٦٧﴾

**“Aibu yenu nyinyi na hivyo mnavyoviabudu badala ya Allah! Basi nyinyi hamutii akilini?”**

Maana yake: Je hamzingatii kwa muliyo nayo katika upotevu na ukafiri mkubwa mnaoufuata, ambao hakuna anayeukubali ila mjinga na dhalimu aliye muovu. Aliwashinda kwa hoja na kuwa acha bila ya njia ya kutokea.

Kwa hiyo Akasema Allah تعالیٰ:

وَتِلْكَ حُجَّتُنَا آتَيْنَاهَا إِبْرَاهِيمَ عَلَىٰ قَوْمِهِ ۗ

**“Na hizi ndizo baadhi ya hoja Zetu Tulizompa Ibrahimu juu ya watu wake.” (6:83).**

قَالُوا حَرِّقُوهُ وَانصُرُوا آلِهَتَكُمْ إِن كُنْتُمْ فاعِلِينَ ﴿٦٨﴾ فَلَمَّا بِنَارِ كُونِي بَرْدًا وَسَلَامًا

عَلَىٰ إِبْرَاهِيمَ ﴿٦٩﴾ وَأَرَادُوا بِهِ كَيْدًا فَجَعَلْنَاهُمُ الْأَخْسَرِينَ ﴿٧٠﴾

**68. Wakasema: Mchomeni moto, na muinusuru miungu yenu, ikiwa nyinyi ni watendao jambo!**

**69. Sisi Tukasema: Ewe moto! Kuwa baridi na salama kwa Ibrahimu!**

**70. Wao walimkusudia maovu, lakini Sisi Tukawafanya wao ndio waliokhasiri.**

**Ibrahim عليه السلام Kutupwa Motoni na Allah تعالى Kuudhibiti (Moto huo).**

Pindi hoja zao zilipopingwa na ajizi yao kuonekana wazi, ukweli na haki ilipokuwa dhahiri na batili mpaka kushindwa, walitumia nguvu za ufalme wao.

Wakasema:

حَرِّقُوهُ وَأَنْصُرُوا ءَالِهَتَكُمْ إِنْ كُنْتُمْ فَعَالِينَ ﴿٥٨﴾

***“Mchomeni moto, na muinusuru miungu yenu, ikiwa nyinyi ni watendao jambo!”***

Walikusanya kuni nyingi sana. Amesema As-Suddiy: “Hata ikiwa mwanamke ni mgonjwa, alikuwa akila kiapo kuwa lau atapona basi ataleta kuni za kumchoma Ibrahimu عليه السلام. Kisha walifukua shimo ardhini na kuziwasha (kuni), nao uliwaka kwa kutoa cheche kubwa na miale mikubwa. Hakujaonekana moto kama huo kabla ya hapo. Walimtia Ibrahim عليه السلام kwenye manati (mtambo wa kurushia mawe), kwa kufuata rai iliyotolewa na bedui wa Kikurdi kutoka Ufurusi (Iran)”<sup>1</sup>.

Shu’ayb Al-Jabathi amesema: “Alikuwa anaitwa Hayzan – Allah تعالى Akaijaalia ardhi kummeza na ataendelea kuzama ndani yake mpaka Siku ya Kiyama.” Walipomtupa alisema: ‘Ananitoshia Allah تعالى, Naye ni Mlinzi bora kabisa’<sup>2</sup>”. Kama alivyopokea Al-Bukhaari kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuwa alisema: “Ananitoshia Allah تعالى, Naye ni Mlinzi bora kabisa. Alisema maneno hayo Ibrahim عليه السلام alipotupwa motoni na Muhammad ﷺ aliyasema pale waliposema:

إِنَّ النَّاسَ قَدْ جَمَعُوا لَكُمْ فَاخْشَوْهُمْ فَزَادَهُمْ إِيمَانًا وَقَالُوا حَسْبُنَا اللَّهُ وَنِعْمَ الْوَكِيلُ

***‘Hakika watu wamekukusanyikieni, kwa hiyo waogopeni. Lakini maneno hayo yakawazidishia Imani, wakasema: Allah Atatukifia. Naye ni Mlinzi bora kabisa.’ (3:173)***<sup>3</sup>

Na Sa’id bin Jubayr amepokea kwa Ibn ‘Abbas رضي الله عنهما akisema: “Pindi Ibrahim عليه السلام alipotupwa motoni, mlinzi (Malaika) wa mvua alikuwa akisema: ‘Wakati gani nitaamriwa kuteremsha mvua?’ Lakini Amri ya Allah تعالى ilikuwa ya haraka. Amesema Allah تعالى:

<sup>1</sup> Al-Qurtwubiy 11:303.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:465.

<sup>3</sup> Fat’h ul Al-Baariy 8:77.

يَنْتَازُ كُونِي بَرْدًا وَسَلَامًا عَلَيَّ إِنِّي بَرَاهِيمَ ﴿٦٧﴾

***“Ewe moto! Kuwa baridi na salama kwa Ibrahim!”***

Akasema: ‘Hakubaki moto katika ardhi ila ulizimika’<sup>1</sup>. Ibn ‘Abbaas na Abul Aliyah wamesema: “Lau si usemi wa Allah تعالى:

وَسَلَامًا

***“Na salama.”***

“Ibrahimu عليه السلام angedhurika kwa baridi yake”<sup>2</sup>.

Na amesema Qatadah: “Siku hiyo hakubaki mnyama ila alikuwa anajaribu kuzima moto kwa ajili ya Ibrahimu عليه السلام”<sup>3</sup>. Na Kauli Yake:

وَأَزَادُوا بِهِ كَيْدًا فَجَعَلْنَاهُمُ الْأَخْسَرِينَ ﴿٦٨﴾

***“Wao walimkusudia maovu, lakini Sisi Tukawafanya wao ndio walio khasiri.”***

Maana yake: Walioshindwa, kutwezwa na kuwa chini, kwani walimtakia maovu Mtume عليه السلام, lakini Allah تعالى Aliwachimba wao na Kumuokoa Ibrahim عليه السلام kutokana na moto, na hivyo kushindwa.

\* \* \*

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:466.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:465-466.

<sup>3</sup> Atw-Twabariy 18:467.



وَجَجَيْنَهُ وُلُوطًا إِلَى الْأَرْضِ الَّتِي بَرَكْنَا فِيهَا لِلْعَالَمِينَ  
 ﴿٧١﴾ وَوَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ نَافِلَةً ۗ وَكُلًّا جَعَلْنَا  
 صَالِحِينَ ﴿٧٢﴾ وَجَعَلْنَاهُمْ أَيْمَةً يَهْدُونَ بِأَمْرِنَا  
 وَأَوْحَيْنَا إِلَيْهِمْ فِعْلَ الْخَيْرَاتِ وَإِقَامَ الصَّلَاةِ وَإِيتَاءَ  
 الزَّكَاةِ ۗ وَكَانُوا لَنَا عَبِيدِينَ ﴿٧٣﴾ وُلُوطًا إِتَيْنَهُ حُكْمًا  
 وَعِلْمًا وَجَجَيْنَهُ مِنَ الْقَرْيَةِ الَّتِي كَانَتْ تَعْمَلُ الْخَبِيثَ ۗ  
 إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمَ سَوْءٍ فَسَقِينَ ﴿٧٤﴾ وَأَدْخَلْنَاهُ فِي رَحْمَتِنَا ۗ  
 إِنَّهُ مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٧٥﴾ وَنُوحًا إِذْ نَادَى مِنْ قَبْلُ  
 فَاسْتَجَبْنَا لَهُ فَنَجَّيْنَاهُ وَأَهْلَهُ مِنَ الْكَرْبِ الْعَظِيمِ  
 ﴿٧٦﴾ وَنَصَرْنَاهُ مِنَ الْقَوْمِ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا ۗ إِنَّهُمْ  
 كَانُوا قَوْمَ سَوْءٍ فَأَغْرَقْنَاهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٧٧﴾ وَدَاوُدَ  
 وَسُلَيْمَانَ إِذْ يَحْكُمَانِ فِي الْحَرْثِ إِذْ نَفِثَتْ فِيهِ غَنَمُ  
 الْقَوْمِ وَكُنَّا لِحُكْمِهِمْ شَاهِدِينَ ﴿٧٨﴾ فَفَهَّمْنَاهَا  
 سُلَيْمَانَ ۗ وَكُلًّا آتَيْنَاهُ حُكْمًا وَعِلْمًا وَسَخَرْنَا مَعَ دَاوُدَ  
 الْجِبَالَ يُسَبِّحْنَ وَالطَّيْرَ ۗ وَكُنَّا فَاعِلِينَ ﴿٧٩﴾ وَعَلَّمْنَاهُ  
 صَنْعَةَ لَبُوسٍ لَكُمْ لِتُحْصِنَكُمْ مِنْ بَأْسِكُمْ ۗ فَهَلْ أَنْتُمْ  
 شَاكِرُونَ ﴿٨٠﴾ وَلَسَلِيمَانَ الرِّيحَ عَاصِفَةً تَجْرِي بِأَمْرِهِ إِلَى  
 الْأَرْضِ الَّتِي بَرَكْنَا فِيهَا ۗ وَكُنَّا بِكُلِّ شَيْءٍ عَالِمِينَ ﴿٨١﴾  
 وَرَبِّ الشَّيْطَانِ مَنْ يُغْوِصُونَ لَهُ وَيَعْمَلُونَ عَمَلًا  
 دُونَ ذَلِكَ ۗ وَكُنَّا لَهُمْ حَافِظِينَ ﴿٨٢﴾

وَجَجَيْنَهُ وُلُوطًا إِلَى الْأَرْضِ الَّتِي  
 بَرَكْنَا فِيهَا لِلْعَالَمِينَ ﴿٧١﴾ وَوَهَبْنَا  
 لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ نَافِلَةً ۗ وَكُلًّا  
 جَعَلْنَا صَالِحِينَ ﴿٧٢﴾ وَجَعَلْنَاهُمْ  
 أَيْمَةً يَهْدُونَ بِأَمْرِنَا وَأَوْحَيْنَا إِلَيْهِمْ  
 فِعْلَ الْخَيْرَاتِ وَإِقَامَ الصَّلَاةِ وَإِيتَاءَ  
 الزَّكَاةِ ۗ وَكَانُوا لَنَا عَبِيدِينَ ﴿٧٣﴾  
 وُلُوطًا إِتَيْنَهُ حُكْمًا وَعِلْمًا وَجَجَيْنَهُ  
 مِنَ الْقَرْيَةِ الَّتِي كَانَتْ تَعْمَلُ  
 الْخَبِيثَ ۗ إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمَ سَوْءٍ  
 فَسَقِينَ ﴿٧٤﴾ وَأَدْخَلْنَاهُ فِي رَحْمَتِنَا ۗ  
 إِنَّهُ مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٧٥﴾

71. Na Tukamuokoa yeye na Lutow Tukawapeleka kwenye nchi Tulioibariki kwa ajili ya walimwengu wote.

72. Naye Tukampa Is'haaq, na Ya'qub kuwa ni ziada. Na wote Tukawajaalia wawe watu wema.

73. Na Tukawafanya maimamu wakiongoa watu kwa Amri Yetu. Na Tukawafunulia watende

***kheri, na washike Sala, na watoe Zaka, na walikuwa wanatuabudu Sisi tu.***

***74. Na Lutwi Tukampa hukumu na elimu na Tukamuokoa na ule mji uliokuwa ukifanya maovu. Hakika hao walikuwa watu wabaya, wachafu.***

***75. Na Tukamuingiza katika Rehema Yetu. Hakika yeye ni miongoni mwa watenda mema.***

**Kuhamia Shamu kwa Ibrahimu عليه السلام na Lutwi عليه السلام**

Anasema Aliyetukuka huku Anatupasha habari kuwa Alimuokoa Ibrahimu عليه السلام kutoka katika moto uliowashwa na watu wake, na Akamtoa kutoka kwao, akahamia Shaam (Syria Kubwa) na kufika katika ardhi tukufu. Na Kauli Yake:

وَوَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ نَافِلَةً<sup>ط</sup>

***“Naye Tukampa Ishaq, na Ya’qub kuwa ni ziada”.***

‘Atwaa’ na Mujaahid wamesema: *“Naafilatan”* inamaanisha zawadi<sup>1</sup>. Ibn ‘Abbaas, Qatadah<sup>2</sup> na Al-Hakam bin Utaybah<sup>3</sup> wamesema: *“Naafilatan”* (Atwiya) ni zawadi ya mtoto aliye na mtoto (wa kiume). Maana: Ya’quub عليه السلام alikuwa mtoto wa Is’haaq عليه السلام. Hii ni kama alivyosema Allah تعالى:

فَبَشِّرْنَهَا بِإِسْحَاقَ وَمِنْ وَرَاءِ إِسْحَاقَ يَعْقُوبَ ﴿٧١﴾

***“Basi Tukampa habari njema ya Is’haaq na baada ya Is’haaq Ya’quub.” (11:71).***

‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam amesema: *“Aliomba mtoto mmoja, aliposema:*

رَبِّ هَبْ لِي مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٧٢﴾

***‘Ee Mola wangu Mlezi! Nipe mtoto awe miongoni mwa watenda mema.’***

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:471.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:471.

<sup>3</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 5:643.

Hivyo, Allah تعالى Akampa yeye, Is'haaq عليه السلام, na Akampa Ya'quub عليه السلام kama nyongeza na zawadi.

وَكُلًّا جَعَلْنَا صَالِحِينَ ﴿٧١﴾

**“Na wote Tukawajaalia wawe watu wema.”** Maana yake: Wote walikuwa wazuri na watu wema.

وَجَعَلْنَاهُمْ أئِمَّةً

**“Na Tukawafanya maimamu.”**

Maana yake: Ruwaza na kielelezo chema kufuata.

يَهْدُونَ بِأَمْرِنَا

**“Wakiongoa watu kwa Amri Yetu.”**

Maana yake: Kulingania katika Dini Yake kwa Amri Yake. Allah تعالى Anasema:

وَأَوْحَيْنَا إِلَيْهِمْ فِعْلَ الْخَيْرَاتِ وَإِقَامَ الصَّلَاةِ وَإِيتَاءَ الزَّكَاةِ ۗ

**“Na Tukawafunulia watende kheri, na washike Sala, na watoe Zaka.”**

Hapa pametajwa ujumla wa ibada, kisha ikafuatiwa kutajwa ibada mahususi.

وَكَانُوا لَنَا عِبْدِينَ ﴿٧٢﴾

**“Na walikuwa wanatuabudu Sisi tu.”**

Maana yake: Walifuata yale waliyokuwa wakiamrisha watu.

**Kutajwa Lutwi** عليه السلام

Kisha Allah تعالى Anamtaja Luutw عليه السلام, ambaye jina lake kamili lilikuwa Lutwi bin Haraan bin Azar عليه السلام. Alimuamini Ibrahim عليه السلام na kumfuata, hivyo kuhama naye, kama Anavyosema Allah تعالى:

﴿ فَقَامَنَ لَهُ لُوطٌ وَقَالَ إِنِّي مُهَاجِرٌ إِلَىٰ رَبِّي ۗ

**“Basi Lutwi akamuamini na akasema (Ibraahim): Hakika mimi nahamia katika (nchi Aliyoniamrisha) Mola wangu Mlezi.” (29:26).**

Allah تعالى Alimpa hukumu na elimu, Akamfunulia (kwa Kumteremshia Wahyi) na Akamjaalia kuwa Nabii Aliyempeleka katika mji wa Saduum na vitongoji vyake, lakini walimkataa na kumpinga, hivyo Allah تعالى Aliwaangamiza, kama Anavyotuambia sehemu nyingi katika Kitabu Chake Kitukufu. Kwa hiyo Akasema:

وَجِئْنَاهُ مِنَ الْقَرْيَةِ الَّتِي كَانَتْ تَعْمَلُ الْخَبِيثَۃَ ۗ إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمَ سَوْءٍ فَسَقِينَ ﴿٧٦﴾  
وَأَدْخَلْنَاهُ فِي رَحْمَتِنَا ۗ إِنَّهُ مِنَ الصَّالِحِينَ ﴿٧٧﴾

**“Tukamuokoa na ule mji uliokuwa ukifanya maovu. Hakika hao walikuwa watu wabaya, wachafu. Na Tukamuingiza katika Rehema Yetu. Hakika yeye ni miongoni mwa watenda mema”.**

وَنُوحًا إِذْ نَادَىٰ مِنْ قَبْلُ فَاسْتَجَبْنَا لَهُ فَنَجَّيْنَاهُ وَأَهْلَهُ مِنَ الْكَرْبِ الْعَظِيمِ ﴿٧٨﴾  
وَنَصْرَانَهُ مِنَ الْقَوْمِ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا ۗ إِنَّهُمْ كَانُوا قَوْمَ سَوْءٍ فَأَغْرَقْنَاهُمْ أَجْمَعِينَ

**76. Na Nuhu alipoita zamani, Nasi Tukamuitikia, na Tukamuokoa yeye na watu wake kutokana na shida kubwa.**

**77. Na Tukamnusuru na watu waliozikanusha Ishara Zetu. Hakika hao walikuwa watu wabaya. Basi Tukawazamisha wote.**

### Kutajwa Nuhu عليه السلام na Watu Wake

Allah تعالى Anatupasha habari, Alivyomjibu mja na Mtume Wake ﷺ, Nuhu عليه السلام, alipomuomba dhidi ya watu wake pale walipomkadhibisha:

فَدَعَا رَبَّهُ أَنِّي مَغْلُوبٌ فَانتَصِرْ ﴿٧٩﴾

**“Ndipo akamuomba Mola wake Mlezi: Kwa hakika mimi nimeshindwa, basi ninusuru.” (54:10).**

وَقَالَ نُوحٌ رَبِّ لَا تَذَرْنِي عَلَى الْأَرْضِ مِنَ الْكَافِرِينَ دَيَّارًا ﴿٨٠﴾ إِنَّكَ إِن تَذَرْنَاهُمْ يَضِلُّوا  
عِبَادَكَ وَلَا يَلِدُوا إِلَّا فَاجِرًا كَفَّارًا ﴿٨١﴾

**“Na Nuhu akasema: Mola wangu Mlezi! Usimuache juu ya ardhi mkazi wake yeyote katika makafiri. Hakika ukiwaacha watapoteza watu Wako wala hawatazaa ila watoto waovu wenye kufuru (kama wao).” (71:26-27).**

Hivyo, hapa Akasema:

إِذْ نَادَىٰ مِنْ قَبْلُ فَاسْتَجَبْنَا لَهُ فَنَجَّيْنَاهُ وَأَهْلَهُ

**“Alipoita zamani, Nasi Tukamuitikia, na Tukamuokoa yeye na watu wake”.**

Maana yake: Walioamini pamoja naye, kama Anavyosema Aliyetukuka mahala pengine:

وَأَهْلَكَ إِلَّا مَنْ سَبَقَ عَلَيْهِ الْقَوْلُ وَمَنْ ءَامَنَ وَمَا ءَامَنَ مَعَهُ إِلَّا قَلِيلٌ ﴿٤٠﴾

**“(Na wapakie watu wako) wa nyumbani kwako isipokuwa wale ambao imewapitia hukumu (ya Allah). Na wachukue wote walioamini. Na hawakuamini pamoja naye ila wachache tu.” (11:40)**

Na Kauli Yake:

مِنَ الْكُرْبِ الْعَظِيمِ ﴿٧١﴾

**“Kutokana na shida kubwa.”**

Maana yake: Kutokana na shida, kukadhibishwa (kukataliwa) na udhia (madhara). Hakika yeye aliwalingania watu wake kwa muda wa miaka elfu moja ila hamsini, akiwaita kwa Allah تعالى, na hakuna waliyoamini ila wachache tu. Watu wake walimchimba na kupanga kumuudhi, huku wakiusiana karne baada ya karne, kizazi baada ya kizazi, kumpinga yeye. Na Kauli Yake:

وَنَصَرْنَاهُ مِنَ الْقَوْمِ

**“Na Tukamnusuru na watu”.**

Maana yake: Tulimuokoa na Kumsaidia dhidi ya watu.

الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا إِيَّاهُمْ كَانُوا قَوْمٍ سَوَاءً فَأَغْرَقْنَاهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٧٧﴾

**“Waliozikanusha Ishara Zetu. Hakika hao walikuwa watu wabaya. Basi Tukawazamisha wote.”**

Maana yake: Allah تعالى Aliwaangamiza wote kwa ujumla, na hakubaki juu ya ardhi yeyote miongoni mwao, kama alivyoomba Mtume wao (dhidi yao).

وَدَاوُدَ وَسُلَيْمَانَ إِذْ يَخْتَصِمَانِ فِي الْخُرُوبِ إِذْ نَفَسَتْ فِيهِ غَنَمُ الْقَوْمِ وَكُنَّا لِحُكْمِهِمْ شَاهِدِينَ ﴿٧٨﴾ فَفَهَّمْنَاهَا سُلَيْمَانَ ۗ وَكُلًّا آتَيْنَا حُكْمًا وَعِلْمًا ۗ وَسَخَرْنَا مَعَ دَاوُدَ الْجِبَالَ يُسَبِّحْنَ وَالطَّيْرَ ۗ وَكُنَّا فَاعِلِينَ ﴿٧٩﴾ وَعَلَّمْنَاهُ صَنْعَةَ لَبُوسٍ لَّكُمْ لِيُحِصَنَكُمْ مِنْ بَأْسِكُمْ ۗ فَهَلْ أَنْتُمْ شَاكِرُونَ ﴿٨٠﴾ وَلَسُلَيْمَانَ الرِّيحَ عَاصِفَةً تَجْرِي بِأَمْرِهِ إِلَى الْأَرْضِ الَّتِي بَارَكْنَا فِيهَا ۗ وَكُنَّا بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمِينَ ﴿٨١﴾ وَمِنَ الشَّيَاطِينِ مَنْ يَغُوضُونَ لَهُ ۗ وَيَعْمَلُونَ عَمَلًا دُونَ ذَلِكَ ۗ وَكُنَّا لَهُمْ حَافِظِينَ ﴿٨٢﴾

**78. Na Daawuud na Sulaymaan walipokata hukumu katika kadhiya ya konde walipolisha humo mbuzi wa watu usiku. Na Sisi Tulikuwa wenye kushuhudia hukumu yao hiyo.**

**79. Tukamfahamisha Sulaymaan. Na kila mmoja wao Tulimpa hukumu na elimu. Na Tuliifanya milima na ndege kuwa pamoja na Daawuud imnyenyeekee na imtakase Allah. Na Sisi ndio Tuliofanya hayo.**

**80. Na Tukamfundisha kuunda mavazi ya vita kwa ajili yenu ili yakuhifadhini katika kupigana kwenu. Je! Mtakuwa wenye kushukuru?**

**81. Na Tukamsahilishia Sulaymaan upepo wa kimbunga wendao kwa amri yake kwenye ardhi Tuliyoibarikia. Na Sisi ndio Tunaojua kila kitu.**

**82. Na pia mashetani wanaompigia mbizi na kufanya kazi nyenginezo. Na Sisi Tulikuwa walinzi wao.**

**Dawud عليه السلام na Sulaymaan عليه السلام na Ishara Walizopewa pamoja; Kutajwa Kisa cha Watu ambao mbuzi wao Walilisha Usiku Kondeni.**

Amepokea Abu Is'haaq رحمه الله تعالى kutoka kwa Murrah bin Mas'ud ambaye amesema: "Konde hiyo ilikuwa na mizabibu, vikole vyake vilivyokuwa vikining'inia"<sup>1</sup>. Hii ndiyo iliyokuwa rai ya Shurayh<sup>2</sup>. Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema neno: "*Nafash*" inamaanisha kulisha"<sup>3</sup>. Shurayh, Az-Zuhriy na Qatadah wamesema neno: "*Nafash*" haipatikani ila usiku"<sup>4</sup>. Qatadah akaongeza: "(Na neno) *Al-Hamli* ni kulisha wakati wa mchana"<sup>5</sup>. Na amepokea Ibn Jariir رحمه الله تعالى kutoka kwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه kwa Kauli Yake:

وَدَاوُدَ وَسُلَيْمَانَ إِذْ يَحْكُمَانِ فِي الْحَرْثِ إِذْ نَفَشَتْ فِيهِ غَنَمُ الْقَوْمِ

***"Na Dawudi na Sulaymaan walipokata hukumu katika kadhiya ya konde walipolisha humo mbuzi wa watu usiku'.***

Akasema: Zabibu zilizokuwa zimemea na vikole vyake viliharibiwa na mbuzi. Dawud عليه السلام alitoa hukumu kuwa mwenye konde (la mizabibu) akae na mbuzi'. Sulaymaan عليه السلام akasema: 'Sio hivyo, ewe Nabii wa Allah!' Akasema: 'Ni vipi basi?' Sulayman عليه السلام akasema: 'Mpe mizabibu mwenye mbuzi aishughulikie mpaka imee na kunawiri kama ilivyokuwa, na mpe mbuzi mwenye mizabibu na mwache afaidike nayo mpaka mizabibu imee kama ilivyokuwa. Hapo mizabibu arudishiwe mwenyewe, na mbuzi nao warudishwe kwa mwenyewe'. Kwa hiyo Akasema:

فَفَهَّمْنَهَا سُلَيْمَانَ

***"Tukamfahamisha Sulaymaan"***<sup>6</sup>. Hivyo ndivyo alivyopokea Al-'Awfiy kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما<sup>7</sup>. Na Kauli Yake:

فَفَهَّمْنَهَا سُلَيْمَانَ وَكُلًّا ءَاتَيْنَا حُكْمًا وَعِلْمًا

***"Tukamfahamisha Sulaymaan. Na kila mmoja wao Tulimpa hukumu na elimu".***

<sup>1</sup> At-Tabari 18:474. Isnadi yake ina dosari.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:475.

<sup>3</sup> At-Tabari 18:477, 478.

<sup>4</sup> At-Tabari 18:477, 478.

<sup>5</sup> At-Tabari 18:477.

<sup>6</sup> At-Tabari 18:475.

<sup>7</sup> At-Tabari 18:475. Isnadi yake ni dhaifu.

Amepokea Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى kuwa pale Iyaas bin Mu'awiyah alipochaguliwa Qadhi, Al-Hasan alikuja kwake na kumkuta Iyaas akilia. Al-Hasan akamuuliza: "Kwa nini unalia?" Iyaas akasema: "Ewe Abu Sa'id! Imenifikia kuwa kuna Kadhi wa aina tatu: Kadhi aliyejitahidi akakosea, hivyo atakwenda Motoni; na Kadhi mwingine aliyemili (kupendelea) kwenye matamano, naye pia yuko Motoni; na mtu aliyejitahidi na kupatia (hukumu kuwa sawa), huyo yuko Peponi". Akasema Al-Hasan Al-Baswri رحمه الله تعالى : "Hakika kwa yale aliyotuelezea Allah تعالى kuhusu Dawud عليه السلام na Sulaymaan عليه السلام na Manabii na hukumu walizotoa ni dalili kuwa haya wanayosema watu ni uongo. Amesema Allah تعالى:

وَدَاوُدَ وَسُلَيْمَانَ إِذْ سَخَّرْنَا فِي آلِ حَارُثٍ إِذْ نَفَسْتُمْ فِيهِ غَمِّ الْقَوْمِ وَكُنَّا لِحَكْمِهِمْ

شَاهِدِينَ ﴿٢٦﴾

***"Na Daud na Sulayman walipokata hukumu katika kadhiya ya konde walipolisha humo mbuzi wa watu usiku. Na Sisi Tulikuwa wenyewe kushuhudia hukumu yao hiyo".***

"Allah تعالى Alimsifu Sulayman عليه السلام lakini hakumshutumu Dawud عليه السلام". Kisha yeye – Al-Hasan – akasema: "Allah تعالى Amechukua mambo matatu kutoka kwa mahakimu: Wasiuze haki kwa thamani ndogo, wasifuate matakwa na matamano yao na wasimuogope yeyote katika hukumu zao". Baada ya hapo akasoma:

يَدَاوُدُ إِنَّا جَعَلْنَاكَ خَلِيفَةً فِي الْأَرْضِ فَاحْكُم بَيْنَ النَّاسِ بِالْحَقِّ وَلَا تَتَّبِعِ الْهَوَىٰ

فَيُضِلَّكَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ ۗ

***"Ewe Daud! Hakika Tumekujaalia kuwa Khalifa katika ardhi, basi wahukumu watu kwa haki wala usifuate matamano ya nafsi yasije yakakupoteza na njia ya Allah..." (38:26).***

فَلَا تَخْشَوُا النَّاسَ وَآخِشُونَ

***"Basi msiwaogope watu, bali Niogopeni Mimi." (5:44)***

وَلَا تَشْتَرُوا بِآيَاتِي ثَمَنًا قَلِيلًا

***"Wala musibadilisha Aya Zangu kwa thamani ndogo." (5:44)<sup>1</sup>***

<sup>1</sup> Tahdhib Taarikh Dimishq 3:184 na Ibn Abi Haatim 8:2458.



Nikasema: Ama Manabii wote walikuwa ni wenye kulindwa na madhambi, wakisaidiwa na Allah تعالى. Ama wasiokuwa wao imethibiti katika Sahihi Bukhari kutoka kwa Amr bin Al-Asw رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema:

«إِذَا اجْتَهَدَ الْحَاكِمُ فَأَصَابَ، فَلَهُ أَجْرَانِ، وَإِذَا اجْتَهَدَ فَأَخْطَأَ، فَلَهُ أَجْرٌ»

*“Anapojitahidi hakimu na akasibu, atakuwa na ujira mara mbili. Na pindi anapojitahidi na akakosea, basi atapata ujira mara mmoja”<sup>1</sup>.*

Hadithi inakataa ule muono wa Iyaas aliyedhania kuwa lau atajitahidi upeo wake, akaisoma vyema kesi na kutosibu katika hukumu yake, atakwenda Motoni. Na Allah تعالى Anajua zaidi.

Na imekuja katika vitabu vya Suna – Hadithi: Makadhi wapo wa aina tatu: Makadhi wawili watakuwa motoni na mmoja atakuwa peponi. Kadhi aliyejua haki akahukumu kwa mujibu wa haki hiyo, huyo atakuwa peponi. Na kadhi aliyehukumu baina ya watu kwa kutojua fani hiyo. Huyo atakuwa motoni. Na kadhi aliyejua haki, kisha akaipindisha, huyo atakuwa motoni”<sup>1</sup> Kisa hiki katika Qur’ani kinafanana na ripoti iliyonukuliwa na Imaam Ahmad katika Musnad wake kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه aliyesema kuwa Mtume ﷺ amesema:

«بَيْنَمَا امْرَأَتَانِ مَعَهُمَا ابْنَانِ لَهُمَا، إِذْ جَاءَ الذُّبُّ فَأَخَذَ أَحَدَ الْاِبْنَيْنِ فَتَحَاكَمَتَا إِلَى دَاوُدَ، فَقَضَىٰ بِهِ لِلْكُبْرَىٰ، فَخَرَجَتَا فِدْعَاهُمَا سُلَيْمَانُ فَقَالَ: هَاتُوا السُّكَيْنَ أَشْمُهُ بَيْنَكُمَا: فَقَالَتِ الصُّغْرَىٰ: يَرْحَمُكَ اللهُ هُوَ ابْنُهَا لَا تَشْمُهُ، فَقَضَىٰ بِهِ لِلصُّغْرَىٰ»

*“Pale wanawake wawili walipokuwa pamoja na watoto wao wawili, alikuja mbwa mwitu na kumchukua mtoto mmoja kati yao, wakenda kwa Daudi kuhukumiwa. Alihukumu kuwa mtoto ni wa mwanamke mkubwa (kati ya hao wawili). Hapo wakaondoka, kisha Sulaymaan akawaita, akasema: ‘Nipatieni kisu ili nimgawe baina yenu’. Yule mwanamke mdogo akasema: ‘Allah Akurehemu, huyo mtoto ni wake (yaani wa mwanamke mkubwa), usimgawe’. Akahukumu kuwa huyo mtoto ni wa mwanamke mdogo”<sup>2</sup>.*

Na wameipokea Bukhaariy na Muslim katika Sahihi zao<sup>3</sup>. Na Nasaa’iy akaweka mlango katika Kitabu chake cha hukumu<sup>4</sup>. Na Kauli Yake:

<sup>1</sup> Fat’h Al-Baariy 13:318.

<sup>2</sup> Ahmad 2:322.

<sup>3</sup> Al-Bukhaariy 6769 na Muslim 1720.

<sup>4</sup> An-Nasaa’iy katika Al-Kubraa 5958.

وَسَخَّرْنَا مَعَ دَاوُدَ الْجِبَالَ يُسَبِّحْنَ وَالطَّيْرَ

**“Na Tuliifanya milima na ndege kuwa pamoja na Daud imnyenyeeke na imtakase Allah”.**

Na hiyo ni kwa sababu ya sauti yake nzuri katika kusoma Kitabu Chake cha Zaburi. Alipokuwa akisoma kwa sauti nzuri, ndege walikuwa wakisimama angani na kurudia baada yake na milima ilikuwa ikirudisha sauti yake kwa mwangwi. Na kwa hilo alipokuwa Mtume ﷺ akipita kwa Abu Musa Al-Ash'ariy akiwa anasoma Qur'ani usiku, naye alikuwa na sauti nzuri sana, alisimama na kusikiliza kisomo chake. Akasema:

«لَقَدْ أُوتِيَ هَذَا مِزْمَارًا مِنْ مَزَامِيرِ آلِ دَاوُدَ»

*“Hakika amepatiwa huyu mizumari (sauti nzuri) kati ya mizumari ya familia ya Daud”.*

Akasema: “Ewe Mtume wa Allah! Lau ningejua kuwa unanisikiliza ningefanya vizuri zaidi”<sup>1</sup>. Na Kauli Yake:

وَعَلَّمْنَاهُ صَنْعَةَ لَبُوسٍ لَكُمْ لِيُتَخَصَّنَكُمْ مِنْ بَأْسِكُمْ

**“Na Tukamfundisha Kuunda mavazi ya vita kwa ajili yenu ili yakuhifadhini katika kupigana kwenu.”**

Maana: Utengenezaji wa nguo za chuma (deraya). Amesema Qatadah: “Hakika nguo hizo za chuma kabla yake zilikuwa za pamba, Daudi عليه السلام ndiye wa kwanza wa kutengeneza vikuku vya chuma”<sup>2</sup>. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَأَلْنَا لَهُ الْحَدِيدَ ۖ أَنْ أَعْمَلَ سَدِغَاتٍ وَقَدِيرٍ فِي السَّرْدِ

**“Na Tukamlainishia chuma. Tukamuambia: Tengeneza (nguo za chuma) pana na upime vizuri katika kuunganisha...” (34:10-11),**

Maana: Usifanye vikuku vya deraya kupwaya hivyo kufanya msumari kutingika, wala usikaze sana msumari, hivyo kikuku kutozunguka. Kwa hiyo Akasema:

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Baariy 8:711.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:480.

لِتُحْصِنَكُمْ مِنْ بَأْسِكُمْ ط

**“Ili yakuhifadhini katika kupigana kwenu.”** Maana: Katika vita.

فَهَلْ أَنْتُمْ شَاكِرُونَ ﴿٣٦﴾

**“Je! Mutakuwa wenye kushukuru?”** Maana: Neema ya Allah تعالی juu yenu pale Alipomfunulia mja Wake, Daud عليه السلام kumfundisha yeye hayo kwa ajili yenu.

**Uwezo wa Sulayman عليه السلام Haukuwa na mfano Wake**

Na Kauli Yake:

وَلَسَلِيمَنَّ الرِّيحَ عَاصِفَةً

**“Na Tukamsahilishia Sulayman upepo wa kimbunga.”** Maana yake: Tulimsahilishia Sulayman عليه السلام upepo wa dharuba.

تَجْرِي بِأَمْرِهِ إِلَى الْأَرْضِ الَّتِي بَرَكْنَا فِيهَا

**“Wendao kwa amri yake kwenye ardhi Tuliyoibarikia.”** Maana yake: Ardhi ya Shaam<sup>1</sup>.

وَكُنَّا بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمِينَ ﴿٣٧﴾

**“Na Sisi ndio Tunaojua kila kitu”.**

Alikuwa na mkeka uliotengenezwa kwa mbao ambao alikuwa anaweka juu yake vitu vyote vya ufalme wake anavyohitajia; farasi, ngamia, hema na jeshi, kisha alikuwa anauamrisha upepo kumchukua yeye, naye alikuwa akikaa chini yake. Na Ndege walimpatia kivuli na kumlinda na joto, na humpeleka anapotaka kwenda katika ardhi. Kisha hushuka chini na kumuekea vitu vyake na msafara wake. Amesema Allah تعالی;

فَسَخَّرْنَا لَهُ الرِّيحَ تَجْرِي بِأَمْرِهِ رُحَاءً حَيْثُ أَصَابَ ﴿٣٨﴾

**“Basi Tukamtiishia upepo unaokwenda pole pole kwa amri yake, anakotaka kufika.” (38:36).**

Na Amesema Aliyetukuka:

<sup>1</sup> Shaam ni ile inayoitwa Syria Kubwa iliyokuwa inajumlisha pamoja nchi zifuatazo: Palestina, Lebanon, Jordan na Syria.

غُدُوها شَهْرٌ وَرَوَّاحُها شَهْرٌ

**“Safari yake ya asubuhi (mwendo wa) mwezi, na safari yake ya jioni mwezi mmoja.” (34:12)**

Na Kauli Yake:

وَمِنَ الشَّيْطَانِ مَنْ يُغْوِصُونَ لَهُ

**“Na katika mashetani wanaompigia mbizi.”**

Maana yake: kwenye maji kumtolea lulu, vito na vyenginevyo.

وَيَعْمَلُونَ عَمَلًا دُونَ ذَلِكَ

**“Na kufanya kazi nyenginezo”,**

Maana yake: nyenginezo, zisokuwa hizi, kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَالشَّيْطَانِ كُلِّ بَنَاءٍ وَغَوَّاصٍ ﴿٣٧﴾ وَءَاخِرِينَ مُقَرَّنِينَ فِي الْأَصْفَادِ ﴿٣٨﴾

**“Pia na (Tukamtiishia) mashetani, kila ajengaye na azamiaye (lulu). Na wengine wafungwao minyonyoroni.” (38:37-38).**

Na Kauli Yake:

وَكُنَّا لَهُمْ حَافِظِينَ ﴿٣٧﴾

**“Na Sisi Tulikuwa walinzi wao.”**

Maana yake: Allah تعالى Alimlinda na Kumhifadhi asije akadhuriwa na mmoja kati ya mashetani. Wote walikuwa chini ya Udhubiti Wake, Nguvu na Miliki Yake, na hakuna yeyote miongoni mwao aliyejaribu kumkaribia yeye. Bali aliwahukumu wale aliokuwa akitaka kuwahukumu na alimuacha huru au kumfunga yeyote aliyetaka. Allah تعالى Anasema:

وَأَخِرِينَ مُقَرَّنِينَ فِي الْأَصْفَادِ ﴿٣٨﴾

**“Na wengine wafungwao minyonyoroni.” (38:38).**

\* \* \*

\* وَأَيُّوبَ إِذْ نَادَى رَبَّهُ أَنِّي مَسَّنِيَ  
 الضُّرُّ وَأَنْتَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ ﴿٨٣﴾  
 فَاسْتَجَبْنَا لَهُ فَكَشَفْنَا مَا بِهِ مِنْ ضُرِّهِ  
 وَآتَيْنَاهُ أَهْلَهُ وَمِثْلَهُمْ مَعَهُمْ رَحْمَةً  
 مِّنْ عِنْدِنَا وَذَكَرَى  
 لِلْعَبِيدِينَ ﴿٨٤﴾ وَإِسْمَاعِيلَ وَإِدْرِيسَ  
 وَذَا الْكِفْلِ كُلًّا  
 مِّنَ الصَّابِرِينَ ﴿٨٥﴾ وَأَدْخَلْنَاهُمْ فِي رَحْمَتِنَا  
 إِنَّهُمْ مِّنَ الصَّالِحِينَ ﴿٨٦﴾ وَذَا النُّونِ إِذْ ذَهَبَ  
 مُغْضِبًا فَظَنَّ أَنْ لَنْ نَقْدِرَ عَلَيْهِ فَنَادَى  
 فِي الظُّلُمَاتِ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ  
 سُبْحَانَكَ إِنِّي كُنْتُ مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٨٧﴾  
 فَاسْتَجَبْنَا لَهُ وَنَجَّيْنَاهُ مِنَ الْغَمِّ  
 وَكَذَلِكَ نُصَيِّبُ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٨٨﴾  
 وَذَكَرْنَا إِذْ نَادَى رَبَّهُ رَبِّ لَا تَذَرْنِي فَرْدًا  
 وَأَنْتَ خَيْرُ الْوَارِثِينَ ﴿٨٩﴾ فَاسْتَجَبْنَا لَهُ  
 وَوَهَبْنَا لَهُ يَحْيَىٰ وَأَصْلَحْنَا لَهُ زَوْجَهُ  
 إِنَّهُمْ كَانُوا يُسْرِعُونَ فِي  
 الْخَيْرَاتِ وَيَدْعُونَنَا رَغَبًا وَرَهَبًا  
 وَكَانُوا لَنَا خَشِيعِينَ ﴿٩٠﴾ وَالَّتِي أَحْصَانَتْ  
 فَرْجَهَا فَنَفَخْنَا فِيهَا مِنْ رُّوحِنَا  
 وَجَعَلْنَاهَا وَابْنَهَا آيَةً لِّلْعَالَمِينَ ﴿٩١﴾

\* وَأَيُّوبَ إِذْ نَادَى رَبَّهُ أَنِّي مَسَّنِيَ  
 الضُّرُّ وَأَنْتَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ ﴿٨٣﴾  
 فَاسْتَجَبْنَا لَهُ فَكَشَفْنَا مَا بِهِ مِنْ  
 ضُرِّهِ وَآتَيْنَاهُ أَهْلَهُ وَمِثْلَهُمْ مَعَهُمْ  
 رَحْمَةً مِّنْ عِنْدِنَا وَذَكَرَى  
 لِلْعَبِيدِينَ ﴿٨٤﴾

**83. Na Ayyuub, alipomuita Mola wake Mlezi, akasema: Mimi yamenipata madhara. Na Wewe Ndiye Unayerehemu kuliko wote wanaorehemu.**

**84. Basi Tukamuitikia, na Tukamuondolea madhara aliyokuwa nayo, na Tukampa watu wake na mfano wao pamoja nao kuwa ni rehema inayotoka Kwetu, na ukumbusho kwa wafanyao ibada.**

### Nabii Ayyuub عليه السلام

Allah تعالى Anatufahamisha kuhusu Ayyuub عليه السلام, na mitihani iliyomsibu, hivyo kuathiri mali yake, watoto wake na siha ya mwili. Alikuwa na mifugo mingi, na mashamba, watoto wengi na nyumba nzuri, naye alijaribiwa kwa vitu hivi, kumfanya akose kila kitu alichokuwa nacho. Kisha akajaribiwa kuhusiana na mwili wake, akatengwa peke yake, ukingoni mwa mji, na hapo

hakukuwa na yeyote aliyekuwa akimtizama na kumuuguza kwa huruma mbali na mkewe, aliyekuwa akimtizama. Panasemwa kuwa ilifika wakati alipokuwa na mahitajio, hivyo akaanza kuwatumikia watu (kwa ujira).

Kwa sababu yake, Mtume ﷺ amesema:

«أَشَدُّ النَّاسِ بَلَاءَ الْأَنْبِيَاءِ، ثُمَّ الصَّالِحُونَ، ثُمَّ الْأَمْثَلُ فَالْأَمْثَلُ»

*“Watu wenye mitihani, balaa na majaribio makubwa zaidi ni Manabii, kisha watu wema, kisha walio chini yao kwa ubora na walio chini yao”<sup>1</sup>.*

Kulingana na Hadithi nyingine:

«يُنْتَلَى الرَّجُلُ عَلَى قَدْرِ دِينِهِ، فَإِنْ كَانَ فِي دِينِهِ صَلَابَةٌ زِيدَ فِي بَلَاءِهِ»

*“Mtu hujaribiwa kulingana na kiwango cha Dini yake, ikiwa ameshika vilivyo Dini yake, mtihani wake huwa mgumu zaidi”<sup>2</sup>.*

Nabii Ayyuub عليه السلام, alikuwa na subira na uvumilivu wa hali ya juu, na ni kigezo chema katika hilo. Yazid bin Maysarah amesema: “Pindi Allah تعالى Alipomjaribu Ayyub عليه السلام kwa kuondokewa na familia yake, mali na watoto wake, na hakubaki na chochote, alijihimiza katika kumdhukuru Allah تعالى, na akasema, ‘Ninakusifu kwa kila jinsi ya Sifa Njema, Mfalme wa wafalme, Aliyenitunukia huruma na Kunipa mali na watoto, na hakukuwa na pembe yoyote ya moyo wangu ambayo ilikosa hisia ya vitu hivi. Kisha Ulivichukua vyote hivyo, hivyo Kuufanya moyo wangu kuwa mtupu na hakukuwa na chochote chenye kusimama baina yangu na Wewe. Lau adui yangu Iblis atajua hilo, ataona wivu sana’. Pindi Ibilisi aliposikia hilo, alifadhaika, naye Ayyuub عليه السلام akasema: ‘Ewe Mola wangu Mlezi! Ulinipa mali na watoto, wala hakukupatikana yeyote aliyekuja kusimama mlangoni mwangu kulalamika makosa niliyomfanyia. Wewe Unajua hilo. Nilikuwa na kitanda kilichotayarishwa kwa ajili yangu, lakini nilikiacha na kusema ndani ya nafsi yangu: Hakika

<sup>1</sup> Atw-Twabaraniy 24:245, 246.

<sup>2</sup> Ahmad 1:180.

hukuumbwa kulala kwenye kitanda cha raha na starehe. Nilikiacha kwa ajili Yako tu<sup>1</sup>". Hii imenukuliwa na Ibn Abii Haatim رحمه الله تعالى.

Amepokea Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«لَمَّا غَافَى اللهُ أُيُوبَ أَنْطَرَ عَلَيْهِ جَرَادًا مِنْ ذَهَبٍ، فَجَعَلَ يَأْخُذُ مِنْهُ بِيَدَيْهِ وَيَجْعَلُهُ فِي نَزْوِهِ، قَالَ: فَقِيلَ لَهُ: يَا أُيُوبُ أَمَا تَنْسِيْعُ؟ قَالَ: يَا رَبِّ وَمَنْ يَنْسِيْعُ مِنْ رَحْمَتِكَ»

*"Pindi Allah Alipomponya Ayyuub, Alimpelekea mvua ya nzige wa dhahabu, akawa anawachukua kwa mkono wake na kuwatia kwenye nguo yake. Akasema: Akaambiwa: 'Ewe Ayyuub! Je, bado hujashiba (hujatosheka)?' Akasema: 'Ewe Mola wangu Mlezi! Ni nani anayeshiba Rehema Zako?'<sup>2</sup>"*

Msingi wa Hadithi hii imerekodiwa katika Sahihi mbili, kama tutakavyoona chini. Na kauli Yake:

وَأَتَيْنَهُ أَهْلَهُ وَمِثْلَهُمْ مَعَهُمْ

***"Na Tukampa watu wake na mfano wao pamoja nao".***

Imeripotiwa kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: "Alirudishiwa tena vitu vyote"<sup>3</sup>. Hii pia imesimuliwa na Al-'Awfiy kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما<sup>4</sup>. Riwaya sawa na hii imepokewa kutoka kwa Ibn Mas'ud na Mujaahid, na hii ndiyo iliyokuwa rai ya Al-Hasan na Qatadah<sup>5</sup>. Mujaahid amesema: "Aliambiwa: 'Ewe Ayyuub! Watu wako watakuwa nawe Peponi; ukitaka, Tutawarudisha kwako, au ukitaka Tutawaacha kwa ajili yako Peponi na Tutakulipa wengine mfano wao'. Alisema: 'Hapana, niwachieni kwa ajili yangu Peponi'. Hivyo waliachwa kwa ajili yake Peponi, naye akapatiwa wengine mfano wao duniani".

<sup>1</sup> Hilyat Al-Awliyyaa' 5:239.

<sup>2</sup> Ibn Abi Haatim 8: 2461.

<sup>3</sup> Atw-Twabariy 18: 506, 507.

<sup>4</sup> Atw-Twabariy 18: 506, 507.

<sup>5</sup> Atw-Twabariy 18: 506, 507.

رَحْمَةً مِّنْ عِنْدِنَا

**“Kuwa ni Rehema inayotoka Kwetu.”**

Maana yake: Tulifanya hayo kwa Rehema kutoka kwa Allah تعالى.

وَذِكْرَىٰ لِلْعَابِدِينَ ﴿٨٥﴾

**“Na ukumbusho kwa wafanyao ibada.”**

Maana yake: Tulimfanya kuwa kielelezo ili wale wenye kupatikana na mitihani wasidhanie kuwa Tunafanya hayo kwao kwa sababu Hatuwajali.

Kwa ajili hiyo waweze kumchukua kuwa ruwaza njema ya subira na uvumilivu katika kukubali Kudura (*Qadar*) ya Allah تعالى na kuichukua mitihani kwa Anayowajaribu waja Wake kama Anavyopenda na Anavyotaka. Hakika ni kuwa Allah تعالى Ndiye Mwenye Hekima kwa hilo.

وَإِسْمَاعِيلَ وَإِدْرِيسَ وَذَا الْكِفْلِ ۗ كُلٌّ مِّنَ الصَّابِرِينَ ﴿٨٦﴾ وَأَدْخَلْنَاهُمْ فِي رَحْمَتِنَا ۗ  
 إِنَّهُمْ مِّنَ الصَّالِحِينَ ﴿٨٧﴾

**85. Na Ismaail, na Idrisa, na Dhul-Kifl– wote walikuwa miongoni mwa wanaosubiri.**

**86. Na Tukawaingiza katika Rehema Yetu. Hakika wao walikuwa katika watu wema.**

**Ismaail عليه السلام, Idrisa عليه السلام na Dhul-Kifl عليه السلام**

Ismail عليه السلام alikuwa mtoto wa Ibrahim عليه السلام. Tayari ashatajwa katika Sura Maryam, ambamo pia alitajwa Idrisa عليه السلام. Kulingana na muktadha na hakika Dhul-Kifl عليه السلام ametajwa pamoja na Mitume, yaonesha kuwa pia naye alikuwa Mtume. Wengine wanasema kuwa alikuwa ni mtu mwema, mfalme na hakimu mwadilifu. Ibn Jariir رحمه الله تعالى aliacha kutoa tafsiri yoyote ya kukata na ya kuamua<sup>1</sup>. Na Allah تعالى Anajua zaidi.

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:507.



وَدَا أَلْتُونِ إِذْ ذَّهَبَ مُغْنَضِبًا فَظَنَّ أَنْ لَنْ نَقْدِرَ عَلَيْهِ فَنَادَى فِي الظُّلُمَاتِ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ سُبْحَانَكَ إِنِّي كُنْتُ مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٨٧﴾ فَاسْتَجَبْنَا لَهُ وَخَيَّرْنَاهُ مِنَ النَّعْمِ  
وَكَذَلِكَ نُوحِي الْمُؤْمِنِينَ ﴿٨٨﴾

**87. Na Dhun-Nuun alipoondoka hali ameghadhibika, na akadhani ya kwamba hatutakuwa na Uweza juu yake. Basi aliita katika giza: Hapana mungu isipokuwa Wewe Subhanaka, Uliyetakasika. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu.**

**88. Basi Tukamuitikia na Tukamuokoa kutokana na dhiki. Na hivyo ndivyo Tunavyowaokoa Waumini.**

### Yunus عليه السلام

Kisa hiki ambacho kimetajwa hapa na pia katika Sura Asw-Swifaat na katika Suratu Nuun (Al-Qalam – 68). Yunus bin Matta عليه السلام alitumwa na Allah تعالى kwa watu wa kijiji cha Ninawa (Nineveh), nacho ni kijiji ambacho kipo Mosul (Iraq kaskazini). Aliwaita katika njia ya Allah تعالى, lakini walimkataa na kuendelea na ukafiri wao. Hivyo, aliwaacha watu wake kwa hasira, na kuwatisha kwa adhabu baada ya siku tatu. Walipohakikisha hilo kuwa anasema ukweli na kuwa Nabii hasemi uongo, walikwenda jangwani pamoja na watoto wao, ng'ombe na kundi la kondoo pamoja na mbuzi. Waliwatenga mama na watoto wao, baadaye wakamuomba kwa unyenyekevu Allah تعالى na wakakiri Kwake, ilhali ngamia na watoto wao wakiguna, ng'ombe na watoto wao wakilia, na kondoo na watoto wao wakilia, hivyo Allah تعالى Akanyanyua kutoka kwao adhabu. Amesema Allah تعالى:

فَلَوْلَا كَانَتْ قَرْيَةً ءَامَنَتْ فَنفَعَهَا إِيمَانُهَا إِلَّا قَوْمَ يُونُسَ لَمَّا ءَامَنُوا كَشَفْنَا عَنْهُمْ عَذَابَ  
الْخِزْيِ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَمَتَّعْنَاهُمْ إِلَىٰ حِينٍ ﴿١٠٩﴾

***“Kwa nini usiweko mji ulioamini, ili Imani yake iwafae? Isipokuwa watu wa Yunus, walipoamini Tuliwaondolea adhabu ya hizaya katika maisha ya dunia na Tukawasterehesha kwa muda (Tulioutaka).” (10:98).***

Na ama Yunus عليه السلام, alikwenda na kupanda safina pamoja na watu, nayo ikasukwasukwa baharini. Watu waliogopa kuwa watazama, hivyo wakapiga kura kumchagua mtu watakaye mtupa baharini. Kura hiyo ikamshukia Yunus عليه السلام, lakini walikataa kumtupa baharini. Hili lililotokea mara ya pili na ya tatu. Amesema Allah تعالى:

فَسَاهَمَ فَكَانَ مِنَ الْمُدْحَضِينَ ﴿١٤١﴾

***“Na wakapiga kura, basi akawa miongoni mwa walioshindwa.” (37:141),***

Maana: Kura ilikwenda dhidi yake, hivyo Yunus عليه السلام alisimama, akatoa nguo zake na kujitupa baharini. Na alivyosema Ibn Mas’ud رضي الله عنه Kisha Allah تعالى Akapeleka kutoka Bahari ya Kijani, kulingana na Nyangumi mwenye kukata bahari mpaka akaja na kummeza Yunus عليه السلام pindi alipojitupa baharini. Allah تعالى Alimfunulia nyangumi asile nyama wala kuivunja mifupa yake, (kama kwamba Amesema) Yunus عليه السلام si chakula kwako, bali tumbo lako ni jela kwake. Na Kauli Yake:

وَدَا النُّونِ

***“Na Dhun-Nuun.”*** Maana yake: Hapa inamaanisha swahiba wa Nyangumi, na ni sawa kuitwa hivyo kwa ajili ya kuchunga mnasaba wa tukio lenyewe.

إِذْ ذُهِبَ مُغْضِبًا

***“Alipoondoka hali ameghadhibika”.***

Ad-Dhahaak amesema: “Kuwakasirikia watu wake”<sup>1</sup>.

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:511.

فَطَّنْ أَنْ لَنْ نَقْدِرَ عَلَيْهِ

**“Na akadhani ya kwamba Hatutakuwa na Uweza juu yake.”**

Maana yake: Kumdhiki na kumbana ndani ya tumbo la nyangumi. Imepokewa mfano wa hii kutoka kwa Ibn ‘Abbaas, Mujaahid, Dhahaak na wengineo<sup>2</sup>. Hii ndiyo rai iliyochaguliwa na Ibnu Jariir رحمه الله تعالى, na akatoa ushahidi wa Kauli Yake Aliyetukuka kwa hilo:

وَمَنْ قَدِرَ عَلَيْهِ رِزْقُهُ فَلْيُنْفِقْ مِمَّا آتَاهُ اللَّهُ لَا يُكَلِّفُ اللَّهُ نَفْسًا إِلَّا مَا آتَاهَا سَيَجْعَلُ

اللَّهُ بَعْدَ عَشْرٍ يُسْرًا ﴿٦٥﴾

**“Na yule ambaye amepungukiwa riziki yake, atoe katika kile alichopewa na Allah; Allah Hamkalifishi mtu yeyote ila kwa kadiri ya alichompa. Atajaalia Allah baada ya dhiki faraji.” (65:7).**

Na Kauli Yake:

فَنَادَى فِي الظُّلُمَاتِ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ سُبْحَانَكَ إِنِّي كُنْتُ مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٦٧﴾

**“Basi aliita katika giza: Hapana mungu isipokuwa Wewe Subhanaka, Uliyetakasika. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu”.**

Amesema Ibn Mas’ud رضي الله عنه: “Giza la tumbo la nyangumi, giza la bahari na giza la usiku”<sup>3</sup>. Na hivyo ndivyo ilivyopokewa kutoka kwa Ibn ‘Abbaas, ‘Amr bin Maymuun, Sa’id bin Jubayr, Muhammad bin Ka’b, Ad-Dhahaak, Al-Hasan na Qataadah<sup>4</sup>. Salim bin Abu Al-Ja’d amesema: “Giza la nyangumi ndani ya tumbo la samaki mwingine katika giza la bahari”<sup>5</sup>. Ibn Mas’ud, Ibn ‘Abbaas na wengineo رضي الله عنهم wamesema: “Hii ni kwa sababu nyangumi alimchukua kwenye bahari, akiipasua mpaka akafika chini kabisa ya hiyo bahari. Yunus عليه السلام akasikia mawe chini ya bahari yakimdhukuru Allah تعالى na Kumtakasa. Kwa kusikia hayo na hapo akasema:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:514, 515.

<sup>2</sup> Al-Qurtwubiy 11:333.

<sup>3</sup> Atw-Twabariy 18:516, 517.

<sup>4</sup> Atw-Twabariy 18:517.

لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ سُبْحَانَكَ إِنِّي كُنْتُ مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٨٧﴾

**'Hapana mungu isipokuwa Wewe Subhanaka, Uliyetakasika.  
Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu'<sup>1</sup>.**

Na amesema Awf Al-A'raby: "Yunus عليه السلام alipojikuta ndani ya tumbo la nyangumi, alidhania kuwa ameaga dunia. Kisha alisogeza miguu yake. Alipoitingisha miguu yake, alisujudu pale alipokuwa, kisha akaita: 'Ewe Mola wangu Mlezi! Nimechukua kwa sababu Yako Msikiti (sehemu ya kusujudu) katika sehemu ambayo hakuna yeyote aliyefika'<sup>2</sup>". Na Kauli Yake:

فَاسْتَجَبْنَا لَهُ وَخَيَّرْنَاهُ مِنَ الْغَمْرِ

**"Basi Tukamuitikia na Tukamuokoa kutokana na dhiki."**

Maana yake: Tulimtoa katika tumbo la nyangumi na giza hilo.

وَكَذَلِكَ نُجِي الْمُؤْمِنِينَ ﴿٨٨﴾

**"Na hivyo ndivyo Tunavyowaokoa Waumini."**

Maana yake: Wakiwa katika shida na wakatuomba Sisi na kutubia Kwetu, hasa wakituomba kwa maneno haya (kwa du'aa hii) katika hali hiyo ya balaa na dhiki. Mtume ﷺ amehimiza sana kumuomba Allah تعالى kwa maneno haya. Amepokea Imamu Ahmad kutoka kwa Sad bin Abi Waqqaasw رضي الله عنه amesema: "Nilimpitia 'Uthmaan bin 'Affaan رضي الله عنه Msikitini, nikamsalimia. Alinitizama lakini hakurudisha salamu yangu. Nikaenda kwa 'Umar bin Al-Khatwaab رضي الله عنه, nikamuambia: 'Ewe Amiri wa Waumini! Je, kumetokea lolote katika Uislamu?' Nikasema hilo mara mbili. Akasema: 'Hapana, kwa nini unauliza?' Nikasema: 'Hapana, ila nilimpitia Uthman رضي الله عنه kitambo kidogo Msikitini na kumsalimia, naye alinitizama lakini hakurudisha salamu'. 'Umar رضي الله عنه alituma aitwe 'Uthmaan رضي الله عنه na kumuuliza: 'Kwa nini hukurudisha salamu za nduguyo?' Akasema: 'Sikufanya hilo'. Sa'd رضي الله عنه akasema: 'Nikamuambia: Ndio, umefanya'. Ikafika hadi akaapa, nami nikaapa. Kisha 'Uthman رضي الله عنه akakumbuka na kusema: 'Ndio, umesema kweli, naomba msamaha kutoka kwa Allah تعالى na ninarudi (ninatubia) Kwake. Kweli

<sup>1</sup> Ibn Abi Shaybah 11:541 na 13: 578.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18: 518.

ulinipitia hivi punde ilhali nimeshughulika sana na fikira ya jambo nililosikia kutoka kwa Mtume ﷺ, ambalo silifikirii ila macho yangu na moyo wangu hufinikwa'. Sa'd رضي الله عنه akasema: 'Nami nitakuambia jambo lenyewe. Mtume ﷺ alituambia sehemu ya kwanza ya dua, kisha Mbedui mmoja alikuja na kumshughulisha. Baada ya hapo Mtume ﷺ alinyanyuka, nami nikamfuata. Nilipohofu kuwa ataingia nyumbani mwake, nilipiga miguu yangu chini. Mtume ﷺ aligeuka na kunitizama, akasema:

«مَنْ هَذَا، أَبُو إِسْحَاقَ؟»

'Ni nani huyu, Abu Is'haaq?'

Nikasema: 'Ndio, Mtume ﷺ'. Akasema:

«فَمَنْ؟»

'Una nini?'

Nikasema: 'Hakuna lolote, ila ulituambia kipande cha kwanza cha dua, kisha Mbedui aliyekuja alikushughulisha'. Akasema:

«نَعَمْ دَعْوَةٌ ذِي الثُّورِ إِذْ هُوَ فِي بَطْنِ الْحَوْبِ»

'Ndio, dua ya Dhin Nuun alipokuwa ndani ya tumbo la nyangumi:

لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ سُبْحَانَكَ إِنِّي كُنْتُ مِنَ الظَّالِمِينَ ﴿٢١﴾

**'Hapana mungu isipokuwa Wewe Subhanaka, Uliyetakasika. Hakika mimi nilikuwa miongoni mwa wenye kudhulumu.'**

فَإِنَّهُ لَمْ يَدْعُ بِهَا مُسْلِمٌ رَبَّهُ فِي شَيْءٍ فَطُرُقًا إِلَّا اسْتَجَابَ لَهُ»

*'Kwa hakika hakuna Muislamu anayemuomba Mola wake Mlezi chochote au lolote kwa kusoma dua hiyo isipokuwa anajibiwa<sup>1</sup>'*

Na pia imepokewa na At-Tirmidhiy na An-Nasaa'iy katika kitabu chake *Al-Yawm Wal Laylah*<sup>2</sup>. Na amepokea Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى kutoka kwa Sa'd رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

<sup>1</sup> Ahmad 1:170.

<sup>2</sup> Tuhfat ul-Ahwadhiy 9:479 na an-Nasaa'iy katika Al-Kubraa 6:168.

«مَنْ دَعَا بِدُعَاءِ يُونُسَ اشْتَجِبَ لَهُ»

“Yeyote mwenye kuomba kwa dua ya Yunus, atajibiwa”.

Akasema Abi Said: Akimaanisha:

وَكَذَلِكَ نُشِجِي الْمُؤْمِنِينَ ﴿٨٨﴾

**‘Na hivyo ndivyo Tunavyowaokoa Waumini!’**

وَزَكَرِيَّا إِذْ نَادَى رَبَّهُ رَبِّ لَا تَذَرْنِي فَرْدًا وَأَنْتَ خَيْرُ الْوَارِثِينَ ﴿٨٩﴾ فَاسْتَجَبْنَا لَهُ  
وَوَهَبْنَا لَهُ إِسْحَاقَ وَيَعْقُوبَ وَأَصْلَحْنَا لَهُ زَوْجَهُ إِنَّهُمْ كَانُوا يُسْرِعُونَ فِي الْخَيْرَاتِ  
وَيَدْعُونََنَا رَغَبًا وَرَهَبًا ۗ وَكَانُوا لَنَا خَشِيعِينَ ﴿٩٠﴾

**89. Na Zakariyya alipomuita Mola wake Mlezi: Mola wangu Mlezi!  
Usiniache peke yangu, na Wewe Ndiye Mbora wa wanaorithi.**

**90. Basi Tukamuitikia, na Tukampa Yahya na Tukamponyeshea  
mkewe. Hakika wao walikuwa wepesi wa kutenda mema, na  
wakituomba kwa shauku na khofu. Nao walikuwa wakitunyeyeka.**

Zakariyya عليه السلام na Yahya عليه السلام

Allah تعالى Anatupasha habari ya mja Wake, Zakariyya عليه السلام, aliyemuomba Allah تعالى Ampe kijana atakayekuwa Nabii baada yake. Na hakika tumetangulia kukieleza kisa kwa kina katika mwanzo wa Suratul Maryam na pia katika Suratul ‘Imraan. Na hapa simulizi yake imefupishwa.

إِذْ نَادَى رَبَّهُ

**“Alipomuita Mola wake Mlezi.”**

Maana yake: Kwa siri, kuificha kutoka kwa watu wake.

<sup>1</sup> Al-Haakim 2:584.

رَبِّ لَا تَذَرْنِي فَرْدًا

**“Mola wangu Mlezi! Usiniache peke yangu.”**

Maana yake: Bila ya kuwa na kijana wala mrithi atakayesimama baada yangu kati ya watu.

وَأَنْتَ خَيْرُ الْوَارِثِينَ ﴿٨٤﴾

**“Na Wewe ndiye Mbora wa wanaorithi.”**

Hii ni dua na mfumo wa sifa iliyonasibiana sawa sawa na suala lenyewe. Amesema Allah Aliyetukuka:

فَأَسْتَجِبْنَا لَهُ وَوَهَبْنَا لَهُ يَحْيَىٰ وَأَصْلَحْنَا لَهُ زَوْجَهُ

**“Basi Tukamuitikia, na Tukampa Yahya na Tukamponyeshea mkewe.”**

Maana yake: mkewe. Amesema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما, Mujahid na Sa’id bin Jubayr: “Alikuwa tasa, asiyezaa, kisha akazaa”<sup>1</sup>. Na Kauli Yake:

إِنَّهُمْ كَانُوا يُسْـَٔرُونَ فِي الْأَخْيَرَاتِ

**“Hakika wao walikuwa wepesi wa kutenda mema.”**

Maana yake: katika kufanya matendo ya kujikurubisha kwa Allah تعالى na kuwa mtiifu.

وَيَدْعُونَنَا رَغَبًا وَرَهَبًا ط

**“Na wakituomba kwa shauku na khofu”.**

Amesema Thawriy رحمه الله تعالى: “Kwa shauku ya kutarajia (thawabu) kwa Tuliyonayo na khofu kwa (adhabu) iliyo Kwetu”<sup>2</sup>.

وَكَاُنُوا لَنَا خٰشِعِينَ ﴿٨٥﴾

**“Nao walikuwa wakitunyeyekea”.**

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:520.

<sup>2</sup> Tafsir Ath-Thawriy 204.

Amepokea 'Aliy bin Abi Twalhah kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: "Hii inamaanisha kusadiki kwa Aliyoteremsha Allah تعالى<sup>1</sup>."

Na amesema Mujaahid: "Waumini wa kweli"<sup>2</sup>.

Na amesema Abu Al-Aliya: "Wakiwa na khofu"<sup>3</sup>.

Na amesema Abu Sinaan: "*Al-Khushu'* ni khofu ya lazima ambayo haitakiwi itoke nyoyoni mwetu kabisa".

Na pia kutoka kwa Mujaahid: "*Khaashi'iyn*", Maana: kunyenyekea. Na amesema Al-Hasan, Qatadah na Adh-Dhahaak: "*Khaashi'iyn*", Maana yake: wale wenye kujidhalilisha kwa Allah تعالى<sup>4</sup>. Na kauli zote hizi zinakaribiana.

وَأَلَّتِي أَحْصَنَتْ فَرْجَهَا فَنَفَخْنَا فِيهَا مِنْ رُوحِنَا وَجَعَلْنَاهَا وَابْنَهَا آيَةً لِلْعَالَمِينَ ﴿٩١﴾

**91. Na mwanamke aliyelinda uke wake, na Tukampulizia katika roho Yetu, na Tukamfanya yeye na mwanawe kuwa ni Ishara kwa walimwengu.**

### Kutajwa kwa Isa عليه السلام na Maryam, Aliye mkweli

Hivi ndivyo Aliyetukuka Anavyotaja kisa cha Maryam na mtoto wake, Isa عليه السلام baada tu ya Kutaja kisa cha Zakariyya عليه السلام na mtoto wake Yahya عليه السلام. Ametaja kisa cha Zakariyya عليه السلام mwanzo, kikifuatiwa na kile cha Maryam kwa sababu kimoja kimefungamana na chengine. Kisa cha mwanzo ni cha mtoto aliyezaliwa na mwanamume mkongwe aliyekula chumvi nyingi kutokana na mwanamke ajuza, aliyekuwa tasa, bila kupata mtoto alipokuwa msichana mdogo. Kisha Allah تعالى Akataja kisa cha Maryam ambacho ni cha ajabu zaidi, kwani katika kesi hii mtoto anazaliwa kutoka kwa mwanamke bila kupitia kwa mwanamme. Visa hivi pia vimetajwa katika Sura ya Imraan na Sura ya Maryam. Hapa Allah تعالى Anataja kisa cha Zakariyya عليه السلام na Kukifuatisha na kisa cha Maryam, Aliposema:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 2:16.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 2:16.

<sup>3</sup> Atw-Twabariy 2:16.

<sup>4</sup> Al-Kashshaaf 3:133, Al-Baghawiy 3:267 na Ibn Abi Shaybah 13:580.



وَأَلَّتْ أَحْصَنَتْ فَرْجَهَا

**“Na mwanamke aliyelinda uke wake.”**

Maana yake: Maryam. Hii ni kama ile Aya iliyoko katika Sura ya At-Tahrim (66:12):

وَمَرْيَمَ ابْنَتَ عِمْرَانَ الَّتِي أَحْصَنَتْ فَرْجَهَا فَنفَخْنَا فِيهِ مِنْ رُوحِنَا

**“Na Maryam mtoto wa ‘Imraan aliyejihifadhi nafsi yake na Tukampulizia humo roho Yetu...” (66:12).**

Na Kauli Yake:

وَجَعَلْنَاهَا وَأَبْنَاهَا آيَةً لِلْعَالَمِينَ ﴿٥١﴾

**“Na Tukamfanya yeye na mwanawe kuwa ni Ishara kwa walimwengu.”**

Maana yake: Dalili kuwa Allah تعالی ni Muweza wa Kufanya kila kitu, na kuwa Yeye Anaumba Atakacho. Na,

إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَنْ يَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٨٢﴾

**“Hakika Amri Yake Anapotaka kitu chochote ni kukiambia: ‘Kuwa’, basi mara huwa.” (36:82)**

Na hii ni kama Kauli Yake:

وَلِنَجْعَلَهُ آيَةً لِلنَّاسِ

**“Na ili Tumfanye Muujiza kwa wanadamu...” (19:21).**

\* \* \*

إِنَّ هَذِهِ أُمَّتُكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَأَنَا رَبُّكُمْ فَاعْبُدُونِ  
 ٩٢ وَتَقَطُّعُوا أَمْرَهُمْ بَيْنَهُمْ ۗ كُلٌّ إِلَيْنَا رَاجِعُونَ ﴿٩٣﴾  
 فَمَنْ يَعْمَلْ مِنَ الصَّالِحَاتِ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَا كُفْرَانَ  
 لِسَعْيِهِ وَإِنَّا لَهُ كَاتِبُونَ ﴿٩٤﴾ وَحَرَامٌ عَلَى قَرِيْبَةٍ  
 أَهْلَكْنَاهَا أَنَّهُمْ لَا يَرْجِعُونَ ﴿٩٥﴾ حَتَّىٰ إِذَا فُتِحَتْ  
 يَا جُوجُ وَمَأْجُوجُ وَهُمْ مِنْ كُلِّ حَدَبٍ يَنْسِلُونَ ﴿٩٦﴾  
 وَأَقْتَرَبَ الْوَعْدُ الْحَقُّ فَإِذَا هِيَ شِدْخُصَةٌ أَبْصَرُ الَّذِينَ  
 كَفَرُوا يُبَوِّئُنَا قَدْ كُنَّا فِي غَفْلَةٍ مِّنْ هَذَا بَلْ كُنَّا  
 ظَالِمِينَ ﴿٩٧﴾ إِنَّكُمْ وَمَا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ  
 حَصْبُ جَهَنَّمَ أَنتُمْ لَهَا وَرِدُونَ ﴿٩٨﴾ لَوْ كَانَتْ  
 هُنَّ لَاءِءَ آلهَةٍ مَا وَرَدُوها ۗ وَكُلٌّ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٩٩﴾ لَهُمْ  
 فِيهَا زَفِيرٌ وَهُمْ فِيهَا لَا يَسْمَعُونَ ﴿١٠٠﴾ إِنَّ الَّذِينَ  
 سَبَقَتْ لَهُمْ مِنَّا الْحُسْنَىٰ أُولَٰئِكَ عَنْهَا مُبْعَدُونَ ﴿١٠١﴾ لَا  
 يَسْمَعُونَ حَسِيسَهَا ۗ وَهُمْ فِي مَا اشْتَهَتْ أَنفُسُهُمْ  
 خَالِدُونَ ﴿١٠٢﴾ لَا يَحْزَنُهُمُ الْفَرَعُ الْأَكْبَرُ وَتَتَلَقَّيْهُمْ  
 الْمَلَائِكَةُ هَذَا يَوْمُكُمْ الَّذِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ ﴿١٠٣﴾

إِنَّ هَذِهِ أُمَّتُكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَأَنَا  
 رَبُّكُمْ فَاعْبُدُونِ ﴿٩٢﴾ وَتَقَطُّعُوا  
 أَمْرَهُمْ بَيْنَهُمْ ۗ كُلٌّ إِلَيْنَا  
 رَاجِعُونَ ﴿٩٣﴾ فَمَنْ يَعْمَلْ مِنَ  
 الصَّالِحَاتِ وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَا كُفْرَانَ  
 لِسَعْيِهِ وَإِنَّا لَهُ كَاتِبُونَ ﴿٩٤﴾

92. Kwa hakika huu umma  
 wenu ni umma mmoja, na  
 Mimi ni Mola wenu Mlezi.  
 Kwa hivyo niabuduni Mimi.

93. Nao wakalikata jambo  
 lao hili mapande mapande  
 baina yao. Wote watarudi  
 Kwetu.

94. Na atendaye mema  
 naye ni Muumini basi haita-  
 kataliwa juhudi yake. Na  
 hakika Sisi Tunamuandikia.

Wanadamu ni Umma  
 mmoja

Kuhusu Kauli Yake:

إِنَّ هَذِهِ أُمَّتُكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً

“Kwa hakika huu umma wenu ni umma mmoja...”

Wamesema Ibn ‘Abbaas, Mujahid, Sa’id bin Jubayr na ‘Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam yafuatayo: “Dini yenu ni Dini moja”. Na amesema al-Hasan al-

Baswriy الله تعالى kuhusu Aya hii: “Anawabainishia wanayotakiwa kuyaacha na kuyafanya, kisha akasema:

إِنَّ هَذِهِ أُمَّتُكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً

***‘Kwa hakika huu umma wenu ni umma mmoja’***

Maana yake: Mwenendo wenu ni mmoja. Na Ibara ya ***“Kwa hakika huu”*** katika sarufi ya kiarabu ni nomino. Na, ***“Ummah wenu”*** ni kiarifu, yaani shari’ah yenu hii iliyowabainishia na kuwawekea wazi, ***“Ni ummah mmoja.”***

Na hivyo Akasema:

وَأَنَا رَبُّكُمْ فَاعْبُدُونِ

***“Na Mimi ni Mola wenu Mlezi. Kwa hivyo niabuduni Mimi.”***

Hii ni kama Alivyosema:

يَتَأْتِيهَا الرُّسُلُ كُلُّوَا مِنَ الطَّيِّبَاتِ وَاعْمَلُوا صَالِحًا

***“Enyi Mitume! Kuleni vyakula vizuri na fanyeni mema.”*** Mpaka

وَأَنَا رَبُّكُمْ فَاتَّقُونِ

***“Na Mimi ni Mola wenu Mlezi, basi Niogopeni.”*** (23:51-52).

NaMtume ﷺ amesema :

«نَحْنُ مَعَاشِرَ الْأَنْبِيَاءِ أَوْلَادُ عِلَاتٍ دِينَنَا وَاجِدُ»

***“Sisi kongamano la Manabii ni ndugu kutoka kwa mama tofauti, na Dini yetu ni moja”***<sup>1</sup>.

Hii ina maana kuwa makusudio makubwa ni kumuabudu Allah تعالى Peke Yake asiye na mshirika, japokuwa sheria ya kila Mtume ﷺ ilikuwa tofauti, kama Anavyosema Allah تعالى:

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Baariy 6:550.

لِكُلِّ جَعَلْنَا مِنْكُمْ شِرْعَةً وَمِنْهَا جَاءَ

**“...Na kila (umma) katika nyinyi Tumeujaalia sheria na njia yake...”  
(5:48).**

Na Kauli Yake:

وَتَقَطُّعُوا أَمْرَهُمْ بَيْنَهُمْ

**“Nao wakalikata jambo lao hili mapande mapande baina yao.”**

Maana yake: Umma zilitofautiana kwa Mitume yao; baadhi yao waliwaamini na wengine kuwakataa. Na kwa hiyo Akasema:

كُلُّ إِلَيْنَا رَاجِعُونَ ﴿٢١﴾

**“Wote watarudi Kwetu.”**

Maana yake: Siku ya Kiyama, na kulipwa kila mmoja kulingana na amali yake. Ikiwa ni nzuri, basi itakuwa kheri kwake na ikiwa ni shari basi itakuwa ni shari kwake (hivyo kupata adhabu). Kwa hiyo Akasema:

فَمَنْ يَعْمَلْ مِثْرَ الْفَلَّاحِ وَالصَّالِحِ وَهُوَ مُؤْمِنٌ

**“Na atendaye mema naye ni Muumini.”**

Maana yake: Akiwa anaamini moyoni na kutenda amali njema.

فَلَا كُفْرَانَ لِسَعْيِهِ

**“Basi haitakataliwa juhudi yake.”**

Hii ni kama Kauli Yake:

إِنَّا لَا نُضِيعُ أَجْرَ مَنْ أَحْسَنَ عَمَلًا ﴿٢٢﴾

**“Hakika Sisi hatupotezi ujira wa wale wanaofanya vitendo vizuri.” (18:30)**

Maana yake: Juhudi zake hazitaruka patupu; nazo ni amali zao bali watashukuru na wala hawatadhulumiwa uzani wa atomu (chembe ndogo kabisa). Na kwa hiyo Akasema:

وَأِنَّا لَهُ كَنُتُوبٌ ﴿٩٤﴾

**“Na hakika Sisi Tunamuandikia.”**

Maana yake: Anaandika amali zake zote wala hakitapotea kitu chochote.

وَحَرَامٌ عَلَىٰ قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَاهَا أَنَّهُمْ لَا يَرْجِعُونَ ﴿٩٥﴾ حَتَّىٰ إِذَا فُتِحَتْ يَأْجُوجُ وَمَأْجُوجُ  
وَهُمْ مِّنْ كُلِّ حَدَبٍ يَنْسِلُونَ ﴿٩٦﴾ وَأَقْتَرَبَ الْوَعْدُ الْحَقُّ إِذَا هِيَ شَاخِصَةٌ أَبْصَرُ  
الَّذِينَ كَفَرُوا يَتَوَيَّلُنَا قَدْ كُنَّا فِي غَفْلَةٍ مِّنْ هَذَا بَلْ كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿٩٧﴾

**95. Na haiwi kwa wana-mji Tuliouangamiza, ya kwamba hawatarejea,**

**96. Mpaka watapofunguliwa Maa’juuju na Maa’juuju, wakawa wanateremka kutoka kila mlima;**

**97. Na miadi ya haki ikakaribia. Hapo ndipo yatapokodoka macho ya waliokufuru (na watasema:) Ole wetu! Bila ya shaka tulikuwa tumeghafilika na haya, bali tulikuwa wenye kudhulumu.**

**Wale Walioangamizwa Hawatarudi Duniani**

Anasema Aliyetukuka:

وَحَرَامٌ عَلَىٰ قَرْيَةٍ

**“Na haiwi kwa wana-mji”.**

Amesema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما: “Imewajibika, Maana: Imekadiriwa kuwa watu wa kila mji ulioangamizwa hawatarudi tena duniani kabla ya Siku ya Kiyama”. Hivyo ndivyo alivyoeleza kwa uwazi kabisa Ibn ‘Abbaas, Abu Ja’far Al-Baaqir, Qatadah na wengineo<sup>1</sup>.

<sup>1</sup> Al-Baghawiy 3:267; Atw-Twabariy 18:525; na Ar-Raaziy 22:191.

## Yaa'Juuju na Maa'Juuju

Na Kauli Yake:

حَتَّىٰ ۚ إِذَا فُتِحَتْ يَأْجُوجُ وَمَأْجُوجُ

**“Mpaka watapofunguliwa Ya'juuju na Maa'juuju,”**

Hakika tumetangulia kueleza kuwa hawa ni katika kizazi cha Adam عليه السلام; pia wao ni kizazi cha Nuuh عليه السلام kupitia kwa mtoto wake Yaafith (Japheth), ambaye ni baba wa Waturuki. Na Waturuki kinahusisha kile kikundi kilichoachwa nyuma ya kizuizi (ukuta) uliojengwa na Dhul-Qarnayn. Na Akasema:

• هَذَا رَحْمَةٌ مِّن رَّبِّي ۖ فَإِذَا جَاءَ وَعْدُ رَبِّي جَعَلَهُ دَكَّاءَ ۗ وَكَانَ وَعْدُ رَبِّي حَقًّا ﴿٩٧﴾  
وَتَرَكْنَا بَعْضَهُمْ يَوْمَئِذٍ يَمُوجُ فِي بَعْضٍ ۗ

**“Akasema: Hii ni rehema itokayo kwa Mola wangu Mlezi. Na itapofika ahadi ya Mola wangu Mlezi Atauvunja vunja. Na ahadi ya Mola wangu Mlezi ni kweli tu. Na siku hiyo tutawaacha wakizongana wao kwa wao.” (18:98-99).**

Na Akasema katika Aya hii Tukufu:

حَتَّىٰ ۚ إِذَا فُتِحَتْ يَأْجُوجُ وَمَأْجُوجُ وَهُمْ مِّن كُلِّ حَدَبٍ يَنْسِلُونَ ﴿٩٦﴾

**“Mpaka watapofunguliwa Ya'juuju na Maa'juuju, wakawa wanateremka kutoka kila mlima.” (21:96)**

Maana yake: Watakwenda haraka haraka ili kueneza ufisadi. *Hadab* ni sehemu ya ardhi yenye mwinuko. Hii ndio rai ya Ibn 'Abbaas, 'Ikrimah, Abu Swaalih, Ath-Thawriy na wengineo<sup>1</sup>. Na hii ndiyo sifa yao katika hali ya kutoka kwao, kama kwamba msikilizaji anashuhudia hilo:

وَلَا يُنَبِّئُكَ مِثْلُ خَبِيرٍ ﴿١٤﴾

**“Wala hatakuambia kama Yule Aliye Mjuzi wa kweli kweli.” (35:14)**

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:532.

Hii ni habari inayotolewa na Mjuzi Anayejua yaliyotokea na yanayokuja baadaye, ambaye Anajua ya ghaibu mbinguni na ardhini. Hapana apasaye kuabudiwa ila Yeye. Na amepokea Ibn Jariir رحمه الله تعالى kutoka kwa 'Ubaydullaah bin Abi Yazid kuwa amesema: "Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما aliwaona vijana wakicheza na kupigana wao kwa wao, akasema, hivi ndivyo *Ya'juuju na Maa'juuju*, watakavyotokea"<sup>1</sup>. Hakika kumetajwa kutokea kwao katika Hadithi nyingi za Mtume ﷺ.

### Hadithi ya Kwanza

Amepokea Imaam Ahmad kutoka kwa Abi Sa'id Al-Khudriy رضي الله عنه kuwa amemsikia Mtume ﷺ amesema:

«تَفْتَحُ يَأْجُوجَ وَمَأْجُوجَ، فَيَخْرُجُونَ عَلَى النَّاسِ، كَمَا قَالَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ: ﴿وَهُمْ مِنْ كُلِّ حَدَبٍ يَنْسِلُونَ﴾ فَيَغْشَوْنَ النَّاسَ وَيَنْحَارُ الْمُسْلِمُونَ عَنْهُمْ إِلَى مَدَائِنِهِمْ وَحُصُونِهِمْ، وَيَضُمُونَ إِلَيْهِمْ مَوَائِبَهُمْ، وَيَسْرَبُونَ مِيَاةَ الْأَرْضِ، حَتَّى إِنَّ بَعْضَهُمْ لَيَمُرُّ بِالنَّهْرِ فَيَسْرَبُونَ مَا فِيهِ حَتَّى يَتْرَكُوهُ يَابِسًا، حَتَّى إِنَّ مَنْ بَعْدَهُمْ لَيَمُرُّ بِذَلِكَ النَّهْرِ فَيَقُولُ: قَدْ كَانَ هَهُنَا مَاءٌ مَرَّةً، حَتَّى إِذَا لَمْ يَثِقْ مِنَ النَّاسِ أَحَدٌ إِلَّا أَحَدٌ فِي حِصْنٍ أَوْ مَدِينَةٍ، قَالَ قَائِلُهُمْ: هَؤُلَاءِ أَهْلُ الْأَرْضِ قَدْ فَرَعْنَا مِنْهُمْ بَقِيَّ أَهْلِ السَّمَاءِ، قَالَ: ثُمَّ يَهْرُؤُ أَحَدُهُمْ حَرْبَتَهُ، ثُمَّ يَرْمِي بِهَا إِلَى السَّمَاءِ فَتَرْجِعُ إِلَيْهِ مُخْضَبَةً دَمَا لِلْبَلَاءِ وَالْفِتْنَةِ، فَيَبْتِنَا هُمْ عَلَى ذَلِكَ، بَعَثَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ دُودًا فِي أَعْنَاقِهِمْ كَتَغَابِ الْجِرَادِ الَّذِي يَخْرُجُ فِي أَعْنَاقِهِ، فَيَضْحَبُونَ مَوْتَى لَا يَسْمَعُ لَهُمْ حِسٌّ، فَيَقُولُ الْمُسْلِمُونَ: أَلَا رَجُلٌ يَشْرِي لَنَا نَفْسَهُ فَيَنْظُرَ مَا فَعَلَ هَذَا الْعَدُوُّ؟ قَالَ: فَيَتَجَرَّدُ رَجُلٌ مِنْهُمْ مُحْتَسِبًا نَفْسَهُ، قَدْ أَوْطَنَهَا عَلَى أَنَّهُ مَقْتُولٌ، فَيَنْزِلُ فَيَجِدُهُمْ مَوْتَى، بَعْضُهُمْ عَلَى بَعْضٍ، فَيُنَادِي: يَا مَعْشَرَ الْمُسْلِمِينَ، أَلَا أُبَشِّرُوكُمْ أَنَّ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ قَدْ كَفَاكُمْ عَدُوَّكُمْ، فَيَخْرُجُونَ مِنْ مَدَائِنِهِمْ وَحُصُونِهِمْ، وَيُسْرَبُونَ مَوَائِبَهُمْ، فَمَا يَكُونُ لَهُمْ رَغِيٌّ إِلَّا لِحُومِهِمْ، فَتَشْكُرُ عَنْهُمْ كَأَحْسَنِ مَا شَكَرْتَ عَنْ شَيْءٍ مِنَ النَّبَاتِ أَصَابَتْهُ قَطْرَةٌ

*“Watafunguliwa Yaa'juuju na Maa'juuju,, nao watatoka kwa watu, kama Anavyosema Allah Aliyetukuka:”**Wakawa wanateremka kutoka kila mlima**” Watawafunika na kuwashinda watu, na Waislamu watarudi kwenye miji yao na ngome zao, huku*

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:528.

wakiwachukua wanyama wao. Na wao Yaa'juuju na Maa'juuju, watakunywa maji yote ya ardhi mpaka baadhi yao wataupita mto na kunywa maji yake, kuuacha mkavu kabisa, kisha wale watakaokuja baada yao watapita mahali hapo na kusema: 'Hapa kulikuwa na maji wakati mmoja'. Kisha hakutakuwa hata mmoja aliyebaki isipokuwa wale walioko kwenye ngome na mijini. Baadaye mmoja wao atasema: 'Tumewashinda watu wa ardhini; sasa watu wa mbinguni ndio wamebakia'. Mmoja wao atautingisa mkuki wake na kuutupa mbinguni, nao utarudi ukiwa una damu, kama mtihani na majaribio kwao. Ilhali hili linatokea, Allah Atawatuma funza shingoni mwao, kama funza walio kwenye kokwa ya tende au katika mwanzu wa pua ya kondoo, watapambazukiwa wakiwa maiti bila ya hisia yoyote. Kisha Waislamu watasema: 'Nani atajitolea kutazama aliyoyafanya huyu adui?' Mmoja wao atakuja mbele na kujitoa, akijua kuwa atauliwa katika kutekeleza hilo. Atateremka na kuwakuta wamekufa, baadhi yao juu ya wengine. Hapo ataita: 'Enyi kongamano la Waislamu! Pateni bishara njema kuwa Allah Aliyetukuka Amewatosheleza dhidi ya adui yenu'. Kisha watatoka katika miji na ngome zao, na kuwaacha wanyama wao wawe ni wenye kulisha, lakini hawatapata chochote cha kula ila nyama za watu hao Yaa'juuju na Maa'juuju. Hata hivyo wataweza kujaza (matumbo yao kwa kula nyamafu hiyo) kuliko malisho yoyote waliokula kabla ya hapo"<sup>1</sup>. Pia Hadithi hii imenukuliwa na Ibn Maajah<sup>2</sup>.

## Hadithi ya Pili

Amepokea Imamu Ahmad kutoka kwa An-Nawwaas bin Sam'aan Al-Kilaabiy رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alimtaja Dajjaal asubuhi moja. Wakati mwingine alikuwa anamuelezea kama ambaye si lolote wala chochote na mara nyingine akamnyanyua mpaka tukahisi kuwa yuko katika miti ya mitende<sup>3</sup>. Akasema:

<sup>1</sup> Ahmad 3:77.

<sup>2</sup> Ibn Maajah 2:1363.

<sup>3</sup> Hilo lilipotokea, aliona katika nyuso zetu. Tulimuuliza kuhusu hilo, "Ewe Mtume wa Allah! Ulimtaja Dajjaal asubuhi ya leo na ukamzungumzia kama si chochote, na sasa unamzungumzia kama mwenye uwezo mpaka tunahisi kama yupo katika mitende". Kipande hiki hakipo katika mswada wa asili wa Ibn Kathir, lakini kipo katika kitabu cha Hadithi cha Imaam Ahmad.



«غَيْرِ الدَّجَالِ أَخُونِي عَلَيْكُمْ. فَإِنْ يَخْرُجْ وَأَنَا فِيكُمْ، فَأَنَا حَاجِبُهُ دُونَكُمْ، وَإِنْ يَخْرُجْ وَلَسْتُ فِيكُمْ، فَكُلُّ أَمْرٍ حَاجِبٌ نَفْسِهِ، وَاللَّهُ خَلِيفَتِي عَلَى كُلِّ مُسْلِمٍ، وَإِنَّهُ شَابٌ جَعْدٌ قَطَطٌ، عَيْنُهُ طَافِيَةٌ، وَإِنَّهُ يَخْرُجُ خَلَّةً بَيْنَ الشَّامِ وَالْعِرَاقِ فَعَاثُ بَيْنَنَا وَشِمَالًا، يَا عِبَادَ اللَّهِ اتَّبِعُوا»

*“Yapo mambo mengine ninayowahofia zaidi ya Dajjaal. Ikiwa atatokea nikiwa nanyi, nitapambana naye kwa niaba yenu. Akitokea nikiwa sipo nanyi, kila mmoja wenu itabidi apambane naye mwenyewe, na Allah Atamtizama kila Muislamu kwa niaba yangu. Yeye (Dajjaal) atakuwa ni kijana, mwenye nywele ndogo, zilizo panda na jicho lenye kuelea. Atatokeza sehemu iliyo baina Syria na Iraq, naye ataeneza fitina kuliani na kushotoni. Enyi waja wa Allah! Simameni imara (kuweni thabiti)”.*

Tukasema: “Ewe Mtume wa Allah! Atabaki kwa muda gani hapa ardhini?”

Akasema:

«أَرْبَعُونَ يَوْمًا، يَوْمَ كَسَنَةِ، وَيَوْمَ كَشْفِهِ، يَوْمَ كَجُمُعَةٍ، وَسَائِرَ أَيَّامِهِ كَأَيَّامِكُمْ»

*“Siku arobaini: siku moja kama mwaka, na siku moja kama mwezi, na siku moja kama wiki na siku zilizobakia kama siku zenu (za kawaida)”.*

Tukasema: “Ewe Mtume wa Allah! Siku hiyo itakayokuwa kama mwaka, itatutosheleza kwayo Swala ya mchana na usiku”. Akasema:

«لَا، افْدُرُوا لَهُ قَدْرَهُ»

*“Hapana, lakini ukadirieni kulingana na kipimo chake (na swali kulingana na kipimo hicho chako)”.*

Tukasema: “Ewe Mtume wa Allah! Je, kasi yake itakuwa namna gani?”

Akasema:

«كَالغَيْبِ اسْتَذْبَرْتَهُ الرِّيحُ»

*“Kama kiwingu kinachopelekwa na upepo”.*

Akasema:

«يَمُرُّ بِالْحَيِّ فَيَدْعُوهُمْ فَيَسْتَجِيبُونَ لَهُ، فَيَأْمُرُ السَّمَاءَ فَتُمْطِرُ، وَالْأَرْضَ فَتَنْبِتُ، وَتَرْوِحُ عَلَيْهِمْ سَارِحَتَهُمْ، وَهِيَ أَطْوَلُ مَا كَانَتْ دُرَى، وَأَمَدَهُ خَوَاصِرَ، وَأَسْبَعَهُ ضُرُوعًا، وَيَمُرُّ بِالْحَيِّ فَيَدْعُوهُمْ فَيَرُدُّونَ عَلَيْهِ قَوْلَهُ، فَتَبْعُهُ أَمْوَالُهُمْ فَيُضِيحُونَ مُسْجِلِينَ، لَيْسَ لَهُمْ مِنْ أَمْوَالِهِمْ شَيْءٌ، وَيَمُرُّ بِالْخَرِيَةِ فَيَقُولُ لَهَا: أَخْرِجِي كُتُوزَكَ، فَتَبْعُهُ كُتُوزَهَا كَيْعَاسِيبِ النَّحْلِ - قَالَ: - وَيَأْمُرُ بِرَجُلٍ فَيَقْتُلُ، فَيَضْرِبُهُ بِالسَّيْبِ فَيَقْطَعُهُ جَزَلَتَيْنِ رَمِيَةَ الْغَرَضِ، ثُمَّ يَدْعُوهُ فَيَقْبِلُ إِلَيْهِ، يَتَهَلَّلُ وَجْهَهُ، فَيَبْتِمَا هُمَ عَلَى ذَلِكَ، إِذْ بَعَثَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ الْمَسِيحَ عِيسَى ابْنَ مَرْيَمَ، فَيَنْزِلُ عِنْدَ الْمَنَارَةِ الْبَيْضَاءِ شَرْقِيٍّ دِمَشْقَ بَيْنَ مَهْرُودَتَيْنِ، وَأَضْمَا يَدَيْهِ عَلَى أَجْنِحَةِ مَلَكَتَيْنِ، فَيَبْعُهُ فَيَدْرِكُهُ فَيَقْتُلُهُ عِنْدَ بَابِ لُدِّ الشَّرْقِيِّ - قَالَ: - فَيَبْتِمَا هُمَ كَذَلِكَ، إِذْ أَوْحَى اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ إِلَى عِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ عَلَيْهِ السَّلَامُ أَنِّي قَدْ أَخْرَجْتُ عِبَادًا مِنْ عِبَادِي، لَا يَدَانِ لَكَ بِقَتَالِهِمْ، فَحَرِّزْ عِبَادِي إِلَى الطُّورِ، فَيَبْعُثُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ يَأْجُوجَ وَمَأْجُوجَ، كَمَا قَالَ تَعَالَى: ﴿وَهُمْ مِنْ كُلِّ حَدَبٍ يَسْلُونَ﴾»

*“Atakuja kwa watu na kuwaita katika njia yake, nao watamuitikia. Ataiamuru mbingu, nayo itanyesha; na ardhi, nayo itamea mimea, kisha hayawani wao watarudi jioni wakiwa na nundu ndefu na matiti yakiwa yamejaa maziwa na ubavu wao ukiwa mpana na mnono. Kisha atawajia watu wengine, naye atawaita katika njia yake lakini wao watakataa, hivyo mali yao itamfuata. Watakumbwa na ukame, wakiwa hawana mali yao kabisa. Kisha atatembea na kupita kwenye ardhi kame, naye ataiambia: ‘Toa hazina yako’, na hazina yake itatoka kama sega la nyuki. Kisha ataamuru mtu auliwe, naye atampiga kwa upanga na kumkata vipande viwili, na (ataviweka vipande hivi mbali mbali) kama masafa baina ya mlenga shabaha na dango lake. Kisha atamuita, na mtu huyo atakuja kwake uso wake uking’ara. Hapo Allah Atamtuma Masihi Isa bin Maryam, ambaye atateremka kwenye mnara mweupe upande wa mashariki ya Damaskas, akiwa amevaa nguo mbili zilizotiwa rangi hafifu ya manjano na mikono yake ikiwa imeegemea mabawa ya Malaika wawili. Atamtafuta (Dajjaal) mpaka atakapompata kwenye mlango wa mashariki wa Ludd, ambapo atamuua. Kisha Allaah Atamfunulia*

*Isa bin Maryam maneno yafuatayo: 'Nimewaleta miongoni mwa waja Wangu watu ambao hakuna atakayeweza kupigana nao. Wachukue waja Wangu kwenye usalama wa mlima (Twuur)'. Kisha Allah Atawaleta Yaa'juuju na Maa'juuju, kama Anavyosema: "wakawa wanateremka kutoka kila mlima".*

فَيْرِزِعْبُ عِيسَى وَأَصْحَابُهُ إِلَى اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ، فَيُرْسِلُ اللَّهُ عَلَيْهِمْ نَعْمًا فِي رِقَابِهِمْ  
فَيَضْبِحُونَ فَرَسَى كَمَوْتِ نَفْسٍ وَاحِدَةٍ، فَيَهْبِطُ عِيسَى وَأَصْحَابُهُ فَلَا يَجِدُونَ فِي  
الْأَرْضِ بَيْتًا إِلَّا قَدْ مَلَأَهُ زَهْمُهُمْ وَتَنَّتُهُمْ، فَيْرِزِعْبُ عِيسَى وَأَصْحَابُهُ إِلَى اللَّهِ عَزَّ  
وَجَلَّ، فَيُرْسِلُ اللَّهُ عَلَيْهِمْ طَيْرًا كَأَغْنَقِي الْبُخْتِ، فَتَحْمِلُهُمْ فَتَطْرَحُهُمْ حَيْثُ شَاءَ اللَّهُ

*"Isa na wafuasi wake watamuomba Allah, na Allah Atawapelekea wadudu watakaovamia shingo zao, na asubuhi wote watakuwa wameangamia. Kisha Isa na wafuasi wake watahuka chini na hawatapata hata sehemu moja katika ardhi ambayo isiyo na uvundo na harufu yao. Hapo Isa na wafuasi wake watamuomba tena Allah, Naye Atatuma ndege wenye shingo kama za Ngamia, nao watazibeba na kuzitupa Anapotaka Allah".*

Ibn Jaabir amesema: "Amenihadithia Atwaa' bin Yazid As-Saksakiy kutoka kwa Ka'b au mtu mwingine: 'Watazitupa kwenya Mahbal'. Ibn Jaabir akauliza: 'Ewe Abu Yazid, na Mahbal ni wapi?' Akasema: 'Upande wa mashariki (panapo chomoza jua)". Akasema:

«وَيُرْسِلُ اللَّهُ مَطَرًا لَا يَكُنْ مِنْهُ بَيْتٌ مَدْرٍ وَلَا وَبَرٍ أَرْبَعِينَ يَوْمًا، فَيُنْجِلُ الْأَرْضَ حَتَّى  
يَبْرُكَهَا كَالرَّلْفَةِ، وَيُقَالُ لِلْأَرْضِ: أَنْبِي نَمْرِكِ وَرُدِّي بَرَكَتِكَ، قَالَ: فَيَوْمَئِذٍ يَأْكُلُ  
النَّمْرُ مِنَ الرَّمَانَةِ فَيَسْتَطِيلُونَ بِحُفَيْفِهَا، وَيُبَارِكُ فِي الرِّسْلِ حَتَّى إِنَّ اللَّفْحَةَ مِنَ الْإِبِلِ  
لَتَكْفِي الْفَيْئَامَ مِنَ النَّاسِ، وَاللَّفْحَةَ مِنَ الْبَقْرِ نَكْفِي الْفَيْحَ، وَالشَّاةُ مِنَ النِّعَمِ تَكْفِي  
أَهْلَ الْبَيْتِ، قَالَ: فَيَبْتَمِئُ هُمْ عَلَى ذَلِكَ، إِذْ بَعَثَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ رِيحًا طَيِّبَةً،  
فَتَأْخُذُهُمْ تَحْتَ آبَائِهِمْ فَتَقْبِضُ رُوحَ كُلِّ مُسْلِمٍ - أَوْ قَالَ: كُلِّ مُؤْمِنٍ - وَيَبْقَى شِرَارُ  
النَّاسِ، يَتَهَارَجُونَ تَهَارُجَ الْحُمْرِ، وَعَلَيْهِمْ تَقَوْمُ السَّاعَةِ»

*"Na Allah Atateremsha mvua, hakutasimama nyumba ya udongo au (hema) la manyoa ya ngamia kwa siku arobaini, na ardhi*

*itaoshwa hata iwe kama kioo. Kisha ardhi itaambiwa: Toa matunda yako na rudisha baraka yako. Siku hiyo, kikundi cha watu kitaweza kula Rumani (komamanga) moja na kupata kivuli chini ya ngozi yake, na kila kitu kitabarikiwa. Ngamia wa maziwa atatoa maziwa mengi yatakayowatosha kikundi kizima cha watu, na ng'ombe wa maziwa atatoa maziwa mengi ambayo yatawatosha ukoo mzima, na kondoo atatosha nyumba nzima. Wakati huo Allah Aliyetukuka Atatuma upepo mzuri ambao utafika kwapani mwao, hivyo kuchukua roho ya kila Muislamu – au kila Muumini – na watabaki watu waovu tu wakifanya anasa na starehe kama nyumbu, na Kiyama kitakuja kwao”<sup>1</sup>.*

Hii pia ilinukuliwa na Muslim<sup>2</sup> lakini sio na Al-Bukhaari. Pia imerekodiwa na watu wa Sunan, kwa Isnadi tofauti. At-Tirmidhiy amesema: “Ni Hadithi Hasan Swahihh”<sup>3</sup>.

### Hadithi ya Tatu

Ampokea Imaam Ahmad kutoka kwa Ibn Harmalah, naye kutoka kwa halati wake (mama mdogo) aliyesema: “Mtume ﷺ alitoa khutbah, naye wakati huo alikuwa na kitambaa kidoleni mwake alichokuwa ameumwa na nge. Akasema:

«إِنَّكُمْ تَقُولُونَ: لَا عَدُوَّ لَكُمْ، وَإِنَّكُمْ لَا تَزَالُونَ تُقَاتِلُونَ عَدُوًّا، حَتَّى يَأْتِيَ بِأَجُوجَ وَمَاجُوجَ: عِرَاضَ الْجُوذِيِّ، صِفَارَ الْعُيُونِ، صُهَبَ الشَّعَافِ، مِنْ كُلِّ حَدَبٍ يَنْسِلُونَ  
كَأَنَّ وُجُوهَهُمُ الْمَجَانُّ الْمُطْرَقَةُ»

*‘Hakika nyinyi munasema: Hatuna adui kwa hakika nyinyi mutaendelea kupigana na adui mpaka watakapokuja Yaa’juuju na Maa’juuju. Hao wana nyuso pana, macho madogo na nywele nyekundu, wakimiminika kutoka katika kila mlima, nyuso zao zikitizama chini kama ngao zilizong’arishwa”<sup>4</sup>.*

<sup>1</sup> Ahmad 5:181.

<sup>2</sup> Muslim 4:2250.

<sup>3</sup> Abu Daud 4: 496, Tuhfatul al-Ahwadhiy 6:499, An-Nasaa’iy katika Al-Kubraa 6:235 na Ibn Maajah 2:1356.

<sup>4</sup> Ahmad 5:271.

Ibn Abi Haatim amenukuu Hadithi ya Muhammad bin Amr kutoka kwa Khalid bin Abdallah bin Harmalah Al-Mudlajiy kutoka kwa mama mdogo wake, aliyemsikia Mtume ﷺ, akitaja riwaya iliyo sawa na hii<sup>1</sup>.

Na imethibitika katika Hadithi kuwa Isa bin Maryam عليه السلام atatimiza amali ya Hajj kwenye *Bayt Al-Atiq* (Nyumba Kongwe – Al-Ka’bah). Amepokea Imaam Ahmad kuwa Abu Sa’id رضي الله عنه amesema: “Mtume ﷺ amesema:

«لِيَحْجَنَ هَذَا الْبَيْتُ وَلِيَعْتَمِرَنَّ بَعْدَ خُرُوجِ يَأْجُوجَ وَمَأْجُوجَ»

*‘Bila shaka atakuja kwenye Nyumba hii na kufanya Hajj na ‘Umrah, baada ya kutoka kwa Yaa’juuju na Maa’juuju’.*

Hadithi hii imenukuliwa na Al-Bukhaari<sup>2</sup>. Na Kauli Yake:

وَأَقْرَبَ الْوَعْدُ الْحَقُّ

**“Na miadi ya haki ikakaribia.”**

Maana yake: Siku ya Kiyama, hali hizi zikifika na mitetemeko ya ardhi na balaa kufika. Saa (Kiyama) itakuwa imefika, kukaribia kutukia, hapo makafiri watasema: “Hii ni Siku ya shida na taabu sana”.

Kwa hiyo Allah تعالی Akasema:

فَإِذَا هِيَ شَخِصَةٌ أَبْصَرُ الَّذِينَ كَفَرُوا

**“Hapo ndipo yatapokodoka macho ya waliokufuru.”**

Maana yake: Kwa shida ya yale wanayo yashuhudia kwa mambo yaliyo makubwa.

يَنوِيلُنَا

**“Ole wetu!”**

Watasema ole wetu (tumeangamia).

<sup>1</sup> Ibn Abi Haatim 8:24607.

<sup>2</sup> Ahmad 3:27 na Al-Bukhaariy 1593.

قَدْ كُنَّا فِي غَفْلَةٍ مِّنْ هَذَا

**“Bila ya shaka tulikuwa tumeghafilika na haya.”**

Maana yake: Hapa duniani.

بَلْ كُنَّا ظَالِمِينَ ﴿٧٧﴾

**“Bali tulikuwa wenye kudhulumu.”**

Wataikubali dhuluma waliyoifanya kwa nafsi yao wakati ambapo kukubali huko hakutawasaidia.

إِنكُمْ وَمَا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ حَصْبُ جَهَنَّمَ أَنْتُمْ لَهَا وَرِدُونَ ﴿٧٨﴾ لَوْ  
كَانَ هَتُولَاءِ ۗ إِلَهَةً مَا وَرَدُوهَا ۗ وَكُلٌّ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٧٩﴾ لَهُمْ فِيهَا زَفِيرٌ وَهُمْ فِيهَا لَا  
يَسْمَعُونَ ﴿٨٠﴾ إِنَّ الَّذِينَ سَبَقَتْ لَهُمْ مِنَّا الْحُسْنَىٰ أُولَٰئِكَ عَنْهَا مُبْعَدُونَ ﴿٨١﴾ لَا  
يَسْمَعُونَ حَسِيسَهَا ۗ وَهُمْ فِي مَا اشْتَهَتْ أَنفُسُهُمْ خَالِدُونَ ﴿٨٢﴾ لَا يَحْزَنُهُمُ الْفَرَعُ  
الْأَكْبَرُ وَتَتَلَقَّيْنَهُمُ الْمَلَائِكَةُ هَذَا يَوْمُكُمْ الَّذِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٨٣﴾

**98. Hakika nyinyi na hao munaowaabudu badala ya Allah ni kuni za Jahanamu; huko mtaingia tu.**

**99. Lau kuwa hawa ni miungu, wasingeliingia. Na wote watadumu humo.**

**100. Lao wao humo ni kupiga mayowe, na wala hawatasikia (jenginelo).**

**101. Ama wale ambao wema Wetu umewatangulia, hao watatenganishwa na hayo.**

**102. Hawatausikia mvumo wake, na wao watadumu katika yale zinayoyatamani nafsi zao.**

**103. Hicho Kitisho Kikubwa hakitowahuzunisha. Na Malaika watawapokea (kwa kuwaambia): Hii ndiyo Siku yenu mliyo kuwa mkiahidiwa!**

## Washirikina na miungu yao ni Kuni za Jahanamu

Allah تعالیٰ Anasema, watu wa Makka, washirikina waki-Kuraysh na wale wenye kufuata dini yao ya kuabudu masanamu.

إِنَّكُمْ وَمَا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ حَصَبُ جَهَنَّمَ

**“Hakika nyinyi na hao mnaowaabudu badala ya Allah ni kuni za Jahanamu.”**

Amesema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما: “Vijiti vya kuwashia moto”<sup>1</sup>, Maana: Kama katika Kauli Yake:

وَقُودُهَا النَّاسُ وَالْحِجَارَةُ

**“Na Moto ambao kuni zake ni watu na mawe...” (66:6).**

Na katika riwaya kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema:

حَصَبُ جَهَنَّمَ

**“Ni kuni za Jahanamu.”** Maana yake: Kuni za Jahanamu kwa lugha ya Zanjiyyah<sup>2</sup>. Na wamesema Mujaahid, ‘Ikrimah na Qataadah: “Kuni zake”. Na Adh-Dhahaak amesema:

حَصَبُ جَهَنَّمَ

**“Ni kuni za Jahanamu.”** Maana yake: “Kile kinachotupwa ndani yake.”<sup>3</sup> Hii pia ni rai iliyotolewa na wengineo.<sup>4</sup> Na Kauli Yake:

أُنْتُمْ لَهَا وَرُدُونَ ﴿٧﴾

**“Huko mtaingia tu.”** Maana yake: Mtaingia ndani yake.

لَوْ كَانَتْ هَتُؤُلَاءِ ءِالِهَةً مَا وَرَدُوهَا ۗ

**“Lau kuwa hawa ni miungu, wasingeliingia.”**

<sup>1</sup> Al-Qurtwubiy 11:343.

<sup>2</sup> Zanj katika lugha ya Kiarabu ya kisasa inahusisha mtu yeyote mweusi. Imefasiriwa katika Lisan Al-‘Arab na Asw-Swihaah kama watu wa Sudan ya zamani, na wingi wake ni Zunuz, ambayo pia ni jina la kabila la Kiarabu la Qahtwaani.

<sup>3</sup> Atw-Twabariy 18:536.

<sup>4</sup> Atw-Twabariy 18:536.

Maana yake: Kama masanamu na miungu ya uongo ambayo mmeabudu badala ya Allah تعالى, na lau ingekuwa ni miungu ya kweli hawangeingia Motoni.

وَكُلٌّ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿٩٢﴾

**“Na wote watadumu humo.”** Maana yake: Wenye kuabudu (mushirikina) na vyenye kuabudiwa (masanamu) watabaki humo daima dawamu na milele

لَهُمْ فِيهَا زَفِيرٌ

**“Wao humo ni kupiga mayowe.”**

Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

لَهُمْ فِيهَا زَفِيرٌ وَشَهِيقٌ ﴿٩٣﴾

**“Humo wawe wanapiga makelele (kama milio ya punda) na kutoa kwikwi.” (11:106).**

Maana ya Zafiir ni kutoa pumzi na Shahiiq ni kuvuta hewa.

وَهُمْ فِيهَا لَا يَسْمَعُونَ ﴿٩٤﴾

**“Na wala hawatasikia (jenginelo).”**

## Hali ya Watu Wema

Na Kauli Yake:

إِنَّ الَّذِينَ سَبَقَتْ لَهُمْ مِنَّا الْحُسْنَىٰ

**“Ama wale ambao wema Wetu umewatangulia”.**

Amesema ‘Ikrimah: “Rehema”. Na wengine wamesema: “Kupata Neema na Baraka”.

أُولَٰئِكَ عَنَّا مُبْعَدُونَ ﴿٩٥﴾

**“Hao watatenganishwa na hayo.”<sup>1</sup>**

Pale alipotaja Aliyetukuka watu wa Motoni na adhabu watakazopatiwa kwa sababu ya kumshirikisha Allah تعالى, Amefuatisha kwa Kutuelezea watu wema miongoni mwa waliomuamini Allah تعالى na Mitume Wake. Na hao ndio walio

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:541.



tanguliziwa kutoka kwa Allah تعالى furaha, kwani wao walitanguliza amali njema duniani. Kama Alivyosema Aliyetukuka:

﴿لِّلَّذِينَ أَحْسَنُوا الْحُسْنَىٰ وَزِيَادَةٌ﴾

**“Wale waliofanya wema watapata (jaza ya) wema wao na zaidi...”**  
(10:26).

Na Amesema:

﴿هَلْ جَزَاءُ الْإِحْسَنِ إِلَّا الْإِحْسَنُ﴾

**“Hakuna malipo ya ihsani ila kulipa ihsani vile vile.”** (55:60).

Kama vile walivyofanya matendo mema duniani, Allah تعالى Atawafanyia ihsani kwa hatima yao na thawabu zao, na Kuwaepusha na adhabu na Kuwapatia jaza na thawabu nyingi. Akasema:

﴿أُولَٰئِكَ عَنْهَا مُبْعَدُونَ ﴿١١٠﴾ لَا يَسْمَعُونَ حَسِيسَهَا﴾

**“Hao watatenganishwa na hayo. Hawatausikia mvumo wake”**,

Maana yake: Hawatahisi moto miilini mwao. Na Kauli Yake:

﴿وَهُمْ فِي مَا أَشْتَهَتْ أَنفُسُهُمْ خَالِدُونَ ﴿١١١﴾﴾

**“Na wao watadumu katika yale zinayoyatamani nafsi zao.”**

Watasalimika kwa wanayohofia, na kuwatisha, watapata wanayoyapenda na kutamani. Inasemwa kuwa hii iliteremshwa kuwatoa wanaoabudiwa badala ya Allah تعالى, ambao ni Uzayr na Masihi kutoka katika orodha ya wanaoabudiwa kutiwa motoni. Hii ni kama alivyopokea Hajjaaj bin Muhammad Al-A'war kutoka kwa Ibn Jurayj na 'Uthmaan bin 'Atwaa' kutoka kwa 'Atwaa' kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما:

﴿إِنَّكُمْ وَمَا تَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ حَصَبُ جَهَنَّمَ أَنتُمْ لَهَا وَرْدُونَ ﴿١١٢﴾﴾

**“Hakika nyinyi na hao mnaowaabudu badala ya Allah ni kuni za Jahanamu; huko mtaingia tu”**.

Kisha Akawavua (Akawatoa), Akasema:

﴿إِنَّ الَّذِينَ سَبَقَتْ لَهُم مِّنَّا الْحُسْنَىٰ﴾

**“Ama wale ambao wema Wetu umewatangulia.”**

Pakasemwa: “Hao ni Malaika na Isa عليه السلام na mfano wao miongoni mwa wanaoabudiwa badala ya Allah تعالى. Hii ndiyo iliyokuwa rai ya ‘Ikrimah, Al-Hasan na Ibn Jurayj.” Na amesema Muhammad bin Is’haaq bin Yasaar رحمه الله تعالى katika kitabu chake cha Sira.

“Kulingana na niliyoyasikia, Mtume ﷺ alikaa siku moja na al-Walid bin Al-Mughirah Msikitini, naye An-Nadhr bin Al-Haarith alikuja na kukaa nao. Pia walikuwepo wanaume wengine wa Quraysh Msikitini. Mtume ﷺ alizungumza, kisha An-Nadhr bin Al-Haarith alikuja kwake na Mtume ﷺ akazungumza naye mpaka akamshinda kwa hoja. Kisha akamsomea na kuwasomea:

إِنَّكُمْ وَمَا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ حَصَبُ جَهَنَّمَ أَنتُمْ لَهَا وَرِدُونَ ﴿٩٢﴾

**“Hakika nyinyi na hao mnaowaabudu badala ya Allah ni kuni za Jahanamu; huko mtaingia tu.’**

Mpaka kwenye Kauli Yake:

وَهُمْ فِيهَا لَا يَسْمَعُونَ ﴿٩٣﴾

**‘...na wala hawatasikia (jenginelo).’**

Kisha Mtume ﷺ aliinuka, akaenda kukaa na ‘Abdallah bin Aziba’ra As-Sahmiy. Walid bin Mughirah alimuambia Abdallah bin Aziba’ra, ‘Naapa kwa Allah تعالى, An-Nadhr bin Haarith hakumuweza kabisa mtoto wa ‘Abdul-Mutwtwalib katika hoja. Muhammad ﷺ anadai kuwa sisi na miungu yetu hii tunayoiabudu ni kuni za Moto’. ‘Abdallah bin Aziba’ra akasema: ‘Naapa kwa Allah تعالى, lau nitakutana naye nitamshinda kwa hoja. Muulize Muhammad ﷺ kama kila kinachoabudiwa badali ya Allah تعالى kitaingia Motoni pamoja na wanaomuabudu, kwani sisi tunaabudu Malaika, na Mayahudi wanamuabudu ‘Uzayr, ilhali Wakristo wanamuabudu Masihi, ‘Isa bin Maryam’. Walid na waliokaa pamoja naye walishangaa kwa aliyosema Abdallah bin Aziba’ra, nao wakadhania kuwa amekuja na nukta nzuri sana. Akasema haya kwa Mtume ﷺ, aliyesema:

«كُلُّ مَنْ أَحَبَّ أَنْ يُعْبَدَ مِنْ دُونِ اللَّهِ، فَهُوَ مَعَ مَنْ عِبَدَهُ، إِنَّهُمْ إِنَّمَا يَعْبُدُونَ الشَّيْطَانَ وَمَنْ أَمَرَهُمْ بِعِبَادَتِهِ»

**‘Kila anayependa kuabudiwa badala ya Allah atakuwa pamoja na**

wanaomuabudu, kwani kwa hakika wanamuabudu Shetani na kila aliyewaambia wamuabudu yeye."

Kisha Allah Akateremsha:

إِنَّ الَّذِينَ سَبَقَتْ لَهُمْ مِنَّا الْحُسْنَىٰ أُولَٰئِكَ عَنْهَا مُبْعَدُونَ ﴿٩٢﴾ لَا يَسْمَعُونَ  
حَسِيسَهَا ۖ وَهُمْ فِي مَا اشْتَهَتْ أَنفُسُهُمْ خَالِدُونَ ﴿٩٣﴾

**"Ama wale ambao wema Wetu umewatangulia, Hao watatenganishwa na hayo. Hawatausikia mvumo wake, na wao watadumu katika yale zinayoyatamani nafsi zao."**

Maana yake: Isa عليه السلام, Uzayr na wanaoabudiwa miongoni mwa watawa na wanazuoni waliojiweka katika utiifu wa Allah تعالى, lakini wapotevu waliwaabudu na kuwafanya miungu badala ya Allah تعالى. Na ikateremka kwa wanayoyataja kuwa wanaabudu Malaika na kuwa wao ni mabinti wa Allah:

وَقَالُوا اتَّخَذَ الرَّحْمَنُ وَلَدًا ۗ سُبْحٰنَهُ ۗ بَلْ عِبَادٌ مُّكْرَمُونَ ﴿٩٤﴾

**"Na wanasema: Ar-Rahman, Mwingi wa Rehema, Ana mwana! Subhanahu, Ametakasika na hayo! Bali hao (wanaowaita wana) ni watumwa waliotukuzwa."** Mpaka kwa Kauli Yake:

وَمَنْ يُقُلْ مِنهُمْ إِنِّي إِلٰهُ مِّنْ دُونِهِ ۖ فَذَٰلِكَ نَجْزِيهِ جَهَنَّمَ ۗ كَذَٰلِكَ نَجْزِي الظَّٰلِمِينَ ﴿٩٥﴾

**"Na yeyote kati yao atakayesema: Mimi ni mungu, badala Yake, basi huyo Tutamlipa malipo yake Jahanamu. Hivyo ndivyo Tuwalipavyo wenye kudhulumu." (21:26-29).**

Na kuhusiana na suala la Isa عليه السلام kuwa yeye anaabudiwa badala ya Allah تعالى, na kustaajabu kwa Al-Walid na wengine waliokuwepo kwa hoja iliyotolewa (na 'Abdallah bin Aziba'ra) maneno yafuatayo yaliteremshwa:

﴿٩٦﴾ وَكَلَّمَا ضُرِبَ ابْنُ مَرْيَمَ مِثْلًا إِذَا قَوْمُكَ مِنْهُ يَصِدُّونَ ﴿٩٧﴾ وَقَالُوا ۗءَأَلٰهَتُنَا خَيْرٌ أَمْرُ  
هُوَ ۗ مَا ضَرَبُوهُ لَكَ إِلَّا جَدَلًا ۗ بَلْ هُمْ قَوْمٌ خَصِمُونَ ﴿٩٨﴾ إِنَّ هُوَ إِلَّا عَبْدٌ أَنْعَمْنَا عَلَيْهِ  
وَجَعَلْنَاهُ مِثْلًا لِّبَنِي إِسْرَءِيلَ ﴿٩٩﴾ وَلَوْ نَشَاءُ لَجَعَلْنَا مِنْكُمْ لِبَنِي إِسْرَءِيلَ فِي الْأَرْضِ مِثْلًا لِّقَوْمٍ  
﴿١٠٠﴾

وَأَنَّهُمْ لَعَالِمٌ لِّلسَّاعَةِ فَلَا تَمْتَرُنَّ بِهَا

***“Na alipopigiwa mfano mwana wa Maryam, mara watu wako wakaupigia kelele. Wakasema: ‘Je, miungu yetu ni bora au yeye?’ Hawakuelezi hayo ila kwa kujadiliana tu; bali hao ni watu wagomvi. Hakuwa Nabii Isa ila ni mja Tuliyeemmesha na Tukamfanya mtihani mzuri kwa wana wa Israili. Na kama Tungalipenda Tungewafanya Malaika kuwa wakazi wa ardhi hii badala yenu. Na kwa kweli (Nabii Isa) ni alama ya Kiyama; msikifanyie shaka...” (43:57-61),***

Maana yake: Kwa aliyopewa mikononi mwake katika Ishara na miujiza kwa kuhuisha wafu na kuwaponya wagonjwa, inatosha kuwa dalili ya kukaribia Kiyama. Akasema:

فَلَا تَمْتَرْنَ بِهَا وَاتَّبِعُونِ هَذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ ﴿٦١﴾

***“Msikifanyie shaka na ifuateni. Hii ndio njia iliyonyooka.” (43:61)<sup>1</sup>***

Na hili alilosema Abdallah bin Aziba’ra ni kosa kubwa, kwani Aya yenyewe inawahutubia watu wa Makka kuhusu kuabudu kwao masanamu wasiokuwa na uhai, hivyo kutoweza kufikiria.

Hilo lilikuwa ni kemeo na kutwezwa kwa kuwaabudu kwao, hivyo Akasema Aliyetukuka:

إِنَّكُمْ وَمَا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ حَصَبُ جَهَنَّمَ

***“Hakika nyinyi na hao munaowaabudu badala ya Allah ni kuni za Jahanamu”.***

Na vipi hili litahusishwa na Masihi, ‘Uzayr na wengine waliofanya amali njema nao hawakuridhia kuabudiwa na wanaowaabudu? Na Kauli Yake:

لَا تَحْزَنُهُمُ الْفَرَعُ الْأَكْبَرُ

***“Hicho Kitisho Kikubwa hakitowahuzunisha”.***

Panasemwa: “Muradi wa hilo ni mauti, kama alivyopokea ‘Abdur-Razzaaq kutoka kwa Yahya bin Rabi’ah kutoka kwa ‘Atwaa’. Au palisemwa kuwa kitisho kikubwa kinamaanisha kupulizwa parapanda, kama alivyopokea Al-Awfiy

kutoka kwa Ibn 'Abbaas<sup>1</sup>, na Abu Sinaan, Said bin Sinaan Ash- Shaybaaniy. Hii ndiyo iliyokuwa rai ya Ibn Jariir رحمه الله تعالى katika tafsiri yake. Na Kauli Yake:

وَتَلَقُّهُمْ الْمَلَائِكَةُ هَذَا يَوْمُكُمْ الَّذِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٩٢﴾

***“Na Malaika watawapokea (kwa kuwaambia): Hii ndiyo Siku yenu mliyokuwa mkiahidiwa!”***

Maana yake: Malaika watawaambia kwa kuwabashiria Siku hiyo ya Miadi watakapotoka kwenye makaburi yao.

هَذَا يَوْمُكُمْ الَّذِي كُنْتُمْ تُوعَدُونَ ﴿٩٣﴾

***“Hii ndiyo Siku yenu mliyokuwa mkiahidiwa!”***

Maana yake: Tarajieni yaliyo mazuri kabisa.

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Ibn Hishaam 1:384.

يَوْمَ نَطْوِي السَّمَاءَ كَطَيِّ السِّجِلِ لِلْكِتَابِ ۗ كَمَا بَدَأْنَا  
 أَوَّلَ خَلْقٍ نُعِيدُهُ ۗ وَعَدَّا عَلَيْنَا ۗ إِنَّا كُنَّا فَعْلِينَ ۝  
 وَلَقَدْ كَتَبْنَا فِي الزَّبُورِ مِنْ بَعْدِ الذِّكْرِ أَنَّ الْأَرْضَ  
 يَرِثُهَا عِبَادِيَ الصَّالِحُونَ ۝ إِنَّ فِي هَذَا لَبَلَاغًا  
 لِقَوْمٍ عَابِدِينَ ۝ وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً  
 لِّلْعَالَمِينَ ۝ قُلْ إِنَّمَا يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَهُكُمُ  
 إِلَهُ وَاحِدٌ ۗ فَهَلْ أَنتُمْ مُسْلِمُونَ ۝ فَإِن تَوَلَّوْا فَعَلْنَا  
 بِأَذْنَتِكُمْ عَلَىٰ سَوَاءٍ ۗ وَإِن أَدْرَىٰ أَقْرَبُ أَم بَعِيدٌ مَّا  
 تُوعَدُونَ ۝ إِنَّهُ يَعْلَمُ الْجَهْرَ مِنَ الْقَوْلِ وَيَعْلَمُ مَا  
 تَكْتُمُونَ ۝ وَإِن أَدْرَىٰ لَعَلَّهُ فِتْنَةً لِّكُمْ وَمَتَّبِعْ إِلَىٰ  
 حِينِ ۝ قُلْ رَبِّ أَحْكُم بِالْحَقِّ ۗ وَرَبُّنَا الرَّحْمَنُ  
 الْمُسْتَعَانُ عَلَىٰ مَا تَصِفُونَ ۝

يَوْمَ نَطْوِي السَّمَاءَ كَطَيِّ السِّجِلِ  
 لِلْكِتَابِ ۗ كَمَا بَدَأْنَا أَوَّلَ خَلْقٍ  
 نُعِيدُهُ ۗ وَعَدَّا عَلَيْنَا ۗ إِنَّا كُنَّا  
 فَعْلِينَ ۝

**104. Siku Tutakapozikunja mbingu kama mkunjo wa karatasi za vitabu. Kama Tulivyolianza umbo la mwanzo Tualirudisha tena. Ni ahadi iliyo juu Yetu. Hakika Sisi ni watendao.**

**Kukunjwa mbingu Siku ya Kiyama**

Anasema Aliyetukuka: Hili litatokea Siku ya Kiyama (bila shaka yoyote),

يَوْمَ نَطْوِي السَّمَاءَ كَطَيِّ السِّجِلِ لِلْكِتَابِ ۗ

**“Siku Tutakapozikunja mbingu kama mkunjo wa karatasi za vitabu”.**

Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَمَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ ۗ وَالْأَرْضُ جَمِيعًا قَبْضَتُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۗ وَالسَّمَوَاتُ مَطْوِيَّاتٌ  
 بِيَمِينِهِ ۗ سُبْحٰنَهُ وَتَعٰلَىٰ عَمَّا يُشْرِكُونَ ۝

**“Na hawakumheshimu Allah heshima ipasayo. Na Siku ya Kiyama ardhi yote itakuwa Mkononi Mwake, na mbingu zitakunjwa katika**

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:542.

***Mkono Wake wa Kuume. Ameenpukana na upungufu na Yu wa juu kabisa kuliko yale wanayomshirikisha.” (39:67)***

Na hakika amepokea Al-Bukhaariy kutoka kwa Naafi’ kutoka kwa Ibn ‘Umar رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ اللَّهَ يُفِضُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ الْأَرْضِينَ وَتَكُونُ السَّمَوَاتُ بِبَيْتِهِ»

*“Hakika Allah Atazikamata ardhi Siku ya Kiyama na mbingu zitakuwa kwenye Mkono Wake wa kulia”.*

Hii ilirekodiwa na Bukhari peke yake<sup>1</sup>. Na Kauli Yake:

كَطَيَّ السَّجِلَّ لِلْكِتَابِ

***“Kama mkunjo wa karatasi za vitabu”.*** Maana ya *Ssijill* ni kitabu. Na amesema As-Suddiy kuhusu Aya hii: *“As-Sijill”* ni Malaika aliyewakilishwa kuweka rekodi; pindi mtu anapoaga dunia, kitabu (chake cha amali) kitachukuliwa juu hadi *“As-Sijill”* ataikunja na kuiweka kando mpaka Siku ya Kiyama”. Hata hivyo, muono ulio sawa ni ule uliopokewa kutoka kwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما kuwa *As-Sijill* ina maana ya sahifa (ya amali)<sup>2</sup>. Hii pia imepokewa kutoka kwake na ‘Aliy bin Abi Twalhah na Awfiy<sup>3</sup>. Na limepokewa hilo kutoka kwa Mujahid, Qatadah na wengineo<sup>4</sup>. Huu ndio muono uliochaguliwa na Ibn Jariir رحمه الله تعالى, kwa kuwa matumizi haya ni mashuhuri sana katika lugha ya Kiarabu. Kwa kuzingatia hilo, inakuwa maana yake: ***“Siku ambayo mbingu zitakunjwa kunjwa kama karatasi.”*** Hii ni kama Aya ifuatayo:

فَلَمَّا أَسْلَمَا وَتَلَّهٖ لِلْجَبِينِ ﴿١٠٣﴾

***“Basi wote wawili walipojislamisha (kwa Allah), na akamlaza kifudufudi (amchinje).” (37:103)***

Na hili lina mifano mengi katika lugha ya Kiarabu. Na Allah تعالى Ndiye Mjuzi zaidi, Maana yake: Kusujudu kwa paji lake la uso.

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Bari 13:404.

<sup>2</sup> At-Twabariy 18:543.

<sup>3</sup> At-Twabariy 18:543.

<sup>4</sup> At-Twabariy 18:543.

كَمَا بَدَأْنَا أَوَّلَ خَلْقٍ نُعِيدُهُ وَعَدَّا عَلَيْنا إِنَّا كُنَّا فاعِلِينَ ﴿١٠٤﴾

***“Kama Tulivyoanza umbo la mwanzo Tatalirudisha tena. Ni ahadi iliyo juu Yetu. Hakika Sisi ni watendao.”***

Maana yake: Hii bila shaka yoyote itafika Siku ambayo Allah تعالی Atawaumba upya viumbe Vyake. Kama Alivyowaumba hapo awali, kwa hakika Ana uwezo wa Kuwaumba tena.

Hii kwa yakini itakujafika na kupita kwa sababu ni mojawapo ya mambo ambayo Allah تعالی Ameahidi, Naye Havunji Ahadi Yake kabisa. Yeye ni Muweza kabisa Kufanya hivyo. Kwa hiyo Akasema:

إِنَّا كُنَّا فاعِلِينَ ﴿١٠٥﴾

***“Hakika Sisi ni watendao”.***

Na amepokea Imaam Ahmad kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Alisimama mbele yetu Mtume ﷺ kutoa mawaidha, akasema:

«إِنَّكُمْ مَحْشُورُونَ إِلَى اللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ حُفَاءَ عُرَاةٍ غُرُلًا، كَمَا بَدَأْنَا أَوَّلَ خَلْقٍ نُعِيدُهُ  
وَعَدَّا عَلَيْنا، إِنَّا كُنَّا فاعِلِينَ»

*‘Hakika nyinyi mtakusanywa mbele ya Allah Aliyetukuka mkiwa bila viatu, uchi na hamjatahiriwa. Tunakirudisha kama tulivyoanza Uumbaji wa kwanza. Hii ni ahadi Kwetu Sisi. Hakika Sisi ni watendao’<sup>1</sup>*

Akataja Hadithi kwa ukamilifu wake. Pia Hadithi hii imenukuliwa katika Sahihi mbili, na Al-Bukhaari ameitaja katika Tafsiri yake ya Aya hii<sup>2</sup>.

وَلَقَدْ كَتَبْنَا فِي الزَّبُورِ مِنْ بَعْدِ الذِّكْرِ أَنَّ الْأَرْضَ يَرِثُهَا عِبَادِيَ الصَّالِحُونَ ﴿١٠٦﴾  
إِنَّ فِي هَذَا لَبَلَاغًا لِقَوْمٍ عابِدِينَ ﴿١٠٧﴾ وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ ﴿١٠٨﴾

<sup>1</sup> Ahmad 1:235.

<sup>2</sup> Fat’h Al-Baariy 8:292 na Muslim 4:2194.



**105. Na hakika Tulikwishaandika katika Zaburi baada ya Kumbukumbu, ya kwamba nchi watairithi waja Wangu walio wema.**

**106. Hakika katika haya yapo mawaidha kwa watu wafanyao ibada.**

**107. Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote.**

### **Ardhi Itarithiwa na Watu Wema**

Anasema Aliyetukuka Kutupasha habari kwa Kudura Yake kuwa waja Wake wema watapata furaha hapa duniani na Akhera, ambao watairithi hii ardhi hapa duniani na Akhera. Hii ni kama Anavyosema Aliyetukuka:

إِنَّ الْأَرْضَ لِلَّهِ يُورِثُهَا مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ ۗ وَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ ﴿١٢٨﴾

**“Hakika ardhi ni ya Allah, Atamrithisha Amtakaye katika waja Wake; na mwisho mwema ni kwa wamchao.” (7:128)**

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ ءَامَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ ﴿٥١﴾

**“Bila shaka Sisi Tutawanusuru Mitume wetu na wale walioamini katika maisha ya dunia na siku watakaposimama mashahidi.” (40:51).**

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ

**“Allah Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, kuwa Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wale waliokuwako kabla yao, na kwa yakini Atawasimamishia Dini yao Aliyowapendelea.” (24:55).**

Allah تعالیٰ Anatueleza kuwa hii imerekodiwa katika Vitabu vya Sharia na Qadar (Kudura), kwa hiyo haina budi kutokea. Kwa hiyo Akasema Aliyetukuka:

وَلَقَدْ كَتَبْنَا فِي الزُّبُورِ مِنْ بَعْدِ الذِّكْرِ

**“Na hakika Tulikwishaandika katika Zaburi baada ya Kumbukumbu.”**

Amesema Al-A'mash: Nilimuuliza Said bin Jubayr kuhusu Aya ifuatayo:

وَلَقَدْ كَتَبْنَا فِي الزُّبُورِ مِنْ بَعْدِ الذِّكْرِ

**“Na hakika Tulikwishaandika katika Zaburi baada ya Kumbukumbu.”**

Akasema: *Az-Zabuur* inamaanisha Taurati, Injil na *Qur'ani*<sup>1</sup>. Mujaahid amesema: “*Az-Zabuur* inamaanisha Kitabu”<sup>2</sup>. Ibn 'Abbaas, Sha'biy, Hasan, Qatadah na wengine wamesema: *Az-Zabuur* ni kile ambacho kimeteremshwa kwa Daud na *Adh-Dhikr* ni Taurati”. Mujaahid amesema: *Az-Zabuur* ina maana ya Vitabu vilivyokuja baada ya *Adh-Dhikr*, na *Adh-Dhikr* ni Mama wa Kitabu (*Umm Al-Kitaab*) ambacho kipo kwa Allah تعالى.<sup>3</sup> Hii pia ilikuwa ndio rai ya Zayd bin Aslam: “Hicho ni Kitabu cha kwanza”. Thawriy رحمه الله تعالى amesema: “Hicho ni *Al-Lawh Al-Mahfuudh*”. Na amepokea Mujaahid kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما:

أَنَّ الْأَرْضَ يَرِثُهَا عِبَادِيَ الصَّالِحُونَ ﴿١٥١﴾

**“Ya kwamba nchi watairithi waja Wangu walio wema.”**

Maana yake: Ardhi ya Peponi<sup>4</sup>. Na hivyo ndivyo alivyosema Abu Al-Aliyah, Mujaahid, Said bin Jubayr, Ash-Sha'biy, Qatadah, As-Suddiy, Abu Swaalih, Ar-Rabii bin Anas na Ath-Thawriy<sup>5</sup>, Allah تعالى Awarehemu. Na Kauli Yake:

إِنَّ فِي هَذَا لَبَلَاغًا لِقَوْمٍ عَابِدِينَ ﴿١٥٢﴾

**“Hakika katika haya yapo mawaidha kwa watu wafanyao ibada.”**

Maana: Bila shaka katika *Qur'ani* hii ambayo Tumeiteremsha kwa mja Wetu Muhammad: “Yapo mawaidha (ya wazi)”, yenye manufaa na yanawatosha, “Watu wafanyao ibada”. Na hao ni wale wenye kumuabudu Allah تعالى kwa njia Aliyoiweka katika sheria Yake, Anayoipenda na inayomridhisha, na watachagua kumtii Allah kuliko kumfuata shetani au matamano ya nafsi zao.

<sup>1</sup> At-Tabari 18:547.

<sup>2</sup> At-Tabari 18:547.

<sup>3</sup> At-Tabari 18:547.

<sup>4</sup> At-Tabari 18:549.

<sup>5</sup> At-Tabari 18:549, 550.

## Muhammad ﷺ ni Rehema kwa Walimwengu Wote

Na Kauli Yake:

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ ﴿١٧﴾

**“Nasi Hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote”.**

Allah تعالی Anatufahamisha kuwa Amemfanya Muhammad ﷺ kuwa ni Rehema kwa walimwengu wote. Maana: Amemtuma kuwa ni rehema kwao wote. Hivyo yeyote mwenye kuikubali rehema hii na kuishukuru neema hii, atafaulu hapa duniani na Kesho Akhera. Na mwenye kuikataa na kuipinga atakhasirika hapa duniani na Kesho Akhera. Kama Anavyosema Aliyetukuka:

﴿ أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ بَدَلُوا نِعْمَتَ اللَّهِ كُفْرًا وَأَحَلُّوا قَوْمَهُمْ دَارَ الْبَوَارِ ﴾ ﴿١٨﴾ جَهَنَّمَ  
يَصْلَوْنَهَا وَيُنْسَوْنَ الْفَرَاژَ ﴿١٩﴾

**“Je, hukuwaona wale waliobadilisha Neema ya Allah kwa kukufuru; na wakawafikisha watu wao katika nyumba ya maangamizo, ambayo ni Jahanamu. Wataingia na ni mahali pabaya kabisa pa kukaa kiumbe.” (14:28-29).**

Na Allah تعالی Amesema katika Kuisifu na Kueleza Qur’ani:

﴿ قُلْ هُوَ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا هُدًى وَشِفَاءً ۗ وَالَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ فِي ءَاذَانِهِمْ وَقْرٌ وَهُوَ عَلَيْهِمْ عَمًى ۗ أُولَٰئِكَ يُنَادَوْنَ مِن مَّكَانٍ بَعِيدٍ ﴾ ﴿٤١﴾

**“Sema: Hii (Qur’ani) ni uongofu na poza kwa wale walioamini; na wale wasioamini umo uzito katika masikio yao; na hiyo (Qur’ani) ni giza kwao. Hawasikii kama kwamba hao wanaitwa, na hali ya kuwa wako mbali kabisa.” (41:44).**

Na amesema Muslim katika Sahihi yake: Ametuhadithia Ibn Abi ‘Umar, ametuhadithia Marwaan Al-Fazari, kutoka kwa Yazid bin Kaisaan, kutoka kwa Ibn Abi Haazim kuwa Abi Hurayrah رضي الله عنه amesema: “Palisemwa: Ewe Mtume ﷺ, omba dhidi ya washirikina”. Akasema:

﴿ إِنِّي لَم أَنبُتُ لَكُمْ، وَإِنَّمَا بُعِثْتُ رَحْمَةً ۗ ﴾

**“Hakika mimi sikutumwa kulaani, bali nimetumwa kuwa Rehema”.**

Hii imepokewa na Muslim peke yake<sup>1</sup>.

Na imepokewa na Imaam Ahmad kuwa 'Amr bin Abi Qurrah Al-Kindiy amesema: "Hudhayfah alikuwa katika Madaa'in (miji), naye alikuwa akitaja vitu ambavyo Mtume ﷺ alisema. Hudhayfah akafika kwa Salmaan, na Salmaan akasema: 'Ewe Hudhayfah, Mtume ﷺ alikuwa akikasirika na hivyo kuzungumza kulingana na hali hiyo, na mara nyingine alikuwa akiridhia na akizungumza kulingana na hali hiyo. Nafahamu kuwa Mtume ﷺ alituhutubia, akasema:

«أَيُّمَا رَجُلٍ مِنْ أُمَّتِي سَبَيْتُهُ [سَبَّهَ] فِي عَضْبِي أَوْ لَعَنْتُهُ لَعْنَةً، فَإِنَّمَا أَنَا رَجُلٌ مِنْ وَرْدِ  
آدَمَ أَغْضَبُ كَمَا تَغْضَبُونَ، إِنَّمَا بَعَثَنِي اللَّهُ رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ فَاجْعَلْهَا صَلَاةً عَلَيْهِ يَوْمَ  
الْقِيَامَةِ»

*'Mtu yeyote katika umma wangu ambaye nimemsema vibaya au kumlaani nikiwa na ghadhabu – hakika ni kuwa mimi ni mwanadamu miongoni mwa wana wa Adam, nami nakasirika kama mnavyokasirika. Hata hivyo, bila shaka Allah Amenituma kuwa ni rehema kwa walimwengu wote, nayo itajaaliwa kuwa baraka kwake Siku ya Kiyama''<sup>2</sup>.*

Na imepokewa na Abu Daud kutoka kwa Ahmad bin Yunus, naye kutoka kwa Zaidah<sup>3</sup>.

Huenda pakasemwa: Wanaokufuru watapata aina gani ya rehema kutoka kwake? Jawabu la swali hilo ni lile ambalo Abu Ja'far bin Jariir رحمه الله تعالى amenukuu kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kuhusiana na Aya ifuatayo:

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِّلْعَالَمِينَ ﴿١٠٤﴾

***"Nasi hatukukutuma ila uwe ni Rehema kwa walimwengu wote".***

Amesema: "Mwenye kumuamini Allah تعالى na Siku ya Mwisho, ataandikiwa rehema hapa duniani na Kesho Akhera. Ama kwa asiyemuamini Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ, hatalindwa na mitetemeko ya ardhi na kupigwa mawe yaliyowapata Umma (kaumu) zilizopita"<sup>4</sup>.

<sup>1</sup> Muslim 4:2006.

<sup>2</sup> Ahmad 5:437.

<sup>3</sup> Abu Daawud 5:45. Kuna Hadithi mfano wa hii katika Sahihi Muslim namba 2601.

<sup>4</sup> Atw-Twabariy 18:552. Sanadi yake ni dhaifu.

قُلْ إِنَّمَا يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَهُكُمُ إِلَهُهُ وَاحِدٌ ۗ فَهَلْ أُنْتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿١٠٨﴾ فَإِنْ تَوَلَّوْا  
 فَقُلْ ءَاذَنْتُكُمْ عَلَىٰ سَوَاءٍ ۗ وَإِنِ أَدْرَىٰ أَقْرَبُ أَم بَعِيدٌ مَّا تُوعَدُونَ ﴿١٠٩﴾ إِنَّهُ يَعْلَمُ  
 الْجَهْرَ مِنَ الْقَوْلِ وَيَعْلَمُ مَا تَكْتُمُونَ ﴿١١٠﴾ وَإِنِ أَدْرَىٰ لَعَلَّهُ فِتْنَةٌ لَّكُمْ وَمَتَاعٌ  
 إِلَىٰ حِينٍ ﴿١١١﴾ قُلْ رَبِّ أَحْكُم بِالْحَقِّ ۗ وَرَبُّنَا الرَّحْمَنُ الْمُسْتَعَانُ عَلَىٰ مَا تَصِفُونَ ﴿١١٢﴾

108. Sema: Hakika imefunuliwa kwangu ya kwamba hakika Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu. Je! Mumesilimu?

109. Na kama wakigeuka, basi sema: Nimekutangazieni sawa sawa, wala sijui yako karibu au mbali hayo muliyoahidiwa.

110. Hakika Yeye Anajua kauli ya dhahiri na Anajua muyafichayo.

111. Wala sijui pengine huu ni mtihani tu kwenu na starehe mpaka muda kidogo.

112. Sema: Mola wangu Mlezi! Hukumu kwa haki. Na Mola wetu Mlezi ni Mwingi wa Rehema, Aombwaye msaada juu ya munayo yazua.

Hoja katika Madhumuni ya Wahyi ni Kumuabudu Allah تعالیٰ

Allah تعالیٰ Anasema huku Akimuamuru Mtume Wake ﷺ Awaambie washirikina:

قُلْ إِنَّمَا يُوحَىٰ إِلَيَّ أَنَّمَا إِلَهُكُمُ إِلَهُهُ وَاحِدٌ ۗ فَهَلْ أُنْتُمْ مُسْلِمُونَ ﴿١٠٨﴾

“Hakika imefunuliwa kwangu ya kwamba hakika Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu. Je! Mumesilimu?”

Maana: Je, mtafuata hayo na kujisalimisha kwayo?

فَإِنْ تَوَلَّوْا

“Na kama wakigeuka”. Maana: Wakipuuza kwa unayowaitia.

فَقُلْ ءَاذَنْتُكُمْ عَلَىٰ سَوَاءٍ ۗ

“Basi sema: Nimekutangazieni sawa sawa”.

Maana yake: Nimetangaza nitakuwa na vita na nyinyi kama ambavyo mmo katika hali ya vita nami. Mimi niko mbali nanyi kama mulivyo mbali nami. Hii ni kama Kauli Yake Aliyetukuka:

وَإِنْ كَذَّبُوكَ فَقُلْ لِي عَمَلِي وَلَكُمْ عَمَلُكُمْ أَنتُمْ بَرِيئُونَ مِمَّا أَعْمَلُ وَأَنَا بَرِيءٌ مِمَّا تَعْمَلُونَ ﴿١٠٤﴾

**“Na kama wakiendelea kukukadhibisha sema: ‘Mimi nina amali yangu na nyinyi muna amali yenu. Nyinyi hamna dhima na ninayoyatenda mimi (hamtalipwa nyinyi), wala mimi sina dhima na munayoyatenda nyinyi (sitalipwa mimi)?” (10:41).**

Na Akasema:

وَأِمَّا تَخَافَنَّ مِنْ قَوْمٍ خِيَانَةً فَأَنْذِرْ إِلَيْهِمْ عَلَىٰ سَوَاءٍ

**“Na kama ukiogopa hiyana kwa watu basi watupie ahadi yao kwa usawa.” (8:58),**

Maana yake: Hapo nyote, nyinyi na wao watajua kuwa ahadi waliokuwa nayo imebatilika. Na hivyo ndivyo ilivyo hapa:

فَإِنْ تَوَلَّوْا فَقُلْ ءَاذَنْتُكُمْ عَلَىٰ سَوَاءٍ

**“Na kama wakigeuka, basi sema: Nimekutangazieni sawa sawa.”**

Maana yake: Tayari nimewajulisha kuwa mimi niko mbali nanyi (hatuna uhusiano wowote), nanyi mko mbali nami, kwa kujua kwangu hilo.

### Hakuna Ajuaye Wakati wa Kiyama

Na Kauli Yake:

وَإِنْ أَدْرِي أَقْرِبُ أَمْ بَعِيدٌ مَّا تُوعَدُونَ ﴿١٠٥﴾

**“Wala sijui yako karibu au mbali hayo muliyoahidiwa.”**

Maana yake: Bila shaka kitafika, lakini sina elimu kwa ukaribu au umbali wa siku hiyo.

إِنَّهُ يَعْلَمُ الْجَهْرَ مِنَ الْقَوْلِ وَيَعْلَمُ مَا تَكْتُمُونَ ﴿١٠٦﴾

**“Hakika Yeye Anajua kauli ya dhahiri na Anajua muyafichayo.”**

Maana yake: Allah تعالى Ndiye Mwenye Kujua ghaibu yote; na Anajua wafanyao

waja Wake kwa dhahiri na ya siri. Pia Anajua yanayoonekana na yaliyofichana; na Anajua ya siri na yaliyo zaidi ya siri. Anajua wanayofanya waja Wake kwa wazi na kwa siri, Naye Atawajazi (Atawalipa) kwa hayo madogo na makubwa. Na Kauli Yake:

وَإِنْ أَدْرَىٰ لَعَلَّهُ فِتْنَةٌ لَّكُمْ وَمَتَّبَعٌ إِلَىٰ حِينٍ ﴿١٠٤﴾

**“Wala sijui pengine huu ni mtihani tu kwenu na starehe mpaka muda kidogo.”**

Maana: Sijui, huenda huo ukawa ni mtihani kwenu na starehe kwa muda mfupi. Ibn Jariir رحمه الله تعالى amesema: “Huenda hiyo imecheleweshwa kwenu ni mtihani na starehe kwa muda maalumu”<sup>1</sup>. Na hii imezungumziwa na ‘Awn kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما. Na Allah تعالى Anajua zaidi. Na Kauli Yake:

قَالَ رَبِّ أَحْكُم بِالْحَقِّ ۗ

**“Akasema Yeye (Muhammad): Mola wangu Mlezi! Hukumu kwa haki.”**

Maana yake: Tuhukumu baina yetu na baina ya kaumu yetu walioikanusha haki. Amesema Qatadah: “Walikuwa Manabii wakisema:

رَبَّنَا أَفْتَحْ بَيْنَنَا وَبَيْنَ قَوْمِنَا بِالْحَقِّ وَأَنْتَ خَيْرُ الْفَاتِحِينَ ﴿١٠٥﴾

**‘Mola wetu Mlezi! Hukumu baina yetu na baina ya wenzetu hawa kwa haki, Nawe Ndiye Mbora wa wanaohukumu.’ (7:89)**

Na Mtume ﷺ aliamriwa kusema hayo pia”<sup>2</sup>. Na imeripotwa kutoka kwa Maalik bin Zayd bin Aslam رضي الله عنه: Alikuwa Mtume ﷺ anapohudhuria vita vyovyote vile, husema:

رَبِّ أَحْكُم بِالْحَقِّ ۗ

**“Mola wangu Mlezi! Hukumu kwa haki”.** Na Kauli Yake:

وَرَبُّنَا الرَّحْمَنُ الْمُسْتَعَانُ عَلَىٰ مَا تَصِفُونَ ﴿١٠٦﴾

**“Na Mola wetu Mlezi ni Mwingi wa Rehema, Aombwaye msaada juu ya mnayoyazua.”**

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:554.

<sup>2</sup> Ibn Abi Hatim (13766) Isnadi yake ni dhaifu.

Maana yake: Juu ya yale mengi wanayoyasema na kuzua kwao uongo, miongoni mwa aina mbali mbali za uzushi ambao unatofautiana uzito wake. Allah تعالی Ndiye Msaidizi wenu kwa hayo.

Huu ndio mwisho wa Tafsiri ya Suratul Ambiyaa. Sifa zote njema na Shukrani Anastahiki Allah تعالی.





# Tafsiri ya Suratul Hajj

## Sura ya 22

### Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

### سُورَةُ الْحَجِّ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ أَنْقُوا رَبِّكُمْ إِنَّ زَلْزَلَةَ السَّاعَةِ شَيْءٌ

عَظِيمٌ ۝ يَوْمَ تَرَوُنَّهَا تَذْهَلُ كُلُّ مُرْضِعَةٍ عَمَّا

أَرْضَعَتْ وَتَضَعُ كُلُّ ذَاتِ حَمَلٍ حَمْلَهَا وَتَرَى النَّاسَ

سُكَرَىٰ وَمَا هُمْ بِسُكَرَىٰ وَلَٰكِنَّ عَذَابَ اللَّهِ شَدِيدٌ ۝

وَمِنَ النَّاسِ مَنْ يُجَادِلُ فِي اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ وَيَتَّبِعُ كُلَّ

شَيْطَانٍ مَّرِيدٍ ۝ كُيِّبَ عَلَيْهِ أَنَّهُ مَن تَوَلَّاهُ فَأَنَّهُ يُضِلُّهُ

وَيَهْدِيهِ إِلَىٰ عَذَابِ السَّعِيرِ ۝

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ أَنْقُوا رَبِّكُمْ إِنَّ

زَلْزَلَةَ السَّاعَةِ شَيْءٌ عَظِيمٌ ۝

يَوْمَ تَرَوُنَّهَا تَذْهَلُ كُلُّ مُرْضِعَةٍ

عَمَّا أَرْضَعَتْ وَتَضَعُ كُلُّ ذَاتِ

حَمَلٍ حَمْلَهَا وَتَرَى النَّاسَ سُكَرَىٰ

وَمَا هُمْ بِسُكَرَىٰ وَلَٰكِنَّ عَذَابَ

اللَّهِ شَدِيدٌ ۝

1. Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi. Hakika tete-meko la Saa (ya Kiyama) ni jambo kuu.

2. Siku mtapoiona, kila mwenye kunyonyesha atamsahau amnyonyeshaye, na kila mwenye mimba ataharibu mimba yake. Na utaona watu wamelewa, na kumbe hawakulewa. Lakini adhabu ya Allah ni kali.

### Vitisho vya Saa (Kiyama)

Anasema Aliyetukuka huku Akiwaamuru waja Wake wamche Yeye, kwa Kuwaeleza yatakayowakabili katika vitisho vya Siku ya Kiyama ambacho kitakuja kwao na mitetemeko ya ardhi na vituko vyengine. Kama Allah تعالیٰ Anavyosema:

إِذَا زُلْزِلَتِ الْأَرْضُ زِلْزَالَهَا ۖ وَأُخْرِجَتِ الْأَرْضُ أَنْفَاقَهَا ۖ

**“Itakapotetemeshwa ardhi mtetemeko wake (mkubwa). Na itakapotoa ardhi mizigo yake.” (99:1-2)**

Amesema Aliyetukuka,

وَحُمِلَتِ الْأَرْضُ وَالْجِبَالُ فَدُكَّتَا دَكَّةً وَاحِدَةً ۖ فَيَوْمَئِذٍ وَقَعَتِ الْوَاقِعَةُ ۖ

**“Na ardhi na milima ikaondolewa na ikavunjwa mvunjo mmoja. Siku hiyo hilo tukio litakuwa limekwishatokea.” (69:14-15).**

Na Amesema Aliyetukuka:

إِذَا رُجَّتِ الْأَرْضُ رَجًا ۖ وَنُسَّتِ الْجِبَالُ بَسًا ۖ

**“Ardhi itakapotetemeshwa mtetemesho mkubwa. Na milima itakaposagwasagwa.” (56:4-5).**

Pakasemwa kuwa mitetemeko hii itatokea bila shida yoyote mwisho wa maisha ya dunia, mwanzo wa vitisho vya Kiyama. Na amesema Ibn Jariir رحمه الله تعالى: Amempokea ‘Alqamah akisema:

إِنَّ زَلْزَلَةَ السَّاعَةِ شَيْءٌ عَظِيمٌ ۖ

**“Hakika tetemeko la Saa (ya Kiyama) ni jambo kuu.”**

Maana yake: Kabla ya Kiyama<sup>1</sup>. Na wakasema wengine: “Bali hivyo ni vitisho, fadhaa, mitetemeko na balaa yatakayotokea Siku ya Kiyama katika uwanja (wa hukumu) baada ya kutoka makaburini. Na hii ndiyo iliyochaguliwa na Ibn Jariir رحمه الله تعالى akitoa dalili kwa Hadithi zifuatazo:

Amepokea Ahmad kutoka kwa Imraan bin Huswayn رضي الله عنه amesema kuwa pale Mtume ﷺ alipokuwa katika moja ya safari zake na baadhi ya Maswahaba walikuwa nyuma. Alinyanyua sauti yake na kusoma Aya hizi mbili:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:557.

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ آتِفُوا رَبِّكُمْ ۚ إِنَّ زَلْزَلَةَ السَّاعَةِ شَيْءٌ عَظِيمٌ ﴿١٠﴾ يَوْمَ تَرَوُنَّهَا تُذْهِلُ  
كُلُّ مُرْضِعَةٍ عَمَّا أَرْضَعَتْ وَتَضَعُ كُلُّ ذَاتِ حَمَلٍ حَمْلَهَا وَتَرَى النَّاسَ سُكَرَىٰ وَمَا  
هُم بِسُكَرَىٰ وَلَٰكِنَّ عَذَابَ اللَّهِ شَدِيدٌ ﴿١١﴾

**“Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi. Hakika tetemeko la Saa (ya Kiyama) ni jambo kuu. Siku mtapoiona, kila mwenye kunyonyesha atamsahau amnyonyeshaye, na kila mwenye mimba ataharibu mimba yake. Na utaona watu wamelewa, na kumbe hawakulewa. Lakini adhabu ya Allah ni kali.”**

Pindi Maswahaba wake waliposikia hilo walifanya haraka ili kumfikia kwani walijua kuwa alikuwa anataka kusema jambo. Walipofika, alisema:

«أَتَذُرُونَ أَيُّ يَوْمٍ ذَاكَ، ذَاكَ يَوْمٌ يُنَادَىٰ آدَمُ عَلَيْهِ السَّلَامُ، فَيَنَادِيهِ رَبُّهُ عَزَّ وَجَلَّ،  
فَيَقُولُ: يَا آدَمُ ابْعَثْ بَعَثَكَ إِلَى النَّارِ، فَيَقُولُ: يَا رَبِّ وَمَا بَعَثَ النَّارَ؟ فَيَقُولُ: مِنْ  
كُلِّ أَلْفٍ تِسْعِمِائَةٍ وَتِسْعَةَ وَتِسْعُونَ فِي النَّارِ، وَوَاحِدٌ فِي الْجَنَّةِ»

*“Je, mnaifahamu hiyo ni siku ipi? Hiyo ni siku ambayo Adam عليه السلام ataitwa. Mola wake Mlezi Atamuita na kusema: ‘Ewe Adam! Wapeleke Motoni katika kizazi chako walioandikiwa kuingizwa (huko)’. Naye akasema: ‘Ewe Mola wangu Mlezi! Ni wangapi watapelekwa Motoni?’ Atasema: ‘Kwa kila elfu, mia tisa na tisini na tisa (999) watapelekwa Motoni na mmoja ni wa Peponi’.*

Maswahaba wake walikufa moyo na kuacha kutabasamu. Alipoona hili, alisema:

«أُبَشِّرُوا وَاعْمَلُوا، فَرَأَى الَّذِي نَفْسُ مُحَمَّدٍ بِيَدِهِ إِنَّكُمْ لَمَعَ خَلِيقَتَيْنِ مَا كَانَتَا مَعَ شَيْءٍ؛  
فَطُ إِلا كَثْرَتَاهُ بِأَجُوجَ وَمَأْجُوجَ، وَمَنْ هَلَكَ مِنْ بَنِي آدَمَ وَبَنِي إِبْلِيسَ»

*‘Pateni bishara njema na fanyeni amali, naapa kwa Yule Ambaye nafsi ya Muhammad iko Mikononi Mwake, mtahukumiwa na viumbe aina mbili ambao ni wengi sana (kwa idadi), Yaa’juuju na Maa’juuju na wale ambao tayari wamepita (kufa) miongoni mwa kizazi cha Adam na kizazi cha Iblis’.*

Hapo walifurahi, kisha akasema:

«اعْمَلُوا وَأَبشُرُوا، فَوَالَّذِي نَفْسُ مُحَمَّدٍ بِيَدِهِ، مَا أَنْتُمْ فِي النَّاسِ إِلَّا كَالشَّامَةِ فِي  
جَنْبِ الْبَعِيرِ أَوْ الرُّمَةِ فِي ذِرَاعِ الدَّائِيَةِ»

*'Fanyeni amali na furahini, naapa kwa Yule Ambaye nafsi ya Muhammad iko Mikononi Mwake, kulinganisha na wanadamu nyinyi ni kama kiwaa cheusi (doa) kwenye ubavu wa ngamia au alama kwenye mguu wa mbele wa mnyama'<sup>1</sup>.*

Na hivyo ndivyo alivyopokea At-Tirmidhiy na An-Nasaa'iy katika mlango wa Tafsiri katika Sunan zao, na akasema At-Tirmidhiy kuwa hii ni Hadithi *Hasan Sahih*<sup>2</sup>.

### Maelezo Mengine ya Hadithi Hii

Amepokea At-Tirmidhiy kutoka kwa 'Imraan bin Huswayn رضى الله عنه kuwa pindi ilipotemshwa Aya ifuatayo,

يَتَأَيُّهَا النَّاسُ اتَّقُوا رَبَّكُمْ

***"Enyi watu! Mcheni Mola wenu Mlezi."***

Mpaka kwenye Usemi Wake:

وَلَكِنَّ عَذَابَ اللَّهِ شَدِيدٌ

***"Lakini adhabu ya Allah ni kali"***.

Mtume ﷺ alisema:

«أَتَذَرُونَ أَيُّ يَوْمٍ ذَلِكَ؟ قَالُوا: اللَّهُ وَرَسُولُهُ أَعْلَمُ. قَالَ: - ذَلِكَ يَوْمٌ يَقُولُ اللَّهُ  
لِأَدَمَ: ابْعَثْ بَعَثَ النَّارِ، قَالَ: يَا رَبِّ وَمَا بَعَثَ النَّارِ؟ قَالَ: تَشْعِمَانِي وَتَشْعَمُ  
وَتَسْعُونَ إِلَى النَّارِ وَوَاجِدُ إِلَى الْجَنَّةِ»

*"Je, mnaifahamu hiyo ni siku ipi?" Wakasema: "Allah na Mtume Wake wanajua zaidi". Akasema: "Hiyo ni siku ambayo Allaah*

<sup>1</sup> Ahmad 4:435.

<sup>2</sup> Tuhfatul al-Ahwadhiy 9:12 na An-Nasaa'iy katika Al-Kubraa 6:410.

Atamuambia Adam: "Wapeleke Motoni katika kizazi chako walioandikiwa kuingizwa (huko)". Naye akasema: "Ewe Mola wangu Mlezi! Ni wangapi watapelekwa Motoni?" Akasema: "Mia tisa na tisini na tisa (999) watapelekwa Motoni na mmoja ni wa Peponi".

Waislamu walianza kulia, kisha Mtume ﷺ akasema:

«قَارِبُوا وَسَدُّوا، فَإِنَّمَا لَمْ تَكُنْ نُبُوَّةً فَطَّ إِلَّا كَانَ بَيْنَ بَدَنِيهَا جَاهِلِيَّةً، قَالَ: نَيْرِخَدُ الْعَدْدُ مِنَ الْجَاهِلِيَّةِ، فَإِنْ تَمَّتْ، وَإِلَّا كُمَلْتُمْ مِنَ الْمُتَأَيِّبِينَ، وَمَا مَثَلُكُمْ وَمَثَلُ الْأَنْسَامِ إِلَّا كَمَثَلِ الرَّقْمَةِ فِي ذِرَاعِ الدَّابَّةِ، أَوْ كَالشَّامَةِ فِي جَنْبِ الْبَعِيرِ»

"Karibianeni na kuweni imara, kwani hakukuwa na Nabii ila kulikuwa baina yake ujahiliya (ujinga) kabla ya kuja kwake. Akasema: Kwa hiyo idadi fulani itachukuliwa miongoni mwa wakati wa ujinga, na ikiwa haitoshi, itatimizwa kutokana na wanafiki. Na mfano wenu kulinganishwa na kaumu nyingine ni kuwa mutakuwa kama alama kwenye mguu wa mbele wa mnyama, au kiwaa cheusi (doa) ubavuni mwa ngamia".

Kisha akasema:

«إِنِّي لَأَرْجُو أَنْ تَكُونُوا رُبُعَ أَهْلِ الْجَنَّةِ»

"Hakika mimi natarajia kuwa mutakuwa robo (1/4) ya watu wa Peponi".

Wakasema: "Allahu Akbar (Allah ni Mkubwa)". Kisha akasema:

«إِنِّي لَأَرْجُو أَنْ تَكُونُوا ثُلُثَ أَهْلِ الْجَنَّةِ»

"Hakika mimi natarajia kuwa mtakuwa thuluthi (1/3) ya watu wa Peponi".

Wakasema: "Allahu Akbar". Kisha akasema:

«إِنِّي لَأَرْجُو أَنْ تَكُونُوا نِصْفَ أَهْلِ الْجَنَّةِ»

"Hakika mimi natarajia kuwa mutakuwa nusu (1/2) ya watu wa Peponi".

Wakasema: "Allahu Akbar". Kisha yeye (mpokezi) akasema: "Sijui kama alisema thuluthi mbili (2/3) au hakusema"<sup>1</sup>.

Hadithi pia ilinukuliwa na Imaam Ahmad<sup>2</sup>. Kisha at-Tirmidhiy akasema: "Hii ni Hadith *Hasan Sahih*." Katika kuitafsiri Aya hii, Imamu Bukhari amenukuu kutoka kwa Abii Said رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ amesema;

«يَقُولُ اللَّهُ تَعَالَى يَوْمَ الْقِيَامَةِ: يَا آدَمُ، قِيْلُ لَكَ رَبَّنَا وَسَعْدَيْكَ، فَبَدَأَ بِصَوْتٍ: إِنَّ اللَّهَ بِأَمْرِكَ أَنْ تُخْرِجَ مِنْ دُرِّيَّتِكَ بَنَاتًا إِلَى النَّارِ، قَالَ: يَا رَبِّ وَمَا بَعَثَ النَّارَ؟ قَالَ: مِنْ كُلِّ أَنْفٍ - أَرَاهُ قَالَ - تِسْعِمَائَةٍ وَتِسْعَةٌ وَتِسْعُونَ، فَجِيئَ تَصْعُ الْحَائِلِ حَمَلَهَا وَنَسِيبُ الْوَالِدِ وَوَرَى النَّاسِ سُكْرَى وَمَا هُمْ بِسُكْرَى وَلَكِنَّ عَذَابَ اللَّهِ شَدِيدٌ»

"Allah Aliyetukuka Atasema siku ya Kiama: 'Ewe Adamu!' Atasema: 'Nimekuitikia Ewe Mola wetu.' Sauti ya anayenadi itasema: 'Hakika Allah Anakuamuru kuwapeleka Motoni katika kizazi chako kilichoandikiwa kwenda huko.' Adamu atasema: 'Ewe Mola wangu, ni wangapi watu hao?' Allah Atasema: 'Katika elfu moja - ninafikiri, alisema mia tisa na tisini na tisa. Siku hiyo mja mzito atajifungua, na kijana atazeeka. **"Na utaona wamelewa kumbe hawakulewa, lakini adhabu ya Mwenyezi Mungu ni kali."**

Na jambo hilo lilikuwa zito kwa watu kiasi cha kuzibadili nyuso zao, Mtume ﷺ amesema:

«مِنْ يَأْجُوجَ وَمَأْجُوجَ تِسْعِمَائَةٍ وَتِسْعَةٌ وَتِسْعُونَ، وَمِنْكُمْ وَاحِدٌ، أَنْتُمْ فِي النَّاسِ كَالشُّعْرَةِ السُّودَاءِ فِي جَنْبِ الثَّوْرِ الْأَبْيَضِ، أَوْ كَالشُّعْرَةِ الْبَيْضَاءِ فِي جَنْبِ الثَّوْرِ الْأَسْوَدِ، وَإِنِّي لَأَرْجُو أَنْ تَكُونُوا رُبْعَ أَهْلِ الْجَنَّةِ، فَكَبَّرْنَا. ثُمَّ قَالَ: ثَلَاثُ أَهْلِ الْجَنَّةِ، فَكَبَّرْنَا. ثُمَّ قَالَ: شَطْرُ أَهْلِ الْجَنَّةِ، فَكَبَّرْنَا»

"Mia tisa na tisini na tisa kutoka kwa Yaa'juuju na Maa'juuju na mmoja kutoka kwenu. Nyinyi miongoni mwa wanadamu ni kama

<sup>1</sup> Tuhfatul Al-Ahwadhiy 9:9. Isnadi yake ni dhaifu.

<sup>2</sup> Ahmad 4:432.

nywele nyeusi kwenye upande (ubavuni) wa fahali mweupe au nywele nyeupe ubavuni mwa fahali mweusi. Natumai kuwa nyinyi mutakuwa robo ya watu wa Peponi". Hapo tulisema: "Allahu Akbar". Kisha akasema: "Thuluthi ya watu wa Peponi". Tukasema: "Allahu Akbar". Kisha akasema: "Nusu ya watu wa Peponi". Tukasema: "Allahu Akbar."<sup>1</sup>

Hii imenukuliwa na Bukhaariy katika sehemu nyingine.<sup>2</sup> Pia imenukuliwa na Muslim na An-Nasaa'iy katika Tafsiri yake.<sup>3</sup>

Hadithi na ripoti kuhusiana na vitisho vya Siku ya Kiyama ni nyingi mno na hapa si mahali pa kuzinukuu zote hizo. Kwa hiyo, Allah تعالى Akasema:

إِنَّ زَلْزَلَةَ السَّاعَةِ شَيْءٌ عَظِيمٌ ﴿١﴾

**"Hakika tetemeko la Saa (ya Kiyama) ni jambo kuu."**

Maana yake: Ni jambo kubwa, wasiwasi wenye kutisha na tukio lenye kuogofya. Tetemeko ni lile litakalotokea kwa watu watakapojawa na woga na wasiwasi, kama Alivyosema Allah تعالى:

هَنَالِكِ أَبْتُلَى الْمُؤْمِنُونَ وَزُلْزِلُوا زِلْزَالًا شَدِيدًا ﴿١﴾

**"Hapo Waislamu walitiwa mtihani na wakatetemeshwa kwa matetemesho makali." (33:11)**

Kisha Akasema:

يَوْمَ تَرَوْنَهَا تَذْهَلُ كُلُّ مُرْضِعَةٍ عَمَّا أَرْضَعَتْ

**"Siku mtakapokiona Kiama Kila mwenye kunyonyesha atamsahau amnyonyeshaye."**

Maana yake: Atashughulishwa kwa atakayoyaona katika vitisho, jambo ambalo litamfanya awasahau walio karibu na vipenzi vyake kwake na anaowaonea

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baariy 8:295.

<sup>2</sup> Fat'h Al-Baariy 6:440.

<sup>3</sup> Muslim 1:201 na An-Nasaa'iy katika Al-Kubraa 6:409.

upole na huruma kabisa. Mshtuko wake utamfaya amuwache mtoto katika hali ya kumnyonyesha, Allah تعالى Anasema:

كُلُّ مُرْضِعَةٍ

**“Kila mwenye kunyonyesha.”**

Wala Hajasema mama mwenye mtoto mchanga wa kunyonyeshwa. Na Amesema:

عَمَّا أَرْضَعَتْ

**“Amnyonyeshaye.”**

Maana yake: Mtoto wake amnyonyeshaye ambaye hajaachishwa kunyonya. Na Kauli Yake:

وَتَضَعُ كُلُّ ذَاتِ حَمْلٍ حَمْلَهَا

**“Na kila mwenye mimba ataharibu mimba yake.”**

Maana yake: Kabla ya ujauzito kufikia muda wake kwa sababu ya ukali na ukubwa wa vitisho vyake.

وَتَرَى النَّاسَ سُكَرَىٰ

**“Na utaona watu wamelewa.”**

Na pia inasomwa: “Sakraa”, Maana yake: Kwa uzito wa hali yenyewe, pale watakapopoteza akili na kufinikwa masikio yao kwa jinsi ambayo kila awaonaye atadhani kuwa wamelewa.

وَمَا هُمْ بِسُكَرَىٰ وَلَٰكِنَّ عَذَابَ اللَّهِ شَدِيدٌ

**“Na kumbe hawakulewa. Lakini adhabu ya Allaah ni kali.”**

وَمِنَ النَّاسِ مَن تَجَدَّلُ فِي اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ وَتَتَّبِعُ كُلَّ شَيْطَانٍ مَّرِيدٍ ﴿٢٠﴾ كَتَبَ عَلَيْهِ أَنَّهُ

مَنْ تَوَلَّاهُ فَأَنَّهُ يُضِلُّهُ وَيَهْدِيهِ إِلَىٰ عَذَابِ السَّعِيرِ ﴿٢١﴾

**3. Na miongoni mwa watu wapo wanaobishana juu ya Allah bila ya elimu, na wanamfuata kila shetani aliye asi.**



**4. Ameandikiwa kwamba anayemfanya kuwa rafiki, basi huyo hakika atampoteza na atamuongoza kwenye adhabu ya Moto mkali.**

### **Kushutumiwa kwa Wafuasi wa Shetani**

Allah تعالى Anawashutumu wenye kukataa Ufufuo na wenye kukataa kuwa Allah تعالى ni Muweza Kufufua maiti, wenye kukengeuka kwa aliyoyateremsha Allah kwa Mitume wake kumfuata kila shetani aliyekengeuka miongoni mwa wanadamu na majini. Hii ni hali ya wafuasi wa uzushi na upotevu, wanaokengeuka na haki na kufuata batili, huacha aliyoteremsha Allah تعالى kwa Mtume wake miongoni mwa haki iliyo wazi na kufuata maneno ya viongozi wa upotevu wenye kuwaita watu kufuata uzushi, matamano yao na rai zao. Allah تعالى Anasema kuhusiana nao na mfano wao:

وَمِنَ النَّاسِ مَن يُجَادِلُ فِي اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ

**“Na miongoni mwa watu wapo wanaobishana juu ya Allah bila ya elimu.”**

Maana yake: Elimu iliyo sawa na sahihi.

وَيَتَّبِعُ كُلَّ شَيْطَانٍ مَّرِيدٍ ﴿١٠﴾ كُتِبَ عَلَيْهِ

**“Na wanamfuata kila shetani aliye asi. Ameandikiwa.”**

Amesema Mujaahid: “Hii ina maana ya shetani”<sup>1</sup>. Maana yake: Hilo ni jambo lililokadiriwa.

أَنَّهُمْ مِّن تَوَلَّاهُ

**“Kwamba anayemfanya kuwa rafiki.”**

Maana yake: Anamfuata na kumuiga.

فَأَنَّهُمْ يُضِلُّهُمُ وَيَهْدِيهِ إِلَىٰ عَذَابِ السَّعِيرِ ﴿١١﴾

**“Basi huyo hakika atampoteza na atamuongoza kwenye adhabu ya Moto mkali.”**

<sup>1</sup> Al-Muharrar Al-Wajiz 4:107.

Maana yake: Atampoteza katika dunia hii na Siku ya Akhera atampeleka katika adhabu kali, kwenye Moto usioweza kuvumilika, uchungu na kuumiza sana. Na hakika amepokea As-Suddiy kuwa Abi Maalik amesema: "Aya hii iliteremshwa kuhusu An-Nadhwr bin Al-Haarith"<sup>1</sup>. Na hivyo ndivyo alivyosema Ibn Jurayj<sup>2</sup>.



---

<sup>1</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 6:8.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:566.

يَتَأَيُّهَا النَّاسُ إِن كُنْتُمْ فِي رَيْبٍ مِّنْ أَلْبَعَثِ فَإِنَّا خَلَقْنٰكُمْ  
 مِّن تَرَابٍ ثُمَّ مِّن نُّطْفَةٍ ثُمَّ مِّن عَلَقَةٍ ثُمَّ مِّن مُّضْغَةٍ مُّخَلَّقَةٍ  
 وَغَيْرِ مُخَلَّقَةٍ لِّنُبَيِّنَ لَكُمْ<sup>ط</sup> وَنُقِذُوا فِي الْأَرْحَامِ مَا نَشَاءُ إِلَىٰ أَجَلٍ  
 مُّسَمًّى ثُمَّ نُخْرِجُكُمْ طِفْلًا ثُمَّ لِيَتَلَفَعُوا أَشْدَّكُمْ<sup>ط</sup>  
 وَمِنْكُمْ مَّن يُتَوَفَّىٰ وَمِنْكُمْ مَّن يُرَدُّ إِلَىٰ أَرْذَلِ الْعُمُرِ  
 لِكَيْلَا يَعْلَمَ مِن بَعْدِ عِلْمٍ شَيْئًا<sup>ط</sup> وَتَرَىٰ الْأَرْضَ هَامِدَةً  
 فَإِذَا أَنْزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَاءَ اهْتَزَّتْ وَرَبَّتْ وَأَبْتَتَتْ مِنْ كُلِّ  
 رَوْحٍ بَهيجٍ ﴿٥﴾ ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ وَأَنَّهُ يُخَيِّ الْمَوْتَىٰ  
 وَأَنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٦﴾ وَأَنَّ السَّاعَةَ آتِيَةٌ لَا رَيْبَ  
 فِيهَا وَأَنَّ اللَّهَ يَبْعَثُ مَنْ فِي الْقُبُورِ ﴿٧﴾ وَمِنَ النَّاسِ مَن  
 يُجَادِلُ فِي اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ وَلَا هُدًى وَلَا كِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿٨﴾  
 ثَانِي عَطْفِهِ لِيُضِلَّ عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ لَهُ فِي الدُّنْيَا خِزْيٌ<sup>ط</sup>  
 وَنُذِيقُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَذَابَ الْحَرِيقِ ﴿٩﴾ ذَٰلِكَ بِمَا  
 قَدَّمْتَ يَدَاكَ وَأَنَّ اللَّهَ لَيْسَ بِظَلِيمٍ لِّلْعَبِيدِ ﴿١٠﴾ وَمِنَ  
 النَّاسِ مَن يَعْبُدُ اللَّهَ عَلَىٰ حَرْفٍ فَإِنْ أَصَابَهُ خَيْرٌ اطْمَأَنَّ  
 بِهِ<sup>ط</sup> وَإِنْ أَصَابَتْهُ فِتْنَةٌ أُنْقَلَبَ عَلَىٰ وَجْهِهِ خَسِرَ الدُّنْيَا  
 وَالْآخِرَةَ<sup>ط</sup> ذَٰلِكَ هُوَ الْخُسْرَانُ الْمُبِينُ ﴿١١﴾ يَدْعُوا مِن  
 دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَضُرُّهُ وَمَا لَا نَفْعَ لَهُ<sup>ط</sup> ذَٰلِكَ هُوَ الضَّلَالُ  
 الْبَعِيدُ ﴿١٢﴾ يَدْعُوا لَمَن ضُرُّهُ أَقْرَبُ مِن نَّفْعِهِ<sup>ط</sup> لَيْسَ  
 الْمَوْلَىٰ وَلَيْسَ الْعَشِيرُ ﴿١٣﴾

يَتَأَيُّهَا النَّاسُ إِن كُنْتُمْ فِي رَيْبٍ مِّنْ  
 أَلْبَعَثِ فَإِنَّا خَلَقْنٰكُمْ مِّن تَرَابٍ ثُمَّ  
 مِّن نُّطْفَةٍ ثُمَّ مِّن عَلَقَةٍ ثُمَّ مِّن  
 مُّضْغَةٍ مُّخَلَّقَةٍ وَغَيْرِ مُخَلَّقَةٍ لِّنُبَيِّنَ لَكُمْ<sup>ط</sup>  
 وَنُقِذُوا فِي الْأَرْحَامِ مَا نَشَاءُ إِلَىٰ أَجَلٍ  
 مُّسَمًّى ثُمَّ نُخْرِجُكُمْ طِفْلًا ثُمَّ  
 لِيَتَلَفَعُوا أَشْدَّكُمْ<sup>ط</sup> وَمِنْكُمْ مَّن  
 يُتَوَفَّىٰ وَمِنْكُمْ مَّن يُرَدُّ إِلَىٰ أَرْذَلِ  
 الْعُمُرِ لِكَيْلَا يَعْلَمَ مِن بَعْدِ عِلْمٍ  
 شَيْئًا<sup>ط</sup> وَتَرَىٰ الْأَرْضَ هَامِدَةً فَإِذَا  
 أَنْزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَاءَ اهْتَزَّتْ وَرَبَّتْ  
 وَأَبْتَتَتْ مِنْ كُلِّ رَوْحٍ بَهيجٍ ﴿٥﴾  
 ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ وَأَنَّهُ يُخَيِّ  
 الْمَوْتَىٰ وَأَنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٦﴾  
 وَأَنَّ السَّاعَةَ آتِيَةٌ لَا رَيْبَ فِيهَا  
 وَأَنَّ اللَّهَ يَبْعَثُ مَنْ فِي الْقُبُورِ ﴿٧﴾

5. Enyi watu! Ikiwa nyinyi  
 muna shaka ya kufufuliwa  
 basi kwa hakika Sisi  
 Tulikuumbeni kutokana na  
 udongo, kisha kutokana na  
 mchanganyiko wa mbegu

*ya uzazi, kisha kutokana na kipande cha damu iliogandana, kisha kutokana na kipande cha nyama chenye umbo na kisichokuwa na umbo, ili Tukubainishieni. Nasi Tunakiweka katika matumbo ya uzazi Tunachokitaka mpaka muda uliowekwa. Kisha Tunakutoeni kwa hali ya mtoto mchanga, kisha mfikie kutimia akili. Na wapo katika nyinyi wanaokufa, na wapo katika nyinyi wanaorudishwa kwenye umri wa unyonge kabisa, hata mtu awe hajui kitu baada ya kuwa anakijua. Na unaiona ardhi imetulia kimya, lakini Tunapoyateremsha maji juu yake husisimka na kututumka, na kumea kila namna ya mimea mizuri.*

**6. Hayo ni kwa sababu hakika Allah Ndiye Haki, na kwamba hakika Yeye Ndiye Mwenye Kuhuisha wafu, na kwamba hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.**

**7. Na kwamba hakika Saa itakuja hapana shaka kwa hilo, na kwamba hakika Allah Atawafufua walio makaburini.**

### **Ushahidi wa Kufufuliwa Katika Kuumbwa Binadamu na Mimea**

Pale Allah تعالى Alipomtaja mwenye kukanusha ufufuo na mwenye kupinga kiama. Pia Ametaja dalili ya Nguvu Zake na Uweza Wake wa Kufufua ambao unaonekana kutokana na njia ya jinsi Anavyoanzisha Uumbaji. Akasema:

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ إِنْ كُنْتُمْ فِي رَيْبٍ مِّنَ الْبَعْثِ

**“Enyi watu! Ikiwa nyinyi muna shaka ya kufufuliwa”.**

Maana yake: Katika shaka, “Ya kufufuliwa”, nayo miadi, na kusimama roho na miili, Siku ya Kiyama.

فَإِنَّا خَلَقْنَاكُمْ مِّنْ تُرَابٍ

**“Basi kwa hakika Sisi Tulikuumbeni kutokana na udongo”.**

Maana yake: Asili na chanzo chenu ni kuumbwa na mchanga (vumbi), nayo ni ile asili ambayo aliumbiwa kwayo Adam عليه السلام.

ثُمَّ مِّنْ نُطْفَةٍ

**“Kisha kutokana na mchanganyiko wa mbegu ya uzazi (Nutfah)”.** Maana: Kisha Akakifanya kizazi chake kutokana na mchujo wa maji yaliyo dhalili.

**Hatua za Ukuaji wa Tone la Manii Katika Mfuko wa Uzazi**

ثُمَّ مِنْ عَلَقَةٍ ثُمَّ مِنْ مُضْغَةٍ

***“Kisha kutokana na kipande cha damu iliogandana (‘Alaqah), kisha kutokana na kipande cha nyama chenye umbo (Mudhwghah).”***

Na hilo ni kuwa pale tone la manii linapodondoka katika mfuko wa uzazi wa mwanamke, inabaki katika hali hiyo kwa muda wa siku arobaini, na kuongezwa vitu juu yake, hadi linabadilika kuwa “Alaqah” pande jekundu la damu (lenye kunin’ginia) kwa idhini ya Allah تعالى, na kinabaki katika hali hiyo kwa muda wa siku arobaini. Baadaye linabadilika na kuwa nofu la nyama: kipande cha nyama kisichokuwa na umbile wala muundo wa aina yoyote ile. Kisha kinaanza kuchukua umbile na muundo fulani, kichwa, mikono, kifua, tumbo, mapaja, miguu na viungo vingine vinaanza kukua. Wakati mwingine mwanamke anaharibu mimba kabla ya kijusi kukamilika kimaumbile na wakati mwingine anaharibu baada ya umbile kukamilika. Kwa ajili hiyo, Akasema Aliyetukuka:

ثُمَّ مِنْ مُضْغَةٍ مُخَلَّقَةٍ وَعَجْرٍ مُخَلَّقَةٍ

***“Kisha kutokana na kipande cha nyama chenye umbo (lililo kamilika) na kisichokuwa na umbo (Yaani lisilo kamilika).”***

Maana yake: Kama mnavyoshuhudia.

لِنَبِّئَنَّ لَكُمْ وَنُقَرُّ فِي الْأَرْحَامِ مَا نَشَاءُ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى

***“Ili Tukubainishieni. Nasi Tunakiweka katika matumbo ya uzazi tunachokitaka mpaka muda uliowekwa.”***

Maana yake: Wakati mwingine kijusi kinabaki katika mji wa uzazi bila kutoka na kuharibika. Hii ni kama alivyosema Mujahid kuhusu Kauli ya Aliyetukuka:

مُخَلَّقَةٍ وَعَجْرٍ مُّخَلَّقَةٍ

***“Chenye umbo na kisichokuwa na umbo.”*** Akasema: “Nacho ni kijusi chenye umbo na kisichokuwa na umbo. Zinapopita siku arobaini na kuwa kipande cha nyama, Allah تعالى Anamtuma Malaika, anayempulizia roho na humuunda kama Anavyotaka Allah تعالى, mzuri au mbaya, mwanamume au mwanamke, na kumuandikia riziki na ajali yake, na kama ni mwema au muovu”.

Hii ni kama ilivyothibiti katika Sahihi mbili kutoka kwa Ibn Mas'ud رضي الله عنه kwamba: Ametuzungumzia Mtume ﷺ naye ndiye Msema kweli wa kusadikika:

«إِنَّ خَلْقَ أَحَدِكُمْ يُجْمَعُ فِي بَطْنِ أُمِّهِ أَرْبَعِينَ لَيْلَةً، ثُمَّ يَكُونُ عَلَقَةً مِثْلَ ذَلِكَ، ثُمَّ يَكُونُ مُضْغَةً مِثْلَ ذَلِكَ، ثُمَّ يَبْعَثُ اللَّهُ إِلَيْهِ الْمَلَكَ فَيُؤَمِّرُ بِأَرْبَعِ كَلِمَاتٍ: يَكْتَبُ رِزْقَهُ وَعَمَلَهُ وَأَجَلَهُ، وَشَقِيئِي أَوْ سَعِيدِي، ثُمَّ يُنْفَخُ فِيهِ الرُّوحُ»

*“Hakika kila mmoja katika nyinyi hukusanywa umbo lake katika tumbo la mamake kama mchanganyiko wa mbegu ya uzazi kwa muda wa siku arobaini; kisha kipande cha damu kwa muda kama huo; kisha kipande cha nyama kwa muda kama huo. Kisha hutumwa Malaika na akaamrisha mambo mane: Kuandika riziki yake, ajali yake, amali yake, na kama ni mwema au muovu. Kisha humpulizia roho ndani yake”<sup>1</sup>.*

## Hatua za Ukuaji wa Mwanadamu Kutoka Utoto Hadi Utuuzima

Na Kauli Yake:

ثُمَّ نُخْرِجُكُمْ طِفْلًا

**“Kisha Tunakutoeni katika hali ya mtoto mchanga”.**

Maana yake: Dhaifu katika mwili wake, masikizi na uoni wake, hisia zake, nguvu na akili yake. Kisha Allah تعالى Anampatia nguvu kidogo kidogo na Huwafanya wazazi wake wawe wapole kwake na kumpenda usiku na mchana. Kwa hiyo, Akasema:

ثُمَّ لَتَبْلُغُوا أَشَدَّكُمْ

**“Kisha mufikie kutimia akili”.**

Maana yake: Kutimia na kukamilika nguvu na kuzidi mpaka anafika uchangamfu wa ujana na uzuri wa maumbile.

وَمِنْكُمْ مَنْ يُتَوَفَّى

**“Na wapo katika nyinyi wanaokufa”.**

Maana yake: Katika ujana wao na nguvu.

<sup>1</sup> Fat'hul Al-Baariy 6:418 na Muslim 4:2036.

وَمِنْكُمْ مَّن يُرَدُّ إِلَىٰ أَرْذَلِ الْعُمُرِ

**“Na wapo katika nyinyi wanaorudishwa kwenye umri wa unyonge kabisa.”**

Maana yake: Ukongwe na uzee, na udhaifu wa nguvu, akili na fahamu, na kushuka polepole ufahamu, uzulufu na udhaifu wa fikra. Kwa hiyo, Akasema:

لِكَيْلَا يَعْلَمَ مِن بَعْدِ عِلْمٍ شَيْئًا

**“Hata mtu awe hajui kitu baada ya kuwa anakijua.”**

Hii ni kama Allah تعالى Alivyosema:

✽ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِّن ضَعْفٍ ثُمَّ جَعَلَ مِن بَعْدِ ضَعْفٍ قُوَّةً ثُمَّ جَعَلَ مِن بَعْدِ قُوَّةٍ

ضَعْفًا وَشَيْبَةً يَخْلُقُ مَا يَشَاءُ وَهُوَ الْعَلِيمُ الْقَدِيرُ ﴿٥٤﴾

**“Allah Ndiye Aliyekuumbeni katika udhaifu, na baada ya udhaifu Akafanya nguvu, kisha baada ya nguvu Akaufanya udhaifu na uzee. Anaumba Apendavyo; Naye ni Mjuzi, Mwenye Uweza.” (30:54).**

### Mfano Mwingine wa Ufufuo Kutoka katika mimea

Na Kauli Yake:

وَتَرَى الْأَرْضَ هَامِدَةً

**“Na unaiona ardhi imetulia kimya”.**

Hii ni dalili nyingine juu ya Uweza na Nguvu za Allah تعالى katika Kuhuisha maiti kama Anavyoihuisha ardhi iliyokufa na kutulia. Nayo ni ile ardhi isiyo na uhai, ambayo hakuna kinachomea ndani yake. Amesema Qataadah: “Iliyo momonyoka, ardhi yenye vumbi”. Na amesema As- Suddiy: “Iliyokufa”.

فَإِذَا أَنْزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَاءَ اهْتَزَّتْ وَرَبَّتْ وَأَبْتَتَ مِن كُلِّ رَوْحٍ بِهِجٍ ﴿٥٥﴾

**“Lakini Tunapoyateremsha maji juu yake husisimka nakututumka, na kumea kila namna ya mimea mizuri.”**

Maana: Allah تعالى Anapoiteremshia mvua, **“Husisimka.”** Maana: Mimea huanza kumea, na kuhuika baada ya kufa kwake. **“Na kututumka”** Maana:

Inanyanyuka baada ya kutulia ndani yake, kisha humea kwayo aina tofauti ya matunda, mazao na mimea yenye rangi, ladha, harufu, umbile na manufaa tofauti. Kwa hilo, Anasema Aliyetukuka:

وَأُنَبِّتُ مِنْ كُلِّ رَوْحٍ بِهِيجٍ ﴿٥﴾

**“Na kumea kila namna ya mimea mizuri.”**

Maana yake: Umbo zuri na harufu nzuri. Na Kauli Yake:

ذَلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ

**“Hayo ni kwa sababu hakika Allah Ndiye Haki.”**

Maana yake: Muumbaji, Mwenye Kudhibiti, Mwenye Kufanya Atakalo.

وَأَنَّهُ سَمِيُّ الْمَوْتَىٰ

**“Na kwamba hakika Yeye Ndiye Mwenye Kuhuisha wafu.”**

Maana: Kama Alivyoihuisha ardhi iliyokufa na kumea kwayo aina mbalimbali za mimea.

إِنَّ الَّذِي أَحْيَاهَا لَمُعِي الْمَوْتَىٰ إِنَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٦﴾

**“Bila ya shaka Aliyehiusha ardhi Ndiye Atakayehiusha wafu. Hakika Yeye ni Muweza wa kila kitu.” (41:39)**

إِنَّمَا أَمْرُهُ إِذَا أَرَادَ شَيْئًا أَنْ يَقُولَ لَهُ كُنْ فَيَكُونُ ﴿٧﴾

**“Hakika Amri Yake Anapotaka kitu ni Kukiambia tu: Kuwa! Na kikawa.” (36:82)**

وَأَنَّ السَّاعَةَ آتِيَةٌ لَا رَيْبَ فِيهَا

**“Na kwamba hakika Saa ya kiyama itafika, hapana shaka kabisa kuhusu hiyo.”**

Maana yake: Bila shaka yoyote itafika.

وَأَنَّ اللَّهَ يَبْعَثُ مَنْ فِي الْقُبُورِ ﴿٨﴾

**“Na kwamba hakika Allah Atawafufua walio makaburini.”**



Maana yake: Atawarudisha katika uhai baada ya kuwa kwenye makaburi wakiwa mchanga; Atawaumba tena kwa mara nyingine baada ya kuwa si chochote.

Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَضَرَبَ لَنَا مَثَلًا وَنَسِيَ خَلْقَهُ ۗ قَالَ مَنْ يُحْيِي الْعِظْمَ وَهِيَ رَمِيمٌ ﴿٧٨﴾ قُلْ يُحْيِيهَا الَّذِي أَنْشَأَهَا أَوَّلَ مَرَّةٍ ۗ وَهُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيمٌ ﴿٧٩﴾ الَّذِي جَعَلَ لَكُم مِّنَ الشَّجَرِ الْأَخْضَرِ نَارًا ۗ فَإِذَا أُنْتَمِتُمْ مِثْلَهُ تُوَفَّدُونَ ﴿٨٠﴾

*“Na Akatupigia mfano, na akasahau Kuumbwa kwake akasema: ‘Nani atakayeihisha mifupa na hali imesagika?’ Sema: ‘Ataihu isha Yule Aliyeiumba mara ya kwanza, Naye ni Mjuzi wa kila namna ya Kuumba. Ambaye Amekufanyieni moto katika mti mbichi, mkawa nanyi kwa mti huo mnauwasha.” (36:78-80)*

Na Aya katika mada hii ni nyingi sana. Imekuja,

وَمِنَ النَّاسِ مَن يُجَادِلُ فِي اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ وَلَا هُدًى وَلَا كِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿٨١﴾ ثَانِي عِطْفِهِ ۗ لِيُضِلَّ عَن سَبِيلِ اللَّهِ ۗ لَهُ فِي الدُّنْيَا خِزْيٌ ۗ وَنُذِيقُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَذَابَ الْحَرِيقِ ﴿٨٢﴾ ذَٰلِكَ بِمَا قَدَّمْتَ يَدَاكَ وَأَنَّ اللَّهَ لَيْسَ بِظَلْمٍ لِّلْعَبِيدِ ﴿٨٣﴾

**8. Na katika watu wapo wanaobishana juu ya Allah bila ya elimu, wala uongofu, wala Kitabu chenye nuru.**

**9. Anayegeuza shingo yake ili kupoteza watu waache njia ya Allah. Duniani atapata hizaya, na Siku ya Kiyama Tutamuonjesha adhabu ya kuunguza.**

**10. (Ataambiwa): Hayo ni kwa sababu ya iliyotanguliza mikono yako. Na hakika Allaah si dhalimu kwa waja.**

## Kubainishwa Hali ya Viongozi wa Uzushi na Wale Waliowaongoza katika Upotevu

Alipotaja Aliyetukuka hali ya wapotevu wajinga wenye kuiga katika Kauli Yake:

وَمِنَ النَّاسِ مَن يُجَادِلُ فِي اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ وَيَتَّبِعُ كُلَّ شَيْطَانٍ مَّرِيدٍ ﴿٥١﴾

***“Na miongoni mwa watu wapo wanaobishana juu ya Allah bila ya elimu, na wanamfuata kila shetani aliye asi.”***

Ametaja katika hali hii walinganizi wa upotevu miongoni mwa viongozi wa ukafiri na uzushi. Akasema:

وَمِنَ النَّاسِ مَن يُجَادِلُ فِي اللَّهِ بِغَيْرِ عِلْمٍ وَلَا هُدًى وَلَا كِتَابٍ مُّبِينٍ ﴿٥٢﴾

***“Na katika watu wapo wanaobishana juu ya Allah bila ya elimu, wala uongofu, wala Kitabu chenye nuru.”***

Maana yake: Bila akili ya sawa wala andiko lililo sahihi na la wazi, bali kulingana na rai na matamano.

Na Kauli Yake:

ثَانِي عَطْفِهِ

***“Anayegeuza shingo yake.”***

Amesema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما na wengineo: “Kuwa na kiburi katika kufuata haki anapoitwa kwayo”<sup>1</sup>.

Na amesema Mujaahid, Qataadah na Malik kutoka kwa Zayd bin Aslam:

ثَانِي عَطْفِهِ

***“Anayegeuza shingo yake.”***

Maana yake: Kuigeuza shingo yake, anakengeuka kwa anayoitiwa katika haki, na kuikunja shingo yake kwa kiburi”. Kama Kauli Yake:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:573.

وَفِي مُوسَى إِذْ أَرْسَلْنَاهُ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ بِسُلْطٰنٍ مُّبِينٍ ﴿٣٨﴾ فَتَوَلَّىٰ بِرُكْبٰهٖ

**“Na katika habari za Musa, Tulipompeleka kwa Firauni na hoja wazi kabisa. Lakini akakengeuka kwa nguvu zake...” (51:38-39).**

Na Amesema Aliyetukuka:

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا إِلَىٰ مَا أَنْزَلَ اللَّهُ وَإِلَىٰ الرَّسُولِ رَأَيْتَ الْمُنٰفِقِينَ يَصُدُّونَ عَنكَ

صُدُّوۡدًا ﴿٦١﴾

**“Na wanapoambiwa: ‘Njoooni katika yale Aliyoyateremsha Allah, na njoooni kwa Mtume’, utawaona wanafiki wanajiweka mbali nawe kabisa.” (4:61).**

Na Amesema Aliyetukuka:

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا يَسْتَغْفِرْ لَكُمْ رَسُولُ اللَّهِ لَوۡآءُ رُءُوسِهِمْ وَرَأَيْتَهُمْ يَصُدُّونَ وَهُمْ

مُستَكْبِرُونَ ﴿٥﴾

**“Na wanapoambiwa: ‘Njoooni ili Mtume wa Allah Akuombeeni msamaha (kwa makosa yenu)’, huvigeuza vichwa vyao; na unawaona wanajizuia na wakijiona wakubwa.” (63:5).**

Na Luqmaan alimuambia mtoto wake:

وَلَا تُصَعِّرْ خَدَّكَ لِلنَّاسِ

**“Wala usiwatazame (watu) kwa upande mmoja wa uso.” (31:18)**

Maana yake: Unamili (unageuka) kwao kwa kiburi na majivuno. Na Amesema Aliyetukuka:

وَإِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِ آٰيٰتُنَا وَلَّىٰ مُسْتَكْبِرًا

**“Na wanaposomewa Aya Zetu, huzipa mgongo kwa kujivuna.” (31:7)**

Na Kauli Yake:

لِيُضِلَّ عَن سَبِيلِ اللَّهِ

**“Ili kupoteza watu waache njia ya Allah.”**

Huenda muradi wake ukawa ni wenye kupinga kwa inadi au muradi wake

ukawa kuwa yule mwenye kufanya hilo ameumbwa hivyo ili awe ni mmoja wa wale wanaopoteza wengine katika njia ya Allah تعالى. Kisha Anasema Aliyetukuka:

لَهُ فِي الدُّنْيَا خِزْيٌ ط

**“Duniani atapata hizaya.”**

Nayo ni kutwezwa na udhalilifu, kama vile anavyojivuna na kuwa na kiburi kwa ishara na Aya za Allah تعالى. Hivyo Allah تعالى Anamdhalilisha duniani na Atamuadhibu ndani yake (duniani) kabla ya Akhera, kwa kuwa hamu yake yote ni dunia hii na ndiyo anayojua.

وَنذِيقُهُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ عَذَابَ الْحَرِيقِ ﴿٥١﴾ ذَلِكَ بِمَا قَدَّمْتَ يَدَاكَ

**“Na Siku ya Kiyama Tutamuonjesha adhabu ya kuunguza. (Ataambiwa): Hayo ni kwa sababu ya iliyotanguliza mikono yako...”**

Maana yake: Ataambiwa hayo kwa kufokewa, kukaripiwa na kutwezwa.

وَأَنَّ اللَّهَ لَيْسَ بِظَلَّامٍ لِّلْعَبِيدِ ﴿٥٢﴾

**“Na hakika Allah si dhalimu kwa waja”.**

Hii ni kama Kauli Yake:

خَذُوهُ فَأَعْتَلُوهُ إِلَىٰ سَوَاءِ الْجَحِيمِ ﴿٥٣﴾ ثُمَّ صُبُّوا فَوْقَ رَأْسِهِ مِن عَذَابِ الْحَمِيمِ ﴿٥٤﴾

ذُقْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْكَرِيمُ ﴿٥٥﴾ إِنَّ هَذَا مَا كُنْتُمْ بِهِ تَمْتَرُونَ ﴿٥٦﴾

**“Kuambiwa: ‘Mkamateni na mumtupe katikati ya Jahanamu. Kisha mwagieni juu ya kichwa chake (maji ya moto) adhabu ya maji ya moto’. Aambiwe: ‘Onja! Ulikuwa ukijidai kuwa wewe ni mwenye nguvu, mheshimiwa! Hakika hii ndiyo ile adhabu muliyokuwa mukibishana.’ (44:48-50).**

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَعْبُدُ اللَّهَ عَلَىٰ حَرْفٍ ط فَإِنِ أَصَابَهُ خَيْرٌ طَطْمَأَنَّ بِهِ ط وَإِنِ أَصَابَتْهُ فَتْنَةٌ

أَنْقَلَبَ عَلَىٰ وَجْهِهِ خَسِرَ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةَ ط ذَلِكَ هُوَ الْخُسْرَانُ الْمُبِينُ ﴿٥٧﴾ يَدْعُوا مِن

دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَضُرُّهُ وَمَا لَا يَنْفَعُهُ ط ذَلِكَ هُوَ الضَّلَالُ الْبَعِيدُ ﴿٥٨﴾ يَدْعُوا لِمَن

ضُرُّهُ أَقْرَبُ مِن نَّفْعِهِ ط لَيْسَ الْمَوْلَىٰ وَلَيْسَ الْعَشِيرُ ﴿٥٩﴾

**11. Na katika watu wapo wanaomuabudu Allah kwa ukingoni. Ikimfikia kheri hutulia kwayo, na ukimfikia msukosuko hugeza uso wake. Amekhasiri dunia na Akhera; hiyo ndiyo khasara iliyo wazi.**

**12. Badala ya Allah, yeye huomba kisichomdhuru wala kumnufaisha. Huko ndiko kupotolea mbali!**

**13. Humuomba yule ambaye bila ya shaka madhara yake yapo karibu zaidi kuliko manufaa yake. Kwa hakika huyo ni mlinzi muovu, na rafiki muovu.**

### Maana ya Kumuabudu Allah تعالیٰ kama Vile Upo Ukingoni

Na wamesema Mujaahid, Qataadah na wengineo:

عَلَىٰ حَرْفٍ<sup>ط</sup>

**“Kwa ukingoni”.** Juu ya shaka<sup>1</sup>. Na wakasema wengineo: “Pembezoni, na miongoni mwayo ni ukingo wa jabali, yaani pembezoni mwake, yenye maana kuingia katika Dini ukingoni mwake. Na pindi anapopata anayoyapenda anaendelea (na Dini), kinyume na hivyo anaondoka (anaacha)”. Amepokea Al-Bukhaari kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema:

وَمِنَ النَّاسِ مَن يَعْبُدُ اللَّهَ عَلَىٰ حَرْفٍ<sup>ط</sup>

**“Na katika watu wapo wanaomuabudu Allah kwa ukingoni”.**

Watu walikuwa wanakuja Madinah (kusilimu) na ikiwa wake zao watazaa wavulana na farasi (jike) wao wakizaa wana, walikuwa wanasema: ‘Hii ni Dini nzuri’, lakini ikiwa wake zao na farasi wao hawatazaa, walisema: ‘Hii ni Dini mbaya’<sup>2</sup>”.

Na amepokea Al-Awfiy kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما: “Ilikuwa mmoja wao anapokuja Madina (nayo ni ardhi iliyoathiriwa na ugonjwa wa kuambukiza). Akibaki katika siha nzuri hapo, na farasi wake akazaa mwana na mkewe kuzaa mvulana, ataridhika na kutulia na kusema, ‘Sijafikiwa kuanzia nilipokuwa katika Dini yangu hii ila mazuri na kheri’.

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:576.

<sup>2</sup> Fat’hul Al-Baariy 8:296.

وَإِنْ أَصَابَتْهُ فِتْنَةٌ

**'Na ukimfikia msukosuko'.**

*Fitnah* hapa ina maana ya msukosuko na balaa, Maana: akifikiwa na ugonjwa wa Madina, na mkewe kuzaa msichana na sadaka kuchelewa, anakuja kwake shetani, akasema: 'Naapa kwa Allah تعالى! hujafikiwa kuanzia ulipoingia na kufuata Dini yako hii ila mabaya', na hiyo ndiyo *Fitna*<sup>1</sup>. Na hivyo ndivyo alivyotaja Qataadah, Adh-Dhahaak, Ibn Jariir رحمه الله تعالى, na wengineo miongoni mwa watangu wema katika kuifasiri Aya hii<sup>2</sup>. Na amesema Mujaahid kuhusu Kauli Yake:

أَنْقَلَبَ عَلَى وَجْهِهِ

**"Hugeza uso wake".**

Maana yake: Anaritadi na kukufuru<sup>3</sup>. Na Kauli Yake:

خَيْرَ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ

**"Amekhasiri dunia na Akhera".**

Maana yake: Hafaidiki na chochote hapa duniani. Ama kuhusu Kesho Akhera, hakika amemkanusha Allah تعالى, hivyo huko atakuwa katika upeo wa maangamivu na udhalilifu. Kwa hiyo Akasema Aliyetukuka:

ذَلِكَ هُوَ الْخُسْرَانُ الْمُبِينُ ﴿٥٠﴾

**"Hiyo ndiyo khasara iliyo wazi".**

Maana yake: Hii ndiyo khasara kuu na faida mbaya. Na Kauli Yake:

يَدْعُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَضُرُّهُمْ وَمَا لَا يَنْفَعُهُمْ

**"Badala ya Allah, yeye huomba kisichomdhuru wala kumnufaisha".**

Maana yake: Miongoni mwa masanamu na miungu ya uongo anaowaomba kwa msaada, usaidizi na riziki – hawana uwezo wa kumnufaisha wala kumdhuru yeye,

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:575.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:576.

<sup>3</sup> Atw-Twabariy 18:576.

ذَٰلِكَ هُوَ الضَّلَالُ الْبَعِيدُ ﴿١٧﴾

**“Huko ndiko kupotolea mbali!”**

Na Kauli Yake:

يَدْعُوا لِمَن ضَرُّهُ أَقْرَبُ مِن نَّفْعِهِ ۗ

**“Humuomba yule ambaye bila ya shaka madhara yake yapo karibu zaidi kuliko manufaa yake”.**

Maana yake: Upo uwezekano mkubwa zaidi kumdhuru kuliko kumnufaisha hapa duniani, na Akhera atamfanya awe ni mwenye kudhurika kwa yakini kabisa.

Na Kauli Yake:

لَيْسَ الْمَوْلَىٰ وَلِيَّسَ الْعَشِيرُ ﴿١٨﴾

**“Kwa hakika huyo ni mlinzi muovu, na rafiki muovu”.**

Amesema Mujaahid: “Yaani Masanamu”<sup>1</sup>. Hii ina maana ya uovu ulioje kwa rafiki huyu ambaye unamuomba badala ya Allah تعالیٰ miungu mingine ambayo huamini kuwa watamsaidia.

وَلَيْسَ الْعَشِيرُ ﴿١٨﴾

**“Na rafiki muovu.”**

Mwenye kutangamana, na kuamiliana na mtu huyo.

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:579.

إِنَّ اللَّهَ يُدْخِلُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جَنَّاتٍ  
 تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ إِنَّ اللَّهَ يَفْعَلُ مَا يُرِيدُ ﴿١٤﴾ مَنْ  
 كَانَتْ يُظُنُّ أَنْ لَنْ يَنْصُرَهُ اللَّهُ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ فَلْيَمْدُدْ  
 بِسَبَبٍ إِلَى السَّمَاءِ ثُمَّ لْيَقْطَعْ فَلْيَنْظُرْ هَلْ يُذْهِبَنَّ كَيْدَهُ مَا  
 يَغِيظُ ﴿١٥﴾ وَكَذَلِكَ أَنْزَلْنَاهُ آيَاتٍ يَتَذَكَّرُ وَأَنَّ اللَّهَ  
 يَهْدِي مَنْ يُرِيدُ ﴿١٦﴾ إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَالَّذِينَ هَادُوا  
 وَالصَّٰدِقِينَ وَالنَّصِرَىٰ وَالْمَجُوسَ وَالَّذِينَ أَشْرَكُوا إِنَّ اللَّهَ  
 يَفْصِلُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ  
 ﴿١٧﴾ أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يَسْجُدُ لَهُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَمَنْ  
 فِي الْأَرْضِ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ وَالنُّجُومُ وَالْجِبَالُ وَالشَّجَرُ  
 وَالْدَّوَابُّ وَكَثِيرٌ مِنَ النَّاسِ ۗ وَكَثِيرٌ حَقَّ عَلَيْهِ الْعَذَابُ ۗ  
 وَمَنْ يَنْ يَنْ اللَّهَ فَمَا لَهُ مِنْ مُكْرِمٍ ۗ إِنَّ اللَّهَ يَفْعَلُ مَا يَشَاءُ ﴿١٨﴾  
 ﴿١٩﴾ \* هَذَا نِ حَصَمَانِ اَحْتَصَمُوا فِي رَيْبِهِمْ ۗ فَالَّذِينَ  
 كَفَرُوا قُطِعَتْ لَهُمْ رِيَابٌ مِّنْ نَّارٍ يَصُبُّ مِنْ فَوْقِ رُءُوسِهِمْ  
 السَّخِيمُ ﴿٢٠﴾ يُصْهَرُ بِهِ مَا فِي بُطُونِهِمْ وَالْجُلُودُ ﴿٢١﴾ وَهُمْ  
 مَقْمِعٌ مِّنْ حديدٍ ﴿٢٢﴾ كُلَّمَا أَرَادُوا أَنْ يَخْرُجُوا مِنْهَا  
 مِنْ غَمٍّ أُعِيدُوا فِيهَا وَذُوقُوا عَذَابَ الْحَرِيقِ ﴿٢٣﴾

إِنَّ اللَّهَ يُدْخِلُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا  
 الصَّالِحَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا  
 الْأَنْهَارُ إِنَّ اللَّهَ يَفْعَلُ مَا يُرِيدُ ﴿١٤﴾

**14. Hakika Allah Atawa-  
ingiza walioamini na waka  
tenda mema katika Bustani  
zipitazo mito kati yake.  
Hakika Allah Hutenda  
Atakayo.**

**Malipo ya Watu Wema**

Pindi Allah تعالى Alipotaja watu wapotevu waovu Akafuatisha kwa Kuwataja wema waliofaulu miongoni mwa wale ambao wame-amini kwa mioyo yao na kusadikisha Imani yao kwa amali zao. Hivyo, wakafanya mema kwa aina zote za kujikurubisha kwa Allah تعالى na kuacha maovu. Kwa ajili hiyo, watarithi yale majumba ya daraja ya juu katika bustani za Peponi. Na pale Alipotaja Aliyetukuka kuwa Amewapoteza wale na

Akawaongoza hawa, Akasema:

إِنَّ اللَّهَ يَفْعَلُ مَا يُرِيدُ ﴿١٤﴾

**“Hakika Allah Hutenda Atakayo”.**



مَنْ كَانَ يَظُنُّ أَنْ لَنْ يَنْصُرَهُ اللَّهُ فِي الْآخِرَةِ فَلْيَمْدُدْ بِسَبَبٍ إِلَى السَّمَاءِ ثُمَّ لِيَقْطَعْ فَلْيَنْظُرْ هَلْ يُذْهِبَنَّ كَيْدَهُ مَا يَغِيظُ ﴿٥١﴾ وَكَذَلِكَ أَنْزَلْنَاهُ آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ وَأَنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يُرِيدُ ﴿٥٢﴾

**15. Anayedhani kwamba Allah Hatamnusuru (Mtume) katika dunia na Akhera na afunge kamba kwenye dari kisha ajitie nayo kitanzi. Atazame je hila yake itaondoa hayo yaliyomkasirisha?**

**16. Na namna hivi Tumeiteremsha (Qur'ani) kuwa ni Aya zilizo wazi, na hakika Allah Humuongoa Amtakaye.**

**Bila Shaka Allah تعالی Atamnusuru Mtume Wake ﷺ.**

Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: "Yeyote anayedhania kuwa Allah تعالی Hatamnusuru Muhammad ﷺ hapa duniani na Kesho Akhera, 'Na afunge kamba,

إِلَى السَّمَاءِ

**'Kwenye dari'.** Maana yake: Dari ya nyumba yake,

ثُمَّ لِيَقْطَعْ

**'Kisha ajitie nayo kitanzi'.** Hiyo ndiyo iliyokuwa rai na muono wa Mujaahid, 'Ikrimah, 'Atwaa', Abuu Al-Jawzaa', Qatadah na wengineo<sup>2</sup>. Na maana yake ni: Yeyote anayedhania kuwa Allah تعالی Hatamnusuru Muhammad ﷺ na Kitabu Chake na Dini Yake, muache aende na ajiue ikiwa hilo linamkasirisha yeye sana. Hakika ni kuwa Allah تعالی Atamnusuru yeye (Muhammad – ﷺ). Amesema Allah تعالی:

إِنَّا لَنَنْصُرُ رُسُلَنَا وَالَّذِينَ آمَنُوا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيَوْمَ يَقُومُ الْأَشْهَادُ ﴿٥١﴾

**"Bila shaka Sisi Tutawanusuru Mitume Wetu na wale walioamini katika maisha ya dunia na siku watakaposimama mashahidi."**(40: 51).

Na kwa hiyo Akasema:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:581.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:580-583.

فَلْيَنْظُرْ هَلْ يُذْهِبَنَّ كَيْدَهُ مَا يَغِيظُ ﴿١٧﴾

**“Atazame je hila yake itaondoa hayo yaliyomkasirisha?”**

Amesema As-Suddiy: “Maana yake ni katika jambo la Muhammad ﷺ<sup>1</sup>. Na ‘Atwaa’ Al-Khuraasaanii amesema: “Muache atizame ikiwa anaweza kutibu na kuondoa hasira anayoihisi moyoni mwake”. Na Kauli Yake:

وَكَذَلِكَ أَنْزَلْنَاهُ

**“Na namna hivi Tumeiteremsha”.** Maana yake: Qur’ani.

ءَايَاتٍ بَيِّنَاتٍ

**“Kuwa ni Aya zilizo wazi”.** Maana yake: Zilizo wazi kwa lafudhi na maana yake, ni hoja kutoka kwa Allah تعالى kwa wanadamu.

وَأَنَّ اللَّهَ يَهْدِي مَنْ يُرِيدُ ﴿١٨﴾

**“Na hakika Allah Humuongoa Amtakaye”.**

Maana yake: Anampoteza Amtakaye na Humuongoa Amtakaye, Naye Ndiye Mwenye Hekima timilifu na haki ya kufanya hilo.

لَا يُسْئَلُ عَمَّا يَفْعَلُ وَهُمْ يُسْئَلُونَ ﴿١٩﴾

**“Haulizwi Anayoyafanya lakini wao viumbe wataulizwa.” (21:23)**

Ama Hekima na Rehema Yake, Uadilifu Wake, Elimu Yake, Ufalme Wake na Nguvu Zake, hakuna anayeweza kupindua Hukumu Yake, Naye ni Mwepesi wa Kuhesabu.

إِنَّ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَالَّذِينَ هَادُوا وَالصَّالِحِينَ وَالنَّصَارَى وَالْمَجُوسَ وَالَّذِينَ أَشْرَكُوا إِنَّ

اللَّهَ يَفْصِلُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ إِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدٌ ﴿٢٠﴾

**17. Hakika walioamini, na ambao ni Mayahudi na Wasabai na Wakristo na Majusi na wale washirikina – hakika Allaah Atawapambanua baina yao Siku ya Kiyama. Hakika Allah ni Shahidi wa kila kitu.**

<sup>1</sup> Ar-Raaziy 13:15.

## Allah تعالی Atahukumu Makundi Siku ya Kiyama

Allah تعالی Anatueleza kuhusu wafuasi wa dini mbali mbali, Waumini (Waislamu) na wengineo kama Mayahudi na Wasabai. Tayari tumeeleza maana yao katika Suratul Baqarah<sup>1</sup> na kutofautiana watu juu yao. Pia wapo Wakristo, Majusi na wengineo wanaomshirikisha Allah تعالی kwa kuabudu wengine pamoja Naye. Hakika Yeye Aliyetukuka Anasema:

يَفْصَلُ بَيْنَهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ

**“Hakika Allah Atawapambanua baina yao Siku ya Kiyama”.**

Naye Atawahukumu baina yao kwa uadilifu. Atawaingiza wale waliomuamini Peponi na waliomkufuru Motoni, kwani Yeye ni Shahidi juu ya amali zao, Naye Anajua yote wasemayo na watendayo kwa siri na kuyaficha vifuani mwao.

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يَسْجُدُ لَهُ مَنْ فِي السَّمَوَاتِ وَمَنْ فِي الْأَرْضِ وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ  
وَالنُّجُومُ وَالْجِبَالُ وَالشَّجَرُ وَالْدَّوَابُّ وَكَثِيرٌ مِّنَ النَّاسِ ۗ وَكَثِيرٌ حَقَّ عَلَيْهِ الْعَذَابُ ۗ وَمَنْ  
يُنِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِن مُّكْرِمٍ ۗ إِنَّ اللَّهَ يَفْعَلُ مَا يَشَاءُ ۝

**18. Je! Huoni kwamba vinamsujudia Allah vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi, na jua, na mwezi, na nyota, na milima, na miti, na wanyama, na wengi miongoni mwa watu. Na wengi imewastahiki adhabu. Na anayefedheheshwa na Allaah hana wa kumheshimu. Hakika Allaah Hutenda Apendayo.**

## Kila Kitu Kinamsujudia Allah تعالی

Allah تعالی Anatufahamisha kuwa Yeye Peke Yake Ndiye Mwenye Kustahiki Kuabudiwa Peke Yake bila kushirikishwa. Kwa hakika kila kitu kinamsujudia kwa zile Nguvu Zake na Utukufu Wake kwa kupenda au kutopenda, na kila kitu kinasujudu kulingana na maumbile yake. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

أَوَلَمْ يَرَوْا إِلَىٰ مَا خَلَقَ اللَّهُ مِن شَيْءٍ يَتَفَيَّؤُا ظِلَالُهُ عَنِ الْيَمِينِ وَالشَّمَائِلِ سُجَّدًا لِلَّهِ وَهُمْ

دَاخِرُونَ ﴿٢٨﴾

<sup>1</sup> Suratul Baqarah (2): 62.

***“Je, hawavioni vitu vyote Alivyoviumba Allah – ambavyo vivuli Vyake vinazunguka kutoka kulia na kushoto – vinavyomsujudia Allah, hali ni vyenye kumnyenyekea.” (16:48).***

Na Amesema hapa:

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ يَسْجُدُ لَهُ مَن فِي السَّمَوَاتِ وَمَن فِي الْأَرْضِ

***“Je! Huoni kwamba vinamsujudia Allah vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi.”***

Maana yake: Miongoni mwa Malaika katika maeneo ya mbinguni na viumbe wote – miongoni mwa wanadamu, majini, wanyama na ndege.

وَأَن مِّن شَيْءٍ إِلَّا يُسَبِّحُ بِحَمْدِهِ

***“Na hakuna chochote ila kinamsabih (Allah) kwa Sifa Zake njema.” (17:44).***

Na Kauli Yake:

وَالشَّمْسُ وَالْقَمَرُ وَالنُّجُومُ

***“Na jua, na mwezi, na nyota.”***

Hivi vinatajwa kwa majina kwa kuwa vinaabudiwa badala ya Allah تعالى, hivyo Allah تعالى Akaeleza kuwa navyo vinamsujudia Muumba Wake na kuwa vimetwezewa Kwake.

لَا تَسْجُدُوا لِلشَّمْسِ وَلَا لِلْقَمَرِ وَاسْجُدُوا لِلَّهِ الَّذِي خَلَقَهُنَّ

***“Basi msilisujudie jua wala mwezi; bali msujudieni Allah Aliyeviumba.” (41:37).***

Na katika Sahihi mbili kutoka kwa Abi Dharr رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ aliniambia:

«أَتَدْرِي أَيْنَ تَذْهَبُ هَذِهِ الشَّمْسُ؟»

*“Je, unajua liendapo jua hili?”*

Nikasema: “Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ wanajua zaidi”. Akasema:

«فَإِنَّهَا تَذْهَبُ فَتَسْجُدُ تَحْتَ الْعَرْشِ، ثُمَّ تَسْتَأْمِرُ قَبِيْرِيْكَ أَنْ يُقَالَ لَهَا: ارْجِعِيْ مِنْ حَيْثُ جِئْتِ»

*“Hakika hilo (jua) linakwenda na kusujudu chini ya Arshi (kiti cha Enzi), kisha linangoja amri. Karibuni litaambiwa: ‘Rudi ulikotoka’<sup>1</sup>”.*

Na Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: Alikuwa mtu akasema: “Ewe Mtume wa Allaah! Nilijiona ndotoni jana usiku, kama kwamba ninaswali nyuma ya mti. Nilisujudu na mti nao ukasujudu kwa sijdah yangu, nami nikausikia ukisema: ‘Ee Allah! Niandikie kwayo Kwako ujira na Uniondoshee kwayo dhambi, niwekee Kwako na nitakabalie kama Uliyomtakabalia mja Wako Daud’”. Akasema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما: “Mtume ﷺ alisoma Aya ya sajdah, kisha akasujudu, nami nikamsikia akisema maneno kama yale aliyoambiwa na mtu yule kuwa mti ulisema.” (At-Tirmidhiy, Ibn Maajah na Ibn Hibbaan katika Sahihi yake)<sup>2</sup>. Na Kauli Yake:

وَأَلَدَّوَابُّ

**“Na wanyama”.** Maana: Hayawani wote. Na imekuja katika Hadithi iliyopokewa na Imaam Ahmad kuwa Mtume ﷺ amekataza kutumia migongo ya wanyama kama jukwaa la kuzungumza kwani huenda akawa yule mwenye kupandwa ni bora na anamdhukuru zaidi Allah تعالى kuliko mwenye kupanda<sup>3</sup>. Na Kauli Yake:

وَكَثِيرٌ مِّنَ النَّاسِ ط

**“Na wengi miongoni mwa watu”.** Maana yake: Wanamsujudia Allah تعالى kwa khiyari yao, kupenda kwao, wakiabudu na kunyenyekea kwayo.

وَكَثِيرٌ حَقَّ عَلَيْهِ الْعَذَابُ ؕ

**“Na wengi imewastahiki adhabu”.** Maana yake: Mwenye kujiepusha kusujudu, kukataa na kuwa na kiburi.

وَمَنْ يُنِ اللَّهُ فَمَا لَهُ مِن مُّكْرِمٍ ؕ إِنَّ اللَّهَ يَفْعَلُ مَا يَشَاءُ ﴿٢٢﴾

**“Na anayefedheheshwa na Allah hana wa kumheshimu. Hakika Allah Hutenda Apendayo”.**

Na imepokewa na Abi Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Baariy 6:342 na Muslim 1:138.

<sup>2</sup> Tuhfatul Al-Ahwhadiy 3:181, Ibn Maajah 1:334 na Ibn Hibbaan 4:191.

<sup>3</sup> Ahmad 3:441.

«إِذَا قَرَأَ ابْنُ آدَمَ السَّجْدَةَ اعْتَزَلَ الشَّيْطَانُ يَبْكِي، يَقُولُ: يَا وَيْلَهُ أَمَرَ ابْنُ آدَمَ  
بِالسُّجُودِ فَسَجَدَ فَلَهُ الْجَنَّةُ، وَأَمَرَ ابْنُ الشُّجُرِدِ فَأَبَيْتُ فَلِيَ النَّارُ»

*"Pindi anaposoma mwana wa Adam Aya ya sajda, shetani anajitenga huku analia na kusema: 'Ole wangu! Mwana wa Adam aliamrishwa kusujudu, naye akasujudu, hivyo Pepo ni yake; nami niliamriwa kusujudu, nikakataa, hivyo Moto ni wangu."* (Muslim)<sup>1</sup>.

Imamu Ahmad amenukuu kutoka kwa Ukba bin Amir رضي الله عنه amesema: Nimesema: Ewe Mjumbe wa Allah! Je Sura ya Al-Hajj imefadhilishwa kuliko sura nyingine kwa sababu ya kuwa na sehemu mbili za kusujudu Sijida ya Kisomo?" Mtume ﷺ akasema; 'Ndio. Ambaye hataki kuzisujudu asizisome sehemu hizo.' Amesimulia Abuu Daudi na At-Tirmidhi, Na hakika amepokea Abu Daud katika Al-Maraasiyl kutoka kwa Khaalid bin Ma'daan رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«فُضِّلَتْ سُورَةُ الْحَجِّ عَلَى سَائِرِ الْقُرْآنِ بِسَجْدَتَيْنِ»

*"Suratul Hajj imefadhiliwa juu ya Qur'ani yote kwa sijdah mbili"*.

Kisha akasema Abu Daud: "Na hakika hii ina isnadi yake, yaani kwa njia nyingine isiyokuwa hii, nayo haisihi"<sup>2</sup>.

Na amepokea Al-Haafidh Abu Bakar Al-Ismaa'iliy رحمه الله تعالى kutoka kwa Abul Jahm kuwa 'Umar رضي الله عنه alisujudu sijdah mbili za Suratul Hajj alipokuwa Al-Jabiyah<sup>3</sup>, na akasema: "Hakika hii imefadhilishwa kwa sijda mbili."<sup>4</sup>

Na imepokewa na Abu Daud na Ibn Maajah kutoka kwa 'Amr bin Al-'Aswi رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alisoma sijda kumi na tano (15) katika Qur'ani, miongoni mwazo ni tatu katika Surah fupi na katika Suratul Hajj sijda mbili. Huu ushahidi unaipa nguvu baadhi ya maandiko kwa mengine<sup>5</sup>.

<sup>1</sup> Muslim 1:87.

<sup>2</sup> Abu Daawud katika Al-Maraasiyl 78.

<sup>3</sup> Huu ni mji ulioko Palestina ulio karibu na mji wa Al-Quds. 'Umar رضي الله عنه alipita katika kijiji hiki alipokuwa anakwenda kupokea funguo za mji wa Al-Quds kutoka kwa kasisi wa mji huo aliyekuwa akiitwa Sophronius – Mfasiri.

<sup>4</sup> Al-Bayhaqi 2:317.

<sup>5</sup> Abu Daawud 1401 na Ibn Maajah 1075.

\* هَذَا خِصْمَانِ اِخْتَصَمُوا فِي رَيْبٍ ط فَالَّذِينَ كَفَرُوا قُطِعَتْ لَهُمْ رِيَابٌ مِّنْ نَّارٍ  
 يُصَبُّ مِنْ فَوْقِ رُءُوسِهِمُ الْحَمِيمُ ﴿١٤﴾ يُصْهَرُ بِهِ مَا فِي بُطُونِهِمْ وَالْجُلُودُ ﴿١٥﴾ وَهُمْ  
 مَقْنَعٌ مِّنْ حَدِيدٍ ﴿١٦﴾ كُلَّمَا أَرَادُوا أَنْ يَخْرُجُوا مِنْهَا مِنْ غَمٍّ أُعِيدُوا فِيهَا وَذُوقُوا  
 عَذَابَ الْحَرِيقِ ﴿١٧﴾

**19. Hawa wagomvi wawili waliogombana kwa ajili ya Mola wao Mlezi. Basi waliokufuru watakatiwa nguo za moto, na yatamiminwa juu ya vichwa vyao maji yanayochemka.**

**20. Kwa maji hayo vitayayushwa viliomo matumboni mwao, na ngozi zao pia.**

**21. Na kwa ajili yao yatakuwapo marungu ya chuma.**

**22. Kila wakitaka kutoka humo kwa sababu ya uchungu watarudishwa humo humo, na wataambiwa: Onjeni adhabu ya kuungua!**

### Sababu ya Kuteremshwa

Imenukuliwa katika sahihi mbili kuwa Abu Dharr رضي الله عنه aliapa kuwa aya hii:

\* هَذَا خِصْمَانِ اِخْتَصَمُوا فِي رَيْبٍ ط

**“Hawa wagomvi wawili waliogombana kwa ajili ya Mola wao Mlezi”.**

Imeteremshwa kwa Hamzah na masahibu wake wawili رضي الله عنهم , na ‘Utbah na sahibu wake wawili, siku ya Badr pale walipokuja mbele kubariziana katika pambano la mmoja mmoja. Hii ni lafudhi ya Al-Bukhari katika kuifasiri Aya hii<sup>1</sup>. Kisha amepokea Al-Bukhari kutoka kwa Aliy bin Abi Twalib رضي الله عنه kuwa alisema: “Nitakuwa wa kwanza kupiga magoti mbele ya *Rahman* ili utesi uwe ni wenye kutatuliwa Siku ya Kiyama”. Qays amesema: “Kuhusu wao ndio Aya imeteremshwa:

<sup>1</sup> Fat’h Al-Baariy 8:297 na Muslim 4:2323.

﴿ هَذَا نِ حَصْمَانِ أَحْتَصِمُوا فِي رَيْبِمْ ﴾

**'Hawa wagomvi wawili waliogombana kwa ajili ya Mola wao Mlezi'.**

Akasema (Qays): 'Hao ni wale waliobariziana siku ya Badr: 'Aliy, Hamzah na 'Ubaydah na upande mwingine ni Shaybah bin Rabi'ah, 'Utbah bin Rabi'ah na Al-Walid bin Rabi'ah'. Hii imepokewa na Al-Bukhaari peke yake<sup>1</sup>.

Na amepokea Ibn Abi Najih kutoka kwa Mujaahid kuhusu Aya hii: "Ni Mfano wa kafiri na Muumini kubishana kwao kuhusu ufufuo". Kulingana na riwaya nyingine ya Mujaahid na 'Atwaa' kuhusu Aya hii: "Hao ni Waumini na Makafiri". Na kauli ya Mujaahid na 'Atwaa': "Hakika muradi wa hawa ni Makafiri na Waumini, yamehusisha rai zote, na inajumlisha kisa cha siku ya Badr na nyenginezo. Hakika ni kuwa Waumini wanataka kuinusuru Dini ya Allah Aliyetukuka, ilhali Makafiri wanataka kuizima nuru ya Imani, kuishinda haki na kujitokeza batili". Hii ni rai iliyochaguliwa na Ibn Jariir رحمه الله تعالى, nayo ni nzuri.

### Malipo ya Makafiri

﴿ فَالَّذِينَ كَفَرُوا قُطِعَتْ لَهُمْ ثِيَابٌ مِّن نَّارٍ ﴾

**"Basi waliokufuru watakatiwa nguo za moto".**

Maana yake: vipande vya moto vilivyotayarishwa kwa ajili yao. Sa'id bin Jubayr amesema: "Ya shaba, kwani hiyo ina uharara zaidi ya vitu ikipashwa moto"<sup>2</sup>.

﴿ يُصَبُّ مِّن فَوْقِ رُءُوسِهِمُ الْحَمِيمُ ﴾ ﴿ يُصْهَرُ بِهِ مَا فِي بُطُونِهِمْ وَالْجُلُودُ ﴾

**"Na yatamiminwa juu ya vichwa vyao maji yanayochemka. Kwa maji hayo vitayayushwa viliomo matumboni mwao, na ngozi zao pia."**

Maana yake: Pindi maji yaliyochemshwa yenye upeo wa uharara na kuchemshwa, yakamiminwa juu ya vichwa vyenu.

Na amepokea Ibn Jariir رحمه الله تعالى kutoka kwa Abi Hurayrah عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ amesema:

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baariy 8:297.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:590.



إِنَّ الْحَمِيمَ لِيُصَّبُ عَلَى رُؤُوسِهِمْ فَيَنْفُذُ الْجُمْجُمَةَ حَتَّى يَخْلُصَ إِلَى جَوْفِهِ، فَيَسْلُتُ مَا فِي جَوْفِهِ حَتَّى يَبْلُغَ قَدَمَيْهِ، وَهُوَ الصَّهْرُ، ثُمَّ يُعَادُ كَمَا كَانَ»

*“Hakika maji yaliyochemshwa yatamiminwa juu ya vichwa vyao, nayo yatapenya kwenye mafuvu ya vichwa vyao mpaka yafike ndani, na yaliyo ndani yatayeyusha mpaka yafike miguuni mwao. Huku ni kuyeyuka, kisha atarudishwa katika hali yake ya mwanzo.”<sup>1</sup>*

Na imepokewa na At-Tirmidhiy, aliyesema ni Hasan Sahihi<sup>2</sup>. Na hivyo ndivyo alivyopokea Ibn Abi Haatim. Kisha amepokea Ibn Abi Haatim kutoka kwa ‘Abdallaah bin As-Sariy amesema: “Malaika atakuja kwake, akiwa amebeba chombo na koleo kwa sababu ya uharara wake. Atakapokileta chombo hicho karibu na uso wake, atakikwepa. Atanyanyua nyundo aliyoichukua na atampiga kwenye kichwa chake, kufanya ubongo wake kumwagika nje, kisha ataurudisha ubongo kichwani mwake. Hivi ndivyo Alivyosema Allah تعالى katika Aya:

يُصَهَّرُ بِهِ مَا فِي بُطُونِهِمْ وَالْجُلُودُ ﴿٢١﴾

***“Kwa maji hayo vitayayushwa viliomo matumboni mwao, na ngozi zao pia.”<sup>3</sup>***

Na amesema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuhusu Kauli Yake:

وَهُمْ مَقْنَعٌ مِّنْ حَدِيدٍ ﴿٢٢﴾

***“Na kwa ajili yao yatakuwapo marungu ya chuma.”***

Akasema: “Watapigwa nayo, na kwa kila pigo, kiungo kitang`oka kutoka kilipo, na hapo watayaita mauti”<sup>4</sup>. Na Kauli Yake:

كُلَّمَا أَرَادُوا أَنْ تَخْرُجُوا مِنْهَا مِنْ غَمٍّ أُعِيدُوا فِيهَا

***“Kila wakitaka kutoka humo kwa sababu ya uchungu watarudishwa humo humo.”***

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:591.

<sup>2</sup> Tuhfah Al-Ahwadhiy 7:301.

<sup>3</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 6:21.

<sup>4</sup> Atw-Twabariy 18:593.

Amepokea A'mash kutoka kwa Abi Dhibyaan kuwa Salmaan amesema: "Moto ni mweusi wenye kiza, mwale wake na makaa yake hayang'ari." Kisha akasoma:

كَلَّمَا أَرَادُوا أَنْ يَخْرُجُوا مِنْهَا مِنْ غَمٍّ أُعِيدُوا فِيهَا

***'Kila wakitaka kutoka humo kwa sababu ya uchungu watarudishwa humo humo'.***

Na Kauli Yake:

وَذُوقُوا عَذَابَ الْحَرِيقِ ﴿٢٠﴾

***"Na wataambiwa: Onjeni adhabu ya kuungua!"***

Hii ni kama Kauli Yake:

وَقِيلَ لَهُمْ ذُوقُوا عَذَابَ النَّارِ الَّتِي كُنْتُمْ بِهَا تُكَذِّبُونَ ﴿٢٠﴾

***"Na "wataambiwa: Onjeni tu adhabu ya Moto ambayo mulikuwa mukiikadhibisha." (32:20).***

Na maana yake ni kuwa watadhalilishwa kwa maneno na matendo.

\* \* \*

إِنَّ اللَّهَ يُدْخِلُ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ  
 جَنَّاتٍ تَجْرَى مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ يُخَلِّدُونَ فِيهَا مِنْ أَسَاوِرَ  
 مِنْ ذَهَبٍ وَلُؤْلُؤًا ۗ وَلِبَاسُهُمْ فِيهَا حَرِيرٌ ﴿٢٣﴾ وَهُدُوا إِلَى  
 الطَّيِّبِ مِنَ الْقَوْلِ وَهُدُوا إِلَى صِرَاطٍ الْحَمِيدِ ﴿٢٤﴾ إِنَّ  
 الَّذِينَ كَفَرُوا وَيَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ وَالْمَسْجِدِ  
 الْحَرَامِ الَّذِي جَعَلْنَاهُ لِلنَّاسِ سَوَاءً الْعِضْكَ فِيهِ وَالْبَادِ ۗ  
 وَمَن يَرِدْ فِيهِ بِإِلْحَادٍ بِظُلْمٍ نَّذِقْهُ مِن عَذَابِ أَلِيمٍ ﴿٢٥﴾  
 وَإِذْ بَوَّأْنَا لِإِبْرَاهِيمَ مَكَانَ الْبَيْتِ أَن لَّا تُشْرِكْ بِي شَيْئًا  
 وَطَهِّرْ بَيْتِيَ لِلطَّائِفِينَ وَالْقَائِمِينَ وَالرُّكَّعِ السُّجُودِ  
 ﴿٢٦﴾ وَأَذِّنْ فِي النَّاسِ بِالْحَجِّ يَأْتُوكَ رِجَالًا وَعَلَى كُلِّ  
 ضَامِرٍ يَأْتِينَ ۖ مِن كُلِّ فَجٍّ عَمِيقٍ ﴿٢٧﴾ لِيَشْهَدُوا مَنَفَعٍ  
 لَهُمْ وَيَذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ فِي أَيَّامٍ مَّعْلُومَةٍ عَلَىٰ مَا رَزَقْنَاهُمْ  
 مِن بَهِيمَةٍ ۗ فَكُلُوا مِنهَا وَأَطِيعُوا أَلْبَاسَ الْفَقِيرِ  
 ﴿٢٨﴾ ثُمَّ لِيَقْضُوا تَفَثَهُمْ وَلِيُوفُوا نُدُورَهُمْ وَلِيَطَّوَّفُوا  
 بِالْبَيْتِ الْعَتِيقِ ﴿٢٩﴾ ذَلِكَ وَمَن يُعْظَمِ حُرْمَتَ اللَّهِ فَهُوَ  
 خَيْرٌ لَهُ عِنْدَ رَبِّهِ ۗ وَأُحِلَّتْ لَكُمُ الْأَنْعَامُ إِلَّا مَا يُتَىٰ  
 عَلَيْكُمْ ۗ فَاجْتَنِبُوا الرِّجْسَ مِنَ الْأَوْثَانِ وَاجْتَنِبُوا  
 قَوْلَ الزُّورِ ﴿٣٠﴾ حَتَّىٰ تَخْفَأَ لِلَّهِ غَيْرَ مُشْرِكِينَ بِهِ ۗ وَمَن  
 يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَكَأَنَّمَا خَرَّ مِنَ السَّمَاءِ فَتَخْطَفُهُ الطَّيْرُ أَوْ  
 تَهْوَىٰ بِهِ الرِّيحُ فِي مَكَانٍ سَحِيقٍ ﴿٣١﴾

إِنَّ اللَّهَ يُدْخِلُ الَّذِينَ ءَامَنُوا  
 وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرَى  
 مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ يُخَلِّدُونَ فِيهَا مِنْ  
 أَسَاوِرَ مِنْ ذَهَبٍ وَلُؤْلُؤًا ۗ وَلِبَاسُهُمْ  
 فِيهَا حَرِيرٌ ﴿٢٣﴾ وَهُدُوا إِلَى الطَّيِّبِ  
 مِنَ الْقَوْلِ وَهُدُوا إِلَى صِرَاطِ  
 الْحَمِيدِ ﴿٢٤﴾

**23. Hakika Allah Atawa-ingiza walioamini na wakatenda mema katika Bustani zipitiwazo na mito kati yake. Watapambwa humo kwa mapambo ya mikononi ya dhahabu na lulu. Na mavazi yao humo ni hariri.**

**24. Na wataongozwa kwenye maneno mazuri, na wataongozwa kwenye njia ya Ahimidiwaye.**

### Malipo ya Waumini

Pindi Alipoeleza Allah تعالى hali ya watu wa Motoni, Allah تعالى Atulinde na adhabu zao, na walio nayo katika adhabu, kisasi, kuchomwa na minyonyoro—

na nguo za moto ambazo zimetayarishwa kwa ajili yao, Anatueleza kuhusu hali ya watu wa Peponi – tunamuomba Allah تعالى kwa Fadhila Zake na Ukarimu Wake Atuingize Peponi. Akasema:

إِنَّ اللَّهَ يُدْخِلُ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ

**“Hakika Allah Atawaingiza walioamini na wakatenda mema katika Bustani zipitiwazo na mito kati yake.”**

Maana yake: Mito hii inapita sehemu zote, chini ya miti na makasri, na wakazi wake watayasarifu na kuyapeleka wanapotaka.

مُخَلَّوْنَ فِيهَا

**“Watapambwa humo.”** – Kwa vito,

مِنْ أَسَاوِرَ مِنْ ذَهَبٍ وَلُؤْلُؤًا

**“Kwa mapambo ya mikononi ya dhahabu na lulu.”**

Maana yake: Mikononi mwao, kama alivyosema Mtume ﷺ kwa Hadithi iliyoafikiwa usahihi wake:

«تَبْلُغُ الْجَنَّةِ مِنَ الْمُؤْمِنِ حَيْثُ يَبْلُغُ الْوُضُوءَ»

**“Vito vya Muumini (Peponi) vitafika pale panapofika udhu.”**<sup>1</sup>

Na Kauli Yake:

وَلِبَاسُهُمْ فِيهَا حَرِيرٌ ﴿٢٣﴾

**“Na mavazi yao humo ni hariri.”**

Kinyume na mavazi ya watu wa Motoni, watu wa Peponi watakuwa na nguo za hariri, *sundus* na *istibraaq*. Kama Anavyosema Aliyetukuka:

عَلَيْهِمْ ثِيَابٌ سُنْدُسٌ خُضْرٌ وَإِسْتَبْرَقٌ ۖ وَخُلُوعًا مِنْ أَسَاوِرَ مِنْ فِضَّةٍ وَسَقَنَهُمْ رَبُّهُمْ شَرَابًا

طَهُورًا ﴿٢٤﴾ إِنَّ هَذَا كَانَ لَكُمْ جَزَاءً وَكَانَ سَعْيَكُمْ مَشْكُورًا ﴿٢٥﴾

<sup>1</sup> Muslim 1:219.

**“Juu yao wana nguo za hariri laini, za kijani kibichi na za hariri nzito. Na watavikwa vikuku vya fedha na Mola wao Mlezi Atawanyweshwa kinywaji safi kabisa. Awaambie: Hakika haya ni malipo yenu; na amali zenu zimekubaliwa.” (76:21-22).**

Na katika Sahihi:

«لَا تَلْبَسُوا الْحَرِيرَ وَلَا الدِّيَابَجَ فِي الدُّنْيَا، فَإِنَّهُ مِنْ لِبْسِهِ فِي الدُّنْيَا لَمْ يَنْبَسُهُ فِي  
الْآخِرَةِ»

*“Msivae hariri wala dibaji (nguo ya hariri au hariri ya kimashariki au nguo yenye taraza) duniani, kwani atakayezivaa hapa duniani hatazivaa Akhera”<sup>1</sup>.*

‘Abdallah bin Zubayr رضي الله عنهما amesema: “Yeyote asiyevaa hariri Akhera hakuvingia Peponi (mavazi ya peponi ni hariri)’. Amesema Allah تعالى:

وَلِبَاسُهُمْ فِيهَا حَرِيرٌ ﴿٢٣﴾

**‘Na mavazi yao humo ni hariri’<sup>2</sup>.**

وَهُدُوا إِلَى الطَّيِّبِ مِنَ الْقَوْلِ

**“Na wataongozwa kwenye maneno mazuri”.**

Hii ni kama Kauli Yake:

وَأَدْخَلَ الَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا  
بِإِذْنِ رَبِّهِمْ تَحِيَّاتٌ فِيهَا سَلَامٌ ﴿٢٤﴾

**“Na wale walioamini na kufanya vitendo vizuri wataingizwa katika bustani zipitazo mito mbele yake, wakae milele humo kwa idhini ya Mola wao Mlezi. Maamkiano yao humo yatakuwa Salaamun ‘Alaykum za kila upande, (Amani tu juu yenu na furaha na salama).” (14:23).**

Na Kauli Yake Allah تعالى,

<sup>1</sup> Muslim 3:1642 na 1638.

<sup>2</sup> An-Nasaa’iy katika Al-Kubraa 5:465.

وَأَمَلَيْكُمُ يَدْخُلُونَ عَلَيْهِمْ مِنْ كُلِّ بَابٍ ﴿٢٣﴾ سَلَامٌ عَلَيْكُمْ بِمَا صَبَرْتُمْ فَنِعْمَ عُقْبَى الدَّارِ ﴿٢٤﴾

**“Na Malaika wanawaingilia katika kila mlango. (Wakiwaambia) Assalamu Alaikum! Amani iwe juu yenu, kwa sababu ya mlivyosubiri! Basi ni mema mno malipo ya Nyumba ya Akhera.” (13:23-24)**

Na Kauli Yake Allah تعالى،

لَا يَسْمَعُونَ فِيهَا لَغْوًا وَلَا تَأْتِيهَا إِلَّا قِيْلًا سَلَامًا سَلَامًا ﴿٢٥﴾

**“Hawatasikia humo maneno ya upuuzi wala maneno ya madhambi. Isipokuwa maneno ya salama na amani.” (56:25-26).**

Wataongozwa mahali ambapo watasikia maneno mazuri. Na Kauli Yake:

وَيُلْقُونَ فِيهَا تَٰحِيَّةً وَسَلَامًا ﴿٢٦﴾

**“Na watakuta humo heshima na amani.” (25:75).**

Sio kama watakavyodhalilishwa watu wa Motoni kwa maneno ya kukaripiwa na kubezwa kwayo watakapoambiwa:

وَذُوقُوا عَذَابَ الْحَرِيقِ ﴿٢٧﴾

**“Onjeni adhabu ya kuungua!” (22:22).**

وَهُدُوا إِلَى صِرَاطِ الْحَمِيدِ ﴿٢٨﴾

**“Na wataongozwa kwenye njia ya Ahimidiwaye”,**

Maana yake: Mahali ambapo watamhimidi kwayo Mola wao Mlezi kwa Kuwafanyia ihsani, Kuwaneemesha na Kuwafadhilisha, kama ilivyokuja katika Hadithi Sahihi:

«إِنَّهُمْ يُلْهَمُونَ التَّسْبِيحَ وَالتَّحْمِيدَ كَمَا يُلْهَمُونَ التَّنْسِيءَ»

**“Hakika wao watapatiwa ilhamu kwa maneno ya Kumtakasa na Kumsifu, kama vile wanavyopatiwa ilhamu ya kupumua”<sup>1</sup>.**

Na hakika wamesema baadhi ya wafasiri kuhusu Kauli Yake:

<sup>1</sup> Muslim 4:2180, 2181.

وَهْدُوا إِلَى الطَّيِّبِ مِنَ الْقَوْلِ

**“Na wataongozwa kwenye maneno mazuri.”**

Maana yake: Kwa Qur’ani. Na pamesemwa: “*Laa ilaaha illa Llaahu* – Hapana mungu wa kuabudiwa kwa haki ila Allah”. Na pamesemwa: “Ni Kumtaja Allah تعالى kuliko katika sheria (Uislamu)”.

وَهْدُوا إِلَى صِرَاطِ الْحَمِيدِ ﴿٢٣﴾

**“Na wataongozwa kwenye njia ya Ahimidiwaye.”**

Maana yake: Njia nyoofu hapa duniani. Na yote haya hayaendi kinyume na tuliyojataja. Na Allah تعالى Anajua zaidi.

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَيَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ وَالْمَسْجِدِ الْحَرَامِ الَّذِي جَعَلْنَاهُ لِلنَّاسِ سَوَاءً الْعَبْقُوفِ فِيهِ وَالْأَبَادِ ۗ وَمَن يَرِدْ فِيهِ بِالْإِحَادِ يُظَلَمِ نُدْقَهُ مِن عَذَابِ الْبَئِيسِ ﴿٢٤﴾

**25. Hakika wale waliokufuru na wakazuilia njia ya Allah na Msikiti Mtakatifu, ambao Tumeufanya kwa ajili ya watu wote sawasawa, kwa wakao humo na wageni. Na kila atakayetaka kufanya upotofu humo kwa dhuluma, basi Tutamuonjesha adhabu chungu.**

**Onyo kwa Wanaozuia Njia ya Allah تعالى na Msikiti Mtakatifu**

Allah تعالى Anawakemea makafiri kwa kuwazuilia Waumini kuuja Msikiti Mtakatifu na kutekeleza ibada yao ya Hijjah, huku wakidai kuwa wao ndio walinzi wake,

وَمَا كَانُوا أَوْلِيَاءَهُ ۗ إِنَّ أَوْلِيَاءَهُ إِلَّا الْمُتَّقُونَ

**“Nao hawakuwa walinzi wake. Hakuna walinzi wake isipokuwa wacha Mungu tu.” (8:34).**

Katika Aya hii kuna dalili ya kuwa iliteremka Madina. Kama Anavyosema Aliyetukuka katika Suratul Baqarah:

يَسْأَلُونَكَ عَنِ الشَّهْرِ الْحَرَامِ قِتَالٍ فِيهِ ۗ قُلْ قِتَالٌ فِيهِ كَبِيرٌ ۗ وَصَدٌّ عَن سَبِيلِ اللَّهِ وَكُفْرٌ بِهِ وَالْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَإِخْرَاجُ أَهْلِهِ مِنهُ أَكْبَرُ عِنْدَ اللَّهِ ۗ

**“Wanakuuliza kupigana vita miezi mitakatifu. Sema: Kupigana vita katika miezi hiyo ni dhambi kubwa. Na kuzuilia watu wa Dini ya Allah, na kumkanusha, na kuwazuilia watu na Msikiti huo mtakatifu, na kuwatoa humo watu waliomo, ni dhambi kubwa zaidi mbele ya Allah.” (2:217).** Na Amesema hapa:

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَيَصُدُّونَ عَن سَبِيلِ اللَّهِ وَالْمَسْجِدِ الْحَرَامِ

**“Hakika wale waliokufuru na wakazuilia njia ya Allah na Msikiti Mtakatifu”.**

Maana yake: Sio tu wao ni makafiri bali wanawazuilia watu katika njia ya Allah تعالى na kuingia katika Msikiti Mtakatifu. Hiyo ina maana ya kuwazuilia na Msikiti Mtakatifu kwa wenye kutaka kwenda huko, japokuwa Waumini wana haki zaidi kuliko mwengine yeyote kwenda huko. Muundo wa ibara hii ni kama ile inayopatikana katika Aya:

الَّذِينَ ءَامَنُوا وَتَطْمَئِنُّ قُلُوبُهُمْ بِذِكْرِ اللَّهِ أَلَا بِذِكْرِ اللَّهِ تَطْمَئِنُّ الْقُلُوبُ ﴿٢٨﴾

**“Wale walioamini na zikatulia nyoyo zao kwa kumdhukuru Allah. Sikilizeni! Kwa kumtaja Allah nyoyo hutulia.” (13:28)**

Maana yake: Katika sifa zao ni kutulia nyoyo zao katika kumkumbuka na kumtaja Allah تعالى.

## Masuala ya Kukodisha Nyumba Makka

Na Kauli Yake:

الَّذِي جَعَلْتَهُ لِلنَّاسِ سَوَاءً الْعَنِكْفُ فِيهِ وَالْبَادِ

**“Ambao Tumeufanya kwa ajili ya watu wote sawasawa, kwa wakaao humo na wageni”.**

Maana yake: Wanawakataza watu kufika Msikiti Mtakatifu, ambao Allah تعالى Amejaalia ni wenye kufikiwa na kila mmoja sawasawa kisheria, bila ya tofauti baina ya wanaoishi humo na wageni.

سَوَاءً الْعَنِكْفُ فِيهِ وَالْبَادِ

**“Kwa ajili ya watu wote sawasawa, kwa wakaao humo na wageni”.**



Sehemu ya usawa huu ni kuwa kila mmoja ana haki sawa katika kuweka makazi mahali popote katika mji na kuishi humo, kama 'Aliy bin Abi Twalhah alivyopokea kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kuwa amesema yafuatayo kuhusu Aya hii:

سَوَاءٌ أَلْعَيْكُفُ فِيهِ وَالْأَبَادُ<sup>١</sup>

***“Kwa ajili ya watu wote sawasawa, kwa wakaao humo na wageni’.***

Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: ‘Wote, watu wa Makka na wengine wanaweza kuishi katika Msikiti Mtakatifu’<sup>1</sup>. Na amesema Mujaahid kuhusu Aya Yake:

سَوَاءٌ أَلْعَيْكُفُ فِيهِ وَالْأَبَادُ<sup>٢</sup>

***“Kwa ajili ya watu wote sawasawa, kwa wakaao humo na wageni”.***

Watu wa Makka na wengineo wote wanaruhusiwa kukaa humo. Hii ndiyo iliyokuwa rai ya Abu Swaalih, 'Abdur-Rahman bin Saabitw na 'Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam. Na amepokea 'Abdur-Razzaaq kutoka kwa Ma'mar kutoka kwa Qataadah: “Ni sawa ikiwa wakaazi wa mji au wageni”. Na masiala haya wametofautiana kwayo Ash-Shaafi'iy رحمه الله تعالى na Ishaah bin Rahwayh رحمه الله تعالى katika Msikiti wa Khayf, Ahmad bin Hambal رحمه الله تعالى hakuwepo.

Ash-Shaafi'iy رحمه الله تعالى alikuwa na rai kuwa sehemu zote za Makka zaweza kumilikiwa, kurithiwa na kukodishwa, na alitumia Hadithi ya Usaamah bin Zayd رضي الله عنهما kama dalili, aliyesema: “Nilisema, Ewe Mtume wa Allah! Je, utakwenda kesho na kukaa katika nyumba yako ya Makka?” Akasema:

«وَهَل تَرَكْنَا عَقِيلًا مِنْ رَبَاعٍ؟»

***“Na je 'Aqiyl bin Ribaah ametuachia chochote?”***

Kisha akasema:

«لَا يَرِثُ الْكَافِرُ الْمُسْلِمَ وَلَا الْمُسْلِمُ الْكَافِرَ»

***“Kafiri hamrithi Muislamu wala Muislamu hamrithi kafiri”.***

Na Hadithi hii imetolewa katika Sahihi mbili<sup>2</sup>. Na kama ilivyothibiti kutoka kwa 'Umar bin Khattwaab رضي الله عنه kuwa alinunua nyumba Makka kutoka kwa

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:596.

<sup>2</sup> Al-Bukhaariy 6764 na Muslim 1614.

Swafwaan bin Umayyah kwa Dirham elfu nne (4000) na akaifanya kuwa jela. Hii ndiyo iliyokuwa rai ya Twaawuus na 'Amr bin Diynaar. Ama Is'haaq bin Rahwayh رحمه الله تعالى alikuwa na muono na rai kuwa (nyumba za Makka) haziwezi kurithiwa au kukodishwa. Hii ilikuwa ni rai ya watu wema waliotangulia wengi, na Mujaahid na 'Atwaa' wamesema hivyo. Is'haaq bin Rahwayh رحمه الله تعالى alitumia kama dalili Hadithi iliyopokewa na Ibn Maajah kuwa Alqamah bin Nadhwlah رضي الله عنه amesema: "Aliaga dunia Mtume ﷺ, Abu Bakar na 'Umar رضي الله عنهما, na hakuna aliyedai rasilimali yoyote huko Makka ila wanyama walishao. Yeyote anayetaka kuishi humo atachukua makaazi humo, na asiyetaka kuishi humo atawaacha wengine wachukue makaazi yao."<sup>1</sup> 'Abdur-Razzaaq رحمه الله تعالى amepokea kuwa Abdallah bin Amr amesema: "Haikubaliwi kuuza au kukodisha nyumba katika mji wa Makka". Pia alisema, akimnukuu Ibn Jurayj: "Atwaa' alikataza kukodisha nyumba katika Haram, na aliniambia kuwa 'Umar bin Al-Khatwaab رضي الله عنه aliwakataza watu kutia lango katika nyumba za Makka kwa sababu mahujaji walikuwa wakikaa kwenye uga wake. Mtu wa kwanza kutia lango nyumbani kwake ni Suhayl bin 'Amr. 'Umar bin Al-Khatwaab رضي الله عنه alimuita na kumuuliza kuhusu hilo, naye akasema: 'Nisikilize, ewe Amiri wa Waumini! Mimi ni mtu wa biashara, nami nataka kulinda mgongo wangu (mali yangu) kwa kutia milango miwili'. Akasema: 'Unaweza kufanya hivyo'". Amepokea 'Abdur-Razzaaq رحمه الله تعالى kutoka kwa Mujaahid kuwa 'Umar bin Al-Khatwaab رضي الله عنه alisema: "Enyi watu wa Makka! Msitie milango kwenye nyumba zenu na waacheni Mabedui waishi watakapo"<sup>2</sup>. Akasema: Ametupasha Ma'mar kwa aliyosikia kutoka kwa 'Atwaa' akisema yafuatayo kuhusu Aya ifuatayo:

سَوَاءٌ أَلْعَبِكُمْ فِيهِ وَالْأَبَادِ

***"Kwa ajili ya watu wote sawasawa, kwa wakao humo na wageni."***

Akasema: 'Wanakaa wanapotaka". Na amepokea A-Daraqutwniy kutoka kwa 'Abdallah bin 'Amr رضي الله عنه: "Yeyote anayekodisha (kutoza ujira) nyumba Makka, anakula moto"<sup>3</sup>. Imaam Ahmad akachukua msimamo wa kati na kati (kulingana na alivyopokea mwanawe, Saalih kutoka kwake), akasema: "Nyumba zinaweza kumilikiwa na kurithiwa, lakini hazifai kukodishwa ili kuweza kuowanisha baina ya dalili (za pande zote mbili)". Na Allah تعالى Anajua zaidi.

<sup>1</sup> Ibn Maajah 3107.

<sup>2</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 4:633.

<sup>3</sup> Ad-Daraqutwniy 2:300.

## Onyo Kali kwa Wanaotaka Kufanya Upotofu katika Haram

Na Kauli Yake:

وَمَنْ يُرِدْ فِيهِ بِالْحَادِ بِظُلْمٍ نَذِقْهُ مِنْ عَذَابِ أَلِيمٍ ﴿٢٦﴾

***“Na kila atakayetaka kufanya upotofu humo kwa dhuluma, basi Tutamwonjesha adhabu chungu.”***

Maana yake: Anakusudia kufanya humo jambo ovu miongoni mwa maasi makubwa. Na Kauli Yake,

بِظُلْمٍ

***“Kwa dhuluma”***. Maana yake: Kwa kukusudia kufanya dhuluma, na si katika jambo lisilofahamika vyema, kama ilivyopokewa na Ibn Jurayj kutoka kwa Ibn ‘Abbaas kuwa maana yake ni kukusudia<sup>1</sup>.

Na amepokea ‘Aliy bin Abi Twalhah kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuwa amesema: ***“Kwa dhuluma”***. Maana yake: kwa kumshirikisha<sup>2</sup>. Na amepokea Al-‘Awfiy kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuwa amesema: ***“Kwa dhuluma”***. Maana: matendo maovu kwa kuhalalisha alichoharamisha Allah تعالى, kama kumtendea ubaya mtu au kuuu. Kwa hali ambayo unamdhulumu mtu asiyekudhulumu na unawaua wale wasiopigana nawe. Ikiwa mtu atafanya haya, hivyo itakuwa ni wajibu kupata adhabu iumizayo<sup>3</sup>. Na amesema Mujaahid:

بِظُلْمٍ

***“Kwa dhuluma”***. Maana yake: Kufanya ndani yake amali mbaya na hii ni katika sifa ya kipekee ya Haram, ambayo mtu anayetaka kufanya uovu ataadhabiwa, ikiwa hii ndiyo nia yake hata kama hajaanza kufanya tendo hilo. Hii ni kama alivyosema Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى katika Tafsiri yake kutoka kwa ‘Abdallah, kwa maana Ibn Mas’ud رضي الله عنه kuhusu Kauli Yake:

وَمَنْ يُرِدْ فِيهِ بِالْحَادِ بِظُلْمٍ

***“Na kila atakayetaka kufanya upotofu humo kwa dhuluma.”***

Akasema: “Lau mtu anataka kutekeleza upotofu kwa dhuluma ndani yake, Allah تعالى Atamfanya aonje adhabu chungu iumizayo<sup>4</sup>. Hii pia ilipokewa na

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18: 601.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:600.

<sup>3</sup> Atw-Twabariy 18:600.

<sup>4</sup> Atw-Twabariy 18:601.

<sup>5</sup> Ahmad 1:428.

Ahmad<sup>5</sup>. Nikasema: Isnadi yake ni Sahihi kulingana na sharti ya Al- Bukhaariy, na uwezekano mkubwa ni kuwa ni *Mawquuf*<sup>1</sup> na sio Marfu<sup>2</sup>. Na Allah تعالیٰ Anajua zaidi. Na amesema Sa'id bin Jubayr: "Kumtusi mjakazi na lolote zaidi ya hapo ni dhuluma". Na amesema Habiyy bin Abi Thaabit:

وَمَنْ يُرِدْ فِيهِ بِإِلْحَادٍ بِظُلْمٍ

**"Na kila atakayetaka kufanya upotofu humo kwa dhuluma".**

Akasema: "Kuhodhi (bidhaa) Makka". Hii ndiyo iliyokuwa rai ya wengine wengi. Na amesema Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kwa Kauli ya Allah تعالیٰ:

وَمَنْ يُرِدْ فِيهِ بِإِلْحَادٍ بِظُلْمٍ

**"Na kila atakayetaka kufanya upotofu humo kwa dhuluma."**

Akasema: "Imeteremka kwa 'Abdallah bin Unays. Mtume ﷺ alimtuma yeye na watu wawili, mmoja wao alikuwa ni Muhaajir na wa pili ni Answaar. Hao walianza kujigamba kwa nasaba zao, naye 'Abdallah bin Unays alikasirika na kumuua Answaar. Baada ya hapo akaritadi na kukimbilia Makka. Kisha maneno haya yakateremshwa kumhusu:

وَمَنْ يُرِدْ فِيهِ بِإِلْحَادٍ بِظُلْمٍ

**"Na kila atakayetaka kufanya upotofu humo kwa dhuluma'.**

Kumaanisha yeyote mwenye kukimbilia *Haram* kufanya matendo maovu, maana - kwa kuacha Uislamu". Ripoti hizi ni Athari ambazo ni dalili kuwa mambo haya ni miongoni mwa upotofu na uovu, lakini ni jumla zaidi kuliko tukio hilo na zinajumlisha vitu vilivyo vibaya zaidi. Na kwa hiyo pindi watu wa ndovu walipopanga kuiharibu Nyumba (Ka'bah), Allah تعالیٰ Aliwatumia dhidi yao ndege makundi kwa makundi:

تَرْمِيهِمْ بِحِجَارَةٍ مِّن سِجِّيلٍ ﴿٤﴾ جَعَلَهُمْ كَعَصْفٍ مَّأْكُولٍ ﴿٥﴾

**"Wakawapiga kwa mawe ya udongo wa kuchoma. Akawafanya kama majani yaliyoliwa (yakatapikwa)." (105:4-5),**

<sup>1</sup> Ni Hadithi ambayo imeishia kwa Swahaba wa Mtume ﷺ. Haya yanaweza kuwa ni maelezo anayotoa Swahaba. *Mawquuf* wakati mwingine inaitwa *Athaar*.

<sup>2</sup> Hii ni Hadithi ambayo inaonesha kuwa imefika kwa Mtume ﷺ ama kwa vitendo, maneno kwa kuwa imeunganika moja kwa moja.

Maana yake: Akawahilikisha na Kuwafanya kuwa funzo na onyo kwa kila mmoja anayetaka kufanya kitendo kiovu hapo. Hivyo, ikaripotiwa katika Hadithi kuwa Mtume ﷺ amesema:

«يَغْزُوا هَذَا الْبَيْتَ جَيْشٌ حَتَّىٰ إِذَا كَانُوا بِبَيْدَاءٍ مِّنَ الْأَرْضِ خَسِفَ بِأَوْلِيهِمْ وَأَخْرَجَهُمْ»

*“Nyumba hii itavamiwa na jeshi, hata watakapokuwa katika badiya (uwanja mpana ulio wazi), watamezwa na ardhi wa kwanza na wa mwisho wao.”<sup>1</sup>*

وَإِذْ بَوَّأْنَا لِإِبْرَاهِيمَ مَكَانَ الْبَيْتِ أَن لَّا تُشْرِكْ بِي شَيْئًا وَطَهِّرْ بَيْتِيَ لِلطَّائِفِينَ  
وَالْقَائِمِينَ وَالرُّكَّعِ السُّجُودِ ﴿٢٦﴾ وَأَذِّنْ فِي النَّاسِ بِالْحَجِّ يَأْتُوكَ رِجَالًا وَعَلَىٰ  
كُلِّ ضَامِرٍ يَأْتِينَ مِنْ كُلِّ فَجٍّ عَمِيقٍ ﴿٢٧﴾

**26. Na pale Tulipomuweka Ibrahimu pahala penye ile Nyumba Tukamuambia: Usinishirikishe na chochote; na isafishe Nyumba Yangu kwa ajili ya wanaoizunguka kwa kutufu, na wanaokaa hapo kwa ibada, na wanaorukuu, na wanaosujudu.**

**27. Na watangazie watu Hija; watakuja kwa miguu na juu ya kila ngamia aliye konda, wakija kutoka katika kila njia ya mbali.**

### Kujengwa kwa Ka'bah na Kulinganiwa Hijjah

Huku ni kukaripiwa kwa Maquraish waliokuwa wakiabudu asiyekuwa Allah تعالى na kumshirikisha pamoja Naye katika sehemu ambayo kuanzia mwanzo ilianzishwa kwa msingi wa Tawhidi na kuabudiwa kwa Allah تعالى tu, bila ya kumshirikisha. Allah تعالى Anatuambia kuwa Alimuonesha Ibrahimu عليه السلام mahali pa Nyumba, yaani Alimuongoza kwayo, kumkabidhi na kumpatia idhini ya kuijenga. Wanachuoni wengi wanachukulia kuwa huu ni uthibitisho kuwa Ibrahimu عليه السلام alikuwa wa mwanzo kuijenga Nyumba hiyo na kuwa haikujengwa kabla ya wakati wake (Ibrahimu عليه السلام). Imenukuliwa katika Sahihi mbili kuwa Abu Dharr رضي الله عنه amesema: Niliuliza: “Ewe Mtume wa Allah! Ni Msikiti gani uliojengwa mwanzo?” Akasema:

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baariy 4:397.

## «الْمَسْجِدُ الْحَرَامُ»

“Msikiti wa Al-Haram (ulio Makka).” Nikasema: “Kisha upi?” Akasema:

## «بَيْتُ الْمَقْدِسِ»

“Bayt Al-Maqdis.” Nikasema: “Je, kulikuwa na muda gani baina yao?” Akasema:

## «أَرْبَعُونَ سَنَةً»

“Miaka arobaini.”<sup>1</sup> Na hakika Allah تعالى Amesema:

إِنَّ أَوَّلَ بَيْتٍ وُضِعَ لِلنَّاسِ لَلَّذِي بِبَكَّةَ مُبَارَكًا

**“Kwa yakini Nyumba ya kwanza iliyowekwa kwa ajili ya watu ni ile iliyoko Bakkah (Makka), yenye baraka.” (3:96),**

Mpaka mwisho wa Aya zinazofuatia. Na Amesema Aliyetukuka:

وَعَهْدَنَا إِلَىٰ إِبْرَاهِيمَ وَإِسْمَاعِيلَ أَن طَهِّرَا بَيْتِيَ لِلطَّائِفِينَ وَالْعَاكِفِينَ وَالرُّكَّعِ

السُّجُودِ ﴿١٢٥﴾

**“Na Tulimuusia Ibrahimu na Ismaa’il (Tukamuambia): Itakaseni Nyumba Yangu kwa ajili ya wale wanaoizunguka kwa ajili ya kutufu na wanaokaa hapo na kwa ajili ya wanaorukuu na kusujudu hapo pia.” (2:125)**

Na Amesema Aliyetukuka hapa:

أَنْ لَا تُشْرِكُوا بِي شَيْئًا

**“Usinishirikishe na chochote.”** Maana yake: Ijenge kwa Jina Langu tu.

وَطَهِّرَا بَيْتِيَ

**“Na isafishe Nyumba Yangu.”**

Qatadah na Mujaahid wamesema: “Kutokana na ushirikina.”<sup>2</sup>

<sup>1</sup> Fat’h Al-Baariy 6:469 na Muslim 1:370. Hadithi hii pia ilinukuliwa na Ahmad, Abu Daawuud, At-Tirmidhiy, An-Nasaa’iy na Ibn Maajah.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:604.

لِلطَّائِفِينَ وَالْقَائِمِينَ وَالرُّكَّعِ السُّجُودِ ﴿٢٣﴾

**“Kwa ajili ya wanaoizunguka kwa kutufu, na wanaokaa hapo kwa ibadah, na wanaorukuu, na wanaosujudu.”**

Maana yake: Ijaalie safi na halisi kwa hawa wanaomuabudu Allah تعالى Peke Yake, asiyekuwa na mshirika. Wenye kutufu wanajulikana kwani hii ni ibada inayofanywa katika Ka’bah peke yake na sio katika sehemu nyengine yoyote kwenye ardhi.

وَالْقَائِمِينَ

**“Na wanaokaa hapo kwa Ibada.”** Maana: Katika Swala. Na kwa hiyo Akasema:

وَالرُّكَّعِ السُّجُودِ ﴿٢٤﴾

**“Na wanaorukuu, na wanaosujudu”.** Twawaf na Sala zimetajwa pamoja kwa sababu zote mbili zinafungamana na Kaaba. Twawaf inafanywa kwa kuizunguka Ka’bah na Swala inatekelezwa kwa kuelekea katika hali nyingi, ila kwa hali chache, kwa mfano ikiwa mmoja hana uhakika wa Qiblah, kwenye vita na anaposwali Sala za Suna na anapokuwa safarini. Na Allah تعالى Anajua zaidi. Na Kauli Yake:

وَأَذِّنْ فِي النَّاسِ بِالْحَجِّ

**“Na watangazie watu Hija.”** Maana yake: Watangazie watu Hija na waite waje watekeleze amali ya Hija kwenye Nyumba hii ambayo Tumekuamuru uijenge. Panasemwa kuwa Ibrahim عليه السلام alisema: “Ewe Mola wangu Mlezi! Na vipi nitabalighisha (nitafikisha) kwa watu ilhali sauti yangu haiwafikii wao?” Aliambiwa: “Waite wao, Nasi Tutafikisha”. Hivyo, Ibrahim عليه السلام alisimama na kusema: “Enyi watu! Hakika Mola wenu Mlezi Amechukua Nyumba, kwa hiyo njooni mufanye Hija kwayo”. Pamesemwa kuwa milima ilinyenyekeka (kwa kujivuta chini) mpaka ikafika sauti yake sehemu zote za ulimwengu, na wale waliokuwa ndani ya matumbo ya mama zao na waliokuwa katika migongo ya baba zao waliusikia mwito. Kila kitu kilichosikia wito huo kilitikia, katika miji, jangwa na vitongoji, na kila aliyeandikiwa na Allah تعالى kuhiji mpaka Siku ya Kiyama: ‘Tuko katika utumishi Wako, Ewe Allah تعالى,

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:605, 606, 607.

Tuko katika utumishi Wako.’ Huu ni muhtasari wa masimulizi kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما, Mujaahid, ‘Ikrimah na Sa’id bin Jubayr<sup>1</sup> na wengine miongoni mwa wema waliotangulia. Na Allah تعالى Anajua zaidi. Imepokewa kwa urefu na Ibn Jariir رحمه الله تعالى na Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى. Na Kauli Yake:

يَأْتُوكَ رِجَالًا وَعَلَىٰ كُلِّ ضَامِرٍ

**“Watakuja kwa miguu na juu ya kila ngamia aliyekonda”.**

Huenda Aya hii ikachukuliwa kama dalili na hoja na wale wanazuoni ambao wana rai kuwa Hija iliyofanywa kwa miguu ni bora kwa mwenye kuweza kufanya hivyo kuliko ya mwenye kupanda (kipando), kwa sababu ibara iliyotumika “kwa miguu” imetangulizwa, kutajwa na hiyo ni kwa sababu ya kuipa umuhimu nguzo hiyo na kuonesha ni jinsi gani pia ukubwa wa azma yao, Na amepokea Waki’ kutoka kwa Abu Al - ‘Umayy kutoka kwa Abu Halhalah kutoka kwa Muhammad bin Ka’b kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Sijuti kwa lolote isipokuwa kwa ile hakika kuwa nimependa kuwa nimefanya Hija kwa miguu (kutembea), kwa sababu Allah تعالى Anasema:

يَأْتُوكَ رِجَالًا

**“Watakuja kwa miguu.”<sup>1</sup>**

Hata hivyo wanazuoni wengi waona kuwa kutekeleza Hija kwa kupanda (kipando) ni bora zaidi, kwa kufuata mfano wa Mtume ﷺ, kwani yeye alitekeleza Hija kwa kupanda pamoja na kuwa alikuwa na nguvu. Na Kauli Yake:

يَأْتِينَكَ مِنْ كُلِّ فَجٍّ

**“Wakija kutoka katika kila njia.”**

Maana yake: Njia, kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَجَعَلْنَا فِيهَا فِجَاجًا سُبُلًا

**“Na Tukaweka humo mabarabara, wazi wazi.” (21:31).**

<sup>1</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 6:35.



عَمِيقٌ ﴿٢٧﴾

“Amiyq”.

Maana yake: Mbali. Hii ni rai ya Mujaahid, ‘Atwaa’, As-Suddiy, Qataadah, Muqaatil bin Hayyaan, Ath-Thawriy na wengineo<sup>1</sup>. Na Aya hii ni kama Kauli ya Aliyetukuka kutupasha habari ya Ibrahimu عليه السلام aliposema katika Dua yake:

فَأَجْعَلْ أَفْعَدَةً مِّنَ النَّاسِ تَهْوَىٰ إِلَيْهِمْ

“Na ujaalie nyoyo za watu zielekee kwao.” (14:37).

Hakuna hata mmoja miongoni mwa Waislamu asiyependa kuiona Ka’bah na kutufu ndani yake, watu wanakuja sehemu hii kutoka kila pembe ya dunia.

لِيَشْهَدُوا مَنَفَعَهُ لَهُمْ وَيَذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ فِي أَيَّامٍ مَّعْلُومَةٍ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُمْ مِّنْ بَهِيمَةِ  
الْأَنْعَامِ ۗ فَكُلُوا مِنْهَا وَأَطْعِمُوا الْبَائِسَ الْفَقِيرَ ﴿٢٨﴾ ثُمَّ لِيَقْضُوا تَفَثَهُمْ وَلِيُوفُوا نُذُورَهُمْ  
وَلِيَطُوفُوا بِالْبَيْتِ الْعَتِيقِ ﴿٢٩﴾

**28. Ili washuhudie manufaa yao na walitaje Jina la Allah katika siku maalumu juu ya nyama hoa aliowaruzuku. Basi kuleni katika hao na mlisheni mwenye shida aliye fakiri.**

**29. Kisha wajisafishe taka zao, na waondoe nadhiri zao, na waizunguke Nyumba ya Kale.**

**Hija ina Manufaa katika maisha ya Duniani na Akhera**

Amesema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuhusu Aya hii:

لِيَشْهَدُوا مَنَفَعَهُ لَهُمْ

“Ili washuhudie manufaa yao”.

Akasema: “Manufaa hapa duniani na Kesho Akhera”. Ama manufaa ya Akhera ni kupata Radhi za Allah تعالى. Na ama manufaa ya kidunia ni kule kupata

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:608.

manufaa ya kimwili, wanyama wa kuchinja na biashara<sup>1</sup>. Na hivyo ndivyo alivyosema Mujaahid na wengineo: “Hayo ni manufaa ya kidunia na Akhera”<sup>2</sup>. Hii ni kama Kauli Yake:

لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَبْتَغُوا فَضْلًا مِّن رَّبِّكُمْ

**“Si vibaya kwenu kuitafuta Fadhila ya Mola wenu Mlezi (kwa kufanya biashara njiani munapokwenda kuhiji).” (2:198)**

Kauli Yake Allah تعالى:

وَيَذَكِّرُوا أَسْمَ اللَّهِ فِي أَيَّامٍ مَّعْلُومَةٍ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُم مِّن بَهِيمَةِ الْأَنْعَامِ

**“Na walitaje Jina la Allah katika siku maalumu juu ya nyama hoa aliowaruzuku”.**

Amepokea Shu’bah na Hushaym kutoka kwa Abu Bishr kutoka kwa Sa’id kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Siku maalumu (zinazojulikana) ni siku kumi (za Dhul Hijjah)”<sup>3</sup>. Al-Bukhaari ameipokea hii ikiwa na silsila (Isnadi) iliyokatika kwa njia inayoonesha kuwa ameikubali<sup>4</sup>.

Na imepokewa mfano wake kutoka kwa Abi Musa al- Ash’ariy, Mujaahid, Qataadah, ‘Atwaa’, Said bin Jubayr, Al-Hasan, Adh - Dhahaak, ‘Atwaa’ Al-Khuraasaaniy na Ibraahim An-Nakhaa’iy<sup>5</sup>.

Bukhaariy amepokea kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuwa Mtume ﷺ amesema:

«مَا الْعَمَلُ فِي أَيَّامٍ أَفْضَلَ مِنْهَا فِي هَذِهِ»

**“Hakuna ibada iliyo bora kuliko ile inayofanywa katika siku hizi”.**

Wakasema: “Hata Jihadi katika Njia ya Allah تعالى?” Akasema:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:609.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:609.

<sup>3</sup> Fat’h Al-Baariy 2:531; Atw-Twabariy 4:208.

<sup>4</sup> Fat’h Al-Baariy 2:531.

<sup>5</sup> Atw-Twabariy 18:610 na Ar-Raaziy 23:26.

«وَلَا الْجِهَادُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ إِلَّا رَجُلٌ يُخْرِجُ يُخَاطِرُ بِنَفْسِهِ وَمَالِهِ فَلَمْ يَرْجِعْ بِشَيْءٍ»

*"Hata Jihadi katika Njia ya Allah, isipokuwa kwa mtu anayetoka akaitia hatarini nafsi na mali yake na asirudi na chochote"*<sup>1</sup>.

Na imepokewa na Imamu Ahmad kutoka kwa Ibn 'Umar رضي الله عنهما kuwa Mtume ﷺ amesema:

«مَا مِنْ أَيَّامٍ أَعْظَمَ عِنْدَ اللَّهِ وَلَا أَحَبَّ إِلَيْهِ الْعَمَلُ فِيهِنَّ مِنْ هَذِهِ الْأَيَّامِ الْعَشْرِ فَأَكْبِرُوا فِيهِنَّ مِنَ التَّهْلِيلِ وَالتَّكْبِيرِ وَالتَّحْمِيدِ»

*"Hakuna miongoni mwa siku zilizo na uzito (na kubwa) mbele ya Allah wala zinazompendeza amali ndani yake kuliko masiku haya. Basi ongezeni (na zidisheni) ndani yake Tahlili (kumpwekesha Allah), Takbiri (kumtukuza Allah) na Tahmidi (kumsifu Allah)"*<sup>2</sup>.

Na amesema Al-Bukhaariy: "Na alikuwa Ibn 'Umar na Abu Hurayrah رضي الله عنهما wakitoka kwenda sokoni katika siku kumi (za Dhul Hijjah) huku wanatoa Takbiri, na watu wakitoa Takbiri kwa Takbiri zao (baada yao)"<sup>3</sup>.

Na siku hizi kumi inajumlisha siku ya 'Arafah ambayo imethibiti katika Sahihi Muslim kutoka kwa Abi Qataadah رضي الله عنه aliyesema: Mtume ﷺ aliulizwa kuhusu fungu ya siku ya 'Arafah. Akasema:

«أَخْتَسِبُ عَلَى اللَّهِ أَنْ يُكَفِّرَ السَّنَةَ الْمَاضِيَةَ وَالْآتِيَةَ»

*"Natumai kwa Allah kuwa inafuta dhambi za mwaka uliopita na unaofuata"*<sup>4</sup>.

Na pia inajumlisha siku ya kuchinja, ambayo ni siku kubwa zaidi ya Hija, na hiyo imenukuliwa katika Hadithi kuwa ni siku bora zaidi mbele ya Allah تعالى. Na Kauli Yake:

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baariy 2:530.

<sup>2</sup> Ahmad 2:75.

<sup>3</sup> Al-Bukhaari: Idi mbili, mlango wa Fadhila za Amali katika Siku za Tashriq.

<sup>4</sup> Muslim 2:819.

عَلَىٰ مَا رَزَقَهُم مِّنْ بَهِيمَةِ الْأَنْعَامِ ط

**“Juu ya nyama hoa aliowaruzuku.”**

Maana yake: Ngamia, ng'ombe na kondoo, kama Alivyoeleza Aliyetukuka katika Suratul An'aam:

ثُمَّ نَبِيَّةَ أَزْوَاجِ ط

**“(Amekuumbieni) namna nane za wanyama.” (6:143).**

فَكُلُوا مِنْهَا وَأَطِعُوا أَبْيَاسَ الْفَقِيرِ ﴿١٨﴾

**“Basi kuleni katika hao mlisheni mwenye shida aliyefakiri.”**

Hii ni kama ilivyothibiti kuwa Mtume ﷺ alipochinja mnyama wake, aliamuru kuwa sehemu ya kila mnyama ichukuliwe na kupikwa, naye akala sehemu ya nyama na akanywa sehemu ya mchuzi wake.<sup>1</sup>

فَكُلُوا مِنْهَا

**“Basi kuleni katika hao.”**

Amepokea Hushaym kutoka kwa Huswayn kuwa Mujaahid amesema yafuatayo kuhusu Kauli Yake:

وَإِذَا حَلَلْتُمْ فَاصْطَادُوا ؕ

**“Na mkishatoka katika Hija yenu basi windeni (mukitaka).” (5:2),**

فَإِذَا قُضِيَتِ الصَّلَاةُ فَانْتَشِرُوا فِي الْأَرْضِ

**“Na itakapokwisha Sala, tawanyikeni katika ardhi.” (62:10) <sup>2</sup>**

Na hii ni chaguo la Ibn Jariir رحمه الله تعالى katika Tafsiri yake. Na Kauli Yake:

أَبْيَاسَ الْفَقِيرِ ﴿١٨﴾

**“Mwenye shida aliye fakiri.”**

<sup>1</sup> Ahmad 1:314.

<sup>2</sup> Tabari 18:611.

Amesema 'Ikrimah: "Huyo ni yule mwenye shida sana ambaye shida yake iko wazi, na fakiri aliyejizuia kuomba omba"<sup>1</sup>. Na amesema Mujaahid: "Huyo ni yule ambaye hanyooshi mkono kuomba (au kutaka usaidizi)"<sup>2</sup>. Na Kauli Yake:

ثُمَّ لِيَقْضُوا تَفَثَهُمْ

**"Kisha wajisafishe taka zao".**

Amepokea 'Aliy bin Abi Twalhah kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: "Huko ni kutoka katika Ihramu kwa kunyoa, kuvaa nguo, kukata kucha na mfano wake"<sup>3</sup>. Na hivyo ndivyo alivyopokea 'Atwaa' na Mujaahid kutoka kwake<sup>4</sup>. Na hivyo ndivyo alivyosema 'Ikrimah na Muhammad bin Ka'b Al-Quradhwiyy<sup>5</sup>.

Na Kauli Yake:

وَلْيُوفُوا نُذُورَهُمْ

**"Na waondoe nadhiri zao".**

Amepokea 'Aliy bin Abi Twalhah kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: "Hiyo ina maana ya nadhiri yoyote iliyowekwa ya kuchinja ngamia"<sup>6</sup>. Na Kauli Yake:

وَلْيَطُوفُوا بِالْبَيْتِ الْعَتِيقِ ﴿٢٤﴾

**"Na waizunguke Nyumba ya Kale".**

Amesema Mujaahid: "Hiyo ni twawafu ya wajibu siku ya kuchinja"<sup>7</sup>. Na amepokea Ibn Abi Haatim kuwa Abi Hamzah amesema: Aliniambia Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: "Je, umesoma Suratul Hajj pale Allah تعالى Anaposema:

وَلْيَطُوفُوا بِالْبَيْتِ الْعَتِيقِ ﴿٢٤﴾

**"Na waizunguke Nyumba ya Kale."**

<sup>1</sup> Tabari 18:612.

<sup>2</sup> Tabari 18:612.

<sup>3</sup> Tabari 18:613.

<sup>4</sup> Tabari 18: 610.

<sup>5</sup> Tabari 18:610.

<sup>6</sup> Tabari 18:614.

<sup>7</sup> Ad-Dur Al-Manthur 4:643.

Kwani mwisho wa Hija ni kufanya twawafu kwenye Nyumba ya Kale". Nikasema: "Na hivyo ndivyo alivyofanya Mtume ﷺ. Aliporudi kutoka Mina siku ya kuchinja, alianza na kupiga mawe kwenye Jamrah, akilipiga kwa vijiwe saba, kisha akachinja na kunyooa, kisha aliondoka na kutufu kwenye *Ka'aba*"<sup>1</sup>. Na katika Sahihi mbili kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: "Watu waliamriwa kumaliza kwa kuzuru *Kaa'ba* kwa kuitufu, lakini wanawake wenye hedhi walisahilishiwa (kusamehewa)"<sup>2</sup>.

بِالْبَيْتِ الْعَتِيقِ ﴿٢٦﴾

**"Kwa Nyumba ya Kale."**

Ilio nyuma ya *Hijr*, ambayo asili yake ilikuwa ndani ya *Ka'aba* kwa mujibu wa ujangaji wa bwana wetu Ibrahim عليه السلام pale mwanzo, lakini Maqureysh wakaitoa kutoka kwenye *Ka'aba* (pale walipoijenga tena upya) kwa sababu walipungukiwa na pesa. Kwa hiyo, Mtume ﷺ alitufu nyuma ya *Al-Hijr* na akasema kuwa *Al-Hijr* ni sehemu ya *Ka'aba*. Hakuzitambua pembe mbili za Shaami kwa sababu hazikujengwa sawasawa kwenye misingi ya asili ya Ibrahim عليه السلام. Na amepokea Qatadah kuwa Al-Hasan Al-Baswriy رحمه الله تعالى amesema yafuatayo kuhusu Aya ifuatayo:

وَلَيَطُوفُوا بِالْبَيْتِ الْعَتِيقِ ﴿٢٧﴾

**"Na waizunguke Nyumba ya Kale."**

Akasema: "Kwa sababu hiyo ilikuwa Nyumba ya kwanza iliyowekwa kwa ajili ya watu"<sup>3</sup>. Na hiyo ndiyo iliyokuwa rai ya 'Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam<sup>4</sup>.

Na kutoka kwa 'Ikrimah aliyesema: "Hakika hiyo iliitwa Nyumba ya Kale, kwa sababu ilibakia (iliokolewa) kutokana na mafuriko wakati wa Nuuh عليه السلام". Na amesema Khuswayf: "Hakika iliitwa Nyumba ya Kale kwa sababu hakuishinda juu yake jabari (dhalimu) yeyote)."

<sup>1</sup> Ibn Abi Hatim 8:2490.

<sup>2</sup> Fat'h Al-Baari 3:684 na Muslim 2:963.

<sup>3</sup> Al-Qurtwubiy 12:52

<sup>4</sup> Tabari 18:615.

ذَٰلِكَ وَمَنْ يُعْظِمِ حُرْمَتِ اللَّهِ فَهُوَ خَيْرٌ لَهُ عِنْدَ رَبِّهِ ۗ وَأُحِلَّتْ لَكُمْ الْآتَعَمُّ إِلَّا مَا  
يُتَلَىٰ عَلَيْكُمْ ۗ فَاجْتَنِبُوا الرِّجْسَ مِنَ الْأَوْثَانِ وَاجْتَنِبُوا قَوْلَ الزُّورِ ﴿٢٣﴾ حُتْفَاءَ اللَّهِ  
غَيْرِ مُشْرِكِينَ بِهِ ۗ وَمَنْ يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَكَأَنَّمَا خَرَّ مِنَ السَّمَاءِ فَتَخَطَّفَهُ الطَّيْرُ أَوْ تَهْوَىٰ بِهِ  
الرِّيحُ فِي مَكَانٍ سَحِيقٍ ﴿٢٤﴾

**30. Ndio hivyo iwe! Na anayevitukuza vitakatifu vya Allah basi hayo ndiyo kheri yake mbele ya Mola wake Mlezi. Na mumehalalishiwa nyama hoa ila wale mliosomewa. Basi jiepusheni na uchafu wa masanamu, na jiepusheni na usemi wa uongo.**

**31. Kwa kumtakasikia Imani Allaah, bila ya kumshirikisha. Na anayemshirikisha Allah ni kama kwamba ameporomoka kutoka mbinguni, kisha ndege wakamnyakua au upepo ukamtupa pahala mbali.**

### Ujira kwa Kuepuka Maasi

Anasema Aliyetukuka: “Haya ni yale Tuliyo waamrisha nyinyi kufanya katika taratibu za Hija, na kwa thawabu nyingi atakazopata”.

وَمَنْ يُعْظِمِ حُرْمَتِ اللَّهِ

**“Na anayevitukuza vitakatifu vya Allah.”**

Maana yake: Atakayejipusha na maasi na Aliyoyaharamisha na ikawa kufanya maasi hayo ni kosa kubwa kwake.

فَهُوَ خَيْرٌ لَهُ عِنْدَ رَبِّهِ ۗ

**“Basi hayo ndiyo kheri yake mbele ya Mola wake Mlezi.”**

Maana yake: Atapata kheri na thawabu nyingi kwayo (kwa kutekeleza hayo). Hiyo ni kama yule anayefanya utiifu atapata thawabu nyingi na ujira mkubwa, hivyo hivyo kwa mwenye kuacha ya haramu na kujiepusha na yaliyokatazwa, atapata thawabu nyingi.

## Uhalali wa Nyama Hoa

Na Kauli Yake:

وَأُحِلَّتْ لَكُمْ الْبَهِيمَةُ إِلَّا مَا يُتْلَى عَلَيْكُمْ

**“Na mumehalalishiwa nyama hoa ila wale mlisosomewa.”**

Maana: Tumewahalalishia nyinyi nyama hoa wote. Na Kauli Yake:

مَا جَعَلَ اللَّهُ مِنْ بَهِيمَةٍ وَلَا سَائِبَةٍ وَلَا وَصِيلَةٍ وَلَا حَامٍ

**“Mwenyezi Mungu Hakujaalia uharamu wowote juu ya “Bahira” wala “Saiba” wala “Wasila” wala “Hami.” (5:103)**

إِلَّا مَا يُتْلَى عَلَيْكُمْ

**“Ila wale mlisosomewa.”** Maana yake: Kuharamishwa kwa mzoga damu na nyama ya Nguruwe.

وَمَا أَهْلٌ لغيرِ اللَّهِ بِهِ وَالْمُنْحَنِيقَةُ

**“...na mnyama aliyechinjwa si kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na aliyekufa kwa kunyongeka koo....” (5:3)**

Amesema hilo Ibn Jariir رحمه الله تعالى, aliyepokea kwa Qatadah<sup>1</sup>.

## Amri ya Kujiepusha Ushirikina na Uongo

Na Kauli Yake:

فَأَجْتَنِبُوا الرِّجْسَ مِنَ الْأَوْثَانِ وَأَجْتَنِبُوا قَوْلَ الزُّورِ ﴿٢٤﴾

**“Basi jiepusheni na uchafu wa masanamu, na jiepusheni na usemi wa uongo.”**

Hapa inabainisha neno *Ar-Rijs*, maana kujiepusha na uchafu, ambao ni masanamu. Na kumshirikisha Allah تعالى kumeambatanishwa na kauli ya uongo, hii ni kama Aya ifuatayo:

قُلْ إِنَّمَا حَرَّمَ رَبِّي الْفَوَاحِشَ مَا ظَهَرَ مِنْهَا وَمَا بَطَنَ وَالْإِثْمَ وَالْبَغْيَ بِغَيْرِ الْحَقِّ وَأَنْ

تُشْرِكُوا بِاللَّهِ مَا لَمْ يُنَزَّلْ بِهِ سُلْطَانًا وَأَنْ تَقُولُوا عَلَى اللَّهِ مَا لَا تَعْمَلُونَ ﴿٢٥﴾

<sup>1</sup> Tabari 18:618.



**“Sema: Mola wangu Mlezi Ameharamisha mambo machafu, yaliyodhihirika na yaliyofichika, na dhambi na kutoka katika taa (ya wakubwa) pasipo haki, na kumshirikisha Allah na ambacho Hakukiteremshia dalili na kusema juu ya Allah msiyoyajua.”(7:33).**

Na hiyo inajumlisha ushuhuda wa uongo. Na katika Sahihi mbili kutoka kwa Abi Bakrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«أَلَا أُنَبِّئُكُمْ بِأَخْبِرِ الْكِبَائِرِ؟»

“Je, siwajulishi madhambi yaliyo makubwa?”

Tukasema: “Ndio, ewe Mtume wa Allah!” Akasema:

«الْإِشْرَاكَ بِاللَّهِ وَعُقُوقُ الْوَالِدَيْنِ»

“Kumshirikisha Allah, kuwaasi wazazi wawili”.

Na alikuwa ameegemea, akaketi wima, akasema:

أَلَا وَقَوْلُ الزُّورِ، أَلَا وَشَهَادَةُ الزُّورِ»

“Tahadharini, na kauli ya uongo, na ushuhuda wa uongo.”

Aliendelea kukariri mpaka tukasema: “Laiti angenyamaza.”<sup>1</sup>

Na amepokea Imamu Ahmad kuwa Khuraym bin Faatik al-Asadiy رضي الله عنه amesema: “Mtume ﷺ aliswali Swala ya Asubuhi, na pindi alipomaliza, alisimama na kusema:

«عَدَلْتُ شَهَادَةَ الزُّورِ الْإِشْرَاكَ بِاللَّهِ عَزَّ وَجَلَّ»

‘Ushuhuda wa uongo ni sawa na kumshirikisha Allah Aliyetukuka’

Kisha akasoma:

فَاجْتَنِبُوا الرِّجْسَ مِنَ الْأَوْثَانِ وَاجْتَنِبُوا قَوْلَ الزُّورِ ﴿٢٤﴾ حُنْفَاءَ لِلَّهِ غَيْرَ مُشْرِكِينَ بِهِ<sup>٢</sup>

**‘Basi jiepusheni na uchafu wa masanamu, na jiepusheni na usemi wa uwongo. Kwa kumtakasikia Imani Allah, bila ya kumshirikisha.’<sup>2</sup>**

Na Kauli Yake:

<sup>1</sup> Fat’h Al-Baariy 10:419 na Muslim 1:91. <sup>2</sup> Ahmad 4:321.

حُتَفَاءَ لِلَّهِ

**“Kwa kumtakasikia Imani Allah.”**

Maana yake: Kumtakasia Dini Yake kwa kumnyenyekea, kujiepusha na batili na kutafuta pamoja na kuitaka haki. Kwa hiyo Akasema:

غَيْرَ مُشْرِكِينَ بِهِ<sup>٤</sup>

**“Bila ya kumshirikisha.”**

Kisha Akawapigia washirikina mfano kwa upotevu walio nao, uangamivu na kuwa mbali sana na uwongofu wa kweli. Akasema:

وَمَنْ يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَكَأَنَّمَا خَرَّ مِنَ السَّمَاءِ

**“Na anayemshirikisha Allah ni kama kwamba ameporomoka kutoka mbinguni.”**

Maana yake: Kuanguka kutoka kwayo.

فَتَخَطَّفَهُ الطَّيْرُ

**“Kisha ndege wakamnyakua.”**

Maana yake: Ndege wakamkamata hewani,

أَوْ تَهْوَىٰ بِهِ الرِّيحُ فِي مَكَانٍ سَحِيقٍ ﴿٥﴾

**“Au upepo ukamtupa pahala mbali.”**

Maana yake: Mbali na hatari kwa yeyote mwenye kutua hapo. Kwa hiyo, imekuja katika Hadithi ya Baraa' رضي الله عنه:

«إِنَّ الْكَافِرَ إِذَا تَوَفَّتْهُ مَلَائِكَةُ الْمَوْتِ وَصَعِدُوا بِرُوحِهِ إِلَى السَّمَاءِ، فَلَا تَنْفَعُ لَهُ أَبْوَابُ السَّمَاءِ بَلْ تُطْرَحُ رُوحُهُ طَرْحًا مِنْ هُنَاكَ»

*“Hakika kafiri anapotolewa roho na Malaika wa mauti na akapanda na roho yake mbinguni, kamwe milango ya mbingu haitafunguliwa kwake; kinyume chake, roho yake itarushwa chini kutoka huko”.*

Kisha akasoma ayah hii<sup>1</sup>. Hakika Hadithi hiyo tayari tumeitaja katika maelezo yetu ya Suratul Ibrahimu<sup>2</sup>.

Na hakika Allah تعالى Amewapigia washirikina mfano mwingine katika Suratul An'am, nayo ni Kauli Yake:

قُلْ أُنَدِّعُوا مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَا يَنْفَعُنَا وَلَا يَضُرُّنَا وَنُرَدُّ عَلَىٰ أَعْقَابِنَا بَعْدَ إِذْ هَدَيْتَنَا اللَّهُ  
كَالَّذِي اسْتَهْوَتْهُ الشَّيَاطِينُ فِي الْأَرْضِ حَيْرَانَ لَهُ أَصْحَابٌ يَدْعُونَهُ إِلَىٰ الْهُدَىٰ أُنْتِنَا  
قُلْ إِنَّ هُدَىٰ اللَّهِ هُوَ الْهُدَىٰ

*“Sema: Je, tuwaabudu wasiokuwa Allah ambao hawatupi faida wala hawawezi kutudhuru, na turudishwe nyuma baada ya Allah Kutuongoza, tuwe sawa na wale ambao mashetani wamewapoteza; akiwayawaya katika ardhi? Wanao marafiki wanaowaita katika uongofu (wakisema): Njooi kwetu. Sema: Uongozi hasa ni uongozi wa Allah.” (6:71).*

\* \* \*

<sup>1</sup> Ahmad 4:287.

<sup>2</sup> Tazama maelezo katika Tafsiri ya Surah Ibrahimu (14): 27.

ذَٰلِكَ وَمَنْ يُعْظِمَ شَعِيرَ اللَّهِ فَإِنَّهَا مِنْ تَقْوَى الْقُلُوبِ ﴿٣٢﴾ لَكُمْ فِيهَا مَنَافِعُ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ثُمَّ مَحْلُوهَا إِلَى الْبَيْتِ الْعَتِيقِ ﴿٣٣﴾ وَلِكُلِّ أُمَّةٍ جَعَلْنَا مَنْسَكًا لِّيَذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَىٰ مَا رَزَقْنَاهُمْ مِنْ بَهِيمَةٍ ۗ فَلَا تَهْكُرُوا إِلَهَهُ وَاحِدًا ۗ فَلَهُ أَسْلِمُوا ۗ وَبَشِّرِ الْمُخْبِتِينَ ﴿٣٤﴾ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَّت قُلُوبُهُمْ وَالصَّابِرِينَ عَلَىٰ مَا أَصَابَهُمُ وَالْمُفِئِمِي الصَّلَاةَ وَبِمَا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ﴿٣٥﴾ وَالَّذِينَ جَعَلْنَاهَا لَكُمْ مِنَ شَعِيرٍ ۗ اللَّهُ لَكُمْ فِيهَا حَزِيرٌ ۗ فَاذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهَا صَوَافٍ ۗ فَإِذَا وَجَبَتْ جُنُوبُهَا فَكُلُوا مِنْهَا وَأَطْعِمُوا الْقَانِعَ وَالْمُعْتَرَّ ۗ كَذَٰلِكَ سَخَّرْنَاهَا لَكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٣٦﴾ لَنْ يَنَالَ اللَّهُ هُتُومَهَا وَلَا دِمَاؤَهَا وَلَكِنَّ يَتَأَلَّهُ التَّقْوَىٰ مِنْكُمْ ۗ كَذَٰلِكَ سَخَّرَهَا لَكُمْ لِتُكَبِّرُوا اللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَاكُمْ ۗ وَبَشِّرِ الْمُحْسِنِينَ ﴿٣٧﴾

ذَٰلِكَ وَمَنْ يُعْظِمَ شَعِيرَ اللَّهِ فَإِنَّهَا مِنْ تَقْوَى الْقُلُوبِ ﴿٣٢﴾ لَكُمْ فِيهَا مَنَافِعُ إِلَىٰ أَجَلٍ مُّسَمًّى ثُمَّ مَحْلُوهَا إِلَى الْبَيْتِ الْعَتِيقِ ﴿٣٣﴾

**32. Ndio hivyo! Na anayetukuza ibada za Allah, basi hayo ni katika unyenyekevu wa nyoyo.**

**33. Katika hao nyinyi muna manufaa mpaka muda maalumu. Kisha pahala pa kuchinjwa kwake ni kwenye Nyumba ya Kale.**

**Ubainifu wa kuchinja na Kutukuza Ibada za Allah**

Anasema haya Aliyetukuka:

وَمَنْ يُعْظِمَ شَعِيرَ اللَّهِ

**“Na anayetukuza ibada za Allah”.** Maana yake: Kufuata mamrishi Yake.

فَإِنَّهَا مِنْ تَقْوَى الْقُلُوبِ ﴿٣٢﴾

**“Basi hayo ni katika unyenyekevu wa nyoyo”.**

Na katika hiyo ni kutukuza na kutoa kichinjwa cha Ngamia kwa njia nzuri, kama alivyopokea Al-Hakam kutoka kwa Miqsam kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Kuwatukuza ni kuchagua mnyama mnono, mwenye siha na aliye bora (kwa ajili ya kumchinja)”<sup>1</sup>. Na amesema Abu Umamah bin Sahl: “Ilikuwa tukiwanonesha dhabihu tukiwa Madina, na Waislamu walikuwa wakiwanonesha”. Imepokewa na Bukhari<sup>2</sup>.

<sup>1</sup> Tabariy 18:621.

<sup>2</sup> Fat’h Al-Baariy 10:11.

Na katika Sunan Ibn Maajah kutoka kwa Abi Raafi' رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alichinja kondoo wawili wakubwa, wanono na wenye pembe<sup>1</sup>. Na hivyo ndivyo alivyopokea Abu Daud na Ibn Maajah kutoka kwa Jaabir رضي الله عنه aliyesema: Alichinja Mtume ﷺ kondoo wawili waliohasiwa, wanono na wenye pembe<sup>2</sup>. Na 'Aliy رضي الله عنه amesema: Mtume ﷺ ametuamuru kuwatazama macho na masikio, na kutowachinja *Muqaabalah, Mudaabarah, Sharqaa* wala *Kharqaa*". Imepokewa na Ahmad na watu wa Sunan, na akaisahihisha At-Tirmidhiy<sup>3</sup>.

Na ama "*Muqaabilah*" ni yule ambaye sikio lake limekatika sehemu ya mbele. Na "*Mudaabarah*" ni yule ambaye sikio lake limekatika sehemu yake ya nyuma. Na "*Sharqaa*" ni yule sikio lake limekatika kwa urefu (katikati), kama alivyosema Ash-Shaafi'iy na Al-Asma'iy. Na ama *Kharqaa*' ni yule ambaye sikio lake lina tundu. Na Allah تعالى Anajua zaidi. Na Al-Baraa' رضي الله عنه amesema: Amesema Mtume ﷺ:

«أَرَبُّعٌ لَّا تَجُوزُ فِي الْأَصَاغِي: الْعَوْرَاءُ الْبَيِّنُ عَوْرَهَا، وَالْمَرِيضَةُ الْبَيِّنُ مَرَضُهَا،  
وَالْعَرَجَاءُ الْبَيِّنُ طَلْعُهَا، وَالْكَسِيرَةُ الْبَيِّنُ لَأْتُنِّي»

*"Wanyama aina nne hawafai kuchinjwa kwa ajili ya dhabihu: Chongo iliyo wazi (kuwa na jicho moja), aliye na maradhi bayana kabisa, wenye vilema vya wazi na waliovunjika mifupa, ambaye hakuna anayetaka kumchagua".*

Imepokewa na Ahmad na watu wa Sunan, na ikisahihishwa na At-Tirmidhiy<sup>4</sup>.

## Manufaa ya Ngamia wa Kuchinjwa

Na Kauli Yake:

لَكُرْفِيَا مَنفَعُ

***"Katika hao nyinyi muna manufaa."*** Maana yake: kwenu nyinyi mna manufaa kwa ngamia waliowekwa kuwa vichinjwa kwa kupata maziwa yao, sufi, nywele zao na pia kuwapanda.

<sup>1</sup> Ahmad 6:8, na ni yeye pekee aliyepokea Hadithi hiyo kama ilivyoielezwa na mwandishi wa Jaami' Al-Masaaniyd was Sunan 14:21.

<sup>2</sup> Abu Daud 3:231 na Ibn Maajah 2:1043.

<sup>3</sup> Ahmad 1:108, Abu Dawud 3:237, Tuhfatul Al-Ahwadhiy 5:82, An-Nasaa'iy 7:217 na Ibn Maajah 2:1050.

<sup>4</sup> Ahmad 4:284, Abu Dawud 2802, At-Tirmidhiy 1497, An-Nasaa'iy 7:215 na Ibn Majah 3144.

لَكُرْفِيهَا مَنَفَعُ إِلَى أَجَلٍ مُّسَيِّ

**“Katika hao nyinyi mna manufaa mpaka muda maalumu.”**

Amepokea Miqsam kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema yafuatayo kuhusu Aya ifuatayo:

لَكُرْفِيهَا مَنَفَعُ إِلَى أَجَلٍ مُّسَيِّ

**“Katika hao nyinyi mna manufaa mpaka muda maalumu.”**

Akasema: ‘Mpaka mtakapoamua kuwafanya dhabihu (wa kuchinja)’<sup>1</sup>. Panasemwa: “Ni kwake kunufaika naye hata kama ni dhabihu, akihitajia kufanya hivyo kama ilivyothibiti katika Sahihi mbili kutoka kwa Anas رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alimuona mtu akimpeleka dhabihu wake, akamuambia:

«ارْكَبْهَا»

“Mpande Akasema: ‘Hakika huyu ni dhabihu wangu’. Akamuambia:

«ارْكَبْهَا وَيُحَكِّ»

“Mpande ole wako!” Katika usemi wake wa pili au watatu<sup>2</sup>.

Na katika riwaya ya Muslim kutoka kwa Jaabir رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«ارْكَبْهَا بِالْمَعْرُوفِ إِذَا أَلْجَيْتَ إِلَيْهَا»

“Mpande kwa wema kulingana na mahitaji yako”<sup>3</sup>.

Na Kauli Yake:

تُرْمَحِلُّهَا إِلَى الْبَيْتِ الْعَتِيقِ ﴿٢٦﴾

**“Kisha pahala pa kuchinjiwa kwake ni kwenye Nyumba ya Kale.”**

Maana: Mwishowe wanaletwa katika sehemu ya Nyumba ya Kale – ambayo ni Ka’bah, kama Anavyosema Aliyetukuka:

هَدْيًا بَلِغَ الْكَعْبَةِ

**“Mnyama huyo apelekwe iliko Ka’bah.” (5:95).** Na pia,

<sup>1</sup> Tabari 18:623.

<sup>2</sup> Fat’hul Al-Baari 5:450 na Muslim 2:960.

<sup>3</sup> Muslim 2:961.

وَأَهْدَىٰ مَعَكُوفًا أَنْ يَبْلُغَ مَحَلَّهُ<sup>٥</sup>

“...Na wakawazuilia wale wanyama (wa kuchinjwa) wasifike mahala pake...” (48:25).

وَلِكُلِّ أُمَّةٍ جَعَلْنَا مَنَسَكًا لِّيَذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُمْ مِنْ بَهِيمَةِ الْأَنْعَامِ ۗ فَإِنَّهُمْ  
إِلَيْهِ وَاحِدٌ ۖ فَلَهُ أَسْلِمُوا ۗ وَبَشِّرِ الْمُخْبِتِينَ ﴿٥٥﴾ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَّتْ قُلُوبُهُمْ  
وَالصَّابِرِينَ عَلَىٰ مَا أَصَابَهُمْ وَالْمُقِيمِي الصَّلَاةِ وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ﴿٥٦﴾

34. Na kila umma Tumewafanyia mahala pa kuchinjia dhabihu wa ibada ili walitaje Jina la Allah juu ya vile walivyoruzukiwa katika wanyama wa mifugo. Basi Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu. Jisalimishieni Kwake tu, na wabashirie wanyenyekevu,

35. Ambao, anapotajwa Allah nyoyo zao hutetemeka, na wanaovumilia kwa yanaowasibu, na wanaoshika Swala, na wanatoa katika Tulivyowaruzuku.

### Ibada ya Kuchinja ni Sharia Iliyowekwa kwa Kila Umma Duniani

Allah تعالیٰ Anatueleza kuwa kuchinja na kumwaga damu kwa Jina la Allah تعالیٰ ni sharia iliyowekwa kwa mataifa yote. Amepokea ‘Aliy bin Abi Twalhah kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema:

وَلِكُلِّ أُمَّةٍ جَعَلْنَا مَنَسَكًا

“Na kila ummah Tumewafanyia mahala pa kuchinjia dhabihu wa ibada”.

Maana yake: Sherehe. ‘Ikrima amesema: “Kuchinja mihanga”. Na Kauli Yake:

وَلِكُلِّ أُمَّةٍ جَعَلْنَا مَنَسَكًا

“Na kila umma Tumewafanyia mahala pa kuchinjia dhabihu wa ibada”.

Zayd bin Aslam amesema: “Hii inamaanisha Makka; Allah تعالى Hakuchagua sherehe za kidini mahala pengine popote kwa Umma wowote”<sup>1</sup>.

لَيَذَكَّرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَىٰ مَا رَزَقَهُمْ مِّنْ بَهِيمَةٍ آلَا تَعْمُرُونَ

**“Ili walitaje Jina la Allah juu ya vile walivyoruzukiwa katika wanyama wa mifugo”.**

Imenukuliwa katika Sahihi mbili kuwa Anas رضي الله عنه amesema: “Mtume ﷺ alileta kondoo wawili wanono, wenye pembe; akasema: *Bismillah* (Kwa Jina la Allah تعالى) na *Allahu Akbar* (Allah ni Mkubwa), kisha akaweka mguu wake juu ya shingo zao”<sup>2</sup>. Na Kauli Yake:

فَاللَّهُمَّ إِلَهُ وَاحِدٌ فَلَهُ أَسْلَمُوا

**“Basi Mungu wenu ni Mungu Mmoja tu. Jisalimishieni Kwake tu”.**

Maana yake: Mungu wenu ni Mmoja tu, japokuwa sheria za Manabii zimetofautiana na kutengua moja katika nyingine. Manabii wote waliwaita wanadamu kumuabudu Allah تعالى Peke Yake bila ya mshirika wala mwenzu. Allah تعالى Anasema:

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِي إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنَا فَاعْبُدُونِ ﴿٢١﴾

**“Na Hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila Tulimfunulia ya kwamba hakuna aabudiwaye ila Mimi, basi Niabuduni.” (21:25).**

Allah تعالى Anasema:

فَلَهُ أَسْلَمُوا

**“Jisalimishieni Kwake tu”.**

Maana yake: Jisalimisheni kwa Amri Zake na mumtii Yeye kwa ikhlaswi. Na Kauli Yake:

<sup>1</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 6:48.

<sup>2</sup> Fat'h ul Al-Baariy 10:25 na Muslim 3:1556.



وَبَشِّرِ الْمُخْبِتِينَ ﴿٣٢﴾

**“Na wabashirie wanyenyekevu.”**

Mujaahid amesema yafuatayo kuhusu neno *Mukhbitiin*, “Hao ni wale wenye kuridhia”<sup>1</sup>. Ath-Thawriy رحمه الله تعالى amesema: “Hao ni wale wenye kuridhia na wenye kukubali Kudura ya Allah na kujisalimisha Kwake”<sup>2</sup>. Ni bora kuifasiri kwa ibara inayokuja baadaye, ambayo ni:

الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَّتْ قُلُوبُهُمْ

**“Ambao, anapotajwa Allah nyoyo zao hutetemeka.”**

Maana yake: Nyoyo zao zinamuogopa. Na Kauli Yake:

وَالصَّابِرِينَ عَلَىٰ مَا أَصَابَهُمْ

**“Na wanaovumilia kwa yanaowasibu.”**

Maana yake: Misiba na mitihani. Na Kauli Yake:

وَالْمُقِيمِي الصَّلَاةِ

**“Na wanaoshika Sala.”**

Maana yake: Wanatekeleza majukumu yao walioamriwa na Allah تعالى, jukumu la kutekeleza Swala ya faradhi. Na Kauli Yake:

وَمِمَّا رَزَقْنَاهُمْ يُنفِقُونَ ﴿٣٤﴾

**“Na wanatoa katika Tulivyowaruzuku.”**

Maana yake: Riziki ambayo wamepewa na Allah تعالى. Wanatumia kwa ajili ya familia zao na watumishi wao, na kwa masikini na mafakiri; wanaishi na watu kwa ukarimu na huruma huku wakibaki katika mipaka iliyowekwa na Allah تعالى. Hii ni tofauti kabisa na wanafiki, ambao wako kinyume na haya yote, kama tulivyoelezea katika Tafsiri ya Surah Baraa’ah (9)<sup>3</sup>. Na Allah تعالى Ndiye Mwenye Sifa Njema zote, Neema na Baraka.

<sup>1</sup> Tabari 18:628.

<sup>2</sup> Tafsiyr Ath-Thawriy 213.

<sup>3</sup> Tizama Tafsiri ya 9:67.

وَالْبُدْنَ جَعَلْنَاهَا لَكُمْ مِّنْ شَعْتِيرِ اللَّهِ لَكُمْ فِيهَا خَيْرٌ فَأَذْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهَا صَوَافٍ إِذَا  
 وَجَبَتْ جُنُوبَهَا فَكُلُوا مِنْهَا وَأَطِعُوا الْقَانِعَ وَالْمُعْتَرَّ كَذَلِكَ سَخَّرْنَاهَا لَكُمْ لَعَلَّكُمْ  
 تَشْكُرُونَ ﴿٣٦﴾

**36. Na ngamia wa sadaka Tumekufanyieni kuwa ni kudhihirisha matukuzo kwa Allah; kwa hao mna kheri nyingi. Basi litajeni Jina la Allah juu yao wanapo simama kwa safu. Na waangukapo ubavu kuleni katika hao na walisheni walio kinai na wanaolazimika kuomba. Ndio kama hivi Tumewafanya hawa wanyama dhalili kwenu ili mpate kushukuru.**

### Amri ya Kuchinja Ngamia wa Sadaka

Hapa Allah تعالى Anawakumbusha waja Wake kwa neema Aliyowapatia, kwa kuwaambia ngamia wa sadaka kwao na kuwafanya kuwa moja ya ishara Yake. Hakika Yeye Amekadiria kuwa waletwe kwenye Ka'aba (Nyumba) Yake Tukufu; bila shaka, wao ndio bora kabisa kwa wanaotolewa sadaka kwa ajili ya Allah تعالى, kama Anavyosema:

لَا تُحِلُّوا شَعْتِيرَ اللَّهِ وَلَا الشَّهْرَ الْحَرَامَ وَلَا الْهَدْيَ وَلَا الْقَلَائِدَ وَلَا آمِينَ النَّبِيِّتِ الْحَرَامِ

**“Msivunje heshima ya matukufu ya Allah wala heshima ya mwezi uliotukuzwa, wala heshima ya wanyama wanaopelekwa Makka, wala heshima ya wale wakusudiyao kwenda kwenye Nyumba Takatifu.” (5:2).**

Na hapa Anasema:

وَالْبُدْنَ جَعَلْنَاهَا لَكُمْ مِّنْ شَعْتِيرِ اللَّهِ

**“Na ngamia wa sadaka Tumekufanyieni kuwa ni kudhihirisha matukufu ya Allaah”.**

Ibn Jurayj amesema: ‘Atwaa’ ameifasiri Aya hii kwa kusema, ‘Ng’ombe na Ngamia’<sup>1</sup>. Rai mfano wake imenukuliwa kutoka kwa Ibn ‘Umar رضي الله عنهما, Sa’id bin Musayyib na Hasan Baswriy<sup>2</sup>. Mujaahid amesema: “Al-Budn

<sup>1</sup> Tabari 18:630.

<sup>2</sup> Muslim 2:882.

inamaanisha ngamia”<sup>1</sup>. Na katika nukuu nyingine inasemwa kuwa *Budhu* ina maana ya ngombe, kisha kongamano la wanachuoni limesema kuwa itawatoshelezea watu saba kushirikiana kuchinja ngamia mmoja. Kulingana na mapokezi ya Muslim kutoka kwa Jaabir bin ‘Abdallah رضي الله عنه na wengine wamesema: “Mtume ﷺ alitumuru kushirikiana katika kuchinja mnyama, ngamia kwa watu saba na ng’ombe mmoja kwa watu saba”<sup>2</sup>. Na Kauli Yake:

لَكَمْ فِيهَا خَيْرٌ<sup>ط</sup>

**“Kwa hao mna kheri nyingi”.** Maana yake: Thawabu Kesho Akhera.

فَادْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَيْهَا صَوَافٍ<sup>ط</sup>

**“Basi litajeni Jina la Allaah juu yao wanaposimama kwa safu”.**

Imepokewa na al-Mutwalib bin ‘Abdallah kuwa Jaabir bin Abdallah رضي الله عنه amesema: “Niliswali pamoja na Mtume ﷺ siku ya Idil-Adhha. Alipomaliza, alimleta kondoo, akamchinja huku akisema:

«بِاسْمِ اللَّهِ وَاللَّهِ أَكْبَرُ، اللَّهُمَّ هَذَا عَنِّي وَعَمَّنْ لَمْ يُضَحَّ مِنْ أُمَّتِي»

*‘Kwa Jina la Allah, na Allah ni Mkubwa. Ewe Allah, huyu ni kwa niaba yangu na yeyote katika Umma wangu aliyekosa kuchinja”.*

Hii imepokewa na Ahmad, Abu Daud na At-Tirmidhiy<sup>3</sup>. Muhammad bin Ishaq رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Yazid bin Al-Habiyb kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنه kuwa Jaabir رضي الله عنه amesema: “Mtume ﷺ alichinja kondoo wawili siku ya Idi, na pindi alipowalaza ili kuwachinja alisema:

«وَجَّهْتُ وَجْهِيَ لِلَّذِي فَطَرَ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضَ حَنِيفًا مُسْلِمًا وَمَا أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ،  
إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ لَا شَرِيكَ لَهُ، وَبِذَلِكَ أُمِرْتُ  
وَأَنَا أَوَّلُ الْمُسْلِمِينَ، اللَّهُمَّ مِنْكَ وَلَكَ عَن مُحَمَّدٍ وَأُمَّتِهِ»

*‘Nimegeuza uso wangu kwa Yule Aliyeumba mbingu na ardhi, nikiwa muongofu, mtii (mkweli na mwenye ikhlaswi halisi, nikinyenyekea*

<sup>1</sup> Ibn Abi Shaybah, sehemu ambayo haijchapishwa 367.

<sup>2</sup> Muslim 2:882.

<sup>3</sup> Ahmad 3:356, Abu Daawud 3:230 na Tuhfah Al-Ahwadhiy 5:113.

*Kwake tu), nami si miongoni mwa wanaomshirikisha (Allah). Hakika Swala yangu, Ibada zangu (zote nyingine), uzima wangu na kufa kwangu; ni kwa Allah. Muumba wa walimwengu wote. Hana mshirika wake kabisa. Na haya ndiyo niliyoamrisha, na mimi ni wa kwanza wa waliojisalimisha. Ewe Allah, tumetoka Kwako na tunarudi Kwako, kwa niaba ya Muhammad na Ummah wake.”*

Kisha akasema: “*Bismillah na Allahu Akbar, na akawachinja*”<sup>1</sup>. Na amepokea ‘Aliy bin al-Husayn kutoka kwa Abu Raafi’ رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ alipokuwa anataka kuchinja, alikuwa akinunua kondoo wawili wanono, wenye pembe, walio wazuri. Alipomaliza kuswali na kuhutubia watu, alikuwa akimleta mmoja wao pale alipokuwa amesimama kwa ajili ya Sala, akamchinja mwenyewe na kisu, kisha akasema:

«اللَّهُمَّ هَذَا عَنْ أُمَّتِي جَمِيعِهَا: مَنْ شَهِدَ لَكَ بِالتَّوَجِيدِ وَشَهِدَ لِي بِالْبَلَاغِ»

*“Ewe Allah, huyu ni kwa niaba ya Umma wangu wote: yule anayekupwekesha na kushuhudia kuwa nimefikisha.”*

Kisha analetwa mwingine, na akamchinja yeye mwenyewe. Kisha akasema:

«هَذَا عَنْ مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ»

*“Huyu ni wa Muhammad na ahli (familia) ya Muhammad”.*

Kwayo akawalisha masikini wote, akala mwenyewe pamoja na familia yake. Imepokewa na Ahmad na Ibn Maajah.<sup>2</sup>

Na amepokea al-A’mash kutoka kwa Abi Dhawabiyaan kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema yafuatayo kuhusu Aya ifuatayo:

فَادْكُرُوا اسْمَ اللَّهِ عَلَيْنَا صَوَافٍ

***“Basi litajeni Jina la Allah juu yao wanaposimama kwa safu.”***

Akasema: ‘Kusimama kwa miguu mitatu, ikiwa mguu wa mbele wa kushoto umefungwa’. Akasema: “*Bismillaahi na Allahu Akbar Laa ilaaha illaa Llaahu” Allaahumma Minka wa Laka* (Kwa Jina la Allah تعالى, Allah ni Mkubwa. Hapana

<sup>1</sup> Abu Daawud 3:230, 231.

<sup>2</sup> Ahmad 6:8 na Ibn Maajah 2:1043, 1044.

mola apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah تعالی. Ewe Allah تعالی, kutoka Kwako na Kwako)". Na katika Sahihi mbili kutoka kwa Ibn 'Umar رضي الله عنهما kuwa alikuja kwa mtu aliyempigisha ngamia wake magoti kwa ajili ya kumchinja. Akamuambia: "Msimamishe na huku umemfunga, hii ndio Sunnah ya Abul Qasim (Maana: Mtume Muhammad ﷺ)"<sup>1</sup>. Na Kauli Yake:

فَإِذَا وَجَبَتْ جُنُوبَهَا

**"Na waangukapo ubavu".**

Amepokea Ibn Najiyh kuwa Mujaahid amesema: "Hii ina maana anapoanguka chini kwenye ardhi"<sup>2</sup>. Nayo ni riwaya ya Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما, na Muqaatil bin Hayyaan ana rai kama hiyo. 'Abdur-Rahman bin Zayd bin Aslam amesema:

فَإِذَا وَجَبَتْ جُنُوبَهَا

**"Na waangukapo ubavu".**

Maana: Wanapokufa<sup>3</sup>. Na kauli hii ndio muradi wa Ibn'Abbaas na Mujaahid, kwani hairuhusiwi kula ngamia aliyechinjwa mpaka afe na harakati zake ziwe zimetulia. Na imepokewa katika Hadithi iliyo *Marfuu*:

«لَا تُعْجَلُوا النَّفْسَ أَنْ تَزْهَقَ»

*"Msifanye haraka mpaka muhakikishe kuwa mnyama amekufa"*<sup>4</sup>.

Na hakika amepokea Ath-Thawri رحمه الله تعالى katika Jaami' yake kuwa 'Umar bin Al- Khatwaab رضي الله عنه amesema hilo, na inaungwa mkono na Hadithi ya Shaddaad bin Aws رضي الله عنه katika Sahihi Muslim:

«إِنَّ اللَّهَ كَتَبَ الْإِحْسَانَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ فَإِذَا قَتَلْتُمْ فَأَحْسِنُوا الْقِتْلَةَ، وَإِذَا ذَبَحْتُمْ فَأَحْسِنُوا الذَّبْحَةَ، وَلْيُجِدْ أَحَدُكُمْ شَفْرَتَهُ، وَلْيُرِخْ ذَبِيحَتَهُ»

*"Hakika Allah Aameamrisha ihsani (wema) kwa kila kitu: Kwa hiyo, Mnapoua uweni vizuri, na mkichinja chinjeni vizuri. Kila mmoja wenu na akitie kisu chake makali, na akipunguzie chungu kichinjwa chake"*<sup>5</sup>.

<sup>1</sup> Al-Bukhaariy 1713.

<sup>2</sup> Tabari 18:635.

<sup>3</sup> Tabari 18:635.

<sup>4</sup> Al-Bayhaqiyy 9:278.

<sup>5</sup> Muslim 3:1548.

Na Abil Waaqid Laythiy رحمه الله تعالى amepokea kutoka kwa Mtume ﷺ amesema:

«مَا قُطِعَ مِنَ الْبَيْمَةِ وَهِيَ حَيْثُ فَهُوَ مَيْتَةٌ»

*“Chochote kinachokatwa kutoka kwa mnyama akiwa hai kitu hicho kinakuwa na hukumu ya mzoga”.*

Hii imenukuliwa na Ahmad, Abu Daud na Tirmidhi, aliyesema ni Sahihi<sup>1</sup>. Na Kauli Yake:

فَكُلُّوا مِنْهَا وَأَطِعُوا الْقَانِعَ وَالْمُعْتَرَّ

***“Kuleni katika hao na walisheni waliokinai na wanaolazimika kuomba”.***

Amri hii sio ya wajibu. Amepokea Al-‘Awfiy kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما: “Al-Qaani”<sup>2</sup>, Ni yule aliyekinai na kutosheka kwa anachopatiwa akiwa nyumbani kwake, na “Al-Mu’tarr”<sup>3</sup>, Ni yule anayejizuia kwako na kugusana mabega nawe ili umpe nyama, lakini hakuombi<sup>2</sup>. Na hivyo ndivyo alivyosema Mujaahid na Muhammad bin Ka’b Al-Quradhiy<sup>3</sup>. Na amepokea Aly bin Abi Twalhah kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Al-Qaani”, ni yule anayezuiliwa na kiburi kuomba, na “Al-Mu’tarr” ni yule mwenye kuomba<sup>4</sup>. Na hii ni kauli ya Qatadah, Ibrahimu An-Nakha’iy na Mujaahid kulingana na riwaya kutoka kwake<sup>5</sup>. Na pamesemwa kinyume na hivyo. Aya hii imechukuliwa kama dalili na wanazuoni wanaosema kuwa nyama ya *Udh-hiyah* igawanywe mara tatu: Thuluthi ni ya mwenye kuchinja atakula kwayo, thuluthi nyingine awapatie marafiki zake na thuluthi itolewe sadaka kwa masikini. Kwa kuwa Allah تعالى Anasema:

فَكُلُّوا مِنْهَا وَأَطِعُوا الْقَانِعَ وَالْمُعْتَرَّ

***“Kuleni katika hao na walisheni waliokinai na wanaolazimika kuomba”.***

Hata hivyo, hapana dalili katika Aya hii kwa rai hiyo. Kulingana na Hadithi Sahihi, Mtume ﷺ aliwaambia watu:

<sup>1</sup> Ahmad 5:518, Abu Daawud 3:277 na Tuhfah al-Ahwadhiy 5:55.

<sup>2</sup> Tabari 18:636.

<sup>3</sup> Tabari 18:636.

<sup>4</sup> Tabari 18:636, 637.

<sup>5</sup> Annasai 7:234

«إِنِّي كُنْتُ نَهَيْتُكُمْ عَنِ ادِّخَارِ لُحُومِ الْأَصْحَابِ فَوْقَ ثَلَاثِ، فَكُلُوا وَادَّخِرُوا مَا بَدَأَ لَكُمْ،

*“Hakika nilikuwa nimewakataza kuweka nyama ya udh’hiya zaidi ya siku tatu, lakini sasa kuleni kwayo na wekeni kama munavyoona kuwa ni sawa”<sup>1</sup>.*

Na katika riwaya nyingine:

«فَكُلُوا وَادَّخِرُوا وَتَصَدَّقُوا»

*“Kuleni, wekeni na toeni sadaka.”<sup>2</sup>*

Na katika riwaya nyingine:

«فَكُلُوا وَأَطِيعُوا وَتَصَدَّقُوا»

*“Kuleni, walisheni wengine na toeni sadaka.”<sup>3</sup>*

Na ama ngozi za wanyama wa chinjo, imenukuliwa katika Musnad wa Imaam Ahmad kutoka kwa Qatadah bin An-Nu’maan kuhusu Hadithi ya Udh-hiyah:

«فَكُلُوا وَتَصَدَّقُوا، وَاسْتَمْتِعُوا بِجُلُودِهَا وَلَا تَبِيعُوهَا»

*“Kuleni, toeni sadaka, tumieni ngozi zao lakini musiuze.”<sup>4</sup>*

Imepokewa na Al-Baraa’ bin ‘Azib رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ أَوَّلَ مَا نَبْدَأُ بِهِ فِي يَوْمِنَا هَذَا أَنْ نُصَلِّيَ، ثُمَّ نَرْجِعَ فَنَتَّحَرَّ، فَمَنْ فَعَلَ ذَلِكَ فَقَدْ أَصَابَ سُنَّتَنَا، وَمَنْ ذَبَحَ قَبْلَ الصَّلَاةِ فَإِنَّمَا هُوَ لَحْمٌ قَدَّمَهُ لِأَهْلِهِ لَيْسَ مِنَ التُّسْكِ فِي شَيْءٍ»

*“Hakika kitu cha kwanza tunachotakiwa kufanya siku yetu hii (‘Idi) ni kuswali, kisha tunarudi kwa ajili ya kuchinja. Yeyote mwenye kufanya hilo amepata Sunna yetu. Na yeyote mwenye kuchinja kabla ya Swala, hakika huyo atakuwa amechinja tu nyama kwa ajili ya familia yake, sio udh-hiyah.”*

<sup>1</sup> Nasaa’iy 7:234.

<sup>2</sup>An-Nasaa’iy 7:170.

<sup>3</sup>Fat’hul Al-Baari 11:29.

<sup>4</sup>Ahmad 4:15.

Imepokewa na (Bukhari na Muslim)<sup>1</sup>. Na katika Sahihi Muslim: “Na msiwe ni wenye kuchinja mpaka achinje Imamu”. Na imewekwa katika Sheria kuwa kuchinja ni siku ya *Nahr* na siku tatu za *Tashriyq*<sup>2</sup>, baada yake kulingana na Hadithi ya Jubayr bin Mutw’im رضي الله عنه alisema kuwa Mtume ﷺ amesema:

«أَيَّامُ التَّشْرِيقِ كُلُّهَا ذَبْحٌ»

“Siku za *Tashriyq* zote ni za kuchinja”.

Imenukuliwa na Ahmad na Ibn Hibbaan.<sup>3</sup> Na Kauli Yake:

كَذَلِكَ سَخَّرْنَاهَا لَكُمْ لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٣٦﴾

**“Ndio kama hivi Tumewafanya hawa wanyama dhalili kwenu ili mupate kushukuru”.**

Amesema Allah تعالى kuwa kwa ajili ya hii:

سَخَّرْنَاهَا لَكُمْ

**“Tumewafanya hawa wanyama dhalili kwenu.”**

Maana yake: Tumewadhalilishia, Tumewanya dhalili kwenu, muktaka mutawapanda au muktaka mutakunywa maziwa yao au muktaka munaweza kuwachinja.

Kama Alivyosema Aliyetukuka:

أُولَئِكَ يَرَوْنَ أَنَّا خَلَقْنَا لَهُمْ مِمَّا عَمِلَتْ أَيْدِينَا أَنْعَمًا فَهُمْ لَهَا مَلَائِكُونَ ﴿٣٦﴾

**“Je, hawaoni kwamba Tumewaumbia kutokana na iliyofanya mikono yetu wanyama wa mifugo, na wao wakawa wenye kuwamiliki.” (36:71)**

<sup>1</sup> Fat’hul Al-Baari 2:526 na Muslim 3:1553. Na kauli iliyo baada yake: “Na wala musichinje ...” Amesema Dkt. Ibraahim Al-Banna: “Ibara hii haipo katika Sahihi Muslim”.

<sup>2</sup> Tazama Tafsiri ya Suratul Baqarah (2): 203 kwa ziada.

<sup>3</sup> Ahmad 4:82.



Mpaka Kauli Yake:

أَفَلَا يَشْكُرُونَ ﴿٧٣﴾

*“Basi je, hawashukuru.” (36:73).*

Na Akasema katika Aya hii Tukufu:

كَذَلِكَ سَخَّرْنَا لَكُم لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٧٤﴾

*“Ndio kama hivi Tumewafanya hawa wanyama dhalili kwenu ili mupate kushukuru.”*

\* \* \*

لَنْ يَنَالَ اللَّهُ لُحُومَهَا وَلَا دِمَائُهَا  
 وَلَكِنْ يَنَالُهُ التَّقْوَىٰ مِنْكُمْ ۚ كَذَٰلِكَ  
 وَسَخَّرَهَا لَكُمْ لِتَكْبِرُوا اللَّهَ عَلَىٰ مَا  
 هَدَلَكُمْ ۗ وَبَشِّرِ الْمُحْسِنِينَ ﴿٣٧﴾

لَنْ يَنَالَ اللَّهُ لُحُومَهَا وَلَا دِمَائُهَا وَلَكِنْ يَنَالُهُ التَّقْوَىٰ  
 مِنْكُمْ ۚ كَذَٰلِكَ سَخَّرَهَا لَكُمْ لِتَكْبِرُوا اللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَلَكُمْ ۗ  
 وَبَشِّرِ الْمُحْسِنِينَ ﴿٣٧﴾ \* إِنَّ اللَّهَ يُدْفِعُ عَنِ الَّذِينَ  
 ءَامَنُوا ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ خَوَّانٍ كَفُورٍ ﴿٣٨﴾ أُوذِنَ لِلَّذِينَ  
 يُقْتَلُونَ بِأَنَّهُمْ ظَلِمُوا ۗ وَإِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ نَصْرِهِمْ لَقَدِيرٌ  
 ﴿٣٩﴾ الَّذِينَ أُخْرِجُوا مِنْ دِينِهِمْ بِغَيْرِ حَقٍّ إِلَّا أَنْ  
 يَقُولُوا رَبُّنَا اللَّهُ ۗ وَلَوْلَا دَفْعُ اللَّهِ النَّاسَ بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ  
 هَدَمَتِ صَوَامِعُ وَبِيَعٌ وَصَلَوَاتٌ وَمَسَاجِدٌ يُذَكَّرُ فِيهَا اسْمُ  
 اللَّهِ كَثِيرًا ۗ وَلَيَنْصُرَنَّ اللَّهُ مَنْ يَنْصُرُهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ  
 لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٤٠﴾ الَّذِينَ إِنْ مَكَّنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ أَقَامُوا  
 الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ وَأَمَرُوا بِالْمَعْرُوفِ وَنَهَوْا عَنِ  
 الْمُنْكَرِ ۗ وَاللَّهُ عَقِيبُ الْأُمُورِ ﴿٤١﴾ وَإِنْ يُكَذِّبُوكَ فَقَدْ  
 كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ وَعَادٌ وَثَمُودٌ ﴿٤٢﴾ وَقَوْمُ إِبْرَاهِيمَ  
 وَقَوْمُ لُوطٍ ﴿٤٣﴾ وَأَصْحَابُ مَدْيَنَ ۗ وَكَذَّبَ مُوسَىٰ  
 فَأَمَلَيْتُ لِلْكَافِرِينَ ثُمَّ أَخَذْتَهُمْ ۗ فَكَيْفَ كَانَ نَكِيرِ ﴿٤٤﴾  
 فَكَأَيِّنْ مِنْ قَرْنٍ أَهْلَكْنَاهَا وَهِيَ ظَالِمَةٌ لَهَا فَيَٰهَا خَائِبَةٌ عَلَىٰ  
 عُرُوشِهَا ۗ وَيَوْمَ تُعْطَلُ وَقَصْرٍ مَشِيدٍ ﴿٤٥﴾ أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي  
 الْأَرْضِ فَتَكُونُ لَهُمْ قُلُوبٌ يَعْقِلُونَ بِهَا أَوْ آذَانٌ يَسْمَعُونَ  
 بِهَا ۗ فَإِنَّهَا لَا تَعْمَىٰ الْأَبْصَارُ وَلَكِنْ تَعْمَىٰ الْقُلُوبُ الَّتِي فِي  
 الصُّدُورِ ﴿٤٦﴾

لَنْ يَنَالَ اللَّهُ لُحُومَهَا وَلَا دِمَائُهَا  
 وَلَكِنْ يَنَالُهُ التَّقْوَىٰ مِنْكُمْ ۚ كَذَٰلِكَ  
 وَسَخَّرَهَا لَكُمْ لِتَكْبِرُوا اللَّهَ عَلَىٰ مَا  
 هَدَلَكُمْ ۗ وَبَشِّرِ الْمُحْسِنِينَ ﴿٣٧﴾

**37. Nyama zao hazimfikii  
 Allah wala damu zao, lakini  
 unamfikia uchamungu  
 wenu. Namna hivi Tume-  
 wadhhalilisha kwenu ili  
 mumtukuze Allah kwa  
 Alivyokuongoeni. Na waba-  
 shirie wafanyao mema.**

**Makusudio ya Kuchinja  
 Mbele ya Allah ni Ikhlasu ya  
 Mjia na Uchamungu Wake**

تعالي الله:  
 "Hakika Amewawekea  
 Sheria ya kuchinja wanyama  
 wa Udh'hiya ili mupate  
 kumkumbuka munapo-  
 chinja, kwani Yeye Ndiye  
 Muumba na Mwenye  
 Kuruzuku. Hakuna kinacho-  
 mfikia chochote katika  
 nyama na damu, kwani Yeye  
 Aliyetukuka ni Mkwasi na  
 tajiri kushinda viumbe  
 wote".

Na hakika walikuwa wakati  
 wa Ujaahiliyyah (ujinga)

walipokuwa wakichinja kwa ajili ya miungu yao, walikuwa wakiweka baadhi ya nyama za Udh'hiyya kwa miungu yao na kunyunyizia damu juu yao. Akasema Aliyetukuka:

لَنْ يَنَالَ اللَّهُ لُحُومَهَا وَلَا دِمَائُهَا

***“Nyama zao hazimfikii Allah wala damu zao”.***

Amepokea Ibn Abi Haatim kuwa Ibn Jurayj amesema: “Walikuwa watu katika zama za ujinga wakiweka nyama zao na kunyunyiza damu juu ya Ka’aba, na Maswahaba wa Mtume ﷺ wakasema: ‘Sisi tuna haki zaidi kufanya hayo’. Hapo Allah تعالى Akasema;

لَنْ يَنَالَ اللَّهُ لُحُومَهَا وَلَا دِمَائُهَا وَلَكِنْ يَنَالُهُ التَّقْوَىٰ مِنْكُمْ<sup>١</sup>

***“Nyama zao hazimfikii Allah wala damu zao, lakini unamfikia uchamungu wenu.”***

Maana yake: Analikubali hilo na kulipatia ujira, kama ilivyokuja katika Hadithi Sahihi:

«إِنَّ اللَّهَ لَا يَنْظُرُ إِلَىٰ صُورِكُمْ وَلَا إِلَىٰ أَلْوَابِكُمْ، وَلَكِنْ يَنْظُرُ إِلَىٰ قُلُوبِكُمْ وَأَعْمَالِكُمْ»

*‘Hakika Allah Hatizami sura wala rangi zenu, lakini anatazama mioyo yenu na amali zenu’<sup>1</sup>.*

Na Kauli Yake:

كَذَلِكَ سَخَّرَهَا لَكُمْ

***“Namna hivi Tumewadhilisha kwenu”.***

Maana yake: kwa ajili hiyo Tumewafanyia sahali na wepesi ngamia (wa kuchinjwa) kwa ajili yenu.

لِتُكَبِّرُوا اللَّهَ عَلَىٰ مَا هَدَيْتُمْ<sup>٢</sup>

***“Ili mumtukuze Allah kwa Alivyokuongoeni”.***

<sup>1</sup> Muslim 4:1987.

Maana yake: Ili Mumtukuze kama Alivyowaongoa katika Dini na Sheria Yake Anayoipenda na Kuiridhia, na Akawakatazeni kutenda Anayochukia na Kuyakataza. Na Kauli Yake:

وَنَشِرِ الْمُحْسِنِينَ ﴿٢٧﴾

**“Na wabashirie wafanyao mema.”**

Maana yake: Ewe Muhammad ﷺ wabasharie wema, katika amali zao wakiwa wamesimama imara juu ya mipaka ya Allah تعالیٰ, huku wakifuata Sheria Aliyowaletea, wakimsadiki Mtume kwa aliyoyafikisha na aliyokuja nayo kutoka kwa Mola Wake Mlezi Aliyetukuka.

### Kuchinja ni Sunnah Inayopendeza

Mnyama mmoja anatosheleza kwa niaba ya familia nzima. Amesema Ibn ‘Umar رضي الله عنهما: Mtume ﷺ aliendelea kuchinja kwa muda wa miaka kumi. Hii imenukuliwa na At-Tirmidhiy<sup>1</sup>. Na amesema Abu Ayyub رضي الله عنه: “Alikuwa mtu katika zama za Mtume ﷺ akichinja kondoo mmoja kwa ajili yake na familia yake. Na walikuwa wakila kutokana na kichinjo hicho na kuwalisha wengine, mpaka watu wakaanza kujifakhiri na kujiona (kwa kuchinja zaidi ya kondoo mmoja) na mambo yamefikia hapa unapoonaa”. Hii imenukuliwa na At-Tirmidhiy, aliyeisahihisha na Ibn Maajah<sup>2</sup>. Na ‘Abdallah bin Hishaam alikuwa akichinja kondoo mmoja kwa niaba yake na familia yake. Imepokewa na al-Bukhaariy<sup>3</sup>. Ama kuhusu umri wa mnyama anayetakiwa kuchinjwa anafaa awe kama alivyopokea Muslim kutoka kwa Jaabir رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«لَا تَذْبَحُوا إِلَّا مُسِنَّةً، إِلَّا أَنْ تَغْسَرَ عَلَيْكُمْ فَتَذْبَحُوا جَذَعَةً مِنَ الضَّأْنِ»

*“Musichinje isipokuwa mnyama aliyekomaa, ila linaposhindikana hilo, kwa hiyo chinjeni kondoo mdogo.”<sup>4</sup>*

<sup>1</sup> Tuhfatul Al-Ahwadhiy 5:96.

<sup>2</sup> Abu Daawud 5:90 na Ibn Maajah 2:1051.

<sup>3</sup> Fat’hul Al-Baari 13:213.

<sup>4</sup> Muslim 3:1555.

﴿ إِنَّا لِلَّهِ يُدْفَعُ عَنِ الَّذِينَ ءَامَنُوا ۗ إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ كُلَّ خَوَّانٍ كَفُورٍ ﴾

**38. Hakika Allah Huwakinga walioamini. Hakika Allah Hampendi kila khaini mwingi wa kukanya mema.**

### Bishara Njema ya Kulingwa Walioamini

Aliyetukuka Anatupasha habari kuwa Yeye Huwakinga waja Wake wanaomtegemea na kurudi Kwake (kwa kutubia); Anawalinda wao na shari ya watu waovu, na vitimbi vya walioasi; Anawahifadhi, Anawalinda na Kuwanusuru. Kama Anavyosema mahali pengine:

أَلَيْسَ اللَّهُ بِكَافٍ عَبْدَهُ ۗ

**“Je, Allah si wa kumtosheleza mja Wake?” (39:36).**

﴿ وَمَنْ يَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ فَهُوَ حَسْبُهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ بَلِغُ أَمْرِهِ ۗ قَدْ جَعَلَ اللَّهُ لِكُلِّ شَيْءٍ قَدْرًا ﴾

**“...Na anayemtegemea Allah Yeye Humtosha. Hakika Allah Anatimiza Amri Yake. Allah Kajaalia kila kitu na kipimo Chake.” (65:3).**

Na Kauli Yake:

﴿ إِنَّا لِلَّهِ لَا نُحِبُّ كُلَّ خَوَّانٍ كَفُورٍ ﴾

**“Hakika Allah Hampendi kila khaini mwingi wa kukanya mema.”**

Maana yake: Hawapendi miongoni mwa waja Wake wenye sifa hizi, nayo ni khiyana katika ahadi na miadi ambayo kwamba mtu hafanyi aliyosema, na ukafiri ni kukataa neema, ambapo mmoja wao hazitambui au kutoshukuru kwayo.

أُذِنَ لِلَّذِينَ يُقْتَلُونَ بِأَنَّهُمْ ظَلَمُوا ۗ وَإِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ تَصْرِيهِمْ لَقَدِيرٌ ﴿٣٨﴾ الَّذِينَ أُخْرِجُوا  
 مِنْ دِيَارِهِمْ بِغَيْرِ حَقٍّ إِلَّا أَنْ يَقُولُوا رَبُّنَا اللَّهُ ۗ وَلَوْلَا دَفْعُ اللَّهِ النَّاسَ بَعْضَهُمْ بِبَعْضٍ  
 هَدَمَتِ صَوَامِعُ وَبِيَعٌ وَصَلَوَاتٌ وَمَسَاجِدٌ يُذَكَّرُ فِيهَا اسْمُ اللَّهِ كَثِيرًا ۗ وَلَيَنْصُرَنَّ اللَّهُ  
 مَنْ يَنْصُرُهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٣٩﴾

**39. Wameruhusiwa kupigana wale wanaopigwa vita kwa sababu wamedhulumiwa - na kwa yakini Allah ni Muweza wa Kuwasaidia.**

**40. Wale ambao wametolewa majumbani mwao bila haki, ila kwa kuwa wanasema: Mola wetu Mlezi ni Allah! Na lau kuwa Allah Hawakingi watu kwa watu, basi hapana shaka zingelivunjwa nyumba za watawa, na makanisa, na masinagogi, na misikiti, ambamo ndani yake Jina la Allah linatajwa kwa wingi. Na bila ya shaka Allah Humsaidia yule anayemsaidia Yeye. Hakika Allah ni Mwenye Nguvu Mtukufu.**

### **Idhini ya Kupigana, nayo ni Aya ya Kwanza ya Jihadi**

Amepokea Al-'Awfiy kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: "Hii iliteremshwa kwa Muhammad ﷺ na Maswahaba zake, walipofukuzwa kutoka Makka"<sup>1</sup>. Na Mujaahid, Adh-Dhahaak na wengine miongoni mwa wema waliotangulia, kama vile Ibn 'Abbaas, 'Urwah bin Az-Zubayr, Zayd bin Aslam, Muqaatil bin Hayyaan, Qatadah na wengineo رضي الله عنهم wamesema: "Hii ni Aya ya kwanza iliyoteremshwa kuhusiana na Jihadi"<sup>2</sup>. Na amepokea Ibn Jariri رحمه الله تعالى kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: "Pindi Mtume ﷺ alipotolewa Makka, Abubakar رضي الله عنه alisema: 'Wamemtoa Mtume wao. Hakika sote twatoka kwa Allah تعالى na Kwake tutarudi; bila shaka wataangamia". Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: "Kisha Allah تعالى Akateremsha:

أُذِنَ لِلَّذِينَ يُقْتَلُونَ بِأَنَّهُمْ ظَلَمُوا وَإِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ نَصْرِهِمْ لَقَدِيرٌ ﴿٢٥﴾

**'Wameruhusiwa kupigana wale wanaopigwa vita kwa sababu wamedhulumiwa - na kwa yakini Allah ni Muweza wa Kuwasaidia'.**

Akasema Abubakar رضي الله عنه: "Nikajua kuwa kutakuwa na vita (na mapambano)". Akaongeza Imaam Ahmad: Amesema Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: 'Hiyo ni Aya ya kwanza iliyoteremshwa kuhusiana na vita'<sup>3</sup>. Na amepokea At-Tirmidhiy na An - Nasaa'iy katika Sunan zao<sup>4</sup>, na akasema At-Tirmidhiy: Hii ni Hadithi Hasan (Nzuri). Na Kauli Yake:

<sup>1</sup> Tabari 18:643.

<sup>2</sup> Tabari 18:643, 644 na Ad-Durr Al-Manthuur 6:87.

<sup>3</sup> Ahmad 1:216.

<sup>4</sup> Tuhfatul Al-Ahwadhiy 9:15 na An-Nasaa'iy katika Al-Kubraa 6:411.

وَإِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ نَصْرِهِمْ لَقَدِيرٌ ﴿٤٦﴾

**“Na kwa yakini Allah ni Muweza wa Kuwasaidia”.**

Maana yake: Yeye ni Muweza wa Kuwasaidia na Kuwanusuru waja Wake Waumini pasi na kupigana, lakini Anataka waja Wake wafanye juhudi kubwa katika kumtii, kama Anavyosema:

فَإِذَا لَقِيتُمُ الَّذِينَ كَفَرُوا فَضَرْبَ الرِّقَابِ حَتَّىٰ إِذَا أَخْنَثْتُمْهُمْ فَشُدُّوا أَلْوَتَاقَ فَإِمَّا مَنًّا بَعْدَ  
وَأِمَّا فِدَاءً حَتَّىٰ تَضَعَ الْحَرْبُ أَوْزَارَهَا ۗ ذَٰلِكَ وَلَوْ يَشَاءُ اللَّهُ لَانتَصَرَ مِنْهُمْ وَلَٰكِن لِّيَبْلُوَ  
بَعْضَكُمْ بِبَعْضٍ ۗ وَالَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَلَن يُضِلَّ أَعْمَالَهُمْ ﴿٤٥﴾ سَيَسْئَلُهُمْ  
بِأَنفُسِهِمْ ۗ وَيُدْخِلُهُمْ الْجَنَّةَ عَرَّفَهَا لَهُمْ ﴿٤٦﴾

**“Basi munapowakuta waliokufuru wapigeni shingoni mwao, mpaka mukiwadhoofisha wafungeni pingu. Tena waachilieni kwa hisani au wajikomboe, mpaka vita vipoe. Ndio hivyo. Na lau Angelitaka Allah Angewashinda Mwenyewe, lakini haya ni kwa sababu Akutieni mitihani nyinyi. Na waliouliwa katika Njia ya Allah Hatazipoteza amali zao. Atawaongoza na Awatengezee hali yao. Na Atawaingiza katika Pepo Aliyowajulisha.” (47:4-6).**

Na Amesema Aliyetukuka:

قَتَلْتَهُمْ يُعَذِّبُهُمُ اللَّهُ بِأَيْدِيكُمْ وَيُخْرِجُهُمْ وَيَنْصُرْكُمْ عَلَيْهِمْ وَيَنْصُرْ قَوْمَ  
مُؤْمِنِينَ ۗ وَيُذْهِبْ غَيْظَ قُلُوبِهِمْ وَيَتُوبَ اللَّهُ عَلَىٰ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٩﴾

**“Piganeni nao, Allah Awaadhibu kwa mikono yenu, na Awahizi na Akunusuruni muwashinde, na Avipoze vifua vya kaumu ya Waumini, na Aondoe hasira ya nyoyo zao. Na Mwenyezi Mungu Humkubalia toba ya amtakaye. Na Allah ni Mwenye Kujua Mwenye Hekima.” (9:14-15).**

<sup>1</sup> Ahmad 1:216.

<sup>2</sup> Tuhfatul Al-Ahwadhiy 9:15 na An-Nasaa'iy katika Al-Kubraa 6:411.

Na Amesema:

وَلَتَبْلُوكُنَّكُمْ حَتَّىٰ نَعْلَمَ الْمُجَاهِدِينَ مِنكُمْ وَالصَّابِرِينَ وَتَبْلُؤَ أَخْبَارَكُمْ ﴿٣١﴾

**“Na bila shaka Tutakujaribuni mpaka Tuwadhahirishe wapiganao Jihadi katika nyinyi na wanaosubiri. Nasi Tutazifanyia mitihani habari zenu.” (47:31).**

Na Ayah kuhusiana na haya ni nyingi. Na kwa hiyo akasema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما katika Kauli Yake:

وَإِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ نَصْرِهِمْ لَقَدِيرٌ ﴿٣٢﴾

**“Na kwa yakini Allah ni Muweza wa Kuwasaidia.”**

Na tayari hilo Amefanya<sup>1</sup>. Na hakika Allah تعالى Amefaradhisha Jihadi kwa wakati unaofaa, kwani walipokuwa Makka, washirikina walikuwa wengi sana kuliko waislamu, lau Angewaamrisha waislamu kupigana kwa kipindi kile ambapo wao walikuwa wachache kiasi cha wastani wa asilimia kumi tu, Na lau kama wangepigana wakati huo, matokeo yangekuwa mabaya sana.

Na kwa hiyo pindi walipo kula kiapo cha utii watu wa Yathrib usiku wa ‘Aqabah, kwa Mtume ﷺ. Watu wa Yathrib walikuwa zaidi ya themanini, wakasema: “Ewe Mtume ﷺ! Je, hatuwavamii watu wa bonde, wakimaanisha watu wa Mina, usiku wa Mina ili tuwapige?” Akasema Mtume ﷺ: “Hakika mimi sijaamrisha kupigana.”<sup>2</sup>

Walipovuka mipaka washirikina na wakamtoa Mtume ﷺ baina ya migongo yao na wakaamua kumuua; na walipowafukuza na kuwatoa Swahaba wake na kuwapeleka hapa na pale. Kufatia hali hiyo wengine wakaenda Ethiopia na wengie Madina. Na pindi walipotulia na kustakiri Madina na Mtume ﷺ akawaunga na kukusanyika pembezoni mwao, na wakasimama kumnusuru, na wakawa na Dola ya Kiislamu, na ngome ambayo wanaweza kurudi kwayo; Allah تعالى Aliwafaradhisha Jihadi dhidi ya maadui, hivyo ikawa Aya hii ni ya mwanzo aliyoteremsha. Amesema Aliyetukuka:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:643.

<sup>2</sup> Dalaa’il An-Nubuwaah cha Al-Aswbahaaniy 265.



أَذِنَ لِلَّذِينَ يُقْتَلُونَ بِأَنَّهُمْ ظَلَمُوا وَإِنَّ اللَّهَ عَلَىٰ نَصْرِهِمْ لَقَدِيرٌ ﴿٤٦﴾ الَّذِينَ أُخْرِجُوا  
مِن دِينِهِمْ بغيرِ حَقٍّ

***“Wameruhusiwa kupigana wale wanaopigwa vita kwa sababu wamedhulumiwa - na kwa yakini Allah ni Muweza wa Kuwasaidia – Wale ambao wametolewa majumbani mwao pasipo haki”.***

Amepokea Al-‘Awfiy kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Walitolewa kutoka Makka kuelekea Madina pasi na haki yoyote, yaani Muhammad ﷺ na Maswahaba wake”<sup>1</sup>.

إِلَّا أَنْ يَقُولُوا رَبُّنَا اللَّهُ

***“Ila kwa kuwa wanasema: Mola wetu Mlezi ni Allah!”***

Maana yake: Hawakuwafanyia lolote watu wao au kufanya kosa lolote dhidi yao, ila wao walimpwekesha Allah تعالى na kumuabudu Yeye bila kumshirikisha. Ama kwa hawa washirikina hilo ilikuwa ni dhambi kubwa sana, kama Anavyosema Aliyetukuka:

مُخْرِجُونَ الرُّسُولَ وَإِيَّاكُمْ أَنْ تَتُومِنُوا بِاللَّهِ رَبِّكُمْ

***“Wakamfukuza Mtume na nyinyi kwa sababu munamuamini Allah, Mola wenu Mlezi...” (60:1).***

Kisha Akasema Aliyetukuka:

وَلَوْلَا دَفَعُ اللَّهُ النَّاسَ بَعْضَهُم بِبَعْضٍ

***“Na lau kuwa Allah Hawakingi watu kwa watu.”***

Maana yake: Isingekuwa kwa ile hakika kuwa Allah تعالى Anawakinga watu kwa njia ya watu wengine, na kuzuilia ubaya wa watu kwa wengine kwa njia ya hali yoyote Anayoiweka na Kuikadiria, ardhi ingeharibika na wenye nguvu wangewaangamiza wanyonge. Na Kauli Yake:

<sup>1</sup> Tabari 18:643.

### هُدِّمَتْ صَوَامِعُ

**“Basi hapana shaka zingevunjwa Swawaami.”** Maana yake: Hekalu ndogo zinazotumiwa na watawa. Hii ilikuwa rai ya Ibn ‘Abbaas, Mujaahid, Abul ‘Aliyah, ‘Ikrimah, Adh-Dhahaak na wengineo رضي الله عنهم<sup>1</sup>. Qatadah amesema: “Hii inamaanisha nyumba za ibada za Wasabia”. Kulingana na ripoti nyingine, amesema: “Swawaami’ za Wapagani (Wafursi waliokuwa wakiabudu moto)”. Muqaatil bin Hayyaan amesema: “Hizi ni nyumba kando ya barabara (zilizokuwa barabarani).” Na Kauli Yake:

### وَبِيعُ

**“Na Biyaa.”** Hizi ni kubwa kuliko Swawaami’ na zinachukuwa watu wengi zaidi wenye kufanya Ibadah; Wakristo pia wanazo. Huu ulikuwa muono wa Abul ‘Aliyah, Qatadah, Adh-Dhahaak, Ibn Sakhr, Muqaatil bin Hayyan, Khuswayf na wengineo<sup>2</sup>. Amepokea Ibn Jubayr kutoka kwa Mujaahid na wengineo kuwa hii inamaanisha masinagogi ya Mayahudi. Na Allah تعالى Anajua zaidi. Na Kauli Yake:

### وَصَلَوَاتُ

**“Swalawaat”.** Amepokea al-Awfiy kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Swalawaat” Ina maanisha makanisa<sup>3</sup>. ‘Ikrima, Adh- Dhahaak na Qatadah wamesema kuwa hilo linamaanisha masinagogi ya Mayahudi. Abul ‘Aliyah na wengine wamesema: “Swalawaat inahusisha sehemu za Ibadah za Wasabia”. Amepokea Ibn Abi Najiyh kuwa Mujaahid amesema: “Swalawaat” ina maanisha sehemu ya Ibada kwa Watu wa Kitabu na pia Waislamu zilizo barabarani<sup>4</sup>. Misikiti ni ya Waislamu. Na Kauli Yake:

### يُذَكَّرُ فِيهَا أَسْمُ اللَّهِ كَثِيرًا

**“Ambamo ndani yake Jina la Allah linatajwa kwa wingi”.**

Pamesemwa kuwa kiwakilishi katika neno lake Allah تعالى (ndani yake) kinahusisha **Masaajid** (misikiti) kwani hili ni neno karibu zaidi na maneno yaliyotajwa. Adh-Dhahaak amesema: “Katika majumba yote hayo Jina la Allah تعالى Hutajwa sana”. Ibn Jariri رحمه الله تعالى amesema: “Rai iliyo sahihi na sawa ni kuwa nyumba za watawa, makanisa ya Wakristo, masinagogi ya Mayahudi

<sup>1</sup> Tabari 18:647, Ad-Durr Al-Manthuur 6:59, 60 na Ar-Raaziyy 3:36.

<sup>2</sup> Tabari 18:648.

<sup>3</sup> Tabari 18:649.

<sup>4</sup> Tabari 18:650.

na Misikiti ya Waislamu, ambamo Jina la Allah تعالى Hutajwa kwa wingi, yangeharibiwa – kwa sababu haya ni matumizi ya kawaida yaliyo maarufu kwa lugha ya Kiarabu”<sup>1</sup>. Na wamesema baadhi ya wanazuoni: “Huu ni ule mfumo wa kutaja orodha kuanzia ya chini kuelekea ya juu (ndogo hadi kubwa), kwa sababu misikiti ndio inayojengwa sana, na wenye kuabudu ni wengi pia tena wenye nia safi na malengo yaliyo sahihi.” Na Kauli Yake:

وَلْيَنْصُرَنَّ اللَّهُ مَن يَنْصُرُهُ

**“Na bila ya shaka Allah Humsaidia yule anayemsaidia Yeye.”**

Hii ni kama Aya ifuatayo:

يَتَأَيُّمُ الَّذِينَ ءَامَنُوا إِن تَنْصُرُوا اللَّهَ يَنْصُرْكُمْ وَيُثَبِّتْ أَقْدَامَكُمْ ﴿٧٧﴾ وَالَّذِينَ كَفَرُوا فَتَعَسَا  
هُمُ وَأَصْلٌ أَعْمَلَهُمْ ﴿٧٨﴾

**“Enyi mlioamini! Mukimnusuru Allah Naye Atakunusuruni na Ataithibitisha miguu yenu. Na waliokufuru, basi kwao ni maangamizo, na Atavipoteza vitendo vyao.” (47:7-8).**

Na Kauli Yake:

إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٧٩﴾

**“Hakika Allah ni Mwenye Nguvu Mtukufu.”**

Allah تعالى Anajisifu Mwenyewe kuwa Ana Nguvu na Utukufu. Kwa Nguvu Zake Ameumba kila kitu na Kupima kila kitu kulingana na kipimo barabara; kwa Nguvu Zake Hatenzwi nguvu na mwenye nguvu wala Hashindwi na mshindi, bali kila kitu ni dhalili mbele Yake na Anahitajiwa na kila kitu. Yeyote mwenye kunusuriwa na Mwenye Nguvu na Utukufu, yeye ndiye mshindi na adui yake ndiye mwenye kushindwa. Amesema Allah تعالى:

وَلَقَدْ سَبَقَتْ كَمَتُنَا لِعِبَادِنَا الْمُرْسَلِينَ ﴿١٧١﴾ إِنَّهُمْ لَهُمُ الْمَنْصُورُونَ ﴿١٧٢﴾ وَإِنَّ جُنَدَنَا  
لَهُمُ الْغَالِبُونَ ﴿١٧٣﴾

**“Na bila ya shaka Neno Letu lilikwishatangulia kwa waja wetu walio tumwa. Ya kuwa wao bila ya shaka ndio watakaonusuriwa. Na kwamba jeshi Letu ndilo litakaloshinda.” (37:171-173).**

<sup>1</sup> Tabari 18:650.

Na Amesema Aliyetukuka:

كَتَبَ اللَّهُ لَأَعْلَبَنَّ أَنَا وَرُسُلِيَّ إِنَّ اللَّهَ قَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٥٨﴾

**“Allaah Ameandika: Hapana shaka Mimi na Mtume Wangu Tutashinda. Hakika Allah ni Mwenye Nguvu, Mwenye Kushinda” (58:21).**

الَّذِينَ إِنْ مَكَّنَّاهُمْ فِي الْأَرْضِ أَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ وَأَمَرُوا بِالْمَعْرُوفِ وَنَهَوْا عَنِ الْمُنْكَرِ ۗ وَاللَّهُ عَزِيزٌ أَلِيمٌ ﴿٤١﴾

**41. Wale ambao Tukiwapa madaraka katika nchi husimamisha Swala, na wakatoa Zaka, na wakaamrisha mema, na wakakataza mabaya. Na kwa Allah ndio marejeo ya mambo yote.**

### Wajibu wa Waislamu Wanapopata Madaraka

Amepokea Ibn Abi Haatim رَضِيَ اللهُ عَنْهُ kuwa ‘Uthmaan bin ‘Affaan رَضِيَ اللهُ عَنْهُ amesema: Aya hii iliteremka kwetu:

الَّذِينَ إِنْ مَكَّنَّاهُمْ فِي الْأَرْضِ أَقَامُوا الصَّلَاةَ وَآتَوُا الزَّكَاةَ وَأَمَرُوا بِالْمَعْرُوفِ وَنَهَوْا عَنِ الْمُنْكَرِ ۗ

**“Wale ambao Tukiwapa madaraka katika nchi husimamisha Swala, na wakatoa Zaka, na wakaamrisha mema, na wakakataza mabaya.”**

Kwani sisi tulikuwa tumetolewa na kufukuzwa kwenye majumba yetu kwa dhuluma kwa sababu ya kusema: ‘Mola wetu Mlezi ni Allah تَعَالَى’. Kisha tukapatiwa madaraka na kumakinishwa katika ardhi, hivyo tukasimamisha Swala, tukatoa Zaka, tukaamrisha mema na kukataza mabaya, na kwa Allah ndio marejeo ya mambo yote. Hiyo inanihusu mimi na Maswahaba wangu”<sup>1</sup>. Abul ‘Aliyah amesema: “Hao ni Maswahaba wa Mtume Muhammad ﷺ”. Na

<sup>1</sup> Ibn Abi Haatim 8:2496, 2497.

amesema Asw-Swabaah bin Swaadah Al-Kindiy: Nimemsikia ‘Umar bin ‘Abdul-‘Aziz رحمه الله تعالى akihutubu huku anasema:

الَّذِينَ إِن مَّكَّنْتَهُمْ فِي الْأَرْضِ

**“Wale ambao Tukiwapa madaraka katika nchi”.**

Kisha akasema: “Jueni kuwa hilo si kwa viongozi peke yao, lakini ni kwa viongozi na raia. Je nisiwajulisheni kwa mnayotarajia kupata kutoka kwa viongoni wenu na wajibu wa viongozi juu yenu?. Haki yenu kwa kiongozi ni kuwa ni lazima awatizame kuhusiana na wajibu wenu kwa Allah تعالى na kuwarudishia haki ambazo mnazo baadhi yenu kwa wengine, na awaongoze katika njia nyoofu kwa kadiri ya uwezo wake. Ama wajibu wenu kwake ni kuwa mumtii bila udanganyifu wala kuchukia, na mumtii katika hali ya siri na dhahiri”. Na amesema ‘Atwiyah Al-‘Awfiy: Hii ni kama Aya ifuatayo:

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ ءَامَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ

**“Allah Amewaahidi wale walioamini miongoni mwenu na wakatenda mema, ya kwamba Atawafanya makhalifa katika ardhi.’ (24:55)**

Na Kauli Yake:

وَاللَّهُ عَاقِبَةُ الْأُمُورِ

**“Na kwa Allah ndio marejeo ya mambo yote.”**

Hii ni kama Aya:

وَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ

**“Na mwisho mwema ni wa wachamungu.” (28:83)**

Na amesema Zayd bin Aslam:

وَاللَّهُ عَاقِبَةُ الْأُمُورِ

**“Na kwa Allah ndio marejeo ya mambo yote.”**

Na kwa Allah تعالى watapata thawabu kwa waliyokuwa wakifanya<sup>1</sup>.

<sup>1</sup> Ibn Abi Haatim 8:2498.

وَإِنْ يُكَذِّبُوكَ فَقَدْ كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ وَعَادٌ وَثَمُودٌ ﴿٤٢﴾ وَقَوْمَ إِبْرَاهِيمَ وَقَوْمَ لُوطٍ ﴿٤٣﴾ وَأَصْحَابَ مَدْيَنَ ۗ وَكَذَّبَ مُوسَىٰ فَأَمَلَيْتُ لِلْكَافِرِينَ ثُمَّ أَخَذْتُهُمْ ۗ فَكَيْفَ كَانَ نَكِيرِ ﴿٤٤﴾ فَكَايِنٍ مِّن قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَاهَا وَهِيَ ظَالِمَةٌ فَهِيَ خَاوِيَةٌ عَلَىٰ عُرُوشِهَا وَيَبْرِئُ الْمُعْتَظَلَةَ وَقَصْرٍ مَّشِيدٍ ﴿٤٥﴾ أَفَلَمْ يَسْمُرُوا فِي الْأَرْضِ فَتَكُونَ لَهُمْ قُلُوبٌ يَعْقِلُونَ بِهَا أَوْ آذَانٌ يَسْمَعُونَ بِهَا ۗ فَإِنَّهَا لَا تَعْمَى الْأَبْصَارُ وَلَكِن تَعْمَى الْقُلُوبُ الَّتِي فِي الصُّدُورِ ﴿٤٦﴾

42. Na wakikukanusha basi walikwishakanusha kabla yao watu wa Nuuh, na kina 'Aad na kina Thamud,

43. Na watu wa Ibrahim na watu wa Lutwi.

44. Na watu wa Madiana. Na Musa pia alikanushwa. Nikawapa muda makafiri, kisha nikawatia mkononi. Basi ilikuwaje adhabu Yangu!

45. Miji mingapi Tuliangamiza iliyokuwa ikidhulumu, ikawa imebaki magofu, na visima vilivyoachwa, na majumba yaliyokuwa madhubuti?

46. Je! Hawatembei katika ardhi ili wapate kuwa na nyoyo za kuzingatia, au masikio ya kusikilia? Kwani hakika si macho yanayopofuka, lakini zinazopofuka ni nyoyo ziliomo vifuani.

### Matokeo ya Wasioamini

Hapa Aliyetukuka Anamliwaza Mtume Wake, Muhammad ﷺ kwa kumkanusha waliompiga vita miongoni mwa watu wake.

وَإِنْ يُكَذِّبُوكَ فَقَدْ كَذَّبَتْ قَبْلَهُمْ قَوْمُ نُوحٍ

“Na wakikukanusha basi walikwishakanusha kabla yao watu wa Nuuh”.

Mpaka Kauli Yake:

وَكَذَّبَ مُوسَىٰ

“Na Musa pia alikanushwa”.

Maana yake: Mbali na ishara na miujiza iliyo bayana na dalili za wazi kabisa.

فَأَمَلَيْتُ لِلْكَافِرِينَ

**“Nikawapa muda makafiri.”**

Maana yake: Nilichelewesha na kuakhirisha.

نُرَّأَخَذْتُهُمْ<sup>ط</sup> فَكَيْفَ كَانَ نَكِيرِ ﴿٤٤﴾

**“Kisha nikawatia mkononi. Basi ilikuwaje adhabu Yangu!”**

Maana yake: Kisasi Changu na Adhabu Yangu ilikuwa kubwa namna gani? Katika Sahihi mbili imepokewa kutoka kwa Abi Musa Al-Ash'ariy عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ اللَّهَ يُبْلِي لِلظَّالِمِ حَتَّى إِذَا أَخَذَهُ لَمْ يُغْلِبْهُ»

*“Hakika Allah Humuachia dhalimu kuendelea (na dhuluma yake) mpaka Anapomtia mkononi, Hatamuachilia kabisa”.*

Kisha akasoma:

وَكَذَلِكَ أَخَذُ رَبِّكَ إِذَا أَخَذَ الْقَرْيَ وَهِيَ ظَالِمَةٌ إِنَّ أَخَذَهُ أَلِيمٌ شَدِيدٌ ﴿٤٥﴾

**“Na ndio kama hivyo ndivyo inavyokuwa Mola wako Mlezi anapo ikamata miji inapokuwa imedhulumu. Hakika Mkamato Wake ni mchungu na mkali.” (11:102)<sup>1</sup>**

Kisha Akasema Aliyetukuka:

فَكَأَيِّن مِّن قَرْيَةٍ أَهْلَكْنَاهَا

**“Miji mingapi Tuliingamiza”.**

Maana yake: Miji mingapi Tuliihiliki,

وَهِيَ ظَالِمَةٌ

**“Iliyokuwa ikidhulumu”.** Maana: Iliyokanusha na kukadhibisha Mitume wao.

<sup>1</sup> Fat'h ul Al-Baariy 8:205 na Muslim 4:1997.

فَهِيَ خَاوِيَةٌ عَلَى عُرُوشِهَا

**“Ikawa imebaki magofu.”**

Amesema Adh-Dhahaak: “Sakafu zake<sup>1</sup>, Maana yake: ni majumba yake na miji yao yameharibiwa”.

وَبِعَرِّ مُعَطَّلٍ

**“Na visima vilivyo achwa.”**

Maana yake: Hawakuchota maji kwayo, pasi na hata mmoja wao kuja hapo baada ya kuwa vilikuwa vikifikiwa na umati wa watu mara kwa mara.

وَقَصْرِ مَشِيدٍ ﴿١٥﴾

**“Na majumba yaliyokuwa madhubuti?”**

‘Ikrima amesema ina maana myeupe kwa kupigwa plasta (kupakwa chokaa)<sup>2</sup>. Na imepokewa kwa ‘Aliy bin Abi Twaalib, Mujaahid, ‘Atwaa’, Sa’id bin Jubayr, Abi Al-Mulayh na Adh-Dhahaak mfano wa hayo<sup>3</sup>. Na wakasema wengine: “Hizo ni ngome ndefu zilizo madhubuti kabisa (zisizoweza kuingilika)”. Na wengine wakasema: “Al-Mashiyd: Ngome iliyo madhubuti”. Na kauli zote hizi zinakaribiana wala hazipingani baina yao. Hakika ni kuwa umadhubuti wake katika ujenzi, urefu wake na ngome zao hazikuwanusuru wala kuwasaidia dhidi ya adhabu ya Allah تعالى ilipowafikia, kama Alivyosema Aliyetukuka:

أَيْنَمَا تَكُونُوا يُدْرِكُكُمُ الْمَوْتُ وَلَوْ كُنْتُمْ فِي بُرُوجٍ مُّشِيدَةٍ

**“Popote mulipo mauti yatakufikieni, na hata mkiwa katika ngome zilizo na nguvu.” (4:78)**

Na Kauli Yake:

أَفَلَمْ يَسِيرُوا فِي الْأَرْضِ

**“Je! Hawatembei katika ardhi”.**

<sup>1</sup> Tabari 18:653.

<sup>2</sup> Tabari 18:654, 655.

<sup>3</sup> Tabari 18:655 na al-Baghawiy 3:291.



Maana yake: Kwa miili yao na fikra zao pia (kwa kutumia akili zao kutafakari)? Na hiyo ni tosha kama alivyosema Ibn Abi Dun'ya katika kitabu chake *"At-Tafakkur wal I'tibaar"* Wamesema baadhi ya watu wenye hekima: "Uhuishe moyo wako kwa mawaidha, utie nuru kwa kutafakari, ufishe kwa kupa nyongo dunia, utilie nguvu kwa yakini, ukumbushe umauti, ujuze kwa kumalizika kwa dunia, uone mbali kwa misukosuko ya kilimwengu, uonye kwa kupita kwa zama, uoneshe jinsi siku zinavyobadilika, uambie kuhusu habari za waliopita, ukumbushe kwa yaliyo wasibu waliokuwa kabla yake, tembea katika majumba na magofu yao na utizame walivyofanya na yaliyowafika. Maana yake: tizama yaliyowapata Umma waliokanusha kwa kuadhibiwa na kupata ghadhabu kutoka kwa Allah تعالى iliyowashukia."

فَتَكُونُ لَهُمْ قُلُوبٌ يَعْقِلُونَ بِهَا أَوْ آذَانٌ يَسْمَعُونَ بِهَا

***"Ili wapate kuwa na nyoyo za kuzingatia, au masikio ya kusikilia?"***

Maana yake: Wapate kuzingatia na kupata mafunzo ndani yake.

فَأِنَّهَا لَا تَعْمَى الْأَبْصَارُ وَلَكِنْ تَعْمَى الْقُلُوبَ الَّتِي فِي الصُّدُورِ ﴿٤٦﴾

***"Kwani hakika si macho yanayopofuka, lakini zinazopofuka ni nyoyo ziliomo vifuani."***

Maana yake: Kipofu si wa macho, bali ni yule asiyekuwa na uoni. Japokuwa macho yanaweza kuwa yanaona barabara, lakini hayawaidhiki wala hayapati mazingatio.

\* \* \*

وَيَسْتَعْجِلُونَكَ بِالْعَذَابِ وَلَنْ تُخْلِفَ اللَّهُ وَعْدَهُ ۗ وَإِنَّ يَوْمًا عِنْدَ رَبِّكَ كَأَلْفِ سَنَةٍ مِمَّا تَعُدُّونَ ﴿٤٧﴾ وَكَأَيِّن مِّن قَرْيَةٍ أَمَلَيْتُهَا وَهِيَ ظَالِمَةٌ لَّنَا أَخَذْنَا مِنَ الْمَصِيرِ ﴿٤٨﴾ قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّمَا أَنَا لَكُمْ نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٤٩﴾ فَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ ﴿٥٠﴾ وَالَّذِينَ سَعَوْا فِي ءَايَاتِنَا مُعْجِزِينَ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ ﴿٥١﴾ وَمَا أَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ مِن رُّسُولٍ وَلَا نَبِيٍّ إِلَّا إِذَا تَمَنَّىٰ أَلْفَى الشَّيْطَانُ فِي أُمْنِيَّتِهِ فَيَنسَخُ اللَّهُ مَا يُلْقِي الشَّيْطَانُ ثُمَّ يُحْكِمُ اللَّهُ ءَايَاتِهِ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٥٢﴾ لِيَجْعَلَ مَا يُلْقِي الشَّيْطَانُ فِتْنَةً لِلَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ وَالْقَاسِيَةِ قُلُوبُهُمْ ۗ وَإِنَّ الظَّالِمِينَ لَفِي شِقَاقٍ بَعِيدٍ ﴿٥٣﴾ وَلَيَعْلَمَنَّ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ أَنَّهُ الْحَقُّ مِن رَّبِّكَ فَيُؤْمِنُوا بِهِ فَتُخْبِتَ لَهُ قُلُوبُهُمْ ۗ وَإِنَّ اللَّهَ لَهَادٍ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا إِلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٥٤﴾ وَلَا يَزَالُ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي مِرْيَةٍ مِّنْهُ حَتَّىٰ تَأْتِيَهُمُ السَّاعَةُ بَغْتَةً أَوْ يَأْتِيَهُمْ عَذَابٌ يَوْمٍ عَقِيمٍ ﴿٥٥﴾ أَلَمْ لِكُ يَوْمَئِذٍ لِّلَّهِ تَخَكُّمٌ بَيْنَهُمْ ۗ فَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فِي جَنَّاتِ النَّعِيمِ ﴿٥٦﴾ وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِءَايَاتِنَا فَأُولَٰئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ مُّبِينٌ ﴿٥٧﴾

وَيَسْتَعْجِلُونَكَ بِالْعَذَابِ وَلَنْ تُخْلِفَ اللَّهُ وَعْدَهُ ۗ وَإِنَّ يَوْمًا عِنْدَ رَبِّكَ كَأَلْفِ سَنَةٍ مِمَّا تَعُدُّونَ ﴿٤٧﴾ وَكَأَيِّن مِّن قَرْيَةٍ أَمَلَيْتُهَا وَهِيَ ظَالِمَةٌ لَّنَا أَخَذْنَا مِنَ الْمَصِيرِ ﴿٤٨﴾

47. Na wanakuhimiza ulete adhabu, lakini Allah Hatakwenda kinyume na ahadi Yake kabisa. Na hakika siku moja kwa Mola wako Mlezi ni kama miaka elfu munavyo hisabu nyinyi.

48. Na miji mingapi Niliipa muda na hali ilikuwa ime-dhulumu, na kisha Nikaitia Mkononi? Na Kwangu Mimi ndio marudio yote.

**Makafiri Wanataka Adhabu**

Allah تعالى Anamuambia Mtume Wake ﷺ:

وَيَسْتَعْجِلُونَكَ بِالْعَذَابِ

“Na wanakuhimiza ulete adhabu”.

Maana yake: Hawa makafiri, wasiomuamini Allah تعالى,

وَإِذْ قَالُوا اٰللّٰهُمَّ اِنْ كَانَ هٰذَا هُوَ الْحَقُّ مِنْ عِنْدِكَ فَاَمْطِرْ عَلَيْنَا حِجَارَةً مِّنَ السَّمَآءِ  
 اَوْ اَتِنَا بِعَذَابٍ اَلِيْمٍ ﴿٨٢﴾

**“Na waliposema: Ee Allah! Ikiwa haya ni kweli itokayo Kwako basi tunyeshee mawe kutoka mbinguni, au tulettee adhabu yoyote iliyo chungu.” (8:32).**

وَقَالُوا رَبَّنَا عَجِّلْ لَنَا قِطْنَآ قَبْلَ يَوْمِ الْحِسَابِ ﴿٨٣﴾

**“Na wao husema: Mola wetu Mlezi! Tulettee upesi sehemu yetu ya adhabu kabla ya Siku ya Hesabu.” (38:16).**

Na Kauli Yake:

وَلَنْ يُخْلِفَ اللّٰهُ وَعْدَهُ ؕ

**“Lakini Allah Hatakwenda kinyume na ahadi Yake kabisa”.**

Maana yake: Ahadi Yake kukileta Kiyama na Kuwamaliza maadui Zake na Kuwakirimu marafiki Zake wa karibu.

Na Kauli Yake:

وَإِنَّ يَوْمًا عِنْدَ رَبِّكَ كَأَلْفِ سَنَةٍ مِّمَّا تَعُدُّوْنَ ﴿٨٤﴾

**“Na hakika siku moja kwa Mola wako Mlezi ni kama miaka elfu munavyo hisabu nyinyi.”**

Maana yake: Yeye Aliyetukuka Hafanyi haraka kabisa, kwani kwa inayohesabiwa na viumbe Vyake kuwa ni miaka elfu moja Kwake ni kama siku moja tu, Naye Anajua kuwa Anaweza kulipiza kisasi na kuwa hatopitwa na kitu chochote, japokuwa Anachelewesha, Anangojea na Kuakhirisha.

Hivyo, kisha Anasema:

وَكَأَيِّن مِّن قَرْيَةٍ أَمَلَّتْ لَهَا وَهِيَ ظَالِمَةٌ ثُمَّ أَخَذْنَا وَإِلَى الْمَصِيرِ ﴿٨٥﴾

**“Na miji mingapi Niliipa muda na hali ilikuwa imedhulumu, na kisha Nikaitia Mkononi? Na Kwangu Mimi ndio marudio yote.”**

Amepokea Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى kutoka kwa Abu Hurayrah عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ amesema:

«يَدْخُلُ فُقَرَاءُ الْمُسْلِمِينَ الْجَنَّةَ قَبْلَ الْأَغْنِيَاءِ بِنِصْفِ يَوْمٍ خَمْسِمِائَةِ عَامٍ»

*“Masikini (mafakiri) miongoni mwa Waislamu wataingia Peponi kabla ya matajiri kwa nusu siku – miaka mia tano”.*

Na imenukuliwa na At-Tirmidhiy na An-Nasaa’iy kwa Hadithi ya Ath- Thawriy kutoka kwa Muhammad bin ‘Amr. At-Tirmidhiy amesema: “Ni Hadithi Hasan Sahih”<sup>1</sup>.

Na amepokea na Abu Daud, mwisho wa Kitabu cha *Al-Malaahim* (misukosuko mwisho wa zama) katika Sunan yake kutoka kwa Sa’d bin Abi Waqqaasw عنه رضي الله kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنِّي لَأَرْجُو أَنْ لَا تَعْجِزَ أُمَّتِي عِنْدَ رَبِّهَا أَنْ يُؤَخَّرَهُمْ نِصْفَ يَوْمٍ»

*“Hakika mimi natamani kuwa hakutakuwa na uzito kwa Umma wangu mbele ya Mola wao wakicheleweshwa kwa nusu siku”.*

Sa’d عنه رضي الله aliulizwa: “Nusu siku ina maana gani?” Akasema: “Miaka mia tano”<sup>2</sup>.

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّمَا أَنَا لَكُمْ نَذِيرٌ مُبِينٌ ﴿٤٩﴾ فَأَلَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ هُمْ  
مَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ ﴿٥٠﴾ وَالَّذِينَ سَعَوْا فِي ءَايَاتِنَا مُعْجِرِينَ أُولَٰئِكَ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ ﴿٥١﴾

**49. Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni muonyaji kwenu niliye dhahiri.**

**50. Basi walioamini na wakatenda mema watapata maghufira na riziki za ukarimu.**

**51. Na wanaojitahidi kuzipinga Aya Zetu hao ndio watu wa Motoni.**

<sup>1</sup> At-Tirmidhiy 2354 na An-Nasaa’iy katika Al-Kubraa 6:412.

<sup>2</sup> Abu Daud 4:517. Hadithi ina dosari.

## Malipo ya Watu Wema na Watu Waovu

Allah تعالى Anamuambia Mtume Wake ﷺ pale makafiri walipotaka kuharakishwa kwao adhabu:

قُلْ يَتَّيِبُوا النَّاسُ إِنَّمَا أَنَا لَكُمْ نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٤٧﴾

**“Sema: Enyi watu! Hakika mimi ni muonyaji kwenu niliye dhahiri.”**

Maana yake: Allah تعالى Amenituma kwenu kuwaonya kwa adhabu kali itakayokuja wala hesabu yenu haiko mikononi mwangu. Amri yenu iko kwa Allah تعالى, Ambaye Akitaka Atawaletea adhabu kwa haraka na Akipenda Atawacheleweshea, na Akipenda Atawasamehe wenye kumuomba msamaha, na pia Akitaka Atawapoteza waliochagua kuangamia. Yeye Ndiye Mwenye Uweza wa Kufanya Atakalo na Analochagua.

لَا مُعَقَّبَ لِحُكْمِهِ ۚ وَهُوَ سَرِيعُ الْحِسَابِ ﴿٤٨﴾

**“Na hapana wa kupinga Hukumu Yake, Naye ni Mwepesi wa Kuhesabu.” (13:41)**

إِنَّمَا أَنَا لَكُمْ نَذِيرٌ مُّبِينٌ ﴿٤٩﴾ فَأَلْذِيبْ ءَامِنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

**“Hakika mimi ni muonyaji kwenu niliye dhahiri. Basi walioamini na wakatenda mema.”**

Maana yake: Walio na imani nyoyoni mwao na wakasadikisha Imani yao kwa kufanya amali.

هُمْ مَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ ﴿٥٠﴾

**“Watapata msamaha na riziki za ukarimu.”**

Msamaha kwa yaliyopita katika makosa waliyoyafanya na thawabu nyingi kwa matendo machache na madogo. Na amesema Muhammad bin Ka’ab Quradhiy: “Unaposikia Allah تعالى Anasema:

وَرِزْقٌ كَرِيمٌ ﴿٥١﴾

**“Na riziki za ukarimu.” Inamaanisha Pepo”<sup>1</sup>**

Na Amesema Aliyetukuka:

<sup>1</sup> Ad-Durr al-Manthuur 6:63.

وَالَّذِينَ سَعَوْا فِي آيَاتِنَا مُعْجِزِينَ

**“Na wanaojitahidi kuzipinga Ayah Zetu”.**

Amesema Mujaahid: “Wanawakataza watu kumfuata Mtume ﷺ<sup>1</sup>. Na hivyo ndivyo alivyosema ‘Abdallaah bin Az- Zubayr رضي الله عنه, “Kuwavunja moyo”<sup>2</sup>. Na amesema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما: “Kuwapa hima ya kuwapinga Waumini kwa inadi na ukaidi”<sup>3</sup>.

أُولَئِكَ أَصْحَابُ الْجَحِيمِ ﴿٥٨﴾

**“Hao ndio watu wa Motoni”.**

Na huo ni Moto mkali wenye kuleta maumivu na adhabu kali, Allah تعالى Atuepushe nao. Allah تعالى Anasema:

الَّذِينَ كَفَرُوا وَصَدُّوا عَنْ سَبِيلِ اللَّهِ زِدْنَاهُمْ عَذَابًا فَوْقَ الْعَذَابِ بِمَا كَانُوا يُفْسِدُونَ ﴿٥٨﴾

**“Wale waliokufuru na kuzuilia njia ya Allah Tutawazidishia adhabu juu ya adhabu, kwa walivyokuwa wakifisidi.” (16:88).**

وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ وَلَا نَبِيٍّ إِلَّا إِذَا تَمَنَّى أَلْقَى الشَّيْطَانُ فِي أُمْنِيَّتِهِ فَيَنْسَخُ اللَّهُ مَا يُلْقِي الشَّيْطَانُ ثُمَّ يُحْكِمُ اللَّهُ آيَاتِهِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٥٩﴾ لِيَجْعَلَ مَا يُلْقِي الشَّيْطَانُ فِتْنَةً لِلَّذِينَ فِي قُلُوبِهِمْ مَرَضٌ وَالْقَاسِيَةِ قُلُوبُهُمْ وَإِنَّ الظَّالِمِينَ لَفِي شِقَاقٍ بَعِيدٍ ﴿٦٠﴾ وَلَيَعْلَمَنَّ الَّذِينَ أوتُوا الْعِلْمَ أَنَّهُ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ فَيُؤْمِنُوا بِهِ فَتُخْبِتَ لَهُ قُلُوبُهُمْ وَإِنَّ اللَّهَ لَهَادٍ لِلَّذِينَ ءَامَنُوا إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٦١﴾

**52. Na hatukumtuma kabla yako Mtume wala Nabii ila anaposoma, Shetani hutia (fitina) katika masomo yake hayo. Lakini Allah**

<sup>1</sup> Tabari 18:662.

<sup>2</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 6:64.

<sup>3</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 6:64.

***Huyaondoa anayoyatia Shetani; kisha Allah Huzimakinisha Aya Zake. Na Allah ni Mjuzi Mwenye Hekima.***

***53. Hayo ni ili alifanye lile analolitia Shetani liwe ni mtihani kwa wale wenye maradhi ndani ya nyoyo zao, na wale ambao nyoyo zao ni ngumu. Na hakika madhalimu wamo katika khitilafu iliyo mbali (na haki).***

***54. Na ili waliopewa elimu wajue kuwa hayo ni Haki itokayo kwa Mola wako Mlezi na waamini, na zipate kutua nyoyo zao. Na hakika Allah Ndiye Anayewaongoa wenye kuamini kwenye njia iliyonyooka.***

### **Shetani Hutumbukiza Uongo katika maneno ya Mitume na Allah تعالى Huubatilisha**

Hakika wafasiri wengi wametaja hapa kisa cha *Al-Gharaaniq*, na jinsi gani wale wengi waliohamia Habashah (Ethiopia) walirudi (Makka) walipodhania ya kuwa washirikina wa Quraysh wamesilimu, lakini Hadithi zote hizo zimekuja kwa njia ya silsila za upokezi uliokuwa *Mursal*.<sup>1</sup> Na sidhani kabisa kama ipo yoyote iliyo Sahihi. Na Allah تعالى Anajua zaidi.

Amepokea Al-Bukhaari kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema:

فِي أُمَّتِيهِمْ

***“Katika masomo yake.”***

Maana yake: “Anapozungumza shetani hutumbukiza (uongo) katika maneno yake, lakini Allah تعالى Huyabatilisha hayo yaliyotumbukizwa na shetani”<sup>2</sup>.

نُمِّتْكُمْ اللَّهُ أَيْتِيهِمْ

***“Kisha Allah Huzithibitisha Aya Zake”.***

Amepokea 'Aliy bin Abi Twalhah kutoka kwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kuwa,

<sup>1</sup> *Mursal*: Silsila ya mapokezi inayosimama kabla ya Swahaba.

<sup>2</sup> Fat'h Al-Baariy 8:292.

إِذَا تَمَنَّى أَلْقَى الشَّيْطَانَ فِي أُمْنِيَّتِهِ

***“Anaposoma, Shetani hutia (fitina) katika masomo yake hayo....”***

Amesema: “Anapozungumza shetani hutumbukiza (uwongo) katika mazungumzo yake”<sup>1</sup>. Na amesema Mujaahid:

إِذَا تَمَنَّى

***“Anaposoma.”***

Maana yake: Anaposema<sup>2</sup>. Na panasemwa: Inamaanisha kisomo chake.

تَمَنَّى

***“Anaposoma.”***

Maana yake: Kutalii Kitabu cha Allah تعالى,

أَلْقَى الشَّيْطَانَ فِي أُمْنِيَّتِهِ

***“Shetani hutia (fitina) katika masomo yake hayo...”***

Maana yake: katika kisomo chake<sup>3</sup>. Na amesema Adh-Dhahaak:

إِذَا تَمَنَّى

***“Anaposoma.”***

Maana yake: Durusu<sup>4</sup>. Amesema Ibn Jariir رحمه الله تعالى kuwa kauli hii inafanana na kufasiri maneno<sup>5</sup>. Na Kauli Yake:

فَيَنْسَخُ اللَّهُ مَا يُلْقِي الشَّيْطَانُ

***“Kisha Allah Huyaondoa anayoyatia shetani.”***

<sup>1</sup> Tabari 18:667.

<sup>2</sup> Tabari 18:667.

<sup>3</sup> Al-Baghawiy 3:293.

<sup>4</sup> Tabari 18:668.

<sup>5</sup> Tabari 18:668.



Hakika ya maana ya neno *Naskh* katika lugha ya kiarabu ni kuondoa au kunyanyua. Amepokea 'Aliy bin Abi Twalhah kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: "Huyabatilisha (kuyafuta) Allah تعالى aliyoyatumbukiza Shetani"<sup>1</sup>. Na Kauli Yake:

وَاللَّهُ عَلِيمٌ

**"Na Allaah ni Mjuzi."** Maana yake: Kwa yatakyokuwa na kutokea katika mambo na matukio na hakuna linalojificha Kwake.

حَكِيمٌ

**"Mwenye Hekima."** Maana yake: Katika Makadirio Yake, Kuumba Kwake na Amri Yake, Yeye Ndiye Mwenye Hekima iliyotimia na hoja iliyokamilika. Kwa hiyo Akasema:

لِيَجْعَلَ مَا يُلْقَى الشَّيْطَانُ فِتْنَةً لِلَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ

**"Hayo ni ili alifanye lile analolitia Shetani liwe ni mtihani kwa wale wenye maradhi ndani ya nyoyo zao."**

Maana yake: Shaka, ushirikina, ukafiri na unafiki. Ibn Jarir رحمه الله تعالى amesema:

لِلَّذِينَ فِي قُلُوبِهِم مَّرَضٌ

**"Wale wenye maradhi ndani ya nyoyo zao."** Hao ni wanafiki na,

وَالْقَاسِيَةِ قُلُوبُهُمْ

**"Na wale ambao nyoyo zao ni ngumu."** Hao ni washirikina<sup>2</sup>.

وَإِنَّ الظَّالِمِينَ لَفِي شِقَاقٍ بَعِيدٍ ﴿٥٧﴾

**"Na hakika madhalimu wamo katika khitilafu iliyo mbali (na haki)."**

Maana yake: Wapo katika upotevu, kupinga, inadi pamoja na ukaidi wa mbali, yaani mbali sana na haki na njia ya sawa.

وَلِيَعْلَمَ الَّذِينَ أُوتُوا الْعِلْمَ أَنَّهُ الْحَقُّ مِنْ رَبِّكَ فَيُؤْمِنُوا بِهِ

**"Na ili waliopewa elimu wajue kuwa hayo ni Haki itokayo kwa Mola wako Mlezi na waamini."**

<sup>1</sup> Tabari 18:668.

<sup>2</sup> Tabari 18:669.

Maana yake: Wajue wale waliopewa elimu ya manufaa, ambayo kwayo wanaweza kutofautisha baina ya haki na batili. Wale wanaoamini Mtume Wake, wajue kuwa Tulioteremsha kwako ni haki kutoka kwa Mola wako Mlezi, Aliyeteremsha kwa Elimu Yake na chini ya Ulinzi Wake, Naye Ataihifadhi kutokana na kuchang'anyika na chochote. Kwa hakika, ni Kitabu chenye hekima ambacho,

لَا يَأْتِيهِ الْبَطْلُ مِنْ بَيْنِ يَدَيْهِ وَلَا مِنْ خَلْفِهِ تَنْزِيلٌ مِّنْ حَكِيمٍ حَمِيدٍ ﴿٤٧﴾

***“Haitakifia batili mbele yake wala nyuma yake; kimeteremshwa na Mwenye Hekima, Ahimidiwaye.” (41:42).***

Na Kauli Yake:

فَيُؤْمِنُوا بِهِ

***“Na waamini.”*** Maana yake: Wakisadiki pamoja na kukifuata.

فَتُخْبِتَ لَهُ قُلُوبُهُمْ ۗ

***“Na zipate kutua nyoyo zao.”*** Maana yake: Nyoyo zao zinanyenyeka na kujidhalilisha na kuikubali.

وَإِنَّ اللَّهَ لَهَادِ الَّذِينَ ءَامَنُوا إِلَىٰ صِرَاطٍ مُّسْتَقِيمٍ ﴿٤٨﴾

***“Na hakika Allah Ndiye Anayewaongoa wenye kuamini kwenye njia iliyonyooka.”***

Maana yake: Katika dunia na Akhera. Ama katika dunia Anawaongoza katika njia ya haki na Kuwasaidia kuifuata na kwenda kinyume na kuiepuka batili; na katika Akhera inawaongoza katika njia iliyonyooka inayomfikisha katika daraja kuu za Peponi na kumuokoa yeye na adhabu kali iumizayo na tabaka za chini Motoni.

وَلَا يَزَالُ الَّذِينَ كَفَرُوا فِي رِزْوَانٍ مِّنْهُ حَتَّىٰ تَأْتِيَهُمُ السَّاعَةُ بَغْتَةً أَوْ يَأْتِيَهُمْ عَذَابٌ

يَوْمٍ عَقِيمٍ ﴿٤٩﴾ الْمَلَأُ يَوْمَئِذٍ لِلَّهِ يَخْضَعُونَ بَيْنَهُمْ ۗ فَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا

الصَّالِحَاتِ فِي جَنَّاتٍ التَّعْبِيرِ ﴿٥٠﴾ وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا فَأُولَٰئِكَ لَهُمْ

عَذَابٌ مُّهِينٌ ﴿٥١﴾

**55. Na waliokufuru hawatoacha kuwa katika wasiwasi kwa hilo mpaka Saa iwafikie ghafla, au iwafikie adhabu ya Siku Tasa.**

**56. Ufalme wote siku hiyo utakuwa wa Allah. Atahukumu baina yao. Basi walioamini na wakatenda mema watakuwa katika Bustani zenye neema.**

**57. Na waliokufuru na kuzikanusha Ishara Zetu, basi hao watapata adhabu ya kufedhehesha.**

### Makafiri Wataendelea Kuwa Katika Shaka na Kuchanganyikiwa

Anasema Aliyetukuka Kutupasha habari kuhusu makafiri ambao wanabaki katika shaka kuhusiana na Qur'ani hii. Huu ulikuwa ni muono wa Ibn Jurayj <sup>1</sup>رحمَهُ اللهُ تعالى na pia ni rai iliyochaguliwa na Ibn Jariir <sup>1</sup>رحمَهُ اللهُ تعالى.

حَتَّىٰ تَأْتِيَهُمُ السَّاعَةُ بَغْتَةً

**“Mpaka Saa iwafikie ghafla”. Amesema Mujaahid:**

بَغْتَةً

**“Kwa ghafla.”**<sup>2</sup> Na amesema Qatadah: “Bila ya kutarajia”, Amri ya Allah تعالى itawakuta watu bila kutambua. Allah تعالى Hawapatilizi watu ila wanapokuwa wamelewa na kiburi, huku wanastarehe na wakidhanja kuwa adhabu haitawajia. Tujue kuwa Allah تعالى Hawaadhibu ila waovu. Na Kauli Yake:

أَوْ يَأْتِيَهُمْ عَذَابٌ يَوْمٍ عَقِيمٍ ﴿٢٠﴾

**“Au iwafikie adhabu ya Siku Tasa”.**

Amepokea Mujaahid kuwa Ubayy bin Ka'b amesema: “Hiyo ni Siku ya Badr”. Na amesema 'Ikrimah na Mujaahid: “Hiyo ni Siku ya Kiyama, ambayo haitakuwa na usiku wake”<sup>3</sup>. Na hivyo ndivyo alivyosema Adh-Dhahaak na Al-Hasan Al-Baswriy<sup>4</sup>. Na kwa hiyo Akasema:

<sup>1</sup> Tabari 18:670.

<sup>2</sup> Tabari 11:360.

<sup>3</sup> Al-Baghawiy 3:295.

<sup>4</sup> Al-Baghawiy 3:295.

الْمَلِكُ يَوْمَئِذٍ لِّلَّهِ تَحْكُمُ بَيْنَهُمْ

**“Ufalme wote siku hiyo utakuwa ni wa Allah. Atahukumu baina yao.”**

Hii ni kama Aya ifuatayo:

مَلِكِ يَوْمِ الدِّينِ ﴿٤﴾

**“Mwenye kumiliki Siku ya Malipo.” (1:4).**

الْمَلِكُ يَوْمَئِذٍ الْحَقُّ لِلرَّحْمَنِ ؕ وَكَانَ يَوْمًا عَلَى الْكَافِرِينَ عَسِيرًا ﴿٢٦﴾

**“Ufalme wa haki siku hiyo utakuwa wa Mwingi wa Rehema, na itakuwa ni siku ngumu kwa makafiri.” (25:26).**

فَالَّذِينَ ءَامَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ

**“Basi walioamini na wakatenda mema.”**

Maana yake: Wameamini kwa mioyo yao na kumsadiki Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ na wakafanya amali kulingana na wanayoyajua; nyoyo zao zikaafikiana na kauli na amali zao.

فِي جَنَّاتِ النَّعِيمِ ﴿٥٧﴾

**“Watakuwa katika Bustani zenye neema.”**

Maana yake: Watakuwa kwenye neema inayoendelea bila kukatika wala kuondoka.

وَالَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا بِآيَاتِنَا

**“Na waliokufuru na kuzikanusha Ishara Zetu.”**

Maana yake: Nyoyo zao zilikanusha haki na kuipinga, walikadhibisha na kwenda kinyume na ujumbe wa Mitume na kiburi kikawafanya wasiwafuate (Mitume).

فَأُولَٰئِكَ لَهُمْ عَذَابٌ مُّهِينٌ ﴿٥٨﴾

**“Basi hao watapata adhabu ya kufedhehesha.”** Maana yake: Kulipwa kwa kukengeuka kwao kwa kiburi kutofuata haki.

Hii ni kama Kauli Yake:

إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِي سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ ﴿١٠٠﴾

***“Kwa hakika wale wajivunao kufanya Ibada Yangu, bila shaka wataingia Jahanamu, wadhalilike.” (40:60),***

Maana yake: Wakiwa wadogo.

\* \* \*

وَالَّذِينَ هَاجَرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ ثُمَّ قُتِلُوا أَوْ مَاتُوا  
لَيْرِزْقَنَّهُمْ اللَّهُ رِزْقًا حَسَنًا ۗ وَإِنَّ اللَّهَ لَهُوَ خَيْرُ الرَّازِقِينَ ۚ  
﴿٥٨﴾ لَيَدْخِلْنَهُمْ مُدْخَلَ رِزْوَانِهِ ۗ وَإِنَّ اللَّهَ لَعَلِيمٌ حَلِيمٌ  
﴿٥٩﴾ \* ذَلِكَ وَمَنْ عَاقَبَ بِمِثْلِ مَا عُوقِبَ بِهِ ثُمَّ بُغِيَ  
عَلَيْهِ لَيَنْصُرْنَاهُ اللَّهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَعَفُوفٌ غَفُورٌ ﴿٦٠﴾ ذَلِكَ  
بِأَنَّ اللَّهَ يُرِيحُ اللَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَيُورِيحُ النَّهَارَ فِي اللَّيْلِ وَأَنَّ  
اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ ﴿٦١﴾ ذَلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ  
وَأَنَّ مَا يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ هُوَ الْبَاطِلُ وَأَنَّ اللَّهَ  
هُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ ﴿٦٢﴾ أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ أَنْزَلَ مِنَ  
السَّمَاءِ مَاءً فَتُصْبِحُ الْأَرْضُ مُخْضَرَّةً ۗ إِنَّ اللَّهَ لَطِيفٌ  
خَبِيرٌ ﴿٦٣﴾ لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ وَإِنَّ  
اللَّهَ لَهُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ ﴿٦٤﴾ أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ سَخَّرَ لَكُمْ  
مَا فِي الْأَرْضِ وَالْفُلْكَ تَجْرِي فِي الْبَحْرِ بِأَمْرِهِ وَيُمْسِكُ  
السَّمَاءَ أَنْ تَقَعَ عَلَى الْأَرْضِ إِلَّا بِإِذْنِهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ بِالنَّاسِ  
لَرءُوفٌ رَحِيمٌ ﴿٦٥﴾ وَهُوَ الَّذِي أَحْيَاكُمْ ثُمَّ يُمِيتُكُمْ  
ثُمَّ يُحْيِيكُمْ ۗ إِنَّ الْإِنْسَانَ لَكَفُورٌ ﴿٦٦﴾ لِكُلِّ أُمَّةٍ جَعَلْنَا  
مَنْسَكًا هُمْ نَاسِكُوهُ ۗ فَلَا يُنْبِرُ عَلَيْكَ فِي الْأَمْرِ ۗ وَادْعُ إِلَى  
رَبِّكَ ۗ إِنَّكَ لَعَلَىٰ هُدًى مُسْتَقِيمٍ ﴿٦٧﴾ وَإِنْ جَدَلُوكَ  
فَقُلِ اللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿٦٨﴾ اللَّهُ يَحْكُمُ بَيْنَكُمْ يَوْمَ  
الْقِيَامَةِ فِيمَا كُنْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿٦٩﴾

وَالَّذِينَ هَاجَرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ ثُمَّ قُتِلُوا أَوْ مَاتُوا لَيْرِزْقَنَّهُمْ اللَّهُ رِزْقًا حَسَنًا ۗ وَإِنَّ اللَّهَ لَهُوَ خَيْرُ الرَّازِقِينَ ۚ لَيَدْخِلْنَهُمْ مُدْخَلَ رِزْوَانِهِ ۗ وَإِنَّ اللَّهَ لَعَلِيمٌ حَلِيمٌ ﴿٥٨﴾ \* ذَلِكَ وَمَنْ عَاقَبَ بِمِثْلِ مَا عُوقِبَ بِهِ ثُمَّ بُغِيَ عَلَيْهِ لَيَنْصُرْنَاهُ اللَّهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَعَفُوفٌ غَفُورٌ ﴿٥٩﴾ ذَلِكَ وَمَنْ عَاقَبَ بِمِثْلِ مَا عُوقِبَ بِهِ ثُمَّ بُغِيَ عَلَيْهِ لَيَنْصُرْنَاهُ اللَّهُ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَعَفُوفٌ غَفُورٌ ﴿٦٠﴾

58. Na waliohama kwa ajili ya Allah, kisha wakauwawa au wakafa, bila ya shaka Allah Atawaruzuku riziki njema. Na hakika Allah ni Mbora wa wanaoruzuku.

59. Bila ya shaka Atawazingiza pahala watakapoparidhia. Na hakika Allah ni Mjuzi na Mpole.

60. Ndio namna hivi. Na anayelipiza mfano wa alivyoadhibiwa, kisha akadhulumiwa, basi hapana shaka Allah Atamsaidia. Hakika Allah ni Msamehevu Mwenye Maghufira.

### Ujira Mkubwa kwa Wale Waliohama kwa Ajili ya Allah تعالى

Anatupasha habari Allah تعالى kuhusu wale waliohama kwa ajili ya Allah تعالى, kwa kutaka Radhi Zake na Aliyonayo, wakiacha nyuma yao nchi, familia, marafiki na wakaiacha nchi yao kwa ajili ya Allah تعالى na Mtume Wake ﷺ na kuinusuru Dini ya Allah تعالى, **“kisha wakauwawa”** Maana yake: Katika Vita vya Jihadi au **“wakafa.”** yaani bila ya kupigana katika Jihadi, watakuwa wamepata thawabu nyingi na ujira mkubwa sana. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَمَنْ تَخْرُجْ مِنْ بَيْتِهِ مُهَاجِرًا إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ ثُمَّ يُدْرِكْهُ الْمَوْتُ فَقَدْ وَقَعَ أَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ

**“Na anayetoka katika nyumba yake ili kuhama kwa ajili ya Allah na Mtume Wake, kisha yakamfikia mauti (njiani), basi umehakikika ujira wake juu ya Allah...” (4:100).**

Na Kauli Yake Allah تعالى:

لَيَرْزُقْنَهُمُ اللَّهُ رِزْقًا حَسَنًا

**“Bila ya shaka Allah Atawaruzuku riziki njema”.**

Maana yake: Atawapa ujira kutokana na Fadhila Zake na Riziki Zake. Pepo ambayo Atawapa itakayowatuliza macho yao.

وَإِنَّ اللَّهَ لَهُوَ خَيْرُ الرَّزُقِينَ ﴿٥٨﴾ لَيَدْخِلْنَهُمْ مُدْخَلَ بَيْتِ كَثِيرٍ مِّنْ دُونِهِ

**“Na hakika Allah ni Mbora wa wanaoruzuku. Bila ya shaka Atawaingiza pahala watakapoparidhia”.**

Maana yake: Pepo kama Alivyosema Aliyetukuka:

فَأَمَّا إِن كَانَ مِنَ الْمُقْرَبِينَ ﴿٥٩﴾ فَرَوْحٌ وَرَيْحَانٌ وَجَنَّتْ نَعِيمٌ ﴿٦٠﴾

**“Basi akiwa ni miongoni mwa wale waliokaribishwa (na Allah). Basi ni raha kubwa na manukato mazuri na bustani zenye neema.” (56:88-89).**

Allah تعالى Anatueleza kuwa Atampatia raha, starehe, riziki na neema ya Pepo, kama Alivyosema Aliyetukuka hapa:

لَيَرْزُقْنَهُمُ اللَّهُ رِزْقًا حَسَنًا

**“Bila ya shaka Allah Atawaruzuku riziki njema.”**

Kisha Akasema:

لَيَدْخِلْنَهُمْ مُدْخَلَ بَرِّصَوْتِهِ وَإِنَّ اللَّهَ لَعَلِيمٌ

**“Bila ya shaka Atawaingiza pahala watakapoparidhia. Na hakika Allah ni Mjuzi.”**

Maana yake: Kwa anayehama na kupigana Jihadi katika njia Yake na kwa anayestahiki hayo.

حَلِيمٌ

**“Mpole.”**

Maana yake: Ni Mpole, Anasamehe, Anaghufiria madhambi na Anakubali kama kafara kwa kule kuhama kwao na kumtegemea Yeye tu.

Ama kuhusu wale wanaouwawa katika njia ya Allah تعالى miongoni mwa aliyehama au asiyehama, hakika yeye atakuwa hai mbele ya Mola wake Mlezi akiwa anaruzukiwa.

Kama Anavyosema Aliyetukuka:

وَلَا تَحْسَبَنَّ الَّذِينَ قُتِلُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أَمْوَاتًا بَلْ أَحْيَاءٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ يُرْزُقُونَ

**“Wala usiwadhani wale waliouwawa katika njia ya Allah kuwa ni wafu. Bali wahai, wanaruzukiwa kwa Mola wao Mlezi.” (3:169).**

Na Hadithi juu ya jambo hili ni nyingi kama tulivyotangulia kuzitaja. Ama kuhusu wale wenye kufariki kwa ajili ya Allah تعالى akiwa ni mwenye kuhama au si mwenye kuhama, hakika Aya hii tukufu na Hadithi Sahihi zimemdhamini kupata riziki nzuri na kukirimiwa na Allah تعالى.

Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى amesema kuwa Shurahbil bin As-Simtwi amesema: “Kulinda na kukaa kwetu katika kuizunguka ngome moja katika nchi ya Roma ilichukua muda mrefu sana. Salmaan Al-Faarisiy رضي الله عنه alipita na kusema: ‘Hakika nimemsikia Mtume ﷺ akisema:



«مَنْ مَاتَ مُرَابِعًا أُجْرَى اللَّهُ عَلَيْهِ بِمِثْلِ ذَلِكَ الْأَجْرِ، وَأُجْرَى عَلَيْهِ الرَّزْقُ، وَأَمِنْ مِنَ النَّسَّانِينَ، وَأَقْرَبُوا إِنْ شِئْتُمْ: ﴿وَالَّذِينَ هَاجَرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ ثُمَّ قُتِلُوا أَوْ مَاتُوا لَيَرْزُقَنَّهُمُ اللَّهُ رِزْقًا حَسَنًا وَإِنَّ اللَّهَ لَهُوَ خَيْرُ الرَّازِقِينَ﴾ ﴿٥٨﴾ لَيُدْخِلَنَّهُمْ مُدْخَلًا رِضْوَانًا وَإِنَّ اللَّهَ لَكَلِيمٌ حَلِيمٌ ﴿٥٩﴾»

*“Yeyote mwenye kuaga dunia akilinda mipaka ya Uislamu, Allah Atampatia ujira kama ule wa shahidi na Atamruzuku na Kumuepusha na mitihani. Soma ukitaka: ‘Na waliohama kwa ajili ya Allah, kisha wakauwawa au wakafa, bila ya shaka Allah Atawaruzuku riziki njema. Na hakika Allah ni Mbora wa wanaoruzuku. Bila ya shaka Atawaingiza pahala watakapoparidhia. Na hakika Allah ni Mjuzi na Mpole”<sup>1</sup>.*

Na imepokewa tena kutoka kwa ‘Abdur-Rahman bin Jahdam Al-Khawlaaniy kuwa alikuwa pamoja na Fadhwaalah bin ‘Ubayd waliposindikiza majeneza mawili katika kisiwa, mmoja wao akiwa amepatwa na *manjaniiq* (manati) na mwingine alikufa kifo cha kawaida. Fadhwaalah bin ‘Ubayd akakaa kwenye kaburi ya aliyeaga dunia (kwa kawaida), akaambiwa: “Umemuacha shahidi bila kuketi kwenye kaburi lake?” Akasema: “Sina wasiwasi wowote wa kufufuliwa kutoka kwa kaburi lolote kati ya hawa wawili, kwani Allah تعالی Anasema:

﴿وَالَّذِينَ هَاجَرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ ثُمَّ قُتِلُوا أَوْ مَاتُوا لَيَرْزُقَنَّهُمُ اللَّهُ رِزْقًا حَسَنًا

***‘Na waliohama kwa ajili ya Allah, kisha wakauwawa au wakafa, bila ya shaka Allah Atawaruzuku riziki njema’.***

Alizisoma Aya hizi mbili, kisha akasema: ‘Ewe mja wataka nini ikiwa nitaingizwa kwenye mlango kwa Ridhaa Yake na kuruzukiwa riziki njema? Kwa Allah تعالی, sijali kaburi gani kati ya haya mawili Allah تعالی Atanifufua kutoka kwayo”<sup>2</sup>.

<sup>1</sup> Ibn Abi Haatim 8:2503.

<sup>2</sup> Atw-Twabaray 9:182.

ذَلِكَ وَمَنْ عَاقَبَ بِمِثْلِ مَا عُوقِبَ بِهِ

**“Ndio namna hivi. Na anayelipiza mfano wa alivyoadhibiwa.”**

Ametaja Muqaatil bin Hayyaan na Ibn Jurayj kuwa Aya hii iliteremshwa kuhusiana na uvamizi ambao Maswahaba walipambana na washirikina katika mwezi mtukufu wa Muharram (Mfungo Nne). Waislamu waliwasisitiza (washirikina) wasiwe ni wenye kupigana katika miezi Mitukufu lakini wakakataa hilo na wakasisitiza kuwa ni lazima wapigane. Kwa hiyo, Waislamu wakapigana nao, na Allah تعالى Akawatunukia ushindi kutoka Kwake.

إِنَّ اللَّهَ لَعَفُوفٌ غَفُورٌ

**“Hakika Allah ni Msamehevu Mwenye Maghufira.”**

ذَلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ يُوَلِّجُ اللَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَيُوَلِّجُ النَّهَارَ فِي اللَّيْلِ وَأَنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ

ذَلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ وَأَنَّ مَا يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ هُوَ الْبَطْلُ وَأَنَّ اللَّهَ هُوَ

الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ

**61. Hayo ni kwa kuwa Allah huingiza usiku katika mchana, na huingiza mchana katika usiku, na ya kwamba Allah ni Mwenye Kusikia Mwenye Kuona.**

**62. Hayo ni kwa kuwa Allah Ndiye wa Kweli, na kwamba wale wanaowaomba badala Yake, ni batili, na hakika Allah Ndiye Aliye Juu na Ndiye Mkubwa.**

**Muumba wa Dunia na Mwenye Kuiongoza ni Allah تعالى**

Allah تعالى Anatuambia kuwa Yeye Ndiye Muumba, Mwenye Kutawalia mambo yote ya viumbe Vyake kama Atakavyo.

Kama Alivyosema:

قُلِ اللَّهُمَّ مَلِكُ الْمَلِكِ تُؤْتِي الْمَلِكَ مَنْ تَشَاءُ وَتَنْزِعُ الْمَلِكَ مِمَّنْ تَشَاءُ وَتُعِزُّ مَنْ تَشَاءُ

وَتُذِلُّ مَنْ تَشَاءُ بِيَدِكَ الْخَيْرُ إِنَّكَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ ﴿٥٨﴾ تُوَلِّجُ اللَّيْلَ فِي النَّهَارِ

وَتُولِجُ النَّهَارَ فِي اللَّيْلِ ط وَتُخْرِجُ الْحَيَّ مِنَ الْمَمِيتِ وَتُخْرِجُ الْمَمِيتَ مِنَ الْحَيِّ ط وَتَرْزُقُ  
 مَنْ تَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ ﴿٦٧﴾

**“Sema: Ee Allah, Uliyemiliki ufalme wote! Humpa ufalme Umtakaye, na Humuondolea ufalme Umtakaye, na Humtukuza Umtukaye, na Humdhalilisha Umtakaye; kheri imo Mikononi Mwako. Bila shaka Wewe ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu. Wewe Huuingiza usiku katika mchana (mchana ukawa mrefu siku ya joto), na Huuingiza mchana katika usiku (usiku ukawa mrefu siku za baridi), na Hutoa aliye hai katika yule asiye na uhai, na Hutoa mfu katika yule aliye hai; na Humpa riziki Umtakaye bila hesabu.” (3:26-27).**

Na maana ya kuushikanisha usiku kwa mchana na mchana kwa usiku ni kuingiza huu kwa huu na kinyume chake. Wakati mwingine usiku huwa mrefu ilhali mchana ni mfupi kama katika nyakati za baridi, na wakati mwingine mchana huwa mrefu na usiku ukawa mfupi kama katika msimu wa joto.

Na Kauli Yake:

وَأَنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ ﴿٦٨﴾

**“Na ya kwamba Allah ni Mwenye Kusikia Mwenye Kuona.”**

Maana yake: Mwenye Kusikia kauli za waja Wake na Kuwaona, hakuna lolote kuhusiana nao au harakati zao kufichikana Naye kabisa. Pindi Allah تعالى Anapotuambia kuwa Yeye Ndiye Mwenye Kusimamia mambo yote ya viumbe na kuwa Anahukumumu na hakuna awezaye kugeuza Hukumu Yake, Anasema:

ذَٰلِكَ بِأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْحَقُّ

**“Hayo ni kwa kuwa Allah Ndiye wa Kweli.”**

Maana yake: Muabudiwa wa kweli, mbali Naye hakuna anayestahiki kuabudiwa. Hakika Yeye Ndiye Mwenye Ufalme Mkuu; Atakacho huwa (bila pingamizi yeyote) na Asichotaka kiwe hakiwi. Kila kitu kinamhitaji Yeye na kunyenyekea Kwake.

وَأَنْبَ مَا يَدْعُونَ مِنْ دُونِهِ هُوَ الْبَاطِلُ

**“Na kwamba wale wanaowaomba badala Yake, ni batili.”**

Maana yake: masanamu na miungu ya uongo. Na chochote kinachoabudiwa mbali na Allah تعالى ni batili, kwa kuwa hakiwezi kukudhuru wala kukunufaisha. Na Kauli Yake:

وَأَنَّ اللَّهَ هُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ ﴿٦٦﴾

**“Na hakika Allah Ndiye Aliye Juu na Ndiye Mkubwa.”**

Hii ni kama Aya:

وَهُوَ الْعَلِيُّ الْعَظِيمُ ﴿٦٧﴾

**“Na Yeye Ndiye Mkuu, Aliye Juu.” (42:4)**

Na Amesema:

الْكَبِيرُ الْمُتَعَالَى ﴿٦٨﴾

**“Mkuu na Ndiye Aliye Juu.” (13:9)**

Kila kitu kipo chini ya Nguvu Zake, Ufalme na Utukufu Wake; hapana mungu muabudiwa ila Yeye wala Mola Mlezi mbali na Yeye, kwani Yeye Ndiye Mwenye Nguvu na Utukufu kuliko yeyote, Aliye Juu na hakuna aliye juu kuliko Yeye, Yeye Ndiye Mkubwa na hakuna aliye mkubwa kuliko Yeye. Yeye Ndiye Aliyetukuka na Aliyetakasika kwa wanayosema madhalimu, waliyochupa mipaka kwa kiburi kikubwa.

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ أَنْزَلَ مِنَ السَّمَاءِ مَاءً فَتُصْبِحُ الْأَرْضُ مُخْضَرَّةً ۗ إِنَّ اللَّهَ لَطِيفٌ خَبِيرٌ ﴿٦٩﴾ لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَهُوَ الْغَفِيُّ الْحَمِيدُ ﴿٧٠﴾ أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ سَخَّرَ لَكُمْ مَّا فِي الْأَرْضِ وَالْفُلْكَ تَجْرِي فِي الْبَحْرِ بِأَمْرِهِ وَيُمْسِكُ السَّمَاءَ أَنْ تَقَعَ عَلَى الْأَرْضِ إِلَّا بِإِذْنِهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ بِالنَّاسِ لَرُؤُوفٌ رَحِيمٌ ﴿٧١﴾ وَهُوَ الَّذِي أَحْيَاكُمْ ثُمَّ يُمِيتُكُمْ ثُمَّ يُحْيِيكُمْ ۗ إِنَّ الْإِنْسَانَ لَكَفُورٌ ﴿٧٢﴾

**63. Je! Huoni kwamba Allah Huteremsha maji kutoka mbinguni,**

*na mara ardhi inakuwa chanikiwiti? Hakika Allah ni Mpole na Mwenye Kujua.*

**64. Ni Vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi. Na hakika Allah ni Mwenye Kujitoshia na Mwenye Kusifiwa.**

**65. Je! Huoni kwamba Allah Amevidhalilisha kwenu viliomo katika ardhi, na marikebu zipitazo baharini kwa Amri Yake, na Amezishika mbingu zisianguke juu ya ardhi ila kwa Idhini Yake. Hakika Allah ni Mwenye Huruma kwa watu, Mwenye Kurehemu.**

**66. Na Yeye Ndiye Aliyekuhuisheni kisha Akakufisheni, na kisha Atakufufueni. Hakika mwanadamu hana fadhila.**

#### Ishara na Uweza wa Allah تعالى

Hii ni Ishara nyingine ya Uweza na Nguvu Zake (Allah تعالى) kuwa Anatuma upepo kusukuma mawingu ambayo yanaleta mvua katika ardhi tasa, isiyomea chochote, ardhi kavu, yenye vumbi na iliyopasuka.

فَإِذَا أَنْزَلْنَا عَلَيْهَا الْمَاءَ اهْتَزَّتْ وَرَبَّتْ

**“Lakini Tunapoyateremsha maji juu yake husisimka na kututumka.”  
(22:5)**

Na Kauli Yake:

فَتُصْبِحُ الْأَرْضُ مُخْضَرَّةً

**“Na mara ardhi inakuwa kijani kibichi?”**

Hii inaashiria mnyororo wa matukio na jinsi gani kila kitu kinaenda kulingana na maumbile. Hii ni kama Aya nyingine:

ثُمَّ خَلَقْنَا النُّطْفَةَ عَلَقَةً فَخَلَقْنَا الْعَلَقَةَ مُضْغَةً

**“Kisha Tukalifanya tone hilo kuwa pande la damu, na Tulikalifanya pande la damu hilo kuwa pande la nyama.”<sup>1</sup> (23:14)**

<sup>1</sup> Surat Al-Hajj (22:).

Na hakika imethibiti katika Sahihi mbili kuwa baina ya kila hatua moja kwenda nyingine ni siku arobaini.<sup>1</sup> Na pamoja na hivyo imefuatiliwa na kiunganishi (Faa) ambacho katika sarufi ya kiarabu hujulisha utendaji wa jambo hapo hapo na mpangilio. Na hivyo hapa Amesema:

فَتُصْبِحُ الْأَرْضُ مُخْضَرَةً<sup>١</sup>

**“Na mara ardhi inakuwa chanikiwiti?”**

Maana yake: kijani kibichi baada ya kuwa kavu bila uhai. Na hakika wametaja baadhi ya watu wa Hijaaz kuwa ardhi hubadilika kijani baada ya kunyesha mvua. Allah Anajua zaidi. Na Kauli Yake:

إِنَّ اللَّهَ لَطِيفٌ خَبِيرٌ ﴿٣١﴾

**“Hakika Allah ni Mpole na Mwenye kujua.”**

Maana yake: ni Mjuzi kwa mbegu zote zilizomo katika maeneo yote ya ardhi, hata zikiwa ni ndogo namna gani. Hakuna kilichofichikana na Elimu Yake. Kila mbegu inapata sehemu yake ya maji na huanza kumea, kama alivyosema Luqmaan:

يَبْنِيٰ إِيَّهَا إِنْ تَكُ مِثْقَالَ حَبِّ مِّنْ حَرْدَلٍ فَتَكُنْ فِي صَخْرَةٍ أَوْ فِي السَّمٰوٰتِ أَوْ فِي الْأَرْضِ

يَأْتِ بِهَا اللَّهُ إِنَّ اللَّهَ لَطِيفٌ خَبِيرٌ ﴿٣١﴾

**“Ewe mwanangu! Kwa hakika jambo lolote japokuwa lina uzito wa chembe ya hardali, likawa ndani ya jabali au mbinguni au katika ardhi, Allah Atalileta; bila shaka Allah ni Mjuzi wa mambo yaliyofichikana, na Mjuzi wa mambo yaliyodhahiri.” (31:16).**

Na Akasema:

أَلَّا يَسْجُدُوا لِلَّهِ الَّذِي يُخْرِجُ الْخَبْءَ فِي السَّمٰوٰتِ وَالْأَرْضِ

**“(Shetani amezainishia) wasimsujudie Allah Ambaye Huyatoa yaliyofichikana katika mbingu na ardhi.” (27:25).**

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baari 6:350 na Muslim 4:2036.

Na Amesema Aliyetukuka:

وَمَا تَسْقُطُ مِنْ وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٍ فِي ظُلْمَتِ الْأَرْضِ وَلَا رَطْبٍ وَلَا يَابِسٍ إِلَّا فِي

كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٥٨﴾

**“Na halianguki jani ila Analijua. Wala haianguki punje katika giza la ardhi ila Anaijua. Wala hakianguki kilichorutubika wala kilichoyabisika ila Anakijua. Hapana chochote ila kimo katika Kitabu kidhihirishacho kila jambo.” (6:59).**

Na Amesema:

وَمَا يَعْزُبُ عَنْ رَبِّكَ مِنْ مِثْقَالِ ذَرَّةٍ فِي الْأَرْضِ وَلَا فِي السَّمَاءِ وَلَا أَصْغَرَ مِنْ ذَلِكَ وَلَا

أَكْبَرَ إِلَّا فِي كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٥٩﴾

**“Hakifichikani kwa Mola wako Mlezi kitu chochote hata kilicho sawa na uzito wa atomu, la katika ardhi wala katika mbingu. Wala hapana kidogo kuliko hicho wala kikubwa, isipokuwa kimo katika Kitabu kielezacho kila kitu.” (10:61) Na Kauli Yake Allah تعالى،**

لَهُ مَا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ<sup>٤</sup>

**“Ni Vyake vilivyomo mbinguni na vilivyomo katika ardhi.”**

Maana yake: vitu vyote ni miliki Yake, naye ni Mkwasi (tajiri), hivyo Hahitajii chochote bali kila kitu kinamuhitajia na kipo katika hali ya kumnyenyekea Yeye. Na Kauli Yake:

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ سَخَّرَ لَكُمْ مَّا فِي الْأَرْضِ

**“Je! Huoni kwamba Allah Amevidhalilisha kwenu vilivyomo katika ardhi.”**

Maana yake: miongoni mwa wanyama, vitu visivyo na roho, mimea na matunda. Hii ni kama Aya:

وَسَخَّرَ لَكُمْ مَّا فِي السَّمَوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ جَمِيعًا مَتَّعٌ

**“Na Amekutiishieni vilivyomo mbinguni na ardhini vyote vimetoka Kwake...” (45:13)**

Maana yake: hiyo ni kwa ihsani Yake, Fadhila Zake, Neema kutoka Kwake na Huruma Yake kwenu.

وَالْفُلْكَ تَجْرِي فِي الْبَحْرِ بِأَمْرِهِ

**“Na marikebu zipitazo baharini kwa Amri Yake.”**

Maana yake: kwa Kuvitiisha na Kuvisahilisha katika bahari yenye mawimbi makali, marikebu hutembea kwa upole na abiria wake. Huwapeleka hao popote waendapo kwa ajili ya biashara na kwa malengo mengine kutoka ardhi moja hadi nyingine, ili kuleta bidhaa kutoka sehemu moja hadi nyingine na kinyume chake, kwa vyovyote watakavyo au wanavyohitajia.

وَيُمْسِكُ السَّمَاءَ أَنْ تَقَعَ عَلَى الْأَرْضِ إِلَّا بِإِذْنِهِ

**“Na Amezishika mbingu zisianguke juu ya ardhi ila kwa Idhini Yake.”**

Maana yake: lau Angelitaka Angetoa idhini kwa mbingu ili zianguke juu ya ardhi, hivyo kuangamiza waliomo ndani yake, lakini kwa Rehema na Huruma Yake pamoja na Nguvu na Uwezo Wake, Anaizuia (mbingu) isianguke juu ya ardhi, ila kwa Idhini Yake. Kwa hiyo Akasema:

إِنَّ اللَّهَ بِالنَّاسِ لَرءُوفٌ رءِيمٌ ﴿٦١﴾

**“Hakika Allah ni Mwenye Huruma kwa watu, Mwenye Kurehemu.”**

Maana yake: pamoja na dhuluma zao, kama Alivyosema katika Aya nyingine:

وَإِنَّ رَبَّكَ لَذُو مَغْفِرَةٍ لِّلنَّاسِ عَلَى ظُلْمِهِمْ وَإِنَّ رَبَّكَ لَشَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٦٢﴾

**“Na hakika Mola wako Mlezi ni Mwenye Msamaha kwa watu juu ya dhuluma yao, na hakika Mola wako Mlezi ni Mkali wa Kuadhibu.” (13:6).**

Na Kauli Yake Allah تعالى،

وَهُوَ الَّذِي أَحْيَاكُمْ ثُمَّ يُمِيتُكُمْ ثُمَّ يُحْيِيكُمْ إِنَّ الْإِنسَانَ لَكَفُورٌ ﴿٦٣﴾

**“Na Yeye Ndiye Aliyekuhuisheni kisha Akakufisheni, na kisha Atakufufueni. Hakika mwanadamu hana fadhila”.**



Hii ni kama Kauli Yake:

كَيْفَ تَكْفُرُونَ بِاللَّهِ وَكُنْتُمْ أَمْوَاتًا فَأَحْيَاكُمْ ثُمَّ يُمَيِّتُكُمْ ثُمَّ يُحْيِيكُمْ ثُمَّ إِلَيْهِ تُرْجَعُونَ ﴿٢٨﴾

**“Vipi munamkanusha Allah, na hali mulikuwa wafu, Akakuhuisheni; kisha Atakufisheni; kisha Kwake mutarejeshwa.” (2:28).**

قُلِ اللَّهُ يُحْيِيكُمْ ثُمَّ يُمَيِّتُكُمْ ثُمَّ يَجْمَعُكُمْ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَا رَيْبَ فِيهِ

**“Sema: Allah Anakupeni uhai, kisha Anakufisheni, kisha Atakukusanyeni siku ya Kiyama – siku ambayo haina shaka.” (45:26) Na,**

قَالُوا رَبَّنَا آمَنَّا أَلْتَنَّبَنِي وَأَحْيَيْنَا أَلْتُنَّبَنِي

**“Watasema: Mole wetu Mlezi! Umetufisha mara mbili na Umetuhuisha mara mbili.” (40:11).**

Na maana ya maneno ni kuwa vipi munamjaalia Allah تعالى kuwa na miungu wapinzani na munaabudu asiekuwa Yeye, ilhali Yeye Yu Peke Yake katika Uumbaji, Kutoa riziki na Kusimamia mambo?

وَهُوَ الَّذِي أَحْيَاكُمْ

**“Na Yeye Ndiye Aliyekuhuisheni.”**

Maana yake: Amewaumbeni baada ya kuwa hamukuwa chochote kinachotajwa au kukumbukwa, Akakuleteni.

ثُمَّ يُمَيِّتُكُمْ ثُمَّ يُحْيِيكُمْ

**“Kisha Akakufisheni, na kisha Atakufufueni.”**

Maana yake: Siku ya Kiyama.

إِنَّ الْإِنْسَانَ لَكَفُورٌ ﴿٢٩﴾

**“Hakika mwanadamu hana Fadhila.”** Maana yake: Mwenye kukanusha.

لِكُلِّ أُمَّةٍ جَعَلْنَا مَنْسَكًا هُمْ نَاسِكُوهُ ۖ فَلَا يُنْزِعُ عَنْكَ فِي الْأَمْرِ ۖ وَأَدْعُ إِلَىٰ رَبِّكَ ۖ إِنَّكَ لَعَلىٰ  
هُدًى مُّسْتَقِيمٍ ﴿٦٧﴾ وَإِنْ جِدَدُوكَ فَقُلِ ۖ اللَّهُ أَعْلَمُ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿٦٨﴾ اللَّهُ يَحْكُمُ  
بَيْنَكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ ۖ فِيمَا كُنْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿٦٩﴾

**67. Kila umma Tumeujaalia ibada unazozishika. Basi wasizozane nawe katika jambo hili. Na waite watu kuendea kwa Mola wako Mlezi. Hakika wewe uko kwenye Uongofu Ulionyooka.**

**68. Na wakikujadili basi sema: Allah Anajua zaidi mnayoyatenda.**

**69. Allah Atahukumu baina yenu Siku ya Kiyama katika hayo munayokhitalifiana.**

### Kila Watu Wana Matukufu Yao ya Dini

Allah تعالیٰ Anatuambia kuwa amejaalia matukufu ya ibada “Mansak” kwa kila taifa. Ibn Jariir رحمه الله تعالیٰ amesema: “Hii inamaanisha kuwa kuna matukufu ya ibada “Mansak” kwa kila taifa la Nabii”. Amesema: “Asili ya neno “Mansak” katika lugha ya Kiarabu lina maana ya sehemu ambayo mtu anarudi kila mara kwa malengo ya kheri au shari. Hivyo, “Manaasik” Matukufu ya Hajj yanaitwa hivyo kwa kuwa watu wanayaendea mara kwa mara na kukaa huko.”<sup>1</sup> Ikiwa ibara, “Kwa kila taifa Tumewajaalia na matukufu ya kidini” ina maana kuwa kila kaumu ya Nabii ilikuwa na matukufu ya kidini kama ilivyopangwa na Allah تعالیٰ. Kwa hiyo, ibara: “Hivyo waache wao (wapagani) wasizozane nawe kuhusu suala hilo”, yaani washirikina. Ikiwa ibara, “Kwa kila taifa Tumewajaalia matukufu yao ya kidini”, ina maana kuwa ni jambo la Qadar, kama ilivyo katika Aya:

وَلِكُلِّ وِجْهَةٍ هُوَ مُوَلِّئُهَا

**“Na kila mmoja anao upande anaoelekea.” (2:148).**

Kwa hivyo Akasema hapa:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:678, 679.

هُم تَاسِكُوهُ

“**Wanazozishika**”. Maana yake: wanazofanya. Kiwakilishi hapa kinarudi kwa hawa wenye sherehe za kidini na njia, yaani wanafanya haya kwa *Qadar* na matakwa ya Allah تعالى. Kwa hivyo, usibabaikie juu ya hilo ukaacha kufuata haki. Na kwa hiyo Akasema:

وَأَدْعُ إِلَىٰ رَبِّكَ إِنَّكَ لَعَلَىٰ هُدًى مُّسْتَقِيمٍ ﴿٣٨﴾

**“Na waite watu kwa Mola wako Mlezi. Hakika wewe uko kwenye Uongofu Ulionyooka.”**

Maana yake: njia ya wazi iliyo nyoofu ambayo itakuongoza katika lengo lililokusudiwa. Hii ni kama Aya:

وَلَا يَصُدُّنَاكَ عَنْ آيَاتِ اللَّهِ بَعْدَ إِذْ أَنْزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ وَأَدْعُ إِلَىٰ رَبِّكَ

**“Wala wasikuzuie kuzifuata Aya za Allah baada ya kuteremshiwa wewe. Na lingania kwa Mola wako Mlezi.” (28:87).**

Na Kauli Yake:

وَإِنْ جَدَلْتَهُمْ فَقُلْ أَفَلَا أَعْلَمُ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿٣٩﴾

**“Na wakikujadili basi sema: Allah Anajua zaidi munayoyatenda”.**

Hii ni kama Kauli Yake:

وَإِنْ كَذَّبُوكَ فَقُلْ لِي عَمَلِي وَلَكُمْ عَمَلُكُمْ أَنتُمْ بَرِيئُونَ مِمَّا أَعْمَلُ وَأَنَا بَرِيءٌ مِّمَّا

تَعْمَلُونَ ﴿٤٠﴾

**“Na wakikukanusha wewe, sema: Mimi nina amali yangu, na nyinyi muna amali yenu. Nyinyi hamna jukumu kwa niyatendayo, wala mimi sina jukumu kwa muyatendayo.”(10:41).** Na Kauli Yake,

أَفَلَا أَعْلَمُ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿٤١﴾

**“Allah Anajua zaidi munayoyatenda”.**

Hili ni onyo kali na kitisho cha uhakika, kama katika Kauli Yake:

هُوَ أَعْلَمُ بِمَا تُفِيضُونَ فِيهِ كَفَىٰ بِهِ شَهِيدًا بَيْنِي وَبَيْنَكُمْ

**“Yeye Anajua zaidi hayo munayoropokwa; Anatosha kuwa shahidi baina yangu na nyinyi.” (46:8).**

Kwa hiyo Akasema:

اللَّهُ يَحْكُمُ بَيْنَكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ فِيمَا كُنْتُمْ فِيهِ تَخْتَلِفُونَ ﴿٥٨﴾

**“Allah Atahukumu baina yenu Siku ya Kiyama katika hayo mnayo khitalifiana”.**

Na hii pia ni kama Kauli Yake Aliyetukuka:

فَلِذَلِكَ فَادْعُ ۖ وَاسْتَقِمْ ۖ كَمَا أُمِرْتَ ۖ وَلَا تَتَّبِعْ أَهْوَاءَهُمْ ۖ وَقُلْ ءَامَنْتُ بِمَا أَنْزَلَ اللَّهُ  
مِن كِتَابِهِ

**“Basi kwa haya waite! Nawe simama sawa sawa kama ulivyo amrishwa, wala usiyafuate matamanio yao. Na sema: Naamini Aliyoteremsha Allah katika Vitabu.” (42:15).**

\* \* \*

أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۗ إِنَّ  
 ذَلِكَ فِي كِتَابٍ ۚ إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٧٠﴾ وَيَعْبُدُونَ  
 مِنْ دُونِ اللَّهِ مَا لَمْ يَنْزِلْ بِهِ سُلْطَانًا وَمَا لَيْسَ لَهُمْ بِهِ  
 عِلْمٌ ۖ وَمَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ نَصِيرٍ ﴿٧١﴾ وَإِذَا تَنَادَىٰ عَلَيْهِمْ ءَايَاتُنَا  
 بَيِّنَاتٍ نَعْرِفُ فِي وُجُوهِ الَّذِينَ كَفَرُوا الَّتِي كَفَرُوا ۗ أَلَمْ نَكْرَهُ  
 بِكَادُورٍ يَسْطُورٍ ۖ بِالَّذِينَ يَتْلُونَ عَلَيْهِمْ ءَايَاتِنَا  
 قُلْ أَفَأَنْتُمْ بِشِرِّ مِنَ الذِّكْرِ ۗ أَلَا نَارُ وَعْدَهَا اللَّهُ الَّذِينَ  
 كَفَرُوا ۗ وَيَسَّ الَمَصِيرُ ﴿٧٢﴾ يَتَأْتِيهَا النَّاسُ ضُرْبَ مَثَلٍ  
 فَاسْتَمِعُوا لَهُ ۗ إِنَّ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ لَنْ  
 يَخْلُقُوا ذُبَابًا وَلَوْ اجْتَمَعُوا لَهُ ۗ وَإِنْ يَسْلُبْهُمُ الذُّبَابُ شَيْعًا  
 لَا يَسْتَنْقِذُوهُ مِنْهُ ۗ ضَعُفَ الطَّالِبُ وَالْمَطْلُوبُ ﴿٧٣﴾ مَا  
 قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٧٤﴾ اللَّهُ  
 يَضْطَلِّي مِنَ الْمَلَائِكَةِ رُسُلًا وَمِنَ النَّاسِ ۗ إِنَّ  
 اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ ﴿٧٥﴾ يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا  
 خَلْفَهُمْ ۗ وَإِلَى اللَّهِ تُرْجَعُ الْأُمُورُ ﴿٧٦﴾ يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ  
 ءَامَنُوا أَرْكَعُوا وَاسْجُدُوا وَاعْبُدُوا رَبَّكُمْ وَأَفْعَلُوا الْخَيْرَ  
 لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ﴿٧٧﴾ وَجَاهِدُوا فِي اللَّهِ حَقَّ  
 جِهَادِهِ ۗ هُوَ اجْتَبَاكُمْ وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ  
 حَرَجٍ ۗ مِلَّةَ أَبِيكُمْ إِبْرَاهِيمَ ۗ هُوَ سَمَّاكُمُ الْمُسْلِمِينَ مِنْ قَبْلُ  
 وَفِي هَذَا لِيَكُونَ الرَّسُولُ شَهِيدًا عَلَيْكُمْ وَتَكُونُوا شُهَدَاءَ  
 عَلَى النَّاسِ ۗ فَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ وَاعْتَصِمُوا  
 بِاللَّهِ هُوَ مَوْلَاكُمْ ۗ فَبِعَمِّ الْمَوْلَىٰ وَنِعَمِ النَّصِيرِ ﴿٧٨﴾

أَلَمْ تَعْلَمْ أَنَّ اللَّهَ يَعْلَمُ مَا فِي  
 السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ ۗ إِنَّ ذَلِكَ فِي  
 كِتَابٍ ۚ إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٧٠﴾

**70. Je! Hujui kwamba Allah  
 Anayajua yaliyomo mbi-  
 nguni na katika ardhi?  
 Hakika hayo yamo Kitabuni.  
 Hakika hayo kwa Allah ni  
 mepesi.**

Allah تعالى Anatueleza ukamilifu wa Elimu Yake kwa viumbe Vyake, na kuwa Yeye Amevizunguka vyote vili-vyomo mbinguni na kwenye ardhi. Hivyo, hakipiti katika Elimu Yake wizani wa atomu, au ndogo zaidi au kubwa mbinguni na ardhini. Anajua kila kitu hata kabla ya kutokea na Ameandika hayo katika Kitabu Chake, "Al-Lawhul Mahfuudh", kama ilivyori potitiwa katika Sahihi Muslim kutoka kwa 'Abdallaah bin 'Amr رضي الله عنه Mtume amesema:

«إِنَّ اللَّهَ قَدَّرَ مَقَادِيرَ الْخَلَائِقِ قَبْلَ  
 خَلْقِ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ بِخَمْسِينَ  
 أَلْفَ سَنَةٍ، وَكَانَ عَرْشُهُ عَلَى الْمَاءِ»

*"Hakika Allah Amekadiria vipimo vya viumbe miaka elfu hamsini kabla Hajaumba mbingu na ardhi, na Kiti Chake cha Enzi kilikuwa juu ya maji"<sup>1</sup>.*

Na katika Sunan kutoka kwa kikundi cha Maswahaba kuwa Mtume ﷺ amesema:

«أَوَّلُ مَا خَلَقَ اللَّهُ الْقَلَمَ، قَالَ لَهُ: اكْتُبْ، قَالَ: وَ مَا أَكْتُبُ؟ قَالَ: اكْتُبْ مَا هُوَ كَائِنٌ، فَجَرَى الْقَلَمُ بِمَا هُوَ كَائِنٌ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ»

*"Kitu cha kwanza kilichoumbwa na Allah ni kalamu. Akaiambia (hiyo kalamu): 'Andika'. Nayo ikasema: 'Na niandike nini?' Akasema: 'Andika yatakayotokea', hivyo kalamu ikaanza kuandika yatakayo tokea mpaka Siku ya Kiyama"<sup>2</sup>.*

Na kwa hiyo Akasema Aliyetukuka:

إِنَّ ذَلِكَ فِي كِتَابٍ ۚ إِنَّ ذَلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرٌ ﴿٧١﴾

***"Hakika hayo yamo Kitabuni. Hakika hayo kwa Allah ni mepesi."***

وَيَعْبُدُونَ مِن دُونِ اللَّهِ مَا لَمْ يُنَزَّلْ بِهِ سُلْطَانًا وَمَا لَيْسَ لَهُم بِهِ عِلْمٌ ۖ وَمَا لِلظَّالِمِينَ  
مِن نَّصِيرٍ ﴿٧٢﴾ وَإِذَا تَتَلَوْا عَلَيْهِمْ ءَايَاتُنَا بَيِّنَاتٍ تَعْرِفُ فِي وُجُوهِ الَّذِينَ كَفَرُوا  
الْمُنْكَرَ ۚ يَكَادُونَ يَسْطُونَ بِالَّذِينَ يَتْلُونَ عَلَيْهِمْ ءَايَاتِنَا ۚ قُلْ أَفَأَنْتُمْ بِشِرِّ  
مِن ذَالِكُمْ أَتَّارٌ وَعَدَّهَا اللَّهُ الَّذِينَ كَفَرُوا وَيُبْسِ أَلْمَصِيرُ ﴿٧٣﴾

***71. Na wanaabudu badala ya Allah ambavyo hakuviteremshia ushahidi, na ambavyo hawana ujuzi navyo. Na madhalimu hawatakuwa na wa kuwasaidia.***

***72. Na wanaposomewa Aya Zetu zilizo wazi utaona chuki katika nyuso za waliokufuru. Hukaribia kuwavamia wale wanaowasomea hizo Aya Zetu. Sema: Je! Nikuambieni yaliyo mabaya zaidi kuliko haya? Ni Moto. Allah Amewaahidi waliokufuru, na ni marudio mabaya hayo.***

<sup>1</sup> Muslim 4:2044.

<sup>2</sup> Abu Daawud 5:76 na Tuhfah Al-Ahwadhiy 9:232.

**Washirikina Kuabudu Asiyekuwa Allah تعالی na Kuchukia Kwao Ishara Zake**

Anasema Aliyetukuka kwa njia ya Kutupasha habari kuhusu washirikina kwa ujinga walio nao, wakakufuru na kuabudu asiyekuwa Allah تعالی kwa ambacho Hakuteremsha ushahidi wowote, yaani hoja na dalili. Hii ni kama Kauli Yake Aliyetukuka:

وَمَنْ يَدْعُ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ لَا بُرْهَانَ لَهُ بِهِ فَإِنَّمَا حِسَابُهُ عِنْدَ رَبِّهِ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ

الْكَافِرُونَ ﴿١١٧﴾

***“Na anayemuomba - pamoja na Allah - mungu mwengine hana ushahidi wa hili; basi bila ya shaka hesabu yake iko kwa Mola wake Mlezi. Kwa hakika makafiri hawafanikiwi.” (23:117).***

Na hapa Akasema:

مَا لَمْ يُتَزَلْ بِهِ سُلْطَانًا وَمَا لَيْسَ لَهُمْ بِهِ عِلْمٌ

***“Ambavyo hakuviteremshia ushahidi, na ambavyo hawana ujuzi navyo”,***

Maana yake: wasiokuwa na elimu katika suala hilo kwa walilozua; ni katika mambo waliyoyapata kutoka kwa baba zao na waliotangulia, bila dalili wala hoja, na asili yake inatokana na Shetani aliyewatengenezea na kuwapambia. Kwa ajili hiyo, Amewaonya wao Aliyetukuka kwa Kauli Yake:

وَمَا لِلظَّالِمِينَ مِنْ نَصِيرٍ ﴿١١٨﴾

***“Na madhalimu hawatakuwa na wa kuwasaidia.”***

Maana yake: hakuna atakayewasaidia kutokana na Allah تعالی Atakapotuma adhabu Yake kwao. Kisha Akasema:

وَإِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ آيَاتُنَا بَيِّنَاتٍ

***“Na wanaposomewa Aya Zetu zilizo wazi”.***

Maana yake: wanapotajiwa Aya za Qur’ani, hoja na dalili zilizo wazi kwa kuwepo Allah تعالی Mmoja Peke Yake na kuwa hapana apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah تعالی na kuwa Mitume wote walisema haki na kweli,

يَكَادُونَ يَسْطُونَ بِالَّذِينَ يَتْلُونَ عَلَيْهِمْ آيَاتِنَا

**“Hukaribia kuwavamia wale wanaowasomea hizo Aya Zetu”.** Maana yake: hukaribia kuwavamia na kuwadhuru wale wanaowaletea dalili sahihi kutoka katika Qur’ani, na wanawadhuru kupitia mikono yao na ndimi zao.

قُلْ

**“Sema”.** Maana yake: ewe Muhammad kwa hawa watu,

أَفَأُنَبِّئُكُمْ بِشَرِّ مِّنْ ذَلِكَمُ النَّارُ وَعَذَابُ اللَّهِ الَّذِينَ كَفَرُوا

**“Je! Nikuambieni yaliyo mabaya zaidi kuliko haya? Ni Moto. Allah Amewaahidi waliokufuru.”**

Maana yake: Moto, adhabu na ghadhabu ya Allah تعالى ni mbaya zaidi kuliko yale mnayojaribu kuwatishia Waumini, marafiki wa karibu na Allah تعالى hapa duniani. Na adhabu ya Akhera kwa haya munayofanya ni mbaya zaidi kuliko hayo munayodai mnataka kuwafanyia Waumini. Na Kauli Yake:

وَبئْسَ الْمَصِيرُ ﴿٧٠﴾

**“Na ni marudio mabaya hayo.”** Maana yake: ni Moto mbaya kama mashukio ya mwisho, nyumba, marudio na makao!

إِنَّهَا سَاءَتْ مُسْتَقَرًّا وَمُقَامًا ﴿٧١﴾

**“Hakika hiyo ni kituo na makao mabaya.” (25:66).**

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ ضُرْبَ مَثَلٍ فَاستَمِعُوا لَهُ إِنَّ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ لَنْ

يَخْلُقُوا ذُبَابًا وَلَوْ اجْتَمَعُوا لَهُ وَإِنْ يَسْلُبْهُمُ الذُّبَابُ شَيْعًا لَا يَسْتَنْقِذُوهُ مِنْهُ ضَعُفَ

الطَّالِبِ وَالْمَطْلُوبِ ﴿٧٢﴾ مَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ ﴿٧٣﴾

**73. Enyi watu! Unapigwa mfano, basi usikilizeni. Hakika wale mnaowaomba badala ya Allah, hawatoumba hata nzi ijapokuwa watajumuika kwa hilo. Na nzi akiwapokonya kitu hawawezi kukipata kwake. Amedhoofika kweli huyo mwenye kutaka na mwenye kutakiwa.**

**74. Hawakumuadhimisha Allah Anavyostahiki Kuadhimishwa. Hakika Allah bila ya shaka ni Mwenye Nguvu, Mwenye Kushinda.**



**Kutokuwa na Thamani kwa Masanamu na Ujinga wa Wenye Kuyaabudu**

Anasema Aliyetukuka kwa Kututanabahisha kuhusu udogo wa masanamu na ujinga wa wenye kuyaabudu.

يَتَأْتِيهَا النَّاسُ ضُرْبَ مَثَلٍ

**“Enyi watu! Unapigwa mfano”**. Maana yake: mfano kwa kinachoabudiwa na wale wasiomjua Allah تعالى na wenye kumshirikisha.

فَأَسْتَمِعُوا لَهُ

**“Basi usikilizeni”**, Maana yake: usilikizeni na ufahamuni.

إِنَّ الَّذِينَ تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ لَنْ يَخْلُقُوا ذُبَابًا وَلَوْ اجْتَمَعُوا لَهُ

**“Hakika wale munaowaomba badala ya Allah, hawatumba hata nzi ijapokuwa watajumuika kwa hilo.”**

Maana yake: lau watakusanyika wote mnaowaabudu – masanamu na miungu ili wajaribu kumuumba nzi mmoja, hawataweza kufanya hilo.

Kama ambavyo amenukuu Imamu Ahmad kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kwa njia ya *“Marfu.”*

«وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ خَلَقَ [خَلْقًا] كَخَلْقِي، فَلْيَخْلُقُوا مِثْلَ خَلْقِي ذَرَّةً أَوْ ذُبَابَةً أَوْ حَبَّةً»

*“Hakuna dhalimu zaidi kuliko yule aliyejaribu kutaka kuumba kitu kama Uumbaji Wangu! Kama ubavu huo wanao, basi wajaribu kuumba, mdudu, nzi au mbegu ya nafaka.”<sup>1</sup>*

Kadhalika sahihi mbili wameelezea Hadithi hii, kupitia njia ya Umrah kutoka kwa Zur’ah, kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه, kutoka kwa Mtume ﷺ amesema:

«قَالَ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ وَمَنْ أَظْلَمُ مِمَّنْ ذَهَبَ يَخْلُقُ كَخَلْقِي، فَلْيَخْلُقُوا ذَرَّةً، فَلْيَخْلُقُوا  
شُعْبَةً»

**“Allah Aliyetukuka na Kushinda Amesema: Hakuna dhalimu zaidi**

<sup>1</sup> Ahmad 2:391.

*kuliko yule aliyejaribu kuumba kama Uumbaji Wangu! kama ubavu huo unao wajaribu kuumba mdudu au mbegu ya shayiri.”<sup>1</sup>*

Kisha Akasema tena Aliyetukuka:

وَإِنْ يَسْأَلْهُمْ الذُّبَابُ شَيْئًا لَّا يَسْتَنْفِذُوهُ مِنْهُ

**“Na nzi akiwapokonya kitu hawawezi kukipata kwake”.**

Maana; wao wameshindwa kuumba nzi mmoja, bali zaidi ya hilo ni kushindwa kwao anapochukua kitu kutoka kwao miongoni mwa kumzuilia vitu vizuri. Ikiwa wanataka kukipata, hawawezi kabisa, japokuwa nzi ni kiumbe dhaifu na kidogo zaidi miongoni mwa viumbe vya Allah تعالى. Kwa hiyo Akasema:

ضَعْفَ الطَّالِبِ وَالْمَطْلُوبِ

**“Amedhoofika kweli huyo mwenye kutaka na mwenye kutakiwa”.**

Amesema Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما: “Mwenye kutaka” ni sanamu, “Mwenye kutakiwa” ni nzi”<sup>2</sup>. Huu ni muono uliochaguliwa na Ibn Jariir رحمه الله تعالى, na ndiyo uliyo wazi kutokana na muktadha wa Aya. Na amesema As-Suddiy na wengineo: “Mwenye kutaka’ ni mwenye kuabudu, “Mwenye kutakiwa” ni sanamu”<sup>3</sup>. Kisha Akasema:

مَا قَدَرُوا اللَّهَ حَقَّ قَدْرِهِ

**“Hawakumuadhimisha Allah Anavyostahiki kuadhimishwa”.**

Maana yake: Hawajatambua Uweza na Nguvu za Allah تعالى pale wanapoabudu pamoja Naye wengineo ambao hawawezi hata kumuondoa nzi, kwa udhaifu wao na kutoweza kwao.

إِنَّ اللَّهَ لَقَوِيٌّ عَزِيزٌ

**“Hakika Allah bila ya shaka ni Mwenye Nguvu, Mwenye Kushinda.”**

Maana yake: Yeye Ndiye Mwenye Nguvu Ambaye kwamba kwa Uweza Wake na Nguvu Zake Ameumba kila kitu.

<sup>1</sup> Fat’h Al-Baariy 13:537 na Muslim 3:1671.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:685.

<sup>3</sup> Al-Baghawiy 3:298 kutoka kwa Adh-Dhahaak.

وَهُوَ الَّذِي يَبْدَأُ الْخَلْقَ ثُمَّ يُعِيدُهُ وَهُوَ أَهْوَنُ عَلَيْهِ ۗ

**“Na Yeye Ndiye Anayeanzisha Uumbaji, kisha Ataurudisha mara nyengine. Na jambo hili ni jepesi zaidi Kwake.” (30:27).**

إِنَّ بَطْشَ رَبِّكَ لَشَدِيدٌ ﴿٢٧﴾ إِنَّهُ هُوَ يُبْدِئُ وَيُعِيدُ ﴿٢٨﴾

**“Hakika Kutesa kwa Mola wako Mlezi ni kukali. Yeye Ndiye Anayeanzisha na Ndiye Anayerejesha tena.” (85:12-13).**

إِنَّ اللَّهَ هُوَ الرَّزَّاقُ ذُو الْقُوَّةِ الْمَتِينُ ﴿٥٨﴾

**“Hakika Allah Ndiye Mwenye Kuruzuku, Mwenye Nguvu, Madhubuti.” (51:58).**

Na Kauli Yake:

عَزِيزٌ ﴿٥٩﴾

**“Mwenye Kushinda.”**

Maana yake: kwa hakika Amevitweza vitu vyote, na hakuna anayeweza kupingana Naye, na Nguvu Zake na Ushindi Wake wala Utukufu na Ufalme Wake Haushindwi, Naye ni Mmoja tu, Mtenda Nguvu.

اللَّهُ يَصْطَفِي مِنَ الْمَلَائِكَةِ رُسُلًا وَمِنَ النَّاسِ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ ﴿٦٠﴾ يَعْلَمُ

مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ ۗ وَإِلَى اللَّهِ تُرْجَعُ الْأُمُورُ ﴿٦١﴾

**75. Allah Huteua Wajumbe miongoni mwa Malaika na miongoni mwa watu. Hakika Allah ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kuona.**

**76. Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao. Na kwa Allah yatareshwa mambo yote.**

## Allah تعالیٰ Huteuwa Mitume Miongoni mwa Malaika na Binadamu

Anaeleza Aliyetukuka kuwa Yeye Huteuwa miongoni mwa Malaika Mitume kama Apendavyo kwa Sheria Yake na Uweza Wake na pia miongoni mwa Binadamu ili kufikisha risala na ujumbe Wake.

إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ بَصِيرٌ ﴿٧٠﴾

**“Hakika Allah ni Mwenye Kusikia, Mwenye Kuona.”**

Maana yake: Mwenye Kusikia kauli za waja Wake, Mwenye Kuwaona na Anajua nani miongoni mwao anastahiki hayo, kama Alivyosema:

اللَّهُ أَعْلَمُ حَيْثُ يَجْعَلُ رِسَالَتَهُ ۗ

**“Allah Ndiye Mjuzi kuliko wote Kujua wapi Anaweka ujumbe wake...” (6:124).**

Na Kauli Yake:

يَعْلَمُ مَا بَيْنَ أَيْدِيهِمْ وَمَا خَلْفَهُمْ ۗ وَإِلَى اللَّهِ تُرْجَعُ الْأُمُورُ ﴿٧١﴾

**“Anayajua yaliyo mbele yao na yaliyo nyuma yao. Na kwa Allah yatarejeshwa mambo yote.”**

Maana yake: Anajua yatakayotokea kwa Mitume Wake na ujumbe Alioupeleka kwao, kwani hakuna lolote lililofichikana Naye katika mambo yao.

Hii ni kama Alivyosema Allah تعالیٰ:

عَلِيمُ الْغَيْبِ فَلَا يُظْهِرُ عَلَىٰ غَيْبِهِ أَحَدًا ﴿٧٢﴾

**“Yeye Ndiye Mwenye Kujua ya siri, wala Hamdhihirishii yeyote Siri Yake.” (72:26)**

Mpaka kwenye Kauli Yake:

وَأَحْصَىٰ كُلَّ شَيْءٍ عَدَدًا ﴿٧٣﴾

**“Na Amedhibiti idadi ya kila kitu.” (72:28).**

Kwani Yeye, Allah تعالی, ni Mwenye Kuwalinda na Kuwatizama, ni Shahidi kwa yanayosemwa kuwahuu wao, ni Mwenye Kuwahifadhi na Mwenye Kuwanusuru na Kuwasaidia.

﴿ يَا أَيُّهَا الرُّسُولُ بَلِّغْ مَا أُنزِلَ إِلَيْكَ مِنْ رَبِّكَ ۗ وَإِنْ لَمْ تَفْعَلْ فَمَا بَلَّغْتَ رِسَالَتَهُ ۗ وَاللَّهُ يَعْصِمُكَ مِنَ النَّاسِ ۗ ﴾

*“Ewe Mtume! Fikisha uliyoteremshiwa kutoka kwa Mola wako Mlezi. Na ikiwa hukufanya hayo basi hukufikisha ujumbe Wake. Na Allah Atakulinda na watu.” (5:67).*

﴿ يَا أَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا أَرْكَعُوا وَاسْجُدُوا وَاعْبُدُوا رَبَّكُمْ وَأَفْعَلُوا الْخَيْرَ لَعَلَّكُمْ تُفْلِحُونَ ۝ ﴿٦٧﴾ وَجَاهِدُوا فِي اللَّهِ حَقَّ جِهَادِهِ ۗ هُوَ اجْتَبَاكُمْ وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ ۗ مِلَّةَ أَبِيكُمْ إِبْرَاهِيمَ ۗ هُوَ سَمَّاكُمُ الْمُسْلِمِينَ مِنْ قَبْلُ وَفِي هَذَا لِيَكُونَ الرَّسُولُ شَهِيدًا عَلَيْكُمْ وَتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ ۗ فَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ وَاعْتَصِمُوا بِاللَّهِ هُوَ مَوْلَاكُمْ فَنِعْمَ الْمَوْلَىٰ وَنِعْمَ النَّصِيرُ ۝ ﴾

*77. Enyi mlioamini! Rukuuni na msujudu, na muabuduni Mola wenu Mlezi, na tendeni mema, ili mufanikiwe.*

*78. Na fanyeni juhudi kwa ajili ya Allah kama inavyostahiki jihadi Yake. Yeye Amekuteueni. Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika Dini. Nayo ni mila ya baba yenu Ibrahimu. Yeye (Allah) Alikuiteni Waislamu tangu zamani, na katika hii (Qur’ani) pia, ili awe Mtume shahidi juu yenu, na nyinyi muwe mashahidi kwa watu. Basi shikeni Swala na toeni Zaka na shikamaneni na Allah. Yeye Ndiye Mlinzi wenu, Mlinzi bora kabisa, na Msaidizi bora kabisa.*

**Amri ya Kumuabudu Allah تعالى na Kupigana Jihadi**

Imepokewa kutoka kwa 'Uqbah bin 'Aamir رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«فُضِّلَتْ سُورَةُ الْحَجِّ بِسُجُودَيْنِ، فَمَنْ لَمْ يَسْجُدْهُمَا فَلَا يقرأَهُمَا»

*"Imefadhilishwa Suratul Hajj kwa kuwa na sijdah mbili, kwa yeyote asiyesujudu kwazo asizisome."<sup>1</sup>*

Na Kauli Yake:

وَجَاهِدُوا فِي اللَّهِ حَقَّ جِهَادِهِ<sup>٤</sup>

***"Na fanyeni juhudi kwa ajili ya Allah."***

Maana yake: kwa mali zenu, ndimi na nafsi zenu. Kama Alivyosema Aliyetukuka:

اتَّقُوا اللَّهَ حَقَّ تَقَاتِهِ

***"Mcheni Allah kama ipasavyo kumcha." (3:102).***

Na Kauli Yake:

هُوَ آجَبْتِكُمْ

***"Yeye Amekuteueni."*** Maana yake: Enyi Umma huu (wa Uislamu), Allah تعالى Amewateua na Kuwachagua juu ya Umma zote, na Amewafadhilisha na Kuwatukuza na Kuwakirimu kwa Mtume bora na Sheria iliyokamilika.

وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ

***"Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika Dini."***

Maana yake: Hakuwakalifisha kwa msiyoweza wala Hakuwalazimisha kwa jambo lolote zito ila Allah تعالى Aliwajaalia faraja na njia ya kutoka. Hivyo Swala, ambayo ni nguzo kubwa ya Uislamu baada ya Shahada mbili, ni wajibu raka nne kwa mkaazi, zinazo punguzwa kuwa mbili kwa msafiri. Na kulingana na baadhi ya Maimamu, raka moja tu ndio wajibu katika wakati wa hofu, kama ilivyonukuliwa katika Hadithi.<sup>2</sup> Mtu anaweza kuswali akiwa anatembea

<sup>1</sup> Al-Haakim 1:221. Nyongeza, "Kwa yeyote asiyesujudu kwayo asiisome", inajulikana kuwa si sahihi. Chimbuko la Hadithi limetajwa huko nyuma. Tazama Aya ya 18 katika Sura hii.

<sup>2</sup> Abu Daawud 2:38.

au amepanda kipando, akielekea Qiblah au kinyume chake (bila kuelekea Qiblah), na hivyo hivyo katika Swala za Sunna akiwa mtu yupo katika safari, anaweza kuelekea Qiblah au bila kuelekea. Na kusimama ndani yake kunaondoka kwa udhuru wa maradhi; mgonjwa anaweza kuswali kwa kuketi, asipoweza kwa kulala kwa ubavu. Na pia kuna njia nyinginezo zinazokubalika katika ruhusa aliyopewa na wepesi uliowekwa kwa faradhi zote (za Swala) na wajibu mwingine. Kwa ajili hiyo alisema ﷻ:

«بُعِثْتُ بِالْخَيْبَةِ السُّمْحِيَّةِ»

*“Nimetumwa na njia nyepesi ya unyenyekevu.”<sup>1</sup>*

Naye ﷻ aliwaambia Mu'aadh na Abi Musa al-Ash'ariy رضي الله عنهما alipowatuma kuwa maamiri wawili kuelekea Yemen:

«بَشْرًا وَلَا تُنْفِرُوا وَبَشْرًا وَلَا تُعْرَأُوا»

*“Toeni bishara njema wala msiwafukuze (watu). Na fanyeni mambo kuwa sahali na mepesi wala msiyafanye kuwa mazito na magumu.”<sup>2</sup>*

Na Hadithi kuhusu jambo hili ni nyingi sana. Na kwa ajili hiyo amesema Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما kuhusu Kauli Yake:

وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ

*“Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika Dini.”*

Maana yake: kutokana na dhiki. Na Kauli Yake:

مِلَّةً أَبِيكُمْ إِبْرَاهِيمَ

*“Nayo ni mila ya baba yenu Ibraahim.”*

Amesema Ibn Jariir رحمه الله تعالى: “Neno “Milla” hukadiriwa irabu ya fat'ha, katika sarufi ya kiarabu, kutokana na kutanguliwa na Aya:

<sup>1</sup> Ahmad 5:266.

<sup>2</sup> Fat'h Al-Baariy 7:657.

وَمَا جَعَلْ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ<sup>٤</sup>

**“Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika Dini.”**

Maana yake: kutokana na dhiki. Bali kinyume na hivyo Amewasahilishia kama mila ya baba yenu, Ibrahim عليه السلام. Amesema: “Huenda ikawa ina maana ya shikamaneni na mila ya baba yenu, Ibrahim عليه السلام.”<sup>1</sup> Kama itakadiriwa irabu ya *Fat’ha* katika neno lililofichwa, Yaani “shikamaneni” kwa mujibu wa sarufi na kanuni ya lugha ya kiarabu (Nikasema): Na maana ya hii ni kama kauli Yake:

قُلْ إِنِّي هَدَانِي رَبِّي إِلَى صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ دِينًا قِيَمًا مِثْلَ آبَائِهِمْ حَنِيفًا<sup>٥</sup>

**“Sema: Kwa hakika mimi Mola wangu Mlezi Ameniongoa kwenye Njia Iliyonyooka, Dini iliyo sawa kabisa, ambayo ndiyo mila ya Ibraahim aliye kuwa muongofu.” (6:161).**

Na kauli Yake:

هُوَ سَمَنُكُمْ الْمُسْلِمِينَ مِنْ قَبْلُ وَفِي هَذَا

**“Yeye (Allah) Alikuiteni Waislamu tangu zamani.”**

Na kuhusu hili, amesema Imaam ‘Abdallaah bin Al-Mubaarak kutoka kwa Ibn Jurayj kutoka kwa ‘Atwaa’ kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema yafuatayo kuhusu Kauli Yake:

هُوَ سَمَنُكُمْ الْمُسْلِمِينَ مِنْ قَبْلُ

**“Yeye (Allaah) Alikuiteni Waislamu tangu zamani.”**

Hii ina maana ya Allah تعالى<sup>1</sup>. Na hivyo ndivyo alivyosema Mujahid, ‘Atwaa’, Adh-Dhahaak, As-Suddiy, Muqaatil bin Hayyaan na Qatadah<sup>2</sup>.

Amesema Mujahid: “Allah تعالى Amewaita nyinyi Waislamu kabla, katika Vitabu vilivyotangulia na katika **Dhikr**.”

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 18:689.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 18:691.

<sup>3</sup> Atw-Twabariy 18:691, 692.



وَفِي هَذَا

**“Na katika hii pia.”**

Maana yake: Qur’ani<sup>1</sup>. Na hivyo ndivyo walivyosema wengineo, kwa kuwa Allah تعالى Amesema:

هُوَ أَجْتَبَلَكُمْ وَمَا جَعَلَ عَلَيْكُمْ فِي الدِّينِ مِنْ حَرَجٍ

**“Yeye Amekuteueni. Wala hakuweka juu yenu mambo mazito katika Dini.”**

Kisha Akawahimiza kufuata ujumbe ulioletwa na Mtume Wake ﷺ, kwa kuwakumbusha kuwa hii ni mila ya baba yao, Ibrahim عليه السلام. Kisha Akataja Fadhila Zake kwa Umma ambapo Aliwataja na Kuwatukuza tokea hapo zamani katika Vitabu vya Mitume walivyosomewa wanazuoni na wachamungu. Akasema:

هُوَ سَمَّنَكُمْ الْمُسْلِمِينَ مِنْ قَبْلُ

**“Yeye (Allah) Alikuiteni Waislamu tangu zamani.”**

Maana yake: kabla ya hii Qur’ani,

وَفِي هَذَا

**“Na katika hii pia.”**

Na hakika amesema An-Nasaa’iy katika kuifasiri Aya hii: Imepokewa na Al-Haarith Al-Ash’ariy رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«مَنْ دَعَا بِدَعْوَى الْجَاهِلِيَّةِ فَإِنَّهُ مِنْ جِئِي جَهَنَّمَ»

**“Yeyote mwenye kuita katika wito wa kijahili, hakika atakuwa mwenye kutambaa (kwa magoti) katika Moto wa Jahannamu.”**

Mtu mmoja akasema: “Ewe Mtume wa Allah! Na hata akifunga na kuswali?” Akasema:

<sup>1</sup> Al-Qurtwubiy 12: 101.

«نَعَمْ وَإِنْ صَامَ وَصَلَّى، فَادْعُوا بِدَعْوَةِ اللَّهِ الَّتِي سَمَّأْتُمْ بِهَا الْمُسْلِمِينَ الْمُؤْمِنِينَ عِبَادَ اللَّهِ»

“Ndio, na hata akifunga na kuswali. Hivyo, linganieni katika wito wa Allah ambamo Amewaita kwayo Waislamu, Waumini na waja wa Allah.”<sup>1</sup>

Na Kauli Yake:

لَيَكُونَنَّ الرَّسُولُ شَهِيدًا عَلَيْكُمْ وَتَكُونُوا شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ

“Ili awe Mtume shahidi juu yenu, na nyinyi muwe mashahidi kwa watu.”

Maana yake: hakika Tumewajaalieni hivi Umma wa kati na kati, waadilifu, Umma bora na mataifa yote yatashuhudia kwa uadilifu wenu wote. Na siku ya Kiyama mutakuwa,

شُهَدَاءَ عَلَى النَّاسِ

“Mashahidi kwa watu.”

Kwa sababu nyumati zote zitakubali uongozi, ubwana wake na fadhila (ubora) zake pamoja na kutangulia kwake. Kwa hiyo, Siku ya Kiyama ushahidi wao utakubaliwa kama hoja kuwa Mitume walifikisha risala ya Mola wao Mlezi kwao, na Mtume atashuhudia juu ya Ummah huu kuwa alifikisha ujumbe huo kwao. Na Kauli Yake:

فَأَقِمْوْا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ

“Basi shikeni Swala na toeni Zaka.”

Maana yake: itikieni na kubalini neema hii kubwa kwa kushukuru na kutekeleza majukumu yenu kwa Allah تعالیٰ, kwa kufuata yaliyofaridhiwa kwenu na kutii yaliyo wajibu na kuacha ya haramu. Na yaliyo muhimu katika hayo ni kusimamisha Swala na kutoa Zaka. Na hiyo ni ihsani kwa viumbe vya Allah تعالیٰ, kwa Aliyowajibisha matajiri kutoa katika mali yao ili kuwapa mafakiri

<sup>1</sup> An-Nasaa’iy katika Al-Kubraa 6:412 na Ahmad 4:130.

kila mwaka, na kuwasaidia dhaifu (wanyonge) na wenye mahitaji. Hili tayari tumebainisha kwa upana hapo awali katika Aya ya Zaka iliyopo katika Suratut Tawbah (9:5). Na Kauli Yake:

وَأَعْتَصِمُوا بِاللهِ

**“Na shikamaneni na Allah.”**

Maana yake: tafuta msaada na usaidizi kutoka kwa Allah تعالى na mtegemeeni Yeye na pata nguvu kutoka Kwake.

هُوَ مَوْلَانَكُمْ

**“Yeye Ndiye Mlinzi wenu.”**

Maana yake: Yeye Ndiye Mwenye Kuwahifadhi na Msaidizi wenu na Ndiye Atakayewafanya kuwashinda maadui zenu.

فَنِعْمَ الْمَوْلَىٰ وَنِعْمَ النَّصِيرُ

**“Mlinzi bora kabisa, na Msaidizi bora kabisa.”**

Maana yake: Yeye Ndiye Mlinzi bora kwenu na Msaidizi bora dhidi ya maadui zenu.

Na huu ndio mwisho wa Suratut Hajj. Na Allah تعالى Amswalie na Kumbariki Bwana wetu, Muhammad ﷺ, Ahli na Swahaba wake na Awapatie amani na usalama; Allah تعالى Awakirimu na Awaridhie Maswahaba na waliowafuata kwa wema mpaka Siku ya Kiyama.

\* \* \*



## Tafsiri ya Suratul Mu'minin

### Sura ya 23

#### Iliteremshwa Makkah

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

Kwa Jina la Allah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu.

سُورَةُ الْمُؤْمِنِينَ

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

قَدْ أَفْلَحَ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ الَّذِينَ هُمْ فِي صَلَاتِهِمْ خَشِعُونَ  
 ﴿٢﴾ وَالَّذِينَ هُمْ عَنِ اللَّغْوِ مُعْرِضُونَ ﴿٣﴾ وَالَّذِينَ هُمْ  
 لِلزَّكَاةِ فَاعِلُونَ ﴿٤﴾ وَالَّذِينَ هُمْ لِفُرُوجِهِمْ حَافِظُونَ ﴿٥﴾  
 إِلَّا عَلَىٰ أَزْوَاجِهِمْ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ فَإِنَّهُمْ غَيْرُ  
 مَلُومِينَ ﴿٦﴾ فَمَنْ آتَبَعْنِي وَرَاءَ ذَلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ  
 الْعَادُونَ ﴿٧﴾ وَالَّذِينَ هُمْ لِأَمْتِنَتِهِمْ وَعَهْدِهِمْ رَاعُونَ ﴿٨﴾  
 وَالَّذِينَ هُمْ عَلَىٰ صَلَاتِهِمْ يُحَافِظُونَ ﴿٩﴾ أُولَٰئِكَ هُمُ  
 الْوَارِثُونَ ﴿١٠﴾ الَّذِينَ يَرِثُونَ الْفِرْدَوْسَ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿١١﴾  
 وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنسَانَ مِن سُلَالَةٍ مِّن طِينٍ ﴿١٢﴾ ثُمَّ  
 جَعَلْنَاهُ نُطْفَةً فِي قَرَارٍ مَّكِينٍ ﴿١٣﴾ ثُمَّ خَلَقْنَا النُّطْفَةَ عَلَقَةً  
 فَخَلَقْنَا الْعَلَقَةَ مُضْغَةً فَخَلَقْنَا الْمُضْغَةَ عِظْمًا فَكَسَوْنَا  
 الْعِظْمَ لَحْمًا ثُمَّ أَنْشَأْنَاهُ خَلْقًا آخَرَ ۗ فَتَبَارَكَ اللَّهُ أَحْسَنُ  
 الْخَالِقِينَ ﴿١٤﴾ ثُمَّ إِنَّكُمْ بَعْدَ ذَلِكَ لَمَعِثُونَ ﴿١٥﴾ ثُمَّ إِنَّكُمْ  
 يَوْمَ الْقِيَامَةِ تُبْعَثُونَ ﴿١٦﴾ وَلَقَدْ خَلَقْنَا فَوْقَكُمْ سَبْعَ  
 طَرَائِقَ وَمَا كُنَّا عَنِ الْخَلْقِ غَافِلِينَ ﴿١٧﴾

قَدْ أَفْلَحَ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾ الَّذِينَ هُمْ  
 فِي صَلَاتِهِمْ خَشِعُونَ ﴿٢﴾ وَالَّذِينَ  
 هُمْ عَنِ اللَّغْوِ مُعْرِضُونَ ﴿٣﴾  
 وَالَّذِينَ هُمْ لِلزَّكَاةِ فَاعِلُونَ ﴿٤﴾  
 وَالَّذِينَ هُمْ لِفُرُوجِهِمْ حَافِظُونَ ﴿٥﴾  
 إِلَّا عَلَىٰ أَزْوَاجِهِمْ أَوْ مَا مَلَكَتْ  
 أَيْمَانُهُمْ فَإِنَّهُمْ غَيْرُ مَلُومِينَ ﴿٦﴾  
 فَمَنْ آتَبَعْنِي وَرَاءَ ذَلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ  
 الْعَادُونَ ﴿٧﴾ وَالَّذِينَ هُمْ لِأَمْتِنَتِهِمْ  
 وَعَهْدِهِمْ رَاعُونَ ﴿٨﴾ وَالَّذِينَ هُمْ  
 عَلَىٰ صَلَاتِهِمْ يُحَافِظُونَ ﴿٩﴾ أُولَٰئِكَ  
 هُمُ الْوَارِثُونَ ﴿١٠﴾ الَّذِينَ يَرِثُونَ  
 الْفِرْدَوْسَ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿١١﴾

1. Hakika wamefanikiwa Waumini.

2. Ambao ni wanyenyekevu katika Swala zao.

3. Na ambao hujiepusha na mambo ya upuuzi.
4. Na ambao wanatoa Zaka.
5. Na ambao wanazilinda tupu zao.
6. Isipokuwa kwa wake zao au kwa iliyowamiliki mikono yao ya kulia. Kwani hao si wenye kulaumiwa.
7. Lakini anayetaka kinyume cha haya, basi hao ndio warukao mipaka.
8. Na ambao wanazitimiza amana zao na ahadi zao.
9. Na ambao Swala zao wanazihifadhi
10. Hao ndio warithi.
11. Ambao watairithi Pepo ya Firdausi, wadumu humo milele.

### Kufaulu kwa Waumini na Kutaja kwa Sifa Zao Katika Qur'an

Na Kauli Yake:

قَدْ أَفْلَحَ الْمُؤْمِنُونَ ﴿١﴾

**"Hakika wamefanikiwa Waumini."** Maana yake: bila shaka wamefuzu, wamepata wema na kufikia ufaulu. Na hao ni Waumini wenye sifa zifuatazo:

الَّذِينَ هُمْ فِي صَلَاتِهِمْ خَاشِعُونَ ﴿٢﴾

**"Ambao ni wanyenyekevu katika Swala zao".**

Amepokea 'Aliy bin Abi Twalhah kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema:

خَاشِعُونَ ﴿٣﴾

**"Wanyenyekevu."** Ina maana ya kuogopa, kuwa na hofu na kuwa na utulivu<sup>1</sup>. Na hivyo ndivyo ilivyopokewa kutoka kwa Mujaahid, Al-Hasan, Qataadah na Az-Zuhriy<sup>2</sup>. Na 'Aliy bin Abi Twaalib رضي الله عنه amesema: "Unyenyekevu ni unyenyekevu wa moyo"<sup>3</sup>. Na hivyo ndivyo alivyosema Ibrahim An-Nakha'iy.<sup>4</sup>

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 19:9. <sup>2</sup> Atw-Twabariy 19:8,9. <sup>3</sup> Atw-Twabariy 19:9. <sup>4</sup> Atw-Twabariy 19:9.

Na amesema Al- Hasan Al-Baswriy رَحِمَهُ اللهُ تَعَالَى: "Unyenyekevu wao ulikuwa nyoyoni mwao, kwayo wakainamisha macho yao na kuteremsha bawa (la rehema). Na hakika unyenyekevu katika Swala unapatikana kwa aliyeufanya moyo wake kuwa mtupu na kuushughulisha kwa yaliyo mema na kuuathiri. Hapo ndipo utapata raha na pozo la macho, kama ilivyonukuliwa katika Hadithi ya Imaam Ahmad na An-Nasaa'iy kutoka kwa Anas رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«حُبِّبَ إِلَيَّ الطَّيِّبُ وَالنِّسَاءُ، وَجُعِلَتْ قُرَّةُ عَيْنِي فِي الصَّلَاةِ»

*"Nimependekezewa manukato na wanawake na nikajaaliwa Swala kuwa pozo langu la macho."*<sup>1</sup>

Na Kauli Yake:

وَالَّذِينَ هُمْ عَنِ اللَّغْوِ مُعْرِضُونَ ﴿٢٥﴾

***"Na ambao hujiepusha na mambo ya upuuzi."***

Maana: kutokana na batili, nayo inajumlisha ushirikina na maasi (madhambi) na yasiyokuwa na faida kwayo katika kauli na matendo. Hii ni kama alivyosema Aliyetukuka:

وَإِذَا مَرُّوا بِاللَّغْوِ مَرُّوا كِرَامًا ﴿٢٦﴾

***"Na wanapopita penye upuuzi, hupita kwa heshima (yao)."*** (25:72).

Amesema Oatadah: "Naapa kwa Allah تَعَالَى, ulikuja kwao kutoka kwa Allah تَعَالَى kile kilicho waweka wao mbali na madhambi"<sup>2</sup>. Na Kauli Yake:

وَالَّذِينَ هُمْ لِلزَّكَاةِ فَاعِلُونَ ﴿٢٧﴾

***"Na ambao wanatoa Zakah."***

Wafasiri wengi wamesema kuwa maana yake ni Zaka ya mali, japokuwa Aya hii imeteremshwa Makka, na Zaka imefaradhishwa Madina mwaka wa pili baada ya Hijra. Na dhahiri ni kuwa Zaka iliyofaradhishwa Madina ni ile iliyojikita katika *Nuswub*<sup>3</sup> na kiwango hasa (maalumu), na mbali na hilo asli ni kuwa Zaka ilifanywa wajibu Makka. Hii ni kama alivyosema Aliyetukuka katika Suratul An'aam, nayo ni Sura iliyoteremshwa Makka:

<sup>1</sup> Ahmad 3:199 na An-Nasaa'iy 7:61, 62.

<sup>2</sup> Az-Zuhd cha Ibn Al-Mubaarak 55.

<sup>3</sup> Kiwango cha chini cha mali ambayo inamuwajibisha mwenye kumiliki kutoa Zaka.

وَأَتُوا حَقَّهُ يَوْمَ حَصَادِهِ<sup>ط</sup>

**“Na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake...” (6:141).**

Na huenda ikawa maana yake hapa ni kuitakasa nafsi kutokana na ushirikina na uchafu, kama ilivyo katika Aya:

قَدْ أَفْلَحَ مَنْ زَكَّاهَا ﴿٩١﴾ وَقَدْ خَابَ مَنْ دَسَّاهَا ﴿٩٢﴾

**“Bila shaka amefaulu aliyeitakasa (nafsi yake). Na bila shaka amejahasiri aliyeiviza (nafsi yake).” (91:9-10).**

Na huenda maana yake ikawa inajumlisha maana zote mbili, nayo ni kuitakasa nafsi na Zaka ya mali. Kwani hiyo ni sehemu ya kuitakasa nafsi na Muumini aliyekamilika ni yule mwenye kuyashikilia na kuyachunga yote mawili, hili na hili. Na Allah تعالى Anajua zaidi. Na Kauli Yake:

وَالَّذِينَ هُمْ لِفُرُوجِهِمْ حَافِظُونَ ﴿٣١﴾ إِلَّا عَلَىٰ أَزْوَاجِهِمْ أَوْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُهُمْ فَإِنَّهُمْ غَيْرُ

مَلُومِينَ ﴿٣٢﴾ فَمَنْ آتَبَعِي وَرَاءَ ذَلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْعَادُونَ ﴿٣٣﴾

**“Na ambao wanazilinda tupu zao, Isipokuwa kwa wake zao au kwa iliyowamiliki mikono yao ya kulia. Kwani hao si wenye kulaumiwa. Lakini anayetaka kinyume cha haya, basi hao ndio warukao mipaka.” (70:29-31).**

Hii ina maana, wale wanaohifadhi tupu zao kutokana na haramu, hivyo hawaingii katika Aliyowakataza Allah تعالى, nayo ni zinaa na liwati, hawakaribii ila wake zao aliohalalishiwa na Allah تعالى au iliyo miliki mikono yake ya kiume miongoni mwa mateka wa kivita. Na yeyote mwenye kufuata na kutaka Aliyohalalisha Allah تعالى hatalaumiwa kabisa wala hatakuwa na dhambi. Kwa hiyo, Akasema hapa:

فَأِنَّهُمْ غَيْرُ مَلُومِينَ ﴿٣١﴾ فَمَنْ آتَبَعِي وَرَاءَ ذَلِكَ

**“Kwani hao si wenye kulaumiwa. Lakini anayetaka kinyume cha haya...” (70:30-31),** Maana yake: Wasiokuwa wake na vijakazi,

فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْعَادُونَ ﴿٣٢﴾

**“Basi hao ndio warukao mipaka...” (70:31),**



Maana yake: Wavukao mipaka. Na kauli Yake:

وَالَّذِينَ هُمْ لِأَمْتِنَتِهِمْ وَعَهْدِهِمْ رَاعُونَ ﴿٢٣﴾

**“Na ambao wanazitimiza amana zao na ahadi zao.”**

Maana yake: wakiadiniwa hawafanyi hiyana bali wanazirudisha kwa wenyewe, na wanapoahidi au kutoa ahadi basi huzitekeleza hizo. Hawawi wenye sifa kama za wanafiki ambao Mtume ﷺ amesema yafuatayo kuwahu:

«آيَةُ الْمُنَافِقِ ثَلَاثٌ: إِذَا حَدَّثَ كَذَبَ، وَإِذَا وَعَدَ أَخْلَفَ، وَإِذَا أُؤْتِيَ خَانٌ»

*“Alama za mnafiki ni tatu: Anapozungumza husema uongo; anapoahidi hukhalifu; na anapoaminiwa hufanya hiyana.”<sup>1</sup>*

Na Kauli Yake:

وَالَّذِينَ هُمْ عَلَىٰ صَلَوَاتِهِمْ يُحَافِظُونَ ﴿٢٤﴾

**“Na ambao Swala zao wanazihifadhi.”**

Maana yake: wanadumu kuzitekeleza kwa wakati wake kama alivyosema Ibn Mas'ud رضي الله عنه. Nilimuuliza Mtume ﷺ: “Ewe Mtume ﷺ! Ni amali gani inayompendeza sana Allah?” Akasema:

«الصَّلَاةُ عَلَىٰ وَفِيهَا»

*“Swala kwa wakati wake”. Nikauliza: “Kisha ipi (amali gani)?” Akasema:*

«بِرُّ الْوَالِدَيْنِ»

*“Kuwatendea wema wazazi wawili”. Nikauliza: “Kisha ipi (amali gani)?” Akasema:*

«الْجِهَادُ فِي سَبِيلِ اللَّهِ»

*“Jihadi katika njia ya Allah”. Imenakiliwa katika Sahihi mbili<sup>2</sup>.*

Na amesema Qatadah: “Kwa wakati wake na kutimiza rukuu na sijdah zake”<sup>3</sup>. Na hakika Allah تعالى Amezua Kutaja sifa hizi nzuri zenye kusifiwa kwa Swala na Kumaliza na Swala. Na hii ni dalili ya ubora na fadhila kama alivyosema Mtume ﷺ:

<sup>1</sup> Fat'h Al-Baariy 10:522.

<sup>2</sup> Fat'h Al-Baariy 10:414 na Muslim 1:89. <sup>3</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 6:89.

«اسْتَقِيمُوا وَلَنْ تُحْضُوا، وَاعْلَمُوا أَنَّ خَيْرَ أَعْمَالِكُمُ الصَّلَاةُ، وَلَا يُحَافِظُ عَلَى  
النُّصُوءِ إِلَّا مُؤْمِنٌ»

*“Simameni imara (kuweni na msimamo) wala hamutaweza kutekeleza hilo. Na jueni kuwa amali yenu iliyo bora ni Swala. Na hakuna anayehifadhi udhu ila Muumini.”<sup>1</sup>*

Baada ya Allah تعالی Kuwasifu kwa sifa hizi nzuri na matendo mema, Akasema:

﴿أُولَئِكَ هُمُ الْوَارِثُونَ﴾ الَّذِينَ يَرِثُونَ الْفِرْدَوْسَ هُمْ فِيهَا خَالِدُونَ ﴿﴾

***“Hao ndio warithi, ambao watairithi Pepo ya Firdaws, wadumu humo.”***

Na imethibiti katika Sahihi mbili kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِذَا سَأَلْتُمُ اللَّهَ الْجَنَّةَ فَاسْأَلُوهُ الْفِرْدَوْسَ، فَإِنَّهُ أَعْلَى الْجَنَّةِ وَأَوْسَطُ الْجَنَّةِ، وَمِنْهُ  
تُنَجَّرُ أَنْهَارُ الْجَنَّةِ، وَفَوْقَهُ عَرْشُ الرَّحْمَنِ»

*“Mnapomuomba Allah Pepo basi muombeni Firdaws, kwani hiyo ndio sehemu ya juu ya Pepo, katikati ya Pepo, na kutoka kwayo hububujika mito ya Pepo, na juu yake kipo Kiti cha Enzi (Arshi) ya ar-Rahman (Mwingi wa Rehema)”<sup>2</sup>.*

Na amepokea Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه amesema, Mtume ﷺ amesema:

«مَا مِنْكُمْ مِنْ أَحَدٍ إِلَّا وَلَهُ مَنزِلَانِ: مَنزِلٌ فِي الْجَنَّةِ، وَمَنزِلٌ فِي النَّارِ، فَإِنْ مَاتَ  
فَدَخَلَ النَّارَ وَرِثَ أَهْلَ الْجَنَّةِ مَنزِلَهُ، فَذَلِكَ قَوْلُهُ: ﴿أُولَئِكَ هُمُ الْوَارِثُونَ﴾ ﴿﴾»

*“Hakuna yeyote miongoni mwenu ila ana nyumba mbili, nyumba Peponi na nyingine Motoni. Pindi anapokufa na akaingia Motoni, watu wa Peponi watairithi nyumba yake, na hii ni Kauli Yake Aliyetukuka: ‘Hao ndio warithi’.<sup>3</sup>*

Na amepokea Ibn Jurayj kutoka kwa Layth kutoka kwa Mujahid kuhusu Kauli Yake:

<sup>1</sup> Ibn Maajah 2:101.

<sup>2</sup> Fat’h Al-Baariy 13:415.

<sup>3</sup> Ibn Maajah 2:1453.

أَوْلَاتِكُمْ هُمُ الْوَارِثُونَ ﴿٦٣﴾

**“Hao ndio warithi’.**

Hiyo ina maana kuwa Waumini watarithi nyumba za makafiri kwani wao waliumbwa kwa ajili ya kumuabudu Allah تعالی Peke Yake bila ya mshirika. Hivyo pale Waumini walipofanya waliyoamrisha katika ibada, ilhali makafiri walipuuza yale waliyombiwa kwayo, Waumini walipata sehemu ambayo wangepewa (makafiri) lau wangemtii Mola wao Mlezi. Kadhia hii ni kama ambavyo imeelezwa katika *Sahih Muslim* kutoka kwa Abu Burdah, kutoka kwa baba yake kutoka kwa Mtume ﷺ amesema:

يَجِيءُ يَوْمَ الْقِيَامَةِ نَاسٌ مِنَ الْمُسْلِمِينَ بِذُنُوبٍ أَمْثَالِ الْجِبَالِ، فَيَغْفِرُهَا اللَّهُ لَهُمْ وَيَضُمُّهَا عَلَى الْيَهُودِ وَالنَّصَارَىٰ

*“Siku ya kiyama watakuja watu miongoni mwa Waislamu dhambi zao ni mithili ya milima, Allah Atawasamehe, na dhambi hizo kuwapa Yahudi na Manasara.”<sup>1</sup>*

Katika tamko jingine la Muslim Mtume ﷺ amesema,

إِذَا كَانَ يَوْمَ الْقِيَامَةِ دَفَعَ اللَّهُ لِكُلِّ مُسْلِمٍ يَهُودِيًّا أَوْ نَصْرَانِيًّا، فَيَقَالَ: هَذَا وَكَأُثْمِكَ مِنَ النَّارِ

*“Siku ya kiyama itakapowadia Allah Atamuelekeza kila Muislamu kwa Yahudi au Mnasara, hapo patasemwa: Huyu atakukombo (ataingizwa) yeye motoni badala yako.”*

‘Umar bin ‘Abd Al-‘Aziz alimtaka Abu Burdah aape mara tatu kwa Allah تعالی ambaye hakuna Mola anayestahiki kuabudiwa ila yeye, yakuwa baba yake alimuhadithia yeye habari hiyo kutoka kwa Mtume ﷺ, akasema: akamuapia yeye hilo.<sup>2</sup> Aya hii ni sawa na Kauli Yake Aliyetukuka:

تِلْكَ الْجَنَّةُ الَّتِي نُورِثُ مِنْ عِبَادِنَا مَنْ كَانَ تَقِيًّا ﴿٦٤﴾

**“Hiyo ndiyo Pepo Tutakayowarithisha katika waja Wetu wale ambao ni wachaji Mungu.” (19:63).**

<sup>1</sup> Muslim 4:2120.

<sup>2</sup> Muslim 4:2119.

Na kama Kauli Yake:

وَتِلْكَ الْحِجَّةُ الَّتِي أُورِثْتُمُوهَا بِمَا كُنْتُمْ تَعْمَلُونَ ﴿٧٢﴾

*“Na hii ni Bustani (Pepo), muliyorithishwa kwa hayo muliyokuwa mkiyafanya.” (43:72).*

وَلَقَدْ خَلَقْنَا الْإِنْسَانَ مِنْ سُلَالَةٍ مِنْ طِينٍ ﴿٧٣﴾ ثُمَّ جَعَلْنَاهُ نُطْفَةً فِي قَرَارٍ مَكِينٍ ﴿٧٤﴾ ثُمَّ خَلَقْنَا النُّطْفَةَ عَلَقَةً فَخَلَقْنَا الْعَلَقَةَ مُضْغَةً فَخَلَقْنَا الْمُضْغَةَ عِظْمًا فَكَسَوْنَا الْعِظْمَ لَحْمًا ثُمَّ أَنْشَأْنَاهُ خَلْقًا آخَرَ ۚ فَتَبَارَكَ اللَّهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ ﴿٧٥﴾ ثُمَّ إِنَّكُمْ بَعْدَ ذَلِكَ لَمَيِّتُونَ ﴿٧٦﴾ ثُمَّ إِنَّكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ تُبْعَثُونَ ﴿٧٧﴾

**12. Na kwa yakini Tumemuumba mwanadamu kutokana na asili ya udongo.**

**13. Kisha Tukamjaalia awe tone ya mbegu ya uzazi katika kalio madhubuti.**

**14. Kisha Tukaiumba tone kuwa damu iliyoganda, na Tukaiumba damu kuwa pande la nyama, kisha Tukaliumba pande la nyama kuwa mifupa, na mifupa Tukaivika nyama. Kisha Tukamfanya kiumbe mwengine. Basi Ametukuka Allah Mbora wa waumbaji.**

**15. Kisha hakika nyinyi baada ya hayo mutakufa.**

**16. Kisha hakika nyinyi Siku ya Kiyama mtafufuliwa.**

**Ishara za Allah تعالى Katika Hatua za Uumbaji wa Mwanadamu Kuanza na Mchanga hadi Tone la Manii.**

Anasema Aliyetukuka Akitupasha sisi habari kuhusu mwanzo wa Kuumbwa mwanadamu kutokana na asli ya udongo. Naye alikuwa ni Adam عليه السلام, Allah تعالى Alimuumba kutokana na udongo mkavu unaotoa sauti, unaotokana na matope meusi yaliyovunda. Na amesema Ibn Jariir رحمه الله تعالى: “Hakika aliitwa ‘Adam’ عليه السلام udongo kwa kuwa ameumbwa kutokana nao”<sup>1</sup>.

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 19:15.

Na amesema Qatadah: "Adam عليه السلام aliumbwa kutokana na udongo"<sup>1</sup>. Na hii ni dhahiri zaidi katika maana yake na karibu zaidi na mtiririko wake, kwani Adam عليه السلام aliumbwa kutokana na udongo unaonata, nao ni udongo mkavu unaotoa sauti, unaotokana na matope meusi yaliyovunda. Na huko ni Kuumbwa kwa mchanga, kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَمِنَ آيَاتِهِمْ أَنْ خَلَقَكُمْ مِنْ تُرَابٍ ثُمَّ إِذَا أَنْتُمْ بَشَرٌ تَنْتَشِرُونَ ﴿٢٠﴾

***"Na katika Ishara Zake ni huku Kukuumbeni kwa udongo, kisha mumekuwa watu munaonea kila mahali."*** (30:20).

Na amepokea Imaam Ahmad kutoka kwa Abi Musa رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«إِنَّ اللَّهَ خَلَقَ آدَمَ مِنْ قُبْضَةٍ قَبْضَهَا مِنْ جَمِيعِ الْأَرْضِ، فَجَاءَ بَنُو آدَمَ عَلَى قَدْرِ الْأَرْضِ، جَاءَ مِنْهُمْ الْأَخْمَرُ وَالْأَبْيَضُ وَالْأَسْوَدُ وَبَيْنَ ذَلِكَ، وَالْخَيْثُ وَالطُّيْبُ وَبَيْنَ ذَلِكَ»

*"Hakika Allah Alimuumba Adam kutokana na Fumba la mchanga Alilochukua kutoka maeneo yote ya ardhi, hivyo watoto wa Adam walikuja kwa kiasi hicho cha ardhi, miongoni mwao wakiwa wekundu, weupe na weusi na baina yao. Na wengine wabaya, wazuri na baina yao."*<sup>2</sup>

Na hakika imepokewa na Abu Daud na At-Tirmidhiy mfano wake<sup>3</sup>. Na akasema At-Tirmidhiy: Hii ni Hadith Hasan Sahih.

ثُمَّ جَعَلْنَاهُ نُطْفَةً

***"Kisha Tukamjaalia awe tone ya mbegu ya uzazi..."***

Kiwakilishi hiki kinarejea katika jinsi ya mwanadamu kama Alivyosema katika Aya nyingine:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 19:14.

<sup>2</sup> Ahmad 4:400.

<sup>3</sup> Abu Daawuud 5:67 na Tuhfatul Ahwadhiy 8:290.

وَبَدَأَ خَلْقَ الْإِنسَانِ مِن طِينٍ ﴿٧﴾ ثُمَّ جَعَلَ نَسْلَهُ مِن سُلَالَةٍ مِّن مَّاءٍ مَّهِينٍ ﴿٨﴾

**“...Na Akaanzisha umbo la mwanadamu kwa udongo. Na kisha Akakifanya kizazi chake kwa mchujo wa maji yaliyodhalili.” (32:7-8)**

Maana yake: Dhaifu, kama Alivyosema:

أَلَمْ نَخْلُقْكُمْ مِّن مَّاءٍ مَّهِينٍ ﴿٢١﴾ فَجَعَلْنَاهُ فِي قَرَارٍ مَّكِينٍ ﴿٢٢﴾

**“Je, Hatukukuumbeni kwa maji yaliyo dhalili? Kisha Tukayaweka mahali pa tulivu.” (77:20-21).**

Hii ina maana ya mfuko wa uzazi, maji ambayo yametayarishwa na kuundwa kwa ajili ya hilo,

إِلَىٰ قَدَرٍ مَّعْلُومٍ ﴿٢٣﴾ فَقَدَرْنَا فَنِعْمَ الْقَادِرُونَ ﴿٢٤﴾

**“Mpaka muda maalumu. Na Tukaikadiria (wakati wa kutoka mtoto) Nasi ni wazuri kabisa wa kukadiri.” (77:22-23),**

Kumaanisha muda unaojulikana na ajali maalumu mpaka ifike na kwenda kutoka hali moja hadi nyingine na sifa moja hadi nyingine. Kwa ajili ya hiyo, Amesema hapa:

ثُمَّ خَلَقْنَا النُّطْفَةَ عَلَقَةً

**“Kisha Tukaiumba tone kuwa damu iliyoganda.”**

Maana yake: Tulilifanya tone, ambalo ni maji yanayotoka kwa kuchupa yatokayo kwenye mifupa ya mwanamume, nao ni mgongo wake na kifua cha mwanamke, nayo ni mifupa ya kifua chake, baina ya mtulinga na matiti. Kisha ikawa nyekundu iliyoganda, mfano wa donge la damu (lenye kuning'inia) iliyorefuka. Amesema 'Ikrima: “Nayo ni damu”.

فَخَلَقْنَا الْعَلَقَةَ مُضْغَةً

**“Na Tukaiumba damu iliyoganda kuwa pande la nyama.”** Nacho ni kipande cha nyama (chenye kuning'inia) kisichokuwa na muundo wala umbile.

فَخَلَقْنَا الْمُضْغَةَ عِظْمًا

**“Kisha Tukaliumba pande la nyama kuwa mifupa.”** Maana yake: Tukalipa muundo, wenye kichwa, mikono, miguu yenye mifupa, neva na mishipa.

فَكَسَوْنَا الْعِظْمَ حَمًّا

**“Na mifupa Tukaivika nyama”.** Maana yake: Tukajaalia juu ya hayo kitu cha kuivika na kuipa nguvu.

ثُمَّ أَدْشَأْنَتْهُ خَلْقًا ءَاخَرَ

**“Kisha Tukamfanya kiumbe mwengine.”**

Maana yake: Tukapuliza roho, hivyo Kuifanya itaharaki na kuwa kiumbe kingine kabisa, chenye kusikia, kuona, kufahamu na kutaharaki.

فَتَبَارَكَ اللَّهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ ﴿٢٠﴾

**“Basi ametukuka Allah Mbora wa waumbaji.”**

Na amepokea Al-'Awfiy kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema:

ثُمَّ أَدْشَأْنَتْهُ خَلْقًا ءَاخَرَ

**“Kisha Tukamfanya kiumbe mwengine.”**

Maana yake: “Tunaibadilisha kutoka hali moja hadi nyingine mpaka akatoka akiwa mtoto mchanga, kisha akakua akawa kijana, kisha akabaleghe, kisha akawa barobaro, kisha akawa mtu mzima na baadaye mzee na kisha mkongwe aliye dhaifu”<sup>1</sup>. Amepokea Imaam Ahmad رحمه الله تعالى katika Musnad wake kutoka kwa Abdallah bin Mas'ud رضي الله عنه aliyesema: Ametuzungumzia Mtume ﷺ naye ndiye msema kweli wa kusadikika:

«إِنَّ أَحَدَكُمْ لَيَجْمَعُ خَلْقَهُ فِي بَطْنِ أُمِّهِ أَرْبَعِينَ يَوْمًا نُطْفَةً، ثُمَّ يَكُونُ عَلَقَةً مِثْلَ ذَلِكَ، ثُمَّ يَكُونُ مُضْغَةً مِثْلَ ذَلِكَ، ثُمَّ يُرْسَلُ إِلَيْهِ الْمَلَكُ فَيَنْفُخُ فِيهِ الرُّوحَ وَيُؤَمِّرُ بِأَرْبَعِ كَلِمَاتٍ: رِزْقِهِ، وَأَجَلِهِ، وَعَمَلِهِ، وَهَلْ هُوَ شَقِيحٌ أَوْ سَعِيدٌ، فَوَالَّذِي لَا إِلَهَ غَيْرُهُ إِنَّ أَحَدَكُمْ لَيَعْمَلُ بِعَمَلِ أَهْلِ الْجَنَّةِ حَتَّىٰ مَا يَكُونُ بَيْنَهُ وَبَيْنَهَا إِلَّا ذِرَاعٌ، فَيَسْبِقُ عَلَيْهِ الْكِتَابُ فَيُخْتَمُ لَهُ بِعَمَلِ أَهْلِ النَّارِ فَيَدْخُلُهَا، وَإِنَّ الرَّجُلَ لَيَمْتَلُ بِعَمَلِ أَهْلِ النَّارِ حَتَّىٰ مَا يَكُونُ بَيْنَهُ وَبَيْنَهَا إِلَّا ذِرَاعٌ، فَيَسْبِقُ عَلَيْهِ الْكِتَابُ فَيُخْتَمُ لَهُ بِعَمَلِ أَهْلِ الْجَنَّةِ فَيَدْخُلُهَا»

**“Hakika kila mmoja wenu katika nyinyi hukusanywa umbo lake katika tumbo la mamake kama mchanganyiko wa mbegu ya uzazi**

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 19:18. Sanadi yake ni dhaifu.

*ya mwanamume na mwanamke kwa muda wa siku arobaini; kisha kuwa kipande cha damu kwa muda kama huo; kisha kipande cha nyama kwa muda kama huo. Kisha hutumwa Malaika akampulizia roho ndani yake, na akaamrisha mambo mane: Riziki yake, muda wake, amali yake. Na je yeye ni mwema au muovu, naapa kwa Allah Ambaye hakuna mwengine anayestahiki kuabudiwa isipokuwa Yeye, hakika mmoja wenu anaweza kufanya amali za watu wa peponi, mpaka inakuwa baina yake na pepo isipokuwa dhira moja, hivyo basi, hutanguliwa na maandiko, huthibitishwa kuwa yeye ni mtu wa motoni na huingia motoni. Hakika mmoja anafanya amali za watu wa motoni hadi inakuwa baina yake yeye na moto ni usawa wa dhira moja, humtangulia yeye maandiko, huthibitishwa kuwa yeye ni mtu wa peponi.”<sup>1</sup>*

Pia imepokewa na Al-Bukhari na Muslim<sup>2</sup>. Na Kauli Yake:

﴿فَتَبَارَكَ اللَّهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ﴾

**“Basi Ametukuka Allah Mbora wa waumbaji.”**

Maana yake: pindi Allah تعالى Alipotaja Uweza na Ustadhi Wake wa Kuumba *Nutfah* hii kutoka hali moja hadi hali nyingine, muundo mmoja hadi mwingine mpaka ikatokeza sura iliyokuwa ya mwanadamu aliye sawa na kukamilika kimaumbile, Akasema:

﴿فَتَبَارَكَ اللَّهُ أَحْسَنُ الْخَالِقِينَ﴾

**“Basi Ametukuka Allaah Mbora wa waumbaji”.**

Na Kauli Yake:

﴿ثُمَّ إِنَّكُمْ بَعْدَ ذَلِكَ لَمَيِّتُونَ﴾

**“Kisha hakika nyinyi baada ya hayo mtakufa”.**

Maana yake: Baada ya kuumbwa huku hapo awali bila ya chochote, mutaelekea kufa.

<sup>1</sup> Ahmad 1:382.

<sup>2</sup> Fat'h al-Baariy 6:418 na Muslim 4:2036.



ثُمَّ إِنَّكُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ تُبْعَثُونَ ﴿١٧﴾

**“Kisha hakika nyinyi Siku ya Kiyama mtafufuliwa.”**

Maana yake: Mutaumbwa tena upya.

ثُمَّ اللَّهُ يُنشِئُ النَّشْأَةَ الْآخِرَةَ ﴿٢٠﴾

**“Kisha Allah Ndiye Atakayeumba umbo la baadaye.” (29:20)**

Maana yake: Siku ya Ufufuo (kurudi), wakati ambao roho zitarudi katika miili na viumbe vyote kuhesabiwa. Hapo kila mmoja atalipwa kwa amali yake, ikiwa ni nzuri basi atapata kheri nyingi na zikiwa ni mbaya basi ni adhabu kali kwake.

وَلَقَدْ خَلَقْنَا فَوْقَكُمْ سَبْعَ طَرَائِقَ وَمَا كُنَّا عَنِ الْخَلْقِ غَافِلِينَ ﴿١٧﴾

**17. Na kwa yakini Tumeziumba juu yenu njia saba. Nasi Hatukuwa wenye Kughafilika na viumbe.**

### Ishara Yake katika Kuumba Mbingu

Baada ya Allah تعالی Kutaja Kuumbwa kwa binadamu, Alifuatisha Kutaja Kuumbwa kwa mbingu saba. Mara nyingi sana Anataja Aliyetukuka Kuumbwa kwa mbingu na ardhi pamoja na Kuumbwa kwa mwanadamu, kama Alivyosema Aliyetukuka:

لَخَلْقُ السَّمَوَاتِ وَالْأَرْضِ أَكْبَرُ مِنْ خَلْقِ النَّاسِ ﴿٥٧﴾

**“Kwa yakini umbo la mbingu na ardhi ni kubwa kuliko umbo la wanadamu...” (40:57).**

Na Aya kama hiyo inapatikana mwanzo wa Sura Aliyf Laam Miym Sajdah, ambayo Mtume ﷺ alikuwa akiisoma asubuhi ya siku ya Ijumaa. Mwanzo wake inataja Kuumbwa kwa mbingu na ardhi, kisha inabainisha Kuumbwa kwa mwanadamu kutokana na mchujo wa manii kutoka kwa udongo. Pia inaeleza kuhusu ufufuo, thawabu na adhabu na mambo mengineo katika malengo.

Na Kauli Yake:

سَبْعَ طَرَائِقَ

*"Njia saba".*

Amesema Mujaahid: "Maana yake ni mbingu saba."<sup>1</sup> Na hii ni kama Kauli Yake:

تُسَبِّحُ لَهُ السَّمَوَاتُ السَّبْعُ وَالْأَرْضُ وَمَنْ فِيهِنَّ

*"Zinamtukuza mbingu zote saba na ardhi na vilivyomo ndani yake."*  
(17:44).

Na pia Kauli yake,

أَلَمْ تَرَوْا كَيْفَ خَلَقَ اللَّهُ سَبْعَ سَمَوَاتٍ طِبَاقًا

*"Je, hamuoni jinsi Allah Alivyoumba mbingu saba tabakatabaka."*  
(71:15). Pia,

اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمَوَاتٍ وَمِنَ الْأَرْضِ مِثْلَهُنَّ يَتَنَزَّلُ الْأَمْثُرُ بَيْنَهُنَّ لِيَتَعَلَّمُوا أَنْ اللَّهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ وَأَنَّ اللَّهَ قَدْ أَحَاطَ بِكُلِّ شَيْءٍ عِلْمًا

*"Allah ni Yule Ambaye Ameziumba mbingu saba, na ardhi kuwa mfano wa hizo. Amri (Zake) zinashuka baina yao, ili mujue kwamba Allah ni Mwenye Uweza juu ya kila kitu, na kwamba Allah Amekizunguka kila kitu Kukijua."* (65:12)

Na hivyo ndivyo Alivyosema hapa:

وَلَقَدْ خَلَقْنَا فَوْقَكُمْ سَبْعَ طَرَائِقَ وَمَا كُنَّا عَنِ الْخَلْقِ غَافِلِينَ

*"Na kwa yakini Tumeziumba juu yenu njia saba. Nasi Hatukuwa wenye Kughafilika na viumbe."*

Maana yake: Anajua kila kinachokwenda ardhini na kinachotoka, kinachoteremka kutoka mbinguni na kinachoelekea juu (mbinguni). Naye Yupo pamoja nanyi popote mlipo, na Allah تعالی Anaona yote mnayoyafanya.

<sup>1</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 6:94.

Kwa Allah تعالى Hakuna mbingu iliyofichika ndani ya mbingu nyingine, wala ardhi kwa ardhi. Na hakuna jabali wala mlima ila Anajua muundo wake, wala bahari ila Anajua kila kilichomo ndani yake. Anajua idadi ya kila kilichomo katika majabali, milima, mchanga, bahari, mandhari na miti.

وَمَا تَسْقُطُ مِنْ وَرَقَةٍ إِلَّا يَعْلَمُهَا وَلَا حَبَّةٍ فِي ظُلْمَتِ الْأَرْضِ وَلَا رَطْبٍ وَلَا يَابِسٍ إِلَّا فِي

كِتَابٍ مُبِينٍ ﴿٥٩﴾

***“Na halianguki jani ila Analijua. Wala haianguki punje katika giza la ardhi ila Anajua. Wala hakianguki kilichorutubika wala kilichoyabisika ila Anakijua. Hapana chochote, ila kimo katika Kitabu kidhihirishacho kila jambo.” (6:59)***

\* \* \*

وَأَنْزَلْنَا مِنَ السَّمَاءِ مَاءً بِقَدَرٍ فَأَسْكَنَتْهُ فِي الْأَرْضِ ط وَإِنَّا  
 عَلَىٰ ذَهَابٍ بِمَاءِ لَقَدِرُونَ ﴿١٨﴾ فَأَنْشَأْنَا لَكُمْ بِهِ جَنَّاتٍ  
 مِّنْ نَّجِيلٍ وَأَعْتَبْنَا لَكُمْ فِيهَا فَاوَكُهُ كَثِيرَةً وَمِمَّا تَأْكُلُونَ ﴿١٩﴾  
 وَشَجَرَةً تَخْرُجُ مِنْ طُورٍ سَيْنَاءَ تَنْبُتُ بِالذَّهْنِ وَصَبْغٍ  
 لِلْأَكْلِينَ ﴿٢٠﴾ وَإِنَّ لَكُمْ فِي الْأَنْعَامِ لَعِبْرَةً لِّتُسَفِّحُوا مِمَّا  
 فِي بُطُونِهَا وَلَكُمْ فِيهَا مَنَافِعُ كَثِيرَةٌ وَمِمَّا تَأْكُلُونَ ﴿٢١﴾ وَعَلَيْهَا  
 وَعَلَىٰ الْفَلَكَ تُحْمَلُونَ ﴿٢٢﴾ وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِهِ  
 فَقَالَ يَنْقُورِ آعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِنِّ إِلَهٍ غَيْرُهُ ط أَفَلَا  
 تَتَّقُونَ ﴿٢٣﴾ فَقَالَ الْمَلَأُوا الَّذِينَ كَفَرُوا مِن قَوْمِهِ مَا هَذَا  
 إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُرِيدُ أَنْ يَتَفَضَّلَ عَلَيْكُمْ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ  
 لَأَنْزَلَ مَلَائِكَةً مَا سَمِعْنَا بِهَذَا فِي آبَائِنَا الْأَوَّلِينَ ﴿٢٤﴾ إِنْ  
 هُوَ إِلَّا رَجُلٌ بِالْجَبَلِ بِمَاءِ جَنَّةٍ فَنَزَّلْنَا بِهِ مِنَ السَّمَاءِ حَتَّىٰ جِيءَ ﴿٢٥﴾ قَالَ  
 رَبِّ انصُرْنِي بِمَا كَدَّبُونِ ﴿٢٦﴾ فَأَوْحَيْنَا إِلَيْهِ أَنْ اصْنَعْ  
 الْفَلَكَ بِأَعْيُنِنَا وَّوْحَيْنَا فَإِذَا جَاءَ أَهْرَابًا وَقَارَ السُّيُوفِ  
 فَاسْتَلَقَ فِيهَا مِن كُلِّ زَوْجٍ بَئِينٍ وَأَهْلَكَ إِلَّا مَن  
 سَبَقَ عَلَيْهِ الْقَوْلُ مِنهُمْ ط وَلَا تُحِطُّبِنِي فِي الَّذِينَ ظَلَمُوا ط  
 إِنَّهُمْ مُّغْرَقُونَ ﴿٢٧﴾ فَإِذَا اسْتَوَيْتَ أَنْتَ وَمَنْ مَعَكَ عَلَى  
 الْفَلَكَ فَقُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي نَجَّيْنَا مِنَ الْقَوَيمِ الظَّالِمِينَ  
 وَقُلِ رَبِّ أَنْزِلْنِي مُنْزَلًا مُّبَارَكًا وَأَنْتَ خَيْرُ الْمُنْزِلِينَ ﴿٢٨﴾  
 إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَآيَاتٍ وَإِن كُنَّا لَمُبْتَلِينَ ﴿٢٩﴾

وَأَنْزَلْنَا مِنَ السَّمَاءِ مَاءً بِقَدَرٍ  
 فَأَسْكَنَتْهُ فِي الْأَرْضِ ط وَإِنَّا عَلَىٰ  
 ذَهَابٍ بِمَاءِ لَقَدِرُونَ ﴿١٨﴾ فَأَنْشَأْنَا  
 لَكُمْ بِهِ جَنَّاتٍ مِّنْ نَّجِيلٍ وَأَعْتَبْنَا  
 لَكُمْ فِيهَا فَاوَكُهُ كَثِيرَةً وَمِمَّا تَأْكُلُونَ  
 ﴿١٩﴾ وَشَجَرَةً تَخْرُجُ مِنْ طُورٍ سَيْنَاءَ  
 تَنْبُتُ بِالذَّهْنِ وَصَبْغٍ لِلْأَكْلِينَ ﴿٢٠﴾  
 وَإِنَّ لَكُمْ فِي الْأَنْعَامِ لَعِبْرَةً ط  
 تَسَفِّحُوا مِمَّا فِي بُطُونِهَا وَلَكُمْ فِيهَا  
 مَنَافِعُ كَثِيرَةٌ وَمِمَّا تَأْكُلُونَ ﴿٢١﴾  
 وَعَلَيْهَا وَعَلَىٰ الْفَلَكَ تُحْمَلُونَ ﴿٢٢﴾

18. Na Tumeteremsha kutoka mbinguni maji kwa kiasi na Tukayatuliza katika ardhi. Na hakika Sisi Tunaweza Kuyaondoa.

19. Kwa maji hayo Tukakufanyieni bustani za mitende na mizabibu, munapata humo matunda mengi, na katika hayo munakula.

20. Na mti utokao katika mlima wa Sinai, unatoa mafuta na kuwa kitoweo kwa walao.

**21. Na hakika munayo mazingatio makubwa katika nyama ho - Tunakunywesheni katika vile viliomo matumboni mwao, na nyinyi mnapata katika hao manufaa mengi, na pia munawala.**

**22. Na juu yao na juu ya marikebu mnabebwa.**

**Ishara za Allah تعالی na Baraka Zake katika Mvua, Mimea, Miti na Ng'ombe**

Anataja Aliyetukuka Neema Zake nyingi zisizohesabika Alizomtunukia mja Wake, kwayo Anateremsha mvua,

بِقَدْرِ

**"...kwa kiasi..."** Kumaanisha kinachohitajika, sio nyingi sana inayoharibu ardhi na majumba, wala sio kidogo sana isiyotosha kwa mimea na matunda, lakini kwa kadiri inayohitajika kwa ajili ya kunyweshea, kunywa na faida nyingine.

Ikiwa kuna ardhi inayohitaji maji mengi kwa ajili ya kunyweshea lakini udongo wake ulio na rutuba utachukuliwa mvua ikinyesha juu yake, hivyo Allah تعالی huleta mvua kwayo kutoka ardhi nyingine, kama ilivyo kwa ardhi ya Misri (Egypt), ambayo inasemekana ni ardhi kavu.

Allah تعالی Anapeleka maji kutoka mto Naili kwayo, hivyo kuleta udongo mwekundu kutoka Ethiopia inaponyesha huko. Maji yanakuja yakiwa yamebeba udongo mwekundu ambao unatumika kunywesha ardhi ya Misri, na ule ambao unatuwama na kubaki huko (Misri) unatumika kwa ukulima kwa sababu ardhi ya Misri haina rutuba, na sehemu nyingi yake ni mchanga. Ametakasika Aliye Mpole, Mwenye habari zote, Mwenye Kurehemu na Msamehevu.

Na Kauli Yake:

فَأَسْكَنْهُ فِي الْأَرْضِ ط

**"Na Tukayatuliza katika ardhi."**

Maana yake: Tumeyajaalia maji yanapoteremka kutoka kwenye mawingu yatulie katika ardhi, na Tunaifanya ardhi iyakubali na kufyonzwa na kwayo hulishwa mbegu na kokwa. Na Kauli Yake:

وَإِنَّا عَلَىٰ ذَهَابٍ بِهٖ لَقَدِيرُونَ ﴿١٨﴾

**"Na hakika Sisi Tunaweza kuyaondoa."**

Maana: lau Tungetaka mvua isinyeshe basi Tungefanya hivyo; na lau Tungetaka kuinyesheza kwenye jangwa na ardhi iliyoachwa, Tungefanya hivyo. Lau Tungetaka Tungeijaalia kuwa chumvi isiyofaidisha katika kunywa au kunyweshea mimea, Tungefanya hivyo; na lau Tungetaka isifyonzwe na ardhi lakini ibaki juu yake, Tungefanya hivyo; na lau Tungetaka iende ndani sana katika ardhi umbali ambao hamtaweza kuyafikia, hivyo kutoweza kunufaika nayo, Tungefanya hivyo. Hata hivyo, kwa ajili ya Upole Wake na Rehema Yake yanateremka maji kutoka mawinguni yakiwa matamu na safi, kisha yakatuwama ardhini na kusababisha kuwepo kwa chemchemu na mito ambayo mnatumia kwa ajili ya kunywesha mimea na matunda, munakunywa na kuwapa wanyama wenu, na munayatumia kuoga, kujitwahirisha na kujisafisha nayo. Hivyo, Yeye Ndiye Mwenye Kustahiki Sifa na Shukrani. Na Kauli Yake:

فَأَنْشَأْنَا لَكُمْ بِهِ جَنَّاتٍ مِّنْ نَّجِيلٍ وَأَعْنَابٍ

**“Kwa maji hayo Tukakufanyieni bustani za mitende na mizabibu.”**

Maana: Tukawatolea kwa Tunayoteremsha kutoka mbinguni bustani na viunga vya miti ya matunda yaliyo mazuri, yaani yenye mandhari nzuri. Na Kauli Yake:

مِّنْ نَّجِيلٍ وَأَعْنَابٍ

**“Za mitende na mizabibu.”** Maana yake: ndani yake imo mitende na mizabibu. Haya ni bustani zilizokuwa zikifahamika vyema na watu wa Hijazi, wala hakuna tofauti baina ya kitu na kifanani chake. Na hivyo hivyo watu wa kila sehemu wana matunda yao ambayo inaashiria Neema ya Allah ﷻ kwao, na ambayo kwayo hawawezi kumshukuru inavyotakiwa. Na Kauli Yake:

لَكُمْ فِيهَا فَوَاكِهُ كَثِيرَةٌ

**“Munapata humo matunda mengi.”** Maana yake: Matunda yote, kama Anavyosema Aliyetukuka mahali pengine:

يُنْبِتُ لَكُمْ بِهِ الزَّرْعَ وَالزَّيْتُونَ وَالنَّخِيلَ وَالْأَعْنَابَ وَمِن كُلِّ الثَّمَرَاتِ

**“Na kwa hayo Hukuotesheeni mimea ya kila namna na mizeituni, mitende, mizabibu na kila matunda...” (16:11).**

Na Kauli Yake:

وَمِنْهَا تَأْكُلُونَ ﴿١٨﴾

**“Na katika hayo munakula.”** Hii ni kama kwamba unangojea kitu kwa kipimo kilichopimwa huku unatizama uzuri wake, unangojea iwe tayari (kwa kuiva) na kisha kula kutoka kwayo. Na Kauli Yake:

وَشَجَرَةً تَخْرُجُ مِنْ طُورِ سَيْنَاءَ

**“Na mti utokao katika mlima wa Sinai.”**

Maana yake: mti wa zeituni. Na *Twur* ni mlima. Na wakasema baadhi ya wanazuoni: “Hakika unaitwa *Twur* ukiwa na miti na ukiwa mkavu (bila ya miti) huitwa *Jabal*, sio *Twur*. Na Allah تعالی Anajua zaidi. Na *Twur Sinai* ni sawa na *Twur Sinin*, na huo ni mlima ambao Allah تعالی Alizungumza na Musa bin ‘Imran عليه السلام, na pembezoni mwake (wa mlima) ipo miti ya mizeituni. Na Kauli Yake:

تَنْبُتُ بِالذُّهْنِ

**“Unatoa mafuta.”** Wamesema baadhi ya wanazuoni: wa sarufi ya lugha ya kiarabu wamesema: Herufi “*Baa*” imekuja kama ziada, hapa “*Baa*” maana yake ni kama kiunganishi kwa maana kutoa mafuta, kama wanavyosema Waarabu: ‘Fulani amenyoosha kwa mikono yake, yaani mkono wake’. Na ama kwa ile kauli inayodhamini kitendo, ina maana ya kutoa mafuta au inakuja na mafuta. Na kwa hiyo Akasema:

وَصَيِّغِ

**“Na kuwa kitoweo.”** Maana yake: Kiungo, kulingana na Qatadah.<sup>1</sup>

لِللَّكَلِينِ ﴿١٩﴾

**“Kwa walao.”** Maana yake: kwayo munafaidika kwa mafuta na kiungo. Na amepokea ‘Abd bin Humayd رحمه الله تعالی katika Musnad na Tafsiyr yake kutoka kwa ‘Umar رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«اتَّبِعُوا بِالزَّيْتِ وَادَّهِنُوا بِهِ فَإِنَّهُ يَخْرُجُ مِنْ شَجَرَةٍ مُبَارَكَةٍ»

**“Kuleni mafuta (ya zeituni) kama kiungo na jipakeni kwani yanatoka kutoka katika mti wenye baraka.”**

<sup>1</sup> Al-Muntakhab cha ‘Abd bin Humayd 13, At-Tirmidhiy 1851 na Ibn Maajah 3319.

Na pia imepokewa na At-Tirmidhiy na Ibn Maajah<sup>1</sup>. Na Kauli Yake:

وَلَنْ لَكُمْ فِي الْأَنْعَامِ لَعِبْرَةٌ نَسَقِيكُمْ مِمَّا فِي بُطُونِهَا وَلَكُمْ فِيهَا مَنَافِعُ كَثِيرَةٌ وَمِنْهَا تَأْكُلُونَ  
 وَعَلَيْهَا وَعَلَى الْفَالِكِ تَحْمَلُونَ ﴿٧﴾

**“Na hakika munayo mazingatio makubwa katika nyama hoa - Tunakunywesheni katika vile vilivyomo matumboni mwao, na nyinyi mnapata katika hao manufaa mengi, na pia mnawala. Na juu yao na juu ya marikebu mnabebwa.” (16:7)**

Anataja Allah تعالى kwa Aliyojaalia kwa Kuumba wanyama hoa kwa manufaa, kwani wanakunywa maziwa yao yanayotoka baina ya choo na damu, wanakula nyama zao na kuvaa nguo zinazotengenezwa na manyoya yao na nywele zao, wanawapanda na kubeba mizigo mizito migongoni mwao kwa ardhi zilizo mbali. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَتَحْمَلُ أَثْقَالَكُمْ إِلَىٰ بَلَدٍ لَّئِمَّ تَكُونُوا بَلِيغِيهِ إِلَّا بِشِقِّ الْأَنْفُسِ ۗ إِنَّ رَبَّكُمْ لَرَءُوفٌ  
 رَّحِيمٌ ﴿٧﴾

**“Na wanyama hao hubeba mizigo yenu kupeleka katika miji msiyoweza kuifika isipokuwa kwa mashaka na taabu. Hakika Mola wenu Mlezi ni Mpole sana na Mwenye Rehema nyingi.” (16:7)**

Na Amesema Aliyetukuka:

أُولَئِكَ يَرَوْنَ أَنَا خَلَقْنَا لَهُمْ مِمَّا عَمِلَتْ أَيْدِينَا أَنْعَامًا فَهُمْ لَهَا مَالِكُونَ ﴿٧﴾ وَذَلَّلْنَاهَا لَهُمْ  
 فَمِنْهَا رَكُوبُهُمْ وَمِنْهَا يَأْكُلُونَ ﴿٨﴾ وَهُمْ فِيهَا مَنَّاعٌ وَمَشَارِبٌ أَفْلا يَشْكُرُونَ ﴿٩﴾

**“Je, hawaoni ya kwamba Tumewaumbia katika vile ilivyovifanya Mikono Yetu wanyama hawa wanaowamiliki. Na Tumewatiishia wanyama hao, basi baadhi yao wanawapanda na wengine wao wanawala. Na katika hao wanapata manufaa mengi mengineyo na vinywaji. Basi je, hawashukuru?” (36:71-73).**

<sup>1</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 6:95.



وَلَقَدْ أَرْسَلْنَا نُوحًا إِلَىٰ قَوْمِيهِ فَقَالَ يَنْقُورِ اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِنْ إِلَهٍ غَيْرُهُ ۗ أَفَلَا تَتَّقُونَ ﴿١٨﴾  
 فَقَالَ الْمَلَأُوا الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَوْمِيهِ مَا هَذَا إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُرِيدُ أَنْ  
 يَتَفَضَّلَ عَلَيْكُمْ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَأَنْزَلَ مَلَائِكَةً مَا سَمِعْنَا بِهَذَا فِي آبَائِنَا الْأُولَىٰ ﴿١٩﴾  
 إِنَّ هُوَ إِلَّا رَجُلٌ بِيَمِينِنَا فَتَرَبَّصُوا بِهِ حَتَّىٰ حِينٍ ﴿٢٠﴾

23. Na hakika Tulimtuma Nuuu kwa watu wake, akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Allaah. Nyinyi hamna mungu asiyekuwa Yeye. Basi je! Hamuogopi?

24. Walisema wale wakuu waliokufuru katika watu wake: Huyu si chochote ila ni mtu tu kama nyinyi. Anataka kujipa ubora juu yenu. Na lau kuwa Allah Amependa basi yakini Angeliteremsha Malaika. Hatukusikia haya kwa baba zetu wa zamani.

25. Huyu si lolote ila ni mtu mwenye wazimu. Basi mngojeeni tu kwa muda.

### Kisa cha Nuhu عليه السلام na Watu Wake

Anatupasha habari Allah تعالى Kuhusu Nuuu عليه السلام pale Alipomtuma kwa watu wake kuwaonya adhabu ya Allah تعالى iliyo kali, kisasi Chake. Na Kumuadhibu kila aliyemshirikisha Allah تعالى na kuhalifu Amri Zake na kuwakadhibisha Mitume Yake:

فَقَالَ يَنْقُورِ اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِنْ إِلَهٍ غَيْرُهُ ۗ أَفَلَا تَتَّقُونَ ﴿١٨﴾

**“Akasema: Enyi watu wangu! Muabuduni Allah. Nyinyi hamna mungu asiyekuwa Yeye. Basi je! Hamuogopi?”**

Maana yake: je, hamumuogopi Allah تعالى pale munapomshirikisha katika lbada? Wakasema wakuu nao ni mabwana na viongozi wao:

مَا هَذَا إِلَّا بَشَرٌ مِّثْلُكُمْ يُرِيدُ أَنْ يَتَفَضَّلَ عَلَيْكُمْ

**“Huyu si chochote ila ni mtu tu kama nyinyi. Anataka kujipa ubora juu yenu.”**

Maana yake: anajiweka juu yenu na kutaka kujifanya mkubwa kwa kudai unabii, lakini yeye ni mwanadamu kama nyinyi. Kwa minajili hiyo vipi atateremshiwa wahyi ilhali nyinyi hamteremshiwi?

وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَأَنْزَلَ مَلَائِكَةً

**“Na lau kuwa Allah Angependa basi yakini Angeliteremsha Malaika.”**

Maana yake: Lau Angelitaka Allah تعالى kumtuma Nabii, Angelimtuma Malaika kutoka Kwake, sio mwanadamu. Hatujasikia kabisa jambo hilo – yaani kutumwa kwa mwanadamu kwa baba zetu wa mwanzo, wanamaanisha kwa hilo watangu wao na mababu zao waliopita. Na Kauli Yake:

إِنْ هُوَ إِلَّا رَجُلٌ بِمِثْلِ مَا أَنْزَلْنَا

**“Huyu si lolote ila ni mtu mwenye wazimu.”** Maana yake: Ana wazimu katika madai yake kuwa Allah تعالى Amemtuma na kumchagua miongoni mwenu kupata wahyi.

فَقَرَّبُوا إِلَيْهِ كَوْنًا حَتَّىٰ يَسْمَعُوا كَلِمَ اللَّهِ

**“Basi mungojeeni tu kwa muda.”**

Maana yake: ngojeeni mpaka afe, na subirini naye kwa muda hata mtakapopumzika naye (atakapoondoka).

قَالَ رَبِّ انصُرْنِي بِمَا كَدَّبُونِ ﴿٢٦﴾ فَأَوْحَيْنَا إِلَيْهِ أَنْ اصْنَعْ الْفُلْكَ بِأَعْيُنِنَا وَّوْحَيْنَا فَإِذَا جَاءَ أَمْرُنَا وَفَارَ التَّنُّورُ فَاسْلُكْ فِيهَا مِنْ كُلِّ زَوْجَيْنِ اثْنَيْنِ وَأَهْلَكَ إِلَّا مَنْ سَبَقَ عَلَيْهِ الْقَوْلُ مِنْهُمْ وَلَا تُخَنِّطْنِي فِي الَّذِينَ ظَلَمُوا إِنَّهُمْ مُغْرَقُونَ ﴿٢٧﴾ فَإِذَا اسْتَوَيْتَ أُنْتِ وَمَنْ مَعَكَ عَلَى الْفُلِّ فَقُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي نَجَّيْنَا مِنَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٢٨﴾ وَقُلْ رَبِّ أَنْزِلْنِي مُنْزَلًا مُبَارَكًا وَأَنْتَ خَيْرُ الْمُنْزِلِينَ ﴿٢٩﴾ إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ وَإِنْ كُنَّا لَمُبْتَلِينَ ﴿٣٠﴾

**26. Akasema (Nuhu): Mola wangu Mlezi! Ninusuru kwa kuwa wamenikanusha.**

**27. Tukampa wahyi: Unda jahazi mbele ya Macho Yetu na uongozi**

**Wetu! Basi itapofika Amri Yetu na ikafurika tanuri, hapo waingize ndani yake wa kila namna dume na jike, na ahali zako, isipokuwa yule ambaye katika wao juu yake imekwishatangulia kauli. Wala usinitajie hao waliodhulumu. Kwani hao bila ya shaka watazamishwa.**

**28. Basi utakapotulia wewe na walio pamoja nawe humo marikebuni, sema: Alhamdulillah Sifa zote njema ni za Allah, Aliyetuokoa na watu madhalimu!**

**29. Na sema: Mola wangu Mlezi! Niteremshe mteremsho wenye baraka, na Wewe ni Mbora wa wateremshaji.**

**30. Hakika katika hayo yapo mazingatio. Na kwa yakini Sisi ni wenye Kuwafanyia mtihani.**

Allah تعالی Anatupasha habari kuwa Nuuh عليه السلام alimuomba Mola wake Mlezi amsaidie dhidi ya watu wake, kama Anavyotaja Allah تعالی katika Aya nyingine:

فَدَعَا رَبَّهُ أَنِّي مَغْلُوبٌ فَأَنْتَصِرْ ﴿٥٤﴾

**“Ndipo akamuomba Mola wake Mlezi akasema: ‘Kwa hakika mimi nimeshindwa, basi ninusuru.” (54:10).**

Na hapa Akasema:

رَبِّ أَنْصُرْنِي بِمَا كَذَّبْتَنِي ﴿٥٥﴾

**“Mola wangu Mlezi! Ninusuru kwa kuwa wamenikanusha.”**

Hapo, Allah تعالی Alimuamuru atengeneze jahazi, lililo barabara na imara. Na kwayo abebe kila jozi ya mnyama, yaani dume na jike kwa kila aina ya mnyama, mimea, matunda na kadhalika. Pia alihitajika awachukue watu wake:

إِلَّا مَنْ سَبَقَ عَلَيْهِ الْقَوْلُ مِنْهُمْ ۗ

**“Isipokuwa yule ambaye katika wao juu yake imekwishatangulia kauli.”**

Maana yake: Wale ambao Allah تعالی tayari Amewaandikia kuangamia. Na hao ni wale katika familia yake ambao hawakuamini kama mtoto na mke wake. Na Allah تعالی Anajua zaidi. Na Kauli Yake:

وَلَا تُخْطِئِي فِي الَّذِينَ ظَلَمُوا إِنَّهُمْ مُعْرَقُونَ ﴿٢٣﴾

**“Wala usinitajie hao waliodhulumu. Kwani hao bila ya shaka watazamishwa.”**

Maana yake: unaposhuhudia mvua kubwa ikinyesha, usiwaonee huruma wala sikitiko watu wako, au kutumainia muda wa ziada kwao ili wapate kuamini, kwani tayari Nimepitisha Kuwagarikisha na watakufa katika hali ya ukafiri na ushirikina. Kisa hiki tayari tumekieleza kwa kina katika Sura Huud, hivyo kutokuwa na haja ya kukirudia tena hapa. Na Kauli Yake:

فَإِذَا أَسْتَوَيْتَ أَنْتَ وَمَنْ مَعَكَ عَلَى الْفُلِّ فَقُلِ الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي نَجَّنا مِنَ الْغَوَامِرِ

الظَّالِمِينَ ﴿٢٤﴾

**“Basi utakapotulia wewe na walio pamoja nawe humo marikebuni, sema: Alhamdulillah Sifa zote njema ni za Allah, Aliyetuokoa na watu madhalimu!”**

Hii ni kama Alivyosema:

وَجَعَلَ لَكُم مِّنَ الْفُلِّ وَالْأَنْعَامِ مَا تَرْكَبُونَ ﴿٢٥﴾ لِتَسْتَوُوا عَلَى ظُهُورِهِمْ ثُمْ تَذْكُرُوا نِعْمَةَ

رَبِّكُمْ إِذَا اسْتَوَيْتُمْ عَلَيْهِ وَتَقُولُوا سُبْحَانَ الَّذِي سَخَّرَ لَنَا هَذَا وَمَا كُنَّا لَهُ مُقْرِنِينَ ﴿٢٦﴾

وَإِنَّا إِلَىٰ رَبِّنَا لَمُنْقَلِبُونَ ﴿٢٧﴾

**“..Na Akakufanyieni marikebu na wanyama munao wapanda. Ili mkae vizuri migongoni mwao, kisha mkumbuke Neema za Mola wenu Mlezi mnapokaa sawa sawa juu yao na msemi: Ametakasika Aliyemfanya huyu atutumikie, na tusingeliweza kufanya haya wenyewe. Na bila shaka sisi tutarudi kwa Mola wetu Mlezi.”**  
(43:12-14).

Na kwa hakika Nuuh عليه السلام alifuata vilivyo aliyoamriwa, kama Anavyosema Allah تعالى:

\* وَقَالَ أَرَأَيْتُمْ فِيهَا بِسْمِ اللَّهِ جَعَلَهَا وَمُرْسَنَهَا

**“Na akasema (Nuuh): Pandeni humo kwa Jina la Allah kuwe kwenda kwake na kusimama kwake...”** (11:41).

Hapo akataja Aliyetukuka mwanzo wa safari yake na mwisho wake. Na Akasema Aliyetukuka:

وَقُلْ رَبِّ أَنْزِلْنِي مُنْزَلًا مُّبَارَكًا وَأَنْتَ خَيْرُ الْمُنزِلِينَ ﴿٢٣﴾

***“Na sema: Mola wangu Mlezi! Niteremshe mteremsho wenye baraka, na Wewe ni Mbora wa wateremshaji.”***

إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ

***“Hakika katika hayo yapo mazingatio.”***

Maana yake: Katika tukio hili, ambalo ni kuwaokoa Waumini na kuwaangamiza makafiri zipo ishara, yaani hoja na dalili zilizo wazi juu ya ukweli wa Manabii kwa waliokuja nayo kutoka kwa Allah تعالی. Na hakika ni kuwa Allah Aliyetukuka ni Mwenye Kufanya Alitakalo na ni Muweza na Anajua kila kitu. Na Kauli Yake:

وَإِنْ كُنَّا لَمُبْتَلِينَ ﴿٢٤﴾

***“Na kwa yakini Sisi ni wenye Kuwafanyia mtihani.”***

Maana yake: Tunawajaribu waja Wetu kwa kuwatumia Mitume.

\* \* \*

ثُمَّ أَنْشَأْنَا مِنْ بَعْدِهِمْ قَوْمًا آخَرِينَ ﴿٣١﴾ فَأَرْسَلْنَا فِيهِمْ  
 رَسُولًا مِّنْهُمْ أَنْ آعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِنْ إِلَهٍ غَيْرُهُ ۗ أَفَلَا  
 تَتَّقُونَ ﴿٣٢﴾ وَقَالَ الْمَلَأُ مِنَ الْقَوْمِ الَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا  
 بِلِقَاءِ الْآخِرَةِ وَأَتْرَفْنَاهُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا مَا هَذَا إِلَّا بَشَرٌ  
 مِّثْلُكُمْ يَأْكُلُ مِمَّا تَأْكُلُونَ مِنْهُ وَيَشْرَبُ مِمَّا تَشْرَبُونَ ﴿٣٣﴾  
 وَلَئِنْ أَطَعْتُم بَشَرًا مِّثْلَكُمْ إِنَّكُمْ إِذَا لَخَسِرُونَ ﴿٣٤﴾ أَيْعِدْكُمْ  
 أَنْكُمْ إِذَا مِتُّمْ وَكُنْتُمْ تُرَابًا وَعِظْمًا أَنْكُمْ تُحْرَجُونَ ﴿٣٥﴾  
 \* هَيَاتَ هَيَاتَ لِمَا تُوعَدُونَ ﴿٣٦﴾ إِنَّ هِيَ إِلَّا حَيَاتُنَا  
 الدُّنْيَا نَمُوتُ وَنَحْيَا وَمَا نَحْنُ بِمَبْعُوثِينَ ﴿٣٧﴾ إِنَّ هُوَ إِلَّا  
 رَجُلٌ أَفْتَرَى عَلَى اللَّهِ كَذِبًا وَمَا نَحْنُ لَهُ بِمُؤْمِنِينَ ﴿٣٨﴾  
 قَالَ رَبِّ انصُرْنِي بِمَا كَذَّبُونَ ﴿٣٩﴾ قَالَ عَمَّا قَلِيلٍ  
 لَيُصْبِحُنَّ نَادِمِينَ ﴿٤٠﴾ فَأَخَذْتَهُمُ الصَّيْحَةَ بِالْحَقِّ  
 فَجَعَلْنَاهُمْ غُنَاءً ۖ فَبَعْدًا لِلْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٤١﴾ ثُمَّ أَنْشَأْنَا  
 مِنْ بَعْدِهِمْ قَوْمًا آخَرِينَ ﴿٤٢﴾ مَا تَسْبِقُ مِنْ أُمَّةٍ  
 أَجَلَهَا وَمَا يَسْتَعْجِرُونَ ﴿٤٣﴾ ثُمَّ أَرْسَلْنَا نُوحًا مِّنْ قَوْمِ  
 جَاءَ أُمَّةٍ رَّسُولًا كَذَّبُوهُ ۖ فَاتَّبَعْنَا بَعْضَهُمْ بَعْضًا وَجَعَلْنَاهُمْ  
 أَحَادِيثَ ۖ فَبَعْدًا لِّقَوْمٍ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٤٤﴾ ثُمَّ أَرْسَلْنَا  
 مُوسَىٰ وَأَخَاهُ هَارُونَ بِآيَاتِنَا وَسُلْطٰنٍ مُّبِينٍ ﴿٤٥﴾ إِلَىٰ  
 فِرْعَوْنَ وَمَلَئِهِ فَاسْتَكْبَرُوا وَكَانُوا قَوْمًا عَالِينَ ﴿٤٦﴾  
 فَقَالُوا أَنُؤْمِنُ لِبَشَرَيْنِ مِثْلِنَا وَقَوْمُهُمَا لَنَا عٰبِدُونَ ﴿٤٧﴾  
 فَكَذَّبُوهُمَا فَكَانُوا مِنَ الْمُهْلَكِينَ ﴿٤٨﴾ وَقَدْ آتَيْنَا  
 مُوسَىٰ الْكِتَابَ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٤٩﴾

ثُمَّ أَنْشَأْنَا مِنْ بَعْدِهِمْ قَوْمًا آخَرِينَ ﴿٣١﴾ فَأَرْسَلْنَا فِيهِمْ  
 رَسُولًا مِّنْهُمْ أَنْ آعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِنْ إِلَهٍ غَيْرُهُ ۗ أَفَلَا  
 تَتَّقُونَ ﴿٣٢﴾ وَقَالَ الْمَلَأُ مِنَ الْقَوْمِ الَّذِينَ كَفَرُوا وَكَذَّبُوا  
 بِلِقَاءِ الْآخِرَةِ وَأَتْرَفْنَاهُمْ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا مَا هَذَا إِلَّا بَشَرٌ  
 مِّثْلُكُمْ يَأْكُلُ مِمَّا تَأْكُلُونَ مِنْهُ وَيَشْرَبُ مِمَّا تَشْرَبُونَ ﴿٣٣﴾  
 وَلَئِنْ أَطَعْتُم بَشَرًا مِّثْلَكُمْ إِنَّكُمْ إِذَا لَخَسِرُونَ ﴿٣٤﴾ أَيْعِدْكُمْ  
 أَنْكُمْ إِذَا مِتُّمْ وَكُنْتُمْ تُرَابًا وَعِظْمًا أَنْكُمْ تُحْرَجُونَ ﴿٣٥﴾  
 \* هَيَاتَ هَيَاتَ لِمَا تُوعَدُونَ ﴿٣٦﴾ إِنَّ هِيَ إِلَّا حَيَاتُنَا  
 الدُّنْيَا نَمُوتُ وَنَحْيَا وَمَا نَحْنُ بِمَبْعُوثِينَ ﴿٣٧﴾ إِنَّ هُوَ إِلَّا  
 رَجُلٌ أَفْتَرَى عَلَى اللَّهِ كَذِبًا وَمَا نَحْنُ لَهُ بِمُؤْمِنِينَ ﴿٣٨﴾  
 قَالَ رَبِّ انصُرْنِي بِمَا كَذَّبُونَ ﴿٣٩﴾ قَالَ عَمَّا قَلِيلٍ  
 لَيُصْبِحُنَّ نَادِمِينَ ﴿٤٠﴾ فَأَخَذْتَهُمُ الصَّيْحَةَ بِالْحَقِّ  
 فَجَعَلْنَاهُمْ غُنَاءً ۖ فَبَعْدًا لِلْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٤١﴾ ثُمَّ أَنْشَأْنَا  
 مِنْ بَعْدِهِمْ قَوْمًا آخَرِينَ ﴿٤٢﴾ مَا تَسْبِقُ مِنْ أُمَّةٍ  
 أَجَلَهَا وَمَا يَسْتَعْجِرُونَ ﴿٤٣﴾ ثُمَّ أَرْسَلْنَا نُوحًا مِّنْ قَوْمِ  
 جَاءَ أُمَّةٍ رَّسُولًا كَذَّبُوهُ ۖ فَاتَّبَعْنَا بَعْضَهُمْ بَعْضًا وَجَعَلْنَاهُمْ  
 أَحَادِيثَ ۖ فَبَعْدًا لِّقَوْمٍ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٤٤﴾ ثُمَّ أَرْسَلْنَا  
 مُوسَىٰ وَأَخَاهُ هَارُونَ بِآيَاتِنَا وَسُلْطٰنٍ مُّبِينٍ ﴿٤٥﴾ إِلَىٰ  
 فِرْعَوْنَ وَمَلَئِهِ فَاسْتَكْبَرُوا وَكَانُوا قَوْمًا عَالِينَ ﴿٤٦﴾  
 فَقَالُوا أَنُؤْمِنُ لِبَشَرَيْنِ مِثْلِنَا وَقَوْمُهُمَا لَنَا عٰبِدُونَ ﴿٤٧﴾  
 فَكَذَّبُوهُمَا فَكَانُوا مِنَ الْمُهْلَكِينَ ﴿٤٨﴾ وَقَدْ آتَيْنَا  
 مُوسَىٰ الْكِتَابَ لَعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٤٩﴾

31. *Kisha Tulileta baada yao umma nyingine.*

32. *Tukawapelekea Mtume miongoni mwao, kuwaambia: Muabuduni Allah! Hamna mungu asiyekuwa Yeye. Jee, hamuogopi?*

33. *Na wakubwa katika watu wake waliokufuru na wakakanusha mkutano wa Akhera, na Tukawadekeza kwa starehe katika maisha ya dunia, walisema: Huyu si chochote ila ni binadamu kama nyinyi; anakula mlacho, na anakunywa mnywacho.*

34. *Na nyinyi mkimtii mtu kama nyinyi basi hakika mtakuwa khasarani.*

35. *Hivyo anakuahidini ati ya kwamba mtakapo kufa na mkawa udongo na mifupa kuwa mtatolewa?*

36. *Hayawi! Hayawi hayo mnayoahidiwa.*

37. *Hapana ila uhai wetu wa duniani tu, tunakufa na kuishi basi. Wala sisi hatutafufuliwa.*

38. *Huyu si lolote ila ni mtu anayemzulia Allah uongo, wala Sisi sio wa kumuamini.*

39. *Akasema: Mola wangu Mlezi! Ninusuru kwa sababu wanarikanusha.*

40. *(Allah) Akasema: Baada ya muda mchache watakuwa wenye kujuta.*

41. *Basi ukawanyakua ukelele kwa haki, na Tukawafanya kama takataka zinazoelea juu ya maji. Ikapotelea mbali kaumu ya madhalimu!.*

### Kisa cha 'Adi au Thamuud

Anatupasha habari Allah عليه السلام kuwa baada ya kaumu ya Nuuh عليه السلام, kulikuja kaumu nyingine. Panasemwa: Muradi wake ni 'Adi, kwani wao walikuja baada ya kaumu ya Nuuh عليه السلام. Na panasemwa: Muradi wa kaumu hii ni ya Thamuud, kwa Kauli ya Aliyetukuka:

فَأَخَذْتَهُمُ الصَّيْحَةَ بِالْحَقِّ

*"Basi ukawanyakua ukelele kwa haki".*

Allah تعالی Aliwatumia kutoka miongoni mwao, naye akawaita kumuabudu Allah تعالی Peke Yake bila ya kumshirikisha, lakini wakamkadhibisha, wakampinga na kukataa kumfuata kwa kuwa alikuwa mwanadamu kama wao, nao walikataa kumfuata Mtume mwanadamu. Wakakanusha kukutana kwao na Allah تعالی Siku ya Kiyama na wakakataa kufufuliwa kimwili.

Hivyo, wakasema:

أَيَعِدُّكُمْ أَنْكُمْ إِذَا مِتُّمْ وَكُنْتُمْ تُرَابًا وَعِظْمًا أَنْكُمْ تُخْرَجُونَ ﴿٣١﴾ \* هَيَّاتَ هَيَّاتَ لِمَا  
تُوعَدُونَ ﴿٣٢﴾

***“Hivyo anakuahidini ati ya kwamba mutakapokufa na mukawa udongo na mifupa kuwa mutatolewa? Hayawi! Hayawi hayo munayoa hidiwa.”***

Maana yake: hilo ni jambo lililo mbali sana.

إِنَّ هُوَ إِلَّا رَجُلٌ افْتَرَىٰ عَلَى اللَّهِ كَذِبًا

***“Huyu si lolote ila ni mtu anayemzulia Allah uongo.”***

Maana yake: kwa aliyokuja nayo katika risala, kuonya kwake na ahadi ya ufufuo.

وَمَا نَحْنُ لَهُ بِمُؤْمِنِينَ ﴿٣٣﴾ قَالَ رَبِّ انصُرْنِي بِمَا كَذَّبْتَنِي ﴿٣٤﴾

***“Wala Sisi sio wa kumuamini. Akasema: Mola wangu Mlezi! Ninusuru kwa sababu wananikanusha.”***

Maana yake: Mtume aliomba dhidi ya watu wake na kumtaka Mola wake Mlezi Amnusuru dhidi yao. Mola wake Akamjibu dua yake.

قَالَ عَمَّا قَلِيلٍ لِّيُصْبِحَنَّ نَدِيمِينَ ﴿٣٥﴾

***“(Allah) Akasema: Baada ya muda mchache watakuwa wenye kujuta.”***

Maana yake: Kwa upinzani wao na inadi yao katika kukataa ujumbe uliowaitea.



فَأَخَذْتَهُمُ الصَّيْحَةَ بِالْحَقِّ

**“Basi ukawanyakua ukelele kwa haki”.**

Maana yake: Wakastahiki hilo kutoka kwa Allah تعالى kwa ukafiri wao na dhuluma yao. Na maana ya dhahiri kuhusu hilo ni kuwa huo ukelele uliochang'anywa na upepo mkali wa baridi,

تُدْمِرُ كُلَّ شَيْءٍ بِأَمْرِ رَبِّهَا فَأَصْبَحُوا لَا يُرَىٰ إِلَّا مَسَكِنَتُهُمْ

**“Unaongamiza kila kitu kwa Amri ya Mola wake Mlezi. Basi wakawa si wenye kuonekana tena ila nyumba zao...” (46:25).**

فَجَعَلْنَاهُمْ غُرَاءً

**“Na Tukawafanya kama takataka”.**

Maana yake: Wakafa na kuhiliki, kama takataka na uchafu ulioachwa na mafuriko, nacho ni kitu kidogo sana na kisicho na maana ambacho hakina faida kwa yeyote.

فَبُعْدًا لِلْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٤٦﴾

**“Ikapotelea mbali kaumu ya madhalimu!”**

Hii ni kama Kauli ya Aliyetukuka:

وَمَا ظَلَمْنَاهُمْ وَلَكِن كَانُوا هُمُ الظَّالِمِينَ ﴿٤٧﴾

**“Wala Sisi Hatukuwadhulumu, bali wao wenyewe walikuwa madhalimu.” (43:76)**

Maana: kwa ukafiri wao, inadi yao na kwenda kwao kinyume na Mtume wa Allaah, hivyo wajihadhari wasikiao katika kukadhibisha Mitume wao.

ثُمَّ أَنْشَأْنَا مِنْ بَعْدِهِمْ قُرُونًا آخَرِينَ ﴿٤٨﴾ مَا تَسْبِقُ مِنْ أُمَّةٍ أَجَلَهَا وَمَا يَسْتَسْخِرُونَ

﴿٤٩﴾ ثُمَّ أَرْسَلْنَا رَسُولَنَا تَتْرًا كُلًّا مَا جَاءَ أُمَّةً رُسُوهَا كَذَّبُوهُ فَاتَّبَعْنَا بَعْضَهُمْ بَعْضًا

وَجَعَلْنَاهُمْ أَحَادِيثَ فَبُعْدًا لِقَوْمٍ لَا يُؤْمِنُونَ ﴿٥٠﴾

**42. Kisha Tukaleta baada yao vizazi vingine.**

**43. Hapana umma uwezao kutanguliza ajali yake wala kuikawiza.**

**44. Kisha Tukawatuma Mitume Wetu, mmoja baada ya mmoja. Kila ummah alipowafikia Mtume wao walimkanusha. Tukawafuatanisha hawa baada ya hawa, na Tukawafanya ni hadithi za kusimuliwa. Wakapotelea mbali watu wasioamini.**

### Kutajwa Mataifa Mengine

Anasema Aliyetukuka:

ثُمَّ أَنْشَأْنَا مِنْ بَعْدِهِمْ قُرُونًا آخَرِينَ ﴿١٥﴾

**“Kisha Tukaleta baada yao vizazi vingine.”**

Maana yake: Mataifa na watu.

مَا تَسْبِقُ مِنْ أُمَّةٍ أَجَلَهَا وَمَا يَسْتَعْجِرُونَ ﴿٥﴾

**“Hapana umma uwezao kutanguliza ajali yake wala kuikawiza.”  
(15:5),**

Maana yake: Bali wanachukua hesabu kulingana na waliokadiriwa na Aliyetukuka katika Kitabu Chake kilichohifadhiwa na Elimu Yake kabla ya Kuumbwa umma baada ya umma, karne baada ya karne, kizazi baada ya kizazi, na waliofuata baada ya waliotangulia.

ثُمَّ أَرْسَلْنَا رُسُلَنَا تَتْرًا ﴿٥٤﴾

**“Kisha Tukawatuma Mitume Wetu, mmoja baada ya mmoja.”**

Amesema Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: “Hiyo ina maana kufuata baadhi yao wengine”<sup>1</sup>. Na hii ni kama Kauli Yake:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 19:34.

وَلَقَدْ بَعَثْنَا فِي كُلِّ أُمَّةٍ رَسُولًا أَنِ اعْبُدُوا اللَّهَ وَاجْتَنِبُوا الصَّغُورَ ۗ فَمِنْهُمْ مَن هَدَى اللَّهُ وَمِنْهُمْ مَن حَقَّتْ عَلَيْهِ الضَّلَالَةُ

***“Na bila shaka Tulimpeleka Mtume katika kila Umma ya kwamba, ‘Muabuduni Allah na muepukeni (Iblisi) muovu. Basi wako miongoni mwao ambao Allah Amewaongoa, na wako miongoni mwao ambao upotofu (upotevu) umethubutu juu yao.....” (16:36)***

Na Kauli Yake:

كُلَّ مَا جَاءَ أُمَّةً رَسُولًا كَذَّبُوهُ

***“Kila umma alipowafikia Mtume wao walimkanusha.”***

Maana: Wengi miongoni mwao. Hii ni kama Kauli Yake Aliyetukuka:

يَحْسِرَةٌ عَلَى الْعِبَادِ ۗ مَا يَأْتِيهِمْ مِّن رَّسُولٍ إِلَّا كَانُوا بِهِ يَسْتَهْزِءُونَ ﴿٣٠﴾

***“Inafaa kusikitikiwa hawa waja; hawakuwajia Mtume yeyote ila walikuwa wanamfanyia mzaha.” (36:30).***

Na Kauli Yake:

فَاتَّبَعْنَا بَعْضَهُم بَعْضًا

***“Tukawafuatanisha hawa baada ya hawa.”***

Maana yake: Tuliwaangamiza, kama Kauli Yake:

وَكَمْ أَهْلَكْنَا مِن الْقُرُونِ مِن بَعْدِ نُوحٍ

***“Na karne ngapi Tumeziangamiza baada ya Nuu...” (17:17).***

Na Kauli Yake:

وَجَعَلْنَاهُمْ أَحَادِيثَ

***“Na Tukawafanya ni hadithi za kusimuliwa.”***

Maana yake: Visa na mazingatio kwa watu. Hii ni kama Kauli Yake:

فَجَعَلْنَاهُمْ أَحَادِيثَ وَمَزَقْنَاهُمْ كُلَّ مُمَزِقٍ

***“Basi Tukawafanya ni masimulizi tu. na Tukawatawanya tawanya.” (34:19)***

ثُمَّ أَرْسَلْنَا مُوسَىٰ وَأَخَاهُ هَارُونَ بِآيَاتِنَا وَسُلْطٰنٍ مُّبِينٍ ﴿٣١﴾ إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَمَلَئِهِ  
 فَاسْتَكْبَرُوا وَكَانُوا قَوْمًا عٰلِينَ ﴿٣٢﴾ فَقَالُوا أَنْتُمْ لِبَشَرَيْنِ مِثْلِنَا وَقَوْمُهُمَا لَنَا عِبْدُونَ  
 ﴿٣٣﴾ فَكَذَّبُوهُمَا فَكَانُوا مِنَ الْمُهْلَكِينَ ﴿٣٤﴾ وَلَقَدْ ءَاتَيْنَا مُوسَىٰ الْكِتٰبَ لَعَلَّهُمْ  
 يَهْتَدُونَ ﴿٣٥﴾

**45. Kisha Tukamtuma Musa na nduguye, Haarun, pamoja na ishara Zetu na hoja zilizo wazi.**

**46. Kumuendea Firauni na wakuu wake. Lakini walijivuna, nao walikuwa watu wajeuri.**

**47. Wakasema: Je, tuwaamini wanadamu wawili hawa kama sisi, na ambao watu wao ni watumwa wetu?**

**48. Basi wakawakanusha, na wakawa miongoni mwa walioangamizwa.**

**49. Na hakika Tulimpa Musa Kitabu ili wapate kuongoka.**

### Kisa cha Musa عليه السلام na Firauni

Anatupasha habari Aliyetukuka kuwa Alimtuma Mtume Wake, Musa عليه السلام na nduguye, Haarun عليه السلام kwa Firauni na wakuu wake kwa ishara, hoja nzito na dalili za wazi. Hata hivyo, Firauni na watu wake walitakabari kuwafuata na kutii amri zao kwa kuwa walikuwa binadamu, kama walivyokuwa kaumu zilizopita walivyokataa risala ya Mitume binadamu. Mioyo yao ilifanana, hivyo Allah تعالى Akamuangamiza Firauni na wakuu wake na Akawagharikisha wote siku moja tu. Na Akamteremshia Musa عليه السلام Kitabu, yaani Taurati, kilichokuwa na hukumu ndani yake, maamrisha na makatazo, na hiyo ni baada ya Kumuangamiza Firauni na watu wake (Wamisri) na Kuwapatiliza wao na adhabu ya kutoka kwa Mwenye Nguvu, Muweza wa Kufanya lolote Alitakalo.

Na baada ya Allah تعالى Kuitenemsha Taurati, Allah تعالى Hakuuamamiza Umma wowote kwa ujumla wake bali Aliwaamuru Waumini kupigana na makafiri, kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَلَقَدْ آتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ مِنْ بَعْدِ مَا أَهْلَكْنَا الْقُرُونَِ الْأُولَىٰ بِصَآئِرٍ لِلنَّاسِ وَهُدًى  
 وَرَحْمَةً لَّعَلَّهُمْ يَتَذَكَّرُونَ ﴿٤٣﴾

*“Na bila shaka Tulimpa Musa Kitabu baada ya kuziangamiza umma za kwanza zilizopita; kiwe kifumbua macho ya watu na kiwe uongofu na rehema, ili wapate kukumbuka.” (28:43).*

\* \* \*

وَجَعَلْنَا ابْنَ مَرْيَمَ وَأُمَّهُ آيَةً وَآوَيْنَهُمَا إِلَى رِبْوَةٍ ذَاتِ  
 قَرَارٍ وَمَعِينٍ ﴿٥٠﴾ يَتَأْتِيهَا الرُّسُلُ كُلُّوَا مِنَ الطَّيِّبَاتِ  
 وَأَعْمَلُوا صَالِحًا إِنِّي بِمَا تَعْمَلُونَ عَلِيمٌ ﴿٥١﴾ وَإِنَّ هَذِهِ  
 أُمَّتُكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَأَنَا رَبُّكُمْ فَاتَّقُونِ ﴿٥٢﴾ فَتَقَطَّعُوا  
 أَمْرَهُمُ بَيْنَهُمْ زُبُرًا ۖ كُلُّ حِزْبٍ بِمَا لَدَيْهِمْ فَرِحُونَ ﴿٥٣﴾  
 فَذَرَهُمْ فِي عَمَرَتِهِمْ حَتَّىٰ حِينٍ ﴿٥٤﴾ أَتَحْسِبُونَ أَنَّمَا  
 نُعِدُّهُم بِرِيءٍ مِنْ مَالٍ وَبَيْنٍ ﴿٥٥﴾ نُسَارِعُ هُمْ فِي الْخَيْرَاتِ  
 بَلْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٥٦﴾ إِنَّ الَّذِينَ هُمْ مِنْ خَشْيَةِ رَبِّهِمْ  
 مُشْفِقُونَ ﴿٥٧﴾ وَالَّذِينَ هُمْ بِآيَاتِ رَبِّهِمْ يُؤْمِنُونَ ﴿٥٨﴾  
 وَالَّذِينَ هُمْ بِرَبِّهِمْ لَا يُشْرِكُونَ ﴿٥٩﴾ وَالَّذِينَ يُؤْتُونَ مَا  
 آتَوْا وَقُلُوبُهُمْ وَجَلَةٌ أَنَّهُمْ إِلَىٰ رَبِّهِمْ رَاجِعُونَ ﴿٦٠﴾ أُولَٰئِكَ  
 يُسْرِعُونَ فِي الْخَيْرَاتِ وَهُمْ هَاهُنَا سَابِقُونَ ﴿٦١﴾ وَلَا تُكَلِّفُ  
 نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا ۗ وَالَّذِينَ كُنْتُمْ بِالْحَقِّ ۗ وَهُمْ لَا  
 يُظَالِمُونَ ﴿٦٢﴾ بَلْ قُلُوبُهُمْ فِي عَمَرَةٍ مِنْ هَذَا وَهُمْ أَعْتَدَلٌ مِنْ  
 دُونِ ذَٰلِكَ هُمْ لَهَا عَمِلُونَ ﴿٦٣﴾ حَتَّىٰ إِذَا أَخَذْنَا مُتْرَفِيهِمْ  
 بِالْعَذَابِ إِذَا هُمْ يَخْرُوتُونَ ﴿٦٤﴾ لَا تَجْرُؤُوا الْيَوْمَ ۖ إِنَّا  
 مِنَّا لَا نُنصِرُونَ ﴿٦٥﴾ قَدْ كَانَتْ آيَاتِي تُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ فَكُنْتُمْ  
 عَلَىٰ أَعْقَابِكُمْ تَنكِصُونَ ﴿٦٦﴾ مُسْتَكْبِرِينَ بِرِيءٍ سَمِيرًا  
 تَهْجُرُونَ ﴿٦٧﴾

وَجَعَلْنَا ابْنَ مَرْيَمَ وَأُمَّهُ آيَةً  
 وَآوَيْنَهُمَا إِلَى رِبْوَةٍ ذَاتِ قَرَارٍ  
 وَمَعِينٍ ﴿٥٠﴾

**50. Na Tukamfanya mwana  
 wa Maryam na mama  
 yake kuwa ni Ishara, na  
 Tukawapa makimbilio  
 kwenda mahali palipoinuka  
 penye utulivu na chem-  
 chem za maji.**

**Kutajwa kwa 'Isa عليه السلام  
 na Maryam**

Anatupasha habari Aliye-  
 tukuka kuhusu mja na  
 Mtume Wake, 'Isa bin  
 Maryam عليه السلام kwa Kuwa-  
 fanya kuwa Ishara kwa  
 watu, yaani hoja ya wazi  
 kwa Uweza Wake kwa  
 Anayotaka. Kwani Yeye  
 Alimuumba Adam عليه السلام  
 bila ya baba wala mama, na  
 Akamuumba Hawa' kutoka  
 kwa mwanamme bila  
 mwanamke, na Akamuumba  
 'Isa عليه السلام kutokana na  
 mwanamke bila mwana-  
 mume na Akawaumba  
 wanadamu waliobakia kwa  
 mwanamume na mwana-  
 mke. Na Kauli Yake:

وَأَوْبَيْنَهُمَا إِلَىٰ رَيْبَةٍ ذَاتِ قَرَارٍ وَمَعِينٍ ﴿٥٠﴾

**“Na Tukawapa makimbilio kwenda mahali palipoinuka penye utulivu na chemchem za maji.”**

Amepokea Adh-Dhahaak kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Ar-Rabwah” ni sehemu ya ardhi iliyonyanyuliwa, na ndio sehemu bora kwa kuotesha mimea”<sup>1</sup>. Na hivyo ndivyo alivyosema Mujaahid, 'Ikrima, Said bin Jubayr na Qataadah<sup>2</sup>.

Amesema Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما: Na Kauli Yake:

ذَاتِ قَرَارٍ

**“Penye utulivu.”**

Maana yake: Penye rutuba.

وَمَعِينٍ ﴿٥١﴾

**‘Chemchem za maji.’**

Maana yake: Chemchem ya maji yanayotiririka juu yake.”<sup>3</sup> Hivyo ndivyo alivyosema Mujaahid, 'Ikrimah, Sa'id bin Jubayr na Qatadah.<sup>4</sup> Na amesema Mujaahid: “Kilima kilicho sawa”<sup>5</sup>.

Na amesema Sa'id bin Jubayr:

ذَاتِ قَرَارٍ وَمَعِينٍ ﴿٥٢﴾

**“Mahali palipoinuka penye utulivu na chemchem za maji.”**

Maana yake: Ni maji yanayomiminika pole pole kutoka kwayo. Na wamesema Mujahid na Qatadah:

<sup>1</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 6:100. Sanadi yake ina dosari, Adh-Dhahaak hakupokea kutoka kwa Ibn Abbas.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 5:536, 537.

<sup>3</sup> Atw-Twabariy 19:38.

<sup>4</sup> Atw-Twabariy 19:39.

<sup>5</sup> Atw-Twabariy 19:38.

وَمَعِينٍ ﴿٥٠﴾

**“Na chemchem za maji.”**

Maana yaake: Maji yanayobubujika<sup>1</sup>.

Na amepokea Ibn Abi Haatim kuwa Said bin al-Musayyib amesema yafuatayo kuhusu Kauli Yake Aliyetukuka:

وَأَوَيْنَهُمَا إِلَىٰ رَبْوَةٍ ذَاتِ قَرَارٍ وَمَعِينٍ ﴿٥١﴾

**“Na Tukawapa makimbilio kwenda mahali palipoinuka penye utulivu na chemchem za maji.”**

Maana yake: Hiyo ni *Damaskas*<sup>2</sup>. Amesema: “Na imepokewa kutoka kwa ‘Abdallah bin Salaam, Al-Hasan, Zayd bin Aslam na Khaalid bin Ma’daan mfano wa hayo”. Na amepokea Ibn Abi Haatim رحمه الله تعالى kutoka kwa ‘Ikrima kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema, hiyo ni mito ya *Damaskas*<sup>3</sup>. Na amepokea Layth bin Abi Sulaym kuwa Mujaahid amesema:

وَأَوَيْنَهُمَا إِلَىٰ رَبْوَةٍ

**“Na Tukawapa makimbilio kwenda mahali palipoinuka.”**

Maana yake: ‘Isa عليه السلام na mamake walipokimbilia hifadhi huko *Damaskas* na ardhi tambarare pembezoni mwake<sup>4</sup>. Na amepokea ‘Abdur-Razzaaq kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuhusu Kauli ya Aliyetukuka:

إِلَىٰ رَبْوَةٍ ذَاتِ قَرَارٍ وَمَعِينٍ ﴿٥٢﴾

**“Penye utulivu na chemchem za maji.”**

Maana yake: Huo ni mji wa *Ramallah* huko *Palestina*.

Na kauli iliyo karibu katika kauli hizo ni ile iliyopokewa na al-‘Awfiy kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما kuhusu Kauli Yake:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 19:39.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 19:37.

<sup>3</sup> Al-Qurtwubiy 12:126.

<sup>4</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 6:100.



وَأَوْبَيْنُهُمَا إِلَىٰ رَبِّوَةٍ ذَاتِ قَرَارٍ وَمَعِينٍ ﴿٥٠﴾

**“Na Tukawapa makimbilio kwenda mahali palipoinuka penye utulivu na chemchem za maji.” (23:50)**

Maana yake: *Ma'iyin* ina maana ya maji yanayotiririka, nao ni mto uliotajwa na Allah تعالى:

قَدْ جَعَلَ رَبُّكِ تَحْتَكِ سَرِيًّا ﴿١٩﴾

**‘Hakika Mola wako Mlezi Amejaalia kijito cha maji chini yako.’ (19:24)**

Na hivyo ndivyo alivyosema Adh-Dhahaak na Qatadah:

إِلَىٰ رَبِّوَةٍ ذَاتِ قَرَارٍ وَمَعِينٍ ﴿٥١﴾

**“Kwenda mahali palipoinuka penye utulivu na chemchem za maji.”**

Nao ni mji wa Baytil Maqdis. Na Kauli hii Allah تعالى Anajua zaidi ndiyo iliyo wazi, kwani imetajwa katika Aya nyingine, na sehemu moja ya Qur’ani inafasiri nyingine, hivyo ni bora zaidi kuifasiri kwa Aya nyingine, kisha Hadithi zilizo sahihi, na kisha athari (ripoti nyingine).

يَتَأْتِيهَا الرُّسُلُ كُلُّوًا مِنَ الطَّيِّبَاتِ وَأَعْمَلُوا صَالِحًا ۗ إِنِّي بِمَا تَعْمَلُونَ عَلِيمٌ ﴿٥٢﴾ وَإِنَّ هَذِهِمَ  
 أُمَّتُكُمْ أُمَّةً وَاحِدَةً وَأَنَا رَبُّكُمْ فَاتَّقُونِ ﴿٥٣﴾ فَتَقَطَّعُوا أَمْرَهُمْ بَيْنَهُمْ زُبُرًا ۗ كُلُّ حِزْبٍ  
 بِمَا لَدَيْهِمْ فَرِحُونَ ﴿٥٤﴾ فَذَرَهُمْ فِي عَمْرَتِهِمْ حَتَّىٰ حِينٍ ﴿٥٥﴾ أَحْسَبُونَ أَنَّمَا نُمِدُّهُم بِهِ  
 مِنْ مَّالٍ وَبَنِينَ ﴿٥٦﴾ نُسَارِعُ لَهُمْ فِي الْخَيْرَاتِ ۗ بَلْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٥٧﴾

**51. Enyi Mitume! Kuleni vyakula vizuri na tendeni mema. Hakika Mimi ni Mjuzi wa munayoyatenda.**

**52. Na kwa yakini huu Umma wenu ni Umma mmoja, na Mimi ni Mola wenu Mlezi, basi Nicheni Mimi.**

**53. Lakini walikatiana jambo lao mapande mbali mbali. Kila kundi likifurahia kwa waliyo nayo.**

**54. Basi waache katika ghafla yao kwa muda.**

**55. Je! Wanadhani ya kuwa kwa vile Tunavyowapa mali na watoto.**

**56. Ndio Tunawahimizia kheri? Lakini wenyewe hawatambui.**

### **Amri ya Kula Halali na Kufanya Matendo Mema**

Anawaamrisha Allah تعالى waja Wake Mitume, amani iwe juu yao wote, kula vyakula vya halali na kusimama wima kutekeleza amali njema.

Hii ni dalili kuwa kula cha halali kinamsaidia mja kufanya amali njema. Manabii walitekeleza hayo kwa njia iliyo bora zaidi, hivyo wakatekeleza kila la kheri kwa kauli na amali, uongofu na nasaha. Allah تعالى Awalipe wote kila la kheri kwa niaba ya watu. Na amesema Sa'id bin Jubayr na Adh-Dhahaak:

كُلُوا مِنَ الطَّيِّبَاتِ

**“Kuleni vyakula vizuri.”**

Maana yake: Halali. Na katika Hadithi Sahihi:

«وَمَا مِنْ نَبِيٍّ إِلَّا رَعَى النَّمْلَ»

**“Na hakuna Nabii ila alikuwa mchungaji.”**

Wakasema: “Na hata wewe, Ewe Mtume?” Akasema:

«نَعَمْ، كُنْتُ أُرْعَاهَا عَلَى قَرَارِيطٍ لِأَهْلِ مَكَّةَ»

**“Ndio, nilikuwa nikichunga kondoo wa watu wa Makka kwa Qiratw chache.”<sup>1</sup>**

Na katika Hadithi Sahihi:

«إِنَّ دَاوُدَ عَلَيْهِ السَّلَامُ كَانَ يَأْكُلُ مِنْ كَنْسَبِ يَدِهِ»

**“Hakika Daud عليه السلام alikuwa akila chakula kwa chumo la mkono wake.”<sup>2</sup>**

<sup>1</sup> Al-Bukhaariy 2262 na Ibn Maajah 2:727. Qiratw ni sehemu moja kwa ishirini (1/20 au 5%) ya Dinari au zaidi kidogo.

<sup>2</sup> Fat'h Al-Baariy 4:355.

Na imenukuliwa katika Sahihi Muslim, Jaami' At-Tirmidhiy na Musnad wa Imamu Ahmad, na lafdhi ni ya kutoka kwake kutoka kwa Abu Hurayrah رضي الله عنه kuwa Mtume ﷺ amesema:

«يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنَّ اللَّهَ طَيِّبٌ لَا يَقْبَلُ إِلَّا طَيِّبًا، وَإِنَّ اللَّهَ أَمَرَ الْمُؤْمِنِينَ بِمَا أَمَرَ بِهِ  
الْمُرْسَلِينَ»

*"Hakika Allah Aliyetukuka ni Mzuri na Hakubali ila zuri. Na hakika Allah Aliyetukuka Amewaamrisha Waumini yale Aliyowaamrisha Mitume."*

Akasema Allah تعالى:

يَتَأْتِيهَا الرُّسُلُ كُلُّوْا مِنَ الطَّيِّبَاتِ وَاعْمَلُوا صَالِحًا إِنِّي بِمَا تَعْمَلُونَ عَلِيمٌ ﴿٥١﴾

**'Enyi Mitume! Kuleni vyakula vizuri na tendeni mema. Hakika Mimi ni Mjuzi wa munayoyatenda.'** (23:51).

Na Akasema tena Allah تعالى:

يَتَأْتِيهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا كُلُّوْا مِنَ طَيِّبَاتِ مَا رَزَقْنَاكُمْ

**'Enyi Mulioamini! Kuleni vizuri Tulivyowaruzuku...'** (2:172).

Kisha akamtaja mtu anayekwenda safari ndefu, nywele zimechafuka na kujaa vumbi:

«وَمَطْعَمُهُ حَرَامٌ، وَمَشْرَبُهُ حَرَامٌ، وَمَلْبَسُهُ حَرَامٌ، وَغُذْيِي بِالْحَرَامِ يَمُدُّ يَدَيْهِ إِلَى  
السَّمَاءِ: يَا رَبِّ يَا رَبِّ فَأَنَّى يُسْتَجَابُ لِذَلِكَ»

*"Na ilhali chakula chake ni cha haramu, kinywaji chake ni cha haramu, kivazi chake ni cha haramu, amekuwa katika haramu! anainua mikono yake mbinguni (kuomba akisema), 'Ewe Mola Mlezi! Ewe Mola Mlezi!' – Je, atakubaliwaje ombi hilo?"<sup>1</sup>. Na amesema at-Tirmidhiy: Hadithi hii ni Hasan Ghariyb.*

<sup>1</sup> Muslim 1:703, Tuhfatul Ahwadhyy 8:335 na Ahmad 2:328.

**Dini ya Mitume wote ni Uislamu na Ukariipaji kwa Walioasi**

Na Kauli Yake:

وَإِنَّ هَذِهِ أُمَّةٌ وَاحِدَةٌ

**“Na kwa yakini huu Umma wenu ni Umma mmoja.”**

Maana yake: Dini yenu enyi kongamano la Manabii ni Dini moja na mila moja, nayo ni kulingania katika kumuabudu Allah تعالى Peke Yake bila ya kumshirikisha. Na kwa hiyo Akasema:

وَإِنَّا رَبُّكُمْ فَأَتَّقُونِ

**“Na Mimi ni Mola wenu Mlezi, basi Nicheni Mimi.”**

Na tayari tumetanguliza maelezo kuhusu hilo katika Suratul Ambiyaa'. Na ibara:

أُمَّةٌ وَاحِدَةٌ

**“Umma mmoja.”**

Imewekwa irabu ya *fat'ha* kwa sababu kikanuni ya lugha ya kiarabu na sarufi yake ni “Hali”. Na Kauli Yake:

فَتَقَطَّعُوا أَمْرَهُمْ بَيْنَهُمْ زُبُرًا

**“Lakini walikatiana jambo lao mapande mbali mbali.”**

Maana yake: Mataifa ambayo yaliletewa Manabii.

كُلُّ حِزْبٍ بِمَا لَدَيْهِمْ فَرِحُونَ

**“Kila kundi likifurahia kwa waliyo nayo.”**

Maana yake: Wanafurahi kwa waliyonayo kwa upotevu walio nao huku wakidhania kuwa wameongoka. Na kwa hiyo Akasema, kwa Kutishia na Kuonya:

فَذَرَهُمْ فِي غَمَرَتِهِمْ

**“Basi waache katika ghafla yao.”**

Maana yake: Katika upotevu wao,

حَتَّىٰ حِينٍ ﴿٥٠﴾

**“Kwa muda”**, Maana yake: Mpaka wakati maalumu kwa kuangamizwa kwao. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

فَمَهْلٍ الْكَافِرِينَ أَمْهَلَهُمْ زُيْدًا ﴿٥١﴾

**“Basi wape makafiri muda – wape muda kidogo.” (86:17).**

Na Akasema:

ذَرَهُمْ يَأْكُلُوا وَيَتَمَتَّعُوا وَيُلْهِمُ الْأَمَلُ ۖ فَسَوْفَ يَعْلَمُونَ ﴿٥٢﴾

**“Waache wale (chakula) na wafurahi na liwadanganye tumaini la uongo. Karibuni hivi watajua.” (15:3).**

Na Kauli Yake:

أَحْسَبُونَ أَنَّمَا نُمِدُّهُم بِهِ مِنْ مَّالٍ وَبَيْنٍ ﴿٥٣﴾ نُسَارِعُ لَهُمْ فِي الْخَيْرَاتِ ۗ بَلْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٥٤﴾

**“Je! Wanadhani ya kuwa kwa vile Tunavyowapa mali na watoto. Ndio Tunawahimizia kheri? Lakini wenyewe hawatambui.”**

Maana yake: Je, wanadhania hawa watu wenye kudanganywa kwa Tunayowapa katika mali na watoto ni kwa sababu ya kukirimiwa na kutukuzwa Kwetu? Si hivyo, jambo hilo si kama wanavyodai katika kauli zao:

نَحْنُ أَكْثَرُ أَمْوَالًا وَأَوْلَادًا وَمَا نَحْنُ بِمُعَدِّيْنَ ﴿٥٥﴾

**“Sisi tunayo mali nyingi na watoto wengi, wala sisi hatuadhibiwa.” (34:35).**

Hata hivyo, ufahamu huu ni makosa, na matumaini yao yataruka patupu. Tunawapa vile vitu ili Kuwafanya kuzidi kuendelea (katika madhambi) na Kuwapa wao muda zaidi. Na kwa hiyo Akasema:

بَلْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٥٦﴾

**“Lakini wenyewe hawatambui.”**

Kama Alivyosema:

فَلَا تُعْجِبْكَ أَمْوَالُهُمْ وَلَا أَوْلَادُهُمْ إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُعَذِّبَهُمْ بِهَا فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا

**“Yasikufurahishe mali zao wala watoto wao. Anataka Allah Awaadhibu kwa hayo katika maisha ya dunia...” (9:55).**

Na Amesema Aliyetukuka:

إِنَّمَا نُمَلِّهِمْ هُمْ لِيَزَادُوا إِثْمًا

**“Hakika Tunawapa muda na wanazidi madhambi katika muda huo.” (3:178).**

Na Amesema Aliyetukuka:

فَذَرْنِي وَمَنْ يُكَذِّبْ بِهَذَا الْحَدِيثِ سَنَسْتَدْرِجُهُمْ مِنْ حَيْثُ لَا يَعْلَمُونَ ﴿٤٤﴾ وَأُمَلِّهِمْ

**“Niche na wanaokadhibisha Hadithi hii. Tutawavuta kidogo kidogo katika Adhabu Yetu kwa mahali wasipopajua. Na Ninawapa muda...” (68:44-45).**

Na Amesema:

ذَرْنِي وَمَنْ خَلَقْتُ وَحِيدًا

**“Niche mimi na Niliyemuumba Peke Yangu.” Hadi Kauli Yake,**

عَنِيدًا ﴿١٦﴾

**“Anazipinga.” (74:11-16).**

Na Amesema Aliyetukuka:

وَمَا أَمْوَالُكُمْ وَلَا أَوْلَادُكُمْ بِالَّتِي تُقَرِّبُكُمْ عِنْدَنَا زُلْفَىٰ إِلَّا مَنْ ءَامَنَ وَعَمِلَ صَالِحًا

**“Na si mali zenu wala watoto wenu watakaokukurubisheni Kwetu katika daraja isipokuwa aliyeamini na kutenda mema.” (34:37).**

Na Aya katika suala hili ni nyingi. Imam Ahmad ameandika kuwa Abdallah bin Masu'd رضي الله عنه amesimulia kuwa Mtume ﷺ amesema kuwa:

«إِنَّ اللَّهَ فَسَمَ بَيْنَكُمْ أَخْلَاقَكُمْ كَمَا فَسَمَ بَيْنَكُمْ أَرْزَاقَكُمْ، وَإِنَّ اللَّهَ يُعْطِي الدُّنْيَا مَنْ يُحِبُّ وَمَنْ لَا يُحِبُّ، وَلَا يُعْطِي الدِّينَ إِلَّا لِمَنْ أَحَبَّ، فَمَنْ أَغْطَاهُ اللَّهُ الدِّينَ فَقَدْ أَحَبَّهُ، وَالَّذِي تَفْسِي بِيَدِهِ لَا يُسَلِّمُ عَبْدًا حَتَّىٰ يَسْلَمَ قَلْبُهُ وَلِسَانُهُ، وَلَا يُؤْمِنُ حَتَّىٰ يَأْمَنَ جَارُهُ بِوَاقِعِهِ»

*"Hakika Allah Amegawa tabia miongoni mwenu kama Alivyowagawanyia riziki zenu. Allah Huwaruzuku vitu vya dunia hii wale Anaowapenda na Asiowapenda, lakini Huwaruzuku mfumo wa maisha wa Uislamu wale tu Anaowapenda. Yeyote atakayeruzukiwa na Uislamu huyo ni kipenzi cha Allah. Naapa kwa Yule Ambaye nafsi yangu ipo Mkononi Mwake kwamba mja hawi Muislamu mpaka usilimu moyo wake na ulimi wake, na hawi Muumini wa kweli mpaka amueke jirani yake katika hali ya amani kutokana na shari zake."*

Wakauliza, 'ni zipi hizo shari zake, Ewe Mtume wa Allah?' Akajibu:

«عَسْمُهُ وَظَلْمُهُ، وَلَا يَكْسِبُ عَبْدٌ مَالًا مِنْ حَرَامٍ فَيَنْفِقَ مِنْهُ فَيَبَارِكَ لَهُ فِيهِ، وَلَا يَتَّصِقَ بِهِ فَيُقْبَلَ مِنْهُ، وَلَا يَتْرُكُهُ خَلْفَ ظَهْرِهِ إِلَّا كَانَ زَادَهُ إِلَى النَّارِ، إِنَّ اللَّهَ لَا يَمْحُو السَّيِّئَ بِالسَّيِّئِ وَلَكِنْ يَمْحُو السَّيِّئَ بِالْحَسَنِ، إِنَّ الْخَبِيثَ لَا يَمْحُو الْخَبِيثَ»

*"Makosa yake na mwenendo mbaya. Hakuna abarikiwaye kwa kuchuma mali kwa njia za haramu na kuitumia, hata akitoa sadaka haitakubaliwa, na ikibakia wakati anafariki dunia itakuwa ni sehemu ya ujira wake Motoni. Mwenyezi Mungu Halifuti tendo ovu kwa tendo ovu lingine, bali Anayafuta matendo maovu ya mja kwa mema anayotenda. Maana uovu hautakaswi kwa uovu."<sup>1</sup>*

إِنَّ الَّذِينَ هُمْ مِنْ خَشْيَةِ رَبِّهِمْ مُشْفِقُونَ ﴿٥٧﴾ وَالَّذِينَ هُمْ بِعَاقِبَتِ رَبِّهِمْ يُؤْمِنُونَ ﴿٥٨﴾  
وَالَّذِينَ هُمْ بِرَبِّهِمْ لَا يُشْرِكُونَ ﴿٥٩﴾ وَالَّذِينَ يُؤْتُونَ مَاءً آتَوْا وَقُلُوبُهُمْ وَجِلَةٌ أَنَّهُمْ إِلَى رَبِّهِمْ  
رَاجِعُونَ ﴿٦٠﴾ أُولَئِكَ يُسْرِعُونَ فِي الْحَيَاتِ وَهُمْ هَاهُنَا سَابِقُونَ ﴿٦١﴾

**57. Kwa hakika hao ambao kwa kumuogopa Mola wao Mlezi wananyenyekea,**

**58. Na wale ambao Ishara za Mola wao Mlezi wanaziamini,**

**59. Na wale ambao Mola wao Mlezi hawamshirikishi,**

**60. Na wale ambao wanatoa walichopewa, na hali nyoyo zao zinaogopa kwa kuwa watarejea kwa Mola wao Mlezi,**

<sup>1</sup> Ahmad 1:387. Usahihi wa matini ya riwaya hii ni kutoka kwa Ibn Mas'ud, si kwa Mtume.

**61. Basi wote hao ndio wanaokimbilia katika mambo ya kheri, na ndio watakaotangulia kuyafikia.**

### Sifa za Watu Wema

Anasema Aliyetukuka:

﴿٥٧﴾ إِنَّ الَّذِينَ هُمْ مِنْ حَشِيَّةٍ رَبِّهِمْ مُشْفِقُونَ

**“Kwa hakika hao ambao kwa kumuogopa Mola wao Mlezi wananyenyekea.”**

Maana yake: Japokuwa wamefikia daraja ya wema, wana Imani na matendo mema, na bado wanamnyenyekea Allah تعالى wakiwa wanamuogopa kutokana na vitimbi Vyake kwao. Kama alivyosema Al-Hasan Al-Baswriy رحمه الله تعالى, “Hakika Muumini amechanganya wema na unyenyekevu, ilhali kafiri amechanganya matendo mabaya na hisia ya usalama”<sup>1</sup>.

﴿٥٨﴾ وَالَّذِينَ هُمْ بِآيَاتِ رَبِّهِمْ يُؤْمِنُونَ

**“Na wale ambao Ishara za Mola wao Mlezi wanaziamini.”**

Maana yake: Wanaamini Ishara Zake za kilimwengu na sheria, kama Kauli Yake Aliyetukuka Akitupasha habari kuhusu Maryam عليه السلام:

وَصَدَقَتْ بِكَلِمَاتِ رَبِّهَا وَكُتِبَ لَهَا

**“...Na akayasidikisha maneno ya Mola wake Mlezi na Vitabu Vyake...” (66:12),**

Maana yake: Aliamini kuwa chochote kilichokuwa ni kwa Matakwa na Kudura Yake, na kuwa lolote lililokadiriwa ikiwa ni Amri, ni katika jambo Alilolipenda na Kulikubali. Na ikiwa ni Katazo, ni jambo ambalo Amelichukia na Kulikataa; na likiwa ni kheri, litakuwa ni ya kweli. Hii ni kama Alivyosema Allah تعالى:

﴿٥٩﴾ وَالَّذِينَ هُمْ بِرَبِّهِمْ لَا يُشْرِكُونَ

**“Na wale ambao Mola wao Mlezi hawamshirikishi.”**

Maana: Hawamuabudu pamoja Naye mwingine yeyote, bali wanampwekesha

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 19:45.



na kujua kuwa Yeye Ndiye wa Pekee anayepaswa kuabudiwa, Mmoja tu, Anayestahiki Kukusudiwa, Ambaye Hana mke wala mtoto, na hakuna anayefanana wala aliye sawa Naye. Na Kauli Yake:

وَالَّذِينَ يُؤْتُونَ مَا آتَوْا وَقُلُوبُهُمْ وَجِلَةٌ أَنَّهُمْ إِلَىٰ رَبِّهِمْ رَاجِعُونَ

***“Na wale ambao wanatoa walichopewa, na hali nyoyo zao zinaogopa kwa kuwa watarejea kwa Mola wao Mlezi.”***

Maana yake: Wanatoa sadaka, huku wakiogopa kuwa hazitakubaliwa kutoka kwao kwa sababu ya kasoro zao au kufeli kutekeleza masharti yanayohitajika ya kutoa. Hii inahusiana na hofu na kuchukua tahadhari, kama alivyopokea Imaam Ahmad kutoka kwa 'Aishah رضي الله عنها aliyesema: “Ewe Mtume wa Allah!

وَالَّذِينَ يُؤْتُونَ مَا آتَوْا وَقُلُوبُهُمْ وَجِلَةٌ

***‘Na wale ambao wanatoa walichopewa, na hali nyoyo zao zinaogopa.’***

Je, huyu ni yule mwenye kuiba, kuzini na kunywa pombe ilhali anamuogopa Allah Mtukufu?” Akasema:

«لَا، يَا بِنْتُ أَبِي بَكْرٍ يَا بِنْتَ الصِّدِّيقِ، وَلَكِنَّهُ الَّذِي يُصَلِّي وَيَصُومُ وَيَتَصَدَّقُ وَهُوَ يَخَافُ اللَّهَ عَزَّ وَجَلَّ»

*“Hapana, ewe binti wa Abubakar. Ewe binti wa As-Siddiq, lakini huyo ni yule mwenye kuswali, kufunga na kutoa sadaka, naye anamuogopa Allah Aliyetukuka”<sup>1</sup>.*

Na hivyo ndivyo alivyopokea At-Tirmidhiy na Ibn Haatim mfano wake, ambamo Mtume ﷺ amesema:

«لَا يَا بِنْتَ الصِّدِّيقِ، وَلَكِنَّهُمْ الَّذِينَ يُصَلُّونَ وَيَصُومُونَ وَيَتَصَدَّقُونَ وَهُمْ يَخَافُونَ اللَّهَ يُقْبَلُ مِنْهُمْ: ﴿أُزِلَّتْكَ بِسْرِعُونَ فِي الْحَرْبِ﴾»

*“Hapana, ewe binti wa As-Siddiq, lakini hao ni wale wenye kuswali, kufunga na kutoa sadaka, ilhali wanaogopa kutokubaliwa kutoka kwao: ‘Basi wote hao ndio wanaokimbilia katika mambo ya kheri.’”<sup>2</sup>*

<sup>1</sup> Ahmad 6:159.

<sup>2</sup> Tuhfatul Al-Ahwadhiy 9:19.

Na hivyo ndivyo alivyofasiri Aya hiyo Ibn 'Abbaas, Muhammad bin Ka'b Al-Quradhiy na Al-Hasan Al-Basriy<sup>1</sup> رضي الله عنهم.

وَلَا تُكَلِّفُ نَفْسًا إِلَّا وُسْعَهَا ۗ وَأَلْدَيْنَا كِتَابًا يَنْطِقُ بِالْحَقِّ ۗ وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ ﴿٥٠﴾ بَلْ قُلُوبُهُمْ  
 فِي غَمْرَةٍ مِّنْ هُنَا ۖ وَهُمْ أَعْمَلُ ۗ مِن دُونِ ذَلِكَ هُمْ لَهَا عَمَلُونَ ﴿٥١﴾ حَتَّىٰ إِذَا أَخَذْنَا  
 مُتْرَفِيهِم بِالْعَذَابِ إِذَا هُمْ يَجْعَرُونَ ﴿٥٢﴾ لَا تَجْعَرُوا أَلْيَوْمَ ۖ إِنَّكُمْ مِنَّا لَا تُنصِرُونَ ﴿٥٣﴾  
 قَدْ كَانَتْ آيَاتِي تَتْلَىٰ عَلَيْكُمْ فَكُنْتُمْ عَلَىٰ أَعْقَابِكُمْ تَنْكِبُونَ ﴿٥٤﴾ مُسْتَكْبِرِينَ بِهِ  
 سَمِيرًا ۖ تَهْجُرُونَ ﴿٥٥﴾

**62. Na Hatuilazimishi nafsi ila kwa kadri ya uwezo wake. Na Tunacho kitabu kisemacho kweli. Nao hawatadhulumiwa.**

**63. Lakini nyoyo zao zimeghafilika na hayo, na wanavyo vitendo vinginevyo wanavyovifanya.**

**64. Hata Tutakapowatia katika adhabu wale waliodekezwa kwa starehe kati yao, hapo ndipo watapoyayatika.**

**65. Musiyayatike leo! Hakika nyinyi hamtanusurika Nasi.**

**66. Hakika zilikuwa Aya Zangu mkisomewa, nanyi mkirudi nyuma juu ya visigino vyenu.**

**67. Na huku mukitakabari na usiku mkiizungumza (Qur'ani) kwa dharau.**

### Hukumu na Uadilifu wa Allah تعالی na Upumbavu wa Washirikina

Anatueleza Aliyetukuka Uadilifu Wake kwa waja Wake hapa duniani, kwa kuwa Hamkalifishi yeyote ila kulingana na uwezo wake, yaani ila kwa anayoweza kubeba na kuyasimamia. Na hakika ni kuwa Siku ya Kiyama Atawahesabu kwa amali zao ambazo Amezinukuu katika Kitabu ambacho hakipotezi wala kufuta chochote.

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 19:45, 46.

Na kwa hiyo Akasema:

وَلَدَيْنَا كِتَابٌ يَنْطِقُ بِالْحَقِّ

**“Na Tunacho kitabu kisemacho kweli.”**

Maana yake: Kitabu cha amali,

وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ

**“Nao hawatadhulumiwa.”**

Maana yake: Hakuna kitakachofutwa katika kumbukumbu ya amali njema. Ama kwa amali mbaya, Atasamehe na Kupuuza mengi kati ya hayo kwa waja Wake Waumini.

Kisha Akasema, Kuwakanusha na Kuwapinga makafiri na washirikina wa Quraysh:

بَلْ قُلُوبُهُمْ فِي غَمْرَةٍ

**“Lakini nyoyo zao zimeghafilika.”**

Maana yake: Katika Kughafilika na upotevu,

مِنْ هَذَا

**“Na hayo.”**

Maana yake: Qur'ani iliyoteremshwa kwa Mtume Wake ﷺ.

Na Kauli Yake:

وَهُمْ أَعْمَلُ مِنْ دُونِ ذَلِكَ هُمْ لَهَا عَمَلُونَ

**“Na wanavyo vitendo vinginevyo wanavyovifanya.”**

Amepokea Al-Hakam bin Abaan kutoka kwa 'Ikrimah kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema:

وَهُمْ أَعْمَلُ

**“Na wanavyo vitendo vinginevyo.”**

Maana yake: Amali mbaya mbali na hiyo, nayo ni ushirikina,

﴿ هُمْ لَهَا عَمَلُونَ ﴾

**'Wanavyofanya.'**

Ambavyo hawana budi kufanya<sup>1</sup>. Hivyo ndivyo imepokewa kwa Mujaahid, Al-Hasan na wengineo<sup>2</sup>. Na wakasema wengine:

﴿ وَهُمْ أَعْمَلٌ مِّنْ دُونِ ذَلِكَ هُمْ لَهَا عَمَلُونَ ﴾

***"Na wanavyo vitendo vinginevyo wanavyovifanya."***

Maana yake: Waliandikiwa juu yao amali mbaya, na bila shaka watafanya hayo kabla ya kufa kwao, ili neno la adhabu lithibiti dhidi yao. Imepokewa mfano wa hii kutoka kwa Muqaatil bin Hayyaan, as-Suddiy na 'Abdur- Rahman bin Zayd bin Aslam<sup>3</sup>. Hii ndio maana iliyo dhahiri yenye nguvu na wazi. Na hakika tayari tumetanguliza Hadithi ya Ibn Mas'ud رضي الله عنه:

«فَرَّ الَّذِي لَا إِلَهَ غَيْرُهُ إِنَّ الرَّجُلَ لَيَعْمَلُ بِعَمَلِ أَهْلِ الْجَنَّةِ حَتَّىٰ مَا يَكُونُ بَيْنَهُ وَبَيْنَهَا إِلَّا ذِرَاعٌ، فَيَسْبِقُ عَلَيْهِ الْكِتَابُ فَيَعْمَلُ بِعَمَلِ أَهْلِ النَّارِ فَيَدْخُلُهَا»

*"Naapa kwa Allah, ambaye hapana Mola asiyekuwa Yeye! Hakika mtu hufanya amali ya watu wa Peponi, mpaka ikawa hapana baina yake na Pepo ila dhiraa (kutoka ncha za vidole mpaka kiwikoni), akatanguliwa na aliloandikiwa, akafanya amali ya watu wa Motoni, akaingia Motoni"<sup>4</sup>.*

Na Kauli Yake:

﴿ حَتَّىٰ إِذَا أَخَذْنَا مُتْرَفِيهِم بِالْعَذَابِ إِذَا هُمْ يَجْعَرُونَ ﴾

***"Hata Tutakapowatia katika adhabu wale waliodekezwa kwa starehe kati yao, hapo ndipo watapoyayatika."***

<sup>1</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 6:107.

<sup>2</sup> Atw-Twabariy 19:49 na Al-Qurtwubiy 12:134.

<sup>3</sup> Atw-Twabariy 19:50.

<sup>4</sup> Ahmad 1:382.

Maana yake: Mpaka watakapokuja kwa waliodekezwa – nao ni waliokuwa wakiishi kwa furaha na neema nyingi hapa duniani adhabu ya Allah تعالى, kisasi na maangamivu kwao,

إِذَا هُمْ يَجْرُونَ ﴿٥٠﴾

**“Hapo ndipo watapoyayatika.”** Maana yake: Watapiga makelele kutaka msaada. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَدَرَنِي وَالْمُكَذِّبِينَ أُولِي النَّعْمَةِ وَمَهْلَهْمُ قَلِيلًا ﴿٥١﴾ إِنَّ لَدَيْنَا أَنْكَالًا وَحِمِيمًا ﴿٥٢﴾

**“Na Niche Mimi na hao wanaonikadhibisha walioneemeka, na uwape muhula kidogo. Hakika Tuna adhabu na Moto uwakao kwa ukali.”** (73:11-12).

Na Amesema Aliyetukuka:

كَمْ أَهْلَكْنَا مِنْ قَبْلِهِمْ مِنْ قَرْنٍ فَنَادَوا وَعَلَىٰ حِينٍ مَنَاصٍ ﴿٥٣﴾

**“Tumeziangamiza ngapi kabla yao, wakapiga kelele wakati huo; lakini wakati wa kuokoka ulikuwa umekwisha kupita.”** (38:3).

Na Kauli Yake:

لَا تَجْعُرُوا أَيُّوْمَ إِتْكَرٍ مِّنَّا لَا تَنْصُرُونَ ﴿٥٤﴾

**“Musiyayatike leo! Hakika nyinyi hamtanusurika Nasi.”**

Maana yake: Hakuna atakayewaokoeni kwa yatakayowakumba, ikiwa mtapiga kelele kwa nguvu au mkanyamaza. Hakuna sehemu ya kukimbilia wala hamtanusurika. Ni lazima itokee: Bila shaka adhabu itawafikia. Baada ya hapo Anataja madhambi yao makubwa, Akasema:

فَدَكَانَتْ ءَايَاتِي تُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ فَكُنْتُمْ عَلَىٰٰٓ أَعْقَابِكُمْ تَنْكِبُونَ ﴿٥٥﴾

**“Hakika zilikuwa Aya Zangu mkisomewa, nanyi mkirudi nyuma juu ya visigino vyenu.”**

Maana yake: Mlipoitwa, mkakataa na mkitakiwa mlilitenga.

ذَلِكُمْ بِأَنَّهُ إِذَا دُعِيَ اللَّهُ وَحْدَهُ كَفَرْتُمْ ۖ وَإِنْ يُشْرَكَ بِهِ تُؤْمِنُوا ۗ فَالْحُكْمُ لِلَّهِ الْعَلِيِّ

الْكَبِيرِ ﴿٥٦﴾

***“Kwa sababu mlikuwa Akitajwa (akiombwa) Allah Peke Yake mnakanusha na Akishirikishwa munaamini. Basi hukumu leo ni Yake tu Allah Aliye Juu Aliye Mkuu.” (40:12).***

Na Kauli Yake:

مُسْتَكْبِرِينَ بِئْسَ سَمِيرًا تَهْجُرُونَ ﴿٧٧﴾

***“Na huku mukitakabari na usiku mkiizungumza (Qur’ani) kwa dharau.”***

Maana yake: Nyumbani (Ka’bah), wanajifakhiri kwa kiburi na kuitakidi kuwa wao ni marafiki wa Allah تعالی hali ya kuwa wao si hivyo. Amesema hivyo An-Nasaa’iy katika Tafsiri yake kuhusu Aya hii katika Sunan yake: Ahmad bin Sulaymaan ametuhadidhia kutoka kwa Ubaidillah kutoka kwa Israa’iyl kutoka kwa ‘Abdul-A’laa kuwa amemsikia Sa’id bin Jubayr akihadithia kutoka kwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Kuzungumza usiku kulichukiza pale ilipoteremka Aya hii:

مُسْتَكْبِرِينَ بِئْسَ سَمِيرًا تَهْجُرُونَ ﴿٧٧﴾

***‘Na huku mukitakabari na usiku mukiizungumza (Qur’ani) kwa dharau’.***

Akasema: ‘Walijifakhiri na kutakabari kuhusu Ka’bah na wakasema, Sisi ndio watu wake tunaokaa kuzungumza usiku’. Walikuwa wakijifakhiri na kukaa na kuzungumza usiku pembezoni mwa Ka’bah. “Hawakuitumia kwa njia nzuri wala hawakuimarisha, kwa hivyo walikuwa wameitupa na kuihama”<sup>1</sup>.

\* \* \*

---

<sup>1</sup> An-Nasaa’iy katika al-Kubraa 6:412.

أَفَلَمْ يَدَّبَّرُوا الْقَوْلَ أَمْ جَاءَهُمْ مَا لَمْ  
 يَأْتِ آبَاءَهُمُ الْأَوَّلِينَ ﴿٦٨﴾ أَمْ لَمْ  
 يَعْرِفُوا رَسُولَهُمْ فَهُمْ لَهُ مُنْكَرُونَ  
 ﴿٦٩﴾ أَمْ يَقُولُونَ بِهِ جِنَّةٌ بَلْ  
 لِلْحَقِّ كَرِهُونَ ﴿٧٠﴾ وَلَوْ اتَّبَعَ  
 الْحَقُّ أَهْوَاءَهُمْ لَفَسَدَتِ  
 السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ وَمَنْ فِيهِنَّ ؕ بَلْ  
 أَتَيْنَهُمْ بِذِكْرِهِمْ فَهُمْ عَنِ  
 ذِكْرِهِمْ مُعْرِضُونَ ﴿٧١﴾ أَمْ  
 تَسْأَلُهُمْ خَرْجًا فَخَرَجَ رِبْكَ  
 خَيْرٌ ۗ وَهُوَ خَيْرُ الرَّزِقِينَ ﴿٧٢﴾  
 وَإِنَّكَ لَتَدْعُوهُمْ إِلَى صِرَاطٍ  
 مُسْتَقِيمٍ ﴿٧٣﴾ وَإِنَّ الَّذِينَ لَا  
 يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ عَنِ الصِّرَاطِ  
 لَنَجْكَوَاتٌ ﴿٧٤﴾ \* وَلَوْ  
 رَحِمْنَاهُمْ وَكَشَفْنَا مَا بِهِمْ  
 مِنْ ضُرِّ لَلْجَوَا فِي طُعْنِهِمْ  
 يَعْمَهُونَ ﴿٧٥﴾ وَلَقَدْ أَخَذْنَاهُمْ  
 بِالْأَعْدَابِ فَمَا أَصْبَرُوا  
 لِلرِّيبِ وَمَا يَنْتَضِرُونَ ﴿٧٦﴾ حَتَّى  
 إِذَا فَتَحْنَا عَلَيْهِمْ بَابًا ذَا  
 عَذَابٍ شَدِيدٍ إِذَا هُمْ فِيهِ مُبْلِسُونَ ﴿٧٧﴾  
 وَهُوَ الَّذِي أَنْشَأَ  
 لَكُمْ السَّمْعَ وَالْأَبْصَرَ وَالْأَفْئِدَةَ ؕ  
 قَلِيلًا مَّا تَشْكُرُونَ ﴿٧٨﴾ وَهُوَ  
 الَّذِي ذَرَأَكُمْ فِي الْأَرْضِ وَإِلَيْهِ  
 تُحْشَرُونَ ﴿٧٩﴾ وَهُوَ  
 الَّذِي يُخَيِّبُ وَيُمِيتُ وَهُوَ  
 آخِطَفُ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ ؕ أَفَلَا  
 تَعْقِلُونَ ﴿٨٠﴾ بَلْ قَالُوا مِثْلَ  
 مَا قَالَ الْأَوَّلُونَ ﴿٨١﴾ قَالُوا  
 أَيُّدَا إِذَا مِتْنَا وَكُنَّا تُرَابًا  
 وَعِظْمًا أَيْنَا لَمَبْعُوثُونَ ﴿٨٢﴾  
 لَقَدْ وَعَدْنَا نَحْنُ وَآبَاؤُنَا هَذَا  
 مِنْ قَبْلُ إِنْ هَذَا إِلَّا  
 أَسْطِيرُ الْأَوَّلِينَ ﴿٨٣﴾

أَفَلَمْ يَدَّبَّرُوا الْقَوْلَ أَمْ جَاءَهُمْ مَا لَمْ  
 يَأْتِ آبَاءَهُمُ الْأَوَّلِينَ ﴿٦٨﴾ أَمْ لَمْ  
 يَعْرِفُوا رَسُولَهُمْ فَهُمْ لَهُ مُنْكَرُونَ  
 ﴿٦٩﴾ أَمْ يَقُولُونَ بِهِ جِنَّةٌ بَلْ  
 لِلْحَقِّ كَرِهُونَ ﴿٧٠﴾ وَلَوْ اتَّبَعَ  
 الْحَقُّ أَهْوَاءَهُمْ لَفَسَدَتِ  
 السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ وَمَنْ فِيهِنَّ ؕ بَلْ  
 أَتَيْنَهُمْ بِذِكْرِهِمْ فَهُمْ عَنِ  
 ذِكْرِهِمْ مُعْرِضُونَ ﴿٧١﴾ أَمْ  
 تَسْأَلُهُمْ خَرْجًا فَخَرَجَ رِبْكَ  
 خَيْرٌ ۗ وَهُوَ خَيْرُ الرَّزِقِينَ ﴿٧٢﴾  
 وَإِنَّكَ لَتَدْعُوهُمْ إِلَى صِرَاطٍ  
 مُسْتَقِيمٍ ﴿٧٣﴾ وَإِنَّ الَّذِينَ لَا  
 يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ عَنِ الصِّرَاطِ  
 لَنَجْكَوَاتٌ ﴿٧٤﴾ \* وَلَوْ  
 رَحِمْنَاهُمْ وَكَشَفْنَا مَا بِهِمْ  
 مِنْ ضُرِّ لَلْجَوَا فِي طُعْنِهِمْ  
 يَعْمَهُونَ ﴿٧٥﴾

68. Je, hawakuifikiri kauli,  
 au yamewajia yasiyo-  
 wafikia baba zao wa  
 zamani?

**69. Au hawakumjua Mtume wao, ndio maana wanamkataa?**

**70. Au wanasema: Ana wazimu? Bali amewajia kwa Haki, na wengi wao wanaichukia Haki.**

**71. Na lau kuwa Haki ingelifuata matamano yao, basi zingeliharibika mbingu na ardhi na waliomo ndani. Bali Tumewaletea ukumbusho wao, nao wanajitenga mbali na ukumbusho wao.**

**72. Au unawaomba ujira? Lakini ujira wa Mola wako Mlezi ni bora, na Yeye Ndiye Mbora wa wanaoruzuku.**

**73. Na kwa yakini wewe unawaita kwenye njia iliyonyooka.**

**74. Na hakika wale wasioiamini Akhera wanajitenga na njia hiyo.**

**75. Na lau Tungeliwarehemu na Tukawaondolea shida waliyo nayo bila ya shaka wangelindelea katika upotofu wao vile vile, wakitangatanga.**

### **Majibu kwa Washirikina na Kukaripiwa Kwao**

Anasema Aliyetukuka huku Akiwashutumu na Kuwasuta washirikina kwa kutoifahamu Qur'ani Tukufu, kuizingatia na kuipa nyongo. Japokuwa hasa wamesemeshwa wao katika Kitabu hiki ambacho Allah تعالیٰ Hakukiteremsha kwa Mtume yeyote kikiwa kimekamili na kitukufu, na hasa kuwa hakuna Kitabu au muonyaji ambaye ametumwa kwa mababu zao walioaga dunia katika wakati wa ujahiliya (ujinga). Watu hawa walioletewa neema hii walikuwa waukubali ujumbe huu na kushukuru, na kujaribu kuufahamu na kusimama kidete kuitekeleza risala hiyo usiku na mchana. Kama walivyofanya wenye busara miongoni mwao waliosilimu na kumfuata Mtume Muhammad ﷺ, Allah Awaridhie wote. Na akasema Qatadah:

أَفَلَمْ يَدَّبَّرُوا الْقَوْلَ

**“Je, hawakuifikiri kauli.”**

Hii ina maana kuwa Wallaahi, lau watu wangezingatia maana na kuifahamu Qur'ani vilivyo, wangepata humo kinga dhidi ya kumuasi Allah تعالیٰ. Lakini



walichukua tu zile Aya ambazo kwa dhahiri zinazoonekana zina utata ndani yake (*Mutashaabihaat*), hivyo wakaangamizwa kwa ajili ya hilo<sup>1</sup>. Kisha Allah تعالی Akasema kwa Kuwasuta makafiri wa Kiquraysh:

أَمْ لَمْ يَعْرِفُوا رَسُولَهُمْ فَهُمْ لَهُدٍ مُنْكَرُونَ ﴿٦٨﴾

**“Au hawakumjua Mtume wao, ndio maana wanamkataa?”**

Maana yake: Je, hawamtambui Muhammad ﷺ, ukweli, uaminifu wake na maadili yake mema ambayo aliinukia nayo miongoni mwao? Je, wanaweza kukanusha au kujadili dhidi ya hayo? Ja'far bin Abi Twaalib رضي الله عنه alimuambia An-Najjaashiy, mfalme wa Habasha: “Ewe mfalme! Hakika Allaah Amemtuma Mtume kwetu ambaye nasaba yake, ukweli na uaminifu wake unafahamika na kujulikana kwetu sana”<sup>2</sup>. Al- Mughiyrah bin Shu'bah رضي الله عنه alisema mfano wa hayo kwa naibu wa Kisra pale alipotaka kubariziana naye. Kadhalika, mfalme wa Bizanta<sup>3</sup>, Hiraql (Heraclius) alipomuuliza Abu Sufyaan Sakhr bin Harb na wenzake – waliokuwa bado ni makafiri wakati huo na walikuwa bado hawajasilimu – kuhusu sifa na maadili, nasaba, ukweli na uaminifu wa Mtume ﷺ, hawakuweza kufanya lolote isipokuwa kusema ukweli na kukubali kuwa kwa hakika Mtume ﷺ alikuwa mtukufu na mkweli<sup>4</sup>. Na Kauli Yake:

أَمْ يَقُولُونَ بئس جنة

**“Au wanasema: Ana wazimu?”**

Kauli hii ni ya washirikina, inasimulia kuhusu Mtume ﷺ. Wao wanasema kuwa ameizua Qur'ani, au alikuwa mwenda wazimu na hakujua analosema. Allah تعالی Anatueleza kuwa mioyo yao haikuamini hayo, walijua vilivyo kuwa waliyokuwa wakisema kuhusu Qur'ani ni uongo mtupu, kwani Qur'an iliyowajia ni Maneno ya Allah تعالی na hayakuweza kuzuilika au kukataliwa. Hivyo, Allah تعالی Anawapa wao changamoto na watu wote duniani waje na mfano wake ikiwa wanaweza – lakini hawakuweza wala hawataweza kufanya hivyo. Kwa hiyo, Akasema:

<sup>1</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 6:110.

<sup>2</sup> Ibn Hishaam 1:357.

<sup>3</sup> Taifa la Kirumi upande wa mashariki ya ardhi.

<sup>4</sup> Fat'h Al-Baariy 1:42.

بَلْ جَاءَهُمْ بِالْحَقِّ وَأَكْثَرُهُمْ لِلْحَقِّ كَارِهُونَ ﴿٦٨﴾

***“Bali amewajia kwa Haki, na wengi wao wanaichukia Haki”.***

Katika kanuni na sarufi ya lugha ya Kiarabu, huenda ibara hii, ni ya kihali, yaani katika ile hali ya kuchukia wakakaribia ukweli. Na huenda ikawa ni ibara ya kihabari yenye kuanza upya. Allah تعالی Anajua zaidi.

### **Haki Haifuati Matamaniao na Matakwa ya Mtu**

Na Kauli Yake:

وَلَوْ اتَّبَعَ الْحَقُّ أَهْوَاءَهُمْ لَفَسَدَتِ السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ وَمَنْ فِيهِنَّ<sup>٤</sup>

***“Na lau kuwa Haki ingelifuata matamaniao yao, basi zingeliharibika mbingu na ardhi na waliomo ndani”.***

Mujaahid, Abu Swaalih na As-Suddiy wamesema: *“Al-Haqq ni Allah, تعالی<sup>1</sup>”*. Maana ya Aya hii ni kuwa lau Allah تعالی Angeitikia yaliyokuwa nyoyoni mwao katika matamaniao na Kuweka sheria ya mambo kwa yanayoafikiana na hayo,

لَفَسَدَتِ السَّمَوَاتُ وَالْأَرْضُ وَمَنْ فِيهِنَّ<sup>٤</sup>

***“Basi zingeliharibika mbingu na ardhi na waliyomo ndani”***. Maana yake: Kwa sababu ya kuharibika matamaniao yao na yasiyowiana. Hii ni kama Alivyotujulisha katika Kauli Yake:

لَوْلَا نُزِّلَ هَذَا الْقُرْآنُ عَلَى رَجُلٍ مِّنَ الْقَرِيبَيْنِ عَظِيمٍ ﴿٣١﴾

***“Kwa nini Qur’ani hii haikuteremshwa kwa mtu mkubwa katika miji miwili hii?” (43:31).***

Kisha Akasema:

أَهُمْ يَقْسِمُونَ رَحْمَتَ رَبِّكَ<sup>٤</sup>

***“Kwani wao ndio wanaogawa Rehema za Mola wako Mlezi?” (43:32).***

Na Amesema Aliyetukuka:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 19:57 na al-Qurtwubiy 12:140.

قُلْ لَوْ أَنْتُمْ تَمْلِكُونَ خَزَائِنَ رَحْمَةِ رَبِّي إِذًا لَأَمْسَكْتُمْ خَشْيَةَ الْإِنْفَاقِ<sup>٤</sup>

**“Sema: Lau kuwa nyinyi mnazimiliki khazina za Rehema za Mola wangu Mlezi, basi hapana shaka mungelizuia kuzitumia kwa ajili ya kukhofu.” (17:100).** Na Amesema Aliyetukuka:

أَمْ هُمْ نَصِيبٌ مِّنَ الْمُلْكِ فَإِذَا لَا يُؤْتُونَ النَّاسَ نَقِيرًا ﴿٥٣﴾

**“Au wao wana nasibu katika mamlaka (na ufalme)? Basi hapo wasingaliwapa watu hata kokwa.” (4:53).**

Na katika haya yote ni kubainisha kushindwa kwa waja na kutofautiana kwao rai na utashi wao. Na Aliyekamilika ni Allah تعالیٰ Peke Yake katika Sifa Zake zote, Kauli Zake, Matendo na Sheria Yake, Uweza na Udhhibiti Wake kwa viumbe Vyake, Utukufu ni Wake. Hapana mungu muabudiwa ila Yeye wala Mola asiye kuwa yeye. Kisha Akasema:

بَلْ أَتَيْنَهُم بِذِكْرِهِمْ

**“Bali Tumewaletea ukumbusho wao...”. Maana yake: Qur’ani,**

فَهُمْ عَن ذِكْرِهِمْ مُعْرِضُونَ ﴿٥٤﴾

**“...nao wanajitenga mbali na ukumbusho wao”.**

## Nabii Haombi Ujira na Anahubiri katika Njia Iliyonyooka

Na Kauli Yake:

أَمْ تَسْأَلُهُمْ خَرْجًا

**“Au unawaomba ujira?”** Amesema Al-Hasan: “Ujira”<sup>1</sup>. Na amesema Qatadah: “Malipo”<sup>2</sup>.

فَخَرَّاجٌ رَبِّكَ خَيْرٌ<sup>٥٥</sup>

**“Lakini ujira wa Mola wako Mlezi ni bora”.**

Maana yake: Wewe hutauliza ujira wala malipo wala chochote kwa kuwaita watu katika uongofu, bali unatarajia kwa hilo kutoka kwa Allah تعالیٰ thawabu kubwa, kama Anavyosema:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 19:58.

<sup>2</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 6:110.

قُلْ مَا سَأَلْتُكُمْ مِنْ أَجْرٍ فَهُوَ لَكُمْ ۗ إِنِ اجْتَبَىٰ إِلَّآ عَلَى اللَّهِ ۗ

**“Sema: Ujira niliokuombeni ni wenu nyinyi. Sina ujira ila kwa Allah...” (34:47).** Na Akasema:

قُلْ مَا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ مِنْ أَجْرٍ وَمَا أَنَا مِنَ الْمُتَكَلِّفِينَ ﴿٤٨﴾

**“Sema (ewe Mtume): Sikuombeni ujira juu ya haya, wala mimi si katika wadanganyifu.” (38:86).**

Na Akasema:

قُلْ لَّا أَسْأَلُكُمْ عَلَيْهِ أَجْرًا ۖ إِلَّآ الْمَوَدَّةَ فِي الْقُرْبَىٰ ۗ

**“Sema: Sikuombeni malipo yoyote kwenu ila mapenzi kujikurubisha..” (42:23).**

Na Akasema:

وَجَاءَ مِنْ أَقْصَا الْمَدِينَةِ رَجُلٌ يَسْعَىٰ قَالَ يَنْفَوْرِمِ اتَّبِعُوا الْمُرْسَلِينَ ﴿٤٩﴾ اتَّبِعُوا مَنْ لَّا يَسْأَلُكُمْ أَجْرًا

**“Na akaja mtu mbio kutokea upande wa mbali wa mjini, akikimbia akasema: Enyi watu wangu! Wafuateni hawa waliotumwa. Wafuateni ambao hawakutakini ujira.” (36:20-21).**

Na Kauli Yake:

وَأَنَّكَ لَتَدْعُوهُمْ إِلَىٰ صِرَاطٍ مُسْتَقِيمٍ ﴿٥٠﴾ وَإِنَّ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ عَنِ الصِّرَاطِ لَنُكَيِّبُونَ ﴿٥١﴾

**“Na kwa yakini wewe unawaita kwenye njia iliyonyooka. Na hakika wale wasioiamini Akhera wanajitenga na njia hiyo”.**

Imamu Ahmad amenukuu kutoka kwa Ibn Abbas رضي الله عنهما, kwamba Mtume ﷺ alijiwa usingizini na Malaika wawili, mmoja akakaa miguuni mwake, na mwengine kichwani pake.

Malaika aliyekaa kichwani pa Mtume akasema: ‘Mfananishie mfano unaolandana na Umma wake.’ Malaika akasema: ‘Hakika mfano wake yeye

na Umma wake, ni kama watu walio safarini, wakafika katikati ya Jangwa, huku wameishiwa na chakula pamoja na masurufu ya safari yatakwawavukisha katika Jangwa au yale yatakwawawezesha kurudi nyuma. Wakati wakiwa katika hali hiyo, ghafla wakatokewa na mtu aliyekuwa na mavazi yenye kupendeza. Akasema: 'Mnaonaje kama nitawapa mbogamboga za majani na kibuyu cha maji?' Wakajibu: 'Ndio.' Akasema: Mtu yule akawaambia: 'Hivi sikuwakuteni katika hali hiyo, nikawafanya iwapo mnataka niwape mbogamboga na kibuyu cha maji sharti mnifuate?' Wakajibu: 'Ndio tutakufuata.' Mtume akasema: 'Hakika mna nyinyi mbogamboga zenye vitamini kuliko hizi, hivyo basi nifuateni mimi.' Akasema: 'kikundi kimoja kikasema: 'umesema kweli, naapa kwa Allah تعالى tutamfuata.' Kikundi kingine kikasema, 'tumeridhia na haya tuliyoypata huku, hivyo tunatosheka nayo.'<sup>1</sup>

### Hali za Makafiri

Na Kauli Yake:

﴿ وَإِنَّ الَّذِينَ لَا يُؤْمِنُونَ بِالْآخِرَةِ عَنِ الصِّرَاطِ لَنُكَيِّبُونَ ﴾

***“Na hakika wale wasioiamini Akhera wanajitenga na njia hiyo.”***

Maana yake: wamepotea na kukengeuka. kama isemwavyo kuwa: Amejitenga fulani na njia anapopotoka na kupotea. Na Kauli Yake:

﴿ \* وَلَوْ رَحِمْنَاهُمْ وَكَشَفْنَا مَا بِهِمْ مِّنْ ضُرٍّ لَّلْجُؤِ فِي طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُونَ ﴾

***“Na lau Tungeliwarehemu na Tukawaondolea shida waliyonayo bila ya shaka wangelindelea katika upotofu wao vile vile, wakitangatanga.”***

Anatupasha Aliyetukuka kuhusu inadi na ukaidi wa ukafiri kwa kuwa hata kama Aliwaondoshea madhara na Kuwafanya waifahamu Qur’ani, bado hawataifuata; wangeendelea katika ukafiri wao, inadi na ukaidi wao wa kuchupa mipaka. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

<sup>1</sup> Ahmad 1:267. Isnadi yake ni dhaifu.

وَلَوْ عَلِمَ اللَّهُ فِيهِمْ خَيْرًا لَأَسْمَعَهُمْ ۗ وَلَوْ أَسْمَعَهُمْ لَتَوَلَّوْا وَهُمْ مُعْرِضُونَ ﴿٦٨﴾

**“Na kama Allah Angelijua wema wowote kwao, Angewasikilizisha; na kama Angewasikilizisha wangeligeuka vile vile wakapuuza.” (8:23).**

Na Amesema:

وَلَوْ تَرَىٰ إِذْ وُفِقُوا عَلَى النَّارِ فَقَالُوا يَلَيْتَنَا نُرُدُّ وَلَا نُكَذِّبُ بِمَا يَدَّبُّ رَبَّنَا وَنَكُونَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿٦٩﴾ بَلْ بَدَأَ هُمْ مَّا كَانُوا يُحْتَفُونَ مِنْ قَبْلُ ۗ وَلَوْ رُدُّوْا لَعَادُوا لِمَا نُهُوا عَنْهُ وَإِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ ﴿٧٠﴾

**“Na ungeona Siku ya Kiyama watakaposimamishwa kwenye Moto, wakawa wanasema, ‘Laiti tungerudishwa ulimwenguni; wala hatutakadhibisha tena Aya za Mola wetu Mlezi, na tutakuwa katika wanaoamini’. Bali yamewadhihirikia waliokuwa wakiyaficha zamani. Na kama wangelirudishwa bila shaka wangeliyarudia waliyokatazwa.” (6:27-28).**

Mpaka Kauli Yake:

بِمَبْعُوثِينَ ﴿٧١﴾

**“Hatutafufuliwa.”**

Haya ni katika yaliyo katika Elimu Yake Aliyetukuka kwani Yeye Ndiye Mwenye Kujua kitu ambacho hakitatukia, na lau kingetokea, Anajua vilivyo kitakavyotokea. Amepokea Adh-Dhahaak kuwa Ibn ‘Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Kila lililomo katika ‘- lau’ ni kitu ambacho hakitatokea kabisa”.

وَلَقَدْ أَخَذْنَاهُمْ بِالْعَذَابِ فَمَا اسْتَكَاثُوا لِرَبِّهِمْ وَمَا يَتَضَرَّعُونَ ﴿٧٢﴾ حَتَّىٰ إِذَا فَتَحْنَا عَلَيْهِم بَابًا ذَا عَذَابٍ شَدِيدٍ إِذَا هُمْ فِيهِ مُبْلِسُونَ ﴿٧٣﴾ وَهُوَ الَّذِي أَنْشَأَ لَكُمُ السَّمْعَ وَالْأَبْصَرَ وَالْأَفْئِدَةَ ۗ قَلِيلًا مَّا تَشْكُرُونَ ﴿٧٤﴾ وَهُوَ الَّذِي ذَرَأَكُمْ فِي الْأَرْضِ وَإِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ﴿٧٥﴾ وَهُوَ الَّذِي يُحْيِي وَيُمِيتُ ۗ وَلَهُ اخْتِلَافُ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ ۗ أَفَلَا تَعْقِلُونَ ﴿٧٦﴾ بَلْ

قَالُوا مِثْلَ مَا قَالَ الْأُولَئِكَ ﴿٦٨﴾ قَالُوا أَءِذَا مِتْنَا وَكُنَّا تُرَابًا وَعِظْمًا أَءِنَّا لَمَبْعُوثُونَ

﴿٦٩﴾ لَقَدْ وَعَدْنَا نَحْنُ وَءَابَاؤُنَا هَذَا مِنْ قَبْلُ إِنْ هَذَا إِلَّا أَسَاطِيرُ الْأَوَّلِينَ ﴿٧٠﴾

**76. Na hakika Tuliwatia adhabu kali; lakini hawakuelekea kwa Mola wao Mlezi wala hawakunyenyeka.**

**77. Mpaka Tulipowafungulia mlango wa adhabu kali, hapo ndipo wakawa wenye kukata tamaa.**

**78. Na Yeye Ndiye Aliyekuumbieni Kusikia na Kuona na nyoyo za kufahamu. Ni kuchache mno kushukuru kwenu.**

**79. Na Yeye Ndiye Aliyekuenezeni katika ardhi, na Kwake Yeye mutakusanywa.**

**80. Na Yeye Ndiye Anayehuisa na Kufisha, na Yake Yeye mabadiliko ya usiku na mchana. Basi je! Hamufahamu?**

**81. Bali wanasema kama walivyosema watu wa kwanza.**

**82. Walisema: Je! Tukishakufa tukawa udongo na mifupa ndio tutafufuliwa?**

**83. Tuliahidiwa haya sisi na baba zetu zamani. Hayakuwa haya ila ni visa vya uongo vya watu wa zamani.**

Anasema Aliyetukuka:

وَلَقَدْ أَخَذْنَاهُمْ بِالْعَذَابِ

**“Na hakika Tuliwatia adhabu kali”.**

Maana yake: Tuliwatia katika mitihani kwa misiba na shida.

فَمَا اسْتَكَثُوا لِرَبِّهِمْ وَمَا يَتَضَرَّعُونَ ﴿٧١﴾

**“Lakini hawakuelekea kwa Mola wao Mlezi wala hawakunyenyeka.”**

Maana yake: Hilo halikuwarudisha wao kutoka katika ukafiri wao wala kwenda kinyume kwao, bali waliendelea katika madhambi na upotevu wao.

فَمَا اسْتَكَاثُوا

*“Lakini hawakuelekea...”*

Maana yake: Hawakuogopa,

وَمَا يَتَضَرَّعُونَ ﴿٦٨﴾

*“Wala hawakunyenyekoa.”*

Ni kama Aliyetukuka alivyosema,

فَلَوْلَا إِذْ جَاءَهُمْ بَأْسُنَا تَضَرَّعُوا وَلَٰكِن قَسَتْ قُلُوبُهُمْ

*“Kwa nini wasinyenyekoe ilipowafikia adhabu Yetu? Walakini nyoyo zao zilikuwa ngumu...” (6:43).*

Na amepokea Ibn Abi Haatim kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Abu Sufyaan alikuja kwa Mtume ﷺ akamuambia: ‘Ewe Muhammad! Nakuomba kwa Jina la Allah تعالى na mahusiano ya ujamaa baina yetu, hakika tumekula nyoya za ngamia na damu’.

Hapo Allah تعالى Akateremsha:

وَلَقَدْ أَخَذْنَاهُم بِالْعَذَابِ فَمَا اسْتَكَاثُوا

*‘Na hakika Tuliwatia adhabu kali; lakini hawakuelekea...’.*

Na hivyo ndivyo ilivyopokewa na An-Nasaa’iy<sup>1</sup>. Na asili ya Hadithi hii katika Sahihi Mbili kuwa Mtume ﷺ aliomba dhidi ya Maquraysh pindi walipokataa na kuasi, akasema:

«اللَّهُمَّ أَعْنِي عَلَيْهِمْ بِسَبْعِ كَسْبِ يُوسُفَ»

*“Ewe Allah, nisaidie dhidi yao kwa kuwatumia wao miaka saba (ya ukame) kama miaka saba ya ukame ya Yusuf”<sup>1</sup>.*

<sup>1</sup> An-Nasaa’iy katika Al-Kubraa 6:413.

<sup>2</sup>Fat’h Al-Baariy 8:435 na Muslim 4:2156.



Na Kauli Yake:

حَتَّىٰ إِذَا فَتَحْنَا عَلَيْهِم بَابًا ذَا عَذَابٍ شَدِيدٍ إِذَا هُمْ فِيهِ مُبْلِسُونَ ﴿٧٦﴾

***“Mpaka Tulipowafungulia mlango wa adhabu kali, hapo ndipo wakawa wenye kukata tamaa.”***

Maana yake: Mpaka ilipofika Amri ya Allah تعالی na Siku ya Malipo kuwajia kwa ghafla na kuwafikia wao adhabu ya Allah تعالی bila kutegemea, hapo watakata tamaa kwa kheri na ushahidi wowote na matumaini yao yote kupotea.

### **Kukumbushwa Neema za Allah تعالی na Uweza Wake Mkubwa**

Kisha Ametaja Allah تعالی Neema Zake kwa waja Wake kwa Kuwapa wao usikivu, uoni na nyoyo za kufahamu.

Na hizo ni akili na ufahamu ambazo kwao wanakuja kujua vitu na kupata mafunzo kwa vilivyo katika ulimwengu katika miujiza na ishara kama dalili ya Upweke wa Allah تعالی, Mwenye Uweza wa Kufanya Atakalo na Kuchagua Atakalo.

Na Kauli Yake:

قَلِيلًا مَّا تَشْكُرُونَ ﴿٧٧﴾

***“Ni kuchache mno kushukuru kwenu.”***

Maana yake: Ni uchache wa kumshukuru kwenu Allah تعالی kwa Neema Aliyokupeni. Hii ni kama Kauli Yake:

وَمَا أَكْثَرُ النَّاسِ وَلَوْ حَرَصْتَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿١٠٣﴾

***“Na wengi katika watu hawatakuwa wenye kuamini hata ukijitahidi vipi.” (12:103).***

Kisha Ametaja Aliyetukuka kwa Nguvu Zake kuu Alizonazo na Ufalme Wake wenye Kushinda, kwani Yeye Ndiye Mwenye Kuanzisha Kuumba na Kuwaweka watu katika sehemu zote za ardhi, kwa mataifa yao tofauti, lugha na sifa zao. Baadaye Siku ya Kiyama Atawakusanya wote pamoja, wa kwanza na wa mwisho, kwa wakati maalumu na hakuna atakayeachwa nje, mdogo au mzee,

mwanamume au mwanamke, mtukufu au mdhalifu, lakini wote watafufuliwa na kurudishwa kama walivyokuwa hapo awali. Na kwa hiyo Akasema:

وَهُوَ الَّذِي تَحِيَّ وَيُحْيِي

**“Na Yeye Ndiye Anayehuisha na kufisha”.**

Maana yake: Ataikusanya mifupa na Kuihuisha na Kuleta umauti kwa mataifa yote,

وَلَهُ اخْتِلَافُ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ

**“Na Yake Yeye mabadiliko ya usiku na mchana”.**

Maana yake: Kwa Amri Yake usiku na mchana vinatiishwa, kila kimoja kikifuata kingine na bila kutoka katika mfumo huo. Hii ni kama Kauli Yake:

لَا الشَّمْسُ يَنْبَغِي هَآءَا أَنْ تُدْرِكَ الْقَمَرَ وَلَا اللَّيْلُ سَابِقُ النَّهَارِ

**“Haliwi jua kuufikia mwezi, wala usiku kuupita mchana...” (36:40).**

Na Kauli Yake:

أَفَلَا تَعْقِلُونَ

**“Basi je! Hamfahamu?”**

Maana yake: Je, nyinyi hamna akili inayowatambulisha kuwa Mwenye Nguvu ni Mjuzi, ambaye vitu vyote hutiihwa Kwake, na ni Mwenye nguvu juu ya vitu vyote na vitu vyote vinanyenyekea?

### **Washirikina Kukanusha Kwao Kufufuliwa Baada ya Kufa**

Kisha Akasema kuhusu wenye kukanusha ufufuo, ambao wamefanana na wakanushaji waliokuwa kabla yao:

بَلْ قَالُوا مِثْلَ مَا قَالَ الْأَوَّلُونَ

قَالُوا أَعْدَا مِثْنَا وَكُنَّا تُرَابًا وَعِظْمًا أَيْنَا

لَمَبْعُوثُونَ

**“Bali wanasema kama walivyosema watu wa kwanza. Walisema: Je! Tukisha kufa tukawa udongo na mifupa ndio tutafufuliwa?”**

Maana yake: Walidhania kuwa hilo haliwezekani kutokea baada ya kuoza na kutokuwa chochote.

لَقَدْ وَعَدْنَا نَحْنُ وَءَابَاؤُنَا هَذَا مِنْ قَبْلُ إِنْ هَذَا إِلَّا أَسْطِيرُ الْأَوَّلِينَ

**“Tuliahidiwa haya sisi na baba zetu zamani. Hayakuwa haya ila ni visa vya uwongo vya watu wa zamani.”**

Wakimaanisha haiwezekani kuwa tutarudishwa tena duniani. Haya yalisemwa na wale waliojifunza kutoka katika watu wa vitabu na tofauti zao. Kukanusha na kukadhibisha huku kwao ni kama Kauli Yake Kutuelezea kuhusu wao:

أَإِذَا كُنَّا عِظْمًا نُحْرَةً ۖ قَالُوا تِلْكَ إِذًا كَرَّةٌ خَاسِرَةٌ ۗ فَإِنَّمَا هِيَ زَجْرَةٌ وَاحِدَةٌ ﴿٧٩﴾  
فَإِذَا هُمْ بِالسَّاهِرَةِ ﴿٨٠﴾

**“Hata tukiwa mifupa mibovu? (Wanasema kwa stihzai): ‘Basi marejeo haya ni yenye hasara kwetu’. Kwa hakika hicho (Kiyama) kitakuwa ukelele mmoja tu. Mara wao viumbe wote watakuwa katika ardhi mpya.” (79:11-14).**

Na Allah تعالی Amesema :

أَوَلَمْ يَرِ الْإِنْسَانُ أَنَّا خَلَقْنَاهُ مِنْ نُطْفَةٍ فَإِذَا هُوَ خَصِيمٌ مُبِينٌ ﴿٧٧﴾ وَضَرَبَ لَنَا مَثَلًا  
وَنَسِيَ خَلْقَهُ ۗ قَالَ مَنْ يُحْيِ الْعِظْمَ وَهِيَ رَمِيمٌ ﴿٧٨﴾ قُلْ يُحْيِيهَا الَّذِي أَنْشَأَهَا أَوَّلَ مَرَّةٍ  
ۗ وَهُوَ بِكُلِّ خَلْقٍ عَلِيمٌ ﴿٧٩﴾

**“Je, mwanadamu hatambui ya kwamba Tumemuumba kwa tone la manii? Amekuwa hasimu yetu aliye dhahiri! Na Akatupigia mfano, na akasahau Kuumbwa kwake (kwa manii) – akasema: ‘Nani atakayeihisha mifupa na hali imesagika?’ Sema: ‘Ataihuisha Yule Aliyeiumba mara ya kwanza, naye ni Mjuzi wa kila (namna ya) Kuumba.” (36:77-79).**

قُلْ لِمَنِ الْأَرْضُ وَمَنْ فِيهَا إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٨٤﴾  
 سَيَقُولُونَ لِلَّهِ ۗ قُلْ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴿٨٥﴾ قُلْ مَنْ رَبُّ  
 السَّمَوَاتِ السَّبْعِ وَرَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ ﴿٨٦﴾ سَيَقُولُونَ  
 لِلَّهِ ۗ قُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ ﴿٨٧﴾ قُلْ مَنْ بِيَدِهِ مَلَكُوتُ  
 كُلِّ شَيْءٍ وَهُوَ يُجِيرُ وَلَا يُجَارُ عَلَيْهِ إِنْ كُنْتُمْ تَعْمُونَ ﴿٨٨﴾  
 سَيَقُولُونَ لِلَّهِ ۗ قُلْ فَأَنَّى تُشْحَرُونَ ﴿٨٩﴾ بَلْ  
 أَتَيْنَهُم بِالْحَقِّ وَإِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ ﴿٩٠﴾ مَا أَخَذَ اللَّهُ مِنْ وَلَدٍ  
 وَمَا كَانَ مَعَهُ مِنْ إِلَهٍ إِذَا أَذَاهُ كُلُّ إِلَهٍ بِمَا خَلَقَ  
 وَلَعَلَّا بَعْضُهُمْ عَلَى بَعْضٍ سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يُصِفُونَ ﴿٩١﴾  
 عَنِ الْعَالَمِينَ ﴿٩٢﴾ عَنِ الْعَالَمِينَ ﴿٩٣﴾ عَنِ الْعَالَمِينَ ﴿٩٤﴾  
 قُلْ رَبِّ إِمَّا تُرِيدُنِي مَا يُوعَدُونَ ﴿٩٥﴾ رَبِّ فَلَا  
 تَجْعَلْنِي فِي الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿٩٦﴾ وَإِنَّا عَلَىٰ أَنْ نُرِيكَ مَا  
 نَعِدُهُمْ لَقَدِيرُونَ ﴿٩٧﴾ أَدْفَعْ بِاللَّيْلِ هِيَ أَحْسَنُ السَّيِّئَةِ ۗ  
 نَحْنُ أَعْلَمُ بِمَا يَصِفُونَ ﴿٩٨﴾ وَقُلْ رَبِّ أَعُوذُ بِكَ مِنْ  
 هَمَزَاتِ الشَّيْطَانِ ﴿٩٩﴾ وَأَعُوذُ بِكَ أَنْ يَحْضُرُونِ  
 حَتَّىٰ إِذَا جَاءَ أَحَدَهُمُ الْمَوْتُ قَالَ رَبِّ ارْجِعُونِ ﴿١٠٠﴾  
 لَعَلِّي أَعْمَلُ صَالِحًا فِيمَا تَرَكْتُ ۗ كَلَّا ۗ إِنَّهَا كَلِمَةٌ هُوَ  
 قَائِلُهَا ۗ وَمِنْ وَرَائِهِمْ بَرْزَخٌ إِلَىٰ يَوْمِ يُبْعَثُونَ ﴿١٠١﴾

قُلْ لِمَنِ الْأَرْضُ وَمَنْ فِيهَا إِنْ  
 كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٨٤﴾ سَيَقُولُونَ  
 لِلَّهِ ۗ قُلْ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴿٨٥﴾ قُلْ  
 مَنْ رَبُّ السَّمَوَاتِ السَّبْعِ وَرَبُّ  
 الْعَرْشِ الْعَظِيمِ ﴿٨٦﴾ سَيَقُولُونَ  
 لِلَّهِ ۗ قُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ ﴿٨٧﴾ قُلْ  
 مَنْ بِيَدِهِ مَلَكُوتُ كُلِّ شَيْءٍ وَهُوَ  
 يُجِيرُ وَلَا يُجَارُ عَلَيْهِ إِنْ كُنْتُمْ  
 تَعْمُونَ ﴿٨٨﴾ سَيَقُولُونَ لِلَّهِ ۗ قُلْ  
 فَأَنَّى تُشْحَرُونَ ﴿٨٩﴾ بَلْ أَتَيْنَهُم  
 بِالْحَقِّ وَإِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ ﴿٩٠﴾

84. Sema: Ni ya nani ardhi na viliomo ndani yake, kama nyinyi mnajua?

85. Watasema: Ni vya Allah! Sema: Basi, je, hamkumbuki?

86. Sema: Ni nani Mola Mlezi wa mbingu saba na Mola Mlezi wa Arshi Kuu?

87. Watasema: Ni vya Allah. Sema: Basi je, hamuogopi?

88. Sema: Ni nani Mkononi Mwake Umo Ufalme wa kila kitu, Naye Ndiye Anayelinda, wala Hakilindwi Asichotaka, kama mnajua?

**89. Watasema: (Ufalme huo) ni wa Allah. Sema: Basi vipi mnadanganyika?**

**90. Bali Tumewaletea Haki, na kwa yakini hao ni waongo.**

### Washirikina Hukubali Kuwepo Muumba Lakini Wanamshirikisha Allah تعالیٰ Katika Ibada

Anakiri Allah تعالیٰ Upweke na kuwa Yeye Yu Pekee katika Kuumba Kwake, Udhhibiti, Mamlaka na Kuongoza, Yeye ni Allah تعالیٰ Ambaye hapana apasaye kuabudiwa kwa haki ila Yeye. Na hakuna afaaye kuabudiwa ila Yeye Peke Yake, hana mshirika. Kwa hiyo Akamuambia Mtume Wake Muhammad ﷺ awaambie washirikina wenye kuabudu asiyekuwa Yeye, mbali ya kuwa wanakubali Ubwana Wake, kuwa hana mshirika katika Ubwana na Umola Wake. Mbali na hilo bado wanamshirikisha katika Uungu Wake na kuabudu wengine mbali na Yeye japokuwa wanatambua kuwa wale wanaowaabudu hawawezi kuumba wala hawamiliki chochote wala hawana udhibiti wa lolote. Hata hivyo, bado wanaamini kuwa viumbe hivi vinaweza kuwaleta karibu na Allah تعالیٰ,

مَا نَعْبُدُهُمْ إِلَّا لِيُقَرِّبُونَا إِلَى اللَّهِ زُلْفَىٰ

**“Sisi hatuwaabudu hawa ila wapate kutufikisha karibu kabisa na Allaah...” (39:3).**

Akasema:

قُلْ لِمَنِ الْأَرْضُ وَمَنْ فِيهَا

**“Sema: Ni ya nani ardhi na viliomo ndani yake”,**

Maana yake: Mwenye Kumiliki kwa Alivyoviumba na vilivyo ndani yake miongoni mwa wanyama, mimea, matunda na aina nyingine nyingi ya viumbe.

إِنْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٢٤﴾ سَيَقُولُونَ لِلَّهِ

**“Kama nyinyi mnajua? Watasema: Ni vya Allah!”**

Maana yake: Watakubali kuwa hilo ni la Allah تعالیٰ Peke Yake bila kuwa na mshirika pamoja Naye. Ikiwa hiyo ndiyo hali,

قُلْ أَفَلَا تَذَكَّرُونَ ﴿٨٤﴾

**“Sema: Basi, je, hamkumbuki?”**

Hakuna anayepaswa kuabudiwa isipokuwa Muumba na Mwenye Kuruzuku wala si mwengine yeyote.

قُلْ مَنْ رَبُّ السَّمَوَاتِ السَّبْعِ وَرَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ ﴿٨٥﴾

**“Sema: Ni nani Mola Mlezi wa mbingu saba na Mola Mlezi wa Arshi Kuu?”**

Maana yake: Ni nani Muumba wa ulimwengu wa juu vikiwemo sayari, mwangaza na Malaika wanyenyekevu Kwake katika maeneo yote na sehemu zote? Na ni nani Mola Mlezi wa Arshi Kuu, yaani ambacho ni sakafu (kipo juu) ya viumbe vyote? Na hivyo, Akasema hapa:

وَرَبُّ الْعَرْشِ الْعَظِيمِ ﴿٨٦﴾

**“Na Mola Mlezi wa Arshi Kuu?”** Maana yake: Kubwa. Na Akasema mwisho wa Sura:

رَبُّ الْعَرْشِ الْكَرِيمِ ﴿٨٧﴾

**“Mola Mlezi wa Arshi Tukufu.” (23:116),**

Maana yake: Nzuri na kupendeza. Hakika Arshi hiyo imechang'anya baina ukubwa wa upana na kuwa juu na uzuri wa kupendeza sana. Na kwa ajili hiyo ndio akasema mwenye kusema: Hakika hiyo imetengenezwa na yakuti nyekundu. Na amesema Ibn Mas'ud رضي الله عنه: “Hakika hakuna usiku wala mchana kwa Mola wenu Mlezi, Nuru ya Arshi inatokana na Nuru”. Na Kauli Yake:

سَيَقُولُونَ لِلَّهِ قُلْ أَفَلَا تَتَّقُونَ ﴿٨٨﴾

**“Watasema: Ni vya Allah. Sema: Basi je, hamuogopi?”**

Maana yake: Ikiwa kweli mnatambua kuwa Yeye Ndiye Mola Mlezi wa mbingu na Mola Mlezi wa Arshi Kuu, je, basi hamuogopi adhabu Yake na kutahadhari adhabu Yake kwa kuabudu kwenu pamoja Naye mwingine yeyote yule na kumshirikisha Yeye na wengine?

قُلْ مَنْ بِيَدِهِ مَلَكُوتُ كُلِّ شَيْءٍ

**“Sema: Ni nani Mkononi Mwake Umo Ufalme wa kila kitu.”**

Maana yake: Ufalme upo Mkononi Mwake.

مَا مِنْ دَابَّةٍ إِلَّا هُوَ آخِذٌ بِنَاصِيَتِهَا

**“...Hakuna kiumbe chochote isipokuwa Allah Anakisarifu na Kukiendesha Atakavyo...” (11:56),**

Maana yake: Anakisarifu na Kukidhibiti. Na alikuwa Mtume ﷺ akisema:

«لَا وَالَّذِي نَفْسِي بِيَدِهِ»

**“Hapana, kwa Yule Ambaye nafsi Yangu iko Mkononi Mwake”.**

Na alipokuwa akila kiapo, alikuwa akisema,

«لَا وَمَقَلْبِ الْقُلُوبِ»

**“Hapana, kwa Mwenye Kugeuza (Kuisarifu) mioyo”.**

Na Yeye Aliyetukuka Ndiye Muumba, Mfalme na Mwenye Kusarifu,

وَهُوَ مُجِيرٌ وَلَا يُجَارُ عَلَيْهِ إِنْ كُنْتُمْ تَعْمُونَ ﴿٥٦﴾

**“Naye Ndiye Anayelinda, wala hakilindwi Asichotaka, kama munajua?”**

Walikuwa Waarabu akiwa mkubwa yeyote miongoni mwao, naye akampa ulinzi mtu hakuna hata mmoja atakwenda dhidi yake, ilhali hakuna hata mmoja anayeweza kumlinda kiongozi huyo. Kwa hiyo, Akasema Allah تعالى:

وَهُوَ مُجِيرٌ وَلَا يُجَارُ عَلَيْهِ

**“Naye Ndiye Anayelinda, wala hakilindwi Asichotaka.”**

Maana yake: Naye Ndiye Bwana Mkuu, na hakuna aliye mkubwa kuliko Yeye. Zake ni Nguvu za Kuumba na Kuamrisha, na hakuna hata mmoja anayeweza

kupindua au kwenda kinyume na Hukumu Yake. Lolote Analotaka linatokea, na Asilotaka, halitatendeka. Na Amesema Allah تعالى:

لَا يُسْأَلُ عَمَّا يَفْعَلُ وَهُمْ يُسْأَلُونَ ﴿٢٣﴾

**“Haulizwi (Allah) Anayoyafanya (kwani yote ni ya haki) lakini wao viumbe wataulizwa.” (21:23),**

Maana yake: Haulizwi kwa Anachofanya kwa sababu ya Ukubwa Wake, Kiburi Chake, Ushindi Wake, Nguvu Zake, Hekima Yake na Uadilifu Wake, lakini viumbe Vyake vyote vitaulizwa kwa walivyofanya, kama Alivyosema Aliyetukuka:

فَوَرَبِّكَ لَنَسْأَلَنَّهُمْ أَجْمَعِينَ ﴿٩٢﴾ عَمَّا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿٩٣﴾

**“Basi ndivyo Wallahi Tutakavyowauliza wote hao Siku ya Kiyama. Juu ya yale waliyokuwa wakiyatenda.” (15:92-93).**

Na Kauli Yake:

سَيَقُولُونَ لِلَّهِ

**“Watasema: (Ufalme huo) ni wa Allah.”**

Maana yake: Watakuja fahamu kuwa Bwana Mkuu Ambaye Analinda wote wala Hana mlinzi, Naye ni Allah تعالى Peke Yake, Hana mshirika kabisa.

قُلْ فَأَنِّي تُسْحَرُونَ ﴿٩٤﴾

**“Sema: Basi vipi munadanganyika?”**

Maana yake: Vipi akili yako itakubali wazo la kuabudu mwingine mbali na Yeye ilhali unatambua na kujua hilo? Kisha Akasema Aliyetukuka:

بَلْ أَتَيْنَاهُم بِالْحَقِّ

**“Bali Tumewaletae Haki.”**

Hilo ni tangazo kuwa hakuna mungu apasaye kuabudiwa kwa haki ila Allah تعالى, Na tumesimamisha dalili sahihi zilizo wazi za kukinaisha kuhusu suala hilo.



وَإِنَّهُمْ لَكَاذِبُونَ ﴿١١٥﴾

**“Na kwa yakini hao ni waongo.”**

Maana yake: katika kuabudu kwao pamoja na Allah تعالى, wala hawana dalili kwa hayo, kama Anavyosema Aliyetukuka mwisho wa Sura:

وَمَنْ يَدْعُ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ لَا بُرْهَانَ لَهُ بِهِ فَإِنَّمَا حِسَابُهُ عِنْدَ رَبِّهِ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ

الْكَافِرُونَ ﴿١١٧﴾

**“Na anayemuomba - pamoja na Allah - mungu mwengine hana ushahidi wa hili; basi bila ya shaka hesabu yake iko kwa Mola wake Mlezi. Kwa hakika makafiri hawafanikiwi.” (23:117).**

Hakika washirikina hawana dalili inayowaongoza wao katika uongo na upotovu wao. Na hakika wanafanya hayo kwa kufuata mababa zao na waliowatangulia waliokuwa wamechanganyikiwa na wajinga. Kama Alivyosema Allah تعالى kuwahusu:

إِنَّا وَجَدْنَا آبَاءَنَا عَلَىٰ أُمَّةٍ وَإِنَّا عَلَىٰ آثَرِهِمْ مُّقْتَدُونَ ﴿٤٣﴾

**“Kwa yakini tuliwakuta baba zetu juu ya desturi zao mahsusi, na hakika sisi tutafuata nyayo zao.” (43:23).**

مَا اتَّخَذَ اللَّهُ مِنْ وَلَدٍ وَمَا كَانَ مَعَهُ مِنْ إِلَهٍ إِذًا لَذَهَبَ كُلُّ إِلَهٍ بِمَا خَلَقَ وَلَعَلَّ

بَعْضُهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يُصِفُونَ ﴿١٦﴾ عَلِيمِ الْغَيْبِ وَالشَّهَادَةِ فَتَعَلَّىٰ

عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿١٧﴾

**91. Allah Hana mwana yeyote, wala Hanaye mungu mwengine. Ingekuwa hivyo basi kila mungu angelichukua alivyoumba, na baadhi yao wangeliwashinda wengine. Allah Ameepukana na sifa wanazomsifu.**

**92. Mjuzi wa siri na dhahiri, na Ametukuka juu ya hayo wanayo mshirikisha nayo.**

**Allah تعالیٰ Hana mshirika**

Allah تعالیٰ Anaitakasa Nafsi Yake, kuwa Yeye Hana mtoto wala mshirika katika Mamlaka Yake, Kuendesha Kwake mambo na Ibada Yake. Akasema Aliyetukuka:

مَا اتَّخَذَ اللَّهُ مِنْ وَلَدٍ وَمَا كَانَ مَعَهُ مِنْ إِلَهٍ إِذًا لَذَهَبَ كُلُّ إِلَهٍ بِمَا خَلَقَ وَلَعَلَّ  
بَعْضُهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ

***“Allah Hana mwana yeyote, wala Hanaye mungu mwengine. Ingekuwa hivyo basi kila mungu angelichukua alivyoumba, na baadhi yao wangeliwashinda wengine.”***

Maana yake: Kama ingepitishwa kuwe na miungu wengi, kila mmoja wao angekuwa na udhibiti hasa kwa kila alichokiumba, hivyo hakungekuwa na nidhamu yoyote ile. Na tunavyoona ni kuwa ulimwengu una nidhamu, unaoshikamana, kwa ulimwengu ulio juu na chini, zinazoshikana moja kwa nyingine kwa njia iliyo nzuri zaidi na upeo wa ukamilifu.

مَا تَرَىٰ فِي خَلْقِ الرَّحْمَنِ مِنْ تَفَوتٍ

***“Huoni tofauti yoyote katika Uumbaji wa Mwingi wa Rehema...”***  
(67:3).

Hata hivyo, lau kungekuwa na miungu wengi, kila mmoja wao angejaribu kumshinda mwenziwe kwa uadui, na mmoja angemshinda mwengine. Hili limetajwa na wanazuoni wa Falsafa<sup>1</sup>, walioieleza kutumia dalili za ukinzani. Nayo ni kuwa lau kungekuwa na waumbaji wawili au zaidi, mmoja wao akataka kuuchezesha mwili ilhali mwingine anataka usimame, na lau wote hawatafanikiwa wanachotaka, basi wote watakuwa si waweza, lakini kwa Yule Ambaye Kuwepo Kwake ni muhimu na lazima (Maana yake Allah تعالیٰ) Hawezi Kushindwa. Haiwezekani kwa muradi wa wote wawili kutekelezwa kwa sababu ya mapambano. Tatizo hili linapatikana tu pale kunapokuwa na wingi wa miungu, hivyo inakuwa ni muhali kuwepo na wingi huo, kwa sababu

<sup>1</sup> Hii ni ibara inayotumiwa kwa wanazuoni wa Kiislamu wanaotumia falsafa katika mafunzo yao.

lau matakwa ya mmoja wao yatatekelezwa na sio kwa mwingine, yule anayeshinda ndiye kuwepo kwake kutakuwa ni muhimu (Maana yake Allah تعالى) na anayeshindwa hawezi kuwa mungu, kwani haiwezekani kwa anayeshindwa kuwepo kwake kuwa ni muhimu.

Kwa hiyo, Akasema Aliyetukuka:

وَلَعَلَّا بَعْضُهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ سُبْحٰنَ ٱللَّهِ عَمَّا يَصِفُونَ ﴿٧١﴾

***“Na baadhi yao wangeliwashinda wengine. Allah Ameepukana na Sifa wanazo msifu.”***

Maana yake: Kwa wanayosema madhalimu waliochupa mipaka wenye inadi katika madai yao kuwa Allah تعالى ana mtoto au mshirika.

عَلِمَ ٱلْغَيْبِ وَٱلشَّهَادَةِ

***“Mjuzi wa siri na dhahiri.”***

Maana yake: Anajua yote yaliyofichikana na viumbe vyake na kwa wanayoona.

فَتَعَلَّىٰ عَمَّا يُشْرِكُونَ ﴿٧٢﴾

***“Na Ametukuka juu ya hayo wanayomshirikisha nayo.”***

Maana yake: Utukufu na Kutakasika ni Kwake juu ya yote yanayosemwa na madhalimu na waongo.

قُلْ رَبِّ إِمَّا تُرِيْبِي مَا يُوعَدُونَ ﴿٧٣﴾ رَبِّ فَلَا تَجْعَلْنِي فِي الْقَوْمِ ٱلظَّٰلِمِينَ ﴿٧٤﴾ وَإِنَّا عَلَىٰ أَنْ نُرِيْكَ مَا نَعِدُهُمْ لَقٰنِدِرُونَ ﴿٧٥﴾ أَدْفَعِ بِٱلَّتِي هِيَ أَحْسَنُ ٱلسَّيِّئَةِ ۖ نَحْنُ أَعْلَمُ بِمَا يَصِفُونَ ﴿٧٦﴾ وَقُلْ رَبِّ أَعُوذُ بِكَ مِنْ هَمَزَاتِ ٱلشَّيْطٰنِ ﴿٧٧﴾ وَأَعُوذُ بِكَ رَبِّ أَنْ يَحْضُرُونِ ﴿٧٨﴾

**93. Sema: Mola wangu Mlezi! Ukinionesha adhabu waliyoahidiwa.**

**94. Mola wangu Mlezi! Usinjaalie katika watu madhalimu hao.**

**95. Na hakika Sisi ni Waweza wa Kukuonesha Tuliyo waahidi.**

**96. Kinga maovu kwa kutenda yaliyo mema zaidi. Sisi Tunajua wayasemayo.**

**97. Na sema: Mola wangu Mlezi! Najikinga kwako na wasiwasi wa mashetani.**

**98. Na najikinga Kwako, Mola wangu Mlezi, wasinikaribie.**

**Amri ya Kuomba Dua Wakati wa Majanga, na Kuondosha Maovu kwa Kutenda Yaliyo Mazuri na Kutaka Ulinzi wa Allah تعالی**

Anasema Aliyetukuka kwa Kumuamuru Mtume Wake ﷺ kumuomba Yeye kwa kutumia dua hii anapokumbwa na matatizo:

رَبِّ إِمَّا تُرِيْبِي مَا يُوعَدُونَ ﴿٣٧﴾

**“Mola wangu Mlezi! Ukinionesha adhabu waliyoahidiwa.”**

Maana yake: Lau Utawaadhibu ilihali ninashuhudia hilo, hivyo Usinifanye mimi kuwa pamoja nao. Hii ni kama ilivyosemwa katika Hadithi iliyonukuliwa na Imaam Ahmad na At-Tirmidhiy, naye akaisahihisha:

«وَإِذَا أَرَدْتَ بِقَوْمٍ فَتَنَّهُ فَتَرَفَنِي إِلَيْكَ غَيْرَ مَمْتُونٍ»

**“Na Ukitaka kuwaonja watu, hivyo nichukue mimi Kwako (nifishe) bila ya Kunitia katika mitihani”.<sup>1</sup>**

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَإِنَّا عَلَىٰ أَنْ نُرِيْكَ مَا نَعِدُهُمْ لَقَدِيرُونَ ﴿٣٨﴾

**“Na hakika Sisi ni Waweza wa Kukuonesha Tuliyo waahidi.”**

Maana yake: Lau Tungetaka, Tungekuonesha adhabu, balaa na mtihani Tutakao wapelekea wao.

<sup>1</sup> Ahmad 5:243 na Tuhfatul Al-Ahwadh 9:108.

Kisha Akasema Aliyetukuka Kumuongoza katika njia bora ya kutangamana na watu, nayo ni kumtendea wema anayemfanyia ubaya, ili kulainisha moyo wake na kuubadilisha uadui kuwa urafiki na chuki kuwa upendo. Akasema Aliyetukuka:

أَدْفَعْ بِأَلَّتِي هِيَ أَحْسَنُ السَّيِّئَةِ

**“Kinga maovu kwa kutenda yaliyo mema zaidi”.**

Na hii ni kama Alivyosema katika Aya nyingine:

أَدْفَعْ بِأَلَّتِي هِيَ أَحْسَنُ فَإِذَا الَّذِي بَيْنَكَ وَبَيْنَهُ عَدَاوَةٌ كَأَنَّهُ وَلِيٌّ حَمِيمٌ ﴿٣٥﴾ وَمَا يُلْقِيهَا إِلَّا الَّذِينَ صَبَرُوا

**“Ondosha ubaya unaofanyiwa kwa wema; tahamaki yule ambaye baina yako na baina yake kuna uadui atakuwa kama ni jamaa yako mwenye kukufia uchungu. Lakini jambo hili hawatapewa ila wale wanaosubiri...” (41:34-35),**

Maana yake: Hakuna atakayesaidiwa wala kupewa ilhamu kufuata nasaha hii au kufikia sifa hii,

إِلَّا الَّذِينَ صَبَرُوا

**“Ila wale wanaosubiri”.**

Maana yake: Wale wenye kusubiri maudhi ya watu kwa kuishi nao kwa wema na uzuri ilihali wao wanatendewa uovu na ubaya.

وَمَا يُلْقِيهَا إِلَّا ذُو حَظٍّ عَظِيمٍ ﴿٣٦﴾

**“Wala hawatapewa ila wenye hadhi kubwa kwa Allah.”**

Maana yake: Duniani na Akhera.

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَقُلْ رَبِّ أَعُوذُ بِكَ مِنْ هَمَزَاتِ الشَّيْطَانِ ﴿٣٧﴾

**“Na sema: Mola wangu Mlezi! Najikinga kwako na wasiwasi wa mashetani”.**

Allah تعالى Amemuamuru kutaka kinga Kwake kutokana na shetani kwa sababu hakuna hila itakayokusaidia dhidi yao wala huwezi kujilinda kwa kuwaonea huruma wao. Tayari tumetangulia kuzungumzia kuhusu *Isti'adhah* (kujilinda) kuwa Mtume ﷺ alikuwa akisema:

«أَعُوذُ بِاللَّهِ السَّمِيعِ الْعَلِيمِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ مِنْ هَمْزِهِ وَنَفْحِهِ وَنَفْثِهِ»

*“Najikinga kwa Allah, Msikivu, Mjuzi kutokana na shetani aliyelaaniwa kutokana na nguvu zake na ufedhuli wake; ushawishi na ushairi wake”<sup>1</sup>.*

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَأَعُوذُ بِكَ رَبِّ أَنْ تَحْضُرُونِ ﴿٢٧﴾

***“Na najikinga Kwako, Mola wangu Mlezi, wasinikaribie.”***

Maana yake: Katika mambo yangu yote ya maisha. Hivyo tumeamriwa kumtaja Allah تعالى mwanzo wa kila jambo, ili kumuondoa shetani wakati wa kula, kujamiiana, kuchinja wanyama kwa ajili ya chakula, na kadhalika. Kuhusu hayo Abu Daud رحمه الله تعالى amepokea Hadithi kuwa Mtume ﷺ alikuwa akisema:

«اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْهَرَمِ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنَ الْهَيْدَمِ وَمِنَ الْغَرَقِ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ أَنْ يَتَحَبَّطَنِي الشَّيْطَانُ عِنْدَ الْمَوْتِ»

*“Ewe Allah, hakika mimi najikinga Kwako kutokana na zee, na najikinga Kwako kutokana na kuvunjwa na kughariki, na najikinga Kwako kutokana na kuvamiwa na shetani wakati wa kufa (kwangu)”<sup>2</sup>.*

حَتَّىٰ إِذَا جَاءَ أَحَدَهُمُ الْمَوْتُ قَالَ رَبِّ ارْجِعُونِ ﴿٢٨﴾ لَعَلِّي أَعْمَلُ صَالِحًا فِيمَا تَرَكْتُ

كَلَّا إِنَّهَا كَلِمَةٌ هُوَ قَائِلُهَا وَمِنْ وَرَائِهِمْ بَرْزَخٌ إِلَىٰ يَوْمِ يُبْعَثُونَ ﴿٢٩﴾

**99. Mpaka yanapomfikia mmoja wao mauti, husema: Mola wangu Mlezi! Nirudishe.**

<sup>1</sup> Abu Daawud 1:490.

<sup>2</sup> Abu Daawud 2:194.

**100. Ili nitende mema sasa badala ya yale niliyo yaacha. Wapi! Hii ni kauli aisemayo yeye tu. Na nyuma yao kipo kizuizi mpaka siku watapo fufuliwa.**

### Matamanio ya Kafiri Wakati wa Kuaga

Anatupasha habari Allah تعالى kuhusu hali ya kutokwa na roho na umauti miongoni mwa makafiri au wale waliopuuzwa Amri za Allah تعالى. Anatuambia anayosema na anavyoomba arudi tena duniani ili aweze kurekebisha makosa yote aliyofanya katika maisha yake. Anasema Aliyetukuka:

رَبِّ أَرْجِعُونِ ﴿١٠٠﴾ لَعَلِّي أَعْمَلُ صَالِحًا فِيمَا تَرَكْتُ كَلَّا

**“Mola wangu Mlezi! Nirudishe. Ili nitende mema sasa badala ya yale niliyoyaacha. Wapi!”**

Hii ni kama Aya ifuatayo:

وَأَنْفِقُوا مِنْ مَا رَزَقْنَاكُمْ مِنْ قَبْلِ أَنْ يَأْتِيَ أَحَدَكُمُ الْمَوْتُ

**“Na toeni katika yale Tuli yokupeni, kabla mmoja wenu hayajamjia mauti.”**

Mpaka Kauli Yake:

وَاللَّهُ خَبِيرٌ بِمَا تَعْمَلُونَ ﴿١٠١﴾

**“Na Allah Anazo habari za munayoyatenda yote.” (63:10-11).**

Na pia,

وَأَنْذِرِ النَّاسَ يَوْمَ يَأْتِيهِمُ الْعَذَابُ

**“Na uwaonye watu siku ambayo itawafikia adhabu.”**

Mpaka Kauli Yake:

مَا لَكُمْ مِنْ زَوَالٍ ﴿١٠٢﴾

**“(Kwamba) nyinyi hamutapata muhamo wowote (wa kuihama dunia)?” (14:44).** Na pia Kauli Yake:

يَوْمَ يَأْتِي تَأْوِيلُهُ يَقُولُ الَّذِينَ نَسُوهُ مِنْ قَبْلُ قَدْ جَاءَتْ رُسُلُ رَبِّنَا بِالْحَقِّ فَهَلْ لَنَا مِنْ

شُفَعَاءَ فَيَشْفَعُوا لَنَا أَوْ نُرَدُّ فَنَعْمَلْ غَيْرَ الَّذِي كُنَّا نَعْمَلُ

***“Siku yatakapotokea matokeo yake hayo watasema wale waliopuuzwa hapo zamani: ‘Kweli Mitume wa Mola wetu walileta haki; Je, tunao waombezi ili watuombe? Au tutarudishwa ili tufanye yasiyokuwa yale tuliokuwa tukiyafanya.’” (7:53).***

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ الْمُجْرِمُونَ نَاكِسُوا رُءُوسِهِمْ عِنْدَ رَبِّهِمْ رَبَّنَا أَبْصَرْنَا وَسَمِعْنَا فَارْجِعْنَا  
نَعْمَلْ صَالِحًا إِنَّا مُوقِنُونَ ﴿٥٣﴾

***“Na ungaliwaona waovu wakiinamisha vichwa vyao mbele ya Mola wao Mlezi, na kusema: ‘Mola wetu Mlezi! Tumekwisha kuona na tumekwisha kusikia basi turudishe, tutafanya vitendo vizuri; hakika sasa tumeyakinisha.’” (32:12).***

Na Amesema Aliyetukuka:

وَلَوْ تَرَىٰ إِذِ وَقُفُوا عَلَى النَّارِ فَمَا لَوْ يَلَيْتُنَا نُزِدُ وَلَا نُكَذِّبُ بِعَايَتِ رَبِّنَا  
***“Na ungeona Siku ya Kiyama watakaposimamishwa kwenye Moto, wakawa wanasema: Laiti tungerudishwa (duniani) wala hatutakadhibisha tena Aya za Mola wetu Mlezi.”***

Mpaka katika Kauli Yake:

وَأَنَّهُمْ لَكَذِبُونَ ﴿٢٨﴾

***“Na bila shaka hao ni waongo.” (6:27-28).***

Na Amesema Aliyetukuka:

وَتَرَى الظَّالِمِينَ لَمَّا رَأَوْا الْعَذَابَ يَقُولُونَ هَلْ إِلَىٰ مَرَدٍّ مِن سَبِيلِ ﴿٤٤﴾  
***“Na utawaona madhalimu watakapoiona adhabu wanasema (kwa masikitiko): Je, iko njia ya kurudi (ulimwenguni tukafanye mema tupate Pepo)?” (42:44)*** Na Amesema aliyetukuka,

قَالُوا رَبَّنَا أَمَتْنَا اثْنَتَيْنِ وَأَحْيَيْتَنَا اثْنَتَيْنِ فَاعْتَرَفْنَا بِذُنُوبِنَا فَهَلْ إِلَىٰ خُرُوجٍ مِن سَبِيلِ ﴿٤١﴾  
***“Watasema: Mola wetu Mlezi! Umetufisha mara mbili na Umetuhuisha mara mbili. Basi tunakiri dhambi zetu. Basi je, iko njia ya kutoka?” (40:11).***



Na Aya baada yake. Na Amesema Aliyetukuka:

وَهُمْ يَصْطَرِّخُونَ فِيهَا رَبَّنَا أَخْرِجْنَا نَعْمَلْ صَالِحًا غَيْرَ الَّذِي كُنَّا نَعْمَلُ ۖ أَوَلَمْ نُعَمِّرْكُم  
مَا يَتَذَكَّرُ فِيهِ مَن تَذَكَّرَ وَجَاءَكُمُ النَّذِيرُ فَذُوقُوا فَمَا لِلظَّالِمِينَ مِن نَّصِيرٍ ﴿٣٧﴾

**“Na humo watapiga makelele: Mola wetu Mlezi! Tutoe Motoni (na Uturejeshe duniani), tutafanya vitendo vizuri visivyokuwa vile tulivyokuwa tukifanya. Allah Awaambie: Hatukukupeni umri wa kuweza kukumbuka mwenye kukumbuka? Na akakujieni Muonyaji. Basi onjeni adhabu madhalimu hawana wa kuwanusuru” (35:37).**

Anataja Aliyetukuka kuwa wataomba warudi tena (duniani), watakapokaribia kufa na Siku ya Ufufuo, watakapokusanywa kuhukumiwa mbele ya Jabari (Allah تعالى) na pale watakapokuwa katika maumivu makali kwa adhabu wanayopata Motoni, lakini maombi yao hayatakubaliwa. Na Kauli Yake hapa:

كَلَّا إِنَّهَا كَلِمَةٌ هُوَ قَائِلُهَا ۖ

**“Wapi! Hii ni kauli aisemayo yeye tu.”**

Neno “Kallaa” (Hapana) ni neno linalotumika kukemea, yaani Hatumjibu kwa anayotaka wala Hatutamkubalia. Na Kauli Yake:

إِنَّهَا كَلِمَةٌ هُوَ قَائِلُهَا ۖ

**“Hii ni kauli aisemayo yeye tu.”**

Maana yake: Kwa aliyoomba kurudi tena duniani ili apate kuwa mwema na kutenda mema; haya ni maneno yake tu, hakuna amali kutoka kwake. Na lau angerudishwa tena (duniani) asingefanya matendo mema na angekuwa amedang'anya katika kauli yake hiyo. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

وَلَوْ رُدُّوْا لَعَادُوْا لِمَا نُهُوْا عَنْهُ وَإِنَّهُمْ لَكَاذِبُوْنَ ﴿٢٨﴾

**“Na kama wangelirudishwa bila shaka wangepyarudia yale waliyokatazwa; na bila shaka hao ni waongo tu.” (6:28).**

Amesema Qatadah: "Wallaahi, hatatamani kurudi kwa watu wake na familia yake, wala kukusanya vitu zaidi vya dunia na kutimiza matamania yake, lakini atatamani arudi ili amtii Allah تعالى. Allah تعالى Amrehemu mtu anayefanya yale ambayo kafiri atatamani kuyafanya pindi atakapoiona adhabu ya Moto.

### Maisha ya *Barzakh* na Adhabu Yake

وَمِن ذَرَابِهِمْ بَرَزَخٌ إِلَى يَوْمِ يُبْعَثُونَ ﴿٢٤﴾

***"Na nyuma yao kipo kizuizi (Barzakh) mpaka siku watakapofufuliwa".***

Amesema Abu Swaalih na wengineo kuhusu Kauli Yake Aliyetukuka:

وَمِن ذَرَابِهِمْ

***"Na nyuma yao."***

Maana yake: Mbele yao. Na amesema Mujaahid: "*Al-Barzakh*" ni kizuizi baina ya dunia na Akhera". Na amesema Muhammad bin Ka'b: "*Al-Barzakh*" ni baina ya dunia na Akhera, haipo pamoja na watu wa dunia, wakila na kunywa wala pamoja na watu wa Akhera, wanaolipwa kwa amali zao". Na amesema Abu Swakhr: "*Al-Barzakh*" ni makaburi ambayo hayapo duniani wala Akhera, na hapo watakaa mpaka Siku ya Ufufuo"<sup>1</sup>. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَمِن ذَرَابِهِمْ بَرَزَخٌ

***"Na nyuma yao kipo kizuizi."***

Maneno haya yana tishio kwa wale madhalimu wakati wanapoaga dunia, kwa adhabu ya "*Barzakh*". Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

مِن ذَرَابِهِمْ جَهَنَّمَ

***"Na nyuma yako iko Jahanamu (inawangoja)..." (45:10).***

<sup>1</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 6:116.

وَمِنَ وَّرَائِهِمْ عَذَابٌ عَظِيمٌ ﴿١٧﴾

**“Na zaidi ya hayo nyuma yao iko adhabu kali...” (14:17).**

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

إِلَى يَوْمٍ يُبْعَثُونَ ﴿١٨﴾

**“Mpaka siku watapofufuliwa.”**

Maana yake: Ataadhibiwa mfululizo bila kupumzishwa mpaka Siku ya ufufuo, kama ilivyokuja katika Hadithi:

«فَلَا يَرَالُ مُعَذَّبًا فِيهَا»

**“Ataendelea kuadhibiwa ndani yake.”**

Maana yake: Katika ardhi<sup>1</sup>.

\* \* \*

---

<sup>1</sup> Tuhfatul Al-Ahwadhiy 4:183.

فَإِذَا نُفِخَ فِي الصُّورِ فَلَا أَنْسَابَ بَيْنَهُمْ يَوْمَئِذٍ وَلَا  
يَتَسَاءَلُونَ ﴿١٠١﴾ فَمَنْ ثَقُلَتْ مَوَازِينُهُ فَأُولَئِكَ هُمُ  
الْمُفْلِحُونَ ﴿١٠٢﴾ وَمَنْ خَفَّتْ مَوَازِينُهُ فَأُولَئِكَ  
الَّذِينَ خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ فِي جَهَنَّمَ خَالِدُونَ ﴿١٠٣﴾ تَلْفَحُ  
وُجُوهُهُمْ النَّارُ وَهُمْ فِيهَا كَالِحُونَ ﴿١٠٤﴾ أَلَمْ تَكُنْ أَتَى  
تُتَلَّى عَلَيْكُمْ فُكْنُتُمْ بِهَا تُكَذِّبُونَ ﴿١٠٥﴾ قَالُوا رَبَّنَا غَلَبَتْ  
عَلَيْنَا شِقْوَتُنَا وَكُنَّا قَوْمًا ضَالِّينَ ﴿١٠٦﴾ رَبَّنَا أَخْرِجْنَا  
مِنْهَا فَإِنِ عُدْنَا فَإِنَّا ظَالِمُونَ ﴿١٠٧﴾ قَالَ آخِضُوا فِيهَا وَلَا  
تُكَلِّمُونِ ﴿١٠٨﴾ إِنَّهُ كَانَ فَرِيقٌ مِّنْ عِبَادِي يَقُولُونَ رَبَّنَا  
ءَامَنَّا فَآغْفِرْ لَنَا وَارْحَمْنَا وَأَنْتَ خَيْرُ الرَّاحِمِينَ ﴿١٠٩﴾  
فَاتَّخَذْتُمُوهُمْ سَخِرِيًّا حَتَّى أَنْسَوَكُم ذِكْرِي وَكُنْتُمْ مِنهُمْ  
تَضْحَكُونَ ﴿١١٠﴾ إِنِّي جَزَيْتُهُمُ الْيَوْمَ بِمَا صَبَرُوا أَنَّهُمْ هُمُ  
الْفَآبِزُونَ ﴿١١١﴾ قُلْ كَمْ لَبِئْتُمْ فِي الْأَرْضِ عَدَدَ سِنِينَ ﴿١١٢﴾  
قَالُوا لَبِئْنَا يَوْمًا أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ فَسَلِّ الْعَادِينَ ﴿١١٣﴾ قُلْ إِن  
لَبِئْتُمْ إِلَّا قَلِيلًا ۗ لَوْ أَنَّكُمْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١١٤﴾ أَفَحَسِبْتُمْ  
أَنَّكُمْ خُلِقْتُمْ عَبَثًا وَأَنْكُمْ إِلَيْنَا لَا تُرْجَعُونَ ﴿١١٥﴾ فَتَعَلَى  
اللَّهُ الْمَلِكُ الْحَقُّ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْكَرِيمِ ﴿١١٦﴾  
وَمَنْ يَدْعُ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ لَا بُرْهَانَ لَهُ بِهِ فَإِنَّمَا  
حِسَابُهُ عِندَ رَبِّهِ ۗ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الْكَافِرُونَ ﴿١١٧﴾ وَقُلْ  
رَبِّ اغْفِرْ وَارْحَمْ وَأَنْتَ خَيْرُ الرَّاحِمِينَ ﴿١١٨﴾

فَإِذَا نُفِخَ فِي الصُّورِ فَلَا أَنْسَابَ  
بَيْنَهُمْ يَوْمَئِذٍ وَلَا يَتَسَاءَلُونَ ﴿١٠١﴾  
فَمَنْ ثَقُلَتْ مَوَازِينُهُ فَأُولَئِكَ هُمُ  
الْمُفْلِحُونَ ﴿١٠٢﴾ وَمَنْ خَفَّتْ  
مَوَازِينُهُ فَأُولَئِكَ الَّذِينَ خَسِرُوا  
أَنفُسَهُمْ فِي جَهَنَّمَ خَالِدُونَ ﴿١٠٣﴾  
تَلْفَحُ وُجُوهُهُمْ النَّارُ وَهُمْ فِيهَا  
كَالِحُونَ ﴿١٠٤﴾

101. Basi litapopulizwa baragumu hapo hautakuwapo ujamaa baina yao siku hiyo, wala hawatalizana.

102. Ama wale ambao mizani zao zitakuwa nzito, hao ndio wenye kufanikiwa.

103. Na wale ambao mizani zao zitakuwa nyepesi, hao ndio waliozitia khasarani nafsi zao, na katika Jahannamu watadumu.

104. Moto utababua nyuso zao, nao watakuwa na nyuso zilizo kunjana.

### Kupulizwa kwa Baragumu na Kupimwa Amali Katika Mizani

Allah تعالى Anatueleza kuwa pindi baragumu litakapopulizwa kwa ajili ya kukusanywa pamoja, na watu watasimama kutoka makaburini mwao,

فَلَا أُنسَبُ بَيْنَهُمْ يَوْمَئِذٍ وَلَا يَتَسَاءَلُونَ ﴿١٠١﴾

***“Hapo hautakuwapo ujamaa baina yao siku hiyo, wala hawataulizana.”***

Maana yake: Siku hiyo haitawanufaisha (nasaba au ujamaa) wala baba hatamuuliza mtoto wake wala kumhudumia.

Allah تعالى Anatueleza:

وَلَا يَسْأَلُ حَمِيمٌ حَمِيمًا ﴿١٠٢﴾ يُبْصِرُونَ ﴿١٠٣﴾

***“Wala jamaa hatamuuliza jamaa (yake). Ingawa watafanywa waonane...” (70:10-11),***

Maana yake: Hakuna jamaa atakayemuuliza jamaa mwenziwe, naye anamuona, na hata kama ana mizigo mizito juu ya mgongo wake. Na hata kama alikuwa ni kipenzi chake mno miongoni hapa duniani, hatamtizama wala hatambebea mzigo wake hata uzito mdogo wa mbu.

Allah تعالى Amesema:

يَوْمَ يَفِرُّ الْمَرْءُ مِنْ أَخِيهِ ﴿١٠٤﴾ وَأُمِّهِ وَأَبِيهِ ﴿١٠٥﴾ وَصَلْحَتِهِ وَبَنِيهِ ﴿١٠٦﴾

***“Siku ambayo mtu atamkimbia nduguye. Na mamaye na babaye. Na mkewe na wanawe.” (80:34-36).***

Na Ibn Mas'ud رضي الله عنه amesema: “Itapofika Siku ya Kiyama Allah تعالى Atawakusanya wa mwanzo na wa mwisho, kisha atanadi mwenye kunadi: ‘Tambueni kuwa yeyote anayedaiwa na mwenziwe, aje hapa mbele na kuichukua haki yake. Hapo mtu atafurahi ikiwa anadai, au amedhulumiwa na babake, mtoto wake au mkewe, hata ikiwa ni kitu kidogo sana”.

Hii imeyakinishwa katika Kitabu cha Allah تعالى, ambapo Allah تعالى Amesema:

فَإِذَا نُفِخَ فِي الصُّورِ فَلَا أَنْسَابَ بَيْنَهُمْ يَوْمَئِذٍ وَلَا يَتَسَاءَلُونَ ﴿١٠١﴾

**“Basi litapopulizwa baragumu hapo hautakuwapo ujamaa baina yao siku hiyo, wala hawataulizana”.**

Imepokewa na Ibn Abi Haatim<sup>1</sup>. Na Kauli Yake:

فَمَنْ ثَقَلَتْ مَوَازِينُهُ فَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿١٠٢﴾

**“Ama wale ambao mizani zao zitakuwa nzito, hao ndio wenye kufanikiwa.”**

Maana yake: Kwa yule ambaye matendo yake mazuri yamezidi matendo mabaya, hata kama ni moja. Amesema hayo Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما<sup>2</sup>.

فَأُولَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ ﴿١٠٣﴾

**“Hao ndio wenye kufanikiwa.”**

Maana yake: Wale ambao wamefuzu na kuokoka na Moto na kuingia Peponi. Na Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Hao ni wale waliofuzu kwa waliyotaka na wameokoka na shari walioikimbia”.

وَمَنْ حَفَّطَ مَوَازِينَهُ

**“Na wale ambao mizani zao zitakuwa nyepesi.”**

Maana yake: Maovu yake yakazidi mazuri.

فَأُولَئِكَ الَّذِينَ خَسِرُوا أَنْفُسَهُمْ

**“Hao ndio waliozitia khasarani nafsi zao...”**

Maana yake: Wamefeli na kuangamia na kumalizikia katika hali mbaya zaidi. Kwa hiyo, Akasema Aliyetukuka:

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 19:72.

<sup>2</sup> Ad-Durr Al-Manthuur 6:418.

﴿١٣٧﴾ فِي جَهَنَّمَ خَالِدُونَ

**“Na katika Jahanamu watadumu.”**

Maana yake: Watabaki humo daima dawamu wala hawatatoka humo.

تَلَفَحُ وُجُوهُهُمْ النَّارُ

**“Moto utababua nyuso zao...”**

Kama Alivyosema Aliyetukuka:

﴿١٣٨﴾ وَتَغَشَىٰ وُجُوهُهُمْ النَّارُ

**“Na Moto utazijia nyuso zao (uzibabue).” (14:50).**

Na Amesema Aliyetukuka:

لَوْ يَعْلَمُ الَّذِينَ كَفَرُوا حِينَ لَا يَكْفُرُونَ عَنْ وُجُوهِهُمْ النَّارَ وَلَا عَن ظُهُورِهِمْ

**“Lau wangejua wale waliokufuru wakati ambao hawatazuia Moto katika nyuso zao wala katika migongo yao...” (21:39).**

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

﴿١٣٩﴾ وَهُمْ فِيهَا كَالِحُونَ

**“Nao watakuwa na nyuso zilizokunjana.”**

Amepokea 'Aliy bin Abi Twalhah kuwa Ibn 'Abbaas رضي الله عنهما amesema: “Maana yake ni kukunja uso”<sup>1</sup>.

أَلَمْ تَكُنْ تَكُنْ ءَايَتِي تُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ فَكُنْتُمْ بِهَا تُكَذِّبُونَ ﴿١٤٠﴾ قَالُوا رَبَّنَا غَلَبَتْ عَلَيْنَا شِقْوَتُنَا

وَكَانَا قَوْمًا ضَالِّينَ ﴿١٤١﴾ رَبَّنَا أَخْرِجْنَا مِنْهَا فَإِنْ عُدْنَا فَإِنَّا ظَالِمُونَ ﴿١٤٢﴾

**105. Je! Hazikuwa Aya Zangu mukisomewa, na nyinyi mukizikanusha.?**

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 19:74.

**106. Na watasema Mola wetu Mlezi! Tulizidiwa na uovu wetu na tukawa watu tuliopotea.**

**107. Mola wetu Mlezi! Tutoe humu Motoni. Na tufanyapo tena basi kweli sisi ni wenye kudhulumu.**

### **Kuwakemea Watu wa Motoni, Kukiri Uovu Wao na Kutaka Kwao Kutoka Motoni**

Haya ni makemeo kutoka kwa Allah تعالى kwa watu wa Motoni kwa ukafiri wao, madhambi yao, kuendea ya haramu na maovu makubwa waliyokuwa wakifanya, kwa sababu ya hayo wakaangamizwa. Akasema Aliyetukuka:

أَلَمْ تَكُنْ تَكُنْ ءِآيَاتِي تُتْلَىٰ عَلَيْكُمْ فَكُنْتُمْ بِهَا تُكَذِّبُونَ ﴿١٠٦﴾

**“Je! Hazikuwa Aya Zangu mukisomewa, na nyinyi mukizikanusha?”**

Maana yake: Hakika Niliwatumia Mitume, Kuwateremshia Vitabu na Kuwaondolea utata, kwa hiyo hamkubaki na hoja yoyote juu ya hayo. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

لَعَلَّآ يَكُونَنَّ لِلنَّاسِ عَلَىٰ اللَّهِ حُجَّةٌ بَعْدَ أَلْرُّسُلِ ۗ

**“Ili watu wasiwe na hoja juu ya Allah baada ya kuletwa hawa Mitume...” (4:165).**

Na Amesema Aliyetukuka:

وَمَا كُنَّا مُعَذِّبِينَ حَتَّىٰ نَبْعَثَ رَسُولًا ﴿١٧﴾

**“Na Sisi si wenye Kuwaadhibu viumbe mpaka Tuwapelekee Mtume.” (17:15).**

Na Kauli ya Aliyetukuka:

كُلَّمَا أَلْقَىٰ فِيهَا فَوْجٌ سَأَلْتَهُم خَزَنَتُهَا أَلَمْ يَأْتِكُمْ نَذِيرٌ ﴿١٠٧﴾

**“Kila mara litakapotupwa humo kundi la wabaya walinzi wake watawauliza: Je, hakukufikieni Muonyaji.”**



Mpaka kwa Kauli Yake:

فَسُحِقًا لِأَصْحَابِ السَّعِيرِ ﴿١٧﴾

**“...Basi kuangamia kumewastahikia watu wa Motoni.”**

Kwa hiyo wakasema:

رَبَّنَا غَلَبَتْ عَلَيْنَا شِقْوَتُنَا وَكُنَّا قَوْمًا ضَالِّينَ ﴿١٨﴾

**“...Mola wetu Mlezi! Tulizidiwa na uovu wetu na tukawa watu tuliopotea.”**

Maana yake: Hakika imesimamishwa hoja juu yetu, lakini tulikuwa watu waovu sana kwa sababu hiyo hatukuweza kufuata (njia), hivyo tulipotoka na kushindwa kuongoka.

Kisha wakasema:

رَبَّنَا أَخْرِجْنَا مِنْهَا فَإِنْ عُدْنَا فَإِنَّا ظَالِمُونَ ﴿١٩﴾

**“Mola wetu Mlezi! Tutoe humu Motoni. Na tufanyapo tena basi kweli sisi ni wenye kudhulumu.”**

Maana yake: Turudishe duniani, na lau tutarudi tena kwa tuliyokuwa tukifanya, bila shaka tutakuwa madhalimu tunaostahiki adhabu. Hii ni kama Alivyosema:

فَاعْتَرَفْنَا بِذُنُوبِنَا فَهَلْ إِلَى خُرُوجٍ مِنْ سَبِيلٍ ﴿٢٠﴾

**“Basi tunakiri dhambi zetu. Basi je, iko njia ya kutoka?”**

Mpaka Kauli Yake:

فَاتَّخِمْ لِبِلِّهِ الْعَلِيِّ الْكَبِيرِ ﴿٢١﴾

**“Basi hukumu leo ni Yake (Mwenyewe tu) Allah Aliye Juu Aliye Mkuu.” (40:11-12)**

Maana yake: Hapana njia ya kutoka kwa kuwa mulikuwa mkimshirikisha Allah تعالى, pale walipompwekesha Waumini.

قَالَ أَحْسَبُوا فِيهَا وَلَا تُكَلِّمُونَ ﴿١٠٨﴾ إِنَّهُ كَانَ فَرِيقٌ مِّنْ عِبَادِي يَقُولُونَ رَبَّنَا ءَأَمَّنَّا  
 فَاغْفِرْ لَنَا وَأَرْحَمْنَا وَأَنْتَ خَيْرُ الرَّاحِمِينَ ﴿١٠٩﴾ فَاتَّخَذْتُمُوهُمْ سِخْرِيًّا حَتَّى أَنْسَوَكُم ذِكْرِي  
 وَكُنْتُمْ مِّنْهُمْ تَضْحَكُونَ ﴿١١٠﴾ إِنِّي جَزَيْتُهُمُ الْيَوْمَ بِمَا صَبَرُوا أَنَّهُمْ هُمُ الْفَآئِزُونَ ﴿١١١﴾

**108. Atasema Allah: Tokomeeni humo, wala musinisemeze.**

**109. Bila ya shaka lilikuwapo kundi katika waja Wangu likisema: Mola wetu Mlezi! Tumeamini; basi tusamehe na Uturehemu, Nawe Ndiwe Mbora wa wanao rehemu.**

**110. Lakini nyinyi mliwakejeli hata wakakusahaulisheni kunikumbuka, na mulikuwa mkiwacheka.**

**111. Hakika Mimi leo Nimewalipa kwa vile walivyosubiri. Bila ya shaka hao ndio wenye kufuzu.**

### Jibu la Allah تعالى Katika Kuwakataza Kwake Makafiri

Hili ni jawabu kutoka kwa Allah تعالى kwa makafiri walipoomba kutoka kwenye Moto na kurudi ulimwenguni. Atasema:

أَحْسَبُوا فِيهَا

**“Tokomeeni humo...”**

Maana yake: Kaeni humo, mkidunishwa na huku mkiwa mmenyongeshwa na kudhalilishwa.

وَلَا تُكَلِّمُونَ ﴿١٠٨﴾

**“Wala msinisemeze.”**

Maana yake: Msirudie hayo katika kuuliza kwenu kwani hamtajibiwa Nami. Amepokea al-Awfiy kuwa Ibn Abbaas رضي الله عنهما amesema yafuatayo kuhusu Aya hii:

أَحْسَبُوا فِيهَا وَلَا تُكَلِّمُونَ ﴿١٠٨﴾

**“Tokomeeni humo, wala musinisemeze”.**

Akasema: Hii ni kauli ya *Ar-Rahmaan* Alipowanyamazisha<sup>1</sup>. Amepokea Ibn Abi Haatim kuwa 'Abdallah bin 'Amri رضي الله عنه amesema: "Watu wa Motoni watamuita Maalik kwa muda wa miaka arobaini (40) bila kujibiwa. Kisha atawaitikia kwa kuwaambia kuwa watabaki humo milele. Wallaahi, kilio chao hakitafalia lolote kwa Maalik na kwa Mola Mlezi wa Maalik. Baada ya hapo watamuita Mola wao Mlezi kwa kusema:

رَبَّنَا غَلَبَتْ عَلَيْنَا شِقْوَتُنَا وَكُنَّا قَوْمًا ضَالِّينَ ﴿١٠٦﴾ رَبَّنَا أَخْرِجْنَا مِنْهَا فَإِنْ عُدْنَا  
فَأِنَّا ظَالِمُونَ ﴿١٠٧﴾

***'Mola wetu Mlezi! Tulizidiwa na uovu wetu na tukawa watu tuliopotea. Mola wetu Mlezi! Tutoe humu Motoni. Na tufanyapo tena basi kweli sisi ni wenye kudhulumu.'* (23:106-107).**

Akasema: Allah تعالى kwa muda ulio sawa na mara mbili ya muda wa dunia. Kisha Atawajibu:

أَحْسَبُوا فِيهَا وَلَا تَكَلِّمُونَ ﴿١٠٨﴾

***'Tokomeeni humo, wala musinisemeze'.***

Akasema: 'Wallaahi, watu hawatatamka hata neno moja baada ya hapo, nao watabaki Motoni huku wanashindana kwa sauti kubwa na ndogo. Sauti zao zinafananishwa na mlio wa punda, ambaye anaanza kwa kubwa na kumaliza kwa sauti ndogo.'<sup>2</sup>

Kisha Allah تعالى Akasema kwa Kutukumbusha kwa madhambi yao hapa duniani na kwa yale waliyokuwa wakifanya mzaha kwayo kwa waja Wake Waumini na marafiki Wake wa karibu (mawalii Wake). Akasema Aliyetukuka:

إِنَّهُمْ كَانُوا فَرِيقًا مِّنْ عِبَادِي يَقُولُونَ رَبَّنَا ءَامَنَّا فَاغْفِرْ لَنَا وَارْحَمْنَا وَأَنْتَ خَيْرُ الرَّاحِمِينَ  
فَاتَّخَذْتُمُوهُمْ سُخْرِيًّا ﴿١٠٩﴾

<sup>1</sup> Atw-Twabariy 19:79.

<sup>2</sup> Az-Zuhd cha Hannaad bin As-Sirriy 1:158.

***"Bila ya shaka lilikuwapo kundi katika waja Wangu likisema: Mola wetu Mlezi! Tumeamini; basi tusamehe na Uturehemu, Nawe Ndiwe Mbora wa wanaorehemu. Lakini nyinyi muliwakejeli."***

Maana: Muliwakejeli na kuwafanyia mzaha kwa kuniita Mimi na kuninyenyekea,

حَتَّىٰ أَسْوَكُم ذِكْرِي

***"Hata wakakusahaulisheni kunikumbuka."***

Maana yake: Uchukivu wenu kwao uliwafanyia musahau Nitakayowafanyia.

وَكُنْتُمْ مِّنْهُمْ تَضْحَكُونَ ﴿٢٩﴾

***"Na mulikuwa mkiwacheka."*** Maana yake: Kwa amali na lbada zao. Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

إِنَّ الَّذِينَ أَجْرَمُوا كَانُوا مِنَ الَّذِينَ ءَامَنُوا يَضْحَكُونَ ﴿٢٩﴾ وَإِذَا مَرُّوا بِهِمْ يَتَغَامَزُونَ

***"Kwa hakika wale waliokuwa wanafanya madhambi walikuwa wakiwacheka walioamini; Na wanapopita karibu yao wakikonyezana (kwa kuwachokoza)." (83:29-30),***

Maana yake: Wakiwasengenya na kuwatukana kwa istihzai. Kisha Akatupasha habari Aliyetukuka jinsi Atakavyowalipa marafiki Zake waja Wake wema, Akasema Aliyetukuka:

إِنِّي جَزَيْتَهُمُ الْيَوْمَ بِمَا صَبَرُوا

***"Hakika Mimi leo Nimewalipa kwa vile walivyosubiri..."***

Maana yake: Kwa madhara na istihzai mlizowafanyia.

أَنَّهُمْ هُمُ الْفَآبِزُونَ ﴿٣٠﴾

***"Bila ya shaka hao ndio wenye kufuzu."***

Nikawajaalia kuwa miongoni mwa waliofaulu kwa kupata ufanisi, usalama, Pepo na kuokolewa na Moto.

قَالَ كَمْ لَبِئْتُمْ فِي الْأَرْضِ عَدَدَ سِنِينَ ﴿٣٠﴾ قَالُوا لَبِئْنَا يَوْمًا أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ فَسَعَلَ الْعَادِيْنَ

﴿٣١﴾ قُلْ إِنْ لَبِئْتُمْ إِلَّا قَلِيلًا ۗ لَوْ أَنكُمْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٣٢﴾ أَفَحَسِبْتُمْ أَنَّمَا خَلَقْنَاكُمْ

عَبَّأَ وَأَنْكُمْ إِلَيْنَا لَا تُرْجَعُونَ ﴿١٠١﴾ فَتَعَالَى اللَّهُ الْمَلِكُ الْحَقُّ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ رَبُّ الْعَرْشِ  
الْكَرِيمِ ﴿١٠٢﴾

**112. Atasema: Mulikaa muda gani katika ardhi kwa hesabu ya miaka?**

**113. Watasema: Tulikaa siku moja au sehemu ya siku. Basi waulize wanaoweka hesabu.**

**114. Atasema: Nyinyi hamukukaa huko duniani ila kidogo, laiti ingelikuwa munajua.**

**115. Je! Mlidhani ya kwamba Tulikuumbeni bure na ya kwamba nyinyi Kwetu hamutarudishwa?**

**116. Ametukuka Allah, Mfalme wa Haki, hapana mungu ila Yeye, Mola Mlezi wa Arshi Tukufu.**

Anatueleza Aliyetukuka jinsi gani walivyopoteza wakati wao katika maisha yao mafupi hapa duniani kwa kushindwa kumtii Allah تعالى na kumuabudu Yeye Peke Yake. Na lau wangesubiri katika muda huu mfupi wa duniani wangefuzu kama walivyofaulu marafiki Wake wa karibu na wacha Mungu.

قَلَّ كَمْ لَبِئْتُمْ فِي الْأَرْضِ عَدَدَ سِنِينَ ﴿١٠٣﴾

**“Atasema: Mulikaa muda gani katika ardhi kwa hesabu ya miaka?”**

Maana yake: Muliishi muda gani ulimwenguni?

قَالُوا لَبِئْنَا يَوْمًا أَوْ بَعْضَ يَوْمٍ فَسَلِّ الْعَادِينَ ﴿١٠٤﴾

**“Watasema: Tulikaa siku moja au sehemu ya siku. Basi waulize wanaoweka hesabu.”**

Maana yake: Wawekao hesabu (na kumbukumbu).

قَلَّ إِنْ لَبِئْتُمْ إِلَّا قَلِيلًا ﴿١٠٥﴾

**“Atasema: Nyinyi hamukukaa huko duniani ila kidogo.”** Maana yake: Muda kidogo sana, kwa kipimo chochote mtakachotumia.

لَوْ أَنَّكُمْ كُنْتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿١٠١﴾

**“Laiti ingelikuwa mnajua.”** Maana: Lau msingechagua dunia ya kupita kwa Akhera inayobakia milele na musingefuja maisha yenu kwa njia hiyo na kughadhibikiwa na Allah تعالى kwa muda huu mfupi. Lau mngesubiri juu ya kumtii Allah تعالى na kumuabudu Yeye tu kama walivyofanya Waumini, mngelifaulu kama walivyofaulu na kufuzu Waumini.

Ibn Abi Hatim amenukuu kutoka kwa Swaf'wan, kutoka kwa Aifal Ibn Abdi Al-Kilai kuwa yeye alimsikia akiwahutubia watu, akasema: Mtume ﷺ amesema;

*“Hakika Allah Atakapowaingiza peponi watu wa peponi, na watu wa motoni Kuwaingiza motoni. Allah Atasema: ‘Enyi watu wa peponi miaka mingapi mmeishi duniani?’ Watajibu: ‘Tumeishi siku moja au baadhi ya siku’ – Hapo Allah Atawaambia: ‘Katika siku hiyo moja au baadhi yake mmeitumia vizuri sana. Hivyo basi, kwa sababu ya Huruma Yangu, Ridhaa Yangu na Pepo Yangu, ishini humo daima dawamu.’ Kisha Atawageukia watu wa motoni, na Kusema: ‘Enyi watu wa motoni, miaka mingapi mmeishi duniani?’ Watajibu: ‘Tumeishi siku moja au baadhi yake.’ Hapo Allah Atasema: ‘Katika siku hiyo moja au baadhi yake mmeitumia vibaya sana. Hivyo basi, kwa sababu ya Hasira Zangu, na kwa kuwa Moto ndio Adhabu Yangu, ishini humo daima milele.”<sup>1</sup>*

**Allah تعالى Hakuwaumba Waja Bure Bure**

Na Kauli Yake Aliyetukuka:

أَفَحَسِبْتُمْ أَنَّمَا خَلَقْنَاكُمْ عَبَثًا

**“Je! Mulidhani ya kwamba Tulikuumbeni bure”,**

Maana yake: Je, munadhania kuwa nyinyi mmeumbwa bure bure bila ya lengo wala mahitajio kutoka kwenu wala hekima yoyote kutoka Kwetu. Na panasemwa: Kwa mchezo, yaani kucheza na kustarehe kama walivyoumbwa wanyama, wasiokuwa na thawabu wala adhabu. Na hakika ni kuwa Tumewaumba kwa ajili ya Ibada na kusimamisha Amri za Allah تعالى.

<sup>1</sup> Usudu Al-Ghaba 1:187.

وَأَنْتُمْ إِلَيْنَا لَا تَرْجِعُونَ ﴿١٠١﴾

**“Na ya kwamba nyinyi Kwetu hamtarudishwa?”**

Maana yake: Hamutarudi katika Nyumba ya Akhera.

Hii ni kama Alivyosema Aliyetukuka:

أَحْسَبُ الْإِنْسَانَ أَنْ يُتْرَكَ سُدًى ﴿٣٦﴾

**“Je, anafikiri mwanadamu kuwa ataachwa bure.” (75:36).**

Na Kauli Yake:

فَتَعَلَى اللَّهِ الْمَلِكُ الْحَقُّ ﴿٣٧﴾

**“Ametukuka Allah, Mfalme wa Haki”.**

Maana yake: Ametakasika na Kuumba chochote bure bure (pasi na lengo lolote lile), kwani Yeye ni Mfalme wa Haki Aliyeepukana na hayo.

لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ رَبُّ الْعَرْشِ الْكَرِيمِ ﴿٣٨﴾

**“Hapana mungu ila Yeye, Mola Mlezi wa Arshi Tukufu.”**

Arshi imetajwa kwa kuwa ni sakafu ya viumbe vyote na imesifiwa kuwa ni Karim, yenye maana ya mandhari nzuri na mfumo mzuri, kama Alivyosema Aliyetukuka:

أُنَبِّئْنَا فِيهَا مِنْ كُلِّ زَوْجٍ كَرِيمٍ ﴿٣٩﴾

**“Tumeotesha humo mimea, ya kila namna nzuri.” (26:7).**

وَمَنْ يَدْعُ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ لَا بُرْهَانَ لَهُ بِهِ فَإِنَّمَا حِسَابُهُ عِنْدَ رَبِّهِ إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ

الْكَافِرُونَ ﴿٤٠﴾ وَقُلْ رَبِّ اغْفِرْ وَارْحَمْ وَأَنْتَ خَيْرُ الرَّاحِمِينَ ﴿٤١﴾

**117. Na anayemuomba - pamoja na Allah - mungu mwengine hana ushahidi wa hili; basi bila ya shaka hesabu yake iko kwa Mola wake Mlezi. Kwa hakika makafiri hawafanikiwi.**

**118. Nawe sema: Mola wangu Mlezi! Samehe na Urehemu Nawe ni Mbora wa wanaorehemu.**

### Shirki ni Dhuluma Kubwa na Wala Hafaulu Mshirikina

Anasema Aliyetukuka Kuwatishia na Kuwahofisha wenye kumshirikisha na vitu vingine na kuabudu pamoja Naye asiyekuwa Yeye. Anatupasha habari kuwa mwenye kumshirikisha Allah تعالى:

لَا بُرْهَانَ لَهُ

**“Hana ushahidi wa hili”.** Maana yake: Hana dalili kabisa. Kwa Kauli Yake Akasema Aliyetukuka:

وَمَنْ يَدْعُ مَعَ اللَّهِ إِلَهًا آخَرَ لَا بُرْهَانَ لَهُ بِهِ

**“Na anayemuomba - pamoja na Allah - mungu mwengine hana ushahidi wa hili...”.**

Na hii ni ibara yenye sharti, na jawabu yake ipo katika Kauli Yake:

فَإِنَّمَا حِسَابُهُ عِنْدَ رَبِّهِ

**“Basi bila ya shaka hesabu yake iko kwa Mola wake Mlezi”.** Maana yake: Allah تعالى Atawahesabu kwa hilo. Kisha Anatupasha habari:

إِنَّهُ لَا يُفْلِحُ الْكَافِرُونَ ﴿١٠١﴾

**“Kwa hakika makafiri hawafanikiwi.”** Maana yake: Kwake Siku ya Kiyama, hawatafaulu wala kuokoka. Na Kauli Yake Aliyetukuka:

وَقُلْ رَبِّ اغْفِرْ وَارْحَمْ وَأَنْتَ خَيْرُ الرَّاحِمِينَ ﴿١٠٢﴾

**“Nawe sema: Mola wangu Mlezi! Samehe na Urehemu Nawe ni Mbora wa wanaorehemu”.**

Huu ni uongofu kutoka kwa Allah تعالى katika kuisoma dua hii, kuomba maghufira, katika hali ya ujumla, inakuwa maana ya kufuta madhambi na kuyaficha machoni mwa watu. Na ‘Rehema’ Maana yake: Ni kumuongoza na kumuafikisha mtu katika kauli na matendo yake.

Hapa ni mwisho wa Tafsiri ya Suratul Mu'minuun.